Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

# HISTORIA KUU YA AFRIKA·

Juzuu Lililofupishwa

# VIII Afrika Kuanzia 1935

MHARIRI ALI A. MAZRUI

Msaidizi wa Mhariri **C. Wondji**



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · VIII

# Afrika Kuanzia 1935

MHARIRI ALI A. MAZRUI
Msaidizi wa Mhariri C. Wondji

Toleo Lisilofupishwa

T' . · CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM · UNESCO

Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL VIII

© UNESCO 1999
ISBN 9976 911 42 4

*Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.*
*Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.*
*Toleo la Tafsiri ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.*

Historia Kuu ya Afrika · VIII

# Afrika Kuanzia 1935

## Toleo Lisilofupishwa

**UNESCO Historia Kuu ya Afrika**

| | |
|---|---|
| **Juzuu I** | *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo** |
| **Juzuu II** | *Staarabu za Kale za Afrika*<br>Mhariri **G. Mokhtar** |
| **Juzuu III** | *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja*<br>Mhariri **I. Hrbek** |
| **Juzuu IV** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*<br>Mhariri **J. Ki-Zerbo na D.T. Niane** |
| **Juzuu V** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*<br>Mhariri **B.A. Ogot** |
| **Juzuu VI** | *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi Miaka ya 1880*<br>Mhariri **J.F. Ade Ajayi** |
| **Juzuu VII** | *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*<br>Mhariri **A. Adu Boahen** |

## Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

| | |
|---|---|
| **Juzuu VIII** | *Afrika Kuanzia 1935*<br>Mhariri **A.A. Mazrui**<br>Mhariri Msaidizi **C. Wondji** |

Toleo lisilofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO

**Limechapishwa na:**

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam, Tanzania

Pamoja na:
UNESCO Publishng
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.

# Yaliyomo

Ufunguo wa ramani ix

Orodha ya michoro x

Orodha ya picha xii

Shukrani za kupatiwa picha xv

Utanguzi xix
Amadou-Mahtar M'Bow, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO (1974-87)

Wasifu wa Mradi xxiv
Bcthwell A. Ogot, Mwcnyekiti wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-83)

Maclezo kwa Msomaji

1. Utangulizi 1
AI A. MAZRUI

*Sehemu ya I - Afrika kwenye muongo wa migongano duniani (1935 - 45)*

2. Pcmbc ya Afrika na Afrika Kaskazini, 1935 - 45; vurugu na Mabadiliko 17
Taycb CHENNTOUF

3. Afrika ya Tropiki na Ikwcta chini ya utawala wa Wafaransa, Wareno na Wahispania 1935 - 45 35
Majhcmout DIOP *pamoja na* David BIRMINGHAM, Ivan HRBEK, Afrcdo MARGARIDO na Djibri) Tamsiv NIAME

4. Afrika chini ya Utawala wa Waingercza na Wabclgiji Michael CHROWDER 46

*Sehemu ya II - Mapambano kwa ajili ya ufalme wa kisiasa: kuanzia 1945 hadi wakati wa uhuru.*

5. Utafute kwanza ufalme wa Kisiasa 60
Ali A. MAZRUI

6. Afrika ya Kaskazini na Pembe ya Afrika 73
Ivan HRBEK

7. Afrika Magharibi, 1945 - 60 94
Jean SURET - CANALE na A. Adu BOAHEN

8. Afrika Magharibi ya Ikweta 115
Elikia M'BOKOLO

9. Mapambano ya uhuru wa Kisiasa Afrika ya Mashariki, 1945 hadi uhuru 132
Michael TWADDLE *pamoja na* Lucile RABEARIMANANA *na* Isaria N. KIMAMBO

10. Afrika ya Kusini Kuanzia 1945 161
David CHANAIWA

*Sehemu ya III - Kutoendelea na mapambano kwa ajili ya uhuru wa kiuchumi*

11. Mabadiliko ya kiuchumi Afrika katika Muktadha wa Ulimwengu 189
Catherine COQUERY - VIDROVITCH

12. Kilimo na maendeleo vijijini tangu mwaka 1935 212
Maxwell OWUSU

13. Maendeleo ya viwanda na kukua kwa miji 1935 - 1980 246
Pierre KIPRÉ

14. Mikakati linganishi ya Ukombozi[1] wa Uchumi katika Afrika 286
Adebayo ADEDEJI

*Sehemu ya IV - Mabadiliko ya kijamii na kisiasa tangu uhuru*

15. Ujenzi wa taifa na mabadiliko ya mifumo ya kisiasa 338

J. Isawa ELAIGWU *pamoja na* Ali A. MAZRUI

16. Ujenzi wa taifa na mabadiliko ya kisiasa 364
Jeseph KI-ZERBO, Ali A. MAZRUI na Christophe WONDJI *pamoja na* A. Adu BOAHEW

*Sehemu ya V - Mabadiliko ya kijamii na kisiasa kuanzia 1935*

17. Dini na mabadiliko ya kijamii 383
Tshishiku TSHIBANGU *pamoja na* J. F. Ade AJAYI *na* Lemin SANNEH

18. Lugha na mabadiliko ya kijamii 400
Alfa I. SOW na Mohamed H. ABDULAZIZ

19. Kukua kwa fasihi ya kisasa tangu 1935 426
Ali A. MAZRUI *pamoja na hayati* Mario de ANDRADE, M'hamed ALAOUI ABDALLAOUI, Daniel. P. KUNENE *na* Jan VANSINA

20 Sanaa na jamii tangu 1935 446
Jan VANSINA

21. Mielekeo ya Falsafa na Sayansi katika Afrika 484
Ali A. MAZRUl *na* J. F. Ade AJAYI *pamojua na* A. Adu BOAHEN *na* Tshishiku TSHIBANGU

22 Mabadiliko ya Elimu na Jamii 523
Aklilu HABTE *na* Teshome WAGAW *pamoja na* J. F. Ade AJAYI

*Sehemu ya VI - Umoja wa Afrika: Ukombozi na kuunganika kuanzia 1935*

23. Afrika na Diaspora 1935 551
Joseph E. HARRIS *pamoja na* Slimane ZEGHIDOUR

24. Dhana ya Upanafrika na Muungano wa Kikanda 572
S.K.B. ASANTE *pamoja na* Davidi CHANAIWA

25. Upanafrika na ukombozi 590
Eden KODJO *na* David CHANAIWA

*Sehemu ya VII - Afrika huru na masuala ya dunia*

26. Afrika na nchi za Kibepari 608
CHINWEIIZU

27. Afrika na nchi za Kisoshalisti 632
Iba Der THIAM na James MULIRA *pamoja na* Christophe WONDJI

28. Afrika na Kanda zinazoendelca 669
Locksley EDMONDSON

29. Afrika na Umoja wa Mataifa tangu 1945 701
Edmond Kwam KOUASSI

30 Kuelckea mwaka 2000 740
Ali A. MAZRUI

Maclezo ya mwisho na Kronolojia ya Mambo ya Sasa ya Afrika katika miaka ya 1990[1] 774

Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika. 799

Wasifu wa Waandishi 801

Bibliografia 804

Faharasa 832

## Ufunguo wa ramani

| | |
|---|---|
| *BAULE* | Vikundi vya kikabila |
| ZAMBIA | Nchi |
| FEZZĀN | Mikoa |
| SAHARA | Mikoa asili |
| —·—·— | Mipaka ya kimataifa |
| • | Miji |
| *Ubangui* | Mito |

Taarifa za ziada na funguo za ramani binafsi

Ufunguo wa ramani

Ufunguo wa ramani

**Orodha ya michoro**


1.1 Ramani ya kisiasa ya Afrika mwaka 1935 pg. 3
10.1 Madini makuu ya Afrika ya Kusini pg. 162
11.2 Ufadhili wa vitega uchumi kwenye nchi za Afrika ya weusi zinazozungumza Kifaransa na Madagaska, 1946-73, kwa mabilioni ya faranga za CFA za 1960 pg. 197
11.3 Faida za SCOA, 1910-60 pg. 199
11.4 Vitega uchumi na akiba Afrika, 1960-83, kuondoa nchi zinazotoa mafuta pg. 203
11.5 Mipango ya ushirikiao na miungano ya sehemu na sehemu ndogo za Africa pg. 206.
12.1 Hatari ya kuenea kwa jangwa Afrika kama ilivyorekodiwa baada ya mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu usababishaji jangwa. pg. 225
12.2 Mgawanyo wa ng'ombe Afrika, pamoja na kijiramani cha ndani kinachoonyesha maeneo makuu ya mbung'o pg. 229
12.3 Ruwaza ya uhamaji wa kazi wa kimataifa Afrika, 1946-52 pg. 231
12.4 Shughuli za madini makuu Afrika pg. 241
12.5 Mgawanyo wa mazao ya biashara Afrika pg. 242
14.2 Makundi ya kijimbo ya MUPOC Afrika pg. 310
14.3 Makundi ya kijimbo ya kiuchumi Afrika pg. 311
14.4 Afrika Magharibi: Mpango Mkuu wa Barabara Kuu (ECA/ECOWAS) pg. 321
14.5 Eneo la Biashara Afrika Mashariki na Kusini: Mpango Mkuu wa Barabara Kuu pg. 314
17.1 Mgawanyo wa Ukristo, Uislamu na dini za asili za Kiafrika ambapo kila dini inamadai kuwa na asilimia 50 au zaidi ya idadi ya watu wa nchi. pg. 382
18.1 Mgawanyo wa lugha rasmi Afrika pg. 404
22.1 Uandikishaji watoto shule Afrika, 1960-1980, na marekebisho ya wastani wa uandikishaji wote kwa viwango pg. 533
22.2 Uandikishaji watoto shule Afrika, 1960-1980, na marekebisho ya wastani wa uandikishaji wote kwa viwango na jinsia pg. 534
22.3 Mifumo ya uandikishaji watoto shule ya msingi Afrika, 1960-80, inayoonyesha idadi ya wanafunzi shule ya msingi na usajili kwa

mamilioni, pamoja na marekebisho ya wastani (asilimia) wa jumla uandikishaji wa shule za msingi pg. 536
29.1 Nchi ya Togo 1919 - Azimio la Wafaransa na Waingereza, 10 Julai 1919 pg. 688
29.2 Kongo-Leopoldville (hivi sasa Jamhuri ya Watu wa Kongo pg. 693
29.3 Algeria pg. 705
29.4 Mfumo wa Umoja wa Mataifa pg. 722

**Orodha ya Picha**

Jalada: Waanzilishi wa Umoja wa Nchi Huru Afrika (1963), michoro asilia kwenyc Bwalo la Afrika


1.1 Mfalme Haile Selassie wa Ethiopia, akihutubia Muungano wa Mataifa pg. 7

1.2 Vijana waandamanaji huko Algiers wakipeperusha bendera ya FLN pg. 14

2.1 Kuja kwa majcshi ya kitaliano huko Uhabeshi pg. 26

2.2 Askari wa Kifaransa katika Jangwa la.Tripolitania pg. 28

2.3 Sayyid 'Abd al-Rahman al-Mahdi, 15 Julai 1937 pg. 33

3.1 Mkutano wa Brazzaville, Februari 1944 pg. 44

4.1 Wapiganaji wa Afrika Mashariki wakati wa vita kuu ya Pili pg. 57

4.2 Siku ya Uhuru, Swaziland pg. 59

5.1 Dedan Kimathi, shujaa wa vita vya MauMau ili kupata uhuru pg.63

5.2 Watu waliokamatwa baada ya fujo za tarehe 8 Mei 1945 huko Algcria pg. 65

5.3 Kwame Nkrumah siku ya kuamkia uhuru wa Ghana pg. 68

6.1 Mkutano wa utamaduni-Mpya, Novcmba 1955 pg. 76

6.2 Ferhat Abbas akihutubia mkutano huko Casablanca, tarche 9 July 1961 pg. 78

6.4 Magofu ya Bandari ya Said baada ya vita vya Suez, 1956 pg. 85

7.1 Obafemi Awolowo wa Nigeria pg. 97

7.2 Dkt. Nnandi Azikiwe wa Nigeria na Mfalme wa Dcvonshire, tarehe 10 Julai 1961 pg. 100

7.3 Mkutano wa RDA huko Bamako, 1946 pg. 104

7.4 Sylvanus Olympio, raisi wa Togo, akitangaza uhuru wa nchi yake, 27 Aprili 1960 pg. 106

7.5 Askari wa kike wenye silaha wa PAIGC pg. 109

7.6 William Tubman, rais wa Liberia pg. 111

8.1 Mwami Kigeri V, Mfalme wa mwisho wa Rwanda pg. 126

8.2 Joseph Kasavubu na Patrice Lumumba wa Kongo na Mfalme Baudouin wa Ubelgiji, Juni 1960 pg. 128

8.3 Viongozi watatu wa UPC pg. 128

9.1 Mfalme Mutesa 11, Kabaka wa Buganda, akiwa ukimbizini pg. 141

9.2 Julius K. Nyererc, rais wa TANU pg. 144

9.3 Jomo Kenyatta, rais wa KANU pg. 147
9.4 Kambi ya Kizuizini ya Langata, Aprili 1954 pg. 149
10.1 Robert Sobukwe, rais mwasisi wa PAC pg. 169
10.2 Mauaji ya Sharpeville, Afrika Kusini, 28 Machi, 1960 pg. 171
10.3 Dkt Eduardo Chivambo Mondlane, muasisi na rais wa kwanza wa FRELIMO pg. 176
10.4 Seretse Khama, chifu wa Wabamangwato akiwa ukimbizini na familia yake pg. 177
10.5 Sally Mugabe, Waziri Mkuu Robert Mugabe, Rais Canaan Banana na Simon Muzenda wa Zimbabwe, 1980 pg. 181
10.6 Kikosi cha SWAPO kikiwa katika ulinzi pg. 183
11.1 Mkutano wa Nchi zinazotoa Mafuta huko Vienna, 21 Novemba 1973 pg. 196
11.2 Bernardo Vieira wa Guinea-Bissau, akikutana na M.A. Qureshi wa Benki ya Dunia, Oktoba 1988 pg. 205
12.1 Mfanyakazi wa kike wa kilimo, Moroko pg. 215
12.2 Ukame huko Algeria, 1947 pg. 227
13.1 Kiwanda cha pamba huko Mahana, Misri ya kaskazini pg. 265
13.2 Makazi yasiyo rasmi pg. 280
14.1 Bwawa la Jinja, Uganda pg. 334
14.2 Bwawa la Akosombo huko Ghana na Bwana Kubwa la Kariba huko Zimbabwe pg. 335
15.1 Mfalme Mutesa 11, Kabaka wa Buganda wa mwisho. pg. 340
15.2 Mkutano Mkuu wa Pili wa nchi za Maghreb, Marrakesh, 15-16 Februari 1989 . pg. 342
16.1 Franz Fanon, mwandishi wa Kifaransa aliyezaliwa Martinique pg. 367
16.3 Amikar Cabral wa Guinea-Bissau, kwenye Ngome ya Mashariki pg. 372
16.4 Tom Mboya wa Kenya pg. 375
16.5 Ahmed Sekou Toure wa Guinea pg. 377
17.1 Mkutano wa Kairo wa wanathiologia wa Dunia ya Tatu pg. 387
17.2 Shehe Amadu Bamba, mkuu wa Wamouridi wa Senegal pg. 390
17.3 Simon Kimbangu wa Kongo ya Kibelgiji pg. 395
19.1 Grioti au mtambaji hadithi wa asili wa Kiafrika pg. 427

19.2 Aimé Céssaire wa Ufaransa na Léopold Sédar Senghor wa Senegal pg. 431
19.3 Wole Soyinka wa Nigeria akipokea tuzo ya "Nobeli ya Fasihi", pg. 435
19.4 Nagib Mahfuz wa Misri pg. 436
19.5 Molàra Ogundipe - Leslie wa Nigeria pg. 437
19.6 André Brink wa Afrika yaKusini pg. 440
20.1 Wasanii wakijishughulisha na shaba huko Foumban, Cameroon pg. 451
20.2 "Usanii wa Kitalii" au "Sanaa ya kiwanja cha ndege" pg. 452
20.3 Sanaa ya Kimakonde pg. 454
20.4 Iba Ndiaye na Senegal na moja ya picha zake na Kofi Antubam wa Ghana akiwa na mojawapo ya sanamu zake. pg. 457
20.5 Viteix wa Angola, akiwa na moja ya picha zake pg. 458
20.6 Bendi ya Fez, Moroko pg. 466
20.7 Mwimbaji wa Kimisri, Umm Khulthum pg. 467
20.8 Baleti ya Kiafrika ya Fodeba Keita pg. 470
20.9 Sanaa ya Kiafrika na ya Kikuba pg. 481
21.1 Cheikh Anta Diop, mwanafalsafa na mwana fizikia wa Senegal pg. 485
22.3 Maabara kwenye Chuo cha Elimu, chuo Kikuu cha Lagos, Nigeria, 1968 na Taasisi ya Ufundi ya Kenya pg. 541
23.1 George Padmore, Paul Robeson, W.E.B. DuBois, Marcus Garvey na Max Yergan pg. 548
23.2 Malcolin X pg. 552
23.3 Tamasha la Notting Hill, London pg. 561
24.1 G. 'Abd al-Nasser wa Misri, M. Kadhaffi wa Libya na Generali M. Fawsi, 24 Juni 1970 pg. 567
24.2 H. Maga wa Dahomey, F. Hauphouët-Boigny na Côte d' Ivoire, H. Dion wa Niger na M. Yameogo na Volta ya Juu, Aprili 1961 pg. 569
24.3 J. Nyerere wa Tanzania A.M. Obote wa Uganda na J. Kenyatta wa Kenya, Juni 1967 pg. 571
25.1 Mkutano wa Waafrika huko Manchesta, Uingereza, Novemba, 1945 pg. 583
25.2 Mkutano wa Kwanza wa Waafrika Wote, Accra, Ghana, Desaba 1956 pg. 585

25.3 Dukie September wa ANC, Steve Biko wa Afrika ya Kusini, Nelson Mandela wa Afrika ya Kusini, na Chifu Albert Luthuli wa Afrika ya Kusini. pg. 583
26.1 Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita wa Wafaransa na Waafrika huko La Baule, Juni 1990 pg. 604
26.2 Uwekaji wa kiwanda cha kuungia huko OCIBA, Libreville, Gabon na Wajapani pg. 605
26.3 Njaa Ethiopia, 1985 pg. 616
27.1 Mao Zedong wa China na K.D. Kanda wa Zambia, Februari 1974 pg. 633
27.2 A. Mikoyan wa Urusi na K. Nkrumah wa Ghana, Januari 1962 pg. 643
27.3 Utandikaji wa reli ya TAZARA iliyojengwa na Wachina pg. 649
27.4 Majeshi ya Kuba huko Angola pg. 657
28.1 Muungano wa Waarabu na Mkutano wa Umoja wa Nchi Huru Afrika, Kairo, 1977 pg. 668
28.2 Fidel Castro wa Cuba na Kundi la 77, 21 Aprili 1987 pg.674
28.3 Marais J.B. Tito wa Yugostavia, A. Benbella wa Ageria, A.M. Obote wa Uganda na H. Bourguiba wa Tunisia kwenye mkutano wa pili wa mataifa yasiyofungamana huko Kairo 1964 pg. 680
28.4 Mkutano wa Nne wa Nchi zizizofungamana na upande wowote, Algiers, Septemba 1973 pg. 680
29.1 Dag hammarskjöld wa Umoja wa Mataifa, Joseph Kasavubu wa Kongo, M. Tshombe wa jimbo lililojitenga la Katanga (hivi sasa shaba), P. Lumumba wa Kongo na Kanali J.D. Mobutu wa Jeshi la Kongo pg. 699
29.2 Amodou-Mahtar M'BOW wa Senegal, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO 1974-87 pg. 715
29.3 S. Nujoma wa Namibia na J. Perez de Cuellar wa Umoja wa Mataifa, siku ya Uhuru wa Namibia pg. 721
30.1 Angie Brooks wa Liberia na Binti wa Mfalme Elizabeth Bagaya wa Uganda pg. 736

## Shukrani kwa Picha

© AFP Photo, Paris, 2.3, 3.1, 6.1, 7.4, 7.6, 20.8, 24.2, 26.1, 27.2
© Agence Nationale de la photographie de presse et d'information, Algiers, 5.2
©Al-Ahram, Kairo, 28.3
© Almasy, Paris, 12.1, 22.2
© APA, picha na Ph. Khedoud, Paris, 13.2 (chini)
© Archives CRDA, Paris, 7.3
© Archives Documetation francaise, Paris, picha na OFIC, 2.2
© Associated Press, London, 29.1 (juu kushoto)
© Atelier R. Minnaert, Ubelgiji, 30.3
© Camera Press, London, 4.2 9.2, 10.5, 22.3 (juu)
© CICIBA, Libreville, Gabon, 20.5
© Collection Musèe de I'Homme, Paris, 20.9 (kushoto) kutoka kwa mkusanyo Musèe d'ethnographic du Trocadéro miaka ya 1920
© College of Art, Ghana, picha na G. Owusu, 24.4 (chini)
© Editions du Seuil, Paris, 16.I
© Ubalozi wa Nigeria Paris, 7.1
© Foundation Books Ltd., Nairobi, 16.4
© FRELIMO, I0.3
© Gamma, picha na Bonotte, Paris, 28.4
© Gamma, picha na P. Giraud, Paris, 19.2 (juu kushoto)
© Gaumont Cinèmathèque, Paris, 12.2
© Gramma, Cuba, 28.2
© HOA QUl, picha na P. Cassard, Paris I7.2
© HOA QUI, picha a M. Huet, Paris, 20.1
© HULTON-Deutsch Collection, London, 10.2, 10.4, 25.1, 25.3 (chini kushoto na chini kulia), 27.3
© IDAF, London, 25.3 (juu kulia)
© IMAPRESS, Paris, 16.5
© IMAPRESS, picha na Kol al-Arab, Paris, 19.4 (juu kulia) Idara ya Huduma za Habari, Serikali ya Ghana, 5.3
© Keysone, Paris, 2.1, 6.2, 6.3, 24.1, 25.3 (juu kushoto)
Legue of Nations, Musèe du Palais des Nations, Geneva, picha na L. Bianco, Geneva, 1.1

Le Nouvel Afrique-Asie, Paris, 7.5, 16.3, picha na L. Lis, Paris, 20.4 (juu)

Picha na Makemba, ENFOTO Agency, Angola, 27.4

© Magnum, Paris, 1.2

© Magnum, picha, na Abba, Paris, 28.1

© Magnum, picha na M. Riboud, Paris, 16.2

© Magnum, picha na S. Salgado, Jr, Paris, 26.3

picha na L. Mbuyamba, Librcvillc, Gabon, 26.2

Maison des Cultures du Monde, Paris, 20.6

© Moorland-Spingarn Research Center, Chuo Kikuu cha Howard, 23.1 (juu kulia, chini kushoto chini kulia), 23.2 picha na J.K. Muiruri, Nairobi, 13.2 (katikati)

© Musèe Royal de l'Afrique centrale, Tervuren, 8.1, 8.2

© Newslink Africa, London 5.1, 9.3, 14.2 juu 22.3 (chini) 25.2 M. Ogundipe-Lesilie, 19.5 Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Addis Ababa (jalada la juu)

© Photochèque du Musèe de l'Homme, Paris, 19.1

© Popperfoto, London, 6.4 *Renue congolaise illustrèe*, 1959, No. 3, Machi uk. 25, 17.3 picha na J. Scott, Paris, 21.1 L.S. Senghor, 19.2 (juu kulia)

© SIPA Press, Paris, 11.1 picha na (ABC), 30.2 (kushoto)

© SIPA Press, picha na L. Chamussy, Paris, 19.6

© SIPA Press, picha na Guner, Paris 19.3

© SPADEM 1993, Paris, 20.9 (kulia) chanzo:Musèe de Grenoble, France

© Sygma, picha na J. Langevin, Paris, 15.2 picha na W. tochtermann, 13.2 (juu)

© Topham, London, 4.1, 7.2, 9.1, 9.4,10.1, 13.1, 14.1, 14.2 (chini) 22.1, 23.1 (juu kushoto) 23.3, 24.3

© UNESCO, Paris, 20.2 na 20.3, picha na P. Migeat, 30.4 (MAB/PNUE), 30.5 (MAB)

© UNESCO, picha na M. Claude, 29.2

© Umoja wa Mataifa 10.6 (UN Photo 146 221/T. Zagozdinski), 29.1 (juu kulia, chini kushoto na chini kulia)

© Picha za Umoja wa Mataifa (15267/J. Isaac) 30.1 (kushoto © U.N, picha na T. Chen)

© World Bank,

© Xinhua News Agency, Beijing, 27.1

# *Dibaji*

**AMADOU - MAHTAR M'BOW**
*Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)*

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odyssey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayoungamisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokeo yake ni kuwa kile walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo waandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kipimo, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, waandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kudumu kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, mkazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoelekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezewa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya

jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imehusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa karne nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokeazaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokea wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kimataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wameihisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umahimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika,* ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezekana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za'aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO iende hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi

1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa)* kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kumi na moja. Zaidi ya hayo, mikutano iliandaliwa kuwawezesha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha sehemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia;* kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imehusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kuteuliwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenye jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa kuwa Afrika huenda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na eneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imeonyesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yameibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwezekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokea ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara hili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika,* na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kuepukana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha

mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakiendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii.Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pekee ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za maoni ambazo yawezekana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadai kufanyike utafiti mpya na wenye uangalifu kwa maeneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaungamishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenye thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayowezesha kueleweka kwa vipengele fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*[1] yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

*Historia Kuu* inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Ametika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika

1 Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu: *Kukaliwa kwa Misri ya Kale na ufasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Pembe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika weusi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.*

harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namna za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa vya watu.

*Historia* hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maeneo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenye kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa elimu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenye ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenye uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na penginepo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoelezea picha hiyo na vilevile kuelewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu mbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyoikamilisha na mchango walioutoa unadhihirisha jinsi watu wenye usuli tofauti lakini wenye moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenye umuhimu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

# *Wasifu wa Mradi*

*B.A. OGOT*[1]
*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

(a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii haimaii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni tamko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo mikuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.

(b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi hutengwa katika kazi ambazo zimechapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchanganuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

(c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.

[1] Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wapya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

(d) Kimsingi, *Historia* inatazamwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadiliwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahsusi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vote vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa mwisho. Inapoona kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwili, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.

Utaratibu kama huu unaoonekana mrefu na mgumu, unaonekana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imeikataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa

asawidi sura. Hutokea pia wataalamu wenye ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsusi kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matoleo ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matoleo ya jalada laini kwa lugha hizo. Matoleo yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mwelekeo kwa mwenendo wa maisha yao, uelewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano miongoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maelewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.

# *Maelezo kuhusu Wendo*

Imekubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejea enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejea mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa karne, vifungu KK na WK nafasi yake huchukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii Ifuatayo:

(i) 2300 KS = - 350

(ii) 2900 KK = - 2900
1800 WK = + 1800

(iii) Karne ya tano KK = Karne ya tano kabla ya enzi ya Ukristo
Karne ya tatu WK = Karne ya tatu ya enzi ya Ukristo.

# 1 Utangulizi

Kwa malengo ya uchanganuzi, juzuu hili la historia ya Afrika limegawanywa katika nyanja za utamaduni, uchumi na siasa. Maana yetu (ya utamaduni) siyo ile maana finyu ya ujuzi wa kisanaa bali hujumuisha maadili na tamaduni katika jamii, toka maadili yale yanayohusu dini mpaka yale ya fasihi. Tunafasiri uwanja wa kisiasa kwa msingi wa namna ya Kiafrika ya uzalishaji na ugawanaji mali. Pia kulingana na ruwaza za ulaji wa Kiafrika na mifumo ifaayo ya ubadilishanaji[1]. Hii huanzia kwenye upatikanaji maji vijijini hadi kwenye utafutaji wa mfumo mpya wa uchumi duniani. Tunafasiri uzoefu wa Afrika (kisiasa) kuhusiana na maadili ya kisiasa, masuala ya uwezo na udhibiti hadi kuhusu sheria za ushirikishwaji katika jamii, hii ni pamoja na harakati za kujikomboa, mabadiliko ya kijamii na ujenzi wa taifa.


Kwa nini muda wetu katika kitabu hiki unaanzia mwaka 1935? Kwa China, vita vikuu vya pili vya Dunia haikuanza wakati Wajerumani walipoivamia Poland mwaka 1939 bali pale Wajapani walipoivamia China mwaka 1937. Sawia, kwa Afrika, Vita Kuu ya Pili ya Dunia haikuanza mwaka 1939 bali mwaka 1935, pale Mussolini alipovamia Ethiopia.


## Maadili, Uzalishaji na Uwezo

Katika uwanja wa utamaduni, kipindi hiki Afrika ilishuhudia awamu muhimu katika kuzifanya dini za kigeni za Kikristo na Kiislamu kuwa za Kiafrika. Makanisa huru ya Kikristo yaliibuka, hususan katika Afrika ya Kati na Kusini. Katika maeneo kama Senegal, Uislamu kwa kina ulikuwa unafanywa kuwa wa Kiafrika chini ya ushawishi wa Amadu Bamba wa Muride.

[1] Kwa majadiliano kadhaa ya kiuchumi, angalia Benki ya Dunia, 1989a na Tume ya Umoja wa Uchumi wa Afrika, 1989

Afrika Kuanzia Mwaka 1935






Angalia: Kati ya 1932 na 1947 Volta ya Juu iligawanywa baina ya Sudani ya Kifaransa, Côte d'Ivoire na Niger. Kwenye kipindi hiki Ouagadougou haikuwa mji mkuu.

Ram: 1.1 Ramani ya kisiasa ya Afrika 1935 (Chanzo: kutoka kwa J. Bartholomew, 'The Citizen's Atlas of the World', *Bartholomew and son ltd*, Edinburg, 1935, kur. 122-3)

Katika uwanja wa lugha, Afrika ilipinga kutumia lugha za Ulaya na kuziweka lugha za taifa katika maandishi kwa kutumia tahajia ya Kirumi. Katika kipindi hiki Afrika haikushuhudia mapambano makali katika uzalendo wa kiisimu kama ilivyojitokeza kwa uzalendo wa kisiasa.

Kwa upande mwingine, ingawaje fasihi ya Kiafrika na sanaa za maonyesho zilikuwa zikielezwa kwa lugha za kigeni zilikazia mshikamano katika ukombozi wa kisiasa.

Katika uwanja wa uchumi, juzuu hili limejadili masuala ya umaskini na maendeleo duni katika viwango vya kiulimwengu hadi kwenye kijiji. Tunatarajia kuonyesha kwa upana zaidi maendeleo duni na ufukara uliopo Afrika.[2]

Katika uwanja wa kidemografia kuna ushahidi usiohitimishwa unaopendekeza kuwa vifo vya watoto vinavyotokea Afrika vinapungua toka watoto 40 hadi 24 kwa kila watoto elfu moja. Kuna ushahidi pia kwa matarajio ya umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 40 hadi miaka 50.

Kuhusu suala la uzalishaji wa chakula, mwaka 1980 kulikuwa na ushahidi uzalishaji uliongezeka kwa asilimia 3. Badiliko hili lilikuwa na maana, serikali zishukuriwe kwa kuanzisha sera nzuri zaidi zilizosaidia kuinua mapato kutokana na kilimo, uzalishaji wa chakula umezidi ongezeko la watu katika Afrika kwa mara ya kwanza katika miaka kumi na tano. Kuhusu mambo ya siasa katika kipindi hiki, mambo muhimu yanayoelezwa katika juzuu hili ni pamoja na ukombozi toka utawala halisi wa wakoloni hasa kipindi cha mpaka miaka ya 1960. Halafu kipindi cha mapambano ya Afrika dhidi ya serikali za Wazungu wachache katika nchi kama Zimbabwe kitashughulikiwa. Mapambano katika makoloni ya Afrika ambayo yalikusudiwa kuwa sehemu ya Nchi za Ulaya kama Algeria, na makoloni ya Ureno, ambapo Waafrika walipambana na hatimaye kunyakua uhuru wao na kuunda serikali na kujenga taifa. Haya mawili yaliyotajwa mwisho yamo katika awamu ya baada ya ukoloni. Mwisho tutachanganua ukombozi baada ya ukoloni toka uhusiano tegemezi na serikali zilizopita za kikoloni – mapambano dhidi ya ukoloni mamboleo.

Katika awamu ya baada ya ukoloni mwenendo wenye umuhimu mahususi unahusu dhana nzima ya kubadilisha uongozi wa kisiasa katika nchi za Afrika. Aina mbalimbali zimetumika, hizo ni pamoja na kurithi madaraka baada ya kifo cha kawaida cha kiongozi wa nchi. Mifano mizuri inajumuisha ule wa Daniel Arab Moi aliyemrithi Jomo Kenyatta wa Kenya na Chadli Bendjedid aliyemrithi Houari Bouhemedienne.

[2] Rejea J. Ravenhill (Mh.), 1986; Pia namshukuru Wanjiku Kironjo wa Kenya kwa kunitia hamasa

Kuna kuchukua madaraka baada ya mauaji ya kiongozi wa nchi, mauaji ya kisiasa au "ajali" zinazotatanisha. Wakati katika Nigeria, al-Haji Shehu Shagari alipochukua madaraka mwaka 1979, watatu kati ya viongozi sita waliomtangulia walikuwa wameuawa: kiwango cha "uuaji" wa asilimia 50.

Kwa hivi sasa ubadilishanaji wa madaraka ya kisiasa katika Afrika unafanywa kwa mapinduzi ya kijeshi. Zaidi ya mapinduzi sabini ya serikali yametokea katika Afrika tangu uhuru, hususan upande wa kaskazini mwa Ikweta. Kuna ubadilishanaji zaidi wa madaraka unaofanya baada ya mapinduzi ya kiraia. Nchini Uganda ilitokea mwaka 1966 wakati Obote alipompindua Rais - Mfalme Mutesa. Baada ya hapo kuliendelea kuwa na mabadiliko ya uongozi wa kisiasa baada ya vita halisi. Mfano mzuri ni wa Lule alipopata madaraka baada ya vita kati ya Tanzania na Uganda mnamo mwaka 1978-9. Tumeshuhudia pia mabadiliko ya uongozi wa kisiasa baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe; mfano dhahiri kabisa ni wa Jeshi la Museveni lililopata madaraka nchini Uganda baada ya Obote na Okello.

Zaidi ya hayo, kulikuwa na kurithiana kisiasa baada ya machafuko. Hali hii imetokea mara mbili nchini Sudani: kuanguka kwa utawala wa Jenerali Aboud mwaka 1964 na yale machafuko ya kudai demokrasia ya mwaka 1985 yaliyouangusha utawala wa Nimeiri.

Kuna mifano ya kurithiana kisiasa baada ya utawala wa kijeshi kukabidhi madaraka kwa raia kwa hiari. Hii inajumuisha Jenerali Obasanjo wa Nigeria kuachia madaraka kwa raia mnamo mwaka 1979. Luteni J. Rawlings wa Ghana alifanya vivyo hivyo mwaka 1979.

Ama kuhusu kuachia madaraka baada ya kushindwa kwenye uchaguzi, Mauritius imekuwa ndiyo mfano pekee kwa muda mrefu hapa Afrika. Katika juzuu hili sura ya 15 na 16 zitatalii sababu za kuwa na ugiligili wa kiasasi katika Afrika baada ya Ukoloni. Mwisho kuna kurithiana kisiasa baada ya kujiuzulu au kustaafu kwa kupenda, mfano wazi zaidi ni wa Rais Léopold Sédar Senghor wa Senegal.

Tunatarajia kuonyesha kuwa migogoro ya kisiasa katika Afrika inajumuisha masuala ya namna ya kufanya mataifa yetu kuwa na utamaduni ulioshikamana na kufanya nchi zetu kuwa halali na zenye mamlaka. Juzuu hili litashughulikia suala la haki za binadamu katika Afrika baada ya ukoloni.

Kwa sababu ya tabia mahususi ya karne ya ishirini ya kuwa karne ya uchumi wa kweli wa dunia na siasa za dunia, historia ya Kiafrika inaweza kueleweka kikamilifu katika muktadha mpana wa historia ya dunia. Kinachojitokeza kutokana na hadithi za kipindi hiki ni namna Waafrika walivyosaidia kurudisha utu huko Ulaya, na jinsi Ulaya ilivyosaidia kurudisha Uafrika Afrika. Historia ya kuondoa ukoloni katika karne ya ishirini ni moja ya mambo makubwa ya kipindi chote cha

kihistoria ya binadamu. Mikinzano ya kipekee ilisuluhishwa katika mchakato huu.[3]


Jambo muhimu kulitaja hapa ni kuwa kusingelikuwa na taifa la Nigeria, Kenya au Ivory Coast bali ni kwa sababu ya wakoloni Wazungu. Hivyo Ulaya ndiyo mzazi haramu wa urazini wa kitaifa wa Waafrika walio wengi. Je ubeberu wa Magharibi ndio pia chanzo cha urazini wa Afrika yote? Ili kulijibu hili, kuibuka kwa utambulisho mpya na nia mpya kati ya watu wa Afrika ni lazima kuchunguzwe. Kama urazini wa kitabaka katika Afrika sehemu fulani ni matokeo ya ukuaji wa ubepari, urazini wa utaifa katika bara la Afrika kwa sehemu fulani umetokana na ukuaji wa ubeberu. Ni kutokana na hilo kwamba ubeberu wa Ulaya ulisaidia watu kujitambua, kwa mfano Mkikuyu kumtambua Myoruba kama "Mwafrika mwenzake" na ukasaidia watu wa Algeria kutambua kuwa Wazulu ni wenzao katika bara la Afrika.

Kuna ukweli kuwa Waafrika kwa muda mrefu wanafahamu na wana uzoefu wa fahari yao ya kujitambua kama Wakikuyu, Waamhara, Wayoruba, Wabeba, Wazulu na Waarabu bila ya kusaidiwa na Wazungu. Lakini katika kitabu chake cha *Falsafa ya Mapinduzi*, Gamal Abd al-Nasser alitoa mwito kwa Wamisri kukumbuka kuwa wao sio tu Waarabu na Waislamu bali pia ni Waafrika. Alikuwa anarejea kwa uwazi katika juhudi za pamoja dhidi ya utawala wa kigeni katika bara nzima la Afrika. Ubeberu wa Ulaya uliamsha urazini wa bara la Afrika.

Ethiopia ni mfano wa wazi wa suala hili. Wakati Waitaliano walipoipiga Ethiopia mwaka 1935, Ethiopia ilijitambua kuwa ni sehemu halisi ya hali ya Afrika wakati huo kutokana na Wazungu kuvamia ardhi yao na uonevu kwa watu wao. Kuwepo kwa ubeberu wa Wazungu na ubaguzi wa rangi kulisaidia kukuza chombo cha utambuzi mpya wa Afrika yote.

Hata hivyo kuna athari gani za Afrika kwa nchi za Magharibi? Kwa kupigania uhuru wake, Afrika ilisaidia pia kubadilisha mwelekeo wa Wazungu na kwa hakika historia ya dunia pia. Juzuu hili kwa hakika linakazia maendeleo ya kihistoria katika Afrika yenyewe. Lakini ni muhimu kukumbuka kuwa Afrika halikuwa bara lililokuwa tulivu tu kwa ajili ya wengine kufanya wanavyotaka. Juhudi zilizofanywa na Afrika zimesaidia kubadili matarajio ya wale wengine. Historia yote ya kuondokana na ukoloni katika karne ya ishirini inabidi iangaliwe kama sehemu ya mfumo ambao wanaokandamizwa wamejifunza

[3] Tunafafanua 'kuondoa ukoloni' kuna mchakato ambamo sheria za kikoloni iliishia, asasi za kikoloni zilipvunjwa na tabia na mitindo ya kikoloni kuachwa. Kinadharia jitihada za kuondoa ukoloni zinaweza kuchukuliwa ama na nguvu za utawala au watawaliwa. Katika hali halisi, kuondoa ukoloni mara nyingi kunalazimishwa na jitihada za wanaokandamizwa.



*1.1 Mfalme Haile Selassie akihutubia Umoja wa Mataifa kuhusu uvamizi wa Ethiopia dhidi ya Italia*

kikamilifu wao ni nani na wanaokandamiza wameanza kujifunza juu ya uwajibikaji wa kiutu. Historia ya Afrika tangu 1935 ni lazima ishughulikiwe katika muktadha wa mikinzano mikubwa huo.

## Waafrika ni nani?[4]

Alikuwa mshairi na mwanadiplomasia wa Sierra Leone, Davidson Abioseh Nicol, aliyeandika hivi mwaka 1969:

Wewe siyo nchi, Afrika,
Wewe ni dhana,
Iliyopo katika fikra zetu,
kwa kila mmoja wetu.
Ili kuficha woga wetu wenyewe.
Na kuota ndoto zetu wenyewe[5]

Afrika kwa hakika ni zaidi na ni pungufu ya nchi moja. Zaidi ya nchi harusini zenye mipaka bandia ilizushwa na Ulaya na kwa kipindi kinachoshughulikiwa katika juzuu hili zilijita "mataifa". Nchi zote kasoro Jamhuri ya Afrika Kusini na Namibia kufikia mwaka 1980 zilikuwa zimejiunga na shirika la kimataifa liitwalo Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU). Ndiyo, Afrika ni dhana, mimba yenye

[4] Sehemu hii ni ya A.A. Mazrui, 1986, Sura 1 na 5

[5] Tazama D.A. Nocol, 1967

ndoto za mamilioni ya watu. Lakini ni kwa namna ipi, hali ya utambulisho ambao Waafrika wanao kama Waafrika ni matokeo ya kihistoria ya kuathiriana na Wazungu?

Ukweli ni kwamba michakato inayohusiana ilikuwa inafanya kazi pamoja. Kwanza kabisa kuna ushindi wa utengenezaji wa ramani uliofanywa na Wazungu katika historia ya dunia kisayansi na kitaalamu. Walikuwa ni Wazungu walitoa majina kwa mabara yote ya dunia, bahari zote kuu, mito mingi mikuu na maziwa makubwa na nchi zilizo nyingi. Ulaya iliiweka dunia katika hali ya sasa na tunafikiria Ulaya kuwa iko juu ya Afrika na si chini yake. Ulaya ndiyo iliyoweka majira ya dunia, mstari wa Greenwich ukaanzisha saa ya ulimwengu wote. Pia Ulaya ndiyo iliyotoa jina la mstari wa Kansa na Kaprikon.

Zaidi ya hayo, Ulaya ndiyo iliyoamua wapi bara moja juu ya sayari hii ya dunia liishie na lingine lianzie. Kwa Afrika, Wazungu waliamua bara hili liishie katika Bahari ya Shamu na siyo Ghuba ya Uajemi. Wazungu inawezekana siyo walizobuni jina la "Afrika" lakini wamechangia sana katika kufanya ardhi ya bara hili tunayoitambua leo.

Njia ya pili ambayo Ulaya ilifanya Afrika kuwa ya Kiafrika ni mbinu ya ubaguzi wa rangi. Yanayohusiana na ubaguzi wa rangi ni ubeberu na ukoloni; mambo hayo mawili yalisaidia kuongeza ujitambua zaidi kwa Waafrika na ilisaidia katika uanzishaji wa *Pan Africanism* (Afrika yote) katika kipindi hiki.

Urazini wa Weusi walio chini ya jangwa la Sahara ni namna moja ya utambulisho wa Uafrika; hali hii ilizaliwa kutokana na kiburi cha ubaguzi wa rangi wa Wazungu. Ulijieneza Bara zima hasa kutokana na kuvamiwa kwa Ethiopia mwaka 1935. *Negritude,* vuguvugu la wasomi lilianzishwa kutokana na utamaduni maalum wa kiburi cha ubeberu wa Kifaransa. Ni kutokana na usuli huu ndipo Ulaya inaonekana kuwa ilifanya Afrika kuwa Afrika yote. Kipindi kinachoshughulikiwa katika juzuu hili ni umuhimu mahususi katika mlolongo huu.

## Enzi za Afrika nzima

Katika karne ya ishirini, historia ya Waafrika ilihusishwa kwa karibu sana na mwelekeo wa kiulimwengu. Sura ya 39 juu ya Afrika na Umoja wa Mataifa waonyesha uhusiano huo kisiasa. Kipindi kinachoshughulikiwa katika juzuu hili ni pamoja na kutokomea kwa enzi za silaha za nyuklia na kuibuka kwa enzi za anga - mabadiliko mawili muhimu katika mahusiano yetu na ulimwengu. Sura zitakazofuata zitagusia juu ya mwelekeo huo wa kisayansi, kuna mambo mawili ya kuzingatia. Ni kwa namna gani Afrika imeathirika na kutawaliwa na uvumbuzi

huu mkubwa wa kiteknolojia? Ni kwa njia gani Afrika imechangia katika mageuzi haya makubwa?

Kwa uhakika kulikuwa na vichocheo kiulimwengu vya aina mbili: Mdororo mkuu wa shughuli za kiuchumi na vita vikuu vya pili. Kati ya vichocheo hivi viwili, ni kipi viliathiri historia ya Waafrika zaidi na kwa undani, na kipi kilirudisha zaidi utu wa nchi za Magharibi? Matokeo ya kuanguka kwa Wall Street (mtaa uliokuwa makao ya biashara kubwa za kibepari) mwaka 1929 uligusa watu kwa muongo mzima uliofuata na ulijumuisha baadhi ya madhira ya mdororo wa uchumi kama kuibuka kwa Hitler.

Je, Mdororo Mkuu wa uchumi uliwaumiza watu wa dunia ya Magharibi mara moja na wakati huohuo kusaidia Afrika kujikomboa? Kama hivyo ndivyo, kulikuwa na uwiano gani halisi? Ni kwa namna gani Ulaya wakati huohuo ikafanywa kuwa na utu zaidi? Ni kwa vipi Afrika ikawa Afrika kwa wote? Baadhi ya masuala haya yatawekwa wazi katika sura zinazohusika.

Lakini kama kila mgogoro mkubwa wa ulimwengu unahusisha Afrika, tumefikia mahali ambapo mgogoro mkubwa wa Afrika pia ni sehemu ya ulimwengu. Katika kipindi hiki kinachoshughulikiwa katika juzuu hili ni kweli kuwa kila kinachotikisa Afrika ni dhahiri kuwa kitakuwa kwa kiasi fulani kinahusisha dunia nzima. Kwa mfano mgogoro wa mwanzoni mwa mwaka 1960 wa Kongo-Léopoldville na ule wa Chadi wa 1970 na vita vya ukombozi vya kusini mwa Afrika ni mifano michache. Ushahidi unazidi kuonyesha kuwa kwa vile kuna sehemu ya Afrika inayohusishwa katika kila tatizo lolote la kiulimwengu, basi kuna sehemu ya dunia inayohusishwa kwa kila msiba unaoipata Afrika. Mgogoro wa Suez utajitokeza katika juzuu hili kama kiungo kimoja kikuu cha masahibu ya dunia na mwelekeo wa Afrika.

Zaidi ya hayo, vita vya Biafra, ukiangalia jinsi nchi zilivyounga mkono upande mmojawapo, vilikuwa ni "vita vidogo vya dunia" bila ya matumizi ya nyuklia. Ulionyesha jinsi Afrika inavyoshirikishwa katika dunia pana ya ushindani wa kiulimwengu. Pia ilionyesha kuwa utambulisho wa Uafrika uliozaliwa kutokana na ubaguzi wa rangi na kutawaliwa na wakoloni ulikuwa dhaifu na usio na uhakika.

Unyonyaji wa pamoja waliofanyiwa Waafrika haukuwa msingi wa kutosha wa kuwa na umoja wa Waafrika. Kuungana dhidi ya ukandamizaji wa kigeni ilikuwa ni jambo moja: kuungana kwa maendeleo ya ndani ni jambo lingine. Kipindi cha awali cha historia kimeonyesha kuwa Waafrika ni mahodari wanapoungana kwa ajili ya ukombozi. Sehemu ya baadaye ya enzi hii imeonyesha kuwa Waafrika ni wazito kuungana kwa ajili ya maendeleo ya kisiasa na kiuchumi. Nguvu yote kati ya utambuzi wa Uafrika na maendeleo ya Waafrika katika kipindi hiki iliishia katika siasa za Uafrika kwa Wote."

## Mvurugiko wa vuguvugu la "Uafrika kwa Wote"

Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ulipozaliwa Addis Ababa Mei, 1963, kulikuwa na mkuu wa nchi mmoja ambaye alikosekana; huyo alikuwa Rais Sylavanus Olympio wa Togo, ambaye aliuawa mwanzoni mwa mwaka ule. Haya yalikuwa mauaji ya kwanza ya Mkuu wa nchi yaliyotokea baada ya ukoloni katika Afrika. Mapinduzi yaliyofuatia yalikuwa ya kwanza ya aina yake kusini mwa Sahara. Jukwaa likawa tayari kwa tafsiri ya uhuru katika Afrika ambayo kila mara ulishuhudia machafuko na vifo. Juzuu hili litashughulikia enzi hii ya mapinduzi ya kiserikali.

Mada nyingine katika juzuu hili ni kueleza juu ya *Pan Africanism* na malengo yake ya kuikomboa Afrika na kuleta Umoja wa Afrika, na mitazamo mbalimbali iliyotumiwa kufikia malengo hayo, kama inavyofafanuliwa katika sera na shughuli za Nkurumah na Nyerere, zikihusishwa na zile za kundi lisilo na msimamo mkali la Monrovia na za kundi lenye msimamo mkali la Kasablanka. Mgawanyiko mmojawapo kati ya kundi lenye msimamo mkali na lile lisilo na msimamo mkali juu ya *Pan Africanism* mapema mwaka 1960 ulihusu suala la mizania ya kijiografia ya umoja wa Afrika. Kundi lenye msimamo mkali lilitaka umoja wa Bara zima la Afrika na lilipinga umoja wa maeneo; kundi lenye msimamo usio mkali lilikubali majaribio ya umoja wa kikanda kwanza katika kuelekea kwenye umoja wa Afrika nzima. Huu ulikuwa mgawanyiko mlalo wa *Pan Africanism* – kutoafikiana kwamba upana wa umoja wa Afrika uweje.

Kutoafikiana kwingine kulikuwa juu ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika uwe na kina gani. Huu ulikuwa mgawanyiko – wima. Je kuwe na muungano wa kisiasa wa haraka na kuunda nchi moja, au nchi za Afrika zikusudie kuwa na aina fulani tu za umoja – kama ushirikiano wa kidiplomasia wa siasa za nje, au ushirikiano wa kiuchumi, au ushirikiano wa mawasiliano na kushirikiana huduma. Kina kilichofikiriwa mwanzo OAU ilipoanzishwa mwaka 1963 kilikuwa si kirefu bali upana wa umoja ulikuwa ni kwa Bara zima, ukijumuisha nchi za Kiarabu na nchi za Afrika ya weusi.

Mwaka 1966 na mwaka 1967 kwa mfuatano huo, matukio mawili yaliyotokea yalisaidia kubadili chanzo cha mgawanyiko kati ya wenye msimamo mkali na wale wasio na msimamo mkali katika siasa za Afrika.

Mwezi Februari 1966 Rais Kwame Nkrumah wa Ghana alipinduliwa katika mapinduzi ya kijeshi. Mwaka uliofuatia Rais Julius Nyerere alitangaza msimamo wake mkali kwa kuanzisha Azimio la Arusha la Ujamaa na Kujitegemea. Toka wakati huo Julius Nyerere alianza kuonekana kama mmoja wa sauti ya wenye

siasa kali katika jukwaa la Afrika. Dar es Salaam ikawa makao makuu ya shughuli za ukombozi za OAU iliyokuwa inawakilishwa na Kamati ya Ukombozi wa Afrika.

Hata hivyo mwaka 1973 wakati OAU ilipokuwa inaadhimisha miaka kumi tangu ilipoundwa ilionekana kama kwamba siasa kali ilikuwa inadidimia. Gamal 'Abd al-Nasser alikufa mwaka 1970, Nkurumah alikuwa uhamishoni na alifariki muda mfupi baadaye. Milton Obote alipinduliwa na Idi Amin na nchi kama Kenya, Coted'Ivoire* ziliegemea zaidi upande wa kulia katika miaka ile kumi. Historia ikasaidia kuokoa siasa kali ya Afrika hususan OAU ilipoanza mwongo wake wa pili. Mambo mawili muhimu mwaka 1974 yalichangia kwa jambo hili. Moja lilikuwa mapinduzi ya Ethiopia, ambayo kwayo nchi hii ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya watu katika Afrika ilikuwa inaingia katika kufuata mtazamo wa siasa za Marx na Lenin.

Lakini pia mwaka 1974 kulitokea mapinduzi huko Lisbon, Ureno. Mapinduzi hayo yaliiangusha himaya ya Ureno. Sura zijazo zitaonyesha jinsi himaya hii kongwe kuliko himaya zote za Wazungu Afrika ilivyosambaratika haraka, ikiacha nyuma wanachama wapya wenye siasa kali wakikaribia kuingia kwenye siasa za OAU. Kwa hakika suala la uhuru wa Angola kwa muda mrefu lilikuwa na mgawanyiko. Wenye siasa zisizo na msimamo mkali katika Afrika walipendelea serikali ya umoja wa kitaifa unaojumuisha vyama vitatu vya ukombozi (MPLA, UNITA na FNLA) wakati wenye msimamo mkali walipendelea MPLA peke yake. Angola, mwanachama mpya mwenye msimamo mkali, ikawa inatarajia kujiunga na safu ya walio mrengo wa kushoto katika OAU.

Miaka mitano baadaye Zimbabwe huru ilipendelea mrengo wa kushoto katika OAU. Kwa maneno mengine, kati ya sababu zilizopendelea wenye msimamo mkali katika miaka ya 1980 katika OAU ilikuwa ukweli kuwa kila nchi ya Kiafrika iliyopata uhuru kati ya 1975 na 1980 ilichagua itikadi ya mrengo wa kushoto; hii inamaanisha makoloni yote yaliyokuwa ya Ureno pamoja na Zimbabwe.

Pili, kila mapinduzi ya kweli katika Afrika kiitikadi yalionekana kusogea upande wa mrengo wa kushoto. Mapinduzi muhimu zaidi ya miaka 1970 ni ya Ethiopia. Somalia pia ilielekea kushoto wakati wa msimamo wa miaka ya 1960. Pia Libya ilikuwa na msimamo mkali wa kweli chini ya Muammar Kadhaffi.

Mapinduzi ya kijeshi katika Afrika yalikwama na mielekeo mchanganyiko ya kiitikadi. Mapinduzi ya Ghana na Burkina Faso ya mwaka 1980 yalikusudiwa

*Kuanzia 1985 serikali ya nchi ambayo zamani iliitwa "Ivory Coast" kwa Kiingereza iliamua kuwa jina lake litakuwa 'Côte d'Ivoire katika lugha zote.

kujaribu kuelekea kwenye itikadi za kushoto, ambapo mapinduzi ya Guinea (Konakry) ya mwaka 1984 yalikuwa ya kuelekea kulia.

Kwa wastani, tangu kuanzishwa OAU kwa ujumla katika miaka ya 1980 iliinamia kwa namna fulani upande wa kushoto. Upigaji kura juu ya Jamhuri ya kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahara (SADR) ulionyesha muungano mpya wa kati-kushoto ambao ulifanyika tangu 1974.

Nini matumaini ya mbele? Kwa kawaida mambo ya siku zijazo siyo suala la kuzingatiwa na mwana historia. Hata hivyo tulipoipa sura ya mwisho ya juzuu hili kichwa cha "kuelekea mwaka 2000" tulikuwa kwa undani tunatambua kuwa historia ya nyuma inaweza kutumika kukadiria mwelekeo wa baadaye. Waafrika wamefanikiwa kujiona ni wamoja katika ukombozi; lakini bado hawajaweza kujiona kwa kiasi cha kuridhisha kuwa ni wamoja katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na hawajaungana kisiasa.

Vipi kuhusu Umoja wa Uafrika wa wanawake? Mahali gani wanawake wanaingia katika mlinganyo huu wa Kiafrika? Katika sura ya 19 juu ya maendeleo ya fasihi ya kisasa ya Waafrika linatajwa shairi la Leopold Senghor liitwalo "mwanamke aliye uchi, mwanamke mweusi". Katika shairi hilo Afrika ni mwanamke (umejifunika katika rangi yako ambayo ndiyo maisha, katika fani ambayo ndio uzuri).

Habari za kujitawala katika juzuu zinaweza kuonekana katika hatua tatu: hatua ya mapambano yakujitawala (mapambano ya kudai uhuru); hatua ya kutumia uwezo wa kujitawala (matumizi ya nguvu za dola); hatua ya kuwakilishwa nchi za nje (alama ya mahusiano baina ya madola). Tunatarajia kuonyesha katika juzuu hili kuwa mwanamke Mwafrika amekuwa na umuhimu katika hatua ya kwanza na ya tatu.

Kama wapiganaji, wanawake Waafrika walikuwa ni sehemu ya harakati za mapambano ya kulipa nguvu bara la Afrika.

Kama wanadiplomasia, wanawake Waafrika baadaye waliwakilisha tawala huru ambazo walisaidia Afrika kuzipata katika mambo ya dunia. Lakini kwa ujumla, katika mgawanyo wa mamlaka, wanawake Waafrika walionekana kuwa wako pembezoni na siyo katikati ya siasa.

Mmoja wa wanadiplomasia mashuhuri miaka ya 1980 alikuwa Bibi Dulcie September. Aliuawa na watu wasiojulikana Machi 1988 huko Ufaransa ambako alikuwa mwakilishi wa ANC. Kwa namna fulani tunaweza kusema kufa kwake kulikuwa sehemu ya mapambano ya kurudisha utu wa "mtu mweupe". Sasa ni muhimu kufikiria mada hii ya Afrika na urudishaji wa utu wa Ulaya.

## Afrika, Mkombozi wa Ulaya

Kumekuwapo na tabia katika historia ya kisasa kufikiria Afrika kuwa ni Bara lililotulia, mpokeaji wa mambo kuliko chanzo cha mambo. Katika miongo ya karibuni Afrika imetimiza jukumu kuielezea upya itikeli ya ubaguzi wa rangi katika mfumo wa dunia. Kuliko bara lo lote ulimwengu, Afrika imesaidia kufanya ubaguzi wa rangi katika nchi moja yoyote kuwa suala la kimataifa. Baadhi ya sura katika juzuu hili zitaonyesha kuwa kutokana na shinikizo kali kutoka kwa viongozi wa Afrika wa kabla na baada ya ukoloni, mapambano dhidi ya mfumo wa ubaguzi wa rangi yalifanywa kuwa suala la kimataifa. Watu wenye asili ya Afrika huko Marekani walijiunga na mapambano hayo mapema sana. Hawa Waafrika, Wamerikani pia walisaidia kuanzisha mageuzi ya mahusiano ya kijamii katika Amerika.

Juzuu hili pia litaonyesha kuwa Afrika ilikuwa na jukumu muhimu la kuuvua ukoloni uhalali wake chini ya maadili ya kimataifa na hasa chini ya Sheria ya Mataifa. Kwa karne nyingi, kanuni za dola na historia ya kidemokrasia ya Ulaya ilizifanya iwe halali kwa mamlaka ya Ulaya kutawala jamii isiyokuwa ya Ulaya. Ilichukua mapambano ya pamoja ya watu wenye asili ya Afrika na Asia kupinga baadhi ya majivuno na mtazamo wa kiUlaya juu ya sheria za kimataifa. Nchi za Magharibi zilisaidiwa kujirudishia utu wake.

Tutaona ya kuwa mapambano ya Afrika yalikuwa na matokeo mapana zaidi kwa wakati wetu. Wakati Chama cha Ukombozi cha Taifa cha Aljeria (National Liberation Front FLN) kilipopigania uhuru hakikuathiri tu hali ya baadaye ya Algeria, bali pia hali ya baadaye ya Ulaya. Aliporudia madaraka, de Gaulle alisisitizia kuwa na katiba mpya, na Jamhuri ya Tano ya Ufaransa ikazaliwa. Ufaransa yenye nguvu chini ya De Gaulle ikatokea pia kuwa nguzo muhimu kwa mafanikio ya Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC) katika miaka yake ya mwanzo. Dira ya De Gaulle juu ya utukufu wa Ufaransa ikaleteleza kuangalia upya jukumu la Ufaransa katika Ushirika wa Kijeshi wa Atlantiki ya Kaskazini (NATO) na uondoaji wa vituo vya majeshi ya Marekani huko Ufaransa. Hivyo, wakati wapiganiaji uhuru wa Afrika wakiwa katika harakati za kugeuza mwelekeo wa nchi yao, bila kukusudia wakati huo, pia walishiriki katika kubadili mwelekeo wa historia ya nchi za Magharibi..

Wapiganaji uhuru Waafrika katika makoloni ya Angola, Msumbiji, Guinea-Bissau, Visiwa vya Cape Verde na Sao Tome na Principe walifanikiwa kubadili mwelekeo wa historia ya Ureno. Sulubu za vita vya kupambana na ukoloni katika makoloni ya Ureno ndizo hatimaye zilisababisha mapinduzi ya kijeshi ya Ureno



Picha 1.2 Tarehe 11 Desemba 1960, huko Salembier, Wilaya kwenye mji wa Algiers, waandamanaji vijana kwa mara ya kwanza waliweza kupperusha benera ya rangi ya kijani na nyeupe ya chama cha ukombozi cha front de Liberation Nitionale (FLN)

mnamo April 1974. Wapigania uhuru wa Msumbiji, Angola na Guinea-Bissau walisaidia kufanya Ureno kuwa nchi ya kidemokrasia. Hivyo utamaduni wa kisiasa wa Ureno ulirudishiwa utu wake.

Awamu inayofuata ya Afrika kwa ujumla ni kukunja pazia la ukoloni mamboleo wa magharibi. Hii ni pamoja na kupunguza nguvu ya Magharibi katika Afrika kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine kuongeza nguvu ya Afrika juu ya nchi za Magharibi. Baadhi ya sura juu ya uchumi katika juzuu hili zitafafanua mkakati huo wa nguvu kinzo.

Katika Afrika Magharibi, mshindani wa asili wa Nigeria siyo Libya bali Ufaransa. Nigeria ni kubwa kwa mbali kuliko nchi yoyote katika eneo lile; idadi ya wakazi wake mwaka 1980 ilikuwa milioni mia moja. Hii ni idadi kubwa kuliko idadi ya watu katika yaliyokuwa makoloni ya Ufaransa ya Afrika Magharibi kwa pamoja. Hatimaye Nigeria ilibidi ichukue uongozi wa kuondoa ukoloni katika eneo lake.

Uingereza ilikuwa na ushindani mdogo na Nigeria katika Afrika magharibi, hii kwa namna moja ni kutokana na sababu ya kuwa haikuwekeza sana fedha kama Ufaransa. Ilitumia watumishi Waingereza wachache sana na haikutumia kabisa wanajeshi toka Uingereza katika makoloni yake. Fedha ya Uingereza haikulinganishwa kwa namna yoyote ile na fedha ya koloni lake lolote la zamani. Tofauti na Waingereza, Benki kuu ya Ufaransa iliilinda sarafu ya *CFA franc* ya yaliyokuwa makoloni yake.

Kwa msingi wa data juu ya utajiri wa madini na viwanda ulioshughulikiwa katika juzuu hili, tunaweza kukisia ya kuwa nchi yenye nguvu kubwa ya pili katika Afrika katika karne ya ishirini na moja pengine itakuwa Afrika Kusini inayotawaliwa na weusi. Kufuatia kuanguka kwa siasa ya ubaguzi wa rangi, wananchi weusi wa Afrika Kusini watapata na urithi wao wa haki ya kuzaliwa. Watarithi utajiri wa madini wa nchi mojawapo tajiri sana duniani, madini ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa dunia ya Magharibi.

Wananchi weusi wa Afrika Kusini pia watarithi uchumi mkuu wa viwanda katika Afrika uliojengwa kwa nguvu kazi yao weusi na utaalamu wa Magharibi. Tatu, watu weusi wa Afrika Kusini wanaweza kurithi miundo mbinu ya nyuklia na kuwa nchi ya weusi ya kwanza kuwa na nguvu za nyuklia.

Kwa muda mrefu Afrika imepiga kite chini ya mnyororo wa chuma: Je mnyororo huo sasa unaweza kugeuzwa ukawa kidani cha dhahabu? Afrika kwa muda mrefu imeathirika kutokana na mnyororo wa miiba; Je kuna shada la maua upeoni? Juzuu hili linatoa takwimu kwa ajili ya kukokotolea uwezekano.

Mng'ao wa dhahabu ya Afrika Kusini usituzue kuona vizuri kabla ya wakati.

Juhudi za kihistoria za kulegeza mnyororo wa chuma zimekuwa na mafanikio yake lakini mapambano yaendelee. Juzuu hili linahusu miaka ya mwisho ya siasa za Afrika kulaani ukoloni na pia kuhusu mwanzo wa ukombozi wa Afrika. Mahali ambako spishi ya binadamu ilianzia, uhuru wa binadamu hatimaye utapatikana.

Katika kuanza hadithi ya Afrika katika mfululizo huu wa UNESCO, tumeona bara lililorithisha spishi ya binadamu kujaza sayari ya dun'ia. Mwisho wa hadithi ya Afrika sasa tutaona bara lililo njiani kurudisha utu wa spishi hiyo katika misingi ya uadilifu. Miaka tangu 1935 imewazindua Waafrika na kuwatia katika kina kipya cha utambulishi wa binadamu kiulimwengu. Hiyo ndiyo hadithi ya juzuu hili.

# 2 Pembe ya Afrika na Afrika

Katika miaka ya 1930 Pembe ya Afrika na Afrika Kaskazini zilitikiswa na migogoro na mabadiliko yaliongezeka na kuharakishwa na vita. Kipindi baada ya vita uwiano mpya ulianzishwa na mara ukatishiwa na vuguvugu za kisiasa zilizoibuka kutokana na vita, vikiwa vyenye nguvu na imara.

## 1935–1940: Miaka ya migogoro ya kiuchumi, kijamii na kisiasa

Uchumi wa nchi mbalimbali za Afrika Kaskazini na Pembe ya Afrika uliweza kuunganishwa katika mzunguko wa uchumi wa dunia tokea kipindi cha pili cha karne ya kumi na tisa, na uchumi wao ulikuwa ukiathiriwa na mabadilikobadiliko ya kimataifa. Biashara ya nje iliathiriwa sana na zahama za uchumi wa Ufaransa, Uingereza na Italia na kuanguka, ingawa mahuruji yalikuwa nafuu kuliko maduhuri kwani uathiriko huo ulitokea kwa idadi ndogo ya madini na mazao ya kilimo ambayo awali yalisafirishwa kwenda Ulaya.

Huko Aljeria thamani ya maduhuri ilipungua kwa nusu kati ya mwaka 1929 na 1935. Huko Tunisia mahuruji yalipungua kati ya miaka 1930 na 1935. Kati ya mwaka 1929 na 1931 biashara ya nje ya Moroko ilififia na hatimaye kuanguka; thamani ya mahuruji mwaka 1936 ilikuwa nusu ya ile ya mwaka 1926. Katika Libya, mabadiliko ya kupanda na kushuka yalikuwa machache kutokana na udhaifu wa biashara ya nje ambayo hata hivyo ilipungua kwa asilimia 30 kati ya mwaka 1925 na 1934[1].

Kuanguka kwa mahitaji kulisababisha mgogoro wa madini ambao ulitokea kwanza huko Tunisia. Bei ya chuma katika soko la dunia ilianza kushuka mwaka

[1] J.L. Miege, 1968, uk. 186

1925 na mahuruji ya mazao ya madini makuu yaliteremka ghafla toka faranga milioni 330 mwaka 1930 hadi faranga milioni 100 mwaka 1932. Katika mwaka 1931 na 1932 karibu machimbo yote ya risasi na zinki yalifungwa na machimbo ya manganisi yalipunguza shughuli zake[2]. Katika Aljeria uzalishaji katika sekta ya madini ulipungua kwa asilimia 75 kwa madini ya chuma katika mwaka 1929 na 1932.

Mazao ya kilimo ambayo kimsingi yalizalishwa kwa ajili ya kusafirishwa nje yalipungua sana ikilinganishwa na uzalishaji wa madini. Huko Libya kuporomoka kwa mauzo kuliathiri bidhaa zilizouzwa Tropolitania na walowezi wa Italia. Kufuatia kuanguka kwa bei ya pamba katika soko la dunia, wakulima wa Misri walijikuta wanashindwa kulipa mikopo waliyochukua kwa ajili ya kuendeleza umwagiliaji. Serikali ikawa na mlundikano wa pamba na mwaka 1931 Benki ya Mikopo ya Kilimo (ACB) ilianzishwa kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Huko Aljeria kulikuwa na tatizo la mazao ya biashara kupata soko huko Ufaransa, ingawaje soko la mvinyo lilinufaika kutokana na hatua zilizochukuliwa na Bunge la Ufaransa kulilinda. Kuanguka kwa bei ya nafaka katika soko la dunia kulichochea migogoro ya wakulima; toka 1929 mpaka 1939 mavuno yalikuwa mabaya. Kutoka mwaka 1928 shughuli zote za kilimo nchini Tunisia ziliathiriwa na migogoro hadi 1935 na hata baadaye. Hii ilisababisha kuanguka kwa ghafla kwa mapato ya wakulima. Huko Moroko mapato ya wakulima yalianguka kwa asilimia 60 kati ya 1930 na 1933.[3]

Ikilinganishwa na shughuli za madini na kilimo kwa ajili ya kusafirisha nje, mazao ya ufundi na yale ya viwandani katika nchi hizo hayakuathirika moja kwa moja wakati wa mdororo wa uchumi wa dunia; hata hivyo kuanguka kwa uchumi kwa namna fulani kulichochea migogoro ya ndani hasa kati ya mafundi stadi wa Aljeria na Tunisia.

## Umuhimu wa zahama hizo

Mdororo wa uchumi wa dunia ulizidi kuharibu zaidi hali ya zahama za ndani na kufifia kwa hali ya uchumi katika nchi mbalimbali kulikuwa wazi hata kabla ya kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya uchumi wa dunia. Hali kadhalika, kuboreka kwa uchumi wa dunia hakukuuboresha papo kwa papo uchumi wa Misri na Maghreb.

[2] R. Galissot, 1964 uk. 56
[3] R. Galissot, 1964, uk. 67

Urefu wa kipindi cha ukoloni na kiwango cha mageuzi hutuwezesha kubainisha aina mbalimbali za migogoro. Huko Libya matatizo ya kiuchumi yalikuwa ni yale ya maendeleo katika kilimo ambayo yalikuwa tu ndiyo yameanza, ambapo huko Moroko mgogoro ulikuja baada ya hatua za awali na furaha ya kupanuka kwa uchumi. Huko Aljeria na Tunisia mgogoro ulikuwa wa uchumi wa kikoloni kwani misingi yake ilitikiswa. Huko Misri mbali na mdororo wa uchumi wa dunia, kulikuwa na maendeleo kidogo ya kiuchumi na hii iliipa nchi mageuzi ya mwelekeo wake kwa ujumla.

Libya ilifanywa koloni la Italia mwaka 1916 bali utawala na maendeleo vilizuiwa na upinzani hadi 1931. Uvamizi na ushindi wa Waitalia uliitia Libya hasara kubwa ya binadamu na uchumi. Uchumi asili ambao ulikuwa usaidie kutatua matatizo yaliyotokana na vita vya Waitalia uliathiriwa vibaya na soko la dunia ambalo halikuwa linaunganisha uchumi wote. Mwaka 1928 ukoloni wa kiuchumi ulitelekezwa na kuwekwa ukoloni wa ulowezi mahali pake. Sheria za mwaka 1928 zilileteleza wimbi la kwanza la uhamiaji na kufuatiwa na la pili toka mwaka 1938 lililoanzishwa na Mussolini. Lakini kama ilivyokuwa Algeria katika kipindi cha pili cha karne ya kumi na tisa, ukoloni wa wakulima huko Libya ulipata shida ya kutokuwa na mtaji na pia kukosekana kwa soko kubwa na wafanyakazi wa mishahara.

Huko Moroko baada ya mgogoro wa kwanza wa ukuaji wa 1924 na 1925 upanukaji ulirejea mpaka 1931. Kati ya hapo na 1936 biashara ya nje ilididimia na biashara za kubahatisha, hususan katika kilimo na madini ziliathirika. Hata hivyo shughuli za viwanda zilisaidia kunyanyua biashara mpya kama ya usagishaji nafaka, usindikaji na utafutaji wa mafuta, utengenezaji wa tumbaku na viwanda vya manyoya ya farasi viliendelezwa. Kwa ujumla, ingawa ukuaji wa miaka 1925-1930 ulipotea, shughuli za viwanda ziliweza kuistahimili zahama na kufufuka.[4]

Huko Tunis na Algeria kimsingi matatizo yalikuwa yale ya uchumi wa kikoloni ambao umeshuhudia mageuzi ya haraka na vipindi vya kupanuka. Huko Tunisia uchumi ulidhoofishwa na mfululizo wa majanga ya asili: ukame ukifuatiwa na mafuriko na uvamizi wa nzige, ambayo yote yalikutana na mdororo wa uchumi wa dunia wa mwaka 1930 na 1931. Huko Algeria mgogoro wa kijadi ulikuzwa na zahama ya sekta ya kikoloni ambayo ilikuwa ya kwanza kuathiriwa na mdororo wa uchumi wa dunia.

Ingawaje uliathiriwa na mdororo wa uchumi wa dunia, uchumi wa Misri ulinufaika kutokana na mambo mawili: Kwanza kuanzishwa kwa shirika la Misr ambalo

[4] R. Galissot, 1964, uk. 72

lilianzisha kampuni za meli mwaka 1932 na 1934, kampuni ya kuchambua na kusokota pamba mwaka 1937, na kampuni za biashara mwaka 1940. Pili, kurudishwa kwa uhuru wa fedha na kodi ya ushuru mwaka 1930. Mambo haya mawili yaliwezesha kuendelea kwa viwanda ambako hakukusita mpaka wakati wa vita.

Katika Pembe ya Afrika, udhaifu wa mabadiliko ya kiuchumi na wa kuunganishwa kwa eneo hilo katika mkondo wa biashara wa dunia vilipunguza athari za mdororo wa uchumi wa dunia zilizotarajiwa.

Katika Sudan, kuanzishwa kwa mtandao wa reli na kilimo cha pamba kule Misri vilifanya uchumi uweze kuhisi mabadiliko yoyote ya kimataifa. Reli muhimu kimkakati kutoka kaskazini mwa mpaka wa Khartoum iliyojengwa na Lodi Kitchener mwanzoni mwa karne ya ishirini iliunganishwa na maeneo yanayolima pamba ya Bahari ya Shamu mwaka 1924. Pamba ya Wamisri iliendelezwa baada ya vita vikuu vya kwanza katika Gezira Mashariki ambapo umwagiliaji toka bwawa la Sennar ulifanyika. Kanda nyingine za kilimo zilianzishwa na mwaka 1929 makubaliano kuhusu namna ya kugawana maji ya mto Nili yalitiwa saini huko Misri[5]. Maendeleo yaliyotokea kwa pamoja ya mtandao wa reli na kilimo cha pamba yaliongeza ukubwa wa uchumi wa fedha na miaka ya 1930 pamba ndiyo lilikuwa zao kuu la biashara ya nje. Wakulima waliathiriwa moja kwa moja na mgogoro ambao baadaye kwa namna fulani uliathiri wafanyakazi wa serikali ya Sudan.

Huko Ethiopia, mwanzoni mwa karne ya ishirini biashara ya nje ilikuwa ndogo na haikuzidi faranga milioni 50. Mahuruji makuu yalikuwa pembe za ndovu, dhahabu na kahawa, wakati bidhaa za pamba, silaha na risasi zilikuwa ndizo maduhuri. Usafirishaji wa bidhaa kutoka bara hadi bandarini uliwezekana baada ya reli ya Jibuti kufika Addis-Ababa mwaka 1917.

Kuongezeka kwa idadi ya watu[6] na kukua kwa miji tayari kulikuwa kumeanza kuonekana katika takwimu kabla ya 1930, lakini kwa wakati ule suala hilo halikupewa umuhimu na waendeshaji wafawidhi wa makoloni. Ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa miji ulitokana na mgeuko wa polepole na wa zamani ukawa mkubwa na kuwa sehemu ya muundo wa jamii katika kipindi cha 1930 hadi 1945.

[5] Collectif, 1966, uk. 472

[6] Takrimu zote za idadi ya watu kwenye kipindi baina ya vita ni za wastani

## Kuongezeka kwa idadi ya watu na kukua kwa miji

Mpaka katikati ya karne ya ishirini, hali ya zamani ya kuwa na kiwango kikubwa cha uzazi na vifo iliendelea. Hata hivyo sensa za idadi ya watu zilizoshafanywa wakati wa kipindi cha baina ya vita vikuu zinaonyesha mwanzo wa kukengeukwa kwa viwango hivyo. Huko Moroko ingawaje kiwango cha vifo kilipungua kwa kiasi kikubwa, kiwango cha uzazi kiliongezeka kwa wastani wa watoto 38 kwa kila watu 1,000 kati ya mwaka 1932 hadi 1935 mpaka wastani wa watoto 44 kati ya mwaka 1941 mpaka 1945[7]. Katika Aljeria Kaskazini kiwango cha uzazi kilikadiriwa kuwa watoto 38 kwa watu 1,000 kati ya mwaka 1921 na 1925 na kilipanda hadi watoto 43 kwa watu 1,000 kati ya mwaka 1926 na 1930. Baadaye kilipungua hadi watoto 42 kwa kila watu 1,000 kati ya 1936 na 1940. Kiwango cha vifo kilipungua toka watu 19.8 kwa kila watu 1,000 katika kipindi cha mwaka 1921 hadi 1925 hadi watu 16.6 kwa kila watu 1,000 kati ya mwaka 1936 na 1940[8].

Moroko ilikuwa na kiwango cha juu cha uzazi katika Maghreb na katika Tunisia; idadi ya watu iliongezeka kwa asilimia 25 kati ya 1936 na 1946. Huko Algeria mabadiliko makubwa ya kidemografia ambayo yalikuwa madogo mwaka 1921 yaliongezeka mwaka 1931 na kutoka mwaka 1921 hadi 1936 kulikuwa na ongezeko la asimilia 1.53[9]. Idadi ya watu huko Misri iliongezeka kwa wastani wa watu 180,000 kila mwaka kutoka 1920 hadi 1940. Kwa upande mwingine Libya ilikuwa na watu wachache na ikapoteza watu wengi sana wakati wa mapambano ya kupinga uvamizi wa Waitaliani, hasa huko Sirenaika ambako majeshi yalikaa kwa muda mrefu.

Ingawa kupanuka kwa miji kwa namna moja kulitokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, lakini kwa kiasi kikubwa kulikuwa ni matokeo ya watu wa vijijini kuhamia mijini kipindi kifupi kabla ya vita vikuu vya pili. Matokeo yake ni kuwa na mitaa ya vibanda vibanda. Wakazi wa vijijini wakitafuta kazi au misaada walihamia mijini ambako waliishi kandokando ya miji. Kwa Moroko, Algeria na Tunisia uhamaji wa namna hiyo uliendelea hadi nchi ya Ufaransa.

Uhamaji ulianza Moroko kabla ya kuanzishwa kwa himaya lindwa na ukaongezeka mwaka 1931 kutokana na mgogoro, na baadaye mwaka 1937 ukaongezeka zaidi kutokana na ukame na homa kali ya chawa. Huko Tunisia na Algeria mitaa ya vibanda vibanda ilipanuka wakati huohuo. Idadi ya watu wa mji

[7] J.L. Miege, 1950, uk. 55
[8] C.R. Ageron, 1979, Juz. 2, 471-2
[9] A. Nouschi, 1962, uk. 31

wa Tunis ilikuwa inakua kwa asilimia 1.04 kwa mwaka kati ya 1921 na 1936, na idadi ya watu kandokando mwa mji ilikuwa inaongezeka kwa asilimia 2.61. Nchini Libya mji pekee mkubwa ulikuwa Tripoli ambao idadi ya watu iliongezeka haraka lakini Oasisi ziliendelea kubaki ndiyo vituo vikubwa vya kiuchumi. Nchini Misri ni Kairo pekee ndiyo iliyopata athari za wahamiaji toka vijijini na idadi ya watu iliongezeka toka 865,000 mwaka 1920 hadi 1,527,000 mwaka 1940[10]. Nchini Moroko upanukaji wa miji uliharibu utaratibu wa awali wa miji kulingana na ukubwa, na kati ya mwaka 1931 na 1936 Kasablanka ukawa mji wenye watu wachache zaidi ukiwa na wakazi 275,000 mwaka 1936 dhidi ya watu 163,000 mwaka 1931. Idadi ya watu wa mijini nchini Algeria ilikadiriwa kuwa 508,235 mwaka 1926 na iliongezeka maradufu mwaka 1948[11].

Katika Pembe ya Afrika, idadi ya watu wa Sudan iliongezeka mara dufu kati ya mwanzo wa karne na mwaka 1939 iliposikia milioni 6[12]. Huko Ethiopia maendeleo ya uchumi yaliyoletwa na Waitalia yalileta upanukaji wa miti. Mwaka 1935 mji wa Addis Ababa ulikuwa na wakazi zaidi ya 100,000[13]. Katika mji wa Jibuti, kutokana na ujenzi wa reli, idadi ya watu ilikuwa karibu nusu ya idadi ya nchi nzima

## Zahama za Kisiasa

Nchi zote za Afrika ziliwekwa chini ya utawala wa Wazungu katika karne yote ya kumi na tisa na mwanzoni mwa karne ya ishirini isipokuwa Ethiopia ambayo ilitawaliwa mwaka 1935 tu. Katika miaka ya kabla ya vita vikuu vya pili upinzani dhidi ya hadhi ya koloni au nchi lindwa ulitokea kupitia milolongo ya migogoro ya kisiasa ambayo ilisitishwa mara vita vikuu vya pili vilipoanza.

### *Kukua kwa Misri na Libya*

Wakati wa wimbi la pili la uhamiaji la *Ventimila*,[14] wakati huohuo Baraza kuu la kifashisti lilitoa amri huko Libya kuwa majimbo manne ya pwani yaani Tripoli Misurata, Benghazi na Dera yawe sehemu ya nchi ya Italia. Majimbo haya pamoja na Sahara ya Libya ambayo ilibakisha hadhi yake kama koloni yakawa chini ya madaraka ya moja kwa moja ya gavana-jenerali. Katika utawala ni nafasi za chini

[10] P. Leon, 1978, uk. 479

[11] C.R. Ageron, 1979, Juz. 2 uk. 473

[12] Collectif, 1966, Juz. 2, uk. 472

[13] Collectif, uk. 482

tu ndiyo zilitolewa kwa wananchi maalum, yaani ni Walibya ambao wanaweza kusoma na kuandika. Hii iliwatenga baadhi ya Walibya katika maisha kiutawala na kisiasa. Baadhi yao walikimbilia Misri ambako, kwa msaada wa Waingereza, walianzisha propaganda dhidi ya Waitalia.

Wasiwasi wa Waingereza kuhusu Italia, na propaganda za Waitalia huko Misri na vitendo vyake kule Libya na Ethiopia kulileteleza utiwaji wa sahihi mkataba tarehe 26, Agosti, 1936. Uhuru wa Misri ulithibitishwa na ushirikiano na Uingereza ulikubaliwa ambapo Uingereza ilikubali kuilinda Misri dhidi ya uvamizi wowote mradi Misri itoe huduma zote katika himaya yake vinapotokea vita.

Pia Uingereza ilikubali kuiunga mkono Misri katika lengo lake la kuzima majaribio ya kujisalimisha na kujiunga na Umoja wa Mataifa (League of Nations). Zaidi ya hayo, ukubwa wa jeshi la Misri lililoruhusiwa kuwa Sudan haukuwekewa kiwango maalumu.

Mkataba huu, ambao ulikuwa upitiwe na kufanyiwa marekebisho baada ya miaka ishirini, ulikuwa ni hatua moja mbele ukilinganisha na sheria ya umoja ya mwaka 1929. Hata hivyo haukuahidi kutoa uhuru kamili. Wanajeshi 10,000 Waingereza waliwekwa katika Ukanda wa Mfereji (wa Suez) kuhakikisha usalama wa njia za mawasiliano na kama kutatokea wasiwasi wa kimataifa au vita waliruhusiwa kukalia nchi nzima. Hivyo hali kama ilivyokuwa iliendelea nchini Sudan. Mwezi Aprili 1937, mkutano wa Montreux ulipiga marufuku amri ya kujisalimisha na hivyo Misri ikawa na sheria zake za fedha. Mwaka 1940 kanuni za pamoja ziliwekwa sahihi kati ya Uingereza na Ufaransa na hivyo kumaliza mfumo wa deni la utawala.

Mbali na makubaliano madogo ya Waingereza, kutiwa sahihi mkataba wa 1936 na kuondoka kwa majeshi ya Uingereza ulikuwa ndiyo mwanzo wa ushindi wa Chama cha Wafd na Nahhas Pasha. Alitawala maisha ya kisiasa ya Wamisri tangu 1924, na alitamani madaraka kamili mbali na migawanyiko kadhaa na kuondoka kwa wananchi wakereketwa tangu 1930. Wafd ilibakia kwenye madaraka hadi mwishoni mwa mwaka 1937. Katika uchaguzi wa mwaka 1938 kilipoteza nguvu yake wakati mfalme Farouk, aliyeungwa mkono sana na watu, alipomfukuza Nahhas Pasha na kuvunja bunge.

*Migogoro ya uhusiano kati ya Ufaransa na Maghreb*

Kuingia kwenye madaraka kwa chama cha *Popular Front* kulileta matumaini na baadaye kuondosha fikra potofu na katika mwongo wa 1930-40 uhusiano wa

[14] 'Ventimila': Masetla elfu ishirini a Kiitaliano

Ufaransa na Maghreb ulipata mgogoro wake wa kwanza. Umoja wa Wamoroko *(League of Moroccan Action)* ulianzishwa mwaka 1933 uliweka mipango ya mageuzi ambayo yalikosoa maonevu ya utawala wa nchi lindwa na kuweka kanuni ya kuheshimu uhuru wa kitaifa iliyoashiriwa na Sultani Mohamed V. Utawala wa Kifaransa ulitekeleza madai madogomadogo. Kuundwa kwa serikali ya *Popular Front* kuliwezesha kuzinduliwa kwa madai kwa kupeleka ujumbe Paris na kuanzisha vuguvugu la umma. Lakini mtikisiko maalum wa 1937 ulizimwa vikali baada ya serikali ya Blum kuanguka, na kuvunjwa kwa umoja wa Wamoroko (18 Machi, 1937).

Huko Tunis, Wadesturi pia waliweka matumaini kwa *Popular Front* na Agost 28 1936, H. Bourguiba aliwasilisha programu mpya ya chama ya *Neo-Destur*. Tarehe 4 Machi 1937 kulikuwa na matukio ya umwagaji damu katika machimbo ya fosfati (mbolea ya chumvichumvi) ya Metlaoni. Baadaye kurudi kwa 'Abd al-'Aziz Ta 'albi nchini Tunisia tarehe 5 Julai kuliashiria kudhoofika kwa hali na kuupa mbegu mpya mjadala na mapambano kati ya *Destur* ya zamani na *Neo-Des*tur. Matukio yaliongezeka sana mpaka machafuko ya tarehe 9 Aprili 1938 na kuondolewa kwa vizuizi tarehe 18 Agosti kuliacha nchi ambamo *Neo-Destur* haikuwa na uongozi lakini ilikuwa ndiyo sauti ya wananchi wa Tunisia.

Huko Algeria, kuingia madarakani kwa *Popular Front* kuliongeza matumaini. Wawakilishi waliochaguliwa, ma-*Ulama* na Wakomunisti waliitisha mkutano wa Waislamu (7 Machi 1936) ambao ulitoa hati ya madai ya Waislamu wa Aljeria ambayo yalidai kuwa na usawa na kuheshimu hadhi ya Muislamu.

Serikali ya Bluu ilitoa rasimu ya Sheria iliyowapa haki ya kupiga kura Waaljeria wasomi lakini pendekezo hilo lilikataliwa na Messali Hadj, ambaye alitaka uhuru upatikane haraka, na kutokana na upinzani toka kwa walowezi haukuweza kupitiwa na Bunge.

Mwishowe, mbali na kushindwa kwa madai haya, hali iliyoleteleza kuanzishwa kwa *Popular Front* ilisaidia vyama vya kizalendo kuwa na umoja na kutawanya mawazo yaokwa mapana zaidi.

*Kukua kwa Sudan Kisiasa*

Hali ya kisiasa ya Sudan ilikuwa inatatanisha kwa kumilikiwa kwa pamoja kati ya Uingereza na Misri, na suala la uhusiano na Misri tangu awali lilikuwa chanzo cha migawanyiko miongoni mwa wazalendo. Wakati ambapo machafuko yenye misingi ya kidini kama yale yaliyoongozwa na Wad-Halula (Mahdist) yalizimwa kikatili, mawazo ya wazalendo yalisambaa kwa wasomi. Vyama vya siri viliibuka

na kudai kumalizika kwa umilikaji wa pamoja na uhuru au muungano na Misri. Chama kilichokuwa na msimamo wa juu zaidi kilikuwa *White Flag* kilichoanzishwa mwaka 1924 na Al-Latif ambaye alipendelea uhuru wa Sudan na muungano wa bonde la mto Nili.

Mwaka 1936, kufuatia mkataba na Uingereza, Misri ilirudishiwa haki zake ilizokuwa imepoteza. Wazalendo wa Sudan ambao hawakushauriwa, waliuona mkataba huo kama changamoto kwao. Mwaka 1938 walianzisha *General Graduates Congress* ambacho mwanzoni kilijitokeza kama shirika la hisani ili kiweze kupata kutambuliwa rasmi.

### *Vita vya Ethiopia na matokeo yake*


Utamalaki wa Italia kwa Ethiopia mwaka 1935, ulisababisha kupotea kwa taifa la mwisho huru la Kiafrika. Hii ilikuwa na athari kubwa kwa wazalendo Waafrika na baadhi ya Waamerika Weusi.

Uvamizi wa Waitalia kaskazini mashariki mwa Afrika uliositishwa mwaka 1896 kwa ushindi wa mfalme Menelik kule Adowa, ulianzishwa tena na ufashisti wakati wa miaka ya baina ya vita vikuu. Kisingiziokilichotumiwa na Waitalia ni mgogoro wa mpaka wa Ogaden kati ya Somalia na Ethiopia. Baada ya kushindwa kwa tume ya usuluhishi iliyokuwa imeteuliwa na Umoja wa Mataifa na kukataa kwa Uingereza na Ufaransa kuzuia uvamizi wa Waitalia, jeshi la kifashisti la askari 400,000 wakiwa na zana bora zaidi waliteka Tigre kiulaini. Addis Ababa ilitekwa mwaka 1936 baada ya kupigwa mabomu, na mfalme alikimbilia Uingereza.

Himaya ya Italia katika Afrika ya Mashariki iliyokuwa na nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia ilikuwa ni dhahiri kwa miaka michache, na mfalme wa Italia alichukua cheo cha "Maliki wa Ethiopia." Afrika ya Mashariki iliyotawaliwa na Italia ilikuwa na watu milioni 12 na iligawanywa katika majimbo makubwa matano, kila moja likiwa chini ya gavana, na magavana wote wakawa chini ya kaimu mfalme au gavana mkuu. Ingawaje, licha ya idadi kubwa ya askari wa kifashisti kutumika ili kudumisha dola hilo la kipolisi, mapambano ya kijeshi yaliendelea kusini magharibi ambako kulikuwa na upinzani.

## Vita na Amani, 1940 - 1945

Tangu 1940 hadi 1945 kukua kwa nchi mbalimbali kulihusishwa na vita, lakini kisiasa migogoro ya kabla ya vita ilifuatiwa na kuiibuka kwa uzalendo wenye nguvu na madai mengi zaidi kuanzia mwaka 1943.



PICHA 2.1 *Kuingia kwa majeshi ya Kitaliano huko Uhabeshi*

## Nchi mbalimbali Vitani

Tofauti na vita vikuu vya kwanza vya dunia, vita vikuu vya pili vya Dunia vilifanya Afrika Kaskazini na Pembe kuwa maeneo ya vita. Uhamasishaji wa kijeshi uliathiri watu wengi zaidi, uchumi ulielekezwa kwenye nguvu za kivita na mwisho wa shughuli za kijeshi ulileta magumu ya kiuchumi na kijamii.

*Ushiriki katika Mapambano*

Kuanzia mpaka wa Algeria na Tunisia hadi karibu na Aleksandria, maeneo ya mapigano yalikuwa yameunganika kwa karibu zaidi. Kwa Waingereza Misri ilikuwa ni eneo muhimu siyo tu kwa sababu ya kuwepo mfereji wa Suez lakini pia kama kituo kikuu cha kuongozea vita. Desemba 1940 Wavell alirudisha nyuma shambulio la Waitalia lililoongozwa na Graziani. Baadaye askari wa Afrika wa Rommel (Rommel's Afrika Korps) walisimamishwa huko Al-'Alamein. Tarehe 23 Januari 1943 majeshi ya Uingereza yaliingia Tripoli na kikosi cha Leclerc, ambacho kilianzia Chad, kilifika punde baadaye na kujiunga na Kikosi cha Nane.[15]

Huko Tunisia, vitisho vya Waitalia vilikuwa na uzito kutokana na kuwapo kwa kundi kubwa la Waitalia na madai yao ya zamani kule.

[15] I.S. El-Hareir, 1985

Kufika kwa Waingereza na Wamarekani kulichochea mipango ya Wajerumani na mamia ya ndege zao zilitua karibu na Tunis tarehe 9 Novemba 1942. Usiku wa tarehe 13 na 14 Novemba waliuvamia mji mkuu na kushikilia vituo vingi vya mji. Washirika walijibu shambulio hili kutokea Aljeria, na mwezi Novemba 1942 jeshi la Uingereza lilianza kampeni ya Tunisia. Komandi Kuu ya Washirika *(Allied High Command)* ilianza kujibu mapigo tarehe 22 Aprili, na mwezi Mei, kuingia Tunis kwa Waingereza, na Wamarekani kuingia Bizerta kulikuwa ndiyo mwisho wa kampeni yao ya Tunisia.

Mara tu Waitalia walipoingia kwenye vita walishikilia miji miwili ya mpakani huko Sudan na ardhi yote ya Somalia iliyokuwa chini ya Uingereza. Lakini tangu 1941 majeshi ya Uingereza yaliyateka tena maeneo yaliyokuwa chini ya Waitalia na Mei 5, 1941 Haile Selassie aliweza kurudi katika mji mkuu wa Ethiopia.

Nchi za Afrika Kaskazini na Pembe ziligeuzwa kuwa uwanja wa vita na pia zilitoa askari kwa ajili ya majeshi ya Uingereza. Toka 1943 hadi 1945 wanaume 385,000 kutoka Afrika Kaskazini, wakiwemo watu 290,000 kutoka Algeria, Tunisia, na Moroko, walishiriki katika kuikomboa Ufaransa.[16]

Jeshi la Waafrika lilishiriki katika kuikomboa Korsika, na katika Kampeni ya Italia na ile ya Provence kabla ya kuelekea kaskazini kuungana na jeshi kubwa zaidi la Ufaransa.

Waingereza walitaka mkataba wa 1936 uanze kufanya kazi na hawakutarajia kupata msaada wo wote wa maana wa kijeshi kutoka Misri ambayo, hata hivyo, ilivunja uhusiano wake wa kidiplomasia na Ujerumani mara tu vita vilipotangazwa na pia ilivunja uhusiano na Italia tarehe 12 Juni 1940. Azimio la vita na Wajerumani na Wajapani lilikuja baadaye (26 Februari 1945). Sambamba na Waingereza, Wasudani walishiriki katika vita vya kuikomboa Ethiopia, na wakimbizi wa Ethiopia katika Sudan waliandaliwa kijeshi na Jenerali Wingate na walikwenda Gojam.

Sambamba na kuhamasisha wanaume kulikuwa na sera ya uchumi iliyoweza kusaidia nguvu za vita. Tangu Oktoba 1939 uchumi wa Moroko ulitangazwa kuwa ni uchumi wa vita na uchumi wa Algeria na Tunisia uliimarisha (ili uchangie vita).

Kituo cha Ugavi cha Mashariki ya Kati kilichoanzishwa huko Kairo wakati wa kiangazi cha mwaka 1941 kilishughulikia kuendeleza uzalishaji na kuielekeza upya biashara, wakati ambapo viwanda vya ndani vilikuwa tayari vinatumika kikamilifu.

*Matatizo ya Uchumi wakati wa Amani*

Kutokana na kuvurugwa kwa usafirishaji, biashara ya nje ilianguka, na kupanda

[16] P. Leon, 1978, uk. 557



*Picha 2.2 Askari wa Kifaransa wakiwa vitani kwenye jangwa la Tripolitania*

kwa bei kulileteleza kuanzishwa kwa biahsara ya magendo. Zaidi ya hayo, mahitaji ya vita yalileta ukuaji wa viwanda wa kiasi fulani; ukuaji huo ulizorota wakati yaliporejeshwa mahusiano ya kibiashara na Ulaya. Ukweli ni kwamba wakati wa vita Misri ilinufaika: kuongezeka kwa ukubwa wa jeshi la Misri na malipo yaliyolipwa na nchi marafiki kwa raia walioajiriwa yaliongeza mahitaji ya bidhaa zilizotengenezwa viwandani. Uwekezaji ulielekea kwenye viwanda wakati Kituo cha Ugavi cha Mashariki ya Kati kilitoa ushauri wa kiufundi kwa mameneja wa viwanda au kutoa mali ghafi. Kati ya 1939 na 1945 uzalishaji viwandani uliongezeka kwa asilimia 38.[17] Huko Maghreb vita vilidhihirisha utegemezi (wa nchi hizo) kwa uchumi wa Ulaya. Huko Tunisia, kuzuiwa kwa vyanzo vya uzalishaji wa malighafi, kulitoa mwanya kwa uchimbaji wa madini ya liginati (makaamawe yasiyokomaa), na ili kuchukua nafasi ya bidhaa za Ufaransa ilifufua viwanda vya ufundi sanifu. Kwa vile maduhuri yalikuwa machache kama siyo kutopatikana kabisa, biashara nyingi zilianzishwa huko Aljeria tangu 1940, na kampuni kadhaa kubwa zilianzisha matawi yake (*Lesieur oil, Saint-Gobain pottery* na *Lafarge*

[17] S. Radwan, 1974, uk. 193

*cement)*. Uchumi wa Moroko ulilazimika kufanya juhudi kama hizo kwa uzalishaji wa nyumbani. Matokeo yake ukubwa wa uwekezaji wa viwandani ulikua na kuwa sawa na ule uliokuwapo miaka 27 kabla.

Kurudia kwa amani kulileta msitisho wa ukuaji wa viwanda, na hali ya kiuchumi na kijamii iliendelea kuwa mbaya kutokana na kurejea kwa askari waliokuwa vitani, kufungwa kwa viwanda vilivyohudumia vita na hali ya hewa isiyofaa kwa kilimo. Huko Misri kulitengwa fungu la fedha za kuwasaidia wafanyakazi wa serikali na wale waliopunguzwa jeshini. Ili kupambana na ukosefu wa kazi mpango wa miaka mitano wa kundeleza miradi mikubwa ulipewa pauni milioni 25 mwaka 1945. Ardhi ya serikali pia iligawanywa kwa wakulima kwa masharti nafuu lakini hatua zote hizi hazikufua dafu katika kurudisha hali nzuri ya kijamii. Tangu 1945 kurudishwa kwa mikondo ya biashara huko Tunisia hakukuweza kuzuia miaka mitatu ya njaa mfululizo kufuatia ukame uliosababisha kukosekana kwa mavuno ya nafaka. Matokeo yake maelfu ya wakazi wa vijijini walifurika kuelekea kaskazini.[18]

Kwa kila nchi mikondo ya biashara ilirudia ruwaza zake za kabla ya vita. Biashara zilizoanzishwa wakati wa vita zilikuwa za wasiwasi kutokana na mtaji mdogo uliotumika na bidhaa kutokuwa na ubora uliotazamiwa. Nyingi ya biashara hizo zililazimika kufungwa. Wakati wa vita, nchi lindwa na makoloni yalionyesha majukumu yao kama vituo vya nyuma ya medani, na itikadi ya kikoloni ilisaidia kuendeleza mipango ya viwanda huku kukiwa na matarajio ya vita vikuu vya tatu. Huko Aljeria mpango wa miaka ishirini ulitayarishwa ukigusa kila sehemu lakini baada tu ya kuuanza ulitelekezwa. Wazo la kuwa kurudisha ukuaji wa viwanda kutatatua matatizo ya kiuchumi liliishia ndoto za mchana.

## Mabadiliko ya Kisiasa

Matokeo ya vita yalidhoofisha Ufaransa na Uingereza, na Italia ikawa kati ya walioshindwa. Tangu mwaka 1943 uzalendo ukawa wa vitendo, na tokea 1945-1946 ukapinga kurudishwa katika hali ya awali ya kuwa koloni au nchi lindwa.

Tangu kuanza kwa vita chama cha *Algerian People's Party* kilichoongozwa na Messali Hadj na kusambaratika baada ya viongozi wake kufungwa, kilitoweka kabisa katika ulingo wa kisiasa.Chama cha Kikomonisti hakikuweza kuendesha shughuli zake, au kililazimishwa kuzifanya kichini chini, na viongozi mashuhuri wa Waislamu na vyombo vyao vya habari vilinyamazishwa.

[18] P. Sebag, 1951, kur. 163-4

Wazalendo walipojiunga upande wa washirika vita vilibadilisha msimamo yao na ilibidi kuangalia upya mitazamo yao. Kwa hakika Ferhat Abbas, H. Bourguiba na sultani wa Moroko kwa uwazi walieleza misimamo yao kuhusu kujiunga na Ufaransa, kwa ajili ya demokrasia na ushindi kwa washirika. Uhamasishaji ulifanywa bila kipingamizi na wazalendo kadhaa waliitwa kujiunga na jeshi la Ufaransa au kujiunga wenyewe kwa hiari.

Jinsi mapambano yalivyoendelea, kukawa na mabadiliko katika mwelekeo wa maoni ya umma na ule wa wazalendo. Mwisho wa mapigano mwaka 1940 Ufaransa na Uingereza walipoteza kwa kiasi kikubwa hadhi waliyokuwa wameijenga kwa karibu karne nzima. Wazalendo walipata nguvu kutokana na kudhoofika huko, pia kutokana na kuweko kwa divisheni za jeshi la Ufaransa huko Algiers, Rabat na Tunis, na vilevile kutokana na kuingia kwa Uingereza na Marekani. Wakati wa kutia sahihi mapatano ya kusimamisha vita kwa muda, wazalendo walisisitiza ushiriki wa nchi zao katika vita. Wafd aliikumbusha Uingereza juu ya msaada usiokadirika uliotolewa na Misri kwa nchi marafiki wakati wa vita. Propaganda za maadui (Axis) hazikufanikiwa katika kuwabadilisha wazalendo na maoni ya umma juu ya kuwasaidia Washirika. Wakati huohuo upinzani wa ukoloni wa mataifa makuu mawili ulikaribishwa kwa matumaini makubwa. Kama ilivyokuwa kuhusiana na na pointi kumi na nne za Wilson, mwaka 1918, wazalendo waliegemea juu ya msimamo uliochukuliwa na mataifa makubwa na kauli zao zilifasiriwa kuwa na maana ya ukombozi wa watu kwenye makoloni. Uingereza ilidai kuwa mkataba wa 1936 utumike katika Misri lakini serikali na vyama vya upinzani walisisitiza kanuni ya kutopigana vita na walitaka kurekebisha mkataba na hata kupata uhuru. Wahamiaji wa kutoka Libya huko Misri walidai uhakikisho toka kwa Waingereza juu ya uhuru wa nchi yao.

Msimamo wa Ufaransa huko Algeria, Tunisia na Moroko haukuelekea katika kutafuta mwafaka, hivyo migogoro ya kabla ya vita ilianza tena na ilikuzwa kwa kuwasilisha madai mbalimbali.

Tarehe 11 Januari 1944 sultani wa Moroko akihimizwa na Marekani alipokea "Ilani ya Chama cha Istaklal" iliyotiwa sahihi na wawakilishi 58. Ilani hiyo ililaumu moja kwa moja utawala wa nchi lindwa hiyo na ikadai uhuru. Licha ya na upinzani wa Ufaransa, wito huo ulihamasisha watu. Januari 28 kadhia za Rabati zilizimwa na jeshi na mwanzoni mwa Februari mji wa Fez uliwekwa chini ya usimamizi wa jeshi. Kadhia ziliendelea mwezi wote na watu wasiopungua arobaini walipoteza maisha na mamia kujeruhiwa.

Wakati Bey Munsif alipoingia madarakani utawala wa Bey ukawa ndiyo ishara ya utaifa wa Tunisia. Mwezi Agosti 1942 Bey alituma ujumbe kwa kuondolewa

kwake na kuachia madaraka, Vichy akidai mageuzi makubwa katika muundo wa nchi lindwa. Kadhia kadhaa zilimsababishia mgongano na utawala wa Ufaransa na Desemba 1942 aliunda wizara mpya bila kushauriana na jenerali mkazi. Kutokana na Bey Munsif lakini itikadi ya *Umunsif* ilizaliwa.[19] Mwezi Novemba, 1944 katika Ilani ya Medani ya Tunisia *Neo-Destur* ilipigania kuwa na serikali ya madaraka ya ndani kwa misingi ya kidemokrasia, na kuundwa kwa bunge kufuatia kura ya maoni ya nchi nzima.

Huko Aljeria, tarehe 10 Aprili, 1941, Ferhat Abbas alimpelekea ujumbe Marshal Petain uliokuwa na kichwa "Aljeria ya Kesho". Uzalendo wa Algeria ulihimizwa kwa kutua kwa Waingereza na Wamarekani, na mwezi Februari, 1943 "Ilani ya Watu wa Aljeria" ilichapishwa. Iliushutumu ukoloni na kuelezea kanuni ya haki za watu wa Aljeria kujitawala.

Katika Pembe ya Afrika, baada ya kuondolewa kwa Italia, madai yalitolewa kwa Waingereza. Eritrea na Somalia ziliwekwa chini ya utawala wa kijeshi na huko Ethiopia Haile Selassie alifanikiwa kuanzisha mamlaka yake na kuweza kulinda uhuru wa nchi yake. Mwaka 1942 nchini Sudan, chama cha Wahitimu *(General Graduates Congress)* kilidai kutambuliwa kwa haki yao ya kujitawala wenyewe na kutambua utaifa wa Sudan, na kuanzishwa kwa Chombo cha Uwakilishi cha Wasudani kitakachokuwa na madaraka ya kuidhinisha sheria za nchi.

Kukataliwa kwa madai hayo kulisababisha chama cha wahitimu kujigawa katika makundi mawili; Kundi kubwa liliongozwa na *al-Ashikka* (Ndugu wa Damu) lilidai kuwa na serikali ya Sudan iliyoungana na Misri. Kundi la pili lililowakilishwa na chama cha Umma (Umma Party) lilidai uhuru ambao utafanya urafiki na Uingereza na Misri. Mwaka 1944 chama kilipinga kuanzishwa kwa Baraza la Ushauri la Kaskazini *(Northern Consultative Council)* kwa madai kuwa halikuwa na uwakilishi unaofaa; na pia ilikuwa inahisiwa kuwa Baraza hilo lingeweza kupendelea kulitenga eneo la kusini na hivyo kusababisha eneo hilo kupata uhuru wa peke yake au kujiunga na Uganda.

### *Matatizo katika mwaka 1945 na 1946: kuimarisha uzalendo na kuanzishwa kwa umoja wa nchi za Kiarabu.*

Wakati ambapo kushindwa kwa Waitalia kulileta uwezekano wa kufanya mabadiliko katika Pembe ya Afrika na katika Libya, mahali penginepo wakoloni walionyesha

[9] R. Le Tourneau, 1962, uk. 105

kuwa tayari kufanya marekebisho kidogo tu chini ya mfumo wao wa utawala na maslahi yao.

Huko Moroko tarehe 8 Machi, 1945, chama cha Istiklai kwa kusaidiwa na sultani Sidi Mohammed Ben Yusef kilidai haki ya nchi yao kuwa Mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Generali mkazi alikataa kushughulikia suala hili na alijibu wito wa uhuru kwa mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Huko Tunisia mapambano yalianza kwa kuanzisha mgomo huko Sfaksi mwezi Juni, 1946, ulioanzishwa na UGTT (*General Union of Tunisian Workers*). Baadaye, mwezi Agosti chama cha Tunisian National Front kilianzishwa kwa ushirikiano wa vyama vyote vya siasa. Huko Aljeria, maandamano ya Setif ya tarehe 8 Mei, 1945 yaliyoandaliwa na Marafiki wa Ilani na Uhuru, yalizimwa kwa kumwaga damu; hii iliimarisha misimamo ya wahusika, na wazalendo wengi walifikia hitimisho kuwa mapambano ya silaha hayangeweza kuepukika.

Japo miaka ya 1943 na 1944 kauli kadhaa za Wafaransa zilionyesha uwezekano wa kuwepo mabadiliko, katiba ya mwaka 1946 haikutoa suluhisho la suala la uhusiano kati ya Ufaransa na nchi za Maghreb. Katika muundo wa Muungano wa Ufaransa, nchi lindwa zilifanywa majimbo shiriki na kuruhusiwa kuteua wawakilishi katika vyombo vya muungano wa Ufaransa. Kwa hakika, Tunisia na Moroko zilibakia nje ya muungano wa Ufaransa, na kuendelea kuwa na hadhi yao ya nchi lindwa. Ama kuhusu Aljeria, Bunge halikukubali pendekezo lolote lililowasilishwa na wawakilishi wa Aljeria. Tarehe 20 Septemba, 1947, sheria ijulikayo kama Sheria za Aljeria ilikuwa imependekezwa na serikali ilipitishwa. Sheria hii iliondoa kabisa matumaini ya uhuru na iliendeleza udhibiti wa wazungu wachache.[20]

Huko Libya, kushindwa kwa Wajerumani na Waitalia kuliwawezesha Waingereza na Wafaransa kugawana utawala wa nchi. Hata hivyo Muungano wa Jamhuri za Kisovieti (USSR) ilipinga na hivyo suala la Libya ikabidi liwekwe mbele ya kikao cha Umoja wa Mataifa kilichokuwa kifanyike tarehe 15 Septemba 1948.

Kabla ya mwisho wa uhasama, vyama vya Upinzani vya Misri vilidai serikali ishughulike na kudai uhuru kamili kutoka kwa Uingereza. Mwezi Julai 1945 Wafd ilimpa Balozi wa Uingereza waraka kuhusu azma ya Misri, na miezi mitano baadaye serikali iliomba majadiliano yaanze. Mbali na makubaliano yanayostahili yaliyofikiwa na Waingereza, rasimu ya mkataba ya Oktoba 1946 ilipokelewa vibaya na Wamisri kiasi cha kuifanya serikali ya Nukrashi Pasha kuamua kuvunja mazungumzo na London na kulipeleka suala la Misri kwenye Umoja wa Mataifa.

[20] T. Chenntouf, 1969, uk. 141



*Picha 2.3 Sayyid Abd al-Rahman al-Mahdi akiwa anajiandaa kwa ziara ya London 15 July 1937*

## *Kuanzishwa kwa Umoja wa Nchi za Kiarabu*

Hamu ya nchi za Kiarabu kuwa na umoja ilianza tangu mwisho wa vita vikuu vya Kwanza ya Dunia, na kuanzia 1942 na kuendelea Waingereza waliwatia moyo kwa kuziunga mkono mfululizo rasimu zao mbili kabla rasimu iliyoungwa mkono na Misri haijakubaliwa. Hadi mwisho wa mkutano wa Kairo, azimio la Umoja wa Nchi za Kiarabu lilitiwa sahihi na Misri, Syria, Irak, Lebanoni, Transjordan (Ukingo wa Kushoto), Saudi Arabia na Yemen tarehe 22 Machi 1945. Kila nchi huru ya Kiarabu ilikuwa na haki ya kujiunga. Kanuni ya mamlaka na kutoingiliwa zilitiliwa umuhimu, na maamuzi yaliyochukuliwa na wengi yalizifunga nchi zile tu zilizoyakubali.

---

Katika Sudani, mazungumzo ya Waingereza na Wamisri ili kupitia mkataba wa 1936 yalianzisha upya madai yao ya kisiasa. Vyama viwili vilipeleka ujumbe kutoa pendekezo kwa serikali ya Misri la kuwa na programu ya kuweka serikali ya kidemokrasia nchini Sudani, iliyoungana na Misri na yenye rafiki na Uingereza. Ingawa Misri iliyakataa mapendekezo hayo, Uingereza iliihimiza Sudani iwe serikali ya madaraka. Hivyo mwaka 1948, katiba ilitayarishwa na kuweka kipengele cha kuwa na bunge lililochaguliwa na umma na baraza la utendaji lenye mawaziri Wasudani. Chama cha Ashikka kiliugomea uchaguzi wa bunge na hivyo chama cha Umma kikawa na wajumbe wengi kwenye Bunge na hivyo kuwa na wajumbe wengi katika baraza la utendaji, lakini muundo wa kisiasa ulikuwa chini ya udhibiti mkali wa gavana jenerali.

Baada ya kuwa huru tena, Ethiopia ikisaidiwa na Marekani, ilirudia sera yake ya Usasa. Eritrea ambayo iliwekwa chini ya utawala wa Uingereza hadi 1952, ilijadiliwa katika mapendekezo mengi kwenye Umoja wa Mataifa kabla ya kuunganishwa na Ethiopia huku ikiwa na sehemu kubwa ya mamlaka yake ya ndani. Mwaka 1946, watu wa Somalia waligawanywa kati ya jimbo la kaskazini la Kenya, majimbo ya Haud na ya Ogaden huko Ethiopia, na katika Somaliland iliyotawaliwa na Ufaransa, Italia na Uingereza. Baada ya uchaguzi, pwani ya Somalia ya Ufaransa ikawa "nchi ya ng'ambo", na sehemu ya Somalia iliyobaki ikajikuta inatawaliwa na Waingereza. Waingereza waliunga mkono Umoja wa Vijana wa Somalia katika azma yao ya kuwa na Somalia Iliyoungana, lakini mradi huo ulishindikana kutokana na mtazamo wa Umoja wa Mataifa.

Katika kuchipuka kwa Afrika ya sasa, zahama na mabadiliko ya miaka kumi tangu 1935 hadi 1945 yalikuwa muhimu, na matokeo yake katika mambo mengine, tunayaona hadi leo. Isitoshe, hiki kilikuwa ni kipindi ambapo hali ya kutokuendelea na ya utaifa ilijidhihirisha, na mchakato uliounda hali hiyo kuharakishwa bila kizuizi.

# 3

# Afrika ya Propiki na Ikweta chini ya utawala wa Wafaransa, Wareno na Wahispania 1935-45

## Utangulizi

Afrika ya Tropiki na Ikweta chini ya utawala wa Wafaransa, Wareno na Wahispania ilienea toka visiwa vya Cape Verde katika Bahari ya Atlantiki hadi Msumbiji katika Bahari ya Hindi. Makoloni ya Wafaransa yaliunda eneo moja lililozunguka makoloni mbalimbali ya Waingereza. Makoloni ya Wareno yalijumuisha nchi tatu za Bara na funguvisiwa mbili ambazo hazikukaribiana. Koloni la Wahispania lililokuwa kusini mwa eneo hilo liliunganisha Rio Muni katika bara na kisiwa cha Fernando Poo, wakati koloni la kaskazini lilidhibiti pwani ya Sahara.

Kipindi cha kati ya 1935 na 1945 ambacho kilichukuliwa kuwa ndicho "kipindi cha ustawi wa ukoloni", ingefaa kichukuliwe kuwa ni "muongo wa wastani" wa sera za mlengo wa kulia kule Ulaya. Katika miaka hii, makoloni ya nchi nne za kibeberu za Ulaya yaliumia sana kutokana na mshituko wa Ulaya katika vita yake yenyewe.

Katikati ya miaka ya 1930, Hispania iliraruliwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, Ureno ilishuhudia kuimarika kwa utawala wa kifashisti wa Salazar aliyechukua madaraka 1932, na Ufaransa ikakaliwa na manazi mwaka 1940 na kutawaliwa na mshirika wao, yaani serikali ya Vichy. Katika sura hii tutashughulika na matokeo ya kuibuka kwa ufashisti wa Ulaya kwa himaya za Ureno, Ufaransa na Uhispania.

Huko Ureno, kuimarika kwa udikteta wa mlengo wa kulia kulikomaza sera ya kikoloni ya ukandamizaji ambayo tayari ilikuwapo, ambapo huko Ufaransa kugawanywa kwa nchi kulibadilisha mwelekeo wa uwajibikaji. Ushindi wa Jenerali Franco ulibadilisha sera za makoloni ya Hispania na ubaguzi wa rangi ulioongezeka.

Sura hii inatarajia kuonyesha kuwa muongo wa 1935–1945 ulikuwa ni mwongo muhimu zaidi katika historia ya Ukombozi wa Waafrika kuliko vilivyokuwa katika historia ya ubeberu wa Ulaya. Kwa hakika, upinzani wa

Waafrika ulijionyesha kisiasa, kijeshi, kiuchumi na za utamaduni. Kisiasa muongo huu ulishuhudia kuibuka kwa uzalendo wa kisasa. Kijeshi, Waafrika walishiriki katika mapambano na udikteta wa kifashisti wa Ulaya. Kitamaduni, upinzani wa Waafrika wakati mwingine ulijidhihirisha kidini. Uislamu ulikuwa na majukumu muhimu ya kisiasa, na vivyo hivyo Ukristo na hata dini za kijadi za Kiafrika.

Kwa upande wa uchumi, upinzani ulijionyesha kwa kuanzishwa kwa vyama vya wafanyakazi, vyama vya ushirika na madai ya mgawano sawa wa mapato kutokana na matunda ya na uchumi unaoibuka.

Kwa hiyo, vita kuu vya pili vilichochea mageuzi ya haraka ambayo yalisababisha kudidimia kwa ukoloni.

Ni ipi hulka ya utawala wa kikoloni katika kipindi hiki? Ni kwa vipi himaya mbalimbali za Ulaya ziliendesha mambo yake? Muundo wa ubeberu ulikuwa vipi? Ni maswali haya ya msingi ambayo tutajaribu kuyajibu.

## Sera ya ukoloni ya Ufaransa

Katika kipindi hiki miliki za Ufaransa zilikuwa katika mashirikisho mawili ya makoloni na nchi mbili zenye mamlaka yake zenyewe. Shirikisho la Afrika Magharibi ya Kifaransa, Dakar ukiwa ndiyo makao yake makuu, ambalo lilihusisha Senegal, French, Sudan ya Kifaransa (Mali), French Guinea ya Kifaransa, Upper Volta (sasa Burkina Faso) Côte d'Ivoire, Dahomey (sasa Benin), Niger na Mauritania. Afrika ya Kiikweta ya Wafaransa, ikiwa na makao makuu Brazzaville ilijumuisha makoloni ya Kongo ya Kati (sasa Kongo), Chadi, Ubangui-Chari (sasa Jamhuri ya Afrika ya Kati) na Gabon. Makoloni ya zamani ya Wadachi, Kameroon na Togo, yaligawiwa kwa Uingereza na Ufaransa na kuwekwa chini ya mamlaka ya Shirikisho la Mataifa.

Magavana-jenerali na makamishna wakuu walitawala makoloni kwa amri ambazo zilitekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Ufaransa. Baraza la Serikali ambalo lilimsaidia gavana-jenerali au kamishna mkuu liliundwa na maofisa waandamizi lakini jukumu lake la msingi lilikuwa ni kutoa ushauri tu. Gavana-jenerali alikuwa na madaraka kamili: alidhibiti utawala, alikuwa kamanda wa jeshi na aliteua na kufukuza maofisa mbalimbali kama alivyopenda.

Gavana-jenerali na makamishna wakuu walisaidiwa na ofisi za utawala ambayo

kazi yake ilikuwa kuhakikisha uendeshaji mzuri wa utawala. Zilizokuwa muhimu zaidi ni ofisi za Fedha, Ujenzi, Elimu, Masuala ya Uchumi na Afya. Koloni la Afrika la Kiikweta la Wafaransa, kwa vile lilikuwa na uhaba wa njia za mawasiliano, mara nyingi lilichukuliwa kama koloni pekee lililotawaliwa na gavana-jenerali wa Brazzaville.

Kila koloni lilitawaliwa na luteni gavana aliyepokea amri kutoka kwa gavana-jenerali na kusaidiwa na Baraza la Utawala. Kila koloni liligawanywa katika wilaya zilizojulikana kama *Circonscriptions au Cercles*, katika Afrika Magharibi zilikuwapo mia moja, na katika Afrika ya kiikweta zilikuwapo kama hamsini, na kila mojawapo ilitawaliwa na ofisa wa wilaya. Katika Kameruni kulikuwa na wilaya kati ya sitini na sabini, na huko Togo zilikuwako kumi[1] Chini kabisa ya ngazi ya utawala kulikuwa na watawala wenyeji waliotokana na nasaba tawala za zamani.

Uendeshaji wa makoloni ulianzisha urasimu, na mwaka 1937 nusu ya waendeshaji 385 walikuwa wanafanya kazi mijini ambako walitumia mbinu walizofundishwa katika *Ezoleolonial e* (shule za ukoloni) bila kujali hali halisi ya kienyeji.

Kamanda wa wilaya alikuwa wakati huo huo mkuu wa kisiasa, mkuu wa polisi, mwendesha mashtaka mkuu na rais wa mahakama ya wenyeji, na hivyo kuwa mwakilishi mkuu wa mamlaka ya wakoloni aliyejulikana kwa Waafrika. Yeye ndiye aliyeweka viwango vya kodi ya kichwa, kodi ya maendeleo na ushuru; alidai nguvu kazi isiyo na malipo, alikusanya mazao ya kuuza nje, alihamasisha watu kwa kazi ya lazima na kulazimisha watu kutumikia jeshi. Alipimwa uwezo wake wa kazi kwa faida aliyoipatia Ulaya, na hivyo alijihusisha zaidi na kuchunga maslahi ya vyama vya wafanya biashara na makampuni makubwa.

Hivyo, kamanda wa wilaya na mkuu wa jimbo walisababisha madhara makubwa sana vijijini. Machifu wa vijiji walikuwa walamba viatu vya wakubwa. Walidharauliwa na watu wao au walisifiwa na utawala wa kikoloni kutegemea namna walivyomudu kukusanya kodi ya maendeleo.

Mbali na mabadiliko machache iliyoyapendekeza, serikali ya chama cha *Popular Front* ya Juni 1936 haikuleta mabadiliko yoyote katika mfumo wa kikoloni. Utaratibu wa mashauriano na watu ulibuniwa na utawala wa kikoloni lakini

1 Jina la Cerles lilikuwepo huko Afrika Magharibi ya Kifaransa na Togo wakati mwaka 1934 wilaya 49 za Afrika ya Ikweta ya Kifaransa zilipunguzwa hadi 20 na kuitwa idara; huko Cameroon nchi iligawanyika kwenye mikoa 15-20 ikiwa ni pamoja na kata 60-70. J. Suret-Canale, 1964, uk. 391

ulipindishwa kwa ujanja. Ukweli ni kwamba, ni wale tu waliochaguliwa kutoka halmashauri nne za Senegal (Saint-Louis, Dakar, Goree, Rufisque) walioshiriki katika kutoa ushauri.

## Sera ya Ukoloni ya Ureno

Mwaka 1930, Antonio Salazar, Waziri wa Makoloni alibadilisha sera ya kikoloni kwa kuyapuuza maslahi ya kiuchumi ya makoloni kwa manufaa ya Ureno yenyewe. Nchini Ureno kwenyewe, huduma zinazotolewa na serikali zilipunguzwa, na katika makoloni, unyonyaji wa kikoloni uliojikita kwenye kazi za lazima, ulipaji wa kodi ya mazao, na mikataba ya kuuza wafanya kazi wa migodi huko Afrika kusini uliongezeka. Muundo wa utawala ulikuwa sawa na ule wa Kifaransa, ambapo piramidi ya kiutawala ilianzia kwa gavana-jenerali hadi kwa machifu wa wilaya. Wote hao walikuwa na madaraka kama yale ya wenzao Wafaransa na waliwajibika kwa serikali ya Lisbon.

Sera ya ubaguzi iliwashusha Waafrika hadi chini kabisa katika muundo wa jamii; Waafrika walikuwa na haki chache sana na walilazimika kushiriki kazi za lazima.. Nje kidogo ya miji michache kulikuwa na maendeleo ya viwanda kidogo. Makoloni ya Ureno yalijibainisha kwa kukosa ubunifu na kukuza unyonyaji.

Katika visiwa vya Cape Verde matokeo ya mdororo mkuu wa uchumi yalichukua sura ya maelfu ya wafanyakazi wahamiaji kurudi baada ya kurejeshwa nyumbani kutoka Marekani. Walirudi na fedha walizozipata katika Dunia Mpya, na hivyo kuwafanya watu wa Cape Verde waendelee kukimbilia Amerika. Muda mfupi kabla ya kuanza kwa vita vikuu vya pili, ukame ulisababisha wahamiaji wengi kufurika mjini Dakar na baadaye mwaka 1941–1942 ukame ulisababisha vifo vya watu 20,000. Japo nchi yao haikuchukuliwa kama koloni halisi chini ya utaratibu *indigenat*, watu wa Cape Verde hawakuchukuliwa kuwa Wareno halisi. Jeshi lililowekwa kwenye visiwa wakati wa vita halikutoa msaada wowote kwa walioathirika na ukame. Hata hivyo uraia wao wa Ureno, na kiwango chao cha elimu kiliwawezesha watu wa visiwa vya Cape-Verde kupata kazi huko Guinea ya Ureno na Angola, ambako baadaye wengine walijihusisha na mapambano ya ukombozi.

Guinea ilikuwa na maendeleo madogo. Juhudi za kuanzisha kazi za lazima zilikwamishwa na uhamaji wa watu kwenda Senegal na Guinea ya Ufaransa. Zaidi ya hayo, uhamaji wa watu kutoka Cape Verde, ambao walikuwa wafanyakazi wasaidizi wa utawala, wakulima wadogo au mafundi, ulikuwa na athari kubwa.

Visiwa vya Sao Tome na Prinsipe vilikuwa mfano dhahiri wa mashamba makubwa ya makoloni ambapo karibu ardhi yote ya kilimo ilimilikiwa na kampuni

zinazohusiana. Katika hali hii, jukumu kubwa la utawala wa kikomi lilikuwa kuwapatia wafanyakazi ambao waliwaleta kutoka Angola na makoloni mengine ingawa kati ya 1920 na 1940 idadi yao ilipungua toka 40,000 hadi 30,000. Wakati huo huo kupungua kwa rutuba asilia katika udongo kulisababisha kuanguka kwa zao la kakao.

Huko Angola na Msumbiji, kuanguka kwa bei ya mazao ya kikoloni kuliwaathiri sana wakulima wadogowadogo. Ureno chini ya Salazar iliwekeza kidogo sana kwenye makoloni, na kwa Msumbiji, mapato makubwa yalitokana na watu waliopelekwa kufanya kazi katika migodi ya Afrika Kusini na kulipwa Rand. Ilikuwa si rahisi kwa Waafrika kuepuka udhibiti maradufu wa utawala na wa walowezi. Mwaka 1933 waziri wa makoloni alishauri kuwasafirisha kwa kiasi kikubwa wafanyakazi wa Ulaya wasio na ajira kwenda Afrika ili kuinasua Ulaya kutokana na migogoro ya kikazi, na kuhakikisha Afrika ya Wareno inakuwa "nyeupe".

Lakini walowezi hawakuwa na ujuzi wala mtaji hivyo waliendelea kuishi kwa kuwanyonya wazalendo kupindukia. Waliajiriwa kwenye kazi za chini sana na hivyo kuzuia Waafrika kushika nafasi hizo. Kwa hali hiyo, kigingi hiki imara cha kiutaratibu kilichowatenganisha Waafrika na Wazungu kilimaarisha na kuhalalisha ubaguzi wa rangi.

Kufuatia mkataba uliofanywa mwaka 1939 na Vatikani, mapatano kati ya serikali na kanisa Katoliki ya mwaka 1940 yalizifanya misioni za kikatoliki kuwa ni mkono wa dola katika kutoa elimu kwa Waafrika. Hii ilileta matatizo mara kwa mara huko Guinea ambako nguvu za kijadi, zilizoimarishwa na kuwapo kwa Uislamu imara, zilipinga juhudi za kulifanya koloni kuwa la Kikatoliki.

## Sera ya Ukoloni ya Hispania

Huko Hispania, utawala wa zamani wa kifalme ulitoa aula kwa Kuba na baadaye Moroko. Kabla ya vita vya wenyewe kwa wenyewe Afrika ya Ikweta haikuwa na utawala wake yenyewe na kwa hiyo ilikosa kuwa na mtazamo wake wa kisiasa. Visiwa vya Fernando Poo vilikuwa na kilimo cha usafirishaji mazao nje ambapo Bara ya Rio Muni (sasa Guinea ya Ikweta) ilizalisha mbao za tropiki. Katika visiwa vya Fernando Poo kukataa kwa wenyeji wa Bubi kufanya kazi kwenye mashamba kulifanya kilimo kitegemee nguvukazi kutoka nje. Mwaka 1930, kufuatia kuingilia kati kwa Shirikisho la Mataifa, usafirishaji wa wafanyakazi wa Kikru kutoka Liberia ulizuiwa na baadaye kusimamishwa kabisa.

Franco alipoingia madarakani utawala wake uliipa Guinea ya Ikweta na Sahara ya Hispania uhuru wa kifedha, lakini alionyesha shauku zaidi kwa Guinea ambako uwekezaji ulikusudiwa kuchota faida kutoka kwenye koloni na kuweka utawala wa kibaguzi wa kikandamizaji.

## Vita Vikuu vya Pili

Vita vikuu vya pili vya dunia viliharakisha mabadiliko ya mikabala katika makoloni ya Ufaransa katika Afrika ambapo sera mpya zilikuwa zinajitokeza. Himaya za Ureno na Hispania zilibakia kando kwani ghuba ya Iberia haikushiriki moja kwa moja vitani.

Wananchi katika makoloni ya Ufaransa waliandikishwa jeshini kwa mujibu wa sheria. Kutoka mwaka 1930 na kuendelea wanaume 15,000 waliandikishwa kila mwaka kuingia kwenye *Tirailleurs Senegalais* (Wapiganaji wa Kisenegali) jina lililotumiwa kuelezea askari wote weusi chini ya jeshi la Ufaransa bila kujali asili yao. Mwaka 1939-1940 Waafrika 80,000 walipelekwa Ufaransa na kati ya mwaka 1943 na 1945 Waafrika 100,000 na zaidi walipelekwa Italia. Juhudi za Waafrika katika vita zilikuwa ni pamoja na kuzalisha mali ghafi na vyakula muhimu.

Kufuatia mapatano ya kusimamisha vita kwa muda ya tarehe 22 Juni 1940 ilikuwa ni katika Afrika ambapo mapigano kati ya Utawala wa Vichy na Ufaransa Huru yalikuwa makali. Afrika Magharibi ikiongozwa na Gavana Jenerali Boisson ilitangaza kumwunga mkono Marshal Pétain ambapo Afrika ya Ikweta iliungana na Félix Eboué, mtawala mweusi kutoka Guyana ambaye alikuwa na Gavana wa Chadi.

Wakati Uingereza na Ufaransa Huru wakijitahidi bila mafanikio kuiteka Dakar, Afrika ya Ikweta ikawa ndiyo kituo kikuu cha Ufaransa Huru huko Eboliue akiwa ndiye Gavana Jenerali.

Katika maeneo ya kilimo ya makoloni, wakulima walilazimishwa kulima mazao ya nafaka kwa ajili ya vita. Kwenye maeneo ya msitu walitakiwa kuzalisha mpira ambapo iliwalazimu kuingia ndani msituni kutafuta utomvu wa mpira. Wengi wao walikufa wakijaribu kutafuta mpira. Wakati mwingine kijiji chote kilichukuliwa kufanya kazi za kujenga barabara au kulima mashambani.mwaka 1942 Wajoola wa Basse-Kasamansi, wakiongozwa na Aline Sitoé, waliasi dhidi ya madai haya, wakidai kuwa wakoloni walikuwa wakiwadai wakulima mazao mengi kuliko walivyoweza kuzalisha. Wajoola kadhaa waliuawa na Aline Sitoé alipelekwa uhamishoni. Kutokana na kuajiri na kuandikisha watu jeshini, nguvukazi ilipungua, uzalishaji ukaporomoka, na watu wakakimbia ili kuwatoroka mawakala wa ukoloni wa Kifaransa.

Huko Senegal mahuruji ya karanga yalishuka toka tani 580,000 kabla ya vita hadi tani 174,500 mwaka 1941. Vibarua wa msimu waliletwa kutoka nchi jirani na baadaye uzalishaji ukapanda hadi kufikia tani 429,000 mwaka 1945. Ili kuboresha usafirishaji uliokuwa na matatizo wakati wa vita, kampuni ya Ufaransa ya Lesieur iliruhusiwa kujenga matanki ya mafuta mjini Dakar, na hivyo kuanzisha ujenzi wa viwanda. Katika maeneo yenye unyevunyevu ya pwani, baadhi ya mahuruji yalianguka na mengine kushamiri, hata hivyo bila ya kuongeza uwezo wa Waafrika wa kununua vitu.

Katika Afrika Magharibi unyonyaji wa kiuchumi uliambatana na ushadidishaji wa sera za kikoloni. Utawala wa Vichy ulikandamiza asasi zote za uwakilishi, sheria za uhalifu zilifanywa kuwa kali zaidi, na zilianzishwa hatua mpya za ubaguzi wa rangi.

## Hali ya kisiasa na kijamii

Kutoka mwaka 1935 hadi 1945, muundo wa kijamii wa makoloni ya Ureno na Hispania haukubadilika sana. Maisha ya mjini hayakuwapo kabisa, ambapo maeneo ya vijijini yalikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha nguvukazi na ukwapuzi wa mazao ya kikoloni.

Katika makoloni ya Ufaransa, dalili za mabadiliko zilijitokeza zaidi. Hata hivyo kuingia madarakani kwa chama cha Popular Front hakukubadilisha kwa haraka sera za kikoloni Kuhalalishwa kwa vyama vya wafanyakazi tarehe 11 Mei 1937 kulichangamsha maisha ya mijini. Wafanyakazi walikuwa wengi na walijiandaa vizuri kuanzisha mgomo wa wafanyakazi wa reli mwaka 1938 katika mji wa Thiés.

Vita vilisababisha kuwa na idadi ndogo ya wahamaji toka vijijini kuhamia mijini. Wakala wa utawala wa kikoloni walizidi kuwashinikiza wananchi kwa kuzitweza baadhi ya famila za kitemi, na hivyo kuuteteresha muundo wa utawala wa wenyeji.

Upinzani wa Waafrika dhidi ya utawala wa Ufaransa ulianza nyuma kabla ya mwongo wa 1935-1945. Katika miaka ya 1930, makabila ya Kimoori na Kirikaybat yalizishambulia sehemu za Wafaransa huko Mauritania. Ni katika mwaka 1935 tu ndipo Tinduf, sehemu ya mwisho kudhibitiwa, ilipokaliwa na kuwa kiungo cha kwanza kati ya Moroko na Afrika Magharibi.[2]

Wakati huo huo Wamisionari walipokuwa wakieneza Ukristo, amani ya kikoloni na kukua kwa biashara kulisaidia kueneza Uislamu, hususan tarika za Muridi huko Senegal na Hamal huko Sudan ya Kifaransa.

[2] J. Suret-Canale, 1964, uk. 530

Umuridi ulianzishwa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na Sheikh Ahmadu Bamba katika nchi ya Wolof huko Senegal. Kilikuwa kikundi kisicho na ghasia na kilihimiza wafuasi wake kuwa watiifu. Bila ya kuupa changamoto utawala wa kikoloni, Bamba alianzisha muundo msonge ambao uliwapa watu wa vijijini mlinzi wa kibaba dhidi ya walowezi ambao walichukua nafasi ya watawala wa jadi. Hivyo Umuridi ulionekana kuiga muundo ulioanzishwa na wakoloni. Baada ya kifo cha Ahmadu Bamba, tarika hiyo ilijikita katika mfumo wa kikoloni, ikisaidiwa na machifu wa Muridi waliokuwa wazalishaji wakuu wa karanga. Katika miaka ya 1930 Wamuridi walikalia kikweli kweli ardhi ya huko Jolof na Kayor, jambo ambalo lilisitishwa mwaka 1936 katika mgogoro kati ya watangulizi wa Kimuridi na vikundi vya Wafulbe vya Baol. Ingawa hukumu ya mahakama ya wakoloni iliwapa ushindi na kuwatambua Wafulbe kama ndiyo wamilikaji wa halali, utawala uliruhusu wakulima wa karanga kuteketeza vijiji vya wachungaji.

Kufikia mwaka 1945 kulikuwa na wastani wa Wamuridi 100,000 wakizalisha theluthi moja ya karanga zote zilizozalishwa Senegal. Wakati huohuo Tuba, mji mkuu wa Umuridi, ulivutia maelfu ya wahujaji waliotaka kuzuru kaburi la Ahamadu Bamba na kutoa zawadi zao kwa kiongozi wa umoja huo.

Uhamalli ulizaliwa Sudan (sasa Mali) kutokana na Sheikh Hamallah, sufii aliyevutia maelfu ya wafuasi kushambuliwa vikali na tarika zilizokuwepo. Alipigania heshima na utambulisho wa watu wa Afrika. Mwaka 1933 alikamatwa na kufungwa kwa miaka miwili. Mapigano kati ya wafuasi wa Uhamalli na wanachama wa vikundi vingine ambayo chanzo chake kilionekana kuwa cha kitheolojia, kwa kweli yalificha azma ya Wahamalli ya kuwapinga wale waliokuwa wakishirikiana na utawala wa kikoloni, au wale waliokuwa wamenyamaza tu. Mwaka 1940 migongano kati ya wanaomuunga na wasiomuunga mkono Sheikh Hamallah ilisababisha majeruhi 400 na Mratibu huyo akahukumiwa kupelekwa uhamishoni Ufaransa ambako alifariki mwaka 1942.

## Vyama vya kwanza vya wafanyakazi na siasa mpya

Hamasa ya kwanza ya kisiasa ilitokea Senegal katika Halmashauri Nne zilizokuwa chini ya Blaise Diagne, Naibu Waziri wa makoloni, mwaka 1931, na mfadhili wa Maonyesho ya Kikoloni.[3] Alishutumiwa na kikundi cha *Young Senegal,* kilichoongozwa na Tiecouta Diop, kuwa alikuwa wakala wa unyonyaji wa kikoloni.

3 Kuhusu Blaise Diagne na sera zake, angali UNESCO, Historia Kuu ya Afrika, Juz. VII, Sura ya 25, uk. 642-7.

Mapambano haya ya kisiasa yalitokea katika Halmashauri hizo nne, hivyo hayakuutishia mfumo wa kikoloni. Blaise Diagne alipokufa mwaka 1934, msaidizi wake wa zamani, Galandou Diouf, ambaye awali alimgeuka, alichagnliwa na Bunge la nchi hiyo.

Magazeti mengi yaliyochapwa kwa mkono yalitolewa Dahomey na mwaka 1936 idadi yao ilikuwa zaidi ya dazani. Yaliyojulikana zaidi ni gazeti la *Voix du Dahomey, Courrier du Golfe du Benin*, the *Phare du Dahomey* na *L'Etoile du Dahomey.*

La muhimu zaidi lilikuwa ni upinzani wa kuibuka kwa kiuchumi uliofanywa na Waafrika, na maendeleo ya kutoa madai kwa pamoja. Baada ya kutangaza rasmi amri ya tarehe 20 Machi, 1937, ambayo iliruhusu makubaliano ya pamoja na uchaguzi wa wajumbe, vyama vya kwanza vya wafanyakazi vilizaliwa. Katika mwaka huo huo migomo ilitokea kwa kiwango kisichotarajiwa, na vuguvugu la vyama vya wafanyakazi lilifikia kilele kwa mgomo wa wafanyakazi wa reli katika sehemu ya Thiés mwaka 1938. Ikiwa inakabiliwa na upinzani wa vibarua wa reli ya Dakar-Niger, serikali ya kikoloni ilitumia jeshi kuzima mgomo. Watu 6 walifariki na 53 walijeruhiwa. Hata hivyo serikali ilikubali kutoiwekea vikwazo wala vizuizi haki ya kujumuika, na kwamba familia za walioathirika zingepewa fidia na madai yao yangefanyiwa kazi.

Kwa mujibu wa waziri wa makoloni, kulikuwa na migomo thelathini na tatu katika makoloni ya Ufaransa ya Afrika Magharibi kati ya mwaka 1937 na 1938. Mgogoro mkubwa zaidi ulitokea Thiaroye mwaka 1944. Mgogoro huu wa vyama vya wafanyakazi ulitokea nje ya vyama. Chama cha Kijamaa cha Wasenegal (*Senegalese Socialist Party*) kiliundwa mwaka 1935 na mwanasheria Lamine Gueye ambaye aliongoza kampeni ya kumwondoa Galandou Diouf aliyekuwa Mwakilishi bungeni. Chama cha Wafanyakazi wa Ufaransa kilijaribu kujiwekea mizizi Senegal, lakini vita viliyamaliza majadiliano yote ya kisiasa yaliyokuwa yameanza.

## Mkutano wa Brazzaville

Mwaka 1943 Kamati ya ukombozi wa kitaifa ya Ufaransa (French Committee of National Liberation) ilisimikwa nchini Algeria ikiwa ni ishara ya kumalizika kwa enzi za ufashisti, angalao katika himaya ya Wafaransa Makoloni ya Ufaransa ya Afrika yalimuunga mkono Jenerali de Gaulle. Kamati iliitisha mkutano wa Ufaransa ya Afrika katika mji wa Brazzaville mwezi January-Februari 1944 ambao ulikuwa na lengo la kuimarisha mfumo wa kikoloni na kuuhifadhi ili usiingiliwe na athari toka nje-hususan athari za kutoka Amerika. Jenerali de Gaulle alielewa kuwa asingeweza kuomba mchango mkubwa zaidi wa Waafrika kwenye vita bila ya



*picha 3.1 Mkutano wa Brazzaville, mwezi Februari 1944: katikati kushoto, Gavana-Jenerali Felix Eboue; katikati kulia, Jenerali Charles de Gaulle.*

kuwaahidi kuwa kutakuwa na mabadiliko. Haikuwa rahisi tena kuzungumzia ukombozi na demokrasia na wakati huohuo kuwanyima Waafrika haki zao za msingi. Alitanganza:

> Katika Ufaransa ya Afrika, kama ilivyo katika nchi nyingine ambako watu wanaishi chini ya bendera yetu, hakutakuwa na maendeleo mpaka yawe yenye manufaa kwa wenyeji, kihali na kimali, katika ardhi yao ya asili; mpaka wapande hatua kwa hatua hadi kwenye kiwango ambapo wataweza kushiriki katika kuendesha mambo yao nchini mwao. Ni wajibu wa Ufaransa kuhakikisha kuwa hili inafanikiwa. Hilo ndilo lengo ambalo tumejiwekea. Hatutapuuza urefu wa hatua ambazo itabidi zipitiwe.[4]

Kauli ya kiongozi wa Ufaransa Huru haikwenda mbali kiasi cha kutangaza kuwa mataifa yana haki ya kujitawala, hata kama hilo linadokezwa katika kauli yake, mathalani katika usemi wake kuhusu kushiriki katika kuendesha mambo yao nchini mwao.

Bwana Pléven, kamishina wa makoloni, aliuongoza mkutano huo ambao

[4] Mkutano wa Wafrika na Wafransa, 1944, uk. 38, imenukuliwa na J. Suret-Canale, 1964, 597-8

uliwajumuisha magavana jenerali na maofisa mashuhuri wa kikoloni, lakini hapakuwa na mwakilishi yeyote wa Waafrika. Mkutano uliweka kanuni moja ya msingi ya kuwa "wazo lo lote la kuwa na madaraka" lazima liondolewe. Mkutano huo ulipendekeza kuyapa makoloni Bunge la Shirikisho, na ingawa ulipendekeza kuheshimu mila za Kiafrika, lakini ulipinga matumizi ya lugha za Kiafrika katika Elimu.

*Afrika ya Tropiki na Ikweta chini ya utawala wa Ufaransa, Ureno na Hispania 1935-45*

Mamlaka ya kikoloni yalitambua haja ya mabadiliko lakini hayakuwa yamekadiria kasi ya kujitokeza kwa Waafrika katika majukwaa ya kimataifa. Wakati wa kuondoa ukoloni. Kanuni za Brazzaville zilikuwa ndizo kikwao kikuu kilichozuia mamlaka ya Ufaransa kuelewa dhamiri ya watu ya kujivua pingu za ukoloni. Hata kukaliwa kwake na Manazi hakukuifundisha Ufaransa madhila ya ubeberu.

## Hitimisho

Mielekeo ya kifashisti huko Ulaya ilifanya hali kuwa mbaya zaidi katika himaya za Ufaransa, Ureno na Hispania, ambazo zilikuwa tayari zinajulikana kwa ubaguzi wa rangi na unyonyaji.

Mwongo wa 1935-1945 ulidhihirisha mfumo mpya wa upinzani ambayo ulijumuisha vyama vya kisiasa, dini na uasi wa utamaduni, harakati mpya za vyama vya wafanyakazi, wepesi wa kufanya migomo, na kuibuka kwa uandishi wa habari wa kisiasa wa Kiafrika. Vita Vikuu vya Pili katika jukumu lake kama kichocheo, havikuifundisha Ulaya kupunguza ubeberu wake, bali viliifundisha lakini uliifundisha Afrika kuwa na uzalendo zaidi. Baada ya vita, mfumo wa kikoloni haukuweza kuvumilika tena, ukichukulia kuwa Waafrika walipigana bega kwa bega na wakoloni kwa ajili ya uhuru. Kuzaliwa kwa vyama vya siasa kama kile cha F. Houphouet Boigny kilichojulikana kama *Rassemblement Democratique African* kilichoanzishwa mwaka 1946, kuliingiza Afrika ya Kitropiki katika duru la mapambano ya ukombozi ambayo yalianzia katika makoloni ya Ufaransa mwaka 1945[5]. Katika makoloni ya Ureno na Hispania, tawala za kifashisti za nchi hizo ziliondosha uwezekano wowote wa kuwa na vyama vya kisiasa au vya wafanyakazi. Mwamko wa wananchi wa makoloni haya ulikuja baadaye; huko Ureno, mwamko huo hatimaye uliutikisa udikteta na kuchangia katika ukombozi wa watu wa Ureno.

[5] Chama cha RDA kilianzishwa Bamako (Sudani yaKifaransa, hivi leo Mali

# 4 Afrika chini ya utawala wa Waingereza na Wabelgiji

## Je, maeneo ya Afrika yaliyotawaliwa na Waingereza na Wabelgiji yanaweza kutazamwa pamoja?

Kati ya mwaka 1935 na 1945 Uingereza ilikuwa na nchi kumi na sita barani Afrika katika himaya yake, ikilinganishwa na Ubelgiji ambayo ilikuwa na koloni moja kubwa ambalo ni Kongo na kijikoloni-lindwa kidogo katika nchi ya Ruanda-Urundi (sasa Rwanda na Burundi). Uingereza ilibuni mifumo tofauti tofauti ya utawala katika makoloni yake, na katika koloni moja kungeweza kuwapo na taratibu mbalimbali za uendeshaji wa mambo zilizotumika sambamba. Hivyo ni vigumu kutoa maelezo ya jumla kuhusu taratibu za utawala wa kikoloni wa Uingereza. Jumuiya ya walowezi weupe wa Rhodesia ya Kusini (sasa Zimbabwe) ilipata madaraka ya kudhibiti mambo yake ya ndani tangu mwaka 1923. Waafrika katika nchi yenye wakazi wachache ya Bechuanaland (sasa Botswana) walitawaliwa kwa utawala wa mlango wa nyuma katika maeneo manane ya kikabila; utawala wa kampuni moja katika milki ya Tati; hakimu wa Kiingereza katika milki ya kifalme; na mwishowe na mahakimu wa amani wa kilowezi katika maeneo mbalimbali yaliyohifadhiwa kwa ajili ya wakulima Wazungu. Huko Nigeria utawala wa mlango wa nyuma wa Majimbo ya Kaskazini ulikuwa tofauti kabisa na ule wa Majimbo ya Kusini.

Utawala wa Wabelgiji wa Kongo ulitilia maanani tofauti za muundo wa jamii na mahitaji mahsusi ya milki kubwa za mashamba na migodi. Utawala wa mlango wa nyuma wa mtindo wa Kibelgiji haukuwa na nafasi katika misongamano mipya ya mijini kama ilivyokuwa Leopoldville (sasa Kinshasa) na Elizabethville (sasa Lubumbashi), ambayo yote ilipanuka kwa kasi kubwa wakati wa vita vikuu vya pili vya Dunia. Huko Urundi, mamlaka ya machifu yaliendelea ambapo Ruanda Ufalme ulipewa umuhimu zaidi, na utatu wa jeshi, ardhi na machifu wakuu

waliondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na chifu mmoja. Katika Ubelgiji ya Kongo idadi kubwa ya machifu wa jadi iliondolewa na nafasi zao kuchukuliwa na "machifu wa wazungu". Hata hivyo, Wabelgiji waliendelea kuuita utawala wao, katika koloni la Kongo na katika nchi-lindwa, kuwa ni wa mlango wa nyuma.

Zaidi tofauti kati ya utawala wa Waingereza na wa Wabelgiji kati ya mwaka 1935 na 1945, miundo yote miwili ilipitia majaribu ambayo yalikuwa na athari kubwa kwa ruwaza za utawala wa kikoloni na pia kwa namna Waafrika walivyoukabili. Mdororo mkuu wa uchumi ukifuatiwa na Vitu Vikuu vya Pili vya Dunia vilisaidia kuleta mabadiliko makubwa kwa pande zote mbili, kwa watawala na watawaliwa huko Uingereza na hasa Afrika ya Kibelgiji, ambako baada ya Manazi kuiteka Ubelgiji, Kongo iligeuka kuwa dola-huru la kikoloni.

Katika kushughulikia historia ya Uingereza na Ubelgiji katika Afrika kati ya mwaka 1935 na 1945, ni muhimu kuonyesha kwa mapana fomyula za kisiasa na kiuchumi zilizotumiwa, na kujibu maswali muhimu ya jinsi aina tofauti za utawala zilivyoathiri maisha ya Waafrika waliotawaliwa. Hapa ndipo mkuu wa uchumi na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia viposaidia kuwafanya watu waelewe athari za utawala wa kikoloni na namna wananchi walivyopambana nao. Mpaka hivi karibuni, ilikuwa inakubalika kwa ujumla kuwa Vita Vikuu vya Pili ndivyo vilivyofikisha ukoloni kipeoni katika historia yake Afrika. Baadhi ya Wanazuoni wanadai kuwa mdororo mkuu wa uchumi ulikuwa pia chanzo cha mabadiliko yaliyoleta uondoshaji wa ukoloni.[1] Kabla ya vita, kuanguka kwa soko la dunia kuliwafanya watawala wa makoloni washindwe kuwatosheleza watu wao katika makoloni, na hivyo kuondoa imani juu ya makusudio yao ya ya kibeberu. Katika miji haja ya kuwa na mageuzi ya sera za kikoloni ilianza mapema, na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilitoa mwanya kwa mageuzi yaliyokuwa yamefikiriwa au kutekelezwa. Katika himaya ya Waingereza ya Afrika Magharibi, mageuzi ya kijamii na kiuchumi yaliyokusudiwa na Sheria ya Kikoloni ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii ya mwaka 1940, na mabadiliko ya kikatiba yaliyofafanuliwa wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, yalikuwa na chimbuko lake katika harakati za kabla ya vita. Zaidi ya hayo, mdororo mkuu wa uchumi ulishusha kwa ghafla uwezo wa Waafrika wa kununua vitu; hii iliongeza kutoridhika kwao na utawala wa kikoloni. Kwa wanazuoni wengine, mabadiliko yaliyoletwa na Ofisi ya Kikoloni ya Waingereza yalikuwa ni matokeo ya kuongezeka kwa shinikizo la wazalendo ambalo lilichangiwa na zahma ya Abyssinia ya mwaka 1936.

[1] Wasomi wa Kifransz wamevutiwa zaidi na dhima ya mdororo wa kiuchumi katika historia ya Afrika wakati wa ukoloni

# Mawanda ya miundo ya kisiasa na kiuchumi katika Afrika iliyokuwa chini ya Uingereza na Ubelgiji

Katika makoloni ya wazungu kama lile la Rhodesia ya Kusini au jimbo la Katanga la Kongo ya Kibelgiji, Wazungu wahamiaji walikuwa ndiyo wakala wakuu wa unyonyaji wa raslimali. Waafrika waliwafanyia kazi Wazungu ambao walichukua ardhi yao. Huko Afrika Kusini maeneo yaliyokaliwa na Wazungu na Waafrika yalitengwa kikamilifu na Sheria ya Kugawa Ardhi ya mwaka 1930.

Nchi za Rhodesia ya Kaskazini (sasa Zambia) na Swaziland zilizochukuliwa na serikali ya Kiingereza kuwa ni maeneo ya Wazungu walowezi, ingawaje zilikuwa mbali kutoka Afrika Kusini. Idadi ya Wazungu walowezi ilikuwa ndogo sana na walihodhi eneo ndogo sana la ardhi na shughuli zao zilikomea kulikopita reli na kwenye vitongoji vya mashamba ya wazungu. Waafrika walio wengi walisimamiwa na watumishi wa serikali ya Kiingereza, ambao walifuata sera ya utawala wa mlango wa nyuma iliyolingana na ile iliyokuwa inatumika kule Swaziland ambako ardhi kubwa na yenye rutuba ilichukuliwa kwa nguvu na Walowezi Wazungu toka kwa Waafrika kwa njia zisizo halali.

Mbali na kutangaza mwaka 1923 kuwa mahitaji ya Waafrika yatakuwa na umuhimu wa kwanza, Kenya nayo ilichukuliwa kuwa ni koloni la Wazungu walowezi. Wakiwa na viti 11 vya kuchaguliwa katika Baraza la Kutunga Sheria walowezi waliweza kuchunga maslahi yao mpaka katikati ya miaka ya 1930, wakati utawala huko Kenya ulipowasilisha mabadiliko ya jumla ya mfumo wa biashara ili kulinda uzalishaji wa wakulima Wazungu walowezi dhidi ya Wakikuyu na Waluyha wenye mashamba[2]. Hii ilikuwa ni kinyume cha kule Rhodesia ya Kusini ambako walowezi waliweza kuanzisha ukiritimba katika soko la wenyeji. Hata hivyo utawala wa Kenya uliwakubalia walowezi baadhi ya madai yao miaka kadha baadaye ili kufanikisha juhudi za vita vikuu. Hata hivyo imani ya Waafrika kwanza kwa Waafrika wa Kenya lilionekana kuwa ni unafiki tu, japo liliwapa nafasi nzuri zaidi kuliko Waafrika wa Rhodesia ya Kaskazini ambao hadi mwaka 1930 mustakbali wa nchi yao ulihusishwa zaidi na maslahi ya walowezi.

Sera katika makoloni manne ya Waingereza huko Afrika Magharibi, yaani Nigeria, Ghana, Sierra Leone na Gambia, ilikuwa tofauti kabisa. Huko Waafrika walionekana kama wakala wakuu wa uzalishaji na kunyang'anya ardhi kwa ajili ya wakulima Wazungu kulipigwa marufuku.[3] Hata hivyo kulikuwa na upekee katika

[2] D. Anderson na D. Throup, 1985, uk. 328

[3] R. Shenton, 1986, anajadili vizuri uhusiano wa wafanyabiashara wa kibepari na wakulima wa karanga na pamba Nigeria ya Kskazini.

sheria hiyo, hasa pale makampuni ya migodi yaliporuhusiwa kuchukua ardhi katika nchi ya Ghana, Sierra Leone na Nigeria.

Nchini Sudan, utawala ulithamini uchukuaji wa ardhi ya ekari milioni moja kwa ajili ya kilimo cha pamba. Nchini Nigeria serikali ilichukua ardhi kwa ajili ya migodi ili kutoa nishati kwa ajili ya reli.[4] Katika makoloni haya ya Uingereza mbinu ya utawala ilikuwa ni ya mlango wa nyuma kwa kutumia machifu, ambao walikuwa ndiyo watendaji wa serikali za mitaa na walihusika binafsi na uendeshaji wa sheria. Walikuwa chini ya usimamizi wa maofisa wa Kiingereza machifu waliokuwa na nafasi kama hizo kwa kawaidha waliendelea kuzishikilia hata baada ya uhuru. Katika nchi zilizotawaliwa kwa utawala wa mlango wa nyuma, wazungu walihusika kidogo katika maisha ya moja kwa moja ya Mwafrika, ingawaje wakati wa kutekeleza mambo yaliyohusu koloni zima, chifu alikuwa wakala wa serikali kuu.

Baina ya makoloni yaliyokuwa na utawala wa moja kwa moja na yale ya utawala wa mlango wa nyuma, kulikuwa na yale makoloni ambayoraslimali zao za kilimo na madini zilinyonywa na kampuni ambazo zilidhibiti uendeshaji wa maisha ya kila siku ya wafanyakazi Waafrika na familia zao. Mfano mzuri wa koloni la aina hii ni Kongo ya Kibelgiji na mashamba yake makubwa, na makampuni makubwa ya migodi.

Katika sehemu kubwa ya ardhi ambayo haikuwa chini ya milki ya Kampuni, sera rasmi ilikuwa kuiweka ardhi ya kilimo katika mikono ya Waafrika na kuwatayarisha kuwa wamiliki wa ardhi. Katika maeneo haya Wakongo walikuwa chini ya mfumo wa utawala sawa na ule wa utawala wa Wafaransa ingawaje ulijengwa kutokana na utawala wa mlango wa nyuma wa Waingereza. Ili kuunda maeneo ya utawala yanayofaa, Wabelgiji walipunguza idadi ya machifu wadogo, na kuwaweka pamoja katika makundi (*Secteurs*) na kisha kuyaundia mabaraza yaliyoendeshwa na mmoja wa machifu katika kundi hilo. Katika maeneo yaliyoitwa ya wapagani ya Nigeria Kaskazini na katika Tanganyika (sasa Tanzania), mfumo kama huo ulitumika, ingawaje tofauti kubwa kati ya mfumo huo na ule wa Wabelgiji ni kuwa Wabelgiji hawakujali sana mila za jadi wakati wa kuteua machifu au katika kurekebisha muundo uliokuwapo kabla ya ukoloni. Katika baadhi ya sehemu za Nigeria Mashariki, Waingereza waliwaondoa Warrant Chiefs waliowaweka wenyewe na badala yao walirudisha mabaraza ya jadi ambayo yalifanya maamuzi kimila. Machifu wa Kibelgiji kwa upande mwingine, walipewa uhuru mdogo tu wa

[4] Kimsingi ardhi yote ya Nigeria ya Kaskazini ilikuwa ya Waingereza, lakini ardhi yaNigeria ya Kusini ilishikiliwa na "wenyeji" na utawla wa Waingereza ulibakia kwenye hatua za kudhibiti utengaji wa ardhi wa Waafrika kwa wasi Wafrika, ingawa wao hawakujijumuisha kwenye kategoria hii! Angalia Lord Itailey, uk. 731-5

kimila. Machifu wa Kibelgiji kwa upande mwingine, walipewa uhuru mdogo tu wa kufanya mambo, kama ilivyokuwa katika mfumo wa Wafaransa, walisimamiwa kwa karibu sana.[5] Huko Nigeria Kaskazini mbali na ukweli kwamba utawala wa mlango wa nyuma uliwapa mamlaka kiasi maamiri na wakuu wa wilaya, bado waliendelea kubaki chini ya usimamizi mkali wa utawala wa Uingereza. Zaidi ya hiyo kufikia miaka ya 1930 Waingereza walikwishabadilisha muundo wa utawala wa wenyeji katika maeneo ya kiamiri kiasi cha kuonekana kuwa ni muundo wa "jadi".

Katika milki ya mashamba na makampuni ya migodi, ubora wa utawala wa jamii uliweza kutofautiana sana. Kufikia miaka ya 1930 *Union Miniere* ilianzisha sera ya kampuni kuwalea wafanyakazi wake, sera ambayo Kongo ilisifika kwayo: Wafanyakazi walipewa mikataba ya miaka mitatu mitatu, na walihimizwa kuleta familia zao ili waishi nazo, walipewa nyumba na walilishwa vizuri, walipata huduma za matibabu, na saa za kazi zilipunguzwa hadi saa nane au tisa. Aidha waliruhusiwa kupumzika siku nne kila mwezi. Wafanyakazi waliishi katika *cite-des travailleurs* chini ya msimamizi wa *chef de camp* (kiongozi wa kambi) aliyeteuliwa na kampuni, ambaye kazi yake ilikuwa kuamua migogoro na kusikiliza malalamiko. Waafrika walibaki na fursa kidogo sana ya kujiamulia mambo. Hivyo *Union Minière* iliwashikilia sana wafanyakazi wake.

Katika mashamba ya chai ya Nyasaland (sasa Malawi), wafanyakazi walijiona kama watumwa tu. Walifanya kazi chini ya mfumo wa *thangata* ambao mpangaji kwenye eneo la ardhi inayomilikiwa na Mzungu alilazimika kufanya kazi bila malipo kwa miezi miwili; mwezi mmoja ni wa kodi na mwezi wa pili ni kodi ya pango.[6] Katika miaka ya vita, wakulima walowezi walidhibiti kikamilifu maisha ya wafanyakazi na familia zao bila kuingiliwaji sana na utawala wa Waingereza. Wafanyakazi waliweza tu kuonyesha upinzani wao kimyakimya.[7]

Makundi mawili ya mkoloni yaliwakilisha mifano miwili maalum. Mfano wa kwanza ulikuwa ni wa maeneo matatu yaliyomilikiwa na Balozi za Uingereza katika Afrika Kusini ambayo yangeweza kushirikishwa kwenye Muungano wa Afrika Kusini. Kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1909 ya Afrika Kusini.Kusini[8] Katika hali hiyo, utawala wa Waingereza haukuwa na malengo ya muda mrefu, na

[5] Tazama M. Crowder, 1970, uk. 320-50
[6] L. Vail, 1977, kk. 365, na 1983, uk. 50-1
[7] R. Palmer, 1986, uk. 119-21
[8] Sheria ya Afrika ya Kusini, 1909: xi Majimbo Mapya na Mikoa: Sehemu ya 151. Angalia G.W. Eybers, 1918, uk. 554

yao ya kukataa kuingizwa ndani ya Muungano (wa Afrika Kusini) waliouchukia. Maeneo haya yaliendeshwa na Balozi wa Uingereza ambaye pia alikuwa mwakilishi mkuu wa Uingereza kwa serikali ya Afrika Kusini, na hivyo maamuzi yote yaliyohusu maeneo hayo yalichukuliwa kwa tahadhari kwa kuzingatia uwezekano wa serikali ya Afrika Kusini kujibu.

Kundi la pili liliundwa na yaliyokuwa makoloni ya Ujerumani yaliyowekwa chini ya uangalizi wa Uingereza na Ubelgiji na Shirikisho la Mataifa baada ya Vita Vikuu vya Kwanza. Kiutendaji Waingereza na Wabelgiji hawakuwajibika sana kwa Shirikisho la Mataifa, Shirikisho halikuwa na njia ya kushinikiza mabadiliko au mageuzi kwa niaba ya nchi lindwa. Wabelgiji waliheshimu zaidi miundo ya 'jadi' katika Ruanda-Urundi kuliko walivyofanya kule Kongo. Nchini Tanganyika (zamani *German East Africa*) Waingereza waliamua kuwa koloni hilo la walowezi la zamani liachiwe Waafrika badala ya Wazungu wahamiaji kuliendeleza. Nchi lindwa ya Waingereza ya Togo iliunganishwa kiutawala na nchi ya Ghana (zamani *Gold Coast*), ambapo sehemu za kaskazini na kusini za Kameruni ziliunganishwa na Nigeria Kaskazini na Kusini kwa mfuatano huo.[9] Nchi ya udhamini ya Ruanda-Urundi, ambayo iliendeshwa kipekee, iliingizwa chini ya mamlaka ya gavana-jenerali wa Kongo ya Wabelgiji.

Mifumo ya mamlaka ya Waingereza na Wabelgiji ilikuwa na aina anuwai za utawala. Hata hivyo kulikuwa na tofauti moja kubwa baina yao. Katika makoloni ya Wabelgiji, Waafrika siyo tu kwamba hawakuwa na haki kisiasa, bali katika kipindi hicho haikutarajiwa kuwa wangepata haki hiyo. Katika makoloni ya Waingereza, ukiondoa koloni la Rhodesia na maeneo yaliyokuwa chini ya balozi, malengo ya muda mrefu ya sera za kikoloni yalikuwa ni kukabidhi kwa Waafrika wajibati za kisiasa. Sera hii ilikuwa ni mabaki ya mwelekeo wa usimilishaji wa sera za kikoloni za Waingereza za karne ya kumi na tisa, wakati Waafrika walioelimika na kuwa na kiasi fulani cha mali waliporuhusiwa kupiga kura. Makoloni hayo ya Waingereza yalikuwa mstari wa mbele katika msafara wa kuelekea uhuru. Kwa upande mwingine, kuwepo kwa masetla na mapuni ya migodi kulizuia ukabidhi wa mamlaka ya kisiasa. Pia ubora wa uhuru ulitegemea kiwango na namna Waafrika walivyopewa fursa ya kushika miundo hasa ya madaraka ya kisiasa, na kupata elimu, katika miaka iliyotangulia. Kushindwa vibaya kwa uhuru wa Kongo kulikuwa ni matokeo ya wazi ya kushindwa kwa Wabelgiji kutoa elimu ifaayo kwa Waafrika na kuwashirikisha katika maisha ya kisiasa ya koloni.

Katika kipindi hiki mambo matatu muhimu yalisaidia kutoa mwanga kwa

[9] Mwaka 1939, Majimbo ya Kusini yaligawanya kwenye Majimbo ya Mashariki na Magharibi wakati meruni ya Kusini ilitawaliwa kama mojawapo ya majimbo ya Mashariki

Katika kipindi hiki mambo matatu muhimu yalisaidia kutoa mwanga kwa watawala juu ya vitendo vya Waafrika. Mdororo Mkuu wa Uchumi, mgogoro wa Uhabeshi na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia.

## Mdororo mkuu wa uchumi

Athari za zahama iliyoanza mwaka 1929 ziliendelea kuwepo mpaka uchumi ulipofufuka kutokana na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Matokeo ya zahama hiyo yalitofautiana toka koloni moja hadi jingine kutegemea madini yaliyosafirishwa nje, mazao yaliyolimwa na mbinu za uzalishaji zilizotumika, au namna mnyumbuko wa kilimo cha kujikimu au uchumi wa viwanda ulivyokuwa. Vivyo hivyo, ingawa nchi zote za kusini mwa Sahara zilikumbwa na matatizo makubwa, Afrika Kusini iliweza kujijengea msingi wake wenyewe wa viwanda na kuweka misingi ya hegemonia yake ya kiuchumi maeneo mengine ya kusini mwa Afrika na Afrika ya kati. Kuhusu wakulima wadogo wadogo, sasa walilazimika kuzalisha maradufu ili waweze kupata mapato yanayolingana na ya wakati wa nyuma: Kutoka mwaka 1929-1930 na 1933-1934 bei ya karanga ilishuka kutoka £9 kwa tani hadi karibu £2 kwa tani.

Kwanza kabisa, katika Kongo ya Wabelgiji utawala ulihakikisha kuwa hakukuwa na uzorotaji wa uchumi kwa kuwalazimisha Wakulima wadogowadogo kuzalisha mazao ya kusafirisha nje na mazao ya chakula. Katika migodi ililazimisha bei zilizokuwa chini ya bei za soko. Zaidi ya hayo, upatikanaji wa uhakika wa chakula rahisi kwa wafanyakazi ulisaidia kupunguza gharama za nguvu kazi bila kupunguza ujira. Pili, katika makoloni tunayoyazungumzia, Waafrika walilazimika kulipa kodi ya moja kwa moja katika kipindi hiki chote na kuanguka kwa bei za mazao walizolipwa Waafrika hakuwasaidia kupunguziwa kodi. Hivyo basi iliwalazimu kuzalisha zaidi ili kuweza kulipa kodi. Tatu, katika makoloni kama la Kongo ya Wabelgiji, mpomoko wa uchumi ulilazimisha punguzo kubwa katika idadi ya wafanyakazi wa ajira, hivyo wafanyakazi wengi walirudi vijijini kulima ili waweze kulipa kodi. Mwishowe, Waafrika wengi walihiyari kulima eneo kubwa zaidi la ardhi ili wapate uwezo wa kuendelea kununua bidhaa kutoka nchi za nje. Matokeo ya yote haya ni kuwa mazao ya kuuza nje yaliongezeka japo mapato yote hutoka kwa wakulima huenda hayakupanda kutoka kiwango cha mwaka 1928-1929 hadi kufikia Vita Vikuu vya Pili vya Dunia.

Kwa jumla Waafrika walioathirika kidogo tu kutokana na mdororo wa uchumi ni wale waliojihusisha tu na kilimo cha kujikimu. Walikuwa wamezoea kulipa kodi, na walijihusisha kidogo sana na mazao ya fedha. Lakini kwa wale

waliotegemea zaidi mazao ya kuuza nje ya nchi mshituko ulikuwa mkubwa sana.

Athari za ujumla za mdororo wa uchumi kwa Waafrika wazalishaji vijijini ni kuongezeka kwa hali ya kutoridhika na utawala wa kikoloni. Kutoridhika huko kwa watu wa vijijini kulipanda mbegu ya utaifa ambayo wanasiasa wazalendo waliirutubisha zaidi miaka ya 1940.

Makali ya mdororo wa uchumi wa dunia yaliiathiri zaidi migodi ya shaba ya Katanga na Rhodesia Kaskazini (Zambia). Kuanzia 1930 hadi 1932, bei ya shaba iliporomoka kwa 60%, na huko Katanga wafanyakazi waliopunguzwa walirejeshwa vijijini.

Kutokana na kushuka kwa bei, ujira wa wale waliobaki kazini pia ulishushwa. Nafuu ya uchumi ilianza kuonekana katikati ya miaka ya 1930, lakini ni mpaka Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilipoanza ndipo mapato yaliweza kufikia kiwango kilichokuwapo kabla ya mdororo. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dhahabu duniani, ukwasi uliotokana na dhahabu huko Afrika Kusini uliusisimua uchumi wa makoloni ya Uingereza ya Afrika ya kati na kusini mwa Afrika. Katika migodi ya dhahabu ya Rand mahitaji ya wafanyakazi yalikuwa makubwa kiasi cha serikali ya Muungano kulegeza amri ya kupiga marufuku kuingiza wafanyakazi kutoka kaskazini ya latitudo ya 22$^0$ kusini. Hii ilitoa mwanya wa kazi kwa watu wengi ambao kama si kazi hiyo wangepata taabu sana katika kulipa kodi yao. Mfano mzuri ni wa watu wa Busutoland (sasa Lesotho) na koloni lindwa la Bechuanaland (sasa Botswana).

Kwa wafanyakazi wa mashambani popote pale walipokuwa athari za mdororo wa uchumi zilikuwa ni zilezile: Kufukuzwa kazi au kupunguzwa mshahara. Iwe wakulima Wazungu, wageni waliomiliki mashamba au mabepari uchwara walioinukia katika Ghana, Nigeria Magharibi au Uganda, hao wote walilazimika kupunguza wafanyakazi, wengi wao wakiwa wahamiaji. Huko Uganda, mishahara kwa kazi za kilimo katika baadhi ya maeneo ilipungua kufikia nusu yake kati ya mwaka 1929-1934 na hasa kuathiri Ruanda na Burundi ambako wafanyakazi wengi wahamiaji ndiko walikotoka.

Waliathiriwa zaidi na mdororo wa uchumi walikuwa wakulima walowezi na waajiriwa wa wageni kwenye mashamba na makampuni ya migodi. Hawa ama waliachishwa kazi, au waliishi kwa taabu sana baada ya bei za mazao kushuka sana, na hawakuwa na njia nyingine ya kujisaidia. Kampuni zilizokuwa zinaingiza na kusafirisha bidhaa nazo ziliathiriwa sana. Kampuni ndogondogo nyingi zilifungwa au zilichukuliwa na kampuni kubwa kubwa. Kwa mara nyingine tena idadi kubwa ya wazungu na Waafrika waliosoma waliachishwa kazi. Waafrika walioachishwa kazi waliingia katika vyama vya siasa ambavyo vilipinga utawala

wa kikoloni, na waliporudi vijijini kwao walikwenda na fikra mpya. Waafrika wachache wafanyabiashara walinusurika hadi miaka ya 1930 walikuwa wamechoshwa na utawala wa kikoloni ambao mwanzo waliuunga mkono.

Kwa tawala żote za kikoloni, mdororo wa uchumi ulimaanisha kuanguka kwa mapato yao yalitokana na kodi ya bidhaa zinazoingizwa na zile zinazosafirishwa nje. Kitu ambacho tawala hizo ziliweza kukifanya mara tu ni kuachisha kazi wafanyakazi. Waafrika walijikuta katika soko la nguvukazi ambalo halikuweza kuajiri ziada hii ya Waafrika wasomi. Wakati huo huo kupunguzwa kwa kasi kwa watumishi Wazungu kulisababisha wataalamu wengi wa kigeni kuondoka. Idadi ya Wazungu nchini Kongo ilipungua kutoka 25,700 mwaka 1930 hadi 17,600 mwaka 1934. Upunguzaji huo wa watumishi pia ulisababisha upunguzaji wa huduma zilizotolewa na utawala, hasa katika sekta za afya, elimu na ujenzi. Hivyo Waafrika wachache wasomi ambao awali waliandaliwa kusaidia dola la kikoloni sasa walilichukulia kuwa limefilisika.

Ingawa kazi za maendeleo hata mara moja hazikuwekwa katika ajenda bayana na utawala wa kikoloni, lakini zilifanywa na tawala za wenyeji katika kujenga barabara, reli, madaraja na bandari. Miradi mingi kati ya hiyo, ambayo ilianzishwa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao huenga ng'ambo, iliahirishwa au kuachwa kabisa wakati wa mdororo wa uchumi, na kazi za ujenzi hazikurudia kiwango kile cha awali cha mwishoni mwa miaka ya 1920 hadi wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Sheria ya Waingereza ya Maendeleo ya Makoloni ya mwaka 1929, iliyotungwa kabla ya mdororo wa uchumi, ilikusudiwa kuchochea miradi ya uzalishaji katika makoloni, ili mradi miradi hiyo ilete manufaa kwa uchumi wa nchi tawala. Kutokana na hilo, daraja la Zambezi iliamuliwa lijengwe siyo kwa faida ya Nyasaland (Malawi) bali ili kuvipa soko viwanda vya chuma na chuma cha pua vya Waingereza vilivyokuwa vimekwama.

Baadhi ya watekelezaji wa sera za kikoloni walikuwa wanaelewa kuwa ingeshindwa; hao ni pamoja na Philip Mitchell aliyekuwa gavana wa Uganda mwaka 1935 hadi 1940 na ambaye mwaka 1939 alielezea picha ya hali halisi ya kudorora kwa makoloni. Kwa hivyo wakati huo huo upinzani wa Waafrika dhidi ya utawala wa kikoloni uliochochewa na mdororo ukizidi kupamba moto, ukosoaji wa aina hiyo hiyo ulikuwa ukifanywa ndani ya ofisi yenyewe ya makoloni. Maendeleo yanayofanana na haya hayakutokea Ubelgiji ingawaje yalitokea Ufaransa.

## Athari za Vita Vikuu vya Pili kwa makoloni ya Waingereza ya na Wabelgiji katika Afrika

Makoloni ya Waingereza na Wabelgiji, ambayo yalikuwa na mahusiano madogo wakati wa miaka ya mdororo wa uchumi yaliyohusu mipaka na uhamiaji wa wafanyakazi yalilazimika kuwa na umoja zaidi wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Mwezi Mei 1940 Ubelgiji ilitekwa na Ujerumani na koloni lake la Kongo likawa ndiyo kitovu cha kuwepo kwake kama taifa huru, kama ilivyokuwa *French Equatorial Africa* kwa Ufaransa. Hata hivyo Kongo ya Wabelgiji ilijiendesha kama dola la koloni huru; serikali ya Ubelgiji iliyokuwa uhamishoni mjini London ilitoa udhibiti mdogo sana. Ukweli ni kwamba serikali ya Ubelgiji iliyokuwa uhamishoni iliitegemea Kongo kwa asilimia 85 ya matumizi yake.

Uingereza, ilinusurika kutekwa, iliendelea kudhibiti makoloni yake kama ilivyokuwa kabla ya vita, lakini sasa iliyategemea makoloni yake katika kupata askari na wapagazi kwa ajili ya jeshi lake, na pia mazao ya kilimo na madini kwa ajili ya viwanda vyake. Hali iligeuka kuwa mbaya zaidi baada ya kuanguka kwa himaya za kikoloni za Ulaya katika Asia ya Kusini Mashariki kwa Japan, na hivyo kupoteza rasilimali za bati, mpira na mazao ya minazi. Makoloni yote warika ya Afrika yakawa wazalishaji wakuu wa bidhaa hizo muhimu. Tangu mwaka 1941 Kongo ya Wabelgiji ilibadilisha mwelekeo wa biashara yake; asilimia 85 ya bidhaa zilizosafirishwa nchi za nje zikawa zapelekwa Uingereza, Marekani, Rhodesia na Afrika Kusini ikilinganishwa na 5% ya mwaka 1939. Athari za mahitaji ya washirika ya bidhaa za Kongo ya Wabelgiji, ambazo awali zilipatikana toka kusini mashariki ya Asia, ilikuwa kubwa. Uzalishaji wa bati ulipanda kutoka tani 2,750 mwaka 1939 hadi tani 17,300 mwaka 1945. Mazao mengine kama mpira, mafuta ya mawese, zinki na makaa pia yalipanda kwa kiwango hicho au kikubwa zaidi. Kulikuwa na ongezeko la aina hiyohiyo katika makoloni ya Waingereza: Madini yaliyosafirishwa nje kutoka Afrika yalikuwa muhimu kwa ushindi wa nchi washirika, hususan katika utengenezaji wa mabomu ya atomi ambao ulitegemea wa madini ya urani kutoka Kongo ya Wabelgiji.

Hasahasa matumizi ya rasilimali ya nguvukazi ya makoloni yalikuwa makubwa. Kwanza makonoloni yote ya Waingereza yalitoa askari na vibarua. Baadaye mzigo mkubwa ulibebwa na wale waliobaki nyuma kwa jinsi mahitaji ya mazao ya kilimo na madini yalivyoongezeka. Hii iliambatana na mahitaji ya miradi ya ujenzi wa barabara zilizohitajika kwa ajili ya vita, au, kwa Kongo ya Wabelgiji, mahitaji ya nguvukazi katika viwanda ili kuzalisha bidhaa ambazo hapo awali zilikuwa


zinaagizwa kutoka Ulaya. Ili kuhakikisha kuwa uzalishaji wa malighafi muhimu katika Kongo ya Wabelgiji unaongezeka raia walihamasishwa katika mtindo wa kijeshi. Wakulima wadogowadogo walilazimishwa kujiunga na kazi za kulazimishwa, na mazao yalichukuliwa na serikali. Sera rasmi iliyowekwa Desemba 1933 ilitenga siku 60 kwa wanaume wote walioishi katika jumuiya za kijadi kufanya kazi za lazima, na sera hiyo ilifuatwa kwa dhati. Mwaka 1944 idadi ya siku za lazima za kufanya kazi iliongezeka hadi siku 120. Wale walioshindwa kufanya kazi hizo walipelekwa mbele ya mahakama ya kipolisi. Katika himaya za Waingereza, utaratibu wa kazi za lazima haukufuatwa sana, ila katika migodi ya bati ya Nigeria na katika mashamba ya mkonge ya Tanganyika. Ingawa kwa kiasi kikubwa uandikishaji wa askari na vibarua wa jeshi kinadharia ulikuwa wa hiari, lakini kiutendaji aghalabu ulikuwa wa lazima. Wakala wakuu wa uandikishaji walikuwa machifu, ambao wakati mwingine walilazimisha watu ili kuhakikisha idadi inayohitajiwa na utawala inapatikana.

Waingereza na Wabelgiji walikuwa na mbinu mbili tofauti katika kuwahamasisha Waafrika. Wabelgiji hawakuona kuwa Waafrika wanaweza kuwa na majukumu ya kisiasa hapo baadaye, hivyo basi hawakufanya juhudi ya kuomba badala ya kudai msaada wao. Kwa upande mwingine Waingereza walijaribu kuwashawishi Waafrika kushiriki katika vita kwa kuwaeleza mara kwa mara kuwa walikuwa washirika wa watawala wao katika kupigania demokrasia.

Mwanzo tu wa vita, Sheria ya Kikoloni ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii ilionyesha badiliko hilo la fikra ya Waingereza katika uendeshaji wa makoloni yake: Sasa maendeleo yalitakiwa yafanywe, siyo kwa faida ya nchi inayotoa msaada, bali kwa kuzingatia mahitaji muhimu ya koloni linalohusika. Na ile kanuni ya kuwa makoloni yajigharimie yenyewe iliondolewa.

Ingawa majadiliano ya hali ya baadaye ye makoloni yalianza wakati wa vita, hakukuwa na uhakika nani awe mrithi wa madaraka na hakukuwa na ratiba ya kuonyesha lini madaraka yatahamishiwa kwa Waafrika. Katika Nigeria na Ghana, mageuzi madogomadogo yalifanywa zaidi wakati wa vita, ambapo katika Kongo ya Wabelgiji hapakuwa na mwafaka uliyofanywa kuhusu majukumu ya Waafrika kisiasa katika koloni. Baada ya vita, utaratibu wa awali wa utawala wa kikoloni chini ya udhibiti kutoka makao makuu ulirudishwa tena. Mwaka 1950 ndipo Ubelgiji ilianza kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Kongo.

Katika makoloni ya Waingereza wazo lililozaliwa kutokana na mdororo wa uchumi, kuwa serikali za Ulaya ziwajibike kwa uchumi na ustawi wa jamii wa makoloni yake, lilipaliliwa wakati wa vita. Mipango iliandaliwa kwa ajili ya



PICHA 4.1 *Bunduki nzito ya ulinzi wa anga ikitumiwa na askari wa Afrika Mashariki wakati wa Vita Vikuu vya Pili, 3 Desemba 1945.*

kuendeleza asasi za elimu ya juu, vyama vya wafanyakazi, na asasi za utafiti.

Mageuzi ya mwanzo ya muda yalifanywa kwa ya msukumo wa Marekani, pia kutoka ndani au nje ya ofisi ya makoloni na pia ili kukwepa kurudiwa tena kwa machafuko kama yaliyotokea West Indies mwaka 1940, ambayo yalisababishwa na hali mbaya ya kiuchumi na kijamii. Baada ya vita, mara ikawa wazi kuwa programu hii ya majaribio ya mageuzi ilikuwa haikidhi haja. Licha ya kufufuka kwa uchumi kulikofuatia, vita vilizidisha kutoridhika kwa watu wa mijini kulikoanza miaka ya 1930, kwani bei zilidhibitiwa na serikali, na ni serikali za Ulaya ndizo zilizonufaika kutokana na kupanda kwa bei.

Huko Kenya, serikali iliwahakikishia wakulima Wazungu bei nzuri ambazo zilikuwa kubwa mara mbili ya zile zilizotolewa kwa wakulima Waafrika na hii ilizidisha sana mingongano ya kimaslahi kati ya makundi hayo mawili.

Ingawa wakulima Waafrika hawakunufaika kutokana na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia, lakini walipaswa kununua bidhaa zilizoingizwa nchini kwa

bei ya juu. Matokeo yake yalikuwa kushuka kwa thamani ya fedha ambako kuliathiri wafanyakazi wa vijijini na mijini. Idadi ya wakazi wa mijini iliongezeka kutokana na viwanda kuanzishwa ili kuzalisha bidhaa ambazo hazikuweza kupatikana kutoka nje ya nchi, na kutokana na miradi ya kujenga barabara ambayo ilikuwa muhimu kwa ajili ya vita. Katika Kongo ya Wabelgiji, kuhama kwa makundi makubwa kutoka vijijini kulichochewa na vita, ambapo Waafrika walikimbia ili kuepuka kuandikishwa jeshini, na kodi kubwa iliyowekwa sambamba na kushuka kwa thamani ya fedha kuliandaa mazingira mazuri ya kueneza uchochezi wa kisiasa na migomo. Katika Afrika iliyotawaliwa na Waingereza kulikuwa na migomo mingi ya kudai mishahara mikubwa zaidi wakati wa vita. Nchini Kongo wafanyakazi wa kampuni ya *Union Miniere* waligoma mwaka 1941 na walilazimishwa kurudi kazini baada ya jeshi kuingilia kati, na wagomaji sabini kuuawa.

Katika makoloni ya Waingereza vita vilitoa wa matumaini kwa wasomi ambao baadhi yao walichukua nafasi za mameneja Wazungu na maofisa walioitwa kwenda vitani. Hususan, walitiwa moyo na Azimio la Atlantiki *(Atlantic Charter)* la 1941 ambalo lilisisitiza umuhimu wa kila jamii kuchagua serikali yake yenyewe na kuwa huru. Kukataa kwa waziri mkuu wa Uingereza kufuata azimio hilo kwa himaya zake katika Afrika kuliibua uchungu wa wazalendo dhidi ya utawala wa kikoloni.

Katika makoloni ya Wabelgiji Afrika, kiwango cha juu cha elimu kilikuwa shule ya msingi, juu ya hapo elimu ilitolewa na shule za seminari za Wakatoliki. Wanaume waliochukuliwa kutoka mashamba yao kwenda vitani au kuwa vibarua walijifunza ujuzi mpya na kuongeza upeo wao na waliporejea kwenye nchi zao matarajio yao yalikuwa yamebadilika. Katika makoloni ya Wabelgiji, wakati wa vita, wasomi Waafrika walijaribu kwa mara ya kwanza kubomoa nadharia ya utawala wa kikoloni katika njama za haraka zilizofanywa na maofisa wa chini wa jeshi. Nchini Nigeria na Ghana askari waliokuwa wanarejea walikuwa wanaharakati imara na wakati mwingine waliongoza vyama vya siasa vilivyodai serikali ya madaraka kwa Waafrika.

## Mwisho: Afrika iliyotawaliwa na Waingereza na Wabelgiji katika mkesha wa mapambano ya kudai uhuru

Mwaka 1935 ilikuwa ni vigumu kufikiria kuwa katika robo tu ya karne, makoloni ya Waingereza na Wabelgiji katika Afrika yangekuwa huru. Uhuru lilikuwa neno lililotumiwa kwa shida na wanasiasa Waafrika, na hadi 1945 lilibakia kuwa lengo lao la mbali. Muongo wa 1935 - 1945 ulikuwa muhimu katika historia ya mkoloni, ambao ulikumbwa na mabadiliko yaliyotokana na jumla ya athari za mdororo



Picha 4.2 *Siku ya Uhuru wa Swaziland: Chifu Sobhuza 11, Simba wa Swaziland, anakagua gwaride*

mkuu wa uchumi na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, ingawa kulikuwa na maendeleo fulani yaliyoanza kutokea hata kabla ya matukio hayo mawili.

Kwanza, sera ya elimu iliyokuwapo kutoka mwishoni mwa karne ya kumi na tisa katika makoloni ya Waingereza barani Afrika iliibusha tabaka la wasomi wenye mwamko wa kisiasa, na kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya wingi wa wasomi miongoni mwa wakazi wa koloni na ukuaji wa vuguvugu thabiti la kifaifa. Pili, kufikia katikati ya miaka ya 1930, Waafrika wengi walihusika moja kwa moja na uchumi wa kikoloni, na hivyo karibu wote waliathiriwa na sera za utawala wa kikoloni.

Mdororo Mkuu wa uchumi na Vita Vikuu vya Pili vya Dunia viliwezesha wasomi wachache, na wakulima wadogowadogo na wafanyakazi wa ujira kuona vizuri zaidi maonevu ya mfumo wa kikoloni. Hali iliwafanya wakoloni wakabiliane na Afrika iliyokuwa tofauti na ile ya miaka ya mwanzo ya 1930. Tofauti na Waingereza, Wabelgiji hawakuwa wamejiandaa kwa mabadiliko haya, hivyo matokeo yake yalikuwa ni maafa makubwa.

# 5

# Utafute kwanza ufalme wa kisiasa

"Utafute kwanza ufalme wa kisiasa, na vitu vyote utaongezewa"[1] Aliposema maneno hayo Kwame Nkrumah aliamini kuwa uhuru wa kisiasa ulikuwa ndiyo ufunguo wa mengine yote yanayoweza kurekebisha hali ya Afrika. Kiundani kauli hiyo ilikuwa na falsafa ya kuona siasa kama msingi wa maisha ya binadamu; ni falsafa tofauti na ile inayozingatia uchumi kuwa msingi wa mambo yote.

Kwa namna fulani Kwame Nkrumah alikuwa sahihi kwa kuipa siasa umuhimu huo. Afrika ya kikoloni awali ilibidi itafute uhuru wa kisiasa kabla ya kitu kingine chochote kuongezwa juu yake. Uhuru wa kisiasa (au "ufalme ya kisiasa") kwa hakika ulikuwa sharti muhimu kabla ya Afrika kupata au kufikia matarajio yake ya msingi. Hata hivyo halikuwa sharti linalotosheleza.

Kufikia miaka ya 1980, katika nchi yake mwenyewe Nkrumah, Ghana, hali ilionyesha kuwa kinyume na mawazo yake. Hali ya Ghana ilionyesha kudai kuwa: "utafute kwanza ufalme wa kisiasa na mengine yote yatapunguzwa hapo". Uchumi ulikuwa mbaya zaidi kuliko wakati nchi ilipopata uhuru wa kisiasa; mfumo wa elimu ulididimia na miundombinu ilichakaa. Tukichukua mfano wa Ghana kama msingi wa uchambuzi wetu, tujiulize mizania katika kutafuta ufalme wa kisiasa ikoje. Nini matokeo ya kupambana kwa ajili ya "mengine yote" yanayostahili kuongezwa. Haya ndiyo baadhi ya maswali yatakayojadiliwa katika sura hii.

## Utaifa unazaliwa upya

Mapambano kwa ajili ya ufalme wa kisiasa au uhuru wa kisiasa katika makoloni ya Afrika yalikuwa katika awamu nne. Awamu wa kwanza ilikuwa kabla ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia; hii iliashiriwa na madai ya wasomi ya kutaka uhuru

[1] K. Nkrumah, 1957, uk. 164

mkubwa zaidi. Baadaye kukawa na awamu ya kujihusisha na mapambano dhidi ya unazi na ufashisti. Tatu, kulikuwa na mapambano yasiyotumia nguvu kudai uhuru kamili baada ya Vita Vikuu vya Pili. Mwisho kukawa na vita vya kugombea ufalme wa kisiasa - vita vya msituni dhidi ya serikali za Wazungu wachache, hasa kuanzia mwaka 1960 na kuendelea.

Baadhi ya vikundi vya mwanzo vya wasomi vilikuwa katika muundo wa vyama vya utamaduni na vikundi vyenye maslahi maalumu. Katika kipindi kati ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, aina mbalimbali za vyama vya kikabila na kiukoo vilianzishwa katika makoloni mbalimbali, kiasi vikiwa vimetiwa hamasa na umoja kati ya wafanyakazi wahamiaji wa mijini, na kiasi vikitokana na utambuzi wa jumla wa kukengeushwa kwa Waafrika katika mazingira ya unyonyaji wa kikoloni. Katika maeneo ya Waislamu katika Afrika, vyama vya utamaduni wakati mwingine vilihusishwa na dini zaidi kuliko ukabila.

Kulikuwa na misukosuko ya aina nyingi kati ya miaka ya Vita Vikuu vya Kwanza na vya Pili vya Dunia. Kwa mfano, mwezi Mei 1935 kulikuwa na migomo ya Waafrika na machafuko katika ukanda wa Shaba wa Rhodesia ya Kaskazini (Zambia). Huko Nigeria, vikundi ama aina ya watu wenye dhamira moja vilianzishwa. Vyama vya Utamaduni na vya wasomi Waafrika na watu wenye asili ya Afrika vilianzishwa nje ya Afrika. *Léopold Sédar Senghor na Aimé Césaire* walianzisha *l'e'tudiant noir* (Chama cha Wanafunzi Weusi) kule Ufaransa. Nao Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta na W.E. DuBois walikuwa wapigania Umoja wa Waafrika nchini Uingereza na Marekani.

Ni kweli kuwa vyama hivyo vya awali vilikuwa kimsingi ni vya wasomi na vikundi vingi vilikuwa hasa hasa mijini, lakini siasa za umma zilianza katika kipindi hicho hicho cha kati ya vita vikuu vya dunia. Habib Bourguiba alianzisha kampeni ya raia kutotii huko Tunisia ambayo ilisababisha machafuko mjini Tunis.

Mbinu zilizotumika dhidi ya ubeberu katika hatua hii kimsingi zilikuwa si za fujo na si za uchochezi, mbali na yale mapambano ya Wahabeshi dhidi ya Waitalia. Kadri Vita Vikuu vya Pili vilivyoendelea, Afrika kwa ujumla ilibidi ichague kati ya ubeberu chini ya uliberali (siasa za wastani) wa kibwanyenye, na ubeberu chini ya Manazi na mafashisti. Utata huu ulikuwa mbaya zaidi katika makoloni ya Wafaransa kwa kuwa Ufaransa yenyewe ilikuwa imetekwa na kugawanywa.

Ushiriki wa Waafrika katika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia ulikuwa mkubwa katika bara lote. Je kushiriki kwa Afrika kulikuwa ni suala la ushirikiano na mataifa tawala? Au ichukuliwe kuwa ilikuwa awamu maalum ya mapambano dhidi ya ukoloni?

Kwa ujumla falsafa iliyokuwapo ilipendelea "mazimwi" ambayo Waafrika tayari waliyajua (hususan Uingereza na Ufaransa Huru) kuliko mazimwi mapya ya Manazi na mafashisti. Madai ya Hitler ya mwaka 1936 kutaka kurudishiwa makoloni ya Ujerumani yalifanya hofu kuzagaa katika maeneo yale ambayo awali yalitawaliwa na Wajerumani. Kwa mfano Ligi ya Tanganyika ilianzishwa mwaka 1938 kupinga Tanganyika kurudishwa kwenye utawala wa Wajerumani.

Kushiriki kwa Afrika katika vita haukuwa mwenendo wa kushirikiana na mabeberu bali ilikuwa ni njia ya kupambana dhidi ya utwazi mbaya zaidi. Ilikuwa ni sehemu muhimu sana ya mapambano ya Afrika ya kupinga unyonyaji wa kutoka nje na kudai haki za binadamu.

Kwa hakika vita yenyewe ilichangia katika kudhoofisha tawala za kibeberu katika pande zote za mgogoro. Kushindwa kwa Ufaransa kulisaidia kuteketeza imani ya Wafaransa kuwa Ufaransa haishindiki. Uingereza ilifilisiwa na kuchakazwa na vita, na ilipoteza azma yake ya kuwa na himaya kubwa mno. Katika kipindi cha miaka miwili tangu kumalizika kwa mgogoro uliokuwa umeikumba dunia, Uingereza ikaiachia India ijitawale. Vita vilisaidia kuibua juu zaidi dhima ya Marekani na Urusi katika ulimwengu, dhima ambayo kuanzia wakati huo iliizidi ile ya Ulaya ya kibeberu.

Kuzaliwa kwa Umoja wa Mataifa mwaka 1945 pia kulisaidia kutika uondoshaji ukoloni duniani kote. Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa likawa ndiyo mpiga debe mkuu dhidi ya ukoloni.

Dhana ya vita hivyo kama mapambano dhidi ya udhalimu na utiishaji ilionekana haiendani na ukoloni. Kwanza ukoloni wenyewe ulikuwa ni aina ya udhalimu na utiishaji. Wakati Winston Churchill na Franklin D. Roosevelt walipotia sahihi Azimio la Atlantiki (Atlantic Charter) mwezi Agosti, 1941 hawakuwa tu wanalaani uonevu katika Ulaya. Bila kuelewa, walikuwa wanatia sahihi hati ya kifo cha wazo zima la "Ukoloni wa halali" katika karne nzima ya ishirini.

Waafrika wenyewe walikuwa ndivyo nguvu muhimu sana dhidi ya ukoloni katika Afrika kwa kadiri walivyozidi kujiandaa taratibu, kuelezea madai yao kwa ufasaha zaidi, na hatimaye kuwa tayari kwa mapambano ya silaha.

Kulikuwa na jadi kadhaa za mapambano ya Waafrika katika kipindi hiki. Kulikuwa na jadi ya uaskari, jadi ya Jihad, jadi ya uasi wa Kikristo, na jadi ya uhamasishaji usiotumia nguvu. Sasa tuangalie kwa undani kila mkakati wa kupinga ukoloni, tukizingatia kuwa mikakati hiyo wakati mwingine ilikuwa inasaidiana na kuimarishana badala ya kutumika kipekee tu.



Picha 5.1 Dedan Kimathi shujaa wa vita vya Mau Mau kwa ajili ya Uhuru, aliteuliwa tarehe 21 Oktoba 1956 na kisha akanyongwa

## Mapambano ya uaskari wa jadi

Dhana hii inahusishwa na Shule ya Historia ya Waafrika ya Dar es Salaam, na hutilia mkazo "upinzani wa msingi." Shule ya Dar es Salaam ilitumia neno "msingi" kikronolojia, kwa maana ya upinzani wa awali kabisa wakati Wazungu wanapoingia na kushinda. Hapa maana ya msingi ni ya kiutamaduni zaidi kuliko kikronolojia. Wapiganaji wa MauMau waliwapinga Waingereza hadi mwishoni mwa miaka ya 1950, lakini kwa misingi ya desturi za Wakikuyu za upiganaji na imani za kidini zinazohusika, pamoja na alama za tamaduni za uaskari za kienyeji, zikiwemo sherehe za viapo. Harakati hizi zilikuwa za "msingi" kwa maana hiyo.

Lakini upinzani wa Waafrika wakati mwingine ulichochewa na tamaduni nyingine zilizokuwapo Afrika, ambazo hasa ni pamoja na nguvu za Uislamu.

## Jadi ya Jihadi katika Mapambano ya Waafrika

Majuzuu ya awali ya UNESCO ya *Historia Kuu ya Afrika* tayari yamegusia jinsi jadi ya jihadi (ikiwa na maana ya harakati katika njia ya Mungu) ilivyotumwa katika upinzani dhidi ya kuingia ubeberu katika usultani wa Sokoto nchini Nigeria ilivyotumika na kikundi cha Mahdiyya katika Sudani Mashariki, na ilivyotumiwa na utaifa uliotukuka wa Sayed Muhammad 'Abdallah Hassan.

Moyo wa Mahdiyya ulidumu nchini Sudan na alisaidia sana katika mapambano dhidi ya ubeberu wa Uingereza na ujipanuaji wa Misri. Mbinu za Mahdiyya zilibadilika jinsi muda ulivyokwenda lakini ile tabia yake ya msingi ya kupinga ubeberu iliendelea.

Wakati Algeria inaokolewa kutokana na maovu ya Vichy, uendelezaji wa hali ya wenyeji ulikuwa ni wa bandia tu. Kwa hakika, mwaka ambapo Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilipomalizika ulikuwa ni mbaya kabisa kati ya miaka ya ukandamizaji wa Ufaransa kwa Algeria. Utumiaji nguvu katika kuzima machafuko ya Setif na Kabylie uliofanywa na majeshi ya ulinzi na polisi ya Wafaransa ulisababisha vifo vya Waalgeria Waislamu 10,000. Moto wa jadi ya jihadi uliwashwa upya na kiwango hiki kikubwa cha mashahidi waliojitoa mhanga. Kufikia mwaka 1954 chama cha *National Liberation Front* kilikuwa tayari kurithi mwenge wa kurunzi la jihadi kutoka kwa shujaa wa Algeria wa karne ya kumi na tisa 'Abd al-Kadir al-Jazairi. Mapiduzi mapya ya Algeria yalikuwa yameanza.


Mapinduzi ya Misri ya mwaka 1952 yalianzisha uhusiano tofauti na Uislamu. Gamal 'Abd al-N asser, kiongozi wa mapinduzi aliifasili Misri kama kituo cha dunia tatu: Uislamu, Ulimwengu wa Waarabu na Afrika. Mapambano dhidi ya ubeberu yalikuwa yatazamwe katika muktadha wa nguvu tatu za upinzani wa Kiislamu, utaifa wa Kiarabu, na Upana-Afrika.

Hata hivyo bado al-Nasser alifanya tahadhari kuhusu kile alichokiona kuwa ni "ukereketwa" wa Ujahidi na wa Kiislamu - hasa kikundi kilichojulikana kama (Udugu wa Kiislamu).Alipiga marufuku Alikifungia kikundi hicho na baadhi ya viongozi wake walitiwa kizuizini. Gamal `Abd al-Nasser alitaka kuwe na uhamasishaji wa kisiasa wa Waarabu wote dhidi ya Usayuni na ubeberu wa Ulaya.

Ingawa umoja wa Waarabu wote ulitumia jeshi katika mapambano dhidi ya Israel, lakini nguvu kubwa ya mapinduzi ya Misri iliegemea katika uhamasishaji wa umma bila kutumia nguvu.

Wazalendo wengine Waafrika waliathiriwa zaidi na kiongozi wa India, Mahatma

Mohandas Gandhi. Yote haya yalikuwa ni sehemu ya mkakati mpana zaidi wa uhamasishaji kisiasa bila matumizi ya nguvu. Mkakati huo ulikuwa tofauti, lakini pia uliimarisha, nguvu za uaskari wa jadi, na urithi wa jihadi.



picha 5.2 *Mkusanyiko wa watu waliokamatwa kwa nguvu baada ya upinzani wa tarehe 8, Mei 1945 nchini Algeria.*

## Jadi ya Ukristo wenye siasa kali

Uislamu si dini pekee iliyopinga utawala wa kikoloni. Kulikuwa na maasi ya kushangaza zaidi ya Ukristo dhidi ya ubeberu wa Ulaya. Maana, mbali na Afrika Kaskazini na bonde la mto Nili, Ukristo uliingia Afrika ukiamhatana na ukoloni wa Wazungu.

Ubia kati ya ubeberu wa Wazungu na misioni za Wakristo uliathiri sera za elimu katika makoloni. Mgawanyo wa majukumu kati ya kanisa na dola katika "kuelimisha wazawa" ulitofautiana toka koloni moja hadi jingine, lakini hakukuwa na shaka juu ya ubia uliokuwapo kati ya kanisa na dola.

Tukiangalia ubia huu kati ya ukoloni wa Wazungu na misioni za Wakristo, inashangaza kuona kuwa shule za wamisioni zilifundisha baadhi ya Waafrika wazalendo wa kisasa wa awali kabisa. Shule za misioni zilisaidia katika kuendeleza siyo tu mawazo ya kiroho ya Kikristo bali pia itikadi za magharibi zisizofungamana na dini. Waafrika wazalendo wenye msimamo mkali walioibuka kutoka shule za misioni ni pamoja na watu mashuhuri kama Julius K. Nyerere, Tom Mboya, Eduardo Mondlane, Robert Mugabe, Léopold Sédar Senghor na pia Kwame Nkrumah.

Hata hivyo Ukristo wa Kizungu haukutoa tu Waafrika wapinzani wasiofungamana na dini, bali ulitoa pia Waafrika wapinzani waliofungamana na dini dhidi ya mfumo wa Ukristo wa Kiulaya. Mmoja wa watu waliofanikiwa zaidi katika kipindi hiki cha kihistoria ni Simon Kimbangu[2]. Kufikia miaka ya 1980, Kanisa la Kimbangu halikuwa limekiuka tu ukoloni, lakini lilikuwa limepata heshima ya kimataifa kiasi cha kuwa dhehebu la kwanza la Kiafrika kusajiliwa na Baraza la Makanisa Duniani. Lilikuwa na waumini kama milioni nne.

Dhana ya Makanisa Huru (yaliyojitenga) na ya milenia wakati wa kipindi cha ukoloni ilikuwa sehemu ya mapambano ya Afrika ili kurudisha utambulisho wake na kutetea hadhi ya utamaduni wake. Makanisa ya kawaida ya KiMagharibi yalikuwa goigoi katika kujiunga na mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi na ubeberu katika Afrika. Lakini watu binafsi kutoka makanisa hayo walijiunga na mapambano dhidi ya ukandamizaji tangu awali kabisa. Baadaye Waafrika mashuhuri wa kwanza kutunukiwa tunzo za Nobel walikuwa ni Wakristo waliopambana dhidi ya ubaguzi wa rangi: Chifu Albert Luthuli na Askofu (sasa Askofu Mkuu) Desmond Tutu, wote kutoka Afrika kusini. Ni katika Afrika ya Kusini pia ambako Hastings Kamuzu Banda, mzee wa kanisa la Scotland aliongoza Nyasaland hadi kupata uhuru na kuwa Jamhuri mpya ya Malawi.

Tunaweza kuthibitisha kuwa mchango wa Wakristo katika kuondoa ukoloni ulikuwa na sura tatu; kupitia wahitimu wa shule za misioni, kupitia makanisa huru ya Kikristo kutokana na uongozi wa makanisa ya kawaida kubadilika na kuwa na msimamo mkali.

## Mkakati wa uhamasishaji wa kisiasa usiotumia nguvu

Kampeni za raia kutokuwa watiifu zilizinduliwa huko Afrika Kusini chini ya uongozi wa Mahatma Mohandas Gandhi kati ya mwaka 1906 na 1908. Kufikia mwaka 1950 vyama vya *African Congress* na *Indian Congress* katika Afrika Kusini vilijaribu kuratibu juhudi za Waafrika, Wahindi na "machotara" katika kampeni

[2] Tazama pia Sura 17 chini, na UNESCO, Historia Kuu ya Afrika, Juz. VIII

ya umma dhidi ya sheria ya vitambulisho (Pass Law), sheria ya makazi ya makundi maalumu (*Group Areas Act*) iliyoendeleza ubaguzi wa rangi, na sheria ya mamlaka ya Wabantu (*Bantu Authorities Act*) iliyoundwa kuendeleza ukabila wa Waafrika. Kampeni hiyo ilifanikiwa kama zoezi la umoja kati ya wanaokandamizwa, ingawaje lilishindwa katika malengo yake dhidi ya wakandamizaji.

Kwame Nkrumah wa Afrika magharibi alivutiwa sana na mawazo ya Mahatma Mohandas Gandhi. Mkakati wake wa "Vitendo Chanya" (*Positive action*) kwa uhuru zaidi katika Ghana ulitiwa moyo na mkakati wa Gandhi wa *Satyagraha* (nguvu ya roho)[3]. Katika Rhodesia ya Kaskazini, Kenneth Kaunda alikuwa mfuasi wa Gandhi wakati wa ukoloni.

Upinzani wa Waafrika kwa matumizi ya silaha ulikuwa wazi katika mkutano wa watu wote wa Afrika (*All-Africa People's Conference*) uliofanyika Ghana mwaka 1958. Waalgeria, ambao walikuwa katika mapambano ya silaha dhidi ya Ufaransa, waliona ugumu kupata kibali cha Waafrika wote katika mkutano huo cha kuweza kuendelea na mapambano ya silaha.

Kwa ujumla, miaka ya 1950 ndiyo ilikuwa muongo wa mwisho wa mikakati ya Ki-Gandhi ya ukombozi wa Afrika. Baada ya uhuru wa Algeria mwaka 1962, ikawa wazi zaidi kuwa maeneo yaliyokuwa magumu kuyakomboa kwa amani yalikuwa ni yale yaliyokuwa yanatawaliwa na Wareno au yaliyodhibitika na utawala wa Wazungu wachache. Katika maeneo hayo yote, mbinu za Gandhi za raia kutokuwa watiifu hazingeweza kufanikiwa. Wakati wa mapambano kamili ya ukombozi kwa silaha ulikuwa umefika katika Afrika ya Kusini.

## Mkakati wa ukombozi kwa kutumia silaha:

Mikakati ya kimataifa zaidi ya kuondoa ukoloni katika Afrika ni ile iliyohitaji silaha za kisasa. Mbinu za jadi (kama zile zilizotumika wakati wa vita vya MauMau) ziliegemea kimsingi kwenye kujitegemea kijadi na silaha zilizotengenezwa kienyeji. Jihadi ilikuwa inahusishwa na nguvu za kimataifa (katika Uislamu) lakini katika Afrika bado ilikuwa si ya kimataifa sana. Mkakati wa Wakristo wakereketwa na uhamasishaji wa kisiasa usiotumia nguvu, hata pale vilipoathiriwa na Gandhi, mwishowe vilikuwa ni mkakati wa kitaifa katika kila koloni linalohusika.

Lakini sura ya kisasa ya mapambano ya vita - katika makoloni ya Ureno, Afrika ya Kusini na pia Algeria ilionyesha mapambano ya hali ya juu ya kimataifa. Silaha za kisasa zilizotumiwa Afrika ya Kusini kwa wingi na zilitoka nchi za kijamaa

[3] Tazama K. Nkrumah, 1957



picha 5.3 *Kwame Nkrumah siku ya mkesha wa Uhuru wa Ghana katika viwanja vya zamani vya mchezo wa "Polo", tarehe 5 Machi, 1952.*

za nje. Kushiriki kwa majeshi ya Kuba katika mapambano ya kuikomboa Angola kulidhihirisha kiwango cha juu zaidi cha msaada wa kutoka nchi za nje katika vita vya ukombozi wa Afrika.

Hata hivyo ushiriki wa mataifa ya nje haukuishia kwa wapigania ukombozi tu, pia upande wa wakoloni na wakandamizaji wabaguzi ulipata msaada. NATO – Umoja wa Kujihami wa Ulaya Magharibi, kwa muda mrefu walitoa msaada wa wazi au wa kificho kwa wakoloni wa Kireno katika kuendeleza ukandamizaji wao wa kikaidi. Katika kuangalia misaada ya kutoka nje, utashangaa ukilinganisha Kuba na Israel zilivyokuwa zinasaidia nchi zilizoko kusini mwa Afrika, hasa miaka ya 1970 na kuendelea, wakati nchi hizo zikiwa katika msigano mkubwa. Kuba ilisaidia kuwapa mafunzo askari weusi wapigania uhuru; Israel nayo ilisaidia kuwafundisha askari wa jeshi la Afrika Kusini ili kupinga mapinduzi. Kuba ikipanua huduma kwa wakulima wa Angola, na wakati huo huo Afrika Kusini ilisaidiwa na Israel katika mipango yake ya silaha za nyuklia, ukiwemo utengenezaji wa bomu la nyuklia.[4]

Kwa ujumla, mapambano ya silaha Kusini mwa Afrika yalifanikiwa vizuri. Vita dhidi ya Wareno, vilikuwa vya msuguano, na hatimaye vilisababisha mapinduzi ya Ureno ya mwezi Aprili 1974, na hivyo kuiangusha himaya ya Ureno punde baadaye. Katika Zimbabwe, mapambano ya silaha yalileta uhuru mwaka 1980, na katika Namibia mwaka 1990.

Lakini je "mengine yote" yataongezwa kwenye "ufalme wa kisiasa" katika Afrika Kusini uhuru utakapopatikana? Uhuru wa kisiasa haukusaidia mara zote, kuleta, mafanikio katika sehemu nyingine za Afrika. Katika nchi ambazo uchumi wake umeteketezwa kama nchi ya Ghana na kwa nchi zilizoharibiwa kisiasa kama Uganda, ni sahihi zaidi kuzungumzia matokeo mabaya ya uhuru.

Kuna habari kuwa Kwame Nkrumah aliwahi kusema kuwa uhuru wa Ghana hautakuwa na maana iwapo haukuambatana na uhuru wa Afrika yote. Je, aliposema "ufalme wa kisasa" Nkrumah aliimanisha uhuru wa kila nchi ya Afrika pekee? Au Mpana-Afrika huyu Mkuu wa Ghana alimaanisha ukombozi kamili wa Bara la Afrika kwa ujumla?

Katika muktadha wa falsafa ya Kwame Nkrumah kwa ujumla, huenda alimaanisha hatua zifuatazo: Uhuru wa nchi moja ya Afrika utasaidia kupatikana kwa uhuru wa nchi inayofuata - Mkabala wa hatua kwa hatua wa kuondoa ukoloni wa kisiasa. Ni pale tu Afrika yote itakapokuwa huru ndipo "ufalme wa kisiasa"

[4] Kwa kuhusiana na programu ya Afrika Kusini ya Nyuklia, lazima R.W. Walters, 1987

wa bara lote utaweza kuongezewa "vingine vyote". Sasa tuiangalie kwa makini zaidi hatua hii ya mwisho ya kutafuta "ufalme wa kisiasa".

## Mapinduzi na ufalme wa kisiasa

Sifa muhimu za awamu hii ni kwamba ushirikiano kati ya ubaguzi wa rangi na ubepari katika Afrika Kusini huenda unakaribia kuvunjika. Ingawa kuvunjika kwa ushirikiano kunaweza kuathiri ubaguzi wa rangi, ubepari katika Afrika Kusini unaweza kuendelea kuwepo hata baada ya mapambano kuisha. Ufalme wa kisiasa unaweza usiwe na nyongeza ya ujamaa.

Robo karne iliyopita, Kwame Nkrumah aliitahadharisha Afrika kuhusu mikuki miwili inayoning'inia juu yake, mkuki wa ubaguzi wa rangi na mkuki wa silaha za nyuklia zikiwa mikononi mwa maadui. Wakati ule Wafaransa walikuwa wanafanya majaribio ya silaha za atomiki katika Sahara. Wakati huohuo kulikuwa na najisi ya silaha za nyuklia katika Afrika Kaskazini na ubakaji wa kibaguzi katika Afrika ya kusini. Baadaye Ufaransa iliisaidia Israel kukuza uwezo wake wa nyuklia. Baadaye Israel nayo iliisaidia Afrika Kusini kuanzisha silaha za nyuklia. Lakini matumizi ya silaha za nyuklia katika Afrika Kusini yatasababisha jinamizi la "wazungu wengi wanaondoka".

Ikiwa siasa ya ubaguzi wa rangi haitasaidiwa na silaha za nyuklia, je itasaidiwa na ushirikiano wake na ubepari? Ukweli ni kuwa ushirikiano huo tayari upo katika mvutano mkali. Wakati ubaguzi wa rangi ulipoingilia sana sheria za ugavi na mahitaji, ubepari ulianza kujihisi umesalitiwa. Halikadhalika, wakati uchumi wa kibaguzi unaposhindwa kufanya kazi vizuri, ubepari haujisikii vizuri. Ilitokea wakati wa biashara ya watumwa. Ubepari wakati fulani ulishamiri kwa kutegemea utumwa. Baadaye teknolojia ikawa bora zaidi na hivyo kufanya nguvu kazi ya watumwa kuwa haina maana ukilinganisha na kazi ya ujira. Na hivyo Uingereza, nchi iliyokuwa inaongoza kwa matumizi ya nguvu za watumwa katika karne ya kumi na nane ikawa ndiyo nchi inayoongoza kwa ukomeshaji wa utumwa katika karne ya kumi na tisa. Halikadhalika, ushirikiano kati ya ubepari na siasa ya ubaguzi wa rangi ulikuwa na manufaa ya kiuchumi. Sasa ubepari unaweza kushamiri kwa kuondolewa siasa ya ubaguzi wa rangi.

Kwanza kabisa, uwezo wa watu weusi wa kununua vitu sasa unaweza kupanuka sana pakiwepo utaratibu mzuri wa uchumi. Pili, ujuzi wa watu weusi umefikia viwango vipya na unaweza kufanya nguvu za uzalishaji ziwe na ufanisi zaidi. Tatu, elimu na mfumo mzuri wa mafunzo kwa weusi unaweza kufanya mageuzi ya haraka nchini Afrika Kusini na kuifanya nchi tajiri na yenye viwanda vikubwa.

Nne, upinzani kwa siasa ya ubaguzi wa rangi unasababisha nchi kuyumba jambo ambalo si zuri kwa ubepari. Tano, kuyumba huko kunasababisha kutokuwa na uhakika wa mambo ya baadaye - uwekezaji wa kibepari ni aina ya upangaji wa kiuchumi, wenye kuhitaji kiasi fulani cha uhakika kuhusu hali ya baadaye.

Pia kuna ukweli kuwa uonevu unaozidi kuongezeka nchini Afrika Kusini haukubaliki sehemu muhimu kwa maoni ya umma katika ulimwengu wa magharibi - na hivi vikundi vilivyokasirishwa na siasa hiyo vimeanza kushinikiza viwanda makampuni yanayomiliki maduka. Ubepari lazima ulinde maslahi yake katika hali hii ya mabadiliko.

Kwa hali yo yote, ushindi dhidi ya siasa za ubaguzi wa rangi siyo lazima uwe ushindi dhidi ya ubepari. Kuna kiwango cha maendeleo ya kibepari ambacho kikifikiwa kinafanya ubepari usiweze kubadilika. Karl Marx alifikiria kuwa ubepari ni ngazi ya maendeleo iliyo chini ya ujamaa ambapo maendeleo ya kibepari yakifikia kilele chake, matokeo yake ni kuwa na mapinduzi ya kijamaa. Lakini historia ya hivi karibuni imetuonyesha kuwa kuna hatua katika maendeleo ya kibepari ambayo ikifikiwa mapinduzi ya kikomunisti takribani hayawezi kutokea. Marekani na nchi nyingi za Ulaya Magharibi zimefikia kiwango hicho.

Lakini ni jambo gani litakalofanya mapinduzi ya kikomunisti yasiwezekane katika nchi za kibepari zenye maendeleo ya juu ya viwanda? Ubashiri wa Karl Marx juu ya kuongezeka kwa tabaka la wafanyakazi bado haujatokea katika nchi za kibepari zinazoongoza. Kilichotokea ni kuongezeka kwa mabwanyenye. Ubashiri wa Marx kuhusu kuongezeka kwa dhiki haujatokea. Wafanyakazi wa magharibi wana mengi zaidi ya kupoteza kuliko "minyororo" yao. Urazini wa matabaka haukujitokeza zaidi ya ule wa kitaifa. Marx alidunisha uwezo wa ubepari kushirikisha, kubadili na kurubuni wengine ili waungane nao. Ubepari ulioshamiri unaweza kufanya hayo yote.

Lakini hata kama nchi ya Afrika Kusini haijafikia hatua ya kutoweza kubadili ubepari, inaonyesha kuwa chini ya utawala wa weusi, Afrika kusini inayo nafasi nzuri ya kuendelea na mfumo wa kibepari kwa vile masharti muhimu kwa mapinduzi ya kijamaa bado hayajafikiwa.

Kuhusu bomu la atomi, hilo litakuwa ni sehemu ya urithi ambao watu weusi wa Afrika Kusini watarithi. Kwa hiyo, kutakuwa na taifa la kwanza la watu weusi lenye kumiliki nguvu za nyuklia mwishoni mwa karne ya ishirini. Ufalme wa kisiasa nchini Afrika Kusini utakuwa na "nyongeza nyingi" kuliko mahali pengine po pote katika Afrika. Vitu kama viwanda vya hali ya juu vilivyojengwa kwa jasho la weusi na teknolojia ya magharibi, maliasili ya madini, nidhamu itokanayo na mapambano ya muda mrefu ya kudai haki, na sifa mpya ya kuwa na nyuklia,

vyote hivyo vitaimarisha maana ya ufalme wa kisiasa wa Afrika Kusini chini ya utawala wa walio wengi kabla ya mwisho wa karne hii.

Hata hivyo ni mpaka utajiri wote wa Afrika utakapodhibitiwa na utawala wa kweli wa Afrika - kutoka Cape hadi Kairo, kutoka Dar es Salaam hadi Dakar - ndipo tutaweza kutathmini waziwazi usemi usiosahaulika wa Kwame Nkrumah kuwa *"utafute kwanza ufalme wa kisiasa, na vingine vyote utaongezewa."*

[1] Kuhusiana na harakati za uhuru za Moroko, tazama A. al-Fasi, 1954; A. Ayache, 1956, D.E. Ashford, 1961; J.L. Miege, 1950; na J. Waterburg, 1970 na 1975

# 6 Afrika ya Kaskazini na Pembe

Mwishoni mwa Vita vya Dunia vya Pili, nchi zote za eneo hili zilikwishawekwa chini ya udhibiti wa kisiasa na wa kijeshi wa mataifa ya kigeni. Makoloni ya Kitaliana, Somalia, Eritrea na Libya zilikwishatekwa na washirika na hivyo yakajikuta chini ya mamlaka ya Waingereza na Wafaransa.

## Maghreb

Ingawa mamlaka ya Ufaransa yalidhoofishwa baada ya ushinde wake mwaka 1940, lakini ilitwaa tena na hata kuimarisha mashiko yake katika nchi tatu za Maghreb ilizokuwa ikizidhibiti. Tabia hii ya ukaidi ndiyo iliyosababisha vita vya kikoloni katika Indochina ya Kifaransa (sasa Viet Nam). Licha ya mabadiliko yaliyofanywa ndani ya Maghreb, hali ya ukoloni ya utegemezi, unyonyaji na ukosefu wa uhuru wa kisiasa haikubadilika.

## Moroko

Kunako Aprili 1947, Sultani Mohamed bin Yusufu (baadaye Mfalme Mohamed V)[1] alilipatia vuguvugu la kizalendo la Moroko msukumo mpya katika hotuba aliyoitoa mjini Tangier. Kuanzia wakati huo akawa kitovu, na kiongozi katika harakati za kutafuta uhuru. Kati ya 1947 na 1952 lilifuata wimbi la maandamano na migomo dhidi ya ukoloni.

Kunako Oktoba 1950, Sultani aliiomba serikali ya Kifaransa itoe ruhusa ya kujitegemea kisiasa na kiuchumi na kupanua haki za kikatiba na kisiasa za serikali

[1] Kuhusiana na harakati za uhuru za Moroko, tazama A. al-Fasi, 1954; A. Ayache, 1956, D.E. Ashford, 1961; J.L. Miege, 1950; na J. Waterburg, 1970 na 1975

ya Sharif. Wafaransa walipokataa, madola sita huru ya Kiarabu yaliuomba Umoja wa Mataifa kuhudhurisha suala la uhuru wa Moroko likajadiliwe, lakini ombi lao lilikataliwa kila mara. Kwa kutambua dhima kuu ya Sultani, Wafaransa walimwondoa madarakani mwaka 1953, lakini baada ya kufukuziwa Korsica na baadaye Malagasi nchi yote ikaanzisha mapambano dhidi ya vikundi kama kile cha chama cha wakoloni.

Mapambano ya kitaifa yalichukua mikondo anuwai: Istiklal *Organisation secrete* au hilali nyeusi *Black Crescent* viliundwa, migomo na maandamano ya mitaani ikaongezeka na bidhaa za Ufaransa kususiwa. Katika Rif na Atlas ya Kati; Jeshi la Ukombozi lililoundwa na Waberiberi wa mashambani, lilishambulia bandari na makambi ya kijeshi ya Wafaransa.

Hadi 1955 ongezeko la vurugu liliilazimisha serikali ya Kifaransa kuangalia upya sera yake kuhusu Moroko. Wakati huo huo, vita katika Algeria na ushinde wa karibuni katika Vietnam vikaonyesha kutingwa kwa jeshi la Kifaransa kuhimili harakati za mapana za umma. Kunako Agosti 1955 mazungumzo ya kwanza na wawakilishi mbalimbali wa makundi ya kisiasa ya Moroko yalianzishwa na hatua kuchukuliwa kumrudisha Sultani. Tarehe 26 Novemba 1955 alirudi kwa ushindi nchini kwake. Sidi Bekkai aliunda serikali ya kwanza huru ya Moroko na tarehe 2 Machi 1956, Uhuru wa Moroko ukatangazwa. Mwezi Aprili, na halafu Julai ya mwaka huohuo, nchi lindwa za Hispania za ukanda wa kaskazini na kisha ukanda wa kimataifa wa Tangier ziliingizwa katika ufalme wa Moroko. Hivyo sehemu zote za Moroko kama ilivyokuwa kabla ya ukoloni, isipokuwa vijisiwa vya Kihispania vya Ifri, Mellila na Seuta, ziliunganishwa tena, (Ifri ilijumuishwa katika 1968).

## Tunisia

Kulikuwa na namna ya kufanana kati ya mapambano ya ukombozi wa Moroko na Tunisia: nchi zote mbili zilipambanishwa na mkoloni yuleyule, zilikuwa na jumuiya yenye ushawishi wa Kifaransa, na ziliathiriwa na hali ya kimataifa.[2] Lakini katika Tunisia, tafauti na Moroko, kulikuwa na kushiriki mapema kwa vyama vya wafanyakazi, mgawanyiko mkali katika chama cha Destur-Mamboleo kati ya Habib Bourguiba na Salah bin Yusuf, na utuvu wa kiasi wa *bey*, mkuu rasmi wa dola.

Baada ya kuanzishwa Umoja wa Kitaifa wa Tunisia mwezi Agosti 1947, Watunisia walidai uboreshaji wa viwango vya maisha na kudai uhuru wa kisiasa.

[2] Tazama H. Bourguiba, 1954; D.L. Ling,

Mwaka 1949 uongozi wa Destur-Mamboleo ulifafanua mkakati wa mapambano ya uhuru. Ingawa Watunisia wote walitaka uhuru kamili, Bourguiba alikuwa tayari kufanya suluhu za kimkakati ili kuweza kupata lengo lake hatua kwa hatua. Mwezi Agosti 1950, Wafaransa walikubaliwa uhuru kiasi wa ndani, na serikali mpya, yenye idadi sawa ya mawaziri wa Kifaransa na Kitunisia, iliundwa. Mara Destur-Mamboleo kikapandisha madai yake na katika 1951, kutokana na shinikizo la walowezi wa Kifaransa, Ufaransa ilikataa madai ya kuwa na Bunge la Watunisia tu. Mwanzoni mwa 1952, Ufaransa ilisitisha mazungumzo na Wazalendo wa Tunisia, ikapiga marufuku mkutano wa chama cha Destur-Mamboleo na kuwatia mbaroni viongozi wote wawili, yaani Bourguiba, aliyekuwa na msimamo mkali, na Chenik, aliyekuwa na msimamo wa wastani, pamoja na wengi wengineo.

Licha ya kukolezwa ukandamizaji wa Kifaransa, migomo na maandamano yaliendelea, na mwanzoni mwa 1954 hali ya kutoridhika ilienea kwenye maeneo ya vijijini. Kwa mara ya kwanza, wakulima walijiunga katika makundi yenye silaha, *fellaghas,* ili kuwashambulia wakoloni wa Kizungu, kuvuruga mawasiliano na kupigana na vikosi vidogovidogo vya Kifaransa. Operesheni za jumla za Polisi na jeshi za kuzima maasi hayo zilishindwa kusiyatisha.

Kufuatia ushinde wa Wafaransa katika Dien Bien Phu (7 Mei 1954), ulitokea mgogoro wa kiserikali huko Paris uliozua serikali ya Mendes-France. Bourguiba na wengine waliachiwa na mazungumzo kuanzishwa tena. Walihitimisha katika Juni 1955 ambapo Tunisia ilijipatia madaraka ya ndani kwa masharti ya kuahidi kulinda maslahi ya Wafaransa na kuendeleza uhusiano wa karibu na Ufaransa. Ufaransa iliendelea kudhibiti sera ya nje, ulinzi na usalama wa ndani. Ingawa mapatano haya yalikubaliwa na Bourguiba na wanachama wengi wa chama cha Destur-Mamboleo, kundi la mrengo wa kushoto likiongozwa na Salah bin Yusufu lilihanikiza kuendelea na mapambano ya silaha kama njia ya kuilazimisha Ufaransa kutambua haja ya kutoa uhuru kamili kwa Tunisia. Mwezi Novemba 1955, Salah bin Yusuf alitimuliwa kwenye chama ambacho tangu hapo na kuendelea, kilifuata sera ya wastani.

Kishindo cha matukio katika Moroko, na hasahasa zaidi katika Algeria, kilisukuma Ufaransa kukubali majadiliano mapya na tarehe 20 Machi 1956, Paris ilitia sahihi hati ya kutambua mamlaka kamili ya Tunisia.



Picha 6.1 *Mkutano wa Destur-Mamboleo, Novemba 1955, katikati ni Bourguiba*

## Vita vya Algeria[3]

Marefu na machungu ya vita hivi yalisababishwa na azma ya kikaidi ya Wafaransa kung'angania nchi hii na dhamira ya wananchi wa Algeria ya kupata uhuru. Ingawa muafaka ulikwishafikiwa na serikali ya Ufaransa huko Tunisia na Moroko, sera ya aina hiyo haikukubalika asilani kwa Algeria. Imani potofu kuhusu "Algeria ya Wafaransa" ilitokana na kuwako kwa walowezi wa Kifaransa karibu milioni moja (waliojulikana kama *pieds-noirs*, miguu myeusi), uwekezaji mkubwa katika kilimo na migodi, na athari ya utetezi wa Algeria katika siasa za Wafaransa. Jambo la ziada lilikuwa ugunduzi wa mafuta na gesi katika Sahara mwenye miaka ya 1950.

Mwaka 1954, Wazungu walishikilia asilimia 23 ya ardhi ya kilimo ndani ya maeneo yenye kusheheni rutuba. Baina ya 1936 na 1954 idadi ya Waalgeria Waislamu ilipanda kutoka milioni 6.3 hadi milioni 8.7, ambapo idadi ya Wazungu ilipanda kutoka 940,000 hadi milioni moja. Kipato cha mwaka cha Mualgeria mwajiriwa katika kilimo kilikuwa cha wastani wa faranga za zamani 22,000, ikilinganishwa na faranga za zamani 260,000 kwa Mzungu. Mashambani kulikuwa na karibu watu milioni moja wasiokuwa na kazi, na kusababisha kuhamia mijini au Ufaransa: mwaka 1957 kulikuwa na Waalgeria karibu 300,000 wenye kufanya kazi Ufaransa.

Baraza la Algeria lilikuwa na wajumbe 120, nusu yao Wafaransa, nusu nyingine Waalgeria Waislamu, lakini utiifu wa Waislamu hawa kwa mabavu ya kikoloni ulimaanisha kuwa majadiliano yote kuhusu mambo yote muhimu kitaifa yaliepukwa. Kwa jumla hata madai ya wastani kabisa ya usawa wa kiraia na wa kisiasa yalikandamizwa na kuzimwa.

Vyama vikuu viwili vya kitaifa viliendelea na sera yao ya kujadiliana, ambapo *Union democratique du manifeste algerien* (UDMA), kilichoongozwa na Ferhat Abbas, kilijaribu kuwashawishi Wafaransa kukubali Jamhuri ya Algeria huru lakini yenye kushirikishwa (na Ufaransa). Kwa upande wa *the mouvement pour le triomphedes libertes democraliques* (MTLD), kilichoongozwa na Messali Haji, utambuzi wa mamlaka ya Algeria lilikuwa ndilo sharti kuu. Kushindikana kwa sera hizi kulisababisha vyama hivi kutoungwa mkono na tabaka la wenye hali bora waishio mjini, na tabaka la wafanyakazi pia.

[3] Kazi muhimu zaidi kuhusiana na mada hii ni F. Abbas, 1962; A. Nouschi, 1962; M. Lacheraf, 1063, G.C. Gordon, 1966; Y. Courriere, 1968-72; J.C.L. Vatin, 1974; C.R. Ageron, 1979; M. Kaddache, n.d A.K. Saadallah, 1981



*Picha 6.2 Ferhat Abbas akihutubia umma huko Kasablanca, 9 Julai 1961 mbele ya Mfalme*

Mwaka 1953-1954, MTDL liligawanyika katika makundi matatu: "Wamessali," waliomuunga mkono bila sharti lolote kiongozi wa zamani (aliyehamishiwa Ufaransa mwaka 1952), "Wanakati" na *Comite revolutionnaire d'unite et d'action* (CRUA) waliohubiri maasi na mapinduzi. Tarehe 1 Novemba 1954, "machifu wa kihistoria" tisa wa mapinduzi ya Algeria waliamua kuanza maasi ya silaha. Kwa makusudi haya nchi nzima iligawiwa katika wilaya tano za kijeshi, kila moja ikiwa chini ya amiri jeshi.

Jeshi la *Armee de la liberation nationale (ALN)* likianza na watu kati ya elfu mbili na elfu tatu, liliongoza mashambulio ya kwanza katika Milima ya Aures na Kabylie kabla ya kusambaa nchini kote kufikia kiangazi cha 1955. Kwanza, ALN liliundwa na wakulima lakini baadaye likaungwa mkono na wanachama wa tabaka za mjini baada ya kudhihirika kuwa malipizo ya Wafaransa yalielekezwa kwa Waalgeria Waislamu wote bila kuchagua.

Ingawa Wafaransa waliongeza vikosi vyao vya kijeshi toka wanajeshi 56,000 hadi 500,000 mwaka 1960, hawakuweza kuzima nia ya Waalgeria ya kutaka uhuru. Mapambano ya silaha yaliamsha uzalendo wao na kuwageuza maaskari shupavu ambao walikuwa wakifisha njozi ya Wafaransa ya kutokuwapo kwa taifa la Algeria. Katika upeo wa mapigano ALN kilikuwa na wanachama kama 130,000 katika makundi ya msituni.

Tangu Mei 1955, *Front de liberation nationale* (FLN) kilikuwa chombo cha juu kabisa cha kisiasa cha watu wa Algeria. Vyama vya siasa na vikundi vilivyo vingi vilivunjwa kwa ufanisi na kuingizwa katika FLN isipokuwa Messali Haji aliyeanzisha chama chake na kushirikiana na Ufaransa kwa mafanikio. Tangu 1956 na kuendelea Chama cha Kikomunisti cha Algeria kilishirikiana na ALN.

Kunako Agosti 1956, kwenye mkutano wa kwanza wa FLN, msimamao mkali ulitangazwa: Uarabu na Uislamu wa taifa la Algeria ulithibitishwa tena pamoja na haki yake kamili ya kujitawala. Tatizo la Algeria likatwaa sura ya kimataifa na kuungwa mkono, ndani ya Umoja wa Mataifa, na nchi za Kiarabu, Kiasia na Kijamaa na kupata misaada ya kifedha na kijeshi kutoka tawala za Kiarabu zenye kupenda maendeleo.

Nchini Ufaransa, mawazo yaligawanyika kati ya wale waliotaka kumaliza vita hivi vipya na makundi ya mrengo wa kulia walioitaka vita vishadidishwe. Serikali dhaifu za Jamhuri ya Nne (nchini Ufaransa) ziliwapa madaraka makubwa mno majenerali waliokuwa wakiongoza vita. Mkakati uliotumiwa na majeshi ya Kifaransa ulikuwa ni kuzingira vijiji vyote ili kuvuruga mtandao wa wasaidizi wa FLN, mbinu ya kisaikolojia ya kukitenga FLN na watu, na kujenga uzio wa umeme kwenye mipaka ya Tunisia na Moroko ili kuzuia vifaa kuingizwa.

Ingawa uzingiraji huu uliwatenganisha mamilioni ya wakulima na nchi yao, utawala wa vitisho ulifikia kilele chake mwaka 1957 kwenye vita vya Algiers, ambapo mateso, vifungo, na adhabu viliivunja ALN mjini na kuanzisha wimbi la upinzani katika Ufaransa na duniani kote. Mwaka huohuo, mpaka wa Algeria - Tunisia ulizibwa na uzio wa umeme. Hata hivyo, hakuna hata moja ya hatua hizi iliyoweza kusitisha upinzani wa silaha hadi siku ya mwisho.

Vita vya Algeria ilisababisha mgogoro wa kisiasa katika Ufaransa ulioishia kumwingiza de Gaulle madarakani mwezi Mei 1958. De Gaulle, aliyeungwa mkono na utawala wa wachache wa Kifaransa na walowezi wa Kifaransa katika Algeria, alikuwa na malengo yaliyokaribiana na yale ya kundi dogo la wamiliki mitaji ya fedha na viwanda wa Kifaransa. Mpango wa Konstantini wa 1958 ulikuwa jaribio la mwisho la kuirudisha Algeria mikononi mwa Ufaransa. Mradi ulipendekeza mageuzi ya kilimo na ya viwanda nchini humo, lakini ungekuwa na manufaa machache tu kwa Waalgeria.

Kwa kuitikia mageuzi yaliyotokea Ufaransa, mwezi Septemba 1958 FLN ikajitangaza kuwa serikali iliyoko uhamishoni, yaani GPRA (*Gouvernement provisoire de la Republique algerienne*), ambayo kiongozi wake wa kwanza alikuwa Ferhat Abbas. Mwaka 1961 uongozi wa serikali hiyo ulichukuliwa na Yusuf Ben Khedda, ambaye alikuwa na siasa kali zaidi.



*Picha 6.3 Septemba 20, 1959, Messah Haji aliidhinisha azimio la Generali Charles de Gaulle kuhusu Algeria*

Huku ikikabiliwa na kushindwa kwa operesheni za kijeshi na mpango wa Konstantini, serikali ya de Gaulle ikaamua kujadiliana, jambo ambalo lilizusha uasi wa kifashisti katika Algiers mnamo Januari 1960 wakati wa "juma la vizuizi." Kunako Machi, de Gaulle alizima njozi ya kuwepo kwa Algeria ya Wafaransa kwa kutumia wito wa *Algérie Algérienne* (Algeria ya Waalgeria) na majadiliano yakaanza katikati ya mwaka huo.

Njama ya Majenerali, ya Aprili 1961 ikiongozwa na majenerali wanne wa vyeo vya juu, ilikuwa ni utapatapaji wa mwisho wa "mashabiki" wa Algeria ya Kifaransa kabla ya kuunda kikosi cha mapambano ya kudumu chini ya *Organisation armee secrete* (OAS)..

Kushikilia kwa Ufaransa kwamba Sahara na utajiri wake wa mafuta itengwe kutoka jimbo la Algeria kikawa kikwazo kikubwa katika majadiliano. Hata hivyo, mwaka 1962 makubaliano ya Evian, yenye kutangaza kuwa hatima ya Algeria iamuliwe kwa kura ya maoni, yalitiwa sahihi, na tarehe 1 Julai 1962 matokeo yakawa kura asilimia 99.7 zilichagua uhuru.

Kufuatia matokeo hayo, matendo ya vurugu ya OAS yaliua fursa zote za Wazungu wachache kubakia ndani ya Algeria huru kama ilivyotajwa ndani ya

makubaliano ya Evian. Hivyo kufikia mwisho wa mwaka chini ya asilimia 20 ya Wazungu ndio waliobakia.

Gharama ya ukombozi huu uliokomesha kipindi cha ukoloni katika Maghreb ilikuwa nzito: karibu Waalgeria milioni moja walikufa, milioni nyingine mbili walihamishwa makazi na majumba elfu kumi yaliteketezwa. Vita vya Algeria hatimaye viliilazimisha Ufaransa kutambua haki ya kila taifa kujitawala.

## Libya[4]

Mwaka 1948 Libya ilikuwa chini ya mamlaka ya kijeshi ikingojea uamuzi wa Umoja wa Mataifa (UNO) kuhusu hali yake ya baadaye. Baada ya Uingereza na Ufaransa, sasa ilikuwa ni zamu ya Marekani kuja na kujenga kituo cha ndege za kivita karibu na Tripoli. Punde si punde, maslahi ya mibabe mitatu ya Magbaribi yalikwaana na matakwa ya watu wa Libya na sera ya Waarabu, Waasia na nchi za Kisoshalisti. Waingereza walileta mpango wa Bevin-Sforza wakipendekeza udhamini wa Uingereza katika Sirenaika, Wataliana katika Tripolitania na Wafaransa katika Fezzan. Badala ya kuigawa nchi katika sehemu tatu, Jamhuri ya Kisovieti ya Kisoshalisti (Urusi) ilipendekeza udhamini wa pamoja wa kimataifa chini ya UNO, Walibya, kwa upande wao, walionyesha upinzani wao kwa maandamano makubwa katika Tripoli. Mwezi Mei 1949 Umoja wa Mataifa ulikataa mpango wa Uingereza na mwezi Novemba, Urusi ilipendekeza uhuru wa mara moja kwa Libya. Pendekezo hilo lilikataliwa na Umoja wa Mataifa ambao ulipiga kura kuwa Libya itambuliwe kama dola huru lenye mamlaka kabla ya tarehe 1 Januari 1952.

Uhuru wa Libya, haukuwa zawadi kutoka Umoja wa Mataifa, bali ulikuwa ni matokeo ya mapambano magumu dhidi ya ukoloni yaliyoamsha maoni ya dunia. Waingereza walimpendelea mkuu wa madhehebu ya Sanusiyya, Mohammad Idris, ambaye tabia zake za kushikilia ukale zilizusha upinzani miongoni mwa mabwenyenye wazalendo wa Tripoli. Kwa upande wake, Idris alishuku mawazo ya kijamhuri ya mabwenyenye wa Kiliberali wa Tripoli.

Suitafahamu hii ilitumiwa na Uingereza kuanzishia majadiliano, hata hivyo, mwezi Juni 1949 Sirenaika ilitangazwa kuwa nchi huru. Katiba ilimpa Emir Idris karibu madaraka yasiyokuwa na mpaka na migomo na maandamano vikazimwa vikali kwa msaada wa majeshi ya Kiingereza.

[4] Kuhusiana na Historia ya Libya kabla ya mapinduzi, Tazama E.E. Evans Pritchard, 1949; I.R. Khalidi, 1956; M. Khadduri, J. Norman, 1963; N.I. Proshin, 1975

Licha ya tabia ya kupinga maendeleo ya utawala wa Idris, ilidhihirika wazi kuwa uhuru kamili wa Libya unaweza kupatikana tu kupitia muungano chini ya himaya yake. Baada ya majadiliano marefu suhulu ilikubaliwa na Libya ikawa shirikisho la majimbo matatu - Tripolitania, Sirenaika na Fezzan - yote yenye kujitegemea kabisa, chini ya serikali kuu dhaifu sana. Tarehe 24 Desemba 1951, Ufalme wa Libya ukawa huru na **emir** wa zamani wa Sirenaika akawa mtawala wa kwanza.

Libya ilipata uhuru ikiwa na athari kubwa ya kikoloni; zaidi ya hayo ilikuwa imeathiriwa vibaya na vita na tayari ilikwisha kuwa miongoni mwa nchi zilizoachwa nyuma kimaendeleo za Afrika ya Kaskazini; katika kilimo, mahusiano ya kikabaila yalitawala, idadi kubwa ya wenyeji bado waliendesha maisha ya Kinomadi au ya Kinomadinomadi, asilimia 85 ya watu hawakujua kusoma wala kuandika, viwanda vilikuwa karibu hakuna, na mabenki mengi, maduka ya jumla na mashamba yalikuwa mikononi mwa wageni wasio kuwa Walibya.

Mwaka 1952 vyama vyote vya siasa vilipigwa marufuku na mashirika mengine kudhibitiwa barabara. Madola ya Magharibi yalitumia matatizo ya dola hili jipya kuingia nalo mikataba ya misaada ambayo ilisababisha utegemezi mpya. Vituo vya kijeshi vya Marekani, Uingereza na Ufaransa vilidumishwa; kiasi cha mtaji wa nje katika uchumi wa Libya kilikuwa asilimia 75 na maslahi ya walowezi wa Kitaliana yalilindwa.

Kati ya 1953 na 1956 Libya ilitoa tahafifu kwa uchimbaji wa mafuta kwa makampuni mbalimbali ya Kimarekani, Kiingereza, Kifaransa na Kitaliana. Uchimbaji wa kibiashara ulianza mwaka 1960, na uzalishaji ukaongezeka haraka sana, lakini kushamiri kwa utoaji wa mafuta hakukuwa na matokeo mazuri. Libya, kwa upande mmoja, ikawa moja ya nchi tajiri kabisa katika Afrika, lakini kwa upande mwingine, uchumi, uliojikita kwenye zao moja ulitegemea mabadiliko ya soko la dunia. Zaidi ya hayo, ingawa uchimbaji wa mafuta uliwapatia Walibya kazi nyingi, lakini kazi hizo hazikuwa za kitaalamu, zilifanywa na wahamiaji kutoka nchi nyingine za Kiarabu. Kushamiri kwa uchumi kulifuatwa na mfumko wa bei uliokuwa pigo hasa kwa matabaka ya watu maskini zaidi. Matumizi ya serikali yenye kuongezeka kwenye huduma za jamii na elimu hayakutosheleza na hapakuwa na uwekezaji katika viwanda wala kilimo.

Mwaka 1963 muundo wa shirikisho uliondoshwa lakini urafiki wa karibu na madola ya Magharibi uliendelea. Usiri wa utawala wakati wa vita vya 1967 ulizua malalamiko yaliyoonyesha athari yenye kukua ya utaifa wa Waarabu miongoni mwa mabwenyenye wa Kilibya na wasomi. Hapakuwa na chama cha wananchi hata kimoja kilichoweza kuipindua serikali, hivyo basi kazi hiyo ikawaangukia kundi

la maofisa wa kijeshi likiongozwa na Kapteni Muammar Kadhaffi kupindua na kutwaa madaraka tarehe 1 Septemba 1969. Ukisukumwa na mawazo ya umoja wa Waarabu, Ujamaa wa Kiarabu na Uislamu, uongozi mpya ulizindua mapinduzi ambayo yalikuja kubadilisha vipengee vyote vya maisha ya Libya.

## Misri

Baada ya kuvunjika kwa mazungumzo kati ya Waingereza na Wamisri kunako Januari 1947, Misri iliamua kupeleka suala la mahusiano yake na Uingereza kwenye Umoja wa Mataifa. Baada ya vikao kadhaa vya Baraza la Usalama, suala la Misri liliahirishwa kwa muda usiojulikana.

Wakati huu tatizo la Palestina lilijitokeza kwenye medani ya kimatifa kwa mara ya kwanza. Tatizo lilikuwa la Palestina kufanywa koloni la watu wenye asili ya Kizungu waliodhamiria kupafanya makazi yao ya kudumu kwa kisingizio kwamba miaka 2000 iliyopita Palestina ilikuwa miliki ya babu zao. Bila kuungwa mkono na Uingereza na Marekani, hapana shaka kuwa wazo la Wayahudi la kuunda dola la Israel lisingeweza kutekelezwa.[5]

Kushindwa kwa Umoja wa Waarabu (Misri, Jordan, Syria, Iraq na Lebanon) kuingilia kijeshi mwishoni mwa mwaka wa 1948 kwa niaba ya Wapalestina kulielezwa kuwa kulitokana na mgogoro ndani ya mfumo wa madaraka ya kisiasa katika dunia ya Waarabu. Hususani; jeshi na wanajeshi wake wa vyeo vya chini ndio waliotambua kwanza kushindwa na uzembe wa serikali zilizokuwepo. Miongoni mwa jamii iliyobaki, ushinde ulishadidisha mapambano ya kudai uhuru kamili usiodhibitiwa na nchi za nje.

Katika uchaguzi wa Misri wa 1950, chama cha Wafd kilitwaa madaraka tena, lakini hakikuweza kutatua mgogoro wa kiuchumi au kuleta utulivu kwa jumla.[6] Ikikabiliwa na wimbi la maandamano na migomo, serikali ilianza majadiliano mapya na Uingereza. Uingereza ilipoonyesha kutokubali, bunge la Misri lilitangua peke yake mkataba wa 1936 na makubaliano ya 1899 juu ya Miliki ya ubia katika Sudan, tarehe 15 Oktoba 1951.

Tarehe 25 Januari 1952, mamia ya maelfu ya Wamisri waliandamana mitaa ya Kairo wakidai ususiaji kamili wa Waingereza, kupeleka jeshi la Misri katika eneo

[5] Kuhusiana na suala la Wapalestina, mgogoro kati ya Waarabu na Waisraeli pamoja na masuala la Kimataifa, zipo taarifa za kutosha; tazama marejeo ya R.M. De Vore, 1977, vitabu vya M. Rodison, 1968a na 1968b.

[6] Tazama M. Colombe, 1951; N. Tomiche, 1966; J. Carque, 1968; P.J. Vatikiotis, 1969; H. Mahmoud, 1970 na 1973

la Mfereji wa Suez, na kukamilisha mkataba wa urafiki na Urusi. Maandamano hayo yaliingiliwa na wachochezi wa Ikulu na kushindikana kudhibitiwa tena, na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mali na kuanguka kwa serikali ya Wafd, na vyama vya siasa na ufalme kupoteza thamani.

"Maofisa Huru," umoja wa maofisa wa ngazi za kati, wakiongozwa na Gamal Abd al - Nasser, wakatokea kuokoa jahazi. Tarehe 23 Julai 1952 walishika vituo muhimu vya mtandao wa Kairo, wakaitwaa madaraka bila kumwaga damu na kumlazimisha Mfalme Farouk, tarehe 26 Julai, kuacha madaraka.

Mapinduzi kwanza yalichukuliwa kama mfano bora wa tukio la kijeshi na ilichukua muda fulani kabla ya welekea wake dhidi ya ukabaila na ubeberu kuonekana. Mageuzi ya kilimo ya kwanza ya mwaka 1952 yaliathiri asilimi 10 tu ya ardhi yenye kulimika lakini yaliashiria hatua ya kwanza katika kudhibiti madaraka ya tabaka la makabaila. Vyama vya siasa vya zamani vilivunjwa kwa kukataa kushirikiana na utawala, na mwezi Juni 1963, Baraza la Juu la Mapinduzi lilifuta ufalme na kuitangaza Misri kuwa jamhuri na Jenerali Naguib kuwa rais wake wa kwanza. Baada ya miaka 2000 ya utawala wa kigeni, kwa mara nyingine tena Misri ilitawaliwa na mkuu wa dola aliyekuwa Mmisiri mzawa.

Ndani ya Baraza la Mapinduzi kundi lililoongozwa na al-Nasser lilitetea sera kali zaidi katika sera za ndani na za nje, ambapo kundi la Naguib lilitaka kurudisha utawala wa kiraia. Sera hii ya kushikilia ukale pia ilisisitiza Uislamu na kuungwa mkono na Udugu wa Waislamu. Mwaka 1954 jaribio la kumwua al-Nasser lililofanywa na mwanachama wa Udugu wa Waislamu lilisababisha kujiuzulu kwa Naguib na Gamal 'Abd al-Nasser akawa mkuu wa dola.

Katika miaka ya mwanzo, sera ya nchi za nje ya Baraza la Mapinduzi ilijikita kwenye mambo mawili: Sudani na Mfereji wa Suez. Mkataba wa Uingereza na Misri uliotiwa sahihi mwezi Februari 1953 ulikuwa ndio mwisho wa Mamlaka ya Pamoja na uliipa Sudani uchaguzi kati ya uhuru au muungano na Misri. Ni mpaka Sudani ilipokataa muungano tu ndipo al-Nasser alipozindua sera kakamavu zaidi ya Kiarabu.

Kunako Oktoba 1954 mkataba ulitiwa sahihi ambao kwao Waingereza walikubali kuondosha majeshi yao kwenye Ukanda wa Mfereji, na kutambua umuhimu wa kimataifa wa Mfereji wa Suez, lakini pia mkataba ukauelezea kuwa ni sehemu ya Misri.

[7] Utawala wa nasaba ya ma-plobmy, ulifuatiwa na utawala wa Warumi, Wabizanti, Waarabu na nasaba kadhaa za Wakurdi, nasaba ya Muhammad 'Ali ilikuwa na asili ya Albania

[8] Tazama E. Lengyel, 1957



PICHA 6.4 Magofu ya Bandari ya Said, kwenye Ukanda wa Mfereji wa Suez, ambayo yanaonyesha athari za vita ya Suez, 1956

dhidi ya makubaliano ya Baghdad yaliyoonekana kuwa jaribio la kuhifadhi athari ya Magharibi katika eneo hilo.[8]

Mwaka 1955 mvutano na Israel uliendelea kuwa mkali. Magharibi iliendeleza mmiminiko wa silaha katika Israel, lakini madai ya Misri ya msaada wa aina hiyo yalipokataliwa, al-Nasser akatangaza mnano Septemba 1955, mauziano ya zana za kijeshi na Chekoslovakia.

Athari ya mara moja ya tukio hili ilikuwa ni kukataa kwa Uingereza, Marekani na Benki ya Dunia kugharimia mradi wa Bwawa la Juu katika Aswan. Jibu la al-Nasser kwa msimamo huu likawa kutangaza tarehe 26 Julai 1956 kuwa Kampuni ya Mfereji wa Suez imetaifishwa na kwamba mapato kutokana na Mfereji

[8] Tazama E. Lengyel, 1957

yangetumika kugharimia bwawa hilo. Uingereza, Ufaransa na Marekani walipinga vikali, lakini mbinu zao mbalimbali za kidiplomasia za kuilazimisha Misri kukana haki zake zilishindikana. Kunako Oktoba, Israel, Uingereza na Ufaransa ziliishambulia Misri kwa nia ya pamoja ya kumpindua al-Nasser na kuifanya Misri kijikoloni tena.

Majeshi ya Israel yalivuka na kuingia Sinai tarehe 24 Oktoba na kuelekea Mfereji wa Suez. Mashambulizi ya anga ya Wafaransa na Waingereza yalianza tarehe 31 Oktoba, ambapo katika Umoja wa Mataifa azimio la Marekani - Urusi la kuitaka Israel kuondoka mara moja lilipingwa kwa kura ya turufu na Uingereza na Ufaransa. Baadaye, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ulitaka mapigano yasimamishwe, lakini ilichukua shinikizo la pamoja la Marekani na Urusi kuilazimisha Uingereza na Ufaransa kuacha uhasama tarehe 6 Novemba.

Kwa Uingereza na Ufaransa, kushindwa huku kwa "diplomasia ya mtutu wa bunduki" kulikuwa na maana ya kupoteza zaidi athari, si katika eneo la Uarabu tu bali pia katika Dunia ya Tatu yote. Kwa upande mwingine, Misri na Rais al-Nasser wakawa ishara ya ukinzani dhidi ya ubeberu.

## Sudan

Historia ya Sudani ya baada ya vita ilinasibishwa na mambo matatu makuu: mapambano ya uhuru, uhusiano na Misri na kuibuka kwa tatizo la kusini.[9]

Licha ya katiba ya 1948 iliyotoa nafasi kwa baraza la kutunga sheria lililochaguliwa kwa kura ya watu wote au baraza la utendaji lenye mawaziri wa Ki-Sudani, gavana-mkuu wa Kiingereza aliachiwa haki ya kura ya turufu na madaraka mengine mengi.

Waingereza walipendelea zaidi Chama cha Umma na misimamo yake dhidi ya Misri na ya ukale, kuliko sera ya Chama cha Ashikka iliyokuwa ya maendeleo zaidi na iliyosisitiza juu ya "Umoja wa Bonde la Nili".

Mapinduzi ya 1952 katika Misri yalipokewa vyema katika Sudani ambako mfalme wake, Farouk, hakuwa anapendwa, na kwa sababu Jenerali Naguib alikuwa na uhusiano wa karibu na nchi hiyo. Kunako Novemba 1953, Chama cha Muungano wa Kitaifa kipya kilichorithi chama cha Ashikka, kilishinda uchanguzi, lakini kupinduliwa kwa Jenerali Naguib na mtazamo hasi wa al-Nasser kwa mfumo wa vyama vingi, vilikuwa na athari mbaya hata miongoni mwa wafuasi wa zamani

9 Tazama J.S.R. Duncan, 1957; P.M. Holt, 1961; Abdu al-Rahman, 1969

wa muungano. Mwezi Desemba, viongozi wa madhehebu ya dini yenye nguvu kabisa walitangaza kuwa walikuwa tayari kushiriki katika mapigano ya kuleta uhuru kamili kwa Sudani. Mwezi Desemba 1955 bunge la Sudani lilitangaza kuwa Sudani ingekuwa Jamhuri huru na tarehe 1 Januari 1956 uhuru ulitangazwa rasmi.

Tangu Agosti 1955 tatizo la Sudani ya kusini lilianza kuleta usumbufu pale Kikosi cha Equatoria cha jeshi la Sudani kilipoasi dhidi ya utwaaji polepole wa utawala na vituo vya kijeshi na watu wa kaskazini. Mgogoro huu ulikuwa matokeo ya sera ya Waingereza ya kuendeleza kusini kwa kuitenganisha na kaskazini. Huko Kusini Waingereza walikataza kueneza Uislamu, wakati huohuo wakihimiza misioni za Kikristo, na katika shule za misioni lugha ya Kiingereza tu ilitumika, ambapo Kaskazini Kiarabu kilikuwa lugha ya kufundishia na baadaye kikawa lugha rasmi.

Hivyo tafauti za kitamaduni na za kijamii kati ya Waislamu wasema Kiarabu wa kaskazini na Waniloti au Wasudani wa Kati wa upande wa kusini wenye kufuata dini za kienyeji zilikuzwa, ingawa, wakati wa awali wa ukoloni kulikuwa na dalili kadha zenye kuashiria kuwa uhusiano kati ya wakaskazini na wa kusini ungeweza kuendelezwa kirafiki.

Wasudani wa kaskazini walilaumiwa kwa kuzorotesha mahusiano kutokana na tabia yao. Walipoanza kutwaa utawala wa majimbo ya kusini, mwaka 1954-1955; hawakuzingatia tofauti za kitamaduni au manung'uniko ya wenyeji na viongozi wao wa kisiasa.

## Pembe ya Afrika

Vita ya ukinzani, halafu Vita Vikuu vya Pili na uvamizi wa Wataliana, vilisababisha zaidi ya vifo 760,000 na hasara ya vifaa ilihesabiwa kufikia pauni milioni 180[10] katika Ethiopia. Baada ya ushindi wa Italia, utawala wa Ethiopia ulibakia kabisa chini ya udhibiti wa Uingereza. Licha ya azimio ndani ya mkataba wa 1942, la uhuru na kujitegemea kwa Ethiopia, maafikiano ya kijeshi yaliyoambatana nalo yalihifadhi na kuhalalisha udhibiti huu: Ogaden Haud na maeneo makubwa yenye kupakana na Somalia ya Kifaransa, Kiingereza na Kitaliana yalipaswa kubakia chini ya utawala wa majeshi ya Kiingereza, kwa muda usiojulikana.

Kunako 1944, mkataba mpya uliwezesha kuachia huru sehemu kubwa ya Ethiopia isipokuwa Ogaden na Eneo la Hifadhi lote ambalo halikupaswa kurudishwa kwenye utawala kamili wa Ethiopia hadi 1954.[11]

[10] R.K. Pankhurst, 1955, uk. 54809
11R.K. Pankhurst, 1981

Chini ya utawala wa kijeshi wa Uingereza, vyama vya siasa vyenye kuakisi hali changamani ya kimbari na ya kidini viliibuka katika Eritrea. Watigre wa Kikristo kutoka Nyanda za Juu walianzisha Chama cha Muungano kilichoungwa mkono na serikali ya Ethiopia (Uhabeshi) na kanisa, ambapo kikundi cha Wakristo wachache kilishikilia Chama cha Maendeleo Huria, kikiwa na nia ya kuunda Eritrea huru. Shirikisho la Waislamu na vyama vyote viwili hivi viliunda Jumuiya ya Uhuru iliyoitwa Jumuiya ya Kidemokrasia.

Mwaka 1950 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimio la kuunda shirikisho kati ya Ethiopia na Eritrea; Eritrea ingekuwa na katiba yake, baraza la kutunga sheria na serikali. Kunako Machi 1952, uchaguzi wa kwanza wa kibunge ulifanywa: vyama vya Kiislamu na vya Kikristo vikafungana. Shirikisho lilikuwa na maana ya ushindi kwa Chama cha Muungano kilichotokeza kuwa chama tawala katika serikali, ambapo viongozi wengi wa Jumuiya ya Uhuru walihama na kuwa wakimbizi.

Hali yenye utata ilijitokeza ambapo, kwa upande mmoja, kulikuwa na Eritrea yenye bunge lililochaguliwa, na vyama vyake na katiba ya kimaendeleo zaidi, na kwa upande mwingine, Uhabeshi, ambako Mfalme Haile Selassie alidhibiti hatamu zote za mamlaka. Aliondosha kwa utaratibu asasi za kidemokrasia moja baada ya nyingine katika Eritrea hadi hatima yake katika 1962, ambapo bunge la Eritrea lilipiga kura kuondosha hadhi ya shirikisho na halafu kujivunja lenyewe. Eritrea ikawa sehemu kamili ya himaya ya Ethiopia na viongozi wa upinzani makimbizini na vikundi vya msituni, vikaanza mapigano dhidi ya utawala na majenshi ya Ethiopia.

Waingereza waliposhindwa katika jaribio lao la kuunda upya udhibiti wa Kiingereza wa Afrika ya Mashariki ya Kitaliana ya awali, walipendekeza mwungano wa nchi zote za Somalia. Kama ilivyotarajiwa, mpango ulishindikana kutokana na upinzani wa Ethiopia na Ufaransa. Hata hivyo, ni katika kipindi hiki cha muungano wa muda wa Wasomali chini ya utawala wa Kiingereza ambapo vuguvugu la Umoja wa Wasomali liliibuka miongoni mwa vijana wasomi.

Katika mkataba wa amani wa 1947 Italia ilikana miliki ya makoloni yake, lakini ikataka, kama katika Tripolitania, kupewa angalau udhamini wa Somalia. Kunako 1948-1949, suala hili lilipojadiliwa katika Umoja wa Mataifa, wimbi la maandamano ya wananchi liliibuka Mogadishu na mahala pengine dhidi ya kurudi kwa Wataliana. Maandamano haya yaliungwa mkono na wanawake walioandaliwa na Umoja wa Vijana wa Somalia (SYL). Licha ya haya, nchi kubwa tatu za Magharibi zilipendelea udhamini chini ya Italia ingawa Urusi iliunga udhibiti wa pamoja wa nchi kubwa nne. Kunako Novemba 1949, Somalia iliwekwa chini ya

udhamini wa Kitaliana kwa miaka kumi chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa.

Katika Nchi ya Somalia yenye kudhaminiwa na Waingereza hapakuwa na uwakilishi wa vyama vya siasa, baraza la kutunga sheria liliundwa mwaka wa 1957 na madaraka yake yalibanwa sana hadi 1960. Kunako 1954, mkataba uliohamishia Ethiopia sehemu zilizokaliwa na Wasomali za Haud na Eneo la Hifadhi uliwasha msisimko mpya wa kizalendo. Maandamano makubwa yalitokea, mjumuiko wa kitaifa ulioitwa Chama cha Muungano wa Kitaifa uliundwa ili kuanzisha kampeni ya kuikomboa Haud na kutwaa uhuru. Uhuru na kuungana na Somalia vikawa ndiyo malengo ya vyama vyote. Kunako 1959 baraza la kutunga sheria liliundwa upya likiwa na uwakilishi mwingi zaidi wa Wasomali. Matukio yalichochewa na kukaribia kwa tarehe ya uhuru wa Somalia, 1 Julai 1960, na uunganishwaji na Somalia. Tarehe 26 Juni 1960, siku tano kabla ya Somalia, Somalia ya Kiingereza ilipata uhuru kamili na nchi zote mbili zikaungana kama ilivyokubaliwa hapo awali.

Koloni dogo la Kifaransa lililoitwa *Cote Francaise des Somalis* hadi 1967, na baadaye *Territoire Francais des Afars et des Issas* (TFAI) liliwakilisha eneo muhimu kimkakati kwa Ufaransa, pakiwa na bandari iliyojengwa mahali pazuri sana, na mwanzo wa reli pekee ya Ethiopia.[12] Ufaransa, kwa hiyo, ilipinga madai ya uhuru na kuwako kwa mbari mbili zinazotafautiana lakini zenye idadi sawa kuliupatia utawala wa kikoloni kisingizio cha kuahirisha suala hilo kwa muda usiojulikana.[13]

Uhasama kati ya makundi mawili ulikuzwa na utawala uliowapendelea Wanomadi wa Afar dhidi ya Wasomali, ingawa kabla ya 1958 hapakuwa na tofauti za kisiasa kati ya mbari hizi mbili. Viongozi wote wawili, Mahmud Harbi na Hassan Gouled walikuwa wa asili ya Wasomali wa Issa, lakini wa kwanza aliunga mkono muungano na Somalia huru na wa pili alitaka umoja wa karibu na Ufaransa. Harbi alipokuwa makamu wa raisi kwenye Baraza la Mawaziri, mwelekeo wake wa Umoja wa Wasomali haukuchelewa kumlazimisha kukimbilia ng'ambo. Kura ya maoni ya de Gaulle ya 1958 ilithibitisha kubakia kwenye jumuiya ya Ufaransa kwa *Cote Francaise de Somalis* na ilichukua miaka ishirini kabla ya chama cha TFAI kupata uhuru.

[12] Tazama V. Thomposon na R. Adloff, 1968; P. Oberle, 1971' na R. Saint - Veran, 1977

[13] Angalia maoni ya gazeti la *Le Monde* (26 Aprili, 1964) kuwa "utawala una mawazo yaliyo na msingi, kuwa ushindani kati ya wa Afar na Wasomali ndio hakikisho bora la utangamano" imedondolewa katika *Politika Frantisei* v Aziii I v Afrika 1965 uk. 175

Viongozi wa kisiasa wa wakati huu walikuwa ni Waafars walioungwa mkono na utawala wa Wafaransa, wanasiasa wa Kisomali wa mstari wa mbele wakiwa nje ya nchi makimbizini, na chama pekee kilichotambuliwa cha Kisomali, *la Ligue Populaire Africaine pour l' Independence* (LPAI) hakikutokea hadi 1972, ingawa chama chenye msimamo mkali cha *Front de la Liberdtion de la Cote des Somalis* (FLCS) kilidumu kama kikundi cha kichinichini. Mwaka 1967, kufuatia kura ya maoni mpya ya kuhusu kupewa uwezo mkubwa zaidi wa kujisimamia, chama cha *Afaz L'Union Nationale pour L'Independence* (UNI) kilitawalia serikali mpya ya TFAL.

Baada ya mapinduzi ya Ethiopia mwaka 1974, mapambano ya msituni dhidi ya Wafaransa yaliandaliwa na FLCS. Mwaka 1975 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimio la kuipatia TFAL uhuru mara moja.

Kunako Machi 1977, vyama vya LPAI na FLCS vilivyojaa Wasomali na baadhi ya wafuasi wa zamani wa UNI viliunda *Rassemblement Populaire pour L'Independence* (RPI) chini ya uongozi wa Hassan Gouled. Chama hicho kilishinda uchaguzi na kura ya maoni na Gouled akachaguliwa kuwa raisi wa serikali yenye mawaziri kumi, nusu yao wakiwa wa Afar. Nchi ikawa huru kabisa tarehe 26 Juni 1977, ikiwa na jina la Jamhuri ya Jibuti (Djibouti) na kuwa mwanachama wa arobaini na tisa wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika na mwanachama wa ishirini na mbili wa Umoja wa Waarabu.

## Itikadi za Mapambano ya Ukombozi

Katika kipindi hiki kinachojadiliwa, itikadi kuu tatu zilitawala katika nchi za Kiarabu za Afrika ya Kaskazini: Uislamu, utaifa na ujamaa. Athari na vishindo vyake vilitofautiana, lakini itikadi iliyotawala katika hatua hii ya mapambano dhidi ya ukoloni ilikuwa ni utaifa wa Kiarabu.

Uislamu ulikuwa itikadi kongwe kabisa iliyoingiliana na maisha ya watu walio wengi, ikizindua maoni yao juu ya ulimwengu na mielekeo yao kuhusu mambo ya kisiasa na ya kijamii. Uislamu aghalabu ulichukua dhima muhimu katika kuwahamasisha watu na katika baadhi ya nchi, *maulama* wa Kiislamu walishiriki au hata kuongoza kampeni dhidi ya ukoloni. Hii ilitokea hasa Algeria katika "Chama cha Maulama wa Algeria". Mara tu vikundi vya ukombozi vya kitaifa vilipoanza kutetea utamaduni wa Waarabu-Waislamu uliotishiwa na uvamizi wa utamaduni wa Magharibi, vilichukua sura ya kidini. Mnamo 1950 vikundi vya kidini vilianza kushughulika zaidi huku vikiakisi hisia za matabaka ya wanyonge, vikashahidisha misingi ya imani na maadili ya Kiislamu na kupinga tabaka tawala za Kimagharibi na ubeberu.

Tapo la Udugu wa Waislamu, lililoanzishwa 1927[14] na Hassan al-Banna, mwalimu wa Kimisri, lilikua bila kutetereka, likivutia wanachama wengi kupitia shughuli za kibinadamu na za kijamii. Zaidi ya Uislamu tapo hili lilikuwa na muundo wa utaifa wa Kimisri. Tapo lilipendekeza mabadiliko sahili tu ya kijamii yaliyotegemea kushikilia kwelikweli *sharia* na kuepuka tabia ya kufanya mambo "kidunia" ya wazalendo huria (wa Kiliberali). Katika kipindi kati ya mwisho wa vita na majilio ya utawala wa kijeshi, Udugu wa Waislamu ulichukua dhima nzito na ya makeke katika siasa za Misri. Baadhi ya vikundi ndani ya Udugu vilijiingiza katika vitendo binafsi vya kigaidi vilivyolenga wanasiasa na majeshi ya Kiingereza katika ukanda wa Mfereji wa Suez.

Ingawa umetengwa kutokana na vurugu zake, Udugu wa Waislamu bado upo leo, na bado una athari miongoni mwa mabwanyenye uchwara wa Kimisri, wasomi wasio na kazi na tabaka la chini la watumishi wa serikali. Matawi ya Udugu, au makundi ya aina hiyo, yaliibuka katika nchi nyingine za Kiislamu na za Kiarabu, na matapo haya ya kijahidina ni washindani muhimu kabisa kwa wazalendo na wajamaa.

Tapo la wazalendo la Kiarabu limeundwa na mielekeo miwili, mwelekeo wa umoja wa Waarabu na mwelekeo wa utaifa. Mapambano dhidi ya ukoloni ya kipindi cha kati ya vita zaidi yaliimarisha uzalendo. Katika Afrika ya Kaskazini itikadi ya umoja wa Waarabu ilivuma miongoni mwa baadhi ya vikundi vya wasomi tu. Ni vita vya ukombozi wa Algeria vilivyoleta mabadiliko katika nchi za Maghreb.

Tapo la kitaifa la Misri liliandaliwa kudai uhuru kamili na jitihada zake zilielekezwa kwenye kupatikana "Umoja wa bonde la Nili,". Hata kwa utawala wa kijeshi, muungano na Sudani hadi 1955 ulibakia kuwa moja ya suala kuu la kisiasa.[15]

Wazo la umoja wa Waarabu lililojitokeza wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza katika sehemu ya Asia ya ulimwengu wa Waarabu, kwa muda mrefu, lilidhihakiwa katika Misri. Hata hivyo wananadharia wa umoja wa Waarabu wengi walisisitiza dhima ya uongozi wa Misri katika mchakacho unaotarajiwa wa muungano.[16] Katika nchi za Kiarabu, utaifa ulijitokeza kwanza kama ukinzani dhidi ya utawala wa kigeni. Katika kipindi cha kati ya vita, uliunganisha uongozi wa kidini na makabaila, lakini athari yao hata hivyo ilipungua; Uislamu ukawa wa kimaadili zaidi kuliko

[14] Kuhusiana na tapo hili, tazama R.P. Mitchell, 1969, I.M. Husayni, 1952

[15] Abdel-Malek, 1969

[16] H.Z. Nuseibeh, 1956

kisiasa. Uislamu unafanya sehemu moja na muhimu ya utaifa wa Waarabu; utamaduni na ustaarabu wa Kiarabu ulitengenezwa na Uislamu na maisha ya Kiislamu yanashuhudia asili yake katika Uarabu.

Mwelekeo wa Waislamu wa kijadi na wana mapokeo kuhusu utaifa wa Waarabu ulikuwa hasi. Kwa maoni yao utaifa ulikuwa unaharibu umoja wa Uislamu kwa kuunyima tabia yake ya kilimwengu na kwa kuchangia kwenye wazo potofu kwamba awali ya yote Uislamu ni dini ya Kiarabu. Zaidi ya hayo, kwa wanateolojia, Mwislamu halisi hana budi kumtii Mungu tu na *Umma* wa Kiislamu (jumuiya ya Kiislamu yenye kuvuka utaifa), ambapo wazalendo wanatanguliza taifa la Kiarabu kama kitu kitukufu kabisa. Kwa upande mwingine, walifanya jitihada za kuchanganya Uislamu ndani ya itikadi na programu zao, lakini zaidi kama jambo la kitamaduni au la kijamii au kama dini tu - bado mashaka yanaendelea kuwako juu ya dhima inayotekelezwa na Uislamu katika utaifa wa Waarabu.

Ingawa madhumuni ya Umoja wa Waarabu ya itikadi ya utaifa yalitangazwa kwa nguvu zaidi baada ya vita kuliko kabla, harakati dhidi ya ukoloni ziliandaliwa kufuatana na utaifa halisi wa mahala, kama mfano wa Misri unavyoonyesha. Mfarakano kati ya utaifa wa umoja wa Waarabu na utaifa wa mahala uliongezeka baada ya vita. Matapo ya kitaifa ya maskani yalikuwa na madhumuni kuntu na yalijiamini zaidi kwa kuhusishwa karibu na hali ya kijamii na ya kiuchumi.

Katika mapambano dhidi ya utawala wa kikoloni, jamii za nchi za Kiarabu katika Afrika ya Kaskazini hazikutaka kuunda upya dola bora la Kiislamu wala jumuiya ya umoja wa Waarabu. Uhuru wa taifa ulitafutwa na jamii na kwa ajili ya jamii inayoishi nchini humo. Ilikuwa ni kwa sababu hizi za kiutekelezaji ndipo utaifa wa mahala ukatawala imani za umoja wa Uarabu au umoja wa Uislamu kama itikadi ya kampeni dhidi ya mapambano ya ukoloni.

Mawazo ya kijamaa yalikwishasambaa miongoni mwa wasomi wachache katika nchi za Kiarabu za Afrika ya Kaskazini, lakini hayakujitokeza katika programu za kitaifa. Chama cha Kikomunisti kilikuweko, ingawa kwa siri, katika Misri na Sudani, lakini huko Maghreb uanachama wake ulikuwa wa Wazungu zaidi.[17] Hivyo vyama hivi havikuweza kushiriki katika harakati za kitaifa za ukombozi.[18] Hii inaweza kuelezwa kwa kiasi fulani na kushindwa kwa jaribio la kwanza la tapo la Kimaksi la Kiarabu kujirekebisha kuchukuana na muktadha wa kijamii-

17 M.S. Angwani, 1969

18 Tazama A. Abdel-Malek, 1966

kitamaduni wa ulimwengu wa Kiarabu, na kwa taswira yake ya tapo lenye sura ya uzunguzungu, lisilo sadifu hali halisi ya kitaifa.[19]

Wakati huo huo, ushindi wa Urusi ya Kisovieti katika Vita Vikuu vya Pili, na mafanikio yake kuwa taifa kuu kitasnia, ulizivutia nchi nyingi za Kiarabu kuelekea ujamaa. Aina mbalimhali za ujamaa wa Kiarabu zilijitokeza, zikichukua baadhi ya mafunzo ya Marx lakini zikikataa kuchangia katika mawazo yake ya kilimwengu yenye kujumuisha ukana Mungu na umataifa.

Katika takriban aina zote za ujamaa wa Kiarabu, baadhi ya hatua za maendeleo ya ubepari zilikataliwa. Ujamaa ulieleweka kama msururu wa njia za kifundi na za kimpangilio zilizounganishwa zaidi zaidi na shughuli za serikali na upanuzi wa kazi zake za kiuchumi.

Hivyo mbiu-kauli za kijamaa zilitumiwa kuhudumia utaifa wa Kiarabu. Ujamaa ulionekana kuwa njia ya kupatia madhumuni ya taifa na kujenga upya nchi. Ukimulikwa kwa mwanga huu, ujamaa unaonekana kuwa ni sura nyingine ya utaifa.

# 7 Afrika Magharibi 1945-60

## Utangulizi

Kwa watu wa Afrika waliodhalilishwa na utawala wa kikoloni, kumalizika kwa Vita Vikuu vya Pili kulileta matumaini makubwa.Ushinde wa ufashisti ulikuwa ni ushinde wa imani ambayo misingi yake ilikuwa ni ileile ya ukoloni: ubaguzi wa rangi, utukuzaji wa mabavu, na kukatalia watu uhuru. Mwaka 1941, Mkataba wa Atlantiki uliweka, kama madhumuni ya Washirika katika vita, "haki ya mataifa yote kuchagua aina ya serikali ambayo wangependa iwatawale." Katika fikra za watia sahihi, kifungu hiki kilikusudiwa kutumika Ulaya tu, lakini watu wa Afrika walidai haki hii kwa manufaa yao. Azikiwe katika Nigeria, G.E. Moore katika Gold Coast (Pwani ya Dhahabu) pamoja na Albert George Caulker katika Sierra Leone, wote walidai makusudio ya Mkataba huu[1]. Baada ya kushiriki katika vita hivi kwa kuheshimu haki hii, wananchi wa Afrika Magharibi walijiandaa kusaili utawala wa kikoloni.

Usaili huu ulirahisishwa kwa upande mmoja na ukinzani wa ukoloni wa Urusi (USSR) na wa Marekani (USA); na kwa upande mwingine kwa ongezeko la nguvu za vyama vya mrengo wa kushoto katika Ufaransa na Uingereza.

Hali ya kisiasa katika Afrika Magharibi ilikwisha badilishwa na Vita Vikuu vya Pili. Awali ya yote, uandikishaji wa lazima jeshini ulisababisha ghadhabu kali, hususani miongoni mwa wanawake ambao waume zao, watoto na wajukuu zao

[1] P.O. Esedebe, 1971, uk. 24; A.A. Boshen, 1986 uk. 141-2 A.A. Mazrui na M. Tidy 1984 uk. 12-14

walitenganishwa nao. Pili, Waafrika waliotumikia jeshi katika Burma na India, walikutana na matapo ya kudai uhuru huko. Hivyo wakafahamu mikakati na mbinu dhidi ya ukoloni. Zaidi ya hayo, mara baada ya kurejea, askari hawa walitarajia kupata malipo maridhawa atetezi wa malengo haya ya umma, lakini hili halikutokea mara kwa mara.

Mara baada ya vita, upungufu wa bidhaa ulikuwa bado umetapakaa na mipango ya kwanza ilikuwa kukuza ugavi wa bidhaa ghafi. Baada ya neema kurudi, madhumuni yale yale yalishikiliwa, pamoja na jitihada za kuboresha miundombinu, afya na elimu.

Hili lilikuwa jibu la madai ya wengi, lakini pia la kuwa na wafanyakazi walioelimika vyema na wenye afya.

Uzorotaji wa uchumi katika Afrika Magharibi ulikuwa umeongezeka wakati wa vita, kiasi cha kulazimisha nchi mama kuwekeza; hivyo istilahi "msaada" ikatokea na kujijenga. Uchumi nyang'anyi wa kikoloni uliendelea hadi mwisho wa miaka ya 1950, na uzalishaji wa kilimo kwa mahuruji na uchimbaji migodi uliendelezwa ndani ya mpangilio huu. Mambo hayo takriban hayakuweko katika nchi za Kifaransa kabla ya 1949-1951. Miji mikuu ya bandari ikashuhudia mwanzo wa maendeleo ya tasnia: mageuzi ya bidhaa mahuruji na mabadilisho ya bidhaa maduhuli kwa bidhaa zilizosindikwa ndani.

Kijamii, shule za msingi mpya na vyuo vikuu vishiriki vilifunguliwa katika Nigeria na Gold Coast wakati miji ilikuwa ikiongezeka, na vijana wakihamia mijini kutoka shamba mara baada ya kumaliza shule. Baada ya vita wengi pia walirudi nchini mwao baada ya kumaliza masomo ya juu huko ng'ambo, hasa katika sehemu za Kiingereza za Afrika Magharibi.

Mageuzi haya yalisababisha ongezeko la idadi ya watu katika tabaka mbili za kijamii, tabaka za kati kwa upande mmoja (weledi, wanataaluma, watumishi wa serikali, wafanyabiashara n.k.) na wafanyakazi kwa upande mwingine (walimu, wafanya biashara wadogo, wafanya kazi wa reli, wachimba migodi n.k.). Juu ya yote, mageuzi haya yalizaa msongamano wa watu katika miji mikuu au katika vituo vya utawala na vya uchimbaji migodi. Katika zoni za mashamba, ambako idadi kubwa ya watu wakiendelea kuishi, idadi ya wakulima na wafanyakazi mashambani iliongezeka, hasa katika Gold Coast, katika Cote'd Ivoire (Pwani ya Pembe za Ndovu), na katika Nigeria. Makoloni manne ya Kiingereza yalikuwa yameendelezwa zaidi kuliko ya Kifaransa na ya Kireno: mtandao wao wa reli ulikuwa mpana zaidi, na uzalishaji wa kilimo na wa migodi ulikuwa wa juu zaidi. Kijamii na kitamaduni, Nigeria, ikiwa na idadi kubwa zaidi ya watu kuliko makoloni yote ya Kifaransa, ilikuwa pia, kwa karibu karne nzima, ikijivunia kundi la wasomi

walioiga tabia za Waingereza, na magazeti ya Kiafrika.

Katika muongo uliofuata mara baada ya vita, mabadiliko ya kisiasa yalitia fora: ndani ya kipindi hiki, kati ya makoloni kumi na tano ya Afrika Magharibi, kumi na moja yalikwishakujipatia uhuru wa kisiasa kufika mwaka 1960. Makoloni manne kati ya haya yalikuwa ya Kiingereza — Nigeria, Gold Coast (Ghana), Sierra Leone na Gambia — na tisa yalikuwa ya Kifaransa — Dahomey (sasa Benin), Guinea, Cote'd Ivoire, Mali, Mauritania, Niger, Senegal, Togo, na Volta ya Juu (Burkina-Faso). Mengine yalikuwa ya Kireno — visiwa vya Cape Verde na Guinea Bissau. Gold Coast lilikuwa koloni la kwanza la Kiingereza kutwaa uhuru, likifuatiwa na Nigeria, halafu Sierra Leone na Gambia. Mwaka 1958 Guinea lilikuwa koloni la kwanza la Kifaransa kupata uhuru, na mengine yote yalipata uhuru mwaka 1960. Makoloni ya Kireno yalikuwa ya mwisho kutokomeza ukoloni katika Afrika Magharibi.

Matukio haya sahili yalizua maswali kadha; la kwanza likiwa kwa nini ukoloni ulifikia mwisho Afrika magharibi miaka kumi na tano baada ya mwisho wa Vita Vikuu vya Pili? Pili, kwa nini koloni la Kiingereza likawa la kwanza kupata uhuru kusini mwa Sahara? Tatu, kwa nini Guinea iliongoza njia katika kupata uhuru katika Afrika Magharibi ya Kifaransa ambapo makoloni mengine yote yalipata uhuru mwaka 1960? Mwisho, kwa nini makoloni ya Kireno yawe ya mwisho kujipatia uhuru? Ili kuyajibu maswali haya, sura hii itachunguza hali ya makoloni ya Kiingereza, Kifaransa na Kireno moja baada ya jingine.

## Afrika Magharibi ya Kiingereza

Katika makoloni haya, kukomeshwa kwa ukoloni kunaweza kunasibishwa na mambo matatu makuu ambayo yanayohusu pia makoloni mengine yote kwa kiasi fulani. Jambo la kwanza na la muhimu kabisa lilikuwa kuibuka kwa utaifa wa Kiafrika; la pili lilikuwa namna, madhumuni na shughuli za vyama vya siasa na matapo ya kitaifa; jambo la tatu lilitokana na matendo na majibu ya Waingereza kulipokabiliwa na mambo ambayo wazalendo na wafuasi wao waliyoyaanzisha na kuyadai.

Harakati za kizalendo na za kupinga ukoloni za Kiafrika zilianza tangu enzi za uasisi wa mfumo wa ukoloni katika Afrika; hata hivyo utaifa na ukinzani dhidi ya ukoloni vilifikia kilele cha hisia za chuki kwa wageni katika muongo uliofuatia mwisho wa Vita Vikuu vya Pili.

Hili linaweza kuelezwa kwanza kabisa kwa athari ya vita vyenyewe na kukatishwa tamaa kulikosababishwa na mtazamo wa serikali ya Kiingereza kuhusu

Mkataba wa Atlantiki[2] Halafu, Mkutano wa Umoja wa Kiafrika uliofanyika Manchester 1945 ulitoa msukumo kwa harakati za kitaifa kwa kuzipatia makali. Mkutano huu ulikuwa wa aina yake kwa kuwa, kwa mara ya kwanza kabisa, Waafrika walikuwa wanatekeleza sehemu muhimu wakati wa maandalizi na wa



*Picha 7.1 obafemi Awolowo wa Nigeria, kiongozi wa Action Group Party, kilichoanzishwa 1950.*

tukio lenyewe, mbali na kuhudhuria kwa wingi. Zaidi ya hayo, kwa mara ya kwanza mkutano ulidai "uhuru kamili kabisa", Afrika iliyoungana, na uchumi wa kijamaa. Mkutano ulisawidi mikakati ya kutekelezwa ili kupata uhuru, matumizi ya nguvu yakiwa ni hatua ya mwisho iwapo hapana budi. Istilahi za Kimarx zilizagaa, zikichochea wafanyakazi, wasomi na wakulima kuunda vyama kupambana na nyonyaji wa kibeberu na kupata uhuru. Kwa maelezo kuntu, washiriki walizindua kampeni za kudai uhuru na kuunga mkono matapo yaliyopo ya kudai uhuru.

[2] P.O Esedebem 1971, uk. 24

Waliohudhuria ni pamoja na Kwame Nkurumah (Gold Coast), A. Awolowo (Nigeria), Jomo Kenyatta (Kenya) na Hastings Banda (Malawi), ingawa hapakuwa na Waafrika waliohudhuria kutoka makoloni ya Kifaransa, Kireno wala Kibelgiji.

Hata hivyo, mambo yaliyosababisha kuibuka kwa utaifa yalikuwa bado ni kukatishwa tamaa na hasira iliyoletwa na kuharibika kwa hali ya uchumi na ya kijamii baada ya vita, na hisia ya kutoridhika iliyozushwa na mabadiliko yasiyotosheleza. Migomo ya wafanyakazi wa Nigeria tangu 1945 mpaka 1948, maandamano ya waliokuwa askari wa vita yaliyofuatiwa na ususiaji na uporaji wa bidhaa za Wazungu katika Gold Coast mwaka wa 1948, yote yalichochewa na hisia hii ya kero ya baada ya vita. Matukio haya yalichangia kuenea na kuimarisha harakati dhidi ya ukoloni. Kijamii, ujenzi wa chuo kikuu kimoja tu kwa Afrika Magharibi ya Waingereza nzima badala ya chuo kimoja kwa kila koloni ulizidisha hali ya kutoridhika. Kwa upande wa siasa, katiba zilizoanza kutumika mwaka wa 1946 katika Nigeria, Gold Coast na Sierra Leone mwaka mmoja baadaye, zilianzisha mabaraza ya kutunga sheria ambamo idadi kubwa ya wajumbe walipaswa kuteuliwa na gavana au kuchaguliwa na machifu wa jadi. Kote katika Sierra Leone na Nigeria, hatua hizi mpya ziliyawezesha majimbo ya kaskazini kuyatawala majimbo ya kusini yenye athari kubwa zaidi ya Kimagharibi, jambo ambalo liliwakasirisha wasomi na kukazia dhamira yao ya kukomesha mfumo wa ukoloni.

Jambo jingine lililochangia katika kutelekeza mfumo wa ukoloni lilikuwa ni hulka, madhumuni na mikakati ya vyama vya siasa vilivyoanzishwa baada ya Vita Vikuu vya Pili. Jambo hili linaeleza kwa nini Gold Coast lilikuwa koloni la kwanza la Kiingereza kupata uhuru, na pia kwa nini, katika makoloni mengine, majimbo ya kaskazini yalitawala medani ya siasa.

Wakati wa muongo uliofuata Vita Vikuu vya Pili,[3] idadi kubwa ya vyama vya siasa ilizuka Afrika nzima na hasa katika Afrika Magharibi ya Waingereza. Mafanikio yake katika vita vya uhuru yalitokana na hulka yake: tofauti na vile vya kabla ya vita, vyama hivi havikuwa vya wasomi wachache wala vya watu wa mijini tu. Kwa viwango tofauti, vyama viliungwa mkono na watu anuwai; vyama vya wafanyakazi, askari wa zamani, vyama vya wanawake, wanafunzi, wakulima, machifu wa jadi n.k. Kutokana na msaada huu, haikuwezekana tena kwa mamlaka za kikoloni kutovijali. Vyama vya wafanyakazi vilifanya kazi maalumu katika Gold Coast ambapo *Jumuiya ya Vyama vya Wafanyakazi* (TUC) iliunga mkono *Mkutano wa Chama cha Umoja wa Wananchi* (CPP) na kuwa na dhima kuu

[3] T. Hodgkins, 1961, uk. 179-209

katika kampeni yake. Pili, vyama hivi viliandaliwa vyema, vikiwa na ofisi, mabango, vifaa vya propaganda na zaidi ya yote wafanyakazi wanaotenda kazi katika ngazi za taifa, jimbo na za mitaa. Tatu, baadhi ya vyama vipya vilikuwa tayari kutumia njia zozote ziwezekanazo ili kukidhi madhumuni yao. Njia zao za amani na za kikatiba zilikuwa zinaelekezwa kwenye mashirika ya kimataifa kama UNO na serikali zinazopinga ukoloni kama Marekani au Umoja wa Kisovieti. Njia zao za mabavu na zisizokuwa za kikatiba zilikuwa ni pamoja na migomo na mashambulizi ya asasi za kikoloni. Ufanisi wa vyama vipya ulitokana pia na mvuto wa viongozi kama Kwame Nkrumah katika Gold Coast na N. Azikiwe katika Nigeria. Madhumuni yao na misemo yao ilikuwa mikali sana; kwa mfano walidai "kujitegemea sasa" dhidi ya mabadiliko tu ya utawala wa kikoloni. Chama kilichoandaliwa vyema, chenye nidhamu kabisa na kikali kuliko vyote vya Afrika Magharibi ya Kiingereza kilikuwa Chama cha Umoja wa Wananchi (CCP) katika Gold Coast. Juu ya yote chama kiliongozwa na Kwame Nkrumah, kiongozi mwingine mwenye bashasha. Yote haya yanasaidia kueleza ufanisi wa CPP katika Gold Coast lakini pia kwa nini Gold Coast ilikuwa koloni la kwanza la Kiingereza kupata uhuru kusini mwa jangwa la Sahara.

Hata hivyo, palikuwa na tofauti za mawazo kati ya vyama, jambo linaloelezea tofauti za tarehe za uhuru na aina za serikali zilizoigwa na nchi mara baada ya kupata uhuru. Kwanza kabisa baadhi ya vyama vilikuwa vya kitaifa ambapo vingine vilikuwa na misingi ya kimbari au ya kijimbo. Hivyo, katika Gold Coast, vyama viwili kati ya vitatu vilikuwa vya kitaifa, lakini katika makoloni mengine vilikuwa vya kijimbo kimsingi, na kulikuwa na mikingamo kati ya makundi ya mbari na kati ya Waislamu na Wakristo. Pale ambapo vyama katika Gld Coast viliweza kuafikiana juu ya msingi wa uhuru na tarehe yake, maswali haya yalikuwa mambo ya kubishaniwa katika makoloni mengine. Aidha, tukiondosha Gold Coast majimbo ya kaskazini ya makoloni yote yalikuwa na watu wengi zaidi ya majimbo ya kusini, hii ikiwa na maana kwamba mapambano kati ya vyama yalisababisha kaskazini kutawala kusini kisiasa. Hata hivyo, watu wa kusini walikuwa karibu siku zote wameendelea zaidi kuliko watu wa kaskazini kiuchumi. Elimu ya Magharibi na usasa vilihusika, na dosari hii ya kisiasa iliimarisha umajimbo, ikiwaghadhibisha na kuwaudhi watu wa kusini.

Mkabala wa utawala wa kikoloni wa Kiingereza kufuatana na madai na shughuli za vyama na mashirika ya kisiasa, pia ulitokea kuwa jambo kuu katika kuelezea



Picha 7.2 *Dkt Nnamdi Azikiwe, Gavana Mkuu wa Nigeria, akiwa na Duke wa Devonshire, London, 10 Julai 1961*

matokeo ya harakati za uhuru. Tajriba ya Waingereza kuhusu migogoro na madai ya kitaifa inaanzia karne ya kumi na nane ikihusisha Marekani, Kanada na Australia, na kufikia upeo wake katika India miaka ya 1940. Hivyo, Waingereza walikwishakubali kanuni ya kujitawala kuwa ni hatima isiyokuwa budi ya makoloni yote. Katika Afrika Magharibi ya Waingereza, vyama vya *Labour* na *conservative* na makampuni mengi yaliyosimikwa katika makoloni haya yalifikia hatima hii kuanzia mwisho wa miaka ya arobaini. Kwa upande mwingine, hapakuwa na mwafaka juu ya urefu wa kipindi cha lazima cha kujifunza juu ya kujitawala, hapakuwa na programu ya kujinasua na ukoloni iliyoandaliwa kabla, na mwanzoni palikuwa na upinzani kwa jitihada na shinikizo zilizofanywa na wazalendo.

Kuanzia katikati ya miaka ya hamsini, harakati za wazalendo wa Kiafrika zilifikia kilele cha makali yake na Waingereza waliamua kutokuzipinga. Walichagua

kuachana na washirika wao, na vyombo vyao, mathalani, waali - watawala wa kijadi, na kusalimu amri kwa au kujadiliana na wazalendo. Katika Afrika Magharibi, Waingereza walitegemea zaidi njia za amani na za kikatiba. Pamoja na hayo, mashambulio ya bunduki mwaka 1948 katika Gold Coast, kufungwa kwa Nkrumah na wafuasi wake mwanzoni mwa miaka ya hamsini, bila kusahau ukandamizaji wa mgomo wa 1955, yote haya yanaonyesha kuwa matumizi ya nguvu na vurugu havikuepukika kabisa.

Kama ilivyothibitishwa na matokeo ya uchaguzi wa 1951 na 1956 ambapo Nkrumah na chama chake kilishinda, takriban vyama vyote katika Gold Coast na wananchi walio wengi walikwishafikia maafikiano kuhusu masuala ya uhuru. Kwa hiyo Uingereza ilipanga tarehe 5 Machi 1957 iwe siku ya uhuru. Mwisho wa miaka ya hamsini, baada ya msururu wa mikutano ya katiba, vyama vyote katika Nigeria na Sierra Leone vilifikia makubaliano, na Uingereza ilikubali madai yao ya uhuru. Hivyo ilikuwa ni watu wa Afrika Magharibi walioanzisha harakati za uhuru, badala ya Ofisi ya Makoloni, Bunge la Uingereza au maoni ya Waingereza.

## Afrika Magharibi ya Wafaransa na Togo

Mbali na Guinea na Jibuti, makoloni yote ya Kifaransa katika Afrika yalipata uhuru mwaka mmoja, 1960. Matokeo haya yalitokana na hulka ya madai na matendo ya wazalendo, hulka ya vyama vya siasa na zaidi ya yote majibu ya Ufaransa na hasa yale ya Jenerali de Gaulle.

Afrika Magharibi ya Wafaransa, iliyokuwa shirikisho la makoloni manane hadi 1958 yaliyoitwa Majimbo ya Nje baada ya 1946 yalifanya kitengo kimoja cha utawala chini ya mamlaka ya Gavana Jenerali mwaka 1946 aliyeitwa baadaye Kamishna Mkuu wa Jamhuri (*Haut Commissaire de la Republique*). Sehemu ya Ufaransa ya Togo, jimbo mdhamana, ilikuwa na hadhi ya peke yake.

Ikilinganishwa na Afrika Magharibi ya Waingereza, Afrika Magharibi ya Wafaransa ilikuwa nyuma kwa mambo yote. Nje ya komuna kamili tatu katika Senegal (Dakar, Rufisque na St Louis) ambako wakazi wote walikuwa raia wa Ufaransa, serikali ya kikoloni iliwahini maisha ya kisiasa ya aina yoyote wenyeji wote ndani ya makoloni. Zaidi ya hayo walipaswa kushindania hata kazi za chini na "walowezi maskini wa kizungu" ambao hawakuweko katika Afrika Magharibi ya Waingereza.

Mwisho wa vita uliamsha harakati kali kutokana na sababu zilizokwishatajwa, lakini pia kutokana na mageuzi ya ghafla ya hadhi ya kisiasa ya makoloni. Mwanzoni mwa 1944, Mkutano wa Afrika ya Kifaransa, katika Brazzaville, uliokutanisha

Gavana na walowezi, uliondosha "wazo lolote la kujitenga". Uliahidi tu uwezekano wa "kushiriki" kwa Waafrika katika kuendesha mambo yao, ahadi ambayo Waafrika waliamua kuitwaa kama ilivyo.

Kwa mara ya kwanza, katika 1945, kikundi cha wenyeji wachache waliweza kuchagua wawakilishi katika bunge la taifa la Ufaransa. Kupitia uwakilishi huu wa kikoloni, Jenerali de Gaulle alitarajia kufidia (pengo la) mlipuko wa upinzani wa mrengo wa kushoto uliotabiriwa katika Ufaransa, kwani wakoloni walimwunga mkono, na alitarajia kuwa wawakilishi wa raia wa makoloni wangepiga kura kufuatana na matakwa ya utawala wa Ufaransa. Ukweli ni kwamba, wale waliofanya kampeni kuunga mkono kumalizika kwa utawala wa kikoloni walichaguliwa. Katika Senegal, wakili Lamine Gueye na mhitimu kijana wa Chuo Kikuu, Leopold Sedar Senghor, walichaguliwa na wote wawili walijiunga na chama cha Kisoshalisti. Katika Guinea na Dahomey, Yasini Diallo na Suru - Migan Apithy walijiunga na kundi la Kisoshalisti, ambapo Felix Houphouet-Boigny, mwakilishi kutoka Cote d'Ivore na Fily Dabo Sissoko, mwakilishi katoka Sudani-Niger, nawalifanya urafiki na kundi la Kikomunisti.

## Usimilishaji na uendelezaji wa utawala wa kikoloni

Baraza la kwanza lililochaguliwa lilikuwa na wingi wa wajumbe wa mrengo wa kushoto, ambao karibu wawakilishi wote wa wenyeji kutoka nje walijiunga nao. Katiba, iliyosawidiwa kwa kiasi na mwakilishi wa Senegal Senghor, iliyaingiza makoloni yote katika Jamhuri na kuanzisha istilahi "Unioni francaise" au muungano wa Kifaransa, ukitoa bado uwezekano wa kubadilika kuelekea uhuru.

Zaidi ya hayo, mwezi Aprili 1946, baraza la wawakilishi lilipiga kura kuunga mkono sheria ya Houphouet-Boigny iliyopiga marufuku kazi za kulazimishwa. Mwezi Mei 1946, walipiga kura kuunga mkono sheria ya Lamine Guaye iliyowapatia uraia wa Kifaransa wenyeji wote wa makoloni ya Kifaransa, na kuingiza hatua mbalimbali za kufuta dhana ya *indigenat* na kuanzisha uhuru wa magazeti na wa kujumuika.

Mrengo wa kulia uliendesha kampeni kali ya kupinga katiba, na katika uchaguzi wa watu wote katiba hii ilikataliwa. Katika Baraza la wawakilishi la pili lililochaguliwa katika Juni 1946, kufutwa kwa kazi za kulazimishwa na kutoa uraia vilibakizwa lakini uwezekano wowote wa mabadiliko kuelekea uhuru ulizimwa. Katiba zote mbili ziliasisi usimilishaji uliosaki (uliokita mizizi) katika Senegal. Huu ulikubaliwa kwa sababu wawakilishi wa Kiafrika waliogopa kuwa ushirikisho uliopendekezwa na wawakilishi wa mrengo wa kulia ungewafikisha

kwenye uhuru wa mtindo wa Afrika Kusini, jambo ambalo lingewapatia madaraka wakoloni. Kinyume cha hayo, walipendelea kuendelea kuungwa mkono na utawala wa mrengo wa kushoto wa kati.

## Maendeleo ya Vyama

Vyama (vya siasa) vikaundwa katika Afrika Magharibi ya Kifaransa. Katika muktadha huu wa usimilishaji. Vyama hivi ama vilishirikishwa na vyama vya Kifaransa au vilikuwa ni maendelezo ya moja kwa moja ya vyama hivyo, kama ilivyokuwa kwa *Federation du parti socialiste du Senegal.* Chama cha Kikomunisti kiliunda vikundi vya mtalaa vya kikomunisti (GECS) ambavyo kazi yake ilikuwa ni kuunda vyama au matapo dhidi ya ukoloni.

Wakikabiliwa na upinzani wa kikoloni katika kiangazi cha 1946, baadhi ya wawakilishi wa Kiafrika waliitisha mkutano katika Bamako mwezi Oktoba 1946. Marius Moutet, Waziri wa Kisoshalisti aliyeshughulikia nchi za nje za Kifaransa, alitoa maagizo ya kuuzuia. Aliwashinikiza wawakilishi wa kisoshalisti waepuke kuhudhuria, na wajumbe kutoka Afrika ya Ikweta ya Kifaransa hawakuweza kuhudhuria. Mkutano huu ulifanyika, hata hivyo, na uliishia kuunda *Rassemblement democratique africain* (Mshikamano wa Kidemokrasia wa Kiafrika au RDA), Houphouet-Boigny akiwa rais wake. Chama hiki kilishirikisha vyama vya Kiafrika vya kienyeji kwa misingi ya mapambano dhidi ya ukoloni. Wawakilishi wake (7 kwa jumla katika Bunge mwaka 1946) waliunda urafiki na makundi ya kikomunisti.

## Vita Baridi na jitihada za kurudisha ukoloni

Katiba ilikwisharuhusu kuanzisha Mabaraza makuu ambayo yaligeuka kuwa Mabaraza ya nchi mwaka 1952. Isipokuwa katika Senegal, katika makoloni uchaguzi wa wajumbe wa vyombo viwili vya uwakilishi vyenye idadi kubwa ya wajumbe wa wakoloni ulifanyika. Katika ngazi ya shirikisho, Baraza Kuu lilichaguliwa na mabaraza ya nchi. Kazi za mabaraza haya zilikuwa ni ushauri na kupigia kura bajeti, huku Magavana wakiwabakia na madaraka yao yote.

Kufukuzwa kwa mawaziri wa kikomunisti Ufaransa mwezi Mei 1947 na kuanzishwa kwa Vita Baridi kuliambatana na sera ya kurejesha ukoloni. Katika Afrika Magharibi ya Kifaransa, sera ya ukandamizaji ililengwa katika Cote d'Ivoire, kulikokuwa ngome ya RDA. Felix Houphouet Boigny, kiongozi wa *Parti democratique de Cote d'Ivoire* (PDCI, sehemu ya RDA), alikuwa daktari Mwafrika, chifu wa zamani wa jimbo na mkulima mkubwa, na alikwishaunda



Picha: 7.3 *Mkutano wa RDA (Rassembelement Democratique African) huko Bamako, 1946· katikati ni Felix Houphouet-Boigny Kushoto ni Gabriel d'Arboussier*

*Syndicat- agricole africain* (Umoja wa Kilimo wa Waafrika) mwaka 1944. Akiwa mwakilishi wa tabaka la kati la wakulima katika Cote d'Ivoire, alidai kufutwa kwa marupurupu yaliyotolewa kwa misingi ya rangi na kazi ya kulazimisha, jambo ambalo lilimwezesha kuwatumia wafanyakazi ambao hadi wakati huo waliweza kuajiriwa na Wazungu tu. Madai haya yaliungwa mkono na tapo la umma lililowakilishwa na PDCI.

Ili kuidhoofisha Cote d'Ivoire, nchi ya Volta ya Juu (Upper Volta) ilirejeshwa mwaka 1947, na halafu mwaka 1949 na 1950, mabavu yalitumiwa kama silaha ya mwisho. Vijiji viliteketezwa, wakulima waliuawa, maiti ya Seneta Victor Biaka Boda iligunduliwa ikiwa imechomwa kabisa, na karibu viongozi wote wa nchi na wa mitaa wa PDCI walikamatwa.

Hatua hizi zilimlazimisha Houphouet-Boigny asalimu amri. Mwishoni mwa mwaka 1950, aliamua kuafikiana na sera ya serikali na kupiga kura kuunga mkono

kutolewa kwa fedha za kijeshi kwa ajili ya vita katika Indo-China. Ndani ya RDA sehemu za Senegal na Niger tu zilikataa kukubali mabadiliko haya.

## Shinikizo la umma na kuelekea kwenye Uhuru

Licha ya kugeuka kwa Houphouet-Boigny, vitendo vilivyofanywa kulalamikia hatua za ubaguzi kwa misingi ya rangi vilianza kuenea tangu 1951. Kikiongozwa na Sekou Toure, *Parti democratique de Guinee* (kilichoshirikishwa na RDA) kiliongoza vita dhidi ya uchifu uliokuwa nyenzo muhimu katika utawala wa kikoloni. Huku ikichochewa na uzorotaji wa hali ya makoloni yake-ushinde wa Dien Bien Phu, uhuru wa Tunisia na Moroko, kuanza kwa vita vya Algeria — serikali ya Ufaransa ilibidi ikubali kusikiliza. "Sheria ya muhtasari" iliyosawidiwa na waziri wa Kisoshalisti wa nchi za Kifaransa za ng'ambo, Gaston Deferre, ilianza kufanya kazi mwaka 1957, ikazipa nchi za ng'ambo madaraka kiasi ya kujitegemea, ambapo serikali ya Ufaransa ikijiandaa kuvunja mashirikisho.

Madhumuni ya sheria ya muhtasari yalikuwa kuwashirikisha viongozi wa Kiafrika katika sera ya kikoloni bila ya kuwapa madaraka halisi. Sheria hii ilishindwa kuzuia matarajio ya kupata uhuru ambayo sasa yalikuwa yakielezwa waziwazi na chama kipya cha mwelekeo wa Kimarx. Makundi huru ya kisiasa ya nje na chama cha Kisoshalisti viliungana kufanya *Parti de regroupement africain* (PRA) chama ambacho kilipigia kura hoja ya kudai uhuru mara moja katika Mkutano huko Kotonou Julai 1958.

Wakati huohuo, katiba mpya iliyosawidiwa na Jenerali de Gaulle mara baada ya kurudi madarakani, alikuwa na mipango mipya. Ilitoa madaraka ya kujiamulia mambo kwa Nchi za ng'ambo, ambazo sasa zilifanywa Jamhuri, na Rais aliyechaguliwa kuchukua nafasi ya Gavana. *Union francaise* kilibadilishwa na kuwa *Communaute francaise* lakini kudai uhuru kuliendelea kutochukuana na uanachama katika Jumuiya hii.

Guinea ndilo koloni pekee lililosema "hapana" katika kura ya maoni kuhusu *Communaute francaise*, kwa asilimia 80 ya kura, na kutangaza uhuru wake tarehe 2 Oktoba 1958. Kwa kufuta Afrika Magharibi ya Kifaransa, katiba iliingiza pia mgawanyiko wa makoloni ya Kifaransa. Senegal na Sudan zilijaribu kupinga jambo hili kwa kuunda shirikisho la Mali ambalo lilidai uhuru Septemba 1959, ambao ulitolewa tarehe 20 Juni 1960. Madola mengine yalifuata mkondo na uhuru wao ulipatikana katika mwezi wa Agosti.



*Picha 7.4 Sylvanus Olympio, Rais wa Togo, akitangaza uhuru wa nchi yake, Aprili 27, 1960*

## Vuguvugu la Wafanyakazi na Vyama vya Wafanyakazi

Licha ya maendeleo katika viwanda na huduma, jumuiya ya wafanyakazi ilibakia ndogo: kwa Afrika Magharibi ya Kifaransa na Togo, walikuwako wafanyakazi wenye mishahara 245,538 mwaka 1947, na 412,810 mwaka 1957, hii ikiwa na maana ya asilimia 2 ya watu wote. Mlinganyo ungekuwa mkubwa kidogo laiti watumishi wa serikali na wasomi tawala (waliotekeleza dhima muhimu katika vyama vya wafanyakazi) wangeingizwa pia.

Katika makoloni ya Kiingereza uanachama wa wafanyakazi uliandaliwa kwa mtindo wa TUC ya Kiingereza, kwa kushirikiana na utawala na waajiri. Hata hivyo wakati mwingine walikuwa waanzilishi wa mapambano, kwa mfano wanachama wa chama cha wafanyakazi wa reli huko Gold Coast katika miaka ya arobaini. Katika Gold Coast, TUC haraka iliungana na CPP na kunako Januari 1950 waliitisha mgomo wa wafanyakazi wote kuunga mkono kampeni ya "hatua chanya" za CPP. Katika Nigeria, vuguvugu la chama cha wafanyakazi lilikuwa limegawanyika na kusambaratika.

Katika nchi za Kifaransa, vyama vilivyo vingi vya wafanyakazi vilishirikishwa na CGT ya Kifaransa (*Confederation generale du travail*) lakini vilikuwa na uhuru mkubwa. Viongozi wengi wa vyama vya wafanyakazi walikuwa pia viongozi wa kisiasa ndani ya RDA. Vyama vya wafanyakazi vya Kikristo, vilivyoshirikishwa na *Confederation francaise des travailleurs chretiens* (CFTC) vilipatikana tu katika makoloni ambako misioni zilikwishakuwa na athari, kama vile Dahomey na Guinea ya pwani.

Mapambano ya vyama vya wafanyakazi yalielekezwa sana sana dhidi ya utawala wa kikoloni na uongozi wa Kizungu, yakitoa madai yaliyokusudiwa kuondosha ubaguzi wa rangi, na hivyo yakawa sehemu ya vita dhidi ya ukoloni, na kuungwa mkono na umati wa Waafrika kwa jumla. Kuungwa mkono huku kulilazimisha Utawala kusalimu amri wakati wa mgomo wa wafanyakazi wa reli wa Kiafrika kunako 1947-1948, na pia wakati wa mgomo uliofuata.

Chama cha *Confederation generale du travail africain* (CGT) kiliundwa mwaka 1956 kwa utukutu wa Sekou Touré, na ingawa utawala wa kikoloni ulikuwa unajaribu kuvishawishi vyama vya wafanyakazi kushirikiana nao, CGT ilitayarisha kituo huru cha Kiafrika kilichounganisha vyama vyote. Baada ya kukubali, vyama vya Kikristo vilivunja kauli, na kuunda *Confederation africaine des travailleurs croyants* (CATC). Wito wa umoja hatimaye ulitokea kuwa kweli katika Mkutano uliofanyika Kotono mwezi Januari 1957 na kuunda *Union generale des travalleurs d'Afrique noire* (UGTAN) chini ya uongozi wa Sekou Touré.

## Dhima ya matapo ya kitamaduni na ya kidini

Utambulishi wa Mwafrika ulikiriwa zaidi kwa njia ya kifasihi. Katika Paris mwaka 1947, jarida la *Presence Africaine* lilizinduliwa, na ingawa halikuwa pingamizi kwa utawala kisiasa, lakini lilisaili itikadi ya ukoloni kwa kukiri utambulishi wa kitamaduni wa Kiafrika. Mwaka huohuo, mwanasiasa na mshairi L.S. Senghor, alichapisha diwani yake ya kwanza, kabla ya kuendelea kukuza dhana ya *negritude*. Baadaye dhana hii ilibishaniwa vikali na tapo la kimapinduzi lililoongozwa na Gabriel d'Arboussier mwaka 1949.

Kwenye miaka ya 1947-1950, gazeti la RDA, *Réveil* la Dakar la kila juma, lilianza kuchapisha ushairi wa kimapambano dhidi ya ukoloni, hasa ule wa Keita Fodeba, ambaye tena aliendelea kuunda mchezo wa bale ya Kiafrika, ambayo sahani zake za santuri zilipigwa marufuku katika Afrika Magharibi ya Kifaransa.

Watunzi wa riwaya wapya walitunga tashtiti (simulizi zenye kebehi) juu ya ukweli wa ukoloni. Miongoni mwao ni muhimu kutaja Mongo Beti, Ferdinand Oyono

(Kameruni), Ousmane Sembene (Senegal) na Bernard B. Dadie (Cote d'Ivoire). Katika Gold Coast uandishi huu dhidi ya ukoloni unaweza kupatikana katika kazi za George Awoonor na Graft-Johnson.

Matapo ya kidini yaliakisi pia mabadiliko ya kisiasa na ya kijamii, wakati mwingine yakiambatana nayo. Dini za kilimwengu zilienea dhidi ya aina mbalimbali za ibada za kienyeji, na baada ya kuafikiana kwa kiasi fulani na tawala za kikoloni, Uislamu ulipata ufanisi mkubwa zaidi ya dini nyinginezo. Baadhi ya tarika za Kiislamu zilikubaliwa na mamlaka ya kikoloni. Hata hivyo wengine, kama Wahamalli katika Sudan ya Kifaransa (Sasa Mali), walipata mateso, hivyo kuwaleta karibu na matapo yenye kupinga ukoloni.


Kanisa Katoliki lilikuwa kabisa sehemu ya mfumo wa kikoloni wa Kifaransa, na liliikana RDA likidai kuwa ni wakala wa "ukomunisti usioamini Mungu". Mabadiliko yalikuja baadaye sana, kwa uchapishaji wa *Encyclique Evangelipraecones* tarehe 2 Juni 1953, na mwaka 1956 tu ndipo makasisi wa kwanza wa Kiafrika walipopewa vyeo.

## Afrika Magharibi ya Wareno: Guinea-Bissau na Visiwa vya Cape Verde

Japo makoloni ya Kifaransa na ya Kiingereza katika Afrika Magharibi yalikwishapata uhuru kufikia 1965, makoloni ya Kireno ilibidi yangoje hadi 1973 na 1974. Katika Afrika ya Kireno, kupata uhuru kulikuwa na fujo na umwagaji damu, na kulichukua muda mrefu. Tabia hizi zinaweza kuelezeka kwa matendo na kanuni za ukoloni wa Kireno pamoja na hulka ya matapo ya kitaifa.

Tangu mwanzo, Ureno kama Ufaransa, ilichukulia makoloni yake kama majimbo yake ya nje, lakini, tofauti ya Ufaransa, Wareno waling'ang'ania sana sera hii.

Kipengee kingine cha kufikiria kilikuwa hali yaliyokuwemo makoloni ya Kireno ya Afrika Magharibi mwanzoni mwa miaka ya hamsini. Yakiwa yamevia kwa kulinganisha na nchi za jirani, makoloni ya Wareno hayakuwa na miundombinu, na biashara duni ya kinyang'anyiro iliyokuwapo ilihodhiwa na *Companhia Uniao Fabril* (CUF). Mwaka 1930, Guinea-Bissau na visiwa vya Cape Verde vilikuwa majimbo ya Ureno lakini, nyuma ya unafiki wa usimilishaji, ubaguzi wa rangi ulikuwa wa kinyama mno. Katika Guinea Bissau kwenye miaka ya hamsini, kati ya wakazi nusu milioni, na baada ya karne tano ya kuwako kwa Wareno, watu 8,320 tu ndio walikuwa na haki za kisiasa. Katika visiwa vya Cape Verde, vilivyokuwa na umati mkubwa wa watu na kuteketezwa mara kwa mara na njaa (vifo 30,000 mwaka 1944-1945 miongoni mwa wakazi wasiozidi 150,000). Watu waliohamia kutoka



Picha 7.5 *Askari wa kike wa PAIG (Partido Africanoda Indepedencia da Guinea Cabo Verde)*

bara walisimilishwa, na Ureno iliajiri mameneja wadogo wa ukoloni kutoka huko.

Vyama vya siasa vilitokeza tu uwanjani katika Afrika Magharibi ya Kireno mwishoni mwa miaka ya hamsini. Jitihada zozote za kisiasa kabla ya hapo zilikwamishwa na ukosefu wa kada ya kati na kuzimwa na ukandamizaji.

Katika Oktoba 19, 1956 mtalamu wa kilimo Mguinea aliyezaliwa visiwa vya Cape Verde, Amilcar Cabral, aliunda *Partido african de independencia da Guine et Cabo Verde* (PAIGC) katika Bissau. Tangu 1956 hadi 1959, shughuli zake kimsingi zilikuwa za mjini na za amani, lakini ukandamizaji wa mgomo usiokuwa halali wa makuli katika mwezi 1959 uliposababisha vifo hamsini, chama cha PAIGC kiliamua kupambana kwa silaha. Cabral alibuni njia na programu mpya ya kisiasa kuwashawishi wananchi wa mashambani waafikiane juu ya wazo la kupata uhuru. Tangu 1961 hadi 1963, vijana wakakamavu walifanya kazi kisirisiri vijijini, wakiwafundisha wakazi kwamba hawangeweza kutatua matatizo yao bila kufanya kazi na kupigana kuondosha mfumo wa ukoloni wa Wareno.

Katika 1963 PAIGC kilianzisha mapambano yake ya silaha, kikianza na vikundi vidogo vya msituni vilivyojengwa na kugeuzwa hatua kwa hatua. Wananchi wa mashambani walisaidia na kuauni kweli kweli vikundi hivi vilivyokuwa vikivinjari, hivyo vikaongezeka katika idadi na nguvu. Mara baada ya kukomboa zoni, waliwafukuza watumishi wa serikali wote wa kikoloni na wafanyabiashara, walifuta kodi na haki-za kikoloni, wakakomesha kazi za kulazimishwa na kilimo cha lazima. Kilichofuata ni kuanzisha mfumo mpya wa biashara, wakajenga shule na zahanati za msituni na kuunda demokrasia ya kweli.

Kikiungwa mkono na Kuba na Urusi, chama cha PAIGC kiliendelea licha ya ongezeko la idadi ya askari katika kikosi cha Wareno ambacho kiliongezeka toka 1000 mwaka 1961 hadi 30,000 mwaka 1967, na licha ya kuungwa mkono kifedha na kijeshi na NATO[4] mataifa makubwa ya Magharibi. Mwaka 1967. PAIGC walidhibiti theluthi mbili ya Guinea-Bissau, na hata kuuliwa kwa Amilcar Cabral katika Januari 1973 hakukuweza kupindua tapo la ukombozi. Aibu na kuvunjika moyo kulikoyakumba majeshi ya Ureno katika Afrika ni miongoni mwa sababu za kupinduliwa kwa serikali ya Salazar huko Ureno mnamo Aprili 1974. Serikali mpya ilithibitisha uhuru wa Guinea-Bissau na kutoa Uhuru kwa Angola na Msumbiji.

PAIGC ilidai muungano wa Guinea-Bissau na visiwa vya CapeVerde kutokana na asili moja ya watu wake. Hali ya kisiwa haikuwezesha upinzani kama wa Guinea-Bissau kwenye visiwa vya Cape Verde, lakini baada ya kuanguka kwa ufashisti wa Kireno, PAIGC ilijitwalia nchi na mrithi wa Cabral, Aristide Pereira, aliendesha mazungumzo ya uhuru wake. Alikuwa rais wa kwanza wa Jamhuri ya visiwa vya Cape Verde mwezi September 1974.

## Liberia

Kunako mwaka 1945, Liberia ilikuwa kinadharia moja ya madola manne huru katika Afrika, lakini kimatendo ilikuwa "koloni mamboleo" la Marekani. Utawala na raslimali za nchi zilikuwa mikononi mwa jumuiya ya Waliberia wa Kimarekani walioishi katika wilaya za pwani, na waliowabagua raia walio wengi walioishi bara.

Kwa nje, Liberia haikuwa na uhusiano na matapo dhidi ya ukoloni, na ilikuwa katika ukingo wa kufilisika kiuchumi. Jitihada za William Vacanarat Shadrach T

[4] NATO - North Atlantic Treaty Organization (Umoja wa Kiulinzi wa Mataifa makubwa ya Ulaya na Marekani



*Picha: 7.6 William Tubman, Rais wa Liberia (alipigwa picha hii Septemba 1956).*

ubman, rais tangu 1944 hadi kifo chake mwaka 1971[5] zilikuja kubadilisha hali hii kikweli kweli.

Akitaka kuachana na kabali ya kampuni ya Mpira ya Firestone, Tubman alikaribisha wawekezaji wa nje, wengi wao wakiwa Wamarekani. Hatua ilileta uchanganyaji wa shughuli za uchumi, zaidi ya kutengeneza mpira, hadi ujenzi wa bandari bandia mjini Monrovia, kuchimba mbale za chuma na kujengwa viwanda vya kutengeneza bidhaa nyepesi. Mwaka 1978, Liberia ilikuwa mzalishaji mkuu na msafirishaji nje mkuu wa mbale za chuma katika Afrika. Maendeleo haya yalirahisisha ujenzi wa mtandao mkubwa wa barabara ambao ulichapusha ufunguaji wa bara. Tubman pia alipanua masoko ya nje ya bidhaa za biashara kutoka Liberia; hivyo bidhaa zilizouzwa Marekani zilipungua toka asilimia 90 mwaka 1950 hadi asilimia 60 kuelekea katikati ya miaka ya sabini.

Sambamba na hili, Tubman alifuata sera ya uchangamano na umoja wa taifa, madhumuni makuu yakiwa ni kuondosha mgawanyiko wa kimaisha na mgongamano baina ya watawala wachache wa Kiliberia-Marekani, na umati wa wenyeji. Wenyeji zaidi na zaidi wa Kiliberia waliingizwa ndani ya utawala wa kijanibu, na hivyo kuwa na haki ya kuwakilishwa Bungeni. Zaidi ya hayo, muundo wa Baraza la Wawakilishi ulibadilishwa ili kupokea Waliberia zaidi toka bara. Asasi za elimu pia zilianza kupokea watu wa bara.

Licha ya mafanikio makubwa haya, maisha yalikuwa bado yametawaliwa na wasomi wa Kiliberia-Marekani, hata kufikia 1960. Ukuaji wa uchumi haukuambatana na maendeleo halisi, na uchimbaji madini zaidi uliwanufaisha wawekezaji wa nje. Mwaka 1960, Liberia ilikuwa haijafikia mataifa huru mapya ya Afrika. Kwa miongo miwili iliyofuata, si Tubman wala mrithi wake aliweza kuingiza mabadiliko ya lazima, hali ambayo iliishia kwenye mapinduzi ya kijeshi tarehe 12 na 13 Aprili 1980.

## Hitimisho

Baada ya kuanza na hali ambamo ukoloni ulionekana kuwa hautikisiki, kipindi cha 1945 hadi 1960 kilimalizika na uondoshaji wake katika sehemu kubwa ya Afrika. Uchanganuzi uliotangulia unaonyesha kuwa katika Afrika Magharibi ya Kiingereza na ya Kireno msukumo ulikuwa ni wa Waafrika wenyewe. Hadi Jenerali de Gaulle alipoingia madarakani, hali ilikuwa vivyo katika Afrika ya Kifaransa. Katika Afrika Magharibi, makoloni ya Kiingereza kwa jumla, na hasa, Gold Coast ya

5 J.G. Liabenow, 1969, uk. 73

## Hitimisho

Baada ya kuanza na hali ambamo ukoloni ulionekana kuwa hautikisiki, kipindi cha 1945 hadi 1960 kilimalizika na uondoshaji wake katika sehemu kubwa ya Afrika. Uchanganuzi uliotangulia unaonyesha kuwa katika Afrika Magharibi ya Kiingereza na ya Kireno msukumo ulikuwa ni wa Waafrika wenyewe. Hadi Jenerali de Gaulle alipoingia madarakani, hali ilikuwa vivyo katika Afrika ya Kifaransa. Katika Afrika Magharibi, makoloni ya Kiingereza kwa jumla, na hasa, Gold Coast ya Nkrumah, ndiyo yaliyoonyesha njia. Katika Afrika ya Kifaransa Guinea ya Sekou Toure iliongoza njia. Kipengee kingine muhimu cha mapambano haya ya uhuru kilikuwa ni kukabidhi madaraka kwa wazalendo wa daraja la kati dhidi ya waali wa kijadi. Hatimaye, mapambano ya uhuru yalikuwa na kishindo katika nchi za Ulaya kwa de Gaulle kuingia madarakani Ufaransa na utawala wa Salazar kuanguka nchini Ureno.

# 8

# Afrika Magharibi ya Ikweta

Afrika ya Ikweta ilikuwa ya kwanza kuwa chini ya ukoloni, na pia ikawa moja ya sehemu za mwisho za kontinenti kukombolewa. Ukoloni wa Wareno ulianza zama za ugunduzi na uvamizi wa ufalme wa Kongo na Angola. Ukombozi haukukamilika katika eneo hili hadi mwaka 1975, miaka kumi na tano baada ya wimbi kubwa la kutwaa uhuru.

Pakiwa mahali panapofahamika sana kwa ukatili mkubwa siku za kwanza za ukoloni, Afrika ya Ikweta ilibuni mbinu anuwai, mikakati na fikra za kupata uhuru wake: upinzani wa wakulima, Umasihi wa kisiasa- kidini, chokochoko za kisiasa na kibunge, migomo na maasi ya mijini, na vita vya umma vya ukombozi.
Ukoloni wa Kifaransa haukutaka kuachia madaraka yake. Katika Brazzaville, kwa mfano, ambayo ilikuwa ishara ya ukombozi wakati wa vita, Wafaransa walijaribu kuonyesha nia yao ya kugeuza matendo ya kikoloni, lakini wakati huohuo kukataa maendeleo yoyote ya kuelekea kujitawala. Watu wa Brazzavile hawakuridhika na hali hiyo, hivyo mara tu baada ya uhuru, walisimama kidete kupinga utawala wa Abbe Fulbert Youlou. Wakati huohuo, huko Kongo ya Ubelgiji (Zaire), kulizuka vita vikali vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoanza 1960 na kumalizika 1965.

## Matatizo na Wasiwasi wa baada ya vita

Mara baada ya vita, Afrika ya Kati haikuwakilishwa katika mkutano wa tano wa Umoja wa Waafrika uliofanyika Manchester mwezi Oktoba 1945. Hata hivyo, kimya hiki kilikuwa ni sura ya nje tu. Miaka ya vita ilijidhihirisha kuwa kipindi cha mateso makubwa. Mamlaka za kikoloni hazikusita kutumia njia za kikatili kabisa ambazo zilitumika mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Hata hivyo, wale kwa

kutumia fursa ya vurugu lililosababishwa na maasi ya Luluabourg, waliwakilisha madai yao kwa Mkuu wa Wilaya wakidai serikali iwatambue kama wasomi na walindwe na serikali tofauti na umma wa watu mbumbumbu. Kuanzia hapo dai la "hadhi maalumu" liliongezea nguvu idadi ya wasomi wenyeji. Dai hili linapatikana kwenye makala mengi yaliyochapishwa kwenye jarida maarufu la *La Voix du Congolais* lililoanzishwa Januari 1945.

Katika Kameruni, sehemu ya Wafaransa na ya kusini ndiyo hasa iliyoathiriwa na vita:- — upungufu wa bidhaa za chakula, uandikishaji wa lazima wafanyakazi kwa ajili ya mashamba, ujenzi wa barabara ya Donal-Yaounde-Abong, uchimbaji migodi na ugemaji mpira. Mnamo Agosti 1945, wajumbe wa kikoloni kutoka Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, Afrika Magharibi ya Kifaransa na Malagasi walikutana Duala kwenye Mkutano Mkuu wa Madola ya Kikoloni. Mkutano huu ulisaili haki zilizowekwa katika Mkutano wa Brazzaville na kutupilia mbali marekebisho yote yalipangwa kutekelezwa. Kwa upande mwingine, mnamo Julai 1945, shirikisho la vyama vya wafanyakazi, lililounganisha vyama vyote vya wafanyakazi, liliundwa na kuanza kupambana na utawala wa wakoloni, Makasisi wa Kikatoliki na Walowezi. Septemba 1945 pande zote mbili zilikabiliana wakati wa mgomo wa reli na ghasia katika Duala. Gavana Nicolas aliwaruhusu wakoloni wa Kizungu kutwaa silaha na kuunda kikosi cha polisi, na hivyo kuhalalisha mauaji makubwa. Chama cha umma cha kwanza cha kisasa, *Union des populations des Cameroun* (UPC) hakikuundwa hadi 1948. Kilikuwa sehemu ya *Ressemblement democratique africain* (RDA) ambacho nacho kilishirikishwa kwenye chama cha Kikomunisti cha Kifaransa, na kilikuwa na mbiu-kauli kali zaidi —"Muungano na Uhuru mara moja".

Haijulikani sana watu wa mashambani walikuwa na mawazo gani, lakini yaelekea walitawaliwa na upinzani baridi dhidi ya wawakilishi na ishara za ukoloni. Haya yalitokea hasa kwenye maeneo kulikozuka matapo ya kimasiha na ya kimseto. Katika Kongo ya Wabelgiji, watu wa Kongo waliendelea kuwa watiifu kwa Simon Kimbangu (k.1881 - 1951.) Aidha, mara tu baada ya kuzinduliwa kwa chama cha Abako *(Association des Bakongo)* mwaka 1950, kiliungwa mkono mara moja na umma. Katika Kongo ya Kati kulikuwa na tapo jingine la aina hiyo lililojulikana kama *Amilcalism* au *Matsouanism*. Baada ya kifo cha mwanzilishi wake, Andre Matsoua mwaka 1942, na kuzimwa kwa wafuasi wake, watu wa Lari, ambao walikuwa watii kwake, walisambaratika na kukataa kushiriki kabisa katika aina zote za siasa hadi 1956.

1 R. Pelissier, 1970, uk. 211-27

Huko Gabon, Gavana alitaka kutumia wenyeji wa mashambani na machifu wa jadi dhidi ya wakazi wa mijini. Ili kutekeleza azima hii, aliitisha Mkutano wa kwanza wa Pahouin huko Mitzik, Februari 1947. Mkutano huu ukaugeukia utawala wa kikoloni na kuchagua, kwa kura nyingi sana, mwakilishi wa watu wa mjini Léon M'Ba, kuwa *N'Zoe Fang* (chifu wa Fang) pekee. Hii ilikuwa dalili ya kwanza ya mshikamano kati ya wakazi wa mjini na vijijini, uliokuja kuanzisha matapo ya kitaifa katika Afrika ya Kati ambayo yalikuwa imara sana katika miaka ya hamsini.

## Kukua kwa uchumi, mabadiliko ya kijamii na mivutano ya kijamii

Katika muongo uliofuata Vita Vikuu vya Pili, tawala za kikoloni zilizokuwa katika michakato ya kujenga upya chumi zao, zilitegemea zaidi himaya zao. Ukuaji wa uchumi ulikuwa muhimu katika makoloni yote, ingawa hili halikusaili miundo ya unyonyaji wa kikoloni. Kutokana na tofauti za maendeleo ya uchumi na ya sera, aina mbali mbali kadha za ukuaji na za miundo hazina budi kutofautishwa.

Katika chumi za makoloni, ambazo zaidi zilikuwa za kilimo, uzalishaji wa kibepari ulistawi katika maeneo yaliyokaliwa na wakoloni wa Kizungu, na kuwageuza wakulima waliopokonywa ardhi yao huwa vibarua wa mashambani. Makoloni yaliingizwa ndani ya mfumo wa kibepari wa kimataifa kupitia *economiede traite* au uchumi poraji, yaani, kuunganisha uchumi kandamizi wa biashara wa uliotawaliwa na wakoloni, kibepari na uchumi usio wa kibepari wa kilimo.

Nchi ndogo zilizoonekana kuwa maskini kwa madini (Guinea ya Ikweta, Sao Tome na Prinsipe, Rwanda na Burundi) zilifaa kwa unyonyaji wa aina hii. Ni Sao Tome na visiwa vya Prinsipe tu vilivyokuwa na uchumi wa mashamba makubwa. Kwingineko, uzalishaji ulikuwa wa kiwango cha vishamba vya kifamilia[1] Kahawa, kakao, ndizi na mbegu za mafuta yalikuwa ndiyo mahuruji makuu ya Sao Tome na Prinsipe na Guinea ya Ikweta. Rwanda na Burundi zilikuwa na wakazi wengi mno, kiasi kwamba wakulima kwanza walidhamiria kuondosha njaa (za mwisho zikiwa katika 1916 na 1931), halafu kuzalisha mazao ya kusafirisha nje kama kahawa na chai.

Uchumi wa aina hii unaweza kupatikana pia katika nchi kubwa kama Kameruni, Afrika ya Ikweta ya Kifaransa na Angola. Raslimali za madini zilikuwa bado hazijagunduliwa isipokuwa katika Angola. Baada ya kunyongwa kabisa na kutelekezwa na Dola, Afrika ya Ikweta ya Kifaransa ilipata ahueni katika hali yake. Kutokana na mapendekezo ya mkutano wa Brazzaville, mpango wa miaka kumi uliandaliwa kwa utaratibu wa Mfuko wa uwekezaji wa Maendeleo ya Nchi

za Nje, FIDES (*Fond d'investissement et de development economique et social des Territoires d'Outre Mer),* kwa makusudi ya kuendeleza miundombinu. Katika Kameruni, hata kama kilimo kiliendelea kuwa nguzo ya uchumi, FIDES iliwezesha maendeleo ya viwanda vidogo vidogo vilivyotegemea aluminiamu na usindikaji wa samli. Kameruni ilipopata uhuru wake, viwanda hivi vidogo viliwakilisha asilimia 10 ya pato la taifa.[2]

Kutokana na mahuruji ya kahawa (asilimi 40 mwaka 1962) na mazao anuwai, kilimo kiliendelea kuwa chanzo kikuu cha fedha za kigeni katika Angola. Hata hivyo uchimbaji migodi ulikuwa unaendelea vyema; pamoja na almasi, chuma na mafuta yaliongezwa. Ureno iliendelea kuwa mnufaishwaji mkuu wa unyonyaji huu wa baadaye: mwaka 1960 asilimia 50 ya maduhuli ya Angola yalitoka Ureno. Sekta za Wazungu za uchumi wa Angola zilifaidika mno kutokana na ukuaji huu wa uchumi. Baada ya vita uhamiaji wa Wazungu uliongezeka mfululizo, idadi ya Wazungu ilipanda toka 44,803 mwaka 1940 hadi takriban 335,000 mwaka wa 1974[3] Angola ilikuwa nchi ya ufanisi wa mali kwa karibu Wazungu wote waliokuwa na msingi wa wastani: robo tatu ya mpango wa 1959 - 1964 wa uwekezaji ulikwenda kuendeleza sekta zilizodhibitiwa na wakoloni. Baada ya vita, hatua ya kufanya uchumi uwe wa kimataifa ilianza kutokea, na iliendelezwa zaidi kuanzia 1962 na uwekezaji wa mtaji wa Uingereza, Marekani na Afrika ya Kusini na upanuzi wa biashara na nchi za OECD.

Kuanzia mwaka 1930 uchumi wa Kongo, uliokwisha ingia kikamilifu katika zama za viwanda, ulikuwa na tabia kadha tawala ambazo zilibakia vivyo hadi uhuru; ubadhirifu na ububu, kukolezwa katika mikoa na sekta fulani tu, udhibiti wa vitega uchumi na idadi ndogo ya makundi ya wenye mitaji, ushiriki kamili wa Dola la kikoloni. Baada ya kusitishwa na mgogoro wa kiuchumi wa miaka ya 1930, uchumi wa Kongo ulirudi tena kukua kutokana na Vita Vikuu vya Pili na kutokana na hali ya kimataifa na hali ya uchumi wenyewe. Baada ya hili ikafuata "awamu ya upanuzi usiokikomo wa mfumo wa uzalishaji."[4] Awamu hii iliainishwa na mambo makuu matatu:

(1) Ukuaji wa haja katika sekta ya uchimbaji migodi (kielezo cha 100 mwaka 1950, 175 mwaka 1959) uliowezesha viwanda kuongeza mishahara halisi kwa wafanyakazi wa Kiafrika.[5]

[2] R.A. Joseph, 1977, uk. 11-18
[3] G. J. Bender, 1978, uk. 229
[4] E. M' Bakolo, 1981a, uk. 5
[5] J.L. Lacroix, 1966, uk. 22

(2) kuendelea kwa soko la ndani kulikohusishwa na kuboreshwa kwa jumla kwa mishahara kufuatana na ile ya wachimba migodi.
(3) kuendelea kwa sekta ya viwanda (kielezo cha 100 mwaka 1950, 260 mwaka 1956).

Kunako mwaka 1958, kilimo cha biashara kiliwakilisha asilimia 44.6 tu ya pato ghafi la taifa, migodi 19.8% , viwanda mahuruji 18.8% na soko la ndani 16.8%[6]. Uchumi wa Kongo hata hivyo ulikuwa bado umeathiriwa na utawala wa kikoloni kwa kutumia mabavu kama kimbilio la mwisho na kusigana kukubwa kati ya Waafrika na Wazungu. Waafrika wakiwa asilimia 99 ya watu wote, walidhibiti asilimia 5 tu ya mtaji uliowekezwa, asilimia 55 ya mishahara, 69% ya matumizi, na asilimia 12 ya akiba za binafsi.[7]

Mabadiliko katika jamii yaliyoambatana na mabadiliko haya ya uchumi pia yalikuwa ni pamoja na maendeleo ya jumla ya shule na utawala, na kiasi cha mabadiliko haya kilijumlisha vipengele vilivyoashiria mgogoro halisi.[8]

Ukidhihirisha mgogoro wa kudumu wa jamii za kikulima, ukimbiaji wa mashamba ulikuwa pia katika kiini cha mgogoro mpya, ule wa jamii za mijini. Katika Kongo ya Ubelgiji mlinganyo wa wakazi wa jiji ulipanda kutoka asilimia 8.8 mwaka 1938 hadi 14.8 mwaka 1945 na 24 mwaka 1955[9] Japo ulitokea polepole mahali pengine, uhamiaji mijini kila mahali ulijenga tabaka la wafanyakazi na hasa nusu-wafanyakazi (wasio na ajira ya hakika), idadi ambayo iliongezeka sana baada ya mabadiliko ya kiuchumi ya katikati ya miaka ya hamsini. Hivyo katika Angola mwaka 1960, mtu mmoja kati ya Waafrika watatu alikuwa anaishi katika makazi ya magenge katika maeneo ya miji. Katika maskani ya wenyeji ya Lobito (wakazi 20,000 mwaka 1954), kulikuwa na bomba la maji moja kwa watu 1,200. Katika Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, uundaji wa matabaka ya wafanyakazi ulichapuka baada ya 1954. Tabaka la wenye mishahara liliendelea haraka, ingawa tabaka hili la kijamii halikuwa salama kabisa, likiongezeka toka wafanyakazi waajiriwa 180,000 mwaka 1947 hadi 193,000 mwaka 1950, lakini likapungua hadi 135,000 mwaka 1954 na halafu kupanda tena hadi 190,000 mwaka 1958[10]. Wafanyakazi na vibarua walikuwa takriban ndio waliounda idadi hii, na ukosefu wa ajira ulikuwa wa juu sana. Katika Kameruni kama katika Kongo ya Wabelgiji, hali ya mambo ilikuwa vivyo.

[6] J.L. Lacroix, 1966, uk. 22
[7] F. Bezy (na wenziwe), 1981, u. 11
[8] Kuhusu Kongo ya Kibdajiji, tazama uchambuzi wa M. Murlier, 1962, 89-103, 145-64 na 231-49.
[9] Kama hapo juu uk. 47
[10] E. M'Bokolo, 1981b, uk. 401

Kama ukimbiaji mashamba ulikuwa unayaondoshea mashamba wafanyakazi na vijana wake, hali ya jumla ya jamii za kilimo ilitafautiana sana kati ya mkoa na mkoa. Kwa mfano, kiasi cha ukwasi wa wakulima wa kakao wa Beti - Bahu hakikufanana kabisa na ukata ulioinyemelea jumuiya ya wakulima ya Basa katika Kameruni.[11] Katika Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, wastani wa pato la mwaka kwa takriban wakulima wote ulibadilika kati ya faranga za CFA 1,800 na 2,100, ambapo ujira wa Mfanyakazi ulikadiriwa kuwa faranga 36,000.[12] Kuhusu Kongo ya Wabelgiji, sehemu ndogo ya jamii ya wakulima ilihama kutoka uzalishaji mdogo wa kibiashara hadi ubepari mdogo wa kilimo, wengi wa watu hawa wakiwa wamenufaika kutokana na hatua zilizochukuliwa kuunda jumuiya za kilimo za wenyeji.

Mabadiliko haya ya kijamii pia yaliibuka na ujenzi wa tabaka la kati la matajiri weusi katika ile mikoa iliyokuwa na sera za maendeleo ya uchumi na elimu. Hivyo, watu wa pwani waliokwisha kuwa na uhusiano wa muda mrefu na Wazungu, waliokwishasomeshwa katika shule za misioni na za serikali, walikuwa sehemu ya wapokea mishahara wa tabaka la kati miongoni mwa watumishi wa serikali na makarani. Katika Kongo ya Wabelgiji, pengo la aina hiyo hiyo lilijitokeza ambapo majimbo ya Savana ya kusini yalipendelewa yakilinganishwa na misitu ya Kaskazini. Mamlaka ya kikoloni yalijaribu kutumia tabaka hili kama kundi la kusaidia kupunguza mivutano ya kisiasa iliyokuwa inaendelea. Ni dhahiri hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa upande wa wakoloni wa Kongo ya Kibelgiji waliotoa pendekezo juu ya suala hili kwa serikali ya kikoloni. Katika Kongo ya Kibelgiji, baadhi ya nyaraka zilirekodi wafanyakazi wa tabaka la kati 176,000 kati ya jumla ya watu milioni 13, ingawa nyaraka nyingine zilikadiria wafanyakazi 300,000[13]. Ukaguzi wa ziada wa tarakimu hizi unaonyesha kuwa idadi ya wafanyakazi walipwa mishahara ambao ujuzi wao ulipatikana katika shule za kikoloni, ilizidi ile ya "wajasiriamali" ambao jitihada zao hazikufanikiwa mbele ya mfumo wa kikoloni uliowabana na kuwabagua. Ni hawa hawa walioongoza matapo ya kudai uhuru.

## Matendo ya Kikoloni: uendelezi na kuachana na ukale

Tangu vita kuisha, baadhi ya wakoloni waliweza kuhisi kuwa mageuzi ya kimuundo yalikwishatukia katika jamii za kienyeji, na kwamba mabadiliko yasiyoweza

[11] .A. Joseph, 1977, uk. 124-41
[12] E. M'Bokolo, 1981a, uk. 10-11, F. Bezy 1981, uk. 41-5
[13] E. M'Bokolo, 1981a uk. 3

kurudishwa nyuma yamekwisha fanyika katika fikra za watu. Hata hivyo, mamlaka za kikoloni zilitenda tofauti kufuatana na jadi, hadhi ya koloni linalohusika na maelewano kati ya wahusika.

Katika Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, licha ya tabia bainifu zisizokuwa na mjadala, Wafaransa walisimamia kidete mwongozo wao wa jumla wa sera yao kwa Afrika. Afrika ya Ikweta ya Kifaransa iliweza kufurahia "sheria kuu za uhuru wa bindamau"[14] zilizopitishwa na Jamhuri ya Nne: kukomesha kazi za lazima, utambuzi wa vyama vya wafanyakazi, Waafrika kupewa uraia wa Kifaransa, kuanzishwa kwa mabunge ya kienyeji katika Gabon, Kongo ya Kati, na Ubangi - Chari, na Baraza Kuu katika Brazzaville. Afrika ya Ikweta ya Kifaransa iliwakilishwa na wabunge kadha katika Bunge la Kifaransa na katika Baraza la Muungano wa Kifaransa. Licha ya kuwa Waafrika walio wengi waliachwa katika orodha ya wapiga kura, siasa ilikuwa sehemu ya maisha ya kila siku. Vyama vya siasa viliundwa na uchaguzi ukawa fursa ya malumbano kati ya watu wenye maoni tofauti. Katika Ubangi - Chari na Gabon, ambako kulikuwa na wakoloni wengi kulikuwa na ukinzani wa sera hii mpya, na Utawala haukuwa na haraka kutekeleza hatua mpya: kazi za lazima ziliendelezwa kwa sura ya kificho, wanasiasa walioonekana kuwa huru mno walisumbuliwa, na waliokuwa wastani waliungwa mkono.

Katika Kongo ya Wabelgiji, mamlaka za kikoloni ziliendelea kushikilia sera zao za ubaba zikishirikiana bega kwa bega hadi katikati ya miaka ya hamsini na utawala wa kikoloni, makampuni makubwa na misioni za Kikatoliki. Yakiwa yamebatizwa jina la "utatu wa Kikoloni"[15], makundi haya matatu yalishikamana kwa karibu mno. Mahusiano kati ya dola na makampuni makubwa, hasa makampuni ya 1906 yaliyotawala uchumi wa koloni, yamekwisha tajwa tayari. Misioni za Kikatoliki zilijinufaisha na mapatano yaliyotiwa sahihi mwaka 1906 baina ya Leopold II na Vatican, na hivyo zilikuwa na uzito mwingi: maaskofu wakuu wa koloni ndio hasa waliobuni itikadi ya kikoloni, na misioni ziliwakilishwa na wajumbe zaidi katika "Baraza la Kikoloni" huko Brussels. Vyama vya wanafunzi wa zamani iliongezea uzito huu kwani kwa kutokuwa na vyama, ambavyo vilikatazwa kisheria, vyama vya wanafunzi vilikuwa maabara halisi ambamo takriban viongozi wa baadaye wa matapo yote ya kitaifa waliandaliwa. Kufuatana na misukosuko ya 1944-1945, mamlaka za kikoloni zilikubali mabadiliko machache, lakini kwa kuwa hazikujali

[14] Msemo uliotumiwa na P. Aujoulat, 1956, uk. 263

[15] M. Makombo, 1977, uk. 54

JEDWALI: 8.1 *Wanasiasa katika Nchi za Kiafrika za Ikweta zinazozungumza Kifaransa, usuli wa shughuli zao.*

| | Afrika ya Kiikweta ya Kifaransa 1952 | 1957 | Kongo ya kati 1946-60 |
|---|---|---|---|
| *Wazungu* | | | |
| Wafanyabiashara | 32 | 28 | 12 |
| Wakulima, wapasua mbao | 13 | 3 | 1 |
| Watumishi wa Serikali | 18 | 10 | 8 |
| Wanataaluma ya uhuru | 6 | 7 | 2 |
| Waandishi wa habari | - | 3 | 4 |
| Wasio na kazi maalumu | - | 1 | 1 |
| *Waafrika* | | | |
| Waganga (shule ya uganga ya Dakar) | - | 6 | 2 |
| Walimu wa shule ya msingi | 10 | 34 | 25 |
| Wauguzi | 9 | 20 | 5 |
| Mtawala wa ngazi ya juu | 1 | 7 | 3 |
| Makarani watawala waajiriwa | 33 | 36 | 18 |
| Mafundi sanifu | 1 | 8 | 5 |
| Makatibu wa machifu | - | 2 | - |
| Machifu na wanajamii maarufu | 18 | 14 | 4 |
| Watu walioajiriwa katika sekta za binafsi | 13 | 19 | 25 |
| Wafanyakazi | - | 2 | 5 |
| Wauza maduka, wauza migahawa | 9 | 13 | 10 |
| Wakulima, wapasua mabao | 8 | 11 | 4 |
| Waandishi wa habari | - | 1 | 1 |
| Waajiriwa binafsi wengine | 1 | 1 | 1 |
| Wastaafu | 3 | 3 | 1 |
| Makasisi na mapadri | 1 | 2 | 4 |
| Wanafunzi | - | - | 1 |
| Wasio na kazi | - | - | 1 |
| Wasio na kazi maalum | - | 2 | 14 |
| Jumla | 176 | 233 | 157 |

*Kumbukumbu*
Kwa upande wa Afrika ya Ikweta ya Kifaransa hii inajumuisha wajumbe wa bunge na wa baraza la Muungano wa Ufaransa, wajumbe wa baraza kuu na wajumbe wa nchi (1952), kwa kuongezea, katika mwaka 1957, Mameya na wasaidizi wa mameya wa jamii kamili na wajumbe wa baraza la serikali. Kwa upande wa Kongo ya Kati, sampuli pia ilijumuisha wagombea walioshindwa katika uchaguzi wa makundi haya na viongozi wa vyama.

*Chanzo: Annaire Plitique de l'AEF 1952 na 1957); J.M. Wagnet, 1963, uk.233-47; na E.M. Bikolo, 1981 b, uk.400*

hali ya kisiasa ya mvuvumko wa baada ya vita, mabadiliko haya yaliathiri vipengele vidogo tu, vya maisha. Licha ya uteuzi wa wawakilishi weusi kwenye mabaraza ya majimbo na katika serikali, Wabelgiji waliendelea na imani yao kuwa "hakuna

wasomi hakuna matata". Ni mpaka 1952 ndipo mtu mweusi kutoka Kongo alipoidhinishwa kwa mara ya kwanza kwenda Ubelgiji kusoma katika Chuo Kikuu.

Chini ya kivuli cha usimilishaji wa kinadharia, mamlaka zilizojijenga katika Angola, Sao Tome na Prinsipe, na Guinea ya Ikweta, ziliendeleza ubabe mkali kudumisha hali iliyokuwepo. Likifikiriwa kama taifa la Ureno, kulikuwa na tofauti ya kisheria katika Angola kati ya wenyeji wasiosimilishwa na waliosimilishwa, hawa wa pili walitunukiwa haki zote zilizoambatana na uraia wa Kireno, lakini pamoja na mengine yote walipaswa kujua kusoma na kuandika kwa Kireno, kukana maisha ya kikabila, kuwa watiifu kwa Dola, na wawe wamezaliwa katika ndoa halali kama walikuwa machotara.

Ingawa weupe wote na asilimia 90 ya machotara walikuwa na hadhi ya *assimilados*, lakini chini ya asilimia moja ya weusi walitunukiwa hadhi hii ya fahari. Asilimia 99 ya waliobaki walikuwa *indigenatos* na hivyo walipaswa kufanya kazi ya lazima. Ama kuhusu mfumo wa Kihispania wa *patronato de indigenas*, huu ulijengwa kwenye imani kwamba weusi walikuwa watoto wadogo kiadili, kiakili na kisheria, na ingawa kadi kadha za ukombozi zilitolewa, lakini idadi ilikuwa ndogo sana.

Baada ya kuwekwa chini ya udhamini, hali ya nchi zilizodhaminiwa, ilifafanuliwa, na kinadharia ilifanywa bora kwa misingi ya katiba ya Umoja wa Mataifa. Kifungu cha 76 cha Katiba ya Umoja wa Mataifa kiliamua kuwa mataifa yaliyokabidhiwa nchi hizo yalipaswa "kukuza ... mfululizo wa maendeleo yao kuelekea kujitawala au uhuru." Licha ya usimamizi wa karibu na Umoja wa Mataifa, kasi na aina za mabadiliko zilitofautiana kati ya nchi na nchi. Sehemu ya Kifaransa ya Kameruni ilipata mabadiliko yaliyotolewa na Ufaransa kwa himaya yake yote ya Afrika. Hata hivyo ilikuwa ni lazima kungojea hadi mwaka uliofuata kushuhudia mabadiliko ya aina ya Togo, yaliyoitwa "Jamhuri yenye kujitegemea chini ya udhamini kwa sheria ya muhtasari" ya 1956. Baada ya kuunganishwa na Nigeria na Waingereza, Kameruni ya Magharibi ilibidi isubiri kuona matumaini ya serikali ya ndani yanavyojengeka. Katika Rwanda na Burundi, Wabelgiji waliendeleza sera yao iitwayo "urazinishaji" na "usasishaji" kuhusu miundo ya kisiasa ambayo kuanzishwa kwayo kulichochea mivutano kati ya Watutsi na Wahutu katika nchi zote mbili.[16]

[16] R. Lemarchand, 1970, uk. 118-79 na 315-23

## Maendeleo kuelekea uhuru

Ingawa kujinasua na ukoloni katika mifano mitatu ya Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, - Guinea ya Kihispania na nchi zinazodhaminiwa na Ubelgiji, kulitekelezwa kwa amani, katika mifano miwili — Kameruni na Angola — vita vya ukombozi ilibidi vipiganwe kuzilazimisha serikali za kikoloni kujadiliana. Kongo ya Kibelgiji inawakilisha hali ya katikati: baada ya machafuko, majadiliano yalianza kwa lengo la kuondosha ukoloni.

Katika Ikweta ya Kifaransa, hatua ya kuelekea uhuru ilidhibitiwa na mamlaka za Kifaransa. Vikundi vya kisiasa vya wenyeji viliundwa kimsingi na tabaka la kati la chini linaloinukia, lililofanikiwa kwa kiasi fulani tu kuhamasisha umma. Hata hivyo MESAN, kilichoanzishwa na Barthelemy Boganda, kilikusanya wanachama toka miongoni mwa waajiriwa wa kima cha chini cha mshahara, umati wa mijini na umati wa wakulima maporini, na kupendekeza uundaji wa vyama vya ushirika.[17] Vyama vya Kiafrika vya Afrika ya Ikweta, hata hivyo, viliungwa mkono na umma kutokana na kujishirikisha kiasi na RDA (isipokuwa kwa chama cha MESAN), chama ambacho kilikuwa na urafiki na chama cha Kikomunisti cha Kifaransa, na kwa sababu ya msimamo wa kipinga maendeleo ulioshikiliwa na wakoloni wa Kifaransa. Kamishna Mkuu kutoka 1951 hadi 1958, Paul Chauvet, alichukua hatua zinazofaa kuvunja ubaguzi wa rangi wa weupe na kuleta uhusiano mwema na waali wa Kiafrika. Sheria ya muhtasari ilipopitishwa mwaka 1956, waali hawa walikubali uhuru wa kisiasa bila uhasama wowote kwa Ufaransa na bila haja ya kuvunja uhusiano wa kimuundo na mamlaka ya kikoloni ya zamani. Kunako Agosti 1958, mara kabla ya kura ya maoni ya de Gaulle ya kuasisi "jumuiya" waali hawa walipeleka waraka mrefu kwa Jenerali de Gaulle ambamo walitukuza kazi ya "kustaarabisha" ya Ufaransa. Walikuwa na haki ya kudai uhuru hatimaye, lakini wakatafakari busara ya kuendelea na asasi za shirikisho. Akiwa rais wa Baraza Kuu la Afrika ya Ikweta ya Kifaransa, Barthelemy Boganda alipendekeza shirikisho la karibu sana baina ya makoloni manne ya zamani ya Kifaransa. Chini ya jina la "Jamhuri ya Afrika ya Kati" hii ilikuwa ni hatua ya kwanza kuelekea kile alichokiita Muungano wa Madola ya Afrika ya Kilatini (au ya Kati) zikiwemo pia Kongo ya Kibelgiji, Kameruni, Angola, Rwanda na Burundi. Mpango haukufanikiwa, zaidi kutokana na Gabon: kwa kuwa haikuwa maskini sana, Gabon iliogopa kujikuta inabeba mzogo wa kifedha wa shirikisho la baadaye. Kifo cha Boganda tarehe 29

[17]Kalek, 1977

Aprili 1959 kilipuliza parapanda la kifo cha matumaini ya shirikisho. Hatimaye nchi za Afrika ya Ikweta ya Kifaransa ziliendelea kila moja peke yake kuelekea uhuru.[18].

Uhuru wa Guinea ya Ikweta na ule wa Sao Tome na Prinsipe pia ulipatikana kwa kusimamiwa na mamlaka ya kikoloni. Katika Guinea ya Ikweta madai ya kitaifa yalianza kusikika kwa mara ya kwanza mwaka 1950, chama cha Cruzada Nacional de Liberacion kilipoanzishwa, kikiwa na wanachama mawakala wa utawala wa kikoloni. Majibu ya Hispania yalikuwa ni kuacha mambo yalivyo, na baada ya kujiunga na Umoja wa Mataifa mwaka 1955, ikawa inashambuliwa mara kwa mara na kundi la Kiafro-Asia, lakini iliungwa mkono na Marekani. Ukandamizaji uliishia na mauaji ya viongozi wawili wa kitaifa mwaka 1958 na 1959, na mamia ya Waguinea kukimbilia Gabon na Kameruni kwa usalama wao. Vyama viwili vikuu vilikuwa na maofisa wachapakazi na watu walioviunga mkono nje ya nchi, na vilipata msaada kutoka nchi zilizokwishapata uhuru karibuni kuanzia 1960. Baada ya kukabiliwa na wahaka wa kijamii, Hispania polepole ikasalimu amri. Mwaka 1963, ilitambua vyama vya siasa kabla ya kukubali kanuni ya kujitawala Mwaka 1964, halafu tarehe 12 Oktoba 1968 uhuru ulitangazwa.

Katika Sao Tome na Prinsipe, tapo la kwanza kuu la umma kujitokeza lilizimwa vikali mwaka 1960. Mwaka 1964, OAU ilitambua rasmi Kamati ya Ukombozi ya Sao Tome na Prinsipe (MLSTP). Baada ya "Mapinduzi ya Maua (Mekundu)" ya tarehe 25 April 1974, tapo hili lilishiriki katika majadiliano yaliyopelekea kupata uhuru (Julai 12, 1975).

Katika Rwanda na Burundi, Umoja wa Mataifa, kama mamlaka ya udhamini, ulitekeleza dhima yake kikamilifu, ingawa pamoja na mvuvumko wa mivutano ya kimbari ambayo matendo ya kikoloni yaliihimiza[19] . Katika Rwanda, Wahutu walioelimika waliandaa mashambulizi juu ya Watutsi, ambao si tu walikuwa makabaila wa kisiasa bali pia walikwisha simikwa na Wabelgiji katika nafasi za madaraka, za kidini na za kiutawala. Mwaka 1957 Wahutu wasomi tisa walichapisha ilani ambamo walitaja chuki yao kwa "ukiritimba wa kisiasa kiuchumi kijamii na wa kiutamaduni wa Watutsi" na kuunga mkono kwao kwa "maendeleo halisi ya Wahutu". Huu ndio uliokuwa msingi wa vyama vilivyokuwa vinaibuka, APROSOMA (Chama cha Ukuzaji wa Kijamii wa Umma) na PARMEHUTU

[18] Kongo Agosti 15, 1960; Gabon Agost 17, 1960, Jamhuri ya Afrika ya Kati Agosti 13, 1960

[19] R. Lemarchand, 1970 uk. 188-76 na 324-42

(Chama cha Tapo la Ukombozi wa Wahutu). Watutsi walijibu kwa kung'ang'ania marupurupu yao jambo ambalo lilizaa migongano ya hatari mwezi Novemba 1959, iliyochochewa na Wahutu. Katika Burundi, vyama vya siasa viliundwa kwa misingi ya kiitikadi dhidi ya kimbari. Kunako Novemba 1959, serikali ya Ubelgiji, ikiathirika na matukio katika Kongo, iliainisha hatua ambazo zingezifikisha nchi hizi zilizodhaminiwa kwenye ukombozi. Tamko hili liliumua hasira katika Rwanda, na kipindi cha hadi Julai 1962 kilitapakaa mapambano makali. Ugumu wa ziada ulitokana na Serikali ya Ubelgiji ambayo, kwa kuvunja sera yake ya jadi, ilianza kuunga mkono Wahutu. Uchaguzi wa serikali za mitaa katika Juni na Julai 1960 ulikuwa ni ushindi kwa Wahutu. Hata hivyo ikishawishiwa na Baraza Kuu la



*Picha 8.1 Mwami Kigerri V. Mfalme wa kwanza Rwanda*

Umoja wa Mataifa, serikali ya Ubelgiji iliamua kuahirisha bila muda maalumu uchaguzi uliopangwa tarehe 28 Januari. Tarehe hii "Mapinduzi ya Gitarama" yalitangaza kuundwa kwa Jamhuri, uchaguzi wa mara moja wa serikali na mkuu wa nchi, na kupitisha katiba. Katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 1960 katika Burundi UPRONA (Chama cha Umoja na Maendeleo ya Taifa) huenda kilifisidiwa na kushinda asilimia 19 ya viti vyote. Lakini kilishinda ushindi komesha katika uchaguzi mkuu wa bunge wa Septemba 1961; na serikali ya ndani ilitolewa Desemba 1961. Umoja wa Mataifa haukufanikiwa kuhifadhi muungano kati ya Rwanda na Burundi.

Katika Kongo (Zaire), baada ya machafuko katili ya baada ya vita, haja ya kujiwekea taratibu ilijitokeza, lakini kwa kuwa vyama vya siasa vilikuwa bado vimepigwa marufuku, Wakongo walitumia taratibu mbili maalum: vyama vya wanafunzi wa zamani na jamii za jadi. Vyama hivi vilivyoanzishwa muda mrefu sasa viliingia upeo wa ustawi; vijana wasomi wa Kikongo waliozoea kuwa chini ya malezi ya wamisionari muda wote, wakaambukizwa tabia mbaya ya kuwasilisha kila kitu kwa washauri. Vyama vya kitamaduni navyo vilikuwako kama ABAKO *(Association des Bakongo)* na *Lulua Freres.* Matendo ya wakoloni yalipata matatizo kuanzia mnamo 1955 na kuendelea; sera ya kutochanganya siasa na dini ya waziri mpya wa makoloni ilivunja urafiki kati ya Dola na Kanisa, na magomvi ya lugha baina ya Waflemishi na Wawallooni yakaweka hadharani migawanyiko miongoni mwa wakoloni. Kama inavyoonyesha katika maandishi ya Patrice Lumumba, Waafrika wasomi waliendelea kuamini itikadi ya kikoloni na imani ya jumuiya ya Wabelgiji - Wakongo. Mwanaakademia asiyejulikana Van Bilsen, ndiye aliyefufua mjadala na kuwashawishi baadhi ya Waafrika kuchukua misimamo mikali kwa kuchapisha *Plan de trente ans pour l'emancipation politique de l'Afrique belge* (Mpango wa miaka thelathini kwa ukombozi wa kisiasa wa Afrika ya Kibelgiji). Kundi la Kikatoliki, *Conscience africaine,* lilikubali tamshi la tatizo na ratiba iliyoandaliwa ndani ya mpango, ambapo ABAKO, kikiongozwa na mwanaseminari wa zamani Joseph Kasavubu, kilihitimisha kuwa ukombozi upatikane mara moja. Kunako Desemba 1957, serikali ya kikoloni iliendesha uchaguzi wa serikali za mitaa, lakini ikaishia katika miji mikuu na wilaya za wenyeji, ikiwaacha Wakongo wapigane wenyewe kwa wenyewe, jaribio ambalo lilikoleza migawanyiko ya kimbari. Vyama vya siasa vikaanza kujitokeza wakati huo. Kunako Oktoba 1958, Patrice Lumumba alianzisha *Mouvement national congolais* (MNC), chama pekee kilichokuwa na msingi wa kitaifa. Mgogoro wa kijamii, uliokuwa ukitokota tangu 1957, ulilipuka katika maasi ya makazi ya Waafrika ya Leopoldville (Kinshasa)



*picha 8.2 Kutoka kuhoto hadi kulia: Joseph Kasav[illegible] rais wa Kongo, Waziri Mkuu Patice tumumba, na mfalme Baudouin wa Ubelgiji, mjini Leopoldvil[illegible]sasa Kinshasa Kongo, June 1960*



*Picha 8.3 Viongozi watatu wa UPC (Union ds populations de Camerron): Kutoka kushoto: Ernest Ouandie, Felix Foland Moumie na Abel Kingue.*

kunako Januari 1959. Utawala wa Kikoloni uliporomoka, na kwa kuwa hawakuwa wamefikiria kumalizika kwa ukoloni, mamlaka ya Kibelgiji haraka haraka ikafaragua mpango wa ukombozi. Mkutano uliofanywa Brussels mwezi Januari 1960 uliweka Juni 30 mwaka ule ule kuwa tarehe ya uhuru. Wasomi wa Kikongo waligawanyika vikali baina ya wanamajimbo na Wanautaifa, wanashirikisho na watetezi wa mamlaka moja, wana-wastani na wana-siasa kali. Suluhu ilifikiwa: Mkuu wa dola Joseph Kasavubu aliwakilisha mielekeo ya kijimbo, kishirikisho na kiwastani, ambapo mkuu wa serikali Patrice Lumumba, aliwakilisha matakwa ya kitaifa, umoja, mapinduzi na muungano wa Waafrika. Hayawi yakawa; mgogoro ukatinga mara baada ya uhuru na kuzua vita ya wenyewe kwa wenyewe vya muda mrefu sana.

Katika Kameruni, na Angola, vita vya ukombozi vilileta zinduko kwa mamlaka za kikoloni kuhusu haja ya kutoa uhuru. Licha ya majaribio ya Ufaransa kuhimiza kuibuka kwa vikundi pinzani UPC *(Union des populations du Cameroon)* kiliongoza harakati za kitaifa katika Kameruni.[20]

Chama cha UPC kilikuwa unganishi, katika uanachama wake (wasomi, wakulima maskini, wauza maduka) na itikadi yake, ikiwa ya kitaifa yenye karaha ya Kimarx[21] Chama pia kiliweza kuongeza wafuasi wake kutokana na uhusiano wa karibu na CGT *(confederation generale des travailleurs)* cha Kifaransa na mashirika yake ya umma. Kipigo ulichokipata ukoloni wa Kifaransa mwaka 1954, kwa ushinde wa Dien Bien Phu na tukio la mapinduzi ya Algeria, vilishawishi UPC kuzindua shambulio pana mwaka uliofuata, lililoishia na "juma la damu" la Mei 22-30, 1955. Kirasmi kulikuwa na watu 25 waliokufa wakati wa kuzima mashambulio hayo, ingawa kwa kweli watu mara tano ya hao waliuawa. UPS na mashirika yake yalivunjwa, lakini yakakimbilia msituni, na vyama vidogo vya siasa za wastani vikajichukulia fursa hii, kushinda uchaguzi wa mwaka 1956. Kameruni baada ya kupandishwa hadhi ya "Jamhuri yenye kujitegemea chini ya udhamini" basi ikawa na Ahmadu Ahijo kama makamu wa rais, aliyeanzisha *Union Camerounaise*, ambacho kiliungwa mkono na vyama vya majimbo kadha, pamoja na kusimika kiini chake upande wa kaskazini. UPC kilianzisha mapambano mapya kunako Septemba 1957. Baada ya Ufaransa kuingilia kati, na kufuatia miezi 11 ya

[20] Rwanda na Burundi , 1 July 1961

[21] Baada ya RDA na Chama cha Kikomunist cha Ufaransa kutengana mwezi Oktoba 1950, uhusiano Kati ya UPC na RDA ulikuwa mdogo. Hata hivyo, UPC haikutengwa na RDA hadi July 2, 1955, wakati wa mkutano wa Kamati ya Uratibu ya RDP, Tazama R.A. Joseph, 1971, uk. 186-8 na 190-2

"kurejesha amani" ndipo Um Nyobe (mwasisi wa UPC) alipokamatwa na kunyongwa. Uhuru ulitangazwa tarehe 1 Januari 1960, lakini upinzani wa kichinichini wa vikundi vya UPC, na upinzani wa kisheria, ulikuwa bado hai. Nguvu hizi hazikupunguzwa hadi mwaka 1962, lakini mwisho wa vita vya wenyewe kwa wenyewe haukutangazwa hadi mwaka 1972. Wakati huohuo muungano na sehemu ya kusini ya Kameruni ya Waingereza ulikamilika. Umoja wa Mataifa uliendesha kura ya maoni Februari 1961katika nchi nzima iliyodhaminiwa na Uingereza. Kaskazini ilipiga kura kujiunga na Nigeria, ambapo kusini ilichagua kujiunga upya na Kameruni ya Kifaransa ya zamani. Katiba ya Oktoba 1, 1961 ilianzisha Shirikisho la Jamhuri ya Kameruni.[22]

Katika Angola, harakati za baada ya vita zilizimwa mara. Hata hivyo huko Ureno kwenyewe idadi kadha ya wasomi vijana wengi wao wakiwa karibu na chama cha Kikomunisti, waliendelea kuchochea moto wa kitaifa. Vikundi hivi vya kichinichini vilikua na hivyo kuwa vyama vya siasa; UNA (Muungano wa Watu wa Afrika ya Kaskazini) kilichoanzishwa mwaka 1954, baadaye kikawa FLNA (Chama cha Kitaifa cha Ukombozi wa Angola), MPLA (Tapo la Watu wa Ukombozi wa Angola) kilichoanzishwa mwaka 1956 na wahamasishaji wa vitendo, wengi wao walitokana na chama cha Kikomunisti cha Angola na Chama cha Mapambano cha Waafrika wa Angola. Vurugu za hatari za kwanza zilizuka mwaka 1950 na 1960, kufuatana na mchakacho wa ukombozi katika Kongo ya Wabelgiji, ambako wakimbizi wengi wa Angola walikuwa wakiishi; vurugu hizi ziliandamwa na kandamizo la kikatili sana. Mwaka 1961 maasi yalizuka katika sehemu kadha na Wareno wakajibiza kwa matumizi makubwa ya mabavu: kati ya watu 30,000 na 50,000 walikufa na Waangola 150,000 hadi 200,000 walifanywa wakimbizi katika Kongo[24] Wakati Wareno wakiendelea kukwamishwa na juhudi za kuzima vita vya msituni, tofauti kati ya wazalendo zilijitokeza wazi hadharani. Licha ya Ureno kuendelea kuungwa mkono na wanachama wa NATO, vita hivi, vikiongezwa na vile vya Guinea Bissau na Msumbiji, hatimaye vilidhoofisha uchumi-jamii wa Ureno na kuleta unyongonyevu wa kisiasa uliolipukia kwenye "Mapinduzi ya Maua (mekundu)" ya Aprili 25, 1974. Ikidhamiria kuchapusha mchakato wa kumaliza ukoloni, serikali ya Ureno ilibidi itatue tatizo la Wareno 335,000 (kati yao 172,000 machotara) waliokuwa wakiishi Angola na ambao uchumi wa Ureno usingeweza kuwapatia kazi. Zaidi ya haya, matapo matatu ya Kiafrika yalikuwa

[23] Taarifa kamili, tazama R. Pelissier, 1978, uk. 801-664

yamegawanyika sana; yakiongozwa na tabaka la kati la chini la wakazi wa mijini, FLNA na UNITA (Umoja wa Kitaifa kwa Uhuru Kamili wa Angola, ulioanzishwa mwaka 1966 na waasi wa FLNA) walikwisha jiimarisha vijijini zaidi na kwa misingi waziwazi ya kimbari. Kikiwa na uzoefu mpana wa kijamii na kuwa na mizizi imara mijini, MPLA peke yake kilikuwa na msingi wa kitaifa. Zaidi ya hayo raslimali ya nchi katika kilimo, madini na mafuta iliamsha uchu wa mataifa makubwa.

Kunako Januari 1975 tarehe ya uhuru ilipangwa, lakini mfarakano ulizuka tena, na vita kwa ajili ya Luanda vikaanza; vilidumu hadi Julai 1975, ambapo MPLA iliweza kuwatimulia wapinzani wake nje ya jiji. Uhuru ulitangazwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe vikachukua nafasi ya vita vya ukombozi. Mwaka 1976 MPLA iliifanya Jamhuri ya Watu wa Angola mwanachama wa OAU na wa Umoja wa Mataifa, ingawa majimbo kadha yalikuwa nje ya udhibiti wa mamlaka kuu.

# 9

# Mapambano ya Uhuru wa Kisiasa Afrika ya Mashariki, 1945 hadi Uhuru

Kwa madhumuni ya sura hii " Afrika ya Mashariki " haijumuishi tu makoloni ya zamani ya Waingereza ya Kenya, Uganda, Tanzania (wakati huo zikiwa nchi mbili tofauti, Tanganyika na Zanzibar), Malawi (wakati huo ikiitwa Nyasaland), na Zambia (wakati huo ikijulikana kama Rhodesia Kaskazini), bali pia hujumuisha kisiwa kikubwa cha Bukini (Madagascar), ambacho zamani kilitawaliwa na Wafaransa; pamoja na Visiwa vya Komoro na Reunion, na visiwa vya Maurutius na Ushelisheli, ambavyo hapo zamani vilitawaliwa na Waingereza. Katika Vita vya Pili vya Dunia, Kenya ilikuwa ndiyo kituo kikuu cha himaya ya Waingereza ya Afrika Mashariki, hasa baada ya Singapore kuchukuliwa na Wajapani. Tofauti kati ya "wenye nacho" na "wasio nacho" nchini Kenya zikaongezeka sana kadri jitihada za kuifanya nchi hiyo kuwa chanzo muhimu cha mali ghafi na chakula wakati wa kipindi cha vita huko Uingereza zilivyozidi kuongzeka. Tofauti hizi za ndani zilizokuwa zikizidi kuongezeka, baadaye zikawa ndiyo chanzo kikubwa cha mfano pekee muhimu sana wa maasi ya kupinga ukoloni yaliyowahi kutokea popote katika Afrika ya Tropiki dhidi ya Utawala wa Mwingereza: maasi ya Mau Mau. Lakini miaka mitano kabla ya mlipuko huo wa Mau Mau ukoloni wa Kifaransa katika kisiwa kikubwa cha Bukini ukapata mshituko mkubwa — nao ukiwa umeathiriwa sana na msukosuko wa Vita vya Pili vya Dunia ulioikumba dunia nzima — ambao ulichukua sura ya maasi ya Machi, 1947.

## Bukini[1]

Katika Bukini kulikwisha kuwepo na ukinzani makini dhidi ya ukoloni wa Kifaransa tangu mwanzo kabisa, na baadhi ya maeneo ya kusini katika kisiwa hicho hayakuacha mapambano hayo hadi miaka kumi baadaye. Kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia chama cha kizalendo cha siri kilianzishwa huko Tananarive kikijulikana kama *Vi Vato Sakelika* au V V S, katika Kimalagasi, (maana yake sisisi ni "shina la kijani la mwamba wa chuma")[2]. Wakati wa kipindi kati ya Vita vya Kwanza na vya Pili, chama hicho cha kitaifa kilijishughulisha zaidi na kudai haki sawa kati ya watu wa Bukini na raia wa Ufaransa. Ingawa sera ya Wafaransa ya kusimilisha (kuwafanya watu wajione kuwa Wafaransa) ilifanikiwa kwa muda katika kujenga tabaka bora la Wabukini ambalo Wafaransa waliweza kulishawishi kushirikiana nalo, lakini sera hiyo ilishindwa kabisa kufanya kazi kama mkakati wa muda mrefu. Ukoloni wa Kifaransa katika Bukini ukachochea utamaduni wa kitaifa na uzalendo kati ya wananchi wazawa ambao pengine, katika nchi zilizokuwa zimetawaliwa na Waingereza, ungeweza kulinganishwa tu na maasi ya Mau Mau katika Kenya. Vita vya Pili vya Dunia vikawawezesha wazalendo waali (wa tabaka bora) kuungana na umma katika kutoridhika na hali ya mambo ilivyokuwa.

Hii ilisababishwa na mambo kadhaa. Vita vya dunia nzima lilikuwa tukio ambalo lilimtia kila mtu kiwewe, hali ambayo ilikolezwa zaidi na madhila ya kushindwa. Mnamo mwaka 1940 utawala wa Kifaransa uliokuwepo pale ukatangaza kuwa chini ya utawala wa Vichy (huko Ufaransa), na mara tu Bukini ikawa katika hatari ya kuvamiwa na Waingereza na Wafaransa huru. Mnamo mwaka 1942 kisiwa hiki kikubwa kikavamiwa, na ingawa ugavana-mkuu wa Bukini ulikabidhiwa mteule wa de Gaulle, Waingereza walibaki katika kisiwa hicho hadi mwaka 1946. Makoloni yote ya Ulaya yakapata dhiki ya bidhaa za kutoka nje katika kipindi cha Vita vya Pili vya Dunia, na mfumuko wa bei uliotokana navyo pamoja na hali ya Bukini kama kisiwa kilichotekwa baada ya 1942 vikaleta matatizo zaidi katika ubadilishanaji fedha. Mwaka 1943-4 kulikuwa na njaa kali sana. Ingawa kulikuwa na mazungumzo mengi kuhusu namna ya kuyanufaisha makoloni, kwa mfano, mazungumzo yaliyofanywa katika Mkutano wa Brazzaville mnamo mwaka 1944,

[1] Sehemu hii imetokana na makala ya mwanzo ya M. Twaddle iliyojikita kenye utafiti wa Rabearimana na kasha makala ya mwisho na fupi iliyorudiwa na M. Twaddle. Mawazo yanayoelezwa hapa ni yale ya L. Rubeari mana

[2] Alama za chuma na mawe zinazoashiria usafiri na uadilifu unaotakiwa na waanzilishi na chama

viongozi wa kizalendo waliyapinga mazungumzo hayo kwa mshawasha mkubwa wakisema kuwa "ukoloni haukuwa kitu kingine bali unyonyaji."[3]

Ni kweli kwamba baada ya vita mfumo wa *indigenat* uliofanyisha watu kazi kwa nguvu uliondolewa, na Bukini, pamoja na makoloni mengine ya Kifaransa, ikapewa uwakilishwaji wa kisiasa huko Paris. Ama kwa upande huo Wafaransa walikuwa wakarimu zaidi kuliko wenzao Waingereza katika Afrika Mashariki. Lakini, kwa upande wa uhuru wenyewe halisi, Wafaransa wa makao makuu walikuwa wakaidi wasiotaka kusikia la mtu, kuliko walivyokuwa Waingereza, ambao walikuwa wameanza kulikubali wazo hilo. Ama kwa hakika ni madai ya uhuru ambayo wajumbe wa Bukini walipeleka katika bunge la Ufaransa baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Wakawasilisha muswada wao wa kutaka Bukini iwe taifa huru, ikiwa na serikali, bunge, jeshi na sarafu yake yenyewe.[4] Muswada huo ulishambuliwa mara moja na kikao cha kwanza cha wabunge, ikadaiwa kuwa ulikuwa "unakiuka katiba"; na hivyo, basi, kikao kikamalizika bila muswada huo kufanikiwa. Lakini mfano wa kufuata hapo baadaye ulikuwa umewekwa.

Mazingira ya ndani na hali ya kimataifa baada ya Vita vya Pili vya Dunia, yakapelekea kuongezeka kwa msukumo wa nguvu wa madai ya wazalendo, na kuanzia mwaka 1945 hadi 1960 wazalendo wakawa wanapiga kampeni za kudai uhuru wa nchi yao. Raghba hii ikazaa chama cha siasa kilichojulikana kama *Movement démocratique pour la rénovation malgache* (MDRM = Chama cha Demokrasia cha Kuboresha maisha ya Wabukini).

Chama cha MDRM kilianzishwa Paris mnamo mwaka 1946, chini ya uongozi wa wale wajumbe wawili ambao walikuwa wamechaguliwa na wananchi wazawa wa Bukini, katika mwaka 1945, kuwawakilisha katika Bunge la Paris; wakati huo haki ya kupiga kura ikiwa inategemea sifa ya kumiliki mali. Kimsingi mafanikio ya chama cha MDRM yalitokana na mipango yake kuwekwa kwa namna ambayo ilikiwezesha chama kueleweka na kwa hiyo kuweza kufanya kazi mara moja. Hata hivyo, kulitokea mvutano na mgawanyiko kati ya wanachama wa kawaida na viongozi wa chama juu ya wazo la "taifa huru", mgawanyiko ambao ulipelekea baadhi ya wanachama maarufu wa MDRM kujiunga na vyama vingine vya siri — chama cha JINY[5] na Chama cha Siasa cha Taifa cha Wabukini (PANAMA). Vyama hivi viliongozwa na wazalendo ambao waliamini kwamba Ufaransa

[3] Imenukuliwa na J. Tronchon, 1983, uk. 125

[4] N. Hiseltine, 1971, uk. 174; J. Tronchon, 1983 uk. 127

[5] Jinyu ni ndege wa usiku. Ukweli kwamba jina hili ni la Chama cha Siri kilichoanzishwa wakati wa vita huonyesha nia ya chama hicho ya kukwepa kupelelezwa na Mamlaka ya Ufransa

isingeweza kutoa uhuru kwa nchi hiyo kwa urahisi, kwa hiyo njia pekee ya kujipatia uhuru wao ilikuwa ni matumizi ya nguvu. Pamoja na kuwepo kwa tatizo hili, chama cha MDRM kiliweza kupata ushindi mkubwa katika uchaguzi kisiwani kote, hali ambayo ilileta wasi wasi kwa viongozi mashuhuri katika maeneo ya pwani yaliyokuwa yakiwaunga mkono Wafaransa na utawala uliokuwepo wakati huo. Mnamo Julai 1946 wakaanzisha chama cha *Parti déshérités de Madagascar* (PADESM).

Chama cha PADESM kilipata wanachama wake kutokana na watu mashuhuri wa pwani ambao walikipinga kwa nguvu chama cha MDRM. Kwa makusudi kabisa chama cha PADESM kikakinasibisha chama cha MDRM na Wahova, yaani watu waliokuwa wakiishi karibu sana na Tananarive, na kikaomba kuungwa mkono na mbari nyingine kumi na saba katika Bukini. Utawala wa Wafaransa, ambao sasa ulikuwa na wasi wasi sana na kuinukia kwa Wabukini wazalendo, kupitia chama cha MDRM, ukaharakisha sana kukiunga mkono chama cha PADESM.

Mnamo mwaka 1946, baada ya kuchaguliwa kwa wawakilishi watatu wa chama cha MDRM katika baraza la kutunga sheria, zikachukuliwa hatua za kukikandamiza chama hiki. Magazeti yake yakafungiwa, na wanachama na viongozi wake wakawa wanakamatwa kwa visingizio vya kipuuzipuuzi tu. Hali hii ya mvutano ilizidishwa na kuingilia kati kwa utawala wa kikoloni katika uchaguzi. Lakini pamoja na njama zote hizo wajumbe wengi wa baraza waliochaguliwa walitoka katika chama cha MDRM. Migongano kati ya vyama vya siasa ikazidi kuwa mikali. Kukawa na minong'ono mingi kuhusu kutokea kwa maasi baada ya muda si mrefu. Na kwa hakika ilipofika Machi 29, 1947 maasi hayo yakaanza.

Siku hiyo maasi yalitokea mashariki mwa kisiwa. Hata hivyo katika miji kama Tananarive, Fianarantsoa na Diego Suarez maasi hayakuwa na athari yoyote. Lakini waasi wakaendelea kujiimarisha hadi Julai 1947, walipochukua sehemu kubwa ya eneo la Tanala na Bezzabozano. Lakini, kutokana na matatizo ya mawasiliano kati yao na kutokana na kuzingirwa kwao, waasi wakalazimika kuwa katika hali ya kujihami zaidi baada ya Agosti. Hatimaye maasi yakazimwa na majeshi ya ukoloni wa Kifaransa mwezi Novemba, 1948, mwaka mmoja tangu yaanze.

Kulikuwa na sababu nyingi za maasi ya mwaka 1947; moja kati yake ilikuwa ni matatizo yaliyotokana na vita, ambayo si kwamba yalizidisha madhila kwa watu tu, bali pia yaliwashawishi wazalendo wa Bukini kwamba wangeweza kudai na

kupata uhuru kwa kutumia msaada kutoka nje (hasa Uingereza na Marekani)[6]. Lakini sababu ya msingi ilikuwa ni kule kutozuilika kwa hamu ya kupata uhuru ambayo ilikuwa ikijitokeza miongoni mwa Wabukini baada ya Vita vya Pili vya Dunia.

Mafanikio ya kisiasa ambayo chama cha MDRM kilipata na hali ya wasi wasi ambayo mafanikio hayo yaliieta miongoni mwa watawala wa ukoloni wa Kifaransa ilikuwa kubwa kiasi kwamba maasi yalipoanza tu viongozi wa serikali hiyo ya kikoloni wakatangaza kwamba maasi hayo yalikuwa yakiongozwa na MDRM. Masetla wengi wa Kizungu wakajichukulia sheria mikononi mwao. Lakini, kwa upande wao, mara tu maasi yalipoanza wawakilishi wa MDRM wakajitenga nayo. Magazeti hayakufanya ajizi kueleza jinsi Wabukini walivyoukumbatia utamaduni wa Kifaransa.[7]

Mwamko wa kuyazima maasi hayo ukaenea kote kisiwani. Viongozi wa MDRM, na hata wanachama wa kawaida, wakakamatwa na chama chenyewe kikavunjwa mwezi Mei, tarehe 10, 1947. Kesi zikasikilizwa mahakani kisiwani kote. Kesi kubwa kuliko zote ni ile iliyoendeshwa Tananarive mnamo mwezi Novemba, 1948, ambayo iliishia kwa watu sita kuhukumiwa kifo, wawili kati yao wakiwa wawakilishi wa zamani wa MDRM, Joseph Raseta na Joseph Ravoahangy, na watu kadhaa wakahukumiwa kifungo cha maisha na kazi ngumu.

Nani hasa aliyeyachochea maasi hayo? Watawala wa kikoloni, Masetla wa Kifaransa, chama cha PADESM, wote waliamini kuwa chama cha MDRM ndicho kilichochochea maasi hayo. Wanachama wa MDRM wenyewe, na wale Wafaransa waliokuwa wakikiunga mkono chama kilichokuwa kikitawala wote waliamini kwamba matukio ya mwaka 1947-8 yalitokana na uchokozi wa utawala wa kikoloni ambao ulikuwa umedhamiria kufanya kila lililowezekana kuhakikisha kwamba chama hiki kilichokuwa kikiwasumbua kinatoweka. Kwa upande mwingine, maoni ya wale hasa walioshiriki katika maasi hayo, yalikuwa kwamba hicho kilikuwa chama halisi cha kizalendo ambacho kilitokana na nia thabiti ya baadhi ya Wabukini kuwaondoa Wafaransa nchini Bukini kwa mtutu wa bunduki.

Kwa kawaida inaaminika kwamba uzalendo wa Kimalagasi ulivunjiliwa mbali na hatua hizo za kuzima maasi zilizochukuliwa na watawala wa kikoloni, ambazo

6 J. Tronchon ameandika kwa urefu juu ya sababu za upingani na pia kwenye tasnifu ya C. Guerin du Marteray

7 Tazama L Rabearimana, 1980, uk. 143

ziliua Wamalagasi takriban 100,000[8] Lakini kati ya 1948 na 1956, kipindi ambacho nguvu za dola za kuzima aina yoyote ya maasi zilikuwa kali sana, hamu ya kupata uhuru bado ilikuwepo na ikawa inajitokeza katika makala ya magazeti yaliyochapishwa katika makao makuu. Makala yaliyokuwa yakiandikwa hayakudai tu uhuru wa nchi hiyo bali pia yalidai msamaha kwa maathura wa hatua hizo za kuzima maasi

Migogoro iliyoipata Ufaransa na kwingineko katika Mwungano wa Ufaransa (French Union) — hasa katika Vietnam na Afrika Kaskazini — nayo ilichangia katika nguvu mpya waliyoipata wazalendo wa Kimalagasi. Msaada mkubwa kabisa ambao wazalendo wa ki-Malagasi waliupata, bila shaka ulikuwa ule uliotokana na utaratibu wa Kikatoliki wa kitabaka-msonge, ambao mnamo mwezi Novemba, 1953 ulitambua rasmi uhalali wa madai ya watu wengi ya kutaka uhuru. Kutangazwa huku rasmi kwa kutambuliwa kwa madai ya walio wengi ya kutaka uhuru kulifuatiwa na misaada ya moja kwa moja kwa chama cha kizalendo cha mrengo wa wastani ili kuwatafrisha (kuwavunja moyo) washabiki wao wa mrengo wa kikomunisti. Baada ya hapo chama kilifuata mwelekeo ambao haukuwa na sera ya wazi sana. Hapakuwepo na chama chochote muhimu kilichowaungamisha watu. Kinyume chake, wanasiasa wakawa wamegawanyika, hata kama zaidi ilikuwa kwa chuki za watu binafsi na siyo kwa tofauti za kiitikadi. Hata hivyo mnamo mwaka 1956 hali ikabadilika tena kutokana na vita vya Vietnam, mwanzo wa harakati za ukombozi wa kitaifa katika Algeria, athari za Mkutano wa Bandung mwaka 1955 na kuingia madarakani kwa serikali ya kijamaa katika Ufaransa. Mara baada ya "sheria ya kiunzi" kupitishwa vyama kadhaa vya siasa vyenye kutofautiana (kiitikadi) vikaanzishwa nchini Bukini.

Katika jumla ya vyama vya wastani vilivyoanzishwa wakati huu kulikuwa na chama cha *Parti Social démocrate* (PSD) kilichoanzishwa Majunga mnamo mwezi Desemba, 1956, na Philbert Tsiranana na André Resamp. Kilienea kwanza magharibi na kaskazini ya Bukini, na baada ya muda mfupi tu kikawa na vituo katika kisiwa chote kutokana na utawala wa kikoloni kuwa tayari kusaidia tawi la PADSEM la mrengo wa kushoto, ambalo wanachama wake walikuwa bado wameridhika na mabadiliko ya kiasasi yaliyoletwa na "sheria ya kiunzi." Kulikuwa pia na chama cha Antoine Zafimahova cha *Union démocrate et Sociale de Madagascar* (UDSM) ambacho kilikuwa na wafuasi kusini-mashariki na katika

8 Hii ni idadi iliyotolewa na Balozi wa Chevigne kwenye mitano wake na waandishi wa habari mwaka 1949

eneo la Fianarantsoa. Kilikuwa chama chenye madai ya kawaida sana, mengi yakiwa yanahusu mambo ya kusaidia jamii katika maeneo ya pwani.

Kati ya mwaka 1956 na 1960 kulikuwa na mawazo na mitazamo anuwai ya kisiasa katika Bukini. Hali hii ikapelekea upinzani kati ya vyama vya kisiasa kuwa mkali zaidi na kampeni za siasa zikawa na michuano mikali sana. Chama cha Padre R. Andrianamanjato cha AKFM (*Ankotonny Kongreiny Fahaleovantenan Madagaskara)*, kilichoanzishwa mwaka 1958, kilikuwa chama kimojawapo kati ya vyama vilivyokuwa na msimamo mkali sana.[9] Wazalendo wakapata idadi kubwa zaidi ya viti katika miji muhimu kama Tananarive, Tamatave, Diego Suarez na Talear. Lakini katika uchaguzi wa majimbo uliofanyika 1957 wakashindwa kufanya vizuri. Sababu ya kushindwa huku tunaweza kusema ilitokana na shinikizo la utawala wa kikoloni; lakini pia kulikuwa na mgawanyiko kati ya wazalendo wenyewe.

Jenerali De Gaulle alipotaka kura ya maoni ya wananchi kuhusu kuendelea kwao kuwa sehemu ya Jumuiya ya Ufaransa mnamo Septemba 1958 kura za "NDIYO" zilishinda. Kura za "HAPANA" zilikuwa nyingi katika mji mkuu na pia zilikuwa za kiasi cha kutosha katika Tamatave na Diego Suarez, lakini shinikizo lililotoka katika serikali ya kikoloni na wanasiasa wasio na siasa kali lilikuwa kubwa kiasi kwamba wale waliokuwa wanapendelea uhuru kamili walishindwa. Mnamo Juni 1960, Bukini ilipopata uhuru, chama kilichonufaika zaidi na uhuru huo kilikuwa kile cha Philbert Tsiranana kilichojulikana kama *Parti Sociale démocrate*. Wale waliopigania uhuru kamili kutoka kwa Ufaransa pamoja na chama cha *Parti du congrès de l'indépendance*[10] na kile cha *Mouvement national pour l'indépendance de Madagascar*[11] wakajikuta sasa katika upinzani.

Kufanya tathmini kamili ya harakati za kudai utawala wa kisiasa katika Bukini kunahitaji maelezo mengi na makini zaidi ya nguvu na udhaifu wa uzalendo wa Wamalagasi, ukoloni wa Kifaransa na pia umuhimu wa mwingiliano ulioendelea kuwapo kati ya pande hizo mbili.

[9] Kipingi kai ya vita, AKFM kilishirikiana na Chama cha Kikoministi nchini Ufaransa na wakati wa vita vikuu ya Pili, vyama vyote viwili vilikandamizwa. Tazama V.M. Thompson na

[10] Chama hiki hujulikana kama AKFM

[11] Chama hiki kilianzishwa mwezi Novemba mwaka 1958 na Monja Jona

## Nguvu za mabadiliko katika nchi zilizotawaliwa na Waingereza

Mara tu baada ya Vita vya Pili vya Dunia, Uingereza ikawa na serikali ya Leba ambayo ilikuwa imewania kufanya mageuzi makubwa ya kisoshalisti nyumbani na kufanya mabadiliko katika makoloni. Kama ilivyokuwa kwa wenzao masoshalisti na makomunisti katika Ufaransa katika kipindi hiki, Chama cha Leba hakikuona kupingana kwa aina yoyote kulikokuwepo katika malengo hayo mawili.[12] Kiwango cha mipango ya kijamii na kiuchumi kwa ajili ya maendeleo katika Afrika Mashariki na Kati baada ya vita kilikuwa sawa na "uvamizi wa pili wa ukoloni" katika eneo hilo.[13] Mipango hiyo huanza kufikiriwa kuwa ilikuwa na athari mbaya juu ya kuimarika kwa utawala wa Wakoloni wa Kiingereza kuliko uwakilishi wa mtu mmoja au wawili katika mabaraza ya kienyeji ya kutunga sheria waliopewa Waafrika. Ingawa Waingereza katika Afrika Mashariki na Kati hawakuwa na matatizo yoyote yaliyotokana na kushindwa na kupoteza umaarufu kama ilivyokuwa kwa Wafaransa katika Bukini, wao pia walikuwa na matatizo ya kusawajika kiuchumi kulikotokea nyumbani kwao kutokana na Vita vya Pili vya Dunia. Kwa hiyo Afrika Mashariki na Kati zilikuwa muhimu sana kwa Uingereza kwa ajili ya kufufua uchumi kwa kuuza, katika soko la dunia, bidhaa na mali ghafi zilizopatikana katika makoloni hayo.[14]

### Uganda[15]

Uganda kwenye mwaka wa 1945 ilitofautiana na Bukini katika namna kadhaa. Mbali na kuwa nchi ambayo imezungukwa na nchi nyingine, Uganda haikuwa kisiwa kama Bukini, na ilikuwa ikitawaliwa, siyo tu na taifa la Ulaya lililokuwa limeibuka na ushindi katika vita, lakini pia taifa ambalo sera yake ilikuwa ni kutouondoa utawala muhimu uliokuwa katika mipaka yake, kabla ya ukoloni, yaani Ufalme wa Buganda. Katika Uganda, Waingereza walikuwa wameegemeza utawala wao katika Buganda, wakitambua haki yao ya kuwa na kiasi fulani cha uhuru; wakaanzisha utaratibu usio wa kawaida wa kumiliki ardhi ambao kwa kiasi fulani haukuwa na masharti kwa mujibu wa Mkataba wa Uganda wa 1900; na wakaendesha utawala wao katika maeneo mengine ya nchi ya Uganda iliyokuwa

[12] Tazama D. Gold sworthy, 1971
[13] D.A. Low na J.M. Lon sadale, 1976, uk. 12
[14] Tazama M. Gowen, 1984, uk. 63-75
[15] C. Gertzed, 1976, anatoa maelezo kamili na marejeo

Chini ya Ulinzi wao kwa kuwatumia Baganda (watu wa Buganda) kama watu wa kati.

Kwa hiyo uzalendo wa Uganda, kadri ulivyoendelea kujengeka, ulikuwa na tabia ambayo kwa namna fulani ilionekana kama yenye kupingana, wakati mwingine ukijitambulisha na utukufu na uhuru wa ufamle wa Buganda, na wakati mwingine ukidhihirisha manung'uniko ya namna mbalimbali ya jamii mbalimbali za Uganda ambazo zilidai kupewa hadhi sawa na jamii ya Buganda. Lakini pengine athari kubwa kabisa ya Vita vya Pili vya Dunia juu ya Uganda haikuwa sana katika kuzindukana kwa itikadi ya uzalendo wa kitamaduni kama ilivyokuwa katika manung'uniko ya wazi kuhusu umilikaji mali ambao ulitokana na migongano ya jumla katika sehemu za mijini na vijijini.

Ili kuweza kuielewa vizuri mivutano ndani ya Uganda katika miaka ya 1940 ni muhimu kuzingatia makundi yenye maslahi mbalimbali yaliyoanzishwa na mfumo wa kikoloni na mabwanyenye wadogo ambao walilinda maslahi yao kila ilipotokea haja ya kuanzisha harakati za kitaifa. Kundi la kwanza lilikuwa la wafanyakazi wa serikali ambao malalamiko yao makubwa yalikuwa juu ya ubaguzi wa rangi katika mishahara walipojilinganisha na wenzi wao Wazungu au Wahindi. Kundi la pili lilikuwa lile la wakulima wa mazao ya biashara ambao waliwachukia wenye vinu vya pamba, ambao wengi wao walikuwa Wahindi, na bodi za kitaifa za mauzo kwa kuondolewa sehemu kubwa ya ziada ya mazao yao. Kundi la tatu lilikuwa la wafanyabiashara ambao walikuwa wakidai kukomeshwa kwa ukiritimba wa marupurupu waliyopewa wenye makampuni ya Kihindi na Kiingereza. Sambamba na hawa, kulikuwa na wafanyakazi wa mijini ambao walikuwa wakidai mishahara mikubwa zaidi. Maslahi haya mbalimbali kwa pamoja yalizaa upinzani uliofanywa na idadi kubwa ya watu dhidi ya utaratibu wa kikoloni katika miaka ya 1940.[16]

Mnamo Januari 1945 kulikuwa na ghasia kubwa katika miji kadhaa ya Uganda kuhusu vima vidogo vya mishahara na kupanda kwa maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei wakati wa vita. Waziri Kiongozi wa Buganda aliuawa. Jawabu la Waingereza katika ghasia hizi likawa ni kuzikomesha kwa nguvu, zoezi ambalo makali yake yalikuwa mabaya kiasi cha kuwafanya watu wengi walalamike na kuwaonea imani wale waliokamatwa na kutiwa ndani visivyo halali. Kisha watu hao wakaachiwa baada ya muda si mrefu. Mwaka 1949 kukatokea tena ghasia katika ufalme wa Buganda, ghasia ambazo zilisababishwa na malipo ya chini sana waliyopewa wakulima wa pamba, na mnamo mwaka 1952, watu wengi waliokuwa

[16] Kwa maelezo zaidi tazama M. Mamdani, 1976, Sura 7: D.W. Nabudere, 1980, Sura 8



Picha 9.1 *Mfalme Mutesa II, Kabaka wa Baganda, akiwa ukimbizini, London*

wamefungwa zamani wakahusika na kuanzishwa kwa chama cha Uganda National Congress (UNC) na Milton Obote, na kutayarisha sera yake ya "kujitawala wenyewe sasa."

Kuanzishwa kwa UNC lilikuwa ni jaribio la kwanza la kuanzishwa kwa chama cha kitaifa (kikiungwa mkono na watu wengi) kikiunganisha watu kutoka matabaka bora ya maeneo mbalimbali katika Uganda. Pamoja na kwamba uongozi ulitoka Buganda, chama cha UNC kilipata nguvu katika sehemu za Uganda ambako kulikuwa na wakulima wadogo wadogo wa mazao ya biashara, lakini ambako hakukuwa na sehemu muhimu ya wakulima matajiri. Viongozi walikuwa hasa wafanyabiashara, walimu na watumishi wa serikali. Lakini mnamo mwaka 1955 uzalendo wa kitaifa katika Uganda ukapata pigo kubwa la kushangaza. Andrew Cohen, gavana wa kisoshalisti, ambaye imedaiwa na baadhi ya wanahistoria kuwa

ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa harakati za uhuru wa siasa katika makoloni ya Uingereza huko Afrika Magharibi,[17] akagombana na *Kabaka* wa Buganda juu ya hali ya maendeleo ya baadaye ya Uganda kama taifa moja; *Kabaka* akachukuliwa na kuhamishiwa Uingereza, na ghafula akatokea kuwa shujaa wa harakati za upinzani dhidi ya ukoloni katika Uganda, kinyume na ilivyokuwa katika ghasia za 1949, ambapo yeye alikuwa mmojawapo wa marafiki wa ndani wa ukoloni. Tabaka bora la wakulima wa Buganda likajiunga na UNC kwa wingi sana kati ya 1953 na 1955, ambapo kurudishwa kwa *Kabaka* kulifanya mshikamano kati ya makundi mbalimbali katika UNC usambaratike; na huo ukawa ndio mwanzo wa *Kabaka Yekka* ("mfalme peke yake") kama chama pekee cha siasa katika Buganda.

Chama cha Uganda Peoples Congress kilianzishwa kikiwa ni mrithi wa UNC. Ingawa chama hicho kilijaribu sana kuziunganisha nguvu za wazalendo mbalimbali, lengo hilo kamwe halikuweza kutimizwa. Mnamo mwaka 1962, hatimaye Uganda ilipopata uhuru wake kutoka kwa Waingereza kama nchi moja chini ya uwaziri mkuu wa Milton Obote, ilifanya hivyo kwa kuruhusu kuwepo kwa serikali ya mseto kati ya chama kilichokuwa kitiifu kwa mfalme *Kabaka Yekka* na chama cha Obote cha UPC. Watu waliokiunga mkono chama cha UPC takribani wote walikuwa wanatoka nje ya Buganda — hata kabla Buganda haijaanza kuchagua Wabunge wake kwenda kwenye Bunge la Uganda kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mwuungano huo ukawa wenye matatizo ya hapa na pale na ilipofika mwaka 1966-7 Obote akaamrisha jeshi la Uganda kuiingiza Buganda kwa nguvu katika siasa za kitaifa. Kabla ya uhuru, kwa muda mfupi, 1961-62, Uganda iliongozwa na serikali ya *Democratic Party* (DP).

Kuanzishwa kwa DP kunaweza kuchukuliwa kama mbinu za kuviweka pamoja baadhi ya vikundi ambavyo havikuwemo katika vyama vilivyokuwepo. Vikundi vingine katika medani ya kitaifa vya kijamii ambavyo vilikuwa vimejihisi kutengwa vingehamasishwa na kupanuliwa kwa DP, ambacho kilikuwa kimeanzia Buganda kikiwa kimekitwa kwenye msingi wa dini. Machifu wa Kikatoliki walijikuta wakiwa na marupurupu kidogo sana katika Buganda, na kwa hiyo, kwa kutumia msingi huo wa dini, wakaanzisha chama hicho. Lakini itikadi hiyo ya dini ilitumiwa tu kama mbinu ya kuwaleta pamoja watu katika kujaribu kuanzisha chama cha upinzani cha kitaifa, kikijumuisha watumishi wa serikali na wasomi wengine ambao walijikuta wametengwa na UPC, ambacho kilijaa Waprotestanti. DP kiliungwa mkono na

[17] R. Robinson, 1980, uk. 50-72

watu kutoka ndani na nje ya ufalme wa Buganda. Aidha, pamoja na mwanzo wake wa kiitikadi, tunaweza kusema kwamba chama cha DP kilifanya jitihada kubwa katika kujenga chama cha wananchi wote wa Uganda. Kiliungwa mkono na vyama vya wafanyakazi, tukiachilia mbali Kanisa Katoliki.[18] Katika uchaguzi wa mwisho mwisho mnamo mwaka 1962 DP ndicho kilichofuatia muungano wa UPC-KY[19]. Kwa ujumla, kuinukia kwa utaifa na uzalendo katika Uganda kunadhihirisha migawanyiko ya kiitikadi na kijimbo; migawanyiko ambayo ililizuia tabaka la mabwanyenye wadogo kujitokeza kama tabaka moja na lenye mshikamano ambalo lingeweza kupambana dhidi ya ukoloni, kinyume na hali ilivyokuwa katika nchi jirani ya Tanganyika.

## Tanganyika[20]

Ikiwa mfumuko wa bei na malipo kidogo na yasiyokitwa kwenye vigezo makini waliyopewa wazalishaji bidhaa ndivyo vilivyoweka msingi wa mwamko wa kitaifa miongoni mwa wananchi wa Uganda baada ya mwaka 1945, na ukandamizwaji na kuonewa kwa wasomi wa Kiganda kukasababisha utaifa wa Kiganda kuunganishwa na kutoridhika kwa walio wengi, basi katika Tanganyika kuingilia sana kwa utawala wa Waingereza katika mipango ya kilimo cha Waafrika ndiko kulikopelekea upinzani wa kwanza dhidi ya ukoloni katika sehemu kubwa ya nchi. Sera za kikoloni zilileta mabadiliko ya kiuchumi-kijamii ambayo yaliongeza to fauti za kijimbo na ushindani kati ya makundi yaliyopata elimu katika kuendeleza sehemu walikokuwa wakitoka. Matokeo yake yakawa ni kuanzishwa kwa vyama vya kikabila ambavyo vilitumiwa kuelezea upinzani dhidi ya sera zilizokuwa hazifai. Katika baadhi ya sehemu utaratibu huu ulileta mafanikio makubwa ya kudai kuwa na machifu wakuu wa kuimarisha umoja wa kikabila. Chama cha *Tanganyika African Association* (TAA), ambacho kilianzishwa katika miaka ya 1920 kama chama cha ustawi wa watumishi wa serikali,[21] katika miaka ya 1930 kikawa kimechombeza kuanzishwa kwa matawi yake katika majimbo, ambayo ndiyo mara kwa mara yalisaidia sana katika kuimarisha nguvu ya makao makuu ya chama hicho.

[18] Tazama S. Karungire 1980, uk. 144-69; M. Twaddle, 1978, uk. 255-66, na D.A.L. 1971

[19] Tazama D. Rothchild na M. Rogin, 1966, uk. 337-440

[20] Sehemu hii inashukuru waandishi kadhaa hususan P. Gifford, 1982; R. Tangri, 1975 uk. 245-81; na J. Van Donge, 1985 uk. 265-77

[21] Tazama UNESCO, Historia Kuu ya Afrika, Juz. VII, uk. 671-2



*Picha 9.2 Julius K. Nyerere Rais wa TANU (Tanyika African National Union)*

Katika kipindi cha baada ya vita, upinzani uliojitokeza nchini kote ukiwa umekitwa katika mbari za kijamii ulielekea kukidhoofisha chama hicho, lakini, ajabu pia ni kwamba ukinzani dhidi ya sera za kikoloni ndio ulitokea kuwa mojawapo ya mihimili muhimu kabisa ambayo kwayo uongozi wa kitaifa baadaye ulitiwa nguvu; na ambayo kwayo chama chenye nguvu kabisa cha *Tanganyika African National Union* (TANU) kilianzishwa. Kichocheo cha nguvu yake kilitoka Jimbo la Ziwa, eneo la Tanganyika ambalo lilizalisha karibu nusu ya thamani ya bidhaa zoteza kilimo zilizosafirishwa nje. Upinzani dhidi ya sera za kikoloni zilizowekwa kuhusu mazao ya kilimo ulitokea katika jimbo lote na tawi la TAA nalo likaingia kati kuwaunga mkono wananchi katika malalamiko yao; na hivyo basi likawa limeunganisha chama cha ustawi wa wafanyakazi mijini na kuzungumzia matatizo ya vijijini.

Katika ofisi kuu ya Dar es Salaam shughuli za baada ya vita zilitokana na nguvu ya pamoja ya wafanyakazi wa serikali na wasomi wa mjini waliopigana vita katika Burma. Lakini kufikia mwishoni mwaka 1952 nguvu hiyo ikawa imefifia kwani viongozi wake ambao walikuwa wasemaji hodari walikuwa wamehamishwa Dar es Salaam. Chama kikaelekea kutokuwa na rais na kukawa hakuna mikutano iliyofanyika. Lakini kiongozi mpya akatokea, akaanza kuratibu shughuli za chama, na kukihuisha; na baada ya miaka miwili tu TAA ikawa imebadilika na kuwa chama kamili cha siasa ambacho sasa kilipewa jina la Tanganyika Africana National Union (TANU) tarehe 7 Julai, 1954.

TANU kikaleta uhuru katika mwaka 1961. Mwanzilishi wake mkuu alikuwa mwalimu kutoka katika moja ya jamii ndogo ya watu katika nchi hiyo, Julius Nyerere. Aliweza kuitumia vizuri nafasi ya kimataifa ya Tanganyika kama nchi ya udhamini chini ya Umoja wa Mataifa ili kuharakisha kuuondoa ukoloni.

Mnamo mwaka 1946 Uingereza ikawa haikuridhika na masharti ambayo kwayo mamlaka yake ya zamani katika Tanganyika, chini ya *League of Nations* (Shirikisho la Mataifa), yalikuwa yamebadilishwa kuwa nchi ya udhamini. Kupinga ukoloni tayari ilikwishakuwa fikra yenye uzito mkubwa katika Umoja wa Mataifa, na pakawa mahala muafaka kabisa ambapo malalamiko ya Watanganyika yangeweza kuelezwa wazi. Mnamo mwaka 1956, Edward Twining, akiwa gavana wa Tanganyika, akawashawishi wajumbe wengi wasio-rasmi wa baraza la kutunga sheria, ambao walikuwa wameteuliwa tu, hawakuchaguliwa, kuunda chama cha upinzani ambacho kilijulikana kama United Tanganyika Party (UTP). Lakini chama hicho cha UTP hakikuchukua muda kikaanza kufifia. Mwaka 1960 chama cha TANU kikashinda viti 70 kati ya viti 71 katika kampeni za kwanza za kugombea viti vya baraza la kutunga sheria; ambapo sasa, kwa kufuata utaratibu wa kura, iliwezekana sasa Waafrika kushinda kwa wingi. Nyerere akawa sasa Waziri Kiongozi wa serikali ya Tanganyika ambayo sasa ilikuwa haiongozwi kutoka nje, na ilipofika Desemba, 1961 ikawa nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki, iliyokuwa chini ya Uingereza, kupata uhuru kamili.

Sababu zilizopelekea Tanganyika kupata uhuru haraka — kabla ya Kenya na Uganda — ni pamoja na sifa za uongozi bora alizokuwa nazo Nyerere; muundo thabiti wa TANU; kutokuwepo na mgawanyiko mkubwa wa kimajimbo katika Tanganyika; hadhi yake katika Umoja wa mataifa, kama nchi ya udhamini; na mabadiliko ya ghafla na makubwa juu ya umuhimu wa Tanganyika na Kenya wakati machafuko ya Mfereji wa Suezi yaliyotokea mwaka 1956 yalipoifanya Uingereza ilazimike kuangalia upya na kwa makini azma yake iliyokuwa imeweka kuhusu kuilinda sehemu ya mashariki ya mfereji wa Suez. Kitu kingine ambacho

kilikuwa muhimu katika kuharakisha kujiondoa kwa Uingereza katika himaya yake ya Afrika Mashariki na Kati yalikuwa yale maasi ya Mau Mau katika Kenya.

## Kenya[22]

Kinyume na Wafaransa katika Bukini, Waingereza katika Kenya mwishoni mwa Vita vya Pili vya Dunia hawakujihisi kuwa hatarini sana. Walikuwa wameshinda vita. Kwa hiyo hapakuwepo na lazima ya kufanya mabadiliko ya kisiasa ambayo hayakuwa ya lazima. Hapana shaka kwamba Waafrika walipewa angalau nafasi kidogo ya uwakilishi katika Baraza la Kenya la Kutunga Sheria; kuanzia mwaka 1944 Eliud Mathu akawa ndiye Mwafrika wa kwanza, katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati lililokuwa chini ya utawala wa Waingereza, kuteuliwa kwenye baraza la kutunga sheria. Lakini hapakuwepo na namna yoyote ya kuwaambia masetla ni taratibu zipi zifuatwe katika kuwaajiri wafanyakazi (tofauti na hali ilivyokuwa katika Bukini ambako kuupiga vita mfumo uliokuwa ukitumika wa kuwaajiri wenyeji *indigénat* bila kufuata sheria, uliwafanya masetla wakishambulie sana chama cha MDRM katika Bukini). Kusema kweli kulikuwa na namna fulani ya maendeleo katika uelekeo huo na utawala wa Kiingereza katika Kenya ulikuwa na mipango kadhaa ya kuinua kilimo cha Waafrika, lakini masetla weupe walitegemewa kusaidia tu katika mipango hiyo na siyo kuingiliwa sana katika taratibu au mfumo wao wenyewe.

Ama kwa hakika mambo hayakupata kuwa mazuri hivyo kwa masetla wa Kenya. Mbali na kuongezeka kwa bei ya mzalishaji kutokana na nafasi ya Kenya kama mgavi wa Mashariki ya Kati, Nairobi ilikuwa ndio kituo kikuu cha wazalishaji na wagawaji bidhaa katika himaya ya Waingereza ya Afrika Mashariki na Kati kote; na kutokana na hali hiyo masetla wakajikuta katika kamati nyingi mbalimbali. Masetla wa Kenya walikuwa na nguvu sana baada ya vita kiasi kwamba Hati ya Baraza la Kutunga Sheria Na. 210, ambayo iliongeza uwakilishi usio-rasmi katika baraza la Kenya la kutunga sheria kwa kutoa nafasi ya kuchaguliwa mjumbe mwingine na baraza lote, ilionekana kwa Waafrika wa tabaka bora kama ishara ya mpango wa kuwapa Wazungu idadi kubwa ya wajumbe wa kudumu katika baraza hilo.

22 Sehemu hii inatoa shukrani kwa maelezo ya kwanza yaliyotolewa na C.G. Rosberg na J. Nottingham, 1966; Tazama pia J. Spenser, 1986, na D. Throup, 1985, uk. 399-433. Kuna maeneo yanayofaa katika A. Clayton, 1976; F. Fredi, 1974; na toleo maalum la *Kenya Historical Review*, 1977, linalozungumzia Mau Mau



*Picha 9.3 Jomo Kenyatta, Rais wa KAU African Union) picha ya mwaka 1946-7*

Muda mfupi tu baada ya maasi ya Mau Mau hali ya hatari ikatangazwa mwezi Oktoba, 1952, na chama cha Kenya African Union (KAU) kikamwandikia Katibu wa Makoloni ya Uingereza kikimweleza kwamba matatizo mengi yaliyokuwepo wakati huo yalikuwa yanasababishwa na Waafrika kutoshirikishwa katika shughuli za kiserikali ili kuwafanya wajihisi kuwa sehemu kamili au washiriki katika serikali ya nchi yao.

Maafisa wakuu wa KAU wote walikuwa wametiwa kizuizini kwa kushukiwa kuwa walishiriki katika kuanzishwa kwa Mau Mau. Huko nyuma, hali kama hiyo hiyo pia iliwahi kutokea huko Bukini. Kwa hakika tofauti baina ya tabaka la waali wa Kiafrika na wale watu wenye ghasia za kivita yaelekea kuwa ilikuwa kubwa

zaidi katika Kenya. Kikiwa kimeanzishwa katika mwaka 1944 kama kikundi cha kumuunga mkono Eliud Mathu katika shughuli zake za bunge, chama cha KAU mara kikaonekana kuwa na mwelekeo wa wastani. Jomo Kenyatta akawa rais wake mwaka 1947, mwaka mmoja baada ya kurudi kutoka ukimbizini Uingereza na Urusi alikokuwa amejipeleka yeye mwenyewe. Hata hivyo Kenyatta akakataliwa na watu waliokuwa wakilisha kiapo cha Mau Mau.

Wengi kati ya wafuasi wa Mau Mau walikuwa vijana waliokuwa wakijishughulisha na vyama vya wafanyabiashara na shughuli nyinginezo katika Nairobi. Kwamba Mau Mau chenyewe kilikuwa chama cha siri cha kivita ambacho kilikuwa na lengo la kumwondoa Mwingereza na kurudisha mikononi mwa wananchi wenyewe "ardhi iliyokuwa imeibiwa" ni jambo ambalo liko wazi. Kulikuwa na kampeni za kulishwa viapo miongoni mwa Wakikuyu katika kipindi chote cha baada ya vita, lakini ni katika mwaka 1951 ambapo ghasia zilizohusishwa na kulishwa kiapo zilifikia hatua mbaya sana: maandamano, ghasia na fujo dhidi ya masharti yaliyohusu mlipuko wa ugonjwa wa sotoka, na kuuawa kwa Mkikuyu mtiifu kulikofanywa wazi wazi mbele ya watu na watu wenye silaha, mnamo mwezi Oktoba, 1952. Lakini pengine kutangazwa kwa hali ya hatari mwishoni mwa mwezi Oktoba, kulikofanywa na gavana mpya ambaye ndiyo mwanzo tu alikuwa amefika, na ambaye alishinikizwa na masetla, ndiko kulikosababisha Mau Mau kuanza mashambulio kabla mipango yake haijakamilika vizuri.

Waasi wa Mau Mau hawakuwa na mipango mizuri kama waliyokuwa nayo wenzi wao wa Bukini. Ni wapiganaji wachache sana wa Mau Mau ambao walikuwa wameshiriki katika Vita vya Pili vya Dunia; hakuna miji kamili iliyotekwa, hakuna maeneo yoyote muhimu ya ardhi iliyolimwa yaliyochukuliwa kabisa, na ni raia wachache tu wa Kizungu waliouawa na waasi hao. Ukweli ni kwamba Waafrika wengi walikufa, na maoni ya wanazuoni wengi leo ni kwamba kimsingi Mau Mau vilikuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya Wakikuyu; lakini pia ukweli ni kwamba mauaji haya mengi yalifanyika baada ya serikali kuanza kuwatia kizuizini watuhumiwa wa Mau Mau bila kuwafungulia mashtaka, na baada ya kuanzisha utaratibu wa vijiji vya lazima katika jitihada za kuwatenga wapiganaji wa msituni na wale waliokuwa wakiwaunga mkono vijijini na mijini.

Yaelekea Mau Mau ilihusu mambo kadhaa tofauti tofauti, wakati mwingine yakiingiliana na wakati mwingine yakiwa na mielekeo tafauti: kama migomo ya watu wasio na makazi ya kudumu; upingaji wa sera za kulazimishwa za kuendeleza kilimo; kuhuishwa kwa utamaduni wa wenyeji; vita vya ndani kwa ndani, na vuguvugu la kupinga ukoloni ambalo lilikuwa ni mwangwi wa upinzani uliofanyika



*Picha: 9.4 Kambi ya Kizuizi Langata iliyoanzishwa na Waingereza wakati wa mapambano dhidi ya Mau Mau, Aprili 1954*

mapema wakati wa kuingizwa kwa lazima kwa utawala wa Waingereza katika kipindi cha nusu karne kabla ya wakati huo.[23]

Kulishwa kiapo kulienea katika "Eneo la Wakikuyu Lililotengwa," ambako shughuli ya kuimarisha umiliki wa ardhi ilikuwa ikifanyika kwa haraka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kuongezeka kwa bei za bidhaa zilizozalishwa. Kwa sehemu yoyote ya Afrika ambayo imekaliwa na masetla, eneo hilo la Wakikuyu lilikuwa katika sehemu ya ajabu kidogo, kwa maana kwamba kwa kiasi kikubwa lilikuwa katikati kwa upande wa miundombinu ya barabara na reli, na pia kwa kuwa na ardhi nzuri. Uimarishaji wa umiliki wa ardhi nyumbani, na ukodishaji wa ardhi ya kulima nje ya eneo la makazi, ni mambo ambayo yaliashiria kwamba ni wao, na wao peke yao, ambao hapo baadaye wangekuja kuwa cheche ambayo ingewasha moto wa maasi ya wakulima, maasi ambayo hayakuwagonganisha Waafrika na Weupe tu, bali pia Wakikuyu kwa Wakikuyu.[24]

Katika Nairobi, na katika miji mingine ya nyanda za juu, kulikulwa na Waafrika ambao waliwapelekea chakula na vifaa vingine wapiganaji wa msituni hadi Operesheni Fuawe (*Operation Anvil*), 1954, ilipowaondoa kabisa watu wa namna hiyo mjini humo. Imewahi kusemwa kwamba mshikamano huu wa wafanyakazi na wakulima wadogo wadogo dhidi ya ubeberu unathibitisha kuanza kukua kwa mwamko wa watu wenye kipato cha chini katika Kenya ya kikoloni[25] lakini ushahidi kutoka katika nyimbo za wakati huo za Mau Mau na maandishi ya baadaye unaashiria kuwa ulikuwa zaidi ni upinzani wa wakulima wadogo walionyang'anywa ardhi dhidi ya kuingizwa katika tabaka la wafanyakazi na wale haukuwa mwamko wa kifanyakazi.

Mau Mau yaweza kutazamwa kama utetezi wa utamaduni. Lakini hapa kuna haja ya kuweka tahadhari. Ulishaji kiapo uliambatana sana na utamaduni. Habari za ajabu zaidi kuhusu vipengele vya utamaduni katika Mau Mau zinatoka kwa Wazungu wa wakati huo ambao nia yao ilikuwa zaidi kueleza njozi zao kuhusu Waafrika wenyewe. Pamoja na hayo, katika taratibu zote za ulishwaji kiapo wa Mau Mau kulikuwa na vipengele fulani fulani vya kiutamaduni ambavyo yaelekea vilifanya kazi kama vipingamizi vilivyozuia uingizaji wa watu wasio Wakikuyu katika

[23] R. Buijtenhuijs, 1982, anatoa tafsiri zinazopingana. Tazama D. Throp, 1985, 1987, T. Kanogo, 1987

[24] J. Lonsdale, 1982, uk. 6

[25] R. Buijtenhuijs, 1982, uk. 104, ananukuu maoni ya D.L. Barnett

kundi la wahamasishaji. Katika nyimbo za Mau Mau pia kulikuwa na vipengele vya utamaduni.

Mwisho, Mau Mau haina budi kutazamwa kama chama cha kupinga ukoloni, ingawa kilionekana kama chama cha jimbo tu. Maeneo ya Kikuyu yaliyoathirika zaidi na kuingiliwa na ukoloni na "ardhi iliyoibiwa", yaani Kiambu, na mazingira yake jirani, ndiyo ambayo hayakuwaunga sana mkono waasi, ambapo maeneo mengine mbali na Nairobi, kama vile Nyeri na Fort Hall yalionyesha kuwaunga sana mkono waasi ingawa yenyewe hayakuwa yameingliwa sana ama na ukoloni wa Kiingereza au masetla wa Kizungu. Lakini Robert Buijenhuijs anasema kwamba Fort Hall na Nyeri yalikuwa pia maeneo ya Wakikuyu ambako ukoloni wa Kiingereza uliingilia kwa ukatili mwanzoni mwa karne hii. Ikilinganishwa na sehemu nyingine sehemu ya Kiambu ilitawaliwa pasi na ukatili mwingi.[26]

Kwa vyo vyote vile, iwe ni kuleta maendeleo au kurudi nyuma, walichojali sana wanasiasa wa Kiingereza katika miaka ya 1950 ilikuwa ni ule ugumu wa kulidhibiti eneo lenye ghasia kama hilo. Pengine Waingereza walikadiria kwa kutia chumvi tishio la kivita la waasi wa Mau Mau, na wakakadiria kwa kiwango cha chini kwa namna ambayo jibu la Waingereza lingeweza kuzusha ghasia kubwa na mauaji. Lakini ghasia ni ghasia, na kulingana na mapokeo ya siasa za Waingereza[27] gharama za kuendelea kuwasaidia masetla wa Kizungu zisingeweza kuendelezwa bila kuwa na ukomo. Kwa hiyo, baada ya chama cha Conservative kupata ushindi wake wa tatu mfululizo katika Uingereza mnamo 1959, Ian Macleod akateuliwa kuwa katibu wa makoloni. Hali ya hatari ikaondolewa na ukatayarishwa mkutano wa katiba.

Mkutano huo uliishia na kuwepo kwa wajumbe 65 katika baraza la kutunga sheria Kenya, 33 kati yao wakiwa wamechaguliwa kutokana na viti vya wazi (vya kugombewa). KAU ikafufuliwa kama KANU (the Kenya African National Union) na kikashinda asilimia 67 ya kura zote katika uchaguzi uliofanyika, raisi wake akiwa Jomo Kenyatta, ambaye alikuwa bado kizuizini. Chama cha KANU kilikuwa kinapingwa na KADU (the Kenya Democratic Union), ambacho kiliundwa kwa muungano wa wananchi wa pwani na watu mashuhuri wa bara kutoka makundi madogo madogo ya jamii. Hata hivyo ilikuwa ni baada ya kutolewa kwake kizuizini mnamo mwezi Agosti 1961, mkutano wa pili wa Lancaster House, na ushindi

[26] R. Buijtenhuijs, 1987, uk. 2000-1
[27] Angalia maoni ya Katibu wa Makoloni wa Uingereza, Lord Chandos, 1964, uk. 397

mkubwa sana ambao KANU ilipata katika uchaguza wa Mei 1963, ndipo Kenyatta akawa Waziri Mkuu, na miezi sita baadaye akawa kiongozi wa nchi ambayo ilikuwa na uhuru kamili.[28]

Wakati wa uhuru mashamba ya wakulima wengi wa Kizungu yalinunuliwa chini ya mpango mkubwa wa msaada uliofadhiliwa na serikali ya Uingereza. Tabaka la Kati la watu weusi lilikwishaanza kujengeka katika Kenya ya ukoloni, lakini mizizi yake hasa inatokea mwanzoni kabisa mwa ukoloni ambapo weusi waliweza kuajiriwa kama watumishi wa serikali na pia wakipata mapato (ya ziada) kutoka katika mashamba yao. Katika Kenya uzalendo wa kupinga ukoloni lilikuwa jambo changamani zaidi kuliko vitendo tu vya mabwanyenye weusi wakijifanyia mambo yao wenyewe bila kuhusisha wengine katika maeneo yao na katika mawanda mapana zaidi.

## Nyasaland na Rhodesia Kaskazini[29]

Katika Nyasaland (sasa Malawi) na Rhodesia Kaskazini (sasa Zambia) kuingilia sana kwa Waingereza katika kilimo cha Waafrika kulileta hali ya msukosuko mkubwa katika kipindi cha mara tu baada ya vita;[30] lakini kuanzishwa kwa nguvu kwa Shirikisho la Afrika ya Kati (CAF) mnamo mwaka 1953 ndiko kulikosababisha mlipuko wa umoja wa uzalendo wa waali na kutoridhika na hali hiyo kwa watu wengi katika nchi hizi zote mbili ambazo zilikuwa chini ya utawala wa Waingereza.

Kwa nini kuanzishwa kwa shirikisho hili kulileta kutoridhika kwa kiasi kikubwa kwa Waafrika? Kwa miaka kadhaa masetla wa Kizungu wa Rhodesia Kusini — ambao walikuwa wamejitawala tangu 1923 — walikuwa wamelifikiria sana wazo la "kuungana" na Rhodesia Kaskazini na Nyasaland; nchi zote mbili wakati huo zikiwa zinaongozwa na Ofisi Kuu ya Makoloni ya Uingereza (British Colonial Office), zikiwemo pia nchi za Kenya, Uganda, na Tanganyika; nazo zote mbili zikiwa na Wazungu wachache wakiishi humo. Mara tu baada ya Vita vya Pili vya Dunia serikali mpya ya kisoshalisti katika Uingereza ikatumia kura ya turufu kupinga muungano wa nchi hizo, lakini ikaelekea kupendelea zaidi wazo la "shirikisho"

[28] G. Bennett na C. Rosberg, 1961, uk. 21-2

[29] Sehemu hii inashukuru waandishi kadhaa hususan P. Gifford, 1982; R. Tangri, 1975 uk. 245-81; na J. Van Donge, 1985 uk. 265-77

[30] R. Tangri 1975, uk. 262. Utafiti uliochambuliwa na J. Van Donge unadokeza kuwa upinzani huu unaeleweka vema kwa kuona mapambano ya utaifa kama ushirikiano unaokubalika haraka kutokana na hali ya kisiaa.

kama njia ya kusaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi, na pia kuwa kinga ya kuingiliwa na makaburu kutoka Afrika Kusini. Hata hivyo, upinzani uliotoka katika vyama vya wazalendo wa tabaka bora, kama vile Nyasaland African Congress (kilichoanzishwa mwaka 1940) na mwenzi wake katika Rhodesia Kaskazini (kilichoanzishwa mwaka 1948) ulitosha kuzuia kitu chochote kisifanyike kabla ya Oktoba, 1951, serikali ya chama cha Conservative ilipochukua madaraka huko London.

Serikali hii ilipendelea zaidi maslahi ya kibiashara na masetla weupe waliopendelea shirikisho. Wazo la shirikisho lilipendelewa pia na wafanyakazi wa utumishi (kama Andrew Cohen, kabla hajaenda Uganda na kumtoa nchini *Kabaka*) kwa sababu nyingine za kirasimu na kimaendeleo. Mwaka 1953, Nyasaland na Rhodesia Kaskazini zikalazimishwa kuingia katika shirikisho, ingawa Waafrika walikuwa wanalipinga sana wazo hilo.[31] Katika Rhodesia Kusini, shirikisho lilikaribishwa sana na wajumbe weupe walioruhusiwa kupiga kura kwa sababu ya umuhimu wa kiuchumi wa shaba ya Rhodesia Kaskazini.

Kwa muda upinzani wa Waafrika dhidi ya Shirikisho la Afrika ya Kati ukawa umefifia. Chama cha NAC kikawa na matatizo ya kugombea uongozi ambayo hayakuweza kutatuliwa. Hatimaye mnamo mwaka 1958 Kenneth Kaunda akajitenga na akaunda chama ambacho baadaye kilijulikana kama United National Independence Party (UNIP). Viongozi wa CAF wakafika mbali kiutendaji, kwa kujaribu kuongeza zaidi marupurupu ya weupe kwa kuanzisha uraia mpya wa shirikisho, ambao Waafrika wa Nyasaland, kwa mfano, wangeweza kuununua kwa £5 na kutia sahihi ya kufuta haki zao walizokuwa nazo kama watu "wanaolindwa" na Ofisi Kuu ya Makoloni ya Uingereza. Kukapendekezwa kuwepo na makundi mawili ya wapiga kura; jambo moja lililokuwa wazi ni kwamba Waafrika, kama raia masikini kabisa, wasingenufaika na chochote muhimu, kisiasa, katika mfumo huo.

Sasa kukawa na dharuba za kisiasa. Katikati ya 1958, Hastings Banda, daktari wa tiba ambaye aliwahi kuiwakilisha Nyasaland Congress katika London kabla ya kwenda Ghana, alirudi kama mgombea wa urais wa Nyasaland African Congress. Baada ya kuthibitishwa urais wa chama akaanza kupiga kampeni ya kutoshirikiana na Wazungu; kampeni ambayo iliishia na kupatikana kwa uhuru kutoka kwa Waingereza miaka sita baadaye. Mwaka 1959 hali ya hatari ikatangazwa na chini ya kamata kamata ya Operation Sunrise, Banda na wenzake 200,wahamasishaji

[31] P. Gifford, 1981, anatoa maelezo kamili

wa Congress, walikamatwa na kutiwa kizuizini. Pilika pilika zilizosababishwa na kamata kamata hii pamoja na vurumai zilizoandamana nayo, na matumizi ya majeshi kutoka Rhodesia Kusini, vikapelekea kuundwa kwa tume ya uchunguzi na serikali ya Uingereza mjini London. Tume ya Devlin ikagundua kwamba Nyasaland ilikuwa inakandamizwa na polisi.

Katibu wa makoloni ya Uingereza na gavana wa Nyasaland wakasema kwamba ripoti ya Devlin ilikuwa inapotosha ukweli. Harold Macmillan, ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Uingereza akawa na wasi wasi na akatuma tume nyingine ya kwenda kuchunguza ukweli katika Afrika ya Kati. Tume hiyo ilijulikana kama Tume ya Monckton. Waafrika wachache tu waliruhusiwa kuzungumza na tume hiyo, na kwa vyovyote vile wanachama wa vyama viwili vya Congress (Nyasaland na Rhodesia Kaskazini) hawakuruhusiwa kabisa kuongea na tume. Lakini baadhi ya watu "wasiokuwa na siasa kali" waliweza kuzungumza na tume, na kutokana na maoni yao Monckton akaripoti kwamba upinzani dhidi ya shirikisho katika Rhodesia Kaskazini na Nyasaland ulikuwa mkubwa, wenye mawanda mapana, wa kweli na wa muda mrefu. Akashauri pawepo na "ubia" wa kweli na maendeleo makubwa zaidi ya kiuchumi.[32] Akasema pengine Nyasaland inaweza isiwe na umuhimu sana kama chanzo cha uchumi wa Uingereza, lakini Rhodesia Kaskazini ilikuwa muhimu sana kwa ajili ya kuipatia Uingereza shaba.

Ian Macleod, akiwa Katibu wa Makoloni ya Uingereza, akaandaa taratibu changamani sana za uchaguzi kwa Nyasaland na Rhodesia Kaskazini, na pia kwa Kenya. Matokeo ya uchaguzi huo yakawa: kwa Malawi (kama ambavyo sasa kuanzia wakati huo Nyasaland ilijulikana), ushindi wa chama cha Congress katika mwaka 1961 na kupata uhuru kamili mnamo mwezi Julai 1964; kwa Zambia (kama ambavyo sasa Rhodesia Kaskazini ilijulikana) ushindi ukagawanywa kati ya UNIP na chama ambacho sasa kilikuwa kimepitwa na wakati cha Northern Rhodesian Congress, katika uchaguzi wa mwaka 1962. Baada ya uchaguzi wa mwaka 1963, Zambia ikapata uhuru kamili mwezi Oktoba, 1964.

## Zanzibar

Zanzibar ni kisiwa kidogo sana kikilinganishwa na Bukini; mwaka 1958 kulikuwa na idadi ya watu wapatao chini ya 300,000 katika kisiwa cha Zanzibar na kisiwa jirani cha Pemba. Katika karne ya kumi na tisa, Zanzibar ilikuwa kituo kikuu cha

[32] Ripoti ya Tume ya ushauri, 1960

mtandao mpana sana wa biashara katika Afrika Mashariki chini ya nasaba-tawala ya Kiomani. Mwaka 1890 Zanzibar ikawa chini ya ulinzi wa Waingereza ambao ulidumu hadi Desemba 1963. Mwezi mmoja badaye kukatokea mapinduzi ambayo hayakutegemewa na yaliyomwaga damu nyingi. Kama alivyosema mchochezi mkuu wa mapinduzi hayo muda mfupi baadaye, mapinduzi hayo yalipangwa kwa nia ya "kuwaondoa Waafrika wa Zanzibar katika nira ya ukoloni wa Kiarabu"[33].

Upinzani wa rangi kati ya Waafrika na Waarabu kwa kiasi fulani ulitokana na mabaki ya biashara ya watumwa ya karne ya kumi na tisa, na kwa kiasi fulani ulitokana pia na mpenyezo wa ubepari katika tasnia ya karafuu ambao ulijenga tabaka la mamwinyi wa Kiarabu na tabaka la wanyonge Waafrika; na ukapenyeza pia tabaka jingine la Wahindi wenyeji ambao ndio waliohusika na utoaji pesa.[34] Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, mabadiliko katika serikali za wenyeji chini ya Waingereza na dalili za mwanzo za uhuru viliongeza uzito wa kisiasa wa matabaka haya ya kijamii.

Zaidi ikiwa ni zao la maendeleo ya kisiasa katika bara ya Afrika Mashariki kuliko haja ya kuwepo kwa haraka kwa kitu kama hicho katika Zanzibar yenyewe, dalili za mwanzo za uhuru zilimfanya mwinyi wa Kiarabu — kupitia chama cha takriban Waarabu watupu, *Zanzibar National Party* (ZNP) — kutafuta njia ya kuuondoa utawala wa Kiingereza kabla tabaka nyonge la Waafrika halijajiimarisha vya kutosha kuweza kuchukua madaraka kupitia chama cha Afro-Shirazi Party (ASP), ambacho kilikuwa kinaongozwa na Abeid Karume, rais wa chama cha African Association tangu mwaka 1953. Udogo wa Zanzibar na tabia ya siasa za ana-kwa-ana ukafanya mapambano haya yawe makali na yenye ghasia.[35] Hata hivyo kufikia Desemba, 1963 ikaonekana kana kwamba mbinu hiyo ilikuwa imefaa. ZNP na rafiki zake katika *Zanzibar and Pemba Peoples Party* (ZPPP) — tawi lililojitenga na ASP na lililokuwa likitetea maslahi ya Waarabu — kwa pamoja walipata viti vingi zaidi kuliko ASP katika uchaguzi uliofanyika muda mfupi kabla ya uhuru, na kwa pamoja vikaweza kuipatia Zanzibar uhuru kutoka kwa Waingereza tarehe 10 Desemba, 1963. Lakini mara yakatokea mapinduzi tarehe 12 Januari, 1964.

[33] Uganda Argus, 4 Aprili 1964
[34] Tazama, F. Cooper, 1980
[35] Tazama makala mbili za K. Kyle: 1964a, na 1964b; na Lofchie 1967, uk. 36-42 Uganda Argus, 4 Aprili 1964

Wakati wakitambua mbinu za uchaguzi ambazo kwazo ASP, ikiwa na idadi kubwa ya kura ilizuiwa kupata viti vingi zaidi, wanazuoni wamekuwa na namna mbili za kuelezea nini kilitokea usiku wa mapinduzi, na zote zikidhihirisha kukubali madai kuwa ASP haikuwa na uwezo wa kupanga mapinduzi. Kwanza wanachukulia kujitoa kwa Umma Party, chini ya uongozi wa Abdul Rahman Muhammad Babu katika ZNP na kujiunga na ASP kama tendo lililoinufaisha ASP. Yawezekana chama cha Umma Party kilikuwa kimepanga kufanya mapinduzi yake chenyewe kama kisingezuizwa wiki moja kabla ya kile kilichodaiwa kuwa Mapinduzi ya Okello. Pili, kichocheo hasa cha mapinduzi alikuwa mtu mmoja aliyezaliwa Uganda, John Okello "ambaye alitumia jeshi dogo alilolIandikisha yeye mwenyewe, ambamo kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakikiunga mkono chama cha Umma Party, kuipindua serikali iliyokuwa madarakani na ambayo haikuwa na ulinzi wowote makini."[36] Akiwa mpakarangi wa kujitegemea katika Pemba, aliweza kuingilia kati na kuwapanga mapolisi — ambao walikuwa hawakuridhika wakati wa uhuru, wakubwa wao wa kazi, Waingereza, walipobadilishwa na badala yao wakawekwa maofisa wa Kiarabu — katika kikosi cha washambuliaji ambao walichukua madaraka mjini Zanzibar usiku wa tarehe 11-12 Januari, 1964.[37]

Sasa imedhihirika zaidi kwamba matukio ya usiku huo wa mapinduzi yalikuwa yamesimamiwa na Abeid Karume, raisi wa ASP, na Kamati (yake) ya Watu Kumi na Wanne, kuliko ilivyokuwa inaeleweka hapo awali. Kwa mujibu wa rai hii, Okello alitumiwa kwa makusudi na ASP katika kamati hiyo kama mmojawapo wa waratibu. Lakini madai aliyotoa baadaye yakamfanya asikubalike kama kiongozi wa chama na ikabidi aondoke Zanzibar. Hadi wakati huo Karume alikwishaiunda Zanzibar kama nchi ya chama kimoja chini ya ASP na akawa anafanya mazungumzo ya kuungana na Tanganyika ili kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Aprili, 1964.

## Mataifa Mapya na Makoloni ya zamani

Mchakato wa uhuru wa kisiasa katika Mashariki ya Afrika ulikuwa unahusiana sana na maendeleo ya uzalendo katika makoloni yaliyoanzishwa mnamo karne ya

[36] A. Smith, 1976, uk. 211
[37] Maelezo ya Okello mwenyewe yalichapishwa mwaka 1967

kumi na tisa. Wakati mwingine uzalendo huu ulikuwa ni ule wa mataifa ya kabla ya wakoloni, kama vile Bukini au Zanzibar. Wakati wa harakati za uhuru mara kwa mara kulikuwa pia na mwelekeo wa mtazamo wa Afrika yote (*pan-African*), hasa baada ya uhuru wa Ghana mwaka 1957, kama inavyojidhihirisha katika mambo kama msukumo waliopata Kenneth Kaunda na Hastings Banda kuhusu mapambano yao dhidi ya Shirikisho la Afrika ya Kati katika mkutano wa All-Africa People's Conference (Mkutano wa Watu wote wa Afrika) uliofanyika Accra 1959.[38]

Mfano mwingine wa harakati za mwelekeo wa kiwango cha Afrika yote ni lile jaribio ambalo halikufanikiwa la kuanzisha katika medani ya chini shirikisho la Afrika Mashariki kati ya Uganda, Kenya na Tanzania kwenye miaka ya 1960.[39] Katika Zanzibar pia kulikuwa na dalili za kiwango cha kutafuta Umoja wa Waarabu wote[40]. Na kwa kuwa nchi hizi zote zilikuwa zimetawaliwa na Uingereza, harakati za kupigania uhuru ziliathiriwa pia na mifano ya nyuma ya mapambano ya kuelekea kwenye serikali ya kujitawala wenyewe katika nchi za Umoja wa Madola, kama vile India na Pakistan, na Canada na Australia.

Lakini kwa upande wa Ufaransa hali ilikuwa tofauti. Wafaransa walikuwa wanawania kupanuka kwa Ufaransa kwa kubadilisha umiliki kuwa usawa kwa kutumia mbinu ya kuyafanya makoloni yawe sehemu ya Ufaransa kiutawala. Katika Bukini baada ya Vita vya Pili vya Dunia, Wafaransa walitoa kidogo mno na mapema mno, baada ya kushindwa kwa Vichy, kuwezesha sera hiyo kukubalika bila upinzani wowote. Lakini katika koloni la zamani la Reunion mambo yalikuwa tofauti.

## Reunion[41]

Mwanzoni Reunion ilikaliwa na mabaharia wa Kifaransa na watumwa wa Kiafrika katika karne ya kumi na saba. Katika karne zilizofuata, nchi hiyo ikawa koloni la kilimo cha miwa, likiwa na mmiminiko wa watumwa wa Kiafrika katika karne ya kumi na tisa, na kwa miaka thelathini tena kukapatikana vibarua wa manamba kutoka India. Hadi kufikia mwaka 1946, robo tatu ya eneo linalolimika katika kisiwa hicho likawa limepandwa miwa, na chama cha kikomunisti cha humo nchini na

[38] R.L. Rotberg, 1966, uk. 292

[39] Tazama J.S. Nye, Jr. 1966. Kunatakiwa kufanyika kazi zaidi kuhusiana na suala hili

[40] Tazama A. Clayton, 1981, uk. 40 na uk 46

[41] Kuhusu Reunion, ninamshukuru J. Houbert, 1980, uk. 145-75 na 325-47; na M. Robert, 1976

kile cha French Communist Party vikawa na azma ya kulishambulia tabaka la mamwinyi wa mashamba ya miwa kwa kuwaingiza katika taifa la Kifaransa, na kwa namna hiyo kuinua maisha ya watu masikini. Katika miaka kumi iliyofuata, hali ya maisha ilipanda, lakini si kama ilivyokuwa Ufaransa kwenyewe. Kudumaa kwa uchumi ambako kulikuwa kumeliathiri vibaya eneo hili la volkano lisilolimika, lililoko km 700. mashariki ya Bukini tangu Vita vya Napoleon, sasa kukawa kumemalizika baada ya Reunion (pamoja na *French West Indies*) kugeuzwa kuwa *departement* (jimbo) ya ng'ambo mnamo mwaka 1946.

Kuanzia hapo, Reunion ukawa mfano tofauti kabisa wa kuondokana na ukoloni kwa visiwa vile ambavyo vilikuwa bado vinatawaliwa na Waingereza, yaani Ushelisheli na Maurtius, pamoja na mifano mingine ya bara ambayo imekwishajadiliwa. Lakini baada ya ushindi wa wafuasi wa de Gaulle katika Ufaransa mnamo 1958, wakomunisti wenyeji wakageukia sera ya kutaka Reunion iwe huru; na kama sera hii itaweza kugeuka kuwa madai ya wana-Reunion wengi kutaka uhuru kamili kutoka kwa Ufaransa, shinikizo linaweza kutokea kuilazimisha Reunion kufuata njia ya kawaida katika kufikia kujitawala katika mfumo wa kimataifa.

## Visiwa vya Ngazija (Komoro)[42]

Kiethnografia Visiwa vya Ngazija vinafanana zaidi na Zanzibar na maeneo mengine ya pwani ya Afrika Mashariki kuliko ilivyo kwa wa-Kreole na wakazi wa mijini wa Reunion, Mauritius na Ushelisheli. Wanazungumza Kiswahili. Mayotte ilichukuliwa na wakoloni wa Kifaransa baada ya kununuliwa kutoka kwa Sultani wa pale mnamo mwaka 1841, na visiwa vingine vikafuata katika kinyang'anyiro cha Wazungu cha makoloni mwishoni mwa karne hiyo. Wakati wa ukoloni, visiwa vya Ngazija havikuwa na maslahi makubwa kwa Ufaransa. Ama kwa hakika upingaji wa ukoloni uliofanywa na wazalendo haukujitokeza visiwani humo mpaka mwaka 1968, wakati askari wa miguu na askari wa miavuli wa Kifaransa walipozima kikatili mgomo wa wanafunzi, na watu wakapinga kitendo hicho kwa kuandamana barabarani. Vyama vya kwanza vya kisiasa vikaanzishwa, na kutokana na msukosuko wa siasa katika nchi jirani, yaani Bukini, na kutaifishwa kwa makampuni makubwa ya Kifaransa humo nchini -yakatokea madai katika nchi nzima kudai uhuru wa visiwa vyote vya Ngazija pia.

[42] Maelezo haya yamepatikana kutoka kwa H. Chagnous na A. Haribu, 1980; na T. Flobert, 1976

Wafaransa wakaamua kutaka kura ya maoni ya wananchi wa visiwa vyote, lakini kwa kuwa Mayotte (kisiwa ambacho kina Waislamu wachache zaidi, na kilichoathiriwa zaidi na Wamalagasi Wakristo) kilipiga kura dhidi ya mwelekeo wa jumla wa visiwa vingine, na kikadai kuendelea kuwa chini ya Ufaransa, utaratibu mwingine wa upigaji kura hizo ikabidi ufanywe, wakati huu kura zikipigwa kisiwa hadi kisiwa. Visiwa vyote, kasoro Mayotte, vilijitangazia uhuru wao mnamo Julai 1975. Ni kisiwa cha Mayotte peke yake ambacho kinaendelea kujiita kisiwa cha Ufaransa.

## Mauritius na Ushelisheli[43]

Kisiwa cha Mauritius, kama kilivyo kisiwa cha Ushelisheli, kiko maili mia kadhaa kutoka pwani ya Bukini na kilianza kama koloni la zamani la kilimo cha miwa katika karne ya kumi na tisa. Kazi nyingi katika mashamba ya miwa zilifanywa na watumwa wa zamani na vibarua wa manamba kutoka India, wakati wale makabaila wenye mashamba, Ma-Kreole wa Kifaransa-Kimauritius (machotara wa Kifaransa-Kimauritius), wakawa ndio wenye kufaidi zaidi matunda ya kazi hizo. Kama makoloni mengine ya zamani yaliyokuwa yanalima miwa West Indies na katika Bahari ya Hindi, Mauritius iliathirika vibaya na Mdororo Mkubwa wa Uchumi miaka ya 1930, ambao uliacha hali ya machungu ya migomo na misukosuko ya wafanyakazi. Siasa za Mauritius za baada ya 1945 zilijihusisha zaidi na haki za wafanyakazi katika mashamba ya miwa na katika magati dhidi ya makabaila, madai ya uhuru yakiwa hayapewi sana msukumo hadi hapo baadaye. Ama kwa hakika, kutokana na hali iliyojitokeza katika Reunion baada ya mwaka 1946, mahusiano ya karibu zaidi na Uingereza yakawa ndilo jambo la kuwania. Kwa hiyo, harakati za uhuru katika Mauritius zilikuwa zimeegemea sana katika jitihada za Uingereza katika miaka ya 1960 za kuingia katika Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Ulaya (European Economic Community) wakati sawia na Mauritius ilipokuwa ikielekea kwenye uhuru

Uhuru ulipatikana mwaka 1968 kupitia chama cha Mauritius Labour Party, chama ambacho daima kilionyesha mwelekeo wa uzalendo kuliko vyama vingine vyote, na ambacho idadi kubwa ya wanachama wake walikuwa wale wafanyakazi wa Kihindu wa tabaka la chini wa kisiwa hicho. Hata hivyo kulikuwa na mtego

[43] Kuhusu Mauritius na Shelisheli, ninatoa shukrani kwa J. Houbet, 1980, na L. Favoureu, 1970, ambao wana marejeo mazuri

mwingine, baadhi ya visiwa, ambavyo hadi wakati huo vilikuwa vinahusiana na Mauritius au Ushelisheli, vilikatwa na kuingizwa katika kundi la visiwa vilivyo katika *British Indiana Ocean Territory* (Eneo la Uingereza la Bahari ya Hindi), koloni jipya la baharini ambalo muda mfupi tu baadaye likawa ndiyo mahali kituo cha Marekani cha nyambizi za kinuklia huko Diego Garsia kilipoanzia. Ni jambo lililo wazi kwamba uhuru wa Mauritius uliandamana na masharti haya.[44]

Uhuru wa Ushelisheli pia ulicheleweshwa kwa muda kwa mikakati ambayo ilihusiana na kituo cha kuongozea vyombo vya angani na pia Diego Garsia. Lakini kwanza, si chama cha Albert Rene cha Seychelles Peoples United Party (SPUP) wala chama cha James Mancham cha Seychelles Democratic Party (SDP) ambacho lengo lake la msingi lilikuwa kupata uhuru kutoka kwa Uingereza. Badala yake vyama hivyo vilijishughulisha zaidi na udhibiti wa nafasi za kazi na sera serikalini katika koloni hilo dogo la kisiwani lililoandamwa na ufukara. Ni wakati tu ulipotokea mzozo baina ya SDP na Waingereza juu ya udhibiti wa polisi kisiwani humo kabla ya kupata uhuru kamili, na SPUP kutambuliwa na OAU kama chama cha ukombozi wa taifa, ndipo suala la uhuru likaanza kupewa uzito. Hatimaye Mancham akaungana na Rene kupigania uhuru ambao Uingereza, ikiwa sasa imepania kujitoa katika makoloni yake yaliyobaki upesi iwezekanavyo, haikusita kuutoa mnamo mwaka 1976.

Kwa hiyo ukoloni ukawa umekamilisha mzunguko wake tangu karne ya kumi na nane ulipoanza. Wakati huo visiwa-makoloni kama Ushelisheli, Mauritius na Reunion vilikuwa viungo muhimu sana kati ya dola za Ulaya ambazo kimsingi zilikuwa za baharini. Kisha baada ya kugunduliwa kwa injini za mwakondani, ukaanza sasa utamalaki wa nchi kubwa kubwa za bara kama vile Afrika-kusini mwa Sahara, na watu wa Magharibi wakawa mabwana wa dola za mabara ya tropiki na ambayo yalikuwa na idadi kubwa ya watu. Msukosuko wa Vita vya Pili vya Dunia vilivyoikumba dunia nzima ukazidhoofisha himaya hizo nyingi. Kile ambacho vita vyenyewe havikufanya, kikakamilishwa na "wakulima wadogo ambao hawakutekwa" na vyama vya kizalendo na sera katika kizazi kimoja tu. Lakini baada ya majilio ya enzi za nuklia-joto, ukoloni wa kibahari umeanza kujitokeza tena, ukiwa na umuhimu wa kutisha!

44 Tazama, J. Madeley, 1982

# 10 Afrika ya Kusini Tangu 1945*


## Utangulizi

Kunako mwaka 1935 Afrika ya Kusini tayari ilikwisha kuwa sehemu muhimu kiuchumi kuliko sehemu nyingine zote za Afrika. Wakati huo huo katika theluthi ya mwisho ya karne ya ishirini, Afrika ya Kusini limekuwa pia eneo la Afrika ambalo ni muhimu kupita yote kimkakati. Utukufu wa uchumi wake ulitokana na utajiri wa madini ambayo ni muhimu sana kwa ustaarabu wa viwanda wa Kimagharibi. Kulikuwa pia na kilimo cha mashamba makubwa na uendelezaji wa viwanda vya ndani. Utukufu huo wa kimkakati umetokana na mchanganyiko wa utajiri wa eneo hili na kuongezeka kwa umuhimu wa njia ya Cape kwa ajili ya usafiri wa bahari kati ya Asia na ulimwengu wa Magharibi. Jambo la tatu muhimu ni matatizo ya ubaguzi wa rangi.

Sura hii inahusu mwingiliano baina ya uchumi, mikakati na jamia (makundi ya jamii kwa mujibu wa rangi ya ngozi) katika majaliwa ya Afrika ya Kusini. Katika medani ya uchumi hadithi ya Afrika ya Kusini zaidi ni hadithi ya ardhi, hasa harakati za kupigania ardhi bora na yenye rutuba. Hadithi hiyo pia inahusu mitaji ambayo kimsingi inatokana na au inahusina na shughuli za uchimbaji madini.

Ama kuhusu suala la jamia au rangi, Afrika ya Kusini ndiyo uwanja wa mwisho mkubwa wa mapambano ya kijamia katika bara zima. Miaka ya 1935 hadi 1945 ilidhihirisha mafanikio makubwa ya mapambano dhidi ya ufashisti na ukandamizaji wa kimbari katika Ulaya. Mwaka 1948 ulikuwa ndio mwanzo wa kuinukia kwa aina nyingine ya ufashisti na ukandamizaji wa kijamia katika Afrika ujulikanao

* Dhana "Afrika ya Kusini" katika sura hii inazingatia eneo lote la kusini mwa Afrika na wala sio nchi pekee ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini.




*Picha 10.1 Raslimali kuu za madini katika Afrika ya Kusini*

kama *ubaguzi wa rangi*. Kushindwa kwa Hitler na Mussolini katika nusu ya kwanza ya miaka ya 1940 kwa hakika lilikuwa pigo kubwa sana dhidi ya "utukufu" wa jamia kuu ya Wa-Arya (watu wa jamia ya Kihindi Kizungu)" na sera za Ulaya za uangamizaji wa jamia nyingine. Kushinda kwa "Chama cha Kitaifa" katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini mnamo mwaka 1948 ulikuwa ni ushindi kwa " 'utukufu' wa watu weupe" katika sehemu hii ya Afrika. U-Hitler ulikuwa unazaliwa upya katika ardhi ya Afrika.

Sura hii pia inatoa mitazamo ya kihistoria ya uchumi wa kisiasa wa ukoloni wa Ulaya na majibu ya Waafrika dhidi yake katika Afrika ya Kusini. Dhamira kuu itakuwa ni kutegemeana kati ya matabaka ya kiuchumi kwa upande mmoja na asasi za kisiasa kwa upande mwingine.

## Usuli wa enzi za *ubaguzi wa rangi*

Katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini, jambo kubwa lililojitokeza lilikuwa ni mapambano ya watu wa Ulaya katika kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwa na ukiritimba wa uchumi juu ya ardhi, madini, kazi na huduma za jamii, na kuuzima ushindani wowote wa Kiafrika uliokuwepo au ambao ulifikiriwa kuwepo.

Masetla walitaka zitungwe sheria ambazo zingewaondoa kabisa Waafrika katika ushindani wa aina yoyote juu ya ardhi, madini na bidhaa za kilimo, na wakati huo huo zikiwa zinawahakikishia nguvukazi rahisi ya Waafrika. Watumishi wa serikali na weledi walitaka zitungwe sheria ambazo zingeondolea mbali ushindani wowote kutoka kwa wafanyakazi wa Kiafrika na wakati huo huo zikiweka mzigo wa kodi kwa Waafrika.

Hadi kufikia mwaka 1930, nchi zote mbili zilikwishapitisha msururu wa sheria za kibaguzi kwa madhumuni ya kunyang'anya ardhi na madini ya Waafrika, kupata nguvukazi rahisi ya Waafrika, kudhibiti mijongeo ya vibarua wa Kiafrika na kuondoa ushindani wa kijamia.

Sheria za Usuluhishi katika Viwanda katika nchi zote mbili zilikuwa ni sheria za mahusiano katika kazi katika viwanda vyote, sekta mbalimbali na wafanyakazi wa uchumi wa nchi hizo. Lakini sheria hizo hazikutambua vyama vya wafanyakazi vya Waafrika wala hazikuwatambua wafanyakazi wa Kiafrika kama waajiriwa. Badala yake, sheria hizo ziliyapa mamlaka mabaraza ya viwanda, ambayo yalijumuisha waaijiri na wafanyakazi weupe, kujadili na kuafikiana juu ya mishahara, mazingira ya kazi na mafao ya Waafrika. Waafrika hawakuruhusiwa kuingia katika mipango ya uanagenzi, na hawakuwa na haki ya kugoma wala kulalamika juu ya malipo. Katika Sheria za Fidia za Wafanyakazi, Waafrika hawakuingizwa katika

taratibu za mafao ya kustaafu, mipango ya matibabu, na hatua mbalimbali zilizokuwa zimewekwa kulinda usalama wa wafanyakazi.

Kugawanywa kwa nchi katika ardhi ya Wazungu na ardhi ya Waafrika kulifanywa kwa makusudi kwa lengo la kusambaratisha nguvu na uwezo wa Waafrika katika kujitegemea kwa kuwapa maeneo ya vijijini yaliyotengwa, ambayo hayakuwa na rutuba, na mageto ya mijini.

Hadi kufikia mkesha wa Vita vya Pili vya Dunia, kulikwishakuwepo na uhusiano wa kutegemeana baina ya makoloni ya masetla kwa upande mmoja na nchi za pambizoni kwa upande mwingine, k.m. nchi zilizokuwa chini ya Ubalozi wa Uingereza, kama vile Basutoland (ambayo sasa ni Lesotho), Bechuanaland (ambayo sasa ni Botswana) na Swaziland; nchi zilizokuwa chini ya ulinzi wa Waingereza za Rhodesia Kaskazini (sasa Zambia) na Nyasaland (ambayo sasa ni Malawi), na makoloni ya Kireno ya Angola na hasa Msumbiji. Basutoland, Bechuanaland na Swaziland ndizo zilizokuwa za kwanza kuwa bantustani za pambizoni mwa Jamhuri ya Afrika ya Kusini.[1]

Basutoland ilikuwa imezungukwa kabisa na Jamhuri ya Afrika ya Kusini, ikiwa na idadi ndogo sana ya Wazungu ambao zaidi walikuwa ni maofisa wa serikali, wafanyabiashara na wamisionari; na ilikuwa na wakulima wadogo wadogo na wafugaji katika ardhi iliyomomonyoka. Kimsingi Bechuanaland lilikuwa eneo pana lenye jangwa lililotegemea ufugaji wa ng'ombe na wafanyakazi wahamiaji. Swaziland ndiyo iliyokuwa na hali bora zaidi kati ya nchi hizo tatu kwa sababu ya ardhi yake yenye rutuba, mashapo mengi ya madini ya mbala (mtapochuma), asbesto na madini ya bati, na maendeleo ya shughuli za misitu na kilimo cha umwagiliaji. Lakini sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba walikuwa wamepewa Wazungu.

Koloni la Wareno la Msumbiji kiuchumi lilitegemea mazao ya kilimo yaliyolimwa katika mashamba ya serikali na ya watu binafsi na kusafirishwa nje, ushuru wa forodha na ushuru uliolipwa na Rhodesia kutokana na matumizi ya barabara, reli na bandari ya Beira (Sofala), na ushuru uliolipwa na Afrika ya Kusini kutokana na matumizi ya bandari ya Lourenco Marques (Maputo) na kutoka kwa wafanyakazi wahamiaji. Nchi ya Nyasaland, ambayo ilikuwa chini ya ulinzi wa Waingereza, pia ilikuwa masikini na yenye idadi kubwa sana ya watu. Hapakuwa na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya masetla, wala hapakuhitajika nguvukazi rahisi ya Waafrika; kwa

1 Kuhusu uhusiano wa kihistoria kati ya nchi za Botswana, Lesotho na Saziland naAfrika Kusini, soma R.P. Stevens, 1967; J.E. Spence, 1964 kur. 221-46; na *Migrant Labour in Asrica South of the Sahara*, 1961

hiyo hapakuwepo maeneo yaliyotengewa Waafrika peke yao na hapakuwa na sheria za pasi. Rhodesia Kaskazini ilitegemea tasnia moja tu, uchumi ulioegemea zaidi kwenye bidhaa za kusafirishwa nje ambazo kiini chake kilikuwa ni ule Ukanda wa Shaba. Kutokana na uwezekano wa ushindani wa kijamia katika kazi na huduma, kulikuwa na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Waafrika, sheria za pasi na uingizaji wa wafanyakazi wahamiaji kutoka Nyasaland, Tanganyika na Kongo ya Wabelgiji.

## Wafanyakazi wahamiaji

Uhamiaji wa wafanyakazi mara nyingi unatokana na kichocheo cha uchumi ambacho nacho hutokana na kutokuendelea, ukosefu wa kazi, hali duni za maisha na umasikini wa jumla unaojitokeza katika nchi watokazo watu hao. Lakini katika maeneo ya Afrika ya Kusini mfumo wa uhamiaji wa wafanyakazi ulikuwa umejikita katika mahusiano ya kinchi yaliyokuwa na udhibiti wa hali ya juu.

Katika Basutoland, Bechuanaland, Swaziland, Msumbiji, Angola na Nyasaland kulikuwa na mawakala wengi wa kuandikisha wafanyakazi na ambao kwa makusudi kabisa waliwashawishi wakulima ambao walikuwa hawajui kusoma wala kuandika kwa kuwalipa malipo ya chambele, kuwapa bidhaa za mijini na matangazo yaliyosifia maisha mazuri ya mijini huko Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini. Kulikuwa pia na motisha ya kiuchumi kwa yale makoloni ambayo yalisafirisha nje nguvukazi kutokana na ada za leseni, pasi na hati za ushuhuda; ada ambazo ziliziingizia nchi zilizohusika fedha za kigeni.

Wareno katika Msumbiji walitumia nguvu za kikatili katika kuwaandikisha kazi Waafrika kwa ajili ya nguvukazi ya kusafirisha nje ya nchi,[3] wakisaidiwa na mikataba miwili; Mapatano ya Msumbiji yaliyofanywa katika mwaka 1928 kati yao na Jamhuri ya Afrika ya Kusini, na Mkataba wa Tete, ambao ulifanywa mnamo mwaka 1934 kati yao na Rhodesia Kusini.[4]

Mfumo wa wafanyakazi-wahamiaji umekuwa na athari muhimu sana katika Afrika ya Kusini. Ulisabisha nchi zilizokuwa zikipeleka watu wao kufanya kazi nchi za nje kuzitegemea sana nchi zilizokuwa zikiwapokea watu hao, na ukasababisha mvurugiko wa kijamii kutokana na familia kuvunjika.

Katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini wafanyakazi weupe na mabwanyeye wa vijijini, zaidi wakiwa Waafrikana (makaburu) walikuwa wameunda chama cha

[3] Ibid: also, J. Duffy, 1962; na J.E. Spence, 1964

[4] Migrant labour in Africa South of the Sahara, 1961

*Nationalist Party* ili kushindana na chama cha *United Party*[5], ambacho kilikuwa chama cha mabwanyenye weupe wa mijini, weledi na mabepari wa kimataifa; wengi wao wakiwa wasemaji wa Kiingereza. Tofauti za maoni baina ya Waingereza na Waafrikana juu ya mbinu makini zaidi za kulinda utukufu wa watu weupe dhidi ya Waafrika ziliishia, katika uchaguzi wa mwaka 1948, katika ushindi wa chama cha *Nationalist Party* kilichokuwa kikiongozwa na Dr. Malan.

Wakati huo huo Waafrika wakanzisha vyama vya siasa, kama vile chama cha *African National Congress* cha Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini, vyama vya kujitegemea vya ustawi wa jamii, vyama vya wafanyakazi kama vile chama cha *Industrial and Commercial Workers Union of South Africa and South Rhodesia*, makanisa ya yaliyojitenga na ya Ethiopia[6].

Viongozi wa vyama hivi vya siasa walikuwa wasomi Wakristo walioelimishwa katika shule za misioni. Lengo lao kubwa lilikuwa ni "Haki sawa kwa watu wote, bila kujali mbari wala rangi zao"; mbinu walizotumia ni maazimio ya kikatiba, ujumbe, telegramu, hutuba za kanisani, vijitabu, na mikusanyiko; waliungwa mkono na weupe wasio na siasa kali na wamisionari.

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi walijishughulisha zaidi na masuala ya ujira wa wafanyakazi, mazingira ya kazi, nyumba, ubaguzi wa rangi na haki ya kugoma na kufanya mikutano ya pamoja kujadili masuala yanayohusu maslahi yao. Ingawa kulikuwa na sheria zilizokataza kugoma, lakini wafanyakazi wa Kiafrika waligoma. Baadhi ya wahubiri waliosomeshwa na wamisionari na watu wa kawaida walijiengua kutokana na ubaguzi wa rangi na kujitwalia mamlaka ya ki-ubaba waliyokuwa nayo wamisionari weupe, wakaanzisha makanisa yao yaliyojitenga lakini yaliyofuata mafundisho ya dini na liturujia ile ile ya Kikristo. Baadhi yao walikwenda mbali zaidi, wakahubiri kuukataa na kuuacha kabisa utamaduni wa Kimagharibi na maadili yake. Mwelekeo huu wa kidini unajulikana kama U-Ethiopia na wafuasi wake mara nyingi hujulikana kwa jina la *Vapositori*.[7]

Baada ya kushinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1948, Dr. Malan na chama chake cha *Nationalist Party* akaanzisha rasmi sera ya *apartheid* (Ubaguzi wa rangi) na sera ya serikali ya jamhuri. Afrika ya Kusini ikajitoa katika Jumuiya ya Madola na ikajitangaza kuwa jamhuri huru mnamo mwaka 1961.

Kiuchumi, Vita vya Pili vya Dunia vilileta enzi mpya ya kukua na kustawi kwa haraka kwa uchumi, baada ya kudorora na kudoda kwenye miaka ya 1930.

5 S. Trapdo, 1970; W.R. Duggan, 1973; W.M. Macmillan, 1963; G. Carter, 1959; T.D.

6 Tazama kwa mfano, D. Chanaiwa .

7 B. Sundkler, 1961

Kuyumba kwa Ulaya kijeshi na kiuchumi, kutekwa kwa makoloni ya Ulaya huko Asia na Japani, kulisababisha kuwapo na mahitaji makubwa sana ya mali ghafi na bidhaa za viwandani kwa ajili ya matumizi ya majeshi, na pia mahitaji ya mafunzo, mafuta na sehemu za kupatia ahueni katika Afrika ya tropiki. Ikiwa na muundombinu ulioimarika katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini, mfumo wake wa wafanyakazi-wahamiaji na hali ya tabia-nchi iliyokuwa mwafaka, Afrika ya Kusini iliweza kabisa kumudu mahitaji mapya ya wakati huo. Vita vikawa vimebadilisha sekta ya mijini ya utengenezaji bidhaa kutoka katika tasnia ndogo ndogo na kuingia katika tasnia kubwa kubwa na vikaongeza nafasi ya kiuchumi-kijamii ya mabwanyenye wa mijini dhidi ya mabwanyenye wa kimapokeo wa vijijini.

Miongoni mwa Waafrika vita viliongeza idadi na umuhimu wa tabaka la kati la Waafrika ambalo lilikuwa la wafanyabiashara, weledi mbalimbali, walimu, wahubiri na halikadhalika waliokuwa mameneja wa mashamba yao wenyewe na waashi. Vita pia vilisababisha kuwepo kwa tabaka la wafanyakazi wa chini wa mijini na wanajeshi waliokuwa wamepigana vitani ambao walikuwa na mwamko zaidi wa kisiasa na ambao walisisitiza kupewa ujira mzuri, mazingira mazuri ya kazi, mafao na haki za binadamu. Hata hivyo sehemu kubwa ya Waafrika ilikuwa bado ni ya vijijini na ya watu waliolima mazao ya kujikimu tu.

## Wimbi la Mabadiliko Afrika ya Kusini: kuanzia 1948 hadi 1960

Muongo uliofuatia vita ulitawaliwa na migongano na mabadiliko yaliyoletwa na mapambano baina ya watetezi wa utaifa wa Kiafrika na watetezi wa utaifa wa Kizungu. Majilio ya kile ambacho kilikuja kujulikana kama uzalendo wa kijadi wa Kiafrika yalikuwa ni suala lililohusu bara lote baada ya vita. Kuanzia Cape mpaka Kairo Waafrika wakawa wanadai kukomeshwa kwa utawala wa kigeni, ubaguzi wa rangi na ubeberu, na kuleta uhuru wa kisiasa ulioegemezwa kwenye utawala wa wengi, haki ya kupiga kura kwa wote, na demokrasia katika bunge. Walikuwa wakitangaza imani za umoja wa Waafrika wote na umoja wa weusi wote, na walikuwa wanawania Shirikisho la Mataifa ya Kiafrika.

Katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini, chama kikubwa cha Waafrika kilikuwa *African National Congress* (ANC) amhacho msemaji wake mkuu mwenye ushawishi na mwenye kupendwa na watu wakati huo alikuwa ni yule mshindi wa *Tunzo ya Amani ya Nobel* Chifu Albert Luthuli[8]. Chama cha ANC kilipambana

[8] Tazama kwa mfano, P. Waishe, 1971; na A. Luthuli, 1962

kwa nguvu zaidi katika madai na maandamano yake. Lakini hata hivyo kilikuwa kinapata changamoto kutoka kwa wanachama wengine wa Kiafrika wa chama cha *South African Communist Party,* ambao madai yao yalikuwa makali zaidi, na kutoka kwa *ANC Youth League.* Hiki chama cha mwisho kutajwa kilianzishwa mnamo mwaka 1943 na Aton Muziwakhe Lembede, na kilikuwa na wanachama wa Kiafrika ambao walikuwa wamechoshwa na njozi sera ANC za kufanya mapatano na maliberali weupe na kutokuwa kwao na sera ya wazi yenye kudai utawala wa walio wengi na haki ya kupiga kura kwa wote.

Mwaka 1949 ANC walifanya Mkutano wa Pamoja na Wahindi, Machotara na Weupe wenye siasa ya wastani na wakaanzisha Programu ya Kujenga Taifa.

Mnamo mwaka 1955 Mkutano Mkuu wa watu wote, ukiwakilisha Waafrika, Machotara, Wahindi na Weupe ulipitisha azimio la "Hati ya Uhuru kwa Afrika Kusini ya Kidemokrasia ya Baadaye"; hati ambayo ilipigania Afrika ya Kusini iliyokuwa huru, yenye umoja na isiyo na ubaguzi wa rangi na kupendekeza sheria ya haki za msingi za binadamu.

Ikikabiliwa na umoja wa weusi na mapambano, serikali ya *Nationalist*, ikiungwa mkono na *United Party* na *Progessive Party*, ikaamua kuchukua hatua za ukandamizaji kama zile za kupiga marufuku mikutano, kuweka askari wa doria na kusumbuasumbua watu ovyo, kupiga marufuku vyama vya siasa, na kutesa, kufukuza nchini na kutesa ndani baadhi ya watu.

Mnamo mwaka 1954, ilipodhihirika kwamba sheria za ukandamizaji na ghasia za polisi peke yake vilikuwa vinashindwa kuzivunja nguvu za Waafrika, serikali ya *Nationalist*, chini ya Waziri Mkuu Verwoerd, ikateua Tume ya Tomlinson kama njia nyingine ya kupambana na hali hiyo. Tume hii ikapendekeza kuanzishwa kwa sera ile yenye sifa mbaya ya *Bantustan* ambayo ilipelekea kutungwa kwa sheria ya Wabantu Kujitawala Wenyewe (*Bantu Self-government Act)* na sheria ya Bantu Investment corporation (shirika la Uwekezaji Wabantu ya 1959. Chini ya sheria hiyo, Waafrika waligawanywa katika makazi ya watu weusi, ambayo yaliwiana na makazi ya makundi mbalimbali ya kimapokeo ya Wa-Zulu, Wa-Sotho, Wa-Xhosa, wa-Tswana, wa-Tonga na wa-Venda. Katika maeneo hayo, mataifa hayo yalitegemewa kila moja kuendelea kipekee chini ya utaratibu fulani wa kujitawala wenyewe. Masuala ya ulinzi, usalama wa ndani, mambo ya nchi za nje na bajeti yalidhibitiwa na Afrika Kusini ya weupe kupitia kwa mtawala mkuu.

Sera ya *Bantustan* ilikusudiwa kuimarisha utukufu wa weupe. Lengo lake lilikuwa kuhuisha na kuushajiisha uadui wa makundi mbalimbali ya Waafrika kwa kurejesha nyuma mambo yaliyowaunganisha Waafrika, yaani dhana ya umoja wa Waafrika, elimu, kuoana, maendeleo-miji na utaifa. Kisheria Waafrika wote katika



Picha 10.1 Robert Sobukwe, Rais mwanzilishi wa PAC (Pan African Congress: picha ya mwaka 1963

Afrika Kusini "ya weupe" wakawa ni wageni wa muda tu, pasi na kuwa na uhuru wa kiraia na haki ya kumiliki mali.

Sera ya *Bantustan* ikashindwa kuuvunja uzalendo wa Waafrika, lakini ikawa imeigawa Afrika Kusini zaidi kwa kuzua vikundi tofautitofauti miongoni mwa makundi ya kikabila na kijamia. Ikajenga aina mpya ya uzalendo katika *Bantustan*. Baadhi ya viongozi, hasa Chifu Kaiser Mantanzima wa Transkei na Chifu Gatsha Buthelezi wa *Bantustan* ya Kwa Zulu, wakapata sifa za kitaifa na kimataifa. Wakaanza kudai uhuru kamili.

Kama Nelson Mandela alivyokuwa amesema katika hotuba yake ya mwaka 1953, kwa Waafrika wa Afrika Kusini kusingekuwepo na "njia rahisi ya kupatia uhuru." Maandamano mengine ya amani mnamo mwaka 1956 yakasababishwa watu 156 kushitakiwa katika kesi maarufu ya uhaini, ambayo iliendelea hadi mwaka 1961. Kutokana na tofauti za kimtazamo kati ya viongozi wa ANC, mwezi Aprili, 1959 kukaanzishwa chama kingine kilichojulikana kama *Pana-African Congress* (PAC), Robert Mangaliso Sobukwe akiwa raisi mwanzilishi. PAC kilipinga kabisa sera za umoja wa jamia zote na uongozi wa weupe. Wakati huo huo Shirikisho la Vyama Vyote Huru vya Wafanyakazi wa Kiafrika wa Afrika Kusini *(All-African Federation of Free African Trades Unions of South Africa (FEFATUSA))* likanzishwa kutokana na kutoridhika n maongozi ya chama cha jamia zote cha *South African Congress of the Trades Unions* ambacho kilikuwa kikiiunga mkono ANC.

PAC kikatangaza mwaka 1960 kuwa "Mwaka wa takdiri ya nchi yao, matendo yenye matumaini, uhuru na kujiamulia mambo wenyewe" na kwa kuanzia chama hicho kikachagua kuanza na "kampeni kamambe yenye matumaini dhidi ya Sheria za Pasi". Katika sekula ya PAC iliyojulikana kama *Calling the Nation* (Kuliita Taifa), Sobukwe alidai kuondolewa kwa pasi zote na kuwekwa kwa kima cha chini cha mshahara kwa taifa lote.

Kampeni hiyo, ambayo ilifanyika katika sehemu kadhaa kote Afrika Kusini, iliishia na tanzia la Mauaji ya Sharpeville ambako watu 72 waliuawa na 186 wakajeruhiwa. Serikali ikawalaumu wala-njama wenye mrengo wa kikomunisti kwa kuchochea maandamano, na ikavipiga marufuku vyama vya PAC na ANC. Nelson Mandela, Walter Sisulu na watu wengine wa ANC wakaanzisha chama cha siri kilichoitwa *Umukonto we Sizwe* (Mkuki wa Taifa) ambacho shughuli zake hasa ziliendeshwa huko Rivonia, karibu na Johannesburg. Chama hicho kilivamiwa katika mwaka 1963, na baada ya mashtaka maarufu ya Rivonia, viongozi wake wakafungwa kifungo cha maisha huko Robben Island. Vyama vya PAC na ANC vikalazimika kuendesha shughuli zake kwa siri na wakiwa wanaziendeshea nje ya Afrika Kusini; wakati huo upinzani pekee muhimu wa Kiafrika ndani ya nchi ulikuwa ule ulioongozwa na Steve Biko na *Black Consciousness Movement* (Chama cha Kuzindukana kwa Mweusi).

## Shirikisho la Rhodesia na Nyasaland

Rhodesia Kusini, Rhodesia Kaskazini na Nyasaland zilikuwa na shirikisho lilodumu kwa miaka kumi kuanzia 1953 hadi 1963. Serikali ya Uingereza iliazimia kulitumia



Picha 10.2 *Mauaji ya Sharpeville, Afrika ya Kusini, Machi 28, 1960*

shirikisho hilo kujibu mapigo dhidi ya hisia za Wa-Afrikana ambao walichukia utawala wa Waingereza, wakipendelea kuwa nchi yenye Jamhuri na sera ya ubaguzi wa rangi kwa kuitumia nchi jirani ambayo ilipendelea utawala wa Waingereza na ambayo haikuwa na ubaguzi wa rangi. Wafanyabiashara wa kimataifa wa Uingereza na wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini walitaka shirikisho ili walitumie kama eneo jingine la kuwekeza ili kuepuka uwezekano wa kutaifishwa na Wa-afrikana. Watumiaji wa Kiingereza, weupe wachache wa Rhodesia zote mbili na Nyasaland, baada ya kutupilia mbali uwezekano wa kuungana na Jamhuri ya Afrika ya Kusini, ambayo ilikuwa inatawaliwa na Wa-afrikana, walipendelea shirikisho ili kudhibiti uzalendo wa Waafrika na kuzuia uhuru wa nchi za Rhodesia Kaskazini na Nyasaland, ambazo zilikuwa chini ya Ulinzi wa Dola ya Uingereza. Shirikisho lilikuwa na bunge la shirikisho na mabunge ya nchi zote tatu. Mambo yaliyohusu masuala ya Waafrika kama vile nyumba, sheria za pasi na elimu ya chini, yalishughulikiwa na mabunge ya kila nchi. Katika Shirikisho maslahi ya Waafrika yaliwakilishwa na Halmashauri ya Mambo ya Waafrika ambayo ilikuwa na watu wa jamia zote.

Kama eneo mahususi, shirikisho hilo lilibainishwa na maendeleo makubwa ya uchumi baada ya vita yalioandamana na uwekezaji mkubwa kutoka nchi za nje na uhamiaji kwa wingi wa Wazungu. Lakini vuvumko hilo la uchumi lilikinzana vikubwa na hasira ya Waafrika kwa kuona utajiri mwingi, kazi na ujira vikienda kwa watu weupe na wakati huo huo sheria za kikoloni na kibaguzi zikiendelea kudumishwa.

Kwa juhudi za pamoja vyama vya *Nyasaland African Congress,* kikiongozwa na Dr. Hastings Banda, *Northern Rhodesian African Congress,* kikiongozwa na Harry Nkumbula na Kenneth Kaunda, na *Southern Rhodesian African National Congress,* kikiongozwa na Joshua Nkomo, Ndabaningi Sithole na Robert Mugabe vikahamasisha upinzani mkali dhidi ya shirikisho hilo. Serikali ya Uingereza ikateua Tume ya Monckton kufanya uchunguzi kuhusu shirikisho hilo. Tume hiyo ikahitimisha kwamba "ubia huo ulikuwa ni unafiki tu." Mwaka 1963 shirikisho likavunjwa, Nyasaland ikapata uhuru mwaka huo huo wa 1963, na Rhodesia Kaskazini ikawa Zambia huru mwaka 1964.[9]

Huko Rhodesia Kusini, mabwanyenye wa mijini wa baada ya vita walikuwa wamejaribu kudhibiti mapambano ya uzalendo wa Waafrika wafanyakazi wa mijini na wakulima wa vijijini kwa kujaribu kuwashirikisha na kuwasilimisha, kwa kiwango fulani, wale Waafrika wa tabaka la kati lililokuwa likianza kujitokeza kwa kutumia

[9] P. Keatley, 1963

[10] Tazama kwa mfano, L. Bownam, 1973; D. Chanaiwa, 196b; G. Arrighi, 1970; na E.

sera ya ubia, haki ya kupiga kura ambayo iliegemezwa kwenye sifa za elimu na kumiliki mali na kwa kuwapa upendeleo katika masuala ya elimu, nyumba, afya, biashara na kilimo. Waafrika wa tabaka la kati walipoungana na umma mabwanyenye weupe wa mijini wakajikuta katika hali dhaifu zaidi ya kushindana na ukinzani wa kisiasa wa mabwanyenye weupe wa vijijini na wafanyakazi weupe, ambao waliunga mkono chama cha *Dominion Party* na kutetea maslahi ya uchumi wa kibaguzi wa weupe waliokuwa na haki ya kupiga kura.

Mabwanyenye wa mijini wakaamua kuusambaratisha uzalendo wa Waafrika ili wabakie madarakani.[10] Kwa hiyo Bunge likapitisha sheria kadhaa za ukandamizaji kama ile Sheria ya Kulinda Sheria na Amani (Mamlaka ya Kudhibiti Hali ya Hatari). Waafrika wakaanzisha chama cha *The National Democratic Party* (NDP) kwa kutumia katiba, mbinu na uongozi ule wa chama cha ANC.

Katika hatua za mwisho za kujaribu kuwazima wazalendo wa Kiafrika, serikali ya Uingereza, serikali ya masetla, na baadhi ya viongozi wa Kiafrika wakakubaliana na kuanzishwa kwa katiba ya 1961 ambayo iliweka bunge lenye wabunge 50 weupe na 15 weusi, utaratibu wa usumbufu wenye orodha ya A na B ya taratibu za upigaji kura, baraza la katiba na sheria ya haki za binadamu. Hata hivyo viongozi wa Kiafrika walilazimika kuacha kuunga mkono katiba hiyo kutokana na upinzani mkali uliotoka kwa umma. Chama cha NDP kikapigwa marufuku tarehe 9 Desemba 1961.

Mwaka 1962 chama cha *Dominion Party* ( chama cha mabwanyenye wa vijijini na wafanyakazi), kikiongozwa na Winston Field, kikashinda katika uchaguzi mkuu. Chama hicho kikabadilishwa jina na kuitwa *The Rhodesia Front*, na uongozi wake ukawa chini ya Ian Douglas Smith, badala ya Field.

Tarehe 19 September 1962, Waafrika wakaanzisha chama cha *Zimbabwe African People's Union* (ZAPU), chini ya katiba, uongozi, na mbinu zile zile za chama cha NDP. Mwaka 1963 kikaanzishwa chama cha *Zimbabwe African National Union* (ZANU). Sababu za kujitenga kwa vyama vya ZAPU na ZANU, kama zile za kujitenga kwa vyama vya ANC na PAC, zilikuwa ni kutafrika (kukatisha tamaa) kwa muda mrefu kulikotokana na kutokuwepo na maendeleo yoyote juu ya suala la uhuru, kutofautiana kwa maoni kuhusu kuwepo kwa mapamabano ya silaha dhidi ya kutokuwepo kwa mapambano ya namna hiyo, na mapambano ya ndani kwa ndani juu ya serikali ya ukimbizini.

Kati ya Agosti 1963 na Agosti 1964, vyama vya ZANU na ZAPU vilipambana vikali katika jitihada za kupata wanachama; mapambano ambayo yaliandamana na ghasia na vitisho baina ya wapinzani. Utawala wa Smith, ambao ulikuwa unajitayarisha Kujitangazia Uhuru (*Unilateral Declaration of Inependence UDI*)

kutoka kwa Uingereza, ukaitumia vizuri nafasi hii ya migongano ya Waafrika wenyewe kwa wenyewe. Tarehe 26 Agosti, 1964 vyama vyote vya ZANU na ZAPU vikapigwa marufuku na viongozi wake wote wawili wakawekwa kizuizini kwa muda wa miaka kumi, yaani hadi Desemba 1974. Vyama hivyo viwili vikalazimika kufanya mbinu za kichinichini na kukimbilia uhamishoni huko Zambia, Malawi na Tanzania, ambako vilianzisha mapambano ya silaha chini ya uongozi wa Herbert Chitepo, kwa upande wa ZANU na James Chikerema, kwa upande wa ZAPU. Mnamo mwezi Novemba, 1964, utawala wa Smith ukaendesha kura za maoni ya Wazungu wote kuhusu Kujitangazia Uhuru, kisha mnamo mwezi Mei, 1965 ukafanywa uchaguzi mkuu. Tukio la Kujitangazia Uhuru likatokea tarehe 11 Novemba, 1965.

## Msumbiji

Nchini Msumbiji kipindi cha baada ya vita kilitawaliwa na jitihada za Wareno za kulifanya koloni hilo kuwa la uchumi wa kisetla kama ilivyokuwa katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini. Kisiasa, Ureno ilitaka kuyafanya makoloni yake kuwa katika uhusiano changamani nayo. Ikaeneza fikra isiyo yakini ya *missao civilizado* mpya, ambayo kwayo Ureno ilichukuliwa kama taifa kuu lililoyaunganisha mataifa mengine lakini pasi na kuyachukulia mataifa hayo kama makoloni. Msumbiji ikachukuliwa kama jimbo la Ureno na Waafrika wake wakahesabiwa kuwa raia wa Ureno.[11]

Kiuchumi, Ureno ilikusudia kuitumia vizuri hali ya ustawi mkubwa wa uchumi katika makoloni yake iliyotokea baada ya vita katika kutatua matatizo yake ya ndani ya ukosefu wa ajira, kuongezeka kwa idadi ya watu, na mahitaji ya mali ghafi na masoko. Msumbiji ikaendelea kustawi baada ya vita. Njia za reli, barabara na mabwawa ya nguvu za umeme, kama lile la Kabora Bassa, yakajengwa. Makoloni yakatumia kiasi kama asilimia 25 -30 ya bidhaanje za Ureno na yakachangia kiasi cha asilimia 20 - 26 ya mapato ya taifa la Ureno.

Mkakati wa Ureno ulikuwa ni kuimarisha makazi ya Wareno katika Angola na Msumbiji. Matokeo yake yakawa kwamba makoloni yote mawili yakazidi kufanana na makoloni ya kisetla ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia Kusini, kasoro tu kikwazo cha uchache wa mitaji ya uwekezaji na utawala dhaifu wa makoloni.

[11] Tazama kwa mfano, L.B. Serapiano na M.A. El-Khawas, 1979; J. Sykes, 1971; T.M. Okuma, 1962, D. Barmeet na R. Harvey, 1972

Vyama vya kwanza vya kisiasa vilikuwa ni chama cha *National Democratic Union of Mozambique* (UDENAMO), kilichokuwa kikiongozwa na Adelino Gwambe, ambacho kilizaliwa huko Salisbury (sasa Harare) mwaka 1960; na chama cha *Mozambique African National Union* (MANU), ambacho kilianzishwa Mombasa, Kenya, mwaka 1961. Katika mwezi Juni 1962 vyama hivyo viwili vikaungana na kuanzisha chama kimoja kilichojulikana kama *The Front for the Liberation of Mozambique* (FRELIMO), chini ya uongozi wa Dr. Eduardo Chivanbo Mondlane. Kuanzia na kuanzishwa kwa vyama hivi vya kisiasa kukawa sasa na mabadiliko ya mwelekeo kutoka uzalendo wa kijadi na kuwa vyama vya ukombozi, na kutoka mapambano ya kimaandamano na kuwa mapambano ya silaha.

## Nchi zilizokuwa chini ya makamishna wakuu

Mojawapo ya mambo yaliyokuwa yakiwatatiza sana Waafrika katika Basutoland, Bechuanaland na Swaziland, baada ya vita, ilikuwa ni hadhi yao kitaifa, hasa uwezekano wa kuhamishiwa kwao katika Muungano wa Afrika Kusini, kama ilivyokuwa imependekezwa katika Tume ya Tomlinson juu ya sera ya *bantustani*. Suala jingine likawa ni dhima ya namna mbili kati ya makamishina wakazi na wafalme wa jadi. Kukawa pia na tatizo la maendeleo ya kiuchumi na wafanyakazi wahamaji.

Kutokana na upinzani wa pamoja wa Waafrika na Waingereza kukatishwa tamaa na hamu ya Waafrikana kutaka jamhuri, nchi hizo hazikuweza kuhamishiwa katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini. Masuala ya ndani yaliyobaki yalitatuliwa kikatiba tu. Matamko kuhusu mambo ya utawala yakabadilisha hadhi za wafalme wa jadi kuwa wafalme wa kikatiba na halmashauri za wilaya zikafanywa kuwa ndio vyombo vya msingi vya serikali za kienyeji.

Huko Swaziland, ripoti ya mwaka 1963 ya Kamati ya katiba ikakataliwa na wananchi, na baada ya mkutano mwingine wa katiba uliofanyika mjini London nchi hiyo ikapewa kwanza utawala wa wenyewe, mnamo mwaka 1966, ambao ulifuatiwa na uhuru kamili mnamo mwaka 1969. Kwa upande wa Basutoland, kulikuwa na majadiliano ya katiba huko London mnamo mwaka 1958 na huko Maseru mnamo mwaka 1959, majadiliano ambayo yalifuatiwa na amri-za-baraza katika mwaka 1960 ambazo ziliifanya nchi hiyo kupata serikali ya wenyewe. Tarehe 4 Oktoba, 1966 nchi hiyo ikapata uhuru wake kamili na ikawa Lesotho.

Hadhi ya kikatiba ya Bechuanaland ilikuwa na utata kwa sababu ya masuala mawili. Suala la kwanza lilikuwa mgongano baina ya balozi (kamishna mkuu) wa Uingereza, ambaye alitaka kuwa na mamlaka juu ya kuteuliwa kwa machifu na



Picha: 10.3 *Dkt. Eduardo Chivanbo Mondlane (katikati) mwanzilishi na Rais wa kwanza wa FRELIMO (the Frente de L'iberracao de Mocambique), picha ya 1962*

serikali ya wenyeji, na Tshekedi Khama, Chifu wa Ngwato ambaye aliazimia kulinda mamlaka yake na utamaduni wa kijadi. Akitumia Tangazo la Serikali la Utawala wa Kienyeji la 1943, balozi akateua mabaraza ya ushauri ya Waafrika na Wazungu, na kwa kufanya hivyo akawa anaingiza ubaguzi katika siasa za wenyeji.

Suala la pili lilikuwa lile la kutokukubaliana kwa muda mrefu kulikokuwepo (kulidumu kuanzia 1949 hadi 1956) juu ya ndoa ya Seretse Khama, ambaye alikuwa ndiye mrithi mteule wa ufalme, na mwanamke wa Kizungu. Hali hii ilisababisha Seretse Khama aende uhamishoni Uingereza, na kuondolewa milele yeye na warithi wake katika uchifu.

Baada ya mwaka 1956 nchi hiyo ikarejea tena katika utaratibu wake wa kawaida wa kikatiba. Yale mabaraza mawili ya ushauri yakaunganishwa na kufanywa baraza moja tu la ushauri, baraza la kutunga sheria likaanzishwa mnamo mwaka 1960 na chama cha kwanza cha siasa *Bechuanaland People's Party* (Chama



Picha 10 4 Seretse-Khama. Chifu wa Bamangwato (Bechuanaland) aliyekuwa uhamishoni na mkewe Mwingereza, Ruth Williams na binti yao wa miezi 20, Uingereza, Machi 1952

cha Watu wa Bechuanaland) kikaanzishwa mwaka huo huo. Baada ya nchi kupata serikali ya wenyewe kutokana na Mkutano wa Lobatsi wa 1963, nchi hiyo ikapata uhuru kamili tarehe 30 Septemba, 1966 na kujulikana kama Botswana.

## Afrika ya Kusini kuanzia miaka ya 1960 hadi miaka ya 1980: Mapambano ya Silaha

Dhamira kuu ya historia ya Afrika ya Kusini ya miaka ya 1960 na miaka ya 1970 ilikuwa ni maendeleo ya vyama vya ukombozi na mapinduzi yaliyofanywa kwa mtutu wa bunduki katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Rhodesia, Msumbiji, An-

gola na Namibia. Hatimaye Waafrika wakawa wamekubali kwamba msimamo wa kupendelea mabadiliko ya wastani na uzalendo wa kijadi na mapambano ya kimaandamano haukuwa na nguvu yoyote mbele ya nguvu ya masetla na msimamo wao usiotaka mabadiliko.

Vyama vya kupigania uhuru viliegemezwa katika misingi ya itikadi makini ya ukombozi, viambajengo (vijenzi) vyake muhimu vikiwa ni kuukataa kwa kila hali ubeberu, ukoloni, ubaguzi wa rangi; kutetea siasa ya taifa kujiamulia mambo yake lenyewe, umoja wa Waafrika wote, kutofungamana na upande wowote, haki za msingi za binadamu; na mwisho, kufuata siasa ya usoshalisti wa kisayansi kwa kutumia misingi ya Marx na Lenin, katika maeneo ya uzalishaji katika uchumi, mgawanyo wa mali na raslimali, ulaji na mahusiano ya kijamii.

Mapambano haya ya matumizi ya silaha ambayo yalichukua kipindi kirefu yalianzishwa kwenye mwaka wa 1964. Kwa ndani vyama hivi vya ukombozi vilipata misaada ya kisiasa na ya hali na mali kutoka kwa umma wa mijini na vijijini uliopendelea zaidi mabadiliko ya kimaendeleo. Kwa nje vilipata misaada ya hali na mali zaidi kutoka katika Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchu huru za Afrika (OAU), kutoka kwa mataifa yasiyofungamana na upande wowote, na kutoka Urusi, China, nchi za Skandinavia, na makundi mbalimbali ya ulimwengu wa Magharibi ya wanahuruma na yaliyopendelea mshikamano. Vyama vyenyewe vilishirikiana na kusaidiana katika masuala ya mitandao ya taswira za kiusalama na majeshi. Kambi za kuendeshea shughuli hizi na kufundishia watu zilikuwa na makao yake katika mataifa ya msitari-wa-mbele ya Tanzania, Zambia, na, baadaye, Angola na Msumbiji.

Kinyume chake masetla weupe wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Rhodesia, Angola na Msumbiji walipata misaada ya kidiplomasia, na ya hali na mali kutoka serikali za Kimagharibi, hasa Marekani, Uingereza, Ufaransa na Ujerumani Magharibi.

Kikanda majeshi ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Rhodesia, na Ureno yalisaidiana katika mambo ya usalama na mapambano dhidi ya vita vya msituni. Serikali za Ureno na Rhodesia ziliwaweka Waafrika waliokuwa katika kanda za mapambano katika kambi maalumu zilizojulikana kama "Vijiji Vilivyolindwa" kwa kusudi la kuwatenga na kuwafanya wapigania uhuru wafe kwa njaa.

Mafanikio ya kwanza katika mapambano ya silaha yalikuwa katika makoloni ya Wareno: MPLA na UNITA katika Angola na FRELIMO katika Msumbiji. Katika kujihami Ureno ikaimarisha zaidi mfumo wa "vijiji vilivyolindwa" na ikaanza kutumia njia za kikatili na kikandamizaji. Mnamo mwezi Februari, 1969, Dr. Mondlane akauawa. Akarithiwa na Samora Machel.

Pamoja na misaada mikubwa kutoka serikali za Kimagharibi vita katika makoloni yao vikawa mzigo mkubwa kwa Ureno. Hadi kufikia mwishoni mwa 1960 Ureno ikawa inatumia takribani nusu ya bajeti yake ya mwaka katika vita vya makoloni yake, na wananchi wa kawaida katika Ureno walikwishakata tamaa. Tarehe 25 Aprili, 1974 jeshi likaipindua serikali ya Rais Kaetano na kumweka madarakani Spinola, jenerali ambaye alikuwa mkuu wa serikali ya kijeshi na ambaye alitangaza azma yake ya kukomeshwa kwa ukoloni wa Ureno.

Kutokana na matatizo ya nyumbani na kuongezeka kwa gharama za maisha na hali ya kifedha kulikotokana na vita katika makoloni, Ureno ikawa haina budi kutafuta njia ya haraka ya kuachana na sera za makoloni. Tarehe 8 Septemba, 1974 wakatia saini Mkataba wa Lusaka ambao ulianzisha serikali za mpito katika Angola na Msumbiji, na ukaweka utaratibu wa kuendeshea uchaguzi mkuu. Mnamo mwaka 1975 Angola na Msumbiji zikapata uhuru kamili chini ya vyama vya MPLA na FRELIMO, katika mfuatano huo.

Uhuru wa Angola na Msumbiji ulikuwa na athari kubwa katika mapambano ya silaha huko Afrika ya Kusini, hasa katika Rhodesia na Namibia. Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Rhodesia hazikuwa tena zimekingwa na Angola na Msumbiji. Sera ya Marekani ya nchi za nje kuhusu Afrika ya Kusini, ambayo ilikuwa imekusudiwa kuunga mkono na kusaidia serikali za weupe wachache ghafla ikawa batili. Ian Smith, ambaye alikuwa waziri mkuu wa Rhodesia, akalazimika kuwapa Waafrika madaraka. Mataifa ya Magharibi yakalazimika kubadili sera yao ya kuwapendelea weupe wachache na kuifanya sasa kuwa ya kuridhiana na mataifa ya Kiafrika yaliyokuwa mstari-wa-mbele katika harakati za ukombozi. Masetla wakashinikizwa kufanya maafikiano na viongozi wa Kiafrika juu ya migogoro yao ya ndani. Angola na Msumbiji huru zikawa msaada mkubwa sana kwa vyama vya ukombozi vya Rhodesia, Jamhuri ya Afrika ya Kusini na Namibia kutokana na uzoefu wao wa mipango na mbinu za kijeshi. Wakatoa vituo vyao vya zamani na kambi zao za mafunzo kwa jirani zao waliokuwa wakikandamizwa. Angola, Msumbiji, Botswana, Tanzania na Zambia, zote zikawa katika mstari wa mbele katika kuvisaidia vyama vya ukombozi. Vyama vya ZANU, ZAPU, *South West Africa's People's Organization (SWAPO)*, ANC na PAC vikaweza kuongeza nguvu na moto wa mapambano ya silaha.

Huko Rhodesia, chama cha *United African National Council* (UANC) kilianzishwa chini ya uongozi wa Askofu Abel Muzorewa kutokana na ombwe lililokuwepo katika mamlaka ya uongozi na kwa kuitikia mazungumzo ya amani ambayo yalidhaminiwa na serikali ya Uingereza. Chama cha UANC kilikuwa na azma ya kuondoa ukoloni kwa njia ya maandamano ya kupigania haki. Baadhi ya

wafuasi wenyeji wa ZANU na ZAPU pia walikuwa katika UANC.

Uhuru wa Msumbiji ukaleta matumaini mapya na nguvu mpya kwa vyama vya ZANU, ZAPU na UANC, na ukamfanya Smith akubaliane na ushauri wa kufanya majadiliano ya maafikiano.[12] Kutokana na shinikizo kutoka Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Uingereza na Marekani, Smith akakubali kuwaachilia huru viongozi wa Kiafrika waliokuwa wametiwa kizuizini ili wakashiriki katika mazungumzo ya katiba huko Victoria Falls mnamo mwaka 1974. Kutokana na kutofanikiwa kwa mkutano huo Nkomo, Sithole, Mugabe na Muzorewa wakajaribu kuunda chama kimoja chini ya mwavuli wa chama ch UANC kikiongozwa na Askofu Muzorewa; jaribio hilo halikufanikiwa. Kisha Nkomo na Mugabe kwa pamoja wakaunda chama cha Umoja wa Wazalendo (Patriotic Front) ambacho kiliyashajiisha mapambano ya silaha yakiwa na vituo vyake vikuu huko Zambia na Msumbiji.

Mkwamo huo hatimaye ulitatuliwa katika Mkutano wa Lancaster House wa mwaka 1979 ambapo Smith, Muzorewa na Umoja wa Wazalendo walikubaliana na Katiba ya Lancaster House. Mkutano huo ukaweka taratibu na shuruti za uchaguzi mkuu ambao utasimamiwa na Uingereza, bunge la Waafrika 80 na weupe 20, sheria za haki za binadamu, haki ya kila mtu kupiga kura na kutolewa uhuru mnamo mwaka 1980. Katika uchaguzi mkuu chama cha ZANU-PF kikapata kura nyingi. Akiwa sasa ni Raisi wa chama cha ZANU-PF, Robert Mugabe akawa Waziri Mkuu na akaunda serikali. Mchungaji Canaan Banana akachaguliwa kuwa Raisi. Tarehe 18 Aprili, 1980 koloni la zamani la Rhodesia likawa taifa huru la Zimbabwe.

## Tatizo la Namibia

Katika ukoloni wa Ulaya, Namibia ilianza kama koloni la Ujerumani la Afrika Kusini-Magharibi hadi mwaka 1920 ilipowekwa chini ya udhamini wa Mwungano wa Mataifa (League of Nations) ikiongozwa na Uingereza. Uingereza ikanaibisha uongozi wa nchi hiyo kwa serikali ya Mwungano wa Afrika Kusini ambayo ilikuwa imeegemea sana upande wa Waingereza. Afrika ya Kusini ilipokuwa jamhuri ambayo ilitawaliwa na Wa-afrikana ikaendelea kuitawala Namibia kama jimbo lake. Sheria za Ubaguzi za Afrika ya Kusini pia zikatumiwa Namibia.

Kiuchumi, Namibia ikawa ndipo mahala ambapo Afrika ya Kusini ilipatia mali ghafi na wafanyakazi wahamiaji. Uchumi wa Namibia ulikuwa ni pamoja na uchimbaji migodi (dhahabu, urani, shaba nyekundu, zinki na risasi), kilimo (ufugaji

[12] UNESCO, 1981b



*Picha 10.5 Kuanzia kushoto, Sally Magabe, Waziri Mkuu Robert Mugabe, Rais REv. Canaan Banana na Makamu wa Rais Simon Muzenda Picha ya 1980, wakati wa uhuru wa Zimbabwe*

wa ng'ombe na kondoo) na uvuvi. Ulikuwa ni uchumi wa kikoloni-mamboleo ambao ulikuwa umeelekezwa zaidi nje na ukiwa umekitwa katika utumiaji wa maliasili kwa ajili ya kusafirisha nje.

Kisheria, Namibia ikawa nchi ya udhamini ya Umoja wa Mataifa, umoja ambao ulichukua nafasi ya Mwungano wa Mataifa. Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa likaamua, mnamo mwaka 1966, kwamba kitendo cha Afrika ya Kusini kuichukua na kuitawala Namibia hakikuwa halali. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa likapitisha azimio hilo hilo mnamo mwaka 1969 na baada ya kesi iliyochukua muda

mrefu Mahakama ya Kimataifa ya Kulinda Haki ikatoa uamuzi, mnamo mwaka 1971, ambao uliunga mkono maamuzi ya Umoja wa Mataifa. Kwa hiyo Umoja wa Mataifa ukaanzisha Baraza la Umoja wa Mataifa la Namibia kama mtawala halali wa Namibia, na likakitambua chama cha SWAPO kuwa chama kilichokuwa na uwakilishi halali wa watu wa Namibia. Lakini kutokana na sababu za kisiasa, kiuchumi na kijeshi, Afrika ya Kusini ikakataa kutoa uhuru kwa Namibia, ikiwa imeghairi na kuyadharau maamuzi ya jamii ya ulimwengu mzima.

Uhuru wa Angola na Msumbiji ukabadilisha vikubwa mwelekeo wa mapambano ya silaha katika Namibia na Afrika ya Kusini. Ikiwa inaogopa kwamba Angola na Msumbiji zingeweza kutumiwa kama kipago cha vita vya msituni, Afrika ya Kusini ikaamua kuziyumbisha nchi hizi kwa kuwapa silaha na mafunzo ya kijeshi maadui wao. Katika Namibia Afrika ya Kusini ikafuata mkakati wa pande mbili wa kunyonya raslimali zake, hasa madini, na kuimarisha serikali ya vibaraka wa Afrika ya Kusini.

Chini ya udhamini wa Afrika Kusini chama cha weupe cha *Republic Party* kilichokuwa kikiongozwa na Dirk Mudge na chama cha *South West African National Party*, ambacho kilikuwa na machifu vikaragosi ambao walikuwa wakikipinga chama cha SWAPO, mabwanyenye weupe na wafuasi wao, wakafanya mkutano huko Turnhalle. Huko wakaanzisha chama cha *Democtartic Turnhalle Alliance* na wakakubaliana kufanya mabadiliko madogo madogo ya kuondoa vipengele vya ubaguzi visivyo vya msingi.

Umoja wa Mataifa ukaanzisha mpango wake ambao uliazimia kusimamisha mapambano ya silaha na kuanzisha uchaguzi mkuu kwa ajili ya uhuru wa Namibia. Angola ikaleta majeshi ya Cuba ili kuishinda vizuri UNITA ya Savimbi na Afrika ya Kusini; na Baraza la Congress la Marekani likasitisha kwa muda kuwalipa mamluki wa kivita waliokuwa Angola.

Afrika ya Kusini ikaukataa mpango wa Umoja wa Mataifa na ikaelekea kupendelea zaidi kufanya maafikiano (na viongozi wa Namibia) ili kuzikengeusha lawama zilizokuwa zikitolewa na jamii ya kimataifa, na wakati huo huo ikiimarisha mpango wake wa ukoloni-mamboleo katika Namibia. Mnamo Desemba 1978, Afrika ya Kusini ikadhamini uchaguzi wa wajumbe vikaragosi 50 katika Baraza la Wawakilishi chini ya sheria za kijeshi, wakati ambapo uongozi wote wa ndani wa SWAPO ulitiwa ndani. Kutokana na hali hiyo, mgongano wa Namibia ukawa mapambano yenye sura nyingi zikiwemo SWAPO, nchi za mstari-wa-mbele, Umoja wa Nchi Huru za Afrika na Umoja wa Mataifa katika upande mmoja, na Afrika ya Kusini na Kundi la Kimagharibi la watu walioshirikiana nao kwa upande



Picha 10.6 *Kikosi cha SWAPO (South West Africa People's Organization) kikiwa katika doria.*

mwingine. Hata hivyo, kufikia mwaka 1989, uhuru wa Namibia na ushindi wa SWAPO katika uchaguzi mkuu ukaonekana kuwa dhahiri. Hatimaye mapambazuko ya kisiasa katika Namibia yalikuwa njiani kutokea.

## Jamhuri ya Afrika ya Kusini

Kutokana na mauaji ya kikatili ya Sharpeville na kujiondoa katika Jumuiya ya Madola, chama cha *Nationalist Party* haraka kikaanza kuimarisha mfumo wa ubaguzi na kuigeuza Afrika ya Kusini kuwa dola iliyoendeshwa na polisi kwa kila hali, kwa kuongeza sheria nyingine za ukandamizaji na za kibaguzi. Mwezi Mei, 1963, chama hicho kikapitisha sheria iliyojulikana kama Marekebisho ya Sheria ya

Jumla (*General Law Amendment Act)* ; sheria ambayo iliwapa madaraka polisi kumtia ndani mtu yeyote na asiweze kuonana na mtu kwa muda wa siku 90 ambazo zingeweza kurudiwa tena. Sheria ya mwaka 1965 ya Marekebisho ya Taratibu za Mashtaka ya Jinai (*The Criminal Procedure Amendment Act*), iliwapa mamlaka polisi kumtia kizuizini shahidi wa mahakama bila kuonana na mtu kwa muda wa siku 180, ambazo zingeweza kurudiwa tena. Sheria ya 1968 ya Kupiga Marufuku Kuingilia Mambo ya Siasa (*The Prohibition of Political Interferance Act)* ilizuia chama chochote cha siasa kuwa na wanachama wa rangi mbali mbali. Chama cha *Liberal Party* kiliamua kutoifuata sheria hiyo, lakini chama cha *Progressive Party* kikakubali kuifuata.

Harakati za ukombozi zikazidi kupamba moto. Ndani ya nchi harakati ziliongozwa na wanafunzi na vyama vya wafanyakazi. Mojawapo wa wanafunzi hao alikuwa Steve Biko, mwanafunzi wa uganga katika Chuo Kikuu cha Natal. Akiwa amepoteza imani kabisa na siasa za kibaguzi za chama cha *National Union of South African Students* (NUSAS) kilichodaiwa kuwa cha wanafunzi wa mataifa yote, Biko akawa raisi mwanzilishi wa chama cha *South African Students Organization* (SASO). Chama chao cha kiitikadi kilichojulikana baadaye kama Kuzindukana kwa Mweusi (*Black Consciousness)* kikaleta muungano wa wanafunzi na wafanyakazi. Kwa pamoja vyama hivi vikahuisha mbinu za mapambano ya maandamano zilizokuwa zikitumika kabla ya tukio la Sharpeville. Migomo ya viwandani ilipozidi kuwa mingi na yenye nguvu serikali ikatumia Sheria ya Kudhibiti Ugaidi ya 1967 kumkamata Biko na viongozi wa wafanyakazi. Steve Biko alifia kizuizini tarehe 12 Septemba, 1977 baada ya kuteswa sana na polisi.

Juu ya hayo yote bado upinzani wa kupangwa na wa papo kwa papo uliendeleza mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi ndani ya Afrika ya Kusini. Kati ya Juni na Desemba 1976 wimbi la maandamano na migomo likaitikisa vibaya miji ya Afrika ya Kusini, hasa zile ghasia za wanafunzi katika Soweto ambapo polisi waliwaua wanafunzi 23 na kujeruhi 200. Katika mwaka huo huo chama cha *Azania African People's Organization* (AZAPO) kilianzishwa ili kuleta uhamasishaji madhubuti wa kisiasa.

Serikali ya chama cha *Nationalist Party* ikajibu mapigo kwa kutumia vitendo vikali na vya kikatili vya polisi. Mwezi Novemba weupe wakafanya uchaguzi mkuu na chama hicho cha *Nationalist Party* kikarejeshwa madarakani kwa kura nyingi zaidi. Lakini mzunguko wa ukombozi dhidi ya ukandamizaji ndani ya Afrika ya Kusini, na mapambano ya silaha yaliyokuwa yakiendeshwa na ANC na PAC pamoja na misaada ya nchi za msitari-wa-mbele, Umoja wa Nchi Huru za Afrika,

Umoja wa Mataifa, na sehemu kubwa sana ya jamii ya ulimwengu, yakaendelea kwa nguvu kubwa hadi miaka ya 1980. Hadi kufikia mwishoni mwa 1989 mwafaka wa weupe wa Afrika ya Kusini ukaanza kumomonyoka pande zote.

## Mkakati wa jumla na siasa za kikanda

Katika kipindi hiki cha historia ya Afrika migongano mitatu ya kutoka nje na ya msingi ilisaidia kuongeza thamani ya kimkakati ya Afrika ya Kusini. Migongano hiyo ilikuwa ni: kwanza. Vita vya Pili vya Dunia; pili, Vita Baridi baina ya ulimwengu wa Magharibi na Mshikamano wa Kisovieti; na tatu mgongano wa Waarabu na Waisraeli.

Thamani ya kiviwanda ya madini ya Afrika ya Kusini kwa upande wa Uingereza na himaya yake iliongezeka kufikia viwango vingine kutokana na changamoto ya mataifa adui wao katika Vita vya Pili vya Dunia. Metali muhimu kwa ajili ya viwanda vya nchi za Umoja wa Madola na rafiki zake zilikuwa hatarini. Tishio la pili la kijeshi Afrika ya Kusini kutoka nje lilikuwa latokana na makoloni ya Kiafrika ambayo watawala wake wa Ulaya walikuwa chini ya utamalaki wa Manazi. Kwa mfano, kwa muda fulani Bukini ilikuwa chini ya utawala wa Vichy. Hali hiyo iliendelea hadi Mei 1942 Waingereza walipokivamia kisiwa hicho na hatimaye utawala wa Jenerali De Gaulle ukatambuliwa. Tishio la tatu la kijeshi kutoka nje lilikuwa latokana na meli za kivita au ndege za kivita za Wajapani. Maliasili za Afrika ya Kusini zilikuwa ni kivutio kikubwa sana kwa nchi ya Japan ambayo haikuwa na madini mengi.

Lakini kwa namna nyingi tishio kubwa kabisa kuliko yote lililokuwa likiukabili udhibiti wa Jumuiya ya Madola katika Afrika ya Kusini lilikuwa ni la ndani. Lilikuwa katika Muungano wa Afrika ya Kusini - likichukua sura ya baadhi ya Makaburu kuwaonea imani na kuwaunga mkono Manazi. Lakini kulikuwa na kiasi cha kutosha cha Wa-afrikana waliowaunga mkono weupe waliokuwa wakitumia lugha ya Kiingereza kuweza kuwahakikishia Marafiki zao msaada uliotakikana. Jeshi la Anga la Afrika ya Kusini lilikuwa limepanuliwa na kukawa kumeanzishwa mipango kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza silaha huko Pretoria. Katika kipindi cha Vita vya Pili vya Dunia, umuhimu wa kimkakati wa Afrika ya Kusini kwa ajili ya demokrasia za kiviwanda ulilindwa.

Vita viliishia na kutupwa kwa mabomu ya atomiki huko Hiroshima na Nagasaki. Thamani mpya ya kimkakati ikawa imeongezewa Afrika ya Kati na Kusini - kuwepo kwa madini ya urani. Kwa muda mrefu kidogo Kongo (Zaire) ilikuwa ndio chanzo muhimu kabisa cha urani katika nusu ya kusini ya dunia, na mipango

ya kutafuta vyanzo vingine kusini zaidi ikawa inafanywa. Enzi ya nyuklia ikawa imeingia ulimwenguni, na Afrika ya Kati na Kusini ikawa ni sehemu ya enzi hiyo mpya. Umuhimu wa kimkakati wa eneo hili ukawa umezidi kuwa changamani.

Wakati huo huo ukinzani mpya ukawa umejitokeza katika kipindi cha baada ya vita -Vita Baridi baina ya mataifa ya Magharibi na Mfungamano wa Kisovieti. Vita Baridi vilipoanza mara tu baada ya mwisho wa Vita vya Pili vya Dunia, chuki dhidi ya ukomunisti na Muungano wa Kisovieti ikaanza kujitokeza katika siasa za Afrika ya Kusini. Katika serikali nyingi za Afrika ya Kusini mwelekeo wa kuuona ukomunisti wa ndani kama namna fulani ya "uhaini" ukawa ndio jambo la kulalamikiwa na kupigiwa ngoma. Katika Afrika ya Kusini hali hii ikaishia katika kesi kadhaa za uhaini, ikiwa ni pamoja na ile ya Nelson Mandela na Abram Fischer, wakili mwandamizi wa serikali, ambaye alishitakiwa kwa kuleta ukomunisti na akahukumiwa kifungo cha maisha.

Lakini Muungano wa Kisovieti ulipokuwa unapoteza dalili za kuwepo kwake katika Afrika ya Kusini ukawa unapata hadhi mpya ya kidiplomasia kaskazini mwa Zambezi. Kila nchi ya Kiafrika - iliyokuwa inapata uhuru - ilianzisha mahusiano ya kidiplomasia na USSR. Kwa kitambo fulani Msumbiji na Angola zikawa nchi mbili zilizokuwa marafiki wakubwa sana wa USSR - hadi zikajitangaza zenyewe kuwa jamhuri za mrengo wa ki-Marx na Lenini. Katika mtazamo wa ki-Magharibi umuhimu wa kimkakati wa Afrika ya Kusini kwa ujumla ulikuwa umepata changamoto mpya.

Ukinzani wa kimkakati kati ya Mashariki na Magharibi ulifikia kilele chake lilipokuja suala la kuwepo kwa Wasovieti na Wakuba nchini Angola. Vita baina ya chama-tawala cha MPLA na chama cha UNITA, kilichokuwa kikiongozwa na Jonas Savimbi, vikachukua sura ya kimataifa - Kuba na Muungano wa Kisovieti zikiwa zinakisaidia chama-tawala, na Afrika ya Kusini na Marekani zikitoa ruzuku na kujaribu kukiimarisha chama cha UNITA. Hatima ya Namibia ikajikuta katika msuguano huo - hasa pale Afrika ya Kusini na Marekani zilipotangaza kwamba uhuru wa Namibia ulitegemea kuondoka kwa majeshi ya Kuba katika Angola.

Katika miaka yote ya 1980, kukaendelea kuwapo na mvutano baina ya suala la uhuru wa Namibia, kwa upande mmoja, na mchezo wa kimkakati wa namna ya sataranji kati ya Muungano wa Kisovieti na Marekani, kama ulivyokuwa ukichezwa Afrika ya Kusini, kwa upande mwingine. Sera za Mikhail Gorbachev za *perestroika* na sera ya Marekani ya kuondoa migongano ya kikanda ndizo hatimaye zilisaidia pande zote mbili kufikia muafaka mwaka 1988 - 9.

## Uchumi na siasa za kijiografia

Mgongano kati ya Waarabu na Waisraeli pia ulionyesha umuhimu wa kimkakati wa Afrika ya Kusini. Mwaka 1948 taifa la Kiyahudi lilipokuwa likiinukia katika Mashariki ya Kati Wa-afrikana walikuwa wanachukua madaraka katika Afrika ya Kusini. Mwingiliano wa kihistoria kati ya haya maeneo mawili ya ulimwengu ukawa wa kuendelea kuwepo kwa miaka mingi.

Kiasi fulani cha mwingiliano wa kimkakati kati ya maeneo haya mawili kilitokana na ukweli kwamba pamoja na Afrika ya Kusini kuneemeka sana na utajiri uliomo ardhini kulikuwa na utajiri mwingine wa ardhini ambao eneo hili kwa ujumla halikuwa nao - yaani mafuta. Na kwa hakika mafuta ndio utajiri ambao Mashariki ya Kati ilikuwa nao kwa wingi. Kitu kingine ambacho kinahusiana na siasa za kijiografia za mafuta ni ule ukweli kwamba Mfereji wa Suezi, na Rasi ya Matumaini Mema, kwa muda mrefu sana zimekuwa njia nyingine za kusafirishia mafuta na bidhaa nyingine muhimu za biashara ya kimataifa, hasa kati ya Asia na ulimwengu wa Magharibi. Mgogoro wa Suezi ulisababisha kuwepo kwa mipango ya muda mrefu ya kuwa na meli kubwa sana za mafuta ambazo zilifaa zaidi njia ya Rasi kuliko ile ya mfereji wa Suezi ambayo ni nyembamba sana. Baada ya vita vya Siku-Sita baina ya Waarabu na Wayahudi, mnamo Juni 1967, thamani ya kimkakati ya njia-badala ya Rasi kwa ajili ya meli za mafuta na bidhaa nyingine za kimataifa zilizosafirishwa ikaongezeka vikubwa sana.

Siasa za Mashariki ya Kati na zile za Afrika ya Kusini zilikuwa na maeneo mengine ya mwingiliano. Bada ya kifo cha al-Nasser katika Misri na kuinukia kwa Henry Kissinger kama dalali wa kisiasa katika miaka ya mwanzo mwanzo ya 1970, Muungano wa Kisovieti ukapata vipingamizi katika ulimwengu wa Waarabu. Pingamizi kubwa zaidi lilikuwa kuelekea kwa Misri mrengo wa kulia chini ya urais wa Anwar al-Sadat na kuzidi kupungua kwa siasa kali katika Sudani chini ya Gaffar Nimeiri.

Kufifia kwa athari za Sovieti katika Afrika Kaskazini katika miaka ya mwanzo mwanzo ya 1970 kulikuwa ni kichocheo kikubwa kilichoifanya Sovieti itafute athari kubwa zaidi Afrika ya Kusini. Dau la umuhimu wa kimkakati Afrika ya Kusini lilizidishwa na ukinzani baina ya mataifa makubwa.

Jambo la mwisho kuzingatia katika mwingiliano baina ya Mashariki ya Kati na Afrika ya Kusini linahusu umoja wa kisiasa wa Wafrika na Waarabu. Katika mahusiano baina ya Afrika ya weusi na ulimwengu wa Waarabu umoja umekuwa ni pamoja na kuutangaza ubaguzi wa rangi na Uyahudi kama maadui wasiotofautiana. Mwishoni mwishoni mwa miaka ya 1970 upinzani dhidi ya

uzalendo wa Ki-afrikana na ukinzani dhidi ya Uyahudi vikawa vipengele vilivyochukua nafasi kubwa katika siasa za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Kulikuwa na taashira mbili kubwa zilizoonyesha ukinzani dhidi ya Uyahudi. Taashira moja ni kule kuvunjika kwa uhusiano wa kidiplomasia baina ya Israeli na takribani nchi zote za Kiafrika, hasa mwaka 1973. Taashira ya pili ni kule kufanikiwa kupitishwa kwa azimio la Umoja wa Mataifa katika Baraza lake Kuu, mnamo mwaka 1976, ambalo liliutangaza Uyahudi kuwa aina mojawapo ya ubaguzi wa rangi. Fidia ya mshikamano wa mahusiano baina ya Waarabu na Waafrika ( *quid pro quo* ) ilikuwa ni pamoja na Waarabu kuunga mkono shughuli zote za mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi wa Afrika ya Kusini ( *apartheid* ). Lakini Misri, ikiwa chini ya uongozi wa al-Sadat ilipotia sahihi makubaliano ya Camp David na kuitambua Israeli, mshikamano wa Waarabu na Waafrika dhidi ya Israeli ukawa umedhoofika kwa kiasi fulani. Lakini kwa upande mwingine urafiki wa Israeli na Afrika ya Kusini ukaendelea kuwa imara kwa kiasi kikubwa.

## Hitimisho

Katika sura hii tumejaribu kuonyesha kwamba mambo matatu ambayo yameiathiri Afrika ya Kusini katika kipindi hiki yamekuwa ni uchumi, mikakati na jamia. Kwa upande wa uchumi tumechunguza siasa za ardhi, nguvukazi na mtaji utokanao na madini. Kwa upande wa mikakati tumepeleleza athari ya Vita vya Pili vya Dunia, matokeo ya Vita Baridi baina ya Mashariki na Magharibi na mwingiliano wa kimikakati baina ya Mashariki ya Kati na Afrika ya Kusini kuhusiana na mgongano baina ya Waarabu na Waisraeli.

Lakini kipengele kinachojitokeza katika tajiriba ya Afrika ya Kusini ambacho ndicho kinachozungumziwa sana kimekuwa ni ule msuguano na mvutano wa kijamii katika sehemu hii. Katika kipindi chote tukichunguzacho ubaguzi wa rangi Afrika ya Kusini umejipenyeza katika kila sera na kuvuruga amani katika kila sehemu ya jamii. Thamani ya kiuchumi na kimikakati ya eneo hili ni rasilimali ya muda mrefu. Mageuzi ya kisiasa na kijamii ya mwishoni mwa miaka ya 1980 yanatupa tamaa kwamba madhila ya ubaguzi wa rangi litakuwa ni tatizo la muda tu. Je, yawezekana weusi wa "tabaka la chini" wa Afrika ya Kusini katika karne ya ishirini wakawa ndio tabaka la juu kabisa la Afrika kiuchumi katika karne ya ishirini na moja? Itakuwa ni juu yao kuamua kuitumia nafasi hii ya pekee.

# 11

# Mahadiliko ya kiuchumi Afrika katika muktadha wa Ulimwengu*

Kutokana na zahama ya miaka ya 1930, suala la uchumi likachukua medani ya ulimwengu mzima. Kuanzia wakati huo kila kitu kilichotokea katika sehemu ya kiini kikawa na matokeo hasi kwa sehemu zote za pambizoni, hasa kutokana na kuimarisha ukuaji wa uchumi wa Magharibi.

Vita vya pili vya dunia vilidhihirisha umuhimu wa kimkakati wa Afrika na vikaeneza dhana ya haki ya watu waliokuwa wametawaliwa na wakoloni kujitawala na kujiamulia mambo yao wenyewe.

Ujengaji upya wa nchi na uendelezaji wa viwanda uliotokea baada ya vita ulifuatiwa na hatua ngumu zaidi ya upangaji upya wa uchumi uliooathirika kutokana na makoloni kupewa uhuru. Afua ya jumla ya uchumi iliyopatikana kwenye miaka ya katikati ya 1960 ilileta fikra, ingawa ya muda mfupi, kwamba "maajabu" yalikuwa yametokea. Lakini kudidimia kwa hali hiyo kuliofuatia katika miaka ya 1970 kulileta hali mbaya zaidi katika mahusiano ya Kaskazini - Kusini; na matokeo yake bado hayajatabirika.

## Kuondokana na Mpomoko Mkuu wa Uchumi

### Dhima ya mfumo wa kikoloni katika kupunguza athari za mpomoko

Upangiliaji upya wa uchumi ulianza na mkakati wa kujihami, kukiwa na uimarishaji wa muda mfupi wa sera ya kulinda viwanda katika makoloni. Mapema kwenye mwaka 1928 Ufaransa ilikwisha anzisha "Muungano wa Forodha" ulioiwezesha kuyategemea makoloni. Huko Uingereza azma ya kuirejesha pauni kwenye kiwango

* Sura iliandikwa 1986.

cha dhahabu ilipelekea kupungua kwa mzunguko wa fedha ambako nako kulisababisha kupungua kwa bidhaa zilizosafirishwa nje kwa kiasi cha 30% kati ya 1913 na 1937. Uingereza ikaiegemea Jumuiya ya Madola yake na ikatumia mbinu ya kuvilinda viwanda vyake: kupitia Mkutano wa Uchumi wa Ufalme *(Imperial Economic Conference)* uliofanyika Ottawa mwaka 1932 ikadandia biashara ya madola hayo kwa ajili ya uhai wake. Mwaka 1933 Ureno ilichukua mwelekeo wa kuyashirikisha makoloni yake chini ya udhibiti mkali wa serikali yake, na mnamo mwaka 1937 ikayaeneza mashirika yake ya uchumi na ya kijamii katika makoloni yake: uzalishaji ulielekezwa na kudhibitiwa na dola, ambayo pia ndiyo iliyodhibiti biashara ya nje.[1]

Dola zilitegemea sana muktadha wa uchumi kwani masoko yake ya mikopo yalikuwa yamedhibitiwa sana. Kadri koloni lilivyozidi kuwa karibu na ulimwengu wa Magharibi, ndivyo lilivyozidi kuathirika na taathira za kifedha za kimataifa zilizotokana na msukosuko huo. Lakini msukosuko huo wa fedha wenyewe ulikuwa na athari kidogo katika Maghreb na Afrika ya Tropiki kwa sababu soko la mikopo lilikuwa bado changa. "Kuyategemea makoloni" kukafanya kazi yake ya kupunguza athari za mpomoko kikamilifu: nchi-mama zikapata bidhaa za msingi na nchi za ng'ambo zikawa ndiko mahala pa nchi-mama kupeleka bidhaa zake ambazo hazikuwa na ushindani mkubwa kama vile, nguo, chuma na chuma cha pua. Huko Ufaransa, sera ya kazi kuu za umma kugharimiwa na mikopo iliyotoka nchini humo ilihakikisha kwamba bidhaa za tasnia ya chuma cha pua zilipelekwa katika makoloni, pamoja na kwamba zilikuwa ghali kuliko zilivyokuwa katika sehemu nyingine. Kwa hiyo sekta dhaifu zaidi za uchumi zilisaidiwa. Kwa mfano, bidhaa za viwanda vya nguo vya Ufaransa zilizosafirishwa kwenda Afrika karibu zilifikia mara mbili kati ya 1913 na 1936. Huko Uingereza, kutokana na kupungua thamani kwa sarafu, uchumi ukafufuka, lakini hiyo ilifikiwa kwa kuweka mfumo wa udhibiti, mgawo wa kota na "kupendelea himaya" ambako kulipunguza ushindani lakini kukaongeza kutokuendelea kiufundi.[2]

## Kufufuka kwa uchumi na mfumo wa ulimwengu

Mapatano Mapya ya Kibiashara huko Marekani *(The New Deal)* na Tapo la umma (*Front populaire*) huko Ufaransa vikaleta *uchumi -uliopangwa.* Kwa upande wa Afrika, mabadiliko haya yalikuwa na matokeo ya kuharakisha kujipenyeza kwa ubepari.

[3] Tazama R. Cohen, 1979; na D.O. Meara, 1974

[2] Tazama C. Coquery-Vidrovitch, 1976b

Kuanzia na kipindi cha kufufuka kwa uchumi, ambacho hakikudumu sana, 1936 - 1938, na hasa baada ya Vita vya Pili vya Dunia, haja ya kuwepo na mabadiliko ya kiuchumi yaliyokitwa katika uwekezaji wenye tija ilisisitizwa. Miradi mikubwa mikubwa ikaendeshwa, lakini mara nyingi haikufanikiwa sana kutokana na ukubwa uliokithiri na kutofaa kwake katika mazingira ilimokuwa.

Mabadiliko ya kijamii pia yakaanzishwa na utaratibu wa kikoloni wa kutumikisha watu kazi kwa nguvu ukatoweka na badala yake pakawepo na soko huria la wafanyakazi. Na hapa utawala wa ki-Belgiji uliokuwa na sera za ki-baba ni mfano mzuri: makampuni kama vile *Union miniere du Haut Katanga,* kwa kubadilishana na utiifu kamili wa wafanyakazi, yakawa sasa yanawapa wafanyakazi na familia zao kazi, shule, sehemu za burudani na hali za maisha zilizokuwa duni zaidi kuliko mahali pengine.

Kupigwa marufuku rasmi kwa kazi za kulazimisha (1946 katika Afrika ya Wafaransa) kwaelekea kuwa ndiko kulikokuwa kilele cha mchakato wa marekebisho ya kimuundo ambao ndio ulioanzisha kwa haraka kilimo cha mazao ya biashara kama vile kahawa, kakao na mbao. Utumikishaji watu kazi kwa nguvu likawa jambo lililopitwa na wakati katika muktadha ambamo utaratibu wa uhamaji wa wafanyakazi ulikwishaanza, ukiwa umechombezwa na hali ya ufukara iliyokuwa imejitokeza katika sehemu za vijijini, na ongezeko kubwa la soko la kazi.

Hatua za utegemezi wa nchi za Kiafrika zinatofautiana kulingana na muda ambao nchi inayohusika ilikuwa chini ya ukoloni na pia kama mitaji katika nchi hiyo ilianzishwa mapema huko nyuma au la. Ndiyo maana maendeleo ya Afrika Kusini yalikuwa takribani karne moja mbele ya maendeleo ya Afrika Magharibi, na ulimbikizaji wa mitaji katika Kongo ya Wabelgiji ulikuwa kizazi kimoja mbele. Mabadiliko ya utawala kutoka katika aina iliyozoeleka ya ukoloni wa kibeberu kuingia katika aina ya ubepari wa kitaifa wa watu weupe ukawa ndio ulioshitadi, ukiandamana na vuvumko la dhahabu la kwenye miaka ya 1930. Likiwa limeanza katika mwaka 1933, vuvumko la dhahabu ya Afrika Kusini likafanya nchi hiyo iweze kuzishinda taathira za hali mbaya ya ulimwenguni kote na kuchochoea uundaji upya wa uchumi kwa kustawisha na kupanua sekta ya viwanda mijini. Uzalishaji wa viwanda ukaongezeka kwa 140% kati ya 1933 na 1939, na Pato la Taifa (GNP) likaongezeka mara tatu. Kukabakia tatizo la ubaguzi wa rangi, katika sura ya kuongezeka kwa haraka kwa wafanyakazi weusi wa tabaka la chini mijini. Kunako mwaka 1946 katika Afrika Kusini, Mwafrika mmoja kati ya Waafrika

wanne alikuwa akiishi mjini, na idadi ya weusi ikazidi sana ile ya weupe katika miji.[3]

Katika Afrika ya Tropiki na Kaskazini, athari ya Mpomoko Mkuu wa Uchumi ikaleta matatizo makubwa ya ndani ya kijamii : wakulima wadogo wakawa ndio maathura (waathirika) wakubwa wa mageuko hayo. Sasa kukatokea michakato maalumu kadhaa: ufukara uliozikumba sehemu za vijijini, watu wa vijijini kukimbilia mijini na kugawanyika katika matabaka ya kijamii - upande mmoja kukiwa na sehemu ndogo ya "wenyeji wenye navyo" na upande mwingine kukiwa na umati wa wafanyakazi wa asili ambao hali zao zilikuwa zikizidi kuwa mbaya. Kuanzishwa huku kwa "mabadilishano yasiyo sawa" kunatupa picha ya sifa muhimu za maendeleo duni yaliyopo hii leo.

## Vita vya Pili vya Dunia

### Tamaa ya nchi Mhimili

Katika Makubaliano ya Munich ya mwaka 1937 baina ya Hitler na Mussolini, Hitler alimwachia Mussolini Ulaya Kusini na Afrika Kaskazini. Italia ilikwishaifanya Libya kuwa koloni lake na majeshi ya Italia yalikwishaiteka Ethiopia tangu mwaka 1936. Ukijumuisha Somalia na Eritrea, ambazo zilikwishakuwa chini ya utawala wa Waitalia tangu 1885 na 1890 kwa mfuatano huo, utamalaki wa Abyssinia ukawa umeanzisha Afrika Mashariki ya Waitalia. Mussolini alikuwa ameazimia kuiunganisha sehemu hii na Afrika Kaskazini; ndiyo maana akawa anaziwania sana Misri na Tunisia. Mpango wake juu ya Misri na Tunisia ulikuwa ukikinzana na Uingereza na Ufaransa ya Vichy; Ujerumani na Hispania pia hazikuupendelea mpango huo. Hamu ya Dola (Reich) la Tatu katika Afrika ilikwishaanza miaka mingi kabla ya vita. Ujerumani ilikwishagundua, mnamo mwaka 1938, kwamba Afrika ilikuwa ya kwanza katika mazao ya pamba na karanga, na kwamba ilikuwa na nafasi ya pekee kwa upande wa uzalishaji wake wa madini, na pia ilkuwa na 40% ya akiba ya nguvu ya hidroliki katika ulimwengu mzima. Ujerumani ilikuwa ikipata faida kidogo sana kutokana na utajiri wa Afrika; kwa hiyo ikataka kuiweka sehemu kubwa zaidi ya Afrika chini ya himaya yake. Baada ya kushindwa kwa Ufaransa mnamo mwaka 1940, miradi kadhaa ya kuiweka tena Afrika ya Kusini mwa Sahara chini ya ukoloni ikaendeshwa kwa uangalifu mkubwa.

[3]Tazama R. Cohen, 1979; na D.O. Meara, 1974

## Amerika ilivyoichukulia hali hii

Afrika Kaskazini ilitamaniwa sana wakati huo huo mmoja na Wajerumani, Waitalia na Wahispania, na ilikuwa ikitawaliwa na Wafaransa. Ikiwa imeamua kuingia katika vita dhidi ya nchi mhimili, Marekani ilianza kwa kupeleka majeshi yake Afrika Kaskazini.

Huko Marekani vita vilisababisha uhamasishaji watu kuanzisha viwanda ambavyo viliifanya Marekani iongeze katika uchumi. Utaratibu wa uendeshaji wa uchumi uliopangwa ulikwishaanzishwa kabla ya vita. Katika medani ya kimataifa mbinu ya kukipa-kukodi ikawapatia washirika bidhaa ambazo malipo yake yangetolewa kwa masharti nafuu sana.

## Ngome ya Jumuiya ya Madola[4]

Mnamo mwaka 1939-1940 Uingereza ilianzisha eneo lililotumia sarafu ya Uingereza (Pauni) katika Jumuiya ya Madola, ambalo lilichukua takribani moja ya tatu ya biashara ya dunia. London kikawa ndicho kituo kikuu cha kudhibiti ubadilishanaji wa fedha, hali ambayo iliihakikishia himaya kujitegemea katika masuala ya vyakula na mali ghafi.

## Sera za uchumi katika makoloni

Zaidi ya shinikizo kubwa kwenye makoloni na matumizi makubwa sana ya nguvukazi zao, vita vilichapuza kuenea kwa fikra na hisia dhidi ya ukoloni katika Ulaya na Afrika ambazo punde si punde zikafanya utawala ambao hapo awali ulionekana kuwa mtukufu kuonekana kuwa umepitwa na wakati. Waafrika wakarudi nyumbani kwao na mawazo mapya ambayo walipata kutokana na kukutana kwao na Wazungu na Waasia. Ubora wa mtu mweupe ukaonekana kuwa dhana potofu, na tabaka bora la Waafrika likaitumia vizuri nafasi iliyotolewa na propaganda za wa-Sovieti na wa-Marekani dhidi ya ukoloni. Wakati huo huo umuhimu wa bara hili kiuchumi ukawa unaimarishwa na shida za kuwapatia Washiriki mahitaji. Fikra ya kuwapa Waafrika jazba za kisiasa, kiuchumi na kijamii kutokana na jitihada zao katika vita ikawa imeanza kuota mizizi.

[7] Tazama D.J. Morgan, 1980; pia E.R. Wicker, 1958, kur. 170-92

## *Sera ya Waingereza: Sheria ya mwaka 1940 ya Maendeleo na Ustawi wa Makoloni*

Vita vilipoanza Waingereza wakaanzisha vyombo vya kusimamia viwanda vikubwa ili kufidia kupanda na kushuka kwa bei. Hasa, walipanua upeo wa Sheria ya Maendeleo ya Makoloni ya mwaka 1929 na wakachukua hatua za kuendeleza afya ya jamii na elimu.

Sheria ya 1940 ilitenga kiasi cha £50 milioni, kwa makoloni, katika miaka kumi iliyofuata, na kuanzia wakati huo maendeleo yakabuniwa na kupangwa kwa kutumia utaratibu maalumu wa utawala ambao ulikuwa na mwelekeo wa kimpango na kiutekelezaji. Matayarisho ya vita yalileta upungufu katika bidhaa muhimu, lakini kaida ya kuacha mambo yajiendee holela katika makoloni iliachwa rasmi.

## *Sera ya Wafaransa ya mipango: kutoka Vichy hadi Ufaransa Huru*

Mkutano juu ya uchumi wa Ufaransa na nchi za ng'ambo ( *Conférence économique de la France métropolitaine et d'outre-mer* ) uliofanyika mwaka 1934 ulianzisha wazo la dola kuwajibika katika masuala yanayohusu gharama na mipango katika sekta ya viwanda kwa kuanzisha Kamati ya Viwanda ya Himaya (*Comité des industries de l'Empire*). Kwa kutumia Tapo la Umma (*Front Populaire)*, suala hili lilirejewa tena na mpango wa uchumi ukapendekezwa ukiwa umekitwa kwenye mfumo wa uchumi uliopangwa kuliko kukitwa kwenye shughuli za biashara za watu binafsi tu. Kwa mara ya kwanza ikasisitizwa haja ya kuendeleza shughuli za uzalishaji katika makoloni. Lakini mpango wa ukoloni wa Tapo la Umma ulijikuta unapitwa na wakati, na himaya ya kikoloni pia ikaingia vitani takribani kama ilivyokuwa wakati wa kuanzishwa.

Chini ya serikali ya *Vichy*, timu ya wataalamu ilitayarisha mipango ya kwanza ya uchumi wa Ufaransa. Nia haikuwa ni kuanzisha uwezo wa uzalishaji katika makoloni ambao ungeweza kushindana na nchi mama bali tatizo lilitazamwa kwa kuzingatia jumuiya nzima iliyoundwa na nchi mama na makoloni. Azma kuu ilikuwa ni kulinda biashara ya nje ya himaya ya Ufaransa kwa kuhakikisha kuwa inapata masoko nje ya maeneo yaliyokuwa yanamilikiwa na Ufaransa. Kwa hiyo usasa wa *Vichy* ulitokana na fikra ya kikundi cha waali-tawala ambacho kilitumia vizuri hali iliyotokana na vita kusawidi mpango ambao baada ya vita ulikuwa kiunzi cha sera kamambe ya uchumi wa kikoloni.

# Kuanzia miaka ya baada ya vita hadi kipindi cha kuondokana na ukoloni

## Zahama na migogoro ya ndani

Ilikubalika kwa wote kwamba Afrika ilipaswa kufungua milango kwa mataifa mengine ya ulimwengu, lakini kufunguka huku kwa milango hakukufanyika kwa urahisi kama ambavyo ingetarajiwa. Baada ya miaka mitano ya kiasi fulani cha kutengwa kibiashara, kuanzishwa tena kwa mahusiano ya amani na Magharibi kukaleta madhila makubwa kiuchumi na kijamii ndani ya bara hili.

Wakati wa vita, kuwekwa kwa viwango maalumu vya ujira na kuongezeka kwa bei za bidhaa zilizoagizwa kutoka nje kulisababisha kudorora kwa viwango vya maisha. Tabaka la wafanyakazi wadogo wadogo likaanza kujitokeza mijini kote Afrika; tabaka hilo lilitokana na kumiminika mijini kwa wingi kwa watu ambao hawakuwa na kazi na ambao waliyakimbia maisha ya vijijini kutokana na adha za vita. Ghasia zikatokea katika sehemu nyingi, hasa zikiwa zimechukua sura ya milipuko ya papo kwa papo isiyodhibitika; miji ikawa ndiyo vitovu vya migongano. Dalili ya kwanza kabisa ilijitokeza mnamo mwaka 1944 wakati wa maasi ya Thiaroye (Senegal), ambayo yalianzia katika kambi ya kikoloni ya askari wa miguu waliokuwa wakingojea kuruhusiwa kurudi kwao[5] Maasi makubwa yaliyofuata yalitokea katika mji wa Kostantini huko Algeria (1945) na yale ya Bukini (1947); kulikuwa na migomo huko Abijani, Dakar, Nairobi na Akkra; kulikuwa pia na matatizo huko Elisabethville na Brazzaville, bila kutaja kusitisha kabisa kufanya kazi kwa wachimba migodi katika Rand mwaka 1946. Dhana ya vyama vya wafanyakazi wa Kiafrika ikawa sasa inaelekea katika utaifa, na hatua za ukandamizaji zilizokuwa zikichukuliwa na wakoloni zikasaidia kuvipa vyama hivi sura ya kisiasa; wakati huohuo hatua hizo pia zikavifanya baadhi ya vyama hivyo kurudi katika muundo wa kimapokeo wa upinzani dhidi ya wageni, ukiwakilishwa na vyama vya kimasihi kama vilie Ukibangu na Uhamali.

## Hali ilivyokuwa katika nchi za Magharibi

Kipindi cha kuanzia 1946 hadi 1971 kilikuwa kipindi cha kufufuka haraka kwa uchumi. Hali hii ilisaidiwa na misaada kutoka Marekani ambayo ilikuwa imekitwa katika ukinzani dhidi ya ukomunisti na ujengaji upya wa ubepari huko Ulaya. Mkakati

[5] M. Echemberg, 1978, pp. 109-28




Picha 11.1 Mkutano wa OPEC (Jumuiya ya nchi zinazouza mafuta nje) huko Vienna November 21, 1973

huu ulikuwa umeegemezwa katika mipango miwili mikuu: Mpango wa Marshall wa 1947 na Makubaliano ya Atlantiki ya 1949. Benki ya Kimataifa ya Ujenzi mpya na Maendeleo (*International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)* ) na Mfuko wa Kimataifa wa Fedha (*International Monetary Fund ( IMF)* ) vilianzishwa ili kurekebisha uchumi wa nchi ambazo hazikuwa za kikomunisti. Hali hiyo ilipelekea kuwepo kujitegemea katika nchi zenye viwanda. Nchi za Kafrika zikafaidika kwa kiasi fulani kutokana na "kuhaulishwa kwa teknolojia" na kuhamishia huko mitambo kadhaa ya viwanda, lakini kulikuwa pia na kuongezeka kwa mshikamano na utegemezi katika mashirika makubwa ya kimataifa na nchi zilizokuwa zinazalisha mali ghafi.

# Sera za kikoloni za uchumi

Mkutano wa Brazzaville ulifanyika katika himaya ya Ufaransa mapema sana katika mwaka 1944 na ukafuatiwa na kukomeshwa kwa kazi za kulazimishwa katika mwaka 1946, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Vitegauchumi vya Ki-Uchumi na Ki-Jamii (*Economic and Social Investment Development Fund* ) na "Mpango wa Konstantini" kwa ajili ya Algeria. Mfuko wa Maendeleo ya Makoloni ya Uingereza, ambao ulitayarishwa upya mnamo 1945, ulifuatiwa na uhuru wa India mwaka 1947. Matokeo yake katika Afrika yakawa ni kuongezeka kwa viwanda, mkazo ukiwa unawekwa kwenye miundombinu ya usafiri na




Mchoro: 11.2 *Ugharamiaji wa mitaji ya uwekezaji katika Afrika ya wazungumzaji weusi wa Kifaransa na Madagaska, mnamo 1946-73, katika mabilioni ya 1960 ya kawaida ya fedha ya Kifaransa.*

(Chanzo: C. Coquery - Vidrovitch, Ubeberu wa Kifaransa katika Afrika ya weusi: itikadi ya ubeberu na zana za kisiasa, 1924-75; Uhusiano wa Kimataifa,. 7, 1976 kur. 261-82)

kuongezeka kwa uzalishaji kwa ajili ya nchi-mama. Mpango wa kwanza wa Wafaransa (mpango wa Monnet, 1946-52), ulijumuisha makoloni ya ng'ambo, lakini ule wa pili (mpango wa Hirsch) ulikuwa na mpango tofauti kwa ajili ya French Union, ukiwa na lengo la kuharakisha kujiunga kwao na uchumi wa nyumbani.[6]

[6] Commissarial general au plan, 1954 na 1955; Ministry of Overseas, 1954; Ministry of Cooperation, n.d.


Uingereza ilitumia aina ya upangaji ambayo ilikuwa nyumbufu: kwanza kwa sababu ilikuwa inajishughulisha na kazi kubwa ya ujengaji upya wa nchi nyumbani, na pili, kwa sababu utaratibu wa mambo yote kupangiwa makao makuu ulikuwa unapingana na msimamo wao wa kuanzisha serikali za watu wenyewe. Kwa hiyo mfuko huo ukagawanywa katika Ofisi za Maendeleo na ujengaji upya wa nchi, ofisi moja kwa kila koloni. Msaada wa Kiingereza ulikuwa na mgawanyo wa wazi zaidi kuliko ule wa Kifaransa: nusu ya fedha zote ilitumika kwa ajili ya vitegauchumi vya jamii, 20% ikatumika kwa ajili ya kilimo na 20% ikatumika kwa ajili ya muundombinu wa usafiri. Kwa kila kadhia itikadi kuu ya uendelezaji viwanda kama ufunguo wa maendeleo ilikinzana na kiwango cha matamanio mkubwa ya miradi, upungufu wa wafanyakazi na kutojua vikwazo vya kiekolojia vya maeneo yaliyohusika.

Ikiwa imekusudia kuyashikilia makoloni yake, Ureno nayo ikachukua hatua zile zile zilizochukuliwa na nchi-mama zilizokuwa na msimamo wa wastani: mpango wao wa kwanza wa miaka sita ulianza mwaka 1953. Zikiwa na mwelekeo wa kimaslahi sawa na ule wa Afrika Kusini, Benki za Marekani zikajiingiza katika makoloni ya Ureno ya Afrika mapema sana. Ama kwa hakika maslahi ya Marekani katika makoloni hayo yalianza kuwa muhimu tu pale walipoanza kufanya majaribio ya mwanzo ya kutafuta mafuta, na kuanza kwa vita vya ukombozi katika Angola na Msumbiji. Ni wakati huo, yaani kwenye miaka ya 1960, ambapo makoloni yaliyokuwa yamemilikiwa na Ureno yalipoanza kuwa ya kisasa kwa kasi.

Katika Kongo ya Ubelgiji, ni mwishoni mwa kipindi cha ukoloni tu ambapo serikali ilitayarisha mpango wa maendeleo: mpango huu ulitilia mkazo hasa kilimo cha wakulima wadogo wadogo na serikali kujishirikisha zaidi katika sekta ya viwanda. Mpango huo haukutiliwa maanani. Kutokana na uraisi wa Mobutu ambao madaraka yake yote yaliendeshwa kutoka makao makuu, idara ya mipango ikaanzishwa, lakini ilikuwa na mafanikio kidogo sana kwani serikali haikuwa na uwezo wala mwamko wa kutosha wa kuweza kutekeleza mpango huo.

## Kuondokana na ukoloni katika Afrika ya Weusi

Mshuko wa uchumi wa muda mfupi, lakini mkali, uliofuatia zahama ya uchumi wa dunia wa 1951-2 ulitokea wakati ambapo mahusiano ya utawalaji utegemezi yalikuwa yakisailiwa vikali. Kuanzia wakati huo, kuondokana na ukoloni likawa jambo lililokubalika na hata likawa linapiganiwa sana katika sehemu za kazi na shughuli mbalimbali. Magazeti maalumu ya uchumi yakawa yanaandika wimbi la msimamo usiobadilika wa kupinga ukoloni kwa msingi wa haja ya kuwepo na utaratibu mzuri wa uendeshaji wa shughuli za uchumi.




*Mchoro 11.3* Faida za SCOA, 1910-60 (*Chanzo*: C. Coquery-Vidrovitch, 'L' impact des interets Coloniaux: SCOA e CFAO dans l'ouest africain, 1910-1965', Journal of African History, 16, 1975 Kur.595-621)

Uhuru ukayaingiza mataifa ya Kiafrika katika ushindani wa ubeberu wa kimataifa, ambao ulikuwa na maana ya kuitazama upya sera ya uendeshaji shughuli. Hatua muhimu ya kuanzisha viwanda katika Afrika ya tropiki ikachukuliwa wakati huu.

## Uhuru

Mataifa huru mapya yalilazimika kuuvumila uchumi duni, uzalishaji ukiwa umeelekezwa kwenye bidhaanje na soko dogo sana la ndani. Uhuru ukaja katika kipindi kibaya sana, wakati ambapo bei ya mali-ghafi iliyosafirishwa nje, ambayo ndiyo ilikuwa njia yao kuu ya mapato, ilikuwa ikionekana kuendelea kushuka. Mapato ya nchi na matumizi vikaathirika vibaya, na wakati huo huo kuongezeka kwa idadi ya watu ambako kulikuwa hakujawahi kutokea kwa kiwango hicho kukashamiri.

Hata hivyo baada ya muda mfupi, katika nusu ya pili ya miaka ya 1960, uchumi wa ulimwengu ukaanza kupata nafuu; kwa hakika kwa kipindi fulani ilionekana kana kwamba maajabu yametokea, ambapo katika sehemu chache hali ya maendeleo duni ilikuwa imetoweka.

## Uhusiano baina ya Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC) na nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (ACP)[7]

Pamoja na upinzani kutoka Ujerumani na Uholanzi, Ufaransa bado ilisisitiza kwamba Soko lote la Pamoja liwe wazi kwa makoloni ya Wafaransa na Wabelgiji yaliyoko Afrika. Lengo lilikuwa ni kuipatia Ulaya mahitaji zaidi ya mali-ghafi. Ama kwa hakika mfumo huo ukatokea kuwa utaratibu nyumbufu ulioshawishi mpito kutoka mahusiano finyu ya kikoloni kuingia katika mtandao wa mahusiano ya pande nyingi. Utangulizi wa Mkataba wa Roma unathibitisha "mshikamano unaoishikamanisha Ulaya na nchi za ng'ambo" na uliweka njia kwa ajili ya soko la pamoja la Afrika ukiwa na mambo matatu muhimu:

(1) kufungua taratibu milango ya masoko ya nchi za Kiafrika "zinazoshirikiana" kwa ajili ya bidhaa zitokazo katika nchi za Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya;11 Commissarial general au plan, 1954 na 1955; Ministry of Overseas, 1954; Ministry of Cooperation, n.d.

(2) kufungua milango ya masoko ya nchi za Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya kwa ajili ya bidhaa za nchi zinazoshirikiana chini ya mipango maalumu ya upendeleo;

(3) kuanzishwa kwa programu ya vitega uchumi vya kijamii na kiuchumi katika nchi za ng'ambo, ikifadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF)

Mwanzoni mwa miaka ya 1960, hapakuwa na maswali yoyote yaliyoulizwa kuhusiana na kujiunga kwa washiriki katika Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya, hata kwa mataifa mapya. Mapatano ya Younde ya I na II (1963 na 1969), na yale ya Lome ya I, II, na III (1975, 1980 na 1986), kwa nchi za Kiafrika yalikuwa ni nafasi ya kujadiliana upya juu ya manufaa ya mahusiano na kupata msaada katika kuubadili uchumi wao, hasa katika sekta ya viwanda. Lakini Ulaya, ikiwa sasa imejijenga upya na ikiwa na hakika ya kuweza kujitosheleza yenyewe, ikakubaliana na ulipaji ushuru kwa vitu vichache tu vya tropiki. Hasa, mapatano ya Lome yalikuwa ni

[7] Tazama C. Casgrove-Twitchett, 1978; F. Long, 1980; na C. Coquery-Vuidrovitch 1988, kur. 105-34

JEDWALI 11.1 Vitega Uchumi vya wageni barani Afrika, 1965-83

| | Wastani kwa mwaka wa mtiririko katika Dola bilioni | | | | Asilimia ya jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1965-9 | 1970-4 | 1975-9 | 1980-3 | 1965-9 | 1970-4 | 1975-9 | 1980-3 |
| Nchi zenye Viwanda | 5.2 | 11.2 | 18.4 | 31.3 | 79 | 86 | 72 | 63 |
| Afrika | 02 | 0.6 | 1 | 1.4 | 3 | 5 | 4 | 3 |

Chanzo: World Bank, 1985, uk. 126. Kwa nchi zote zinazoendelea zikijumlishwa kwa pamoja, Thamani bayana ya vitega uchumi vya moja kwa moja iliongezeka katika kipindi hicho kwa asilimia 10 kwa mwaka, bali thamani halisi haikubadilika.

hatua muhimu sana katika sera ya Ulaya, idadi ya washiriki-wenza ikaongezeka toka 18 hadi 46 na kisha 52. Yakiwa yameanza na nchi za ACP (Afrika, Karibiani na Pasifiki) tu mahusiano yote ya kiushirikiano na nchi za ulimwengu wa tatu yakawa yameingia katika hatua mpya. Kuanzishwa kwa STABEX mnamo mwaka 1975, ambayo ilidhibiti bei za bidhaa, na kisha SYSMIN, katika mwaka 1980, ikiwa inafanya kazi ile ile kwa upande wa madini, kukawa kumealika mahitajio ya "utaratibu mpya wa kiuchumi" ambao ulikwishatakiwa kitambo na nchi zenye maendeleo duni tangu mkutano wa UNCTAD mnamo mwaka 1974.

## Zahama ya miaka ya 1970 na ufukara wa Afrika

Nchi za Afrika ya weusi, ambazo ni theluthi mbili ya nchi 25 masikini kabisa ulimwenguni, zinahitajia utaratibu mpya wa kiuchumi, sharti muhimu sana katika uundaji upya wa ndani kwa ndani, ambapo washiriki-wenza wao wa Kaskazini wanafanya "marekebisho ya ndani kwa ndani ya kimuundo" kuwa sharti muhimu katika kupata msaada wowote zaidi. Afrika ya weusi inaelekea kukwama katika

tope. Kwa ujumla Afrika ndilo bara ambalo lina mvuto kidogo kuliko mabara yote kuhusiana na uwekezaji wa kigeni. Tukiacha Zaire (Kongo) Ethiopia na Nigeria, karibu nchi zote za kusini mwa Sahara zina idadi kidogo ya watu (milioni 2 hadi 8) na wakiwa na uwezo mdogo sana wa kununua mali. Tukiacha Nigeria, nchi chache zinazozalisha mafuta haziyazalishi kwa wingi. Makampuni ya mafuta yanaelekea kuyachukulia mashapo ya mafuta yaliyo kusini mwa Sahara kama "akiba" ya wakati wa shida.


Miaka ya 1980 ilishuhudia hali mbaya iliyokuwa ikizidi kudorora, ikichapuzwa na ukame ambao uliathiri zaidi ya nchi 20 na watu kama milioni 35 kati ya 1983 na 1985. Pamoja na ongezeko la muda wa ulipaji madeni, kiasi cha mapato kutokana na bidhaanje ambacho kilikuwa kikitumika kulipia madeni kiliongezeka toka 18% katika mwaka 1980 hadi kufikia 38% katika nchi masikini sana mnamo mwaka 1982. Katika mwaka 1985 makali ya hali hiyo yalidhihirishwa na kushuka kwa takribani 3% ya Pato la Taifa (GNP) kwa kichwa.

Nadharia tete ya ukuaji wa uchumi wa wastani karibu ingewezesha kugeuza mwelekeo huo wa kushuka kwa uchumi katika Afrika ya kusini mwa Sahara. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, hii ingehitaji kiasi kisichopungua dola za Kimarekani bilioni 35.2 kwa mwaka zikiwa katika rasilimali za nje ili kuwezeshaji ulipiaji madeni na kubakisha walau kiasi kidogo cha kuagizia bidhaa kutoka nje. Pamoja na mambo mengine, ongezeko la 20% katika mipango ya misaada baina ya nchi na nchi ambalo lilitarajiwa kati ya mwaka 1985 na 1990 kingekuwa kitu cha lazima. Hii ina maana kwamba mpira unarudi tena katika uga wa nchi zenye viwanda. Ili isitegemee sana misaada ya dharura, ambayo athari zake za kuliyumbisha bara hili zimeonekana dhahiri katika miaka ya karibuni, Afrika haina budi kutatua matatizo yake yenyewe.

Kuhitimisha taswira hii ya kufadhaisha, tunaweza kuongeza kwa kusema kwamba karibu nusu ya wakimbizi wote ulimwenguni ni Waafrika!

## Aina mpya za ubeberu

Sifa kuu ya Afrika ya leo ni kule kuzitegemea sana nchi za ki-Magharibi, hata pengine kuzidi ilivyokuwa hapo zamani. Utegemezi huu unatokana na umasikini na ukoloni ambao umetoweka muda si mrefu uliopita; bila shaka hali hiyo imesababishwa na Magharibi yenyewe, lakini pia ni sifa ya ndani ya Afrika yenyewe, iliyokubaliwa na kuendelezwa, kwani katika mtazamo wa kiutamaduni kiolezi kinachotumika bado ni kile kile cha Ulaya. Ufaransa ndiyo mwingizaji mkuu wa mitaji katika Afrika na kwa ujumla ndiyo inayofanya biashara na Afrika zaidi kuliko nchi nyingine yoyote; na ndiyo itoayo misaada mingi ya kiufundi. Kiolezo




*Mchoro:* 11.4 Vitega uchumi na Akiba katika Afrika, 1960-83, bila kujumlisha nchi zinazosafirisha mafuta nje

(*Chanzo:* World Development Report, World Bank, Washington, D.C. 1985, uk.49)

JEDWALI 11.2 *Mabadiliko ya mzigo wa madeni kwa nchi za Afriko zenye kipato cha chini, 1970-84*

| | 1970 | 1974 | 1976 | 1978 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uwiano wa madeni GNP | 17.5 | 23.5 | 27.7 | 26.9 | 39.8 | 43.4 | 47.7 | 52.0 | 54.5 |
| Uwiano wa madeni na mahuruji | 75.2 | 99.5 | 135.3 | 162.3 | 175.8 | 216.5 | 260.5 | 279.5 | 278.1 |
| Uwiano wa ulipaji Madeni | 6.1 | 8.6 | 8.5 | 9.6 | 12.5 | 13.8 | 15.7 | 16.5 | 19.9 |

*Chanzo*: World Bank, 1985, uk. 24

cha Magharibi cha maendeleo ya uchumi na jamii kinatolewa kama ndiyo maelezo chanya pekee ya maendeleo ya historia ya ulimwengu; msingi wa mfumo huu ni ile fikra ya maendeleo ambayo imefanywa kuonekana kuwa ni maendeleo ya sayansi na teknolojia tu; maendeleo yakitazamwa katika mwelekeo wa hali ya maisha iliyopo hii leo, yana maana ya kujiingiza zaidi na zaidi katika soko la Magharibi.

Hali hii ndiyo inayozua kiolezo cha mafanikio ya kiuchumi, halikadhalika kiolezo cha mchanganuo wa matabaka ya kijamii. Wanamapainduzi wenyeji wa ki-Marx hujaribu kutetea imani ya umuhimu na utukufu wa tabaka la wafanyakazi katika nchi ambako wala haliko. Utegemezi una taathira nyingine: mkengeuko wa kijamii unaojitokeza baina ya umma na waali, hawa tuliowataja nyuma wakiwania hali ya maisha ya ki-Magharibi. Lakini kuliingiza tabaka la watu wachache bora katika mfumo wa kilimwengu kunaashiria kutowathamini wale walio wengi. Vionjo vya wachache hawa huhitaji kuwa biashara iwe na mwelekeo wa kusafirisha bidhaa nje badala ya kujishughulisha na ugavi wa vitu rahisi vya walaji. Katika muktadha huo, kuingiza nchini mitaji na kuhaulishwa kwa teknolojia kunafanywa hasa kwa manufaa ya watawala wachache au makampuni ya kimataifa. Kwa mfano, kampuni ya GECAMINES ya Kongo (Zaire), ambayo kimsingi ndiyo yenye madaraka juu ya uzalishaji wa shaba na metali nyingine zisizo za chuma, imekabidhi jukumu la kutengeneza na kuuza shaba yake kwa makampuni mawili ambayo yanaendeshwa na *Societe Generale de Belgique*. Kuendelea kushuka kwa akiba, hasara katika akaunti zinazotumika pamoja na uwekezaji mdogo wa mashirika ya kigeni, hufanya iwe hapana budi ila kukopa; lakini utaratibu huu hulifanya tatizo la kulipa madeni lizidi kuwa kubwa tu. Aidha upendeleo kwa wateja maalumu na rushwa ni mambo ya kawaida, na wale wanaoendesha uchumi na wandeshaji wa serikalini wanaonekana kujishughulisha na kugawana "keki ya taifa" tu.

## Sera ya uchumi ya nchi za kisoshalisti

Warusi waliamua kwanza kupanua wigo wa mahusiano ya kiuchumi, kibiashara na kiufundi kuvuka Jumuiya ya Mashariki katika Mkutano wa Moscow wa Uchumi uliofanyika mwaka 1952. Mwaka 1956, Khrushchev akaahidi kuzipa misaada nchi ambazo ndio kwanza zilikuwa zimepata uhuru, tena bila kulipia chochote. Kwa upande wa Marekani, makamu wa rais Nixon alitembelea Afrika mara kadhaa, kukaanzishwa ofisi ya Afrika katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, na mifuko maarufu ya Marekani ikadhamini na kufadhili kazi zilizohusu masuala ya Ulimwengu wa Tatu. Katika muktadha wa Vita Baridi, Afrika iliendelea kubainishwa na mambo yaliyotokana na mikakati ya wazi, kama inavyojitokeza katika kuingilia kati mara




PICHA 11.2*Bernardo Vieira, Rais wa Guinea Bissau akutana na M.A.Qureshi, Makamu wa rais mwandamizi wa Banki ya dunia Oktoba 1988.*

kwa mara kwa Wasovieti katika Angola, Msumbiji na Ethiopia. Kwa upande mwingine, China inatoa uchaguzi mbadala kwa Waafrika kwa sababu msisitizo unaowekwa kwenye kilimo cha wakulima wadogo na wakubwa kwa hakika huakisi hali halisi ya Kiafrika.

## Dhima ya mashirika ya kimataifa

Ingawa mara nyingi mashirika ya kimataifa huchukuliwa kuwa na urasimu mwingi sana lakini yanafanya kazi ya kweli kweli hasa, kwa mfano, katika kuupiga vita ujinga wa kutojua kusoma (UNESCO), milipuko ya magonjwa (WHO), ukame na njaa (FAO), n.k. Mashirika haya yanafadhiliwa na Mpango wa Shirika la Umoja




| | |
|---|---|
| ADB | Benki ya maendeleo ya Afrika |
| BCEAO | Benki ya Kati ya nchi za Afrika Magharibi |
| BEAC | Benki ya nchi za Afrika ya Kati |
| BOAD | Benki ya Maendeleo ya Afrika Magharibi |
| CEAO | Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi |
| CPCM | Kamati ya Ushauri ya kudumu ya Maghreb |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| EADB | Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki |
| ECA | Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika |
| ECOWAS | Jumuiya ya Uchumi ya nchi za Afrika Magharibi |
| ENTENTE | Halmashajuri ya maelewano ya nchi |
| OMVS | Mpango wa maendeleo ya Mto Senegali |
| UDEAC | Desturi za Afrika ya Kati na Umoja wa Kiuchumi |
| UEAC | Umoja wa Nchi za Afrika ya Kati |
| UMOA | Umoja wa Mambo ya Fedha wa Afrika Magharibi |
| WACH | Ofisi ya Kubadili hundi za Benki ya Afrika Magharibi |

*Mchoro*: 11.5 Mipango ya ushirikiano na miungano ya sehemu na sehemu ndogo za Afrika
*Chanzo*: UNCTAD, TD/B/609/Add.1, Juz. 111, 1976, uk.xi-xii)

wa Mataifa wa Maendeleo (*United Nations Development Programme (UNDP)* Benki ya Dunia (*World Bank*) na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *International Monetary Fund ( IMF)* ); mashirika ambayo aula zake zinaamuliwa na kigezo cha upatikanaji wa faida, ingawa kadhia hii haikubaliki kwa urahisi katika nyanja zinazoshughulikiwa na UNESCO (elimu, sayansi na utamaduni). Hii ndiyo maana Shirika la Umoja wa Mataifa limeanzisha Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo ( *International Fund for Agricultural Development (IFAD)* ), ambao unatilia mkazo mazao ya chakula, na wakulima wadogo wadogo, ukipitia asasi zilizopo. Kutokana na hali hiyo shirika limechukua mtazamo mpya, na kukubali ukweli kwamba haiwezekani kupata ufumbuzi wa kiuchumi kwa matatizo ya kijamii.

## Waafrika wameichukuliaje hali hii

Jibu la Waafrika kuhusu shinikizo la kimataifa lilikuwa kutofungamana na upande wowote, siasa ambayo ilianzishwa na Nehru, Tito na al-Nasser wakati wa Vita Baridi, na ambayo baadaye ndiyo iliyoziunganisha nchi zote za Ulimwengu wa Tatu. Katika Afrika, siasa ya kutofungamana na upande wowote ilianza mapema kutokana na kushindwa kwa ushirikiano wa Wafrika-Waasia kufuatia Mkutano wa Bandung wa mwaka 1955. Hii ilielezwa wazi wazi katika Makubaliano ya Nchi Huru za Afrika (OAU). Hata hivyo, vigezo vya kutofungamana na upande wowote bado haviko wazi na vinaendelea kudhoofika kutokana na kudorora kwa kila siku kwa utekelezaji wake.

Lakini kinachobakia ni malalamiko ya jumla juu ya Kaskazini. Malalamiko hayo yalianzia UNCTAD, Mkutano wa Biashara na Maendeleo ambao uliitishwa na Umoja wa Mataifa kutokana na shinikizo la nchi zinazoendelea. Nchi wanachama (122 katika mwaka 1982) ndizo zinazokuwa msemaji wa nchi za Ulimwengu wa Tatu dhidi ya mchi zenye viwanda. Azimio na Programu kwa Wote ya mwaka 1974 ilitangaza haja ya kuwepo kwa "utaratibu mpya wa uchumi ambao umekitwa kwenye haki sawa, usawa wa dola, kutegemeana, maslahi ya pamoja na kushirikiana kati ya nchi zote".

Majadiliano ya Kaskazini-Kusini hayajajitokeza tangu kipindi hicho na madai makubwa ya nchi za ACP bado yamekuwa ni kutaka bei ya mali-ghafi zao wananzosafirisha nje iongezeke. Hii ndiyo ingewawezesha kuleta nchini mwao teknolojia inayotakikana kwa ajili ya hatua inayofuata katika kuendeleza viwanda vyao.

Ingawa pamekuwepo na mikataba mingi baina ya nchi moja na nchi nyingine au kati ya mataifa katika bara hili, kujitegemea katika Afrika, katika sura ya

kuwashirikisha Waafrika wote, bado kunazuiwa na kikwazo kilicho na pande mbili: kwa upande mmoja kuna athari ya vuta-nikuvute kuelekea na kutoka katika nchi zenye viwanda; na kwa upande mwingine kuna ushindani wa kisiasa miongoni mwa Waafrika wenyewe.

## Vipengele vipya

Afrika Kusini

Ikiwa ndio msingi wa mkakati wa Magharibi na mahala penye usalama kwa ajili ya vitegauchumi vyake, Afrika Kusini ilikuwa ni mfano mzuri wa ubeberu katika Afrika hadi hivi karibuni tu; na kwa sababu hiyo nchi hiyo ikawa ndio kitovu cha upinzani wa aina mbalimbali:

(1) upinzani dhidi ya ukoloni kwa sababu ya utegemezi ambao uliifanya Namibia na Waafrika wote wa Azania wawe nao;
(2) upinzani dhidi ya ubeberu kutokana na nguvu za kiuchumi na kijeshi ambazo umeonyesha katika Afrika; na
(3) upinzani dhidi ya ubaguzi wa rangi kutokana na serikali yake dhalimu ya *kibaguzi.*

Ubeberu wa Kimagharibi ulipowatelekeza Wana-utaifa wa Kiafrikana, mabadiliko makubwa yakaanza kutokea baada ya kitambo kifupi.

## Kuinukia kwa tabaka la wafanyakazi na vyama vya wafanyakazi

Pamoja na kuongezeka sana kwa mapambano ya wazalendo dhidi ya ukoloni, hapajakuwepo na ubainishaji dhahiri wa madai ya jamii yenye azma za kisiasa.

Katika Afrika ya Ureno, hatari ya kuwa na tabaka la kifanyakazi ilidhibitiwa, katika uendelezaji viwanda ulioanza katika miaka ya 1960, kwa kuanzisha miungano ya vyama vya kitaifa na wafanyakazi wenye ujuzi. Hawa zaidi walifanya kazi kwa manufaa ya Wareno wahamiaji wapya.

Katika sehemu ya Afrika ya weusi inayotumia lugha ya Kifaransa, vyama vya wafanyakazi wa reli na wa utumishi vilikuwa na nguvu kiasi kikubwa. Lakini *usimilisho* na mapokeo ya Kifaransa ya siasa na vyama vya wafanyakazi yaliwekea mipaka madai ya vyama hivyo na kupunguza makali yake.

Katika sehemu ya Afrika itumiayo Kiingereza mapokeo ya wapenda mabadiliko ya vyama vya wafanyakazi yaliweka mbele zaidi majadiliano juu ya ujira kabla ya kuanzisha fujo. Kwa mfano, katika Nigeria mara nyingi migomo iliishia katika nyongeza ya ujira. Wafanyakazi walikuwa na uzoefu na wenye taratibu nzuri, lakini hapakuwa na kupanga ngazi kazini na mishahara haikukawia kufikia skeli ya mwisho.

Serikali nyingi za kisiasa zilividhibiti vyama vya wafanyakazi, hasa Kaskazini mwa Afrika. Hapa pia ilitegemewa kwamba msukumo mkubwa ungetoka Afrika Kusini ambako wakulima wadogo wadogo na watu wa daraja la kati waliwategemea wafanyakazi. Baada ya mlipuko wa migomo katika Durban mwaka 1973, uzimaji migomo hiyo kwa njia za kikatili uliweza kuyazuia maasi ya wafanyakazi. Hata hivyo Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi likawa shinikizo kubwa ambalo baadaye lilizaa matunda makubwa.

## Mapinduzi ya kidemografia na kimiji

Kuanzia miaka ya uhuru, ongezeko la watu lililoanza Afrika Kaskazini mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na katika Afrika ya Weusi kwenye miaka ya 1930, tangu uhuru limegeuka kuwa kubwa kwa kiasi ambacho hakijawahi kutokea. Ukweli huu ni sifa muhimu ya uchumi wa Afrika ya leo, lakini athari zake za muda mrefu si rahisi kuzipima. Hata hivyo, ukweli huo ukitazamwa katika kiwango cha muda mfupi maana yake ni kuendelea kushuka kwa wastani wa pato la taifa. Ongezeko la watu huweza kua na faida za kiuchumi kama vile kupanuka kwa soko la nyumbani, na kuongezeka kwa uzalishaji na kuongezeka pato kutokana na uzalishaji mpana. Hakuna kimoja kati ya vigezo hivi ambacho kimewahi kufanya kazi katika Afrika. Kwa wakati huu, kilicho muhimu zaidi ni mwelekeo-pindu wa ajabu ambao Afrika inaupata kati ya mijini na vijijini.

Nchi nyingi za Afrika zinakabiliwa na wimbi kubwa ambalo halijawahi kutokea la uhamiaji mijini. Hii leo miji ya Kiafrika ndiyo kitovu cha migongano ya kisiasa na kijamii, na mahali ambapo kuna mchemko wa namna mpya mbalimbali za kuingia katika ulimwengu wa kileo, zijulikanazo kama "sekta isiyo rasmi". Wazalishaji wadogo wadogo katika sekta hii isiyo rasmi wameonyesha uwezo mkubwa katika kujinasibisha na ulimwengu wa kileo, na pia wameonyesha ubunifu wa hali ya juu; na pengine wanao uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimuundo kwa kuleta mapinduzi katika nafasi za kazi zilizopo kwa ajili ya watu wa mijini na umma wa vijijini.

JEDWALI 11.3 *Idadi ya watu, jumla ya pato la Taifa (GNP), Jumla ya Pato la Ndani na wastani wa ongezeko la pato kwa kila mtu, 1965-95*

| | 1980 | | | | *Wastani wa ongezeko la pato kwa kila mtu kwa jumla ya pato la taifa na jumla ya pato la ndani(%)* | | | | | | | Matarajio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya watu | GNP ($bn) | GNP (bn) | GNP kwa kila mwaka $bn | | 1965-73 | 1973-80 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1980-5 | 1985-95 ya chini | juu |
| AFRIKA | | | | | | | | | | | | | | |
| Nchi zenye pato la chini | 197 | 52 | 53 | 270 | GDP | 3.9 | 2.7 | 1.7 | 0.7 | 0.7 | 1.6 | 1.4 | 2.8 | 3.2 |
| | | | | | GNP | 1.3. | - 0.1 | -1.7 | -2.6 | -2.6 | -1.5 | -1.7 | 0.5 | -0.1 |
| Pato la kati zinazoagiza mafuta | | | | | | | | | | | | | | |
| Afrika Kaskazini na | | | | | GDP | 5.6 | 7.1 | 0.7 | 6.2 | 1.5 | 1.2 | | | |
| mashariki ya Kati | 31 | 25 | 24 | 830 | GDP | 3.5 | 4.3 | -0.5 | 2.6 | 0.5 | -1.3 | | | |
| | | | | | GDP | 5.1 | 3.6 | 6.9 | -1.0 | -1.8 | -2.1 | | | |
| Afrika ya Sahara | 780 | 26 | 27 | 330 | GDP | 2 | 0.5 | 4.1 | -4.8 | -5.4 | -5.4 | | | |
| | | | | | GDP | | | | | | | | | |
| NCHI ZENYE | | | | | GDP | 4.7 | 2.8 | 1.4 | -0.3 | 2.6 | 4.8 | 2.3 | 2.5 | 4.3 |
| VIWANDA | 714 | 7477 | 7444 | 10480 | GDP | 3.7 | 2.1 | 0.7 | -1.0 | 1.5 | 4.3 | 1.8 | 2 | 3.7 |
| (biashara ya uchumi) | | | | | | | | | | | | | | |

a Asilimia ya chini ya badiliko kwa mwaka
b Matarajio
*Chanzo*: World Bank, 1985, uk.138, 148, 149

Uajiriwaji wafanyakazi kupitia maendeleo ya sekta ya kisasa katika nchi ambazo ongezeko la watu ni zaidi ya 2.5% ni njozi. Kwani, ili watu wapya katika soko la kazi waweze kuingizwa ndani ya jamii ya viwanda itahitaji pawe na kazi za kulipwa kwa 50% ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi, ambavyo katika sehemu nyingi asilimia hiyo ni kati ya 10-20 tu. Miji ya ulimwengu wa tatu inakua kwa namna tafauti na vituo vya viwanda vya karne ya kumi na tisa katika Ulaya. Miji hiyo hii leo inafasiliwa katika dhana ya utata wa miji - takriban kutoweza kabisa kukwepa mzunguko wa umasikini, labda kama mtu atahama nchi.

Mafuriko ya watu mijini yasiyodhibitiwa yanaweza kuwa njia kuu ya kuleta vurumai; kwani mijini ndiko watu, ajira na miundo mbalimbali hupatikana kwa wingi. Huko ndiko pia athari za kiuchumi na kiutamaduni hujidhihirisha, na nguvu za kisiasa huamuliwa ni mahali ambapo, kwa ufupi, mashinikizo mkataa ya kijamii ya kesho yatatokea.

[9] Tazama kwa mfano, S. La-Anyane, 1970 na 1971.

[10] Tazama FAO, 1977

# 12

# Kilimo na maendeleo vijijini tangu mwaka 1935

## Utangulizi

Sera ya kilimo na maendeleo vijijini katika Afrika imepotoshwa na urithi wa uzoefu wa kikoloni ambao ulitilia mkazo juu ya mazao ya kuuzwa nje. Nyakati nyingine, uhimizwaji wa kilimo cha mazao ya kuuzwa nchi za nje ulileta matokeo ya chumi za tamutamu na vinywaji zenye misingi juu ya mimea kama vile majani ya chai, kahawa, miwa ya sukari, na kakao. Sura hii itachunguza hali hii ya upotoshwaji wa uzalishaji ambapo, katika hali mbaya zaidi, Afrika huzalisha mazao ambayo haiyatumii na kutumia mazao isiyoyazalisha. Mtindo umekuwa wa kuzingatia uagizaji wa kutoka nje wa kiasi kinachozidi kuongezeka cha vyakula.

Athari kadha zimesababisha mahitaji ya kuagizia vyakula kutoka nje nazo ni kama vile uongezekaji wa idadi ya watu, mabadiliko katika taratibu za utumiaji wa vyakula, uharibifu wa nyenzo za uzalishaji wa kilimo, kutokuwepo na motisha wa kutosha kwa wakulima, na kuungwa mkono zaidi kwa mazao ya kuuzwa nje. Upotoshi wa pili wa kilimo cha Afrika ni upendeleo kwa sehemu za mijini. Kwa jumla, sera ya kupendelea sehemu za mijini imedidimiza maslahi ya watu wa mashambani na kuyakuza ya wale wanaoishi mijini. Hali hii imetokea katika utoaji wa huduma na pia uendelezaji wa nyenzo za maendeleo.

Sera hii huwakandamiza wakulima, na huelekea kuwaruzuku walaji wa sehemu za mijini badala ya wakulima, japo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) mara nyingi huhimiza kuacha kuwafidia walaji na kutilia mkazo utoaji wa motisha kwa wakulima. Hata hivyo, serikali nyingi za Afrika zimekuwa wafungwa wa sera hii ya kuwaruzuku walaji na mara nyingine, kuibadilisha sera hii kumeleta

fujo zenye umwagikaji wa damu katika miji mikubwa kama vile Tunis, Kairo na Monrovia.

Baadhi ya mambo mengi yanayosababisha mapendeleo ya sehemu za mijini ni mfumo mzima wa elimu ambao waonekana kama uliundwa ili kusababisha kuwepo kwa watu wasiofaa kuishi katika sehemu za mashambani. Wakulima wenyewe walijihisi kuwa walidanganywa iwapo watoto wao walioelimika hawakuyakataa maisha ya sehemu za mashambani. Elimu ilionekana kama njia ya kujikomboa kutokana na kazi za mikono na hasa ya ulimaji shambani. Kwa sababu kama hizi shule katika Afrika ilitumiwa kuipiga vita sekta ya kilimo barani Afrika.

Katika nyakati nyingine upendeleo ulijitokeza kwa namna ya kutafuta misaada kutoka nje ili kuendeleza uzalishaji wa mazao yoliyotumiwa na wakazi wa mijini kama vile ngano. Mojawapo ya mifano ya hali hii ilikuwa mkataba baina ya Kanada na Tanzania wa kuzalisha ngano katika sehemu za karibu na mlima Kilimanjaro. Mradi huu ulikuwa wa gharama kubwa ya kibinadamu na kiekolojia. Wafugaji wa kabila la Wabarabeg walisukumwa mbali katika mahali ambamo kulikuwa hakuma malisho ya kufaa na, pia, uzidishwaji wa kilimo ukaleta uharibifu mkubwa wa mmomonyoko wa udongo katika eneo hili lenye udongo wa volkano. Kwa mara nyingine mbinu za maendeleo ya Afrika zenye kupendelea miji zilisababisha madhara makubwa.

Upotoshi wa tatu wa ukoloni dhidi ya kilimo unahusiana na jukumu la mashirika ya serikali ambayo katika hali ya ukinzano yalikua chini ya tawala za kikoloni na, pia, chini ya tawala za Afrika huru. Uhusikaji wa serikali katika uzalishaji wa kilimo ulidhihirika zaidi katika kilimo cha mazao ya kuuzwa.

Bila shaka mmojawapo wa walioumia zaidi kutokana na urasimu mwingi katika sekta ya kilimo alikuwa ni mkulima. Kinyume na hali ilivyo barani Ulaya, ambapo mbinu za serikali huruzuku nıkulima, katika Afrika mkulima aliuruzuku urasimu. Katika Afrika mashirika makubwa ya serikali yamepunguza faida ya mkulima na kwa hiyo kuathiri vibaya hamasa yake kama mzalishaji.

Sababu mojawapo ya uamuzi wa Rais Ibrahim Babagida wa mwaka wa 1987 wa kuzivunja halmashauri za kuuza mazao za Nigeria ilikuwa ni hamu ya kutaka kuimarisha kiwango cha faida na motisha kwa wakulima. Kiishara uvunjwaji wa halmashauri hizo ulikuwa ni namna moja ya kujikomboa kutokana na ukoloni.

Upotoshi wa nne wa urithi wa kilimo cha kikoloni ulikuwa ni mwelekeo wa kupendelea wanaume. Kilimo kingi cha mapokeo barani Afrika kilihusisha wanawake. Mara nyingi wanawake walikuwa ndio wengi miongoni mwa wakulima wa jamii za Kiafrika. Katika hali hiyo ya jadi wanawake walikuwa na uwezo

mkubwa wa kuamua kiwango cha bei ya mazao. Mabadiliko ya kikoloni yalisaidia katika kuhamisha uwezo kutoka kwa wanawake hadi kwa wanaume, hasa katika kuamua bei ya mazao ya kilimo. Athari moja ilikuwa ni halmashauri za uuzaji wa mazao ambamo wafanyakazi wengi zaidi walikuwa wanaume.

Jambo jingine linalohusiana na mfumo wa kilimo ni kuunganishwa kwa chumi za Afrika na chumi za kimataifa. Chumi za mahali pamoja za kijadi ziliwapa wanawake uwezo mwingi katika mifumo ya uuzaji. Mara tu chumi za Kiafrika zilipohitaji mawasiliano na sehemu za mbali, wengi wa wakurugenzi wa makampuni ya Kiafrika walikuwa wanaume.

Kukigeuza kilimo kuwa cha kisasa pia kumezidisha jukumu la nyenzo za utoaji wa mikopo. Mara nyingi, hali hii imeleta matokeo ya kupanua majukumu ya wanaume na kuchangia kudunishwa kwa wakulima wa kike. Uendeshaji wa sekta ya kilimo ulihama na kuwapendelea wanaume juu ya mambo yaliyohusu mazao ya kuuza. Uzalishaji, utengenezaji, uwekaji wa bei na shughuli za uuzaji nje wa mazao ya fedha, kwa jumla, ni majukumu ambayo yamechukuliwa na wanaume.

Kwa hiyo hizi ni athari nne za upotoshi wa kikoloni dhidi ya kilimo na maendeleo ya Afrika. Sura hii inachunguza misingi ya mielekeo katika historia ya kilimo cha Afrika katika kipindi kinachojadiliwa kwa kuzingatia urithi wa kikoloni na potoshi zake. Muhimu kati ya potoshi hizo ni kupewa aula kwa mauzo ya nje, kutiliwa mkazo kwa sehemu za mijini, jukumu kubwa la serikali, na dhima kubwa ya wanaume. Pia, sura hii itachunguza mambo mengine ambayo yameathiri kasi na mielekeo ya kilimo katika Afrika.

## Uzalishaji wa wakulima wadogo wadogo na wa mashamba makubwa

Katika nchi za Kiafrika baina ya asilimia 60 na asili mia 95 ya wafanyikazi wamo katika kilimo ama cha kujikimu au kilimo cha mauzo ya nje au vyote viwili. Idadi isiyopungua asilimia 80 ya Waafrika nusu bilioni hutegemea kilimo ambapo upandaji, upaliliaji, uvunaji, usindikaji wa kawaida na uuzaji hufanywa na wanawake.[1]

Katika Afrika, mauzo ya nje huchukua kiasi kikubwa zaidi cha uzalishaji wa kilimo ikilinganishwa na hali katika Mashariki ya Kati na ya Mbali. Mauzo ya ndani ni ya kiwango cha chini zaidi yakilinganishwa na sehemu hizo nyingine.[2]

[1] CIDA (Canadian International Development Agency), 1984, uk. 12

[2] K.C. Abercrombie, 1961



PICHA 12.1 *Mfanyakazi wa kike wa shambani, Moroko*

Hali hii inalingana na ukweli kuwa ukoloni ulielekeza chumi za sehemu za mashambani za Afrika kuzingatia kilimo cha mazao ya kuuzwa nje.

Sekta ya mashamba makubwa ambayo hushikilia idadi kubwa zaidi ya mashamba ya mazao ya kuuzwa nje haijakuwa na mchango mkubwa katika juhudi za kupambana na umaskini wa sehemu za mashambani. Pia sekta hii haijachangia maendeleo ya kitaifa yenye kukuza usawa.

Baada ya Vita Vikuu vya Pili, mfumo mpya wa kilimo kilichoendeshwa na mashirika ya serikali ulizuka katika nchi kadhaa za Afrika Magharibi. Upo ushahidi unaoonyesha kuwa makampuni ya kimataifa ya biashara za mazao ya kilimo yataendelea kuwa na umuhimu katika uzalishaji wa kilimo wa baadhi ya nchi za Kiafrika.[3]

## Mipango ya uzalishaji wa kilimo, mipango ya makazi na vyama vya ushirika

Mojawapo ya mipango ya makazi ya wakati wa ukoloni ambayo ilifaulu ulikuwa ni mradi wa mashamba makubwa ya kunyunyuziwa maji na uliotumia mashine ya Gezira ambayo huzalisha pamba ya kuuzwa nje. Mradi huu uliendeshwa kwa pamoja na serikali, wazalishaji Waafrika wenye kukodi mashamba na makampuni mawili ya kibiashara ambayo ndiyo yaliyosimamia uendeleshaji hadi mwaka wa 1950, ambapo ulichukuliwa na shirika la serikali ya Sudan la halmashauri ya Gezira.

Mojawapo ya mipango mikubwa na yenye maafa zaidi ni ule wa uzalishaji karanga Afrika Mashariki ambao uliendeshwa na kampuni ya vyakula ya *British overseas Food Corporation* mnamo mwaka 1946. Wafaransa katika Ufaransa ya Afrika Magharibi na Afrika ya Ikweta, na Wabelgiiji katika Kongo wote walianzisha makazi mengi (*paysannat*) ambayo yalilenga katika kuimarisha uzalishaji wa kilimo cha wakulima wadogo wadogo, na pia kuendeleza mazao ya biashara.

Hadi kufikia mwisho wa wakati wa ukoloni, kulikuwepo na vyama vingi vya ushirika vya kuwahudumia wakulima wadogo wadogo katika uuzaji wa mazao ya kilimo, huduma kwa wakulima, na utoaji wa mikopo. Uimarishaji wa uzalishaji wa kakao nchini Ghana na Nigeria na kahawa nchini Tanzania na Waafrika ulisaidiwa na huduma za vyama hivyo. Katika makoloni ya Wafaransa ya Afrika Magharibi, vyama vya *Societes indigéne de prévoyance* vilisaidia katika kuwaelimisha wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji wa kilimo.

[3] C. Eindstrand na S. Amini, 1975

Tangu wakati wa uhuru mashirika mengi ya serikali na ya umma yamekuwa yakiingilia maendeleo ya kilimo katika sehemu nyingi za Afrika. Kila mahali vyama vingi vya ushirika vinavyosimamiwa na serikali vimezuka. Mipango mipya ya makazi na ya unyunyuziaji maji mashambani imeendelezwa. Miradi hii imetofautiana sana katika viwango, malengo, mbinu, na matokeo. Kulikuwa na miradi midogo ya majaribio ambayo malengo yake yalikuwa ni kutathimini ufanyaji kazi wa mashine na mbinu mpya za uzalishaji katika ekologia na masharti ya kilimo ya Afrika, na pia miradi mikubwa ya kibiashara kama vile bwawa la Aswan lililoko Misri ya Juu. Bwawa la Aswan limewezesha unyunyuziaji maji wa kudumu na kuzidisha maradufu matumizi ya ardhi.[4]

Serikali ya Tanzania ilianzisha mradi wa *ujamaa* ambao uliwaleta pamoja watu waliosambaa mashambani ili kuwawezesha wakulima kupata huduma bora zaidi za kilimo na za aina nyingine.[5] Katika nyakati za awali za uhuru, mbinu ya maendeleo ya miradi ya makazi iliyokuwa inapendwa sana ilikuwa ile ya Waisraeli ya Moshav ambayo ilikuwa mashamba madogo madogo ya watu binafsi lakini kukiwa na huduma za pamoja za ulimaji, uuzaji, na huduma za kijamii. Kwa kuzingatia uzoefu huu washauri kutoka Israeli walikuwa na jukumu muhimu katika kupanga miradi ya makazi katika Tanzania, Kenya na Ghana.[6]

Katika nchi kadhaa miradi ya uzalishaji kwa mashine ilianzishwa ikiwa na lengo la kurahisisha upanuzi wa ardhi ya kilimo ili kuzidisha uzalishaji na kupunguza uhamaji wa waliomaliza shule kutoka sehemu za mashambani kwenda mijini.[7] Ni miradi michache sana kati ya miradi ya mipango ya makazi ya Afrika ambayo ilihusisha umilikaji wa pamoja wa ardhi.[8] Tangu miaka ya muongo wa 1970 miradi kadhaa ya maendeleo iliyokuwa imetungamanishwa, na ambayo ilizingatia upunguzaji wa umaskini, ilianzishwa kutokana na usaidizi wa Benki ya Dunia na mashirika mengine kama vile USAID (*United States Agency for International Development*), Shirika la maendeleo ya Kimataifa la Marekani na CIDA ( Shirika la maendeleo ya Kimataifa la Kanada). Miradi hiyo ilikuwa ni pamoja na ile ya unyunyuziaji maji mashambani, maendeleo ya mifugo, uhifadhi wa udongo na maji, mikopo na uendelezaji wa nyenzo za maendeleo.

[4] The Economist, 25 May 1 - 1 June 1984, uk. 42

[5] J. Nyerere, 1967b.

[6] L. Cliffe na G. Cunningham 1973

[7] D. Olatunbosun, 1967

[8] R. Chambers, 1968

## Uuzaji na taratibu za uwekaji wa bei za mazao ya kilimo

Sura mbili za kilimo cha Kiafrika cha kikoloni na kikoloni mamboleo na maendeleo vijijini zinadhihirika zaidi katika mifumo ya uuzaji na bei ambazo wakulima hukabiliana nazo katika masoko makubwa ya mazao ya kilimo. Haya ndiyo mambo yanayobainisha mapato ya wakulima pamoja na viwango vyao vya maisha.

Tangu Vita Vikuu vya Pili na pia, baada ya kujipatia uhuru, serikali za Kiafrika zenye mifumo unganifu zimezingatia, kwa taratibu, uwekaji wa sera za uzalishaji wa kilimo wa mazao ya kuuza nje na ya vyakula vya ulaji wa ndani.

Njia za uhusikaji wa serikali katika kilimo zimekuwa ni pamoja na kusawasisha bei kwa wakulima na utumiaji wa mazao ya ziada kwa manufaa ya jamii za walimaji na pia kwa manufaa ya maendeleo ya nchi za Kiafrika kwa jumla. Uuzaji wa mazao umebakia, kuwa mojawapo ya vikwazo vya mafanikio katika maendeleo ya kilimo. Tatizo la uuzaji limezuka kutokana na urithi wa kikoloni ambapo kabla ya uhuru idara za ustawi wa kilimo, halmashauri ya uuzaji na uwakala wa uuzaji ulianzishwa ili kuendeleza mazao ya kuuzwa katika masoko ya nje.[9] Kutokana na hali hii, mengi ya mataifa ya Kiafrika yamekuwa na mapato mengi ya kifedha ya kiutawala na kanuni wa utoaji na uhitaji za masharti ya masoko ya nchi za ng'ambo zilizoendelea kiviwanda na pia yakitegemea bei zilizopangwa rasmi na kuthibitiwa na serikali mabadiliko ya bei husababishwa na athari kadhaa nyingine kama vile hali duni za maghala ya kuhifadhia; udhaifu katika uvunaji, utayarishaji na upakiaji; uhaba wa mikopo mitaji, ukosefu wa taarifa kuhusu masoko na bei unaotokana na mawasiliano duni na mitandao duni ya kihuduma na kiasasi.

Mifumo ya kimawasiliano na kiasasi, zilizorithiwa kutokana na enzi ya ukoloni iliundwa ili kusaidia biashara ya kuuza na kununua kutoka nje. Hii ina maana kuwa mifumo hiyo iliundwa ili kuunganisha maeneo ya uzalishaji wa mashamba makubwa na ya mazao ya kuuza nje na bandari na vituo vya kuuzia mazao hayo. Kwa sababu hizi, nyingi za nchi za Kiafrika hazina kabisa huduma za usafiri na uhifadhi wa mazao ya vyakula. Matokeo ya hali hii ni kuwa kiasi kikubwa cha mazao ya ziada huharibika na yale yanayofikia masoko ya mijini huwa na bei kubwa zaidi licha ya kuwepo usimamizi wa bei. Hii husababisha kupanda kwa gharama za maisha kwa walaji wanaoishi katika sehemu za mijini.[10]

Katika nchi nyingi za Kiafrika bei za chini zinazolipwa kwa wakulima mashambani hutokana na uingiliaji wa soko na serikali, jambo ambalo hulazimisha

[9] Tazama kwa mfano, S. La-Anyame, 1970 na 1971

[10] Tazama FAO, 1977

JEDWALI 12.*1 Idadi na nafasi ya biashara ya walaji na jamii za masoko katika nchi zilizochaguliwa, mnamo 1954 na 1957*

| *Nchi** | *Idadi* | | *Biashara (thamani katika £1000s)* | |
|---|---|---|---|---|
| | 1954 | 1957 | 1954 | 1957 |
| *Jamii za walaji* | | | | |
| Rhodesia ya Kaskazini (Zambia) | 24 | 21 | 490 | 2020 |
| Nyasaland (Malawi) | 16 | 12 | 36 | 124 |
| Kenya | 17 | 17 | 3787 | 4510 |
| Tanganyika (Tanzania) | 4 | 5 | 26 | 35 |
| Uganda | 11 | 5 | 128 | 53 |
| Zanzibar (Sehemu ya Tanzania) | 2 | 2 | 2 | 9 |
| Pwani ya Dhahabu (Ghana) | 16 | 6[b] | - | 27[b] |
| Nigeria | 50 | 37 | 41 | 500 |
| Sierra Leone | 2 | 1 | - | 16 |
| *Jamii za Masoko* | | | | |
| Rhodesia ya Kaskazini (Zambia) | 80 | 138 | 3638 | 4578 |
| Nyasaland (Malawi) | 48 | 70 | 68 | 83 |
| Kenya | 297 | 425 | 12264 | 1849<br>1 |
| Tanganyika (Tanzania) | 231 | 462 | 7830 | 1036<br>0 |
| Uganda | 991 | 1373 | 2619 | 4112 |
| Zanzibar (Sehemu ya Tanzania) | 1 | 2 | - | [c] |
| Pwani ya Dhahabu (Ghana) | 363 | 376b | 6059 | 7457 |
| Nigeria | 538 | 1105 | 2188 | 4331 |
| Sierra Leone | 133 | 216 | 138 | 218 |

*Majina ya sasa katika mabano
[a] Mwishoni mwa mwaka
[b] 1955
[c] Pungufu ya £1000

*Chanzo: Waraka wa Ushirikiano wa Habari kwa Nchi Makoloni, Novemba 1955,* Januari 1957, Februari 1958 na Machi 1959 (umetolewa na Muungano wa Ushirika, Manchester, Uingereza)

wakulima wengi kuzalisha mazao ya kukidhia mahitaji yao tu. Vijana wanaoacha shule hukatishwa tamaa ya kufanya kazi ya kilimo, na kwa hiyo kusababisha upungufu wa wafanya kazi mashambani.

## Halmashauri za uuzaji, vyama vya ushirika na usimamizi wa bei

Tangu miaka ya 1930, mbinu tatu muhimu zimetumiwa katika kutatua matatizo ya uuzaji barani Afrika, nazo ni halmashauri na uwakala wa uuzaji, vyama vya ushirika vya uuzaji, na usimamizi wa bei. Katika nchi ambamo kulikuwa na idadi kubwa ya wakulima walowezi wa Kizungu, uzalishaji na uuzaji wa mazao ya bei ya juu ulisimamiwa na mifumo iliyokuwa na ukiritimba au nusu ukiritimba kisheria, na ambayo haikuwahusisha Waafrika. Nchini Algeria, kutokana na agizo la Ufaransa la mwaka wa 1947 mazao mengi ya wakulima wa kisetla yaliuzwa na vyama vya ushirika ambavyo vilipata ruzuku kubwa. Kwingineko katika Afrika ya kikoloni, kabla ya Vita Vikuu vya Pili, biashara ya uuzaji wa nje wa mazao ya kilimo ilitawaliwa na makampuni yaliyowaajiri walanguzi (Waafrika) na pia Walebanoni, Wasiyria na Waasia, walionunua mazao kutoka kwa wakulima na kuyasafirisha hadi kwenye stoo na mabohari ya makampuni hayo. Katika makoloni ya Waingereza ya Kiafrika kampuni kubwa zaidi ilikuwa ni *United Africa Group*.

Katika nchi ambamo uzalishaji wa wakulima wadogo wadogo ulikuwa ndio msingi wa maendeleo kulikuweko na vyama vya kushugulikia uuzaji wa nje wa mazao ya kuuzwa. Hata hivyo, jumla ya mauzo yao yalielekea kuwa ya kiasi kidogo. Kufikia mwisho wa enzi ya ukoloni, kiasi kikubwa zaidi cha uuzaji nje wa mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na yale yaliyozalishwa na Waafrika, kilishughulikiwa na mashirika ya serikali yaliyokuwa na usimamizi kamili wa kununua na kuuza mazao yote yaliokuwa chini ya usimamizi wa bei.

Utozaji wa kodi kubwa uliofanywa kwa wakulima wa mazao ya biashara na halmashauri za uuzaji za wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni ulizuia kukua kwa tabaka la wakulima wadogo wadogo wenye hali nzuri kiuchumi na pia tabaka huru la kati.[11] Baada ya uhuru, kiasi kikubwa cha pesa ambacho serikali na mashirika yake yalizipata kilizusha ufisadi mkubwa wa kisiasa na kiutawala kwa kuwa usimamizi wa fedha hizo kuliingia mikononi mwa mamlaka ya kisiasa.

Serikali za Kiafrika pia, zilijiingiza moja kwa moja katika uuzaji wa vyakula kwa kusimamia bei. Ilikuzuia kupanda kwa bei za vyakula, katika sehemu za mijini mashirika ya uuzaji huagiza vyakula kutoka nje. Kwa sababu hii, katika nchi nyingi

[11] P.T. Bauer, 1981, uk. 180

za Kiafrika uagizaji wa vyakula kutoka nje umekuwa mojawapo ya matumizi makubwa ya fedha za kigeni. Kwa kuwa mapambano ya wafanyakazi wa mijini, walioandaliwa vizuri yameweza kuzipindua serikali za Kiafrika, hufuatia maandamano na ghasia juu ya bei kubwa za vyakula na gharama za maisha, serikali zimekuwa zikilinda maslahi yake kwa kutopandisha bei za vyakula. Jambo hili hufanyika hata ingawa uwekaji rasmi na usimamizi wa bei huwa na madhara mabaya na, pia, ingawa kusimamia usambazaji na uuzaji wa vyakula kumekuwa kwa gharama kubwa na bila mafanikio mengi.[12] Matokeo makubwa ya sera za usimamiaji rasmi wa bei yamekuwa ni pamoja na ushukaji wa uzalishaji wa ndani na ukuaji wa uuzaji haramu na magendo.

Zaidi ya matatizo ya jumla ya taratibu za uzalishaji, na uuzaji wa mazao ya vyakula umekuwa na matatizo yake maalum. Kwanza ni kuweko kwa wanunuzi na wauzaji wengi mno, ambao huunganishwa na walanguzi wenye mifumo tata ya usambazaji na upatanishi bila kusahau wazalishaji ambao mara nyingi huuza moja kwa moja kwa walaji wa mashambani na kando ya barabara. Kiasi aina kisichopungua aina sita za wasambazaji kimetambuliwa katika Afrika, nao ni walanguzi wanaonunua kutoka mashambani, maajenti rasmi na wasio rasmi, maajenti wa vyama vya ushirika, wauzaji wa jumla na wa rejareja. Hawa wote nyakati fulani fulani hufanya shughuli mbalimbali za uuzaji, ama kama wafanyabiashara binafsi au kwa kushirikiana na wengine.[13] Ingawa wauzaji wa jumla huwa, na kiasi fulani cha ukiritimba wanaposhughulika na wauzaji wa rejareja na walaji, wauzaji wa rejareja hushughulika katika hali ya ushindani mkali. Kwa sababu hizi na kwa kiasi kikubwa, bei huzingatia masharti ya soko japo huweza hubadilikabadilika kutokana na gharama kubwa za usafiri hasara kubwa zinatokana na uhifadhi hafifu na hatari kubwa zilizomo katika biashara hii na Mabishano kuhusu bei huwa mambo ya kawaida.[14]

Matatizo makubwa ambayo yamo katika masoko ya vyakula ya nchi nyingi za Kiafrika pamoja na mfumko wa bei katika masoko ya sehemu za mijini ni dhihirisho la uwili uwekevu na kutoendelea kwa chumi za Afrika ambazo serikali huru ziliziriithi kutokana na ukoloni. Chumi hizi hutawaliwa na shughuli za uzalishaji wa kujikimu usio na kibiashara wa masoko yenye umuhimu mdogo tu[15].

[12] Tazama M. Owusu, 1972

[13] Q.B.O. Anthonio, 1973, kur. 251-2

[14] V.C. Uchendu, 1967, kur. 37-50

[15] Tazama R.H. Bagtes, 1981; J. Heyer et al., 1981 Pbohannam naG. Dalton 1965, kur. 1-32, kuhusu uchumi na masoko ya Afrika

JEDWALI 12.2 Maendeleo ya ushirika wa jamii za Pwani ya Dhahabu (Ghana)

| Mwaka | Idadi ya Jamii | Jumla wanachama | Tani za kokoa | Ushirika wa kokoa kama asilimia ya Idadi ya zao la Pwani ya Dhahabu |
|---|---|---|---|---|
| 1939-40 | 395 | 10282 | 3917 | |
| 1940-1 | 285 | 6539 | 6736 | 2.2 |
| 1941-2 | 265 | 6375 | 9924 | 2.8 |
| 1942-3 | 253 | 6149 | 9446 | 4.0 |
| 1943-4[a] | 254 | 6439 | 12420 | 4.6 |
| 1944-5[b] | 150 | 6102 | 16765 | 6.3 |
| 1945-6 | 97 | 6712 | 14604 | 7.3 |
| 1946-7[c] | 106 | 7948 | 14451 | 7.0 |
| 1947-8 | 134 | 11919 | 21942 | 7.5 |
| 1948-9 | 160 | 13133 | 27720 | 10.1 |
| 1949-50 | 179 | 14612 | 29468 | 11.6 |
| 1950-1 | 199 | 16355 | 31617 | 12.1 |
| 1951-2 | 225 | 18398 | 28818 | 13.7 |
| 1952-3 | 291 | 26287 | 47423 | 19.2 |

[a] Idara ya ushirika iliyoanzishwa mwaka 1944
[b] Muungano wa Ushirikiano wa Pwani ya Dhahabu (Ghana) ulioanzishwa Novemba 1944
[c] Benki ya Ushirikiano ya Pwani ya dhahabu (Ghana) iliyosajiliwa Oktoba 1946

Chanzo: J.C. De Graft-Johnson, 1958, uk.78.

JEDWALI 12.3 *Maendeleo ya Ushirika wa jamii za Kokoa za Nigeria*

| Mwaka | Idadi ya jamii | Jumla ya wanachama | Tani za kokoa | Ushirika wa kokoa kama asilimia ya jumla ya zao la Nigeria |
|---|---|---|---|---|
| *1939-40* | *138* | *9346* | *5915* | *5.24* |
| *1946-7* | *242* | *18594* | *13253* | *11.95* |
| *1947-8* | *283* | *20585* | *11090* | *14.68* |
| *1948-9* | *276* | *19404* | *12918* | *11.96* |
| *1949-50* | *309* | *21299* | *9697* | *9.65* |
| *1950-1* | *319* | *19529* | *10908* | *9.01* |

*Chanzo:* J.C. DeGraft – Johnson, 1958, uk.95

## Vikwazo vya kiekolojia na kijamii dhidi ya uzalishaji wa kilimo baina ya 1960 na 1980.

Kwa jumla vikwazo vya kiekolojia dhidi ya uzalishaji wa kilimo ambavyo vimechangia katika kuongezeka kwa umaskini barani Afrika baina ya miaka ya 1960 na 1980 vimekuwa ni pamoja na vifuatavyo: mifuatano ya majira ya ukame, kuenea kwa jangwa, kuharibika kwa udongo na kuharibiwa kwa misitu. Baadhi ya matatizo hayo ni matokeo ya moja kwa moja ya sera mbaya za kiuchumi na umilikaji wa ardhi. Vikwazo vingine vimekuwa ni ufukara, hali mbaya ya afya, magonjwa, utapiamlo, mapato duni kwa wakulima ambayo yote ni dalili wazi za kutostawi kwa uchumi.

Uhamaji kwa wingi wa wanaume kutoka sehemu za mashambani hadi sehemu za mijini, zenye viwanda, na zenye huduma, huleta hali ya kutotabirika na kuweko kwa kubadilikabadilika kwa wafanyakazi wa sekta ya kilimo. Zaidi ya hayo mfumo wa elimu ambao hauwashawishi watu kuepuka kazi za kilimo; mila, imani na tamaduni za kijadi; mabadiliko katika matumizi na umilikaji wa ardhi; uongezekaji wa haraka wa idadi ya watu, na kuongezeka kwa matumizi ya ardhi; misukosuko ya kijamii na ya kiuchumi, yote haya yameleta vikwazo katika uzalishaji wa kilimo. Kwa mfano, katika miaka ya 1970, wakimbizi wengi, ambao kwa jumla walikuwa wakulima na wafugaji, walitoroka nchini mwao kutokana vita vya vya ukombozi, mapinduzi ya kijeshi, na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Idadi ya wakimbizi hao ilipanda kutoka watu 750,000 hadi kufikia watu milioni 5, ambao walikuwa karibu nusu ya wakimbizi wote duniani.[16]

Baina ya miaka ya 1960 na 1980, idadi ya watu walioishi katika Afrika ya tropiki iliongezeka kwa asilimia sitini na tatu (63%) na kufikia watu milioni 344. Katika muongo wa miaka ya 1970 idadi ya watu barani Afrika iliongezeka kwa wastani wa asilimiambili nukta saba (2.7%) kwa mwaka. Wengi wa watu hawa waliishi katika sehemu za mashambani ambako walisababisha shinikizo kubwa juu ya ardhi, hasa katika baadhi ya sehemu za Kenya, Rwanda, Tanzania na Misri.

Katika baadhi ya nchi za Kiafrika, hasa za Sahel, migogoro ya sekta ya kilimo iliyosababishwa na kutokea kwa duru za haraka haraka za ukame za baina ya miaka ya 1968 na 1974 na pia baina ya 1977 na 1978, ndiyo sababu kubwa za kushuka kwa ukuaji wa uzalishaji wa kilimo (mimea na mifugo); kutuama kwa mauzo ya nje ya mazao ya kilimo pamoja na cha mazao kadha katika soko la

[37] K. Nkhrumah, 1966, G. Kitching, 1980.

JEDWALI 12.4 *Thamani ya ngano na chakula kilichoingizwa katika nchi zilizochaguliwa za Afrika Magharibi katika asilimia*

| Nchi | Mwaka | Asilimia ya jumla ya chakula kama bidhaa iliyoingizwa | Asilimia ya jumla ya ngano kama chakula kilichoingizwa | Nchi | Mwaka | Asilimia ya jumla ya chakula kama bidhaa iliyoingizwa | Asilimia ya jumla ya ngano kama chakula kilichoingizwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nigeria | 1968 | 7.4 | 24.1 | Mali | 1968 | 18.0 | 18.0 |
| | 1969 | 8.3 | 41.2 | | 1969 | 14.2 | 14.2 |
| | 1970 | 7.6 | 26.6 | | 1970 | 26.9 | 26.9 |
| | 1971 | 8.1 | 23.5 | | 1971 | 25.6 | 25.6 |
| | 1972 | 9.6 | 23.5 | | 1972 | 20.2 | 20.2 |
| | 1973 | 10.3 | 29.5 | | 1973 | No data | No data |
| | 1974 | 8..9 | 32.8 | | 1974 | 54.3 | 54.3 |
| | 1975 | 8.0 | 18.4 | | 1975 | 19.4 | 19.4 |
| | 1976 | 8..5 | 22.1 | | 1976 | 16.4 | 16.4 |
| | 1977 | 10.5 | 12.9 | | | | |
| Côte d'Ivoire | 1968 | 12.5 | 14.5 | Upper Volta | 1968 | 18.7 | 18.7 |
| | 1969 | 11.7 | 11.4 | | 1969 | 16.9 | 16.9 |
| | 1970 | 12.6 | 15.5 | | 1970 | 17.3 | 17.3 |
| | 1971 | 12.4 | 5.6 | | 1971 | 17.6 | 17.6 |
| | 1972 | 14.1 | 10.7 | | 1972 | 19.1 | 19.1 |
| | 1973 | 17.5 | 10.5 | | 1973 | 22.4 | 22.4 |
| | 1974 | 14.8 | 6.4 | | 1974 | 31.0 | 31.0 |
| | 1975 | 12.0 | 8.8 | | 1975 | 17.4 | 17.4 |
| | 1976 | 10.8 | 14.3 | | | | |
| | 1977 | 11.7 | 12.3 | Niger | 1968 | 8.4 | 15.9 |
| | 1978 | 11.3 | 11.3 | | 1969 | 9.4 | 10.4 |
| Sierra Leone | 1968 | 17.5 | 10.3 | | 1970 | 10.6 | 25.6 |
| | 1969 | 16.4 | 12.0 | | 1971 | 9.6 | 15.7 |
| | 1970 | 21.5 | 12.5 | | 1972 | 12.6 | 7.1 |
| | 1971 | 19.2 | 13.4 | | 1973 | 15.6 | 9.6 |
| | 1972 | 17.5 | 14.8 | | 1974 | 17.9 | 5.2 |
| | 1973 | 24.0 | 18.0 | | 1975 | 9.3 | 7.6 |
| | 1974 | 22.3 | 13.5 | | 1976 | 6.4 | 6.2 |
| Senegal | 1968 | 34.8 | 9.0 | | | | |
| | 1969 | 31.6 | 11.9 | Chad | 1968 | 10.3 | 39.4 |
| | 1970 | 26.1 | 16.9 | | 1969 | 16.3 | 14.2 |
| | 1971 | 29.2 | 14.5 | | 1970 | 15.7 | 10.9 |
| | 1972 | 25.7 | 11.8 | | 1971 | 15.6 | 15.2 |
| | 1973 | 34.1 | 11.0 | | 1972 | 20.9 | 12.5 |
| | 1974 | 26.7 | 8.5 | | 1973 | 24.7 | 15.3 |
| | 1975 | 22.0 | 16.8 | | 1974 | 20.7 | 15.5 |

*Chanzo:* D.E. Vermeer, 1983, uk. 74-83; imetolewa tena kwaidhini ya Taasisi ya Elimu ya Helen Dwight Reid.;Iimechapwa na Shirika la Uchapaji la Heldref, 4000 Albermarle St, N.W., Washington, D.C. 20016.




Fig: 12.1 Hatari ya kuenea kwa jangwa katika Afrika kama ilivyoelezwa baada ya mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu kuenea kwa jangwa, 1977 (chanzo: imerekebishwa kutokana na UNEP Studies, 1981, tz 2, uk. 7)

dunia; uongezekaji wa haraka wa uagizaji wa vyakula vya nafaka kutoka nje kama vile ngano na mchele na pia uongezekaji wa mahitaji ya misaada ya vyakula na utegemeaji wa misaada kutoka nje.

## Vikwazo vya kiekolojia vya kiasili na vya kibinadamu

Udongo mwingine wa Afrika ni mwembamba, kiasili, mwepesi na wenye upungufu wa mboji. Kwa kuwa una rutuba ya wastani tu udongo huo huhitaji usimamizi wa makini. Imedaiwa kwamba kasi ya uharibifu wa mazingira na kuenea kwa jangwa katika Afrika kumeendelezwa zaidi na kutumiwa kwa teknolojia ya kisasa iliyoletwa wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni katika maeneo yenye unyevunyevu ya tropiki.[17]

Wataalamu wanakubaliana kuwa hali ya hewa ya bara la Afrika inazidi kuwa ya kigeugeu, jambo ambalo hupunguza idadi ya mimea na ya mifugo inayoweza kuzalishwa na pia kuchangia uharibifu mkubwa wa mazingira, hasa katika maeneo Pia, hali hii hufanya iwe vigumu sana kuwa na mipango ya uzalishaji wa kilimo cha muda mrefu Inakadiriwa kuwa kiasi cha kama asilimia 55 ya bara la Afrika kinahatarishwa na kuenea kwa jangwa na asilimia 45 huathiriwa na ukame.[8] Hii ina maana kuwa zaidi ya nusu ya bara hili na idadi ya robo ya watu wake, wengi wao wakiwa katika sehemu za mashambani, hatari.[9] Eneo la kama kilometa milioni kumi za mraba linalopatikana katika nchi 21 limetapakaa mbung'o ambao huzuia ufugaji. Athari mbaya za mambo haya dhidi ya uzalishaji wa kilimo ni wazi. Katika bara zima la Afrika wakulima wengi hutegemea kilimo cha mvua. Kilimo cha kunyunyuzia maji mashambani ni muhimu katika nchi ya Misri peke yake. Kwa jumla hali ya mazingira ya Afrika haifai kwa maendeleo ya unyunyuziaji wa maji mashambani kwa sababu ya uhaba wa maji, uhaba wa udongo mzuri na tatizo la maji kugeuka kuwa ya chumvi. Ni kama theluthi moja tu ya bara hili ambayo hupata zaidi ya mvua ya milimita elfu moja (1000mm) kwa mwaka. Sehemu zenye maji ya kutosha ni kiasi cha robo moja tu ya Afrika ya tropiki. Hali mbaya na ya kutotegemewa ya mvua katika kipindi chote cha mwaka, pàmoja na hali ya juu ya joto na kunyonywa kwa maji na jua, hupunguza sana aina ya mimea na mifugo inayoweza kuzalishwa kwa mafanikio.

[17] Tazama Accelerated Development, 1983, kr. 46-50 na Jedwali 6

[18] S. Galal, 1977, FAO, 1977

[19] UNEP, 1981

Kuendelezwa kwa wingi kwa visima vya maji katika maeneo ya malisho kulikofanywa na mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa baina ya miaka ya 1960 na 1980, hasa katika Afrika Magharibi, kulizusha madhara kama vile uzidishaji wa idadi ya mifugo malishoni, uharibifu wa sehemu za malisho na mmonyonyoko wa ardhi. Kikundi kingine cha vikwazo ambavyo huathiri uzalishaji wa mimea na mifugo ni maadui maarufu kama vile wanyama wagugunaji, ndege, wadudu (hasa nzige) na magonjwa yaletwayo na virusi.



Picha Ukame wa 1947 nchini Algeria kondoo kwenye mtaro usiokuwa na maji

Kwenye ardhi zenye joto na maji ya kutosha, katika sehemu za tropiki, kuwepo kwa mbung'o hutatiza ufugaji wa ng'ombe na kilimo cha mchanganyiko. Mbali na njaa na vyakula visivyo na liskeya kutosha inawezekana kutaja magonjwa yaletwayo na bakteria na vimelea kama vile malaria, mafua na ugonjwa wa kuhara damu. Haya yote huwa na athari zinazodhoofisha nguvu na uwezo wa kibinadamu wa uzalishaji wa kiuchumi.[20]

[20] Tazama P. Richards, 1983, kuhusu uhakiki wa matatizo ya kiekolojia katika kilimo barani Afrika

### Vikwazo vya kijamii dhidi ya uzalishaji

Kati ya vikwazo vya uzalishaji vya kijamii vinavyoikabili Afrika ni mazoea ya kitamaduni ya wakulima wa Kiafrika. Katika mahali kwingi barani Afrika, ugawaji wa ardhi katika vipande vidogo vidogo vya kati ya hekta mbili na kumi, ambao husababishwa na taratibu za umilikaji wa ardhi, umezuia matumizi ya mbinu bora za uzalishaji ambazo zingezidisha uzalishaji katika sehemu zinapofaa.


Umilikaji ama wa kijamii au wa kifamilia wa ardhi na ng'ombe umekwamisha uimarishaji wa mbinu za kusimamia ng'ombe na ardhi[21]. Mara nyingi fikra za Waafrika juu ya ng'ombe zimetajwa kama mojawapo ya mambo yanayosababisha uzalishaji wa kiwango cha chini. Jamii nyingi za Kiafrika zingali zinapendelea idadi kubwa badala ya ubora wa ng'ombe.

Katika eneo kubwa la Afrika, na zaidi katika Afrika Magharibi, umilikaji mkamilifu wa kijamii umebadilishwa au kuondolewa kabisa kutokana na kilimo kufanywa kuwa cha kibiashara. Hata hivyo licha ya kilimo cha kuhamahama na mtindo wa kufyeka na kuacha, uzalishaji mwingi wa Afrika ya tropiki unaendelea kufifia hasa katika sehemu ambamo idadi ya wakaaji imezidi kiwango cha watu sitini kwa kila kilometa moja ya mraba ya ardhi inayolimika.[22] Katika kiwango hicho, uhifadhi wa rutuba ya udongo unakuwa shida kudumisha kwa sababu ya utaratibu wa matumizi ya ardhi unaohusika na kwa hiyo nafasi za kuzidisha uzalishaji inapungua. Kupunguzwa kwa vipindi vya kurudia matumizi ya ardhi husababisha shinikizo dhidi ya udongo na kuzidisha kasi ya upungukaji wa mazao katika sehemu nyingi za Afrika.

Kuweko kwa mitazamo hasi kuhusu kilimo miongoni mwa wasio wakulima kumelaumiwa kuwa ndiko kunakosababisha ukosefu wa maendeleo ya kilimo barani kote Afrika. Katika nchi nyingi za Afrika, kazi ya ukulima haipewi heshima kubwa kwa sababu ya elimu ya kikoloni ambayo ilisisitiza masomo ya nadharia na kuunda taratibu zilizowatunza wafanyakazi wa sehemu za mujini. Tanzania ni mojawapo ya nchi chache za Kiafrika ambazo zimejaribu kuonisha elimu ya shuleni na kilimo katika sehemu za mashambani[23].

Kuna uhusiano wa karibu kati ya elimu na maendeleo ya kilimo hasa kama inavyoonekana katika utoaji wa mbinu mpya za uzalishaji kwa wakulima waliosoma.[24] Hata hivyo katika sehemu nyingi za Afrika ya tropiki ujuzi wa kazi

[22] D. Grigg, 1970
[23] Tazama kwa mfano, N.O. Addo, 1974
[24] D. Grigg, 1970, uk. 152




PICHA *12.2 Maenezi ya ng'ombe barani Afrika. Picha ndogo inaonyesha maeneo yenye mbung'o. Chanzo: imerekebishwa kutoka R. S. Harrison-Church et al., Africa and its Islands, Longman, London, 1971 uk. 91)*

na utaalamu wa wakulima wakongwe ambao hawajui kusoma na kuandika mara nyingi huwa hautiwi maanani na mashirika ya wadhamini na wataalamu wa kilimo wa serikali, hata ingawa kumekuwa na madhara mengi nyanjani yaliyotokana na ushauri wa wataalamu hawa wa kilimo?[25]

Jambo la muhimu kutambua ni kuwa hata ingawa wakulima wa Afrika kwa jumla, hawajui kusoma na kuandika, ni wa kijadi na wamezeeka, lakini wengi wao kwa ujumla wamekuwa tayari kupokea na kutumia mbinu mpya wanapozielewa. Katika kipindi cha baada ya Vita Vikuu vya Pili wamepokea mbinu mpya za uzalishaji mimea mipya, teknolojia mpya ya usindikaji, mbinu mpya za upangaji wa mimea na uhifadhi na, pia, mifumo mipya ya uuzaji. Hata hivyo, badala ya mengi ya mabadiliko hayo kuimarisha hali ya maisha ya wakulima wadogo, wadogo yamezidisha umaskini wa sehemu za mashambani. Hali hii hudhihirisha kuwa mojawapo ya vikwazo muhimu vya uzalishaji wa kilimo ni kuweko kwa ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi katika sehemu za mashambani na pia unyonywaji wa wakulima wadogo wadogo.

## Kilimo na tofauti za kitabaka katika Afrika baada ya ukoloni

Kwa vyovyote vile na bila kuzingatia hali halisi ya tabaka za kijamii katika sehemu za mashambani za Afrika katika kipindi cha baada ya uhuru,[6] viwango vya umaskini na utajiri miongoni mwa wakulima wadogo wadogo na jamii za wakulima wadogo wadogo vimetofautiana sana baina ya nyakati na nchi mbalimbali. Kwa mfano, tukilinganisha Afrika ya Kasikazini ama na Afrika ya Tropiki au na Afrika Kusini katika wakati wa ubaguzi wa rangi.


Asili ya ulimbikizaji wa mali na ukosefu wa usawa katika sehemu za mashambani Kwa jumla ukuaji wa ukosefu wa usawa katika sehemu za mashambani na tofauti za kitabaka katika Afrika umeendelea kuumbika kutokana na siasa za kilimo.[7]

[24] Tazama S. La-Anyame, 1970 na 1971; J. Heyer et al, 1981 na P. Richards, 1983; kwa mjadala juu ya matatizo ya uanzishaji wa mambo mapya katika kilimo

[25] Tazama S. La-Anyame, 1970 na 1971; J. Heyer et al, 1981 na P. Richards, 1983; kwa mjadala juu ya matatizo ya uanzishaji wa mambo mapya katika kilimo

[26] Tazama S. La-Anyame, 1970 na 1971; J. Heyer et al, 1981 na P. Richards, 1983; kwa mjadala juu ya matatizo ya uanzishaji wa mambo mapya katika kilimo

[27] J. Barker, 1948, G. Dharm na S. Radwan, 1983




Mchoro 12 3 *Ruwaza za wahamiaji wa kimataifa katika Afrika, mnamo 1946-52 (Chanzo· G H.T. Kimble,* Afrika ya Tropiki Juzuu 1, Ardhi na kazi, Hazina ya *Karne ya Ishirini, New York, 1960, uk. 584*

Ulezi wa kisiasa, na sera za bei na masoko ambazo ziliendelezwa na mashirika ya masoko ya serikali ama ziliruzuku wakulima wa kibepari wenye mashamba makubwa au kuwanyonya wazalishaji wa mashamba madogo madogo kwa kuyapunguza mapato yao.[28] Makampuni ya kimataifa ya mazao ya kilimo, mashirika ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na halmashauri za serikali huweza kuweka masharti ambayo kwayo wazalishaji wa mashamba madogo madogo huweza kukuza, au kuuza nje mazao ya kawaida na ya viwanda wanayoweza kuzalisha.[29]

Kuingia kwa ubepari na uzalishaji wa mazao ya kuuza katika sehemu za mashambani hakukuzua tu kwa kikundi kidogo lakini kinachoimarika cha

[28] C. Leys, 1975; M. Morris, 1976

[29] C. Windstrand na S. Amin, 1975; S. Bernstein, 1978; M.S. Halfani na J. Barker, 1948, J. Loxley, 1984; L. Freeman 1984

[30] P. Hill, 1970

*JEDWALI 12.6 Mgawanyo wa kazi kati ya wanaume na wanawake katika vijiji vya Afrika*

| *Kazi* | *Jumla ya asilimia ya Wafanyakazi* | |
|---|---|---|
| | *Wanaume* | *Wanawake* |
| Ufyekaji | 95 | 5 |
| Ukatuaji udongo | 70 | 30 |
| Upandaji | 50 | 50 |
| Ulimaji na upaliliaji | 30 | 70 |
| Uvunaji | 40 | 60 |
| Usafirishaji mazao kutoka | 20 | 80 |
| Usafirishaji mazao kutoka shambani hadi nyumbani | 20 | 80 |
| Uhifadhi mazao | 10 | 90 |
| Uandaaji wa mazao ya chakula | 40 | 60 |
| Masoko kwa ajili ya chakula cha ziada | 90 | 10 |
| Uondoaji wa miti ya mazao | 10 | 90 |
| Ubebaji maji na fueli | | |
| Uangalizi wa mifugo | 50 | 50 |
| Uwindaji | 90 | 10 |
| Ulishaji na utunzaji watoto, wanaume na wazee | 5 | 95 |

[a] Kwa kusaidiwa au bila kusaidiwa na watoto

*Chanzo*: ILO, 1985, UK. 120.

mabepari,[30] bali pia muundo wa kuundwa kwa tabaka la wafanyakazi wa mashambani katika Afrika.[31] Katika Afrika ya Kati na ya Kusini, mahitaji ya idadi kubwa ya wafanyakazi katika migodi, na mashamba makubwa ya masetla yalisababisha kuundwa kwa sheria za ardhi, wafanyakazi, na za fedha ambazo zilizalisha na kurasimisha idadi kubwa ya wafanyakazi wa sehemu za mashambani waliokuwa maskini na wa mishahara midogo. Pia sheria hizo zilisababisha kuwepo kwa wakulima ardhi na wafanyakazi wahamiaji ambao wengi wao hawakuwa na mashamba.[32] Katika Afrika ya Magharibi na baadhi ya sehemu za Afrika

[30] P. Hill, 1970
[31] G. Arrighi na J.S. Saul, 1973; K. Post, 1977
[32] M. Morriss, 1976; G.H.T. Kimble, 1960
[33] Tazama kwa mfano, A.L. Mobogunje, 1972; P.Hill, 1970; R. Stavenhagen, 1975.

Mashariki, ustawishaji wa kilimo cha biashara kama vile kakao, majani ya chai, kahawa n.k.ulizusha hali, iliyofanana na ile iliyotajwa hapo juu ya matumizi ya wafanyakazi wa sekta ya kilimo wa kuhamahama kulingana na majira.[3] Nchini Nigeria sehemu zinazozalisha mafuta ya petroli zimewavutia wakulima wadogo wadogo katoka vijiji vya karibu ambao wameyaacha mashamba yao na kutafuta vibarua, vya kitaalamu na visivyo vya kitaalamu katika viwanda.[3]

Kwa hiyo tofauti za kimaeneo za maendeleo ya kiuchumi zilizodhihirishwa, kijiografia, na mkusanyo wa mahali pamoja wa nyezo za uzalishaji, zilizotokana na tofauti kati ya utajiri wa mali asili baina ya maeneo mbali mbali, na pia mwelekeo usioyumba wa kupeleka bidhaa nje wa chumi za Afrika wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Tofauti hizo, pia, zilichangiwa na ukweli kuwa mgawanyo na janibu za kilimo, biashara na viwanda vya nyakati za ukoloni na baada ya ukoloni ulikuwa na uhusiano mdogo sana na masuala ya usawa wa kijamii cha mahitaji ya sasa au ya baadaye ya wakazi wa sehemu za mashambani za Afrika. Mambo haya yote yamechangia sura mbali mbali za ukosefu wa usawa na kuumbika kwa matabaka ya sehemu ya mashambani katika sehemu nyingi za Afrika.

Katika sehemu ambako kulikuwepo na mifumo ama ya nusu ukabaila ya umilikaji wa ardhi au umilikaji wa ardhi wenye umwinyi, kama ilivyokuwa katika baadhi ya sehemu za Afrika Kaskazini, Mashariki na Magharibi, uzalishaji wa mazao ya kuuza uliwageuza mamwinyi mara moja, wakawa wakulima mabepari wenye utajiri ambao hutumia ushawishi na uhusiano wao wa kisiasa ili kuwanyonya maskini pamoja na wakulima wapangaji wenye madeni na wasio na namna za kujilinda. Kwa namna hii wameunda tabaka la wasio na mashamba na wafanyakazi wa kilimo wanaonyonywa.[35] Uzalishaji wa mazao ya kuuza ya thamani kubwa pamoja na jukumu kubwa lililotekelezwa na wafanyakazi wanaume wenye kuhamahama katika uzalishaji huo yalikuwa mambo muhimu katika kuingia kwa ubepari na ambayo yalikuwa na athari kubwa mbaya katika mgawanyo wa kazi za kilimo baina ya wanawake na wanaume. Pia, athari hizo zimedhoofisha uchumi wa kijadi wa familia ambapo wanaume na wanawake waligawanya majukumu, hasa katika sehemu za Kusini mwa Afrikana Afrika Mashariki, kwa kuweka masharti yasiyo ya usawa na pia mzigo mkubwa juu ya wanawake wazalishaji wa kilimo. Wanawake wamelazimika kufanya kazi kwa saa nyingi zaidi, na umaskini umewalemea zaidi wanawake wa sehemu za mashambani na kuzidisha mgawanyiko wa kijinsia. Pia mapato ya wanawake yametishiwa kwa namna nyingine mbali mbali. Kwa mfano, pombe ya kijadi inayotengenezewa nyumbani

[34] E. Chikwendu, 1983

[35] Tazama A. Richards, 1982, kuhusu Misri, kwa mfano

katika baadhi ya nchi za Kiafrika sasa inakabiliwa na ushindani kutoka bidhaa za kisasa zinazotengenezwa na viwanda vya pombe.[36]

## Tabaka na umaskini uliopangwa wa sehemu za mashambani

Tangu kujipatia uhuru, serikali nyingi za Kiafrika zimeanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo na vijiji kama sehemu moja ya mipango ya maendeleo ya kitaifa na kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama vile UNFAO, USAID, CIDA, Benki ya Dunia na Serikali za Kigeni.

Mchango wa misaada ya kigeni, wa kifedha na wa ushauri, katika mipango ya maendeleo ya kilimo na mabadiliko ya sehemu za mashambani umekuwa mkubwa sana. Hata hivyo, mikopo kwa sekta ya kilimo na misaada ya kiasasi kwa jumla imejikita katika mazao ya kuuzwa nje. Pia misaada ya kigeni na ya serikali ya pembejeo, mikopo, na masoko imenyakuliwa na kikundi kidogo cha wakulima matajiri ambao tayari wamekisha neemeka.

Katika sehemu za mashambani za Afrika watu binafsi na makundi yaliyoneemeka na yenye uwezo hutofautiana baina ya nchi na nchi kulingana na asili zao za kijamii, mapato yao, viwango vya maisha, ukubwa wa mashamba na kiasi cha mazao yanayozalishwa kila mwaka. Kila mahali tabaka la wakulima wa mazao ya kuuza huwa mchangayiko. Hata hivyo, katika Afrika nzima makundi mawili ya jumla yanaweza kutambuliwa katika sehemu za mashambani, nayo ni wakulima matajiri na wafugaji wa ng'ombe wenye mashamba makubwa ambao ndiyo matabaka ya wanyonyaji, na lile la wakulima wadogo wadogo na wafugaji maskini ambao ndiyo matabaka yanayonyonywa.[37]

Kundi la wakulima matajiri hujumlisha wenye mashamba ya mazao ya kuuza (kama vile kakao, kahawa na majani chai) ambao huenda wakawa ni pamoja na maafisa wa serikali na majeshi pamoja na wenye biashara kubwa kubwa ambao huwa ni rahisi kupata mikopo na fedha za kitega uchumi. Wengine ni wafanyabiashara, machifu wa kimapokeo na viongozi wa kidini ambao huwa ni rahisi kupata teknolojia mpya, mikopo na huduma na pia huwa na mahusiano na tabaka la watawala katika mikoa na taifa. Wakulima maskini huwa ni wakulima wadogo wadogo na wachungaji ambao kati yao huenda wakawemo wakulima wapangaji wanaogawanya mazao na wenye mashamba, wakulima wanaodaiwa na matajiri wenye mashamba au vibarua wa vijijini wasio na mashamba.

[36] R. Dauber na M.L. Cain, 1980

[37] K. Nkhrumah, 1966, G. Kitching, 1980.

Mapato ya waishio katika sehemu za mashambani za Afrika yamebaki kuwa ya chini kabisa na hali ya maisha ya sehemu hizo, kama inavyotathiminiwa kwa kukadiria asilimia ya idadi ya watu wanaofikiwa na huduma za maji safi na za kuondolewa kwa maji taka imebaki katika hali duni kabisa ya asilimia 21 ya wanaopata huduma ya maji safi na asili mia 28 wanaopata huduma ya kuondolewa maji taka. Uchunguzi uliofanywa mara nyingi katika nchi kadhaa umeonyesha kuwa tofauti za kitabaka na mapato zinazidi kukua. Watu sabini katika kila mia moja ama ni mafukara au wamo ukingoni wa umaskini.

Katika sehemu zote za mashambani za Afrika, na unyonywaji wa wakulima wadogo wadogo ni mambo yanayoendelea.[38] Hali hii ilifanywa kuwa mbaya zaidi na kushuka kwa uchumi wa dunia, mgogoro wa sekta ya petroli ya miaka ya 1970, kushuka kwa bei za mazao ya kuuza, matatizo ya fedha za kigeni yanazozikabili serikali za Afrika, majanga ya kimaumbile na misukosuko ya kisiasa. Upunguzaji wa umaskini katika sehemu za mashambani za Afrika unahitaji mfumo mpya wa kimataifa wa uchumi na pia mfumo mkali wa ugawanyaji upya wa mamlaka amabao utauwezesha umma wa sehemu za mashambani kusimamia kikwelikweli haki zao za kujiamulia mambo juu ya maisha yao na ustawi wao wa kijamii na kiuchumi.

## Kilimo cha Kiafrika katika uchumi wa dunia tangu 1935: Kutoka makoloni-tegemezi hadi kuwa nchi tegemezi mambo leo

Kwa jumla nchi za Afrika ziliingia katika uchumi wa kibepari wa ulimwengu kama makoloni ya tawala za kizungu za kibeberu. Sera za maendeleo ya kiuchumi za serikali za kikoloni, kwa kupitia biashara ya kimataifa, zilitegemea mgawanyo wa kazi ambao ulikuwa na misingi yake katika faida linganishi. Kanuni hiyo, ya unyonyaji, ilizilazimisha nchi za Kiafrika kuelekeza raslimali zao katika uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje na kutumia mapato yao ya fedha za kigeni kwa kuagizia bidhaa za viwandani na kughariamia mahitaji ya vyakula ili kufidia upungufu wa vyakula. Zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa zilizouzwa nje na mataifa ya Afrika zilikuwa,

[40] Tazama kwa mfano Z. Daoud, 1981, kuhusu Moroko na T.L. Blair, 1970, kuhusu Algeria.

JEDWALI 12.7 Mazao ya kikoloni ya biashara ya malighafi na vyakula imeonyeshwa kama asilimia ya mazao ya biashara duniani.

| *Bidhaa za malighafi mnano 1934 au kabla ya hapa.* | *Asilimia ya mazao ya biashara duniani (makoloni)* | *Vyanzo vikuu vya mazao ya biashara ya makoloni pamoja na asilimia zao duniani kwa nchi za Afrika* | *Mazao ya biashara ya nchi za Afrika katika asilimia ya mazao ya biashara ya makoloni.* |
|---|---|---|---|
| Mawese | 98.8[b] | Nigeria (42.9), Belgian Congo (13.9), French West Africa (6.1), Angola (1.2). | 65.0 |
| Bati | 56.9[d] | Nigeria (4.4), Belgian Congo (3.7). | 14.0 |
| Fosfati | 52.0 | French North Africa (34.6), Freanch Equatorial Africa (7.2). | 80.0 |
| Grafati | 46.0 | Madagascar (7.5). | 16.3 |
| Karanga | 28.5[b] | French West Africa (13.2), Nigeria (4.8). | 63.0 |
| Shaba nyekundu | 21.3[d] | Northern Rhodesia (12.3), Belgian congo (8.6). | 98.0 |
| Manganizi | 13.7 | Nigeria (12.4)[e] | 90.5 |
| Kromu | 12.3[b] | Southern Rhodesia (8.6). | 70.0 |
| Mafuta ya Zeituni | 12.9[b] | French Northe Africa (11.2), Libya (?0.4). | 90.0 |
| Ufuta | 8.0[f] | Sudan (2 2), Congo (?0.8), Nigeria (1.3). | 54.0 |
| Dhahabu | 9.2[b] | Southern Rhodesia (2.8), Gold Coast (1.3), Congo (1.4) | 60.0 |
| Asbesto | 9.5[a] | Southern Rhodesia (9.0).95.0 | 95.0 |
| Pamba | 2.5[f] | Uganda (0.9), Sudan (0.5). | 56.0 |
| Sufu | 2.3[b] | French North Africa (2.0). | 87.0 |
| Zinki | 1.9[d] | Northern Rhodesia (1.4). | 74.0 |
| Vyakula1933 | | | |
| Kakao | 74.0[b] | Gold coast (40.6), Nigeria (11.3), French West Africa (6.8), French Cameroons (2.8), britiah Togo (1.9), French Togo (1.1), British Cameroons (0.6). | 88.0 |
| Mahindi | 24 1[d] | French West Africa (5.9) | 24.0 |
| Matunda ya jamii ya machungwa | 9.7[b] | Algeria (1.0). | 10.0 |
| Tumbaku | 4.8[b] | Nyasaland (0.3).[k] | 0.6 |
| Kahawa | 7.6[b] | British East Africa (0.7), Madagascar (0.6). | 17.0 |

[a] Jamii ya metali [b] 1933. [d] 1934. [e] biashara ya nje ya wavu
[a] 1931 [b] 1934-5 [j] iliyochambuliwa
[k] Sehemu ya tumbaku sasa inalimwa Rhodesia (sasa inaitwa zambia na Zimbabwe). Kwa vile idadi ilikusanywa mnamo 1934, kumekuwa na muongezeko wa bei, muongezeko wa uzalishaji wa malighafi nyingi, mfano wa bati, mpira, shaba nyekundu, dhahabu na zinki. Kwahiyo, kama jedwali la mwaka 1936 lingetayarishwa kungekuwa na tofauti ya asilimia ya malighafi na koloni mojamoja.

*Chanzo*: Tatizo la Koloni. Ripoti ya wanachama wa kundi la Elimu la Kifalme la Taasisi ya Mambo ya Kimataifa, 1937, uk. 290

kwa jumla, ni mazao kama vile kahawa, kakao, majani ya chai, sukari, njugu-karanga, pamba na madini kama vile petroli, shaba na fosfati.[39]

Kufikia wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, mauzo ya nje ya nchi za Kiafrika yalikuwa haba mno yakilinganishwa na yale ya Amerika ya Kusini na Asia. Mauzo ya nje ya kilimo, kutoka nchi za Afrika, yalianza kuongezeka katika

[41] C. Ayari, 1983, kur. 8-11

JEDWALI 12.8 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa zao la mnazi duniani*

| *Mwaka* | *Mafuta yaliyolinganishwa na tani 1000* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1954 | 920 | 77 |
| 1955 | 870 | 78 |
| 1956 | 940 | 79 |
| 1957 | 900 | 79 |
| 1959 | 930 | 80 |
| 1961 | 920 | 79 |

*Chanzo*: Shirika la Chakula Duniani (FAO), 1961a, uk. 115

JEDWALI 12.9 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wazao la kahawa duniani*

| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8 (wastani) | 140 | 6 |
| 1948-52 (wastani) | 280 | 13 |
| 1954 | 390 | 16 |
| 1955 | 510 | 18 |
| 1956 | 510 | 20 |
| 1957 | 540 | 17 |
| 1958 | 610 | 17 |
| 1959 | 670 | 15 |
| 1960 | 730 | 18 |

*Chanzo:* Shirika la Chakula Duniani (FAO), 1961a, uk. 161.

kipindi cha baina ya Vita Vikuu. Kufikia wakati wa uhuru, nchi nyingi za Kiafrika zilikuwa zimejipatia umuhimu katika uuzaji wa bidhaa kadhaa za kutumiwa viwandani.

Ingawa Afrika ni muhimu ulimwenguni kwa uzalishaji wa madini ya kimkakati, bara hili kimsingi limebakia kuwa mzalishaji wa mazao ya kilimo. Afrika inaendelea kuzalisha theluthi mbili za mazao yote ya dunia ya mawese, mkonge na kakao. Katika miaka ya muongo wa 1970 kiwango cha kahawa kilichozalishwa na nchi

40 Tazama kwa mfano Z. Daoud, 1981, kuhusu Moroko na T.L. Blair, 1970, kuhusu Algeria.

JEDWALI 12.10 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa karanga duniani*

| *Mwaka* | *Uzito wa zisizomenywa* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1948-52 (wastani) | 2440 | 26 |
| 1957 | 4100 | 30 |
| 1958 | 3630 | 26 |
| 1959 | 3520 | 29 |
| 1960 | 4080 | 29 |

*Chanzo:* Shirika la chakula duniani (FAO), 1961a, uk.118.

JEDWALI 12.11 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa kokoa duniani*

| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8 (wastani) | 490 | 66 |
| 1948-52 (wastani) | 500 | 66 |
| 1954 | 490 | 60 |
| 1955 | 530 | 64 |
| 1956 | 580 | 64 |
| 1957 | 460 | 60 |
| 1958 | 570 | 62 |
| 1959 | 660 | 65 |
| 1960 | 840 | 76 |

*Chanzo:* Shirika la chakula duniani (FAO), 1961b, uk.145 na 161.

21 za Afrika kiliongezeka mara tatu na kufikia karibu asili mia thelathini ya uzalishaji wote wa dunia.[40]

Kiasi cha ukuaji wa uzalishaji wa kilimo wa Afrika katika miongo ya 1950 na 1960 ulikuwa wa kiwango cha juu hasa wa kakao, kahawa, majani ya chai, ndizi,

[42] A.M. Kamarck, 1972

JEDWALI 12.12 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa mpira - wa asili duniani*

| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8 (wastani) | 10 | 1.0 |
| 1948-52 (wastani) | 60 | 3.6 |
| 1957 | 115 | 5.8 |
| 1958 | 125 | 6.3 |
| 1959 | 145 | 7.1 |
| 1960 | 145 | 7.1 |

*Chanzo*: Shirika la chakula duniani (FAO), 1961a, uk. 146.

JEDWALI 12.13 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa mkonge duniani*

| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8 (wastani) | 160 | 62 |
| 1948-52 (wastani) | 225 | 70 |
| 1954 | 290 | 69 |
| 1955 | 300 | 65 |
| 1956 | 310 | 63 |
| 1957 | 325 | 65 |
| 1958 | 350 | 68 |
| 1959 | 370 | 64 |
| 1960 | 375 | 64 |

*Chanzo:* Shirika la chakula duniani (FAO), 1961a, uk. 145.

karanga na pamba. Ukuaji huu wa haraka ulisaidiwa na uendelezaji wa miundombinu na serikali za kikoloni na za baada ya ukoloni. Kuwepo kwa ruzuku ya serikali ya pembejeo kama vile madawa ya kunyunyuzia wadudu, mbolea ya chumvichumvi, na miche yenye kinga dhidi ya magonjwa na pia kwa kuimarishwa kwa mbinu za uzalishaji, mvua ya kutosha na upanukaji wa kilimo cha kibiashara

JEDWALI 12.14 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa pamba duniani*

| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8 (wastani) | 651 | 11.3 |
| 1948-51 (wastani) | 627 | 11.9 |
| 1956 | 787 | 11.0 |
| 1957 | 813 | 12.0 |
| 1958 | 962 | 13.5 |
| 1959 | 953 | 12.5 |
| 1960 | 876 | 11.9 |


*Chanzo*: Kamati ya Uchumi ya Jumuiya ya Madola, 1961, kielelezo 31, imetolewa kwa idhini ya umiliki wa ofisi kuu ya Uingereza.

JEDWALI 12.15 *Sehemu ya Afrika katika uzalishaji wa sukari duniani.*


| *Mwaka* | *Maelfu ya tani* | *Asilimia ya uzalishaji duniani* |
|---|---|---|
| 1934-8[a] | 1100 | 7.4 |
| 1948-52[a] | 1560 | 7.9 |
| 1956[b] | 2230 | 8.9 |
| 1958[c] | 2555 | 8.8 |
| 1959[c] | 2675 | 9.0 |
| 1960[c] | 2400 | 7.6 |


*Vyanzo*: [a]Shirika la chakula duniani (FAO), 1956, uk.73.
[b]Shirika la chakula duniani (FAO), 1958, uk.71.
[c]Shirika la chakula duniani (FAO), 1961a, uk.73.

haya yote yakiwa ni kwa kusabilia (kudidimiza) uzalishaji wa vyakula. Hata hivyo bei za mazao ya kuuzwa nje, ambazo zilisimamiwa na walaji wa nchi zilizoendelea, hupanda na kushuka sana. Hali hii, haikuweza kufidiwa kwa kuongezea viwango vya uzalishaji.




Mchoro 12.4 *Sehemu kuu za madini katika Afrika* (*Chanzo:* Imetolewa na R S. Harrison-Church na wenzake, Afrika na visiwa vyake, Longman London, 1971, uk 99)




JEDWALI 12 5 Mgawanyo wa mazao ya biashara katika Afrika (Chanzo Imetolewana R S Harrison na wenzake, Afrika visiwa vyake, Longman, London, 1971, uk 87

Hali ya chini ya unyumbukaji wa mahitaji ya mazao ya kutumika viwandani kutoka Afrika, ikilinganishwa na bidhaa za kutoka katika viwanda vya mataifa yaliyoendelea, huzidisha tatizo la kupanda na kushuka kwa mapato ya nchi. Upo uhusiano thabiti kati ya uzalishaji wa viwandani wa kimataifa na biashara ya mazao ya kutumika viwanandani ambapo chumi zenye viwanda hukua haraka zaidi kuliko chumi za wazalishaji wa mali ghafi. Kwa namna nyingine, masharti yaliyoingiza Afrika katika masoko ya ubepari wa ulimwengu, katika wakati wa ukoloni, yaliiweka Afrika katika hali ya uzalishaji wa mazao ya kuuza nje ambayo yana matumizi kidogo sana kwa bara hili. Kwa hiyo masharti hayo huzidisha kutoendelea kwa Afrika na pia kuendeleza njaa kwa sababu kilimo cha vyakula huwa hakitiliwi maana kwa kuwa mkazo umo katika uzalishaji wa mazao ya kuuza nje.

*JEDWALI: 12.16 Kiasi cha ukuaji wa kilimo na mazao ya chakula yanayozalishwa katika Afrika*

| | *Jumla* | | | *kwa raslimali* |
|---|---|---|---|---|
| | *1960-70* | *1970-80* | *1960-70* | *1970-80* |
| Mazao ya kilimo Yanayozalishwa nje | | | | |
| Afrika | 2.7 | 1.3 | 0.1 | -1.4 |
| Nchi zinazoendelea | 2.8 | 2.7 | 0.3 | 0.3 |
| Mazao ya chakula Yanayozalishwa | | | | |
| Afrika | 2.6 | 1.6 | 0.1 | -1.1 |
| Nchi zinazoendelea | 2.9 | 2.8 | 0.4 | 0.4 |

KUMBUKA. Taarifa za uzalishaji hupimwa na kitengo cha bei cha nje cha Biashara ya dunia. Kiasi cha Ukuaji katika muongo kimewekwa katika kiwango cha wastani cha miaka mitano, isipokuwa ya 1970 ambayo ni wastani kwa 1969-71

*Chanzo*: Shirika la Chakula Duniani (FAO), 1982a, uk. 41

Utaratibu wa kikoloni wa biashara kati ya Afrika na ulimwengu haujabadilika. Biashara na mataifa ya Ulaya ya Magharibi, ambayo yalikuwa watawala wa kikoloni, ingali ndiyo muhimu sana kwa Afrika. Kwa kweli theluthi mbili za biashara yote ya Afrika huhusisha Ulaya ya Magharibi na hakuna sehemu nyingine yoyote ya Ulimwengu wa Tatu ambayo hukuza mazao ya kuuza inayotegemea Ulaya ya

Magharibi kama Afrika. Jambo hili la faa kuwekwa akilini wakati wa majadiliano juu ya vikwazo vinavyozuia madai ya Ulimwengu wa Tatu ya mfumo mpya wa kiuchumi.

Kuporomoka kwa sekta ya kilimo hasa katika Afrika ya tropiki, ambamo asilimia themanini ya watu hutegemea kilimo, na ambamo huleta sekta hiyo fedha zaidi za kigeni na mapato ya nchi nyingi za Afrika, kulikotokea katika miongo ya 1960, 1970, na 1980, kulisaidiwa na kuzidishwa na kipindi kirefu cha mdororo wa uchumi wa dunia na mfumko wa bei ulioletwa kutoka nje. Pia hali hii ilisaidiwa na mahitaji ya chini na bei za chini za mazao mengi ya kuuzwa nje katika soko la ulimwengu, kushuka kwa thamani ya pesa za nchi za Kiafrika dhidi ya zile za kigeni, kuzidi kwa mzigo wa madeni, kupunguzwa kwa ruzuku za mazao ya kuuzwa nje kutoka nchi muhimu zilizoendelea, na vikwazo juu ya uagizaji wa mazao ya kilimo na bidhaa nyingine zilitokana na viwanda vya Afrika na vya mataifa mengine yanayoendelea vilivyowaajiri watu wengi. Hali hii mbaya imezidishwa na utegemeaji mkubwa wa chumi za Afrika juu ya kilimo cha aina moja.

Muundo wa kilimo cha ulimwengu umebadilika tangu muongo wa 1950. Katika nchi zilizoendelea uzalishaji na uuzaji wa mazao ya kilimo umepata mapinduzi kutokana na utumiaji wa matokeo ya utafiti wa kisayansi na mashine. Bara la Afrika, hali kufaidika na mapinduzi haya ya kilimo, kwani si rahisi kuhamishia magunduzi hayo kwenye mazingira ya kiekolojia na kijamii-uchumi ya Afrika. Hali hii ya kutogharamia utafiti vya kutosha juu ya mimea inayozalishwa kwa kutumia mvua, na pia mimea ya mizizi na ukosefu wa uimarishaji wa teknolojia inayofaa kwa mazingira ya kilimo ya Afrika, pia imechangia kwa kiasi kikubwa, utendaji mbaya wa sekta ya kilimo ya Afrika katika miongo ya 1970 na 1980.

Ukuaji wa uzalishaji wa kilimo wa kila mwaka wa bara la Afrika ulipunguka kutoka asili mia 2.7 katika muongo wa 1960 hadi asili mia 1.3 katika muongo wa 1970 wakati kiwango cha uongezekaji wa idadi ya watu kilizidi kukua. Mabadiliko haya yamemaanisha kuwa uzalishaji wa kila mtu uliongezeka kwa kiwango cha asili mia 0.2 kwa mwaka katika muongo wa 1960 na kushuka kwa asili mia 1.4 kwa mwaka katika muongo wa 1970. Sehemu moja ya upungukaji huu inahusiana na ushukaji wa uzalishaji wa mazao yasiyo ya vyakula kama ya vinywaji na ya nyuzi. Pia uzalishaji wa mazao ya vyakula wa kila mtu ulibadilika kutoka uongezekaji wa kiwango kidogo katika muongo wa 1960 hadi upungukaji wa asili mia 1.1 katika muongo wa 1970.

Tangu Vita Vikuu vya Pili vya Dunia asasi kadhaa zilianzishwa ili, ama kuthibiti biashara ya mazao (km. GATT) au kutoa misaada ya kiuchumi kwa nchi maskini.

Muhimu kati ya asasi hizo ni kama vile Benki ya Dunia, IMF, GATT (1948) IFC, IDA, UNCTAD (1964) na STABEX (1975). Misaada hutolewa ama moja kwa moja kama mikopo, km. Kutoka Benki ya Dunia au IMF, ya muda mrefu au mfupi, au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kupitia uongezaji wa kiwango cha mauzo ya nje ambacho nchi maskini ingeweza kuuza; kushiriki kwa nchi maskini katika mikataba ya mauzo iliyojadiliwa mara kwa mara ambayo ilitoa viwango vya uuzaji kwa nchi husika na kusawasisha mfumko wa bei au kutoa kiwango cha juu zaidi cha bei ya jumla kuliko ambavyo bei ingekuwa kama haikusimamiwa; kuweka mfumo wa jumla wa upendeleo wa viwango vya ushuru wa forodha (kama mtindo wa UNCTAD) kuendeleza utengenezaji wa bidhaa za viwandani katika nchi zinazoendelea; na kufidia au kutoa misaada ya kifedha ili kusawazisha upungufu wa pesa za kigeni kutokana na kushuka kwa mauzo ya nje.[41]

[41] Kwa mfano STABEX; tazama O.H. Kokole, 1981, kuhusu STABEX, kr. 441-59.

# 13 Maendeleo ya viwanda na kukua kwa miji, 1935-80

## Utangulizi

Sura hii inakusudia kuonyesha kuwa maendeleo ya viwanda barani Afrika yamerithi mzigo mzito kama kutokana na mahusiano yasiyolingana yaliyopo baina ya kontinenti chini ya utawala wa wakoloni na nchi tawala za Ulaya. Ni vigumu kwa sasa kubadilisha urithi huo kwa manufaa ya Afrika kwa sababu za makazi na wingi wa vikwazo ambavyo ni vya ndani na nje. Halafu, dhidi ya matokeo ya mlipuko wa miji kwa sasa, inajaribu kugusia baadhi ya sababu za *kustawi kwa viwanda* kwa Afrika siyo wa kulingana, au ni ya nadra sana. Hii ina athari zenye kuzidisha kutofautiana kwa jamii ambako ni miongoni mwa sababu za kuzuia maendeleo ya kweli ya kiuchumi.

Maswali tutakayoangalia moja baada ya jingine yatakuwa: sera za maendeleo ya viwanda Afrika kuanzia miaka ya 1935; sifa kuu za maendeleo ya viwanda kwa upande wa uzalishaji na matumizi; na jukumu lililofanywa na maendeleo ya viwanda katika ukuaji wa miji.

## Sera za Maendeleo ya Viwanda Afrika kuanzia 1930-5 hadi 1980

Mipangilio ya maendeleo ya viwanda katika Afrika, kuanzia miaka ya 1930 hadi 1980, ilifungwa na utekelezaji wa sera ya ujenzi wa viwanda ambayo kwa hali moja au nyingine imebuniwa vizuri; kwa ujumla, inasumbua kuhusu asili ya mahusiano ya uchumi wa nje na malengo ya jumla ya maendeleo ya kiuchumi ya kontinenti. Wakati mabadiliko madogo yalipotokea, baadae yamesababisha utofauti

kati ya wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni, kwa kuzingatia hali ya utata ya nchi ambazo zilikuwa huru kinadharia lakini ambazo uchumi wao ulikuwa unategemea udhibiti toka nje.

Kuhusu maendeleo ya viwanda, inaweza kuonekana toka kwenye uchambuzi wa sera na mwelekeo kwa kipindi cha kuanzia 1935 hadi 1980 kuwa viwanda vya mtindo wa kisasa katika Afrika vilianza kuendelezwa katika sekta ya madini, ikifuatiwa na viwango tofauti vya kilimo. Kazi za kontinenti zilionekana kuwa za ugavi wa bidhaa za msingi kama mali ghafi. Wakati uzalishaji unapokuwa umechelewa, wazo lilikuwa kuleta mwanga kwenye uzalishaji wa viwandani karibu na wateja wake wa Afrika.

## *Sera za kikoloni kuanzia 1930 hadi 1960-5*

Ingawa sera za uchumi za kikoloni zilionyesha sifa zinazofanana kila mahali, katika hilo ziliandaliwa ili kunyonya makoloni hasa kwa manufaa ya mataifa makubwa dhidi ya kivuli cha mfumo wa kibepari uliofanya kazi ulimwengu mzima, na kuanzisha sera maalum kwa ajili ya himaya zao, mara nyingine hata kufikia kwa wenyeji. Kwa kuwa, maendeleo ya viwanda hayakuchukua sehemu sawa na hiyo kwenye sera hizi kwa kila mfano. Licha ya tofauti na kufanana, masuala makuu matatu yanayohitaji kufikiriwa haraka: hii ni mifano ya maeneo ya vichocheo ya Uingereza, Ufaransa na Ubelgiji kwa Afrika.

### *Sera za viwanda katika makoloni ya Waingereza Afrika*

Machapisho kuhusu historia ya uchumi wa Afrika yanatoa ushahidi kidogo wa sera ya viwanda kwa mapana kuhusu sehemu ya mamlaka husika London au kwenye makoloni yao Afrika. Sera rasmi ya maendeleo inayoendeshwa katika Afrika na Wingereza inaweza kuchukuliwa, hususan kwa kipindi kabla ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, kuanzia upimaji wa maeneo au, mara nyingi, kuanzia hatua zilizochukuliwa katika mahali husika.

Kwa kuamini kama ilivyofanya kwenye biashara huria, Ofisi ya Kikoloni ya London ilikuwa ikifanya kazi kuu ya uhamasishaji wa biashara kwenye makoloni; ilishikilia kanuni kwamba jukumu kuu la serikali ilikuwa kuhakikisha uhuru wa kutembea na ulinzi wa wafanyabiashara kwenye makoloni. Kwa kuzingatia sera hii, hadi Vita Kuu ya Pili ya Dunia, viwanda vilibaki kuwa sehemu ya shughuli binafsi, bila ya mamlaka kuhusika kwenye uhamasishaji wa mtaji. Tangu utawala wa kikoloni ulipokumbwa na pigo kubwa na mgogoro wa uchumi kuanzia 1930 na

kuendelea, sera ya kutegemea ufalme ilitetewa na Mkutano wa Ufalme huko Ottawa mwaka 1932. Sera hiyo ilitumika kwenye Makoloni ya Waingereza ya Afrika kuanzia 1935 hadi 1939. Hata hivyo, haikufuatiwa na hatua rasmi zilizofanyiwa marekebisho ili kuvutia baadhi ya mtaji huria unaoongezeka kwa muda Afrika kwa ajili ya maendeleo yake ya viwanda, licha ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya mwaka 1929. Kipindi cha pili kilianza kujitokeza katika miaka ya vita kuanzia 1939 hadi 1945, na kukusanya nguvu hasa baada ya ushindi. Kipindi hiki kiliona uvamizi kwa, ambao Maendeleo ya Makoloni umepitisha Sheria ya Ustawi wa Jamii mwaka 1940.

Ilikuwa mara tu baada ya vita ambapo Uingereza ilipanga mpango wa dhati wa maendeleo ya baadae ya viwanda kwa maeneo yake ya Afrika. Wazo lilikuwa kuhamasisha mifuko ya ufalme kusaidia kwenye 'kufanya makoloni yake kuwa ya kisasa'. Kamati za uchunguzi zilianzishwa kwa sababu zilizosisitiza haja ya kuwa na vivutio rasmi kwa shughuli za viwanda katika Afrika iliyotawaliwa na Waingereza. Hata hivyo, ilikubaliwa kwa ujumla kuwa uanzishaji wa mitaji halisi ya viwanda (isipokuwa Rhodesia Kusini) ilikuwa ndoto ya mchana. Kilichohitajika ilikuwa kuanzisha viwanda vya bidhaa zilizokamilika kwa ajili ya matumizi zilizotengenezwa kwa kutegemea kiwango cha mapato na mahitaji kwa sehemu husika. Haikumaanisha kuwa viwanda vya bidhaa za kusafirisha nje ya nchi, isipokuwa kwa ajili ya bidhaa za msingi, na athari za manufaa ya Waingereza, hususan kwenye makoloni yaliyokuwa na walowezi kama Kenya na Rhodesia Kusini, zilitegemewa kuwa bora zaidi. Kwa hali hii, suala la Rhodesia Kusini, koloni la walowezi *kwa uzuri,* inaonyesha wazi. Kwa ukaribu iliyokuwa na Afrika Kusini, na kutawaliwa na vikundi vya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakihusika na uanzishaji wake, koloni hili kuanzia 1946-7 na kuendelea, lilikuwa na sera ya viwanda ambayo ilikuwa na utaratibu maalum kuhusiana na mambo yanayowahusu walowezi wa Kiingereza wanaoishi kule, ambao walikuwa na shauku ya kusawazisha athari za ushindani wa Afrika Kusini.

Kwa ujumla, sera ya viwanda katika Afrika makoloni ya Waingereza wakati wa kipindi cha ukoloni imebakia kuwa na msukumo mkubwa na mpangilio wa madaraja ambapo Afrika ilitoa mali ghafi za viwanda na kutumia idadi kubwa ya bidhaa za viwanda zilizoagizwa toka nje, zoezi zima likiendeshwa kutumia utaratibu wa kibepari kutokana na mtindo wa maisha na kuingiliwa moja kwa moja na serikali.

## *Makoloni ya Ufaransa*

Kwa miaka mingi hadi mwanzoni mwa miaka ya 1930, maendeleo ya viwanda ya makoloni na nchi zilizokuwa makoloni ya nchi nyingine katika Afrika halikuwa suala kwa viongozi. Sambamba na kanuni ya Sarraut juu ya 'maendeleo ya makoloni', viwanda lilikuwa suala la sekta binafsi pekee. Halikuongelewa hadi kufikia mgogoro wa 1930 ndipo mada ilitajwa kwenye jamii hizo. Mnamo 1934, 'Mkutano wa Uchumi wa Ufaransa' kwa mara ya kwanza ulipanga mawazo mapya maalum na kwa uwazi kuhusu suala hilo. Ikisisitiza kuhusu wajibu wa serikali katika ujenzi wa viwanda kwenye makoloni, mkutano huu ulianzisha wazo la 'kichocheo cha viwanda' kwenye makoloni. Wazo halikuwa kuanzisha au kuendeleza viwanda vya koloni ambavyo vitaleta ushindani na vile vya nchi, bali kujenga karibu na kanda za uzalishaji, viwanda 'vinavyosaidia kuongeza mali ghafi ambayo haijatumika.

Kwa wafanyabiashara, wimbi la mabadiliko ya kisasa lililounga wazo la kujenga viwanda kwenye makoloni kwa kiasi fulani lilianza kupata umaarufu (P. Bernard, L. P. Morard, Maspetiol, n.k.). Athari zake zinaweza kuonekana kwenye muswada wa Mpango wa Miaka Kumi (1942-52) ulioandaliwa na utawala wa Vichy, ambao hata ulifikiria kuanzisha utengenezaji bidha zilizokamilika kwa kiwango fulani kutoka *in situ* utengenezaji wa mali ghafi.

Mnamo 1944, mkutano wa Brazaville ulipendekeza kuwa ujenzi wa viwanda katika makoloni ya Ufaransa Barani Afrika iwe kama 'kanuni kuu, itekelezwe na makampuni binafsi.' Hata hivyo, ulitoa pendekezo kuwa uongozi wa kikoloni uchangie kwenye ufanisi wa majaribio hayo kwa kulipia gharama za viwanda mama, kusaidia viwanda muhimu ambavyo 'vinaonekana kutokuwa na uwezo wa kujiendesha', na kwa kuanzisha vituo vya majaribio na utafiti 'vitakavyosaidia wenye viwanda kusoma au udhibiti wa ubora.' Mawazo haya yameleta mafanikio kwenye mtazamo wa wafanyabiashara wa kikoloni, ambao walishikizwa kwenye uchumi wa kikoloni wa unyanganyi (*economie de traite*). Pia iliondoa wasiwasi wa ushindani na uzalishaji wa viwanda vya ndani ya nchi.

Uanzilishi wa FIDES (*fonds d'investment pour le developpement econimique et social* - Mfuko wa Vitega Uchumi kwa ajili ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii) mnamo 1947, ulikuwa na lengo la kusaidia sera maalum. Haja ya kuijenga upya nchi, ukubwa wa mahitaji ya makoloni na nchi inazozilinda - viwanda vilikuwa kiini cha uchumi wa serikali mwaka 1946 - na kipaumbele kilipewa matumizi yaliyolenga usafiri na muundo msingi dhidi ya athari za Vita Baridi miaka ya 1950.

Mnamo1960, licha ya maendeleo muhimu yakilinganishwa na hali ya mwaka 1935, maeneo yaliyotawaliwa na Ufaransa yalikuwa bado yapo nyuma mno

kimaendeleo ya viwanda na hayakuwa yameendelezwa vizuri hata kuwa wagavi wa mali ghafi za viwandani. Ukulima wa mazao ya biashara pekee ulitoa mazao machache ya aina hiyo (kahawa, kakao, karanga, pamba). Kama ilivyokuwa kwenye maeneo ya ukoloni wa Mwingereza, viwanda havikuwa shughuli muhimu za makoloni haya.

*Sera ya Ubelgiji katika Kongo*

Mnamo 1935, vile vile tangu 1908, Ubelgiji imekuwa na uaminifu kwa urithi ulioachwa na Mfalme Leopold II wa kushirikiana kila mara na wafanyabiashara wakubwa kwa ajili ya maendeleo ya Kongo.

Ilikuwa hasa kwenye sekta ya viwanda, na hususan kwenye madini, ambayo serikali iliamua kushirikiana kwa ubia na wafanyabiashara. Kuhusika kwake ambako kulikuwa kumeelezwa wazi zaidi kwenye sheria ya madini iliyopitishwa 1935, ilichukua muundo wa kuwa na idadi fulani ya hisa kwenye idadi kubwa ya kampuni za kuchimba madini. Mpango kati ya kampuni binafsi na serikali hadi 1956-7 uliacha nafasi kwa sera ya maendeleo ya viwanda iliyoongozwa kwa lengo la kutoa uhuru wa viwanda kwa makoloni.

Kati ya 1935 na 1960, hata hivyo, itakumbukwa kuwa masharti yaliyowekwa na vita vya 1939-45 yanaelekea kuendeleza kwa woga uanzilishi wa viwanda vya wenyeji vya bidhaa, kama ilivyokuwa kwenye maeneo ya Uingereza na Ufaransa. Miaka ya 1950, kwenye ushindani wa kuongezeka kwa matumizi ya Waafrika na Wazungu - kulikuwa na kati ya Wazungu 25000 na 30000 - na kuzingatia manufaa makubwa ya viwanda vya Ubelgiji, viwanda hivi vilipata kiasi kidogo cha soko dogo la ndani na kuongezeka toka asilimia 30 mwaka 1950 hadi asilimia 44 mwaka 1958. Hii iliifanya Kongo ya Wabelgiji katika siku ya uhuru kuwa moja ya makoloni kwenye kontinenti 'yaliyoendelea sana kwa viwanda.'

Kuhitimisha kuhusu suala hili la sera za viwanda za watawala wa kikoloni kati ya 1935 na 1960-5, inaweza kusemwa kuwa wote walitoa matokeo yanayofanana: kwanza, heshima kwa kanuni kuwa makoloni hayataweza kushindana na viwanda vya mataifa tawala na kuendelea kwa udhibiti wa mataifa tawala kwa usafirishaji wa mtaji na mpangilio wa kutegemea teknolojia; pili, na muhimu zaidi kuanzia wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, uanzilishi wa viwanda vyepesi ambavyo vimeweza kutimiza mahitaji ya soko la ndani kwa bidhaa za nyumbani. Hata katika hali ambapo migodi mikubwa ilikuwepo - ambayo ilikuwa katika hali tofauti, kutegemeana na makoloni husika - ilikuwa sera ya kutohamasisha

uendelezaji wa kweli wa viwanda kwenye koloni ambalo litakuwa tishio kwa ukiritimba wa nchi tawala.

Je hii humaanisha kuwa 'makubaliano ya wakoloni' yalikuwa muundo wa kudumu? Kwa kiasi fulani, kwa kuwa inaeleweka kama dalili za mgawanyo wa kimataifa wa kazi za viwandani ambazo mamlaka ya kikoloni imeziunga mkono. Suala la makoloni yaliyo nusu huria katika Afrika ni sehemu ya maendeleo haya kati ya 1935 na 1960, kutegemeana na nchi.

## Sera ya viwanda kwenye nusu-koloni; kuhusu Misri, Liberia na Afrika Kusini

Nchi chache katika Afrika ambazo zilishakuwa huru mwaka 1935 zilikuwa na uwezo kinadharia wa kuamua sera za maendeleo yake kabla ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Mbali na kipindi cha kuanzia 1935 hadi 1941, wakati Ethiopia ilipovamiwa na Italia wakati wa Mussolini, serikali za nchi hizi kila moja ilibuni sera yake yenyewe ya maendeleo ya viwanda. Kweli, athari za upendeleo wa nje, mgongano wa ndani na upendeleo huo ni baadhi ya mifano, ukubwa wa rasilimali zilizopo na mambo muhimu ambayo mabadiliko na mategemeo ya baadae ya nchi hizi yalitegemea, nafasi zote zilizotumiwa na serikali na athari za sera hizo za viwanda. Tutataja kwa kifupi mambo matatu: Misri kabla ya Al-Nasser, Liberia na Afrika Kusini: kila moja inadhihirisha kiwango fulani cha kutegemea sera yao ya viwanda katikati ya karne ya ishirini.

### *Mfano wa Misri kuanzia 1930 hadi 1952*

Miaka ya 1930, sifa mbili zimeonyesha sehemu iliyokuwa na viwanda katika uchumi wa Misri: ukweli kuwa ujenzi wa viwanda ulikwishaanza mapema na athari za kubwa za matakwa ya nje, zimehusishwa na deni la jumla la'nchi.

Katika suala la kwanza, uchunguzi wa hivi karibuni umeonyesha kuwa, kufuatia wimbi la kuiga utamaduni wa Kimagharibi lililoanzishwa na Muhammad Ali, lilianza miaka ya 1890 ambapo ujenzi wa viwanda vya kisasa ulianza. Kutokana na Mgogoro wa 1929, kupungua kwa vitega uchumi vya nje na kuanzishwa kwa sera isiyo wazi ya ulinzi ilichochea kutokea kwa sura mpya kwenye viwanda vya Misri. Kutokana na kiasi kidogo cha fedha na tekuolojia, mtaji wa wenyeji ulitumika kwenye kuzalisha bidhaa zinazoagizwa nje, kulikofanywa ili kukamilisha mahitaji ya bidhaa za watumiaji na bidhaa za kati.

Vita Kuu ya Pili ya Dunia imetilia mkazo mwelekeo huu kutokana na kushuka

ghafla kwa bidhaa zinazoingizwa toka Ulaya. Hata hivyo, kati ya 1945 na 1954, mabadiliko haya hayakuizuia nchi kuishia kutumia mtaji wa nje, angalau kwa majaribio ya upanuzi wa viwanda. Serikali ya Misri ya Mfalme Farouk, iliona kutokana na madeni yao kwa wageni, ilibidi kufanya biashara kwa makini wakati wa kuandaa na kufuatilia sera ya viwanda ambayo ilikuwa inawajali watu wa daraja la kati. Kwa kuwa inaeleweka kuwa suala la makoloni ya Wazungu na sera hiyo ya viwanda imekuwa tishio kwa matakwa ya mabepari wa Ulaya, viwanda mbadala vya bidhaa zinazoagizwa nje vingeshaanzishwa nchini Misri kati ya 1930 na 1954. Sera iliyokusudiwa iliendelezwa na Rais al-Naser baada ya 1956 kuonyesha mwisho wa sera ya viwanda ya Misri ya wakati wa Farouk.

## *Liberia*

Jamhuri ya zamani zaidi katika Afrika ilikuwa katika kipindi cha matatizo ya kifedha kuanzia mwanzoni mwa karne na kufikia 1935 iliharibiwa na kuishiwa kabisa, kiasi kwamba mahakama ya nchi za Ulaya iliamua kuiweka chini ya udhamini wa Shirikisho la Mataifa. Baada ya 1945, chini ya rais William Tubman, uwekezaji binafsi, hasa kwa mtaji kutoka Marekani, ulianza kushamiri tena. Ulielekezwa kwenye uchimbaji wa madini hususan katika madini ya chuma ya daraja la juu kutoka mlima Nimba na madini ya boksiti, na vilitolewa vivutio vya kutosha na sera kwa kutoa upendeleo wa kila aina makampuni ya kigeni.

Sera hii ya viwanda kwa muda mrefu ilibakia kuwa na vikwazo viwili: kwanza, haja ya kuanzisha kiasi kidogo cha muundo msingi unaotakiwa kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya viwanda; na, pili, haja ya kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zilizotengenezwa za watumiaji kwenye jamii yenye asili ya Waafrika Wamarekani wanaoishi kwenye eneo hilo. Mwanzoni mwa miaka ya 1960, Liberia ilianza ujenzi wa viwanda vidogo vya bidhaa za watumiaji kama vile utengenezaji matofali, viwanda vya sabuni, viwanda vya bia, na kadhalika, chini ya udhibiti wa hali ya juu wa wenyeji wa daraja la kati, ambao hawakuwa na uwezo wa kudhibiti migodi yote.

## *Afrika Kusini*

Tofauti na Liberia, na kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko Misri kwa kutegemea utajiri wake mkubwa sana wa madini, Afrika Kusini mnamo 1935 ilikuwa makini 'kutumia nafasi ya kudorora kwa uchumi mwaka 1929 kujiimarisha na msingi thabiti wa

viwanda. Matumizi ya sera ya siku nyingi ya ubaguzi wa ajira za viwandani ilikuwa sababu ya ziada ambayo haikuacha kuhusishwa na matokeo yaliyopatikana.

Mapinduzi kwenye sekta ya madini ambayo yalianza miaka ya 1860 yaliwezesha kuanzia siku za mwanzo kujenga muundo msingi wa mwanzo kabla ya miaka ya 1920. Licha ya kushuka kwa uzalishaji wa madini kati ya mwisho wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na 1921-2, maendeleo ya viwanda yaliendelea kuongezeka kama kutokana na uchimbaji wa migodi ya dhahabu. Mwishoni mwa miaka ya 1920, sera mpya ya viwanda ilianza kutumika; katika jaribio la kudhibiti utegemezi wa uzalishaji usio halali wa vito vya thamani, kulikuwa na wimbi la kubadili sekta za viwanda. Uzorotaji Mkuu wa uchumi umesababisha kuendeleza mwelekeo huu, ikabidi serikali kujihusisha. Hadi Vita Kuu ya Pili ya Dunia, viwanda viliendelea kukua na viliweza kirahisi kujirekebisha na upungufu wa bidhaa zilizoagizwa toka nje.

Hata hivyo, ingawa uwekezaji wa wenyeji ulichochewa - hisa zake za madini zilipanda toka asilimia 15 hadi 40 - athari za kifedha za riba ya nje (hususan Uingereza, na pia Marekani toka miaka ya 1920 na kuendelea) ilikuwa yenye maana sana mwaka 1945. Katika kipindi cha baada ya vita, kulikuwa na maendeleo zaidi kwenye kampuni zilizoanzishwa kwa mtaji toka nje dhidi ya viwanda vinavyokua haraka.

Wakati viwanda vya nchi vilipopata msukumo wa kuzalisha bidhaa badala ya kuagiza nje kwa ajili ya mahitaji ya watumiaji weusi, pia ilikuwa kwenye muktadha mpana zaidi, viwanda vinavyotengeneza bidhaa za kati, na hata bidhaa mtaji, kwa msaada wa mtaji toka nje, ambao ulikuwa na nia ya kutumia mali ghafi ya ndani na kuepuka sera ya ushuru wa forodha ambao umeendelea kuzidi kuwa wa kujilinda tangu miaka ya1930.

Kutokana na hayo, kufikia mwaka 1945, Afrika Kusini ilitokea kuwa inaongoza kwa viwanda kwenye kontinenti, kwa kutokana na sera yake ya ukandamizaji na pia kwa kutumia maliasili yake. Hata hivyo, hali hii, ambayo imerudi nyuma hadi miaka ya 1930, ilikuwa matokeo ya sera muhimu ya viwanda, inayohusu kuanzishwa kwa viwanda vya aina mbali mbali ndani ya nchi. Sera hiyo iliendeshwa na mtaji toka nje, katika baadhi yao kwa ubia na mtaji wa ndani, ingawa siyo zote.

Ingawa uhusiano na sera kama hiyo, maendeleo ya viwanda katika Afrika huru yamezingatia mtindo unaofanana na historia zao.

## 'Uzalendo katika maendeleo ya viwanda' na sera za viwanda za mataifa huru ya Kiafrika

## *Mtazamo wa jumla*

Kinyume na sera za viwanda za utawala wa kikoloni, 'waanzilishi wa mapambano ya uhuru Afrika' wameelekeza mapambano yao kwenye unyonyaji wa watawala wa kikoloni, hususan baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Hata hivyo, mwanzoni mwa miaka ya 1950, wazo kuwa maendeleo ya kiucumi ya makoloni pia yamelazimisha 'maendeleo ya viwanda ya haraka' pia lilipata msukumo. Wakati huo, kila mmoja amegundua kuwa itachukua muda kutimiza lengo la ujenzi wa viwanda na kuwa msaada wa nchi zilizozitawala na mtaji toka nje pia utahitajika. Hata hivyo, wazo hilo lilikuja kuchanganywa na wazo jipya, hasa wakati ambapo mahitaji ya kisiasa yalianza kupata mafanikio. Hii ilikuwa kwamba maendeleo ya viwanda hayakuwa moja ya kazi za kawaida za serikali, bali kanuni za nchi huru na uhuru halisi wa taifa, kama Kwame Nkrumah alivyokwisha sema mwaka 1945.

Hii ilikuwa ndiyo msingi wa 'ujenzi wa viwanda kizalendo' katika Afrika ambao umeendelezwa na uhuru wa kisiasa wa Afrika. Kila mfano, umehusisha sera ya viwanda iliyo wazi kuliko wakati wa utawala wa kikoloni au ukoloni mamboleo. Lakini zaidi ya uzoefu na matamko ya dhamira, sera za viwanda za mataifa huru zinagawanyika katika makundi makubwa mawili, ukiacha suala pekee la Afrika Kusini, hasa baada ya 1948. Kwa upande mmoja, kuliwepo 'sera zisizo za kibepari' na, kwa upande mwingine, sera za nchi zenye uchumi wa 'biashara huria'.

## *Sera za serikali zenye kufuata 'uchumi usio wa kibepari'*

Nkrumah wa Ghana na Boumedienne wa Algeria walichagua sera ya viwanda katika muundo wa 'kisoshalisti'.

Mnamo 1957, Ghana iliingia baada ya ukoloni na uchumi uliokuwa katika hali isiyokamilika. Ingawa alikuwa anaiongoza nchi yake tangu 1951, ilimbidi Kwame Nkrumah kutoa nafasi kwa kuleta usawa wa madaraka ndani ya nchi na hakuanza kuweka mawazo yake kwenye maendeleo ya viwanda kuanza kutumika mpaka baada ya 1959, utekelezaji wa Mpango wa Ghana wa Miaka Mitano. Katika wazo hili, lengo kuu lilikuwa kufanya 'mapinduzi ya viwanda' ambayo yatawezesha kuachana na ubepari; mapinduzi haya yamesababisha ujenzi ulioenea wa viwanda nchini ulioendeshwa hasa na serikali kama mmiliki wa njia muhimu za uzalishaji kwenye viwanda vya ndani ya nchi. Sekta binafsi iliweza kuendelea kuwepo; lakini juhudi za serikali, baadae zitahakikisha kuwa sekta binafsi inachukua heshima ya pekee.

Nkrumah pia ametetea wazo la mafunzo ya utaalamu kwa utaratibu maalum na kupanga mbinu za kuendeleza viwanda. Kipindi cha Pili cha Mpango wa Miaka Mitano (1959-63) na Kipindi cha Kwanza cha Mpango wa Miaka Saba (1964-70) vinaonyesha wazi mbinu za viwanda, kwenye hiyo asilimia 72 ya bajeti ya mikopo mwaka 1959-63 na asilimia 61 mwaka 1964-70 zilitengwa kwa ajili ya viwanda tofauti na asilimia 38 mwaka 1951-7 (kipindi cha Kwanza cha Mpango wa Maendeleo). Kufikia 1965, asilimia 10-12 ya uzalishaji wote wa viwandani ilikuwa ikitoka kwenye sekta binafsi ambayo haikuwepo kabla ya 1961.

Kuanguka kwa Nkrumah mwaka 1966 na mabadiliko yaliyotokea ya utawala na uchaguzi wa njia za uchumi kumeleta uwezekano wa kuendelea na sera hii, ambayo ilichukua zaidi mfano wake katikka mawazo ya Kwame Nkruma ya kutopenda ubepari na siasa kali ya utaifa.

Algeria ilitokea katika kipindi cha ukoloni ikiwa na sekta ya viwanda ambayo ilizalisha kiasi kidogo sana cha Jumla ya pato la Taifa. Si matumizi ya sera ya uagizaji vitu toka nje bila ya udhibiti wa serikali, ambayo imeanza kutumika tangu 1943-5, wala utekelezaji wa 'Mpango wa Constantine' wa kujichumi zaidi, ambao kwenye sekta ya viwanda, ilikuwa ikisaidia katika kuendeleza sera ya matumizi ya mafuta, haikuwa na athari muhimu kwenye maendeleo ya viwanda. Sekta ya viwanda bado ilikuwa duni sana mwaka 1962 na kwa kiasi kikubwa chini ya udhibiti wa Ufaransa, licha ya Mkataba wa Evi.

Kabla ya uhuru, FLN ilikuwa tayari inaendeleza wazo lenye kutabiri 'maendeleo ya viwanda kitaifa'. G. D. de Bernis anakumbushia hili kwa vizuri sana anaposema kuwa 'Maendeleo ya viwanda yangefanikiwa kwa kuanzisha vyama vya ushirika vinavyofanya kazi kwa ajili ya viwanda vikubwa'. Hii ina maana kuwa serikali ilitakiwa kuchukua jukumu kubwa zaidi kwa makusudi; modeli ya kisoshalisti ilikuwa itumiwe kwa kuanzisha ushirika; na viwanda vikubwa ilikuwa vianzishwe. Huu ulikuwa msukumo mkuu wa kanuni ambayo Algeria ilitakiwa kuanza kuitumia, hususan kuanzia wakati wa Boumedienne na kuendelea.

Nchi ilikuwa na bahati ya kuwa na kiasi kikubwa cha rasilimali: ilikuwa na chuma na, zaidi ya yote, mafuta, na ilikuwa ni wakati wa kupanda kwa bei ya mafuta ambako kungetoa rasilimali za kuanza sera rasmi. Katika msingi wa haya mawazo ya FLN, njia kuu tatu zilijitokeza, hasa baada ya 1969: uwekezaji wa rasilimali za serikali, kwa kutaifisha au bila kutaifisha na kuzifanya za serikali, kwenye makampuni makubwa (mara nyingi miradi mama) yenye athari kubwa katika kurekebisha uchumi wa viwanda; matumizi makubwa ya rasilimali na kutoa

madaraka kwa viwanda katika jitihada za kusaidia muingiliano wa kanda ambazo ziliachwa kwenye vyombo vyao vyenyewe wakati wa ukoloni, na baadae kumaliza tofauti za kanda kwa kuwa na viwanda.

Lakini sera ya upendeleo kwa 'maendeleo ya viwanda' haikuelekeza msaada wa serikali kwa sekta binafsi, ambayo ilirekebishwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za watumiaji. Huu ulikuwa msukumo mkubwa wa mwisho wa sera hii ya maendeleo ya viwanda ambayo ilipitishwa, kwa kufanyiwa marekebisho ya hapa na pale bila kujali vikomo, baada ya kifo cha Houari Boumedienne.

Kwa swali kama iwapo masuala ya Ghana na Algeria ni mahsusi, linaweza kujibiwa kuwa pengine yote siyo mahsusi, hasa kwa ajili ya jinsi ya 'uendelezaji wa viwanda', wazo la kupanga bila kusaidiwa na hotuba ya kutopenda ubepari na badala yake kupenda ujamaa na pia nafasi muhimu iliyochukuliwa na sekta ya umma kwenye viwanda zilitakiwa kuwepo kwenye sera za mataifa mengi mapya yenye uchumi wa 'biashara huria'.

## Sera za nchi zinazochagua uchumi wa 'biashara huria': Cote d'Ivoire na Nigeria

Licha ya msingi duni wa viwanda wakati wa uhuru, na ingawa miaka ya 1955-60 ilikuwa miongoni mwa vipindi vigumu vya Uzalendo wa Afrika, nchi kadhaa za Afrika zilishindwa kuwa na viwanda vichache kufuatana na malengo ya ubepari wa kimataifa tangu wakati wa ukoloni. Zilichagua ubepari wa biashara huria kwenye uchumi; maendeleo yake ilielekeza kwenye uchumi wa viwanda uliotakiwa kulingana na uwezo wa soko. Lakini uchambuzi wa sera zao binafsi unaonyesha idadi kubwa ya tofauti ndogo ndogo na hata tofauti, baadhi zimeonyeshwa katika masuala ya Cote d'Ivoire na Nigeria.

Mnamo 1960, Cote D'Ivoire, nchi ya kilimo ambapo mtindo wa kikoloni wa uchumi wa biashara ulishamiri kama ulivyofanya kwenye nchi jirani ya Ghana, ilikuwa na viwanda vichache sana, licha ya kulingana kwa biashara ya nje. Mwaka 1959, uamuzi kwa makusudi ulichukuliwa kubaki katika mfumo wa uchumi wa soko huria. Katika suala la viwanda, wakati ilipotambuliwa kuwa kulikuwa na haja ya maendeleo yaliyo wazi, iliamua kuacha mzigo huo uanzishwe taratibu na sekta binafsi na juu ya yote kwa kuchukua mtaji toka nje. Hii ilikuwa kwenye sheria ya mwanzo ya uwekezaji kwenye kontinenti kutoa masharti nafuu sana kwa makampuni ya kigeni. (cf. sheria ya 3 September 1959), katika njia ya kusamehewa

kodi mbali mbali, kuruhusiwa kuondosha faida nchini, kuhakikishiwa kutotaifishiwa mali au mahitaji ya jamii, na vyombo vingine.

Kutegemeana na kiwango cha chini cha uthabiti wa viwanda pembeni - kulikuwepo utajiri mdogo unaoonekana na utaalamu ulikuwa wa kiwango cha chini - na ili kuheshimu mkakati wa viwanda uliotumiwa kabla ya 1960, mkazo uliwekwa katika mfano wa kwanza kwenye sera ya kutengeneza bidhaa zitakazochukua nafasi ya bidhaa zilizokuwa zikiagizwa toka nje. Serikali ilihusika zaidi na sera zake za kubadili na kuongeza uzalishaji mazao ya kilimo (hususan bidhaa zitokanazo na kilimo), na iliingilia kwa shida sekta hii. Hata hivyo, Mohamed Diawara, aliyekuwa waziri wa mipango na viwanda, aligundua mwaka 1972, kuwa sera hii iliishia 'kulinda faida kwa wafanyabiashara, lakini siyo mara zote kwa jumuiya'. Vivutio vilivyotolewa kwa usafirishaji nje bidhaa na makampuni yaliyoweza kufaidika kutokana na 'wafanyakazi', lakini sera ya kuendeleza uwekezaji wa ndani kwenye eneo hili la biashara kuanzia 1970 na kuendelea, vilikuwa na malengo ya kutoa msukumo mpya kwa maendeleo ya viwanda.

Mwisho, msukumo mkubwa zaidi wa tatu uliojitokeza enzi za Mpango wa Miaka Mitano 1976-80 ulielekezwa kwenye kuongeza rasilimali za ndani hasa kwa kutumia makampuni ya serikali yanayotengeneza mafuta ya mawese, sukari na bidhaa nyingine, katika nadharia ya 'ubepari wa serikali' katika mpito wa kuelekea kwenye 'ubepari wa kawaida'. Kabla ya kutokea daraja la kati la raia, serikali ingehakikisha kuwa nchi inashiriki kwenye uwekezaji viwandani na ingeuza hisa zake kwa wananchi wenye uwezo wa kuendeleza juhudi hizo. Kampuni ya serikali ilidhamiria kutekeleza wajibu huo kama hatua za muda.

Pamoja na sera hii ya Wananchi wa Ivory Coast ambayo baadhi ya wachambuzi wanaisifu kuwa 'maajabu ya Waivory' au kukosolewa sana kwa kupachikwa jina kama 'kukua bila maendeleo', kulikuwapo suala la Nigeria. Nchini Nigeria, kulikuwa na msimamo unaofanana na huu kiasi fulani wa biashara huria kwenye sera ya mabadiliko na kutoa madaraka ya uzalishaji viwandani, na wajibu mkubwa kwa sekta binafsi, hasa baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kuanzia 1967 hadi 1970. Kweli, mnamo 1960, viwanda vilikuwa vichache kwenye uchumi wa Nigeria na vilipata kiasi kidogo cha sehemu ya mpango wa uwekezaji (asilimia 7.66 ya huo uwekezaji kwenye Mpango wa Miaka Mitano wa 1955-60). Kati ya 1960 na 1967, ilianzisha pamoja na kujichagulia biashara huria na njia za kupata misaada ya mtaji toka nje. Serikali ya shirikisho iliingilia kidogo, isipokuwa ilitoa vivutio kwa viwanda vya mafuta. Mgogoro wa kisiasa wa 1966 na vita vya wenyewe

kwa wenyewe vya 1967-70 vilipunguza uwezo wa serikali ya shirikisho kuendelea kufanya mabadiliko.

Mwisho wa vita vya wenyewe kwa wenyewe na haja ya kujenga tena uchumi baada ya kuvurugwa na mgogoro huo, uliokumbana na kupanda bei ya mafuta kati ya 1973 na 1980 na kusababisha kuongezeka kwa mapato ya serikali ya shirikisho na ya taifa, kulitoa msingi kwa ajili ya sera ya muda mrefu ya maendeleo ya viwanda. Hii iligawanywa katika mada kuu tatu: uchaguzi wa uhuru wa kuingiza bidhaa za viwandani ambazo, kwa kutunga sheria ya kuagiza mali ghafi na mashine, kumerahisisha kusaidia na kulinda viwanda vinavyotengeneza bidhaa mbadala za viwandani; msaada wa kiasi au usio wa moja kwa moja unaotolewa na serikali kwa ajili ya viwanda vya bidhaa mtaji, kwa kutegemea teknolojia kutatua matatizo ya maendeleo yaliyofanywa na mbadala wa kuagiza bidhaa; na mwisho, kwa wakati huo huo kama ilivyotoa vivutio kwa ajili ya kuandaa mali ghafi za ndani, zilizopewa jina sera 'ya unigeria' iliwapa raia kipaumbele kwenye sekta mbali mbali za biashara na mkataba wa serikali, na ikatunga sheria kwa ajili ya kuanzisha ubia na mtaji toka nje. Nigeria ilikuwa iwe 'inaongoza' kwenye viwanda vya Afrika.

Kwa ujumla, ikiwa serikali zenyewe zilitamka kuwa za 'kisoshalisti' au katika uchumi wa 'biashara huria', sera za maendeleo ya viwanda katika Afrika huru zinaonyesha sifa moja kwa pamoja, kuwa zote zilipanga kuendeleza mapambano halisi ya kujikwamua dhidi ya maendeleo duni ya viwanda wakati wa ukoloni ili kuhakikisha kiwango cha kujitosheleza kwa viwanda. Lakini Afrika miaka ya 1960, 1970 na 1980 ilikuwa ya wakati wa kuanzia nyuma mno na ilitwishwa mizigo mbali mbali ya mapungufu, na zaidi ya yote kulikuwa na mikabala iliyojitokeza nje ya kontinenti ili kuendeleza au kuhifadhi mgawanyo wa kazi wa kimataifa ambao ulianzishwa kuhusu Afrika, hususan chini ya kivuli cha miaka ya mgogoro wa uchumi kuanzia 1930 hadi 1935 na kuanzia 1973 hadi 1980. Uchambuzi wa sifa za viwanda vya Afrika kuanzia 1935 unadhihirisha udhaifu wa muundo wake na kutokuwa salama, licha ya juhudi za kipindi baada ya ukoloni.

## Sifa za jumla za maendeleo ya viwanda katika Afrika, 1935-80

Maendeleo ya uzalishaji viwandani na ya mchango wa viwanda kwenye Zao Ghafi la Ndani ya nchi za kiafrika yanaonyesha wazi kabisa vipindi viwili: cha kwanza, kuanzia 1935 hadi 1960-5, na cha pili, kuanzia 1960 hadi 1980. Ili kuangalia kila kipindi kwa undani zaidi, inabidi zielezwe sababu maalum za mgogoro wa muundo

wa ndani na matokeo yaliyopatikana na kanda ndogo au sera za viwanda za maeneo yaliyokwishatajwa.

## Hatua za mwanzo za maendeleo ya viwanda kabla ya 1960-5

Mabadiliko katika uzalishaji wa viwanda, kiwango cha maendeleo ya viwanda au mchango wa viwanda kwenye uchumi wa Afrika kabla ya 1960-5, ujenzi wa viwanda vya kisasa kwa kontinenti umeanza kwa kasi ndogo sana.

### *Maendeleo ya uzalishaji na kiwango cha maendeleo ya viwanda*

Data ya takwimu kwa nchi au eneo la koloni kwa kipindi cha 1935-60 zinatofautiana, mara nyingine zisizoaminika, na mara kwa mara hatua kwa hatua. Kwa kuwa si rahisi kupata picha ya jumla kwa muda wote ya kiwango cha uzalishaji na kukua kwa viwanda kwa kontinenti husika. Kwa mara ya kwanza, hata hivyo, hesabu zilizopo zinaonyesha maendeleo mazuri ya uzalishaji viwandani, na kipindi baada ya vita kinaonyesha maendeleo ya kweli. Chati 13.1 inaonyesha nchi tatu ambazo 'zilikwishaendelea kwa viwanda' wakati huo; inaonyesha maendeleo ya kweli mwaka 1960, wakati miaka ya 1950 kilikuwa kipindi ambapo uzalishaji uliongezeka mara mbili.

CHATI 13.1 *Vielelezo vya uzalishaji viwandani kwa nchi fulani, 1939-59/60*

| *Nchi* | *1939* | *1945* | *1950* | *1954* | *1960* |
|---|---|---|---|---|---|
| Misri | 49 | 67 | 98 | 106 | 161 |
| Kongo ya Wabelgiji | 30 | 58 | 100 | 190 | 235 |
| Nigeria | - | - | 100 | 147 | 278 |
| Afrika Kusini | - | 35 | - | 57 | 71 |

KUMBUKA: Msingi seti 100 mwaka 1950-2; kwa Afrika Kusini, msingi wa seti 100 mwaka 1963, na vielelezo ni kwa miaka ya 1948, 1953 na 1958.

*Vyanzo:* S. Radwan, 1981, uk. 200; J. L. Lacroix, 1966, kur 295-6; U. E. Okeke, 1985, kur. 37-7 (imechapwa tena kwa idhini ya *African Review of Business and Technology,* iliyojulikana kama *African Technical Review*) na United Nations, 1970.

Hata hivyo, namba hizi ni za kutilia mashaka katika kipindi kamili, zinahusiana na viwanda kwa kipimo cha wastani. Isipokuwa Afrika Kusini (kwa idadi ya zaidi ya paundi milioni 75 tayari hadi 1938, ukitoa sekta ya madini), thamani ya uzalishaji viwandani kwenye nchi nyingi mwaka 1960 kwa nadra sana ilizidi US $ milioni 200 (Misri). Nigeria ilikuwa katika $ milioni 160, Kongo ya Wabelgiji $ milioni 128, na $ milioni 120 kwa Rhodesia ya Kusini, $ milioni 94.7 Ghana na $ milioni 140 kwa nchi zote za Afrika zilizotawaliwa na Ufaransa (Nchi za Afrika Magharibi na Afrika ya Kati zilizotawaliwa na Ufaransa, Madagascar, Kameruni na Togo). Maghreb kiwango hakikuwa cha juu sana, hata ukihesabu uzalishaji madini.

Viwango vya kukua kwa viwanda, havilingani toka sekta moja hadi nyingine (madini, bidhaa za watumiaji, bidhaa ghafi), vinaonyesha kuwa sera za viwanda zilizotekelezwa hazikuwa na matokeo mazuri. Mbali na madini, sekta nyingine zilikuwa duni sana (kati ya asilimia 0.5 na 3 kutegemeana na nchi na mwaka) na katika mambo fulani kulikuwepo vipindi virefu vya kudorora (kwa mfano, huko Afrika ya Kaskazini kati ya 1948 na 1954).

### *Mchango wa viwanda katika uchumi wa Afrika*

Sehemu iliyochukuliwa na viwanda ni ya kushawishi zaidi kwenye kiwango cha maendeleo ya viwanda katika kontinenti wakati huo.

Licha ya tofauti katika kukadiria, uchunguzi wote uliofanyika unakubali kuwa shughuli za viwanda bado zilikuwa na nafasi ndogo Afrika mwishoni mwa miaka ya 1950. Ukweli, kwa kiasi kikubwa, chati 13.2 inaonyesha, ilikuwa ndogo kwenye nchi nyingi (asilimia 2.6 huko Dahomey, asilimia 3 huko Tanganyika, asilimia 4

CHATI: 13.2 *Asilimia ya mchango wa viwanda kwenye mapato ya taifa ya nchi za Afrika zilizochaguliwa, 1956-60*

| *Mwaka* | *Kongo ya Wabelgiji* | *FWA* | *Nigeria* | *Rhodesia-Nyasaland** |
|---|---|---|---|---|
| 1956 | 8.0* | 2.0 | 2.0 | 11.0 |
| 1960 | 14.0 | 5.5 | 4.5 | 16.0 |

* Hesabu ya 1958

** Rhodesia Kusini pekee kwa mwaka 1960.

*Vyanzo:* United Nations, 1959, uk. 15; P. Kilby, 1975, uk. 472; United Nations, 1970.

huko Togo). Ilikuwa hasa kilimo mara nyingi kutumia taratibu za mwanzo, ambazo zilikuwa nguvu za uendeshaji uchumi kulipokuwa hakuna hata mgodi mmoja. Baadhi ya waandishi wameamua kuhusisha hali hii na idadi kubwa ya walowezi wa Ulaya. Ukweli, hii siyo sahihi. Huko Maghreb, kwa mfano, licha ya kuanzishwa na kuwepo kwa muda mrefu kwa jamii ya walowezi wa Ufaransa, mchango wa viwanda kwenye Zao Ghafi la Ndani la sehemu hiyo ya kontinenti haikuwa ya kutosha tena. Huko Algeria, mwaka 1962 - siku ya uhuru - viwanda vilichangia asilimia 9.36 ya Zao Ghafi la Ndani (asilimia 23.8 ikijumlishwa na madini). Viwanda vilikuwa na umuhimu mdogo kwenye uchumi wa kikoloni isipokuwa katika sura yake ya mwanzo, kama vile madini, na iliajiri wafanyakazi wachache, kama tutakavyoona. Hii haikuwa kwa sababu ya kwamba mbinu za uzalishaji zilirahisishwa kuliko kwingine, lakini ilikuwa dalili ya kuwa na viwanda vichache.

Haya yote yanaelezea mchango wa Afrika kwenye uzalishaji duniani - isipokuwa kwa mali ghafi - na kwenye matumizi ya bidhaa zilizotengenezwa.

## *Nafasi ya Afrika kwenye uzalishaji na matumizi duniani*

Picha ya Afrika kama mgavi mkuu wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda halikuwa jambo jipya mwaka 1935 - kinyume kabisa, picha hiyo tayari inaelezewa tangu siku nyingi nyuma. Nafasi iliyochukuliwa na Afrika Kusini kwenye uzalishaji wa vito vya thamani duniani, ubora uliohakikishwa wa migodi ya chuma huko Liberia, ikiwa na asilimia 65 ya chuma, uzalishaji wa Bouxite nchini Guinea na shaba huko Kongo au Rhodesia Kaskazini, hata kabla ya nchi hizo kuwa huru, zote zimeweka imani kwa wazo hilo kwa kipindi kuanzia 1935 hadi 1965.

Hata hivyo, mbali na mali ghafi chache za madini - vito vya thamani Afrika Kusini, Phosphate huko Moroko na madini yasiyokuwa na chuma kwingine - kulikuwa na shughuli chache za maendeleo Afrika ili kuchukua nafasi ya mbele kwenye sekta hii. Wakati utafutaji madini ulipokuwa unaendelea baada ya 1945, nchi za wakoloni au nchi zenye uwezo mkubwa (kama vile Uingereza huko Misri na Libya, Ufaransa huko Misri, au Marekani huko Liberia) ziliweka ukiritimba kwenye uchimbaji wa madini hayo, kwa ajili ya kampuni za nchi zao hadi kufikia kati kati ya miaka ya 1950.

Uzalishaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda kwa kiasi kikubwa ulitegemea upendeleo na mikakati iliyopangwa na nchi tawala ambayo inaendesha maendeleo yake. Kwa mfano, uchimbaji wa mafuta huko Afrika Kaskazini (Misri, Algeria na Moroko) ulipanda toka mapipa milioni 7 mwaka 1940 (sehemu kubwa toka Misri)

hadi mapipa milioni 17 mwaka 1950 (ambapo kati ya hayo Misri ilitoa asilimia 94) na mapipa milioni 91 mwaka 1960 (asilimia 72.5 toka Algeria na asilimia 26.4 toka Misri), inayowakilisha chini ya asilimia 1 ya uzalishaji wa Mashariki ya Kati. Huko Algeria, utafutaji wa mafuta umeanza rasmi baada ya 1957 (fr. milioni 541.6 zilitumika katika kipindi cha miaka kuanzia 1952 hadi 1956 ikilinganishwa na fr. milioni 679 mwaka 1958 na fr. milioni 917 mwaka 1962).

Hivyo Afrika imechukua nafasi ya uzalishaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda ambayo hailingani na uwezo wake wa maliasili. Lakini zaidi ya hayo, katika viwanda, mchango wa Afrika katika uzalishaji mali duniani ni mdogo sana. Hii inaelezwa na uagizaji mkubwa toka nje bidhaa zilizotengenezwa viwandani kwa nchi za Afrika. Mchanganuo wa bidhaa za viwandani zinazoagizwa toka nje unaonyesha kwa kiasi gani nchi nyingi zinategemea nchi nyingine kwa ajili ya bidhaa za watumiaji. Katika suala la bidhaa mtaji, ilikuwa inategemea nchi nyingine kwa asilimia 100. Hali hii haikubadilika hadi kati ya 1960 na 1965, kutegemeana na nchi.

Chati 13.3 *Asilimia ya mchanganuo wa uagizaji nje bidhaa za viwandani kwa Misri, 1945-60*

| | 1945 | 1952 | 1957 | 1960 |
|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za watumiaji | 43.3 | 34.9 | 54.3 | 22.1 |
| Bidhaa ghafi | 40.7 | 36.7 | 27.7 | 44.3 |
| Bidhaa mtaji | 16.0 | 28.4 | 18.0 | 33.6 |

*Chanzo:* S. Radwan, 1981, uk. 216

Enzi ya baada ya ukoloni katika Afrika ilianza chini ya vikwazo vikubwa: watu walizoea kutumia bidhaa zilizotengenezwa viwandani wakati uchumi wa Afrika ulikuwa bado kwenye enzi ya kabla ya kuwa na viwanda. Ilikuwa, kama tulivyoona hapo juu, ni changamoto ambayo ilitakiwa kuchukuliwa na 'waanzilishi wa mapambano ya uhuru'.

# Maendeleo baada ya Ukoloni, 1960/65-80

## *Maendeleo kwenye uzalishaji na matumizi*

Iwapo mtu ataangalia uzalishaji wa mali ghafi za viwanda au bidhaa zilizozalishwa viwandani, itakuwa hakuna shaka kuwa viwanda katika Afrika vimepata maendeleo kwa idadi kati ya 1960 na 1980. Hata hivyo, maendeleo haya hayakuwa sawa kwa kuangalia muda na nafasi (Chati 13.4). Wakati fulani kulikuwa na ongezeko la haraka katika uzalishaji viwandani (kwa mfano, ilifikia asilimia 400 katika Misri kati ya 1956 na 1971) na kuleta sifa kuu mbili. Kwa upande mmoja, kulikuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mali ghafi za viwanda - za mafuta, lakini pia mawe yenye madini ya thamani na metali. Kwa upande mwingine, kulikuwa na ongezeko kubwa la viwanda vya kutengeneza bidhaa za watumiaji ili kutosheleza mahitaji ya ndani, ikiwa pia kwa lengo la kupata masoko ya nje kwa kupitia biashara ya ndani ya Afrika na kwa kusafirisha katika nchi zenye viwanda vingi, hususan katika suala la bidhaa za kilimo toka kwenye nchi kama Cote d'Ivoire.

Chati 13.4 *Vielelezo vya Usafirishaji nje wa bidhaa za viwandani za Afrika, 1970-8*

| *Maeneo ya kijiografia na kibiashara* | *1970* | *1973* | *1977* | *1978* |
|---|---|---|---|---|
| Afrika Kaskazini | 39 | 65 | 128 | 163 |
| ambayo Maghreb | 26 | 58 | 140 | 183 |
| Wanachama wa ECOWAS | 46 | 78 | - | - |
| ambao Cote d'Ivoire | 25 | 56 | 132 | 122 |
| Afrika Kusini | 49 | 85 | 157 | - |

Tanbihi: Msingi seti 100 kwa 1976.

*Chanzo:* UNCTAD, 1980, kur. 108-29.


Hata hivyo, wakati ongezeko la uzalishaji lilipokuwa dogo katika hali ya uchanga katika nchi nyingi, lilikuwa tayari limeshaanza kwenye nchi nyingine kama Misri, Afrika Kusini na Algeria. Hata hivyo, viwanda hivi vya Afrika vilizalisha sehemu ndogo ya matumizi ya bidhaaa za viwandani, ambayo ilikuwa inakua kwa haraka sana: mwaka 1978, uagizaji bidhaa za viwandani toka nje ulikuwa zaidi ya asilimia 60 ya jumla ya uagizaji bidhaa toka nje kwa nchi nyingi kwenye kontinenti (pamoja na Afrika Kusini), wakati usafirishaji nje bidhaa za viwandani kwa ujumla ulikuwa chini ya asilimia 10 ya mahuruji yote.

Idadi ya mahuruji siyo kwa bidhaa za nishati pekee bali kama matokeo ya mahitaji yaliyoanzishwa ya bidhaa zilizokamilika na zilizokamilika nusu nusu. Kwa hiyo, kulikuwepo maendeleo, ingawa haya yakilinganishwa na kipindi cha mwanzo cha uendelezaji wa viwanda kuliko kulinganisha na mahitaji yanayoendelea kuongezeka. Kwa kuwa viwanda vya bidhaa mtaji ilikuwa sifa ya nadra au haikuwepo kwenye baadhi ya nchi, wazo la kitu gani kinaleta mafanikio kwenye sekta hii linatakiwa kupambanuliwa kwa kina. Hata hivyo, viwanda havikuweza tena kusemwa kuwa na mchango mdogo kwenye uchumi wa nchi.

## Mchango wa viwanda katika uchumi baada ya ukoloni

Licha ya kasoro zinazojitokeza kwenye data ya takwimu katika nchi nyingi, inaeleweka maeneo sahihi yaliyoshikwa na sekta ya ufundi stadi na viwanda vya kisasa, mchango wa viwanda kwa Jumla ya Zao la Taifa umeongezeka kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1950. Kwenye yaliyokuwa makoloni ya nchi za Ulaya - katika mifano ambapo hatua za uthabiti wa kisiasa zimeruhusu - kipindi cha baada ya ukoloni hata hivyo kimewezesha kupiga hatua ya maendeleo, na hapo ikawezesha idadi fulani ya viwanda vidogo kuingizwa kwenye soko la dunia.

Hata hivyo, mbali na ukweli kwamba kasi ilitofautiana kati ya nchi na nchi (Chati 13.6), hii mara nyingi ilikuwa matokeo ya kukua ghafla kwa viwanda vya ndani vya utengenezaji hata kama, katika maneno ya jumla, mchango wa viwanda unaelekea kukua kwa haraka kuliko ule wa kilimo kwenye nchi nyingi. Wazo kuwa matokeo ya kuongezeka huku kwa mchango wa viwanda katika Zao Ghafi la Ndani limefikia kiwango cha maendeleo halisi ya viwanda, kulingana na hayo kuna haja ya kuangaliwa kwa makini.



PICHA 13.1 Kiwanda cha nguo za pamba cha Mahana Kaskazini mwa Misri

CHATI 13.5 *Muundo wa viwanda vya kuzalisha bidhaa nchini Nigeria, 1958-'78 (kwa asilimia)*

| | *1958* | *1963* | *1965* | *1972* | *1975* | *1978* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za watumiaji | 92.3 | 90.6 | 84.2 | 93.3 | 90.9 | 80.9 |
| Bidhaa za uzalishaji | 7.7 | 9.4 | 15.8 | 6.7 | 9.1 | 19.1 |

*Chanzo:* P. N. C. Okiglo, amenukuliwa na U. E. Okeke, 1985, uk. 46.

### *Afrika kwenye uzalishaji viwandani duniani: Vikomo vya 'uendelezaji viwanda kwa raia' kati ya 1960-5 hadi 1980*

Swali. je Afrika huru imejitokeza kuwa imechukua nafasi nzuri zaidi kwenye utengenezaji bidhaa kufikia mwaka 1980, kama ilivyojitokeza kutokea kipindi ambacho kinaonekana kwa kichocheo kilichowekwa makusudi kwa ajili ya kujenga viwanda. Ni vigumu kubadili kila kitu katika kipindi cha miaka 15 hadi 20 ya uhuru, na tena Afrika ilikuwa ikitoa asilimia 0.9 tu ya uzalishaji bidhaa zilizokamilika duniani. Wakati huo huo, hakuna shaka kuwa mchango wake kwenye uzalishaji mali ghafi za viwanda ulikuwa mkubwa kuliko kabla ya 1960-5. Ikiwa, mambo yote yamezingatiwa, Afrika ilikuwa kontinenti lenye viwanda vichache zaidi duniani na ukiangalia kutokana na mchanganuo wa mtiririko wa biashara duniani, ilikuwa kontinenti ambalo lilikuwa hasa mgavi wa mali ghafi za viwanda kwenye nchi zenye maendeleo ya viwanda za Ulaya na Amerika. Hivyo, mwaka 1980 lilikuwa bado ni kontinenti lenye maendeleo duni.

Hali kama hiyo huleta suala la kutaja vikomo vya kile tunachokiita 'uzalendo wa kuendeleza viwanda' na pia kanuni ya sera ya uhuru. Sera ya 'kupinga ubepari' na ile ya 'biashara huria' hazikufanikiwa mpaka sasa kuvunja mpangilio mbovu wa kontinenti kutegemea na kuwa na maendeleo duni ya viwanda. Katika jitihada za kueleza ukweli, maelezo yaliyotolewa yalikuwa ya kisiasa (kama vile maamuzi yaliyopotoka katika mazingira ya kuyumba kisiasa ambako kunawatisha wawekezaji binafsi) au kiufundi (kama vile viwango vya chini vya mafunzo ya utaalamu, kwa mfano, kiwango cha chini cha uwekaji akiba ya fedha ndani ya nchi ambapo haziwezi kutumika kwa usahihi au kwa wakati mwafaka kwenye

CHATI 13.6 *Maendeleo ya asilimia ya mchango wa viwanda kwenye Zao Ghafi la Ndani ya nchi tatu, 1960-74*

| *Miaka* | *Nigeria* | *Algeria* | *Cote d'Ivoire* |
|---|---|---|---|
| 1960 | 4.5 | - | 5.3 |
| 1963 | 7.8 | 23.8 | - |
| 1965 | 8.6 | 25.0 | 19.0 |
| 1968 | 13.1 | 29.0 | 23.8 |

*Vyanzo:* Government of Cote d'Ivoire, 1976 (namba ya mwisho ni kwa 1970); *Comptes economiques, 1963-1968,* imenukuliwa na G. D. de Berns, 1975, uk. 52; Nigerian Federation Office of Statistics, imenukuliwa na U. E. Okeke, 1985, uk. 37.

maendeleo ya viwanda). Maelezo mengine yatabidi kuongezea uchanganuzi huu. Tunahisi kwamba wengi wa 'waanzilishi wa mapambano ya uhuru' hawakusikiliza ushauri juu ya udhaifu wa muundo wa viwanda vya Afrika kama ulivyojitokeza tangu enzi za ukoloni. Udhaifu huu uliongezeka mwaka 1980.

## Udhaifu wa maendeleo ya viwanda

Miongoni mwa yote, pengine vipengele vidogo, udhaifu huu unaletwa na sababu nne: kutegemea moja kwa moja uwekezaji toka nje; fikra potofu juu ya uwezekano wa kuhamisha teknolojia kwa kutumia mashirika toka ng'ambo yanayofanya shughuli zake kwenye kontinenti; uzalishaji mdogo zaidi wa sekta kuu ya viwanda; na kiwango cha chini cha mungiliano wa biashara za viwanda kwenye soko ambalo lina idadi ndogo ya watu wenye vipato vya chini.

### *Uwekezaji katika sekta ya viwanda Afrika: kutegemea nchi nyingine za kigeni tangu 1935*

Hakuna mtu anayeweza kukanusha nafasi iliyoshikiliwa na nchi nyingine nje ya Afrika kwenye ujenzi wa viwanda vya kisasa vya kontinenti la Afrika, angalau tangu 1935. Mpaka hivi karibuni ilikuwa inahesabiwa kuwa na kiasi kikubwa cha mtaji uliowekezwa kwenye viwanda kwa muundo wa uwekezaji wa moja kwa

moja wa sekta ya umma (au uwekezaji wa umma usio wa moja kwa moja kwa msaada 'toka nje') au vingine, uwekezaji binafsi au uwekezaji kupitia mawakala wa kukopa wa kimataifa. Kuhusu nchi za kiafrika zinazoongea Kifaransa, hususan kabla ya 1960, nchi ya Ufaransa (mwekezaji wa umma) na sekta binafsi ya Ufaransa ilitoa asilimia 95-8 ya vitega uchumi vyote vya viwanda, wakati kwenye uchumi wa Kongo ya Wabelgiji, mchango wa makampuni ya kigeni (hasa ya Kibelgiji) na riba mwaka 1958 ilikuwa asilimia 95 (na karibia asilimia 100 kwenye viwanda).

Pamoja na hayo katikati ya miaka ya 1960, njia ya kupata msaada wa mtaji kwa umma na utaifishaji wa makampuni binafsi (mara nyingi yasiyo ya kiafrika) na kile kinachoitwa sera ya 'uasilia' kwenye viwanda (kama kanuni za 1974 na 1977 huko Nigeria), zilisaidia kupunguza tamaa ya wageni kwenye uwekezaji wa viwanda. Kwa ukweli, hata hivyo, imebidi kuweka vivutio mtaji toka nje kwa ajili ya kulipia miradi mipya ya viwanda, ikiwa ni kwa njia ya moja kwa moja au njia nyingine, kutegemea nchi ya kigeni kumekuwa ni ukweli wa maisha usiokwepeka. Ni huku kutegemea kunakoonyesha mwelekeo mkuu uliochukuliwa na viwanda katika nchi nyingi.

Siku za nyuma miaka ya 1930 hadi 1950, sehemu kubwa ya uwekezaji katika viwanda ilienda kwenye migodi ambayo, pamoja na mashamba, yalikuwa na faida kwa makampuni ya Ulaya kuliko viwanda vya kutengeneza bidhaa. Kufuatana na J. Marseille, mapato toka kwenye kampuni za Kifaransa mwaka 1938 yalifikia asilimia 5.6 ya viwanda dhidi ya asilimia 24.9 kwa migodi na asilimia 15.2 kwa mashamba; mwaka 1954, idadi zilikuwa asilimia 6 kwa viwanda, asilimia 9.7 kwa mashamba na asilimia 8.6 kwa migodi. Kwa kutofautiana huko, mwelekeo unaofanana unaonekana kwenye mifano mingine, ambapo malengo makuu yametekelezwa na makampuni ya Ulaya na Amerika.

Leo, hali imebadilika kidogo isipokuwa kwenye mambo fulani: mwaka 1965, asilimia 67.18 ya vitega uchumi iliyopitishwa kwenye serikali za nchi za kiafrika zinazoongea Kifaransa kwa kipindi cha 1965-70 zilielekezwa kwenye madini; mwaka 1976, ukaguzi wa mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi hizi umeonyesha kuwa kiwango kilikuwa kati ya asilimia 60 na 75.

Hali hii ilijitokeza kutokana na haja ya nchi hizo kupata kiasi kidogo cha rasilimali kwa ajili ya kulipia sekta ya viwanda vya kisasa zaidi? Hilo linaweza kuwa kweli, lakini ilikuwa hasa ni matokeo ya mikabala iliyopangwa hasa na mashirika ya kutoka nje bila kujali matakwa ya nchi.

## *Wajibu wa mashirika ya nje kuanzia Vita Kuu ya Pili ya Dunia na fikra duni kuhusu uhamishaj wa teknolojia*

Kabla ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, mashirika ya nje hayakuwa yakijishughulisha sana katika sekta nyingine Afrika, zaidi ya sekta ya madini. Kati ya 1946 na 1955 majaribio makuu yalianza kuendelezwa, aidha kama mpango wa kurekebisha shughuli zilizohusu shughuli za makampuni makubwa ya kikoloni. Hata hivyo, mara tu baada ya idadi kubwa ya nchi kupata uhuru wao makampuni haya yalitambuliwa wazi zaidi na yaliendelezwa na kuwa makubwa zaidi, au kwa kuongeza idadi ya matawi au kampuni zinazojitegemea au vingine kufungua kampuni ndogo za 'kitaifa'. Miongoni mwa sababu zilizoleta maendeleo haya kufanikiwa baada ya miaka ya mwanzo ya 1960 yalikuwa masharti yaliyotolewa na sheria za uwekezaji za serikali mpya na hamu ya kupunguza gharama za uzalishaji kwa kusogea karibu kwenye kanda zinazozalisha mali ghafi zikiwa na wafanyakazi wa ujira mdogo. Tayari tumeshaonyesha kuwa, katika suala la Afrika Kusini, pia kulikuwa na haja ya kuzuia bodi ya sheria ambayo imekuwa ikiwalinda tangu katikati ya miaka ya 1930 na kuendelea. Hadi kufikia 1980, hali hiyo hiyo iliendelea katika idadi kubwa ya nchi huru za Afrika. Kukua kwa shughuli za viwanda za kimataifa kulileta haja ya kupata masoko na hatua za kuzilinda zilizochukuliwa na serikali ziliyapa makampuni hayo uhakika.

Lakini kweli sehemu kubwa ya makampuni haya yamelenga uingizaji bidhaa nchini na madini, yalikuwa njia kuu ya kuhamisha teknolojia katika nchi za Kiafrika: mchango wao kwenye mafunzo ya utaalamu ulikuwa mdogo zaidi kuliko ule wa serikali au hata ule wa makampuni madogo. Teknolojia iliyotumiwa kwenye vitengo vyao vya uzalishaji iliwekewa mipaka kwa kutumia mitambo ya kampuni mama na ilitakiwa kutumiwa ipasavyo kufuatana na maelekezo yake. Huko Cote d'Ivoire, kama ilivyokuwa katika nchi nyingi za Kiafrika, hakukuwa na masharti yoyote ya usambazaji baada ya uzalishaji wa bidhaa mpya ili kuendeleza sekta mpya ya viwanda, wala uanzishaji wowote wa viwanda vipya vya uzalishaji vitakavyoleta ongezeko la ajira. Haya yote yalikuwa na athari mbaya baadae kwenye uzalishaji ulio duni sana (kwenye nchi kama Afrika Kusini na Misri) ambayo ni moja ya sifa za viwanda vya Afrika.

Hii imekuwa moja ya sababu kuu za kutoridhika na jukumu lililotekelezwa na makampuni ya kimataifa, kama ilivyofanya kampuni kutoka nje mikakati ya biashara hizi ambazo, haikujali mipaka ya kimataifa na sera za maendeleo ya viwanda za 'taifa', zimeendelea kuhatarisha viwanda na zinaweza hata kuvidhoofisha zaidi.

## *Muunganiko wa viwanda na kutofaulu kwa mashirika ya Afrika nzima*

Kwa sasa imeshakuwa sehemu maarufu ya kuongelea kuhusu udogo wa masoko ya nchi fulani za Afrika: sababu kubwa za suala hili ni idadi ndogo ya watu katika maeneo makubwa sana ya kontinenti na zaidi ya yote, kiwango cha chini cha mapato. Ilikuwa kwenye ushindani ili kurekebisha kasoro hizi ambapo wazo la kuungana kiuchumi na upatanishi unaofaa wa sera za viwanda ulianza kuwa wa msingi mwishoni mwa miaka ya 1960. Ongezeko la idadi ya mashirika ya kanda ndogo au Afrika yote lilikuwa pia thabiti kwa lengo hilo. Baadhi ya viwanda vimeona mwanga wa siku (kama vile CIMAO -Kampuni ya Sementi ya Afrika magharibi - ambayo ilianzishwa mwaka 1974 kuendeleza Togolese clinker kwa ushirikiano wa Cote d'Ivoire na Ghana), na Mpango wa Utekelezaji (1979) ulioelezwa na OAU umeyapa nguvu mawazo haya.

Inabidi kutambua, hata hivyo, kuwa vikwazo vingi vilikuwa kama sera ya upatanishi na muunganiko, kama vile kiwango cha hisia kuhusu kutumia mamlaka kwenye mambo yanayohusu uchumi, tofauti kubwa sana kuhusu sera za pesa na mikakati ya viwanda, kutokuwa na sera ya teknolojia ya viwanda inayozingatia mahitaji ya watu inapobidi kupambana na changamoto ya kuwa na maendeleo duni, na kadhalika. Kwa kifupi, kushindwa kwa mashirika ya nchi za Kiafrika, kama vile OAU, ECA (Kamati ya Uchumi ya Afrika), ECOWAS (Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi) na UDEAC (*Union douaniere des etats de l'Afrique centrale)*, kwenye eneo hili ni wazi ya kuonekana kwa wote.

Moja ya udhaifu wa viwanda vya Afrika mwaka 1980 ni kutokuwa na uwezo wa kuhimili ushindani kutoka kwenye maduhuli, mwingine ni fidia za serikali au malipo makubwa ya forodha. Kwa kuwa viwanda vya Afrika vilisimamiwa vibaya (licha ya masuala ya biashara za viwanda kwenye baadhi ya nchi) na ilionekana kwa uzalishaji mdogo, bado havikuweza kufanikiwa, bila kuwa na upungufu mkubwa wa fedha, kuingia kwenye ulingo wa kusafirisha nje bidhaa isipokuwa kupitia mikataba ya ushirikiano kati ya mabara - kama vile EEC (Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya)/ACP mikataba ya (Africa/Caribbean/Pacific) - ambayo yalishirikiana kibiashara kwa ajili ya bidhaa muhimu au bidhaa zilizozalishwa na viwanda mbadala wa bidhaa za kuagiza toka nje havikufanikiwa sana kutokana na tabia ya mazoea ya kontinenti ya kuwa 'mgavi' wa mali ghafi ya viwanda.

Jambo muhimu zaidi ni kuwa kwa sababu ya kutegemea kabisa mtaji wa nje na bidhaa zinazotengenezwa kiasi, viwanda vya kisasa katika Afrika havikuleta unganisho la sekta kati ya sehemu zake mbali mbali. Ilikuwa hasa vigumu kuanzisha

uhusiano wa kuheshimiana kati ya sekta za kijiografia, kwa mtazamo wa muunganiko wao. Kutokana na mtazamo wa viwanda, ukweli ni kuwa nchi fulani zilianza kuchukua nafasi za uhuru kendeleza biashara zao nje ya kontinenti, ingawa hii ilihusisha mtaji, bidhaa zinazotokana na madini au mali ghafi za kilimo, yalikuwa matokeo ya hali kama hiyo. Hii ilisababisha kuhatarisha usalama wa viwanda vya Afrika, kwa kuwa haikuwa na uwezo, kwa njia zake yenyewe, kumudu nyongeza ya malipo ya mgogoro au kushuka kwa uwekezaji toka nje ya Afrika.

Mwisho, ukweli uhusiano kati ya viwanda (bidhaa mtaji na utengenezaji) na kilimo ulikuwa duni, wakati zingeendeleza ufanisi wa viwanda na kupanua msingi wa kilimo, uliosababisha uzalishaji wa viwanda vya Afrika kuwa na ushindani kidogo kuliko bidhaa zisizo za Afrika, hata ndani ya nchi fulani zenyewe.

Mzunguko wa kutegemea pamoja na kuwa na maendeleo duni ya viwanda uliendelea kuwepo hata mwaka 1980.

Maoni hayo hapo juu hata hivyo yanahitaji uthibitisho wa hali ya juu. Tangu 1935, kama si mapema zaidi, jiografia ya viwanda ya kontinenti la Afrika imeonyesha aina mbili kubwa za kutolingana ambako kihistoria kunahusishwa na suala la nchi nyingi, kwa jina kutolingana kati ya sekta za kijiografia ambazo mwanzoni zilikuwa hasa za kilimo na zilichelewa kujitokeza kwenye shughuli za viwanda, na kutolingana, hasa ndani ya nchi fulani, kati ya maeneo ya bandari ambako bidhaa hupitia na maeneo ya uzalishaji viwandani. Kutolingana huku kuna athari fulani kwenye mfumo wa anga na mpango wa matumizi ya ardhi, pamoja na sera ya viwanda iliyopitishwa.

Mpangilio wa sehemu ya viwanda mwaka 1935 na 1980 unaonyesha makundi ya kanda ndogo tano ambayo yanatofautishwa kwa umri na ukubwa wa jengo la kiwanda, kiwango ambacho mashine zinaungana na aina zake. Hivi ni viwanda vya Maghreb - Misri; Mashariki ya Kati; kanda ndogo ya Kusini; Afrika ya Kati - Magharibi; na Afrika Magharibi. Kama hitimisho kwa mapitio haya ya sifa za maendeleo ya viwanda, lazima ielezwe kuwa ujenzi duni wa viwanda katika Afrika umeleta maendeleo duni ya kontinenti na kuwa tegemezi mwaka 1980, licha ya maendeleo ya wazi ya 1935. Njia zilizochukuliwa na maendeleo ya viwanda zimeleta au zimesaidia kusisitiza kutolingana ambako mpangilio wa mji wa kisasa unaakisi kwa makosa kama tutakavyoona hapo chini.

CHATI 13.7 *Wingi wa viwanda kijiografia katika nchi zinazoongea Kifaransa mwaka 1970*

| *Mijini na vijijini* | *Asilimia ya makampuni* | *Asilimia ya uwekezaji viwandani* | *Asilimia ya ajira ya viwandani* | *Asilimia ya mapato na matumizi* |
|---|---|---|---|---|
| Dakar (Senegal) | 75.0 | 79.6 | 81.8 | 80.9 |
| Abidjan (Cote d'Ivoire) | 69.5 | 62.2 | 46.5 | 68.5 |
| Bouake (Cote d'Ivoire) | 5.6 | 7.1 | 9.2 | 7.6 |
| Douala (Kameruni) | 51.8 | 44.9 | 44.7 | 61.7 |
| Yaounde Kameruni) | 10.2 | 6.5 | 4.9 | 6.4 |
| Pointe-Noire (Kongo) | 36.1 | 32.4 | 25.5 | 27.6 |
| Brazaville (Kongo) | 40.9 | 20.1 | 25.9 | 28.9 |
| Libreville na Port-Gentil (Gabon) | 75.0 | 81.1 | 81.1 | 93.7 |
| Cotonou (Benin) | 69.0 | 80.4 | 78.1 | 71.4 |
| Lome (Togo) | 85.0 | 90.0 | 96.8 | 87.6 |
| Niamey (Niger) | 45.0 | 56.4 | 50.3 | 17.3 |
| Ouaga na Bobo (Burkina Faso) | 89.0 | 55.7 | 73.5 | 65.6 |
| Bamako (Mali) | 53.0 | 17.0 | ? | ? |
| Segou (Mali) | 10.0 | 23.0 | ? | ? |

*Chanzo:* J. Suret-Canale, 1987, juz. 2, kur. 482-3

## Maendeleo ya viwanda - sababu ya kuibuka kwa miji Afrika, kati ya 1935 na 1980

Historia ya kuibuka kwa miji ya kontinenti hili inaonyesha kuwa kulikuwepo 'vizazi vya mijini'. Hivi vinatofautiana kufuatana na kuhusiana na wakati ilipoanzishwa - kama vile, iwapo makazi ni ya kabla ya ukoloni au ya kikoloni, au miji mipya iliyoanzishwa baada ya enzi ya ukoloni - au kazi kuu inayozifanya kama bandari, vituo vya biashara, makazi ya migodini au makao ya utawala. Historia tayari imeonyesha kuwa karne ya ishirini ni kipindi ambapo inawezekana kusema kuwa imekuwa ya 'mapinduzi ya miji' katika Afrika.

Hata hivyo, bila kujali kama suala ni moja ya mahusiano kati ya maendeleo ya wafanyakazi viwandani na kukua kwa miji au ya mipango ya ujenzi wa miji tangu 1935, itaenda mbali sana ili kupata kiungo cha moja kwa moja miongoni mwa mambo mawili katika suala la Afrika, ingawa kwenye baadhi ya mifano, kukua kwa miji kumechangia kwenye maendeleo ya viwanda kwa kiasi fulani, kama kwenye suala la miji ya migodi ya Tarkwa huko Ghana, Ndola huko Zambia na Mwadui huko Tanzania au vitongoji vya Mauritania, Niger na Afrika Kusini.

## Kukua kwa miji tangu 1935 na mendeleo ya wafanyakazi viwandani

Mara nyingi kuna kutofautiana kwa vipimo vilivyotumika kukadiria jumla ya watu mijini na uwiano wa watu wanaofanya kazi kwenye viwanda vya uzalishaji. Hili ni tatizo la methodolojia (vigezo tofauti hutumika kutambua mambo yanayounda *mji* na takwimu mbali mbali hutumika) kama tatizo la uhifadhi wa hati (mara nyingine sensa zisizokamilika hupatikana kwa miaka tofauti). Matokeo yake, ni vigumu kuamua kwa uhakika kipimo cha kweli cha kukua kwa mji na uwiano wa kukua uliochukuliwa na 'wafanyakazi wa viwandani'. Mara nyingi inabidi turidhike na makadirio.

### *Data ya takwimu kuhusu idadi ya watu na kukua kwa mji kuanzia 1935 hadi 1980*

Kala ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, ambayo ilikuwa kipindi kabla ya takwimu kufanyika par excellence, makadirio ya watu walioishi mijini hayakuwa ya uhakika. Kazi ya kuhesabu watu haikufanyika kwa makini nchini kote. Maeneo machache

tu yalikuwa na moyo kufanya hivyo na hayo hasa yalikuwa Afrika Kaskazini na Afrika Kusini. Hivyo inajulikana kuwa idadi ya watu walioishi mijini huko Afrika Kusini iliongezeka kutoka asilimia 25.1 ya idadi ya watu nchini mwaka 1921 hadi asilimia 31.4 mwaka 1935 na asilimia 38.4 mwaka 1946. Afrika Kaskazini, kuongezeka kwa idadi ya watu mijini ilikuwa kwa usawa: huko Misri, ambayo ilikuwa na wakazi milioni 13 mwaka 1920 na milioni 16 mwaka 1938, idadi ya watu mijini iliongezeka toka watu milioni 6.3 hadi 9 kufikia mwanzo wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Kwenye nchi za Maghreb, idadi ya watu mijini ilikuwa vile vile inaongezeka kwa kasi.

Kwingineko, takwimu zinapatikana kwa shida. Hata hivyo, ukichukua mfano wa nchi za Afrika Magharibi zinazoongea Kifaransa kabla ya 1939, kwenye makazi ya mbali ya kikoloni yaliyogunduliwa na Ufaransa kama miji muhimu kwa wakoloni kabla ya kuanza ukoloni, idadi haikuwa sawia, lakini kwenye maeneo kama vile Cote d'Ivoire, ukweli, idadi imekuwa ikiongezeka tangu 1923-5. Kwenye nchi ya jirani ya Gold Coast na huko Nigeria kabla ya 1935, ongezeko la watu mijini linaweza kuonekana kutoka kwenye sensa zilizofanyika: kwa mfano, idadi ya watu katika miji ya Gold Coast ya angalau wakazi 5000 ilipanda kutoka asilimia 5 mwaka 1921 hadi asilimia 9.3 mwaka 1931.

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, idadi inakuwa sahihi zaidi na tunapata picha halisi ya mlipuko wa idadi ya watu kwenye miji ya Afrika hadi kufikia 1980. Kwa kontinenti kwa ujumla, inakadiriwa kuwa idadi ya watu mijini iliongezeka toka watu milioni 31.8 mwaka 1950 hadi milioni 49.5 mwaka 1960 na 132.9 mwaka 1980, kwa wastani wa ongezeko la asilimia 4.8 kwa mwaka kati ya mwaka 1950 na 1980. Kasi iliongezeka zaidi hasa kuanzia mwaka 1960 na kuendelea.

Si kila nchi au kila mji uliathirika kwa kiwango sawa. Ukweli, licha ya kuongezeka kwake kwa haraka, idadi ya watu mijini katika jumla ya idadi ya watu Afrika bado ilikuwa ya chini sana, ingawa ilikuwa juu zaidi kwenye baadhi ya sehemu za kontinenti (Maghreb, kwa mfano) (Chati 13.8).

Inabidi kuuliza iwapo mgawanyo wa kazi wa watu, na zaidi ya yote ule wa miji, unawezesha kuanzisha uhusiano kati ya watu wanaofanya kazi viwandani na watu wanaoishi mijini.

## *Mwelekeo kwenye mgawanyo wa kazi kwa wakazi wa mijini*

Mahesabu yanaonyesha sehemu sehemu katika suala hili. Hata hivyo, kwa kutabiri hesabu zilizopo, sifa tofauti zinaweza kutumika.

Katika miaka ya 1930, watu wenye uwezo wa kufanya kazi walioajiriwa kwenye migodi wakiondolewa, uwiano wa watu mijini wanaofanya kazi viwandani ulipanda kwa asilimia 20 tu kwa Afrika Kusini. Katika sehemu nyingine, sehemu ndogo sana ya uwiano wa wakazi wa mijini walikuwa wameajiriwa kwenye kazi za viwanda: mwaka 1938, asilimia 1.58 ya wakazi wa miji ya Misri walikuwa wanafanya kazi kwenye viwanda vyenye zaidi ya wafanyakazi watano, wakati huko nchi za Afrika Magharibi zinazoongea Kifaransa uwiano ulikuwa chini ya asilimia 1 katika kipindi mara baada ya mwisho wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Baadae, hasa baada ya 1950, uwiano wa wakazi wa mjini walioajiriwa kwenye sekta ndogo (bila kuhesabu ufundi wa jadi) uliongezeka haraka sana, lakini ilikuwa wakati wote chini ya kiwango cha kukua kwa mji (Chati 13.9). Kuhusu suala la Algeria, kwa mfano, nchi imerekodi kukua kwa haraka kwa ajira za viwandani kati ya 1970 na 1980 (toka ajira 117000 mwaka 1967, ziliongezeka hadi 347000 mwaka 1977 na 400000 mwaka 1980). Hata hivyo, itaonekana kuwa, kwa wastani wa ongezeko la asilimia 4.3 kwa mwaka kati ya 1966 na 1977, idadi ya watu wanaoishi mijini iliongezeka kutoka milioni 4.16 mwaka 1966 hadi kufikia milioni 6.57 mwaka 1977. Viwanda vimebakia kuwa nyuma sana katika huduma na sekta za juu kwa ujumla.

Idadi ya watu waishio katika miji ya Afrika ilianza kuongezeka taratibu hata kabla ya kontinenti kuanza kuendeleza uchumi wa viwanda. Katika miaka ya 1965-80, kivutio cha kazi kiwandani kiliweza kusaidia kama sababu ya kuhamia mijini. Hata hivyo, maendeleo ya dawa za kinga yalisaidia kukua kawaida kwa miji, wakati kuondoka kwa idadi kubwa sana ya wakazi wa vijijini baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia kulichokozwa siyo hasa na ushindani kati ya sekta ndogo na kilimo kama ilivyokuwa mgogoro halisi kwenye kilimo, ambao ilijikuta ikishindwa kumudu uchumi wa pesa.

Ajira za viwanda vya kisasa siyo kishawishi pekee cha uchumi kama huo wa fedha; katika maana pana, inategemea haja ya mapato ya fedha taslimu mara kwa mara na katika uwezo wa pamoja wa mtu mmoja kumudu kupungua kwa biashara ya bidhaa za kilimo. Hii ilikuwa inahusu nchi kama vile Algeria, Kenya na Rhodesia Kusini, ambako makazi ya Wazungu yalileta mgogoro wa ardhi miongoni mwa jumuiya za Kiafrika kutokea siku za mwanzo kabisa, na vile vile nchi hizo

kukumbwa na majanga ya mazingira kama yale ya Sahel na Ethiopia, ambapo swali lilikuwa moja la kupambana kupata riziki kwa ajili ya kuishi. Sababu kubwa inayoleta kukua kwa miji, kuanzia 1935 na kuendelea, ilikuwa zaidi mgogoro kwenye kilimo cha Afrika kuliko maendeleo ya kupata ajira za viwandani kwenye maeneo ya miji.

Kwa kanda ndogo au tofauti za ndani, mfumo unaofanana unaweza kupatikana

CHATI 13.9 *Uhusiano kati ya uhamiaji mijini wa watu na ajira viwandani, 1950-70 (kwa ailimia)*

| | *Afrika Magharibi* | *Afrika Mashariki* | *Mashariki ya Kati* | *Afrika Kaskazini* | *Afrika Kusini* |
|---|---|---|---|---|---|
| 1950 | | | | | |
| Wafanyakazi viwandani (1) | 3.66 | 5.87 | 10.44 | 24.56 | 6.10 |
| Watu mijini (2) | 5.50 | 14.57 | 24.51 | 37.27 | 10.15 |
| Uwiano (1/2) | 66 .54 | 40.29 | 42.59 | 65.90 | 60.10 |
| *1970* | | | | | |
| Wafanyakazi viwandani (1) | 6.32 | 9.54 | 15.75 | 26.35 | 11.30 |
| Watu mijini (2) | 10.69 | 25.16 | 36.61 | 43.76 | 17.27 |
| Uwiano (1/2) | 59.12 | 37.92 | 43.02 | 60.21 | 65.43 |

*Chanzo:* United Nations, 1981, uk. 19

kazini kila mahali katika Afrika, ingawa zinatofautiana ukubwa na kufuata mipangilio tofauti, kutegemeana na kipindi, mfano cha ukoloni, kuanzia miaka ya 1930 na kuendelea, au kipindi baada ya ukoloni (kati ya 1960-5 na 1980).

## *Mipangilio ya ujenzi wa miji na kukua kwa miji wakati wa ukoloni*

Kuanzia 1935 hadi 1960-5 katika suala la nchi zote za Afrika zisizokuwa huru, na kuanzia 1935 hadi 1980 kwa suala la Afrika Kusini, sera za kazi za kikoloni na shughuli zilizofanywa na maeneo ya miji kwenye uchumi wa kikoloni zilikuwa kusaidia kuweka katika mwendo mpangilio wa ujenzi miji ambao ulikuwa

tofauti kabisa na ule wa kipindi kabla ya ukoloni. Hii pole pole imeleta maendeleo katika maeneo ya mijini.

## *Sera za kazi za kikoloni na mwelekeo katika uhamiaji Afrika*

Kabla ya mgogoro wa 1930, sera za kazi za kikoloni zinaweza kuboreshwa kwa kuwa na uhamasishaji wa jumla wa wafanyakazi kwa ajili ya maendeleo ya utajiri wa maliasili uliodhibitiwa na wakoloni katika hali ya migodi, mashamba makubwa, misitu, na kadhalika. Kulikuwa na haja kidogo ya kuhamasisha kiwango cha juu cha utaalamu miongoni mwa wafanyakazi; kinyume na hapo wazo lilikuwa kufanikisha kupata faida kwa kutumia mtaji wa kiwango cha chini na kuajiri wafanyakazi ambao watakaolipwa mishahara midogo. Wakati huo huo, msukumo wa kodi na kuzuka kwa wafanyakazi wa ujira, ambayo yalikuwa ya taratibu sana kwenye baadhi ya maeneo, yalikuwa sababu za muhimu kazini kwenye sera hii.

Katika baadhi ya mifano, mgogoro wa 1930 uliharakisha utaratibu, wakati kwa wengine kuliondoa hatari ya usawa kati ya wafanyakazi wa vijijini na matakwa ya sera ya kazi. Mwaka 1935, sera ya kazi haikutilia maanani mgogoro huu kwenye maeneo ya vijijini, ambao umewavuta maelfu ya wakulima kuandamana hadi mijini. Ilikuwa tukio la mwanzo la watu wengi kuondoka vijijini ambapo linaendelea hadi leo hii. Kwa mfano, watu wa Cairo waliongezeka toka 800000 katikati ya miaka ya 1920 hadi 1400000 mwaka 1938. Kuongezeka kwa msongamano mijini kuliongezewa na kuongezeka kwa umaskini. Claude Liauzu ameonyesha katika suala la Tunisia kuwa idadi ya watu wanaoishi mijini inaendelea kuongezeka haraka zaidi kuliko uzalishaji (kuanzia kwenye msingi wa 100 mwaka 1925-9, takwimu ya idadi ya watu imeongezeka hadi 122 mwaka 1935-9 na hadi 136 mwaka 1940-4, wakati takwimu ya uzalishaji ilisimama kwenye 106 mwaka 1935-9 na ikashuka hadi 65 mwaka 1940-4. Katika kipindi hicho, kukosa ajira mijini ilikuwa jambo la kawaida katika Tunisia. Mahitimisho yanayofanana yamefikiwa kwenye tafiti za miji ya Maghreb na nchi za Afrika Magharibi zilizotawaliwa na Ufaransa.

Huko Afrika Kusini, ilikuwa uhamiaji wa wakulima weupe waliofilisiwa na mgogoro, na vile vile wafanyakazi wao Waafrika, na udhibiti wa waafrika wanaoacha hifadhi walizokuwa wanawajibika nazo kwa kuongezeka kwa idadi ya watu mijini. Katika uhusiano huu, hata hivyo, itabidi ielezwe kuwa sera ya ubaguzi wa makazi, ambayo imeendelea pole pole kujitokeza tangu 1910, imeendeleza sera ambapo Waafrika walikatazwa kuingia mijini lakini siyo kuingia migodini. Zaidi ya hayo, kufikia 1935, Ureno ilishaanzisha huko Msumbiji na Angola Kusini

'mfumo wa mkataba wa muda' kwa wafanyakazi wa Kiafrika waliopelekwa kwenye migodi ya Afrika Kusini. Isipokuwa Afrika Kusini, ambapo baada ya 1948, sera ya *ubaguzi wa rangi* ilisisitiza mwelekeo ulioonekana tayari kabla ya 1935, kuanzia 1945 hadi 1960-5 ni kipindi ambapo sera ya kazi ya kutumia mabavu ilidorora. Mkazo uliongezwa zaidi kwenye kuwaruhusu wafanyakazi wasio na ujuzi kuwa huru kutembea.

Miji mikuu ya miaka ya 1950 ilikuwa miji ambayo mara nyingine ilikuwa fokasi kwa ajili ya viwanda vidogo, lakini mara nyingi ilikuwa miji ya biashara katika hali inayoeleweka ya kusaidia kuendeleza huduma mbali mbali kama vile wafanyakazi wa nyumbani na vibarua. Pia ilitumika kama vituo vya mapokezi kwa idadi kubwa mno ya watu toka vijijini ambao waling'olewa kimaendeleo: mwaka 1954, asilimia 50 ya kazi zote zisizo za kilimo huko Algeria zilikuwa za biashara, ujenzi na huduma mbali mbali. Ajira ya aina hii ilikuwa mara nyingi ni ya muda (asilimia 47 huko Algeria mwaka 1954) na ilikuwa inaandaa watu wanaoishi mijini ambao idadi yao ilikuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa kama ziada ya wahamiaji toka vijijini (katika maghreb, ziada hii ilifikia asilimia 44-53 ya ongezeko la idadi ya watu kabla ya 1960), katika mifano ambapo hao wahamiaji hawakuondoka Afrika kwa pamoja (idadi ya Waalgeria huko Ufaransa iliongezeka kwa 180000 kati ya 1947 na 1955).

Ukuaji wa miji katika Afrika kati ya 1935 na 1960 ulichochewa na uhamaji kwa wingi wa watu toka vijijini uliotokana na mgogoro kwenye maeneo ya vijijini kuliko maendeleo ya viwanda. Ni hali hii ambayo imesababisha dharura, kutoka 1930-5 na kuendelea na hasa baada ya 1945, ya matukio ya kuvamia makazi kwenye maeneo ya mijini kwenye kontinenti.

## *Mpangilio wa maendeleo ya miji na mwanzo wa 'uvamizi' wa makazi*

Mwaka 1935, Afrika tayari ilionyesha hali tofauti kwa kuzingatia mpangilio wa maendeleo ya miji. Kuanzia mwanzoni mwa karne ya ishirini, mambo mawili makuu yalionekana: kwa upande mmoja, ilkuwepo miji mikongwe kabla ya Wazungu, mingi ikiwa Afrika Kaskazini, Sahel ya Afrika Magharibi, Ethiopia na Yoruba (picha 13.1); na kwa upande mwingine, kulikuwepo miji iliyoanzishwa na wakoloni, katika baadhi ya mifano, ingawa siyo kila mara, kutoka kwenye vijiji vya kiafrika kabla ya ukoloni. Kutegemeana na hali, mpangilio wa maendeleo mapya mijini yalionekana dhahiri kuwa chapa ya mamlaka ya serikali ambayo ilikuwa na athari zenye asili ya Ulaya (kwenye suala la makoloni) au vinginevyo

imepata athari kidogo sana za Ulaya (katika suala la Nchi Lindwa za Afrika Kaskazini).

Mwaka 1935, serikali (utawala wa kikoloni au serikali ya mitaa) ilikuwa wakala mkuu anayehusika na uendelezaji wa maeneo yaliyopangiliwa ambayo yalitolewa kwa wakazi kwa ajili ya malengo ya ujenzi (makazi au sehemu za kazi). Utekelezaji uliofanywa na serikali kuhusiana na hili, kuacha nafasi kulianza kuonyesha dalili za ubaguzi kwenye sehemu kubwa ya miji na pia ilionyesha asili ya mshikamano wa kutegemeana kisiasa na kiuchumi ambao jamii ya Kiafrika ilijifunga. Katika Afrika Kaskazini, kwa mfano, *wamedina* na *wasouk* walipinga nyumba za kuishi za Wazungu na sehemu ya wenyeji walio kwenye tabaka la juu na hasa matabaka ya kijamii 'yaliyoiga utamaduni wa Wazungu'. Kwenye Afrika ya Weusi, hususan kwenye maeneo yale ya mijini yaliyoanzishwa na wakoloni, tofauti ilikuwa inaonekana zaidi kati ya 'miji ya Wazungu' na 'vitongoji vya Waafrika' na ilikuwa ushahidi wa ubaguzi ambao ni wa rangi na kijamii.

Tangu miaka ya mwanzo wa karne, hii imekuwa sera maalum huko Afrika Kusini. Hata hivyo, matokeo ya mgogoro wa 1930, hali ilikuwa mbaya zaidi na kukua kwa miji ambayo, kama tulivyoona mapema, ilichochewa na kuhama kwa wingi kwa wakazi maskini wa vijijini kwenda mijini. Hawa wakazi wapya wa mijini, kwa kushindwa kulipa kodi zilizokuwa zikiongezeka au gharama za nyumba za mjini, na kutopata pesa za kutosha kununua vifaa vya ujenzi kama vile sementi, mabati au vigae, walilazimika kwenda kusongamana kwenye *medina* na *souks*. Hadi kufikia miaka ya 1930, kulikuwa na maeneo ya miji yasiyokuwa na mpangilio nje ya udhibiti wa serikali, kama vile dampo za taka taka, mabwawa, makaburi yasiyotumika, na kadhalika, ambayo yalichaguliwa na hawa wakazi wa mijini kujenga nyumba zao kutokana na chochote walichopata. Huko Tunis, ambako ufaransa huiita *bidonville* kwa ajili ya uvamizi wa makazi au mtaa wa vibanda vibanda lilitumika kwa mara ya kwanza mwaka 1931 (kwenye makala ya Dr Materi kwenye *Voix du Tunisien* ya tarehe 6 Novemba 1931), idadi ya wakazi wa hivyo vibanda iliongezeka kutoka 2000 mwaka 1935, hadi 5000 mwaka 1938 na 10000 mwaka 1941; kufikia mwanzo wa vita, Tunis ilizungukwa na makazi ya vibanda. Ilikuwa pia kati ya 1935 na 1945 nyumba za vibanda zilianza kujitokeza Abidjan, Accra, Lagos na Douala. Katika Afrika Mashariki iliyotawaliwa na Waingereza (Nairobi, kwa mfano) au Afrika ya Kati, na zaidi ya yote Afrika Kusini, Sheria za Ardhi na Sheria ya Maeneo ya Miji ya Wenyeji ya mwaka 1923 zilisaidia kuimarisha ubaguzi wa rangi, lakini walishindwa kuzuia maendeleo ya kupanuka kwa vitongoji kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1920 na kuendelea. Kanuni rasmi ilizingatia ukweli kuwa 'Waafrika kwa asili hawakuwa wakazi wa mijini na hawakuwa wamefanikiwa katika maisha ya mjini' kama Kamati Inayoshughulikia Masuala



PICHA 13.2 *makazi ya vibanda: juu, huko Lagos; kati kati, bonde la Mathare huko Nairobi; chini, Belcourt huko Algiers*

ya Wenyeji ilivyosema mwaka 1921.
Baada ya 1945, suala la uvamizi wa makazi lilichukua nafasi kubwa zaidi na kidogo kidogo hasa katika miaka ya 1950, vikaenea kwenye kila mji kwenye kontinenti. Kila mgogoro wa kiuchumi wa koloni, kila kipindi cha ukame au kutopata mavuno (1945-1951-3) kilileta mchango wake wa wakazi wa vijijini kuingia mijini na kuongezeka kwa kodi. Licha ya juhudi za kujenga makazi yaliyopangiliwa mijini au kuandaa nyumba haraka kwa ajili ya mahitaji yanayoongezeka, utawala wa kikoloni na mamlaka ya taifa hazikufanikiwa kudhibiti 'ujenzi vibanda' wa miji ya Afrika ambayo sasa imekuwa ndiyo sura ya kudumu ya mandhari ya Afrika. Swali kuwa je kulikuwepo mabadiliko yoyote kwenye mpangilio wa kukua kwa miji na athari zake na kuachwa kwa vifungo vya wakoloni.

### *Kukua kwa miji na athari zake tangu wakati wa uhuru*

Miaka 20 ya kwanza ya uhuru wa Afrika, hakukuwa mabadiliko yoyote ya msingi katika sababu na athari za watu wengi kuhama vijijini au katika tofauti kati ya kukua kwa miji na ajira mijini, au katika mpangilio wa maendeleo ya miji, licha ya kuwa macho na matukio yaliyotolewa uamuzi mkubwa zaidi wa kutayatua matatizo yaliyosababisha.

### *Mgogoro katika kilimo Afrika na kuongezeka kuondoka kwa wingi wakazi wa vijijini*

Miaka ya 1960, wasi wasi wa kuyumba kisiasa katika baadhi ya nchi za Afrika zilipuuzwa, kilimo katika Afrika kiliweza kumudu idadi ya watu wanaomiminika mijini, kwa kuwa na mabadiliko madogo toka nchi moja hadi nyingine.

Hata hivyo, tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970, ukame na mavuno duni yamesababisha kufuatana kwa miaka mibaya (1972-4, 1979-81) na njaa, hasa katika jangwa la Sahara na Sudani kuanzia Senegal hadi kwenye pembe ya Afrika. Kutofaa kwa njia za ukulima na kwa kiasi fulani sera za haraka za kilimo zilizopitishwa pia zinaeleza kwa nini, hadi kufikia1980, kulikuwepo nchi chache za Afrika ambazo chakula kilichukua asilimia 10 tu ya uagizaji toka nje. Mgogoro

katika kilimo ulikuwa mkali zaidi na ulikuwa kichocheo cha kuondoka kwa idadi kubwa ya watu vijijini kuliko kabla ya 1960. Huko Algeria, kwa mfano, idadi ya wakazi wa mijini iliongezeka mara mbili kati ya 1966 na 1977, toka 3700000 hadi 6800000; kiwango cha kupanuka kwa miji kilipanda toka asilimia 25 mwaka 1954 hadi asilimia 41 mwaka 1977, kwa kiwango cha kukua cha wastani wa asilimia 4.3 kati ya 1966 na 1977. Pia Cote d'Ivoire, matukio yanayofanana yanaweza kuonekana, kwa viwango vya kuongezeka vinavyotofautiana kati ya asilimia 6 hadi 9 kwa miji yenye wakazi 100000 na asilimia 11 kwa Abidjan.

Kitu kinachofafanua zaidi nafasi muhimu ya mgogoro wa vijijini ilikuwa kukua kwa miji katika Sahara ya Afrika, ambapo idadi ya wakazi wa mijini ilikuwa ikongezeka katika viwango kati ya asilimia 3.5 na 5, kama matokeo ya ziada kwenye mizania ya uhamaji kati ya miji na vijiji, kiwango ambacho kila wakati kinatoa ufùmbuzi unaoonekana kuwa wanahamia mijini. Watu wa Ziguinchor, mji wa zamani wa kikoloni na kibiashara huko Casamance (Senegal), uliongezeka mara mbili kati ya 1951 (wakazi 15700) na 1960 (wakazi 31000). Hata hivyo, kutokana na mgogoro kwenye sekta ya karanga, ambayo ilikua vibaya vibaya wakati mahitaji ya fedha yalipokuwa yanaongezeka. Hata hivyo mgogoro wa uchumi wa mijini uliotawaliwa na biashara na kukosa msingi wa viwanda, kiwango cha kukua kwa miji kilipanda haraka hadi kufikia asilimia 8 mwaka baada ya 1961. Idadi ya watu iliongezeka hadi 40000 mwaka 1966 na 70000 mwaka 1971. Ilikuwa na vijana waliohama kutoka vijijini na ilikuwa ni sehemu kubwa ya wafanyakazi wanaolipwa chini ya kiwango cha mshahara (kibarua). Iliwabidi kuishi kwa kutafuta malazi ambayo yalikuwa rahisi iwezekanavyo. Hali kama hiyo ilitokea Rufisque, ambako kulikuwa na kiwango cha kuongezeka cha asilimia 6-6.5 kwa mwaka tangu 1968-70. Miji mingi ya Afrika, ilikuwa na maendeleo ya pekee kwa kuwa na 'nyumba za wenyeji' baada ya uhuru.

## *Nyumba za kujijengea na maendeleo ya miji: kusambaa kwa vibanda*

Kuweko kwa makazi ya vibanda kuzunguka na ndani ya miji ya Afrika, ambayo sasa imekuwa jambo la kawaida, inaonekana kuongezeka baada ya 1960. Akielezea Bonde la Mathare, moja ya makazi maarufu ya vibanda vidogo vidogo huko Nairobi, Wa-Githumo alikuwa na haya ya kusema mwaka 1983:

> *Ni dhahiri kuwa, kuna vibanda vingi Nairobi; Bonde la Mathare ndilo kubwa kuliko yote na linawakilisha moja ya mifano halisi ya*

*vibanda ambavyo vimekuwa ngome ya umaskini, maendeleo duni na maonyesho mengine ya taabu za binadamu. Vibanda vya panya, vivuli, mazizi na aina nyingine za makazi ya aina ya vibanda huko Mathare aidha vimekodishwa au mwenye navyo anaishi humo, aidha halali au kinyume na sheria. Mamia ya maelfu ya familia zinaishi kwenye msongamano mkubwa, usio salama kwa afya na malazi ya kiwango cha chini sana.*

Maelezo kuhusu Bonde la Mathare hayajakutofautiana sana na yale ambayo V. S. Naipaul aliyatoa mwaka 1980 juu ya baadhi ya maeneo ya Kinshasa katika *The return of Eva Poem:*

*Ni wapi wazo la kuwajibika, jamii, taifa, huanza? Mji wa watu milioni mbili, na karibia kutokuwa na usafiri, bila viwanda (kuhudumia hiyo mitambo, iliyojengwa, kama ilivyo katika nchi nyingi sana 'zinazoendelea', njiani toka uwanja wa ndege kuelekea mji mkuu), mji uliojitenga kutoka sehemu nyingine ya nchi ...... Hautakiwi kufanya kazi; unaweza kuruhusiwa kujiangalia .... kunapokuwa na joto kali mifereji inanuka; wakati wa mvua barabara zinafurika. Na mji usiopangiliwa unazidi kupanuka ......*

Maelezo haya yanazua matatizo makuu ya sera za miji katika Afrika baada ya ukoloni, na vile vile yale ya suluhisho la mgogoro wa nyumba mijini linalosumbua wakazi wa mijini. Zaidi ya kipindi cha ukoloni, uchunguzi uliofanywa huko Cote d'Ivoire unaonyesha kuwa 'wahusika' wa nyumba za kujijengea hawakuwa wageni pekee bali pia uwiano mkubwa wa wakazi wa muda mrefu: wageni au wenyeji waliofilisiwa na migogoro ya uchumi, wasiokuwa na kazi, jamii na sababu nyingine, watu waliohusika na uchumi wa biashara na jamii mpya ya wanunuzi, walikuwa wanapatikana pale, wakiishi kwa ujira, mara nyingine kwa kuishi kwenye mabanda ya mbao au matakataka.

Kupambana na tatizo hili, mamlaka iikiuwa na taarifa ya suala hili mapema (angalia itikadi ya 'mwana maendeleo' katika hotuba rasmi mara tu baada ya uhuru). Hata hivyo, usuluhishi na sheria zinazoweza kuzifanya zitekelezeke zimechelewa sana. Wakala wa Mipango Miji na wachora ramani wa miji wamejitokeza na kuongezeka idadi miaka ya 1970 katika nchi nyingi za Afrika, angalau katika masuala hayo ambapo tawala za kikoloni, ambazo zilikuwa

zikijihusisha zaidi na miji mikubwa, hazikuacha chochote baada yao. Kufikia 1980, rasilimali chache sana iliyokuwa kwa ajili ya maendeleo haikuiwezesha serikali kufuatilia jambo ambalo linazidi kuimarika.

'Sekta isiyo rasmi', ambayo ndiyo njia pekee ya kuendelea kuishi katika miji ya Afrika, hasa kwa weusi, imekuwa njia kuu ya shughuli za kiuchumi za mjini kwa idadi kubwa ya watu - kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko sekta ya viwanda ilivyoweza kuwa. Uchunguzi wa kipengele hiki cha uchumi wa mjini ni wa siku za karibuni, lakini tayari unaonyesha mfano bora wa ubunifu ambao wakazi wengi wa mijini katika kontinenti wamelazimika kufanya ili kuishi katika miji ya Afrika ya sasa, mbali na uchumi wa viwanda ambao ulikuwa bado haujaendelea vya kutosha katika Afrika miaka ya 1980.

Si nchi zote katika kontinenti, wala si miji yote ya Afrika, ilikuwa kwenye hali ngumu inayolingana au iliyokuwa imeathirika kwa hali sawa. Kulikuwa na tofauti ndogo za kikanda. Kulikuwa na hali za kutofautiana miongoni mwa nchi hizo kwa kuwa na vipato vya juu kutokana na mafuta au bidhaa zitokanazo na kilimo, ambazo zilikuwa na uwezo wa kulipia maendeleo ya viwanda vyao na hivyo kuongeza kiwango cha ajira mijini, na nchi hizo ambazo zilitakiwa kupambana na mgogoro mkubwa zaidi wa kiuchumi na hivyo zilikuwa na uwezo mdogo mwaka 1980 wa kudhibiti vipengele vyote vya maendeleo ya uchumi. Lakini tofauti hizi zilikuwa za kiwango cha maendeleo duni kuliko tofauti zenyewe. Ingawa Afrika ilikuwa ikienda haraka katika ujenzi mkubwa zaidi wa miji mwaka 1980, kulikuwa na nchi chache sana katika kontinenti ambazo zingeweza kusemwa kuwa zenye maendeleo ya viwanda.

## Hitimisho

Kama tuliyosema hapo juu na ukilinganisha na kipindi kabla ya ukoloni, ilikuwa kipindi cha 'mapinduzi ya viwanda' katika Afrika, lazima ieleweke wazi kuwa yalikuwa mapinduzi ambayo yaliyakabiliana na vikwazo katika hali mbaya zaidi hasa kuanzia 1935 na kuendelea kutokana na hali mbaya ya kimataifa, udhibiti na ongezeko la athari za makazi iliyofanywa na mashirika ya kimataifa yaliyo katika bara yaliyozuia maendeleo ya viwanda, na kufanya hali goi goi iliyorithiwa kutoka kwenye serikali ya kutegemea wakoloni na kuendelezwa na kuvurugwa au makosa ya sera za baada ya ukoloni. Udogo wa vikwazo haukuwa sababu ya miji kukua haraka kuliko viwanda. Inaweza pia kuulizwa - iwapo kuna umuhimu kuendeleza maendeleo ya viwanda katika kontinenti ambalo haliwezi kujilisha lenyewe.

Bado maendeleo ya viwanda Afrika ni muhimu, hasa kwa ajli yake na kwa ajili ya dunia yote. Kwa ajili yake, humaanisha jinsi ya kuweka misingi kwa ajili ya uchumi unaojiendesha wenyewe na kujitosheleza yenyewe kwa rasilimali na teknolojia inayofaa kwa maendeleo yake ya kweli. Pia ni njia ya kuunda hali ambazo zitawezesha uandaaji na utumiaji rasilimali ya wafanyakazi kwa njia ifaayo zaidi na inayounganisha sekta za kilimo na viwanda.

Kwa sehemu nyingine ya dunia, suala ni kwamba, kwa kuweka udhibiti mkubwa zaidi, juu ya uwezo wake mkubwa, Afrika itumie rasilimali yake hiyo kunufaisha mataifa yote ya dunia kuliko kutekeleza malengo ya watu wachache au ya makampuni ya kimataifa; ukinzani kati ya 'uchumi usio huria' na 'uchumi wa kuendesha wenyewe' lazima uondolewe.

Swali kuwa ni kwa jinsi gani inawezekana kufanikisha hili kwa gharama ndogo zaidi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kuliko hivi sasa. Huenda jibu lipo kwenye:

(1) Ushirikiano dhahiri kati ya mataifa ya Afrika na kuongezeka kwa mfungamano wa huduma za viwanda na sera (mtazamo lazima uelekezwe zaidi kwenye eneo la bara kuliko pwani);
(2) Uchaguzi wa viwanda kwa ufahari (viwanda vikubwa vya magereza vimerekebishwa kutengeneza bidhaa kwa ajili ya kusafirisha nje ya Afrika);
(3) Vitega uchumi vilivyobuniwa ili kurekebisha uvumbuzi wa teknolojia kwa mahitaji halisi ya watu wa Afrika.

# 14 Mikakati Linganishi ya Ukombozi[1] wa Uchumi katika Afrika

Mara tu nchi zao zilipopata uhuru, serikali za Afrika kwa dhati zilikuwa na hamu ya kuboresha kiwango cha maisha ya watu wake kwa kuongeza mapato yao na kutoa hudumu muhimu za jamii na suhula za miundombinu. Serikali zote zilishawishika kuwa njia sahihi za kuleta mabadiliko ilikuwa kupitia upangaji wa uchumi. Hakika, kabla ya uhuru wa Afrika, maandishi juu ya maendeleo yalisababisha midahalo iliyohusu kupanga au kutopanga uchumi. Hata hivyo baada tu ya uhuru wa Afrika, midahalo hiyo ilishindwa kirahisi na wapanga mipango wa nchi zilizopata uhuru baada ya kutokomeza ukoloni ambazo zilikuja na mipango iliyowiana na mahitaji yaliyokuwapo ya maendeleo ya nchi na watu wake. Lakini mipango hiyo ambayo mara nyingi ilitayarishwa na wageni ikiwa na ujuzi mdogo wa nchi husika, hivyo ilikosa udhibiti wa kweli, kuungwa mkono kisiasa au uwezo wa utekelezwaji[2]. Na hivyo haishangazi kuwa katika kipindi cha mwongo wa kwanza, maamuzi katika eneo kubwa la mikakati ya maendeleo au itikadi kwa kawaida hayakuwa ni sehemu ya kazi ya wapanga mipango. Ni lazima tutazame mahali pengine ili kutekeleza mabadiliko ya dira ya mikakati mikuu. Hata hivyo ukiondoa nchi chache sana, ushahidi ni vigumu kupatikana wa mkakati ulio wazi na uliofungamana na kukomboa uchumi ukilinganishwa na ule wa ukombozi wa kisiasa ambao nchi zote za Kiafrika zinachangia na unatekelezwa bidii.

Bado, ilitakiwa kwa wazi kwa wote hata kutoka siku za mwanzo za uhuru kuwa Afrika ikienda mbele imeshikana mkono na uchumi wa kikoloni iliyourithi

[1] Tunasafiri kuondoa ukoloni kama kuvunja asasi za kikoloni na kupunguza udhibiti na nguvu za kigeni. Ondoaji wa ukoloni siyo zawadi toka kwa watawala wa kikoloni: inahitaji juhudi za wanaoonewa.

[2] G.K. Helleiner, 1972 uk 533

haitakuwa na mafanikio yo yote. Kwa hakika kama ukweli ungeelezwa mgogoro wa uchumi ulilolikumba bara la Afrika tangu nusu ya pili ya miaka ya 1970 imekuwa kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya kulimbikiza ya kuendelea na utendaji wa uchumi wa Afrika katika kiunzi cha uchumi ulioriithiwa kutoka utawala wa kikoloni: Kwa bahati mbaya imechukua miongo michache ya mwanzo baada ya uhuru kutambua kuwa kama Afrika itaendelea kunyofoa katika mfumo wa uchumi wa kikoloni; na ikiendelea kushindwa kufanikiwa kupenya kutoka uhandisi wa uchumi wa jamii na hivyo kuendelea kuwa sehemu tabaka la chini katika tabaka la uchumi wa kimataifa na nafasi yake ya kuwa chini ya tabaka kunaendelea kutishia kutokuwa imara.[3] Bila shaka, mikakati ifaayo ya ukombozi wa uchumi wa Afrika ni sharti muhimu sana kwa kufikia kiwango cha juu cha ukuaji na uanuwaishaji na kuongeza hatua za kujitegemea na kujiendeleza.

Kwa bahati mbaya, kutoka Afrika nzima na kwa wananchi wengi mageuzi ya haraka ya uchumi ambayo yalitarajiwa wakati wa uhuru hayajapatikana. Badala yake uchumi wa Afrika umetoka kwenye mgogoro mmoja hadi mwingine, mapinduzi ya kuchomoza matarajio yaliyapisha mapinduzi ya kukata tamaa yaliambatana na wimbi la mapinduzi ya kijeshi na ghasia za kisiasa kutoka sehemu mbalimbali za bora hili. Kwa nini nchi za Afrika umeshindwa kufikia ahadi yao ya uchumi wakati wa uhuru? Walikosea wapi? Kujibu maswali haya kisanyansi ni lazima kwanza kabisa tuanze kufanya uchambuzi wa mikakati ya kiuchumi iliyofuatwa na nchi huru za Afrika katika miaka ya 1960.

## Kuelekea Mkakati wa Kijamaa wa kuondoa ukoloni

Kama tulivyogusia, mipango ya maendeleo ya baada ya uhuru katika Afrika imeshindwa kuweka mkakati wa maendeleo uliofungamana au itikadi mara nyingi wamekazia juu ya uchumi mkubwa wa kisasa. Vigezo vya uchumi wa kisasa mamboleo ni hivi: kuongeza Pato la Ndani la Taifa (GDP); kuongoeza uwekezaji na uhamasishaji akiba; kutoa mtaji kwa ajili ya gharama za uendeshaji Jamii; kupanua huduma za jamii; msaada wa nje na uwekezaji binafsi wa nje na motisha ya kuwavutia wawekezaji. Mikakati mingi kati ya hiyo kwa uficho, kama siyo wazi iliidhinisha sera na mikakati ya uchumi wa kikoloni iliyorithiwa kuendelea. Kwa mfano, mpango wa kwanza wa maendeleo[4] wa cóte d'Ivoire baada ya uhuru

[3]. A.A. Mazrui, 1977, uk. 17-18
[4] Cóte d'Ivoire, serikali ya 1961

kwa kipindi cha 1960 - 1970 uliona ni muhimu na kuongoeza fedha za kigeni kwenye pembejeo kwa misingi kuwa raslimali za uwekezaji za taifa hazikutosheleza na kwamba uchumi wa nchi hiyo ulikosa utaalamu. Moja ya malengo makuu ya mpango lilikuwa ni kuanuwaisha mazao ya kilimo kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi, kwahiyo kukazia zaidi uchumi unaoegemea nje. Mpango uliipa serikali jukumu la msingi la kudhibiti mchakato wa maendeleo. Wakati modeli hii ya waivo ilionekana katika nchi nyingi za Afrika zilizopata uhuru karibuni. Makoloni mengi ya Kifaransa yalipiga hatua zaidi kwa kuimarisha uhusiano wa uchumi wao na Ufaransa. Kwa mfano wakati nchi nyingine za Afrika zilianzishwa asasi za fedha huru, nchi zote zilizokuwa makoloni ya Ufaransa ikiondoa Mali na Guinea zilibaki uhusiano wa fedha na Ufaransa katika kanda ya pamoja ya fedha. Kwa kulinganisha na mkakati wa maendeleo wa ukoloni mamboleo, nchi chache za Afrika mara baada ya uhuru zilishughulikia sera na programu ambazo zilifikiriwa zinaondoa ukoloni katika uchumi wao. Lakini nyingi ya nchi hizi zilihusisha kuondoa ukoloni wa uchumi na ari ya kuelekeza jamii zao kuelekea malengo ya *kijamaa*. Ingawaje neno Ujamaa lilipewa maana tofauti na sifa tofauti kama vile ujamaa wa Kiafrika,[5] Ujamaa wa kidemokrasia na ushirika,[6] 'Ujamaa mamboleo Desturi'[7] au 'Ujamaa wa kweli na hisia za pamoja[8] maudhui ya kijamii na kiuchumi yalilingana. Tofauti na nchi zilizofuata mkakati wa uchumi wa ukoloni mamboleo usio na upendeleo. Lengo la nchi hizi lilikuwa siyo tu kuongeza ubora wa maisha ya watu wake bali pia kufikia mbadiliko ya msingi kwa kuendeleza uzalishaji wa bidhaa za muhimu na kwa kufuata mkakati wa uagizaji mbadala wa mazao ya viwanda.

Moja ya alama za wazi za uzoefu wa ujamaa wa awali zilikuwa kukataa unyonyaji mkubwa wa nchi za kigeni au mali binafsi ukweli ni kuwa serikali mbalimbali zilikuwa na ari ya kusisitiza upatikanaji wa mataji mpya kiliko utaifishaji kama ubao wa kuchapia kwa ndoto zao za ujamaa. Lakini nchi moja iliyotofautiana kiwaziwazi kutoka mtazamo huu ilikuwa Mali. Wakati nchi kama Ghana ulikubali uchumi mchanganyiko kama hatua ya mpito katika ujenzi wa jamii ya kijamaa, Mali ilijiandaa kuweka chini ya udhibiti wa dola na ukiritimba moja kwa moja sekta nyingi za kisasa, hususan sekta ya biashara ya nje. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa mwelekeo wa Mali kwani kudhibiti biashara ya nje kulionekana kuwa ni zana muhimu katika kudhibiti ziada ya bidhaa zinazosafirishwa nje. Kufuatana na

[5] Ghana serikali ya 1964, uk. 15
[6] Mali, serikali ya nd, uk. 6
[7] Tunisia, serikali ya 1962, uk. 8
[8] Madagascar, Serikali ya 1964, uk. 9

nadharia ya uchumi ya Marx, utapanga mipango wa Mali waliona kampuni za biashara ya nje kuwa ni mfereji ambao husafirisha nje thamani ya ziada. Wakati huo huo nchi zilizokuwa makoloni ya Ufaransa zilisaini mkataba dhamana ya fedha na hazini ya Ufaransa wa kuwa na fedha za pamoja. Mali ilianzisha fedha zake yenywe zilizoitwa Farnga ya Mali (mali franc).

Algeria, baada ya uhuru mwaka 1962, kufuatia vita virefu vya ukombozi, na vya kumwaga damu nayo ilichagua njia ya kijamaa kwa maendeleo yake. Kwa maneno mengine Kiongozi wa ukombozi wa Algeria na waziri mkuu wa kwanza, Ben Bella alisema:

> Tutafuta uchanganuzi wa uchumi wa Marx kwa sababu tunafikiri ndiyo wenye thamani tu kwa maendeleo ya nchi yetu, lakini bila kuunga mkono itikadi yake, kwa sababu kitendo chetu kinaongozwa na Waelgeria ambao ni Waislamu na Waarabu.[9]

Kwa njia moja kuchagua njia hii Algeria huru ililazimika kwa kuwa nchi ilikuwa inakabiliwa na utupu uliosababishwa na kuhama kwa wazungu ambao walitelekeza mashamba, viwanda na majumba yao. Mali iliyotelezekwa ilichukuliwa na Waalgeria vibarua wa mashamba hayo. Hii ikawa sifa ya pekee ya mfumo wa uchumi wa Algeria. Sekta ya Kilimo iliyojisimamia yenyewe. Mashamba hayo yaliyojisimamia yenyewe yaligeuzwa na kuwa mashirika ya pamoja yaliyoongozwa na baraza la wafanyakazi ambalo liliwachagua viongozi wake. Umilikaji wa mashamba hayo ulirasimishwa na utaifishaji ambao ulihusisha kwa vitendo mashamba yote yaliyokuwa ya Wazungu au karibu hekta milioni 2.3 zilizokuwa zinazalisha asilimia 65 ya nafaka. Mchakato wa utifishaji ulipanuliwa hadi kwenye sekta za uzalishaji viwandani, migodi na mafuta. Hivyo mwishoni mwa miaka ya 1960 sekta ya umma ukiondoa viwanda vinavyojiendesha vyenywe iliwakilisha zaidi ya theluthi moja ya mazao ya viwandani.

Aina hizi mbalimbali za ujamaa zina malengo mengi nayo ni:

(1) Kuondoa ukoloni wa kiuchumi;
(2) Dola kuingilia na kusambaa kote katika maendeleo na udhibiti wa uchumi;

[9] Imetafririwa kutoka Le Monde, 23 Januari 1965; hutoba iliyotolewa kwa Union générale des travailleurs algériens.

(3) Kupigania usawa kiuchumi nafasi sawa za kijamii; na
(4) Kuwekea kikomo majukumu ya sekta binafsi na uwekezaji na mali binafsi.

Lakini katika hoja ya mwisho, kulikuwa na tabia ya kigeugeu kwa baadhi ya serikali. Serikali nyingi haikupenda kukomesha mali binafsi na uwekezaji binafsi. Serikali hizo zilipendelea kudhibiti na kuanisha juhudi za sekta binafsi na zile za sekta ya umma ili kufikia malengo ya kijamii na kiuchumi. Kama ambavyo *Mpango wa Maendeleo wa Miaka Saba wa Ghana 1963/64 - 1969/70* ulivyoweka wazi, 'pendekezo lolote linalodai kuwa sekta ya dola na binafsi katika uchumi mmoja haziwezi kupatana halikubaliki. Sera za Ghana zitaundwa ili kupata mchango wa hali ya juu kutoka kila sekta kuelekea ukuaji wa uchumi kwa ujumla.[10]

Katika Tanzania Ujamaa ulipewa umuhimu mkubwa kama msingi wa kuutokomeza umaskini, kupunguza utegemezi wa nje na kupanga kimsingi uzalishaji na mahusiano ya kijamii kwa jamii ya Watanzania. Kuna ukweli kuwa Tanzania baada ya uhuru mwaka 1961 ilifuata mkakati wa maendeleo usio na upendeleo (liberal) ambao ulikuwa unafuatwa na nchi nyingine za Afrika, kukiwa na marekebisho kidogo katika dhamira hiyo. Ilisisitiza uzalishaji kwa ajili ya kusafirisha nchi za nje.

Ilitafuta kwa bidii pembejeo muhimu kutoka nje, hususan misaada ya kigeni, na ilikazia katika upanuzi wa haraka wa kiundo mbinu. Lakini kinyume na nchi nyingine za Afrika, Tanzania ilianza kueneza itikadi ya kujitegemea. Hata hivyo, hadi wakati wa Azimio la Arusha la mwaka 1967, Tanzania ilikuwa inafuata njia iliyofuatwa na nchi nyingine za Afrika. Joel Samoff kwa ufupi na uwazi anasema:

> Kwa wajamaa ilikuwa wazi kuwa Tanzania ilifuata njia ya nchi nyingine za Kiafrika. Kulikuwa na shule na hospitali nyingi zaidi, nafasi za juu kadhaa zilipewa waafrika, kulikuwa na mwazo mdogo wa viwanda, mara kwa mara kima cha chini cha mshahara kiliongezwa na uchumi ukapanda. Lakini kulikuwa na utegemezi na mtazamo wa nje uliorithiwa wa siasa ya uchumi ya Tanzania. Uchanganuzi wa kushindwa kwa mfumo usiopendelea upande wo wote ndio uliosababisha kuundwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967[11].Hivyo kushindwa kwa mfumo usiopendelea uliongoza sera kutoka mwaka 1961 hadi 1967

[10] Ghana, Serikali ya, 1964, uk. 3.
[11] J. Samoff, 1981, uk. 289

kulisaidia kuuweka wazi mfumo wa Ujamaa. Hii iliurasimisha ujamaa ulioendea kote na mfuatano wa mabadiliko ya kiasasi. Mfumo wa chama kimoja ulikubaliwa rasmi pamoja na ahadi za kuongeza demokrasia ya ushiriki ndani ya kiunzi kipya. Mabali na yote, mkakati wa maendeleo kimsingi ukatangazwa rasmi. Sifa zake kuu ni kutaifisha asasi kuu za uchumi, hususan mabenki, biashara ya bima, biashara ya nje, makampuni ya kutengeneza bidhaa na mashamba makubwa, ufinyaji wa ulaji wa mabepari wenye utajiri mkubwa kwa kuwawekea kanuni ya uingizaji bidhaa kufuatana na ongezeko la kodi uondoaji ukoloni katika mtaala wa shule, kutilia maanani uchumi anuwai na tasnia, na ahadi za sera za kujitegemea zilitangazwa sana.[12]

Lakini kitu cha maana zaidi katika Ujamaa mpya wa Tanzania ni ile itikadi yake ya ujamaa vijijini ambayo misingi yake ni sera ya kujitegemea, inayotilia maanani kundi na kupeana msaada wa hiari kinyume na maadili ya kibepari ya ubinafsi na unyonyaji. Maadili ya uongozi yalisisitiza maadili mema, kufanya kazi kwa nguvu kushikilia maadili, kujikana, na kujitoa kwa huduma ya jumuiya na kukataza viongozi kujihusisha na biashara binafsi na kuwa na nyumba zaidi ya moja. Kwa hatua hivyo, mapato kutokana na kodi ya pango yaliondolewa na hatua za utaifishaji zilienea hata, kwa biashara ndogo ndogo. Kufikia katikati ya mwaka 1980 zaidi ya asilimia 80 ya shughuli za uchumi zilikuwa chini ya sekta ya umma. Lakini pamoja na msimamo wake mkali daima Tanzania imeendelea kutegemea misaada toka nje kwa ajili ya maendeleo yake, uondoaji wa ukoloni wa kiuchumi umeendelea kuuepuka. Ujamaa umekuwa mwanga unaoonekana. Lakini la makini zaidi kwa miaka mingi uchumi umeacha kukua; kwa miaka kadhaa umesimama na mara kadha hujitokea kufikia kiwango cha hasi katika ukuaji. Madhara ya kulimbikiza yote haya yameifanya Tanzania kuainishwa na Umoja wa Matifa kuwa ni nchi maskini sana kati ya nchi zinazoendelea. Ni moja kati ya nchi 27 maskini sana katika Afrika. Hata hivyo kwa kejeli mwaka 1977 Reginald Green alidai kuwa "kipindi cha mpito wa ujamaa katika Tanzania tunaweza kusema kipo karibu kukamilika.[13]

Huko Senegali, Ujamaa wa Kiafrika ulioanzishwa na Waziri Mkuu Mamadou Dia (1957-62) na Leópold Senghor ulihimiza katika kujenga jamii ya kijamaa

[12] Tazama J.K. Nyerere, 1968a and also J. Samoff, 1981, uk. 289

[13] R.H. Green, 1977, uk. 24


iliyojikita katika maadili ya kijima kwa kuendeleza vyama vya ushirika na kwa kujenga upya vijiji vya Senegali kuwa jumuiya za vijijini zinazojitawala zenyewe. Hivyo wote wawili Dia na Senghor waliona kwa ushirika wenye majukumu mengi vijijini utafanywa kitengo cha msingi cha uchumi wa jamii za kijamaa za wakulima. Hakuna haja ya kusema, Senegali muda wote umekuwa mfano mzuri wa uchumi tegemezi. Pamoja na zaidi ya miaka 25 tangu kujitawala, biashara ya nje kwa kiasi kikubwa ipo chini ya Ufaransa, ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikiipa Senegali zaidi ya theluthi mbili za mtaji wa maendeleo ya umma, na karibu mahitaji yake yote ya ufundi na fedha. Wawekezaji wa Ufaransa wanatoa zaidi ya sehemu 4/5 ya mtaji binafsi ambapo miaka mingi hazina ya Ufaransa ilikuwa ikilipia Senegali nakisi ya biashara ya nje.

Hata hivyo, Ujamaa wa Kiafrika wa Senegali ulikuwa na athari kubwa. Kwanza ulikatisha tamaa uibukaji wa mabepari wakubwa katika vijiji na umesukuma mifumo ya maendeleo ya ushirika vijijini. Pili, Ujamaa wa Kiafrika umekuwa ukitumika kuhalalisha uingiaji wa serikali kwa nguvu katika kurekebisha na kudhibiti sekta muhimu za uchumi wa Senegali. Tatu, Ujamaa wa Senegali ulikaribisha mtaji wa nje na mtaji binafsi. Hii haishangazi kwa kuwa Senghor alikuwa wakili mkuu wa mazungumzo ya Uzungu -Uafrika, au Uzungu-Uarabu-Uafrika. Hivyo ilikuwa rahisi kwa serikali yake ya kijamaa kushirikiana na mtaji wa nje na sekta binafsi ya Senegali. Na haikushangaza kuona uchumi wa nchi hiyo ukiendelea kuwa tegemezi.

## Mikatati ya Kisekta ya Kuondoa Ukoloni katika Uchumi

Uchambuzi wa kisekta wa mikakati na sera za maendeleo maikro iliyotekelezwa mara tu baada ya uhuru na serikali za nchi za Afrika utatupa mwangaza zaidi wa juhudi zilizofanya za ukombozi wa kiuchumi. Msisitizo wetu utakuwa kwenye sekta mbili za uzalishaji wa kilimo na viwanda, na sera ya uzawa ya kuifanya kuwa sekta ya kisasa ya uchumi wa waafrika chini ya udhibiti wa waafrika.

Wakati wa ukoloni katika Afrika modeli mbili za muundo wa kilimo zilitumika. Muundo wa kwanza ni wa kilimo cha jadi cha kujikimu ambao ulizingatia vyote, kama njia ya maisha na pia uchumi ambao kuuza mazao ilikuwa ni bahati mbaya kutegemea kupatikana kwa ziada zinazoweza kupelekwa sokoni na mahitaji ya fedha kununulia bidhaa zilizotoka nje na kodi iliyowekwa na serikali. Muundo wa pili ni kilimo cha kisasa cha biashara ambacho kilikuwa kinahusu uchumi wa fedha tu. Katika nchi nyingine za Afrika aina hizo mbili za kilimo ziliwakilishwa




*Kielelezo 14.1 Mwelekeo wa uzalishaji wa chakula kwa kila mmoja: Dunia, nchi zilizooendelea kidogo na Afrika (msingi 1974-76) Chanzo: FAO, Production Yearbook, FAO, ROME, 1982)*

TABLE 14.1 *Average annual growth rates of total public expenditure for all sectors and for the agricultural sector, at constant prices*

| *Area of Africa* | *All sectors* | | | | | *Agriculture* | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *1979* | *1980* | *1981* | *1982* | *Average 1979–82* | *1979* | *1980* | *1981* | *1982* | *Average 1979–82* |
| North | 6.1 | 4.0 | −6.0 | 3.6 | 1.8 | −6.3 | 2.2 | −0.3 | −5.8 | −2.6 |
| West | 9.1 | −15.7 | −18.4 | −1.7 | −7.3 | −10.4 | 18.9 | −5.4 | 8.0 | 2.1 |
| Central West | 20.3 | −3.0 | 3.1 | −8.8 | 2.4 | 68.7 | −7.5 | −34.2 | −34.5 | −9.5 |
| Central | – | – | – | – | – | −13.5 | −48.6 | 10.0 | 39.1 | −0.2 |
| East and Southern | 14.5 | −3.9 | −11.0 | −18.7 | −5.5 | 27.0 | 4.9 | −1.1 | −30.7 | −2.2 |

*Tanbihi : Data katika jedwali ni kutoka nchi 24 tu.*

*Chanzo : FAO, 1983.*

na kilimo.[15] Kwa hakika kielelezo 14.1 kinaonyesha kwa grafu uzalishaji wa chakula kwa kila mtu ulivyoendelea kushuka katika miaka yote ya 1970 na miaka ya mwanzo ya 1980. Utendaji mbaya wa sekta ya chakula ni dalili ya utendaji wote wa sekta ya kilimo kwa ujumla kuwa mbaya. Kwa ujumla sekta hii imekuwa nyuma na utendaji wake umeendelea kuwa mbaya tangu uhuru. Kwa mfano kati ya mwaka 1971 na 1980 uzalishaji katika kilimo uliongezeka kila mwaka kwa wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na asilimia 2.1 miaka ya 1960. Sababu za kushuka huku kwa uzazalishaji zipo wazi katika jedwali 14.1. Serikali za nchi za Afrika hazitekelezi kwa vitendo yale wanayosema kuhusu mikakati ya maendeleo ya kilimo kwa kukipangia raslimali ya umma ya kutosha Data iliyopo inaonyesha kuwa kwa misingi ya kila mtu, matumizi ya serikali katika kilimo yameshuka katika kanda ndogo zote, ushukaji mkubwa ukiwa katika kanda ya Afrika ya kati ambayo pia ina kiwango kidogo zaidi cha mtiririko wa mtaji wa ndani kwa kila mkulima.

Mbaya zaidi ni ukweli kuwa rasilimali kidogo sana zilizopo kwa ajili ya uwekezaji kwenye kilimo zimekuwa zikitumika vibaya kiubadhirifu. Kuna kutegemea sana uwekezaji wa mtaji mkubwa na kuweka mtaji mkubwa sana katika matumizi ya mitambo. Miradi mingi ya umma imejijengea ustawi wa gharama sana na kujali kidogo sana uwezo na mahitaji ya mkulima wa kiafrika. Ingawaje kati ya asilimia 80 na 90 ya wazalishaji wa kilimo ni wakulima wadogo wadogo, hususan kati ya hao, wanaolima mazao ya chakula wengi wao wakiwa wanawake hata hivyo hawapati pembejeo za kilimo za kutosha.

Upungufu wa huduma za kilimo vijijini unaonekana wazi ; aina za kisasa za mbegu, mbolea na dawa za kuulia wadudu huwa hazipatikani kwa urahisi. Barabara za vijijini na huduma nyingi za miundombinu hazitoshelezi. Ukweli ni kuwa hakuna huduma zifaazo na za uhakika za bohari na/au za uhifadhi ya mazao ya nafaka ; kuna juhudi kidogo za kimfumo zinazoshughulika na kutoa chakula kutoka vijijini kuenda mijini au kutoka kijiji kimoja kwenda kijiji kingine. Hii kiuwiano ni kati ya asilimia 20 na 45 ya chakula kinachozalishwa kinaharibika kutokana na kushindwa kuyafikia masoko, na sera ya bei ya mkulima kwa kuifanya bei kuwa ndogo na hivyo kupunguza mapato ya mkulima. Hii ina athari mbaya kwa tija ya kilimo.

Mpango wa utekelezaji wa Lagos (*Lagos Plan of Action*) ulisisitizia utaratibu wa kupuuza wakulima wadogo wadogo kwa kuelezea kuwa mzizi wa tatizo la

JEDWALI 14.1 *Wastani wa kiwango cha ukuaji kwa mwaka ya jumla ya matumizi ya serikali kwa sekta zote na kwa sekta ya kilimo kwa bei isiyobadilika*

| Eneo la Afrika | Sekta zote | | | | | Kilimo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | wastani 1979-82 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | wastani |
| Kaskazini | 6.1 | 4.0 | -6.0 | 3.6 | 1.8 | -6.3 | 2.2 | - 0.3 | -5.8 | -2.6 |
| Magharibi | 9.1 | 15.7 | 18.4 | -1.7 | -7.3 | -10.4 | 18.9 | -5.4 | 8.0 | -2.1 |
| Magharibi Kati | 20.3 | -3.0 | -3.1 | -8.8 | 2.4 | 68.7 | -7.5 | -34.2 | 34.5 | -9.5 |
| Kati | - | - | - | - | - | 13.5 | 48.6 | 10.0 | 39.1 | -0.2 |
| Mashariki na Kusini | 14.5 | -3.9 | -11.0 | -18.7 | -5.5 | 27.0 | 4.9 | -1.1 | -30.7 | -2.2 |

Tanbihi : *Data katika jedwali ni kutoka nchi 24 tu.*

Chanzo : FAO, 1983.

na kilimo cha waafrika, ambacho kilikuwa cha zadi na kujikimu zaidi na kilimo kisicho cha waafrika ambacho kilitawaliwa na jumuiya ya wataalam walowezi ambacho kulizalisha kwa msingi wa mashamba makubwa kwa ajili ya kusafirisha nje. Katika sehemu nyingine hususani Afrika Magharibi aina hizi mbili za kilimo hazina tofauti kubwa kwani wakulima wadogo wadogo nao walizalisha mazao kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Katika hali zote, uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje ulipendelewa na serikali za kikoloni kwa sababu ilikuwa ni chanzo muhimu cha mapato ya fedha za kigeni na mapato ya serikali. Hata hivi leo, katika nchi ambazo hazina mafuta wala madini ya kuuza nje, mazao ya kilimo yanafikia kiasi cha asilimia 80 katika mapato ya fedha za kigeni na mapato ya serikali. Pembejeo za kiufundi kama mbegu bora, mbolea, huduma za mikopo, misaada ya utafiti na huduma vijijini hazijupatina kwa wakulima wa mazao ya chakula. Karibu mazao yote ya kilimo cha kisasa yaliuzwa kupia ushirika wa kilimo. Wakati wa miaka ya vita kuu ya pili na miaka baada tu ya vita, ushirika wa kilimo ulibadilishwa na kuwa bodi za masoko au caisses de stabilisation katika nchi zilizozungumza Kifaransa. Bodi hizo zilipewa uwezo kuwa wanunuzi wa wasafirishaji pekee wa bidhaa zikiwa na mmlaka ya kupanga bei ya mkulima kila msimu wa kilimo. Katika makoloni ya walowezi katika mashariki na kusini mwa Afrika, sera ya kikoloni zilipiga marufuku wakulima wenyeji walowezi weupe katika ushindani. Kwa hakika misingi ya utegemezi mkubwa wa nje kwa uchumi wa Afrika umelalia katika mwainisho huu.

mkubwa juu ya mapato ya fedha za kigeni. Kama alivyoandika Ali Mazrui, juju mpya imerusha laana [kwa Afrika] kutia kiinimacho malengo ikiamsha uchoyo, yenye kustajabisha wenye uchu. Juju mpya inaitwa fedha za kigeni, kupatikana kwa sarafu inayolinganishwa kama namna ya uwezo wa kimataifa.[14] La kusikitisha ni kuwa katika hali hiyo inashangaza kuwa Afrika huru ilifuata kwa nguvu nyingi kuliko kabla ya hapo maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya kuuza nje ya nchi. Jitihada kidogo ziliendelea kutolewa kwa uzalishaji wa chakula. Hivyo kati ya mwaka 1960 na 1965 wakati uzalishaji wa mazao ya kuuza nje ulifikia nyongeza ya asilimia 23.3, mazao ya chakula iliongezeka na kufikia asilimia 6.7 tu. Tangu mwanzoni mwa uhuru, serikali za Afrika zilionekana kudharau ushauri kwa njia ya uhakika zaidi kuinua viwanda........ni kuweka misingi inayotakiwa kwa kuchukua hatua kali za kuinua uzalishaji wa chakula kwa kila mtu anayeshughulika

[14] A.A. Mazrui, 1980a, uk. 65.

chakula katika Afrika ni kwa serikali za nchi hizo hazikutoa kipaumbele kinachotakiwa katika kilimo katika kukipangia raslimali na kutoa umakinifu unaofaa kwa sera za kuinua tija na kuboresha maisha katika vijiji.[16] Mpango uliongezea haya :

Kwa kuboresha wa hali ya chakula katika Afrika, sharti muhimu ni kuwa na nia kubwa kisiasa na kwa kupeleka rasilimali kubwa katika kilimo, kufanya mabadiliko ya lazima kufanya mfumo wa kijamii, kutumia sera zitakazowahimiza wakulima wadogo na wanachama wa ushirika katika kilimo kufikia kiwango cha juu cha tija, na kuweka vyombo vifaavyo vya kuanzisha programu zifaazo na utekelezaji wake.[17] Kwa sekta ya viwanda, suala la *kuwa na viwanda ilionekana na nchi za Afrika zilizopata uhuru kama ndiyo zana kuu ya kuondokana na ukoloni kiuchumi*. Shughuli za utengenezaji wa vitu ulikatishwa tamaa na serikali za kikoloni zilizochukulia kuwa jukumu la uchumi wa Afrika kuwa ni kusaidia uchumi za nchi tawala ambako nchi za Afrika zilitoa mali ghafi ya bidhaa zao walizotengeneza kama inavyoonyesha katika jedwali 14.2 shughuli za utengenezaji bidhaa wakati wa uhuru mwaka 1960 zilikuwa asilimia 7.6 ya Pato la Ndani la Taifa ukilinganisha na asilimia 12 huko Asia kusini mashariki, asilimia 22 huko Latini Amerika. Shughuli za viwanda kabla ya uhuru zilijikita katika usindikaji na nusu usindikaji wa bidhaa za kilimo na misitu na madini, na kwa uzalishaji wa bidhaa nyepesi kwa ajili ya mlaji. Hivyo, baada ya uhuru, serikali za Afrika zilikuwa macho zaidi katika kuendeleza tasnia ya utengenezaji bidhaa.

Hata hivyo, ruwaza ya jumla ya uanzishaji wa viwanda vya utengenezaji bidhaa ulikuwa bila mpango maalumu wa uunganishaji wa sekta zote au na sekta zingine za uchumi. Mikakati ifaayo kuifanya sekta ya viwanda ichangie kikamilifu kwenye maendeleo ya uchumi na kijamii zilikosekana. Kutoka hapo awali, viwanda vilifanywa kuwa ubia na viwanda vya nje au chini ya umiliki kamili wa wageni ambao waliviendesha kwa faida yao wenyewe. Hatimaye pembejeo zote na malighafi ziliingizwa toka nje. Hatimaye ujengaji wa viwanda ulifungua mlango mwingine wa utegemezi katika Afrika. Badala ya kuwa chanzo kikubwa cha akiba ya fedha za kigeni na mapato, viwanda vikawa ndiyo chanzo kikuu cha fedha za kigeni kuvuja. Ingawaje kama tulivyoona katika jedwali: 14.3, sekta ya utengenezaji bidhaa iliendelea haraka kuliko sekta nyingine yoyote isipokuwa madini, biashara na

[16] Umoja wa Nchi Huru za Afrika, 1981

[17] Kama juu, uk. 11 aya ya 18.

TABLE 14.2

| Nchi za | kilimo | viwanda | umeme | madini | ujenzi | biashara | usafir |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zinazosafirisha | | | | | | | |
| Mafuta kwa wingi | | | | | | | |
| 1960 | | | | | | | |
| 1970 | 43.1 | 5.5 | 1.3 | 3.8 | 8.4 | 19.3 | 5.5 |
| 1980 | 30.2 | 5.2 | 0.7 | 18.5 | 6.3 | 24.8 | 3.2 |
| | 16.3 | 6.4 | 0.9 | 8.6 | 14.3 | 24.2 | 6.6 |
| Zisizosafirisha | | | | | | | |
| Mafuta | | | | | | | |
| 1960 | 42.4 | 8.6 | 1.4 | 4.6 | 4.0 | 15.5 | 5.9 |
| 1970 | 35.1 | 11.7 | 1.4 | 5.4 | 4.7 | 17.7 | 6.2 |
| 1980 | 27.7 | 12.4 | 1.7 | 5.1 | 5.4 | 19.2 | 7.2 |
| Zenye maendeleo | | | | | | | |
| Kidogo | | | | | | | |
| 1960 | | | | | | | |
| 1970 | 59.2 | 5.3 | 1.4 | 0.8 | 4.6 | 15.4 | 4.3 |
| 1980 | 50.6 | 8.7 | 1.1 | 0.9 | 3.8 | 17.5 | 5.0 |
| | 44.2 | 8.1 | 1.3 | 1.3 | 4.2 | 17.7 | 6.9 |
| Afrika | | | | | | | |
| Ziazoendelea | | | | | | | |
| 1960 | 42.6 | 7.6 | 1.3 | 4.4 | 5.4 | 16.7 | 5.8 |
| 1970 | 33.4 | 9.5 | 1.2 | 9.8 | 5.2 | 20.1 | 5.2 |
| 1980 | 22.8 | 9.8 | 1.3 | 6.6 | 9.3 | 21.4 | 6.9 |

*Mikakati linganishi ya kuondoa ukoloni wa uchumi Afrika*
*JEDWALI 14.2 Ulinganishi wa pato la Ndani kwa bei za 1970 zisizobadilika katika asilimia*

| Nchi | Kilimo | viwanda | umeme | madini | ujenzi | biashara | usafiri | utawala | mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zinazosafirisha Mafuta kwa wingi | | | | | | | | | |
| 1960 | 43.1 | 5.5 | 1.3 | 3.8 | 8.4 | 19.3 | 5.5 | 7.5 | 5.6 |
| 1970 | 30.2 | 5.2 | 0.7 | 18.5 | 6.3 | 24.8 | 3.2 | 8.3 | 2.8 |
| 1980 | 16.3 | 6.4 | 0.9 | 8.6 | 14.3 | 24.2 | 6.6 | 19.3 | 3.2 |
| Zisizosafirisha Mafuta | | | | | | | | | |
| 1960 | 42.4 | 8.6 | 1.4 | 4.6 | 4.0 | 15.5 | 5.9 | 8.9 | 8.7 |
| 1970 | 35.1 | 11.7 | 1.4 | 5.4 | 4.7 | 17.7 | 6.2 | 9.4 | 8.4 |
| 1980 | 27.7 | 12.4 | 1.7 | 5.1 | 5.4 | 19.2 | 7.2 | 12.8 | 8.5 |
| Zenye Maendeleo Kidogo | | | | | | | | | |
| 1960 | 59.2 | 5.3 | 1.4 | 0.8 | 4.6 | 15.4 | 4.3 | 7.8 | 1.2 |
| 1970 | 50.6 | 8.7 | 1.1 | 0.9 | 3.8 | 17.5 | 5.0 | 7.0 | 5.4 |
| 1980 | 44.2 | 8.1 | 1.3 | 1.3 | 4.2 | 17.7 | 6.9 | 10.0 | 6.3 |
| Afrika Zinazoendelea | | | | | | | | | |
| 1960 | 42.6 | 7.6 | 1.3 | 4.4 | 5.4 | 16.7 | 5.8 | 8.4 | 7.8 |
| 1970 | 33.4 | 9.5 | 1.2 | 9.8 | 5.2 | 20.1 | 5.2 | 9.0 | 6.6 |
| 1980 | 22.8 | 9.8 | 1.3 | 6.6 | 9.3 | 21.4 | 6.9 | 15.7 | 6.2 |

*TANBIHI: Ukuaji wa kisekta kwa 1960-70, data ilikuwa ya nchi 39 za Afrika, ambapo* kisekta 1970-80 kwa ujumla ukuaji wa *Pato la Ndani data yake ni ya kutoka nchi 50 zinazoendelea za Afrika.*
*Chanzo:* ECA sekretarieti.

utawala wa umma katika mwaka 1960 na zaidi kidogo kuliko Pato la Ndani katika miaka ya 1970, sekta ya viwanda hata mpaka leo bado ni sehemu ya wageni na ni sehemu ya mijini iliyozungukwa na bahari kuu ya vijijini isiyo na maendeleo. Kuhusiana na bidhaa za viwandani, Afrika ilikuwa sehemu ya ongezeko la thamani ya asilimia 0.9 tu mwaka 1980 ililinganishwa na sehemu ya asilimia 2.7 na 6.0 kwa Asia kusini mashariki na Latini - Amerika kwa mfuatano huo.
Kufikia mwaka 1980 Afrika ilikuwa kanda ya mwisho katika viwanda duniani. Kama inavyoonyeshwa na Tume ya Uchumi Afrika na utafiti a awali wa mwelekeo wa maendeleo ya Afrika 1983-2008 (*ECA and Africa's Development 1983-2008: A Preliminary Perspective study*).

Bali kwa uzalishaji mdogo wa bidhaa zinazohitajika haraka, sekta na sifa ya viwanda vidogo vya kuzalisha bidhaa za mlaji na kwa usindikaji wenye kiwango kidogo na usindikaji nusu wa madini na malighafi za kilimo, hususan kwa ajili ya kusafirishwa nje. Zaidi ya hayo muundo wa uzalishaji uliopo una msingi wa Kiwanda vidogo vikiwa na ujuzi mdgo wa uchumi viwanda vikubwa ni kwa hatua za mwanzo tu na vimekuwapo katika nchi chache sana. Hivyo uzalishaji wa bidhaa mtaji umekuwa mdogo na matokeo yake Afrika imebakia kuwa nchi mwagizaji mkuu wa bidhaa mtaji na zana zinazotoka nje pamoja na mashine zinazofikia kiwango cha asilimia 35 ya uwekezaji wote wa mwaka katika kanda.[18]

Hata hivyo hali za Afrika baada ya uhuru ziliona kuwa ujengaji wa viwanda ulikuwa na malengo makuu sita nayo ni:

(1) kutosheleza mahitaji muhimu ya watu wote;
(2) kutumia rasilimali asili za nchi.
(3) kuanzisha nafasi za kazi
(4) kuanzisha msingi wa kuendeleza sekta nyingine za uchumi.
(5) kuanzisha msingi wa kuchukua na kukuza maendeleo ya kiteknolojia.
(6) kuifanya jamii iwe ya kisasa.[19]

Cha kusikitisha hakuna hata moja kati ya haya limetekelezwa katika kipindi cha miongo miwili au mitatu iliyopita. Hivyo kwa sababu ya kutofautiana sana kwa viwanda katika Afrika, kuna mahitaji ya ruzuku yasiyoisha kwa namna moja au nyingine, utengemezi uliopo kwa nchi nyingi kati ya hizo juu ya uagizaji nje wa

[18] Tume ya Uchumi Afrika 1983, uk. 11
[19] Umoja wa Nchi Huru za Afrika, 1981, uk. 20

JEDWALI 14.3 Wastani wa Ukuaji kwa mwaka wa bei 1970 katika asilimia

| Nchi | kilimo | viwanda | umeme | madini | ujenzi | biashara | usafiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nchi zinazosarisha mafuta kwa wingi | | | | | | | |
| 1960-70 | | | | | | | |
| 1970-80 | | | | | | | |
| 1960-80 | 5.6 | 8.8 | 3.1 | 28.3 | 6.3 | 12.2 | 3.5 |
| | 1.4 | 10.1 | 6.6 | 1.1 | 11.4 | 5.8 | 8.3 |
| Zisizosafirisha Mafuta | | | | | | | |
| 1960-70 | 6.5 | 12.0 | 8.9 | 10.2 | 10.2 | 10.0 | 9.0 |
| 1970-80 | 1.2 | 4.2 | 5.4 | 3.1 | 5.1 | 4.4 | 5.1 |
| 1960-80 | | | | | | | |
| Zenye maendeleo kidogo | | | | | | | |
| 1960-70 | | | | | | | |
| 1970-80 | -3.6 | 15.4 | 8.9 | 5.2 | 12.6 | 12.2 | 9.9 |
| 1960-80 | 1.7 | 2.4 | 10.5 | 7.3 | 17.1 | 7.6 | 16.1 |
| Afrika zinazoendelea | | | | | | | |
| 1960-70 | 3.7 | 7.1 | 4.6 | 17.3 | 6.3 | 9.1 | 5.1 |
| 1970-80 | 1.3 | 5.5 | 4.2 | 7.3 | 4.1 | 3.2 | 6.4 |
| 1960-80 | | | | | | | |

*JEDWALI 14.3 Wastani wa Ukuaji kwa mwaka wa bei 1970 katika asilimia*

| Nchi | kilimo | viwanda | umeme | madini | ujenzi | biashara | usafiri | utawala | Mengineyo | (GDP) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nchi zinazosafirisha mafuta kwa wingi | | | | | | | | | | |
| 1960-70 | | | | | | | | | | |
| 1970-80 | 5.6 | 8.8 | 3.1 | 28.3 | 6.3 | 12.2 | 3.5 | 10.6 | 1.8 | 9.4 |
| 1960-80 | 1.4 | 10.1 | 6.6 | 1.1 | 11.4 | 5.8 | 8.3 | 11.2 | 4.8 | 7.9 |
| | | | | | | | | | | 8.7 |
| Zisizosafirisha Mafuta | | | | | | | | | | |
| 1960-70 | 6.5 | 12.0 | 8.9 | 10.2 | 10.2 | 10.0 | 9.0 | 9.1 | 11.1 | 4.3 |
| 1970-80 | 1.2 | 4.2 | 5.4 | 3.1 | 5.1 | 4.4 | 5.1 | 6.8 | 3.8 | 3.8 |
| 1960-80 | | | | | | | | | | 4.0 |
| Zenye maendeleo kidogo | | | | | | | | | | |
| 1960-70 | | | | | | | | | | |
| 1970-80 | -3.6 | 15.4 | 8.9 | 5.2 | 12.6 | 12.2 | 9.9 | 13.6 | 12.8 | 4.8 |
| 1960-80 | 1.7 | 2.4 | 10.5 | 7.3 | 17.1 | 7.6 | 16.1 | 17.5 | 9.6 | 3.1 |
| | | | | | | | | | | 4.0 |
| Afrika zinazoendelea | | | | | | | | | | |
| 1960-70 | 3.7 | 7.1 | 4.6 | 17.3 | 6.3 | 9.1 | 5.1 | 7.2 | 4.3 | 5.8 |
| 1970-80 | 1.3 | 5.5 | 4.2 | 7.3 | 4.1 | 3.2 | 6.4 | 6.9 | 6.2 | 5.2 |
| 1960-80 | | | | | | | | | | 5.6 |

TANBIHI: *Ukuaji wa kisekta kwa 1960 – 70, data imekusanywa nchi za 39 Afrika, ambapo kisekta mwaka 1970-80 Pato la Ukuaji wa Ndani data yake ni ya kutoka nchi 50 zinazoendelea za Afrika.*

Chanzo: ECA sekretarieti

pembejeo na kushindwa kwa ujumla kupunguza ukosefu wa ajira au kutoa msukumo kwa uchumi wa Afrika, sekta ya viwanda imekuwa ni sekta ya migogoro na migogoro ya kusimama kwa viwanda sasa inatakiwa viongezwe, katika orodha inayokua na kuathiri bara letu linalozingirwa na lindi la umaskini.[20]
Hivyo kushindwa kwa mikakati ya ujenzi wa viwanda na hizo la kupuuzia kilimo hakuna shaka ndiko kulikochangia kuimarika kwa utegemezi wa uchumi wa Afrika.

## Mikakati ya Uzawa

Tutahitimisha uchambuzi wetu wa mitazamo ya sekta kuu katika kuondoa ukoloni wa kiuchumi kwa kutathmini mikakati ya kufanya uchumi ushikwe na wenyeji ilifuatwa naserikali nyingi za Afrika mwishoni mwa miaka 1960 na miaka ya 1970. Kama iliyoonyeshwa kwenye *ufanyaji uchumi wa Afrika kuwa wa wazawa.*

Uchumi wa dola halisi ya kiafrika wakati wa uhuru ulikuwa wa viwango vitatu. Wazungu wakiwa juu, wakiendesha viwanda vikubwa, biashara kubwa na mashamba makubwa ; Waasia na Walebanoni wakiwa kati, wakishikilia viwanda vya kati na biashara ya jumla na maduka makubwa ya nguo ya rejareja ; na Waafrika wakiwa chini wakishughulika na vishamba vidogovidogo, viduka vidogo (vibahasha) na kuwa vibarua.[21]

Hali katika utumishi serikalini hata hivyo haikuwa na tofauti kubwa. Waafrika walikuwa na kazi za ukarani na utarishi, ambapo Waasia walikuwa katika nafasi za utendaji, kiwango cha kati cha daraja za kiufundi, wazungu wakiwa katika daraja za juu za utawala na utaalamu. Ingawaje hali haikuwa mbaya sana katika koloni la Waingereza la Magharibi mwa Afrika (*British West Afrika*) (hususani Nigeria na Ghana), hali hiyo ilikuwa ndiyo ya kawaida wakati wa uhuru katika koloni la Waingereza la Afrikia mashariki na Afrika ya Kusini, pia katika makoloni ya Ufaransa, Ubelgiji na Ureno. Kwa hakika nyingi ya nchi hizi zilikuwą taifa zikiwa na wahitimu wachache sana wa vyuo vikuu na wahitimu wa shule za juu.

Hivyo basi, kipaumbele cha nchi zilizopaa uhuru za Afrika kilikuwa kufanya utumishi serkalini kushikwa na Waafrika (Africanization). Inakadiriwa kuwa mwaka 1958 idadi ya wazungu watumishi serikalini katika Afrika walikuwa 100,000.[22] Idadi hii haijumuishi watumishi wa vyuo vikuu na wamisheni, wazungu walioajiriwa na mamlaka za wenyeji na wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa, inatoa

[20] A.A. Adedeji, 1984, p.5
[21] A. Adedeji, 1981, uk. 29
[22] N.A. Shaath, 1975, uk. 99

picha ya aina ya ukubwa wa kuwapa madaraka waafrika kiidadi. Haikuwa tu kubadilisha kirahisi mwafrika kuchukua nafasi inayoshikwa na asiye mwafrika. Kuwapa madaraka waafrika katika utumishi serikalini ilionekana kama mchakato wa kugeuza aina ya utumishi wa umma uliorithiwa kutoka wakoloni kuingia utumishi wa umma unaoshikwa na wenyeji.

Katika hali hii, Afrikanaizesheni au kuzifanya ya sekta muhimu za uchumi wa taifa kuwa za wazawa ni upanuzi wa Afrikanaizesheni ya utumishi wa umma iliyofanikiwa vizuri sana. Sera za uzawa zipo katika sura nyingi. Katika upande mmoja kuna utaifishaji, ambao ni uchukuaji wa biashara zote kwa mkupuo na upande mwingine wa sera ya serkali ya kuhusisha na kusimamia utendaji wa wataalamu wa nje katika shughuli mbalimbali kama Leslie L. Rood alivyoonyesha :

> Uchukuaji mwingi wa mali za wageni katika Afrika ulikuwa katika makundi matatu : Utaifishaji wa viwanda vikubwa vilivyomilikiwa na makampuni ya Kimataifa. Utaifishaji wa matawi madodo ya viwanda na makampuni ya Kimataifa, mabenki, bima, na usambazaji wa petroli, na uzawa ya biashara ndogo na za kati zilizomilikiwa na wageni. Hata hivyo kulikuwa na uchukuaji ambao haukuingia katika makundi hayo. Utaifishaji katika nchi za kijamaa ulijumuisha utengenezaji wa bidhaa, majengo na mashamba ; uzawa katika nchi zilizokuwa na uhuru wa biashara uligusa pia makampuni makubwa yaliyomilikiwa na wazungu. Kila aina ya uchukuaji inaweza kuwa kwa uwazi au ya kistaarabu, yenye fidia au usio na fidia, wa kujitolea au wa lazima.[23]

Kutokana na utafiti wa Umoja wa Mataifa,[24] kati ya mwaka 1960 na 1974 kulikuwa na utaifishaji zaidi na uchukuaji katika Afrika kusini mwa Sahara kuliko katika kanda zingine. Mifano 875 ya utaifishaji katika nchi 62 katika kipindi hicho, kati ya hivyo 340 (au asilimia 39) zilikuwa katika Afrika ya weusi. Kanda hii iliongoza kwa kategoria zote za viwanda isipokuwa petroli, na jumla ya thamani ya biashara zilizochukuliwa na kuwa za wenyeji zilikuwa na thamani ya mabilioni ya dola za marekani.[25]

Mifano ya athari za uzawa ya uchumi wa Misri, Ethiopia, Ghana, Kenya,

[23] L.L. Rood, 1976, uk. 430-1

[24] Umoja wa mataifa, Katibu mkuu, 1974

[25] Inakadiriwa kuwa karibu dola bilioni 4 za mali ya raia wa Marekani peke yake zilitaifishwa duniani kote katika kipindi cha 1960-73; hii inaashiria ukubwa wa thamani ya mali iliyohusika.

Nigeria, Senegal, Tanzania, Zambia, na nchi za Kusini mwa Afrika, Botswana, lesotho na Swaziland ni mifano inayoashiria hatua fulani za udhibiti zilizoingizwa mikononi mwa waafrika. Kutawaliwa na mtaji wa nje, utaalamu, teknolojia na utaalamu wa biashara bado kupo katika nchi zote za Afrika.[26] Hivyo sera ya uzawa imekuwa na mafanikio kidogo, lakini :

Sera ya uzawa ifanikiwe vipi ikiwa katika nchi ambayo uchumi wake umesimama ? Kwa kiasi gani nchi iliyozidiwa kwa deni la nje inavyoweza kujaribu kuweka uchumi wake chini ya wenyeji? Nchi ambayo kwa wazi inaegemea kwenye biashara ya nje na kwa mazao machache yanayoathirika kwa urahisi kwa kuuza bidhaa za awali nje na ambako kuna mgawanyiko mkali kati ya sekta ya jadi na sekta ya kisasa ya uchumi uliyowekewa mipaka na usio na msingi imara, hauwezi kuwekwa chini ya wenyeji. Afrika lazima ione uzawa siyo tu kuchukua shughuli zinazoendelea za wataalamu wageni bali kama changamoto ya kugeuza uchumi wa kikoloni uliopo kwa uchumi imara wa kujitegemea wa Afrika wenye mchakato maendeleo unajiendesha na endelevu.

## Mkakati wa Kupenyeza ndani ya Afrika na Kuunganisha Afrika yote

Kama ilivyodokezwa, mgawanyo wa Afrika na kupatikana kwa uhuru wa kisiasa vilitokea kwa kupuuza kabisa historia utamaduni, uchumi na kujitosheleza kisiasa. Hivyo wakati wa uhuru Afrika ilikuwa kama nguo iliyoshonwa kwa viraka mbalimbali ikiwa na idadi kubwa ya nchi ndogo ndogo sana. Zaidi ya hilo kawaida ya utawala wa kikoloni ilikuwa na visehemu vya kisiasa visivyo na uhakika vilivyokuwapo kama kitu kilivyojitenga vikiwa na kamili vikiwa na muundo hafifu unaokiunganisha,. Nchi za Afrika zilipangiwa kuzalisha kwa ajili ya biashara na wakoloni walio tawala nchi hizo soko la kitaifa lilikuwapo ulikuwa dogo na vipande vidogo vidogo kwa ajili ya mazao ya viwandani.

Katika hali hivyo; kushughulikia malengo ya kitaifa ya kuondokana na ukoloni wa kiuchumi ilionekana kutegemea mikakati ya kiuchumi ya kikanda ya kuunganisha na kuanzisha asasi za kimatifa kuinua maendeleo na kufanya juhudi za ukweli ni kuwa ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda na uunganishaji

[26] A. Adedeji, 1981, uk. 45-327

vilitambuliwa kuwa ni sehemu muhimu ya mikakati ya ukombozi wa kiuchumi muda mrefu uliopita kabla ya kupata uhuru wa kisiasa. Ukweli ni kuwa vilianza kama umoja wa Afrika yote (Pan African) wenye lengo la kuunganisha nguvu za Afrika dhidi ya ubeberu na ukandamizaji wa kikoloni. Hivyo mwito wa awali kabisa wa uunganishaji wa kiuchumi ulitolewa kati mkutano wa tano wa Afrika yote uliofanyika Manchester Uingereza mwaka 1945 wakati huo ukiwa na utabiri mkubwa, mkutano ulipendekeza kuanzishwa kwa Umoja wa kiuchumi wa nchi za Afrika Magharibi kama njia ya kupambana na unyonyaji wa rasilimali za uchumi za eneo la Afrika Magharibi na kuhakikisha kushiriki wananchi katika maendelo ya viwanda ya Afrika Magharibi. Azimio la Bandung la 1955 pia lilirejelea haja ya kuwa na ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi za Afrika.

Kutokana na uhusiano huo na Afrika yote (Pan Africanism) mikakati ya uunganishaji kikanda iliyokubaliwa baada ya uhuru ilipendelea kuwa na uunganishaji mapema wa kikanda. Hivyo mwaka 1958 mkutano wa kwanza wa nchi Huru za Afrika uliofanyika Accra, Ghana ulikubaliana kuanzishwa kwa Kamati ya Uchumi na Utafiti wa kila nchi na kuwa na kamati ya pamoja itayokuwa na wawakilishi wa nchi zote za Afrika zilizopata uhuru. Jukumu lao lilikuwa kuimarisha sera za maendeleo ya uchumi ya nchi hizo, kuinua biashara na sera ya viwanda vya pamoja, na kuratibu mipango ya uchumi kati ya nchi mbalimbali kwa lengo la kufikia utaratibu wa ushirikiano wa kiuchumi kwa Afrika yote Baadaye, mwaka 1960 nchi huru za Afrika wakati ule zilitoa mapendekezo ya uanzishaji wa Halmashauri ya Afrika ya ushirikiano wa kiuchumi, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Biashara ya Afrika. Ilipendekezwa kuua mfumo wa upendeleo wa ushuru wa forodha kwa nchi za Afrika.

Matokeo ya hamasa ya pamoja ya kuunganisha uchumi ambayo ilizaa vikundi vya Monrovia, Casablanca, Brazza ville na Maghreb. Vikundi hivi kwa nyakati tofauti vilitoa mapendekezo ya kuanzisha soko la pamoja la Afrika, Chama cha Afrika cha Malipo na Benki ya Afrika ya Maendeleo ya Uchumi.

Lakini kuanzishwa kwa mashirika ya kikanda kulipambana na vikwazo mbalimbali. Kikwazo cha kwanza kabisa kilikuwa nchi mpya zilizopata uhuru zilileta tatizo kwani viongozi wake kitaifa hawakupenda kupunguza madaraka yao waliyopata karibuni kwa ajili ya maamuzi ya pamoja. Ukosefu wa miundombinu kati ya nchi, hususan usafiri na mawasiliano pia yalizuia biashara kati ya nchi na nchi pamoja na usogeaji. Kikwazo cha tatu kilitokana tofauti za itikadi za kisiasa zilizochukuliwa na nchi zilizoibuka. Pia kulikuwa bado na uhusiano mkubwa kati ya nchi huru na wakoloni wa zamani ambao uliendelea kupinga sana nchi za

Afrika kuwa na mahusiano. Hapakuwa hata na shirika moja la kikanda lililokuwapc kabla ya kuanzishwa kwa Tume ya uchumi ya Umoja wa mataifa kwa Afika (ECA) mwezi April 1958. Miaka mitano baadaye Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU ulianzishwa. Tume ya uchumi ya Afrika toka ilipoanzishwa ilikabidhiwa jukumu la msingi la kuanzisha, kusaidia na kushiriki katika maendeleo ya uchumi ya Afrika. ikiwa ni pamoja na vipengele vyake vya kijamii, na kusimamia na kuimarisha mahusiano ya kiuchumi kati ya nchi za Afrika na nchi nyingine za dunia. Kimsing madhumuni ya OAU yalikuwa ya kisiasa lakini yalihusisha ushirikiano na uimarishaji wa ushirika ili kufikia maisha bora kwa watu wa Afrika, kukomesha namna zote za ukoloni; na kukuza ushirikiano wa kimataifa. Wakati mashirika yote mawili yalitakiwa kushirikiana kwa karibu, wajibu wa kukuza ushirikianc wa uchumi na uunganishaji wa Afrika uliachwa kwenye Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA).

Mapema miaka ya 1960, Tume ya Uchumi ya Afrika ilibaini kuwa mtazamo unaofaa wa uunganishaji kikanda ni ule wa taratibu, ambao unaanza na eneo dogo la kijiografia, kinyume na utaratibu wa kulihusisha bara lote. Afrika iligawanywa katika kanda ndogo nne. Mashariki na Kusini, Kati, Magharibi na Afrika Kaskazini Ofisi za kanda hizo zilianzishwa katika kila kanda ndogo. Kazi yake kubwa n kutoa huduma ambazo zinasaidia kufikiwa kwa uamuzi wa pamoja na vitendo katika ngazi ya chini kwa kufanya utafiti unaohusika, kushiriki katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya mashirika ya kimataifa na kutoa msaada wa kiufund papo kwa papo katika misingi ya kuendelea. Hata hivyo ofisi ndogo za kanda mara zilionekana hazifanyi kazi zake vizuri kama ilivyotarajiwa ya kuzifanya nchi za Afrika kuunda taratibu za ushirikiano. Kwanza ni kwa sababu ukosefu mkubwa wa rasilimali. Pili kwa sababu hakukuwa na kifungu kuhakikisha kuwa serikali zinashiriki katika shughuli na programu za kazi za ofisi hizo. Ili kuimarisha majukumu ya Tume ya Uchumi ya Afrika kama kichocheo cha muunganisho wa kikanda Timu ya Ushauri wa maendendeleo ya Umoja wa Mataifa (United Nations Development Advisory Team) UNDATS zilianzishwa ili kuinua uwezo wa utendaji wa ofisi za kanda ndogo. Haukupita muda ilibainika kuwa kilichokuwa kinatakiwa siyo tu chombo cha ushauri bali chombo cha utendaji kitakachoinua ushirikiano wa kiuchumi. Ilipofika mwaka 1977 nafasi ya UNDATS ilichukuliwa Vituo vya Upangaji na Utendaji (Multi-national Programming and Operational Centres MULPOCS). Leo hii kuna vituo vitano vya (MULPOC) katika kanda ndogo bara ni Afrika (Kielelezo. 14.2) utendaji wake unatia matumaini kwa uunganishaji wa uchumi kikanda katika Afrika hapo baadaye.

Wakati huu kuna jumuiya za uchumi kadhaa zilizoanzishwa kwa misingi ya kanda ndogo na zipo katika hatua mbalimbali za uunganishaji. (Kielelezo 14.3). Katika Afrika Magharibi ipo Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (The Economic Community of Weste Africans Stetes ECOWAS) (kielelezo 14.4) na inajumuisha wanachama wa jumuiya nyingine kama vile Jumuiya ya Uchumi ya Afirika Magharibi (West African Economic Community (CEAO), Halmashauri ya Entente na Chama cha Mto Mano (The Concil for the Entente and the Mano River Union. Katika Afrika ya Kati jumuia za uchumi zilizonzishwa baadaye na Tume ya Uchumi ya Afrika mnamo mwaka 1983 ni pamoja na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati iliunganisha nchi tano zilizofanya muunganicho wa Nchi za Afrika ya Kati (*Union douaniere des Estats d'Asnque centrale*) UDEAC) Nchi hizo ni Jamhuri ya Arika ya Kati, Kongo, Chad, Gabon na Jamhuri ya Muungano ya Cameroon. Ziliunganishwa katika kile ambacho hatimaye kilikuwa soko la pamoja la Afrika ya Kati (CACM) pia ilianzishwa Jumuiya ya Uchumi ya nchi za maziwa makubwa (CEPGL) - Communante' economique des pays de Grand Lacs) zikiwa ni Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika Afika Mashariki, Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Mashariki ilianzishwa mwaka 1967 kati ya Kenya, Uganda na Tanzania ambayo ilivunjika (Julai 1977) Tume ya Uchumi ya Afrika kwa kutumia MULPOC ilifanikiwa kuanzisha Eneo la upendeleo wa Kibiashara la na mashariki kusini mwa Afrika (Eastern and Southern African Preferential Trade Area-PTA) ikiwa na makusudio siyo tu ya ukombozi wa kibiashara bali pia ushirikiano na utaaalamu kati ya nchi na nchi katika maendeleo ya viwanda vya msingi na vya kimkakati, uzalishaji wa mazao ya chakula na wanyama, maendeleo ya sayansi na tekuolojia, uchimbaji na matumizi ya rasilimali ya madini, maendeleo ya rasilimali watu na uanzishaji wa mtandao wa usafirishaji na mawasiliano ya anga. (kielelezo 14.5). Katika Afrika Kaskazini Kamati ya kudumu ya ushauri ilianzishwa mwaka 1904. Nchi zilizohusika ni Libya, Moroko na Tunisia.

Kwa ujumla uanachama wa mashirika yenye malengo mengi yapo kama 130 ya kiserikali, mashirika ya kiuchumi wa kisekta yamekusudiwa kuinua ushirikiano wa kiufundi na kiuchumi katika Afrika zaidi ya hayo, kuna mikutano rasmi ya mawaziri na maofisa katika maeneo maalum mbalimbali.

Mbali na uwingi wake utendaji wa mashirika mengi katika kuinua ushirikiano bado haujathibitika kupenyeza ndani ya Afrika kumebanwa, kwanza kabisa na upungufu wa uelewa wa malengo na namna ya ushirikiano wa kiuchumi unavyopaswa kuendeshwa. Kwa mbali mara nyingi, zinapatikana kutoka nchi

zilizoendelea, hata hivyo siyo ya kweli kwa nchi zinazoendelea. Mawazo hayo yanachukuliwa katika kuanzisha na kuendesha vikundi vya kiuchumi vya Afrika. Mawazo hayo ni pamoja na kuwepo kwa vitengo vingi vya uzalishaji, kila kimoja kikizalisha na kuuza sehemu ndogo ya mazao ya taifa; uchumi unaoendeshwa karibu kwa ajira kamili na mitambo iliyotarajiwa kuendeshwa kwa kiwango kidogo na hivyo uwekezaji mpya nao unakuwa mdogo ikilinganishwa na uwezo wa uzalishaji uliopo; mahitaji ya kutosha ya wajasiriamali wenye motisha ya juu na maarifa makubwa ya masoko ya kutoa fedha kwa ajili ya pembejeo na mazao ambao wana uwezo wa kutafiti wa fursa mpya za kiuchumi kama zinavyojitokeza ndani ya nchi na nje ya nchi; pia faida ya ushirikiano ambayo kwa kawaida hugawanywa sawa kati ya nchi zinazoshirikiana kwa sababu uwezo wa kupata faida kutoka ushirika unagawanywa kwa haki na sawa.[27]

Hali inayopatikana Afrika kwa kulinganisha ina sifa zifuatazo:


(1) Upungufu wa wajasiriamali katika sekta ya umma na sekta binafsi;
(2) Uhaba wa waaalamu;
(3) Uzoefu mdogo wa vyanzo vya utoaji wa mali ghafi
(4) Ufinyu wa nafasi za kuchagua teknolojia.
(5) Ufinyu wa uunganishaji wa kiviwanda na
(6) Ufinyu wa masoko ya nyumbani ikilinganishwa na ukubwa wa viwanda.

Kuwapo kwa hali hii, malengo na aina za ushirikiano kimsingi zitatofautiana na utaratibu wa ushirika unaofanywa kati ya nchi zenye uchumi unaotegemea viwanda.

Kwa maneno mengine, ushirikiano wa kiuchumi katika Afrika usiwe ni kusaidia kibiashara tu bali pia katika uzalishaji. Ushirikiano hauna budi kuelekeza kwenye uundaji na utumizi wa uwezo mpya wa uzalishaji, hususan katika uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya pembejeo kwa ajili ya viwanda vingine au ulaji[28]. Ili kufikia lengo hili, ni muhimu kuunganisha uchumi wa nchi mbalimbali na kurekebisha ruwaza za ulaji na uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya nyumbani na kukuza kujitegemea kwa taifa. Hata hivyo mara nyingi sekta mbalimbali za uchumi katika Afrika zimeungana kidhaifu.

Tatizo jingine kubwa ni jinsi ya kufikia namna na njia zinazokubalika za


[27] Tume ya Uchumi ya Afrika, 1976, uk. 50
[28] kwa kuendeleza hoja hii, angalia A. Adedeji, 1976




*Makundi ya kijimbo ya MULPOC Afrika (Chanzo: Tume ya Uchumi ya Afrika, Addis Ababa)*




*Makundi ya kijimbo ya Uchumi Afrika*




*Ramani kamili ya Barabara Kuu za Afrika Magharibi, ECA/ECOWAS*


kugawana gharama na faida ya ushirikiano wa kiuchumi. Hili limekuwa ni jambo muhimu na linazihusu nchi zinazoshirikiana kuchelea uwezekano wa kupoteza mapato kutokana na kuondolewa kwa kodi za mahuruji na maduhuli kutokana na hatua ulegezaji wa masharti ya biashara zilizomo katika utaratibu wa soko la pamoja.

Tatizo hili linahusiana kwa karibu na ufikiriaji wa usawa na uwiano katika vikundi vya kiuchumi ambapo nchi nyingine zimeendelea kwa kasi ndogo kuliko ambavyo zingeendelea kama zingekuwa hazipo kwenye ushirikiano huo uundaji wa kanuni za usawazisho za jumla zinazokubaliwa ili kutatua tatizo la kutowiana ndilo limekuwa tatizo kubwa zaidi linalovikabili vikundi vya uchumi, kwani hatua kama hizo mara nyingi lazima zihusishe siyo tu hasara ya mapato ya kodi inayoondolewa bali pia faida kutokana na mabadiliko ya hali isiyo pimika kama vile utendaji bora wa hali ya uzalishaji wa nchi uliotokana na ushirikiano wa kiuchumi, uendeshaji wa uchumi wa nje na kupanuka kwa ajira.[28] Kikwazo kingine kwa uhsirikiano wa kiuchumi ufaao katika Afrika kimekuwa ni hali ya kuwa na urazini kupita kiasi kwa nchi nyingi za kiafrika juu ya dola zao. Mara nyingi uongozi wa kisiasa umesita kusalimu taifa wao kwa sera muhimu za uchumi.

Upungufu wa miundombinu na kukosekana kwa kiunzi cha kiasasa cha kuinua ushirikiano wa kiuchumi pia kumefanya tatizo la juhudi za ushirikiano wa kikanda kuwa kubwa. Pengo kuu zaidi linajitokeza kwenye ukosefu wa uunganishaji wa kisiasa wa usafiri na mawasiliano katika ya nchi wanachama; kukosekana kwa utaratibu wa ndani ya Afrika wa kuwa na ofisi ya kubadilishana kundi za benki na sarafu ya pamoja na utaratibu wa malipo na kukosekana kwa asasi za maendeleo za kimataifa zenye uwezo wa kubaini miradi, kuandaa, na kukuza uwekezaji na huduma za ushauri kumekuwa ni tatizo kubwa. Kuhusiana na hayo, kuanzishwa kwa ofisi ya kubadilishana hundi za benki na malipo ya nchi za Afrika Magharibi, utaratibu wa malipo wa nchi za Afrika ya Kati, na utaratibu wa malipo wa PTA ni taratibu zilizoanzishwa na Tume ya Uchumi ya Afrika. Taratibu hizi zitasaidia sana. Tume ya Uchumi ya Afrika pia ilianzisha mwongo wa Muungano wa Usafiri na mawasiliano wa Afrika ambao umeanza kuweka msingi wa mtandao wa usafiri na mawasiliano kwa ngazi ya kanda na kanda ndogo.

Tofauti zinazoendelea na kukua kwa mfano kati ya nchi za kijamaa na kibepari

[28] kwa kuendeleza hoja hii, angalia A. Adedeji, 1976




*RAMANI 14.5 Eneo la Mashariki na Kusini Mwa Afrika la Upendeleo wa Kibiashara. Ramani kuu ya mabarabara makuu.*
*(chanzo: imenakiliwa kutoka ramani iliyotolewa na Tume ya uchumi ya Afrika Addis Ababa)*

katika itikadi za kisiasa na maelekezo ya kiuchumi nayo yamechangia katika kudhoofisha taratibu za ushirikiano. Katika hali ya sasa, suala la msingi ni jinsi ya kuweka chombo cha kiasasi cha kuweza kupunguza ugomvi na kuongeza maeneo ya ushirikiano.

Chanzo cha mwisho cha kikwazo kimekuwa ni tabia ya hisia kinzani dhidi ya ushirikiano wa kiuchumi. Hivi sasa juhudi za kisiasa na ukarimu unaofikiwa kwa pamoja mara nyingi hauendani na matendo. Kuna tabia ya matendo yanayofanywa katika ngazi ya taifa kwa tofauti na maazimio yaliyofanywa kwenye mikutano ya kimataifa.

Ikichochewa na sheria ya mwisho ya Lagos ambayo ilikuwa matokeo ya mkutano wa uchumi wa viongozi wa nchi za Afrika uliyofanyika tarehe 28 na 29 Aprili 1980 huko Lagos ambako viongozi wa nchi na serikali walikubaliana kuanzishwa kwa Jumuiya ya Uchumi ya Afrika (AEC) ifikapo mwaka 2000. Hata hivyo Tume ya Uchumi ya Afrika na Umoja wa nchi huru za Afrika zimekuwa zikipunguza na kuimarisha vikundi vya uchumi vilivyopo kikanda ambako havipo ili kuenea katika Bara nzima. Kwa kutia sahihi mkataba wa kuanzishwa kwa jumuiya ya uchumi ya Afrika ya Kati uliyofanywa tarehe 21 Oktoba 1983 na nchi kumi wanachama, sasa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kimeibuka vyombo vitatu vikuu vya ushirikiano wa kiuchumi ambavyo kitafanywa kazi ya kusukuma mbele mikakati ya kupenyeza ndani ya Afrika na kiunzi kwa uunganishaji wa Afrika yote. Navyo ni:

(1) Nchi 16 mwanachama wa Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), ambayo uanzishwaji wake umeitangulia sheria ya mwisho ya Lagos kwa miaka mitano;

(2) Eneo la Upendeleo wa kibiashara la mashariki na kusini mwa Afrika (PTA) lililonzishwa Disemba 1981 na lililotarajiwa kuwa na nchi wanachama 22; na

(3) Jumuiya ya Uchumi ya nchi kumi za Afrika ya Kati (ECCAS)

## Kudhoofika kwa hali ya Uchumi wa Afrika, kuendelea kwa ukoloni mamboleo katika miundo ya uchumi na uchumi tegemezi

Pamoja na mikakati mbalimbali ya kujikomboa kiuchumi iliyochukuliwa na serikali za nchi za Afrika katika viwango vya makro na kisekta, uchumi wa Afrika umebakiza muundo wa kikoloni uliokuwapo kabla ya uhuru (Jedwali 14.4) na haukuleta athari chanya zinazostahili kwa hali za maisha ya watu. Mikakati hakufanikiwa katika kusukuma mageuzi ya kijamii na kiuchumi yaliyotarajiwa, hasa hasa walifanikiwa tu kufanya mabadiliko madogo ya kimuundo.

Kati ya mwaka 1960 na 1980 mapato (DP) ya pamoja ya nchi za Afrika yaliongezeka maradufu kufikia dola za Kimarekani 86 bilioni mwaka 1980 (katika kigezo gharama cha 1980). Hii ina maana ukuaji wa wastani wa kila mwaka wa asilimia 5.6 (angalia jedwali 14.2) wastani wa pato kwa kila mtu liliongezeka kutoka dola za kimarekani 133 mwaka 1960 hadi dola 243 (au dola za Kimarekani 740 kwa bei za 1983). Wakati kupanda huku kunavutia, kwa ujumla mwaka 1980 wastani wa mapato kikanda ilikuwa asilimia 7.6 tu ya dola za Kimarekani 9684 mapato ya wastani ya nchi zenye viwanda. Hali hii inaonyesha kiwango cha kukosa maendeleo kwa nchi za Afrika. Ukuaji wa utendaji haujawa imara na wakati mwingine usiotabirika. Ukweli kuwa kilimo ndiyo sekta inayotawala zaidi na kuwa uchumi wa Afrika unapambana na amtukio ya hali ya hewa na biashara ya kimataifa inasaidia kuelezea hali ya kutokuwa imara na ukuaji ambao ni mdogo. Hivyo kuyumba kwa ukuaji wa pato la ndani (GDP) katika miaka ya 1965-70 kulitokana na rekodi ya utendaji katika kilimo na mahitaji yaliyoongezeka ya mahuruji. Vivyohivyo kupungua kwa ukuaji badi asilimia 4.5 katika miaka mitano iliyofuata ilikuwa kimsingi kwa sababu kuanguka kwa ukuaji wa uzalishaji katika kilimo hadi asilimia 1.4 kila mwaka na hali ya mdororo wa uchumi kufuatia kupanda kwa bei ya mafuta mara nne mwka 1973-4. Hii ilikonga mahitaji ya mahuruji ya kikanda ambayo yalikuwa kwa asilimia 0.5 tu kila mwaka. Nafuu kidogo ilitokea kipindi cha kati ya mwaka 1975 -80. Hata hivyo ilifuatana na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao yasiyo petroli baada ya muda mfupi wa urekebishaji wa gharama za utawala nishati katika nchi zilizoendelea. Hata hivyo hali ilibadilika na kuelekea kuanguka kutokana na bei mpya za mafuta pamoja na matatizo yaliyorundikana yatokanayo na ukame hadi kuanguka kwa mahitaji ya mahuruji na bei na kubanwa kwa fedha za kigeni ambako hakujawahi kutokea. Mwaka 1981, ukuaji wa kikanda uliporomoka hadi kiwango cha hasi cha asilimia 3.0 (kwa bei za 1980), tokeo la kwanza katika historia ya hivi karibuni. Pamoja na hayo ukuaji wa pato la ndani (GDP) wa asilimia 5.8 katika mwaka 1960 ulikuwa kidogo mzuri kuliko wastani wa asilimia 5.2 kila mwaka ulipatikana katika miaka ya 1970.

Jedwali 14.4 *Utamaduni mmoja kwenye nchi za Kiafrika*

| *Nchi* | *Bidhaa kuu ya mauzo nje* | *Mchango kwenye mauzo nje ya jumla (%)* | | | *Mchango kwa huduma za umma (%)* | | | *Mchango kwa pato la mtu (%)* | | | *Mchango kwa mtaji (%)* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* |
| Algeria | Mafuta | – | 67.5 | 91.6 | – | 50.1 | – | – | 18.8 | 381.9 | – | 10.7 | 332.5 |
| Botswana | Almasi | – | 14.7 | 60.8 | – | 16.5 | 89.8 | – | 4.1 | 40.0 | – | 9.2 | 300.0 |
| Kongo | Mafuta | – | 10.5 | 77.9 | – | 4.7 | 128.7 | – | 1.4 | 41.4 | – | 3.1 | 615.4 |
| | Mbao | – | 52.3 | 11.6 | – | 23.7 | 19.1 | 10.4 | 6.5 | 1.3 | 15.5 | 19.5 | 91.1 |
| Côte d'Ivoire | Kakao | 22.4 | 20.5 | 25.2 | – | 26.4 | 25.7 | 7.0 | 8.1 | 9.6 | 45.3 | 19.2 | 95.0 |
| | Kahawa | 48.5 | 33.2 | 20.5 | – | 42.6 | 20.9 | 15.2 | 13.1 | 9.8 | 98.4 | 13.2 | 77.1 |
| | Mbao | 16.3 | 17.9 | 15.1 | – | 23.2 | 15.4 | 5.2 | 7.1 | 6.7 | 33.9 | 5.0 | 56.7 |
| Egypt | Mafuta | – | 4.6 | 57.8 | – | 2.2 | 15.0 | – | 0.6 | 1.8 | – | 3.6 | 31.1 |
| | Pamba | 66.1 | 44.6 | 13.9 | – | 21.0 | 3.6 | 9.9 | 5.6 | 1.9 | 59.7 | 14.6 | 12.3 |
| Ethiopia | Kahawa | 49.0 | 59.3 | 64.1 | – | 38.9 | 47.4 | 1.6 | 4.1 | 7.0 | 13.4 | 32.6 | 96.3 |
| Gabon | Mafuta | 21.4 | 34.3 | 62.3 | – | – | – | 9.0 | 17.6 | – | 20.4 | 19.6 | – |
| | Manganizi | – | 8.5 | 6.6 | – | – | – | – | 4.4 | 4.4 | – | 12.3 | 41.4 |
| Gambia | Karanga | – | 95.1 | 54.1 | – | 190.0 | 35.8 | – | 29.8 | 8.1 | – | 191.6 | 53.1 |
| Ghana | Kakao | 57.3 | 64.2 | 56.2 | – | 68.6 | – | 22.2 | 14.1 | 12.6 | 96.7 | 93.7 | 220.1 |
| Kenya | Mafuta | – | 15.4 | 31.5 | – | 20.7 | 26.0 | – | 3.3 | 7.2 | – | 13.4 | 88.4 |
| | Kahawa | – | 20.5 | 21.0 | – | 27.5 | 17.3 | – | 4.3 | 4.8 | – | 17.7 | 58.8 |
| | Chai | – | 12.1 | 11.2 | – | 16.3 | 9.3 | – | 2.6 | 2.6 | – | 10.5 | 32.5 |
| Liberia | Chuma | 41.9 | 70.1 | 52.7 | – | 221.9 | 153.4 | 128.1 | 39.5 | 30.6 | 115.3 | 169.7 | 208.3 |
| Libya | Mafuta | – | 99.7 | 99.9 | – | 228.0 | – | – | 78.4 | 61.9 | – | 410.5 | 850.6 |
| Malawi | Tumbaku | – | 33.4 | 43.9 | – | 43.0 | 52.9 | – | 6.7 | 11.4 | – | 13.9 | 107.0 |
| Mali | Karanga | – | 14.5 | 2.3 | – | 14.0 | – | – | 1.6 | – | – | 8.6 | 7.5 |
| | Mamba | – | 21.0 | 48.1 | – | 20.5 | – | – | 2.4 | 7.1 | – | 10.7 | 157.6 |
| Mauritania | Chuma | – | 84.8 | 77.8 | – | 48.0 | – | – | 39.5 | 23.6 | – | 163.5 | 247.9 |
| Mauritius | Sukari | 22.0 | 91.6 | 67.0 | – | 149.1 | 125.3 | 29.8 | 38.5 | 30.6 | 67.9 | 243.1 | 653.2 |
| Moroko | Fosfati | 23.7 | 23.1 | 31.2 | – | 16.6 | 17.2 | 5.1 | 3.4 | 5.3 | 45.7 | 13.5 | 557.9 |
| Niger | Urani | – | – | 74.3 | – | – | – | – | – | 5.6 | – | – | – |

| *Nchi* | *Bidhaa kuu ya mauzo nje* | *Mchango kwenye mauzo nje ya jumla (%)* | | | *Mchango kwa huduma za umma (%)* | | | *Mchango kwa pato la mtu (%)* | | | *Mchango kwa mtaji (%)* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* | *1960* | *1970* | *1980* |
| Nigeria | Kakao | 20.6 | 15.0 | 9.0 | – | 19.7 | – | 3.1 | 1.8 | – | 27.1 | 192.9 | 6.0 |
| | Karanga | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – |
| | Mafuta | 2.7 | 57.6 | 95.3 | – | 110.2 | – | 0.4 | 7.1 | – | 3.9 | 596.0 | 615.1 |
| Senegal | Karanga | 83.9 | 37.7 | 13.3 | – | 40.3 | – | 16.5 | 7.1 | 8.3 | 155.7 | 69.8 | 40.1 |
| | Fosfati | 1.6 | 7.8 | 16.4 | – | 8.5 | – | 0.3 | 1.6 | 2.8 | 3.3 | 1.5 | 49.7 |
| | Mafuta | – | 3.1 | 18.7 | – | 3.3 | – | – | 0.6 | 3.3 | – | – | 37.0 |
| Sierra Leone | Chuma | 14.0 | 11.9 | – | – | 18.4 | – | 38.2 | 3.1 | – | 69.0 | 18.6 | – |
| | Almasi | 55.6 | 62.5 | 53.3 | – | 96.6 | 63.3 | 112.2 | 16.4 | 10.2 | 275.0 | 76.1 | 100.0 |
| Sudan | Pamba | 52.2 | 61.3 | 44.9 | – | 32.0 | 21.8 | 9.5 | 9.9 | 1.8 | 10.5 | 10.1 | 62.9 |
| Togo | Fosfati | – | 24.5 | 39.6 | – | 46.5 | – | – | 5.6 | 13.7 | – | 35.1 | 125.2 |
| Tunisia | Mafuta | – | 24.4 | 50.7 | – | – | 40.3 | – | 3.6 | 15.0 | – | – | 141.6 |
| | Fosfati | 17.7 | 20.3 | 3.0 | – | – | 5.6 | 3.1 | 3.0 | 2.1 | 15.0 | 15.3 | 19.4 |
| Uganda | Kahawa | 36.9 | 50.4 | 98.7 | – | 85.2 | 31.0 | 8.5 | 11.9 | 8.9 | 91.3 | 81.6 | 372.0 |
| | Pamba | 32.3 | 17.4 | 1.2 | – | 29.4 | 82.1 | 7.4 | 4.1 | – | 80.0 | 27.8 | 4.6 |
| Cameroon | Mafuta | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – | – |
| | Kakao | – | 23.8 | 21.3 | – | 34.8 | 27.5 | 7.2 | 5.4 | 4.2 | 51.8 | 27.0 | 47.0 |
| | Kahawa | – | 22.8 | 21.7 | – | 33.4 | 25.4 | 4.1 | 5.2 | 6.3 | 36.7 | 25.9 | 48.5 |
| | Mbao | – | 6.5 | 11.3 | – | 9.5 | 14.7 | – | 1.5 | 2.3 | – | 7.6 | 25.1 |
| Tanzania | Kahawa | 13.1 | 17.4 | 23.4 | – | 19.6 | – | 3.9 | 3.8 | 8.2 | 31.5 | 15.1 | 36.4 |
| Zaire | Shaba | 63.6 | – | 43.3 | – | 80.7 | 51.4 | – | 35.4 | 18.7 | – | 106.5 | 49.5 |
| | Kobalti | 22.4 | – | 21.2 | – | 7.5 | 25.2 | – | 3.3 | 6.2 | – | 9.8 | 24.2 |
| Zambia | Shaba | – | 95.2 | 91.3 | – | 149.0 | 132.1 | – | 63.5 | 79.5 | – | 196.4 | 446.0 |
| Zimbabwe | Tumbaku | – | – | 13.5 | – | – | – | – | – | 3.6 | – | – | 76.4 |

*Chanzo:* Selvetaviati ya ICA, IMF, International Financing Statistics: Kitabu cha Mwaka 1982 na 1983 na Juz. 37, no.5 (Mei 1984)

*Chanzo: Sekretarieti ya ICA, IMF, Takwimu za Fedha za Kimataifa: Yearbook 1982 na 1983 na Juzuu 37, No. 5 Mei 1984.*

## Utafutaji wa mfumo mpya wa uchumi wa taifa, kanda na kimataifa

Imeonekana dhahiri kwa nchi nyingi za Afrika kuanzia miaka ya 1970 kuwa kama Afrika inataka kujinasua na mtego wa uchumi duni na kuweka misingi ya michakato ifaayo katika kujikomboa kiuchumi mikakati mipya ya kiuchumi ya kitaifa, kikanda na kimataifa sharti ibuniwe na itekelezwe kwa juhudi zote. Mikakati hiyo, katika kiwango cha taifa ihusishe uanzishaji wa mfumo mpya wa uchumi uliyojikita katika kanuni madhubuti ya kujitegemea na kujiendeleza. Katika kiwango cha kikanda, juhudi zikolezwe kuelekeza mafanikio ya hata za kuongeza kujitegemea kwa pamoja kati ya nchi za Afrika; na katika kiwango cha Kimataifa uanzishaji wa mfumo mpya wa uchumi wa kimataifa.

Katika utafutaji huu wa mikakati ifaayo na ya hakika kwa ukombozi wa kiuchumi, pongezi ziende kwa Tume ya Uchumi ya Afrika kwa kuanzisha *Mkakati wa Afrika kwa Maendeleo katika mwaka 1970* ambao ulikubaliwa na mkutano wa mawaziri Februari mwka 1971. Umoja wa nchi huru za Afrika unapaswa kupongezwa kwa Azimio la Afrika juu ya ushirikiano, maendeleo na uhuru wa kiuchumi lililokubaliwa na wakuu wa nchi na serikali katika mkutano wao kusheherekea miaka kumi ya kuanzishwa umoja huo mwezi mei, 1973. Hata hivyo kabla ya maazimio ya ECA na OAU hayajaanza kufanyiwa kazi, dunia ilikumbana na maamuzi muhimu ambayo yalikuwa na athari mbaya kwa mahusiano ya kiuchumi na kisiasa kati ya nchi za viwanda na Dunia ya Tatu.

Tangazo la Shah wa Iran la Desemba 23, 1973 la kuongeza bei ya mafuta yasiyosafishwa kufikikia dola za marekani 11.65 badala ya bei iliyokuwapo ya dola za marekani 5.04 kwa misingi yake liliutikisa uchumi wa kimataifa kwa kipindi fulani. Uamuzi huu mmoja wa Umoja wa Nchi zinazotoa mafuta (OPEC) ulisifiwa kama hatua ya muhimu katika historia kwani ilisaidia baadhi ya nchi mwanachama wa OPEC kama vile Algeria kutumia nafasi hiyo kutekeleza mkakati wa upenyaji lipizo wa nchi za viwanda kwa kuongoza dai la kuanzishwa kwa mfumo mpya wa uchumi wa kimataifa (NIEO) Kitendo cha OPEC kilionekana kama kielelezo cha mfano wa nchi zinazoendelea zinavyoweza kufanya.

Kikao maalum cha sita cha Baraza Kuu la Umoja wa mataifa kilichofanyika 1974 kilitoa nafasi kwa mshikamano wa Dunia ya Tatu katika madai yao ya kuwa na mfumo mpya wa uchumi kimataifa. Hata hivyo athari za kupanda kwa bei ya mafuta kwa uchumi dhaifu wa nchi za Afrik zinazoagiza mafuta hususan kwenye akaunti zao za nje na gharama za uzalishaji, ulisababisha baadhi yao kujitoa, hususan OPEC iliposhindwa kuanzisha kigenzo cha kurekebisha bei ya mali ghafi

nyingine. Bidhaa nyingine ziliendelea kupangiwa bei katika masoko huru ya kimataifa ambayo kila mara kuna kubadilika kwa mahitaji na bei na ambapo mashirika makubwa ya kimataifa siku zote ndiyo yenye kunufaika. Pamoja na jitihada zote zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa kuunganisha bidhaa mahuruji nyingine na madini, misingi ya uchumi bado haifai. Nchi za viwanda ambazo huagiza bidhaa hizo zimejifungulia uwezekano wa mbadala ambao umeanzisha nguvu ya kinzani dhidi ya mashirika makubwa ya uzalishaji. Wakati huo huo yale yote yaliyofanywa na OPEC ya mapinduzi ya bei yalikuwa ni kianzio cha kukazia malalamiko ya Dunia ya Tatu ya kutaka kuwa na mfumo mpya wa uchumi wa kimataifa ulijikita katika masuala saba ambayo ni:

(1) Kutengemeaa kwa bidhaa;
(2) Kuwa makini katika kushughulikia madeni ya Dunia ya Tatu;
(3) Kuwa na muundo mpya wa biashara ya kimataifa na kuondo sera za kujikinga za nchi za viwanda za kaskazini kwenye nchi za Dunia ya Tatu;
(4) Kusimamisha mtiririko wa rasilimali kutoka nchi maskini kwenda nchi tajiri na kuongeza misaada rasmi wa maendeleo (ODA) hadi asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la uchumi wa viwanda.
(5) kupata kwa urahisi teknolojia ya magharibi.
(6) Kupanga upya uwezo uzalishaji wa nchi za viwanda kwa kutoa upendeleo kwa nchi za Dunia ya Tatu; na
(7) Kufanya mageuzi ya mfumo wa fedha wa kimataifa kama vile Benki ya Dunia na mfuko wa Fedha wa Kimataifa.

Ingawaje Afrika iliungana na nchi nyingine za Dunia ya Tatu kudai NIEO, na kwa hakika mfumo mpya wa uchumi wa kimataifa, Afrika ilichukua jukumu la kuongoza mazungumzo yasiyozaa matunda mara iliendelea kung'amua kuwa ilikuwa ndiyo iko nyuma sana kiuchumi na ni kanda ambayo haijaendelea katika Dunia. Afrika, hususan Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara haitakuwa na uwezo wa kushiriki kwa misingi ya haki na usawa katika NIEO hata kama inajitokeza mpaka kwanza iweke uchumi wa nchi zake katika hali nzuri katika kiwango cha taifa na kikanda na kukubali kuwa na mkakati wa kweli wa kutokomeza ukoloni wa uchumi.

Ni kwa sababu hii Tume ya uchumi ya Afrika (ECA) ikaona na muhimu kuanzisha mfululizo wa vitendo kutoka nusu ya pili ya mwaka 1975 ambavyo vililenga hatimaye kukubali *mkakati wa Maendeleo kwa Afrika kwa Mwongo wa*

*Tatu wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (Development strategy for Arica for the Third United Nations Development Decude)*[30] *na Mpamgo wa Lagos wa Vitendo kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi wa Afrika 1980-2000.*[31]*Lagos Plan of "Action for the Economic Development of Africa 1980-2000).* Msingi wa kinadharia na kitaaluma wa yote mawili ulikuwa ni waraka uliokubaliwa na Tume ya uchumi ya Afrika wa mwaka 1976 uliyoitwa *Kiunzi kilichorekebishwa cha Kanuni za utekelezji wa mfumo mpya wa uchumi Kimataifa katika Afrika,* 1976 - 1981 - 1985. *Framework of Principles for the (Revised Implementation of the New International Economic Order in Africa, 1976-1981-1985.*[32] Waraka huu ulitoa changamoto za busara za kaida katika uwanja wa maendeleo ya uchumi kama ilivyotumiwa kwa uchumi wa Afrika na kwa mpangilio mzuri uliweka wazi mikakati mbalimbali isiyofaa inayotumiwa kuleta ukombozi wa kiuchumi katika Afrika na mageuzi yake ya kuingia kwenye uchumi unaojitegemea na unaojiongeza kindani na uchumi endelevu unaobadilika. Baada ya kuona kuwa maarifa yaliyopo na uzoefu wa jinsi uchumi unavyokua na namna mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanavyoweza kushughulikiwa kuwa mdogo, tume y uchumi ya Afrika ilihoji katika *kiunzi kilichorekebishwa (Revised Framework)* kwamba kwa kuwa utayarishaji wa sera katika Afrika ulichukua umbo katika mifano mingi na miitiko iliyofuatana kutambua wa maovu ya kiuchumi na kijamii yaliyotoka nje ya kanda. Utambuzi na matibabu kwa kiasi kikubwa yaliathiriwa siyo tu na imani thabiti ya uhusiano wa uchumi shiriki kama injini ya ukuaji wa uchumi unaotakiwa na mabadiliko ya kijamii bali pia kwa uaminifu wa tafsiri mahususi ya chanzo cha biashara ya kimataifa.[33] Tume ya uchumi ya Afrika pia iliweka mashaka kawaida za kufikiri kulikonyooka kunaonyesha kwamba ukuaji wa uchumi unachukuliwa kuwa ni mchakato wa mbunio na matokeo yanayopimwa kwa ongezeko au punguzo la GDP au GNP ambayo ni matokeo ya pembejeo nusu mbunio zinazoitwa uwekezaji ambao unahusisha rasilimali inayopatikana kwa fedha za kigeni. Katika mtazamo huo wa kawaida jukumu la pembejeo za asili halichunguzwi na ikitokea likachunguzwa halipewi umuhimu mkubwa katika mchakato wa maendeleo. Kwa

[30] Kama juu, uk. 45
[31] Tume ya Uchumi Afrika, 1981
[32] Tume ya uchumi Afrika, 1976
[33] Tume ya Uchumi Afrika uk. 6-7

sababu ya programu za taifa au mataifa kwa uzalishaji wa pembejeo za asili tumekuwa tukiegemea sana fedha za kigeni kama njia ya uamrisha pembejeo hizo matokeo yake ni mahuruji yetu kuwa ya zao moja tu na fedha zinazoingia za wawekezaji na nia yetu ya kukubali "kuomba" misaada na mikopo toka nje ili kujali za hayo mawili. Udhaifu wetu mkubwa kama watu ni kwa viongozi wetu wa kisiasa, kijamii na jumuiya ya kukosa mwelekeo. Pia wanaongoza viwanda hawajui juu ya nini wanahitaji kuona nchi zetu moja moja au kama kundi, labda katika miaka ishirini na tano kutoka sasa zitakuwa zimefanya. Ni katika taswira hii ya ubinafsi kunufaika hapo baadaye ambayo ndiyo sharti la kuweka sera na kupanga mikakati katika kila nchi iliyoendelea au nchi iliyoendelea nusu. Bila hilo hakuna njia ya uhakika kuelekea mbele inayoweza kufuatwa na mtu binafsi, jumuiya, nchi au kundi la nchi. Na hivyo inakuwa rahisi kupotoka au kupotoshwa.[34]

Mpango wa Utekelezaji wa Lagos (*The Lagos Plan Action*) ulionekana na tume ya uchumi wa Afrika (ECA) ambayo ilitayarisha mkakati wa Monrovia miaka mitatu baada ya kiunzi kilichorekebishwa (Revised Framework) kama *Magna casta* ya uchumi wa Afrika na msingi wa ukombozi wa kiuchumi wa Bara la Afrika. Vyote viwili, *mkakati* na *mpango (strategy* and *plan*) zinalenga kwenye mafanikio ya kuongezeka kwa kujitegemea na himilivu moja ya njia za kuweka pamoja kimataifa nguvu za mahitaji ambazo ndizo zinaelekeza maendeleo yaelekee upande upi na michakato ya ukuaji wa uchumi na ruwaza za mazao; kuongeza vibadala vya pembejeo vinavyopatikana kutokana na uchumi wa Afrika badala ya vile vinavyopatikana nje ya Afrikal na kuongeza ushiriki wa umma wa wananchi katika uzalishaji na utumiaji wa mazao ya jamii. Nyingine, ni kuongeza kujiendeleza - ina maana kuweka kwa makusudi ruwaza na michakato ya maendeleo na ukuaji wa uchumi ambao vijenzi mbalimbali vinajisaidia na kuimarishana ili zitapohusianishwa na nguvu za kimataifa zinazoamua juu ya mahitaji na ugavi, mfumo mzima unakuza nguvu yake ya kujiendesha ya ndani kwa ndani.[35]
Ni mkakati wa maendeleo pekee uliojikita katika kanuni za kujitegemea na himilivu ndio unaweza kuleta badiliko kutoka uchumi wa kikoloni Afrika na kuliongoza Bora kwenye njia ya maendeleo sanifu. Mkakati kama huo ukiwa unaangalia

[34] Azimio la 332 (xiv) la Tume ya Uchumi ya Afrika lililomo katika waraka E/CN.14/INF/109/ Rev. 1. Azimio hili la Tume ya Uchumi ya Afrika baadaye lilijulikana kama mkakati wa Monrovia, kufuatia kukubaliwa kwake mnamo mwezi Julai 1979 na mkutano wa viongozi wa nchi na serikali wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika.

[35] Tume ya uchumi Afrika, 1981

ndani kuliko kukazia nje ya kutegemea fedha za kigeni na hivyo hauwekei umuhimu mkubwa biashara ya nje kama msingi wa kuanzisha maendeleo hususan aina ya biashara ya nje ambayo Afrika imejihusisha kabla na baada ya uhuru. Mkakati wa maendeleo ulioungwa mkono yaani Mkakati wa Monrovia na ule Mpango wa Utekelezaji wa Lagos unaliweka soko la ndani ikiwa ni pamoja na soko la kanda nusu na kanda kama kitovu cha juhudi za maendeleo katika Afrika kuliko soko la Kigeni la nje.[36] Changamoto inayoikabili Afrika ni kuiweka dhana hii katika vitendo katika kiwango cha nchi, kanda nusu na kanda chanzo cha mkakati wa Monrovia na mpango wa utekelezaji wa Lagos. Ni kwa kufanya hivi tu ndipo ukombozi wa uchumi unaweza kupatikana.

Hata hivyo ukombozi huu unaweza kuhitaji zaidi kuliko tu kupunguza nguvu za Kigeni katika uchumi wa Afrika. Inahitaji kuongeza nguvu ya Afrika katika uchumi wa dunia. Rasilimali za Afrika zinaweza kuwa zaidi kuwa chanzo cha kuegemea, rasilimali hizo zinaweza kuwa msingi wa nguvu ya Afrika kupambana na mfumo wa dunia. Katika kiu hii ya kutafuta nguvu unaolingana na nchi nyingine zinazoendelea ni muhimu sana sasa kuliko hapo nyuma.

## Mikakati ya Umoja na nguvu - Lingana[37]

Aina mbili za umoja ni muhimu kwa Afrika na Dunia ya Tatu kufanya mfumo wa dunia uweze kubadilika kwa kupendelea nchi zilizoonewa na hatimaye kutokomeza kabisa ukoloni.

*Umoja – lingana (organic solidarity)* unahusu uunganishaji wa nchi za kusini ulifanwya ili kuongeza kutegemeana kunakokubalika kati ya nchi za Afrika au nchi za Dunia ya Tatu.

*Umoja kimkakati* unahusu ushirikiano kati aya nchi za Dunia ya Tatu katika mapambano yao ya kupata punguzo kutoka nchi za viwanda za kaskazini. *Umoja lingana* unahusu hamu ya kuinua kwa kiasi kikubwa uunganishaji wa uchumi wa nchi za Dunia ya Tatu. Umoja wa mfumo lingana inalenga kupunguza uunganishwaji wa kutegemea wa kusini katika uchumi wa *Kaskazini* msisitizo wa umoja wa mfumo lingana kimsingi ni kwa kuoanisha Uchumi wa nchi za kusini. Msisitizo wa umoja kimkakati ama ni kusini kuachana na kaskazini, kuwa na namna mpya ya uoanishaji wa uchumi au makataba mpya wa kijamii kati ya nchi za

[36] Tume ya uchumi Afrika, 1976

[37] Tume ya Uchumi Afrika uk. 6-7

Kaskazini na za Kusini. Mikataba ya Kaskazini -Kusini inabidi ijadiliwe upya.

Pia kuona kuwa uchumi unaathirika zaidi kwa hali zote kati ya Kaskazini na Kusini kuliko kusini -Kusini. Kwa ujumla, watu wa kusini wanafanya biashara kubwa na Kaskazini kuliko wenyewe kwa wenyewe. Pia wana uhusiano mkubwa wa uzalishaji na nchi za viwanda kuliko wenzao wa nchi zinazoendelea. Lakini uhusiano wa uchumi kati ya Kaskazini na kusini unaharibiwa na mazoea ya kuegemea yanayohusu ubia usio sawa. Mfumo wa mnyonyoro unatoa faida na nguvu ya wenzao kwa nchi za Kaskazini na kuacha nchi za Kusini zikiwa zimedhulika na kunyonywa. Ni njia ipi ya kutokea? Ni kwa jinsi gani aina hizi mbili za umoja zinavyoweza kusaidia kuifanya kuwa nzuri hali ngumu ya Dunia ya Tatu ya utegemezi na kuwepo wa uchumi unaodhulika wakati wote?

Moja ya maeneo ya ushirikiano yaliosahauliwa zaidi ni eneo la nguvu watu na mafunzo kwa nguvu watu. Kumekuwa na mwanzo mzuri wa kubadilishana nguvu watu kati ya nchi za Dunia ya tatu na katika uwanja wa mafunzo ya nguvu watu katika eneo lote la mipaka ya Dunia ya Tatu. Lakini umuhimu wa eneo hili haukutiliwa maanani.

Mara nyingi haibainishwi kuwa mstari unaotenga nchi za Kaskazini na nchi za kusini siyo mapato (Kigezo cha mali) bali teknolojia (kigezo cha ustadi). Mfumo mzima wa utabakishaji wa kimataifa unajikita katika nani anajua nini na siyo nani anamiliki nini. Libya na Saudia wanaweza kuwa na wastani wa juu wa mapato kwa kila mtu kuliko ardhi ya wanachama wa Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC), lakini Libya na Saudia zipo chini Kimaarifa ya uzalishaji na kupanga uchumi kuliko ulaya magharibi. Kwa hakika, wanachama wa OPEC hawana ujuzi wa kutosha kudhibiti na kuchimba mafuta yao.

Hakuna mahali suala hili linaweza kuonyesha dhahiri kuliko Afrika ya kusini na mashariki ya kati. Wazungu milioni tano wa Afrika Kusini wameweza kushikilia utajiri na kuwazidi watu weusi mara kumi zaidi. Pia wanawazidi nchi majirani zao weusi kiuchumi na kijeshi. Maelezo muhimu siyo kuwa Afrika kusini ni tajiri bali ni kwa sababu utajiri ule umepatikana kwa kutumia nguvu kazi za Waafrika na utaalamu wa wazungu. Nchi jirani za Afrika kusini pia walikuwa na nguvu kazi ya waafrika. Baadhi yake ni matajiri katika madini. Kinachokosekana kwa waafrika ni teknolojia ya juu katika uzalishaji na utamaduni unaofuatana nayo wa kupanga utendaji ufaao.

Nchi za Mashariki Kati kielelezo cha kushangaza kilicho wazi juu ya nguvu ya stadi dhidi ya nguvu ya mapato kuanzia mwaka 1970 nchi za Waarabu zilikuwa tajiri kuliko Israeli katika mapato. Na kwa hakika uchumi wa Israeli

ungeanguka kama siyo mabilioni ya dola zinazotoka Marekani na pengine pote duniani wanakoishi Wayahudi. Na bado, pamoja na kuzidiwa kwa idadi na mali, Waisraeli wamekuwa juu dhidi ya Waarabu kijeshi. Uwezo wa ustadi dhidi ya mapato na idadi umeonekana vizuri katika vita moja baada ya nyingine huko Mashariki ya Kati.

Katika nchi zote mbili Afrika kusini na Israeli vigeu vya utamaduni muhimu. Kama Israeli ingekuwa na Wayahudi wa Mashariki ya Kati tu, Waarabu wangeshinda kila vita. Kwa hakika kusingekuwa na umuhimu wa kuwa na vita nyingine zaidi ya ile ya mwaka 1948. Kwani Wayahudi wa Mashariki ya Kati hawatofautiani sana na majirani zao Waarabu katika utamaduni na ustadi. Katika vita dhidi ya Waarabu wenzao, idadi ya Waarabu ingewashinda Wayahudi siku nyingi kabla hata idadi ya Waarabu haijapata nguvu zaidi kutokana naz utajiri wa mafuta.

Kilichofanya Waisraeli kuwashinda wengine wote siyo Uyahudi wao wa asilimia 80 ya idadi yote ya watu bali Uzungu wao ambao ni chini ya nusu ya sekta ya Wayahudi. Ni Wazungu na Wayahudi wa Magharibi walioweka misingi ya tekuolojia iliyoleta mamlaka ya Israeli katika ukanda huo.

Kama hivi ndivyo, hatima ya utabakisho wa kimataifa kwa hakika ni stadi kuliko mapato. Afrika ifanye nini ili kufanya hali kukosa maendeleo ya kiteknolojia iboreshwe?

Jibu la uhakika ni kwa Afrika kupata maarifa kutoka Kaskazini kwa haraka iwezekanavyo. Lakini hiyo ni ngumu. Nchi za Kaskazini mara nyingi zinapenda kuhawilisha aina fulani ya teknolojia hususani kupitia mashirika makubwa ya kimataifa lakini mahitaji ya nchi za kusini zinahitaji uhawilishaji wa teknolojia fulani ili kusaidia kuongeza uhusiano wao tegemezi kati ya nchi kaskazini na nchi za kusini.

Kwa upande mwingine kuna eneo jingine la teknolojia ambalo Kaskazini haipendi kulihawilisha. Eneo maarufu kati ya maeneo haramu kuhawilishwa ni utaalamu ya fizikia ya nyuklia na teknolojia. Kompyuta ni sehemu ya dhana ya utegemezi kupitia uhawilishaji wa teknolojia. Kiwanda cha Nyuklia au tanuri nyuklia ni ishara ya utegemezi kupitia ukiritimba wa kiteknolojia wa kaskazini. Mashirika makubwa ya kimataifa mara nyingi ni zana za kaskazini kupenyeza kusini kupitia uhawilishaji wa teknolojia, nguvu za nyuklia, kwa namna nyingine ni ishara ya mamlaka ya kaskazini kupitia ukiritimba wa kiteknolojia.

Mkakati uwili kwa Afrika na Dunia ya Tatu ni kujifunza kutoka kaskazini na kushirikiana utaalamu kati yao. Utaalamu wa teknolojia unaoweza kuhawilishwa

bure kutoka kaskazini uondokane na ukoloni na uhusishaji na utegemezi uondolewe haraka iwezekanavyo. Vile vipengele vya teknolojia ambavyo kwa makusudi vinamilikiwa na kaskazini viingizwe katika ujasusi wa viwanda vya kusini katika juhudi za kuvunja ukiritimba wa kaskazini.

Mfumo mpya wa uchumi wa kimataifa hautakuwa na manufaa pasipo mfumo mpya wa teknolojia ya kimataifa. Afrika inahitaji mikakati ya pamoja ili kufanikisha haya mawili.

Ingawaje *nguvu ya ustadi* kwa wakati huu bado ipo kwa kiasi kikubwa mikononi mwa nchi za Kaskazini kuna maeneo ambayo nchi za kusini zina nguvu lakini bado hazijatumia nguvu hiyo inavyopaswa.

OPEC ni kielelezo cha *nguvu ya mzalishaji.* Kutoka 1973 hadi 1983, OPEC kwa jumla ilitumia kidogo nguvu wenzo yake. Badala ya kutumia nafasi ya mwongo ule vizuri kuweka shinikizo kwa nchi za kaskazini ili zifanye marekebisho ya msingi katika ruwaza za kanuni za uchumi wa Dunia, OPEC ilisisitizia mchezo wa bei, mchezo ambao ni matunda yake ni makubwa lakini ya muda mfupi.

Kuna suala jingine lenye umuhimu mkubwa la wazalishaji wakubwa kuungana, katika muda mfupi hata kama ni dhaifu kiasi gani katika muda mfupi. Kobalti inaleta matumaini zaidi kama madini ya nguvu wenzo kuliko shaba, na itahusisha nchi chache. Majaribio ya muugano wa wazalishaj wa kobalti ungeweza kulipa iwapo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ingetetea kwa dhati na wazi zaidi. Kwanza, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ina sifa ya kuwa Saudia ya Kobalti soko lake litakapotengemaa miaka ijayo.

Dunia ya Tatu imetumia kidogo uwezo wake wa *nguvu ya mlaji* hususan kikanda lakini pia hata kiviraka kama ilivyo. Mashariki ya Kati na nchi za Afrika kama Nigeria ni muhimu kama walaji wa vifaa vya uraiani na kijeshi, teknolojia na mazao ya nyumbani mara chache Nigeria au nchi binafsi ya mashariki ya kati zimeweza kunyumbua misuli yao na kutishia kuvunja mikataba ya biashara au kukataa kuiandikisha tena inapomalizika. Lakini misuli hiyo kwa kawaida hunyumbuliwa kwa masuala madogo madogo, kama vile kupinga dhidi uonyeshaji wa filamu ya *kifo cha Binti Mfalme (Death of the Princess)* au wakati ujumbe wa Waarabu na Waafrika unapodharauliwa kidiplomasia na nchi za Magharibi. Nguvu ya mlaji ya Afrika na Mahariki ya Kati ingeweza kutunukiwa kama nguvu wenzo kwa kudai mabadiliko ya msingi zaidi katika ruwaza za kubadilishana kati ya nchi za kaskazini na za kusini.

Aina ya nne ya nguvu ambayo haitumiwi ipasavyo na nchi za kusini ni *nguvu ya mdaiwa* Mwalimu Julius nyerere wa Tanzania alipochaguliwa mwenyekiti wa

Umoja wa Nchi huru za Afrika mwezi Novemba 1984 alitambua kuwa maendeleo, deni na ukame mambo matatu yanayoongoza kuhangaisha hali ya Afrika ya sasa. Ni kweli kuwa deni la Afrika ni la kawaida ukilinganisha na lile la Latin Amerika, lakini mwalimu Nyerere alitambua kuwa deni ni chanzo cha nguvu na siyo tu chanzo cha udhaifu. Katika mkutano wake wa kwanza na baada ya kuchaguliwa Nyerere alilalamika kuwa Dunia ya Tatu haikuwa inatumia kitisho cha kushindwa kupata ufanisi zaidi ili kushawishi mabenki ya Magharibi kutoa punguzo kwa wanaodaiwa.[38]

Ukweli ni kuwa Tanzania itaendelea kuwa dhaifu mpaka hapo kutakapokuwa na mkakati umoja wa haja kati ya nchi za Afrika na Latini-Amerika. Utumiaji wa nguvu ya mdaiwa inahitaji makubaliano kati ya wadaiwa. Mabenki ya magharibi yameanzisha namna vya umoja wa mfumo lingana wao wenyewe na pia kama chombo cha kuendeleza ushauri. Wadaiwa Kaskazini wameungana - lakini wadaiwa Kusini mchafukoge. Afrika na Latini - Amerika zinahitaji kuchunguza uwezekano wa kuanzisha mkakati umoja wa asiyenacho na wa mdaiwa ili kusaidia kushawishi wadai wa Kaskazini kutoa punguzo kwenye masuala ya viwango vya aida, ratiba ya malipo, mbinu za malipo na hali ya ruhusa ya kukawiza malipo na hata kusamehewa deni lote inapobidi.

Umuhimu wa maeneo yote haya ya mkakati umoja yalivyo hakuna mbadala wa umoja lingana kwa biashara kubwa, uwekezaji na maingiliano mengine kati ya nchi zenyewe za Dunia ya Tatu Hapa nchi ambazo zimeendelea kidogo (LDCs) zinabanwa katika moja ya mikinzano kadhaa. Katika mahusiano yao na nchi za Kaskazini nchi zilizoendelea kidogo (LDCs) zinahitaji kuamsha uchumi wao. Lakini katika uhusiano wao kwa wao nchi za LDCs zinahitaji kufanya uchumi wao kuwa wa pekee ili kuongeza sifa za pande zote. Uganda wanaweza kufufua viwanda vyake vya pamba na kuuza nyuzi za pamba Kenya na kuingiza katika viwanda vya nguo. Upekee huu utasaidia nchi hizi mbili kuendelea katika upande wa upekee wa pande zote. Lakini ya uhusiano wa Uganda na uchumi wa dunia kwa ujumla unaamrisha kuanuwaisha viwanda vya Uganda kuliko kuvifanya kuwa vya pekee. Hili ni tatizo kubwa ambalo nchi za Dunia ya tatu zinahitaji kulitatua haraka sana. Nchi za Kusini zinahitaji uwiano ufaao kati ya uanuwaishaji kwa mahusiano ya Kaskazini na kusini na kufanya upekee kwa biashara ya Kusini - Kusini.

Suala jingine linalohusiana hili ni ulazima wa kutafuta mbinu mbadala ya malipo

[38] The voice of America's African broadcast a recording of both Nyerere's speech and his press conference; one such broadcast was on 24 November 1984.

kwa biashara ya Kusini - Kusini. Kanuni ya kutumia fedha za Kaskazini kwa biashara ya Kusini - Kusini imekuwa na ugumu mkubwa. Bogi/zimwi la fedha za kigeni limesumbua uchumi wa nchi za Kusini. Tanzania, Zambia na Zimbabwe zimekuwa zikichunguza uwezekano wa kufufua matumizi biashara ya kubadilishana mali (barter) kama msingi angalau wa baadhi ya vipengele vya uhusiano wa kiuchumi. Nigeria katika miaka ya 1980 ilifanya jaribio la biashara - lingana, ikabadilishana mafuta kwa bidhaa za viwandani. Maridhiano mapya baina ya Kenya na Tanzania pia yanafikiria maeneo ya biashara ya kubadilishana kati ya nchi mbili hizi. Katika miaka ya mbele. Kama pamba ya Uganda inalisha viwanda vya nguo vya Kenya kwa mpangilio mzuri zaidi huko mbeleni, haitakuwa sahihi kwa Kenya kuilipa Uganda kwa sharti na sare za kijeshi zilizoshonwa ila kwa fedha za kigeni halisi.


Eneo jingine la umoja lingana kati ya nchi za Dunia ya tatu linahusu suala la kugawana nishati. Kuna miaka ambapo Kenya ilihitaji kupata theluthi moja ya umeme toka bwawa la Jinja huko Uganda. Uganda bado ndiyo mtoaji mkubwa wa umeme wa Kenya.

Bwawa la Akosombo lililopo mto Volta nchini Ghana lilijengwa kwa makusudi ya kuwa chanzo kikuu cha umeme katika ukanda wa Afrika Magharibi. Kwa bahati mbaya kiwango cha maji kimekuwa chini sana kiasi cha kushindwa kutoa umeme kwa nchi jirani. Ghana yenyewe kwa vipindi vipindi imekuwa na mgao wa umeme. Ghana wakati mwingine ilihitaji ushirikiano wa umeme na Cote d'Ivoire. Mabwawa yaliyoko eneo la Kusini mwa Afrika kama bwawa la kariba limekuwa na mafanikio katika kuhudumia ukanda huo. Haya yote yanaashiria hali ya kuwa na umoja lingana wa Afrika yote katika nishati kwa kuwa na miundo iliyounganishwa na umeme wa maji. Kampuni za chuma cha changamano zilizoungana zilikuwa ndiyo mkunga katika kuzaliwa viwanda vya chuma vilivyoungana na ikaonekana kuwa bima dhidi ya vita yo yote uuaji huko ulaya. Ikiwa uzalishaji wa chuma wa ulaya. Ikiwa uzalishaji wa chuma wa ulaya uliunganishwa, viwanda vilitegemeana na hivyo uvamizi wa kivita wa nchi moja kwa baadaye ilikuwa nadra kutokea.


Katika moyo huo huo kuunganisha mifumo ya umeme kati ya nchi za Dunia ya Tatu kungeongeza kuitegemea kunakokubaliwa pande zote. Hali hivyo ingeanzisha kishawishi cha ushirikiano katika maeneo mengine.

Mapambano ya kuwa na Afrika iliyoungana yamekutana na vikwazo vingi kutoka kuanguka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kenya, Uganda na Tanzania hadi kukauka kwa bwawa la Akosombo.

Jaribio lenye faida kwa Afrika kuwekea manani na kujifunza ni mfano wa Asia ya Kusini-mashariki. Mapambano ulinganishaji wa Asia ya kusini-mashariki umekuwa wa mafanikio. Chama cha Nchi za Asia ya kusini-mashariki (ASEAN)



PICHA 14.1 *Bwawa la Uganda*



PICHA 14.2*Bwawa la Ghana*

kimeibuka kama nguvu kubwa ya kiuchumi na kidiplomasia katika mambo ya ukanda huo. Mapambano ya kuwa na muungano zaidi wa nchi za Kiarabu ni hadithi mchanganyo kutoka ahadi chanya za Halmashauri ya Ushirikiano ya Gulf hadi ugomvi/mizozo yenye kuleta madhara pande zote katika siasa za Kiarabu. Libya na Misri zipo karibu kugombana mara kwa mara.

Katika Latin - Amerika uunganishaji wa kikanda pia umekuwa na rekodi mchanganyiko. Amerika ya kati miaka ya 1980 ilikuwa na wasiwasi chini ya mawingu ya vita. Kwa upande mmoja Chile na Argentina kupitia upatanishi wa Vatican zilizima suala nyeti la mkondo wa Beagle. Ushirikiano wa kiuchumi umekuwa wa kupanda na kushuka katika ukanda mzima. Hata hivyo wazo la kuwa na uunganishaji mkubwa bado liko moto. Afrika iangalie hii maabara hii ya kisiasa iliyoko mbali lakini inayovutia sana.

Mduara wa Kaskazini kwa ujumla umegawanyika katika mabonge mawingu ya kiuchumi yanayoendana na mgawanyiko wa kiitikadi. Kugawanywa kulikuwa kati ya dunia ya kijamaa ya COMECON (Council for Mutual Economic Assistance/CMEA), na dunia ya kibepari na NATO (North Atlantic Treaty Organization) na Jumuiya ya Ulaya. Afrika kama ukanda wa Kusini, kwa upande mwingine bado imegawanyika vipandevipande. Ipo katika kutafuta siri ya kipaji cha mshikamano.

Mikakati ya Umoja ipo lakini haifanyi kazi. Lengo hili liko mbali na gumu lakini kufika kwa Afrika ni lazima kuzidi fumbato, au mbinguni kuna faida gani?

Wanafalsafa wamebainisha kati ya uhuru hasi (uhuru wa kutotawaliwa) na uhuru chanya (uhuru wa kushiriki) wakati watumwa wa kiafrika 'walipokombolewa' huko Amerika, kwa hakika walichopewa ni uhuru hasi (uhuru wa kutomilikiwa na wengine). Miaka mia moja baadaye Waafrika popote walipo duniani bado wanatafuta uhuru chanya (uhuru wa kushiriki ipasavyo).

Sawia na hapo, *ukombozi wa Kikoloni hasi* ni sawa ukombozi kutoka utumwa, uhuru wa kutomilikiwa na wengine. Lakini ukombozi chanya utafika wakati waafrika watakaposhiriki kikamilifu katika uchumi wa dunia na kupata mgao ulio sawa katika nguvu za dunia. Haitoshi tu kupunguza nguvu toka nje katika uchumi wetu, ni muhimu katika hatua hiyo. Lakini ni muhimu wakati huo huo kutafuta njia za kuongeza nguvu ya Afrika katika uchumi wa dunia.

Waafrika ni lazima waondokane na kuwa watazamaji katika michezo ya wengine na kuwa wachezaji halisi katika ubao wa chesi wa mustakibali wa dunia.

# MABADILIKO YA KIJAMII NA KISIASA TANGU UHURU

# 15

# Ujenzi wa Taifa na mabadiliko ya mifumo ya kisiasa

Mapambano makubwa ya Afrika kisiasa baada ya kipindi cha ukoloni yanaweza kuwekwa katika shauku kuu mbili - ile ya kupigania kuleta mshikamano wa umoja wa kitaifa wa Ki-Afrika, na ile inayopigania kuimarisha utengamano wa dola za Kiafrika. Mgogoro wa utaifa ni mgogoro wa utambulishi wa pamoja usio kamili. Mgogoro wa dola ni mgogoro unaotokana na mamlaka yenye kuyumba. Masuala haya mawili yanahusiana lakini kila moja lina mantiki yake. Nchi nyingi za Kiafrika zilizopata Uhuru ziliundwa na ukoloni na sasa zinapigania kuwa na mshikamano zaidi. Nchi kama Somalia, kwa upande mwingine, ni taifa asilia linalopigania kuwa na utengemano na umoja wa ndani. Lakini kwa kuwa utaifa na dola katika karne ya ishirini vinahusiana, aina zote mbili za nchi zinaendelea kuwa na matatizo haya mawili ya utambulishi na mamlaka dhaifu katika kipindi cha baada ya ukoloni.

Kwa namna nyingi tishio kubwa kwa utambulishi wa kitaifa katika Afrika huru ni urithishwaji wa mipaka bandia iliyoundwa na tawala za kikoloni. Kipengele muhimu kuliko vyote chenye kutishia utengemano wa dola ni jeshi la kudumu, ambalo pia ni zao la ukoloni. Jamii nyingi za Kiafrika kabla ya ukoloni ziliunda majeshi pale tu haja ilipotokea wakati wa migogoro.

Hata hivyo, katika kupanga utawala wa jadi, watunga sera wa kikoloni walikabiliwa na tatizo kama wadumishe utawala wa jadi na watawala wake au waweke maafisa wasomi wenye mwelekeo wa kimagharibi. Waingereza walipambana na tatizo hili lakini walishindwa kulitatua hata kwenye akili zao wenyewe. Itikadi yao ya "utawala usio wazi" ilipendelea kutumia viongozi wa jadi pale palipostahili, hususan Kaskazini ya Nigeria. Lakini kuanzia miaka ya 1930 na kuendelea watunga sera wa kikoloni kwa kuzingatia mapokeo ya Waingereza walijishughulisha pia na maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii katika makoloni yao ambayo yalihusisha upanuzi wa elimu ya sekondari na elimu ya juu kwa kufuata mtindo wa kimagharibi. Kundi

kubwa la wasomi wachache wa Kiafrika waliokuwa na mwelekeo wa kimagharibi lilianza kutokea.

Katika makoloni ya Kifaransa, dhahiri mwelekeo ulipendelea kuunda tabaka la wasomi kuwatumia wenyeji wenye mtazamo wa Kifaransa badala ya viongozi wa jadi. Lakini hata kwenye milki ya Wafaransa wenyewe kulikuwepo na migongano. Katika makoloni ya Afrika Magharibi warabiti walibakia na mamlaka kiasi: na ufalme ulikuwa na kiasi kikubwa cha mamlaka katika "nchi liundwa" (protectorate), ya Moroko licha ya migongano ya mara kwa mara na watawala wa Kifaransa.

Wakati wa ukoloni, watawala wa jadi walikuwa wakijihami dhidi ya changamoto ya wasomi wenye mwelekeo wa kimagharibi. Tangu kupatikane uhuru viongozi wasomi wenye mwelekeo wa nchi za magharibi wamekuwa wakijihami wa kuogopa upinzani wa kijeshi.

Nchini Ghana baada ya ukoloni, kila mtawala wa kiraia alikuwa ni msomi wa Chuo Kikuu mwenye uelekeo wa nchi za magharibi. Lakini sasa mwelekeo unaonyesha kupendelea wanajeshi kama watawala wasio na mwelekeo mkubwa wa kimagharibi. Nchi nyingine za Kiafrika zimeonyesha pia mwelekeo huo baina ya raia wenye mtazamo wa magharibi na watawala wa kijeshi. Baadhi ya watawala wa Uganda wamekuwa na sifa mchanganyiko. Mheshimiwa Edward Mutesa, Rais wa kwanza, alikuwa mfalme wa jadi na pia alikuwa Mwafrika aliyekuwa na mwelekeo wa nchi za magharibi. Yoweri Museven alikuwa askari na pia msomi wa Chuo Kikuu.

Lakini msingi wa migogoro yote hii unatokana na maana ya michakato miwili pacha kihistoria, ule ujenzi wa taifa, na ule wa ujenzi wa dola katika Afrika ya karne ya ishirini. Hebu kwanza tuwe na uhakika na kuelewa dhana zenyewe za "taifa" na "dola".

## Fasili za taifa na dola

Katika kufasili dhana ya taifa, mara nyingi wanazuoni hutofautisha baina ya sifa yakinishi na sifa za kimtazamo za taifa. Kati ya hizo sifa yakinishi za taifa ni lugha, historia, eneo, utamaduni (wakati mwingine dini huingia humo), utaratibu wa kisiasa na maisha ya kiuchumi. Sifa za kimtazamo wa hisia wa utambulishi, wa pamoja, na hujitoa kutetea, au kwa mwaminifu kwa kundi linalohusika. Sifa hizi za kisaikolojia siyo rahisi kuzipima.



*PICHA 15.1 Mfalme Kabaka wa II wa Buganda katika sare za kijeshi*

Kwa kufuata fasili yetu ya kwanza, Waigbo, Wayoruba au Wahausa - Fulbe kila moja ni taifa huko Nigeria; halikadhalika Wakikuyu au Waluo huko Kenya, Wahutu huko Burundi au Watswana kule Botswana. Kwa madhumuni yetu hapa hata hivyo, fasili inayoendelea kutumika ya taifa ni ile inayodai kwamba taifa ni "watu wanaoishi katika eneo moja waliounganishwa na serikali moja ya nchi au dola." Kwa fasili hii, itatubidi tuseme kwamba Nigeria, Kenya, Burundi na Botswana ni mataifa - na siyo kusema kuwa kuna mataifa mbalimbali ndani ya taifa au dola. Kwa uzoefu wao, waandishi wa nchi za Magharibi wanayo dhana kwamba dola na ujenzi wa taifa ni vitu viwili tofauti ambavyo hatimaye hupelekea kuundwa kwa taifa - dola. Kwa mantiki hii ni kwamba kukua kwa maendeleo ya taifa-dola ni hatua ya juu sana katika harakati za ujenzi wa dola na taifa. Kwa hiyo kwa uzoefu wa nchi za Magharibi, taifa huundwa kwanza kabla ya dola na taifa-dola huwa ndio tokeo la mwendeleo huo.

Kwa upande wetu, utaratibu wa ujenzi wa taifa hauhawilishi kujitoa na uaminifu kwa jamii hizo finyu na kuyapeleka mambo hayo kwenye eneo kubwa zaidi la kisiasa kama Nigeria. Mtu Muigbo, Muyoruba au Mukikuyu ni suala tu la utambulishi. Huwezi kulihamisha. Mtu hawezi kukoma kuwa Muigbo au Muhausa au Mukikuyu kwa kutamka tu. Kwa upande wetu ujenzi wa taifa pana unahusu upanuzi wa upeo na utambulishi wa kikabila ili uhusishe jamii kubwa zaidi kama vile nchi nzima.

Ujenzi wa taifa unahusisha pande mbili za utambulishi. Upande mmoja unahusiana sana na ujenzi wa dola. Upande huu unahusu wajumbe wa dola kuikubali kihalali serikali na utambulishi wake pamoja na serikali kuu kama alama ya taifa. Huu ni ujenzi wa taifa kiwima - kwa maana siyo tu kwamba ipo dola bali pia watu wanayakubali mamlaka ya dola (siyo tu kwa kutumia nguvu) na kuiona serikali yake kuwa ni alama ya kisiasa katika jumuiya yao. Kwa hiyo matukio ya kutaka kujitenga ya huko Nigeria, Ethiopia, Sudan na Zaire ni changamoto kwa mamlaka ya Serikali kuu na ni ishara ya kukataa utambulishi wa pamoja.
Kiulalo, ujenzi wa taifa unadai kukubali raia wote kuwa wahusika sawa na taifa lililoundwa kihalali, linaloimaishwa na hisia ya kuwa waoshiriki katika jumuiya moja ya kisiasa. Hii inafanya wajisikie kwamba wote wanashiriki, kwa ufanisi au vinginevyo katika harakati za maendeleo ya kisiasa. Kwa hiyo, ujenzi wa taifa ni kukubali kwa mapana mchakato wa ujenzi wa dola. Ujenzi wa jumuiya ya kisiasa ndio huupa kamili uhai dola.

Michakato hii ya dola na ujenzi wa taifa huweza kufanyika kwa wakati mmoja na mara nyingi huingiliana. Katika nchi nyingi za Kiafrika zilizowahi kutawaliwa na wakoloni, dola ilitangulia taifa. Makabila mengi yalijikuta yakigawanywa kinasibu katika maeneo ya kiutawala ambayo baadaye yalifanywa kuwa maeneo ya kisiasa-kijiografia yaliyoitwa dola. Jamii nyingi katika dola hizi hazikujitambulisha na dola hiyo kama alama ya jamii ya watu au jumuiya moja ya kisiasa.

Nchi nyingi za Kiafrika zimeibuka kwenye miaka ya 1960, hivyo zimeanza kuimarisha dola zao hivi karibuni. Kadiri uimarishaji wa dola unavyoendelea vivyo hivyo na majaribio ya ujenzi wa taifa yanaendelea. Haya yote hubebesha mizigo mkubwa uwezo wa mifumo ya kisiasa katika nchi zote za Kiafrika.
Zaidi ya yote, kama Sheldom Gellar anavyodai kwa ushawishi, mchakato wa ujenzi wa dola na taifa umepitia hatua za kuibuka kwa "mataifa - dola" ambayo yanatambua utata wa umoja wa kitaifa, kama vile "utofautiano katika umoja" na siyo tu umeja katika utofautiano. Hivyo harakati za ujenzi wa taifa huweza kufanya kuwepo kwa "dola - taifa" na pia "taifa - dola".

Je, ni lazima ujenzi wa taifa uufanye utambulishi wa kitamaduni na kisiasa uwe wa aina moja? Kama asemavyo Clifford Greetz, mwafaka hupatikana kwa pande zote kujirekebisha ili utaratibu wa serikali uweze kuendelea vizuri bila kuathiri mfumo wa kitamaduni wa utambulishi wa mtu binafsi.

Utaratibu wa ujenzi wa taifa unajitahidi kupanua upeo kwa uaminifu wa makabila ili ulingane na ule wa mipaka ya dola, na hatimaye ufanane kiasi na kiwango cha uaminifu kwa makabila madogo.



*PICHA 15.2 Mkutano wa pili wa kilele wa nchi za Maghreb Marrakesh tarehe 15-16 Februari 1989: kutoka kushoto kwenda kulia; Rais Ben wa Tunisia, Rais Muammer Kudhaffi wa Libya, Mfalme Hassani wa II wa Moroko, Rais Chadli Bendjedid wa Algeria na Rais Ould Sid Ahmed Taya wa Mauritania.*

Mwisho, harakati za ujenzi wa taifa katika nchi za Kiafrika zimekumbana na migongano na migogoro. Ukizingatia kuwepo kwa makabila mbalimbali tofauti katika harakati hizi, migogoro ni ya lazima itokee. Jambo muhimu katika mchakato wa ujenzi wa taifa siyo tu migogoro bali ukali wa migogoro hiyo.

Kwa makusudi ya mapitio haya, dhana ya kubadilisha mifumo ya kisiasa kuhusu mifumo ya kisiasa iliyorithishwa na kufanyiwa marekebisho, na/au mifumo mipya

iliyoanzishwa ili kusaidia nchi za Kiafrika katika kujenga mataifa baada ya nchi hizo kupata uhuru kwenye miaka ya 1960.

## Kutoka violezi vya kikoloni hadi kikatiba huru

Mbali na utawala usio dhahiri, Waingereza walianzisha mabaraza ya kutunga sheria katika makoloni yao. Katika kipindi cha kuelekea mwisho wa ukoloni uwiano wa wajumbe wa mabaraza haya ulibadilika badala ya kuwa na wajumbe wengi Wazungu yakawa na waafrika wengi zaidi na wajumbe wajumbe wa kuchaguliwa wakawa wengi zaidi kuliko wajumbe wa kuteuliwa.

Katika miaka ya mwisho ya utawala wa Kikoloni, Waingereza walianzisha mtindo wa utawala wa serikali wa "Westminster" katika makoloni yao. Vyombo vyenye kufanana na bunge, (mara nyingi vikiwa na mabara mawili), vilianzishwa, hivyo Waafrika walianza kujifunza kufanya kazi katika mabaraza ya mawaziri, kutokana na baadhi wajumbe wa kuchaguliwa kuwa mawaziri. Mara nyingi Waingereza waliyakabidhi makoloni yao utawala wa kishirikisho (ambao wao wenyewe hawakuwa nao).

Katika kipindi hiki cha mwisho cha ukoloni, matarajio ya kupata uhuru yaliwezesha makabila mengi au mataifa ya kitamaduni kupigania madaraka ya kisiasa ambayo kwa sasa yalitakiwa yarithishwe kwa dola mpya. Mara nyingi ushindani huu ulisababisha kuwepo kwa "ukabila" mpya uliotokana na kujitambua kutoka watu wengine katika mazingira haya mapya. Hivyo basi, waali wa kisiasa mara nyingi walikwenda kwenye maeneo yao ya kikabila au mikoa yao ili kuunga mkono. Mifano mchache ya vyama vya aina hiyo ni: Chama cha "the *Northern People's Congress* (AG) cha the *Action Group* (AG) cha Nigeria *Confederation des associations tribales du Katanga* (CONAKAT) cha Zaire; *Kabaka Yekka* (KY) na *Domecratic Part* (DP) vya Uganda.

Hata hivyo, vilikuwepo vyama vya kisiasa vilivyokuwa vimesambaa sehemu kubwa ya nchi vikihamasisha umma ili kuleta mwamko wa kisiasa uliovuka makabila finyu. Tumekwishaona kuwa chama cha "*Parti democratique de la Guinea*" (PDG) cha Guinea chini ya Sekou Toure kiliweza kuhamasisha makabila mbalimbali na vyama vya wafanyakazi hadi kufikia mapambano ya kitaifa. Chama cha Senghor cha "*Blocdemocratique Senegalais* (BDS) kilifanikiwa kuwahamasisha Wasenegali wa makabila mbalimbali hadi kupata Uhuru. Uzoefu wake kwa namna fulani ulifanana na ule wa Julius Nyerere wa Tanzania.

Siyo tu kwamba Nyerere anatoka katika kabila dogo la Wazanaki bali pia yeye ni Mkristo katika nchi yenye *Waislamu wengi*. Tanzania ni nchi yenye makabila

mengi lakini siyo nchi dola yenye mataifa mengi kama vile Nigeria. Kiswahili kimeenea sehemu kubwa ya nchi na hivyo kuwa kiungo cha kuondoa tofauti mbalimbali. Nyerere alishiriki katika kuanzisha chama cha siasa cha *Tanganyika African National Union* (TANU) mwaka wa 1954. Chama hiki pekee ndicho kiliiwezesha Tanganyika ipate Uhuru wake bila upinzani mkubwa hadi mwaka 1977 kilipojiimarisha na kuwa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Katika sehemu nyingine kama vile Uganda, wingi wa makabila ulisababisha matatizo. Ingawa Chama cha siasa cha Milton Obote cha *Uganda Peoples Congress* (UPC) kilikuwa cha makabila mengi, bado kilihitaji kuungana na Chama cha Kabaka Yekka (KY) ili kiweze kuunda serikali wakati wa uhuru. Dhima mbili za Kabaka Mfalme, Kabaka wa Buganda, na kama Raisi wa Uganda, zilisababisha matatizo katika ujenzi wa taifa na ujenzi wa alama ya utaifa.

Huko Zaire, mambo ya kisiasa yaliendeshwa kwa fujo na ghasia nyingi. Chama cha Lumumba cha *Mouvement National Congolais* (MNC) kilikuwa ni chama cha kisiasa kilichounganisha makabila mbalimbali. Akiwa mzalendo na mtetezi wa umoja wa Afrika, Lumumba aliweza kuwahamasisha wananchi kwa ujumla ili kudai Uhuru. Vyama vikuu vya upinzani vilivyompinga vilikuwa vikiendeshwa kwa misingi ya ukabila. Chama cha CONAKAT kilichoongozwa na Moise Tshombe kiliamua kujitenga. Hali hii ilisababisha vita vya wenyewe mara tu baada ya Uhuru.

Siyo mapambano yote ya wazalendo katika miaka ya mwisho ya ukoloni yaliishia kupata uhuru kwa amani kutoka kwa Wakoloni. Nchi za Angola, Zimbambwe, Mozambique, Guinea-Bassau na Algeria zilipata uhuru wao kwa mtutu wa bunduki. Chama cha siasa cha *Partido Africano para a Independencia de Guine e Cabo Verde* (PAIGC) cha Guinea-Bissau kiliweza kuhamasisha wananchi wake ili wapambane na ukoloni. Kusema kweli taifa la Guinea - Bissau lilianzishwa kwanza kabla ya utawala wa dola, jambo ambalo si la kawaida katika Afrika. Hapa ujenzi wa taifa ndio uliokuwa sharti la kuwepo kwa dola. Huko Angola, baada ya Wareno kuondoa haraka majeshi yao, ugomvi wa kiraia ulizuka kati ya chama cha kisiasa cha *Movimento Popular de Libertacao de Angola* (MPLA) cha Agostinho Neto, chama cha *Frente Nacional de Libertacao de Angola* (FNLA) cha Roberto Holden na chama cha *Uniao Nacional para a Independencia total de Angola* (UNITA) kilichoongozwa na Jonas Savimbi. Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) uliitambua serikali ya chama cha MPLA ya Agostinho Neto kuwa ndiyo serikali halali ya Angola.

Sehemu nyingine katika Afrika ya Kusini, ubaguzi wa rangi na ukabila ulitawala sana. Chama cha kisiasa cha *Malawi Congress Party* cha Hastings Kamuzu

Banda kiliweza kuhamasisha Waafrika dhidi ya ubaguzi wa rangi na ukoloni nchini Malawi. Banda alifanikiwa kuipatia Uhuru nchi yake ya Nyasaland na baadaye akabadili jina la nchi na kuiita Malawi.

Huko Zimbabwe, mapambano yalikuwa zaidi dhidi ya ubaguzi wa rangi na ukoloni. Afrika Kusini iliendeleza sera yake ya ubaguzi wa rangi hata kufikia kuitawala kwa nguvu Namibia.

Wakati wa Uhuru, mambo kadhaa yaliweza kuonekana katika madola mapya. Wakati wa ukoloni, dini ya kikristo ilipata umuhimu zaidi, japo dini za asili za Kiafrika na Uislamu, ziliendelea kuwepo. Baada ya uhuru, mambo haya yalikuwa na athari zake katika utengamano wa jamii na ujenzi wa taifa.

Mamlaka ya utawala wa jadi yalinusurika kutoweka wakati wa ukoloni ingawa umuhimu wake ulitofautiana baina ya nchi zinazozungumza Kifaransa na zile zinazozungumza Kiingereza. Utawala wa jadi ulipewa umuhimu mkubwa kisiasa katika nchi zinazozungumza Kiingereza kuliko nchi zinazozungumza Kifaransa. Elimu ya kimagharibi ilikuwa ni njia ya kujiendeleza katika jamii. Vyama vya kisiasa vilianza kutokea katika Afrika, na utawala wa kikoloni ulihimiza mfumo wa utawala wa vyama vingi katika nchi nyingi. Msisitizo huu ulikuwa na lengo la kuwagawa wazalendo katika harakati zao za kisiasa au kuuwezesha utawala wa kikoloni kuingiza mtindo wao wa utawala wa kidemokrasia katika makoloni yao.

Hali kadhalika, sheria za Ulaya zilitumika kwa lazima katika makoloni yao ili kusaidia kutawala au kurekebisha tabia za watawaliwa katika makoloni. Urasimu wa utawala wa kikoloni ulirithiwa na watawala wapya. Kimsingi muundo huu ulisaidia kudumisha sheria na amani na kuwezesha kuzichukua rasilimali zilizopo. Ingawa Uingereza ina utawala mmoja licha ya tamaduni zake nyingi, lakini mara nyingi iliyapa makoloni yake mifumo ya shirikisho au nusu shirikisho.

Charles de Gaulle wa Ufaransa alitawala mashirikisho mawili ya makoloni huko Afrika ya Ikweta na Afrika ya Magharibi, lakini nchi nyingi zinazozungumza Kifaransa zilirithi utawala wa serikali moja isipokuwa Kamerumi iliyojaribu kwa muda utawala wa shirikisho baada kuichukua Kamerumi Magharibi kutoka Nigeria. Jaribio la utawala wa shirikisho wa Senegal-Sudan (Mali) ulishindwa.

Hebu sasa tuangalie jinsi viongozi wa Kiafrika walivyopambana na matatizo ya kujenga mataifa kutokana na dola za utawala wa kikoloni walizorithi.

## Taratibu za kuleta umoja na mabadiliko ya mifumo ya kisiasa

Mara tu baada ya nchi za Kiafrika kupata uhuru, viongozi wake walipata changamoto ya kujenga mambo ya msingi ya utaifa na dola ili kuleta maendeleo ya kisiasa. Miongoni mwa mambo hayo ya msingi ni kuweka mamlaka unganifu ya kisiasa (mara nyingi huitwa utaratibu wa ujenzi wa dola); kuleta umoja miongoni mwa makabila mbalimbali (mara nyingi huitwa utaratibu wa ujenzi wa taifa). Kutoa nafasi za ushirikishwaji kisiasa, na kusambaza rasilimali kidogo zilizopo.

Viongozi wapya waliochukua madaraka ya serikali walijikuta wakiwa na matarajio mengi ya kufanya lakini wakawa na uwezo mdogo wa rasilimali wa kuyatimiza. Je, viongozi wapya wa kisiasa walijaribu kubadili mfumo wa kisiasa waliourithi kwa kujenga taifa kutokana na utawala wa dola waliokuwa wakiuongoza? Huku wakitumia mtindo wa urithishwaji, je viongozi wapya wa kisiasa walifanya nini kwa mfumo wa kisiasa waliourithi katika kujenga mchakato wa ujenzi wa taifa?

Utawala wa kikoloni uliwarithisha wanasiasa wazawa utawala wa serikali kuu iliyodhibiti vyombo vya dola, kama vile polisi, jeshi na mahakama. Urasimu wa kiutawala waliourithi haukuwa siyo tu mwajiri mkuu bali pia ulikuwa msukumo mkuu wa kuleta maendeleo. Serikali ilikuwa na raslimali nyingi za kiuchumi katika nchi.

Kwa kuzingatia mambo haya waliyorithishwa, je, viongozi wapya waliweza kujitenga na miundo ya kikoloni ili wafanikishe malengo yao mapya? Kimsingi kulikuwa hakuna marekebisho yoyote ya maana waliyoyafanya katika vyombo vya dola walivyorithi kwa makusudi ya kujenga taifa. Isitoshe, miundo ya kiutawala ya mataifa na makabila mbalimbali ya nchi hizi haingeweza kubadilika ghafla kwa kuwa tu uhuru umepatikana. Wingi huu wa miundo ulikuwa pia ni sehemu ya uridhi wa kikoloni. Mipaka ya mataifa mapya ya Afrika kamwe haikupakana na mipaka ya mataifa ya zamani, himaya wala falme. Viongozi wapya walichukulia suala la ujenzi wa taifa kuwa ni la muda mrefu. Jambo lililoonekana kuwa ni la haraka ni lile la kuimarisha mamlaka ya serikali kuu waliyorithi na baadaye kupenyeza kwa mafanikio katika sehemu za pembezoni, yaani kujenga dola. Mabadiliko ya kuleta marekebisho ya kijamii yalionekana kufaa zaidi kuliko kuleta mabadiliko ya kimapinduzi.

Miundo ya kiutawala iliyoanzishwa na wakoloni siyo tu iliendelea kubakia bali hata malengo yake hayakubadilika. Nchi zinazozungumza Kifaransa za Afrika Magharibi, pamoja na Ghana, Nigeria, Kenya na Uganda, zimeonyesha kuzidisha

urasimu wa kiutawala dhidi ya vyama vya kisiasa. Hii ni kwa sababu urasimu umekuwa ukichukuliwa kama asasi za udhibiti wa kisiasa.

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizojaribu kwa dhati kuweka malengo mapya kwa urasimu wa dola. Kwa kuzingatia Azimio la Arusha, Nyerere alibainisha malengo ya urasimu kiutendaji kuwa ni "kuiwezesha serikali kuu kutoa msaada na mwongozo kwa wananchi wake pamoja na kupima kazi zao ili kuona kama urasimu unasaidia kupunguza athari za mapokeo ya urasimu wa kikoloni ambao unaweza kuzima ari ya wananchi[1]

Katika sehemu nyingi za Afrika, umuhimu wa urasimu wa kiutawala uliongezeka, ingawa haukuwa dhahiri kama malengo yake yalikuwa yamebadilika. Urasimu katika utawala wa kikoloni ulionekana kama chombo cha kudumisha sheria na amani pamoja na unyonyaji. Watawala wachache walioriithi madaraka hawakuongeza malengo mengine zaidi, kama vile kufanya ustawi jamii uwe lengo mojawapo.

Fedha za mataifa mapya pia huakisi tahadhari za watawala walioriithi dola katika kufanya mabadiliko. Nchi nyingi zinazozungumza Kifaransa katika Afrika bado zinaendelea kutumia fedha ya faranga na nchi nyingi zinazozungumza Kiingereza bado ziko katika ukanda wa pauni (shilingi). Nigeria iliacha kutumia fedha ya ukanda wa "sterling" mwaka 1973, wakati Tanzania na Uganda bado zinatumia neno shilingi kama kima cha fedha.

Wingi wa mambo katika nchi za Kiafrika unakwenda hadi kwenye lugha. Nchi zinazozungumza Kifaransa zinatumia Kifaransa kama lugha rasmi, wakati nchi nyingi zinazozungumza Kiingereza bado zinatumia Kiingereza kama lugha rasmi au lugha ya taifa. Katika Afrika Mashariki, Kiswahili kinatumika kama lugha rasmi ya Kenya, Tanzania na kwa muda fulani Uganda. Kuanzishwa kwa lugha ya Kiarabu kama lugha rasmi ya Sudani kulipingwa na wananchi wa Kusini ya Sudani bila mafanikio yoyote. Lakini Kiingereza bado kinatumika Kusini ya Sudani. Liberia iliamua kutumia Kiingereza kama lugha rasmi, wakati Ethiopia inatumia Amharic. Nchi za Angola, Guinea-Bissau, Cape Verde, Sao Tome na Principe na Msumbiji zote zinatumia Kireno kama lugha rasmi. Viongozi wapya walioriithi madaraka hawakutaka kufanya mabadiliko ya kuanzisha lugha ya taifa kutokana na athari za kisiasa ambazo zingeweza kutokea. Kwa viongozi walio wengi suala hili halikuwa na umuhimu wa kwanza.

[1] J.K. Nyerere, 1972, uk. 2

Mfumo wa elimu katika nchi zinazozungumza Kifaransa au Kiingereza haukubadilika kimaudhui. Hata hivyo, kulikuwepo na upanuzi wa mifumo ya shule. Baadhi ya viongozi wapya wa nchi hawakuona umuhimu wa kuyafanyia maudhui mabadiliko katika mfumo wa elimu.

Utawala wa kikoloni ulidhoofisha sana asasi za jadi. Hata hivyo, huko Nigeria na Uganda watawala wa jadi walishiriki kikamilifu katika masuala ya kisiasa na kiutawala. Huko Uganda, Kabaka (Mfalme) wa Buganda aliwahi kuwa Raisi wa nchi nzima mwaka 1963 kama ambavyo mfalme wa Lesotho alivyopanda kisiasa katika utawala mpya. Huko Kaskazini ya Nigeria, Maamiri walijitwalia madaraka ya kutosha kupitia mfumo wa mamlaka ya wenyeji uliorithiwa kutoka kwa watawala wa kikoloni, na ambao haukufanyiwa mabadiliko mukubwa hadi ulipoingia utawala wa kijeshi. Ingawa nchini Tanzania utawala wa kichifu uliondolewa kisheria, bado machifu waliendelea kufanya kazi zao za uchifu ingawa kwa kiwango cha chini sana. Guinea iliondoa utawala wa kichifu baada ya uhuru kwa sababu ya kupinga mabadiliko na vivyo hivyo Rwanda.[2] Katika himaya ya Kifaransa, Wafaransa walikuwa wamefanikiwa kuwatelekeza machifu na kuwainua waali waliorithi utawala wa kisiasa baada ya wao kuondoka.

Mielekeo ya mitazamo kuhusu asasi za jadi katika nchi huru za Afrika imetofautiana ingawa kuna mielekeo mikuu mitatu. Mwelekeo wa kwanza ni wa viongozi waliorithi madaraka ambao miongoni mwao walikuwa sehemu ya utawala wa jadi, kwa sababu hii waliweka mipaka ya madaraka ya machifu katika siasa na utawala, kama ilivyokuwa huko Nigeria kabla ya 1966. Mwelekeo wa pili ni kama ule wa Nkrumah wa Ghana, ambao aliwaondoa Machifu katika medani ya siasa, lakini akawapa madaraka ya kutoa ushauri. Mwelekeo wa tatu ni ule unaoona kwamba Machifu hawana nafasi katika utawala mpya wa kisiasa kama vile Guinea au Rwanda. Hata hivyo, asasi hizi za jadi bado zipo na zinaendelea kushughulikiwa na utawala wa jeshi au utawala wa raia.

## Itikadi na mifumo ya kisiasa

Kwa sababu ya uchanga wa serikali za nchi za Kiafrika, viongozi wengi waliorithi madaraka walipendelea mfumo wa serikali moja. Huko Ghana, Nkrumah alifanikiwa kupata katiba moja ya nchi nzima, hivyo mabaraza ya kutunga sheria

[2] L. Rubin na B. Weinstein, 1974, kur. 213-14

ya majimbo yakapotea. Katika harakati za kuhamasisha watu dhidi ya asasi za kikabaila na nusu-kikabaila huko Ghana, Nkrumah alikuwa akijaribu kuzuia vitisho vya ubabe vya kutaka kuigawa nchi katika utawala wa majimbo. Wakati wa uhuru, Kenya ilikuwa na mabaraza ya kutunga sheria chini ya katiba ya majimbo. Kenyatta alijitahidi sana kudhoofisha na kuua utawala wa majimbo na mabaraza ya kutunga sheria.

Kenya iliondokana na mfumo wa kibunge uliorithiwa wakati wa uhuru. Hivyo, siyo tu kwamba Kenya ilikuwa na katiba ya aina moja wakati ilipokuwa jamhuri bali pia iliingia kwenye mfumo wa kuwa na Rais mtendaji ambaye alitakiwa awe mbunge wa kuchaguliwa. Marekebisho yaliyofanywa na Kenya kwa asasi za kiserikali, kama tulivyokwishaona huko nyuma, yanadhihirisha madai yetu ya mwanzo kwamba aula za viongozi waliorithi madaraka baada ya uhuru zilikuwa ni kuimarisha dola ya kikoloni na serikali kuu waliyoachiwa nayo. Ingawa utawala wa majimbo ulikuwa umedhoofishwa, bado mwangwi wa ukabila uliendelea kusikika katika Siasa.

Kinyume na Kenya, Nigeria ilikuwa ikiendesha serikali ya mfumo wa shirikisho iliyoanza na mikoa mitatu. Siasa za kikabila za kibabe za Nigeria zilisababisha kuwepo kwa mikoa yenye nguvu na serikali kuu dhaifu katika mfumo wa kibunge. Kinyume na Kenya, Nigeria haikufuata utaratibu wa kuwa na Rais baada ya nchi yao kuwa jamhuri. Harakati za kutaka kujitoa kutoka utawala wa serikali kuu zilipamba moto katika nchi nzima. Waziri mkuu wa kwanza baada ya uhuru, Balewa, alikuwa kiongozi dhaifu wa serikali kuu changa.

Nchi zinazozungumza Kifaransa ziliendelea kuwa na serikali moja isipokuwa Kameruni ambayo ilibadilika na kuwa serikali ya shirikisho baada ya kuungana na Kameruni ya Magharibi. Kutokana na kasumba ya kutawaliwa na Wafaransa iliyobaki kwa viongozi, utegemezi wa vyombo vya dola uliimarishwa na haukuonekana kuwa na matatizo ukilinganisha na nchi zinazozungumza Kiingereza, ambazo zilikuwa na historia ya kutawala baadhi ya vyombo vya dola vya kitaifa. Wakati Tanzania, Msumbiji na Guinea-Conakry zilipendelea kufuata siasa ya kijamaa (kisoshalisti), Nigeria, Kenya na Cote d' Ivoire zilipendelea siasa ya kibepari kama msingi wa kuleta maendeleo. Kati ya nchi zote za Kiafrika, ni Tanzania iliyoonyesha kujishughulisha zaidi katika kubuni mipango yenye mikakati maalumu ya kufikia lengo la itikadi ya ujamaa vijijini na Azimio la Arusha.

Katika nchi zenye utawala wa chama kimoja wenye siasa kali, umuhimu wa vyama katika ujenzi wa taifa uliongezeka baada ya uhuru. Chama cha TANU cha Tanzania, Chama cha PAIGC cha Guinea-Bissau, na chama cha PDG cha Guinea ni mifano

ya nchi zenye utawala wa chama kimoja ambapo vyama hivyo vilikuwa kama vyombo vya kukataa kuwa na mahusiano na watawala wa zamani wa kikoloni ili viweze kufanya mabadiliko katika miundo ya kisiasa iliyorithiwa.

Katika nchi nyingi, mwelekeo umekuwa wa kuelekea kwenye utawala wa chama kimoja au utawala wa chama kikuu kimoja. Harakati za kujiimarisha kisiasa baada ya uhuru mara nyingi zimesababisha kuua vyama vya upinzani, kwa kutumia bunge na wakati mwingine kutumia mbinu mbalimbali za kuua kisiasa.

Hivyo, kufikia 1966 mwelekeo ulikuwa wa kuelekea kwenye utawala wa chama kimoja, au chama kikuu kimoja Baadhi ya vyama k.m. huko Kenya, vimeweza kuzuia kuzuka kwa migogoro ya kikabila. Vyama vingine havikuweza kubadili hali ya ukabila iliyokuwepo au kuhamasisha watu bali vimekuwa asasi za kirasimu za kupenya na kudhibiti maeneo ya vijijini. Katika nchi za Nigeria, Zaire na Ghana, migogoro iliyonzia kwenye vyama vya kikabila ilitoa mwanya kwa jeshi kuingilia kati.

Ujenzi wa taifa katika nchi zenye chama kimoja kama vile Tanzania, Guinea-Bissau, guinea-Conakry chini ya Sekou Toure, Cote d'Ivoire, Kenya na Kameruni umeonyesha mwelekeo wa kudumisha umoja nchini kuliko nchi zenye vyama vingi. Nchi zenye vyama vingi kama vile Nigeria, Zaire na Uganda zilipata matatizo ya kudhibiti utaifa wa makabila mhalimbali hata kimoja? Ni vigumu kusema hivyo, kwa sababu kumbukumbu, zinaonyesha kuwa hata katika baadhi ya nchi zenye chama kimoja kama vile Burkina Faso (zamani ikiitwa "Upper Volta"), Mali na Ghana ya Nkrumah, bado mapinduzi ya kijeshi hayakuzuilika.

Tatizo mojawapo la ujenzi wa taifa linalowakabili viongozi wa Kiafrika ni wao kutoonyesha uzalendo wa kikabila huko Nigeria kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe vya 1967-1970. Migogoro ya wenyewe kwa wenyewe ililipuka huko Zaire na kusababisha kuzuka kwa vita vya kiraia (kuanzia 1960–5) vilivyopelekea jeshi kuingilia kati na kumweka Generali Mobutu madarakani. Chadi imekuwa ikikabiliwa na ghasia za wenyewe kwa wenyewe kutokana na mchanganyiko wa masuala mbalimbali ya kidini, kirangi, kikabila na kiitikadi. Nchi ya Sudan iliwahi kupigana vita vya kiraia kuanzia 1955-72 na baadaye ikarudia kupigana vita vya wenyewe kwa wenyewe. Angola iliwahi pia kuwa na vita vya kiraia baada ya uhuru kuanzia 1975 – 6. Mgogoro huo uliendelea hadi mkataba wa amani wa kusitisha mapigano uliposainiwa tarehe 31/5/1991. Ethiopia ilikuwa na vita vya kiraia zaidi ya mara moja kuanzia 1961 hadi 1991.

Migogoro yote hii ni matokeo ya kuwepo kwa ukabila, utaifa na mara nyingine udini. Migogoro hii imewasumbua sana viongozi waliorithi madaraka. Baada ya

uhuru harakati za kutetea utaifa ndani ya makabila hayo zilizuka na kuongezeka ingawa harakati hizo zilififishwa wakati wa kipindi cha uzalendo cha kupigania ukoloni. Hivyo, juhudi za viongozi waliorithi madaraka za kujenga taifa kutokana na dola mara nyingi zilikwazwa na matatizo ya kuwa na utamaduni wa kikabila kabila.

Kwa kuhitimisha, ni kwamba baada ya ukoloni, Afrika iliendelea na miundo ya kisiasa iliyorithi kutoka utawala wa kikoloni. Kumekuwepo na majaribio machache ya kutaka kuzibadilisha kimsingi asasi muhimu za dola kwa madhumuni ya kujenga taifa. Hata hivyo, taasisi za kibunge zilizorithiwa kutoka nchi za Magharibi zilishindwa kuendelea kutokana na vyama vya kisiasa na mabaraza ya kutunga sheria kupungua umuhimu wake na taratibu za chaguzi kuporomoka. Watendaji wa kimila walitokea na kufanya matatizo ya kurithishana mamlaka ya kisiasa yawe magumu zaidi. Lakini je, ni mambo gani yaliyofanya kuwepo kwa mfululizo wa matukio ya jeshi kuingilia kati utawala wa kisiasa katika Afrika, na ni kwa vipi tawala za kijeshi zilikabili miundo ya kisiasa iliyokuwepo katika harakati za ujenzi wa taifa?

## Kuyumba kwa mahusiano ya raia na jeshi

Tangu jeshi la Wamisri limwangushe mfalme Farouk mwaka 1952, mapinduzi ya kijeshi yalienea sehemu kubwa ya Afrika, kwa mfano mapinduzi ya Sudan yalitokea 1958, huko Zaire yalitokea mwaka 1965, Jamhuri ya Dahomey au Benin mapinduzi yalitokea mwezi Desemba 1965, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Nigeria mwezi Januari 1966 na mapinduzi ya Ghana yalitokea mwezi uliofuata. Mfalme Haile Selassie alipinduliwa mwaka 1974 na Moktar Ould Daddah mwaka 1978. Hivi karibuni kulikuwepo na mapinduzi huko Ghana mwezi Desemba 1981, Nigeria mwezi Desemba 1983 na Mauritania mwaka 1984. Katikati ya miaka ya 1980 Afrika ilikwisha kuwa na mapinduzi ya kijeshi zaidi ya 70.

Kwa nini kumekuwepo na mapinduzi mengi ya kijeshi katika Afrika? Zipo sababu kuu nne za mapinduzi ya kijeshi yatokee katika uwanja wa kisiasa wa Afrika. Sababu ya kwanza ni hii ya mazingira ya nchi au mazingira ya kijamii yalivyo, hii sababu inazingatia mazingira ya kisosiolojia, kisiasa na kiuchumi kwa pamoja. Sababu hii ndiyo husababisha kuwepo kwa mifarakano katika mifumo ya kisiasa na kijamii (ukabila, matabaka n.k.), uongozi unaotatanisha, viongozi wa kisiasa wasiofaa, uchumi mbovu na mienendo ya mahakimu isiyofaa katika jamii. Sababu ya pili ya jeshi kuingilia kati masuala ya kisiasa inatokana na mambo ya ndani ya jeshi au mahusiano ya kijamii yaliyopo katika jeshi, hasa ukizingatia viwango tofauti vya elimu na utaalamu wa wanajeshi, raia kuingilia kati masuala ya kijeshi,

utumiaji wa jeshi katika masuala ya kisiasa, migogoro katika makambi ya jeshi, viongozi wa kisiasa kutumia mikinzamo iliyomo ndani ya vikosi vya jeshi, kushindwa katika vita na mifarakano ya kiumri miongoni mwa wanajeshi wa vizazi tofauti. Sababu ya tatu ya kuwepo kwa mapinduzi ya kijeshi katika Afrika ni ya kimataifa yenye kuvuka mipaka ya jamii inayohusika. Miongoni mwa nyanzo hivi ni matokeo ya mapinduzi yanayofanywa katika nchi moja na kisha kuenea katika uchochezi kutoka nje, na maingilio ya moja kwa moja kutoka nje, hasa nchi nyingine; mtawala wa zamani wa kikoloni anapoingilia kati kijeshi.

Hatimaye, tuangalie sababu nyingine, mbalimbali za kuwepo kwa mapinduzi ya kijeshi. Hizi ni pamoja na migogoro ya watu binafsi, kwa mfano mgogoro kati ya kiongozi wa kijeshi na kiongozi wa juu wa kisiasa, matatizo ya kimaendeleo yanayozidi uwezo wa viongozi, matatizo yanayotakana na uhawilishaji wa jeshi kiasasi na jinsi jeshi linavyoelimishwa na kuelewa misingi ya utawala wa kiraia. Baada ya mapinduzi, utawala wa kijeshi hujikuta ukikabiliwa na matatizo yale yale ambayo utawala wa kiraia ulikuwa ukikabiliwa nayo. Matatizo ya dola na ya ujenzi wa taifa pamoja na maendeleo ya kiuchumi ni baadhi ya matatizo ambayo wamekuwa wakikumbana nayo. Kwa kuzingatia mazingira ya nchi kijamii na kisiasa, uzoefu wa Afrika umeonyesha kuwa utawala wa kijeshi umefanya kazi ya usimamizi, umeleta mageuzi au mabadiliko ya siasa kali.[2]

Dhima ya usimamizi, kwa mifumo ya utawala wa kijeshi wa Mobutu huko Zaire, ni kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa na kunakuwepo amani na siyo kuanzisha mabadiliko ya kijami mara nyingi hii hutokanana na hali ya jumla ya kisiasa ambayo jeshi limerithi. Udhibiti wa kutumia nguvu ndio unaoaminika sana.

Kazi ya kuleta mageuzi katika jamii zaidi huhusu kuanzisha utambulishi wa kitaifa za maendeleo ya kiuchumi. Mara nyingi utawala wa siasa kali huwa ni kiungo cha maslahi baina ya maafisa wa jeshi wa ngazi za chini na kati, na umma ambao hapo zamani haukuwa wameshirikishwa katika mfumo wa kitaifa wa siasa. Mara nyingi utawala unaweza kubadilika kutoka utawala wa siasa kali ukapitia mageuzi hadi ukafikia dhima ya kuwa msimamizi, au ukachukua mwelekeo ulio kinyume cha huo.

Katika Afrika tawala zilizoleta mageuzi ni pamoja na tawala za kijeshi za Nigeria ambazo siyo tu ziliunda shirikisho la taifa lenye utawala imara wa serikali kuu, bali pia ziliunda majimbo 12 ya mwanzo na baadaye 19. Wakati wa kilele cha upatikanaji wa mafuta, walianzisha mipango kadhaa ya kiuchumi na waliendelea kuhimiza uchumi wa taifa kushikwa na wazawa.

[2] L. Rubin na B. Weinstein, 1974, kur. 213-14

JEDWALI 15.1 Mabadiliko ya Serikali Afrika, 1962-92

| | Jina la kikoloni | Tarehe ya uhuru | Mji mkuu | Viongozi tangu kupata uhuru | Mapinduzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Algeria | Algeria | 1962 | Algiers | - Ahmed Ben Bella, 19-5 | |
| | | | | - Kanali Houari Boumedienne, | |
| | | | | 1965-78 | 1965 |
| | | | | - Chadli Bendjedid, 1978-92 | |
| | | | | - Mohamed Boudiaf, 1992 | |
| | | | | - Ali Kai, 1992- | |
| Angola | Angola | 1975 | Luanda | Dk. Agostinho Neto, 1975-9 | |
| | | | | Jose' Eduardo dos Santos, 1979- | |
| Benin | Dahomey | 1960 | Porto-Novo | - Hubet Maga, 1960-3 | |
| | | | (jina rasmi) | - Jenerali Chiristopher Soglo, 1963-4 | 1963 |
| | | | Cotonou (jina | - Sourou-Justin Ahamadegbe | |
| | | | linalotumika) | (Makamu Rais), 1964-5 | |
| | | | | - Tahirou Congacou, 1965 | 1965 |
| | | | | - Luteni Kanali Alphonse | 1969 |
| | | | | Alley (Rais), 1967-8 | 1967 |
| | | | | - Dk. Emile Zinson, 1968-9 | 1969 |
| | | | | - Meja Kouandete, 1969 | |
| | | | | - Hubert Manga, 1970 | |
| | | | | - Sourou-Migan Apithy, 1971 | |
| | | | | - Justin Ahomadegbe, 1972 | |
| | | | | - Meja (baadaye Luteni Jenerali) | |
| | | | | Matthieu Kerekou, 1972-91 | 1972 |
| | | | | - Nicéphore Soglo, 1991 | |
| Botswana | Bechuanaland | 1966 | Gaborne | - Bwana Seretse Khama, 1966-80 | |
| | | | | - Dk Quet Masire, 1980- | |
| Burkina | Upper Volta | 1960 | Ouagadougou | - Maurice Yameogo, 1960-6 | |
| Faso (tangu | | | | - Luteni Kanali (baadaye jenerali | |
| 1984) | | | | Sangoule Lami zana, 1966-80 | 1966 |
| | | | | - Kanali Saye Zerbo, 1980-2 | 1980 |
| | | | | - Meja Jean-Baptiste | 1982 |
| | | | | Ouedraogo, 1982-3 | |
| | | | | - Kapteni Thomas Sankara, 1983-7 | 1983 |
| | | | | - Kapteni Blaise Compaoré, 1987 - | 1987 |
| Burundi | Sehemu ya | 1962 | Bujumvue | - Mwami Mwambutsa IV, 1962-5 | |
| | Rwanda- | | | - Kanali Michel Micombero, 1966- 76 | 1966 |
| | Urundi | | | - Luteni Kanali Jean Baptiste Bagaza, | |
| | | | | 1976-87 | 1976 |
| | | | | - Meja Pierre Buyoya, 1987 | 1987 |
| Kameruni | Kameruni | 1960 | Yaoundé | - Ahmadou ahidjo, 1960-82 | |
| | Cameroon ya | | | - Paul Biya, 1982- | |
| | Kifaransa na | | | | |
| | Kameruni na | | | | |
| | Cameroon | | | | |
| Cape Verde | Visiwa vya | 1975 | Praia | - Aristides Perera, 1975-91 | |
| | Cape Verde | | | - Antonio Mascarenhas Monteiro, | |
| | | | | 1991 | |
| Jamhuri ya | Ubangui-Chari | 1960 | Bangui | - David Dacko, 1960-6 | |
| Afrika ya | | | | - Luteni Kanali (Baadaye Mfalme) | |
| Kati | | | | Jean-Bedel Bokassa, 1966-79 | 1966 |
| | | | | - David Dako, 1979-81 | 1979 |
| | | | | - Jenerali André Kokigba, 1981 | |
| Chad | Chad | 1960 | B'Djamena | - Francois Ngarta Tombalbaye, 1960- 75 | |
| | | | | - Meja Jenerali Felix Malloum, 1975-9 | 1975 |
| | | | | - Coukouni Oueddei, 1979-82 | 1979 |
| | | | | - Hisséne Habré, 19-90 | 1982 |
| | | | | - Idriss Deby, 1990- | 1990 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Comoro | Comoro | 1975 | Moroni | - Ahmed Abdallah, 1975<br>- Ali soilih, 197-8<br>- Ahmed Abdallah na Mohamed Ahmed (Marais Wenza), 1978-89<br>- Said Mohamed Djohar, 1989- | <br>1975<br><br>1978 |
| Kongo | Kongo | 1960 | lBrazzaville | - Abbé Fulbert Youlou, 1960-3<br>- Alphonse Massemba- Debat, 1963-8<br>- Kapteni (baadaye Meja) Marien Ngouabi, 1968-77<br>- Kanali Joachim Yhombi Opango, 1977-9<br>- Kanali (baadaye Jenerali) Denis Sassou Nguesso, 1979-91<br>- Jenerali Denis Sassou Nguesso (Rais), 1991-2<br>- Pascal Lissouba, 1992- | <br><br><br>1968 |
| Pwani ya Pembe | Pwani ya Pembe | 1960 | Abidjan | - Felix Houphouét – Boigny 1960 | |
| Djibouti | Somali ya Kifaransa baadaye Afars na Issas | 1977 | Djibouti | - Hassan Gouled, 1977<br>- Hassan Gouled Aptidon, 1977- | |
| Misri | Misri | 122 | Cairo | - Mfalme Farouk, 1937-52<br>- Jenerali Muhammad Naguib, 1952- 4<br>- Luteni Kanali Gamal Abdal – Nasser, 1954-70<br>- Muhammad anwar al-Sadat, 1970-81<br>- Hasmi Mubark, 1981- | <br>1952 |
| Guinea ya Ikweta | Fernando Poo na Rio Muni | 1968 | Malabo | - Francisco Macias Nguema, Nguema, 1968-79<br>- Luteni Kanali (baadaye brigedia Jenerali). Teodoro Obiang Nguema Mbasogo, 1979 | <br><br>1979 |
| Ethiopia | Ethiopia | Karne ya Kwanza ya enzi ya Ukristo | Addis-Ababa | - Mfalme Haile Selassie, 1932-74<br>- Jenerali Aman Andom, 1974<br>- Jenerali Teferi Bante, 1974-7<br>- Luteni Kanali mengitsu Haile Mariam, 1977-91<br>- Ato Meles Zenawi, 1991 | <br>1974 |
| Gabon | Gabon | 1960 | Libreville | - Leon M'Ba, 1960-7<br>- Albert – Bernard (baadaye Omar) Bongo, 1967 | |
| Gambia | Gambia | 1965 | Banjul | - Bwana Dawda Kairaba<br>- Jawara, 1965 | |
| Ghana | Pwani ya Dhahabu | 1957 | Accra | - Kwame Nkrumah, 1957-66<br>- Luteni Jenerali J.A. Ankrch, 1966-9<br>- Brigedia Jenerali A.A. Afrifa, 1969<br>- Dk. Kofi bosia, 1969-72 | <br>1966 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | - Kanali (baadaye Jenerali) I.K. | |
| | | | | - Acheampong, 1972-8 | 1972 |
| | | | | - Luteni jenerali Frederick Akuffu, 1978-9 | 1978 |
| | | | | - Luteni wa jeshi la anga Jerry J. Rawlings, 1979 | 1979 |
| | | | | - Dk. Hilla Limann, 1979-81 | |
| | | | | - Luteni wa jeshi la anga Jerry J. Rawlings, 1981- | 1981 |
| Guinea | Guinea ya Kifaransa | 1958 | Conakry | - Ahmed Sèkou Tourè, 1958-84 | |
| | | | | - Jenerali Lansana Contè , 1984 | 1984 |
| Guinea Bissau | Guinea ya Kireno | 1973 | Bissau | - Luis de Almeida Cabral, 1973-80 | |
| | | | | - Meja João Bernardo Nino Vieira, 1980- | 1980 |
| Kenya | Kenya | 1963 | Nairobi | - Jomo Kenyatta, 1963-78 | |
| | | | | - Daniel T. Arap Moi, 1978- | |
| Lesotho | Basuto | 1966 | Maseru | - Chifu Leabua Jonathan, 1966 | |
| | | | | - Mfalme Moshoeshoe II, aliondolewa 1966-90 | |
| | | | | - Mfalme Letsie II, 1990- | |
| Liberia | | 1847 | Monrovia | - William V.S. Tubman, 1944-71 | |
| | | | | - William R. Tolbert Jnr, 1971-80 | 1980 |
| | | | | - Afisa Sajenti (baadaye jenerali) Samuel K. Doe, 1980-90 | |
| | | | | - Prof. Amos Sawyer, 1990- | |
| Libya | Majimbo ya Italia ya Cyrenaica, Tripolitania, na Fezzãn | 1951 | Tripoli | - Mfalme Idrãs, 1951-69 | |
| | | | | - Kanali Muammar Gadhaffi, 1969- | 1969 |
| Madagscar | Madagascar | 1960 | Antananarive | -Philibert Tsirinana, 1960-72 | |
| | | | | -JeneraliGabriel Ramanantsoa, 972-5 | 1972 |
| | | | | -Kanali Richard Ratsimandrava, 1975 | |
| | | | | -Luteni Mkuu (baadaye Mkuu wa jeshi la wanamaji) Didier Ratsiraka, 1975. | |
| Malawi | Nyasaland | 1964 | Lilongwe | -Dk. Hastings Kamuzu Banda, 1964 - | |
| Mali | Sudan ya Kifaransa | 1960 | Bamako | -Modibo Keita, 1960-8 | |
| | | | | -Luteni (baadaye Jenerali) Moussa Traoré, 1968-91 | 1968 |
| | | | | -Lut eni Kanali Aadou Toumani Touré, 1991 1991-2 | 1992 |
| | | | | -Alpha Oumar Konare, 1992 – | |
| Mauritania | Mauritania | 1960 | Nouakchott | -Moktar Ould Daddah, 1960-78 | |
| | | | | -Luteni kanali Mustapha Ould Mohamed 1978 Salek, 1978-9. | 1978 |
| | | | | -Luteni Kanali Ahmed Ould Bonceif, 1979 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | -Luteni Kanali Mohamed Khouna Ould Haidalla, 1979-84 | |
| | | | | -Kanali Maaouya Ould Sid Ahmed Taya, 1984 - | 1984 |
| Mauritius | Mauritius | 1968 | Port-Louis | Mawaziri Wakuu: | |
| | | | | Bwana Seewosagur Ramgoolam, 1968-82 | |
| | | | | Aneerood Jugnauth, 1982-92 | |
| | | | | -Cassam Uteem (Rais), 1992- | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Aneerood ugnauth, 1992- | |
| Morocco | Morocco | 1956 | Rabat | -Mfalme Mohamed v, 1956-61 | |
| | | | | -Mfalme Hassan II, 1961- | |
| Msumbiji | Msumbuji | 1975 | Maputo | -Samora Machel, 1975-86 | |
| | | | | -Joaguim Alberto Chissano, 1986- | |
| Namibia | Kusini-Magharibi Africa | 1990 | Windhoek | -Kisheria: Baraza la Umoja wa Mataifa Namibia | |
| | | | | -Ki hali halisi: Afrika Kusini | |
| | | | | -Sam Nujoma, 1990- | |
| Niger | Niger | 1960 | Niamey | -Hamani Diori, 1960-74 | |
| | | | | -Luteni Kanali Seyni Kountche, 1974-87 | 1974 |
| | | | | -Brigedia Ali Saibou, 1987 | |
| Nigeria | Nigeria | 1960 | Lagos (toka 1991 Abuja) | -Dk. Nnamdi Azikiwe (Rais) na Bwana Abubakar. Tafawa Balewa (Waziri Mkuu), 1960-6 | |
| | | | | -Jenerali J.T.A. Aguiyi-Ironsi, 1966 | 1966 |
| | | | | -Luteni Kanali (baadaye Jenerali) Yakubu Gowon, 1966-75 | 1966 |
| | | | | -Jeneli Murtala Muhammed, 1975-6 | 1975 |
| | | | | -Jenerali Olusegun Obasanjo, 1976-9 | |
| | | | | -Shehu Shagari, 1979-83 | |
| | | | | -Meja Jenerali M. Buhari, 1983-5 | 1983 |
| | | | | -Jenerali Ibrahim Babangida, 1985- | 1985 |
| Réunion | Réunion | Idara ya Ughaibuni ya Uransa | Mtakatifu Denis | -Rais wa Ufaransa | |
| Rwanda | Sehemu ya Ruanda-Urundi | 1962 | Kigali | -Gréoire Kayibanda, 1962-73 | |
| | | | | -Meja Jenerali Juvenal Habryarimana, 1973- | 1973 |
| Sao Tome na Principe | Sao Tome na Principe | 1975 | Sao Tome | -Mauel Pinto do Costa, 1975-91 | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Miguel Trovoada, 1975-8 | |
| | | | | -Miguel Troroada, 1991- | |
| Senegal | Senegal | 1960 | Dakar | -Léopold Sédar Senghor, 1960-80 | |
| | | | | -Abdon Diouf, 1981 | |
| Shelisheli | Visiwa vya Shelisheli | 1976 | Victoria | -James Mancham, 1976-7 | |
| | | | | -France-Albert René, 1977- | 1977 |
| Sierra Leone | Sierra Leone | 1961 | Freetown | -Bwana Milton Margai, 1961-4 | |
| | | | | -Bwana Albert Margai, 1964-7 | |
| | | | | -Siaka Stevens, 1967 | |
| | | | | -Brigedia Jenerali David Lansana, 1967-8 | 1967 |
| | | | | -Brigedia Jenerali Andrew Juxon-Smith, 1968- | 1968 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | -Jenerali Joseph Saidn Momoh, 1985-91 | |
| | | | | -Kapteni Valentine Strasser, 1992- | 1992 |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Somalia | Somalia ya Italia na Somalia ya Uingereza | 1960 | Mogadishu | -Aden Abdulle Osman (Rais) 1960-7 | |
| | | | | -Mawaziri Wakuu: Abdi Rashid Ali Shirmarke, 1960-4. Abdi Razak Hussen 1964-7 | |
| | | | | -Abdi Rashid Ali Shirmarke (Rais), 1967-9 | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Mohamed Haji Ibrahim Igul, 1967-9 | |
| | | | | -Meja Jenerali Mohamed Siad Barre, 1969-70 | 1969 |
| | | | | -Ali Mahdi Mohamed, 1990- | |
| Afrika Kusini | Muungano wa Afrika Kusini 1910 (1910-61) | 1910 | Pretoria (utawala) Cape Town (utungaji Sheria) | -Jan Smuts, 1939-48 | |
| | | | | -D.F. Malan, 1948-54 | |
| | | | | -J.G. Strijdom, 1954-8 | |
| | | | | -Dk. Hendrik Verwoerd, 1958-66 | |
| | | | | -B.J. Vorster, 1966-78 | |
| | | | | -P.W. Botha, 1978-89 | |
| | | | | -F.W. de Klerk, 1989- | |
| Sudan | Sudan ya Misri ya Kiingereza | 1956 | Khartoum | -Ismail el-Azhari, 1956 | |
| | | | | -Abdallah Khalil, 1956-8 | |
| | | | | -Jenerali Ibrahim Aboud, 1958-64 | 1958 |
| | | | | -Sayed el-Khatim el-Khalifa, 1964-5 | 1964 |
| | | | | -Mohamed Ahmed Mahgoub, 1965-9 | |
| | | | | -Kanali (baadaye Jenerali) Gaffar Mohamed Nimeiri, 1969-85 | 1969 |
| | | | | -Jenerali Abdulraliman Swareldarhab, 1985-6 | |
| | | | | -Luteni Jenerali Omer Hassan Ahmed el-Bashir, 1989- | 1989 |
| Swaziland | Swaziland | 1968 | Mbabane | -Mfalme Sobhuza II, 1921-82 | |
| | | | | -Mama Malkia Indlovukazi Dzeliwe, 1982 | |
| | | | | -Kaimu Malkia Indovukazi Ntombi, 1983-6 | |
| | | | | -Mfalme Mswati III, 1986- | |
| Tanzania | Tanganyika na Zanzibar | 1961<br>1963 | Dar es Salaam (baadaye yakahamishiwa Dodoma) | -Julius K. Nyerere, 1961-85 | |
| | | | | -Ali Hassan Mwinyi, 1985 | |
| Togo | Togo | 1960 | Lomé | -Sylvanus Olympio, 1960-3 | |
| | | | | -Nivolas Grunitzky, 1963-7 | 1963 |
| | | | | -Luteni Kanali (baadaye Jenerali) Etienne Gnassingbe Eyadema, 1967-91 | 1967 |
| | | | | -Jenerali Etienne Gnassingbe Eyadema (Rais), 1991- | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Joseph Kokou Koffigoh, 1991- | |
| Tunisia | Tunisia | 1956 | Tunis | -Habib Bourguiba, 1956-87 | |
| | | | | -Zine El-Abidine Ben Ali, 1987- | |
| Uganda | Uganda | 1962 | Kampala | -Milton Obote, 1962 | |
| | | | | -Mfalme mtesa II, 1963-6 | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Milton Obote, 1963-6 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | -Milton Obote (Rais), 1966-71 | 1966 |
| | | | | -Jenerali (baadaye Jemedari Mkuu) Idi Amin Dada, 1971-9 | 1971 |
| | | | | -Yusufu Lule, 1979 | |
| | | | | -Godfrey Binaisa, 1979-80 | |
| | | | | -Paulo Muwanga, 1980 | 1980 |
| | | | | -Milton Obote, 1980-5 | 1985 |
| | | | | -Tito Okello, 1985-6 | |
| | | | | -Luteni Jenerali Yoweri K. Museveni, 1986- | 1986 |
| Sahara Magharibi | Sahara ya Hispania | (1975) | El-Aaiun | -Inagombaniwa kati ya Polisario na Morocco | |
| Zaire | Kongo ya Ubeligiji | 1960 | Kinshasa | -Joseph Kasavubu (Rais), 1960-5 | |
| | | | | -Mawaziri Wakuu: | |
| | | | | Patrick Lumumba, 1960 | |
| | | | | Joseph Lleo, 1960-1 | 1960 |
| | | | | Cyrille Adoula, 1961-4 | |
| | | | | Moise Tshombe, 1964-5 | |
| | | | | Evariste Kimba, 1965 | |
| | | | | -Jenerali (baadaye Jemedari Mkuu) Mobutu Sese Seko, 1965-92 | 1965 |
| | | | | -Jemedari Mkuu Mobutu Sese Seko (Rais), 1992- | |
| | | | | -Waziri Mkuu: Etienne Tshisekedi, 1992- | |
| Zambia | Rodesia ya Kaskazini | 1964 | Lusaka | -Kenneth D. Kaunda, 1964-91 | |
| | | | | -Frederick J. Chiluba, 1991- | |
| Zimbabwe | Rodesia ya Kusini | 1980 | Harare | -Padri Rais Canaan Banana, 1980-7 | |
| | | | | -Robert G. Mugabe, 1987- | |

*Chanzo*: A.A. Mazrui na M. Tidy, 1984 na kufanyiwa marekebisho na UNESCO, 1992.

wa kijeshi wamediriki kujitwalia sifa za ushujaa wa kitaifa kama ndio alama ya ujenzi wa taifa kwa mfano Gowon na Murtala wa Nigeria, al-Nasser wa Misri, Kadhaffi wa Libya, na Mobutu wa Zaire. Lakini siyo utawala wa kijeshi wala utawala wa kiraia uliofanikiwa kuhamasisha watu wake katika ujenzi wa taifa isipokuwa nchi chache ambazo viongozi wake walifuata itikadi na mfumo wa siasa wa chama kimoja ili wafikie azma yao ya kujenga taifa.

Hivyo, katika Afrika, asasi za kibunge na za vyama vya siasa zimekuwa zikivurugwa mara kwa mara na utawala wa kijeshi. Urasimu katika muundo wa dola umekuwa ndio msingi wa mamlaka changa kwa viongozi wa Kiafrika. Utawala msonge umekuwa ndio kiungo kutoka kwa wakoloni kupitia viongozi waliorithishwa mamlaka, tawala za kijeshi hadi kurudishwa tena kwa utawala wa kiraia baada ya jeshi kujitoa kutoka uwanja wa siasa (pale ilipotokea). Kwa kawaida, mipaka baina ya uwanja wa jeshi na uwanja wa siasa ni midogo sana kiasi kwamba ubadilishanaji wa kuongoza serikali kati ya jeshi na raia ni mambo yanayoweza kuendelea kutokea kwa kitambo fulani.

## Wahenga na haki za binadamu

Ni mambo gani mabaya yametokea katika migogoro ya Afrika baada ya ukoloni ambayo yameathiri, haki za binadamu? Hapa ni lazima tutofautishe baina ya haki za msingi za binadamu na haki binafsi za binadamu. Kwa mfano, serikali inayokubalika na watu, ni haki ya msingi ya binadamu. Lakini, haki ya kupiga kura ni haki binafsi - ni njia ya kujipatia serikali inayokubalika.

Kwa jumla, katika Afrika ya baada ya ukoloni, kuna makubaliano kuhusu haki za kimsingi za binadamu. Kijadi, jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa zikiongozwa kwa misingi ya imani ya - "serikali kwa ridhaa ya watu". Lakini, tunaongelea idhini ya watu gani? Baadhi ya jamii ziliamini katika kupata idhini, siyo tu kwa watu wanaoishi, bali hata ya watu waliokwisha kufa na wale ambao bado kuzaliwa. Kwa mujibu wa taratibu za kimila, wazee walichukuliwa kuwa ni watu wanaoelewa kuhusu mambo ya wahenga na kwamba walishajipatia hekima kutoka kwao kwa njia ya urithishwaji kupitia utamaduni, mila na desturi. Sera zilizokiuka mila na desturi zilichukuliwa kuwa hazikuwa na baraka ya mizimu. Sera ambazo hazikutoa nafasi kwa watoto kuendelea kuishi kwa furaha zilihesabiwa kuwa hazikuwa na idhini ya vizazi vijavyo. Ulikuwa ni wajibu wa watu wanaoishi kufikiria matakwa ya mizimu na wale ambao bado kuzaliwa - na kuyafanyia kazi kikamilifu. "Serikali kwa ridhaa ya watu" haikuwa tukio tu la uchaguzi kila baada ya miaka minne, mitano au sita. Ilikuwa ni mwenendo wa kurithishana taratibu na kawaida za vizazi

vilivyopita na vizazi vijavyo. Makubaliano ya hiari ndio yaliyoongoza katika kupata msimamo halisi wa umma.

Lakini ukweli ni kwamba himaya za nchi za Ulaya Magharibi zilikwisha anzisha dhana mpya ya demokrasia katika Afrika. Uchaguzi mkuu ukawa ndio njia ya haki binafsi ya kupata serikali yenye ridhaa.

Mtindo wa uchaguzi katika nchi za Ulaya Magharibi umekuwa ni wa kushindanishwa. Kuachwa kwa utamaduni wa makubaliano na kufuata utamaduni wa ushindani katika Afrika baada ya ukoloni kumeharibu misingi ya haki za binadamu. Jamii nyingi katika Afrika zimeonyesha kuwa zinahitaji muda wa kujifunza jinsi ya kukabiliana na ushindani wa kisiasa ili ushindani huo usigeuzwe kuwa uwanja wa machafuko ya kisiasa. Matokeo yameonyesha kumekuwepo na chaguzi za hila, unyanyasaji kwa vyama vya upinzani, ukandamizaji kwa wapinzani na uzuaji wa maoni tofauti katika vyombo vya habari na kwingineko. Katika Afrika, dhana ya haki za binadamu ilipata pigo tangu dhana ya haki za msingi za binadamu ilipofasiliwa bila kuingiza haki za msingi za mila (wahenga) wala haki za msingi za vizazi vya baadaye. Pia dhana ya haki za binadamu ilipata pigo tangu haki binafsi zilipofasiliwa kwa misingi ya Ki-Magharibi ya kimamboleo - kuwa "mshindi anachukua haki zote" katika vipindi vya uchaguzi-mkuu. Mapambano ya baadaye baina ya raia wenye mwelekeo wa nchi za Ulaya Magharibi na wanajeshi watumiao silaha za Ulaya Magharibi yamechangia sana katika kuvunja haki za binadamu. Machafuko ya kutisha yalitokea katika miaka ya 1970 katika sehemu kama vile za Uganda wakati wa Idi Amin, Afrika ya Kati wakati wa utawala wa Jean Bedel Bokassa na Equatorial Guinea wakati wa Fransisco Macias Nguema.

Ikiwa masuala ya haki na wajibu yatazingatiwa, itabidi yaanzie kwenye mila na yarithishwe. Ikiwa ujenzi wa taifa umeshindwa kutokana na kukosekana kwa mshikamano wa kitamaduni wa utambulishi kitaifa katika Afrika, pia vivyo hivyo haki za binadamu.

Kuingiliana kwa utamaduni katika Afrika baada ya ukoloni kumetoka siyo tu baina ya kabila moja na jingine (kama ilivyo katika Nigeria), siyo tu baina jamii moja na nyingine (kama ilivyo katika Afrika ya Kusini), siyo tu baina ya kizazi na kizazi kingine (kama ilivyo katika Ethiopia). Angalau katika Afrika jambo jingine la msingi limekuwa ni kutenganisha mambo yaliyopita na mambo ya sasa. Huku kuingiliana kiutamaduni ni sehemu ya usuli wa uonevu, ukandamizaji na utesaji katika Afrika baada ya ukoloni. Ubaguzi wa rangi katika Afrika Kusini ni moja tu ya mambo hayo japo hata zaidi, yanayokiuka misingi ya haki za binadamu. Kuna aina nyingi za uvunjaji wa haki za binadamu katika Afrika, bara la watu weusi. Ni kwa jinsi gani matatizo haya yanaweza kutatuliwa? Njia moja ni hii ya kuwa na

ufuatiliaji na utetezi wa haki za binadamu katika bara zima la Afrika. Afrika inahitaji chombo cha utetezi wa haki za binadamu kama kile cha *Amnesty International* au bora zaidi, Tume ya Ulaya ya Haki za Binadamu. Tunahitaji asasi inayoongozwa na waafrika ili waweze kuwaeleza Waafrika wenzao juu ya maadili ya utendaji wao katika shughuli za umma. Lakini Afrika pia inahitaji mfumo unaohusu Afrika nzima ambao ndani yake utawawezesha raia waliodhulumiwa kuweza kuishitaki serikali yao kwa kukiuka haki za binadamu. Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (uliopitishwa Juni 1981, ulianza kutumika tarehe 21 Ocktoba 1986, wakati uliporidhiwa kwa wingi wa kura) na wa Azimio la Banjul la Haki za Binadamu na wa Haki[8] za jamii ni hatua muhimu kwa Afrika ya kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu katika miongo ijayo. Kwa kiwango hicho, hatua hizi zihesabiwe kuwa sehemu ya harakati ya ujenzi wa taifa na ujenzi wa dola katika Afrika ya baada ya ukoloni.

## Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kuwa ujenzi wa dola na taifa siyo mambo mapya katika Afrika dola na himaya za kabla ya ukoloni zilikabiliana na changamoto hizi. Hata hivyo, nchi nyingi za sasa hazishabihani na mataifa haya kabla ya ukoloni. Mara nyingi jamii zisizohusiana zilijikuta zikiwekwa katika dola moja wakati wa kinyanganyiro cha nchi za Ulaya kugombea makoloni katika Afrika. Tawala za kikoloni zilianzisha asasi kadhaa katika makoloni yao ambayo baadaye yalipata uhuru na kuwa nchi zenye dola kamili. Kwa hiyo, ujenzi wa taifa umekuwa na maana ya kuwaunganisha watu wa aina mbalimbali katika utawala wa dola mpya ili kujenga taifa la kisiasa ambalo watu wake sasa watatakiwa kuwajibika kweli, kutii na kulitetea.

Tuliona hata hivyo kwamba kulikuwa na matatizo ya kufanya mabadiliko ya mfumo wa dola kwa viongozi walioirithi madaraka. Miundo ya kikoloni na hata miundo ya kisiasa kabla ya ukoloni (utawala wa kichifu) iliendelea kuwepo na hii ilifanya taratibu za ujenzi wa taifa kuwa mgumu. Zaidi ya haya, kwa sababu ya kulinda maslahi ya watawala wa baada ya ukoloni ya kujiimarisha katika mamlaka na walizozirithi, watawala hao hawakuchukua hatua za kuleta mabadiliko ya kiasasi au ya kimuundo.

Miundo ya kikoloni iliyorithiwa ilishindwa kufanya kazi sawasawa isipokuwa katika sehemu chache. Hata katika nchi ambazo mfumo wa utawala wa chama kimoja ulifanikiwa katika ujenzi wa dola kama vile Zambia, Malawi, Kameruni na Côte d Ivoire – vyama hivyo kwa kiasi fulani vilikuwa kama vyombo vya udhibiti

(ujenzi wa dola) kuliko kuwa vyombo vya ujenzi wa taifa.

Kwa kawaida kufifia kwa vyama vya kisiasa kulifanya taratibu za ushindani za uchaguzi na taratibu za kiutawala za kibunge kufifia pia. Maingiliano ya kijeshi katika baadhi ya nchi yalikamilisha kifo cha miundo hiyo.Muundo uliodumu zaidi ni ule wa utawala msonge, wa dola ambao ndio umeendelea kuwepo katika tawala nyingi.

Ingawa kuna mabadiliko machache ya kimiundo yaliyofanywa katika nchi za Kiafrika ili kuhamasisha watu kwa ujenzi wa taifa, jitihada hizo zimeshindwa kuzaa matunda kutokana na vipingamizi mbalimbali. Huko nyuma tumeona sababu mbalimbali zilizofanya Afrika ishindwe katika ujenzi wa taifa. Baadhi ya sababu hizo ni mirathi ya utawala wa kikoloni. Sera ya usimilishaji (wa Wafaransa) na mbinu ya utawala wa serikali kuu ilifanya watu katika makoloni ya Wafaransa ya zamani wawe na utamaduni mmoja na misingi ile ile ya kisiasa. Mataifa haya yanaweza kupata matatizo kutokana na utegemezi kwa watawala wao wa zamani wa kikoloni, lakini kwa kuwa msingi wa ukoloni wao ulikuwa na lengo la kujenga utamaduni mmoja, hayatapata matatizo makubwa yakilinganishwa na nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza.

Nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza zilipambwa na majivuno ya kijamii ya Waingereza na utaratibu wao wa kuhimiza utamaduni na utawala wa kujitegemea. Mambo haya yaliweka msingi na kuundwa kwa madola huru. Lakini katika kuanzisha mataifa huru yanayojiamulia mambo yake yenyewe, utawala usio dhahiri uliendeleza taratibu za kimila na miundo ambayo ilitambulisha uasili au tabia zilizokuwepo kabla ya kuundwa kwa taifa, hivyo, kufanya ujenzi wa taifa kuwa mgumu zaidi katika makoloni ya zamani ya Kiingereza kuliko ilivyo katika makoloni ya Kifaransa. Kulihali, ujenzi wa taifa katika nchi yoyote ile ni kazi ngumu ya kisiasa.

Ikiwa asasi za kiutawala za kichifu kabla ya ukoloni ziliendelea kubakia katika tawala mbalimbali, hususani katika makoloni ya zamani ya Waingereza, na kuna vikwazo katika ujenzi wa dola - basi hivyo ni vikwazo halisi hata katika ujenzi wa taifa kama ilivyokuwa huko Nigeria na Uganda. Tawala hizo zimekuwa ndio msingi wa udhibiti wa utaifa finyu wa kikabila.

Ni hivi karibuni tu ambapo nchi za Kiafrika zilianza kurekebisha mifumo yao ya elimu, japo elimu (pamoja na dhima iliyojificha ya kumwezesha mtu aishi na kufuata taratibu za jamii) ni muhimu kwa ujenzi wa taifa. Mambo mengine yanayohusiana nayo ni dhima ya itikadi na elimu ya siasa. Ni nchi chache sana katika Afrika

zilizotumia itikadi katika ujenzi wa taifa. Itikadi ni miongozo inayosaidia nchi ziondokane na miundo ya kiutawala ya kikoloni.

Mwisho kabisa, tunamalizia sura hii kwa kusema kwamba viongozi wengi wa nchi za Kiafrika wamejishughulisha zaidi na kubadili miundo ya kisiasa kwa madhumuni ya kuimarisha nguvu ya dola kuliko ujenzi wa taifa. Kwa vile taratibu za ujenzi wa dola na ujenzi wa taifa katika nchi za Kiafrika zinakwenda sambamba, juhudi zisipochukuliwa kuleta mabadiliko katika miundo ya kisiasa ambayo huongeza ufanisi katika taratibu za ujenzi wa taifa, hata taratibu za ujenzi wa dola zitaendelea kuwa dhaifu. Msako wa mshikamano zaidi katika utaifa na mamlaka yaliyo imara katika dola unaendelea kuwa ndio msingi muhimu zaidi wa matendo ya kisiasa katika Afrika ya baada ya ukoloni.

# 16

# Ujenzi wa Taifa na mabadiliko ya kisiasa

## Utangulizi

Mikinzano miwili imetawala mienendo ya kisiasa katika Afrika katika kipindi kilichoanzia mwaka 1935. Ukinzani baina ya Ujamaa na Ubinafsi kwa upande mmoja na ukinzani baina ya utaifa na usiasa-huria (pluralism) kwa upande mwingine. Wanafikra kama vile Julius K. Nyerere wa Tanzania na Tom Mboya wa Kenya waligundua kuwa Ujamaa wa asili ungeweza kuwa msingi muhimu kwa mifumo ya kisasa ya kisoshalisti. Sekou Toure alitumia Ujamaa wa asili kupinga karibu mifumo yote ya ubinafsi nchini Guinea baada ya ukoloni. Mawazo ya kijamaa yalichangia katika kufikiria uhalali wa kuwa na chama kimoja cha kisiasa nchini Guinea na sehemu nyingine katika Afrika baada ya Ukoloni. Kwa upande wa Gamal 'Abd al-Nasser', yeye alifuata itikadi zote mbili ya ujamaa na ya utaifa lakini kimsingi alipinga itikadi ya usiasa-huria na hakuamini juu ya ubinafsi.

Kulikuwa na awamu ngapi za itikadi katika historia ya Afrika tangu 1935? Je, inawezekana kukigawa kipindi hiki katika awamu tofauti za kiitikadi? Kipindi cha utangamano baina ya utaifa usiasa-huria katika nchi nyingi zinazozungumza Kiingereza na Kifaransa katika Afrika kilitokea miaka ya mwisho ya utawala wa kikoloni (1945-60). Utaifa wa Kiafrika ulijidhihirisha katika misemo ya wito kama vile "mtu mmoja kura moja", demokrasia ya vyama vingi na uhuru wa vyombo vya habari. Kulikuwa na uhusiano kati ya utaifa na usiasa-huria ki-Magharibi zilitumiwa dhidi ya nchi za Magharibi zenyewe. Misemo ya wito kama hiyo haikufua dafu katika utawala wa kikoloni wa Wareno.

Baada ya uhuru, nchi nyingi za Kiafrika zilishuhudia kufifia kwa ujenzi wa taifa na demokrasia ya kiliberali (huria) (1965-85). Baadaye, mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990 kulitokea uamsho wakiliberali uliokuja na

madai ya umma ya demokrasia ya vyama vingi na ubinafsishaji wa uchumi.

Amali za kisiasa katika Afrika zilitawaliwa na kitu ambacho Kwame Nkrumah alikiita "udhamiri" (consciencism) – ambazo ni mwingiliano wa mila asili, Uislamu na utamaduni wa Kikristo wa Ulaya.

Ni kwa namna gani mawazo haya yanayohusishwa na amali za kisiasa yamezingatiwa katika tajiriba ya Kiafrika?

## Ujenzi wa taifa na amali za kisiasa

Kuongezeka kwa ushindi katika kudai mfumo huria katika miaka ya 1989-90 kumeleta tatizo la amali za kisiasa zilizoongoza matendo ya viongozi wa Kiafrika katika miongo michache ya nyuma. Karibu kila nchi katika bara la Afrika imekubali kutekeleza mpango wa kurekebisha uchumi uliopendekezwa na asasi za fedha za kimataifa. Zaidi ya haya, baadhi ya nchi (Benin, Msumbiji, Ethiopia n.k) zimekataa asasi za Umarx-Ulenin, jambo ambalo linaonyesha kuwa asasi hizo hazikuwa zimepata mashiko katika tabaka tawala wala miongoni mwa raia katika jamii. Kwa mara nyingine tena, nchi za Kiafrika zinaelekea kukabiliwa na tatizo la kuchagua mifumo ya kiamali ya kufuata. Utawala wa kikoloni uliharibu asasi nyingi za kisiasa za Kiafrika pamoja na mifumo yake ya amali. Baadhi ya amali ziliendelea kudumu baada ya asasi zinazohusika kutoweka; na mapambano dhidi ya ukoloni yalikuwa ni ya mjadala na pia yalikuwa ni mapambano kudhibiti malengo na misukumo ya matendo ya kisiasa.

Ushindi wa kupata uhuru katika miaka ya 1960 ulikuwa ni muhimu katika kuchagua amali za kisiasa, ambayo matokeo yake yanaonekana kadiri karne hii (ya ishirini) inavyokaribia kwisha kwenye miaka ya mwanzo ya uhuru, ujenzi wa Afrika ulikabiliwa na vipingamizi vingi: umoja wa kitaifa uligongana na baadhi ya maslahi bandia ya makabila: umoja wa Kiafrika ulizuiwa na malengo ya kutaka kuwa na mataifa madogo madogo. Zaidi ya hayo, mipango ya kijamii iliyolenga kuleta maendeleo kwa watu wengi iligongana na baadhi ya amali za jamii mbalimbali za kabla ya ukoloni na za mfumo wa ukoloni.

Mwanzoni, watawala wa Kiafrika walichagua ama kubakia na hali ya ukoloni mamboleo au kuwa na mabadiliko kamili ya amali za Kiafrika na za kimataifa za kijamii na kisiasa. Hata hivyo, kufikia miaka ya 1980, watawala karibu wote walikuwa wakizungumzia amali za aina moja za mapokeo kabla na wakati wa ukoloni.

Kama kianzio cha uhamasishaji wa mawazo, amali huzaa historia, lakini pia amali huzalishia, huathiriwa na kubadilishwa na historia. Nini basi sifa muhimu za

kudumu na ni yepi mabadiliko muhimu katika amali za Kiafrika tangu 1935? Ni zipi nguvu za ujenzi wa taifa tangu harakati za kupigania uhuru hadi kufikia muongo wa mwisho wa karne ya ishirini? Ni amali zipi zinaongoza matukio, asasi na itikadi zinazoelezea mabadiliko hayo?

## Kutoka utawala wa kikoloni hadi usiasa-huria katika kupigania uhuru

Mfumo wa kikoloni ulikuwa umejengwa juu ya mkusanyiko wa amali za kisiasa zenye ufungamano kiasi. Mfumo huu ulianzishwa kwa makusudio mawili ya ustarabishaji na unyonyaji. Katika makoloni ya Waingereza, makusudio haya yalitekelezwa kwa kutumia utawala usio dhahiri. Kwa upande wa mataifa ya kikoloni yaliyokuwa na sera ya usimilishaji, ulazimishaji wa amali za kisiasa za kikoloni ulikuwa wazi zaidi. Baada ya vita vya pili vya dunia, madai ya waafrika ya kutaka wapate uhuru na waunde serikali zao yaliendeleza usiasa-huria kwa upande mmoja na kutetea utaifa kwa upande mwingine.

### Mirathi ya usiasa-huria

Katika nchi zilizokuwa na mabadiliko ya amani ya kuelekea uhuru, usiasa-huria kwa kuzingatia msingi wa uliberali katika nchi tawala. Kwa kuzingatia uhuru wa mtu binafsi, itikadi ya kiliberali iliwapa misingi ya kisheria na mbinu za kisiasa viongozi wa Kiafrika waliokuwa wakipambana na ukoloni.

Afrika kaskazini ilikuwa na usiasa-huria, isipokuwa Algeria: Misri ilitumia katiba ya 1923, na Tunisia katiba ya 1955 ambayo kimsingi ilikuwa ya kiliberali; na Moroko ilikubali utaratibu huo baada ya makubaliano na Mohammad V (1956-61) kati ya ufalme wa jadi na asasi za kibunge. Hata hivyo, baada ya vipindi mbalimbali kupita, nchi za kaskazini ya Afrika zilijikuta zikikataa usiasa-huria.

Katika Afrika ya kusini mwa Sahara, vyama vingi na vikundi mbalimbali vilienea sana kati ya 1945 na 1960. Katika *Gold Coast* chama cha *United Gold Coast Convention* kilikuwa na umri wa miaka miwili tu wakati Kwame Nkrumah alipojitenga na kuanzisha *Convention People's Party*. Huko Nigeria, katiba za 1945 na 1948 ziliruhusu kuwepo kwa vyombo vya habari ambavyo viliungwa mkono na vyama vya vijana, vyama vya wafanyakazi na vyama vya siasa ambavyo vilijikita kwenye majimbo muhimu ya nchi. Huko Sierra Leone na Gambia, usiasa-huria ilianzisha mshikamano wa *Ma-Creoles* dhidi ya wenyeji asilia. Katika the British Central African Federation, majadiliano ya pande tatu yaliendeshwa kati ya Waafrika, Wazungu walowezi na serikali ya London.



16.1 Mwandishi wa Kifaransa Franz Fanon aliyezaliwa Martinique

Katika makoloni yaliyotumia lugha ya Kifaransa kulikuwepo na vyama vile vile vya kisiasa vilivyokwishaenea, usimilisho uliwachagua wawakilishi wa Waafrika kuingia katika mabaraza ya mabunge ya Ufaransa, kuwaingiza viongozi wa kisiasa katika amali za kisiasa za Ufaransa.[1]

Kabla ya uhuru, amali za kisiasa zilizoendelezwa Afrika zilipuuza sifa za kidemokrasia za kijadi, na hivyo kuvuruga mahusiano yaliyopo baina ya masuala ya kisiasa na ya kiraia. Hata hivyo, kuhawilishwa kwa itikadi za kisiasa za nchi za Magharibi kulichochea nguvu ya ujenzi wa taifa na harakati za kudai uhuru. Usiasa-huria uliwezesha vyama vyenye nguvu visikilizwe madai yao na kuwa vyama vya kutegemewa katika kuongoza vyama vingine vyenye misimamo ya wastani au ya kikale ambavyo vilikuwa karibu na utawala wa kikoloni.

[1] Tazama R.F. Betts, 1985, kur. 312-31

## Amali za utaifa

Utaifa wa Kiafrika uliendelea kukua katikati ya mapambano na upinzani kwa utawala wa kikoloni. Hivyo, uhamasishaji wa chama cha Nyerere huko Tanganyika ulionekana kama ni mwendelezo wa mapambano ya vita vya Maji Maji dhidi ya ubeberu wa Kijerumani mnamo miaka ya 1904-6. Huko Zimbabwe, uasi wa 1896-7 dhidi ya utawala wa kikoloni ulirejelewa. Mirathi ya uasi wa kidini na wa kitamaduni ilitumika pia, mathalan huko Kenya wana-harakati KANU (Kenya African National Union) walitumia itikadi ya madhehebu ya Mumbi na Dini ya Musambwa. Mapambano ya kujikomboa yalipata nguvu kutokana na kuhusianishwa, kuhamasishwa na kuhalalishwa na mapambano ya zamani.

Mapambano ya vita vikuu viwili vya dunia, utekaji uliofanywa na majeshi ya kikoloni yaliyodaiwa kuwa "yanatuliza nchi", matumizi ya watu weusi kwa wingi katika vita vya utiishaji upya wa kikoloni-yote haya yaliipa heshima dhana ya kutumia silaha kupinga utawala wa kikoloni. Amali za utaifa wa kimapambano zilitiliwa nguvu na nadharia ya Kimarx-Kilenin, ambayo ilifanya matumizi ya nguvu yawe ndiyo "nyenzo" ya historia, na ubeberu uwe ndiyo hatua ya juu kabisa ya ubepari.

## Utaifa na utamaduni mpana

Itikadi ya taifa - dola, pamoja na ubeberu wa kibepari, ni moja kati ya nguzo mbili zilizoupatia ushindi utawala wa kikoloni. Itikadi hii ilirithishwa katika nchi zilizotawaliwa wakati wa kupata uhuru.

Jambo lingine la muhimu katika utaifa ni dini, kama ilivyoonyeshwa katika maasi ya Mahdi dhidi ya utawala wa kigeni mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, na pia miongoni mwa Wasomali dhidi ya Waingereza na Wataliano, na huko Afrika Magharibi (Senegal, Mali, Mauritania). Dini ya jadi ya Kiafrika pia ilichochea upinzani, kama vile huko Tanganyika kati ya miaka ya 1905-7 ambako wapiganaji wa Maji Maji waliamua kupigana vita na Wajerumani wakitumia imani ya Maji Matakatifu kujikinga dhidi ya risasi.

Ingawa dhana ya ukabila ina maana zaidi ya moja, bado ukabila una sifa za msingi zinazotambulisha utaifa. Hivyo vuguvugu la Mau Mau huko Kenya (1952-60), mbali na kudai ardhi, pia lilipigania kukombolewa kitamaduni kwa Wakikuyu na makundi mengine ya Kiafrika (Meru na Embu). Upinzani wa Washona huko Kusini mwa Zimbabwe, Wafoni huko Dahomey, Wawolof au Wadiola wa Senegal ulikuwa na maana ya kulinda ukabila na wakati huohuo kuendeleza mapambano haya katika kiwango cha kitaifa.

Moja ya kipimo muhimu cha taifa-dola ni eneo au nchi. Badala ya maeneo haya kuwa matokeo ya juhudi za karne nyingi zilizopita, mipaka ya nchi huru za Kiafrika imetokana na ushindi wa wakoloni na nchi zilizoshirikishwa katika utawala wa kikoloni ambao baadaye ulivunjika. Hivyo amali za utaifa mara nyingi zilihusishwa na amali za umoja wa Kiafrika.

Rene Pleven, Mfaransa mashuhuri alisema: "kutawala nchi fulani ni kueneza ustaarabu" Hivyo Ukoloni ambao ni jambo muhimu kiuchumi, ni suala la kiutamaduni pia. Kukaribia mwisho wa karne ya kumi na tisa, E.W. Blyden, mtetezi wa mwamko na fahari ya kijamia ya watu weusi, wa bara hili na wa diaspora (wale ambao wako sehemu za mbali waliotawanyika) na akaanzisha umoja wa Waafrika wa bara zima. Katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini, umoja huu uliongozwa na Waafrika wenye asili ya Kiamerika, kama vile Marcus Garvey wa Jamaica, George Padmore wa Trinidad na W.E.B. DuBois wa Marekani. Ni mpaka mwaka 1945, katika mkutano wa tano wa Umoja wa Waafrika wa bara zima uliofanyika Manchester nchini Uingereza, ndipo umoja huu ulipotoka mikononi mwa Waamerika weusi na kuingia mikononi mwa Waafrika weusi. Wajumbe wawili waliokuwepo katika mkutano huo, Kwame Nkrumah wa Ghana na Jomo Kenyatta wa Kenya, baadaye wakawa waanzilishi wa nchi mpya za Kiafrika zilizopata uhuru.

Huko Afrika Kaskazini, uwanja wa kisiasa ulitawaliwa na mitazamo miwili: mtazamo wa Kiislam wa utaifa na mtazamo huria (wa kiliberali). Palikuwapo pia na mitazamo ya kati yenye kupendelea kuunganika uhuru wa binafsi na uislamu.

Kufikia mwisho wa karne ya kumi na tisa, Mmisri mmoja Muhammad Abduh aliongoza umoja, uliowahimiza watu kuzingatia misingi ya Koran lakini bila kukataa michango ya mawazo kutoka nje, k.m. maendeleo kuelekea kwenye asasi za uwakilishi, au kanuni zinazosisitiza kutenganisha nguvu za kiroho na nguvu za kimwili (kidunia). Wana-Udugu wa Kiislamu walipinga mageuzi ya aina yoyote na wasoshalisti walilaani usasa wa kiliberali wa kibwanyenye.

Mchapuko wa kihistoria wa kuelekea kwenye uhuru ulikuja kabla ya kufanya usanisi wa usasa wa nchi za Kimagharibi na mapokeo ya kitamaduni ya kiasili. Kukosekana huku kwa falsafa ya jumla inayohusu utamaduni wa taifa na ukombozi ulikuwa na athari kubwa katika mabadiliko ya jumla ya baadaye ya nchi za Kiafrika.

Kipindi cha kuanzia 1935 hadi uhuru kilitawaliwa na amali kuu mbili za kisiasa: usiasa-huria na utaifa, ingawa kiundani kulikuwa na mvutano mkongwe zaidi wa kiutamaduni baina ya ujamaa na ubinafsi. Kufikia miaka ya 1960, mipaka ya itikadi hizi ilikuwa iko wazi na ilianza kutoa nafasi kwa amali nyingine.

## Amali za kisiasa tangu uhuru

Kupatikana kwa Uhuru wa nchi za Kiafrika kulipunguza amali za usiasa-huria Mwanzoni, miito ya salamu za kisiasa, nyimbo za taifa na bendera katika nchi mpya zilizopata uhuru zilielezea amali za kujenga umoja kama vile "taifa moja, lengo moja, imani moja" (Senegal), "Umoja, Uhuru, Kazi" (Zimbabwe) "Uhuru na Haki" (Ghana). Nyimbo za Taifa zilisifu harakati za mapambano ya pamoja, Uhuru, Umoja na heshima ya wahenga. Bendera, nembo na alama ya nchi zilitumia ishara za wanyama (tai wa Nigeria, simba wa Senegal, chui wa Zaire). Kuhusu rangi, rangi ya kijani ilitumiwa sana; iliwakilisha rasilimali ya mimea, Uislam au matumaini. Rangi nyekundu pia ilitumiwa kumaanisha damu ya mashahidi, mashujaa waliofia nchi yao katika mapambano au katika mapinduzi rangi ya njano (dhahabu au jua) na rangi nyeusi, ikitambulisha taifa au ikirejelea uislam.

Kwa ujumla, tunapata ujumbe wa kiitikadi wa aina nne: tamko la utambulishi, kiu ya maendeleo, haja ya kuwa na umoja na wito wa kuwa na uhuru na haki ya kijamii.

## Itikadi mpya za kisiasa

Baadhi ya viongozi wa nchi huru za Kiafrika waliunda itikadi zao, miongoni mwao ni al-Nasser, Nkrumah, Senghor, Bourguiba, Sekou Toure, Nyerere, Amilcar Cabral na Kaunda. Gamal 'Abd al Nasser wa Misri alisisitiza msimamo wake wa kuacha kufuata amali huria za Kimagharibi na kuamua kusaka umoja wa Waarabu, Uislam, ujamaa wa Kiarabu , Umoja wa Waafrika wa bara zima na kutaka kuwa raisi mwenye haiba na nguvu. Akiukana mfumo wa demokrasia wa Kimagharibi, alikubali kufuata mfumo wa kijamaa utakaokuza demokrasia ya kiuchumi na kuukomboa umma kwa ujumla. Itikadi hii ya Nasser ilikuwa ni ya kijamaa na inayopinga u-Marxi. Ujamaa wa Kiarabu ulifuata mfumo wa siasa wa chama kimoja ambao ulikataa kumkana Mungu na udikteta wa tabaka la wafanyakazi. Itikadi yake pia ilisisitiza umuhimu wa kuwa na umoja wa Waarabu na hivyo kumweka al Nasser karibu na wafuasi wa Ba'th. Mawazo makuu ya Nasser na Ba'th ni kuwa na demokrasia ya kijamaa, Ujamaa unaoamini kuwepo kwa Mungu, amali za Kiislam (udugu, kulinda jumuiya), umoja wa Waarabu, na kuwategemea watu yalienea sehemu zote za Afrika Kaskazini.

Huko Algeria, mapinduzi ya Kiislam ya kijamaa ya wakulima yalizuka kutokana na mapambano ya kujikomboa yaliyojaribu kuunganisha utaifa na kujitawala wenyewe, chini ya himaya ya Ben Bella kwanza na baadaye chini ya chama cha

Mwisho, mfuasi wa ujamaa wa Kiafrika, Leopold Sedar Senghor,.alikiri kwamba nadharia ya Marxi ina manufaa, lakini alikataa kukubali itikadi inayotetea harakati za kitabaka na inayodai kuwa hakuna Mungu.

Mawazo yote haya yaliyokuja chini ya uainisho wa Ujamaa wa Kiafrika, yalikuwa yameathiriwa sana na Uislam, u-Marxi-Lenini na amali za kijadi za Kiafrika. Je tawala za aina gani zilizotokea katika Afrika kutokana na itikadi hizi za zamani na mpya?

## Amali za Kiafrika za baada ya ukoloni

Aina tano hivi za utawala zilitokea katika Afrika. Aina ya kwanza ni utawala wa kijamaa ambao ulianzishwa na wale viongozi ambao tayari mawazo yao tumekwisha yajadili. Mkondo huu wa kijamaa uliongozwa na Nasser mwaka 1952 wakati alipovunja vyama vyote huko Misri na akaanzisha chama cha serikali cha Umoja wa Waarabu wa kijamaa.[4] Tukio hili liliungwa mkono sehemu nyingi za Afrika kwa kutumia majina mbalimbali (*k.m. Rally front congress nk*) vikundi vyote hivyo vilijipa ukiritimba wa kudhibiti mawasiliano kati ya wanachama na wananchi wa kawaida. Katika miaka ya 1960, Kwame Nkrumah wa Ghana, Sekou Toure wa Guinea, Madibo Keita wa Mali na Julius Nyerere wa Tanzania, wote walizifanya nchi zao kuwa chini za mfumo wa kijamaa wa chama kimoja. Katika miaka ya 1970, viongozi wa Msumbiji, Guinea-Bissau na Angola, pia nao walikubali nchi zao zijiunge na nchi za kijamaa.

Aina ya pili ni utawala wa kijeshi (taz. Sura ya 15). Tawala za aina hii ambazo idadi yake hubadilika mwaka hadi mwaka ni zile ambazo watawala wa kiraia huondolewa na askari kwa njia ya mapinduzi ya kijeshi. Muafaka hufikiwa kwa nguvu kwa kutumia mtutu wa bunduki na utawala wa sheria hukataliwa.

Aina ya tatu ya utawala ni wa ubaguzi wa rangi (apartheid) ambao ulitumika Afrika ya Kusini tu. Utawala huu ulitekeleza amali za kinyama kama zile za kutojali usawa wa binadamu, ubaguzi wa kuwatenga watu kwa rangi zao na mauaji ya kijamii. Utawala huo uliziingiza nchi za mstari wa mbele za kusini mwa Afrika katika machafuko kama vile mapigano ya kikabila vita vya ukombozi (Namibia) mapinduzi ya kijeshi, uhamaji wa watu kwa lazima n.k. na hivyo kuzuia taifa katika nchi nyingi.

Aina ya nne ni utawala uspotaka mabadiliko.. Aina hii inatetea mtazamo wa kibepari katika kuleta maendeleo na ujenzi wa taifa huku watawala wakipendelea mfumo wa chama kimoja na kuhodhi madaraka yote. Aina hii ya utawala

[4] J. Nyerere, 1963 uk. 8

inajumuisha sehemu kubwa ya nchi za Kiafrika zikiwemo Côte d'Ivoire, Sierra Leone, Senegal, Kameruni, Kenya, Zambia, Zaire, Malawi na Gabon. Moja ya amali zao za msingi ni "usasa" au ukuaji wa kiwango cha juu. Asilimia 60 mpaka 80 ya mapato ya mauzo ya nje yanatokana na uuzaji wa bidhaa chache za kilimo na madini. Kutokana na kujenga ubepari wa dola, madaraka na utajiri ni vyombo muhimu sana katika kufanikisha mawasiliano. Watu wa matabaka ya chini, ambao wamenyimwa nafasi ya kufaidika kiuchumi, hawana haki ya kujieleza. Haya ndiyo mazingira yanayofaa katika kujilimbikizia mali kusikozuilika bila kujali maslahi ya watu wa chini wasio na mtetezi. Mfumo huu wa utawala unawakilisha kiini cha matatizo ya Kiafrika, kwani unajumuisha mabaya yote ya mifumo mitatu: urithi wa Kiafrika, ubepari huria na Umarx-Ulenin wa mataifa ya zamani ya Mashariki.



PLATE 16.3 Amilcar Cabral wa Guinea – Bissau, rais wa PAIGC, akiwa vitani upande wa Mashariki

Ni nchi tano tu zinazozingatia amali za usiasa-huria na utawala wa demokrasia wa kibunge. Nchi hizi ni: Gambia, Botswana, Senegal, Namibia na Mauritius. Ni kweli kwamba katika nchi hizi hali ya uchumi inaonekana kuwa ni nzuri kiasi tu kuliko nchi nyingine, hii ina maana kwamba nchi zote za Kiafrika zinakabiliwa na vikwazo

vilevile vya kimuundo. Hata hivyo, kulingana na amali za kisiasa, mazingira ya nchi hizi ni tofauti.

Umoja wa Waafrika wa bara zima na kutofungamana na upande wowote
Mada hizi mbili zitajadiliwa katika sura za 24, 25, na 28 hapa chini. Inatosha tu kusema hapa kwamba ingawa uongozi wa umoja wa Waafrika wa bara zima ulihama kutoka kwa Waafrika weusi wa Amerika na kwenda kwa Waafrika weusi wa Afrika katika mkutano mkuu wa tano wa Umoja wa Waafrika wa bara zima uliofanyika Manchester mwaka 1945, umoja huu wa Waafrika wa bara zima haukuwahi kufanya kazi barani Afrika hadi Ghana ilipopata uhuru wake mwaka 1957. Kwame Nkrumah alitayarisha mikutano miwili Akkra: mkutano wa wakuu wa nchi za Kiafrika zilizokuwa zimepata uhuru na mkutano mkuu wa Waafrika wote. Suala la eneo linalounda Umoja wa Waafrika lihingizwa wakati huu na kupewa fasili za aina mbili: eneo linalovuka Sahara, msingi wa umoja ukiwa ni upekee wa kijiografia ya Afrika, na eneo linalovuka bahari ya Atlantiki, ambalo msingi wake ni upekee unaotambulisha taifa la watu weusi. Kiitikadi, Umoja wa Waafrika wa bara zima ulisisitiza juu ya mada mbili, Umoja wa Waafrika wa bara zima uliotetea ukombozi na umoja wa Waafrika wa bara zima uliosaka muungano wa Waafrika. Mada zote hizi mbili zitajadiliwa baadaye.

Itikadi ya pili iliyopata kuwa sehemu ya mtazamo wa kiulimwengu wa nchi za Kiafrika ilihusu kutofungaman na upande wowote. Hakuna kanuni yoyote ya sera ya nchi za nje katika nusu ya pili ya karne ya ishirini iliyokuwa na athari kubwa kwa mahusiano baina ya nchi ndogo na nchi kubwa kuzidi ile ya kutofungamana na upande wowote. Nkrumah na al-Nasser walikuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa Kiafrika wa siasa ya kutofungamana na upande wowote. Umoja huu ulikuwa ni mshikamano wa utetezi na ulitaka kusafisha mahusiano ya nchi za Mashariki na Magharibi. Tangu mkutano wa wakuu wa nchi uliofanyika Algeria mwaka 1973, umoja huu umetaka mfumo mzima wa kiulimwengu ufanyiwe marekebisho ili kudumisha haki katika mahusiano ya Kaskazini na Kusini.

## Mielekeo mipya ya kisiasa katika Afrika

Mielekeo mipya ilianza kuonekana katika miaka ya 1970 katika siasa za ndani za Afrika. Kwanza, tawala za kijamaa ziliporomoka katika Afrika, na pili, kulikuwepo na mabadiliko ya kutoka utawala wa kijeshi kwenda utawala wa kiraia huko Ghana na Nigeria. Zaidi ya yote utawala wa chama kimoja na wa kidikteta uliachwa, badala yake ikarejeshwa demokrasia huria na mfumo wa vyama vingi vya siasa.

## Kushindwa kwa mfumo wa kijamaa

Mfumo wa kijamaa ulifahamika sana kwa watu katika miongo ya kwanza ya uhuru lakini baadaye ukafifia na kutoweka. Huku kushindwa kwa mfumo wa kijamaa kunatokana na nini?

Hali hii ya kushindwa ilianza miaka ya 1960 na baadaye ilichochewa na kuanguka kwa ukomunisti huko Ulaya ya Mashariki. Inaelekea mazingira ya kijamii na kiuchumi hayakutosheleza kufanya ujamaa ustawi. Mawazo ya watu wengi kuhusu ujamaa katika miongo ya kwanza ya uhuru yalikuwa ni yale yaliyokuwa yakiunga mkono mfumo huo kwa sababu wazalendo wengi wa Kiafrika wa wakati huo walihusisha ubepari na ukoloni mamboleo na ukoloni. Sababu ya pili ni kwamba mtazamo wa kibepari kimaendeleo ulionekana haukidhi haja, ujamaa ukaonekana kuwa ndio unaofaa. Sababu ya tatu ni upotofu ambao ulionekana kuenea haraka miongoni mwa watawala baada ya ukoloni. Sababu ya nne ilikuwa ni imani tu kwamba utamaduni wa jadi wa Kiafrika ulikuwa ni wa kiujima na kwa hiyo ulikuwa wa kijamaa. Sababu hizi ndizo zilizofanya mawazo ya wakati huo yapendelee ujamaa, na mara baada ya uhuru, serikali nyingi za Kiafrika zilizungumzia ujamaa, japo kwa maneno bila ya vitendo.

Sababu ya kwanza ya kisosiolojia iliyokwaza za ujamaa ilihusu ukabila. Ukabila katika Afrika una nguvu kuliko mwamko wa kitabaka. Kwa mfano, wakati Oginga Odinga alipojaribu kuanzisha chama cha kijamaa chenye nguvu, aligundua kuwa wafuasi wake hawakuwa watu wa hali ya chini wa Kenya bali karibu wote walikuwa ni Waluo. Tunaweza kusema kwa uhakika kwamba kila kunapotokea ushindani baina ya nguvu za ukabila za mwamko wa kitabaka, ukabila wakati wote umekuwa ukishinda katika Afrika.

Sababu ya pili ya kisosiolojia iliyokwaza za ujamaa ni nguvu za kitamaduni za tabaka tawala. Hili tabaka tawala lilitokana kwa kiasi kikubwa na Waafrika waliosomea katika nchi za Magharibi na ndio ambao waliochukua madaraka kutokana na elimu ya Kimagharibi. Kwa Waafrika, kuwa mfuasi wa Marxi ilikuwa haiwezikaniki mpaka kwanza mtu huyo apitie utamaduni wa Kimagharibi.

Sababu ya tatu inahusu uwezo wa Afrika wa kiutawala katika kipindi hiki cha historia. Juhudi za pamoja zinazojengwa kwenye mila, jadi, na mahusiano ya kiukoo hazikuiandaa Afrika kwa juhudi za pamoja zinazoendeshwa kwa amri badala ya taratibu za kimila.

Sababu ya nne ya Afrika kutokuwa na mazingira ya kufaa ya kisosiolojia kwa ajili ya mfumo wa kijamaa, inaturudisha nyuma kuangalia uendelevu wa kihistoria. Uchumi wa nchi nyingi za Kiafrika ulikuwa tayari umeshirikishwa katika uchumi

wa kiulimwengu uliotawaliwa na nchi za Magharibi. Nchi za Kiafrika zilizochagua ujamaa nazo zilijikuta zimekwisha ingizwa katika mfumo wa kiulimwengu wa kibepari. Hivi leo nchi kama Tanzania inategemea sana mfumo wa kiulimwengu wa kibepari kuliko hata ilivyokuwa kabla ya kuanzisha jaribio lake la kufuata mfumo wa ujamaa mwaka 1967. Pamoja na mawazo mazuri ya kutia moyo, Afrika bado haijawa na mazingira ya kufaa kwa mfumo halisi wa ujamaa.



16 4 Tom Mboya wa Kenya aliyekuwa kiongozi wa Chama cha Wafanyakazi na Waziri wa Mipango ya Uchumi; aliyeuawa mwaka 1969

## Kurejelea amali za demokrasia huria

Harakati zinazoendelea katika nchi nyingi za Kiafrika hivi sasa zinataka utawala wa chama kimoja na utawala wa kijeshi ukomeshwe na badala yake uruhusiwe mfumo wa vyama vingi na uchaguzi wa ushindani na kuonyesha haki za binadamu. Madai mengine ni haki za kijamii, uwajibikaji, ubinafsishaji, soko huria, ugatuzi wa madaraka (kuyapeleka ngazi za chini) na kuruhusu ushirikishwaji wa matabaka

yote katika kutoa maamuzi ya kuleta maendeleo. Hata wafuasi wa mfumo wa chama kimoja na wale wa mfumo wa kisoshalisti wa maendeleo kama ule wa Nyerere, wameingia katika mfumo huria wa kidemokrasia. Viongozi kama vile Houphouet-Boigny wa Côte d' Ivoire na Kenekou wa Benin wameruhusu mfumo wa vyama vingi na uchaguzi huru. Kumekuwepo na chaguzi huru na zenye ushindani huko Benin, Cape Verder Sao Tome na Principe, Gabon na Senegal.

Katika nchi nyingine kama vile Ghana, Nigeria, Côte d'Ivoire na Kenya, kulikwishakuwa na madai ya demokrasia na utawala wa kiraia tangu mwanzoni mwa miaka ya 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1970 baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa chama kimoja au utawala wa kijeshi wa kidikteta. Kuanguka kwa ukomunisti wa Ulaya mashariki na ule wa Urusi, na shinikizo za shirika la IMF na nchi za Magharibi zenye viwanda vinawalazimisha viongozi wa Kiafrika kukubali mageuzi ya mfumo huria badala ya kuyakandamiza kiholela na kikatili kama ilivyokuwa mwanzo. Hoja mbili zilikuwa zikitolewa mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960 kutetea uanzishwaji wa mfumo wa chama kimoja. Hoja ya kwanza ni ulazima wa kuwa na umoja wa kitaifa dhidi ya kuwa na matabaka au makundi ya makabila, na hoja ya pili ni madai ya kutaka maendeleo.

Hata hivyo, baada ya miongo ya kuwa na mfumo huo wa chama kimoja, hakukupatikana umoja wa kitaifa wala maendeleo katika nchi hizi za Kiafrika. Kinyume chake, ilikuwa dhahiri kwamba ilipofikia mwishoni mwa miaka ya 1970, nchi chache za kidemokrasia kama vile Mauritius na Botswana zilikuwa zimepiga hatua kubwa na nzuri zaidi katika maendeleo ya kiuchumi, utengemano wa kisiasa na ujenzi wa taifa. Yaliyotokea katika nchi zenye chama kimoja cha siasa ni ukandamizaji wa haki za msingi za binadamu, utawala wa kidikteta wa wazi, upotofu ulioakithiri na upendeleo wa ndugu. Vyombo vya dola vilihodhi sehemu kubwa ya shughuli za jamii, viongozi wa chama, viongozi wa kijeshi na wateja wao nao pia walihodhi rasilimali yote na utajiri wa dola. Sasa Waafrika wengi wanajiuliza, kwa nini tuzungumzie juu ya maendeleo na umoja kama amali za lazima? Wanachotaka sasa Waafrika siyo tu kufuata mienendo ya kidemokrasia huria bali pia kurudi kwenye amali zilizowakilishwa na kuashiriwa katika kauli-mbiu za kitaifa, nyimbo za taifa na bendera: Umoja wa kitaifa, maendeleo, uhuru na haki katika jamii.

## Kuelekea itikeli mpya wa kibepari

Katika msukumo wa sasa wa kuelekea kwenye mfumo huria wa kidemokrasia wa maendeleo, je, Afrika ifuate mtazamo wa kimagharibi wa ubinafsishaji na soko huria? Kwa kuzingatia kwamba ukabila na upendeleo wa ndugu bado vina

nguvu, je, hakutakuwa na uwezekano wa soko lote likadhibitiwa au likapendelewa na kabila moja au makabila mawili? Je, kuna haja ya Afrika kuweka sheria za kuzuia uhodhi wa kibiashara wa makabila fulani; kwa mfano uhodhi wa makabila ya Waigbo huko Nigeria au Wakikuyu nchini Kenya kama ulilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya uhuru.



LATE 16.5 Ahmed Sekou Toure, rais wa Jamhuri ya Guinea, 1958-84

Fundisho kubwa la pili ni jinsi gani kupenda ufahari katika uchumi wa Kiafrika kulivyoweza kuendeleza ulaji wa kujionyesha na ulafi wa kikabaila na ushaufu wa kifalme kugawa katika nadharia ya uchumi ya kimapokeo lengo la kupata faida lilitakiwa liambatane na uzalishaji mwingi zaidi lakini katika tabia za uchumi wa Kiafrika, lengo la ufahari linaegemea utumiaji kwa wingi. Zaidi ya yote, bidhaa

nzuri zinazotumiwa mara nyingi zinaagizwa kutoka nje ya nchi na zinahitaji fedha za kigeni. Wakati watu wa nchi za magharibi wanapotaka nchi za Kiafrika zibinafsishe, wanategemea kwamba msukumo wa kupata faida utaachiwa ufanye kazi yake kulingana na nguvu za soko. Lakini kusema kweli, tatizo katika sehemu nyingi za Afrika siyo tu namna ya kuzindua na kuhimiza msukumo wa kupata faida bali pia jinsi ya kudhibiti na kuzuia mwelekeo wa kupenda ufahari. Tunaweza kudai kuwa tatizo hili linahitaji kushughulikiwa haraka kuliko lile la kwanza la kupata faida. Je, ingefaa Afrika ianze kuthamini zaidi uzalishaji na ubunifu kuliko ulimbikizaji wa vitu?

Tatizo la tatu muhimu la kibinafsi katika soko ni tatizo la upotofu. Upotofu unaweza kuua uzalishaji na unajitokeza kote katika sekta ya umma na katika sekta binafsi. Ubinafshaji wa uchumi unaweza kuwa ubinafisishaji wa upotofu. Ubepari umeingia katika Afrika bila itikadi ya kiprotestanti ya kazi na kujinyima. Uprotestanti haukupinga silika ya upataji, bali ulichukizwa na silika ya utumiaji, hususani wa kukithiri. Ubepari uliingia Afrika kwa lengo la kulimbikiza mali lakini bila ya kuwa na nidhamu katika kazi na uangalifu katika matumizi. Maisha ya starehe ya walowezi weupe yalitoa mfano mbaya kwa Waafrika. Nia ya heshima ya Ki-Afrika, ambayo toka mwanzo ilikuwa ni ya kijamii, sasa ilipewa umbo la kikoloni la utamaduni aghali wa utumiaji wa Ulaya.

Kwa kiasi fulani, changamoto hapa inahusu mbinu zinazotumiwa kupata utajiri. Je, utajiri unaundwa au unapatikana? Je, tunaweza kubadilisha silika ya upataji katika Afrika kuwa kitu kingine kinachohusika moja kwa moja na uzalishaji?

Lakini ikiwa mbinu za kupata fedha zinahitaji ubunifu, basi hatima ya kupata utajiri inatakiwa iwe njema, na matumizi ya kifahari kwa kawaida si mema. Itikadi ya Kiafrika ya ujasiri mali inahitaji kufanyiwa marekebisho ya msingi kuhusu namna ya kupata na kutumia utajiri na rasilimali zilizopo katika jamii. Vinginevyo, uzoefu wa Kiafrika unaonyesha kwamba ubinafsishaji siyo lazima iwe ndiyo njia pekee ya kupata soko huru katika tamaduni zote. Mambo mengine ya kijamii, kiadilifu na kisheria yanahitajika pia.

## Hitimisho kronolojia ya itikadi

Ni mielekeo gani ya kimawazo na kiamali imekuweko katika Afrika tangu mwaka 1935? Katika kiwango cha jumla, tumeona ukinzani wa kawaida baina ya ujima na ubinafsi. Tumeona pia ukinzani baina ya usiasa-huria na utaifa, ukinzani wenye kubeba dhana mbalimbali tofauti kama demokrasia na umoja wa Waafrika wa bara zima, dola na ukabila. Sura hii pia imezungumzia kitu ambacho Nkrumah

alikiita udhamiri, kitu ambacho kinachanganya utamaduni wa asili, Uislamu na ustaarabu wa Kikristo wa Ulaya.

Lakini je, kivitendo kuna mielekeo iliyo dhahiri katika Afrika ambayo inaweza kuainishwa katika vipindi vidogo vidogo tangu mwaka 1935?

Tumekwishaona tayari kipindi cha kushamiri kwa muungano baina ya usiasa-huria na utaifa katika miaka ya mwisho ya utawala wa kikoloni. Kauli za kudai ukombozi zilitumika dhidi ya watu wa nchi za Magharibi ili kutetea na kulinda utaifa.

Katika miaka ya 1960, sehemu kubwa ya Afrika ilijikuta iko katika utawala wa mabavu. Tawala nyingi zilidai kuwa zinafuata ujamaa hata kama zilifuata mfumo wa kibepari. Madai kuhusu "ujamaa wa Waarabu" yalikuwa na nguvu katika sehemu za Afrika Kaskazini, al-Nasser alikuwa mwanzilishi wa umoja wa Waarabu wote, Umoja wa Waafrika wa bara zima na umoja wa siasa zisizofungamana na upande wowote.

Hata hivyo, kilichokuwa kikikosekana katika miaka ya 1960 ni tamko tu kwamba itikadi ya U-Marxi-Lenini ni rasmi. Itikadi hii haikuwa na nguvu hadi katika miaka ya 1970 ndipo ilipopata kuwa na mashiko katika bara la Afrika. Kulikuwepo na sababu kuu mbili muhimu: Kwanza, ni mapinduzi ya kijamii yaliyotokea katika baadhi ya nchi na pili, ni kutokana na kuanguka kwa himaya ya Wareno. Mapinduzi ya Ethiopia ya mwaka 1974, yalichukuliwa kuwa ndio kilele cha mapinduzi ya kijamii yaliyowahi kutokea katika Afrika katika nusu ya pili ya karne ya ishirini. Utawala uliomrithi Haile Selassie ulitamka kuwa unafuata mfumo wa U-Marxi-Ulenini. Baada ya kuanguka kwa utawala wa Kireno, Jamhuri ya Bukini, (Malagasy), Kongo, Benin, Angola na Msumbiji, zote zilifuata mwelekeo wa ki Marxi-Lenin. Hiki kipindi cha kushamiri kwa Umarxi-Ulenini kilifikia mwisho katika miaka ya 1980 na usiasa-huria (ilianza kurudi tena katika miaka ya 1990. Nchi nyingi zilirejesha katiba za vyama vingi na kuwa na chaguzi za ushindani, lakini kama mifumo hii mipya ya siasa itadumu au la, ni jambo ambalo litajulikana..

maangamizi, kutokana na matendo mabaya au kukosa kuwa na mahusiano mazuri na majirani au na wahenga au na miungu. Ili kupata afya njema, mponyaji ataulizia juu ya mahusiano haya na atayatatua matatizo haya kwa njia ya maombi, kutoa sadaka au kufanya yote mawili. Dalili za magonjwa ya mwili zilitibiwa na dawa za miti shamba au na manuizo kama ni lazima. Uamsho wa dini ya jadi wa siku hizi unahusishwa na utambuzi wa watawala wa umuhimu unaendelea wa mfumo wa uponyaji wa kijadi katika huduma za afya. Utambuzi huu rasmi umepunguza ulazima wa kufanya mambo haya kwa siri miogoni mwa wateja wasiokwisha wa mfumo wa uponyaji wa jadi.

Halidhalika, siku hizi watu wengi wanatambua thamani ya mapokeo simulizi ya jadi ya Afrika ambayo hadi wakati huu yalikuwa yakirutubishwa na dini za jadi. Wingi wa hekima kutoka vizazi mbalimbali vya Kiafrika unapatikana katika hazina hii ya mapokeo ya mdomo. Busara na heshima waliyo nayo wanavijiji wanaofikiriwa kuwa mbumbumbu inatokana na mwendelezo huu wa mapokeo ya utamaduni wa jadi. Cha muhimu zaidi ni urithi wa maarifa ya sayansi katika kilimo, na afya uliomo ndani ya mapokeo ya jadi, ulikuzwa kwa karne nyingi zilizopita kwa njia ya uchunguzi makini, majaribio na vitendo. Maarifa mengi ya elimu hii yamerithishwa kupitia katika mafunzo ya makuhani na watabiri, ambayo katika sehemu nyingi yameendelea kutolewa kwa uangalifu wa hali ya juu. Uhusiano huu na imani za dini ndio umedumisha mifumo hii ya maarifa na mawazo, ambayo ndiyo msingi wa utamaduni wa kipekee wa Kiafrika, na mchango wa Mwafrika katika hazina ya mawazo ya kiulimwengu.

Ni kejeli kuona kwamha wasomi wa Kiafrika waliosomea nchi za Magharibi walikuwa wakiziacha dini zao bila hata kuzijua. Watu wengi wa Nchi Mpya za huko Kuba, Brazil, Haiti na kwingineko walichagua kwa makusudi kufuata dini za mapokeo ya jadi kutokana na misingi yake mizuri ya kiroho badala ya kufuata Ukristo na Uislamu. Hivyo wengi wameweza kuoanisha vizuri amali za kiroho za Ukristo na za dini ya jadi ya Kiafrika.


Hadi karibuni, wafuasi wa dini ya jadi hawakuwahi kupeleka madai mengi serikalini kama kundi wakidai washirikishwe katika utawala au katika kusimamia masuala ya elimu au raslimali za kiuchumi. Hata hivyo mara kwa mara viongozi walihitaji nguvu za kiutamaduni za dini ya jadi katika harakati za kuuondoa ukoloni, na katika kusaidia itikadi, teolojia na falsafa ya Kiafrika. Katika mazingira ya hivi sasa ya kisiasa-kijamii ya baada ya ukoloni, baadhi ya viongozi wa jadi wanafikiria ni muhimu kuanza kusisitizaia juu ya misingi ya dini iliyokuwepo kabla ya utawala

maangamizi, kutokana na matendo mabaya au kukosa kuwa na mahusiano mazuri na majirani au na wahenga au na miungu. Ili kupata afya njema, mponyaji ataulizia juu ya mahusiano haya na atayatatua matatizo haya kwa njia ya maombi, kutoa sadaka au kufanya yote mawili. Dalili za magonjwa ya mwili zilitibiwa na dawa za miti shamba au na manuizo kama ni lazima. Uamsho wa dini ya jadi wa siku hizi unahusishwa na utambuzi wa watawala wa umuhimu unaendelea wa mfumo wa uponyaji wa kijadi katika huduma za afya. Utambuzi huu rasmi umepunguza ulazima wa kufanya mambo haya kwa siri miogoni mwa wateja wasiokwisha wa mfumo wa uponyaji wa jadi.

Halidhalika, siku hizi watu wengi wanatambua thamani ya mapokeo simulizi ya jadi ya Afrika ambayo hadi wakati huu yalikuwa yakirutubishwa na dini za jadi. Wingi wa hekima kutoka vizazi mbalimbali vya Kiafrika unapatikana katika hazina hii ya mapokeo ya mdomo. Busara na heshima waliyo nayo wanavijiji wanaofikiriwa kuwa mbumbumbu inatokana na mwendelezo huu wa mapokeo ya utamaduni wa jadi. Cha muhimu zaidi ni urithi wa maarifa ya sayansi katika kilimo, na afya uliomo ndani ya mapokeo ya jadi, ulikuzwa kwa karne nyingi zilizopita kwa njia ya uchunguzi makini, majaribio na vitendo. Maarifa mengi ya elimu hii yamerithishwa kupitia katika mafunzo ya makuhani na watabiri, ambayo katika sehemu nyingi yameendelea kutolewa kwa uangalifu wa hali ya juu. Uhusiano huu na imani za dini ndio umedumisha mifumo hii ya maarifa na mawazo, ambayo ndiyo msingi wa utamaduni wa kipekee wa Kiafrika, na mchango wa Mwafrika katika hazina ya mawazo ya kiulimwengu.

Ni kejeli kuona kwamba wasomi wa Kiafrika waliosomea nchi za Magharibi walikuwa wakiziacha dini zao bila hata kuzijua. Watu wengi wa Nchi Mpya za huko Kuba, Brazil, Haiti na kwingineko walichagua kwa makusudi kufuata dini za mapokeo ya jadi kutokana na misingi yake mizuri ya kiroho badala ya kufuata Ukristo na Uislamu. Hivyo wengi wameweza kuoanisha vizuri amali za kiroho za Ukristo na za dini ya jadi ya Kiafrika.

Hadi karibuni, wafuasi wa dini ya jadi hawakuwahi kupeleka madai mengi serikalini kama kundi wakidai washirikishwe katika utawala au katika kusimamia masuala ya elimu au raslimali za kiuchumi. Hata hivyo mara kwa mara viongozi walihitaji nguvu za kiutamaduni za dini ya jadi katika harakati za kuuondoa ukoloni, na katika kusaidia itikadi, teolojia na falsafa ya Kiafrika. Katika mazingira ya hivi sasa ya kisiasa-kijamii ya baada ya ukoloni, baadhi ya viongozi wa jadi wanafikiria ni muhimu kuanza kusisitizaia juu ya misingi ya dini iliyokuwepo kabla ya utawala




*PICHA 17.1 Mgawanyiko wa Ukristo, Uislamu na dini za kijadi za Kiafrika katika Afrika, ambako kila dini inadai kuwa na asilimia 50 au zaidi ya wakazi wote wa nchi husika. (Chanzo: imetoholewa toka The World Almanac of Books and Facts, New York, 1991, © Pharos Books, 1990)*

# 17 Dini na mabadiliko ya kijamii

## Utangulizi

Inasemekana kwamba katika Afrika, dini hutawala maisha binafsi na maisha ya jamii kwa ujumla. Dini haihusu tu mambo ya imani, bali ni sehemu ya maisha, ni msingi wa utamaduni, utambulishi na kaida za amali. Dini ni sehemu muhimu ya mapokeo ya jadi inayosaidia kukuza utengamano wa kijamii na ubunifu wa uvumbuzi.[1]

Tatizo la dini katika jamii ya Kiafrika inayobadilika linatokana na mambo mawili, nguvu ya imani na wingi wa dini. Dini ya jadi ya Kiafrika ilikuwa ni chombo cha kuelewa nguvu za asili na kupangilia maarifa mapya kuhusu binadamu na mazingira yake halisi. Katika uchunguzi wa kutaka kuelewa na kuishi sawasawa na mazingira yalivyo, Waafrika walitambua miungu mingi na wakaanzisha madhehebu mengi. Dini ya mapokeo ya jadi ya Kiafrika haikuwa ya kushawishi watu bali ilikuwa iko wazi kwa watu wote. Hivyo dini ya Kikristo na Kiislamu mwanzoni zilikuwa zikitegemeana na dini ya jadi. Lakini dini ya Kikristo na Kiislamu zote ni dini za ushawishi zinazodai mafunuo ya kweli na ya pekee ambayo hayavumilii kushirikiana na dini nyingine, hasa dini hizo mbili hazipendi kuishi pamoja. Katika ushindani huu, Ukristo wa mwanzo uliondolewa huko Afrika Kaskazini na kwenye bonde la mto Nili, isipokuwa miongoni mwa wakhufu wa Misri na kule Ethiopia. Harakati za vipindi vya matengenezo na utakaso wa dini zilileta mwendelezo kuanzia pale ambapo Uislam na Ukristo ulipokuwa ukifasiliwa

[1]. *Tazama Presence Africaine, 1972; V.Mulago, 1980; M. Glele, 1981.*

katika misingi ya mapokeo ya dini ya jadi ya mazingira ya Kiafrika hadi pale ambapo Uislamu na Ukristo ulitoa misingi ya kuangalia ulimwengu ambayo iliingizwa katika jadi za kifikra za kijamii za Kiafrika na hivyo kuzaa kile ambacho Nkrumah alikiita "uzoefu wa Kiafrika wa dini ya Kiislamu na dini ya Kikristo ya Ulaya."

Shughuli za misioni za Kikristo katika Afrika katika karne ya kumi na tisa, mwanzoni mwa ukoloni, zilichangia kuleta utata kuhusu mambo ya dini. Katika akili ya Waafrika wengi, dini ya jadi ya Kiafrika ilianza kuhusishwa na Afrika iliyoshindwa na kutiishwa. Watu wengi walianza kujitangaza kuwa wafuasi wa Ukristo au Uislam kama dini zinazowakilisha maendeleo na maisha ya baadaye bila kuacha mtazamo wao wa zamani kiulimwengu, na bila kuacha misingi ya imani za dini yao. Elimu ya nchi za Magharibi iliyoendeshwa zaidi na wamisionari wa Kikristo, ikawa ndiyo chombo cha kujipatia maarifa mapya na cha kuwaondoa Waafrika kwenye utamaduni wao wa jadi.

Kwa hiyo, tatizo lililompata Nkrumah na viongozi wenzake katika kipindi cha kuondoa ukoloni lilikuwa ni namna ya kufanikisha mabadiliko ya kijamii na kuanzisha taifa jipya, hasa kwa kuzingatia nguvu za imani za dini na tofauti za mitazamo ya kidini katika jamii. Je, dini ya jadi inatakiwa ifanye nini? Ni jinsi gani mtu anaweza kuwa muumini safi wa Uislam au Ukristo na bado akawa Mwafrika mzuri? Mgongano wa amali na itikadi mbalimbali ulileta kiwewe katika maisha binafsi ya watu na jumuiya, tatizo ambalo limeongelewa sana katika riwaya kadha. Wanahistoria wameonyesha shauku kutaka kujua dhima ya dini mbalimbali za kijadi katika kuhamasisha harakati za mapambano ya ukombozi katika Kenya, Zimbabwe, Moroko, Algeria, Senegal, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (Zaire) na Zambia. Wamefanya utafiti juu ya umuhimu wa dini katika mapambano baina ya makundi mbalimbali yanayohitaji uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe, na vikundi vidogo vinavyopinga dini yenye nguvu inayotaka kulazimisha imani yake iwe ndiyo dini ya taifa.

Ingawa siyo rahisi kupata takwimu sahihi,[2] inaelekea kwamba katika mwaka 1935 karibu asilimia 80 ya Waafrika wote walikuwa wamegawanyika katikati baina ya Uislamu na Ukristo, huku Uislamu ukiwa umezidi kidogo. Tangu hapo, dini zote, Uislamu na Ukristo, zimekuwa zikitoa madai ya ushindani ya kusonga mbele dhidi ya dini ya jadi ya Kiafrika. Hata hivyo, nchi za Kusini na Kati ya

*2. Linganisha, kwa mfano, seti mbili zinazotofautiana za takrimu kwa ajili ya Uganda, 1977, katika Pro Mundi Vita (Brussels), 1985, na M. Glele, 1981.*

Afrika zilizozoea kutoa takwimu zenye kuonyesha kuwa watu wote ni Wakristo, zimegundua idadi ya kutosha ya watu ambao sio Wakristo au ambao wameanza kufufua imani zao za jadi.

Kwa kufuata ueneaji wa wafuasi wa dini kitaifa, kuna nchi ambazo watu wake wote au karibu wote ni Waislam ambako dini ya Kiislamu imetangazwa kuwa ya kitaifa, bila kujali kama sharia inafuatwa au la. Miongoni mwa nchi hizo ni Tunisia, Algeria, Libya, Somalia, Visiwa vya Ngazija na Mauritania. Misri na Senegal ni nchi zenye Waislamu wengi lakini kuna idadi kubwa kiasi ya Wakristo. Kuna nchi ambazo usawa wa Uislamu na Ukristo ni suala muhimu kisiasa. Miongoni mwao ni Sudani, Ethiopia, Chad, Nigeria, Kameruni na Tanzania. Baadhi ya nchi hizi zilitamka rasmi katika katiba zao kwamba dola "haiungi mkono dini yoyote" au ni ya kidunia katika uhusiano wake na dini. Kivitendo, viongozi wote wa Kiafrika ni tabaka tawala dogo ambalo limeelimishwa katika shule na mifumo ambayo ama ni ya Kikristo au ya Kiislamu. Wakati wanadai misingi na amali za jadi za Kiafrika zifufuliwe, ni viongozi wachache waliodiriki kutaka kuudhi hisia za Wakristo na Waislamu kwa kujiunga na dini za jadi[3]

## Umuhimu unaoendelea na dini ya jadi

Umuhimu wa dini ya jadi ya Kiafrika unakwenda mbali zaidi ya takwimu za waumini kufikia asilimia 20 zinavyoweza kuonyesha. Kwa Wakristo na Waislamu wengi, msingi wa amali za kimaadili bado unatokana na elimu ya zamani ya mazingira kuliko imani mpya. Bado wahenga wa zamani wanaheshimiwa kwa kuendelea kutambika: bado watu wanaamini kwamba wahenga wanajishughulisha na maisha ya vizazi vyao; na kwamba nguvu za wema na uovu zinaweza kutumiwa kwa kuwasiliana moja kwa moja na miungu kwa njia ya maombi na sadaka; na kwamba hirizi huweza kumkinga mtu dhidi ya mabaya, n.k. Hata katika sehemu ambako matendo na imani za namna hiyo zimeachwa kutumika kama sehemu ya dini, bado imani hizo zinachukuliwa kuwa ni mila.

Kuna sehemu kubwa ya maisha ya Kiafrika iliyovamiwa na dini zote, yaani ya Kiislamu na ya Kikristo, lakini zimeshindwa kuchukua nafasi yake. Sehemu hii ni ya afya na uponyaji. Katika dini ya jadi, maradhi ya kimwili ni dalili za ugonjwa ambao chanzo chake kinaweza kutokana na hasira ya baadhi ya nguvu za

[3]. *Presence Africaine, 1972; M. Glele, 1981.*

wa kikoloni. Vyama vya waganga wa jadi[4] vinaitaka serikali itenge bajeti kwa ajili ya kuendeleza mifumo ya jadi ya tiba ambayo ingali ya muhimu.

## Ukristo, kuondolewa kwa ukoloni na maendeleo

Ukristo ni mfumo mzuri wa dhima-kinzano ya dini-kama raslimali na kama tatizo-katika mabadiliko ya kijamii ya Afrika. Ukristo ulikaribishwa na umekua kwa sababu ya kujihusisha katika maendeleo ya Afrika.[5] Dhima yake ya ukuzaji wa elimu ya magharibi ilikuwa ndio maendeleo ya Kiafrika. Sehemu zote za Afrika, isipokuwa zile zenye Waislamu wengi, tawala za kikoloni ziliridhika kuwaachia Wamisionari kuwa wasimamizi wakuu wa elimu, haku serikali ikiwapatia msaada wa fedha kutoka mapato ya kodi. Wamisionari walijifunza lugha za Kiafrika walifafanua abjadi na walifanya kazi ya kutafsiri Biblia na kazi nyingine za kidini ili kuanzisha utamaduni wa kusoma katika lugha za Kiafrika na hapo hapo kukuza ujuzi wa kuzoma na kuandika. Misioni za Kikristo zilitawala biashara ya vitabu, uchapishaji na uchapaji, maduka ya vitabu na maktaba. Wamisionari walikuwa pia waanzilishi wa tiba za kimagharibi kwa kujenga hospitali na zahanati. Kwa hiyo mvuto mkubwa wa Ukristo ulikuwa ni uanzishaji wa huduma hizi za kimaendeleo na kuwashawishi watu waachane na mapokeo ya kijadi na kuingia katika ulimwengu wa kisasa.

Wakati huo huo, Ukristo ulikua sambamba na ukoloni. Wamisionari waliokuwa wameshikilia makanisa waliyoyaanzisha walikuwa karibu zaidi na maafisa wa kikoloni na walowezi wa kutoka Ulaya kuliko walivyokuwa kwa wafanyakazi wenzao wa Kiafrika, wasaidizi wao na waumini. Hivyo makanisa yalikuwa ni sehemu ya miundo ya kikoloni ambayo harakati za kupigania uhuru wa Kiafrika zilijaribu kuibadilisha.[6]

Kuondolewa kwa ukoloni kulitakiwa kuanzia kwenye kanisa, siyo tu kwa kubadilisha miundo na kuweka viongozi Waafrika badala ya wazungu, bali pia kwa kuasilisha muundo wa maudhui bila kupoteza kiini cha amali za Kikristo. Kazi hii ya kulifanya kanisa liwe la Kiafrika kiasili ilifanywa na Wakatoliki na Waprostestanti. Hata hivyo ilionekana kwamba suala hilo lilivuka mipaka ya udhibiti, umbo na maudhui ya makanisa ya Kikristo. Lilihusu mkakati mzima wa maendeleo.

[4] M. Last na G. Chavunduka, 1986
[5] J. Mbiti, 1962; R. Sastre, 1962
[6]. A. Hastings, 1979.

Moja ya hati muhimu kuhusu kulifanya kanisa kuwa la Kiafrika kiasili ilitokana na kazi ya pamoja ya mwaka 1956 iliyoitwa *Des pretres noves s'interrogent* (Makasisi Weusi watafakari). Wakati huo huo, chama cha Waafrika cha Utamaduni kilichokuwa na makao yake huko Paris na ambacho kiliongozwa na Alioune Diop, kiliona kwamba suala hili ni la muhimu kuliko yote katika mjadala unaohusu uŋegro (itikadi ya watu weusi). Diop alitumia jarida la *Présence Africaine* kuongoza mjadala kuhusu mtazamo wa dini za Kiafrika hususani utafiti wa kiteolojia. Mwaka 1962 wakati wa Mkutano Mkuu wa Pili wa Vatican, Diop alikusanya maoni ya wanataaluma Wakristo wa Kiafrika, na mwaka 1963 alichapisha toleo maalumu la jarida lake juu ya kazi za Mkutano Mkuu ulioitwa *Personnalité africaine et catholicisme* (Haiba ya Kiafrika na Ukatoliki). Diop alikuwa mtu mashuhuri katika makongamano yote matatu ya kimataifa yaliyofanyika huko Abidjani mwaka 1961, Kotonu mwaka 1970 na Abidjani tena mwaka 1977.



*PICHA 17.1 Kwenye mkutano wa Kairo wa wanathiolojia wa Dunia ya Tatu, wajumbe wa Chama cha Kiekumeni cha Wanathiolojia wa Afrika waliomtembelea Papa Shenouda III, Mkuu wa Kanisa la Kikhufu la Misri.*

Msako wa njia za kulifanya Kanisa la Kikristo liwe la Afrika uliendelea, siyo tu miongoni mwa Wakatoliki bali pia miongoni mwa makanisa ya Waprotestanti. Zaidi ya yote, madhehebu yote, Wakatoliki na Waprotestanti, walijitahidi kufanya kazi pamoja katika viwango vyote, cha upana-Afrika na cha muungano wa madhehebu yote, kwa mfano katika mkutano wa wanateolojia wa Kiafrika ulioitishwa Ibadani mwaka 1969 na Baraza la Makanisa la Ulimwengu. Taasisi kadhaa, ikiwemo Kituo cha Dini za Kiafrika cha Kinshasa (*the Kinshasa Centre of African Religions*) zimejaribu kuakisi umoja huu wa kidini wa bara zima katika majarida na makongamano yao. Haya yote yamechochea kuanzishwa kwa umoja wa wanateolojia wa Kiafrika wa madhehebu yote.

Katika haya yote tunaweza kutambua mielekeo mitatu muhimu kuhusu suala la teolojia ya Kiafrika.

1. Mwelekeo ambao, licha ya kutambua amali zilizomo ndani ya dini ya Kiafrika, ni mwanzo tu wa matayarisho ya kuingiza Injili ya Kikristo.
2. Pili, mwelekeo wa kihakiki unapendekeza teolojia ya Kikristo ya Kiafrika inayotokana na Biblia, na inayofasiriwa kwa mtazamo wa tajiriba ya kihistoria ya Kiafrika, na kuingia kwenye mijadala ya kiteolojia na teolojia za nchi zisizokuwa za kimagharibi.
3. Na tatu, ni teolojia ya watu weusi au teolojia ya ukombozi hususani huko Afrika ya Kusini. Hii ni teolojia inayozingatia tajiriba ya watu wanaokandamizwa, mathalani watu weusi wa huko Amerika ya Kaskazini na makundi ya watu wanaodharauliwa wa huko Amerika ya Kusini.[7]

Sambamba na msako wa teolojia mpya, pamekuwapo na juhudi za kuipangilia liturgia kwa kuzingatia hali halisi ya Afrika. Kwa mfano, mtindo na ala za muziki za Kiafrika zipewe dhima gani? Je ada za Kikristo za ubatizo, ndoa na mazishi zioanishwe vipi na asasi za kifamilia za Kiafrika? Wamisionari walitambua wazi kuwa, ili Kanisa la Kikristo lisipoteze umuhimu kijamii na kisiasa, ilibidi uafrikishaji (kuweka viongozi Waafrika) wa uongozi uende sambamba, au utangulie, uafrikishaji wa asasi za dola.

[7]. V. Y. Mudimbe, 1985.

## Uislamu na usasa

Kinyume na Ukristo ambao ulishirikiana na ukoloni, nchi za Kiislamu ziliweka upinzani mkali dhidi ya ukoloni. Hata hivyo, pamoja na kutiliana shaka na shutuma za hapa na pale, Uslamu ulifaidika na kuwepo kwa ukoloni kutokana na kupanuka kwa mji, kuongezeka kwa njia za usafirishaji kwa kutumia reli, na barabara na kuongezeka kwa mahitaji ya vibarua wahamiaji. Utawala wa kikoloni ulikuwa na wasiwasi kuhusu uhusiano wa kimataifa wa Uislamu na kwa sababu hiyo walifuatilia kwa tahadhari safari za nje, na hata safari za kwenda kuhiji. Lakini ndani ya nchi waligundua kwamba ushirikiano wa jumuiya tulivu za Waislamu ungeweza kunufaisha pande zote mbili. Walihimiza elimu ya msingi ya Kiislamu katika shule za Korani; walipitisha sheria za kuwalinda waislamu ili wawe huru kufuata dini yao, ikiwa ni pamoja na kuruhusu *sha'a* kutumika katika sheria za madai katika jamii za Kiislamu. Waliweka vipingamizi vya kuzuia Wamisionari wa Kikristo katika maeneo ya Waislamu.

Jumuiya nyingi za Kiafrika ambazo mwanzoni zilipinga kuenea kwa Uislamu, baada ya ushindi wa wakoloni, ziliona ni heshima kuingia katika Uislamu kuliko kuingia dini ya watamalaki wao. Pamoja na watu hao kuwa Waislamu kama njia mojawapo ya kuonyesha upinzani, bado kwa kiasi fulani waliendelea kushirikiana na utawala wa kikoloni. Mfano mzuri ni wa Wolof wa Senegal, ambao vita vya mojawapo ya kuonyesha upinzani, bado kwa kiasi fulani waliendelea kushirikiana na utawala wa kikoloni. Mfano mzuri ni wa Wolof wa Senegal, ambao vita vya *Djihad* vilivyopiganwa kabla ya ukoloni, vilishindwa kuwasilimisha, lakini ambao walimaliza kipindi cha ukoloni wakiwa wamesilimu kabisa.[8] Hii ilitokana na kazi ya Shaykh Ahmadu Bamba,[9] mwanzilishi wa kundi la Mauride Masufii. Aliyekuwa ni mtu aliyeheshimika sana katika kipindi cha ukoloni, na alipata nishani kwa kazi yake ya kuandikisha askari katika jeshi la Kifaransa ili wakapigane nchini Ufaransa Vita Vikuu vya kwanza vya Dunia. Mafanikio na umuhimu wa Wa-Muride nchini Segegal hii leo unaonyesha jinsi ambavyo Uislamu umejirekebisha kulingana na mazingira ya kiutamaduni na kijamii ya Kiafrika na kuwa nguvu muhimu ya kidini.

Katika mchakato wa kuondoa ukoloni, Waislamu hawakupata matatizo ya athari za miundo ya kikoloni wala ya ukengeushi wa kiutamaduni waliyokumbana nayo

8. L. Sanneh, 1986.

9. Tazama F. Dumond, 1975; M. klein, 1968; D. C. O'Brien,1971; na L. Brenner, 1984.

Wakristo. Mwanzoni walifikiria kwamba uhuru ni jusura yenye utata[10] kwa sababu ya uhasama waliokuwa nao kwa elimu ya kimagharibi na yao kuwa iliwanufaisha zaidi Wakristo. Ingawa huko Afrika Kaskazini kulikuwapo na ukuaji wa mawazo ya utaifa, Waislamu huko Afrika Magharibi, mwanzoni hawakuzishabikia harakati za utaifa. Walikuwa wako nje ya umoja wa Waafrika wa bara zima (upana-Afrika) ulioanzishwa na Nchi Mpya za ulimwengu na kurithishwa kupitia kwa Wakristo wa Ulaya. Moja ya michango mikubwa ya al-Nasser ni kwamba alikuwa kiungo cha umoja wa Waarabu wa bara zima, umoja wa Waislamu wa bara zima na umoja wa Waafrika wa bara zima. Umaarufu wake ulisaidia kuwavuta viongozi wa Kiisamu wa Afrika Magharibi kuingia katika harakati za utaifa.



PICHA. 17.2 *Sheikh Amadu Bamba, mkuu wa Wa-Muride wa Senegal akiwa "talibe" yake.*

Katika kipindi cha miaka 50, Uislamu ulikuwa umepiga hatua kubwa ya maendeleo ya kisasa katika nchi kadhaa za Kiafrika, hususani kwa kuanzisha mfumo wa elimu ambao ulipanuka kutoka mifumo ya jadi. Kwanza kulikuwawepo na tapo la Ahmadiyya lililokuwa liko nje ya mwelekeo wa Kiislamu wa kijadi, ambalo

[10] C.A. Kane, 1962

Mafunzo haya yalikuwa muhimu huko Nigeria na Sierra Leone. Lilikuwepo pia kundi la Wahhabi ambalo, kutokea ndani ya kundi la mageuzi la Wahhabiyya lililotokea baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, liliunda vikundi viwili vyenye nguvu: Kikundi cha *Subbanu al-Muslim* kilichoongoza na kuleta mabadiliko katika elimu na kikundi cha *Unioni Culturelle Musulmane* (Muungano wa Kiutamaduni wa Waislamu) ambacho sasa ni shirika la kimataifa linaloshughulikia masuala yote ya Kiislamu, yakiwemo mambo ya kisiasa.[11]

Kuenea kwa vuguvugu la mageuzi ya Wahhabiyya kulitokea wakati mmoja na chama cha *Rassemblement démocratique africain* (RDA, (Muungano wa Kidemokrasia wa Afrika), au kundi pekee muhimu la kuondoa ukoloni huko Afrika Magharibi ya Wafaransa. Wahhabi binafsi wengi walijiunga mmoja mmoja na RDA. Kusudi lao kubwa lilikuwa kuanzisha serikali ya kidemokrasia inayozingatia mafundisho ya haki, usawa na *idjma* au "muafaka". Kwa hivyo, Uislamu ulionekana kama nguvu ya kudai uhuru, kuleta umoja na mabadiliko ya kijamii.

Kwa upande wa pwani ya Afrika Mashariki, mawazo ya wanamageuzi yalikuwa kupitia magazeti kama lile la *Al-Islah* (mageuzi) ambalo lilianza kuonekana huko Mombasa, Kenya mwaka 1932. Mwishoni mwa miaka ya 1940 na katika miaka 1950, serikali ya kikoloni ya Uingereza ilihimiza uanzishwaji wa Umoja wa Ustawi wa Waislamu wa Afrika ya Mashariki (East African Muslim Welfare Association) ukiwa chini ya ulezi wa Mtukufu Agha Khan III na Sultani wa Zanzibar, ili kukabili athari za mawazo ya kupinga ubeberu na kujenga utaifa yaliyokuwa yanaenea kutoka Kairo na kwingineko. Halikadhalika, walisaidia kutoa fedha za kuanzishia Taasisi ya Elimu ya Waislam ya Mombasa (*Mombasa Institute of Muslim Education - MIOME*) ambako vijana wengi wa Kiafrika waliweza kupata elimu ya kisasa katika mazingira ya utamaduni wa dini ya Kiislam.[12]

Wanahistoria na wanaitikadi wanadai kwamba kulikuwepo na mazingira yaliyotakiwa katika Afrika kwa uanzishaji wa Ujamaa wa Kiislam. Kwa mujibu wa Mustafa Sibaci,[13] wakati wa kipindi cha Nabii Muhammad na ma Khalifa wanne wa mwanzo, watu waliishi kijamaa. Katika bara la watu weusi, imeonekana kwamba kabla ya ukoloni, jamii ya Kiafrika iliishi kijamaa. Kwa mfano, ilikuwa na hisia za mshikamano wa kijamii, na haki ya pamoja ya kumiliki ardhi. Kusema kweli, Ujamaa wa Kiislam ndiyo itikadi rasmi ya Misri, Algeria na Libya na ya

[11] L. Kaba, 1974; H.M. Amiji, 1984

[12]. H. M. Amiji, 1984, uk. 115.

[13]. L. Sanneh, 1988.

Chama kikuu cha siasa cha Tunisia (Ujamaa wa Desturi). Pia ujamaa huko uko Somalia.

Kuhusu ukombozi wa mwanamke ndani ya Uislamu, kuna mawazo mengi yanayozingatia kanuni za msingi za namna ya kulishughulikia suala hili. Hili ni suala muhimu sana kijamii kwa sababu kuna tatizo linalohusu hadhi za wanawake katika ndoa za wake wengi ambazo kwa kawaida hutambuliwa rasmi na kuingizwa katika sheria ya familia katika nchi za Kiafrika zilizoathiriwa na kanuni na misingi ya dini ya Kiislam.[14]

Tatizo la kuifanya dini ya Kiislam iwe na misingi ya kijadi linatokana zaidi miongoni mwa na watu weusi wa Afrika. Uislamu una sheria nyingi kuliko Ukristo, kwa mfano katika kukubali mabadiliko ya taratibu za ibada (miviga). Pamoja na mipaka iliyokwishawekwa kutokana na hali ya mazingira ya nchi, Waislamu weusi wanafuata masharti yote muhimu yaitwayo nguzo tano za Uislamu:

- Kutangaza imani kwamba Mungu ni mmoja na Muhammad ni Mtume wake.
- Kufanya sala za kila siku, zipatazo sala tano kwa siku.
- Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan, ukiwa na maana ya kutawala matamanio, kujitakasa na kuwasaidia maskini.
- Kutoa sadaka.
- Kwenda kuhiji Makka angalau mara moja katika maisha ya mtu.

Je, mtu anaweza kusema kihalali kwamba kuna dini ya kweli ya ki-Afrika? Akizungumzia suala hili kwa mujibu wa misingi ya dini, Amadou Hampate Ba anadai "Haiwezekani kuwa na Muislam mweusi kama ambavyo haiwezekani kuwa na Mkristo mweusi au Myahudi mweusi". Hata hivyo Uislamu wa Kiafrika unaonyesha kuwa una dalili za uenyeji wa hali ya mazingira yalivyo. Hii ndiyo sababu tarika bado una nguvu, hasa huko Afrika ya Magharibi. Tumekwisha gusia juu ya mkondo wa mageuzi wa Chama cha Utamaduni cha Kiislamu kilichoanzishwa mwaka 1953. Kuhusu mwelekeo wa kimaendeleo wa chama hiki, Vincent Moteil anaeleze kuwa "kinapendelea kila aina ya Uafrika, kinakubali nyimbo, ngoma na sanaa ya Kinegro. Kinasisitizia juu ya ulazima wa kutenganisha katika mambo ya dini, imani na madhehebu kwa upande mmoja, na mahusiano

[14]. Tazama kwa mfano A. Boudhiba, 1975.

katika mambo ya dini, imani na madhehebu kwa upande mmoja, na mahusiano ya kijamii kwa upande mwingine". Hili la mwisho (la mahusiano ya kijamii) kwa maoni yake, linaweza kuvumiliwa na kukubalika. Watu wengine wanafikiri kwamba kufunga mwezi wa Ramadhani huweza kuwa suala la hiari, na kwamba sala za kila siku zinaweza kupunguzwa hadi kufikia mbili au mtu akaziacha kwa sababu "kazi ndiyo sala ya kweli". Kilicho cha muhimu hapa ni uadilifu tabia na mwenendo kijamii. Kuhusu ndoa za wake wengi "lazima kutakuwepo na mabadiliko kutokana na elimu watakayopewa wasichana na vuguvugu la ukombozi wa wanawake.[15]

Kukua kwa dini ya Kiislamu katika Afrika ya sasa ni lazima itakuwa kuliathiriwa na kuwepo kwa Ukristo na dini ya jadi ya Kiafrika. Wakati mazungumzo rasmi na dini ya jadi hayakubaliki, kumekuwepo na majaribio ya kutaka kuanzisha mazungumzo na viongozi wa ngazi za juu wa Kikristo kwenye vituo vya mafundisho ya kanuni za madhehebu mbalimbali. Kituo kimojawapo cha aina hiyo kilifunguliwa huko Tunisia mwaka 1977 chini ya uongozi wa Profesa A. Boudhiba.[16] Nchini Senegal, kwenye Kituo cha "Bopp Centre"[17] kuna juhudi za kujenga ushirikiano wa baina ya Waislamu na Wakristo ili kuleta maendeleo ya kijamii.

Taratibu za kuundoa ukoloni ziliruhusu kuvuka mipaka ya kijanibu kuingilia kati mipaka iliyokuwa imewekwa na ukoloni dhidi ya Uislamu na kusisitiza zaidi sifa za kiulimwengu na za kimataifa za Uislamu. Mahusiano na Mashariki ya Kati, yamefufuliwa na kupanuliwa kupitia hija, Umoja wa Waislamu wa bara wote na mabadilishano ya wanazuoni. Matapo makuu, kama lile la Washia wenye msimamo mkali la Khomeini wa Iran, na la Kadhaffi la itikadi kali, ya mapinduzi yote yalikuwa na matokeo katika Afrika. Hata hivyo, kupitia ushirikano wa Kimataifa, Uislamu umeleta mchango wa uhakika katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Afrika kutokana na msaada wa kifedha uliokuwa ukitolewa katika nchi mbalimbali kutoka nchi za Kiarabu zinazotoa mafuta.

Wachungaji wa mambo ya uhusiano na nchi za Kiafrika na Kiarabu wameeleza kuwa karibu misaada yote ya Kiarabu ilikuwa ikienda kwenye nchi zilizo na uhusiano na Uislamu. Uhusiano huu baina ya misaada ya kiuchumi na utii katika mambo ya dini ulitambuliwa rasmi na Waziri wa Fedha wa Kuwaiti mwaka 1974. Hata hivyo, tangu hapo, misaada ya Kiarabu imekuwa ya aina mbalimbali na

15. V. Monteil, 1964.
16. *Centre d rencontres islamo - chretiennes.*
17. D. El-Hadjdj Badara, 1979.

zisizo za Kiislam. Pia kuna taasisi za Kiarabu zinazotoa misaada ya aina mbalimbali kwa mfano, Benki ya Waarabu kwa Ajili ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika, Mfuko Maalum ulioanzishwa na OPEC kwa ajili ya msaada kwa ajili ya msaada kwa Afrika, na pia Mfuko wa kiufundi wa Kusaidia Waarabu na Waafrika ambao uko chini ya Barza la kiuchumi la Shirikisho la Waarabu.

## Makanisa huru ya Kiafrika na utambulishi wa Kiafrika

Ingawa makanisa ya aina hii yamekuwepo tangu mwanzo wa karne hii na pengine mwishoni mwa karne iliyopita, makanisa huru ya vikundi hivi, yakiwemo madhehebu mbalimbali ama ya Kimessia au ya Kimillenia, yameongezeka sana tangu miaka ya 1960. Mwaka 1970 yalikuwepo mashirika halisi ya makanisa huru ya Kiafrika 6000, yakiwa na waumini wapatao millioni 16. Mwaka 1987, kulikuwepo na makanisa huru na madhehebu yapatayo 10,000, yakiwa na jumla ya waamini millioni 33.[18]

Ingawa makanisa na madhehebu haya yanaenea Afrika nzima, mengi ya makanisa haya yanapatikana zaidi Afrika ya Kusini (3,000), Nigeria (800), Kongo (Zaire) (600), Ghana (400) na Kenya (180). Moja ya kanisa muhimu sana miongoni mwa makanisa haya ni Kanisa la Kristo la Duniani, lililoanzishwa na nabii Simon Kimbangu. Kanisa hili lina wafuasi wapatao milioni, wengi wao wako Konzo, lakini wapo pia walioko Jamhuri ya watu wa Kongo, Angola, Rwanda na Burundi.

Makanisa haya huru na madhehebu yameainishwa katika makundi matano na H.W. Turner.[9] Kundi la kwanza linajumuisha vikundi vya kisiasa-kimasihi, ambavyo kimsingi vina lengo la kuleta ukombozi wa kisiasa na kiutamaduni. Kikundi kimojawapo cha zamani sana miongoni mwa vikundi hivi ni cha *United Native African Church of Nigeria*. Kikundi hiki kilikuwa na nguvu tangu mwaka 1891. Katika kundi hili hili tunaona pia kuna *Harrism* (kutoka kwa William Wade Harris) ambacho kina nguvu huko Côted' Ivoire, Liberia na Ghana. Kimo pia kikundi cha *Aroti* au "waotaji" ambacho kilipigana huko Kenya tangu mwaka 1934 kikidai ukombozi kutoka utawala wa Kiingereza.

Kundi la pili ni lile la vikundi vya ujadi-mamboleo. Katika kundi hili kuna mfano wa shirika linalojuliana kama *Dini ya Musambwa* au dini ya wahenga.

18. D. B. Barrett, 1982, uk. 815
19. H. W. Turner, 1968, uk. 178.

Huko Nigeria dini ya Ugodiani humuabudu "Mungu wa Afrika", anayesemekana kuwa alijifunua kwa mara ya kwanza huko Misri yapata miaka elfu kadhaa iliyopita.

Kundi la tatu ni lile la madhehebu ya mseto. Madhehebu haya yanakubali kupokea mchanganyiko wa imani na taratibu za ibada kutoka Ukristo na mapokeo ya jadi ya Kiafrika. Miongoni mwa madhehebu haya ni madhehebu ya *Bwiti* ya Gabon na madhehebu ya *Deima* ya Côte d' Ivoire.

Makundi mengine yanajitangaza yenyewe kuwa ni yenye kuamini Mungu mmoja au ya Kihebrania kwa maana kwamba makundi haya yanakataa kabisa kuamini dini za mapokeo ya jadi isipokuwa yanasisitiza juu ya Mungu mmoja kama ilivyojidhihirisha katika Agano la Kale.



PICHA 17.3 *Simon Kimbangu wa Kongo ya Wabelgiji (sasa Jamhuri ya Watu wa Kongo) akiwa anahamishwa na kutiwa gerezani huko Elisabethville (sasa Lubumbashi)*

Kundi la tano ni lile la makanisa ya unabii na uponyaji. Hawa wanajiita wenyewe kuwa ni Wakristo, wanaoamini katika Yesu Kristo kama "Mwokozi" na wanaweka mkazo katika mafunuo ya Roho Mtakatifu; na kwa sababu hii wakati mwingine wanajulikana kama "Makanisa ya Roho Mtakatifu". Mfano mzuri ni wa makanisa ya Sayuni, ambayo yameanzishwa kwa wingi huko Afrika ya Kusini na nchi zinazoizunguka.

Zamani ilisisitizwa kuwa kuanzishwa kwa makanisa haya kulitokana na historia na mazingira yaliyofungamana na mambo ya ukoloni, kisiasa, kiutamaduni na kijamii katika harakati za kupigania uhuru. Ilielezwa kwamba kukua na kuenea kwa makanisa haya huru kulitokana na Wakristo wa Kiafrika kusoma kutafsiri maandiko matakatifu katika lugha zao mbalimbali za Kiafrika. "Tafsiri hizi", aliandika J.R. Leferink, "ziliwawezesha Waafrika kulinganisha Ukristo walioletewa na makanisa ya wamisionari na ujumbe waliousoma kwenye maandiko. Hii iliwapa hisia kwamba kuanzia hapo na kuendelea Mungu alikuwa akizungumza nao katika lugha zao na alikuwa karibu nao"

Kwa kifupi, kwa mujibu wa R. De Haes, madhehebu mbalimbali ni matokeo ya vuguvugu lenye athari mbili ya kukatisha tamaa na au ya kiu ya kuzindua hamasa. Kunapotokea matatizo ya kukata tamaa yanayosababishwa na taratibu za jamii na za kanisa katika kipindi fulani, suluhisho hutolewa kutatua tatizo hilo. Hivyo madhehebu haya ni "ishara na ni changamoto" pia.

Sasa inakubalika kwa ujumla kwamba[20] huu mkazo juu ya upinzani na upingaji ni mtazamo finyu sana kuhusu makanisa huru haya. Mtazamo huu umevuruga mambo mengi mazuri katika kukuza teolojia ya Kiafrika ambayo hupokea amali za kiroho za Kiafrika na mafunuo ya Biblia ya Kikristo. Haya makanisa yamefanya kazi kubwa ya kuhifadhi sayansi ya ulimwengu ya Kiafrika ndani ya mipaka ya mafundisho ya Kikristo. Hivyo ilikuwa rahisi kwa watu maskini wa mijini na wanavijiji kujiunga kwa wingi katika makanisa haya bila kulazimika kuacha mtazamo wao wa kiulimwengu. Hususani, mtazamo wa kijadi kuhusu uponyaji na wokozi imani ndio uliowavutia watu wengi kwenye makanisa haya. Yaliwahakikishia usalama wafuasi wao dhidi ya nguvu za uovu na uchawi za kimapokeo. Katika maeneo ya mijini, makanisa haya yaliwapa waumini usalama, mshikamano na ukarimu, mambo ambayo mfumo wa kikoloni haukuweza

[20]. T. O. Ranger, 1986.

kuwapatia. Zaidi ya haya, makanisa ndiyo yaliyodumisha mifumo ya uponyaji ya kimapokeo hadi pale amali zao za kijamii zilipoanza kutambuliwa na watu wengi.

Tunaweza kusema kwa ujumla kwamba kutokea kwa vikundi vingi mbalimbali vya Kimasihi katika jamii za Kiafrika kabla na baada ya uhuru, kulitokana na mahitaji ya kiuchumi-jamii na msako wa njia mpya ya kiroho katika jamii hizi. Vikundi hivi vya kidini vilihoji juu ya mabadiliko yanayotokea katika jamii zinazobadilika za Kiafrika kuhusu dini rasmi ya Kikristo na dini rasmi ya Kiislamu. Lakini je, tunaweza kusema kwamba hatimaye sasa makanisa haya yanaelekea kwenye utatuzi wa tatizo la kuwa na dini nyingi katika Afrika?

## Hitimisho

1. Kipengele cha dini, kinachochukua sura mbalimbali, ni cha muhimu sana katika maendeleo ya historia ya Afrika, ambako dini ina dhima muhimu.
2. Ni jambo la maana kufahamu dhima hii, kuhimiza vipengele vinavyofaa na kulaani vile vyenye matokeo mabaya ambayo ni kinyume cha maendeleo ya Afrika.
3. Ingawa dini ya mapokeo ya jadi ya Kiafrika imemomonyoka kutokana na kuenea kwa dini Kiislamu na Kikirsto, bado iko hai pamoja na ubinadamu wake na misingi yake ya kiroho ambayo imehimili kwa vizazi vya Kiafrika kwa maelfu ya miaka. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba mara nyingi kuna mawazo ya Kiafrika ambayo ni ya kishirikina, kichawi na ya kimiujiza, ambayo huzuia mawazo mazuri ya kujenga ili kuleta maendeleo katika jamii ya Kiafrika.
4. Dini ya Kikristo na ya Kiislamu zimeathiri sana historia ya bara la Afrika, hususani katika miaka zaidi ya 50 iliyopita. Athari zake zinaonekana zaidi katika utayarishaji wa sheria za Kiafrika, kwa mfano sheria ya familia na sheria nyingine za kiraia. Dini hizi zinaonyesha mwelekeo wa sasa wa kiutamaduni - jamii na zinasaidia kuleta maendeleo katika Afrika kwa kuelekeza mtazamo wa mawazo katika uanzishaji na ukuzaji wa miundo ya msingi ya kijamii na kiuchumi ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya Afrika kwa ujumla. Ni jambo la mantiki kwa dini ya Kikristo na ya Kiislamu kuchukua hatua za taratibu za kujirekebisha kulingana na utamaduni wa Kiafrika hasa katika masuala ya imani na miviga.
5. Kuenea kwa tarika za Kiafrika katika Uislamu au kuenea kwa makanisa

huru, madhehebu, umaskini na makanisa mengine ya mseta wa Ukriskto na Uafrika unatufanya kutafakari maswali ambayo vikundi hivi vinauliza kuhusu dini ambazo ziliundwa kihistoria na kudhibitiwa kiutawala msonge, na pia kuhusu jamii za Kiafrika. Makundi haya yanaonyesha makosa na mapungufu katika misingi ya mfumo wa kijamii, yanatuelekeza kwenye matakwa na mahitaji ya kiroho ambayo hayaridhishwi kabisa na mifumo ya sasa ya kisiasa na kiuchumi.

Kwa hiyo, kipengele hiki cha dini, kikifafanuliwa kikamilifu, kuchanganuliwa na kukosolewa, bado kinaweza kutoa mchango katika kuleta mageuzi ya kijamii kwa njia ya maelewano, na hivyo kuleta maendeleo ya kijamii ya kweli ya Afrika mwishoni mwa karne hii ya ishirini.

# 18 Lugha na Mabadiliko ya Kijamii

Sifa kuu za kipindi kinachoanzia 1935 ni kuimarika kwa ukoloni na sera zake za lugha na utamaduni ambazo zilikuwa na athari kubwa, mapambano ya Waafrika kwa ajili ya kupata madaraka na uhuru, kuibuka kwa ukoloni mamboleo, ambao ulibadili hali ya lugha na utamaduni, na utambuzi wa Waafrika juu ya umuhimu wa kulinda na kuendeleza tamaduni na lugha zao za kitaifa.

Kipindi hiki kinaweza kugawiwa katika sehemu tatu: 1935 - 1960; 1960 - 1982; 1982 na kuendelea.

## Lugha za Kiafrika na hatari ya usimilishi, 1935 – 1960

Watawala wa kikoloni, kila mmoja akifanya alivyoona kulingana na mwelekeo wake, mambo yaliyoweza kufanyika na maslahi ya wakati ule, ama waliunda sera za usimilishi wa wazi wa lugha, elimu na utamaduni ama walitumia njia zisizo dhahiri na zilizozingatia mambo kadha tu: Kwa mfano, utawala wa wakoloni wa Kifaransa, uliokuwa na mwelekeo wa kushika kila kitu, ulidhamiria katika kuwaingiza kabisa Waafrika kwenye mfumo wake wa elimu, ilhali Waingereza, ambao waliangalia mambo kiutekelezaji, walifundisha lugha za Waafrika katika miaka ya awali ya shule, wakiandaa njia kwa ajili ya kujifunza Kiingereza.

## Usimilishi kama lengo kuu la kipindi kizima

Kama mwandishi wa Mali Amadou Hampaté Bâ alivyoeleza katika makala yake yenye kichwa cha "Tamaduni za asili na mabadiliko ya kijamii", ukoloni haukupata upinzani mkali. Usimilishi ulikuwa lengo la Waafrika wenyewe pia na ulipingwa

tu katika hatua za baadaye, kuanzia 1954 na kuendelea. Wakati ambapo vita vikuu viwili vya dunia, Mapinduzi ya Kisoshalisti ya Oktoba 1917 na matukio yaliyolenga katika kuwakomboa waliokuwa chini ya wakoloni yalipokuwa yanaitetemesha dunia na kuangusha himaya, Afrika bado ilikuwa ikikabiliwa na vitisho kwa utambulisho wake kitamaduni. Amali za kale zilidharauliwa zilipopambanishwa na amali mpya za Wazungu. Migongano ilitokea kati ya wale ambao kwa kiasi fulani walionekana "wameendelea" au "wamesimilishwa" na "wenyeji". Na kwa Waafrika wengi, usimilishi ulikuwa ni haja kubwa, iliyotokana na tamaa ya kuwa na vipimo vya dini, maadili na utamaduni kama vya walowezi.

## Ukoloni: kipigo cha kudra

Wakati baadhi ya watawala wa kikoloni na wafanyakazi wa kiufundi walijifunza "lugha za kienyeji" hasa kwa matumaini ya kuwaelewa Waafrika na kuzijua siri zao, Waafrika waliokuwa na nafasi waliwapeleka watoto wao katika "nchi mama" za wakoloni ili wakasome huko "Maarifa ya Wazungu" na kugundua sababu za nguvu zao. Kuna mifano kadhaa ya msimamo huo katika fasihi za Kiafrika za wakati huo, za simulizi na zilizoandikwa kwa hati ya Kiarabu (fasihi ya Kiajami).

Ukoloni wa Kizungu ulikubalika karibu kote kama kipigo kilichotokana na kudra. Mweleko uliotetea usimilishaji uliibuka, mara nyingine ukichochewa na watawala wa kikoloni, uliotukuza uzuri wa taratibu za kikoloni, usalama ulioletwa nao, na ugunduzi mkubwa wa "karne ya Wazungu", magari, ndege, radio, reli n.k.

Hata hivyo wachache na tapo la wapinzani wasiojulikana lilisikitika pia likitetea maadili ya wahenga na jadi za zamani. Wachache hao wakawa ndio sauti za watawaliwa ambao ukombozi wao ulichukuliwa kuwa ni jambo lisiloweza kurudishwa nyuma.

## Fasihi kama kimbilio

Fasihi simulizi za lugha za Kiafrika na fasihi ya Kiajami ziliwadharau "wale waliomwiga mtu mweupe" na "wale waliozungumza lugha ya mtu mweupe bila kuielewa". Baadhi ya waali wa kiutamaduni wanaeleza katika kazi zao za kifasihi na kisanii na katika methali na nyimbo walizozitunga, jinsi walivyokata tamaa walipokabiliana na hatari kubwa za wakati wao.

Lugha na fasihi za Kiafrika ziliendelea kuhusiana na kale kwa kuendelea kuonyesha amali za wahenga na kuwa kimbilio lenye thamani. Hata hivyo, hata amali hizo ziliathiriwa na mabadiliko yaliyokuwa yakitokea.

## Ukuzaji wa msamiati na lugha za mawasiliano

Kutokana na mahusiano na Uislamu na Wafanyabiashara wa Kiarabu na Kiasia, pamoja na kukutana na lugha za Kizungu na Ukristo, lugha za Kiafrika zilikuza sana msamiati wake, na utajiri wake wa istilahi za kidini, kiteknolojia, kisayansi na kitamaduni bado ni ushahidi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya kipindi kile cha miaka 25.

Lugha za mchanganyiko wa Kizungu na Kiafrika, kama vile za Kikrio na Kipijini, zilikua na kuwa lugha halisi za Kiafrika katika baadhi ya nchi za pwani ya Atlantiki, kama vile Rasi ya Verde, Guinea-Bissau, Gambia, Sierra Leone na Kameruni. Lugha za Kikrio za Gambia na Kameruni na Kikrio cha Sierra Leone zilikopa maneno mengi kutoka Kiingereza, na Kikrio cha Ras ya Verde na Guinea-Bissau nacho ilikopa kutoka Kireno. Lugha hizi ni za Kiafrika kifonolojia, kimuundo na kisemantiki, ingawa msamiati wake kwa kiwango kikubwa unatokana na lugha za Kizungu.

Kutokana na kutiwa nguvu na watawala wa kikoloni, Kiswahili, Kilingala, Kibambara na Kihausa zilikua sana kama lugha za mawasilino baina ya watu wa makabila tofauti. Zilitumika sana kwenye majeshi ya ulinzi na polisi ya tawala mbalimbali za kikoloni.

Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1920, miongoni mwa watalaamu wa kikoloni na watawala waandamizi, kulikuwa na baadhi walioonyesha hatari za usimilishaji na kutaka ufanywe uchunguzi wa kina wa lugha na fasihi za Kiafrika.

## Maendeleo yaliyopangwa kijanja

Mnamo Juni 1926, mkutano wa kuanzisha Taasisi ya Kimataifa ya Lugha na Ustaarabu wa Kiafrika ulifanyika London. Asasi hiyo mpya ilielezwa kuwa ni chombo kilichoundwa ili kukusanya taarifa za lugha na ustaarabu wa Kiafrika na kuwa kituo cha mahusiano baina ya wataalamu wa masomo hayo.

Taasisi hiyo, ambayo baadaye ilikuwa Taasisi ya Kimataifa kuhusu Afrika (IAI) huchapisha jarida la kila miezi 3, *Africa*, pamoja na vijitabu vya kitaaluma (monografu), maandiko ya Kiafrika juu ya dini, visasili, visakale, mila na asasi za kijamii, hadithi, methali na vitendawili, na vyote hutafsiriwa kwa lugha ya Kizungu.

Tangu mwanzo, Taasisi hiyo ilisisitiza katika kuziandika lugha za Kiafrika kwa kutumia hati za Kirumi na kuendeleza alfabeti ya kurejelea, "Alfabeti ya Kimataifa ya Kiafrika" ambayo bado inajulikana kama "Alfabeti IAI", na ambayo ilikuwa itumike kama msingi wa kuandikia kiasi cha lugha sitini za Kiafrika.

Mnamo Aprili 1929, ilianzisha zawadi "kuwasaidia na kuwatia moyo wenyeji, kwa nia ya kuwafanya watoe, katika lugha zao wenyewe, kazi ambazo zitadumu na ambazo watazionea fahari." Mazoea hayo yaliendelea hadi 1950, ambapo Taasisi hiyo ilianzisha zawadi ya Margaret Wrong, kwa kumbukumbu ya Katibu wa Kamati ya Kimataifa ya Maandiko ya Kikristo Afrika, aliyefariki Uganda 1948. Kuanzia hapo, kazi zilizoandikwa kwa lugha za Kiafrika au Kiarabu hazikuweza kupata zawadi hiyo hadi zilipochapishwa katika Kiafrikaani, Kifaransa, Kiingereza au Kireno.

Maendeleo haya yanaonyesha wazi nia hasa ya ukoloni ya kuunda chombo hicho. IAI iliundwa ili kuwaunganisha wasomi waliosambaa waliohusika na habari za Afrika, kuratibu shughuli zilizosaidia utekelezaji wa ukoloni na kukuza lugha za Kizungu.

Ni muhimu, hata hivyo, kusisitiza juu ya kazi zilizofanywa na wanazuoni na wamisionari ambao, wakiwa na IAI au kwa juhudi zao wenyewe, walitoa vitabu vya rejea kwa lugha za Kizungu na maandiko ya kielimu ya hali ya juu, yakitoa umaizi katika lugha na utamaduni wa Kiafrika. Watawala wa kikoloni, Wamisionari, wataalamu wa aina zote, watetezi wa ubinadamu, na wanaelimu wa ridhaa walikusanya, kunukuu na kufasiri katika lugha za Kizungu makusanyo ya historia, sayansi na fasihi za urithi wa utamaduni wa Kiafrika. Kazi zao zilichapishwa katika majarida ya wakati ule kama Kijarida cha Kamati ya Taaluma ya Historia na Sayansi ya AOF (ambacho baadaye kilijulikana kama Kijarida cha Taasisi ya Kifaransa kuhusu Afrika ya Watu Weusi) ambacho bado kina manufaa hadi leo. Ni kutokana na kazi zao na zile za "watoa taarifa" wao na washirika wengine, ndipo kulikozuka mkusanyiko wa magazeti na fasihi katika Kiyoruba, Kiigbo, Kiewe, Kihausa, Kiakan, Kiduala na Kiswahili, hasa kutoka Nigeria, Ghana, Togo, Kameruni na Tanzania.

## Uundaji wa sera mpya ya lugha na utamaduni 1960-1982

### Kipindi cha kusita na kujaribu

Kupata uhuru kwa nchi nyingi za Afrika mnamo mwaka 1960 kungeweza kuwa fursa nzuri ya kutathmini ukoloni na kutoa mwelekeo mpya katika masuala ya lugha za taifa, tamaduni na elimu. Kwa bahati mbaya, isipokuwa kwa nchi chache tu, utekelezaji wa awali wa watawala wa kikoloni ulichukuliwa kama ulivyokuwa, aghalabu bila mabadiliko hata kidogo. Kwa kweli, mataifa mengi mapya yalitoa




*PICHA: 18.1 Mgawanyo wa lugha rasmi katika Afrika (Chanzo: imenukuliwa kutoka World Almanac and Book Facts, World Almanac of Books and Facts, New York, 1991 © Pharos Books, 1990)*

umuhimu mdogo kwa utamaduni na waliachia ukawa chini kabisa katika aula zao, wakitegemea hasa fadhila za nchi za kigeni na mashirika ya kimataifa.

Ni kwa kidogo kidogo, kwa kuhimizwa na kuchochewa na vyuo vikuu, mashirika ya fedha na asasi binafsi katika nchi nyingi za Ulaya na Amerika, pia kutokana na msukumo kutoka kwa wasomi na kwa kuzingatia matakwa ya vyama vya vijana, wanawake na wafanyakazi, ndipo viongozi wa baada ya uhuru walikubali kuwepo kwa haja ya programu za elimu kukitwa katika lugha za Kiafrika. Hata viongozi waliokuwa na misimamo thabiti kama Rais Kwame Nkrumah wa Ghana hawakuwa tayari kukuza walichoona kuwa ni utitiri wa lugha "zisizoendelea," wakihofia kuwa sera ya namna hiyo ingehatarisha juhudi za mataifa machanga katika kujenga utaifa kwa kuwagawa Waafrika katika kipindi ambacho walitakiwa kuungana.

## Kuachana na ukale

Punde, hata hivyo, raslimali za kutosha zilitolewa kwa ajili ya kutafiti tamaduni na mapokezi simulizi ya Kiafrika.

Kati ya 1962 na 1964, idara na asasi nyingi za utafiti za lugha za Kiafrika zilianzishwa katika vyuo vikuu vipya vya barani, na majarida ya hali ya juu yaliyohusu hasa isimu yalianzishwa, hasa katika vyuo vikuu vya Sierra Leone, Tanzania, Addis-Ababa na Ibadan.

Kwa msaada wa UNESCO, Chama cha Kimataifa cha Wataalamu wa Mambo ya Kiafrika kiliundwa Akkra mnamo 1960, hasa kutokana na kuchochewa na *Société Africaine de culture* (Chama cha Kiafrika cha Utamaduni) na Chuo Kikuu cha Ibadan. Ikitiwa moyo tangu mwanzo na wasomi maarufu wa Kimarekani na Kisovieti, Melville Herskovits na Ivan Posteshkin, asasi hii mpya ilichangia katika kukuza stadi za Kiafrika.

Mwaka 1962, kulingana na shughuli zake chini ya Programu ya Dunia ya Kupambana na Kutojua Kusoma na Kuandika, UNESCO iliamua kutilia mkazo elimu ya watu wazima katika lugha za Kiafrika na kuahidi kuzisaidia nchi za eneo hili kutekeleza azima hiyo. Uamuzi huu ulikuwa ndio hatua ya kwanza ya kutambua lugha hizo na kuziingiza katika sekta ya kisasa ya mfumo wa elimu katika nchi za Kiafrika.

## Mahitaji na hali halisi

Lugha za Kiafrika zilipata hadhi yake kama lugha kamili na majina ya dharau ya "vilugha", "lugha za kikabila", "lugha za kienyeji" yalipotea polepole katika msamiati wa wataalamu. Lakini ilikuwa ni wakati huo ilipotambulika kwamba

kazi nyingi zilizosemwa kuwa ni za kitaaluma juu ya lugha za Kiafrika zilifanywa na wanagenzi wasiokuwa na ustadi wa kutosha katika isimu, na kazi chache tu zilitilia maanani ugunduzi wa Saussure na wanamiundo.

Hivyo, ilikuwa lazima kuanza tena upya. Ilibidi Waalimu wa vyuo vikuu vya Afrika na wasomi wafunzwe isimu na walipewa misaada ya masomo kwenda Marekani, Ulaya Magharibi na Urusi.

## Kushiriki kwa UNESCO

Mara mwongozo wa jumla na maamuzi ya msingi yalipowekwa bayana na nchi husika, msaada wa UNESCO uliwezesha kuundwa kwa programu za utekelezaji kwa nchi na lugha kadha na kuwafunza wataalamu wa mataifa hayo kusimamia utekelezaji wa programu hizo. Orodha kamili ya lugha kuu za Kiafrika iliyopangwa kufuatana na nchi iliyochapishwa na UNESCO mnamo 1985 inaonyesha ugumu wa kazi hiyo.

Hivyo, ilikuwa lazima kuanza tena upya. Ilibidi Waalimu wa vyuo vikuu vya Afrika na wasomi wafunzwe isimu na walipewa misaada ya masomo kwenda Marekani, Ulaya Magharibi na Urusi.

## Kushiriki kwa UNESCO

Mara mwongozo wa jumla na maamuzi ya msingi yalipowekwa bayana na nchi husika, msaada wa UNESCO uliwezesha kuundwa kwa programu za utekelezaji kwa nchi na lugha kadha na kuwafunza wataalamu wa mataifa hayo kusimamia utekelezaji wa programu hizo. Orodha kamili ya lugha kuu za Kiafrika iliyopangwa kufuatana na nchi iliyochapishwa na UNESCO mnamo 1985 inaonyesha ugumu wa kazi hiyo.

## Taaluma kuhusu Afrika nje ya Afrika

Kati ya matokeo makubwa ya uhuru ni kukua kwa taaluma kuhusu Afrika nje ya Afrika, si katika vyuo vikuu vya nchi za kikoloni za hapo awali bali katika nchi nyingi za Ulaya, Amerika na Asia. Kutokana na msukumo wa jumuiya za Wamarekani wenye asili ya Kiafrika, vyuo vikuu vingi vya Marekani, Karibiani na Brazil zilianzisha taasisi za taaluma za Kiafrika, na kuanzisha kozi kuhusu lugha, fasihi na tamaduni mbalimbali za Kiafrika.

Asasi ya Kifaransa ya ushirikiano wa kiutamaduni na kiufundi (ACCT), ambayo mwanzoni iliundwa ili kutetea na kuendeleza lugha na utamaduni wa Ufaransa, imetoa fedha nyingi kwa ajili ya utafiti wa lugha na fasihi ya Kiafrika.

Shauku kuhusu Afrika na lugha na tamaduni zake ilichochea wanafunzi na wasomi wa Kiafrika kujitosa katika kuhimiza nchi za Kiafrika kuwa na raghba, kutoa rasilimali za kutosha, na kusukuma ufundishaji na utafiti wa hali ya juu.

## Matarajio ya baadaye

Kwa jumla, kuinukia kwa Waafrika kuwa "mataifa katika jumuiya ya kimataifa" kulifungua upeo kwa mapana zaidi. Hata hivyo, urithi wao wa karibuni wa kuwa watu waliotawaliwa, ufujaji wa rasilimali na juhudi zao wenyewe hazikuwawezesha kujitazama kwa mapana na kuunda sera za lugha na utamaduni. Inaonekana kuwa viongozi hawajaweza kuzingatia tathmini na ugunduzi mwafaka wa baadhi ya mikutano ya maeneo au ya ulimwengu mzima inayotayarishwa mara kwa mara katika miji mikuu ya Afrika kuhusu utamaduni, lugha ama sera za lugha.

JEDWALI LA 18.1 Mgawanyo wa lugha kuu za Taifa Afrika, kwa kila nchi
Jedwali linaonyesha hali ya lugha na sera za lugha kwa nchi 46 huru za Afrika, kuondoa Algeria, Misri, Libya, Moroko na Tunisia ambapo Kiarabu ndio lugha rasmi. Kuna vyumba kumi na moja ambavyo ukisoma kushoto hadi kulia vinaonyesha ifuatavyo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a | Kuondoa Algeria, Misri, Libya, Moroko na Tunisia ambapo Kiarabu ndio lugha rasmi | | | |
| b | Imeelezwa kwa mamilioni (m) au kama sehemu ya milioni | | | |
| d | Makisio ya idadi ya lugha za Afrika zinazotumika kwenye nchi | | j | Kiwango cha utafiti wa lugha |
| e | Makisio ya idadi ya wasemaji kwa mamilioni au asilimia | | 1 = | kisichotosheleza |
| f | Maeneo ya kijiografia ya lugha kuu kwenye nchi | | 2 = | kinachoridhisha kidogo |
| g | Nchi zingine lugha inapozungumzwa kwa hadhi hiyo au nyingine | | 3 = | kinachoridhisha |
| h | Hadhi rasmi ya lugha chini ya sheria : N = Lugha ya taifa; ) = Lugha rasmi | | 4 = | kizuri |
| i | Matumizi ya lugha nchini | | k | Asasi binafsi na za serikali nchini kuhusiana na lugha |

A = utawala
a = kusoma
E = kufundishia
o = madarasa ya majaribio

1 = Ngazi ya msingi
2 = Ngazi ya sekondari
3 = Ngazi ya elimu ya juu na vyuo
M = kama somo
P = kwenye magazeti
R = kwenye redio
T = kwenye televisheni
L = kuwepo na maandishi

| *Nchi*[a] | *Idadi ya watu (m)*[b] | *Idadi ya lugha*[c] | *Lugha kuu*[d] | *Wasemaji (m)*[e] | *Eneo la kijiografia*[f] | *Kwingine*[g] | *Hadhi*[h] | *Matumizi*[i] | *Utafiti*[j] | *Vyombo vya utafiti*[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ANGOLA | 7 | 11 | Umbundu | 1.5 | Kati | | N | RTL | 2 | Taasisi ya Taifa ya lugha |
| | | | Kimbundu | 1 | N. + Centre | | N | RTL | 2 | Lugha za Kiafrika; Wizara |
| | | | Kikongo | 0.5 | N. | Congo, Zaire | N | RTL | 2 | ya Elimu; lugha Kireno |
| | | | Lunda-Kioko | 0.4 | W. | Zaire, Zambia | N | RTL | 1 | |
| | | | Ngangela | 0.35 | S.-E. | | N | RTL | 1 | |
| | | | Nyaneka-Humbe | 0.2 | S.-W. | | N | RTL | 1 | |
| | | | Kireno | – | Nchi nzima | | O | AaE$_{1,2,3}$ PRTL | 3 | |
| BENIN | 3.5 | 52 | Bariba | 0.35 | N.-E. | Nigeria | N | a RT | 2 | Tume ya Taifa ya lugha |
| | | | Fon | 0.5 | S. + Centre | | N | a RT | 2 | Idara ya Taaluma ya Lugha na |
| | | | Yoruba | 0.35 | S.-E. + Centre | Nigeria, Togo | N | a RT | 4 | simulizi |
| | | | Yom | – | N.-W. | | N | a R | 1 | (Chuo Kikuu cha Taifa cha Benin) |
| | | | Ditammarie | – | N.-W. | | N | a R | 2 | |
| | | | Kifaransa | – | Nchi nzima | | O | A E$_{1,2,3}$ PRTL | | |

| *Nchi* [a] | *Idadi ya watu (m)* [b] | *Idadi ya lugha* [c] | *Lugha kuu* [d] | *Wasemaji (m)* [e] | *Eneo la kijiografia* [f] | *Kwingine* [g] | *Hadhi* [h] | *Matumizi* [i] | *Utafiti* [j] | *Vyombo vya utafiti* [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BOTSWANA | 1 | ± 9 | Setswana | 90% | | RSA, Namibia, Bophutatswana | NO | $AaE_{1,2m}$ PR L | 3 | Kamati ya lugha ya Taifa; Taasisi ya Uchunguzi ya Taifa; Chuo Kikuu cha Botswana |
| | | | English | – | Whole country | | NO | $AaE_{1,2,3m}$ PR L | 4 | |
| BURKINA FASO | 7 | 60 | Moore | 48% | Centre (all parts) | Côte d'Ivoire, Ghana | N | $aE_{0,3m}$ PRTL | 3 | Taasisi ya utafiti wa Kisayansi na teknolojia (DGRFT) |
| | | | Juula (Dyula) | – | W. (all parts) | Mali, Niger, Côte d'Ivoire, Guinea, Senegal | N | $aE_{0,3m}$ PRTL | 3 | Taasisi ya elimu ya watu Wazima (INAFA); Tume ya lugha za taifa (CNLV) |
| | | | Fulfulde | 10.4% | N. | Niger, Mali, Guinea, Senegal, Mauritania | N | $aE_{0}$ PRTL | 3 | SIL, IRAP |
| | | | Dagari-Lobi | 7% | S.-W. | Ghana | N | a R L | 2 | Chuo Kikuu cha Ouagadougou DEPFD |
| | | | Bobo-bwamu | 6.7% | W. | Mali | N | a R L | 2 | |
| | | | Senufo | 5.5% | S.-W. | Côte d'Ivoire, Mali, Niger | N | R | 1 | |
| | | | Gurunsi | 5.3% | Centre + S. | Ghana | N | a PR L | 2 | |
| | | | Bisa | 4.7% | S. | – | N | a R L | 1 | |
| | | | Gulmancema | 4.5% | E. | Benin, Togo, Niger | N | a PR L | 2 | |
| | | | French | 7.5% | Whole country | | N | $AaE_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |
| BURUNDI | 4.2 | 1 | Kirundi | 4.2 | Whole country | Rwanda, Tanzania, Uganda, Zaire | NO | $AaE_{1,2m,3m}$ PR L | 3 | ALLR; ARFA; COO; CEPK; DLLA; CCB |

| *Nchi* [a] | *Idadi ya watu (m)* [b] | *Idadi ya lugha* [c] | *Lugha kuu* [d] | *Wasemaji (m)* [e] | *Eneo la kijiografia* [f] | *Kwingine* [g] | *Hadhi* [h] | *Matumizi* [i] | *Utafiti* [j] | *Vyombo vya utafiti* [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BURUNDI | | | Kiswahili | 10% | | Tanzania, Kenya, Uganda, Zaire, etc. | $E_{3m}$ | R | | |
| | | | French | | Whole country | | O A $E_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| CAMEROON | 8 | 237 | Arabic (Choa) | | Extreme N. | Chad | | R | 1 | CREA; Idara ya lugha na |
| | | | Bamum | | W. | – | a | R L | 2 | Fasihi ya Kiafrika |
| | | | Basaa | | Centre + coast | – | a | PR L | 3 | (Kitivo cha Sanaa); SIL; CERDOTOLA. |
| | | | Beti-Fang | | Centre + S. | Equatorial Guinea, Gabon, Congo | a | PR L | 3<br>3 | |
| | | | Duala | | Coast | – | $a_o$ | R L | 3 | |
| | | | Ejagham | | N.-W. | Nigeria | $a_o$ | R L | 3 | |
| | | | Fe'Fe' | | W. | – | $aE_{01}$ | L | 2 | |
| | | | Fulfulde | | Extreme N., N + Adamawa | Senegal, Sudan | | R L | 3 | |
| | | | Gbaya | | E. | CAF | | R L | 3 | |
| | | | Ghomala | | W. | | a | R L | 3 | |
| | | | Hausa | | Extreme N, N. | Nigeria, Niger | | – | 4 | |
| | | | Lamnso | | N.-W. | | $a_o$ | R L | 2 | |
| | | | Mafa | | Extreme N. | | a | | 2 | |
| | | | Medumba | | W. | | a | R L | 2 | |
| | | | Mungaka | | W. | | a | R L | 2 | |
| | | | Meka | | E. | | | R | 1 | |
| | | | Ngyemboong | | W. | | a | R L | 2 | |
| | | | Vute | | Centte | | a | | 3 | |
| | | | Yemba | | W. | | | R L | 3 | |
| | | | Pidgin English | 20% | Coast, W., S.-W., N.-W. | | | – | | |
| | | | English | | | | O $AaE_{1,2,3}$ | PR L | | |
| | | | French | | | | O $AaE_{1,2,3}$ | PR L | | |

| Nchi[a] | Idadi ya watu (m)[b] | Idadi ya lugha[c] | Lugha kuu[d] | Wasemaji (m)[e] | Eneo la kijiografia[f] | Kwingine[g] | Hadhi[h] | Matumizi[i] | Utafiti[j] | Vyombo vya utafiti[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| CAPE VERDE | 0.3 | 2 | Portuguese Creole | | Whole country | São Tomé, Guinea Bissau | – | | 2 | |
| | | | Portuguese | | Whole country | | O AaE$_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| JAMHURI YA AFRIKA YA KATI | 2 | 44 | Sango | 2 | Whole country | Chad | N AaE$_{o}$ | PRT | 2 | LA, IREM, INEF, CERDOTOLA |
| | | | French | | Whole country | | O A E$_{1,2m,3m}$ | PRTL | | |
| CHAD | 5.5 | 250 | Sara | 19% | S. | CAF | a | R | 2 | INSH, INSE, SIL, Chuo Kikuu Cha CEL, Ukurugenzi wa utamaduni, Ukuzaji wa lugha za taifa. |
| | | | Arabic | 60% | Whole country | Sudan, Niger, etc. | NO AaE$_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| | | | Gorane (Daza) | | Centre, N. | Niger, Libya | | R | | |
| | | | Maba | 12% | E. | Sudan | | R | 1 | |
| | | | French | | Whole country | | O AaE$_{1,2,3}$ | PR L | | |
| | | | Fulfulde | | S.–W. | Cameroon, Niger, etc. | | R | | |
| | | | Massa | | S.–W. | Cameroon | a | R | | |
| | | | Kānembu | | W., N. | Nigeria, Niger | | R | | |
| | | | Tuburi | | S.–W. | Cameroon | a | R | 1 | |
| | | | Moundang | | S.–W. | Cameroon | a | R | 1 | |
| | | | Zaghawa | | N.–E. | Sudan | | R | | |
| | | | Tama | | E. | Sudan | | | | |
| | | | Mimi | | E. | | | | | |
| | | | Bidiye | | Centre–E. | | | | | |
| | | | Dadjo | | E. + Centre | Sudan | | | | |
| | | | Bulala | | Centre, E., W. | | | | | |
| | | | Bagirmī | | S.–W. + S. | | | | | |
| | | | Kotoko | | S.–W. | Cameroon | | | | |
| | | | Migama | | Centre, E. | | a | | 1 | |
| COMOROS | 0.34 | 3 | Arabic | – | Whole country | Somalia, Sudan, etc. | O AaE$_{1,2,3}$ | PR L | 3 | |
| | | | Kiswahili | – | | Tanzania, Kenya, etc. | N | | 3 | |

| *Nchi*[a] | *Idadi ya watu (m)*[b] | *Idadi ya lugha*[c] | *Lugha kuu*[d] | *Wasemaji (m)*[e] | *Eneo la kijiografia*[f] | *Kwingine*[g] | *Hadhi*[h] | *Matumizi*[i] | | *Utafiti*[j] | *Vyombo vya utafiti*[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| COMORO | | | Kifaransa | – | Nchi nzima | | O | $AaE_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| CONGO | 1.4 | 15 | Kikongo | 75% | S. | Angola, Zaire | N | | RTL | 3 | INRAP, INSSED, Idara ya Isimu na Fasihi simulizi |
| | | | Lingala | – | N. | Zaire | N | | RT | 3 | |
| | | | Kifaransa | – | Nchi nzima | | O | $AaE_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| CÔTE D'IVOIRE | 7.3 | 60 | Baule | 1.8 | Kati | Ghana, Togo | | | RT | 2 | ILA, IES, ILENA, IHAAA, CERAV, GRIO, SIL |
| | | | Juula (Dyula) | 1.5 | N.-W. | Mali, Guinea, Burkina Faso | | | RT | 2 | |
| | | | Bete | 0.9 | Kati | | | | RT | 2 | |
| | | | Senufo | 0.8 | N.-E. | | | | RT | 1 | |
| | | | Yakouba (dan) | 0.35 | W. | | | | RT | 1 | |
| | | | Kifaransa | | Nchi nzima | | O | $A\ E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| DJIBOUTI | 0.25 | 3 | Afar | 31% | | | | | RT | – | |
| | | | Kiarabu | 5.4% | | Sudan, Somalia, etc. | O | | RT | 3 | |
| | | | Kisomali | 36% | | Somalia | | | RT | – | |
| | | | Kifaransa | | Nchi nzima | | O | $A\ E_{1,2}$ | PRTL | 4 | |
| GUINEA YA IKWETA | 0.3 | ? | Kispania | – | Nchi nzima | | O | $A\ E_{1,2}$ | PRL | 4 | |
| ETHIOPIA | 30 | 70 | Amharic | 60–65% | Nchi nzima | | N | $AaE_{1,2m,3m}$ | PRTL | 3 | Akademia ya Lugha ya Ethiopia; Taasisi ya Taaluma za lugha, Chuo Kikuu cha Addis Ababa; Idara ya Maendeleo ya Mitaala; Wizara ya Elimu |
| | | | Oromo | 27% | | Kenya | | a | PR | – | |
| | | | Tigrinya | 14% | | | | a | PR | 1 | |
| | | | *Kiingereza* | – | | | | $E_{1m,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| GABON | 1 | 42 | Fang | 35% | N.-W. | Cameroon | | | | 2 | ORSTOM, IRSH |
| | | | Myene | – | W. | | | | | 1 | |
| | | | Kifaransa | – | Nchi nzima | | O | $AaE_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |

| Nchi [a] | Idadi ya watu (m) [b] | Idadi ya lugha [c] | Lugha kuu [d] | Wasemaji (m) [e] | Eneo la kijiografia [f] | Kwingine [g] | Hadhi [k] | | Matumizi [i] | Utafiti [j] | Vyombo vya utafiti [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| GAMBIA | 0.6 | | Mandinka (Malinke) | 42% | | Côte d'Ivoire, Senegal, Mali | | $a_{01}$ | R | 3 | |
| | | | Pulaar (Fulfulde) | 18% | | Guinea, Guinea-Bissau, Senegal, Mali, etc. | | $a_{01}$ | R | 3 | |
| | | | Wolof | 16% | | Senegal, Mauritania | | $a_{01}$ | R | 3 | |
| | | | Joola (Dyola) | 9.5% | | Senegal, Guinea-Bissau | | | R | – | |
| | | | Soninke | 8.7% | | Mali | | | R | 2 | |
| | | | English | | Whole country | | O | $AaE_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| GHANA | 11 | 46 | Akan | 6 | Centre–S. | Côte d'Ivoire | N | $aE_{1,2m,3m}$ | PRTL | 4 | *Kituo cha lugha Ghana* |
| | | | Ewe | 2 | S.–E. | Togo, Benin | N | $aE_{1,2m,3m}$ | RTL | 3 | *Kituo cha utafiti na maendeleo ya Mitaala, shule ya lugha Ghana* |
| | | | Ga | 1 | Accra region | | N | $aE_{1,2m,3m}$ | RTL | 3 | *Chuo Kikuu cha Ghana;* |
| | | | Dangme | 1.5 | S.–E. | | N | $aE_{1,2m,3m}$ | L | 2 | *Chuo Kikuu cha Cape-Coast, Taasisi ya lugha Ghana* |
| | | | Dagare | 0.3 | N.–W. | Burkina Faso | N | $aE_{1,2m,3m}$ | L | 1 | |
| | | | Gonja | 0.02–3 | N.–Centre | | N | $aE_{1,2m,3m}$ | L | 1 | |
| | | | Kasem | – | N. | | N | $aE_{1,2m,3m}$ | L | 2 | |
| | | | Dagbani | 0.35 | N.–E. | | N | $aE_{1,2m,3m}$ | RTL | 1 | |
| | | | Nzema | – | S.–W. | Côte d'Ivoire | N | $aE_{1,2m,3m}$ | R L | 2 | |
| | | | Hausa | – | N. | Niger, Nigeria, etc. | | | R L | 3 | |
| | | | English | – | Whole country | | O | $A'E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| GUINEA | 6.6 | 21 | Pulaar | 2.4 | Middle Guinea | Mali, Senegal, Cameroon, Niger, etc. | N | $AaE_{1,2m,3m}$ | PRTL | 2 | |
| | | | Maninka | 1.7 | Upper Guinea (E) | Mali, Gambia, Burkina Faso | N | $AaE_{1,2m,3m}$ | PRTL | 2 | |

| Nchi [a] | Idadi ya watu (m) [b] | Idadi ya lugha [c] | Lugha kuu [d] | Wasemaji (m) [e] | Eneo la kijiografia [f] | Kwingine [i] | Hadhi [k] | Matumizi [l] | Utafiti [j] | Vyombo vya utafiti [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| GUINEA | | | Soso | 1.3 | Lower Guinea (W) | Sierra Leone | N | AaE$_{1,2m,3m}$ PRTL | 2 | |
| | | | Kisi | – | | Sierra Leone | N | aE$_{1,2m,3m}$ R | 2 | |
| | | | Kpelle | – | | Liberia | N | aE$_{1,2m,3m}$ R | 2 | |
| | | | Loma | – | | | N | aE$_{1,2m,3m}$ R | 2 | |
| | | | Konyagi | – | | | N | aE$_{1,2m,3m}$ R | 2 | |
| | | | B2sari | – | | | N | aE$_{1,2m,3m}$ R | 2 | |
| | | | French | – | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |
| GUINEA-BISSAU | 0.8 | | Balata | 30% | | | | | | |
| | | | Pulaar (Fulfulde) | 21% | | Guinea, Senegal, etc. | | | | |
| | | | Manjaku | 14% | | Guinea, | | | | |
| | | | Mande | 12% | | Senegal, etc. | | | | |
| | | | Crioulo | | | | – | R | | |
| | | | Portuguese | | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ PR L | 4 | |
| KENYA | 14 | 40 | Gikuyu | 20% | | | | aE$_{1}$ R | | *Chuo Kikuu cha Nairobi* |
| | | | Dholuo (Luo) | 14% | | Uganda | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Luluya | 13% | | | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Kikamba | 11% | | | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Kalenjin | 11% | | | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Ekegusi | 6.5% | | | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Kimeru | 5.0% | | | | aE$_{1}$ R | | |
| | | | Kiswahili | 65% | Whole country | Tanzania, Uganda, Zaire, Mozambique, Malawi, Comoros, Somalia, etc. | N | aE$_{1m,2m,3m}$ PRTL | 4 | |

| Nchi[a] | Idadi ya watu (m)[b] | Idadi ya lugha[c] | Lugha kuu[d] | Wasemaji (m)[e] | Eneo la kijiografia[f] | Kwingine[g] | Hadhi[h] | | Matumizi[i] | Utafiti[j] | Vyombo vya utafiti[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KENYA | | | English | 16% | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| LESOTHO | 1.3 | | Sesotho | 99% | Whole country | Botswana, RSA | O | Aa$E_{1,2m,3m}$ | PR L | 3 | |
| | | | English | | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |
| LIBERIA | 1.8 | 25 | Kpelle (Guerzé) | 23% | | Guinea | | | PRT | 1 | |
| | | | Grebo (Kru) | 22% | | | | | RT | | |
| | | | Baso (Bassa) | 16% | | | | | RT | | |
| | | | Loma | 6.6% | | | | | PRT | | |
| | | | Gio | 6.1% | | | | | RT | | |
| | | | Mano | 4.6% | | | | | RT | | |
| | | | Gola | 4.7% | | | | | RT | | |
| | | | English | 40% | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| MADAGASCAR | 3 | | Malagasy | 3 | Whole country | | O | Aa$E_{1,2m,3m}$ | PRTL | 4 | *Taasisi ya Isimu (ILA), Idara ya lugha na fasihi ya Kimalagasi, Akademia ya Malagasi* |
| | | | French | | Whole country | | O | A $E_{1m,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| MALAWI | 5.6 | | Chichewa (Chinyanja) | 80% | Whole country | Mozambique, Zambia, Zimbabwe | N | Aa$E_{1m,2m,3m}$ | PR | 3 | |
| | | | Ilomwe | 15% | | | | | | | |
| | | | Ciyao | 19% | | Tanzania, Mozambique | | | | | |
| | | | Citumbuka | 9% | | | | | | | |
| | | | Chisena | – | (common) | | | | | | |
| | | | Chitonga | – | (common) | | | | | | |
| | | | English | 6% | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ | PR L | 4 | |

| *Nchi*[a] | *Idadi ya watu (m)*[b] | *Idadi ya lugha*[c] | *Lugha kuu*[d] | *Wasemaji (m)*[e] | *Eneo la kijiografia*[f] | *Kwingine*[g] | *Hadhi*[h] | | *Matumizi*[i] | *Utafiti*[j] | *Vyombo vya utafiti*[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MALI | 6 | 12 | Bamana (Mande) | 80% | S. + Centre | Senegal, Côte d'Ivoire, Guinea, Guinea-Bissau, Burkina Faso | N | aE$_{o,m}$* | PRTL | 3 | DNAFLA |
| | | | Fulfulde | 12% | W. + Centre | West African countries | N | aE$_{o,m}$* | PR L | 3 | ISH |
| | | | Soninke | 11% | W. | Gambia | N | a | R | 2 | |
| | | | Senufo | 9.2% | S. | Côte d'Ivoire, Burkina Faso | N | | R | 2 | |
| | | | Songhay | 6.4% | E. | Niger, Benin, Burkina Faso | N | aE$_{o,m}$* | R | 1 | |
| | | | Tamashek | – | N., E. | Niger, Algeria, Libya | N | aE$_{o,m}$* | R | 1 | |
| | | | French | | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| | | | * Bamanam, Fulfulde, Songhany na Tamashek zote zinafundishwa kama masomo na kutumika kwa ufundishaji kwenye madarasa ya majaribio | | | | | | | | |
| MAURITANIA | 1.8 | 7 | Hassaniya (Arabic) | 80% | N. | Arab countries | NO | AaE$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | Taasisi ya Taifa ya Ualimu (IPN), Taasisi ya lugha ya Taifa (ILN) Taasisi ya utafiti wa kisanyasi ya Chuo Kikuu cha Taifa Mouritania (IMRS); |
| | | | Wolof | 3% | S.-W. | Gambia, Senegal | N | aE$_{o}$ | R | 3 | |
| | | | Fulfulde (Pulaar) | 7% | Centre-S., S.-E. | Mali, Senegal, etc. | N | aE$_{o}$ | R | 3 | |
| | | | Soninke | 6% | S., S.-E. | Mali, Côte d'Ivoire, Burkina Faso, Senegal | N | aE$_{o}$ | R | 3 | |
| | | | French | | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| MAURITIUS | 0.9 | | Creole | 94% | Whole country | Reunion, Seychelles | | | PRT | 2 | |

| Nchi [a] | Idadi ya watu (m)[b] | Idadi ya lugha [c] | Lugha kuu [d] | Wasemaji (m) [e] | Eneo la kijiografia [f] | Kwingine [g] | Hadhi [h] | Matumizi [i] | Utafiti [j] | Vyombo vya utafiti [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAURITIUS | | | Hindi | 50% | | | N | $E_{1m,2m,3m}$ PRT | | |
| | | | Tamil | 3.5% | | | | $E_{1m}$ PR | 1 | |
| | | | Telugu | 2.1% | | | | $E_{1m}$ R | 1 | |
| | | | French | 24% | | | N | $E_{1m,2m,3m}$ PRTL | 4 | |
| | | | English | 2.8% | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |
| MOZAMBIQUE | 9.4 | | Imakwa (Ilomwe) | 38% | | Malawi | | R | | |
| | | | Shitsonga | 24% | | Zimbabwe, RSA | | R | | |
| | | | Cisena (Cipodzo) | 10% | | | | R | | |
| | | | Shona | 10% | | Zimbabwe | | R | | |
| | | | Kiswahili | 6.4% | | Tanzania, Kenya, etc. | | R | | |
| | | | Chichewa | 3.2% | | Malawi, Zambia | | R | | |
| | | | Shichopi | 4.5% | | | | R | | |
| | | | Ciyao | 2.2% | | | | R | | |
| | | | Cimakonde | 1.3% | | | | R | | |
| | | | Portuguese | | Whole country | | O | A $E_{1,2,3}$ PR L | 4 | |
| NIGER | 5.2 | 8 | Hausa | 1.8 | Centre–S. | Nigeria. Chad, etc. | N | a$E_{0,3m}$ PRTL | 3 | CELHTO |
| | | | Songhay (Zarma) | 0.9 | W. | Mali, Benin | N | a$E_{0,3m}$ PRTL | 2 | |
| | | | Fulfulde (Pulaar) | 0.6 | Whole country | Mali, Senegal, etc. | N | a$E_{0,3m}$ PRTL | 3 | |
| | | | Tamashek (Touareg) | 0.5 | N. | Mali, Algeria, etc. | N | a$E_{0,3m}$ PRTL | 1 | |
| | | | Kanuri | 0.3 | E. | Nigeria, Cameroon, Chad | N | a$E_{0,3m}$ PRTL | 1 | |
| | | | French | 10% | Whole country | | O | Aa$E_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |

| *Nchi*[a] | *Idadi ya watu (m)*[b] | *Idadi ya lugha*[c] | *Lugha kuu*[d] | *Wasemaji (m)*[e] | *Eneo la kijiografia*[f] | *Kwingine*[g] | *Hadhi*[h] | *Matumizi*[i] | *Utafiti*[j] | *Vyombo vya utafiti*[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NIGERIA | 80 | 394? | Hausa | 32% | N. | Niger, Ghana, Chad, Cameroon, etc. | NO | AaE$_{1,2m,3m}$ PRTL | 4 | Vyuo Vikuu vya Alimadu Bello Zasia, Sekoto, Maiduguri, Ibadan, Ife, Bayero na Kano; Baraza la utafiti wa Elimu ya Taifa, Lagos; Chama cha Kiyoruba, Ibadan; Chuo Kikuu cha Ife, Lagos (angalia orodha juu) |
| | | | Yoruba | 25% | W. | Benin, Togo | NO | AaE$_{1,2m,3m}$ PRTL | 4 | |
| | | | Igbo | 22% | E. | | NO | AaE$_{1,2m,3m}$ PRTL | 4 | |
| | | | Fulfulde (Ful, Fula) | 8.6% | | Cameroon, Niger, Guinea, etc. | N | aE$_{1,3m}$ PR L | 3 | |
| | | | Efik/Ibibio | 5.3% | | | N | aE$_{1,2m,3m}$ PRTL | 2 | |
| | | | Kanuri | 4.1% | | Niger, Chad | N | aE$_{1,3m}$ PRTL | 3 | (angalia orodha juu) |
| | | | Tiv | 2.5% | | | N | aE$_{1,3m}$ RT | 2 | |
| | | | Ijo | 2.0% | | | N | aE$_{1,3m}$ RT | 2 | |
| | | | Edo | 1.7% | | | N | aE$_{1,3m}$ PRT | 2 | |
| | | | Nupe | 1.2% | | | N | aE$_{1,3m}$ RT | 1 | |
| | | | Igala | 1.0% | | | N | aE$_{1,3m}$ RT | 1 | |
| | | | Idoma | 0.9% | | | N | aE$_{1,3m}$ RT | 1 | |
| | | | English | 15% | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |
| JAMHURI YA AFRIKA KUSINI | 31 | 10 | Xhosa | | S. | Lesotho, Zimbabwe | N | E$_{1}$ PR | | |
| | | | Zulu | | E. | Botswana, Mozambique, Swaziland | N | E$_{1}$ PR | | |
| | | | Sotho | | Centre + S. | Lesotho | N | E$_{1}$ PR | | |
| | | | Afrikaans | | | | N | A E$_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |
| | | | English | | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ PRTL | 4 | |

| Nchi[a] | Idadi ya watu (m)[b] | Idadi ya lugha[c] | Lugha kuu[d] | Wasemaji (m)[e] | Eneo la kijiografia[f] | Kwingine[g] | Hadhi[h] | | Matumizi[i] | Utafiti[j] | Vyombo vya utafiti[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RWANDA[a] | 5.3 | 1 | Kinyarwanda | 100% | Whole country | Burundi, Tanzania, Uganda, Zaire | NO | $AaE_{1,2m,3m}$ | PR L | 4 | INRS, MINEPRISEC (Bureau pédagogique), UNR |
| | | | Kiswahili | | Towns | Burundi, Tanzania, Uganda, Zaire | | $E_{2,3m}$ | R | 1 | |
| | | | French | | Whole country | | O | A $E_{1m,2,3}$ | PR L | 4 | |
| SAO TOME AND PRINCIPE | 0.08 | | Creole | | Whole country | | | | | | |
| | | | Portuguese | | Whole country | | O | A $E_{1,2}$ | PR L | 4 | |
| SENEGAL | 5.9 | 19 | Wolof | 80% | Whole country | Gambia, Mauritania | N | $aE_{0,1}$ | RTL | 3 | IFAN, CLAD, Faculty of Arts, University |
| | | | Fulfulde (Pulaar) | 21% | N.–E., S. | Guinea, Mali, Gambia, Burkina Faso, Niger | N | $aE_{0,1}$ | RTL | 2 | |
| | | | Sereer | 13% | Centre, Centre–W. | Gambia | N | $aE_{0,1}$ | RTL | 2 | |
| | | | Joola (Dyola) | 7% | S. | Gambia | N | a | R L | 1 | |
| | | | Mande (Mandinka, Malinke) | 6% | S., E. | Guinea-Bissau, Mali, Gambia | N | a | R L | 1 | |
| | | | Soninke | 2% | E., S. | Mali,Gambia, Mauritania, Guinea | N | a | RTL | 1 | |
| | | | French | 15% | Urban centres | | O | $AaE_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |

| *Nchi*[a] | *Idadi ya watu (m)*[b] | *Idadi ya lugha*[c] | *Lugha kuu*[d] | *Wasemaji (m)*[e] | *Eneo la kijiografia*[f] | *Kwingine*[g] | *Hadhi*[h] | *Matumizi*[i] | *Utafiti*[j] | *Vyombo vya utafiti*[k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SEYCHELLES | 0.06 | | Creole | 100% | Whole country | | O/N | PR L | | |
| | | | French | 15% | | | O/N A $E_{1m,2m}$ | PR L | 4 | |
| | | | English | 35% | Whole country | | O/N A $E_{1,2}$ | PR L | 4 | |
| SIERRA LEONE | 3.1 | 18 | Mende | 31% | | Guinea, Liberia | N $AaE_{1,3m}$ | PR | | |
| | | | Temne | 30% | | Guinea, Liberia | N $AaE_{1,3m}$ | PR | | |
| | | | Limba | 8.4% | | | N | R | | |
| | | | Kono | 4.8% | | | N a | R | | |
| | | | Fulfulde | 3.1% | | Guinea, Niger, etc. | N | R | | |
| | | | Loko | 3.0% | | | N | R | | |
| | | | Kisi | 2.2% | | Guinea | N | R | | |
| | | | Krio | 1.9% | | | | R | | |
| | | | English | | Whole country | | O $AaE_{1,2,3}$ | PRT | 4 | |
| SOMALIA | 5.2 | | Somali | 98% | Whole country | Ethiopia, Kenya, Djibouti | NO $AaE_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | Akademia ya sayansi na sanaa ya Somali, Chuo Kikuu cha Taifa cha Somalia, Idara ya lugha ya Kisomali, |
| | | | Kiswahili | 0.6% | | Tanzania, Kenya, etc. | | | 4 | Wizara ya Elimu, Kitengo cha Maendeleo ya Mitaala, Kituo cha Elimu ya |
| | | | Arabic | 75% | Whole country | Sudan, UAE, etc. | O A $E_{1m,2m,3m}$ | PR | 4 | Watu Wazima. |
| | | | Italian | 10% | | | $E_{3}$ | P | | |
| | | | English | 15% | | | $E_{2m,3}$ | P | | |
| SUDAN | 17.8 | | Arabic | 50% | Whole country | UAE, Somalia, etc. | NO $AaE_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| | | | Dinka | 10% | | | $E_{1,3m}$ | R | | |
| | | | Nuer | 4.5% | | | | R | | |
| | | | Zande | 2.1% | | Zaire | $E_{1}$ | R | | |

| Nchi [a] | Idadi ya watu (m)[b] | Idadi ya lugha [c] | Lugha kuu [d] | Wasemaji (m) [e] | Eneo la kijiografia [f] | Kwingine | Hadhi | Matumizi [i] | | Utafiti [j] | Vyombo vya utafiti [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SUDAN | | | Moru | 1.0% | | | | E$_{1}$ | | | |
| | | | English | | Whole country | | | E$_{1m,2,3}$ | PR L | 4 | |
| SWAZILAND | 0.53 | | Siswati | 91% | | | N | aE$_{1m,2m}$ | PRT | 3 | |
| | | | English | | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| TANZANIA | 18 | 150 | Kiswahili | 90% | Whole country | Kenya, Uganda, Zaire, Burundi, Rwanda, Mozambique, Malawi, Somalia, Zambia, Comoros | NO | AaE$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | Idara ya Kiswahili na fasihi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Baraza la Kiswahili la Taifa, TAKILUKI, EACROTANAL |
| | | | English | 20% | Whole country | | O | A E$_{1m,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| TOGO | 2.3 | 50 | Ewe | 22% | S. | Benin, Ghana | N | AaE$_{1,2m}$ | PRTL | 4 | Akademia ya Kiewe, INRS, CERK, INSE, IPN, Idara ya Isimu, Chuo Kikuu cha Benin. |
| | | | Kabye | 13% | Centre | | N | AaE$_{1,2m}$ | PRT | 3 | |
| | | | French | 35% | Whole country | | O | A E$_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| UGANDA | 12.4 | | Luganda | 39% | | | N | AaE$_{1,2m}$ | PR | 3 | |
| | | | Ateso (+ Karimojong) | 10% | | | N | AaE$_{1,2m}$ | PR | | |
| | | | Runyankore-Rukiga | 15% | | | N | AaE$_{1,2m}$ | PR | | |
| | | | Rutooro | 6.2% | | | N | AaE$_{1,2m}$ | R | | |
| | | | Lwo (Acholi + Lango) | 10% | | | N | AaE$_{1,2m}$ | PR | | |

| *Nchi* [a] | *Idadi ya watu (m)* [b] | *Idadi ya lugha* [c] | *Lugha kuu* [d] | *Wasemaji (m)* [e] | *Eneo la kijiografia* [f] | *Kwingine* [g] | *Hadhi* [h] | *Matumizi* [i] | | *Utafiti* [j] | *Vyombo vya utafiti* [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| UGANDA | | | Lugbara | 3% | | | N | $AaE_{1,2m}$ | PR | | |
| | | | Kiswahili | 35% | | Tanzania, Kenya, etc. | N | $A\ E_{1m,2m}$ | PR L | 4 | |
| | | | English | 21% | Whole country | | | $A\ E_{1m,2,3}$ | PRTL | | |
| ZAIRE | 30 | 220 | Kiswahili | 39% | E., N., S.-E. | Tanzania, Kenya, etc. | N | $A\ E_{1,2,3m}$ | PRTL | 3 | DLLA, CELTA, IRS, BUZATRA, ISP, Centre nat., IPN, etc. |
| | | | Lingala | 25% | N., N.-W. | Congo, CAF | N | $A\ E_{1,2,3m}$ | PRTL | 3 | |
| | | | Ciluba | 22% | Centre-S. | | N | $A\ E_{1,2,3m}$ | PRTL | 3 | |
| | | | Kikongo | 14% | W., S.-W. | Congo, Angola | N | $A\ E_{1,2,3m}$ | PRTL | 3 | |
| | | | French | | Whole country | | O | $A\ E_{1,2,3m}$ | PRTL | 4 | |
| | | | Cinyanja (Chichewa) | 42% | | Malawi, Mozambique | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | 3 | |
| | | | Citonga | 23% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Silozi | 17% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Luvale | 8% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Kikaonde | 7% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Lunda | 5% | | Angola | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | English | 26% | Whole country | | O | $A\ E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| ZAMBIA | 5.1 | 40 | Icibemba | 56% | | Zaire | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | 3 | |
| | | | Cinyanja (Chichewa) | 42% | | Malawi, Mozambique | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | 3 | |
| | | | Citonga | 23% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Silozi | 17% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Luvale | 8% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | Kikaonde | 7% | | | N | $AaE_{1m,2m}$ | PR | | |

| *Nchi* [a] | *Idadi ya watu (m)* [b] | *Idadi ya lugha* [c] | *Lugha kuu* [d] | *Wasemaji (m)* [e] | *Eneo la kijiografia* [f] | *Kwingine* [g] | *Hadhi* [h] | | *Matumizi* [i] | *Utafiti* [j] | *Vyombo vya utafiti* [k] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ZAMBIA | | | Lunda | 5% | | Zaire<br>Angola | N | $A2E_{1m,2m}$ | PR | | |
| | | | English | 26% | Whole country | | O | $A\ E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |
| ZIMBABWE | 7·5 | 8+ | Shona | | | Mozambique | N | $2E_{1}$ | RTL | 3 | University of Zimbabwe |
| | | | Ndebele | | | | N | $2E_{1}$ | RTL | 3 | |
| | | | English | | Whole country | | O | $A\ E_{1,2,3}$ | PRTL | 4 | |

*Source:* UNESCO (1985) *The Definition of a Strategy for the Promotion of African Languages*, meeting of experts held in Conakry, Guinea, 21–25 September 1981, document CLT/85/WS/72 (Paris: UNESCO).

# Mwaka 2000: Changamoto muhimu Kutoka 1982 kutoka mapokezi simulizi hadi mawasiliano simulizi

Bado tuko kwenye hatua ambayo vinasa sauti vinatumiwa kurekodi lugha za Kiafrika na taipureta zinatumiwa kuzinukuu. Hata hivyo, muda umefika wa kusonga mbele na kuwafikia wale waliotangulia katika kutumia santuri za video na vichangua - maneno. Kwani, iwapo lugha za Kiafrika bado hazijakamilika kuwa lugha zinazoandikika, lugha nyingine za dunia, ambazo zimekwishasheheni maandiko, zinakimbilia kwenye mawasiliano simulizi na taswira zenye kuonekana kwa macho. Usimulizi huo hauna uhusiano wowote na mawasiliano ya lugha za Kiafrika, ambapo sauti ya binadamu husambazwa tu kwa ngomezi. Badala yake, ni aina mpya ya mawasiliano simulizi, yanayotokana na tasnia ya maandishi, ambapo video huwa na dhima muhimu.

## Tenda au potea

Kama tamaduni zinaouelezea, lugha za Kiafrika hivi sasa zinapitia mabadiliko ya mara kwa mara, baadhi yake yakiwa yanatokana na kutawaliwa na lugha za kigeni zinazotumika ulimwenguni kote ambazo zinatumika katika vipengele vyote vya maisha ya kila siku.
Kama lugha za Kiafrika zitaendelea kuwepo, basi itabidi zikue, na hiyo ina maana kuwa serikali ni lazima ziunde sera thabiti za lugha. Mageuzi ya teknolojia tunayoyaona mwishoni mwa karne hii yataongoza uundaji wa vitengo vikubwa vya maeneo ya kijiografia - kisiasa na kijamii na utamaduni, ambapo kasi itaondosha umbali na kuzileta karibu pembe za mbali kabisa za dunia kwa kutumia mifumo ya mawasiliano yenye ufanisi wa hali ya juu. Ili kuendeleza utaifa wake katika nafasi iliyopo, Afrika inalazimika kuhakikisha kuwa kompyuta na satelaiti zinazungumza lugha zake.

Inapofikia ukingoni mwa milenia ya tatu, Afrika inakabiliwa na masuala mengi kadha ya kimkakati knhusu utamaduni na lugha. Miaka nenda rudi, lugha zake zimekabili kwa mafanikio hatari knbwa zilizopambana nazo wakati wa ukoloni. Hata hivyo tatizo halitakuwa kulinda maarifa ambayo yanatetereshwa na hali yake ya kuyahifadhi au na namna yanavyowasilishwa kutoka kizazi hadi kizazi.
Kama Afrika haitakuruhusu ihinikizwe na amali za bandia zilizofungwa na kusambazwa kiujanja kila mahali, inabidi ijizatiti kudhihirisha kuwepo kwake

na matendo yake katika kipindi hiki kipya cha kielektroni. Kama maarifa ya kale ya Waafrika yatakusanywa, kusasishwa na kuwasilishwa kwa maandishi na kwa taswira na sauti, itawezekana kwa vizazi vijavyo kujikumbusha kwa kupitia vyanzo hivyo na kuendeleza kiungo muhimu na ukale huo.

# 19

# Kukua kwa fasihi ya kisasa tangu 1935

Kipindi kinachoanzia miaka ya 1930 ndicho hasa kilichoshuhudia kuchanua kwa fasihi andishi ya Afrika.[1] Jinsi elimu rasmi na kujua kusoma na kuandika kulivyoenea, na upatikanaji wa elimu ya Chuo Kikuu kwa Afrika ulivyoongezeka, umma wa Waafrika waliojua kusoma na kuandika uliundwa ambao ulizusha waandishi wapya. Aidha, kundi kubwa la wasomaji na wasikilizaji watarajiwa wa fasihi ya Kiafrika liliibuka.

Ingawa hadithi fupi, insha na wasifu kama tanzu za fasihi zilikuwa na mashiko, tanzu za msingi zaidi za fasihi bunifu za kipindi hiki cha historia ya Kiafrika zilikuwa, kwanza, ushairi na balagha; pili, drama na sanaa za maonyesho; na tatu, riwaya. Labda tanzu ambazo zilikuwa rahisi kuingia kwenye jadi za asili zilikuwa balagha na ushairi. Afrika imekuwa na washairi, walumbi na mamanju. Uhusiano baina ya jadi za asili za ushairi na ulumbi na miundo mipya ya Magharibi kwa namna nyingi haukuwa wa kuumiza sana katika uwanja wa utamaduni wa fasihi.

Lakini kama ushairi ulikuwa muundo wa asili zaidi katika bara hili, riwaya ilikuwa ni muundo wa kigeni kuliko yote. Hata Magharibi utanzu wa riwaya ulikuwa hasa ni zao la karne ya kumi na tisa na mapinduzi ya viwanda. Ni kweli kwamba utambaji wa hadithi ulikuwepo tangu mwanzo huko Magharibi na Afrika. Hivyo kuingia kwenye hadithi fupi hakukuwa na matatizo. Mayeli wa Afrika Magharibi walikuwepo angalau kwa milenia moja nyuma. Uchangamani wa taarifa haukuwa kikwazo. Kwani tendi ndefu na tata zilitambwa Afrika. Lakini riwaya kama muundo wa kisanii unaochanganya hadithi moja na uumbaji wa wahusika, mtiririko na masimulizi ulikuwa nje ya mazoea ya mayeli. Kati ya miundo yote ya kifasihi iliyoingia Afrika

[1] Sura hii inazishukuru kazi za awali za A.A. Mazrui, hususan A.A. Mazrui, 1975a, na A.A. Mazrui na M. Bakari, 1986a na 1986b. .



PICHA 19.1: *Yeli au mtambaji wa kijadi wa Kiafrika*

wakati wa utawala wa ukoloni wa Kizungu, riwaya ilikuwa ni utanzu wa Kizungu hasa.

Sura hii inajadili dhamira kuu zilizoelezwa kwenye fasihi zinavyohusiana na historia ya Afrika bila kujaribu kueleza masuala yote ya fasihi.

Kabla ya kuanza kujadili mada kuu za fasihi ya Kiafrika, hapana budi kusema machache juu ya vikwazo vya kiuchumi na kiufundi vilivyozuia na bado vinazuia utolewaji wa kazi za kifasihi. Uhaba wa matbaa (viwanda vya kupiga chapa,) kutokuwepo kwa wachapishaji wa kutosha katika sehemu nyingi za bara hili nagharama za vitabu ndio vikwazo vikubwa. Zaidi ya hayo, wananchi wachache wanaweza kusoma lugha za Kizungu na wachache zaidi wanaweza kumudu kununua vitabu. Mwandishi wa lugha za Kiafrika naye pia anakabiliwa na matatizo hayohayo. Wasomaji wengi wangeweza kufurahishwa na matini yanayoandikwa, lakini wanashindwa kupata raha hiyo kutokana na lugha inayotumiwa. Hili si tatizo kwa Kiarabu, lakini ni majonzi makubwa kwa uandishi mwingi wa lugha za kusini mwa Sahara.

Wasanii simulizi huachiliwa mbali katika uchunguzi wa fasihi kwa vile hata kama ni wa kisasa, wanajieleza kwa njia zinazohusishwa na ukale. Zaidi ya hayo, wanawafikia tu wale wanaowasikiliza. Aghalabu huwasimulia wenzao wachache, au hadhira ya mahali finyu. Watunzi na watambaji wengi wa jadi simulizi ni wanawake wenye ujuzi na weledi mkubwa wa ulumbi katika ushairi na utambaji wa hadithi.

## Ushairi na siasa

Tuanze kwa kuangalia fasihi ya asili zaidi: ushairi. Kati ya sifa muhimu za ushairi wa Kiafrika wa kipindi hiki ni uhusiano wake na siasa. Sababu kadhaa zilileta uhusiano huu. Sababu mojawapo ni kuwepo uzalendo wa kitamaduni. Pamoja na hii ilikuwepo pia sababu ya matumizi ya methali katika mazungumzo asilia. Kadhalika, sababu nyingine katika tajriba ya ushairi wa Kiafrika ni athari za Biblia na Kurani kama chanzo cha kuchochea ushairi. Lakini juu ya hayo yote vyote viwili viliathiriwa na mihemuko, kama ilivyokuwa kwa Wasomali.

Aina tofauti ya uzalendo wa kitamaduni iliibuka Paris mnamo miaka ya 1930. Wakichochewa na kujiamini "Surrealism II ambayo iliasi" ukandamizaji wa lugha na sanaa ya kibwanyenye, Waafrika walioongea Kifaransa walianzisha vita dhidi ya ukoloni wa akili ya Mwafrika, lakini kwa kutumia viunzi vya Wazungu.[2] Sera ya utawala wa Kifaransa ya kusimilisha kiutamaduni iliwachochea Waafrika kuanzisha vuguvugu la Unegro. Unegro ukawa ni tajiriba yenye umuhimu wa pekee ya Waafrika popote walipo. Waandishi wa Kiafrika na Karibiani waliunda urafiki wa kishairi kunung'unikia kung'olewa kwao kutoka kwenye jadi yao, na kuthibitisha uhalali wa jadi na uasili wa Mwafrika. Urafiki baina ya Aimé Césaire wa Matinique na Léopold Sédar Senghor ulikuwa msingi muhimu wa vuguvugu la fasihi la Unegro. Césaire hasa ndiye aliyeunda istilahi hiyo na kisha akaingia kwenye kile ambacho Nietzche angeweza kukiita "ubadilishaji wa thamani."

Waandishi wengine walijiunga na vuguvugu hili na hivyo nguvu za ushairi na siasa ziliungana. Ilikuwa vigumu kuweka mpaka baina ya wanasanaa na wanahamasa, kati ya mshairi na mwanasiasa. Baadhi ya magazeti ya Kiafrika yalikuwa na dhima kubwa katika muungano huu baina ya sanaa na hamasa. Yalikuwa ni pamoja na *Présence Africaine* (Paris), *Black Orpheus* (Ibadan) na *Transition* (Kampala na Accra)[3].

[2] J. Drysdale, 1964, uk. 15; na Legum, 1963 uk. 505
[3] Tazama P. Benson, 1986

Kwani ulumbi na balagha ni tanzu za fasihi? Ni dhahiri zinaweza kuwa, hasa kwenye jamii zenye mapokezi simulizi. Hebu basi tugeukie kwenye muungano huu maalumu baina ya ulumbi na ushairi.

## Sanaa ya kigeni na hamasa ya Kiafrika

Ni dhahiri kwamba ulumbi na balagha ni tanzu zilizoshamiri za fasihi ya Kiafrika. Mpaka wakati wa uhuru, mwanahamasa wa Kiafrika aliyetumia sanaa kwa ajili ya ulumbi wa kisiasa hakujifunga katika sanaa ya wenyeji tu. Hali kadhalika, mwanasiasa wa Kiafrika aliyetumia ushairi hakujifunga tu katika ushairi wa wenyeji vile vile. Kama ambavyo mpaka kati ya sanaa na hamasa ulivyokuwa na uvulivuli, ndivyo ilivyokuwa kwa mpaka baina ya fasihi ya wenyeji na ile iliyotoka nje. Waafrika walitumia lugha na fasihi za Wazungu kwa ajili ya ukombozi na ulumbi wa Afrika.

Hili linahusiana sana na mapenzi ya Waafrika ya kuchezea maneno. Fasihi ya Kizungu ililazimishwa kufuata kanuni za mazungumzo ya lugha za wenyeji wa Afrika. Umahiri wa kimazungumzo katika lugha nyingi za Kiafrika hulazimisha ufahamu mkubwa wa methali tofauti. Methali pia ndiyo njia kuu ya ulumbi. Mapenzi hayo ya wenyeji juu ya methali yalihamishiwa katika kudondoa fasihi ya kutoka nje. Donatus Nogwa, mhakiki wa fasihi kutoka Nigeria, anatuelezea juu ya msemo wa Kiigbo kuwa kutoa hotuba bila kutumia methali ni kama kujaribu kukwea mnara bila kamba.

Madondoo yalikuwa muhimu si kwa mazungumzo tu bali hata kwa ulumbi wa kisiasa dhidi ya ukoloni. Wanahamasa wapya wa Kiafrika walijitahidi kuwa wanafasihi. Watawala wa Kikoloni wa Afrika katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini ingawa walijali sana "uchochezi" na "ufisadi" walishindwa kujua nguvu za kisiasa za mawazo yaliyowekwa kishairi.

Mnamo November 12, 1956, akilihutubia Bunge juu ya uhuru unaokuja wa Ghana, Nkrumah alianza hotuba yake kwa kukariri usemi wa Edmund Burke: "Tuko katika jukwaa la wazi na dunia inaangalia mwenendo wetu." Nkrumah alisisitiza: "Hali hiyo haijapata kuwa dhahiri kama ilivyo sasa. Namna tutavyojiendesha tutakapokuwa huru haitaathiri Ghana tu bali Afrika nzima."[4] Kama ambavyo wazalendo wa Afrika walivyotumia lugha za Kizungu kwa ajili ya shughuli mpya ya mapambano ya siasa, hivyohivyo ndivyo walivyotumia kwa muda

[4] K. Nkrumah, 1961, uk. 71.

fasihi ya Kizungu kwa malengo ya kitaifa. Ushairi wa Kizungu uliwapatia madondoo yaliyotumiwa katika siku hizo za mwanzo za usomi wa Kiafrika wenye msukumo mpya. Fasihi ya kigeni ilizindua aina tata ya utaifa wa kitamaduni miongoni mwa wimbi jipya la wapigania uhuru wa Kiafrika. Iliwezesha aina mpya ya mazungumzo kwa kutumia methali. Aghalabu iliungana na Biblia au Kurani, au nyimbo za Kikristo na kasida, kutoa msisimko mpya kwa hisia za Waafrika. Fasihi na lugha za Kizungu zilikuwa msingi wa baadhi ya ulumbi ulioibuka katika kipindi hiki cha historia ya Kiafrika. Kama ulumbi na balagha ni tanzu za fasihi, awamu hii ilikuwa ni ya mchanganyiko wa kuvutia wa ushairi wa kigeni na balagha ya Kiafrika.

Lakini ni tabia ya uzalendo wa Afrika, kama ilivyo kwingineko, kuwa waangalifu na wagumu kukubali msukumo uliotoka nje - uwe wa kishairi au wa kiitikadi, wa Shakespeare au wa Lenin. Wazalendo hawakiri kuwepo kwa uzalendo wa kisasa wa Kiafrika unaotokana na maandiko ya wabeberu.

## Utunzi wa Ukombozi

Lakini si wanahamasa wote wa Kiafrika walitumia ushairi wa kigeni kwa ajili ya uzalendo wa Kiafrika. Baadhi ya wanahamasa wapya na wagombea uhuru walikuwa washairi na waandishi wa kubuni wao wenyewe. Baadhi yao walifanya warsha na kuunda asasi za utamaduni kukuza shughuli za kifasihi. Kati yao alikuwemo Agostinho Neto, ambaye baadaye alikuwa raisi wa kwanza wa Angola huru.

Mnamo miaka ya 1950, Amilcar Cabral na Mario de Andrade waliunda kwa siri Kituo cha Taaluma za Kiafrika (*Centro de Estudos Africanos*) wakiwa na lengo kuu la kukuza taaluma inayohusu watu weusi waliokuwa chini ya ukoloni, ikiwa ni pamoja na kuangalia na kukuza fasihi bunifu ya Kiafrika. Tawi la fasihi la asasi hiyo lilikuwa ni *Casa dos Estudantes do Imperio.*

Sanaa na hamasa ziliungana tena. Utawala wa Salazar mjini Lisbon ukipaukana na vuguvugu la kupinga ubeberu lililotokea Afrika ya baada ya vita, aliizuia *Casa dos Estudantes do Imperio* kuanzia 1952-1957. Baada ya hapo kituo hicho kiliendelea kupambana na watawala mara kwa mara mpaka kilipofungwa kabisa mwaka 1965. Kwa hiyo mawazo juu ya kuuthamini Unegro katika Afrika iliyotawaliwa na Wareno yalikuja kama pumzi ya hewa safi.

Ingawa waandishi walikandamizwa, amri za kibeberu hazikuweza kumnyamazisha Craveirinha - labda mshairi asiye Mzungu ambaye alikuwa mashuhuri zaidi Msumbiji - au Agostinho Neto, hata kama mashairi yao ilibidi yachapishwe mbali





Picha 19 2 Juu kushoto: Aimè Cèsaire Mwandishi wa Kifaransa aliyezaliwa Martinique,
Juu kulia: Lèopold Sèdar Senghor wa Senegal, mjumbe wa Akademia ya Kifaransa

na Ureno. Mashairi ya Craveirinha na Neto yalitokea Italia mnamo 1966, kwa mfano. Hamasa na sanaa ziliendelea kuungana kwa nguvu zaidi[5].

Uhusiano tata zaidi baina ya sanaa na hamasa, kati ya ushairi na siasa, ulikuwa katika mawazo ya Léopold Sédar Senghor. Kwa upande mmoja, Senghor alitafuta njia za kuukomboa utamaduni wa Kiafrika kutoka kwenye majivuno ya dharau ya Ulaya. Kwa upande mwingine, aliipenda nchi iliyomtawala. Kwa maneno yake mwenyewe, katika shairi la "Sala ya Amani" [*A Prayer for Peace*] anasema:

Bwana, kati ya mataifa ya watu weupe, aliiweka Ufaransa
Mkono wa kulia wa Baba. (...)
Naam, Bwana, isamehe Ufaransa ambayo inachukia
Watekaji wake lakini yenyewe
Inanitawala mimi kwa nguvu ...
Kwani, nina udhaifu kwa Ufaransa[6].

[5] Tazama C. Wauthier, 1996
[6] L.S Senghor, 1965, uk. 135-6

Kwa hiyo, tunaona kwa Léopold Senghor ushahidi kamili wa muungano baina ya uasi wa kishairi na ushirikiano wa kisiasa, msako wa uasili wa Kiafrika ukiungana na urithi wa kibeberu wa utegemezi wa kitamaduni wa Kiafrika.

Kwa watu kama Neto na Senghor, ni vigumu kuwa na hakika kama tunawaangalia wanasiasa walioingia kwenye fasihi au wanafasihi walioingia kwenye siasa. Iwapo wanasiasa kama Mboya na Awolowo katika miaka ya mwisho ya ukoloni na miaka ya mwanzo ya uhuru walijaribu kuingia kwenye fasihi, waandishi wa kipindi chote hiki kuanzia 1935 aghalabu walijaribu kuwa wanasiasa. Mwanzoni wanahamasa mara nyingi walijishughulisha na sanaa; lakini katika miaka iliyofuatia wasanii wamejishughulisha zaidi na uanasiasa. Inabidi basi tuliangalie kundi hili la waandishi walioingia kwenye siasa (kama kundi tofauti na lile la wanasiasa walio wanafasihi).

## Uasili: Mada saba zinazogongana

Majadiliano yetu ya historia ya fasihi ya Afrika hayawezi kutengwa na yale ya mada za mambo ya jumla, lakini katika sehemu hii tutaangalia kwa makini baadhi ya maeneo makuu yaliyosisitizwa katika fasihi ya wakati huu.

Migongano kadhaa inayohusiana ya kiamali ilijitokeza katika maandishi ya Kiafrika. Kati yake ulikuwepo mgongano baina ya ukale na usasa wa Kiafrika. Mara nyingi, mada za namna hii zilidhihirisha hamu kubwa ya kuonyesha ubora wa kile kilichokuwepo au kingeweza kuwapo zamani.

Kuhusiana na hili, ni mgongano kati ya jadi na usasa. Mgongano huu si sawa sana na ule wa kwanza, kwani mwingiliano wa jadi na usasa unaweza kutokea katika kipindi kilekile cha historia. Na bado hali hiyo inaendelea kujidhihirisha katika Afrika ya leo.

Mada ya tatu, ambayo inahusiana sana na zilizotangulia, lakini ambayo kwa vyovyote si sawa nazo, ni mgongano baina ya uenyeji na ugeni. Mila za wenyeji zinaweza kugombania umaarufu na mila zinazoingia kutoka nje. Mjadala uliopo ni kama kunaweza kuwepo na mkabala wa Kiafrika pekee katika kukuza maisha ya kisasa ambao hayahusishi kuingiza maisha ya Kimagharibi.

Mada ya nne, ambayo haikupata mashiko Afrika mpaka miaka ya 1960 ni mtanziko mkubwa baina ya ujamaa na ubepari, kati ya kutafuta usawa na kusaka utajiri.

Mada ya sita, na ambayo inahusiana sana, inahusu mtanziko baina ya maendeleo na kujitegemea, kati ya mabadiliko ya haraka ya kiuchumi yanayotokana na msaada

kutoka nje kwa upande mmoja na maendeleo ya polepole yanayotokana na juhudi za kutoka ndani kwa upande mwingine.

Mada ya saba, yahusu mwingiliano wa msingi zaidi kati ya Uafrika na ubinadamu, kati ya haki ya Waafrika kama jamia mahsusi ya watu au wakazi wa bara mahsusi na wajibu wa Waafrika kama binadamu.

Mada ya kwanza ya kushabikia ukale ina vipengee vinavyofanana na vuguvugu la Unegro katika sehemu za Afrika zinazozungumza Kifaransa. Kuna utukuzaji wa ukale, na mara nyingine kupenda mno ngoma na midundo kama vipengele vya utamaduni wa kale. Mfano mahsusi ni riwaya ya *Le regard du roi* (Nuru ya mfalme) cha Camara Laye. Kutamani mambo ya kale ya Kiafrika kunachanganywa na dhamira ya mgongano kati ya amali za kimila na usasa.

Lakini maisha ya kisasa ya Afrika hayatofautishwi na mila tu, bali yanaoanishwa sana na kuingia kwa Umagharibi. Ndio maana mjadala wa pili baina ya usasa na mila vimeunganishwa mno na mjadala wa tatu kati ya uenyeji na ugeni. Nguvu za aina tatu zilikuwa zikifanya kazi katika kurahisisha kuingia kwa wageni katika jamii za Kiafrika. Moja ilikuwa hasa elimu ya Kimagharibi, ambayo kilele chake kilikuwa vyuo vikuu kama vile vya Dakar, Ibadan na Makerere. Njia ya pili ya ilikuwa Ukristo wa Kimagharibi, ulioingiza miundo mipya ya itikeli na maelezo. Njia ya tatu ya kuiingilia Afrika ilikuwa teknolojia, hasa vipengele vile vilivyohusu mabadiliko ya kiuchumi na uzalishaji mali.

Waandishi wa kipindi hiki walifahamu zaidi athari za elimu na Ukristo wa Kimagharibi kuliko walivyoonyesha kufahamu athari za sayansi na teknolojia ya Magharibi. Kwa upande wa elimu, walitambua kuwa njia hizi mpya za ufundishaji na mahusiano ziliunda utegemezi wa kitamaduni. Waafrika wapya waliundwa – waliopunguka Uafrika wao kuliko wazazi wao. Jonathan Kariara, akiandika kwa Kiingereza na katika Chuo Kikuu cha Kimagharibi, aliandika juu ya ndoto ambayo alijiona akifungiwa katika udongo wa mfinyanzi, akizibwa pumzi na gimba la kigeni. Kwa upande wa athari ya Kikristo, hii nayo pia imejadiliwa sana katika fasihi ya Kiafrika. Mfano maarufu ni ule wa riwaya ya Mongo Beti ya *Kristo Maskini wa Bomba.** Athari ya Ukristo ilikuwa katika viwango mbalimbali – iliathiri upatikana wa maarifa, njia ya kulea watoto, kaida za kufundwa na unyago na jando, dhana ya usahihi na ukosaji, na miundo ya kueleza mambo ya asili, pamoja na tafsiri pana ya metafizikia na nguvu za kiungu. Ukristo wa Kimagharibi ulikuwa ni sehemu ya msingi ya Umagharibishaji wa Waafrika.

* Imefasiriwa kwa Kiswahili kwa jina la *Kasisi* wa Bomba

Hali hii ilikomaa kiasi cha kuwafanya baadhi ya Waafrika, kama Okot p' Bitek anavyoeleza, kuunda upya miungu yao kufuatana na taswira ya Mungu wa Kikristo. Baadhi ya waandishi wa Kiafrika, kama walivyofanya Wamisionari na wanaanthropolojia wa Magharibi, waliingiza dhana za Wayunani katika imani za Kiafrika.

Kuhusu mjadala baina ya mtu binafsi na jamii, nao pia ulihusishwa kwa kiasi fulani na athari za Ukristo na dhana ya Waprotestanti ya wajibu wa mtu mbele ya Mungu. Katika Afrika, ubinafsi ulikuzwa pia na mawazo ya mali ya binafsi ambayo yaliambatana na ubepari wa Kimagharibi.

Ubinafsi ulishamirishwa hasa na maadili huria mapya yaliyoambatana na itikadi za kisiasa za Magharibi. Umuhimu mkuu ambao uhuria ulitoa kwa ubinafsi ulisaidia kubadili upeo wa kisiasa wa waandishi wa Kiafrika, pamoja na wasomi wengine wa Kiafrika.

Katika siasa, uhuria wa Kimagharibi ulisaidia kuhamasisha madai ya "mtu mmoja, kura moja" na miundo ya kiliberali ya kujitawala. Katika fasihi, ubinafsi ulitoa waandishi wapya. Kwanza, fasihi simulizi ya jadi ilikuwa kwa namna fulani ni fasihi isiyokuwa na watunzi, urithi wa pamoja uliotungwa na wengi bila kumtambua mtu binafsi. Lakini riwaya na mashairi mapya, tamthiliya na hadithi fupi mpya zilikuwa ni kazi za wasanii maalumu, zilizokuwa na majina yao au lakabu zao. Kuanzishwa kwa fasihi katika lugha za Kizungu kulikuwa ni hatua muhimu ya kuachana na jadi ya pamoja ya urithi uliosambazwa kwa masimulizi. Mtindo huu mpya uliambatana na hakimiliki, mirabaha ya watunzi binafsi na kanuni za kupinga uigizaji kinyume cha sheria.

Zaidi ya hayo, baadhi ya miundo ya kisanii waandishi waliyoijaribu ilihitaji uwezo wa mwandishi wa kuunda wahusika wanaoaminika. Hadithi fupi za Afrika zinatokana na ngano; mashairi ya kisasa yanaweza kuwa mwendelezo wa ushairi wa kale, lakini riwaya kama inavyoeleweka kwa kawaida, ni dhahiri kuwa ni muundo wa kigeni ambao sasa unaendelezwa kwa ajili ya Waafrika. Na historia ya riwaya inahusishwa kwa karibu na kuibuka kwa ubinafsi huko Magharibi. Molly Mazrui katika tasnifu yake aliyoiandikia Makerere juu ya mtu binafsi na jamii, anaeleza:




Picha 19.3 Wole Soyinka wa Nigeria akipokea tuzo ya "Nobeli ya Fasihi"

> Watunzi wengi wa riwaya wa Afrika, wameangalia sababu za kuvunjika kwa meli [katika *Robinson Kruso*] na kujaribu kuelewa kama tukio hilo liliweza kuzuilika au la wametuonyesha dhiki ya moyoni na uliokumba watu binafsi na jamii yake kadiri amali na vipimo vya maadili vyenye kubadilika haraka vilivyozidi kushamiri .. zipo sababu nyingi za kulaani kukua huku kwa ubnafsi katika Afrika, lakini miongoni mwa sifa zake nzuri ni kuibuka kwa riwaya ya Kiafrika. Mjadala wa tano uliowaathiri waafrika ulihusu mtanziko kati ya ubepari na ujamaa. Shauku ya awali ya Waafrika juu ya walau matamko ya ujamaa ilihusiana na kiwango cha umoja uliokuwepo kati ya ubepari na ubeberu. Mawazo ya uzalendo wa Afrika yaliambatana na mawazo ya ujamaa[7]

Upingaji wa unyonyaji, uwe wa mabepari wa ndani au mabeberu kutoka nje, ulikuwa ndio umeanza kuwahamasisha wasomi wa Kiafrika kama vile Ousmane Sembene, Aykwei Armah, Chinua Achebe au Wole Soyinka, lakini zaidi ya hao wote ni Franz Fanon.

[7] M. Mazrui, 1972, uk. 407



PICHA 19.4 *Nagib Mahfuz wa Misri, mshindi wa Tunzo ya Nobel ya Fasihi Oktoba 1988*

Mwaka 1988, kiasi cha miaka miwili tu baada ya mafanikio ya mtunukiwa (wa Tunzo ya Nobel) Wole Soyinka, Funzo ya Fasihi ya Nobel ilirudi tena Afrika. Safari hii aliyepata zawadi hiyo alikuwa Nagib Mahfuz, mwanariwaya mkuu wa kisasa wa Misri, anayejali sana masuala ya unyonyaji. Kwa kufuata jadi ya Dickens, kazi zake nyingi za mwanzoni na za kipindi cha kati zililenga maisha ya mafukara wa mijini. Mahfuz alionyesha kujali sana tofauti ndogondogo na hali ya maisha katika mageto ya mijini – hasa katika kazi yake maarufu, *Bonde la al-Midakk*. Athari ya ulimwengu wa Magharibi kwa Afrika ya Kaskazini inaelezwa kwa mapana katika fasihi ya Maghreb. Kiarabu na Kifaransa zinashindana kama lugha za fasini nchini Algeria, Tunisia na Moroko. Majarida kadhaa ya mapitio ya fasihi yamesaidia kukuza vipaji vipya vyenye siasa kali. Jarida la *Al-Fikr* (Fikra) la Tunisia lilikuwa na jukumu muhimu la kihistoria, mara nyingine likichukua sura ya

kisiasa. Afrika Kaskazini inaongoza pia katika fasihi inayohusu ukombozi wa wanawake.

"Ufuataji wa maisha ya Magharibi" kama dhamira ya riwaya ya kisasa ya Misri inajumuisha riwaya ya Tawfik al-Hakim ya *Ndege kutoka Mashariki* na riwaya fupi ya Yahya Hakki ya *Taa ya Umm Hashim*. Mkinzano mkubwa wa kiutamaduni ndio kiini cha kazi hizo.

Huko Afrika Kaskasini, mvutano mara nyingine umekuwa ni kati ya Uislamu na uhamasishaji wa mtazamo wa kidunia. Katika bara zima, kanuni ya usawa aghalabu imewakereketa watunzi wa riwaya, washairi na wanatamthiliya.

Watunzi walibadilika, wakaacha kujishughulisha na suala lililowasumbua Waafrika kabla ya uhuru la kudai uasili, na kujiingiza katika kuleta mabadiliko ya kijamii na haki sawa.

A - Mjadala wa sita unahusiana sana na mpito huu kutoka hali ya kujali mno matatizo ya ukoloni kwenda katika masuala ya kipindi cha uhuru - hasa mjadala kati ya kupendelea maendeleo ya haraka ya kiuchumi na ya nidhamu ya kujitegemea na kujinyima. Mjadala huu kama suala la kifasihi ulipanuliwa zaidi Tanzania, hasa katika kipindi cha Azimio la Arusha na msako wa ujamaa. Muhimu ni kuwa mjadala mkubwa uliohusu kujitegemea nchini Tanzania ulikuwa katika fasihi ya Kiswahili kuliko maandiko ya Kiingereza. Utumiaji wa lugha iliyoeleweka zaidi na jamii ulikuwa ni sifa kubwa ya *ujamaa* na kipimo cha uasili halisi.



Picha 19.5 Molara Ogundipe-Leslie wa Nigeria. Profesa, mshairi, mwandishi wa fasihi na mhakiki

Ni dhahiri fasihi mpya ya kisiasa juu ya utegemezi wa Afrika inahusika na mawazo haya na inahusiana na fasihi ya utegemezi ya Amerika ya Kusini. Msisitizo wa mjadala ni kuwa Afrika inaweza kuwa imepata uhuru wa kisiasa, lakini mapambano ya uhuru wa kiuchumi na uasili wa utamaduni ndio kwanza yameanza. Uchumi wa Afrika bado umeingiliwa na ubepari kutoka nje, na mabwanyenye wapya weusi bado hasa ni washirika wa wageni na maslahi yao. Kuingiliwa kitamaduni ni pamoja na kuwepo kwa utamaduni wa ulaji, kuendelea kwa miundo ya elimu ya kikoloni, kuingiliwa kwa jamii za Kiafrika na vyombo vya habari na huduma za elektroni kutoka nje, kuendelea kwa sera za lugha zinazohudumia matakwa ya wasomi na tabaka tawala ambazo hazijali sana mahitaji ya umma. Kuendelea kwa utamaduni wa wasomi katika Afrika kutawaliwa na lugha za kigeni ni dalili ya utegemezi huu wa utamaduni ulioota mizizi.

Waandishi wa kike waliopinga ukoloni mamboleo ni pamoja na Molara Ogundipe-Leslie wa Nigeria, Abena Busia wa Ghana, na Christine Obbo wa Uganda. Waandishi wa kisiasa kutoka Afrika inayozungumza Kiingereza ambao walijihusisha na utegemezi wa kiuchumi ni pamoja na Adebayo Adedeji wa Nigeria, Issa Shivji wa Tanzania, Dan Nabudere wa Uganda na Atieno Odhiambo wa Kenya. Waandishi wa kisiasa waliojihusisha na utegemezi wa kiutamaduni ni pamoja Chinweizu wa Nigeria, Okot p' Bitek wa Uganda, Ali A. Mazrui wa Kenya na Julius Nyerere wa Tanzania. Maandiko mengi katika eneo hili ni ya kitaaluma au ya mabishano; ni machache tu yamechukua sura ya ushairi au masimulizi ya kubuni. Lakini mtanziko mkubwa baina ya maendeleo tegemezi kwa upande mmoja na kukwama kutokana na kujitegemea kwa upande mwingine unahuisha tu mitanziko ya zamani kama ule baina ya jadi na usasa, na baina ya uenyeji na ugeni. Suala walilopambana nalo waandishi wa mwanzoni mwa miongo ya awali ya karne ya 20 kuhusiana na mivutano ya usasa na uhuru sasa linaangaliwa kuhusiana na mivutano kati ya maendeleo na utegemezi. Lakini mwishowe tuna mjadala wa msingi zaidi ya yote - mjadala baina ya upekee wa Uafrika na wazo la ujumla wa Ulimwengu, baina ya upekee wa Uafrika na mtazamo mpana wa ubinadamu. Waandishi wetu wa kabla ya uhuru walitumia sana wazo la ubinadamu, lakini zaidi kwa lengo la kudai haki za Waafrika.

Chinua Achebe ameelezea juu ya "mzigo wa mtu mweusi," akionyesha kuwa katika Afrika ya kikoloni ilikuwa ni kazi ya mwandishi wa Kiafrika kushambulia ukosefu wa haki uliotokana na ukoloni. Katika Afrika huru, kwa mujibu wa Achebe, mwandishi bado inabidi akubali jukumu la kupingana na ukosefu wa haki kila anapouona, hata kama ukosefu huo wa haki unafanywa na Waafrika dhidi ya Waafrika wenzao.

Kwa upande mmoja, uhuru wa kisiasa umesaidia kupanua upeo wa maadili ya wasomi wa Kiafrika. Kupitia uonevu unaofanywa na Waafrika kwa Waafrika wenzao baada ya uzoefu na kutawaliwa kwa Waafrika na Wazungu, ni kujifunza juu ya mapana ya kilimwengu ya haki na wajibu. Kuwepo kwa msimamo mkali kati ya waandishi ni sehemu ya kujijusurisha katika masuala haya mapya yaliyobidi kuangaliwa. Baadhi ya waandishi wamekwenda zaidi ya kudai haki kwa ajili ya Waafrika, au kwa ajili ya watu weusi - wamevuka hata mipaka ya umoja wa Waafrika kama udugu maalumu, na badala yake wamejaribu kujihusisha na makabwela kwa jumla. Waandishi wamegeuka kuwa wanasiasa, kama wanasiasa walivyogeuka kuwa waandishi hapo zamani. Wanahabari wa mwelekeo huu wa kiulimwengu ni pamoja na Muhammad Sid-Ahmed wa *Al-Ahram* ya Kairo.*

Mada hii ya saba ya mgongano baina ya matakwa-finyu na matakwa ya kiulimwengu, baina ya Uafrika na ubinadamu, labda ndio suala la msingi kabisa la uhasilia. Mvutano baina ya kale na sasa, jadi na usasa mwishowe ni machungu ya vipindi vinavyovuka nyakati mbalimbali. Mivutano baina ya uenyeji na ugeni inahusisha mjadala ulioenea sana. Mgongano baina ya ujamaa na ubepari ni mgongano wa amali. Mtanziko kati ya maendeleo ya haraka na kukwama kutokana na kujitegemea pia unahusu amali, lakini ukichukua sura ya uwekaji wa aula katika sera. Lakini mwishowe, ni uhusiano kati ya mtu binafsi na jamii kwa upande mmoja, na jamii na ulimwengu kwa upande mwingine, ndio msingi wa sanaa yenyewe. Jinsi binadamu anavyohusiana na jamii inayomzunguka, na jinsi jamii hiyo inavyohusiana na ubinadamu wenyewe, pamoja vinaunda hatima ya mjadala wa ujumi kiulimwengu. Senghor ameuita "Ustaarabu wa Kiulimwengu." Waandishi wa Kiafrika tuliowatalii kwenye waraka huu ni sehemu muhimu ya mjadala huo. Wakiwa wamebanwa katika machungu yenye sura nyingi - kulingana na siasa, elimu, lugha, ujumi na ufundi - waandishi wa Kiafrika wanajishughulisha katika kuendesha mapambano ya kurudisha kumbukumbu, kwa nia ya kutambuliwa kikamilifu.

## Juu ya fasihi na vita

Ingawa fasihi ya Kiafrika ya baada ya uhuru imehusika sana na majeshi, imejishughulisha kidogo sana na vita vyenyewe. Na katika kuwajadili askari, waandishi wa Kiafrika wamejishughulisha zaidi na wanajeshi wabaya kuliko mashujaa. Uhusiano wa kiadui umeibuka baina ya waandishi na askari, isipokuwa kwa wapigania uhuru wa Kaskazini na Kusini mwa Afrika. Kizazi kizima cha waandishi wa Algeria kilihamasishwa na mapambano ya silaha. Na hata hivyo,



Picha 19.6 Andre Brink wa Afrika ya Kusini, mwandishi wa upinga ubaguzi

hata washairi wapigania uhuru kama Dennis Brutus wa Afrika Kusini hawana msimamo thabiti kuhusu "mabuti, singe na makonzi."

Maswali mawili yanaibuka: Kwa nini kuna fasihi kidogo sana iliyoandikwa juu ya ushujaa wa kijeshi katika Afrika ya baada ya ukoloni? Na kwa nini kuna maandiko mengi kuhusu ubaya wa majeshi?

Upungufu mkubwa wa fasihi andishi ya ushujaa hautokani na upungufu wa mashujaa. Mashujaa wengi wanaume na wanawake wamekufa kutetea malengo yanayowahusu katika vita vya Afrika tangu uhuru. Lakini aina ya vita hivyo imefanya kuimba nyimbo za sifa juu ya mashujaa hao kuwe ni suala nyeti kisiasa. Kwani. zaidi ya Misri, vita vingi vilivyotokea katika nchi za Afrika huru vimekuwa ni vya wenyewe kwa wenyewe, ambavyo aghalabu vya kutaka kujitenga.

Sababu nyingine ya kutokuwepo kwa ushujaa wa kijeshi katika fasihi ya Kiafrika kunatokana na kutoshiriki sana kwa wasomi katika mapigano katika vita vingi vya Afrika vya tangu uhuru. Washairi na waandishi wamehamasishwa zaidi na kujitoa muhanga kwa wasomi wenzao kuliko vifo vya wakulima wasiojulikana. Kifo cha Christoper Okigbo katika vita vya ndani vya Nigeria kilihamasisha maandiko makubwa kuliko vifo vya Waigbo vijana wasiojulikana nusu milioni. Ali Mazrui aliandika riwaya yake pekee, *majaribu ya Christoper Okigbo* kuelezea* kifo cha msomi mwenzake.

Uchache wa fasihi ya ushujaa wa Waafrika unaweza ukawa umetokana na ukweli kwamba vita dhidi ya mataifa ya nje ndivyo huweza kuzaa uzalendo uzalendo unaoheshimu mashujaa. Kumbe Afrika - hasa ya kusini mwa Sahara - haijawa na vita vingi vilivyopiganwa na maadui kutoka nje tangu uhuru.

Vita ya Oktoba 1973 baina ya Misri na Uyahudi vilichukuliwa kuwa ni vya kishujaa na Wamisri na vilitoa mashairi na nyimbo nchini Misri. Vita vya Moroko vya kushikilia Sahara ya Magharibi pia vilionekana na wengi ndani ya nchi hiyo kuwa ni vya kizalendo - na hivyo navyo pia vilihamasisha nyimbo na ushairi. Sahara ya Magharibi (ambayo inatambulika na Umoja wa Nchi Huru za Afrika kuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi) nayo kwa upande wake imetoa fasihi yake yenyewe ya kishujaa juu ya mapambano yake na Moroko. Vita vya Pembe ya Afrika navyo pia vimezaa ushairi wake wa machungu.

Kwa Chad, Libya ilikuwa ni taifa la kigeni. Mapambano ya Chad dhidi ya mamlaka ya Libya yalisaidia kukuza mashairi simulizi na nyimbo za ushujaa. Mnamo 1987, Chad iliingia ndani ya ardhi ya Libya kwa mara ya kwanza: Uzalendo wa Libya ulichomwa kwa njia mpya. Ilikuwa ni muda kidogo tu Libya ilipojibu mashambulizi kulinda *al-watan* (ardhi ya wahenga wao) na kuhamasisha fasihi yake ya ushujaa. Kusini mwa Sahara, taswira ya mpiganaji inatumika hasa katika lugha za wenyeji - lakini mara nyingi kama sitiari ya kuelezea mapambano yasiyokuwa ya kijeshi.

Kama kuna upungufu wa mashujaa halisi wa kijeshi Kiafrika katika fasihi, kwa nini kuwe na wingi wa mahasidi wa kijeshi wa Kiafrika? Sababu kubwa ni kwamba tangu uhuru askari wameelekea zaidi katika kujishughulisha na siasa kuliko vita. Na bado askari na waandishi wana mawazo tofauti kuhusu mchakato wa kisiasa. Labda uhusiano wa kiadui umekuwepo baina ya waandishi na watawala - wawe watawala hao ni wa kijeshi au kiraia.

Kitabu cha Wole Soyinka ambacho kimeandikwa kwa hasira na hata labda kukosa mantiki, ni *Mtu amekufa*. Ni shutuma kubwa dhidi ya uonevu na hasa

dhidi ya wanajeshi. Ni maelezo ya mateso ya kufungwa aliyoyapata Soyinka wakati wa utawala wa Jenerali Gowon.

Mwandishi wa riwaya mashuhuri wa Somalia, Nuruddin Farah, ameandika riwaya tatu dhidi ya uonevu wa kijeshi nchini mwake. Ingawa anatoka kwenye familia ya washairi wa lugha ya Kisomali, Farah aliacha kutumia lugha yake ya kuzaliwa nayo kama lugha ya kuandikia kazi zake. Sababu alizotoa ni kuwa kulikuwa na ukandamizwaji Somalia. Kama angeandika kwa Kisomali hakuna mtu ambaye angesoma kazi zake. Wakati wa utawala wa Siad Barre, vitabu vya Farah vilipigwa marufuku mahali ambako vingeweza kuuzwa zaidi kwa lugha ya Kisomali - Somalia kwenyewe. Katika tamthiliya zake, Farah aghalabu amekuwa akirudi katika mada ya uonevu. *Yusuf na Kaka Zake* ni hadithi hasa ya ushujaa dhidi ya uchafu wa ukandamizaji.

Kwa ulinganifu, tathmini, bado ni jambo la kutatiza kwamba katika fasihi ya baada ya uhuru vita havijahamasisha "hisia kali za ushairi, zilizokumbukwa wakatowa amani." Pia ni kioja cha kipindi cha baada ya ukoloni kuwa askari wa Kiafrika wanatambuliwa zaidi katika fasihi kama waovu kuliko mashujaa. Hii ni pamoja na riwaya ya Chinua Achebe ya 1987, *Vichuguu vya Savana*, riwaya yake ya kwanza tangu vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Nigeria. Askari wa baada ya ukoloni wameamsha uadui zaidi kuliko kuonekana kuwa ni mashujaa kwa waandishi.

## Hitimisho: Fasihi na Urithi wa Aina Tatu

Kama ilivyo kwa tanzu nyingine za utamaduni, fasihi ya Kiafrika imeathiriwa sana na urithi wa aina tatu. Urithi huo unaweza kuwekwa katika mapokeo matatu ya amali za wenyeji, athari ya Uislamu na athari za utamaduni wa Magharibi. Tanzu mbalimbali za fasihi zimeuchukulia urithi huu kwa njia tofauti.

Iwapo bunilizi za Kiafrika zimetajirishwa sana na uhusiano na Magharibi, ushairi wa Kiafrika wa wenyeji katika bara ya Afrika Magharibi na pwani ya Bahari ya Hindi umetajirishwa sana na uhusiano na Uislamu. Hata katika kipengele chenye utata kidini cha nyimbo, utunzi wake umechanganya Uislamu na Uafrika.

Wasomali wamekuza, kama tulivyoonyesha awali, utamaduni simulizi pekee na hata wamebuni ushairi faraguzi. Shujaa wao mkuu kitaifa wa enzi hizi - Sayed Muhammad Abdallah Hassan - alikuwa (kwa kutumia sitiari ya Waingereza) mchanganyiko wa Shakespeare na Churchill. Mwalimu huyu mwenye sifa za pekee za busara alikuwa mkombozi wa taifa na shujaa wa lugha. Athari yake katika ushairi wa kisasa wa Kisomali ni kubwa kiasi kwamba Sayed anatambuliwa kuwa

ni mmoja kati ya msukumo shadidi wa fasihi ya kisasa ya Kisomali. Waandishi wengi wa Tanzania si Waislamu. Lakini bado taratibu za ushairi wa Kiswahili zinatokana, kwa upande mmoja, na uhusiano baina ya utamaduni wa Kiislamu na Kiafrika. Taswira nyingi zinatokana na maneno yaliyotokana na Kiarabu. Aghalabu kuwepo neno moja la Kibantu na mshabaha wake wa Kiarabu, ni faida kwa washairi wa Kiswahili. Na washairi wanapokwama kupata neno kwa ajili ya dhana mpya marejeo mawili ya kawaida yamekuwa ni urithi wao wa Kibantu na Kiislamu.

Uislamu umechukua dhima iliyokuwa na sura mbili katika lugha na fasihi za Kiafrika. Ili kufuata kanuni, sala ni lazima ziwe kwa Kiarabu. Adhana iwaitayo waumini kusali huwa kwa Kiarabu. Kurani katika utakatifu wake ni lazima isomwe kwa Kiarabu.

Kwa kuangalia juujuu inaonekana kama Uislamu si dini stahamilivu kwa lugha nyingine kuliko Ukristo. Hata Ukatoliki umepunguza matumizi ya Kilatini katika ibada na kaida zake. Yesu alisema Kiaramia, Biblia ni kitabu kilichofasiriwa hata hivyo, kwa hiyo kwa nini kusiwe na tafsiri moja nyingine katika lugha ya Kiafrika? Hivyo Biblia imekwisha fasiriwa katika zaidi ya lugha 100 za Kiafrika. Ni kama kwamba Mungu wa Kikristo ni Mungu aliye uhamishoni. Ukristo ni dini iliyoshindwa kuota mizizi nyumbani ikashamiri ughaibuni. Kitovu chake hakikuwa miongoni mwa Wayahudi na Wasemiti wengine bali miongoni mwa Wazungu - si Mashariki ya Kati bali Magharibi. Kwa hiyo ilikuwa rahisi kulikubali neno la Mungu lililofasiriwa. Kwa upande mwingine, Uislamu ulishamiri kati ya wale walioteremshiwa mwanzo - na katika lugha ulimoteremshiwa, Kiarabu. Kusisitiza kuwa Kiarabu ndio lugha ya ibada ni kusisitiza uasilia. Ni kusisitizia ushairi wa asili wa Kurani. Ushairi wa Kihausa umebaini athari ya Kurani.

Lakini je kusisitiza Kiarabu kitumike katika ibada rasmi kumesaidia au kumekwamisha lugha za Kiafrika zilizokabiliana na Uislamu, na ushairi wa Kiafrika uliokabiliana na Uislamu? Katika Afrika iliyohusiana na Uislamu Kusini mwa Sahara kabla ya ukoloni wa Wazungu, Kiarabu hakikuwa lugha rasmi ya dola bali lugha rasmi ya msikitini. Kwa jumla, athari yake ilikuwa ni kutajirisha lugha kama Kiswahili. Lugha nyingine zilizoathirika na Kiarabu ni Kiwolof, Kisomali, Kitigrinya na Kitigre.

Je ushairi wa Kiafrika ulichukuliaje urithi wa Kiafrika wa aina tatu? Ni jinsi gani fasihi ya Kiafrika imeathiriwa na urithi kutoka nje wa Kimagharibi na Kiislamu? Kuna mawazo ya wanazuoni wa Magharibi yanayowaona Waafrika kuwa hawana uwezo kabisa wa kuwa wasanii. Hebu tuiangalie changamoto hii kwa karibu.

Thomas Jefferson wa Amerika alifikia kiasi cha kuwaona Waafrika kuwa hawana uwezo wa kuwa wasanii au washairi. Katika *Taarifa za Jimbo la Virginia* (Paris 1784), anaeleza mambo yafuatayo yanayoshangaza.

"...sijapata kuona kuwa mtu mweusi ametoa wazo zaidi ya masimulizi ya kawaida; sijapata kuona hata dalili tu ya mchoro au mchongo. Kwa kawaida katika muziki wana kipaji zaidi ya weupe katika usahihi wa sauti na mapigo, na wameweza kubuni vipande vidogo vya nyimbo. Kama wanaweza wakafikia utunzi wa sauti nyingi au upatanifu wa sauti tata, hiyo bado haijahakikishwa."

Iwapo Hegel na Hugh Trevor-Roper waliwaona Waafrika kuwa hawana uwezo wa kuunda historia, Jefferson hapo awali aliwaona kuwa hawana uwezo wa kuwa wasanii. Lakini aina hizo zote mbili za mawazo ya kibaguzi zimepingwa mara nyingi na utafiti wa muda mrefu wa kihistoria na kijamii.

Juu ya imani ya Jefferson kuwa weusi ni watu wasio na ushairi, washairi weusi kutoka Ethiopia waliandika ushairi kabla ya wahenga wa Jefferson wa Visiwa vya Uingereza hawajafunzwa alfabeti ya Kilatini na Warumi. Na jadi ya ushairi wa watu wazungumzao Kiswahili katika Afrika ya Mashariki imewaingia kiasi kwamba katika magazeti ya hivi sasa hawapokei tu "Barua kwa Mhariri" bali "Mashairi kwa Mhariri" karibu kila siku.

Utanzu wenye nguvu zaidi wa fasihi katika Afrika bado unaendelea kuwa ni ushairi wa masimulizi na andishi, kwa lugha za wenyeji na vilevile za wageni. Baadhi ya mashairi yanasherehekea upekee wa Uafrika, wakati mengine ni kilio cha uchungu. Léopold Sédar Senghor anaunganisha Uafrika na Uanauke. Kama Hawa alikuwa mama wa binadamu, na Afrika ilikuwa mama wa Hawa, basi wapi Afrika inaishia na Uanauke kuanza? Senghor anajibu hivi:

Mwanamke uliye utupu, mwanamke mweusi
Katika rangi yako ambayo ni uhai
Katika umbo lako ambalo ni uzuri!
Nimekulia katika kivuli chako
Uzuri wa mikono yako ulifunga macho yangu.
Na sasa katikati ya majira ya joto na adhuhuri
Ninakugundua, dunia iliyoahidiwa ,
Kutoka kwenye kinara cha shingo yako iliyochomwa na jua
Na uzuri wako unanichoma kikamilifu
Na kuninyegeza kama mwali wa tai
Mwanamke uliye utupu, mwanamke mweusi ...

Lakini kuna zaidi ya huzuni na furaha katika fasihi ya Kiafrika - zaidi ya tanzia na ucheshi. Tukimfasili na kumfafanua mwanaubalozi wa Sierra Leone, Davidson Abioseh Nicol:

Wewe si nchi, Afrika,
Wewe ni dhana ...
Wewe si dhana, Afrika,
Wewe ni tazamo la (ulimwengu) usio na mwisho.

# 20 Sanaa na Jamii tangu 1935

Kila mahali katika Afrika leo tunashuhudia ongezeko kubwa la kushangaza la ubunifu katika sanaa linalotokea katika matabaka yote ya kijamii. Shughuli za sanaa zimekuwa maridhawa na tofauti tofauti, ingawa inawezekana kuanisha sifa chache za jumla za kijamii na kitamaduni ambazo zimeathiri mikondo yake mikuu ya maendeleo[1]. Hizi ni pamoja na: upevukaji, lakini usio sawa kote wa athari ya Ulaya, ukuaji wa miji, uibukaji wa matabaka mapya, ugawaji wa muda kitasnia ambao umewezesha kuwepo kwa muda wa mapumziko, fahari iliyopewa usanii na mafunzo ya kiufundi. Dhima ya msanii katika jamii imebadilika kutoka kuwa ile ya fundi mchundo na kuwa ya mwaguzi wa kitamaduni, na mitazamo juu ya kazi za sanaa na matumizi yake imebadilika. Vituo vya utoaji wa kazi za sanaa vimeongezeka, kukiwa na wamiliki wapya, ambao si vitengo vya serikali na sehemu za ibada pekee, bali pia mabaa, kumbi za dansi, asasi za kijeshi, shule na makumbusho. Mitindo imeongezeka, na kutokea kwake kunatokana hasa na miji mikubwa kama vile Kairo, Tunis, Algiers, Fez, Nairobi, Lagos, Dakar, Kinshasa, Luanda na Soweto. Hali hii inaonyesha wazi kuwepo kwa ununuzi wa kifahari[2] na mvuto wa Waali kama kikundi elekezi.

Tutaanza na sanaa onwa na sanaa zinazohusu mwili, halafu tutaangalia sanaa za vitendo: muziki, baadhi ya dansi zikifuatiwa na matamasha. Tunahitimisha kwa

[1] Marejeo mawili ya jumla ni L.J.P. Gaskin, 1965, na D. Coulet-Western, 1975. Kazi ya Mwanzo ya T. Heyse, 1950, bado inafaa. Majarida yanayoripoti kuhusu sanaa za maonyesho ni African Arts, Présence Africaine, Afrique literaire et artistique na West Africa. Upatikanaji wa Orodha ya makumbusho ya Taifa ya Sanaa za Kiafrika ya (Washington) hutupa chanzo kingine cha Marejeo mapya. Marejeo mahsusi na ya jumla

[2] T. Veblen, 1899, toleo la uk. 185-7 na uk. 66-101.

kutoa maoni kadhaa kuhusu dhima ya sanaa za Kiafrika katika muktadha wa Ulimwengu.

## Sanaa onwa

Baada ya 1935, sanaa onwa zinaweza kugawanywa katika makundi manne: za kijadi[3], za kitalii, sanaa pendwa za mjini, na sanaa za kitaaluma, kulingana na maudhui, mitindo, umiliki, malengo na mahali zinapozalishwa. Sanaa ya jadi, aghalabu michongo, lakini pia michoro ya ukutani ya (maumbo ya vitu au viumbe) na na makimba ya kijiometri[4], ilitengenezwa maeneo ya shamba na katika miji michache ya zamani. Vitu vilivyotengenezwa vilikuwa kwa ajili ya matumizi. Vilitumiwa kwenye sherehe za jando na unyago, mazishi, majumba ya baraza, kasri na baadhi ya makanisa ya Kikristo[5]. Sanaa za kitalii ziliwalenga wanunuzi kutoka nje, na maudhui yake yalipendelea mada za kustaajabisha na za juujuu, kwa mitindo sahihi ya makimba, na ilifuata vigezo vilivyoathiriwa na Uzungu.

Sanaa pendwa ya mijini iliibuka takriban mwaka 1930 Afrika ya Kati, lakini mapema zaidi huko Afrika Kaskazini, na ilikuwa ya makimba. Ilihusu hasa michoro ya kurembesha kuta za nyumba za mijini, na picha za watu, ambapo picha za kihistoria, michapo na mapambo zilipendelewa. Aina nyingine ya sanaa pendwa inaonyeshwa katika picha za kuashiria maduka, magari, sinema na kadhalika. Sanaa ya kitaaluma ilishughulikiwa na wasanii waliofunzwa kwa misingi ya Kimagharibi ya uchoraji na uchongaji, kwa kutumia mbinu za Kizungu. Wanunuzi wake walikuwa serikali, makanisa au soko la kimataifa la sanaa.

Makundi hayo si kwamba yaliachana kabisa. Vifaa vya jadi vingeweza kuwavutia watalii, na vilevile vitu vya kitalii vingeweza kuwavutia wasomi wenyeji ambao wangeweza kumudu bei zake. Zaidi ya hayo, baadhi ya wasanii waliingia kwenye fani za sanaa ambazo ni tofauti na zile walizojifunza. Ingawaje kwa jumla, kwa zaidi ya vizazi viwili vinavyojadiliwa hapa, mielekeo hii ya kisanaa iliendelea kuwa tofauti.

3 Istilahi 'Kijadi,' ijapokuwa huendana na matumizi, sio la kupendeza. Sanaa za kijadi zilikuwa zinabadilika mara kwa mara na baadhi ya sanaa za kijadi za 1935 hazikuwepo kabisa miaka ya 1900 au mwaka 1880. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa mwafaka wa istilahi, nitatumia "kijadi" katika makala haya.

4 Upakaji rangi kuta wa kijadi katika sehemu nyingi za Afrika ya Kati na Mashariki uligunduliwa baada ya mitindo mipya ya ujezi wa nyumba iliposhamiri kutoka 1980 na kuendelea.

5 Kuhusu Sanaa za Kikristo, tazama J.F. Thiel na N. Helf, 1984; Anon, na Etudes des religions africaines, 1982 Juzuu 16, Na 31-2.

JEDWALI 20.1 *Kategoria za kijamii za sanaa za maonyesho*

| Kategoria | Aina ya kazi | Lengo | Mdhamini | Mjini/vijijini | Dhima |
|---|---|---|---|---|---|
| Kitamaduni | Nakala zisizo sanifu zimekamilishwa vizuri | Kwa matumizi | Umma Binafsi | Vijijini | Ukufunzi wa Sanaa |
| Utalii | Imesanifishwa Haikukamilishwa vizuri | Ukumbusho | Watalii wageni | Mijini | Ukufunzi wa Sanaa |
| Sanaa pendwa[a] | Imesanifishwa Haikukamilishwa vizuri | Maonyesho | Umma (k.m. kanisa) Binafsi | Mijini | Ukufunzi wa Sanaa |
| Taaluma[a] | Kazi za kufanana zimemalizwa vizuri | Maonyesho | Serikali wageni | Mijini | Wasanii |

a Imetengenezwa hasa baada ya 1935

b Kuondoa maudhui ya kidhamira na mtindo.

Hata hivyo, makundi haya hayahusu usanifu majengo wa kisasa, kwani kusini mwa Sahara usanifu majengo mchache sana uliachiwa wasanifu wa Kiafrika. Usanifu majengo pendwa wa kiuvumbuzi wa wenyeji uliishia kwenye ujenzi wa nyumba za ibada[6].

## Sanaa za jadi

Ingawa kutoweka kwake kulitabiriwa muda mrefu kabla ya 1935[7], sanaa za jadi bado ziko hai na zinashamiri hadi leo. Waafrika wengi bado wana maisha ya kijijini na wanatamani kujieleza kisanii. Ni kweli kwamba uanuae na uzalishaji wa sanaa hizi ulikuwa finyu ilipofika 1935, kwa sababu ya mashindano yaliyotokana na bidhaa rahisi kutoka nje. Baada ya 1960, hata vyombo vya kauri (vya mfinyanzi), ambavyo viliweza kustahimili ushindani wa vyombo vya bati, viliachwa enzi ya plastiki ilipoanza. Nguo za wenyeji zilikuwa ghali zaidi hivyo ziliendelea kuwepo kama vitu vya watalii tu au kwa ajili ya matumizi ya maleba aghali ya kitaifa. Kilio kuwa sanaa za jadi zinazotoweka kilisababisha kuchukuliwa hatua za kiserikali za kupendelea kazi za mikono, hasa huko Tunisia, Ghana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo[8]. Kuingilia kati kwa serikali kulihifadhi au angalau kuchelewesha kutoweka kwa ujuzi wa kiufundi.

Uchongaji na uchoraji katika mazingira ya kijadi ulidumisha maendeleo yake ya kimtindo baada ya 1935. Uchoraji kwa ajili ya dini huko Ethiopia ni mfano mzuri[9], kama ilivyokuwa kwa majengo na uchongaji kwa ajili ya mahekalu ya kijadi kusini mashariki mwa Nigeria[10]. Katika sanaa ya Kuba ya kipindi hiki, malighafi ya uchongaji iliongezeka (kwa mfano mpingo na pembe za ndovu), lakini uchanganyano wa hazina ya mitindo ulipungua. Vinyago vya pwani ya Afrika Magharibi viliongezeka katika uchangamano na ubunifu jinsi ambavyo matumizi yake yalivyobadilika kutoka kwenye shughuli za kidini na kuwa vya tamasha. Wakati mwingine usanifishaji wa mitindo na uwiano na urari bora zaidi ulichukua nafasi ya ufaraguzi (kwa mfano katika sanaa ya Senugo), mara nyingine kinyume chake

[6] H. Schissel, 1985

[7] Kwa mfano, tazama F. Willett, 1971, uk. 239; na W. Gillon, 1984, uk 347-8, hutaja mwisho wa Vita Vikuu II kama Ukomo wa Sanaa ya Kijadi. Vitabu vya hivi karibuni kuhusu Sanaa ya Kisasa huelekea kuiweka tarehe za kutoweka huko kuanzia 1960 na uhuru; K. Fosa 1986

[8] Tume ya sanaa na pour es art métiers indigenes du kongo ya Kibelgiji ni tangu 1934, Shule za Tunisia tangu 1935, Ghana kabla 1929.

[9] U. Eckadrdt na G. Sievernich, 1979, uk. 56-67

[10] H. Cole, 1982

kilitokea (kama katika sanaa ya Baule). Katika sherehe za mafundo ya Wagenya (Kisangani, Kongo) usasishaji wa sanamu ulikuwa ukiendelea.

Huko Afrika ya kaskazini uhuru ulisababisha msisitizo mkubwa katika usanifu majengo wa jadi na ukarabati wa kumbukumbu za kale, kama vile kaburi kuu la Mohamed V. wa Moroko, uhuishaji wa ukataji wa mawe Tunisia, na ukarabati wa majengo wa kila mahali. Kazi mpya zilikuwa ni pamoja na majengo kama ukumbi wa opera wa Kairo wewe kuakisi mapokezi ya Kimamluk[11]

Hata kama kurejea huko kwenye asili ya jadi za kikanda hakukutokea pote, katika sehemu nyingi za Afrika sanaa ya jadi bado iko hai na inashamiri.

## Sanaa ya kitalii

Mnamo 1935, sanaa ya kitalii bado ilikuwa biashara ndogo, isipokuwa kwa Misri ambako vifaa vya bandia vya Kifarao na aina zote za madoido ya ajabu na yenye kupendeza yaliuzika vyema. Lakini utalii tayari ulikuwa ukiongezeka na hivyo uzalishaji uliongezeka kulingana nao. Pale ambapo michongo ya jadi ilipopendwa, nakala mbovu zilizalishwa kwa wingi, na kazi adimu ziliigwa na hata kughushiwa. Kwa mfano, vyombo vya shaba nyeupe vya Kifumba (Kameruni) katika mtindo wa Kiife vilitengenezwa kwa mara ya kwanza kwenye miaka ya 1940. Pili, mitindo iliyokuwepo iliendelezwa zaidi. Sanamu za Kikuba kwa ajili ya soko la watalii mnamo miaka ya 1930 zilitokana na sanamu za kifalme, sanamu za kiganga na sanamu zilizotengenezewa Watemi. Tatu, sanamu za Kizungu, ziwe za Kikristo au kidunia, ziliigwa.


Nafasi ya wamisionari ilikuwa muhimu hapa, si tu kwa kuwa walihimiza uzalishaji wa kazi hizo kwa ajili ya makanisa, bali pia kwa sababu ya shule za ufundi walizozianzisha ambazo zilitoa nguo, mikeka, kauri na kazi za mbao zilizoigizwa kwa ajili ya kuuzwa.

Sanaa ya kitalii inanunuliwa kama ukumbusho. Ujumbe unaotolewa kwa hiyo ni lazima uwe unaojulikana sana wakati huo huo wa kushangaza. Kwa hiyo, mpingo na pembe zilitumika kuwakilisha wanyamapori wa ajabu au mada za porojo kama maisha ya kila siku ya vijijini au ngoma, au mifano ya wanasesere wa maleba, kama wapiganaji wa Kimaasai[12], Wamangbetu[13] wenye vichwa vilivyorefushwa,

11 Anon, 1985

12 Madoli yalitengenezwa Afrika Kusini kutoka 1815 hadi miaka ya 1860, lakini baadaye yakakosa wateae. Mahali pengine aina hii ya zawadi haikupata mashiiko.

13 B. Jules-Rosette, 1984, ni utafiti wa msingi; Tazama P. Ben Amos, 1977, Kuhusu maana na muundo; na C. Geary, 1983, uk. 74-6 na 86-7, kuhusu kuanguka kwa ubora kwa kulinganisha kati ya kazi kijadi za Foumban (Kameruni) na kazi walizopata watalii.



*Picha 20.1 Mafundi mchundo wakitengeneza sanamu za shaba nyeupe "brass" Foumban, Kameruni*

au Dasti "za kawaida" kama zile zinazotengenezwa kwenye karakana ya Massengo ya Brazzaville. Pia kulikuwa na mahitaji yaliyotegemea hali halisi. Katika enzi za usafiri wa bahari, samani kubwa za mbao kama vile masanduku ya Zanzibar au viti vya Benin vilipendwa. Lakini baada ya 1945 enzi ya usafiri wa ndege na utalii wa watu wengi ilihitaji vitu vidogo na vyepesi, kwa mfano viti vya mashogi ya ngamia na meza za kahawa zinazokongoka kwa urahisi. Mito ya kujaza upepo ya Afrika ya Kaskazini, hata kama rangi zake zilikirihisha, iliuzika vizuri, kama ilivyokuwa kwa mazulia mapya yenye michoro ya Maghreb, yaliyoitwa "Beriberi" au "Kabile". Hayo ndiyo yaliyokuwa mahitaji ya sanaa ya kitalii. Zaidi ya hayo, ilibidi iwe ya bei rahisi na inayotengenezeka kwa urahisi, hivyo ikawa ya ovyo ovyo. Bidhaa zenye ubora wa juu kwa ajili ya kusafirishwa nje kama vile mazulia ya Fez na nguo nzuri za Kuba hazikupata soko kubwa.



PICHA 20. 2 *"Sanaa ya kitalii" au "Sanaa ya kwenye viwanja vya ndege"*

Katika awamu ya kwanza hadi kufikia 1950, uzalishaji uliongezwa na shule, viwanda vya sanaa na baadaye vyama vya ushirika. Masoko yalikuwa karibu na mahoteli makubwa kwenye bandari na miji mikuu. Baada ya 1950 sanaa ya kitalii ikawa sanaa ya kwenye viwanja vya ndege. Ili kukidhi haja ya ongezeko la mahitaji ya watalii, mtandao wa wachuuzi walioungana uliundwa, kwa mfano "Wasenegali" wa Afrika Magharibi na Kati. Ughushi wa kazi bora za kale ulienea kadiri watu wa tabaka la kati duniani walivyotamani sanaa za jadi.

Hata hivyo, sanaa ya kitalii iliendelezwa kwa njia mbili tofauti, kama ilivyoonekana katika kazi za Wakamba na Wamakonde wa Tanzania. Mchongaji wa Kikamba Mutisya Munge alitoa mtindo mpya kutoka kwa Wazaramo walio

karibu na Dar es Salaam na kupata soko la zawadi za Noeli kwa Wazungu ambao sasa walikuwa wanamiminika kwenye nyanda za juu za Kenya. Yeye na wenzake waliomwiga walichuuza bidhaa zao. Baada ya 1945 biashara ilishamiri kutokana na idadi kubwa ya askari wa Kiingereza waliowekwa Kenya. Soko la pili kubwa lilikuwa ni la Wamarekani, ambao sasa walihitaji maelfu ya vitu. Duka lililofunguliwa London mnamo 1935 tayari liliwatumia mawakala watano mnamo 1960 na ilipofika 1970 bidhaa zilizoingizwa Marekani zilikuwa na jumla ya vitu robo milioni kutoka Kenya,

Tanzania na Gambia[14]. "Majeshi" ya wapiganaji wa Kimasai na suala wenye aibu "walivamia" nchi za magharibi kila mwaka.

Kwa upande mwingine, wachongaji wa Kimakonde hawakuiga kamwe vitu vya wengine hadi karibuni[15]. Zaidi ya wachongaji mia moja walihama kutoka Msumbiji na wakafanya kazi karibu na Dar es Salaam tangu takriban 1964 na kuendelea, wakiuza bidhaa zao kupitia kwa madalali. Mmoja wao aliunda sanamu mpya ya uwakilishi wa "shetani" ambao uliweza kutoa maumbo mbalimbali mazuri. Kila moja ya sanamu hizo pia sifa za pekee, ilitengenezwa kwa ajili ya kuonyeshwa, na wachongaji waliielezea kuwa inaonyesha ubunifu wao.

Tofauti baina ya michongo ya Kikamba na ile ya Kimakonde zinaonyesha mawanda yote ya sanaa za kitalii. Baadhi ya vitu ni nakala hafifu za sanamu za kijadi, bali vingine ni kazi halisi za sanaa. Kwa kawaida sanaa za kitalii hutokana na sanaa za jadi na msukumo wa ubunifu. Mfano ni utoaji wa michoro midogo ya maisha ya kijijini, ambayo ilinunuliwa na watalii katika miaka ya 1930, na ambayo ilionyesha kumbukumbu ya wahamiaji wa mijini wa karibuni walioyakumbuka maisha ya vijijini yasiyo na utata. Wasanii walidai kuwa tabia yao ya kutoa nakala zisizo na idadi ilitokana na mahitajio ya kiuchumi.

## Sanaa pendwa

Kusini mwa Sahara, sanaa inayojulikana zaidi ni sanaa pendwa ya mijini inayoanza baada ya uhuru. Lakini baadhi ya sanaa pendwa zilianza mapema zaidi na mpaka baina ya sanaa za jadi na pendwa hauonekani vyema vijijini, kwa mfano makaburi yenye vinyago vya sarufi (Cote d' Ivoire, Akan, Mto Cross, Kongo)[16] au sanaa za

[14] M.W. Mount, 1973, uk. 55 na uk. 217, fn. 32.

[15] S.J. Ntiro, 1982, huaminika zaidi kuliko A.J. Stout, 1966. Tazama pia S. Littlefield-Kasfir, na E. Herold, 1983.

[16] K. Nicklin na J. Salmons, 1977; D.R. Rose year, 1984; S. Dornowitiz na R. Mandirola, 1984; P.S. Breidenbach na D.H. Ross, 1978; M. Gilbert, 1981; R.F. Thompson na J. cornet, 1981



*PICHA 20..3: Sanaa ya Makonde*

ukutani za vijiji vya Wandebele huko Transvaal[17]. Sanaa za ukutani zinapatikana pia katika sehemu za Afrika ya Kati na Mashariki. Zilipendwa na Wamisionari Uganda badala ya michoro ya mwili, ambayo hawakuikubali. Mazao mengine ya sanaa pendwa vijijini yamekuwa hasa kwenye madhabahu na makanisani.

Katika majiji, sanaa za ukutani huonekana kwenye kuta za ndani za nyumba, mabaa, michoro ya kuashiria na matangazo[8]. Nyumba za mjini za Wayoruba zina michoro ya sementi ya simba na vinyago vingine vya ujenzi kutoka miaka ya 1930 hadi 1950[19]. Aina pekee ya sanaa onwa pendwa ilikuwa ni mchanganyiko wa sanamu-michoro na vibandiko vya bendera kwa ajili ya vyama vya *asafo* vya miji ya Wafante huko Ghana.

[17] S. Priebatsch na N. Knight, 1979; E.A. Schneider, 1985; C.A.M. Vogel, 1985; T. Mattewz, 1979
[18] U. Beier, 1971; na O. Pritchett, 1979
[19] U. Beier, 1960

Hata hivyo, sanaa pendwa iliyojitokeza zaidi mijini ni ile ya kuchora kwenye turubai. Mada za kinchoro zilizoonyesha taswira za kisasa na zile za kihistoria, zilitumika. Aina hiyohiyo ya sanaa ya michoro iliendelezwa pia kwenye vibuyu, kazi za ufinyanzi na nguo, pamoja na michongo ya pembe za ndovu na mbao. Wachoraji wa awali kama vile Ibrayima Njoga wa Kameruni, A. Onabolu wa Nigeria au A. Labaki na wengine wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo walihamasishwa na kazi hizo za miaka ya 1920. Miaka ya 1930 ndipo michoro ya kukumbuka nyumbani iliyoonyesha fukwe, minazi, vijiji na mandhari za kawaida za miji ilipotokea pwani ya Atlantiki. Mnamo 1960 mtu bado angeweza kuona picha ya ngamia na mchungaji wake chini ya mbingu zenye nyota za Sahara kwenye ukuta wa nyumba ya Mmauritania huko Dakar, au picha kubwa ya tembo kwenye ukuta wa nyumba ya mtengeza saa huko Bujumbura, Burundi[20]. Wakazi wa miji walianza kununua picha za turubai, pamoja na picha za watu maarufu (marabu wa Senegali) au picha zao wenyewe katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mabadiliko ya kuvutia kwenye mada zilizoonyeshwa, yaliyohamasishwa na matukio ya mahali penyewe, yalitokea kwanza Kinshasa, kisha, Lubumbashi, baada ya uhuru, huko Nigeria baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na baadaye zaidi Ghana. Mada za kihistoria zilipendelewa zaidi. Ilipofika 1960 taswira ya kuvutia ya Mamy Wata (au mamba muntu), mwanamke mbembezi aliyeashiria ujusi na ungeushi, ilikuwa imeenea kutoka Ghana hadi Shaba. Mada mpya tata zilichanganywa mnamo 1960 zikionyesha mandhari hafifu ya kitasnia ya Lubumbashi. Mandhari kutoka zama zilizopita za machungu na makangaiko ya wakati ule zilielezea mawazo ya wakazi juu ya historia. Mawazo ya kujitambua kwa wanamji yalijitokeza zaidi.

Sanaa pendwa ya kidini iliendelea Ethiopia na utoaji wa picha takatifu, mandhari za kihistoria na nyaraka ndefu za kiganga. Picha za watu na mandhari zilirudiwarudiwa, lakini mara kwa mara utunzi mpya ulitokea, kama ule wa Mt. Yarid akifuatana na ndege. Yeye ndiye aliyeanzisha muziki mtakatifu nchini humo. Kwingineko Afrika ya kaskazini, kama ilivyostahiki katika mazingira ya Kiislamu, kazi zilizohamasishwa na dini hazikuwa nyingi. Kati yake, ni picha za Ka'ba huko Maka ambazo zilienea sana.[21]

Kutokana na kukua kwa miji na kutamakani kwa wahamiaji, umuhimu wa sanaa pendwa ya mijini uliongezeka kwa haraka. Kazi hizo zinawavutia zaidi

[20] G. Sandrart, 1953, Kielelezo uk. 7 (Bujumbura), katika tukio hili ni ukumbusho wa mnyama ambaye wakati huo alikuwa amekaribia kutoweka katika eneo hilo. J. Beinart, 1968 (Maputo, Johannesburg)

wanahistoria ya jamii, kwani zinaonyesha moja kwa moja mabadiliko ya nyakati tofauti kama yalivyochukuliwa na umma wa wanamiji.

## Sanaa ya kitaaluma

Ilipofika 1913, weledi wa sanaa onwa ya desturi ya Ulaya ulikwishaingizwa Misri kutokana na kuanzishwa kwa shule ya Sanaa Stadi Kairo. Wachoraji na wachongaji wa Misri walishiriki kwenye maendeleo yote ya sanaa ya Ulaya tangu wakati wa wasanii wa hisianafsi wa mwishoni mwa karne ya kumi na tisa hadi wasanii dhati na wasanii wa dhahania na pendwa wa miongo ya karibuni. Hata hivyo bado michoro ya Kimisri inatambulika kwa urahisi kwani mada zake nyingi na baadhi ya miundo yake inarudi kwenye jadi zake za zamani za Uislamu na hata ufirauni[2]. Kwingineko shule za sanaa stadi zilitokea baadaye sana, ya mapema zaidi labda ikiwa idara ya Chuo cha Makerere mnamo 1937. Kizazi cha wasanii wa 1935 - 60 kilifunzwa Ulaya au katika asasi za kitaaluma za ndani.

Mwafrika wa kwanza wa kusini mwa Sahara kujifunza sanaa Ulaya alifika mwishoni mwa miaka ya 1930, wa kwanza akiwa labda Oku Ampofo wa Ghana aliyefika Uingereza mwaka 1932. Kati ya waanzilishi walikuwemo pia Iba Ndiaye (Senegal), aliyekuwa Paris ilipofika 1948, Gerard Sekoto (Afrika Kusini) aliyekuwa Paris ilipofika 1947, Afewerk Tekle (Ethiopia) aliyekuwa London ilipofika 1948, Kofi Antubam (Ghana) aliyekuwa London ilipofika 1946, Ben Enwonwu (Nigeria) aliyekuwa London ilipofika 1944 na Viteix (Angola) aliyekuwa Ureno katika miaka ya 1950[23]. Kizazi hicho kilisaili dhima ya msanii. Iba Ndiaye alieleza haya kutokana na mwamko wao huo:


Kwa kweli wasanii wa michoro wa Kiafrika watafute jibu la swali hili wao wenyewe: Jinsi gani wabaki Waafrika au wawe Waafrika tena, japokuwa wanataka kuwa watu wa kisasa kwa dhati na wanajaribu kujieleza katika lugha onwa ya kiulimwengu* [24]

Hali hii inadhihirisha mtanziko wa msanii wa kitaaluma. Mvutano unaonekana dhahiri kwenye kazi zao, labda zaidi kwenye zile za Enwonwu ambaye mara nyingine hubadili mitindo kutoka kwenye ule wa kimataifa hadi wa "Benin ya kisasa" hata kwenye kazi ileile moja. Hali hiyo haijidhihirishi sana kwenye sanaahisi ya Sekoto

[21] G. Fisseha na W. Raung, 1985; D. Hecht, 1979.
[22] S. El. Mansury, 1984; G. Boctosr, 1969
[23] Kwa ujumla, tazama M.W. Mount, 1973, uk. 160-86 na passim; D. Mestre 1981.
*[25] I. Ndiaye, 1948, uk.8 kwa dondoo kama hili la Kofi Antubam la tangu mwaka 1961, tazama M.W. Mount, 1973, 1973, uk.5



Picha 20.4 Juu: Iba Ndiaye na Senegal, akiwa na mchoro wake mmojawapo; chini: Kofi Antubam wa Ghana, akiwa na moja ya sanamu



Picha Viteix wa Angola, akiwa na mojawapo ya picha zake

na ile ya wasanii wengine wa Afrika ya Kusini kwa kuwa matatizo ya jamii yenye viwanda ambayo walitokana nayo yalifanana na yale yaliyochochea sanaahisi ya Kijerumani.

Wasanii waliokuwa Ulaya wa miaka ya mwishoni mwa 1940 walikuwa ndio wasemeaji wa sanaa ya Kiafrika katika mikusanyiko ya awali ya wasanii huko Paris mnamo 1956 na huko Roma mwaka 1959. Warithi na wafuasi wao punde waliungana na wasanii waliofunzwa kwenye shule za nyumbani na hakuna aliyeanzisha mtindo huru kabisa wa usanii.

Maendeleo ya mwanzo baada ya Vita Vikuu vya Pili yaliwahusu wachoraji wa Ulaya, hasa wahalisia, ambao waliamini kuwa mbinu zingeweza kuhamishika bila kuathiri hata kidogo njia ya udhihirishaji wa hisia ya wanafunzi wao. Mchoraji wa Kifaransa alifungua shule Lubumbashi ilipofikia 1944, mwingine aliifungua shule moja Potopoto (Brazzaville) mnamo 1951 na Dakar mnamo 1961. Shule kama hizo zilianzishwa Maputo mnamo 1960, Harare mnamo 1961, Rorke's Drift, Afrika ya Kusini mnamo 1963 na Oshogbo, Nigeria, mnamo 1961.

Bila kujali maelezo ya waanzilishi wake, ni dhahiri kuwa shule hizo ziliathiri mitindo ya wanafunzi wake. Shule za Lubumbashi, Potopoto na Dakar zilitoa kazi zilizorembwa sana kwa kutumia rangi za ngegu na mchanganyiko, zikiakisi dhana za wakoloni juu ya jinsi sanaa pendwa inavyotakiwa iwe. Maendeleo ya huko Msumbiji na Harare, na hasa Nigeria, yalikuwa tofauti sana. Mchoraji wa kwanza kutoka Msumbiji, Valente Malangatana, aliyeathiriwa na shule ya kimapinduzi ya Kimeksika ya uchoraji wa ukutani, alitoa sanaa iliyotawaliwa na mandhari za kuvutia na matukio, aina ya mada ambazo zilitumiwa na wasanii wengi wa Afrika ya Kusini. Huko Harare uchongaji ulipendwa zaidi kuliko uchoraji na ulikaribia sana sanaa hisia ya Ujerumani.

Karakana ya Oshogbo kwa hakika ndiyo iliyofanikiwa kuliko nyingine zote. Ilitoa mitindo mbalimbali ya kuvutia na wasanii ambao bado wanajishughulisha hadi leo, wakihudumia soko la wageni au wadhamini wa kiserikali wa nyumbani. Wasanii wengi ni wachoraji, na wachache ni wachongaji, hali ambayo inastaajabisha kwani mila za Wayoruba zimeelemea zaidi kwenye uchongaji.

Tarikhi ya upanuzi wa asasi za kitaaluma zilizofundisha sanaa inakwenda sambamba na karakana zilizoanzishwa na wasanii. Chuo cha Makerere (1927) kilifuatiwa na vingine huko Kinshasa (1943), na Khartoum (1945). Baada ya hapo nchi nyingi zilifuatia mnamo miaka ya 1950 na 1960. Wasanii walijikimu kutokana na ada za kiserikali, na mauzo kwa wageni waliomiliki majumba ya maonyesho ambayo yalionyesha sanaa hizo. Hali hii ilibadilika polepole. Nigeria ilibidi ingojee

hadi 1962 kupata jumba lake la kwanza la maonyesho lililoendeshwa na wenyeji na hadi mwishoni mwa miaka ya 1970 kabla ya baadhi ya kazi zake za sanaa kununuliwa na wenyeji kwa bei za juu[25]. Na kwingineko kusini mwa Sahara hali ilikuwa mbaya zaidi.

Serikali za nchi huru zilitumia sanaa kwa umaarufu tu, lakini mara chache sana wasanii waliombwa kusanii kazi za propaganda, na wala hakukuwa na tatizo la uthibiti. Baadhi ya serikali ziliunga mkono wasanii waliotambuliwa rasmi kama vile Kofi Antubam huko Ghana, Afewerk Tekle katika Ethiopia ya Kifalme, Ben Enwonwu huko Nigeria au Liyolo huko Zaire. Hata hivyo mabadiliko bado yanaanza kutokea. Propaganda imekuwa na umuhimu mkubwa. Uhalisia wa ujamaa ungeweza kuwa itikadi rasmi katika baadhi ya nchi. Uhuru wa usanii unaendelea hadi leo, labda kwa sababu ya ukosefu wa welewa sanaa ya kitaaluma ndani ya jamii za Kiafrika, hata kati ya wasomi.

Sehemu kubwa ya sanaa ya kitaaluma imebakia kuwa hasa sehemu ya mkondo mkuu wa sanaa ya kimataifa, ingawa sanaa yakinifu na za kidhahania zimekuwa na wafuasi wachache kuliko sanaa-hisia. Pamoja na sanaa-hisia mpya ya Kiafrika, mtindo mkuu mwingine umekuwa ule wa ujadi mpya, uliosukumwa na utumiaji wa vifaa vya jadi, mara nyingine ukiwa katika kaida za kimtindo, mara nyingine katika dhamira zake. Katika sehemu za Afrika Kaskazini msisitizo wa mistari umebaki na umeelekea katika kaligrafia yenye kisasa na matumizi madogo sana ya maumbo na kuelekea zaidi kwenye sanaa dhahania.

Mielekeo hiyo mikuu si ya kubahatisha. Mwelekeo wa ujadi mpya uliandamana na kupenda Unegro na vuguvugu linayohusiana nao. Mitindo ya sanaa-hisi inahusiana sana na sanaa ya zamani ya Afrika, hasa uchongaji. Sanaa dhahania ina mizizi yake ya Kiafrika kwenye mapambo ya kijiometri au sanaa ya Kiislamu. Ni uyakinifu pekee ndio ulikuwa mpya kabisa. Hata huo vilevile uliakisi ruya juu ya miungu na pepo au ulijengwa kwenye utajiri wa ishara wa sanaa simulizi za ujadi na miviga ya Kiafrika. Wakati huohuo mitindo ya kimataifa ilikuwa na athari kubwa kwa mielekeo hiyo yote, kama ambavyo dhana za kimataifa kuhusu dhima ya msanii na msisitizo mkubwa juu ya ubinafsi na kuthamini sana uhuru wa sanaa ulivyokuwa.

## Sanaa za mwili

Mwili, mapambo na mavazi yake huonyesha ubinafsi pamoja na utambulishi wa makundi mbalimbali (hadhi au kabila) na aina ya tukio (kazi, sherehe, msiba na

[25] M. Crowder, 1978

kadhalika). Hivyo historia ya sanaa za mwili ina matumizi makubwa kwa wanahistoria, ambao kwao inaweza kuwa ni ishara mojawapo nyeti ya mabadiliko ya jamii na athari za kitamaduni[26]

Afrika ya asili imeshuhudia urembushaji anuwai wa mwili kwa kuchanja, kutia chale, kupaka rangi mwilini, mitindo ya nywele na utakataji, kwa mfano mchoro na ukeketaji, ambapo mwili ulibadiliwa, kwa muda mfupi au kwa kudumu. Vito na mavazi vilitimilisha wajihi. Tofauti za jinsia, umri, hadhi ya Kindoa na cheo katika jamii vilionyeshwa. Mitindo ilianzishwa na vikundi vya waali, waliojifanya mifano ya kuigwa ya mengine, maana sanaa ya jadi ya mwili ilikuwa ikibadilika wakati wote.

Ilipofika 1935 utawala wa kikoloni ulikuwa umekwisha kuwa na athari kubwa kwa kupendekeza kuachwa kwa sanaa nyingi za mwili kwa jina la ustaarabu. Michanjo ya michoro na chale zilionekana kuwa ni ushenzi, na hivyohivyo kukaa utupu, hasa kama mwili umechorwa[27]. Zaidi ya hayo, mapambo mengi yalizuiwazuiwa kwa kusingizia gharama, tabia nzuri za kazi au raha. Kusini mwa Sahara, misioni zilipendekeza mitindo ya nguo za heshima kwa wanawake, aina zote za kile kilichoitwa nguo za "Mama Hubbard" (sketi ndefu na blauzi za mikono mirefu)[28]. Wazungu walianzisha mitindo mbalimbali ya mavazi ya kiutawala: shati na kaptura, jaketi za safari, sare za watumishi na askari. Suti rasmi zilizovaliwa kwenye majiji ya hadhi ya juu ya Ulaya zilipendwa na Waafrika waliofuata maisha ya Kizungu na baadaye wanaume wa mijini na vijijini. Katika Afrika ya kaskazini na magharibi, na pia pwani ya mashariki, mavazi ya Kiislamu yalidumu. Mwafrika magharibi alinasa kwenye bubu lake huko Sahel au mavazi ya Kiyoruba huko pwani, Mmoroko alibaki na burnu lake, Msudani na jalaba na Mswahili na kanzu na kofia.

Ilipofika miaka ya 1930[29] Afrika ingeweza kugawanywa katika maeneo makuu matatu kwa kuangalia mavazi, na mgawanyo huo ni muhimu hadi leo. Afrika ya mashariki na kusini, suti rasmi za Kizungu zilianza kuchukua nafasi ya miigo ya

26 M. Cdrowder, 1978, uk. 142-5

27 E.C. Burt, 1984, uk. 60-3 na uk. 80, anataja uhamisho wa Sanaa hizi ulioshawishiwa na Wamisionari kuwa uchoraji wa kutani wakati wa Krismasi miongoni mwa Waluo.

28 Walijishughulisha zaidi na nguo za ndani "hasa" kiasi kwamba baadhi ya misionari waliuza nguo hizo hadi miaka ya mwishoni ya 1950

29 Yanayofuata yalikuwa na muda, kwa kuwa sikuona hata makala moja inayoonyesha ukuaji wa nguo nyakati kabla na baada ya uhuru

30 C.B. Steiner, 1985, uk. 91-110 ni ya msingi. Tazama pia J. Fourneau na L. Kravetz, 1954

sare za kijeshi kuwa nguo zenye hadhi. Kaptura, mashati au jaketi za safari zilianza kuwa nguo za kawaida za kazi, ingawa wakazi wa mjini walipendelea zaidi suruali na mchanganyiko wa kikoi na koti bado lilikuwa vazi la kawaida vijijini. Vikwembe vya wanawake vilipotea polepole na mahali pake pakachukuliwa na magauni ya kimisioni; vikwambe huko mijini vilianza kuhusishwa na mwenendo mbaya. Miongoni mwa wafugaji wa Afrika Mashariki, hasa Kenya na kusini mwa Sudani, sanaa za mwilini za jadi na kutovaa nguo au kuvaa kidogo mno bado kunaendelea miongoni mwa wanaume.

Huko pwani ya Afrika ya magharibi na ya Ikweta, mitindo ya Kizungu ya nguo za kike haikupendwa, na vikwembe vikabaki kuwa nguo za hadhi kubwa. Vikiwa vimetengenezwa hapohapo au vimeagizwa kutoka nje ya nchi, mitindo yake ilibidi ikubaliane na matakwa ya wenyeji na viwanda vya nguo vya Ulaya viliendelea kuzingatia matakwa ya wateja wake wa Kiafrika[30]. Mavazi ya kiume ya sherehe huko pwani ya Afrika ya magharibi hayakuathiriwa na mavazi ya Kizungu, lakini suti zilivaliwa na wataalamu, wasomi na makarani. Wakati huohuo huko Afrika ya Ikweta, suti zilivaliwa na watu wa tabaka la juu, ingawa haikuwa hivyo sana huko Zaire (Kongo) Magharibi. Wakati huo bubu lilishikilia hadhi yake huko Sahel na hata lilienea kuelekea kusini. Kwa ufupi, mitindo ya Kizungu haikupendwa sana huku kama ilivyopendwa Afrika Mashariki na Kusini.

Kwa jumla, Afrika kaskazini ilishikilia mavazi na mapambo yake ya mwili (kujipaka hina). Wanawake walivaa nguo za Kizungu mijini, lakini walizifunika na buibui, kama ambavyo suti rasmi zilivyovaliwa ndani ya bunu au hata jalaba pamoja na makubadhi na Wamoroko. Mavazi ya kazi ya Kizungu yalivaliwa na wanaume, hata hivyo, na huko Misri suti zilikwishakuwa nguo za kawaida kwa muda mrefu kwa watu wa tabaka la kati na la juu. Thamani ya mavazi inaonyeshwa vyema na ugomvi uliotokea kuhusu tarbushi huko Misri, aina ya kofia iliyoonekana kuwa ni ya kudhalilisha na wanaharakati mnamo 1935, lakini ikatetewa sana na wasomi. Siku hizi huvaliwa tu na wafanyabiashara wafuatao jadi.

Utaifa wa baada ya 1945 ulijionyesha kwa mavazi[31] Wataifa walipinga kutovaa nguo na mapambo ya kwenye ngozi kuliko hata Wazungu na walianzisha mavazi ya taifa. Nkrumah alianzisha mtindo wa vazi la taifa 1957 na wasomi wa Afrika Magharibi wakaiga. Nguo za sherehe za Kiyoruba, mitindo ya bubu ya Kano au Bamako[32] ikawa ni ishara ya utaifa. Matokeo yake, ufumaji, darizi na utiaji rangi

[31] Uhusiano wa kawaida kati ya utaifa na nguo umeelezwa vizuri na P. Bogaty rev, 1971.

Tazama pia A. Mazrui, 1970 (sio uchi wala vazi la kizungu).

wa wenyeji ulifufuliwa. Huko Zaire, Mobutu alilazimisha uvaaji wa abako kwa kupitisha sheria, akipiga marufuku suti na tai[33] *Abako* (ikiwa na maana ya "suti zii!") iliashiria usawa kama ulivyotiwa msukumo na vazi la Mao lakini, jinsi tofauti za matabaka zilivyoongezeka Kinshasa, na hivyohivyo ubora wa vitambaa na mishono viliakisi hadhi ya kijamii ya mvaaji.

Vikwembe vilienea tena Afrika ya Kati na ya Ikweta, mitindo na mishono ikiwa na madoido zaidi na kwa kutumia vitambaa ghali. Lakini Afrika ya mashariki na kusini wanawake wa tabaka la juu walipinga kurudi kwake mijini. Mitindo ya nguo za Kizungu ilikuzwa Nairobi zaidi kuliko Dakar[34]. Suti rasmi zilishinda, ingawa si kwa ukamilifu nchini Tanzania. Utaifa haukuonyeshwa sana kwa njia ya mavazi, bali kwa njia nyinginezo.

Huko Afrika ya Kaskazini, maendeleo makubwa yamekuwa katika kujaribu kurudisha buibui kwa wanawake wa mijini Misri[35] kama ishara ya kufuata msimamo mkali wa kidini. Huko Libya na Tunisia kumekuwa na ufufuaji wa vazi la taifa lililotokana na kanzu za mashehe za vijijini.

Hivyo mitindo ya nguo na mapambo iliyobuniwa na Wazungu ilikubaliwa tu na wachache katika kipindi hiki. Haja ya kusisitiza utambulisho wa kitaifa na baadaye hadhi ya kijamii iliacha alama katika historia ya mavazi.

## Muziki na dansi

Muziki wa sauti ulitawala katika sanaa pendwa katika kipindi chote vijijini na mijini, kwani viwanda vya santuri na redio vilihakikisha kuenea kwake kwa umma. Baadhi ya waimbaji walipata umaarufu mkubwa. Wengine walichangia katika mapambano ya uhuru kwa kuwahamasisha watu na kuwasifu viongozi.

Jadi ya muziki wa Afrika imeonyesha kuendelea licha ya shinikizo la nchi za nje. Uwezekano wa kuchanganyika ulikuwa ni mkubwa kutokana na kufanana kwa muziki wa Magharibi na ule wa Afrika Kusini mwa Sahara, ukihusisha matumizi ya "diatomic scale" na ulinganifu wa sauti, na pia tabia ya kuambatisha sauti na ngoma na magita. Licha ya hayo, muziki wa zamani na wa sasa wa Afrika bado una aina zilezile za mitindo ukiwemo mtazamo uleule kuhusu nidhamu ya kimlolongo, dhana ileile ya "mdundo", kani za viambaji, motifu za ridhimu na ufundi wa uimbaji.

33 F.S.B. Kazadi, 1978.

34 F. Court na M. M'Wangi, 1976.

35 J.A. Williams, 1979. Filamu nyingi za Misri hushughulikia suala hili.

Muziki wa ala wa Ulaya haukuwa na athari. Ingawa baadhi ya ala za Kizungu zilitumiwa kuandamana na sauti, hakuna mpiga ala maarufu wa Kiafrika aliyepiga muziki wa kimapokeo (wa Kimagharibi). Watungaji, isipokuwa kwa mmoja au wawili, walitunga muziki wa kanisani, muziki wa sauti, kuliko muziki wa okestra.

Historia ya muziki wa vizazi vya hivi karibuni ni lazima ipambanue maendeleo ya aina mbili tofauti, yale yanayofungamana na sehemu za mashambani na muziki mtakatifu, na yale ya muziki wa baa na kumbi za dansi za mijini, ambako muziki wa mjini uliundwa.

## Muziki wa vijijini na mtakatifu

Katika mwaka 1935 desturi za vijijini bado zilikuwa hazijaingiliwa, na uanuwai wa tungo zilizokuwepo ulianzia nyimbo za kuchombeza hadi za kuomboleza, kuanzia nyimbo za kazi hadi za ukinzani, kuanzia ushairi wa sifa hadi wa dhihaka. Nyimbo za ukinzani zilishamiri wakati wa ukoloni na baadaye kidogo. Baadhi ya nyimbo za ukinzani za Rwenzururu kutoka Uganda zilitumia muziki uliohusishwa na sherehe za kilabuni za hapo zamani, baadhi ya nyimbo za dini na za shule[36]. Athari za nyimbo maarufu za Kizungu zilikuwa na nguvu katika miaka ya 1940 na 1950. Mnamo miaka ya 1950 Wamangbetu wa Zaire waliupenda na mwimbaji wa Kifaransa Tino Rossi[37], na mnamo 1966 nyimbo za Rwenzururu zilikuwa na mahadhi ya *Alpenrosen*, wimbo mfupi wa kihisia wa zamani wa Ulaya ya Kati. Lakini nyimbo za vijijini pia zilibadilika. Katika maeneo mengine aina ya kizamani ya kihistoria ya tendi za kishujaa ilitumika katika kutunga nyimbo mpya za kihistoria. Hivyo mwimbaji mtembezi kipofu wa Kilulua alitunga wimbo unaoelezea historia ya sasa ya Kasai (Zaire) kuhusu machifu na mapepo wao wanaowalinda[38].

Muziki wa dini ulipata umaarufu sehemu ambazo Uislamu ulienea au kutokana na shughuli za kanisa[39] Hata kabla ya 1935, nyimbo za kumtukuza Mungu zilipendwa sana . Kwaya zilianzishwa shuleni, na ilipofikia miaka ya 1950 vikundi vilivyofanana na waimbaji wa Vienna vilionekana Afrika ya Kati, Mashariki na Kusini[40]. Wakatoliki walianza majaribio ya "misa za Kiafrika" tangu miaka ya

[36] P. Cooke na M. Doornbos, 1982

[37] *A. Scohy, 1955, uk. 113*

[38] T.K. Biaya, 1984

[39] H. Weman, 1960

[40] Tazama G. Haezon, 1960, kwa mifano kuanzia 1954 kuendelee, huko Shaba.

1930 na kuendelea[41] Misa zilitungwa na Waafrika, aghalabu wanaseminari na mapadri, mtindo uliofikia kilele chake kabla Baraza la Pili la Vatican la 1964 na matamko yake kuhusu lugha na vitendo vya ibada[42]. Baadaye mwelekeo huo ulipungua, ingawa utungaji wa nyimbo za dini bado ulikuwa na nguvu, kwani hulingana na ufufuaji wa imani ya kidini, uliodhihirika katika bara lote baada ya 1980. Hata hivyo, nyimbo za kumtukuza Mungu hazipendwi na wengi zikilinganishwa na muziki mpya pendwa wa mijini, ambao huathiri maeneo yote ya vijijini.

## Muziki wa mijini wa Afrika Kaskazini

Mnamo 1871 Aida ya Verdi ilionyeshwa kwa mara ya kwanza katika jumba jipya la Opera la Kairo. Hii ilikuwa ni hali halisi ya Misri, nchi pekee ya Afrika iliyoingiza muziki wa ala wa Kizungu. Afrika ya Kaskazini ilikuwa na jadi ya muda mrefu ya muziki wa ala, ambao bado, hata hivyo, ulihusishwa na uimbaji. Katika sehemu ya kwanza ya karne hii, hata hivyo, Sayyed Darwish alianzisha mtindo mpya wa muziki uliochanganya jadi za Ulaya na za Mashariki, ambao ulikuwa na mafanikio makubwa. Katika kujibu mtindo huo kundi la wanamuziki wa Algeria na Tunisia kilianzisha *Rachidiyya*, kikundi ambacho kilitaka kufufua jadi ya zamani ya okestra ya *ma'luf* na nyimbo zake za *nuba. Ma'luf* ikawa ndio ishara ya uhuru katika nchi hizo na Libya. Lakini walikiri uongozi wa Misri kwa kutumia ala za Kizungu, kuwa na kundi kubwa la wanamuziki jukwaani, na hata kuiga baadhi ya melodia na ridhimu.

Muziki wa Moroko, ambao ni mapokeo ya moja kwa moja ya muziki wa kisomi wa Kiarabu, umebaki kuwa wa jadi zaidi. Dafina yake ni pamoja na tarbia za *arubi* za wanawake wa Fez[43], nyimbo za tarika au *haddarat* zinazoimbwa kwa pamoja na wanawake harusini na kwenye sherehe za tohara, lakini zaidi ya hayo yote ni ushairi wa melhun.

Kama ilivyokuwa kwa Afrika ya kusini mwa Sahara, sauti ilibaki kuwa ndio ala kuu, na wasanii waimbaji ndio waliovuma. Wengine walipata umashuhuri wa makwao tu, kama vile Saliha, mwimbaji maarufu wa nyimbo za *ona* wa Badawi

[41] P. Jans, 1960. J.H. Kwabena Nketia 1957 humtaja Ephraim Amu, na kazi zake 1933 za Twenty-five African Songs katika mitindo ya Kiafrika, kama baba wa watunzi wa muziki mtakatifu.

[42] T. Tshibangu, 1960

[43] M. Wl Fasi, 1967. Makala za Kiarabu zilizochapishwa Fez, 1971



PICHA 20.6 Orchestra ya Moroko: ni Orchestra ya muziki wa Kiarabu-Kiandalusia

huko Tunisia, ambapo wengine umashuhuri wao ulienea katika nchi zote zinazozungumza Kiarabu. Mwimbaji mashuhuri kuliko wote katika karne hii alikuwa Umm Khulthum, ambaye alilipata jina lake kutokana na ushairi wa Kiarabu wa kabla ya Uislamu. Alianza uimbaji wake mnamo 1932 na wakati wa al-Nasser alifufua ari ya kurejelea ukuu wa kale wa Uislamu. Hakuna mpaka wa wazi baina ya muziki pendwa wa mijini na ule wa wasomi, hali ambayo inafanana na ile ya kusini mwa Sahara.

## Muziki wa mijini kusini mwa Sahara[44]

Muziki wa mijini ulianza kama kibwagizo cha ngoma katika miji mipya na kama muziki wa baa. Katika miaka ya mwanzo ya 1930, muziki huu uliandamana na ngoma za kienyeji kama ile ya *agbaya* ya Brazzaville na Kinshasa. Mashindano

[44] Sehemu hii imejikita kwenye mchango wa Kazadi wa Mukuna. Tazama pia Kazadi wa Mukuna, 1980



PICHA 20.7 *Mwimbaji Umm Khulthum, wakati akiimba mjini Paris mwaka 1967.*

ya ngoma na kuimba yalikuwa ni ya kawaida katika miji ya pwani ya Afrika Magharibi.

Ilipofikia 1940 mtindo wa aina tofauti wa muziki uliibuka: rumba ya Zaire. Iliifuatia haliaifu ya Ghana ambayo ilikuwa imechanua kufikia mwaka 1930. Matarumbeta yalitawala katika ala zake, na ilikuwa ya aina mbili; ya haraka na ya polepole, yaani *blues*. Hailaifu ikaja kuhusishwa na muziki wa mabwalo ya dansi na mtindo wa dansi wa kimagharibi, licha ya kuwa mdundo na melodia ilikuwa ni ya Kighana[45] Baada ya kilele chake katika miaka ya 1950 hailaifu ilianza kupungua umaarufu wake huko Nigeria na Sierra Leone kwenye miaka ya 1960, wakati mtindo wa Kilatino ulipochukua nafasi yake.

[45] J.H. Kwabena Nketia, 1957.

Gita lilifika Afrika Magharibi mnamo 1935 na lilitumiwa pamoja na ngoma katika mtindo wa muziki ambao kwanza uliitwa *juju* na halafu *miliki*. Muziki wa Kizaire uliathiri sana mtindo huo hadi ilipofikia takriban 1968, ulipoibuka mdundo wa *Afro*, ambao ulikuwa mchanganyiko wa hailaifu na muziki wa *soul* wa Waamerika wenye asili ya Kiafrika. Mdundo wa Afro unahusishwa na mwimbaji nyota wa nyimbo za upinzani Amikulapo Kuti Fela, msemaji wa tabaka la wafanyakazi.

Huko Zaire gita lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko kusini, ambapo lilichukua nafasi ya *likembe* kwa haraka, kwani halikuweza tena kutoa sauti tata zilizokuwa kwenye muziki mpya. Ilipofika 1946 gita lilikuwa limefika Kinshasa. Tukio hili liliambatana na kuingia kwa muziki wa Afro-Kubano. Kuundwa kwa African Jazz mwaka 1953, OK Jazz 1956 na kuendelezwa kwa nyimbo za kishairi katika Kilingala kuliko Kihispania, kulifanya muziki wa Zaire kuibuka kwa nguvu. Idadi ya bendi iliongezeka kutoka 19 mnamo 1960 hadi kufikia zaidi ya 200 mnamo 1984, zikisaidiwa kikamilifu na Umoja wa Wanamuziki. Maendeleo hayo hayakuweza kulinganishwa na mahali popote katika maeneo ya jirani, hivyo muziki wa Zaire ulisambaa kote Afrika ya Kati na pia sehemu nyingine za pwani ya mashariki na kufikia kusini hadi Zimbabwe, ingawa nyimbo za Kilingala hazikueleweka na wengi. Hata hivyo, huko Kinshasa, mada zilibadilika. Tungo za awali za mapenzi yasiyokamilika au beti za kukumbuka za maisha ya vijijini ziliongezewa hata kabla ya 1960 na nyimbo za siasa za kushangilia uhuru, nchi na mashujaa wake. Baada ya 1960 uhakiki wa masuala ya kijamii uliongezeka katika umuhimu wake na ulionyesha uchungu, na kusababisha matatizo kwa nyota mkuu wa muziki Luambo (Franco). Nyimbo za upinzani taratibu zilihamia Kameruni (Makosa)[46] na Gabon. Ilipofikia katikati ya miaka ya 1970 na hasa zaidi 1979, mitindo ilibadilika Kinshasa na kuanza kuakisi ukweli wa kijamii uliokuwepo. Mara nyingine nyimbo zilibaki kuwa ni za kilio cha moyoni zikiambatana na mtindo wa dansi wa vurugu na wa kisarakasi, wa kustaajabisha na wa kupagawa.

Maendeleo mengine makubwa katika muziki yalitokea Afrika ya kusini. *Marabi* ambayo ilianzia kwenye baa za siri za mijini iliathiriwa na muziki wa sauti nyingi wa Kinguni na jazi ya Amerika ya Kaskazini. Mabadiliko ya marabi yalianzisha *kwela*, kwanza Malawi halafu ilipofika miaka ya 1950 Afrika Kusini kwenyewe. Mtindo wa nyimbo uliotokea ulihitaji ustadi zaidi ya ule wa kawaida, na ulienezwa

[46] O. Debhonvapi, 1984, uk. 130; B.Ephoson, 1984; Anon, 1984; H. Kala-Lobe, 1982; C. Monga, 1983

kupitia santuri za Miriam Makeba[47]. Jazi pia iliathiri moja kwa moja muziki wa mjini wa Kenya. Miji ya Afrika Mashariki na ile ya Afrika Kusini iliathiriwa zaidi na vionjo vya Kizungu vilivyohusiana na mitindo ya Ulaya na Marekani kuliko kwingineko katika bara hili[48]

## Dansi

Katika kitabu chake cha *African Dances* [Dansi za Kiafrika] G. Gorer aliandika mnamo 1935 juu ya Afrika Magharibi:

> Wanacheza ngoma kwa furaha na wanacheza kwa msiba; wanacheza kwa mapenzi na wanacheza kwa chuki; wanacheza kuleta utajiri na wanacheza kuepusha mabalaa; wanacheza kwa ajili ya dini na wanacheza kupitisha muda[49]

Urithi mkubwa namna hiyo haupotei haraka, na dansi za Kizungu, za jamii au zile za kisanii, hazikuweza kufua dafu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kani ya sanaa hii, ambayo hata baada ya 1900, aina mpya ya bale ya jadi, *bobongo*, iliweza kukua katika sehemu za Zaire, licha ya ukoloni. Wahamiaji walileta ngoma zao mijini ambazo zilishamiri katika mazingira ya ushindani na vikundi vingine vya kikabila au maeneo. Ngoma hazikuzingatiwa sana na wakoloni mpaka miaka ya 1950, isipokuwa kwa ajili ya kupigwa marufuku, au kuwa kivutio katika maonyesho na kwa ajili ya mapokezi ya wageni mashuhuri. Hata hivyo, mwanzoni mwa miaka ya 1930 kikundi cha wacheza ngoma cha Wadogon kilipelekwa Paris. Kutokana na mwanzo kama huo, vikundi vya wacheza ngoma wa kulipwa vilianzishwa[50]. Katikati ya miaka ya 1950, Fodeba Keita alianzisha kikundi cha *ballets africains*, kwa nia ya kuunganisha ngoma na sanaa za maonyesho. Wakati huo maonyesho ya ngoma yalikuwa ni ya kawaida kwenye mabwalo, viwanjani na mahali pengine[5]

Lakini wakati huo mwelekeo mwingine, utaifa, ulikuwa unaendelea. Ngoma zilikuwa ni sehemu muhimu ya utaifa, ambapo hata Misri, ambako hakukuwa na jadi ya ngoma za vijijini, jadi hiyo ilianzishwa. Penginepo, nchi zote ziligeukia urithi wao wa ngoma kuanzisha vikundi mara baada ya uhuru.

[47] J. Gwanga na E.J. Miller, 1971

[48] Miongoni mwa Mangbetu. A. Schohy, 1955, uk. 113; P.J. Imperato, 1971

[49] Miongoni mwa Mangbetu. A. Schohy, 1955, uk. 113; P.J. Imperato, 1971.

[50] F. Keita, 1957. Hadi 1958 Zaire ilipeleka Bendi yake ya Kwanza "Changwe Yetu" kwenye maonyesho ya Kimataifa kule Brussels.



*PICHA 20.8 Bale ya Kiafrika [ballets africains]Fodeba Keita*

Ngoma za jadi katika mazingira yasiyo ya kijadi zilileta mabadiliko kadha. Kwanza ziliashiria mahusiano mapya na watazamaji, sasa yakiwa si ya kumwangalia mtu bali yaliyojali ada ya kiingilio. Vikomo vya jukwaa na muda vilibadili kabisa uratibu wa ngoma, na msimamo wa wachezaji kuhusiana na uchezaji wao. Matendo ya kustaajabisha kwenye ngoma yalisisitizwa, na mavazi na miondoko ilifanywa kulingana na viwango vya heshima vya mijini. Pia ratiba ilipangwa ili kusisitiza maonyesho ya aina mbalimbali na hivyo ngoma za watu tofauti na za aina tofauti zilichanganywa. Katika ratiba ya 1958 ya *Changwe yetu,* (Zaire) ngoma za vita ziliambatana na ngoma za msiba za eneo jingine, ngoma za mapanga na sarakasi ziliambatana na ngoma za usimikaji wa machifu. Tangu hapo kumekuwa na umoja zaidi wa kisanii.

Ngoma zimehusishwa na mtitiriko wa vitendo vya opera (Nigeria) au mtiririko wa vitendo vya sanaa ya maonyesho, na kuwa sehemu ya sanaa ya maonyesho au mfululizo wa ngoma huelekea katika hitimisho kubwa. Miondoko mipya kabisa ya dansi imetokea.

Wakati huohuo, ngoma za kuburudisha katika miji zimebadilika kidogo tu na ngoma za vijijini zimedumu, wakati mitindo ya dansi za mijini inapata mashiko vijijini. Hadi leo, uchezaji wa dansi umebakia kuwa ni shughuli inayopendwa sana na muziki umeendelea kuwa sanaa inayopendwa zaidi ya nyingine.

## Tamasha na Sanaa za maonyesho

Paredi, vichekesho, hata mazungumzo ya jukwaani ya wacheza ngoma waliojivisha vinyago vilikuwa ni vitu vya kawaida katika Afrika ya kabla ya ukoloni. Nyingi ya jadi hizo zimeendelea. Kuendelea huko mara nyingine hustaajabisha kama ilivyo kati ya maandamano ya sherehe ya Waakan yaliyoelezwa na Bowdich mnamo 1817 na maandamano ya Waakan leo, japokuwa kuna vitendo vingi vilivyofanywa kuwa vya kisasa[51] Ngoma tata za vinyago bado zipo pwani ya magharibi hasa, ziwe zile za jadi ya Sherehe ya Taa ya Sierra Leone au Gambia[54], paredi za *asafo* za Wafanti, mng'aro wa mabaraza ya Waakan, utitiri wa ngoma za majuso (vinyago) za Nigeria, au kanivali ya Luanda. Sherehe za maulidi huko Afrika Kaskazini na sikukuu za miji ya pwani ya Afrika ya Mashariki zimeendelea kuwa na shughuli za burudani.

Vijijini, sherehe za jando, zikichukuliwa kama sherehe kubwa, zilikuwa ni za kawaida mnamo 1935 na hata takriban 1950 wakati V. Turner alipochunguza sherehe za Wandembu, huko Zambia. Miongoni mwa matendo ya zamani ya kustaajabisha ni sherehe za Watsogho wa Gabon ambapo kupagawa ilikuwa ni njia ya kuwasiliana na mapepo. Shauku ya maonyesho bado ipo kila mahali.

Sanaa za maonyesho za jadi kwa maana finyu ya maigizo ya hadithi mbele ya watazamaji hazikuenea sana. Lakini bado maonyesho kama hayo yalifanywa sehemu mbalimbali tangu Mali hadi Mito Panda na Kongo/Zaire. Watawala wa kikoloni walikasirishwa na maonyesho hayo, hadi thamani yake ilipoonekana kwa watalii, baada ya Vita Vikuu vya Pili.

[51] H. Cole, 1975.

[54] Angalia toleo maalum la **Sanaa za Kiafrika,** Juz. 6 Na. 4, 1973 na Juz. 11 Na.3. 1978; pia N. Nzewunwa, 1982; na maelezo mengi katika **Nigeria Magazine**

Baada ya uhuru baadhi ya viongozi walianza kutumia matamasha ya kizamani kuleta shamrashamra katika mikutano ya kisiasa na kwa ajili ya kuzindua miito ya kisasa. Inavyojulikana hadi sasa, mtindo huo ulianzia Guinea kabla ya 1965, kwa kuhamasishwa na mayeli, kisha matumizi ya vikaragosi yaliingizwa Zaire mnamo 1967-70.

## Sanaa za maonyesho

Sanaa za maonyesho halisi, au kuigiza mtiririko wa vitendo jukwaani, aghalabu kwa kufuata desturi za majukwaa za Italia, kukiwa na matini iliyokaririwa kwa ghibu na mara nyingi ikiwa ya lugha ya Ulaya, ni uvumbuzi wa kimji ulio dhahiri[53]. Fani hiyo ilianza kwanza katika misioni na shule, aghalabu ukiwa mchezo wa igizo moja, ukitumiwa kwa ajili ya mafunzo. Mafunzo ya Biblia na maadili, mara nyingi yakiwa na dhihaka, yalitumiwa sana, kwani haikusahaulika kuwa sanaa za maonyesho ni lazima ziburudishe wakati zinafundisha. Maendeleo ya sanaa za maonyesho yalichukua njia tofauti katika maeneo ya Afrika Magharibi, kutegemea kama maeneo hayo yalikuwa chini ya himaya ya Wafaransa au ya Waingereza.

Hali katika Afrika ya Kaskazini ilikuwa tofauti. Huko Misri, sanaa za maonyesho zilishamiri mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Katika miaka ya 1930, sanaa nyingi za maonyesho zilitumia Kiarabu cha mazungumzo. Vichekesho vingi na michezo ya maadili ilitungwa, japo Tawfik al-Hakim na wengine walitunga pia michezo iliyosisitiza matatizo ya kiulimwengu. Ilipofika katikati ya miaka ya 1950 na wakati wa al-Nasser michezo iliakisi maisha ya kijamii, uhalisia lakini pia ilikuwa ya kiishara. Ilipofika 1964, kulikuwa na majumba ya maonyesho tisa au kumi Kairo yaliyoonyesha michezo ya zamani au ya kisasa ya Kiarabu, vichekesho na opera za Kimisri. Hadhira ilifurahia michezo ya uhalisia kama ile ya Yusuf Idris na ile ya kiishara iliyotoa ujumbe wa kimapinduzi, kama ile ya Nu'man Ashur. Tangu hapo mielekeo ya sanaa za maonyesho ya Misri ya kupiga chuku, vichekesho, uhalisia na ya kuashiria iliendelea.

Libya, Tunisia na Algeria zilishiriki katika jadi ya sanaa za maonyesho ya vikaragosi, *Karaguz*, iliyotokea Uturuki. Lakini sanaa hiyo haikuwa na athari wakati wa ukoloni. Maonyesho hayo yaliwaudhi maulama kuhusiana na maadili. Michezo ilionyeshwa hasa kwa Kifaransa na Kiitaliano kwa ajili ya jumuiya za wageni na baadhi ya wasomi. Kabla ya uhuru wa Tunisia na Moroko, michezo mingi ilitafsiriwa

[53] Marejeo ya hivi karibuni yanaweza kupatikana katika Rechercho, Pedagogie et Culture, Juz. 69, 1983, uk. 171; Anon, 1971; R. Mshengu-Kavanagh, 1979, na 1981; M. Schipper, 1982

kutoka lugha za Kizungu kwenda Kiarabu sanifu au cha mazungumzo. Ilipofika mwishoni mwa miaka ya 1960 umma wa wanamiji wa Maghreb kwa jumla walianza kuipenda . Idadi ya vikundi ilianza kuongezeka; michezo ya redio na televisheni ilihitaji maandishi. Na hivyo sanaa ya maonyesho ya kisasa ilianza kukua, hasa katika michezo ya igizo moja, dhihaka au chuku, isipokuwa Algeria ambako dhamira kuu ilikuwa ile ya vita vya uhuru.

Katika nchi za Afrika Magharibi zilizozungumza Kifaransa sanaa za maonyesho za kitaaluma ilianza mnamo miaka ya 1950, kutokana na juhudi ya wanafunzi wa Shule ya William Ponty ya Dakar, ambao walishawishiwa kufanya uchunguzi wa sanaa jadi ya Uhakiki wenye kupinga ukoloni, migongano baina ya wazee na vijana na mwelekeo wa kidhihaka ndio ilikuwa chapa ya tungo hizo. Michezo mingi ilifuata na kanuni zilizopo za sanaa za maonyesho za Ulaya, isipokuwa mazungumzo yalikuwa ya papo kwa papo, lakini michezo ilivyozidi kuwa mirefu sifa hiyo iliachwa..

Waandishi wachache wa tamthiliya kama vile Cheik N'Dao aliyetunga *L'Exil d'Albouri* mnamo 1969 aliingiza ushairi, nyimbo na ngoma akilenga katika sanaa ya maonyesho iliyokamilika. Wengi walifuata mageuzi kama hayo. Bernard Dadié wa Côte dIvolre ni mfano halisi, aliendelea kuandika kwa namna hiyohiyo mnamo miaka ya 1970 kama ilivyokuwa kwa tamthiliya yake ya awali, Assemien Débylé, iliyoonyeshwa Paris mnamo 1937[54]

Baada ya uhuru mkusanyiko wa kawaida wa maonyesho ulitajirishwa na michezo ya propaganda, ambayo ilikubaliwa tu ilipokuwa ya vichekesho[55]. Sanaa za maonyesho hazikupendwa sana kwa kawaida, kutokana na tatizo la lugha kwa upande mmoja, japo waandishi waliandika kwa lugha za Kiafrika. Sababu kubwa zaidi ni kwamba kanuni za sanaa za maonyesho zilikuwa za kigeni mno kwa hadhira ya Kiafrika.

Hata hivyo, mapema 1947, Fodeba Keita[56] alikwishajaribu kujitoa katika kanuni hizo. Ngoma na kwaya ziliambatana na vitendo na zilielezea kile kilichosemwa na mhusika mkuu, zikifuata taratibu za Kimande (Kimalinké) na Kiyunani za zamani. Lakini ngoma na shani vilihinikiza utajiri na utata wa mtiririko. Zaidi ya hayo, bale za namna hiyo ziliwalenga zaidi watazamaji wa ughaibuni kuliko wale wa uenyejini. Na hivyo sanaa za maonyesho na bale zilijikuta zikijitenga na utamaduni wa wananchi wenyewe wa Afrika ya Magharibi iliyozungumza Kifaransa.

[54] B. Traore, 1969; W. Zimmer, 1985
[55] N.S. Hopkins, 1971
[56] F. Keita, 1957, P. Paricy, 1971, uk. 54-6

Wakati huohuo sanaa za maonyesho zilikuwa zimeendelea kwa njia tofauti katika makoloni ya awali ya Waingereza Afrika Magharibi. Katika miaka ya 1920 sanaa za maonyesho za mchanganyiko kwa Kiingereza na lugha za wenyeji zilishamiri huko Ghana, zikifuatiwa katika miaka ya 1930 na sanaa za maonyesho zilizohamasishwa na mitindo ya Ulaya lakini zilizotumia lugha za wenyeji, mafanikio ya kwanza yakiwa mchezo wa F.K. Fiawoo ulioandikwa kwa Kiewe[57]. Jadi zote mbili, ile ya sanaa mchanganyiko na ile ya kitaaluma, zilipata mafanikio makubwa.

Mtindo wa sanaa mchanganyiko ulikuzwa na H. Ogunde, ambaye alitunga mchezo wa kimuziki kwa Kiyoruba, uliotokana na muziki na ngoma, na kuachia maneno yaongezwe. Kwa njia hiyo jadi ya opera ya Afrika Magharibi ilianza. Ogunde alioanisha maonyesho ya jadi na mazungumzo, matumizi ya jukwaa na vipengele vingine vya jadi ya sanaa ya maonyesho mchanganyiko.

Kwa upande wa taaluma, W. Soyinka aliibuka. Alifunzwa London, na nyumbani Nigeria mwaka 1959, alitunga michezo ya kwanza ya kitaaluma kikweli. Alizoea mbinu za Kizungu na kuzioanisha na vipengele vya maonyesho vya Kiyoruba katika michezo yake. Mfano wake ulifuatwa na waandishi wengine wenye vipaji kama vile J.P. Clark[58].

Wakati huohuo huko Ghana, E.T. Sutherland mwaka 1961 alitunga fani mpya ambayo kwanza iliitwa ya kimuziki na baadaye opera. Ilikuwa ni ya maigizo-bubu ya wachezaji, yakiambatana na kwaya na waimbaji. Michezo ilikuwa ni ya Kifante kukiwa na mwelezaji wa Kiingereza[59]. Lakini opera ilijidhihirisha katika Afrika na tungo za Duro Lapido, ambaye alitoa kazi yake ya kwanza mnamo 1961 katika kituo cha sanaa cha Oshbogo. Kuanzia 1962 hadi 1964 alitunga michezo kadhaa juu ya wafalme wa kihistoria wa Oyo ambayo ilianzisha mtindo mkuu wa opera ya Kiyoruba.

Tangu miaka ya 1960 fani na maudhui hayakukubalika sana. Msukumo ulitokana hasa na mapokezi simulizi, lakini michezo iliangalia pia hali iliyokuwepo wakati ule. Kutoridhika mara nyingi kulionyeshwa kwa dhihaka. Baadhi ya waandishi wakuu wa tamthiliya kama Soyinka waligeukia katika kukata tamaa badala ya dhihaka. Feni Osofisan, mwandishi aliyejulikana sana na vijana, aligeukia zaidi michezo ya siasa ya kimapinduzi. Lakini japo walimpinga Soyinka, yeye na

57 Kujibu mashindano yaliyotayarishwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kiafrika [International African Institute]

58 O. Ogunba, 1966, O. Obumba na A. Irele, 1978; Y. Ogunbiyi, 1981; M. Etherton, 1982; A. Ricard, 1975

59 K. Muhindi, 1985; S. Acquaye, 1971; O. Chinyere, 1980.

wenzake walifuata kwa karibu lugha, muundo na mada za Soyinka[60]

Katika Afrika Mashariki sanaa ya maonyesho ilikua polepole zaidi. Kitovu chake kilikuwa Chuo cha Makerere mnamo miaka ya 1960. Kutokana na watu kutopenda michezo ya Kiingereza, lugha za wenyeji kama vile Kiswahili na Kiganda zilitumiwa, na baadaye Kiluo na Kikikuyu pia. Mtindo wa michezo ya igizo moja ulivukwa na Ngugi tu mnamo 1966. Udhibiti ulikuwa ınkali wakati mwingine huko Uganda, lakini ulikuwa tatizo hata katika nchi nyingine pia.

Ubaguzi wa rangi huko Afrika Kusini unaweza kuwa ndiyo sababu ya kudumaa sanaa ya maonyesho kwa ajili ya watazamaji wa Kiafrika. Kazi za Mphalele zilikuwa ni kwa ajili ya kusoma kuliko kuchezwa jukwaani.Sanaa za maonyesho za Kiafrika zilipata mwanya kutokana na kuonyeshwa kwa King Kong mnamo 1959 na kikundi cha Chuo Kikuu cha Witwatersrand. Wakati huohuo, hata hivyo, Gibson Kente alianza kutunga michezo iliyopendwa zaidi. Sanaa hii ya vitongojini ilionyeshwa katika mabwalo ya jumuiya na ililenga katika kuburudisha tangu 1958 na kuendelea hadi mwishoni mwa miaka ya 1960. Mwishoni mwa miaka ya 1970. Thieta ya umma ya majaribio na vikundi vingine vilianza kuonyesha michezo ya kisiasa iliyoandikwa na Credo Mutwa na wenzake. Aina hii ya tamthiliya ilishamiri hadi wakati wa ghasia za Soweto, licha ya kukandamizwa ambako kulifanya michezo itungwe bila kuwepo matini iliyoandikwa kuepuka udhibiti. Mpaka hivi karibuni[61] hali ya kisiasa imezuia kukua kwa aina nyingine ya sanaa ya maonyesho zaidi ya ile ya masuala ya kisiasa.

Sanaa za maonyesho za Kizungu hazikukubaliwa kwa urahisi Afrika kutokana na kanuni, tabia yake ya kuwa ya kimaandishi na kutowashirikisha watazamaji. Lakini zilipovunja kanuni zake, kuingiza vionjo vya wenyeji, kutumia lugha ya wenyeji na kuruhusu ushiriki wa watazamaji japo kidogo tu, sanaa za maonyesho zilipendwa. Mara nyingine michezo ilikuwa ni vichekesho vya kimuziki tu vikiwa na maudhui kidogo, lakini tungo pendwa ziliweza kufikia kiwango cha juu cha ubora wa tamthiliya na fasihi, kwa mfano sanaa za maonyesho na opera za Nigeria.

## Sinema na televisheni

Redio, televisheni na kwa kiwango kidogo, sinema ni mawasiliano ambayo tabia yake ilikaribia ile ya aina za zamani za mapokezi simulizi. Sinema ndio zilianza: Filamu za kigeni zilionyeshwa Misri tangu takriban 1905 na kusini mwa Sahara

[60] C. Dunton.

[61] M. Hommel, 1962, toleo maalum. Theatre Quarterly, Juz.7, 1977-8; M. Mabogoane, 1983

kuanzia miaka ya 1920, katika majumba machache ya sinema yaliyokuwapo mijini na pia kwa njia ya maonyesho yaliyosafirishwa kwenye maeneo ya vijijini. Tangu mwanzo, sinema zilipokelewa vyema, hata kama umma haukuzielewa vizuri. Hii ilisababisha kutungwa kwa kiasi kikubwa cha filamu, zote zikiwa za kuelimisha, zilizolenga hadhira ya umma wa Kiafrika lakini zikiwa zimepigwa na wageni.

Redio zilianza hasa miaka ya 1930 lakini zimekuwa tu chombo cha umma halisia tangu 1960 na kuendelea tu wakati redio rahisi za transista zilipofurika barani. Zilibakia chini ya serikali na zilianza kuchukua dhima yake kuu ya kuelekeza mawazo ya umma katika miaka ya kuelekea uhuru.

Televisheni zilianza kwa kurusha matangazo huko Ibadan mnamo 1959, ikifuatiwa na Kairo mwaka mmoja baadaye. Chombo hiki kilienea polepole zaidi kwa sababu ya gharama za uanzishaji wake katika miundombinu. Aidha vyombo vyenyewe vilikuwa ghali. Hata hivyo, ilipofikia 1985 karibu nchi zote za Afrika zilikuwa zimekwishaanzisha mtandao wa televisheni na walikuwa wakijaribu kufikia nchi nzima.

## Sinema

Filamu ya kwanza kabisa iliyopigwa inaweza kuwa *Ghézal, Msichana wa Carthage* (1924), toleo la Kitunisia, ikifuatiwa mara na *Leila* na *Zainab* ya Misri mnamo 1926. Hizi zilipata msukumo wake kutokana na mtindo wa sanaa za maonyesho, lakini punde tu kanuni hizo zilivunjwa. Studio za Misri zilifunguliwa 1934 na tasnia hiyo ikaanza. Hali hiyo ni tofauti sana na ilivyokuwa kwenye makoloni. Sababu za kisiasa na kifedha zinaelezea kwa nini katika nchi nyingi waongozaji wa filamu walianza kutokea tu katika miaka ya 1970.

Utoaji wa filamu ni biashara. Inahitaji kiasi kikubwa cha mtaji kwa ajili ya utoaji, uundaji wa mtandao wa usambazaji na kwa ajili ya ujenzi au urekebishaji wa majumba ya sinema. Ni Misri pekee wameweza kujenga tasnia inayojitegemea; katika nchi nyingine serikali zimebidi kutoa fedha ili kuanzisha tasnia ya filamu. Tasnia ndogo imeundwa huko Nigeria na Moroko, na Senegali iliweza kuanzisha mtandao wa usambazaji baada ya 1969 na kujenga majumba ya sinema na sasa inaelekea katika kujitosheleza. Huko Algeria, Tunisia, Mali na Burkina Faso, serikali zimefadhili filamu za propaganda na za elimu lakini si filamu ndefu za hadithi.

Serikali nyingi zilisita kuwekeza sana katika tasnia hii kwa sababu, tofauti na imani ya wengi, filamu si chombo cha habari cha umma. Hailingani na redio au televisheni, ambavyo kwa hivyo vimekuwa vikipewa aula wakati wote. Wakati Upper Volta (sasa Burkina Faso) ilipovunja umiliki wa wasambazaji wa nje mnamo

1969, kulikuwa na majumba tisa tu ya sinema nchini. Gabon ilikuwa na majumba manane tu. Senegali leo ndio yenye miundombinu mizuri zaidi katika Afrika ya Tropiki na ina majumba ya sinema 80 na watazamaji milioni 13 kwa mwaka. Filamu ya Sheikh-Umar Sissoko, *Nyamaton* iliyoonyeshwa katika tamasha la filamu la Wagadugu la 1986 ilikuwa ya mafanikio makubwa, ikivutia watazamaji 35,000 katika kipindi cha wiki mbili. Ikilinganishwa na watazamaji wa televisheni wa kila siku, idadi hiyo ni ndogo sana[62]

Sinema huleta ushindani usioisha. India, Misri, Ufaransa, Uingereza na Marekani zote zinatafuta mgawo wa soko na serikali za kitaifa ni lazima zilinde maslahi yao pamoja na kuunda sera za utamaduni zao wenyewe. Uchaguzi wa umma unahusika na kuonyeshwa sana kwa filamu za India na Misri katika Afrika ya Tropiki. Moja ya tano ya soko lililobaki ndio eneo la mashindano ya nchi za Magharibi. Ufaransa na Marekani ndio wanaoongoza, lakini katika miaka 1980, washiriki wengine wa kigeni, hasa Kuba na nchi za Amerika ya Kilani pia ziliingia[6].

Tunapoijadili filamu kama fani mojawapo ya sanaa ni muhimu kuzingatia yote yanayotawala tasnia hii ikiwa ni pamoja na uwezekano wa udhibiti, kwani huathiri sana kazi za watengeneza filamu. Leo hii Afrika ina zaidi ya watoa filamu 250 waishio na kufanya kazi katika nchi 40 tofauti. Uchambuzi utahusu vituo vikuu vya uzalishaji tu.

Sinema ya kwanza ya Misri ilikuwa ya mapenzi na iliwapendeza watu wa mijini wa tabaka la kati. Mnamo 1939 filamu za uhalisia wa kisasa zilionyeshwa pamoja na za muziki na chuku. Vita vikuu vya pili vilisababisha sinema kuwa biashara yenye mafao makubwa, lakini maudhui yalikuwa hafifu na ya kukimbia ukweli. Mnamo miaka ya 1950 filamu za vita, za upelelezi, za sanaa ya jadi na zenye kuhuisha sinema za matukio ya kweli ziliibuka. Katika miaka ya 1960 uhalisia ulioathiri watu wengi uliendelezwa, masuala ya wakati uliopo kama vile midahalo kuhusu hadhi ya wanawake yakawa ni mada za filamu, na maigizo ya kazi mashuhuri za fasihi yalifanywa. Wahakiki mara nyingi hushutumu filamu za Misri kwa kutokuwa za kina na kuwa na muundo rahisi, lakini umma unazipenda. Kila mwaka tasnia hiyo hutoa idadi ya filamu ambayo inalingana na idadi iliyotolewa na Afrika ya Tropiki kwa kipindi cha robo ya karne.

Huko Maghreb[64] vituo vya wastani viliibuka huko Algiers na Moroko. Serikali ya Algeria iliamua tangu mwanzo kutoa ruzuku kwa ajili ya kutoa filamu za propa-

[62] M. Diawara, 1986 na 1987; P. Michaud, 1986
[63] M. Shirazi, 1987
[64] M. Berrah et al, 1981; G. Hunnebelle, 1972, uk. 105-94

ganda juu ya vita vya uhuru na juu ya dola ya ujamaa, hata hivyo hawajaweza kuzuia ukosoaji wa urasimu wao katika matoleo ya hivi karibuni. Moroko ilitoa filamu za kibiashara na filamu za kitaaluma. Zile ambazo zinajulikana zaidi ni za kuashiria na zinafanana na za Bunuel.

Nchi za Afrika Magharibi zinazozungumza Kifaransa zilianza kujaribu kutoa filamu mnamo miaka ya 1950, kwanza Paris, kisha Dakar[65]. Filamu ya kwanza ndefu ya hadithi ilikuwa *La Noire de...* ya Usmani Sembene ya 1966. Sembene ametawala utoaji wa filamu katika Afrika izungumzayo Kifaransa kwa muda mrefu na ni mwongozaji pekee wa filamu aliyepata ruzuku ya fedha kwa ajili ya filamu zake. Alianzisha jadi ya kitaaluma. Filamu zake zinaonyesha mgongano kati ya wakoloni au maisha ya Kizungu na hali halisi ya Kiafrika, kukiwa na mivutano baina ya matabaka ya kijamii. Mashujaa wa kabla ya ukoloni husifiwa, kama ilivyokuwa katika filamu yake yenye sehemu sita ya *Samory*, ambayo ni utendi wa televisheni.

Licha ya upungufu wa msaada wa kifedha, kiasi cha waongoza filamu mia mbili wamejitokeza katika Afrika izungumzayo Kifaransa. Matoleo yao mengi ni ya mafunzo na ya kitaaluma na watu hawayapendi mengi kati yao. Lakini baadhi ya watoaji wa filamu kama vile Suleimani Cissé au Sheikh Umar Sissoko wamevuka sifa za Sembene. Hali ya kishairi ya filamu za Cissé imemletea sifa wakati *Nyamaton* ya Sissoko, ambayo nusu ni kumbukumbu, na nusu ni hadithi ya kubuni, ilikuwa ya mafanikio makubwa. Watu walipenda kuona jamii waliyoifahamu, na zaidi kwa sababu lugha iliyotumiwa ni Kibamana. Hadithi za upelelezi za Kameruni ni aina ya kisasa zaidi, iliyofuata vionjo vya watu.

Huko Nigeria sinema zilifuata jadi ya sanaa za maonyesho za Kiyoruba na zilitumia miundombinu yake ya kifedha. Filamu ndefu za hadithi zilianza katokea mnamo 1972 tu, mwaka ambao mchezo wa W. Soyinka ulipigwa filamu. Nigeria imetoa filamu moja ndefu ya hadithi kila mwaka tangu 1975, licha ya kuwa sinema hazipewi ruzuku.

Filamu zinazotumia matukio yaliyobuniwa na Waafrika katika Afrika Kusini zinaanzia 1975. Zinashindana na filamu zinazotengenezwa kwa ajili ya watazamaji wa Kizungu pamoja na zile zinazotengenezwa na serikali kwa ajili ya "Wabantu", na zinadhibitiwa. Filamu ya kwanza ya Kizulu ilikuwa *Ikati elimnyama* "Paka mweusi". Muhimu zaidi ilikuwa ni utoaji wa filamu za siri za kumbukumbu na za

[68] Filamu ya P.S. Vieyra iitwayo **Afrique-sur-Seine** inajulikana kuwa filamu ya kwanza ijapokuwa jambo hili linapingwa na V. Bachy, 1983, katika J. Binet uk. 24

matukio yaliyohusu ubaguzi wa rangi. Lakini ni dhahiri kwamba filamu za Kiafrika hazijashamiri[66]

Umma wa kawaida umepokea filamu vyema zaidi kuliko sanaa za maonyesho. Lakini mafanikio ya filamu za Kiafrika yakilinganishwa na yale ya filamu kutoka nje, hasa filamu za Kihindi na za Kimisri, yanaonyesha ukweli kuwa watengenezaji wa filamu wa Kiafrika, wanaolenga kufundisha, wamesahau kuburudisha. Shauku ya filamu hizo imekuwa juu ya siasa, maadili na elimu; zinaonyesha matatizo ya utambulishi au ni za kitamaduni mno. Umma unataka hadithi na unapenda mno tungo za upelelezi, vituko vya ujasiri, ulimbwende na vitendo vya ushujaa. Na ni sasa ndipo baadhi ya waongozaji wamefahamu matakwa hayo.

## Televisheni

Televisheni ilifika Kameruni na Burundi mnamo 1984, baadaye zaidi kuliko nchi nyingi. T.M. Azonga ameeleza jinsi chombo hiki kilivyoonwa na watazamaji: Sasa wangeweza kuwaona watu wao wawapendao, kugundua nchi yao na matukio ya sasa, kuona dunia ikijifunua mbele yao. Haistaajabishi kuona kuwa televisheni iliipita redio kwa umaarufu na kwamba watazamaji walikuwa tayari kutumia pesa nyingi ili kuipata. Ilipofika 1986, seti 50,000 zilikuwa zimenunuliwa Kameruni. Katika nchi ya jirani ya Gabon, mtu mmoja kati ya kila watu kumi na mbili alikuwa na televisheni na huko Nigeria mtu mmoja kati ya kila watu watano alitazama telegvisheni kila siku.

Mafanikio hayo yasingeweza kudharauliwa na Serikali. Walijifunza juu ya nguvu hii kutoka televisheni ya Nigeria ambayo ilianza 1959[67], na kutoka Kairo ambako ilianza 1960. Televisheni iliruhusu serikali kuonyesha matukio na hivyo mara nyingi ilishawishi zaidi kuliko redio au chombo kingine cha habari. Serikali ingeweza kuelekeza maudhui ya utaifa na kujenga utamaduni wa taifa. Nchi nyingi zimejaribu pia kuathiri watu wa nchi jirani nje ya mipaka yao. Mtu anaweza kuelewa kwa nini serikali zilikuwa tayari kutumia fedha nyingi juu ya miundombinu ya televisheni. Jinsi nchi ilivyokuwa tajiri ndivyo zilivyokuwa na miradi mikubwa ya mtandao. Si kwamba tu Gabon imepanua idhaa zake mbili za rangi ili kuweza kufikisha matangazo kote katika nchi hiyo isiyo na watu wengi, inajenga pia satelaiti ili kuweza kupeleka matangazo yake katika sehemu kubwa ya Afrika ya kati. Hivyo

[66] M. Pheto, 1981; T. Keya, 1981

[67] O. Ikime, 1979, S. Olusola, 1979

inashindana na Kongo ambayo nayo inadhamiria kuwa na satelaiti yake yenyewe[68]

Lakini televisheni inahitaji kuwa na vipindi vingi: saa moja kwa siku ya habari na matukio ya wakati huo, vipindi vya watoto, kumbukumbu, ambazo aghalabu huhusu maendeleo vijijini, filamu zinazoendelea kwa muda mrefu na vichekesho, bila kusahau vipindi vya michezo na kuonyesha sherehe za kitaifa. Mahitaji ni makubwa na gharama za uendeshaji huweza kuwa kubwa mno kama vipindi vyote vitakuwa ni vya asili. Hivyo vituo huweka filamu za zamani na hukodisha haki ya kuonyesha filamu za muda mrefu za kigeni, kwa hiyo kuingiza upya chanzo muhimu cha mkengeuko wa kitamaduni.

Je televisheni ni sanaa ya asili? Ilianzisha tanzu mpya kabisa: filamu mfulizo (inayoendelea kwa muda mrefu,) ambayo kwa kulinganisha na filamu ya kawaida, uhusiano wao ni sawa na ule wa utendi na hadithi fupi. Huko Nigeria filamu ndefu ya "Mwalimu Mkuu wa Kijijini" iliendelea kwa karibu kizazi kizima. Saa sita au zaidi za televisheni huweza kutumiwa kuendeleza mada kubwa, kama ile ya historia ya makhalifa au ngano ya Samory. Tanzu zote za sinema zinaweza kubadilishwa kuwa za televisheni, kutoka kumbukumbu hadi katuni za watoto. Si vipindi vyote vinaweza kuchukuliwa kuwa ni sanaa hata kama vinavutia kiasi gani, kwa mfano mechi za mpira wa miguu. Hata hivyo, bado tanzu kadhaa za televisheni zinaweza kuwa sanaa na kuonyesha miundo mingi inayojulikana kutoka mapokeo simulizi. Chombo hiki bado ni kipya mno kuweza kutathimini mchango wake katika sanaa za vitendo.


## Sanaa ya Afrika katika muktadha wa dunia

Uchongaji wa Kiafrika ulileta mapinduzi katika sanaa ya Kizungu tangu 1905 na kuendelea. Ilipofika 1935 uchoraji wa kijiometri na usanaa-hisia wa Kijerumani ulikuwa umepitwa na wakati lakini athari ya sanaa ya Kiafrika ilidumu na hadi leo hii bado inaendelea kutawala uchongaji, kama kazi za Zadkine, Moore, Archipenko na wengineo zinavyoonyesha. Kwa njia hiyo kanuni za sanaa ya zamani ya Afrika imekuwa sehemu ya maumbo ya kimataifa[69].

Muziki wa Kiafrika umetoa pia mchango wake vyema hata kabla ya 1935 kwa kuchangia katika utungaji wa jazi na muziki wa Kilatino wa asili ya Kiafrika, mikondo ambayo nayo imechangia katika muziki wa kisasa wa Afrika.

[68] P. Michaud, 1986. Tofauti na Nyumba ya Redio, Kinshasa na uwekaji wa mtandao pale, ni mojawapo ya miradi ya maendeleo mikubwa ambayo nchi imeanzisha tangu 1970.

[72] M. Loiris na J. Delange, 1967, uk. 117-61; D. Ola, 1980; F. Willett, 1971, S. Burron, 1983, na C. Einstein, 1915, kwa manifesto yake.




*PICHA 20.9 Sanaa ya Kiafrika na ya Kijiometri: Kushoto: Kiti cha Kifalme kilichochongwa kutokana na mbao; mfalme wa Baraza lake, Kana, Datomey; Kulia: "Nabii," sanamu ya Ossi Zadkine, 1914*

Wakati wa kilele cha kipindi cha ukoloni, baada ya 1920, urithi wa kisanii wa Afrika ulikuwa na athari ndogo, tukiachilia mbali msukumo wa Le Corbusier uliotokana na usanii majenzi wa Mzab wa Algeria ya kusini. Wakoloni wenye majivuno waliwaona Waafrika kama wanafunzi kuliko kuwa walimu. Hata hivyo, baada ya uhuru sanaa za Kiafrika zilianza tena kuathiri ulimwengu. Hadhira ya kimataifa ilionyeshwa sanaa nyingi zaidi ya zamani ya Kiafrika, muziki mpya na tungo za sanaa za maonyesho au bale, na angalau filamu moja, *Le mandat* ya O. Sembene ilipata mafanikio ya dhati ya kupendwa huko Ulaya.

Ikiwa sanaa bora ya zamani imepewa hadhi ya juu, sanaa-onwa ya kisasa ndiyo imeanza tu kujulikana na watu wa kimataifa. Utambuzi kamili hata wa sanaa bora ya zamani ya Afrika, bado haujakamilika. Licha ya maonyesho mengi ya kisasa tangu Paris hadi Tokyo, Prague hadi New York, sanaa ya zamani ya Afrika bado imetengwa na hazina ya kile kinachochukuliwa kuwa ni "sanaa adhimu." Ni makumbusho ya Metropolitan ya New York pekee yanayoonyesha uchongaji wa zamani wa Kiafrika kwa utaratibu wa kudumu, japo bado kama "sanaa ya kishenzi." Sanaa bora ya zamani haijaingia Louvre, lakini imekwishafika katika majumba makubwa ya mnada. Wakati huohuo, wasanii wa kisasa, wanamuziki, waandishi wa tamthiliya na watoaji wa filamu bado wanapambana ili watambuliwe. Mapambano hayo sasa yameanza kuzaa matunda, kama ilivyoonyeshwa na Tunzo ya Nobel ya W. Soyinka na ushindi wa medali ya dhahabu ya 1987 katika tamasha la filamu la Cannes.

## Hitimisho

Nusu ya karne tangu 1935 haiingii vizazi viwili vya wasanii bali vitatu: wahenga, waanzishaji wa sanaa ya kisasa na wafuasi. Karata ilitupwa baina ya 1945 na 1965, wakati ambapo miaka kadhaa ya majaribio ilijichanganya katika jadi mpya ambayo baadaye wasanii waliiendeleza kuitumia. 1960 si tarehe muhimu katika sanaa: sanaa mpya ni matokeo ya kipindi kirefu cha matarajio ya utaifa, na sio uhuru wa kisiasa. Kwa jumla sanaa mpya hazitokani na jadi za Wazungu, ingawa zilianza wakati wa kilele cha athari ya utamaduni wa Kizungu. Maendelezo ya kipindi cha awali ndiyo yanayodhihirika zaidi kwenye sanaa za vijijini na pendwa. Tofauti ya dhahiri iko tu katika sanaa za maonyesho kwa kadiri zinavyojihusisha na kanuni za Kiitaliano, na katika sinema ambazo, zaidi ya zile za Misri, bado hazijawa sanaa pendwa.

Hivi karibuni, D. Niven alieleza juu ya uhusiano wa karibu kati ya wasanii wa kitaaluma na viongozi wa kisiasa[70]. Hii ni sura moja ya ukweli mpana: sanaa zimeakisi kwa uaminifu historia inayobadilika ya jamii za Kiafrika na mivutano yake. Jinsi watu wa mijini walivyotawala ndivyo sanaa yao ilivyotawala pia. Jinsi matabaka ya kijamii yalivyoundwa na mianya baina yao kuwa makorongo, kila tabaka lilipata udhihirishaji wake wa kisanii, kama ni wa kitaaluma au pendwa. Ni katika muziki tu ambako ndiko tofauti hiyo haiko dhahiri sana, na hasa kwa kuwa takriban hakuna wanamuziki wa kitaaluma.

Jamii za Kiafrika, mara nyingine tena, ni waongozaji wa majaliwa yao na wanapata ndoto na sitiari zao, sanaa zinazoonyesha matarajio yao yenye tata. Sanaa hizo ni mpya kwa sababu zinaakisi Afrika mpya.


# 21

# Mielekeo ya Falsafa na Sayansi katika Afrika

## Sura hii ni kwa heshima ya Sheikh Anta Diop

Je, kutawaliwa kisiasa kunakuwa na athari gani kwenye falsafa na sayansi ya jamii fulani? Afrika nzima imekuwa chini ya utawala wa kigeni kwa viwango vinavyotofautiana kwa kipindi chote kuanzia 1935, hata pale ambapo uhuru wa kisiasa ulikuwa umeshapatikana. Kwa hali hiyo suala kuu linalotakiwa kufikiriwa katika sura hii linahusiana na athari ya hali hii ya udunifu kwenye bahari ya Afrika ya elimu na utaalamu. Je, ukoloni ulikuwa kichocheo kipya cha maendeleo ya kisayansi na mabadiliko ya kitekuolojia? Je, falsafa rasmi ya Afrika ilitajirishwa na ukoloni? Je, falsafa ya Kiafrika ilizaliwa rasmi kutokana na mwingiliano wa Afrika na dunia ya Magharibi? Ama ukoloni ulikuwa na athari zilikwamisha falsafa na sayansi kwa pamoja?

Tunatarajia kuonyesha kwamba kiasi fulani, kwa sababu ya ukoloni, mchango wa mwanasayansi wa Kiafrika kwenye bahari ya elimu ya binadamu umekuwa mdogo katika kipindi kinachoanzia 1935. Lakini tunatarajia pia kuonyesha kwamba sayansi kwa wakati wote imekuwa kitu muhimu mno kuweza kupimika kwa kuangalia shughuli za wanasayansi peke yao. Kama ambavyo historia haitengenezwi na wanahistoria bali na jamii, vivyo hivyo sayansi haianzishwi na wanasayansi peke yao bali na jumuiya pana zaidi. Tunatarajia kuonyesha jinsi jamii ya Kiafrika ilivyokuwa mhimili mmojawapo wa sayansi na teknolojia ya magharibi, haswa kwa kuingizwa chini ya ukoloni. Wakati ambapo ukoloni ulileta ugumu katika maendeleo ya sayansi na teknolojia katika Afrika yenyewe, hali hiyo hiyo ya ukoloni ilikuwa ukanda wa kupitisha mchango wa Afrika wa nyenzo kwa ajili ya sayansi na teknolojia ya dunia ya magharibi.



*PICHA 21.1 Sheikh Anta Diop, Mwanafalsafa wa mwanafizikia, akiwa katika maabara yake ya IFAN,Dakar, Senegal*

Balı hali halisi ya Kiafrika haitokani tu na ukoloni. Msukumo uliokuwa na nguvu zaidi kuliko ukoloni katika Afrika ni utamaduni wenyewe wa Waafrika. Uchunguzi wa mwenendo wa sayansi na teknolojia katika Afrika ni lazima kwa hiyo, kutambua nafasi pekee ya amali na jadi katika falsafa na sayansi ya Waafrika.

Sura hii itajishughulisha na uzoefu wa Afrika katika falsafa na sayansi, na kuchunguza elimu kama jambo mujarabati. Kutokana na hali hiyo, tutakapojadili sayansi kutakuwepo na falsafa nyingi na kinyume chake. Lakini falsafa na sayansi vitatazamwa — kwa kukopa msamiati wa Marx - kama sehemu ya kikorombwezo Msingi utakuwa utamaduni wenyewe.

Sura hii inajadili sayansi na falsafa katika Afrika kuanzia 1935. Lakini kuna namna ambavyo falsafa na sayansi vinavuka mipaka ya eneo la kijiografia na muda wa kihistoria. Majadiliano ya sayansi na falsafa hayawezi kubanwa katika mipaka ya kijiografia ya Afrika na katika kikomo cha historia cha kipindi cha kuanzia 1935. Gharama ya kujishughulisha na sayansi na falsafa za ulimwengu kama hizo ni ile hali isiyokwepeka ya kuvunja mipaka ya eneo na muda. Tunajaribu kuelewa himaya ya sayansi na falsafa ya Kiafrika katika muktadha wa utamaduni, pamoja na nguvu zake zote na udhaifu wake wote.

Lakini ili kuelewa upekee wa Afrika, tunahitaji kuilinganisha na ustaarabu mwingine uliopo. Kile ambacho ni cha Kiafrika peke yake hakiwezi kugundulika bila kudadisi yale mambo ya kawaida kwa binadamu wote.

## Sayansi ya kijadi

Mkusanyiko wa elimu na utaalamu ambao ulihimili jamii za kabla ya ukoloni katika kilimo, afya, sanaa za ufundi na viwanda ndio kwanza unaanza kutambuliwa na kuthaminiwa. Katika kipindi cha ukoloni elimu hiyo pamoja na utaalamu vilidharauliwa kama ushirikina na mambo yasiyo ya kisayansi. Elimu na Ukristo wa Magharibi, na mara nyingine hata sheria za kikoloni na sera zilizotengenezwa kwa makusudi, vyote hivi vilitumiwa kuangamiza misingi ya elimu ya mapokeo kama hiyo, na watu walifundishwa kuidharau. Imegundulika kwamba leo hii pamoja na madawa, kilimo, sayansi na teknolojia ya magharibi, bado elimu na utaalamu wa mapokeo katika kilimo, matibabu na imani vimeendelea kuwa na nguvu katika maisha ya idadi kubwa ya Waafrika.

Inatakiwa tubainishe sura mbili za sayansi ya mapokeo. Mosi, dhima ya wanafikra na wabunifu binafsi katika kukuza maarifa na utaalamu katika utamaduni iliwekwa chini ya dhima ya jamii nzima. Hivyo kupotea kwa uhuru na haki ya kujitawala wakati wa ukoloni hakungekosa kuwa na athari kali katika maendeleo na ukuaji zaidi wa maarifa hayo. Pili, jamii za kimapokeo hazikutofautisha kati ya elimu iliyopatikana kwa kutafakari, kufanya majaribio, kubuni au imani. Hakukuwa na msigano kati ya sayansi na dini, sayansi na falsafa ama sayansi na sanaa. Maarifa ya kisayansi hayakuangalia tu kimahesabu na kimaslime kwa hiyo sayansi ya magharibi haikuweza kuthamini njia wala kuona thamani ya sayansi ya jadi katika Afrika hadi hatua ya (nadharia ya) uwianisho katika sayansi ya magharibi ilipoanza kubadilisha msisitizo wake kutoka utaratibu wa kuangalia kitu kimoja kimoja kuelekea kwenye michangamano ya vitu katika haliasili na hapo ndipo vielelezo vya Kimagharibi vya maendeleo vilipoanza kutiliwa shaka[1].

Wakati wa ukoloni, wakulima wadogo wadogo wa Afrika walilazimishwa kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vya wazungu chini ya masharti yaliyotolewa na sayansi ya kilimo ya magharibi ambayo iliundwa katika nchi za hali ya hewa ya wastani. Mazoea ya kilimo yaliyobuniwa katika Afrika kwa karne

[1] R. Schrama, kur. 391-9. Tazama pia A.O. Aunya, 1987, uk. 141-60.

nyingi ili kuhifadhi rutuba ya ardhi kwenye hali za kitropiki yalizuiwa: Wakulima hawa walilazimishwa kufuata utamaduni wa zao moja badala ya ule wa mazao mengi, kutekeleza kilimo shadidi kwa kutumia mbolea badala ya kuruhusu kilimo cha mzunguko ili kuruhusu ardhi kupumzika kwa kipindi fulani. Sasa, kwa kuwa udongo wa Afrika umechoka kutokana na kuzalisha mazao ya biashara, na umekuwa duni kiasi kwamba inakuwa vigumu kuulazimisha kuzalisha chakula cha kutosha kukimu idadi ya watu inayoongezeka, wanasayansi wanaanza kumakinikia mantiki na hekima ya kaida nyingi za mapokeo za kilimo cha kitropiki.

Kama ambavyo ilikuwa imetarajiwa, Waafrika wengi kaskazini na kusini mwa Sahara walikuwa na wataalamu wenye elimu ya kina kuhusiana na hali ya hewa na tabia za udongo wa Afrika. Walitumia uangalifu mkubwa kuchagua maeneo ya kuselelea na ya kulima, na jamii zingine zilikuwa na matambiko ya kurekebisha desturi za kilimo kwa sherehe za kila mwaka na kaida za maviga. Watu kama Wahausa, Waberberi na Waighbo walikuza kilimo kwa mashindano na kutoa vyeo vya heshima kwa mshindi mkubwa kuliko wote. Ujuzi wa mapokeo katika kilimo, na uhifadhi wa udongo bado vinaweza kuonekana katika sehemu nyingi za Afrika ambapo matuta yanatengenezwa katika kilimo cha milimani, bila kuathiriwa na sayansi ya kilimo ya ukoloni.

Watu wengi wa Afrika wanayo elimu ya kina kuhusu mimea na miti mbalimbali ya kitropiki inayopatikana kwenye maeneo ya jirani. Hata vichaka katika sahara vilijulikana kwa Waberberi na wanamali wa Kiarabu na wakulima. Sehemu nyinginezo zilikuwa na mwainisho wa kina wa mimea ulioiweka kwenye familia na vikundi vidogo vidogo kufuatana na sifa zake za kiutamaduni na kimiviga, sifa ambazo hazilingani na ainisho za siku hizi za elimu mimea. Sifa hizo zilikuwa changamani na zenye utondoti kiasi kwamba wana sayansi wa mimea wa siku hizi wanayo mengi ya kujifunza kutokana na msingi wa ulinganisho na uainisho huo. Siku hizi elimu ya sifa za madawa yanayotumika katika mifumo ya tiba inachunguzwa na wafamasia waliofunzwa Magharibi[2].

Kutoka Rasi hadi Kairo, taarifa zilikusanywa na kuchunguzwa kuhusu hulka na tabia maalumu za watu na wanyama. Madhumuni hasa ya uchanganuzi kama huo mara nyingi yalikuwa ni kugundua jina la "kweli" la kitu, kwani ni kwa kujua jina la kweli la kitu na kulitumia katika manuizo ndipo kitu chenyewe kinapoweza kudhibitiwa[3].

[3] Boubaou Hama, 1981, uk. 170-2.

[2] M. Last na G.L. Chavunduka, 1986. Tazama pia C. Wilcocks, 1962; na J.B. London, 1976

Vivyo hivyo taratibu zenye utondoti mkubwa kuhusu mahusiano katika ulimwengu wa mizimu zilidhihirishwa, zikionyesha tabia za miungu na mizimu (majini katika Afrika ya Waislamu) kutokana na ruwaza za tabia za watu na wanyama, na mara nyingine kutumia ruwaza hizo zilizobuniwa za ulimwengu wa mizimu kama vielelezo vya jamii ya kibinadamu. Maafikiano yaliyojikita kwenye msingi wa uehunguzi wa kina na uehanganuzi mara nyingine yaligeuziwa kuwa visasili vya uumbaji, vyenye kusimba imani kuhusu asili ya binadamu na saikolojia jamii. Mara nyingine watu wa Mirsi walichanganya mawazo ya kifarao na ya Kiislamu. Lakini mfano wa Wadogon wa Mali ndio umeelezewa vizuri katika Afrika Kusini mwa Sahara, ambapo Marcel Griaule na Germaine Dieterlen walisema:

Miongoni na hata nje ya jumla hii ya imani kunaonekana utaratibu wa ishara mantiki ukidhihirisha mfumo wa mawazo ambayo hayawezi kuelezewa tu kisahili kwa kuyaita kisasili. Kwani muundo huu wa dhana unapochunguzwa unadhihirisha mfungamano wa ndani, busara ya siri na welewa wa ukweli wa msingi unaofanana na ule ambao sisi Wazungu tunafikiri tumeupata[4].

Kulikuwa na nadharia changamano za namba, uchunguzaji wa nyota, na mambo mengine ya asili ambayo yalitumika kuleta mpangilio wa mambo yanayohusiana na jamii, asili na metafizikia. Kutokana na mpangilio huo waaguzi walijaribu kubuni mwelekeo wa matukio na kuwashauri wateja wao kuhusu kile kilichotarajiwa na jinsi ya kuzuia kuingiliwa na nguvu za uovu.

Miongoni mwa wakulima, vilikuwemo vikundi vya wataalamu, hasa wawindaji wakiwa watu binafsi na washirika, ambao walipata elimu ya wanyama wa kitropiki na kuanisha kufuatana na utamaduni. Wafugaji kama vile Wafulbe, Wamasai na baadhi ya Wasomali walipata elimu pana kuhusu wanyama wao na mahitaji yao ya kibiolojia, pamoja na elimu ya wanyama wa ulimwengu kwa ujumla. Kutokana na hili wengi waliendeleza elimu na utaalamu mkubwa kuhusu maradhi na tiba ya wanyama, wakijumuisha mbinu maalumu za upasuaji wa wanyama. Elimu kubwa kati ya hii imepanuliwa hadi kwenye tiba ya upasuaji kwa ajili ya watu, na sasa inaaminika kwamba tiba ya siku hizi yaweza kujifunza kutokana na utaratibu wa upasuaji wa kijadi kama ulivyotumika kwenye tiba ya kugandisha ngozi na njia za mapokeo za kuunga mifupa iliyovunjika.

[4] M. Griaule na G. Dieterlen, 1954, kwenye D. Forde, 1954, uk. 83. Tazama pia C.H. Long, 1985, uk. 369-70

Mfumo wa tiba ya mapokeo ulijumuisha elimu juu ya uhusiano wa magonjwa, viumbehai vidogovidogo na bakteria, ambavyo vipo katika kiini cha dawa za kisayansi za magharibi. Utamaduni wa tiba ya Wayoruba tayari alikwishaji-egemeza kwenye dhana ya "minyoo" na "wadudu" ambao walikuwa wadogo kiasi cha kutoonekana. Vijidudu hivi na minyoo hii ilikuwa na dhima yenye manufaa na pia ya kuleta madhara kwenye miili. Baadhi waliuvamia mwili kutokana na chakula kisichofaa, ulafi, matumizi mabaya ya mwili au kuuweka mwili katika mazingira mabovu. "Wadudu" wengine walipigana na ugonjwa na kujaribu kuuweka mwili kwenye uwiano bora kiafya.

Nadharia ya ugonjwa ya vijidudu na minyoo ilienea zaidi katika Afrika kuliko watu walivyofikiria. Lakini wauguzi wa asili waliendelea na fikra kwamba afya ilikuwa na mambo mengi zaidi ya kudhibiti athari za madhara ya bakteria kwenye maeneo ya mwili na kwamba mahusiano ya kijamii na ya kiroho ya mgonjwa nayo yalihitaji kuchunguzwa na kurekebishwa. Mwelekeo huu wa ujumla wa matibabu sasa unaanza kukubalika na kutumika katika madawa ya Magharibi na hasa katika matibabu ya akili. Matabibu wa Kiafrika wameonyesha manufaa ya kushirikisha jumuiya za kienyeji katika kutibu wagonjwa wa akili.

Ni kweli busara hii ya kuunganisha afya ya kimwili, kijamii na ya kiroho inaanza kukubalika. Kukubalika huku kunatakiwa kutuelekeze kwenye kuelewa vizuri zaidi mawazo asili ambayo katika kupangilia elimu, hayakukubali kuwepo kwa mgawanyo baina ya elimu viumbe na jamii, au elimu jamii na elimu ya kiungu. Jambo hili linapaswa likomeshe dhana ya kibaguzi ya kuainisha mawazo asilia kama mawazo ya kabla ya sayansi. Mkazo katika mkabala jumuishi, hata hivyo, haupaswi kuziba elimu halisi ya kisayansi ambayo ilihusika katika mifumo ya utabibu na kilimo kuanzia Marrakesh hadi Maputo.

Kwa hakika, sayansi na teknolojia ya Kiafrika katika kipindi cha kabla ya ukoloni ilitosha kuhimili maisha, hasa katika maeneo ya matunzo ya afya, kilimo, madawa ya mifugo na usindikaji wa viwandani kama vile kuhifadhi chakula, ufuaji wa metali, kuchachua, kutengeneza rangi, sabuni, marashi na bidhaa nyingine za kutunza mwili. Sasa ni kwa vipi Afrika imekuja kuwa nyuma sana kisayansi na kiteknolojia?

## Uvurugaji wa teknolojia ya Afrika

Hali duni ya sasa ya sayansi na teknolojia katika Afrika ni matokeo ya athari ya Magharibi kwenye bara hili, hasa tangu kuanzishwa kwa ukoloni. Wazungu hawakuonyesha haraka yoyote ya kupunguza uongozi wao katika sayansi na teknolojia dhidi ya Afrika, kwa kubuni mpango wowote ambao ungeleta maendeleo ya kisayansi na ya kiteknolojia katika Afrika. Hawakuamsha wala kuendeleza taratibu za kisayansi na za kiteknolojia zilizokuwepo. Silaha kubwa waliyotumia katika kuzuia maendeleo ya Afrika katika sayansi na teknolojia ilikuwa ni shule. Kwanza, elimu rasmi katika ukoloni wa Afrika ilihusishwa na kufundisha dini zaidi kuliko kueneza sayansi. Shule nyingi zilikuwa ni za wamisionari Wakristo. Kwa vyovyote Biblia haikuwa kitabu cha muongozo wa teknolojia. Na bado katika miongo ya awali ya karne ya ishirini Biblia ndiyo iliyoamua matamanio na malengo ya wamaizi wa Kiafrika walioknwa wanaibuka.

Jambo jingine lililozuia sayansi katika Afrika katika kipindi hiki ni mwelekeo wa jumla wa kifasihi katika shule za kikoloni. Wanafasihi mashuhuri wa Magharibi ndio waliotawala kama mifano kwa wanafunzi wa shule za kikoloni kuliko mifano ya wanasayansi wa Magharibi. Katika vitabu vya wasifu wa kizazi cha kwanza cha viongozi wa Kiafrika katika nusu ya pili ya karne ya ishirini, mtu anakatishwa tamaa kwa kutoona katika orodha hiyo ya viongozi wa nchi, mwanasiasa yeyote aliyehamasishwa na Copernieus, Galileo, Isaae Newton, Charles Darwin au Albert Eistein[5].

Jambo la tatu la kikoloni lililozuia maendeleo ya sayansi katika Afrika katika sehemu kubwa ya karne ya ishirini lilikuwa ni usahaulifu. Ni watoto wachache wa Kiafrika nje ya Ethiopia walifahamu chochote kuhusu makanisa yaliyodidimia ya Lalibela kama mafaniko ya kiuhandisi. Ni watoto wachache nje ya Afrika ya Kusini walifahamu choehote kuhusu magofu ya Zimbabwe Kuu - na mara nyingi majengo hayo yalifikiriwa kuwa ya wageni au ya vikundi visivyoeleweka kama "Wahamita". Muhtasari wa mafunzo ya wakoloni ulikataa kukiri kwamba Misri ya kale ilikuwa ni ustaarabu wa Kiafrika, na kwamba ulikuwa wa watu weusi. Waalgeria walifundishwa kwamba nehi yao iliknwa ni kisehemu eha Ufaransa ambacho hakikuendelea.

[5] Kwa mifano mingine, tazama J.A. Rogers, 1972; tazama pia S.F. Mason, 1962.

Kasi ya kuleta sayansi katika Afrika ya karne ya ishirini ilipungua kwa kiasi fulani kutokana na kwamba Waafrika walifanywa wasahau kwamba wao wenyewe walikuwa wameshapata mafanikio ya kisayansi. Usahaulifu huu wa kiteknolojia wa pamoja ulileteleza udodaji wa pamoja wa kisayansi. Pia ulilea unyonge wa kiteknolojia kwenye mioyo ya idadi kubwa ya kizazi kipya katika Afrika ya ukoloni. Unyonge na utegemezi wa Afrika vilikuwa pande mbili za sarafu moja ya kikoloni[6].

Mbali na suala la umisionari (Biblia kama aula) suala la fasihi (lugha ya Kizungu na fasihi yao kama kielelezo) na suala la usahaulifu (kufuta kabisa ubao wa kitekinolojia wa Waafrika), utaratibu wa kikoloni pia ulizuia maendeleo ya sayansi kwa sera yake ya "kuleta suluhu" hasa katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini. Sera za kikoloni zilizojengwa kwenye msingi wa "kuleta suluhu" na "sheria na utaratibu" zenyewe hazikuwaamini raia jasiri katika makoloni hayo. Chini ya hali kama hizo wabunifu walionekana kama "wajuvi", wenye hoja walionekana kama "waehochezi" na waliojiamini walionekana kama "mafidhuli".

Mwishowe, udhibiti wa uchumi na vikwazo vilivyotiwa kuzuia viwanda katika Afrika navyo pia vilizuia kuenea kwa sayansi na teknolojia ya Magharibi. Tuehukue mfano wa nguo. Pamba ililimwa kwa ajili ya kusafirishwa nje. Huko Ulaya watu walijifunza kuhusu rangi asili na ruwaza za kisanii kutoka sehemu mbalimbali za Afrika, na nguo duni zilizoigiza ruwaza na rangi hizo ziliingizwa Afrika, na kulazimisha nguo zilizofumwa kwa mikono kutoweka masokoni na kuzifanya kuwa nguo za nadra na za kifahari zilizovaliwa kwenye sherehe na matukio ya kimiviga pekee. Vivyohivyo vyombo vya jikoni, vifaa vya ujenzi, mapambo ya vito, vipodozi, vyakula na vinywaji vya kutoka nje vilianza kuchukua nafasi ya vile vilivyotengenezwa Afrika. Hii ni mbali na mahitaji mapya yaliyojitokeza katika kipindi vha ukoloni, kama vile vifaa vya shule na vya hospitali, karatasi na bidhaa nyingine za viwandani ambazo zilitakiwa ziagizwe kutoka nje[7].

Maeneo ya machimbo ya madini yaligawanywa kwa makampuni ya kimataifa kwa makubaliano, na Waafrika waligeuka kuwa wavamizi haramu kwenye machimbo ya ardhi yao.

Ni katika miaka ya 1940 tu ndipo Waingereza walijaribu kwenda mbele kidogo ya ukoloni wa sheria na utaratibu na kuingia kwenye kile kilichojulikana kama

[5] Kwa mifano mingine, tazama J.A. Rogers, 1972; tazama pia S.F. Mason, 1962.

[7] Angalia kwa mfano, P. Kilby, 1969; P. Pugh na J.F.A. Ajayi, 1990. Kwa athari za mtaji kwa watu wa Nyanda za juu za Joss, angalia B. Frend, 1981.

"maendeleo na ustawi wa koloni." Pia walianzisha mfuko kwa jina hilo "Mfuko wa maendeleo na ustawi wa koloni."

Ni katika awamu hii ya maendeleo ya ukoloni ambapo fursa ilitolewa ya kupanua elimu hasa katika kiwango cha juu, kwa kutoa msaada wa masomo kwa Waafrika kwenda kusomea Ulaya, na zaidi kwa kuanzisha taasisi zilizoweza kutoa masomo ya shahada, mwanzoni zikiwa kama vituo vya nje au tawi la vyuo vikuu vya nchini kwao, kama vile Ibadan, Legos, Makerere, Dakar, na Lovanium pamoja na vituo vya kale zaidi kama vile Fourah Bay na Fort Hare. Muhtasari wa masomo na walimu wa vyuo hivyo walidhibitiwa na vyuo vikuu vya Ulaya ambavyo ndivyo vilivyotoa digrii hizo. Walidumisha hadhi ya juu na kuanzisha utafiti wa kisayansi kwenye maeneo ambayo maprofesa hao, wengi wao wakitokea Ulaya, walikuwa na uwezo mkubwa nayo. Nyanja walizozitumia zaidi yalijumuisha madawa ya tropiki ya watu na mifugo, hasa kuhusu vimelea na virusi; magonjwa ya milipuko, chunguzi za biokemikali, na kuweka misingi ya taaluma za kihospitali katika nyanja za fizikia (taaluma ya ionosifia); kemia (vitu asilia); biolojia (ekolojia na mikolojia). Maeneo makuu ya kuzingatia yalikuwa ni kuendeleza na kuongezea tafiti zilizokuwa zikifanywa huko nje kwenye vyuo vikuu[8]. Hata hivyo hawakuhusisha maeneo muhimu kama vile jenetiki, biotekinolojia, sayansi ya upashanaji habari wala tckinolojia ya kompyuta.

Vyuo hivyo vilikuwa ni kwa ajili ya kufundisha sayansi zaidi kuliko vya kuendeleza utafiti wa kisayansi. Elimu tegemezi kama hiyo ilizuia uasilishaji. Iliendeleza watu binafsi sio katika utamaduni na jamii yao bali nje ya utamaduni na jamii zao. Ilimtenga msomi na kumweka nje ya umma wa jamii yake na hivyo kulemaza ubunifu wake. Uhamaji wa wataalamu kwenda dunia ya Magharibi ulianza mapema katika nchi kama vile Misri kutokana na kutengwa huko na jamii zao.

Taasisi za utafiti wa kisayansi na mafunzo zilizohitajika kwa ajili ya kunyonya rasilmali za Afrika zilijengwa na kuendelezwa katika nehi za Ulaya. Katikati ya Vita viwili Vikuu vya Dunia, vituo vya kukusanya data na vielelezo vya wanyama na mimea na "vioja" vingine yote ya mazingira fulani, ufundi na mambo mengine ya kienyeji "yasiyokuwa ya kienyeji" vilianzishwa kama vituo vya nje vya majumba ya makumbusho ya huko kwao, bustani za mimea na wanyama na taasisi za utafiti wa kilimo na misitu ambapo tafiti za msingi na matumizi ya tafiti hizo yaliendelezwa. Kwa kawaida, wakati Waingereza walitarajia kila koloni au kikundi cha kikanda cha makoloni kuanzisha na kupatia vituo hivyo fedha za kujiendesha, mashirika ya utafiti ya huko Ufaransa yalifadhili vituo vyao, na Wabelgiji na Wareno

[8] Kwa mfano, J.F.A. Ayayi na T.N. Tamuno, 1973; na K. King, 1984.

walitarajia kwamba makampuni yaliyoteuliwa kuendesha shughuli katika makoloni yao yangekuwa ndio wafadhili wa kifedha wa shughuli za kisayansi[9].

Katika kipindi hicho cha katikati ya vita hadithi zilizotawala katika vituo hivyo, hasa kwenye ile miaka ya mpomoko, ni zile za kutelekezwa, ukosefu wa watumishi na wa fedha. Taasisi ya Pasteus ya Ufaransa ilifanikiwa kufanya utafiti mkubwa huko Afrika ya Kaskazini katika madawa ya kitropiki na kufanikiwa kupata tunzo mbili za Nobel, moja kwa Alphonse Laverane mwaka 1907, kwa ajili ya kazi yake kuhusu malaria iliyofanyika zaidi huko Algeria, na ya pili kwa Henri Nicolle mnamo 1928 kwa utafiti wake wa homa ya matumbo uliyofanyika zaidi huko Tunis. IFAN (*Institut francais d'Afrique Noir*; Taasisi ya Wafaransa ya Afrika Nyeusi), taasisi ya uchunguzi iliyojishughulisha na maswala mengi ilianzishwa huko Dakar mnamo 1936 ikiwa na matawi kwenye kila koloni la Wafaransa huko Afrika ya Magharibi. Taasisi hiyo pia ilipata mafanikio katika kusisimua utafiti na baadaye ilikuja kuwa kituo cha kazi nyingi alizofanya Sheika Anta Diop. Mnamo 1947 Wabelgiji walianzisha kituo muhimu cha IRSAC (Institut pour la recherche scientifique d'Afrique Centrale: Kituo cha utafiti wa sayansi katika Afrika ya Kati) ili kuhudumia nchi zote zilizokuwa chini ya Wabelgiji katika Afrika. Madhumuni ya IRSAC yalielezwa kama ni kutoa ufadhili, kutangaza, kutenda na kuratibu uchunguzi kuhusu sayansi jamii na ile ya asili, hasa katika maeneo ya Kongo ya Ubelgiji na Rwanda-Urundi. Kituo cha utafiti wa kilimo tayari kilishaanzishwa huko Kongo ya Ubelgiji mwaka 1933 na baadaye kilikuja kupata hadhi kubwa ya kimataifa: *Institut national d'études agronomiques au Kongo* (Taasisi ya Taifa ya Mafunzo ya Kilimo). Makao makuu ya kituo hicho yalijengwa katikati ya msitu wa Ikweta.

Katika maeneo mengi ya Afrika, vituo vingi vilivyojengwa havikuwa maabara ya sayansi au taasisi za utafiti ila vingi vilikuwa karakana za kukarabati njia za reli, telegrafu, vituo vya redio na vifaa vya kuchunguzia au vituo vya kufanyia majaribio ya jinsi ya kuboresha mazao na usindikaji wa mazao ya biashara kwa ajili ya kuuza nje. Mifano mizuri ya mambo hayo iliweza kuonekana wazi kwenye maeneo waliyolowea Wazungu hao kama vile Algeria, Rhodesia na Afrika ya Kusini. Pia ni kwenye maeneo hayo, hasa kwenye machimbo, ambapo fursa ya kuanzisha viwanda ilijitokeza. Huko Afrika ya Kusini hazina kubwa ya utajiri wa dhahabu na almasi ilivutia kiasi kikubwa cha vitega uchumi na fedha pamoja na walowezi waliofika kuendesha vitega uchumi hivyo na kusimamia teknolojia ya

[9] J.W. Froje, 1989, uk. 19-22.

kuchimba madini. Utajiri kwenye maeneo ya machimbo, uhuru uliopatikana kwa jamii za walowezi baada ya vita vya Afrika Kusini, na uhaba wa bidhaa za viwandani zilizoagizwa kutoka nje uliojitokeza wakati wa Vita vya I vya Dunia, kwa pamoja vilichangia kuleta usitawi wa ghafla katika sekta ya uzalishaji katika uchumi wa Afrika Kusini. Hili lilileteleza kupanuka kwa vyuo vikuu na taasisi za utafiti na hivyo kuimarisha msingi wa sayansi na teknolojia ya Magharibi huko Afrika Kusini kwa ajili ya Weupe peke yao[10].

Athari za sayansi na teknolojia ya Magharibi kwa Afrika katika kipindi cha ukoloni zilidumaza zaidi maendeleo. Waafrika wachache walifanikiwa kufika Ulaya kwa ajili ya mafunzo, lakini ni wanafunzi wachache sana wa Kiafrika waliochagua kusoma uhandisi au sayansi ya juu kwa vile hawakuwa na maeneo ya kutekeleza kile ambacho wangesomea kwenye nyanja hizo ndani ya mfumo wa utumishi finyu wa kikoloni. Zaidi Waafrika walikwenda kusomea ili wawe wachungaji, walimu, watawala na wanasheria[11]. Kwa hali hiyo hatuwezi kutarajia kumpata mtafiti wa sayansi miongoni mwa kizazi cha kwanza cha viongozi wa juu, ijapokuwa mmoja alielimishwa kwenye ufamasia (Ferhat Abbas wa Algeria), na watatu kati yao walikuwa madaktari wa madawa (Felix Houphouet-Boigny, Agostinho Neto na Kamuzu Banda). Hata hivyo elimu ya mapokeo iliendelea kudhihirisha nguvu zake za kiutamaduni hata miongoni mwa wasomi walioelimishwa huko Magharibi, na wengi waliohitimu kwenye vyuo vikuu walitafuta fursa ya kuaguliwa na waganga na wapiga ramli wa asili.

## Maendeleo tangu uhuru

Katika nusu ya pili ya karne ya ishirini, wakati nchi nyingi za Kiafrika zilipojipatia uhuru, utafiti wa juu wa kisayansi katika Afrika ulipatikana katika aina nne za taasisi. Kategoria ya kwanza ni vyuo vikuu, ambavyo kuanzishwaji kwake kulipata msukumo mkubwa kufuatia mwamko wa mwanzo wa utaifa wa miaka ya 1950 na miaka ya 1960. Vyuo hivi vilitoa vituo vilivyoenea sana vya utafiti wa juu wa sayansi katika idara zao za sayansi, uhandisi, kilimo na tiba. Nchi kama vile Nigeria, Ghana, Cote d'Ivoire zimeweza kuhimili kiwango cha juu cha upanuzi wa vyuo vikuu na vyuo vikuu maalumu vichache vinavyojishughulisha na sayansi na teknolojia ya kilimo, ijapokuwa bado havijaanzishwa vya tiba.

[10] A.C. Brown, 1988.

[11] Kwa mifano mingine ya kuigwa, tazama J.A. Rogers, 1972; tazama pia S.F. Mason, 1962.

Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki kilipokuwa hai (1963-1970), labda ndicho kilichokuwa jaribio kubwa zaidi la kitaaluma kwa Afrika nzima. Ufundishaji na utafiti wa madawa na kilimo vilitakiwa viendelezwe na kuwa maalumu kwa chuo cha Makerere huko Uganda; ufundishaji na utafiti wa uhandisi ulikabidhiwa kwa chuo cha Nairobi. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitengwa maalamu kwa ajili ya sheria, na baadaye kupanuka kuwa na utafiti wa kilimo na uchumi. Karibu asasi zote za Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki mwanzoni zilitengwa kuhudumia sio tu nchi zilimokuwa asasi hizo bali Jumuiya nzima ya Afrika ya Mashariki (Kenya, Tanzania na Uganda). Kwa bahati mbaya chuo hiki kilivunjika na kuwa vyuo vikuu vitatu kwenye nchi hizo tatu.

Kategoria ya pili ya asasi ni taasisi na vituo vya utafiti vya taifa, vilivyoendeshwa kibinafsi au kwa fedha ya umma. Kenya na Nigeria zina taasisi za aina hiyo za kudhibiti magonjwa, misitu na kilimo; Zaire (Congo) na Ghana zina taasisi za uchunguzi wa fizikia ya nyuklia; Nigeria taaluma ya bahari. Nigeria, Zimbabwe na Kongo (Zaire) zimekuwa makini sana katika madawa asili ya mitishamba kama eneo la utafiti wa kisasa.

Kategoria ya tatu ya taasisi ya utafiti katika Afrika ni ile ya mashirika ya kikanda kwa ajili ya Afrika nzima. Mengi kati ya haya hujihusisha utafiti wa hali ya hewa na ekolojia ambao ni maalumu kwa maeneo fulani ya Afrika kama vile Sahel; mengine zimeshirikiana kwenye masuala ya kikanda kama yale yanayohusiana na nzige.

Shirika maalumu la kitaalamu au la kisayansi kwa Afrika yote ni lile la chama cha wataalamu au akademia ya wataalamu. Sheikh Anta Diop alijaribu hata huufanya utafiti wa Kiafrika uvuke nje ya mipaka ya Afrika na kuhusiha dunia ya watu weusi kwa jumla. Hayo ndiyo yaliyokuwa madhumuni ya Chama cha Watafiti Weusi wa Ulimwengu ambacho kilianzishwa mwaka 1976, na ambacho raisi wake alikuwa Diop.

Kategoria ya mwisho ya asasi zinazofanya na kukuza utafiti wa kisayansi na wa kitekuolojia katika Afrika ni ile ya vyombo vya utafiti vya kimataifa na vya mabara mengi ambavyo vinavuka kiwango cha udugu wa kisayansi wa Afrika Yote. Mwafrika ndiye anayeongoza Kituo cha Kimataifa cha Fiziolojia ya Wadudu na Ekolojia (ICIPE), ambacho kilijizatiti katika kuelewa dunia ya wadudu. Akademia ya Sayansi ya Afrika ambayo makao yake makuu yako Nairobi inatoa jarida lake linaloitwa *Ugunduzi na Bidaa* ambalo linafadhiliwa kwa pamoja na

Akademia ya Sayansi ya Dunia ya Tatu[12]. Taasisi ya Chuo Kikuu cha Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Rasilmali Asili katika Afrika (INRA) ipo Yamusukro huko Cote d'Ivoire.

Nigeria ndio wenyeji wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Tropiki (IITA) ikiwa na lengo la kuboresha mazao mbalimbali ya Afrika ya chakula nje ya mazao ya biashara. Maabara ya radio-kaboni ya Sheikh Anta Diop huko IFAN Dakar ilijumuisha malengo ya taifa, ya Afrika Yote na ya bara lote kwa vipindi tofauti. Maabara hiyo ilianzishwa mwaka 1966 ikiwa na madhumuni ya kuchunguza athari za mnururisho wa nishati duni na ukadiriaji wa tarehe kwa njia ya kaboni - 14[13].

Katika miaka ya 1970, Umoja wa Nchi Huru za Afrika, UNESCO na ECA kwa pamoja wamekuwa wakijihusisha kwa kiasi fulani na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika Afrika. Mkutano wa kwanza wa Mawaziri wa Nchi Wanachama za Afrika wenye madaraka juu ya matumizi ya sayansi na teknolojia katika maendeleo, ulifanyika huko Dakar, Senegal, mnamo Januari 1974. Mkutano huu ulitayarishwa na UNESCO ikishirikiana na OAU pamoja na Shirika la Uchumi la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika. Mkutano huu ulipitisha mapendekezo ya sera kuhusu sayansi na teknolojia.

Mkutano wa Kikanda wa Afrika ulifanyika huko Kairo, Misri, mwaka 1978, ukiwa ni matayarisho ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Sayansi na Tekuolojia kwa Maendeleo (UNCSTD), ambao ulifanyika huko Vienna, Austria, Agosti 1979. Lengo lake kubwa lilikuwa ni kutafuta njia ya kuondoa tofauti za kiuchumi kati ya Dunia ya Tatu na nchi zenye viwanda.

Katika kikao cha kumi na sita cha kawaida cha Wakuu wa Nchi na Serikali wanachama wa OAU kilichofanyika huko Monrovia, Liberia, Julai 1979, Tamko la Ahadi la Monrovia lilipitishwa. Katika Tamko hilo Wakuu wa nchi na serikali wanachama wa OAU walieleza nia yao ya kutumia sayansi na teknolojia katika maendeleo, na kuimarisha uwezo wa nchi zao wa knjitegemea katika uwanja huu. Mkutano Usio wa Kawaida wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa OAU uliofanyika huko Lagos, Nigeria, tarehe 28-29 April 1980, pia ulipokea *Mpango wa Utendaji wa Lagos*. Sura ya V ya mpango huo ndio hasa iliyohusu sayansi na

[12] Mwezi Juni 1986, Akademia ya Sayansi ya Afrika ilifadhili tukio muhimu la pekee la Kimataifa kule Nairobi-Kongamoano la Kwanza la Mtandao wa Mashirika ya Kisayansi ya Kiafrika – ambalo lilionyesha eneo jipya la mashirikiano miongoni mwa wasomi na wanasayansi wa Afrika na sehemu nyingine duniani

teknolojia na kuvuta nadhari kwenye wajibu wa sayansi na teknolojia katika maendeleo jumuifu ya vijijini.

Kongamano kuhusu sayansi na utamaduni wa Kiafrika kama msingi wa maendeleo liliandaliwa na OAU ikishirikiana na UNESCO huko Libreville, Gabon, kuanzia 23 hadi 27 Januari 1981; Azimio moja lililopitishwa kwenye Kongamano hili liliitaka OAU iandae mkutano wa wanasayansi wa Afrika. Miaka minne baadaye, mkutano wa kawaida wa ishirini na moja uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 18-20 Julai 1985 ulipokea Programu ya Aula ya Afrika ya Kufufua Uchumi, 1986-90. Aya ya 34 ya programu inasema: "Uzoefu unaonyesha kwamba hakuna nchi yoyote iliyofikia ushindi katika (knjenga) msingi wake wa sayansi na teknolojia." Katika kikao hiki Wakuu wa Nchi na Serikali wanachama wa OAU walipokea azimio lililoitaka UNESCO kuanzisha Programu ya Msaada kwa Afrika katika nyanja za utafiti wa sayansi na uendelezaji wa utafiti, hususani kwa lengo la kuendeleza uwezo wa kisayansi na wa kiteknolojia wa nchi za Kiafrika katika nyanja za jiolojia, mikrobiolojia, kilimo, chakula na afya; na pia kuhusu maji yaliyo juu na chini ya ardhi.

Mwishowe Mkutano wa Pili wa Mawaziri wenye wajibu wa kuangalia matumizi ya sayansi na teknolojia katika maendeleo ya Afrika, uliofanyika Arusha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 6-15 Julai 1987, ulipitisha Programu Maalumu ya Msaada kwa Afrika katika nyanja za Utafiti wa Kisayansi na Kiteknolojia, na pia Utafiti na Maendeleo. Mwishowe vipaumbele vya utafiti zilipendekezwa, pamoja na utaratibu na mbinu za kufuata ili kukuza sayansi na teknolojia kwenye ngazi tatu: taifa, kanda ndogo, na kanda[14].

*Institut Africain d'études Prospectus* (INADEP: Taasisi ya Kutabiri Mambo ya Afrika) ilianzishwa huko Kinshasa mwaka 1989 kama jibu kwa ombi lililoletwa na wanasayansi wa Kiafrika pamoja na maofisa waandamizi kwenye Kongamano Kubwa lililofanyika huko Kinshasha, Kongo, mwaka 1985, lililokuwa na mada kuhusu Afrika na mustakabali wake. Kituo cha Taaluma ya Misri ya Kale (CECAD) kilichotiwa wakfu kwa kumbukumbu ya Sheikh Anta Diop kiliunganishwa na taasisi hii.

Taasisi ya Watu Weusi (IBP) ilianzishwa huko Wagadugu, Burkina Faso, mwaka 1990 kwa madhumuni ya kuendeleza elimu pana iwezekanavyo ya kisayansi ya

[14] CASTAFRICA Mpango Maalum wa Msaada kwa Afrika katika nyanja za Sayansi na Utafiti wa Kiteknolojia na Maendeleo, 1987.

dunia ya watu weusi. Shirikisho la Sayansi na Teknolojia ya Afrika Yote (PUST) lilianzishwa tarehe 30 Juni 1987, makao yake makuu yakiwa huko Brazaville, Kongo. Shirikisho hili ni kubwa kuliko vyama vingine vya kimataifa vya utafiti. Katika Mkutano wake Mkuu wa Pili, PUST ilipendekeza sekta mbalimbali za utafiti kama aula muhimu katika kuendeleza Afrika na kwa ustawi wa watu wake, zikijumuisha mada mbalimbali kuanzia madawa asili na taaluma ya mimea ya madawa, hadi matumizi ya amani ya utafiti wa nyuklia (katika kilimo, tiba na uchumi).

Labda chombo cha kiliulimwengu kilicho muhimu kuliko vyote kilichoshughulikia sayansi katika Afrika ni kile cha Programu ya Umoja wa Mataifa ya Mazingira (UNEP) ambacho makao yake makuu yako Nairobi. Shirika hili linahimiza na kukuza utafiti wa ekolojia na hali ya hewa sio tu katika Afrika bali duniani kote. Vita vyake viwili vikuu katika miaka ya 1990 kati ya mambo mengine vinahusiana na ongezeko la joto ulimwenguni na kupungua kwa ozoni, masuala ambayo tutayarejelea hapo baadaye.

Afrika ya baada ya ukoloni Afrika inajaribu kutoka kwenye athari ya kupumbazwa ya utawala wa kikoloni juu ya uwezo wake wa utafiti wa kisayansi na uvumbuzi wa kiteknolojia. Kasi ya kuondokana na athari hizo imekuwa ndogo, ijapokuwa inaonekana. Wanasayansi mashuhuri binafsi wamejitokeza hivi karibuni katika nyanja zote, japo hakuna uwanja au nchi yoyote nje ya Afrika ya Kusini na kidogo huko Misri ambako wamepatikana wataalamu wa kutosha kuweza kukuza sayansi kwa kujitegemea. Wanasayansi wengi wa Kiafrika wanadumu ama kwa vile wanafanya kazi kwenye mashirika yanaopata misaada kutoka nje au wana uhusiano na asasi za utafiti za huko ng'ambo. Wengine hupata mafanikio makubwa katika kazi zao walizofanyia kwenye maabara ya ng'ambo katika miradi ambayo wao wenyewe hawaidhibiti. Matokeo ya utafiti wa wanasayansi wengine hayakuweza kuingizwa kwenye viwanda kwa kuwa viwanda vyenyewe vimefungiwa kwenye teknolojia nyingine zilizotayarishwa tangu awali huko nchi za nje. Wanasayansi wa Kiafrika wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kutokana na ukosefu wa fedha, na vifaa, maji na umeme usioaminika, ukosefu wa vifaa vya kompyuta na njia nyingine za kuwasiliana na wenzi wao, huku wakikabiliwa na hali ya kisiasa inayoyumba. Jambo hili linazidi kudhihirisha dhana ya kuwa sayansi haiendelezwi na wanasayansi pekee bali na jamii nzima kwa ujumla. Kwa hivyo, mwelekeo mkuu wa sayansi katika Afrika ni ule wa kuanzishwa kwa sera ya sayansi katika nchi za Afrika, na kuongezeka kwa mtandao wa taasisi za utafiti ambazo zinaweza

kukuzwa ili kujenga msingi wa kutosha kuweza kusonga mbele. Vituo vinavyotumainiwa, ijapokuwa vina matatizo mengi ni pamoja na vyuo vikuu vya kitaifa, vituo vya kitaifa vya utafiti, asasi za Afrika Yote, vyama vya kitaalamu vya Afrika Yote, na taasisi za utafiti za bara lote na jumuiya za wanazuoni.

## Mchango wa Afrika katika kuendeleza viwanda vya Ulaya

Ni wazi kutokana na ushahidi uliopo kwamba athari ya Afrika kwenye mabadiliko ya teknolojia ya Magharibi katika nusu ya pili ya karne ya ishirini, kama ilivyokuwa kwenye karne zilizotangulia, imekuwa kubwa na ya kina sana kuliko athari ya Magharibi kwenye maendeleo ya viwanda, sayansi na teknolojia katika Afrika.

Viwanda na teknolojia ya Magharibi bado kwa kiasi kikubwa vinategemea aina nyingi za madini kutoka Afrika. Kwa kawaida Dunia ya Tatu inazalisha theluthi moja ya madini muhimu katika uchumi, lakini nchi zinazoendelea zinatumia moja ya ishirini tu ya madini hayo. Mchango wa Afrika kwenye akiba na uzalishaji ni mkubwa sana.

Katika kipindi kinachohusishwa ndani ya juzuu hili, mara nyingine Afrika inakuwa na hadi asilimia 90 ya akiba ya dunia ya kobati, kiasi kikubwa zaidi kikipatikana huko Kongo (Zaire). Wakati mwingine Afrika imekuwa na zaidi ya asilimia 80 ya akiba ya dunia ya kromu, zaidi ya asilimia 50 ya akiba ya dhahabu na karibu nusu ya akiba ya sayari nzima ya platini na karibuni akiba yote ya kile kinachoitwa almasi ya viwanda "isiyo ya kikomunisti". Haya ndiyo madini muhimu ya viwandani.

Kisha yapo madini fuweli ya Afrika, ambayo ni muhimu sana kwa teknolojia. Katika kipindi hiki bara hili limekuwa na hadi theluthi moja ya akiba ya urani ya dunia. Mchango wa Afrika kwenye gesi za asili unapanuka, hasa katika nchi za Afrika ya Kaskazini. Na bila shaka Afrika inawakilishwa vizuri na Nigeria, Algeria, Libya na Gabon kwenye Chama cha Nchi Zinazosafirisha Nje Mazao ya Petroli (OPEC). Ni lazima pia ikumbukwe kwamba Kongo (Zaire) ni chanzo kikuu cha radia inayopatikana kwenye mbale ya urani.

Vito na metali za thamani za Afrika zina manufaa kidogo zaidi kwenye maendeleo ya teknolojia. Kiasi kikubwa cha vito vya almasi ya dunia bado kinatoka Afrika. Katika kipindi hiki kuanzia 1935 Afrika imekuwa na kiasi kisichopungua asilimia 80 cha tantali. Kiasi cha madini ya fedha ya ulimwengu kilichopo Afrika ni kidogo, lakini Afrika ina aina nyingi mbalimbali za mawe ya thamani, kuanzia johari ya rangi ya samawati hadi topazi, malakite hadi opali, rubi hadi tanzaniti.

Mashapo ya metali za Afrika pia yanajumuisha kiasi kikubwa cha manganizi, mbale ya chuma, shaba, vanadiamu (elementi ya kuimarisha chuma cha pua isiyopatikana kwa urahisi), boksiti (mbale kuu ya alumini), risasi na zinki. Kisha yapo mashapo yasiyo ya metali katika Afrika. Akiba kubwa ya fosfati imeenea kutoka Moroko hadi Senegal. Huko Bukini (Madagascar,) Afrika ina mlundikano mkubwa kuliko yote inayofahamika duniani ya mashapo ya vipande vidogovidogo vya grafiti. Na katika kipindi hiki Jamhuri ya Watu wa Kongo imekuwa na akiba ya potashi iliyoonekana kuwa miongoni mwa akiba kubwa zaidi ya madini hayo duniani.

Magharibi, pamoja na kuwa mlaji mkuu wa utajiri wa madini ya Afrika ilikuwa meneja mkuu wa utajiri huo. Kampuni chache cha Kimagharibi ndizo zilizodhibiti usindikaji, utengenezaji na uuzaji wa rasilmali za Afrika. Majina machache yaliyounda awamu hii ya mchango wa Afrika kwenye maendeleo ya teknolojia ya Magharibi ni pamoja na *Anglo-American, DeBeers, Roan Selection Trust* na *Union Minière* ya zamani. Haya yalikuwa mbali kabisa na mashirika makubwa ya mafuta - *Shell, British Petroleum* (BP), *Gulf, Exxon, Mobil, Chevron, Texaco* na mengineyo.

Katika maeneo mawili makuu ya uzalishaji katika Afrika (kilimo na madini) uchimbaji wa madini ndio uliohitaji mtaji na ufundi mkubwa zaidi. Kutokana na ukosefu wa uhawilishaji wa kutosha wa ujuzi wa kiufundi na wa kiuendeshaji kutoka Magharibi kwenda kwa Waafrika, uchimbaji wa madini katika Afrika ulibakia kuwa hifadhi ya watu wa Magharibi peke yao hata pale serikali za Kiafrika zilipomiliki shughuli za uchimbaji.

Wakati mchango wa Afrika kwenye maendeleo ya viwanda huko Magharibi ulikuwa zaidi kwenye biasharanje ya nguvukazi (biashara ya watumwa), Wamarekani ndio waliokuwa waagizaji wakuu wa nguvukazi ya watumwa. Katika awamu hii ya baadaye ya mchango wa madini kwenye teknolojia na maendeleo ya viwanda ya Magharibi kuanzia 1935, Ulaya ndiyo iliyokuwa mwagizaji mkuu. Hata hivyo katika awamu zote mbili, rasilmali za Afrika zilikuwa ndio msingi wa karibu sekta zote za ustaarabu wa kiteknolojia ya Magharibi. Hatima ya yote, mchango wa Afrika kwenye sayansi na tekuolojia ya kipindi hiki unakwenda mbali zaidi kuliko ule wa dunia ya mwanasayansi binafsi wa Afrika. Katika kipindi hiki kuanzia 1935, mchango mkubwa kuliko yote wa Afrika katika uwanja huu unaonekana kwenye athari za nguvukazi na rasilmali za Afrika kwenye viwanda na maabara ya ulimwengu.

Isaac Newton, ambaye hakuwa mnyenyekevu wala mjitwezaji, wakati mmoja alikiri kwamba, akiwa mwanasayansi, aliweza kuona vile kwa sababu alikuwa "amesimama kwenye mabega ya majitu." Si migongo ya wafanyakazi wa Magharibi tu iliyohimili kuongezeka kwa teknolojia ya Magharibi katika awamu ya siku hizi ya sayansi na teknolojia. Kulikuwepo pia na mchango kutoka rasilmali na nguvukazi ya Waafrika na Waasia ehini ya utawala wa Wazungu. Waafrika wamechangia kwenye sayansi ya Magharibi kuanzia kwenye mashamba makubwa ya watumwa huko katika Dunia Mpya hadi kwenye machimbo ya Kimberley.

Hata hivyo, mnamo 1958 Ulaya ya Mashariki ndiyo iliyoanzisha zana za anga kwa Sputniki. Mtu wa kwanza mweusi kwenda katika anga alipaswa kuisubiri Marekani ifikie kwenye mbio za anga. Afrika ilikuwa ikishiriki kwenye kipindi kipya, nusu kupitia rasilimali zake, nusu kupitia diaspora ya watu weusi huko Marekani, na nusu nyingine kupitia vituo vya kuchunguza anga kama kile kilichopo Kenya, na zaidi kupitia kwenye kikundi kidogo, lakini umuhimu kihistoria, cha wanajimu wa Kiafrika. Ustaarabu ulikuwa ukitafuta mpaka mpya wa anasa bunifu - na Afrika ilikuwa ni sehemu ya jitihada hizo.

## Katikati ya kuongezeka kwa joto la ulimwengu na majira ya baridi ya nyuklia

Lakini sambamba na kuongezeka kwa mpumbao wa ulimwengu kuhusu sayari nyingine, kulikuwepo na wasiwasi wa ulimwengu kuhusu usalama wa sayari ya Dunia yenyewe. Mwanzoni utamaduni wa Kiafrika, katika amali zake, uliyahifadhi zaidi mazingira kuliko ambavyo sayansi ya Magharibi inaendelea kufanya.

Baya zaidi, amali za Kiafrika zilizokuwa za kimazingira zaidi zilikuwa zikipigwa vita. Utamaduni asili wa Kiafrika unaanzia kwenye mazingira yanayosema kwamba ni dunia nzima na sio "mtu" peke yake aliyekuwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Na jamii nyingi za Kiafrika ziliyatukuza mambo kadhaa ya asili, wanyama walifanywa vizimu, zilitenga misitu kadhaa na kuifanya makazi ya wahenga. Tamaduni za Kiafrika hazikuweka tofauti kubwa kati ya jamia za wanadamu na zile za spishi nyingine.

Falsafa kama hizi ni za kuhifadhi mazingira — kwa kushirikisha utakatifu na mazingira hayo. Lakini Waafrika wengi waliotekwa na ukoloni waliruhusu amali hizi kuchafuliwa na uanzishaji wa biashara mpya na ufujaji mpya ambao uliingizwa na ubeperi wa Magharibi pamoja na ukoloni. Kwa hiyo mazingira ya Kiafrika

yaliharibiwa kutokana na vitendo vya wageni, na pia ulafi wa wale wanaoweza kuitwa ni wasaliti wa ekolojia. Kilichotia uchungu zaidi ni kumalizika kabisa kwa misitu ya mvua ya Afrika na kuhatarishwa kwa spishi nyingi za wanyama wa Afrika. Ukataji miti bado unachangia kwenye kuongezeka kwa joto la hali ya hewa. Hali ya hewa ya dunia inazidi kuleta wasiwasi inapounganishwa na dioksidi ya kaboni pamoja na gesi nyingine zinazonyonya nishati ya jua.

Katika juhudi ya kurekebisha hali hii, Umoja wa Mataifa uliamua kuweka makao yake makuu ya Programu ya Mazingira ya ulimwengu (UNEP) huko Afrika (Nairobi). Afrika ilikuwa inapambana ili kuchakua upya uongozi wake wa kiadili katika Sayari ya Dunia dhidi ya hatari zote za teknolojia mpya na kutojali kunakoambatana na enzi hizi za viwanda. Baada ya kupuuzwa katika kipindi cha mwanzoni, ilipofikia 1980 UNEP ilianza kuchukuliwa kwa dhati zaidi.

Ni moja ya kejeli za historia ya himaya kwamba hatari za matumizi ya mafriji sasa zimewaandama wanadamu kuhusiana na tabaka la ozoni. Afrika pamoja na maeneo mengine ya Dunia ya Tatu yanakaribishwa kuachana na ujuzi huu mpya mara tu baada ya kuupata. Teknolojia mpya zilizojifunzwa na Afrika na kanda nyingine zinazoendelea nazo pia zinachangia kwenye kuongezeka kwa kiwango cha gesi kama vile monoksidi ya kaboni. Tayari viwango hivi vilishakwishakuwa vya hatari kutokana na athari za viwanda pamoja na ruwaza za ulaji wa dunia ya viwanda.

Hata hivyo ipo hatari nyingine inayoikabidi sayari ya Dunia: ile ya kutokuwepo na kitu kingine zaidi ya majira ya baridi katika umbo la hali ya baridi ya nyuklia. Jamia ya binadamu imeingia katika zama za nyuklia tangu 1935. Ilipofikia kwenye miaka ya 1980 hatari ya kutisha ya kuitumbukiza dunia kwenye majira ya baridi yasiyokoma sasa imeeleweka na idadi kubwa ya jamii ya wanasayansi kote duniani. Vita vya nyuklia vinaweza kumaanisha kuwa sio mwisho wa majira ya baridi bali ni ushindi wa mwisho wa majira hayo. Vita vya aina hiyo vinaweza kuliweka jua mbali zaidi na makazi ya watu kuliko kulisogeza karibu nao.

Mwaka 1960 Kwame Nkrumah alihisi hatari ya sayansi hii mpya, lakini alikuwa na wasiwasi wa jinsi ambavyo Afrika ingetakiwa kukabiliana na suala hilo. Nkrumah alionyesha hasira kali wakati Ufaransa ilipolitumia jangwa la Sahara kwa ajili ya majaribio yake ya nyuklia, na alishikilia kwa nguvu mali zote za Wafaransa zilizokuwa nchini Ghana.

Lakini Kwame Nkrumah aliishi katika kipindi ambapo iliaminika kuwa ingewezekana kutofautisha kati ya elimu "salama" ya nyuklia kwa madhumuni ya

amani na teknolojia ya nyuklia ya hatari kwa ajili ya vita[15]. Kwa kuongozwa na fikra hizi, Nkrumah alianzisha programu ya utafiti wa nyuklia katika nchi yake mwenyewe. Alitangaza kwamba ni lazima Afrika iingie katika kipindi cha nyuklia na kujifunza sayansi na teknolojia yake mpya. Alidai pia kwamba uchaguzi wa ujamaa ni lazima uoanishwe imara na moyo wa kisayansi. Kwa Nkrumah ujamaa ulikuwa ni falsafa ambayo wakati huohuo ilitakiwa pia knwa sayansi. Kwa maneno yake mwenyewe "ujamaa bila sayansi ni bure[16]."

Jaribio la Ghana la kuingia katika kipindi cha atomi lilikuja baada ya Kongo (Zaire). Wabelgiji walikuwa wameshaanzisha utafiti wa tanuri la nyuklia mwishoni mwa miaka ya 1950 katika nchi ya Kongo. Kongo ilipopata uhuru wake na kuitwa Zaire utafiti huo uliendelea na watendaji Waafrika wa kisayansi waliongezeka. Pamoja na mabadiliko yote yaliyoikumba jamii ya Kongo katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, utafiti wa nyuklia bado unaendelea huko Kinshasa.

Huko Nigeria Raisi Shehu Shagari (1979-83) pia alihimiza nchi yake yenyewe kuanza kufuatilia suala la nyuklia. Tofauti na Kongo na Ghana, utawala wa Shagari kwa kiasi fulani ulitetea uchaguzi wa nyuklia kutokana na sababu za kivita. Kwa maoni ya Shagari bado kulikuwepo na kiungo kati ya ubaguzi wa rangi na tishio la nyuklia. Katika siku za Nkrumah tishio la nyuklia lilikuwa huko kaskazini, katika Sahara, wakati tishio la ubaguzi wa rangi lilikuwa huko Kusini, Afrika ya Kusini. Lakini ilipofikia kipindi cha Raisi Shagari matishio yote mawili yalionekana huko Kusini. Ubaguzi wa rangi ulikuwa umepata uwezo wa kinyuklia. Shagari aliliona suala la Nigeria kufukuzia teknolojia ya nyuklia kama sehemu ya jibu dhidi ya ongezeko la nguvu za nyukilia za Afrika ya Kusini kuanzia miaka ya 1970 na kuendelea.

Hata hivyo maendeleo ya sasa yanatufanya tuisaili maana inayotolewa na Afrika katika knikumbatia teknolojia ya nyuklia. Zaidi ya hayo, ni kwa namna gani Afrika itapendekeza uendeshaji wake wa jadi wa mazingira uliokuwa wa kujinyima na wa kuheshimu maumbile, na hivyo kuvutia dunia nzima upande wake ili kuzuia ukumbatiaji zaidi wa amali za Magharibi, ili kuhakikisha kuwa sayari yetu inaendelea kuwepo?

Je, uhusiano wa maelewano wa Waafrika na hali ajili unaoelezewa bila haki yoyote kama "desturi za kabla ya sayansi," unaweza kushawishi watu kukataa matokeo

[15] K. Nkrumah, 1961, uk. 213

[16] Tazama Ghana Today, Juz. 8, Na. 21, 1964, uk.1

ya ustaarabu wa kujiangamiza na kukubali sera ambazo zinatupilia mbali tishio la majira ya baridi ya nyuklia? Kama historia inalo somo la kufundisha, basi somo hilo ni kwamba Magharibi haiwezi kuendelea kuipuuza Afrika, elimu na uwezo wake, bila kuathirika.

## Sayansi watu na sayansi-jamii

Athari ya Afrika kwenye sayansi watu na sayansi jamii imechukua miundo miwili. Athari moja inajikita kwenye upekee wa bara la Afrika lenyewe, na mvuto wa bara hili kwa wanazuoni na wanasayansi kutoka duniani kote. Athari nyingine imetokana na michango ya watafiti na wanasayansi jamii wa Kiafrika, ambayo imesukuma mbele mipaka ya elimu na nadharia kwa pamoja.

Mvuto wa kisayansi wa Afrika ulijumuisha mvutano wa tamaduni zake kwa wanaathropolojia, wa kijamii na kiutamaduni, mafumbo ya visukuku kwa wanaakiolojia, na changamoto za mapokeo simulizi kwa wanahistoria. Kwa kujifunza Afrika, dunia imejifunza mengi kujihusu yenyewe, na spishi ya binadamu imejifunza kuhusu hulka yake na vyanzo vyake.

Kilichosukuma mbele mipaka ya sayansi jamii na sayansi watu sio Afrika kama chombo cha taaluma tu. Msukumo umetoka pia kwa wanasayansi na watafiti wa Kiafrika wenyewe.

Kwa namna moja sayansi jamii zipo katikati ya sayansi ya vitu halisi kwa upande mmoja na falsafa kwa upande wa pili. Nadharia nyingi za kijamii zinaendelea miongoni mwa wanasosiolojia, wachumi, wanasayansi, wanasiasa na wengineo na zinafanya kazi kama daraja kati ya masuala ya wanasayansi ya mambo asili na yale ya wanafalsafa. Sura hii kwa kiasi fulani inajihusisha na sayansi jamii kwa kuangalia wajibu huo wa daraja kati ya sayansi na falsafa.

Afrika imetoa uwanja muhimu kwa ajili ya utayarishaji wa nadharia kuu kuhusu ukuaji wa uchumi katika jamii zisizokuwa na maendeleo makubwa ya viwanda katika karne ya ishirini. Diaspora ya Waafrika imejipambanua zaidi katika nadharia ya uchumi huria - kwa kumrejelea Sir Arthur Lewis kutoka St. Lucia katika Visiwa vya British West Indies, ambaye alishinda Nishani ya Nobeli ya sayansi na uchumi katika mwaka 1979 (akishirikiana na Mmarekani mmoja, Theodore W. Shiltz). Mafanikio ya Lewis yalikuwa katika taaluma ya maendeleo na uchumi - hususani nadharia yake iliyounganisha masharti ya biashara ya Kaskazini-Kusini na viwango lingamishi vya tija ya nguvukazi katika nchi za viwanda na zile zenye maendeleo kidogo ya viwanda.

Katika nadharia ya uchumi wa msingi, Samir Amin wa Misri alikuwa mtangulizi katika miaka ya 1970 katika kudadisi hali ya ubadilishanaji wa uchumi usiolingana katika ulimwengu ambapo ubepari umeenea kote duniani. Mara nyingi kazi ya Samir Amin ilikuwa ni mchanganyiko wa kusifika wa nadharia halisi na data ngumu za kijarabati kutoka nchi kama vile Cote d'Ivoire.

Adebayo Adedeji wa Nigeria alichukua msimamo wa katikati ya nadharia ya uchumi wa wapenda maendeleo ya wastani na ya wale wenye msimamo mkali. Akiwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika (ECA), katika miaka ya 1970 na 1980 Adedeji aliyasaili mawazo ya kawaida ya kawaida ya kiuchumi ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kuhusu sababu za kudumu kwa maendeleo duni katika Afrika. Yeye na ECA walisisitiza vizingiti vya kiulimwengu dhidi ya maendeleo ya Afrika. ECA ikishirikiana na Umoja wa Nchi Huru za Afrika ilitoa uchanganuzi wa uchumi wa msingi kwa ajili ya Mpango wa Utekelezaji wa Lagos, ambao ulipokelewa mwaka 1980 na Wakuu wa Nchi za Kiafrika.

Katika sayansi ya siasa Afrika ilitoa changamoto katika ujenzi wa taifa, uundaji wa dola, utegemezi wa kisiasa, maendeleo ya kisiasa na kudhoofika kwa kisiasa. Nadharia za kimataifa kuhusiana na mambo yote haya katika kipindi cha baada ya ukoloni zimeathiriwa sana na matatizo na mafanikio ya uzoefu wa Afrika. Nadharia za chama kimoja, mahusiano ya jeshi na raia, falsafa za ujamaa asili, vyote kwa pamoja vimechangamshwa sana na ukweli wa siasa za Afrika.

Ni vema kukumbuka kwamba Kwame Nkrumah alichapisha kitabu chake cha *Ukoloni Mamboleo: Hatua ya mwisho ya Ubeberu* kabla ya kupinduliwa mwaka 1966. Na Ali Mazrui aliendeleza mawazo yake kuhusu "Utegemezi Mamboleo na Kumegukameguka kwa Afrika" katika tasnifu ya Udaktari wa Falsafa (D.Phil) ya Chuo Kikuu cha Oxford katika miaka ya 1960 na kuyachapisha katika kitabu chake kilichofuata cha *Kuelekea Amani ya Afrika Nzima (1967)*[17].

Afrika ilikuwa maabara kubwa zaidi ya taaluma ya lugha. Ikiwa na moja ya kumi ya idadi yote ya watu duniani, Afrika ina karibu robo ya lugha zinazozungumzwa duniani licha ya kuwa chimbuko la lugha yenyewe ya binadamu. Lugha katika karne ya ishirini ni kutoka lugha za toni kama vile Kiyoruba hadi lugha kama vile Kixhosa, kutoka lugha za Kisemiti kama vile Kiamhariki na Kiarabu hadi Kibantu cha Kusini kama vile Kindebele na Kichewa[18].

[17] Tazama K. Nkrumah, 1966; na A.A. Mazrui, 1967.

[18] Papua New Guinea inatambuliwa sana kuwa na idadi kubwa ya lugha mbalimbali kwa kila maili moja ya mraba, duniani – lugha nyingi kati yao zikiwa na wazungumzaji wachache tu.

Kuanzia 1935 wanazuoni wasio Waafrika waliokuwa na maoni kuhusu uainishaji wa lugha za Kiafrika ni pamoja na M. Guthrie wa Uingereza na J.H. Greenberg wa Marekani. Wanazuoni kama vile Guthrie na Greenberg walilazimika kusimama juu ya mabega ya wanaisimu wa Kiafrika[19].

Idadi ya lugha za wenyeji zinazozungumzwa katika Afrika inakadiriwa kuanzia mamia hadi kwenye maelfu kwa kiasi fulani kutegemea na pale ambapo lahaja moja inadhaniwa kuishia, na lugha nyingine tofauti kuanzia.

Idadi kubwa ya Waafrika wanasema zaidi ya lugha moja. Jambo hili pia linaleta mvuto wa taaluma ya isimu-jamii. Afrika pia ni maabara ya taaluma ya sera ya lugha na muungano wa kitaifa. Wanazuoni kama vile Pathé Diagne wa Senegal na Muhamad Hassan Abdulaziz wa Kenya ni miongoni mwa waliochangia sana kaatika mjadala wa kitaaluma kuhusu mambo haya[20].

Anthropolojia ya kijamii na ya kiutamaduni ilianza kama somo kwa upande mmoja kutokana na msisimko wa taaluma ya jamii za Kiafrika. Vitabu cha Jomo Kenyata *Kukabiliana na Mlima Kenya* kilichochapishwa 1938 kilikuwa ni hatua kubwa katika kuunda upya ethnolojia ya Kiafrika. Katika kampasi za vyuo vya Afrika neno "anthropolojia" bado lilikuwa halijajitanzua kutoka sifa zake hasi za awali za kuwa ni "sayansi ya taaluma ya jamii zisizostaarabika." Vyuo vingi Vikuu vya Afrika vinapendelea istilahi ya "sosioloji" ili kuwakilisha kwa pamoja jamii za viwanda na zile za kabla ya viwanda. Lakini mipaka ya eneo hili zima la sayansi jamii imepanuliwa na changamoto zinazoletwa na ukweli wa jamii za Kiafrika.

Mapokeo simulizi ya Afrika yamechokoza sayansi za historia katika kutafuta njia za kunufaika kutokana na upokezaji wa ushahidi huu usioandikwa. Huenda hakuna ukanda mwingine wowote duniani uliosaidia zaidi kupanua mbinu anuwai za historia kuliko Afrika.

Hasa kwa vile tamaduni nyingi za Kiafrika hazikuwa zimeandikwa, taaluma zake zilidai uchunguzi na aina tofauti za habari zilizohifadhiwa. Mapokeo simulizi, ushahidi wa kiisimu, mbinu mpya za kiakiolojia — vyote kwa pamoja vilifikia viwango vya juu vya mchangamano kutokana na changamoto ya Afrika.

Kabla ya kipindi cha juzuu hili, tayari *Egyptology* (taaluma ya Misri ya Kale) ilishakuwa sayansi wazi kwa haki yake yenyewe. Hakuna nchi yoyote duniani isipokuwa Misri mbayo iliwahi kulazimisha sayansi kubuni taaluma maalumu kwa ajili ya masomo yanayohusu maisha ya nyuma ya nchi hiyo[21].

Lakini ilikuwa hasa katika kipindi hiki cha baada ya 1935 ambapo paleontolojia na paleanthropolojia vilipata mafanikio ya kuvutia katika Afrika ya Mashariki. Utafiti katika Tanzania, Kenya, Ethiopia na kwingineko umerudisha uelewa wa binadamu nyuma zaidi kuelekea asili za spishi kuliko ilivyoweza kufanyika hapo kabla. Jina la akina Leakey huko Kenya limekuwa jina la kawaida

kimataifa, Lakini nyuma ya jina hilo mashuhuri upo msururu wa jeshi la wanapaleontolojia, wanaakiolojia na wanapaleanthropolojia wakishughulikia mawanda ya ushahidi uliohitaji uangalifu kuhusu asili ya spishi pekee iliyokuwa ikijifunza maisha yake ya nyuma.

Taaluma jamii ya spishi nyingine pia imekwenda mbali zaidi katika Afrika kuliko ilivyofanya katika ukanda mwingine wowote duniani. Uchunguzi kuhusu sokwe na nyani — viumbe waliokaribia sana ubinadamu — umefanyika kwa tahadhari kubwa ukiwa na matokeo ya kuvutia kwenye maeneo kama vile Rwanda na Kongo (Zaire). Kwa kuwaelewa vizuri zaidi nyani, je tunajifunza zaidi juu ya binadamu? Kwa mara nyingine tena Afrika imetoa vielelezo vya kuifundisha jamia ya binadamu kujihusu yenyewe. Wanazuoni wa Magharibi kama vile Jane Goodall wamekuwa washirika bora wa kisayansi katika taaluma ya ndugu wa mwituni wa *Homo Sapiens*.

Kipindi cha baada ya 1935 pia kimeshuhudia changamoto mpya kwenyc nadharia za Wazungu kuhusu ni nani aliyekuwa wa kwanza kuvuka Atlantiki. Je, alikuwa Christopher Columbus - ama walikuwepo manahodha wa Kiafrika kabla yake? Changamoto hii kuhusiana na kielelezo cha Columbus imetoka Afrika na pia kwenyc diaspora wa Waafrika. Ivan Van Sertima ndiye aliyeongoza changamoto hii ya mtawanyiko. Akiwa amezaliwa Guyana, Van Sertina aliifanya athari yake ya kitaaluma isikike huko Marekani. Kitabu chake cha 1977 - *"Walifika Kabla ya Columbus Kuwepo kwa Waafrika katika Amerika ya Kale" (They came before Columbus: The African Presence in Ancient America)* kilichapishwa katika matoleo zaidi ya kumi. Manahodha wa Van Sertina wa kabla ya Columbus walihusishwa hasa na Bonde la Nili na Mediterania. Ushahidi wake ulitofautiana, ukianzia na sanaa za "Kiafro" za uchongaji za mawe za kabla ya Kristo zilizopatikana Meksiko zenye mfanano mkubwa na sura za "Kinegro"[22].

Changamoto ya moja kwa moja ya bara la Afrika dhidi ya kielelezo cha Columbus katika kipindi hiki (tofauti na changamoto ya Diaspora) inadai kuwa manahodha wa Kiafrika wa Kabla ya Columbus walitoka Afrika Magharibi na

[20] Tazama Sura 18.

[21] UNESCO Historia Kuu ya Afrika, imeelezea zaidi sulubu na mbinu za histori ya Kiafrika. Kamati ya Kimataifa ya Sayansi ya majuzuu haya ya UNESCO ina wajumbe ambao ni wagunduzi wa methodolojia katika uwanja wa fasihi simulizi, wanahistoria wa kiisimu na wanaakiolojia.

[22] Tazama 1 Van Sortima, 1984, ambacho kina baadhi ya picha za "Africoid".

siyo Bonde la Nili na Mediterania. Pathé Diagne, mwanazuoni kutoka Senegal alianzisha mradi mmoja katika miaka ya 1980 kutafiti, kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Cornell, dhima ya Bakari II katika kuivuka Atlantiki, hasa kabla ya 1312. Nadharia yake tete ilikuwa kwamba safari za Mansa Bakari II na zile za Christopher Columbus zilihusiana.

Lakini hatupaswi kutia msisitizo mkubwa kupita kiasi kwenye tofauti kati ya nadharia za Diaspora za kabla ya Columbus, zinauotaja manahodha kutoka Bonde la Nili, na nadharia za Afrika kabla ya Columbus zinazotaja manahodha wa Afrika Magharibi. Mnamo 1962 chombo rasmi cha Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo ya Watu wa Rangi (NAACP) huko Marekani kilichapisha makala ya Harold G. Lawrence yenye kichwa cha habari *"Wapelelezi wa Kiafrika Katika Dunia Mpya" (African Explorers of the New World)*. Katika makala hayo Lawrence alimrejelea Abubakari II wa Mali na kusema aliwaajiri manahodha wa Kiarabu na kuwapatia armada ya meli na mabaharia Waafrika ili kujaribisha bahati zao huko Magharibi. Suala la Waafrika kuvuka Atlantiki kabla ya Columbus bado kabisa kufikia hatima yale, na huenda ikawa vigumu kuthibitishwa kikamilifu. Lakini maelezo mibadala ya vichwa vya mawe vya Kinegro vilivyopatikana huko Meksiko kabla ya Kristu nayo pia hayajatoa ushawishi wa kutosha.

Wakati mara nyingi historia na sayansi za jamii zimejaribu kuelezea asili ya vitu, mara nyingine fasafa na dini zimekabiliana na tofauti kati ya kitu chenye mwisho na kile kisicho na mwisho, kati ya kitu chenye kikomo na kile kinachodumu milele, kati ya kitu chenye mwanzo na kile ambacho labda hakina mwanzo. Sasa tuziangatie imani na falsafa hizi zisizoeleweka kwa urahisi.

## Katikati ya vyanzo na "mwisho wa wakati"

Je, maendeleo haya yote ya kihistoria na ya kisayansi yamekuwa na athari gani kwenye falsafa katika kipindi hiki cha historia ya Afrika? Kama ni Columbus au Bakari "aliyevumbua Dunia Mpya" je, ni kwa namna gani matarajio ya mwisho wa dunia yalivyoathiri mawazo ya kifalsafa katika Afrika — bila kujali kuwepo au kutokuwepo majira ya baridi ya kinyuklia?

Kwa ujumla wazo la "mwisho wa dunia" limekuwa na umuhimu mkubwa zaidi katika Afrika ya Uislamu kuliko lilivyokuwa nje ya eneo hilo. Uislamu una dhana ya Kiama - siku ya kifo cha ulimwengu wote, itakayotangulia siku ya Hukumu. Uislamu pia una dhana ya *Akhir al-Saman*, yaani mwisho wa wakati.

Kusema kweli Ukristo una dhana inayofanana na dhana hii ya Kiislamu, lakini dhana hizi za Kikristo zimekuwa na athari ndogo zaidi katika Afrika zinapolinganishwa na zile za Kiislamu. Sababu moja inaweza kuwa ni ile ya kiwango cha juu cha falsafa ya majaliwa ambacho Uislamu umekiweka katika Afrika — upotoshaji wa dhana ya *Inshallah.*

Dini asili ya Waafrika inajihusisha zaidi na mwanzo wa wakati kuliko mwisho wake. Uhenga ni muhimu zaidi kuliko hitimisho. Kila utamaduni wa Kiafrika unaongozwa na visasili viwili vya msingi — kisasili cha chanzo na kisasili cha madhumuni ya pamoja. Kisasili cha mwanzo kwanza kinajumuisha jamii — Chimbuko la Kiafrika. Kisasili cha madhumuni ya pamoja kinaipatia jamii hisia za upekee wake na malengo yake katika historia.

Kilicho dhahiri ni kwmba kisasili cha Kisemiti (Chimbuko kulingana na Biblia na Korani) kimeendelea kuleta changamoto kwenye visasili vya wenyeji wa Afrika juu ya uhenga kwa mfano wa Kintu akiwa kama Muganda wa kwanza au Mumbi kama Mkikuyu wa kwanza. Kwa asili Muganda wa kwanza au Mkikuyu wa kwanza ndio waliokuwa wanadamu wa kwanza. Lakini dhana ya Adam na Eva imepunguza sana hadhi ya waasisi wa Afrika wakati ambapo sayansi ya Magharibi tayari ilikuwa katika hatua ya kukubaliana na hoja kwamba kisayansi Afrika ndipo mahali asili kwa spishi za binadamu. Sasa visasili vya Kiafrika kuhusu asili vinafedheheshwa na dini za Magharibi wakati uleule ambapo Sayansi ya Magharibi inaonyesha kwamba lazima bustani ya Eden ilikuwa Afrika.

Mara nyingine visasili vya dini za Kiafrika vinapendekeza kwamba Mungu ana mwanzo — lakini hana mwisho. Hili si tofauti sana na nadharia za kisayansi zinazohusiana na vyanzo vya ulimwengu. Nadharia ya "Kishindo Kikuu" kuhusu chanzo cha ulimwengu inaashiria kuwepo kwa mwanzo — lakini si lazima kuwepo na mwisho. Kile kinachoanzishwa si lazima kiwe na mwisho; kile kinachozaliwa sio lazima kife.

Nadharia ya Kikristo ya kuzaliwa kwa Yesu ina ukinzani zaidi. Yesu alizaliwa. Lakini je, angeweza kufa hata katika kipindi hicho cha kipekee cha muda wa siku tatu wakati wa Pasaka? kama alikufa na kufufuka, je, kifo cha mtoto wa Mungu kinaweza kutokea tena?

Visasili vingi vya mwanzo katika Afrika vinajumuisha asili ya kifo chenyewe. Kisasili cha huko Sierra Leone kilielezea kwamba hapo kale kifo kiliishi pamoja na Mungu, na kiliendelea kumsihi Mungu akipatie uhuru wake. Lakini Mungu alikuwa amemwahidi binadamu kwamba ijapokuwa kifo kilikuwa kimeruhusiwa

kuja duniani, Binadamu asingekufa. Yalikuwepo mambo mawili ambayo Mungu alitakiwa ayashughulikie kukiruhusu kifo kwenda popote pale kilipotaka kwenda, na kumlinda Binadamu. Mungu aliamua kumtumia Binadamu ngozi mpya ambazo zingemkinga dhidi ya elementi hizo na kumwokoa kwenye kifo. Lakini mjumbe aliyetumwa kupeleka ngozi hizo aliviziwa njiani na nyoka ambaye aliiba ngozi hiyo. Je. nyoka huyo alikuwa ni kifo mwenyewe aliyejificha ndani ya umbo la nyoka? Binadamu alichelewa sana kugundua kwamba ngozi za kumkinga dhidi ya kifo zilikuwa zimeibwa njiani.

Bila shaka hadithi kama hii ilisimuliwa kabla watu wa Sierra Leone hawajafahamu chochote kuhusu tabaka la dunia la ozoni. Huenda wana haki ya kuangalia chanzo chao cha kisasili hiki kama ubashiri. Sasa binadamu atahitaji lile tabaka la ziada la ngozi ambalo Mungu alikuwa amepania kumpatia ili kumkinga dhidi ya kifo. Bado binadamu anaendelea kumlaumu nyoka aliyemvizia mjumbe yule aliyetumwa kumpelekea ngozi kutoka kwa Mungu.

Kisasili hiki cha Sierra Leone ni mwangwi wa kisasili cha Kisemiti kuhusu kuanguka kwa Adamu kwa matumizi maalumu ya nyoka. Shetani, kama kifo katika kisasili cha Kiafrika, hapo mwanzoni aliishi na Mungu na kisha akataka kuondokana naye. Kilichofanywa na kisasili cha Sierra Leone ilikuwa ni kuunganisha dhana ya shetani na dhana ya kifo kwenye kiumbe kimoja. Katika Chimbuko la Kibiblia kwa upande mwingine, Shetani alikuwa chombo cha kuleta kifo kwa jamii ya binadamu.

Lakini Mungu katika mwanzo pia alimtaka Binadamu "kuujaza ulimwengu na kuutiisha." Binadamu alifanywa bwana wa dunia na viumbe wake wote. Sayansi ya kisasa pamoja na tekuolojia vilimwezesha binadamu "kutiisha" dunia na viumbe wake wote.

Dhamira za umilele na kutokuwa na kikomo zimekuwa ni sehemu ya falsafa ya Kiafrika kuanzia "mwanzoni mwa wakati." Bila shaka kumekuwepo na mwendelezo pamoja na mabadiliko katika uzoefu wa falsafa ya Afrika. Sasa tutazame zaidi mwelekeo mahsusi wa kifalsafa katika miaka hii.

## Mikondo mitatu ya falsafa

Kuanzia 1935 falsafa ya Kiafrika inaweza kuwekwa kwenye kategoria au mikondo mbalimbali. Katika sura hii maainisho yenye uhakika zaidi ni yale ya kiutamaduni, kiitikadi na ya kihakiki. Kila moja ya shule hizi ina tabia inayojidhihirisha wazi -

japo ni vema kutilia maanani kwamba maainisho haya ni kwa ajili ya kufanyia uchanganuzi na huruhusu kiasi kikubwa cha kuingiliana.

Shule ya falsafa ya msimamo wa kiutamaduni imejikita kwenye mapokeo ya asili. Mara nyingine huitwa "ethno-falsafa", lakini tunapendelea istilahi ya "falsafa ya kitamaduni" hasa kwa vile ni sahihi zaidi katika hali hii. Kufungamana kwa sehemu kubwa kwa falsafa hii na kabila fulani (kama falsafa ya Walugbara) ni sifa mojawapo ya falsafa hii. Falsafa ya utamaduni ina mwelekeo mkubwa zaidi wa ujima, na inaenezwa zaidi na mapokeo simulizi. Lakini suala la ujima halipaswi kupigiwa chuku sana. Walikuwepo pia wavumbuzi binafsi. Mkusanyiko huu wa mawazo ya Kiafrika ni wa kisosiolojia — ukizingira maisha ya jamii fulani, kanuni zinazoiongoza na urithi wa hekima ya wahenga wa vizazi vyote, pengine ukiongozwa na watu binafsi wenye sifa za kipekee.

Kama huko Magharibi falsafa inaanza kwa wazo na sayansi jaribati inaanza kwa mguso, falsafa ya utamaduni katika Afrika haionyeshi tofauti kali kati ya wazo na mguso. Kama tulivyogusia hapo awali, hoja kamili kuhusu jambo moja katika falsafa ya utamaduni ya Afrika linasema:

> Tunahisi
> Kwa hivyo tuna***fikiri***
> Kwa hivyo tuna***ishi***.

Kwa upande wa wakati, falsafa ya mwelekeo wa kiutamaduni katika Afrika inajumuisha kipindi cha kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na hata kipindi cha baada ya ukoloni. Inaweza kuelezewa kama mapokeo ya falsafa ya zamani na ya kudumu zaidi kuliko yote katika Afrika.

Lakini kwa madhumuni ya sura hii tunatofautisha kati ya utamaduni na itikadi. Hapa tunazingatia maana finyu ya itikadi, kuwa ni mkusanyiko wa mawazo, yanayoelekezwa kwenye sera, ambayo yamelenga katika kutawala utekelezaji wa kisiasa ma kuelezea malengo ya kisiasa. Kwa vyovyote utamaduni hujumuisha itikadi — na falsafa ya mwelekeo wa kiutamaduni kwa maana yetu hujumuisha malengo na matendo ya kisiasa. Bali utamaduni, ni maisha yote kwa jumla na sio tu katika medani ya mahusiano ya kisiasa. Shule ya falsafa ya kiutamaduni ya Afrika inajumuisha mambo kama vile mahusiano kati ya binadamu na kiasili, kati ya watu hai na mizimu, kati ya mume na mke, na pia kati ya watawala na raia katika zile jamii za Kiafrika ambazo kwa asili zilikuwa na watawala waliotambulika.

Mkondo wa kiitikadi wa fikra za Kiafrika ni finyu na wa kisiasa zaidi. Mkondo huu umejikita hasa kwenye ukoloni na kipindi baada ya ukoloni — na hujumuisha fikra za *"udhamiri"* za Kwame Nkrumah hadi za kitabu cha viumbe *"Waliolaamiwa"* cha Franz Fanon. Mawazo au falsafa za aina hii hazikujitokeza sana wakati wa kabla ya ukoloni. Mawazo ya kiitikadi katika maana hii yanatokana na ukoloni na maisha baada ya ukoloni. Falsafa ya utamaduni inaelezwa katika lugha za wenyeji. Falsafa ya kiitikadi katika Afrika Nyeusi zaidi inaelezwa katika lugha za Wazungu.

Kama tulivyoonyesha, falsafa ya kiutamaduni ni ya kiujima na ya malimbikizo. Jadi hii haitegemei watu binafsi mashuhuri wenye kufikiri. Wako Ma-plato, Ma-Locke, Ma-rousseau na Ma-Hegel wachache sana katika Afrika. Mkondo wa falsafa ya utamaduni kwa kawaida ni mtiririko wa hekima ya pamoja inayojilimbikiza kupitia vizazi vingi.

Falsafa ya kiitikadi katika Afrika ya kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni inamkuza mtu binafsi kama ndiye chemchemi ya mawazo. Sasa falsafa ya Kiafrika inaanza kufunzwa zaidi kama mawazo ya watu binafsi kama vile Amikar Kabral na Gamal 'Abd al Nasser' badala ya kuwa falsafa za makundi vya kiutamaduni kama vile Wazulu au Waberiberi.

Kama falsafa ya kiutamaduni ni maalumu kwa kabila mahsusi (kwa mfano falsafa ya Wayoruba), falsafa ya kiitikadi ina mwelekeo wa kuwa maalumu kwa Afrika, katika maana ya kujumuisha Afrika kama kitu kimoja au uzoefu wa watu weusi duniani kote. Kwa maneno mengine, wakati chemchemi ya falsafa ya kiitikadi ni nyembemba zaidi kuliko ile ya falsafa ya kiutamaduni (fikra ya mtu binafsi badala ya busara ya pamoja), mada yake ni pana zaidi (kwa vile inajumuisha kwa pamoja Afrika na watu weusi badala ya kikundi kidogo cha kabila fulani).

Labda thamani kuu ya falsafa ya kiutamaduni ni utambulisho. Yale mambo mengine yote yanaimarisha kujitambua na kujitambulisha, kwa mfano kama Wawolof. Kwa upande mwingine, upeo wa thamani ya falsafa ya kiitikadi umeelekea kwenye ukombozi. Miongoni mwa wanafikra wapo wanaohusisha ukombozi na Afrika Yote, na wengine wanaohusisha ukombozi na uwezo asilia wa watu weusi. Bila shaka zipo amali nyingine zinazotoa mchango katika suala hili. Lakini kutokana na hali ya athari ya ukoloni katika historia ya Afrika kwenye kipindi hiki, msisitizo wa kisiasa wa itikadi ya Afrika ulijikita kwenye ukombozi.

Ijapokuwa hatutakiwi kuchanganya jambo hili na upopulisti (mfumo wa kisiasa unaojali maoni na fikra za umma), kimsingi falsafa ya kiutamaduni ni falsafa ya

umma. Falsafa hii mara nyingi sana inakuwa na mawazo yanayoeleweka kwa watu wa kawaida. Falsafa hii inaelezwa katika lugha zinazoeleweka kwa raia wa kawaida, lugha za asili za Kiafrika. Ingawa kuna msigano hapa na pale, kwa mfano fikra ya Ogotommeli ya Wadogon, hasahasa falsafa ya kiutamaduni inahusu maisha ya kawaida yanayojulikana, yanayoweza kueleweka na mwanaume au mwanamke wa kijijini.

Kwa upande mwingine, falsafa ya kiitikadi kimsingi ni ya wasomi, hata pale inapojaribu kujifananisha na umma wa kawaida. Amikar Kabral alijitambulisha na Waafrika wa kawaida kabisa, Franz Fanon aliwanyanyua wafanyakazi wa tabaka la chini kabisa na kuwafikisha kwenye kiwango cha juu cha kuheshimika kuliko ilivyokuwa imefikiriwa na Karl Marx ambaye aliwashuku. Pamoja na hayo yote, si Marx, Fanon wala Kabral anayeeleweka kwa mwanakijiji wa kawaida huko Burkina Faso au miongoni mwa Wakarimojong wa Uganda. Mawazo ya Marx na Fanon ni mazungumzo miongoni kwa waali wa Kiafrika wanaoishi mijini na wanaofuata amali za Magharibi.

Tatizo la msingi la mawazo ya kiitikadi kwa Afrika linaendelea kuwa ni lugha zinazotumika kuielezea falsafa hiyo. Wakati kwingineko kote sayansi jarabati inaanza kwa zile hisi tano (kugusa, kuona, kunusa, kusikia na kuhisi) falsafa ya kiisimu mara nyingi inajishughulisha na njeo tano (iliyokuwepo, iliyopo, itakayokuwepo, inayopaswa kuwepo na itakayodumu milele).

Katika Afrika kilicho muhimu zaidi ya falsafa ya lugha ni lugha ya falsafa. Sehemu kubwa kupita kiasi ya itikadi za kipindi cha ukoloni na zile za baada ya ukoloni imo katika lugha za Kizungu. Taaluma rasmi ya falsafa katika vyuo vikuu vya Kiafrika inaendeshwa kwa lugha za watawala wao wa kikoloni — Kiingereza, Kifaransa, Kireno na nyinginezo. Wanafikra wengi mashuhuri katika Afrika ya leo — kuanzia Edward Blyden hadi P.J. Hontonji wamefanya mazungumzo yao ya msingi kwa lugha za Kizungu. Tofauti kubwa inajitokeza kwenye nchi za Kiafrika zinazozungumza Kiarabu.

Kwa upande wa wanafikra wa Kiafrika waliopata msukumo wa itikadi za nje, ni vigumu sana kiisimu-jamii kwa Mwafrika kubobea sana kwenye Umarx bila kupata athari kubwa za Magharibi. Mwafrika anajifunza lugha yake ya kwanza ya Kizungu sio tu kwa kutaka kupata ujuzi wa lugha bali kama sehemu ya mchakato mkubwa wa kielimu wa kuingizwa katika utamaduni wa kigeni.

Ni utumwa huu wa lugha ambao umeifanya falsafa ya kiitikadi katika Afrika kuwa ya kisomi pamoja na kwamba imani ya falsafa hiyo inapinga kabisa nadharia

za utawala wa tabaka aali. Sehemu kubwa ya falsafa ya watu kama vile Edwardo Mondlane ilitetea ukombozi na ilijihusisha kimaadili na watu wa kawaida wa Afrika. Lakini falsafa nyingi za kiitikadi kwa bahati mbaya zilijijengea kizuizi cha kiisimu ambacho kilizitenga na watu wa kawaida. Hiyo ndiyo tofauti ya kimsingi zaidi baina ya mkondo wa falsafa ya kiutamaduni ya Kiafrika (iliyoenezwa kwa njia ya masimulizi kwa lugha za wenyeji) na mkondo wa falsafa ya kiitikadi (iliyoenezwa kwa maandishi, kwa kutumia lugha za Kizungu).

Sehemu ya Afrika iliyozungumza Kiarabu haikutegemea sana lugha za Kizungu. Kiarabu kilijaza pengo hilo. Kitabu cha *Falsafa ya Mapinduzi* cha Abd al-Nasser kiliandikwa kwa Kiarabu. Katika Afrika inayozungumza Kiarabu imekuwa vigumu kutenga falsafa ya kiutamaduni na ile ya kiitikadi kutoka kwenye dini. Mambo yaliyohusu Msikiti na hakimu, kanisa na serikali, yote yalijitokeza waziwazi.

Falsafa ya kiitikadi huko Moroko katika kipindi hiki ilijumuisha mambo yaliyohoji kama katika Uislamu kulikuwa na dhana iwezayo kulinganishwa na haki ya kiungu ya wafalme. Kilichosisimua zaidi ni ile *fatwa* (maoni ya kisharia) ya Shekh al-Islam Moulay al-Arbi Alawi iliyotolewa Desemba 1963. Aliamuru kwamba uhalali wa mfalme utategemea kama alipata madaraka hayo kupitia shura (ushauri) na kwa kibali cha Umma (jumuiya ya waumini). Fatwa ilikuwa changamoto ya moja kwa moja kwa kanuni ya kurithi utawala na sifa za utambulisho za mfalme Hassani II wa Moroko. Mijadala kuhusu hali ya uhalali wa ufalme imekuwa ikiendelea tangu wakati huo[23].

Huko Libya ufalme ulipinduliwa Septemba 1969. Wakati Muammar Kadhaffi alipoanzisha "mapindduzi yake ya kiutamaduni" mnamo 1973, alijaribu kukomesha tofauti kati ya itikadi na utamaduni. Alianzisha falsafa ya Libya iliyoitwa "Nadharia ya Tatu ya Ulimwengu" iliyojumuisha Umoja wa Kiarabu — Kiislamu, ujamaa wa Kiarabu — Kiisalamu na demokrasia ya umma wa Libya.

Tunisia iliupeleka mjadala kuhusu usasa na mapokeo katika mawazo ya Afrika ya Kaskazini kwenye hatua za juu zaidi. Kwa namna fulani, Tunisia ilikuwa inaendeleza ubishani ulioanzishwa kuhusu uislamu wa kisasa kwenye kizazi cha nyuma na Muhannad Abduh wa Misri na mwalimu wake Jamal al Din al Afghani. Hata hivyo kwa kejeli, Habib Burguiba wa Tunisia hakufuata nyayo za Abduh wala za Afghani. Tamaa ya Burguiba ilikuwa ni kuunda upya Tunisia kwa sura ya

[23] J. Benomar, 1988, uk. 550-1. Tazama pia M.W. Suleiman, 1989, uk. 16-27.

mapinduzi ya Kifaransa. Kwa kutaka kupunguza dhima ya Uislamu katika jamii ya Tunisia, Burguiba alifungulia wazi mbubujiko wa mawazo ya falsafa na maandishi kuhusu ushindani kati ya usasa na mapokeo, kati ya Magharibi na uislamu. Kwa mara nyingine tena falsafa ya kiutamaduni na ya itikadi ziliungana katika jamii ya Kiafrika[24].

Tapo la tatu la falsafa ya Kiafrika baada ya zile za kiitikadi na kiutamaduni ni ile ya kihakiki. Kama ilivyo ile ya mkondo wa kiitikadi, shule ya kihakiki pia ni zao la kipindi cha ukoloni na cha baada ya ukoloni. Matapo yote mawili kimsingi yanatumia lugha za Kizungu na pia yameathiriwa sana na mapokeo ya elimu ya Magharibi.

Lakini, wakati tapo la kiitikadi lina uelekeo wa kimakusudi wa kisiasa, lile la kihakiki lina mwelekeo finyu zaidi wa kitaaluma. Wakati tapo la kiitikadi linajihusisha zaidi na ukombozi, lile la kihakiki limalenga zaidi kwenye maadili ya kiagnostiki (yasiyoamini kuwepo na mtu anayezijua habari za Mungu) au yasiyozingatia amali yoyote. Wakati mara nyingi tapo la kiitikadi lina mwelekeo wa kitaifa, lile la kihakiki linalenga kwenye urazini peke yake.

Tapo la kihakiki katika falsafa ya Kiafrika nalo pia lina dhana ya "ukombozi" — lakini kinachotakiwa kukombolewa ni falsafa yenyewe na siyo Afrika. Operesheni ya Wokozi inatakiwa ili kuikomboa falsafa ya Afrika kutoka ethnolojia (kama ilivyo kwenye falsafa ya kiutamaduni) na kutoka kwenye itikadi (kama ilivyoelezewa).

Tapo la kihakiki linatamani kuirudisha falsafa kwenye mtazamo wa kisayansi. "Pambano na kitu halisi" kimsingi ni ashirio la kutumia vipimo vya urazini. Fumbo lenyewe ni kwamba falsafa ya kihakiki pia ni mwaliko wa kutumia kiasi fulani cha ujarabati - kigezo cha kugusa katika maana maalumu ya uhalisia.

Wanafalsafa wa Kiafrika wa tapo hili la kihakiki ni pamoja na F. Crahay, B,F. Eboussi, P.J. Huntonji, K. Anthony Appiah, M. Towa na S. Adotevi. Kwa kiasi fulani tamaa yao ni kuifanya falsafa ya Kiafrika kuwa ya kisayansi zaidi, yenye nidhamu zaidi na kali zaidi. Wametangaza vita dhidi ya kile Huntonji (akishirikiana na wanaumiundo) alichokiita "utokuwaza".

Hata hivyo kuna shule nzima ya mawazo katika kipindi hiki cha Historia ya Afrika ambayo inajivunia kile tunachokiita "utovusayansi". Tayari tulisharejelea salamu za Aimé Césaire kwa

... Wale wasiovumbua baruti wala dira
Wale ambao hawakudhibiti gesi wala umeme
Wale ambao hawakuvinjari bahari wala anga ...

Mawazo ya Magharibi yana mkondo mzima mdogo wa kitu kinachoitwa "falsafa ya sayansi." Kinachojumuishwa katika ajenda ya Kiafrika ni kile kinachoweza kuitwa falsafa ya utovusayansi. Sasa yafaa tuugeukie mkusanyo huu wa amali za falsafa ya Kiafrika.

## Falsafa ya Utovusayansi

Tayari tulishaona jinsi mapinduzi ya viwanda ya huko Ulaya yalivyoisukuma sayansi mbele ya teknolojia yake - na hivyo kuchapusha hatua za mabadiliko ya kijamii na ya viwanda. Baada ya kupata ushindi wa kusifika katika teknolojia, Ulaya ilianza harakati za kuitiisha dunia.

Kiburi cha kiutamaduni cha Ulaya kiliathiri utu wa Mwafrika na wakati mwingine kilipotosha aula za falsafa ya Kiafrika. Shule moja ya mawazo ya Kiafrika ilichagua kusisitiza kwamba kabla ya kuingia kwa Wazungu Afrika ilikuwa na ustaarabu wake changamani ambao Wazungu waliuona kama halali na muhimu — ustaarabu ambao zilitoa wafalme wakau, miliki za kuvutia na ujuzi wa teknolojia anuwai. Shule hii ya mawazo ya Kiafrika iliiangalia Misri kama ustaarabu wa Kiafrika na kusisitiza michango ya Misri kwenye miujiza ya baadaye ya Uyunani ya Kale. Kujitolea nafsi kitaalamu kwa Sheikh Anta Diop ili kuonyesha kwamba ustaarabu wa Misri ya Kale haukuwa tu wa Kiafrika bali wa mtu mweusi kulisababisha kuwepo kwa shule hii mashuhuri ya mawazo sio tu katika Afrika bali pia miongoni mwa Waafrika waliotawanyikia huko Amerika.

Shule hii ya falsafa ya Kiafrika tunaweza kuiita falsafa ya njozi ya utukufu. Falsafa hii inatamani kusisitiza zama tukufu katika historia ya Afrika.

Kinyume na falsafa ya njozi ya utukufu ni kile tunachoweza kukiita njozi ya kupenda ushenzi. Hiki ndicho kitu kinachoishughulisha falsafa ya utovusayansi. Hapa msisitizo sio katika kupata mafanikio ya utukufu, bali ni katika kufanikisha ukawaida; sio katika ukuu wa historia ya Afrika, bali maadili ya kijiji; sio katika wajenzi wa ngome za Afrika bali katika wafugaji wa Afrika.

Unegro wangu siyo mnara wala kanisa kuu
Unajikita ndani katika udongo mwekundu[25]. (Aimé Césaire, 1969).

Kama Jan-Paul Sartre alivyodokeza, kushangilia huku ya kwamba mtu hajaweza kutengeneza baruti au dira, au kujenga minara au makanisa makubwa, ni madai ya kuonea fahari "ukosefu wa ufundi." Kwa viwango vyetu utovusayansi ni jambo la kusifika. Mwaka 1963 Sartre alisema, "Kile kinachoweza kuonekana kama upungufu kimekuwa chanzo chanya cha utajiri[26]."

Ngozi ya utakufu kama falsafa inasisitiza dhima ya Afrika katika historia ya sayansi na mafanikio ya kiteknolojia. Lakini Leopold Senghor anaona kuwa ndizo chimbuko la kipaji cha Afrika ni hisi — silika, hekima ya tajiriba tuvu, na silika zilizoelimishwa na historia. Silika ya kibinadamu ni mwongozo mzuri kwa tabia kuliko kompyuta sahihi ya yenye usahihi zaidi.

Njozi ya utukufu ina mwelekeo wa kuheshimu staarabu za kisomo. Sera ya utamaduni ya Nkrumah akiwa Raisi wa Ghana mara nyingine ilijaribu kudai kwamba kila mafanikio ya historia ya sayansi na utamaduni kabla ya kuundwa kwa kompyuta yalikuwa na asili ya Kiafrika. Sera ya utamaduni ya Nkrumah ilikuwa ni ya njozi ya utukufu ya waziwazi.

Njozi ya utukufu ni tawi la historiografia ya Kiafrika iliyotukuzwa. Ina mwelekeo wa kukubali amali za Kizungu wakati huo huo ikitupilia mbali "taarifa" za Wazungu kuhusu Afrika. Mwelekeo wa utukufu ni mwepesi kupokea imani ya Magharibi ya kwamba jamii zinazoheshimika sio za "kikabila" na zina mifumo ungamifu ya kisiasa, yenye wafalme na miundo ya kihimaya, yenye kumbukumbu za matofali na chokaa, na mwishowe zikiwa zimejikita kwenye mfumo wa kanuni ya dola. Kwa mwelekeo wa falsafa ya utukufu, ni tusi kuziita jamii za Wakarimajong au za Wabarabeg "jamii zisizo na serikali," hapa tena kuna kukubali kigèzo cha Magharibi cha heshima ya kisiasa (dola ndiyo kigezo hasa).

Kinyume chake, falsafa ya utovusayansi inakataa amali za Magharibi lakini inakumbatia habari "taarifa" za Magharibi. Inakataa kigezo cha Magharibi kinachohusu ustaarabu wa kuheshimika - minara, makanisa makuu au dola — na kukubali maelezo ya Magharibi kuhusu Afrika yasemayo kwamba Afrika ni nchi isiyo na sayansi wala teknolojia iliyoendelea. Hata hivyo njozi ya ushenzi hujivunia kutokuwa na utovusayansi, wakati Magharibi hudharau hali hiyo.

[25] Kama hapo juu. Tazama pia A.A. Mazrui, 1986, uk. 72-6

[26] J.P. Sartre, 1963, Sehemu hii ya uchanganuzi

Kuelekea kwenye falsafa ya utamaduni mtambuko (wenye kuvuka tamaduni nyingi) Fikra hizi ndizo zinazounganisha falsafa ya utovusayansi na mapokeo ya Rousseau ya "Mshenzi Mwungwana" kwa upande mmoja na mawazo ya Mahatma Ghandhi kuhusu ustaarabu kwa upande wa pili.

Wanafalsafa wa Kiafrika wa mrengu wa utovusayansi hawajavutiwa na mafanikio ya kiteknolojia ya Magharibi. Wanafikra hao wa Kiafrika wamegundua hisi imara zaidi za maadili miongoni mwa wanavijiji wa bara la Afrika wanaojishughulisha na teknolojia kwa kiwango kidogo sana. Mawazo ya Rousseau kuhusu athari mbaya na za kupotosha za utamaduni wa viwanda, yakiunganishwa na falsafa ya Gandhi ya ufumaji, yanafanana sana na mwelekeo huu wa ukale katika mawazo ya Afrika ya leo. Kukutana kwa unegro, Ugandhi na mawazo ya Rousseau kuhusu "mshenzi mwungwana" ni eneo mojawapo la falsafa ya utamaduni mtambuko.

Tunaehopaswa kukumbuka ni kwamba mielekeo yetu mitatu ya asili ya falsafa ya Kiafrika - utamaduni, itikadi na uhakiki — bado haijapata mipaka ya kudumu. Mara nyingi mawazo ya Kiafrika ya Uislamu na mawazo ya Kiafrika ya Ukristo yamevuka utamaduni na itikadi kwa maana yetu.

Utamaduni mtambuko wa kilimwengu unajumuisha athari za Umarx-Lenin kuhusu mawazo asili ya ujima. Wanafikra wa Kiafrika kama vile Senghor na Nyerere walisisitiza kwamba Ujamaa wa Kiafrika haudaiwi chochote na mapambano ya kitabaka. Mara nyingi swali limeulizwa endapo dhana ya "tabaka" ilikuwa na asili yoyote ya Kiafrika au la. Je, kwa nini lugha nyingi za Kiafrika hazina neno la "tabaka"?

Tafsiri za Kiafrika za usasa katika mawazo ya Uislamu pia ni sehemu ya utamaduni mtambuko. Miongoni mwa wanafikra wa kwanza wa Kiislamu wa Kiafrika katika nusu ya pili ya karne ya ishirini ni mwanateolojia wa Sudan, Mahmoud Muhammad Taha. Dhana yake kuhusu uwili wa Ujumbe wa Ufunuo wa Kiislamu ilikuwa ni mtambuko wakati zaidi kuliko mtambuko utamaduni. Taha alifanya jitihada za taaluma za kupatanisha maadili ya jamii ya karne ya ishirini na moyo wa enzi za kale za mtume Muhammad. Alitoa hoja kimtambuko wakati anatoa hoja kwamba ujumbe mmoja wa Mtume ulilengwa tu kwa wafuasi wake wa wakati wake (Waarabu wa karne ya saba) na ujumbe wa pili wa Kiislamu ulilengwa kwa kipindi chochote kile. Siri ya uchaji wa kweli wa Mungu sio tu kutambua uwili wa mtambuko wakati wa ujumbe wa Kiislamu bali pia ni kuweza kutofautisha kati ya jambo maalumu la kihistoria la karne ya saba na lile ambalo

kwa kweli ni la milele. Mohmoud Muhammad Taha aliilipia ghali bidaa yake ya kisomi ya mtambuko wakati. Utawala wa Gaffar Nimeiri wa Sudan ulimnyonga kwa kukufuru na kukana dini mnamo 1985.

Wanamawazo wengi wa Kikristo katika Afrika wamesonga mbele zaidi ya kutafsiri Injili. Mara nyingi wameongoza katika kutafsiri upya ustaarabu wa utamadini mtambuko wa Afrika. Katika uwanja huu ushindi wa kusifika ulifika na kitabu cha Padre Tempel, *Falsafa ya Kibantu*. Kilikuwa juu ya mtazamo wa mawazo ya mapokeo yanavyoonekana huko nje. Mtazamo wake kiasi ulikuwa wa utetezi, lakini kimsingi ulikuwa ni Ukristo wa Kizungu. Tempel alirithiwa na shule nzima ya wafafanuzi wa Kikristo wa urithi wa wahenga wa Afrika. Mara nyingine Ukristo wa msingi wa waandishi umepotosha Uafrika wao - na ulichora sura ya urithi asili kwa mtazamo wa Kikristo.

Licha ya mtazamo wa Kikristo na ule wa Kiulaya, hakuna shaka yoyote kwamba jitihada za Waafrika walioingia Ukristo za kufafanua urithi wa wahenga weusi zilisaidia sana katika kuufanya urithi huo wa kiutamaduni ueleweke katika sehemu nyingine duniani. Vitabu kama kile cha John Mbiti *Dini na Falsafa za Kiafrika* vimetafsiriwa katika lugha mbalimbali kuanzia Kijapani hadi Kifini, lakini mara chache sana kwenye lugha za Kiafrika. Tumerudi tena kwenye tatizo la lugha ya falsafa katika Afrika, kitu kilichotofautiana sana na msisitizo wa Waingereza kwenye falsafa ya lugha.

Kwa kauli ya utamaduni mtambuko, Julius Nyerere ni bingwa wa falsafa za siasa za Kiafrika. Ameandika falsafa nyingi kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili. Amejaribu kuvunjilia mbali vikwazo vya lugha baina ya falsafa ya utamaduni wa wahenga na mwelekeo mpya wa itikadi ya kipindi cha baada ya ukoloni. Ameruhusu lugha zote kutajirishana kwa vile mawazo ya lugha zote yamepitia katika taamuli yake.

Dhana yake ya ujamaa kama msingi wa usoshalisti wa Kiafrika yenyewe ilikuwa ni wazo bora la mpito wa utamaduni mtambuko. Kwa asili dhana ya *ujamaa* ilimaanisha umoja wa mbari. Lakini Nyerere aliibadilisha kutoka kwenye kanuni ya hatari ya upendeleo wa kimbari na kuifikisha uzito uliovuka ule wa neno la Kizungu la "usoshalisti". Kimatendo kanuni zake za ujamaa hazikufanikiwa - kutokana na sababu za nje na za ndani. Lakini, kama msomi, Nyerere ni mtu mwenye mawazo asilia.

## Hitimisho

Sura hii imeanza kwa kauli ya kwamba mchango wa Afrika katika sayansi na teknolojia haupaswi kupimwa tu kwa kuangalia shughuli za wanasayansi na wahandisi wa Kiafrika. Athari za ukanda huu zinajumuisha dhima ya nguvukazi ya Waafika na rasilmali halisi katika mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni. Madini muhimu ya bara hili yalitumika katika viwanda na kuchochea maabara ya ulimwengu wa Magharibi sio tu katika kipindi cha baada ya 1935 bali pia kwa vizazi vingi vilivyotangulia[27].

Utawala wa kikoloni wenyewe haukuwa na rutuba ya kutosha kustawisha sayansi na teknolojia ya asili. Shule za kikoloni zilifanikiwa kuwapatia Waafrika wawili Nishani ya Nobel ya Fasihi (Soyinka na Mahfuz), Nishani mbili za Amani (Lithuli na Tutu), Nishani ya Nobel ya uchumi kwa Mwafrika wa diaspora (Arthur Lewis) — lakini hakupatikana mshindi wa Kiafrika kwa nishani yoyote katika tawi la sayansi asilia. Shule za kikoloni zilikuwa ni maabara yenye ufanisi mkubwa katika taaluma za kijamii, lakini maabara hayo hayakuwa karakana zenye ufanisi katika sayansi na teknolojia[28].

Kwa upande mmoja, madini ya Kongo (Zaire) kama vile kobalti, yaliweza kuendesha injini za jeti za huko Magharibi wakati ambapo hakukuwepo na chanzo kingine cha bidhaa hiyo nje ya Afrika. Ni kwa njia hii ambapo ukoloni wa Magharibi katika Afrika ulichochea mabadiliko ya teknolojia huko Magharibi - huku ukizuia maendeleo ya aina hiyo hiyo ndani ya Afrika yenyewe.

Mara nyingi vita ni mama wa uvumbuzi. Mara nyingine vita vya ukombozi katika Afrika vilisababisha kuzaliwa kwa mifumo ya kusifika ya teknolojia ya kati. Vita vya Mau Mau vya miaka ya 1950 vilisababisha kutengenezwa kwa silaha za kwanza za moto huko msituni. Katika vita vya wenyewe kwa wenyewe huko Nigeria, upande wa Biafra ulionyesha ustadi mkubwa katika ufaraguzi wa teknolojia. Biafra ilitoa mifano ya kukumbuka ya magari ya deraya na vifaru — nusu.

Katika uwanja wa falsafa, ukoloni ulisaidia kukuza matapo ya kiitikadi na yale ya kihakiki, yote yakiwa na athari kubwa ya Magharibi, na yakieleza kwa lugha za Kizungu. Tawi halisi la zamani kuliko yote la falsafa ya wenyeji ni lile la kiutamaduni — ambalo mizizi yake imejikita katika mitazamo na fikra za wenyeji. Kwa hakika, kwamba falsafa ya kiutamaduni katika Afrika katika kipindi hiki cha

[27] Kwa maingiliano ya ustaarabu ya kale zaidi, soma J.G. Jackson, 1970

[28] Kulikuwa na wawekezaji na wagunduzi weusi wa viwango chini ya kategoria ya tunzo ya Nobel. Tazama, kwa mfano, J.A. Rogers, 1972

baada ya ukoloni inapatikana kwa njia ya masimulizi na ya maandishi pia, ni ya kiungu na ya kidunia, na vyanzo vyake viko katika dhana na lugha za kienyeji za Afrika[29].

Nyuma ya mielekeo yote hii lipo swali muhimu tulilouliza mwanzoni mwa sura hii. Je, kutawaliwa kisiasa kumekuwa na maana gani kwenye dhima ya Afrika katika maendeleo ya sayansi na falsafa? Ni vigumu kukadiria gharama na faida katika uwanja wa sayansi na teknolojia. Kwa jumla, si wanasayansi wa Kiafrika ambao wamekuwa na athari kubwa zaidi kwenye sayansi na teknolojia ya ulimwengu. Rasilimali za Afrika pamoja na wafanyakazi wa Kiafrika ndio walionufaisha viwanda vya nchi za nje.

Kwa upande wa falsafa, ukoloni unaweza ukawa umeanzisha mchakato ambao baadaye ungekuwa wa manufaa, na tayari urithi wa kikoloni umeshaanzisha jitihada hiyo maalumu. Leo shauku yetu kwa Fanon, Kabral, Nkrumah, Senghor na Gamal Abd al-Nasser ni sehemu kamili ya mchakato huo.

Tayari shule ya mrengu wa kihakiki inajishughulisha na dhana maalumu kama zile za "kipindi baada ya usasa" na "utenguzi" na matatizo ya kijamii yaliyofafanuliwa kwa uangalifu kama "hali ya kipindi cha baada ya ukoloni." Wanamawazo kama vile Kwame Anthony Appiah na Nkiri Nzugwu ni miongoni mwa kikosi cha mbele cha upeo huu mpya wa kisomi.

Kwa hakika karne ya ishirini na moja itasherekea falsafa hii ya kihakiki ya Afrika — falsafa rasmi yenye nidhamu na kali.

Je, Waafrika ni watu wa kihistoria? Ni jambo la kushangaza kwamba hadi katikati ya nusu ya pili ya karne ya ishirini Waafrika wamelazimika kujenga utambulisho wao kama watu wenye rekodi ya mambo yao ya kale, na wenye kale inayostahili kurekodiwa.

Je, Waafrika ni watu wenye falsafa? Labda mshangao utakuwa mkubwa zaidi kwenye jambo hili — kwani hata Waafrika wenyewe wamegawanyika kuhusu jibu la swali hili. Mkondo wa kihakiki katika falsafa ya Kiafrika unakaribia sana kusema kitu kinachofanana na hiki:

Labda kwa sasa kuna kiasi fulani cha falsafa ya Kiafrika. Lakini huko nyuma hakukuwepo na kitu kama hicho. Kulikuwepo na kutoa falsafa kuhusu Afrika ambako kulifanywa na Wazungu. Kilichokuwepo ni ethnolojia, na ethnolojia sio mada ya kifalsafa.

[29] Tazama UNESCO, 1985-6.

Je, Waafrika ni watu wa sayansi? Kwa mara nyingine tena Waafrika wamegawanyika katika suala hili. Wanaunegro, wanawavulia kofia wale ambao hawakuvumbua dira wala kompyuta, ilihali Sheikh Anta Diop alikaribia sana kuhusisha sayansi yote ya maana na kazi ya akili ya Mwafrika.

Ni wazi kwamba kipindi cha makubaliano katika Afrika kinafikia mwisho wake. Hii ndio maana ya kelele zote hizi za wanazuoni. Bara lenye dukuduku linapata mambo mapya ya kubishania na imani mpya za kujadili. Vielelezo kadhaa vya zamani vinakufa - na vipya ndio viko chunguni vinapikwa. Labda hii ndiyo masuala ya sayansi na falsafa.

# 22 Mabadiliko ya Elimu na Jamii

## Utangulizi

Elimu ni njia ambayo jamii inaongeza maarifa yaliyo muhimu kwa ajili ya kuishi na kujihimili na huyafikisha maarifa hayo kwa kizazi kingine, hasa kwa kuwafundisha vijana wao. Inaweza kuwa kwa njia zisizo rasmi majumbani, kazini au kwenye michezo. Lakini kwa kawaida, huwa ni rasmi na hutolewa katika maeneo yaliyochaguliwa kwa ajili ya kuwaongoza vijana na kwa ajili ya kuwaadilisha watu wazima. Vijana hufunzwa ili wapate maarifa, stadi na kukuza vipaji kwa ajili ya kuendeleza na kulinda asasi za msingi na maadili ya jamii, pamoja na kuyabadili ili yaweze kulingana na mabadiliko ya hali na changamoto mpya zinazojitokeza.[1]

Katika Afrika kabla ya ukoloni, kama tulivyoona katika majuzuu yaliyotangulia, kulikuwa na mifumo mbalimbali ya elimu iliyotimiza haja hii katika sehemu mbalimbali za bara hili. Kulikuwa na aina kuu tatu za elimu zilizojulikana sana elimu ya wenyeji, elimu ya Kiislamu na ile iliyoitwa ya Ukristo wa Afrika, yaani mila za Kikristo za awali zilizoendelea kuwepo Ethiopia na miongoni mwa Wakopti wa Misri.[2] Katika mila za Waislamu na za Wakristo wa Afrika, jamii iliheshimu sana kujua kusoma na kuandika na mafunzo kwa jumla, yalisaidia kufunua maajabu ya Korani takatifu na Maandiko Matakatifu, na yalikuwa yakifunzwa hasa kwa watawala na viongozi wa dini tu, makundi mawili ya watu walioheshimiwa zaidi katika jamii. Vinginevyo, tamaduni zilibaki kuwa za masimulizi zaidi. Juhudi za wamisionari wa Ulaya na wa Marekani kueneza ukristo katika karne ya kumi na tisa ziliamsha ari ya kupata

[1] P.C. Lloyd, 1972 uk. 160 kwa msisitizo. Waandishi wanaushukuru mchango wa Mary Achatz, Chuo cha Elimu, ChuoKikuu cha Michigan, Ann Arbor, Marekani

[2] A.A. Mazrui na T.G. Wagow, 1985; J.F.A. Ajayi, 1985

elimu ya Kimagharibi. Ilipanua mawanda ya kujua kusoma na kuandika si kwa lugha za Kizungu tu, bali pia lugha kadhaa za Kiafrika, nyingi zikiandikwa kwa mfumo ulioundwa kwa mara ya kwanza kwa kutumia herufi za kirumi, na hivyo aghalabu zikishinda majaribio ya awali ya kuandika baadhi ya lugha hizo kwa herufi za Kiarabu.

Kuenea kwa kusoma na kuandika lugha za Kiafrika kuliongeza uwezekano wa mabadiliko ya kijamii kwa idadi kubwa ya watu waliojua kusoma na kuandika lugha za Kiafrika na kuleta mageuzi kutoka utamaduni uliotegemea sana masimulizi na kuwa ule unaotegemea maandishi. Wakati wa ukoloni, hata hivyo, uwezekano huu ulivizwa, na badala yake umuhimu wa kundi dogo la watu waliojua kusoma na kuandika lugha za Kizungu ulisisitizwa. Ni ujuzi wa lugha za Kizungu ndio uliompatia mtu kazi ya utarishi, ukarani, ufundi stadi na mara chache kazi za kitaalamu. Kiwango cha uwezo katika elimu na lugha za Kizungu kikawa ndio alama mpya ya cheo, na aghalabu, hicho kililingana na kiwango cha mapato na mamlaka ya kazi inayohusika katika jamii.[3]

Kwa hivyo, ilipofika 1935, elimu ya magharibi ilishinda mifumo yote ya elimu ya kabla ya ukoloni katika umuhimu wake. Katika elimu ya magharibi, elimu ya lugha za Kizungu ilikuwa na umuhimu zaidi kuliko elimu ya lugha ya Kiarabu au lugha nyingine za Kiafrika. Elimu ya magharibi ikawa kipengele kimojawapo cha uundaji wa matabaka, kilichoelekea kuwatenga wasomi walioelimishwa magharibi na umma ambao mara nyingi ulidharauliwa kama "wajinga" au "wasiojua kusoma na kuandika" na hiyo ilikuwa licha ya usanii mkubwa wa tamaduni simulizi zilizotumiwa katika ujuzi wa matumizi anuwai ya maneno, hasa kutokana na toni za lugha nyingi zinapozungumzwa. Kwa tawala za kikoloni, elimu ya Kimagharibi ikawa silaha yenye nguvu ya kuingiza utamaduni mpya, kuzifinyanga akili za wasomi walioelimishwa magharibi kupenda aina fulani za utamaduni wa Kizungu kama vile nguo, chakula, sheria, mifumo ya serikali na bidhaa zinazotoka Ulaya. Kwa kupitia elimu ya Kimagharibi, na kushinikizwa na sheria za kikoloni kuhusiana na ndoa, mirathi, na umiliki wa ardhi, pamoja na mafunzo ya Kikristo kuhusu kuwa na mke mmoja, wasomi walishawishiwa kuondokana na mfumo wa kijumuiya wa jamii za kimila za Kiafrika, na kuelekea katika mfumo mpya wa ubinafsi, familia ya baba, mama na watoto wao tu, mali binafsi na kujilimbikizia mali. Wasomi walianza kutojua sana na kutojali juu ya historia, mawazo ya kidini, nguo, mapishi,

[3] M.Bray *na wenzake*, 1986, Sura 4, kurasa 58-78.

sanaa, muziki na hata maisha kwa jumla ya Kiafrika, ambao walibakia kwa kiasi kikubwa katika miji mikubwa lakini wakiendelea kutawala maisha katika vijiji pia.

Lakini bado, kama tulivyoona katika sura nyingine katika juzuu hili, ni wasomi haohao wa elimu ya magharibi, wakiwa wamejitenga kiasi fulani na umma, ambao walikuwa katika nafasi ya kuongoza mapambano dhidi ya ukoloni, kueleza manung'uniko ya umma wa wakulima vijijini na yale ya vyama vya wafanyakazi, wanawake wafanyabiashara na wasio na ajira mijini. Kwa hakika, wakoloni walikuwa wamepiga chuku juu ya kiwango cha kujitenga kwa wasomi na wasomi walithibitisha hivyo mara kwa mara, hasa pale wale wanaogombea uongozi wa siasa walipokabiliwa na haja ya kuonyesha umaarufu wao na uwezo wa kushinda au kupata kuungwa mkono na umma. Kiwango cha elimu ya magharibi na ujuzi wa lugha za magharibi ulikuwa ni kipengele muhimu cha kuweza kukubaliwa na umma. Hasa, elimu ya magharibi iliwawezesha viongozi wa kitaifa kuvuka mipaka ya ukabila inayowekwa na lugha za Kiafrika na kujaribu kuzungumza kwa niaba ya watu wote waliozungumza lugha mbalimbali na wa mataifa mbalimbali waliokuwa ndani ya mipaka ya nchi zilizotengwa na wakoloni. Hapo ndipo walipowapita viongozi wa kijadi, kwa mfano, ambao ndio walikuwa washindani wao wakuu katika kuwarithi wakoloni, lakini wao waliweza kujieleza hasa kwa watu wa makabila yao tu. Hivyo kutokea kwa mawazo yaliyoelezwa na Awolowo mwaka 1947 kwamba wasomi, ingawa ni wachache mno, ndio waliokuwa wanaielewa siasa na "... hawa walumbi wachache ndio waliopangiwa kutawala ..."[4] Kiwango cha elimu ya magharibi, aghalabu kikichanganywa na kipindi cha kusafiri au kusoma ughaibuni, kiliwapa viongozi kadhaa waliokuwa wasomi mtazamo wa Afrika yote ambao uliwaunganisha na viongozi wengine wa Afrika, na mtazamo huu ulikuwa ni kipengele kingine muhimu cha mapambano ya utaifa.

Hivyo, viongozi wengi wa kitaifa walithamini elimu yao, na waliona katika elimu hiyo silaha kubwa ya ujenzi wa taifa na mageuzi ya kijamii ili kupata ukombozi wa fikra dhidi ya ukoloni na kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi. Baadhi ya wasomi wangependa kutoa hoja juu ya ufanisi wa elimu kama njia ya kuleta mageuzi ya kijamii: kulingana na Marl Marx, "Si ufahamu wa watu unaongoza maisha lakini ... kuishi kwao katika jamii ndiko kunakoleta ufahamu."[5] Viongozi wa kitaifa, hata hivyo, hawakuwa na wasiwasi huo. Katika Afrika ya kikoloni, aina na

[4] Katika *The Path to Nigerian Freedom* [Njia ya Uhuru wa Nigeria] kama ilivyonukuliwa na B. Davidson, 1978, uk. 197.

[5] K. Marx, 1859, tafsiri ya N.I. Stone, 1904, uk. 11.

kiwango cha elimu hakikuamua ufahamu wa watu, bali pia nafasi yao katika jamii na mtindo wao wa maisha. Viongozi wa kitaifa waliona msisitizo wa mafunzo ya ufundi na urekebishaji wake ili yakubaliane na hali ya Afrika ilikuwa ni njia tu ya kuendeleza malengo ya unyonyaji wa tawala za kikoloni. Ni msisitizo wa namna hiyo ndio uliozaa "elimu ya Wabantu" ya Afrika Kusini. Wasomi waliona kuwa elimu ya kimagharibi iliyosisitiza uwezo wa kitaaluma ingeweza kuwapatia Waafrika maarifa na welewa unaohitajika katika kuzifanya jamii za Kiafrika kuwa za kisasa, utaalamu wa kazi unaotakiwa katika huduma za kikoloni, na kuwafunza warasimu wa Kiafrika watakaochakua nafasi ya maofisa wa kikoloni.[6]

Hivyo mahitaji ya vyombo bora zaidi vya elimu vilipewa umuhimu mkubwa na vyama vyote vya kitaifa vya Afrika. Msisitizo ulikuwa katika kupanua elimu ya msingi, uboreshaji wa shule za sekondari na vyuo vya Afrika. Viongozi wa siasa walifahamu kuwa kama elimu ingetumiwa kuondoa fikra za kikoloni na kuleta maendeleo ya kiuchumi, mfumo uliorithiwa kutoka kwa tawala za kikoloni hauhitaji tu kupanuliwa na kuimarishwa bali pia kurekebishwa na kufanywa ufae mahitaji ya jamii za Kiafrika za baada ya ukoloni. Hivyo historia ya elimu kote Afrika

[6] E. Ashby na M. Anderson, 1966, hasa kurasa 236-47.

katika kipindi cha hivi sasa inazungukia katika masuala mawili ya upanuzi na urekebishaji. Wakati madhumuni ya upanuzi yalikuwa wazi, mpango wa urekebishaji ulikuwa tata na mgumu zaidi kufikiwa kuliko ilivyofikiriwa katika shamrashamra za baada ya uhuru.

## Kuendelea kufaa kwa mifumo ya kabla ya ukoloni

Sababu moja ya wasomi wa magharibi kutojitenga kabisa na umma, licha ya elimu ya mishemi na shinikizo nyingine za mifumo ya kikoloni, ni kuendelea kwa jadi za elimu za kabla ya ukoloni kupitia mafunzo ya majumbani na kwenye dini. Athari ya nyumbani haikuweza kufutwa kabisa na kwenda shule kulikotokea baadaye kwani katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya maisha, mtoto wa Kiafrika alikuwa karibu sana na mama yake na kwa kawaida mama alimfunza mwanawe lugha yake pamoja na maadili ya utamaduni wake. Hata pale ambapo mama mwenyewe alikuwa amepitia elimu na mawazo ya kidini ya kigeni, msingi aliokuwa nao katika utamaduni wake unaweza kuwa umedhoofika, lakini si kupotea kabisa.[7] Pili, mahitajio ya kidini kwa jamii, hasa katika maeneo ya Kiislamu na Ukristo wa Afrika, zilihitaji kuendelea kwa mifumo ya elimu ya kijadi. Kwa kweli hakukuwa na mfumo wa elimu ya kikoloni uliokatiza mfumo wa elimu ya kijadi katika familia na Kanisa la Ethiopia. Kanisa la Othodoksi liliendelea kuratibu na kusaidia asasi nyingi za elimu ambazo zimebakia kuwa msingi wa maisha ya Waethiopia kiutamaduni, kiroho, kisomi, kisanii na kisayansi.[8] Katika ngazi ya awali, kulikuwa na *Nebab Bet* (shule ya kusoma), ambako familia chache za watawala na wengineo waliokuwa na matumaini waliwapeleka watoto wao, hasa kuwa watawa na makasisi. Wanafunzi wengi walikuwa wanaume na ni baadhi tu ya wale waliofaulu ndio waliokwenda *Quedasse Bet* (Shule ya Vitabu na maandiko matakatifu), na ni wateule wachache tu waliomaliza masomo magumu ya theolojia na falsafa. Mchakato wote huo ulikuwa wa miaka 28, na ulikuwa wa kazi ngumu na ulihitaji kujinyima. Hata hivyo, wale waliofanikiwa kufikia hali hiyo ya taaluma ya hali ya juu walionewa wivu na wenzao, waliheshimiwa na jumuiya za Wakristo na watawala. Aghalabu wakati huo huwa na umri mkubwa. Wengi wao

[7] J.F.A. Ajayi, 1985, kurasa 15-16; A.A. Mazrui na T.G. Wagaw, 1985, kurasa 39-44.
[8] T.G. Wagaw, 1979, sura 1.

hawakujaribu kuwa na familia, lakini walitumia maisha yao katika ibada na uanazuoni kama watawa.

Vivyo hivyo, mahitaji ya kidini ya jumuiya za Waislamu yalihakikisha kuendelezwa kwa elimu ya Kiislamu si katika familia tu bali pia katika asasi nyingine zilizo rasmi na zisizo rasmi za kidini na kielimu.[9] Kwa kuwa waadhi wa Kur'ani unahitaji kueleweka katika asili yake ya Kiarabu ambacho ilishushwa, wazazi wengi wa Kiislamu walitaka watoto wao, hasa wa kiume, kuhudhuria shule za Kur'ani kwa muda wote au kwa vipindi tu, kujifunza Kur'ani ghibu na sarufi ya msingi ya Kiarabu utotoni mwao. Elimu ya ziada ilikuwepo katika *'ilm* (asasi rasmi za shule au *madrasa* (madarasa yanayoendeshwa na *maalimu* katika misikiti). Masomo yanayofunzwa ni pamoja na *tafsir* (maelekezo juu ya Kur'ani), *hadith* (maelekezo ya Mtume hasa kuhusiana na tabia ya mtu katika mambo kama vile ndoa, talaka na mirathi) na *fikh* (mitalaa inayohusu sheria ya Kiislamu au *Shari'a*).

Licha ya kuwepo kwa vipindi vya uadui na migongano, tawala za kikoloni hazikupinga kuenea kwa elimu ya Kiislamu katika ngazi za msingi katika maeneo ya wenyeji. Hata hivyo, walielekea kukatisha tamaa elimu ya juu, hasa iliyoleta uhusiano wa kimataifa uliokuwa na mwelekeo wa kupinga ukoloni kama ilivyokuwa mahali kama vile Al-Azhar ya Kairo. Tawala za kikoloni zilijaribu kudhibiti mahujaji, wakipendelea kuchagua na ikiwezekana kuwafadhili wanazuoni wasiopenda mabadiliko. Hali hiyo haikuweza kuzuia wanazuoni wenye moyo kuendelea na tabia ya kusafiri na kuwasikiliza wanazuoni walioheshimika, wakishika kazi zao na kufaidika na yaliyomo katika maktaba zao. Kwa njia hiyo, vituo vya wenyeji vya elimu ya juu viliibuka, kama vile Msikiti wa Riyadha wa Lamu katika pwani ya Afrika ya Mashariki, ambao uliwavutia wanafunzi kutoa eneo kubwa la sehemu hizo.

Tatizo kubwa lilikuwa ni hofu iliyowapata Waislamu kutokana na elimu ya magharibi, iliyofadhiliwa kwa kiwango kikubwa na Wamisionari wa Kikristo kama silaha ya kueneza neno la Mungu. Kutokana na sababu hiyo hakukuwa na pengo tu baina ya elimu ya magharibi na elimu ya asili ya Kiislamu bali kulikuwa na hali ya uadui. Katika sehemu chache tawala za kikoloni ziliwakataza Wamisionari wa Kikristo magharibi kwa kutumia tawala za wenyeji, lakini njia hiyo haikufanikiwa sana kuziba pengo au kupunguza uadui. Mashirika machache ya Kiislamu yalifanikiwa yalipofadhili elimu ya magharibi katika mazingira ya Uislamu,

[9] A.A. Mazrui na T.G. Wagaw, 1985, kurasa 48 – 53; M. Bray na wenzake, 1986, sura 5

wakifundisha Kur'ani na Kiarabu, pamoja na kusoma na kuandika kwa Kiingereza, na hesabu za msingi katika shule za Kimagharibi. Kwa kiasi kikubwa, hata hivyo, elimu ya Kiislamu na ya Magharibi haikutangamana na hiyo ikawa sababu ya maendeleo yasiyolingana kwani elimu ya Magharibi iliendelea kuipita elimu ya Kiislamu kama njia ya kupata kazi katika sekta za kisasa za jamii na kama ishara ya hadhi katika kipindi cha ukoloni.

Elimu ya wenyeji katika utamaduni simulizi pia iliendelea bila kutambuliwa na shule za magharibi.[10] Kinyume na dhana potovu iliyoibuka wakati wa ukoloni, mfumo huu wa elimu ulivuka mipaka ya kuingizwa katika jamii kwenye mfumo wa familia pana, uwekaji wa marika, na mifumo ya jando na unyago kama ile ya Poro na Bundo ya maeneo ya Magharibi ya Atlantiki. Katika ngazi za msingi, mtoto alifunzwa katika mazingira yasiyo rasmi ya familia kupitia mafumbo ya maneno, ngoma na michezo ya namna hiyo, ili kuijua vyema lugha ya awali. Alifunzwa kuhesabu, na katika kutamba hadithi, alifunzwa kuthamini utamaduni, maadili, jinsi anavyoiangalia dunia na historia yake. Kwa kupitia aina fulani ya uanagenzi, mtoto alijifunza stadi mbalimbali. Katika mchakato huo mtoto alijifunza mazingira, mimea na wanyama, stadi za uwindaji na uvuvi, uundaji wa vifaa, utunzaji wa nyumba kwa wasichana na kilimo kwa wavulana, ujenzi wa nyumba, sanaa, muziki, uchezaji ngoma, dini na mengineyo. Kutokuwepo kwa urasmi katika mchakato huo kusitufumbe macho yetu kwa makusudi yaliyofanywa kumwelimisha mtoto au kiwango ambacho jamii ilitegemea elimu hiyo kuendelea kuwepo na kuendelea kwa watu binafsi kutumia maarifa mapya na hatua walizozichukua katika kuyaendeleza.

Elimu ya juu ilitengwa kwa ajili ya mafunzo ya watawala na makasisi. Watawala, hasa katika mifumo yenye utawala mkuu wa dola, walijifunza kwa kina historia ya jumuiya, misingi ya kisheria ya madai ya ardhi na mali nyingine muhimu, sheria na mila, kazi na wajibu wa mtawala, na kadhalika. Kipindi cha kabla ya kutawaza kiliendeleza elimu hiyo, kwa kusisitiza mielekeo na tabia zinazotegemewa kuwa nazo mtawala, ambapo kutawazwa kwenyewe kulilenga katika kumbadilisha mtawala kutoka kuwa mtu hadi kuwa mfalme ambaye kwa asili huwa kama Mungu. Makasisi walipitia mafunzo magumu yaliyodumu kwa miaka kadhaa na yaliyohusu nyanja nyingi. Ilibidi ajue vyema falsafa ya dini na maana za mikarara mbalimbali mtakatifu, visaasili, tenzi za kusifu miungu n.k. Alitakiwa pia kutambua dalili za

[10] M. Bray na wenzake, 1986, Sura 6; N.K. Dzobo, 1975.

magonjwa mbalimbali na kujua dawa za mitishamba na za kimila kwani kasisi hakuwa tu mbashiri aliyekuwa kiungo cha mawasiliano baina ya mteja na miungu, alikuwa pia mganga, na katika maeneo makame, mtengeza mvua aliyedhibiti nguvu za asili. Alitakiwa kujua, kwa viwango mbalimbali vya utimilifu, uanishi tabia za mimea na wanyama, si kama mtu tu aliyejua biolojia na utaalamu wa dawa, bali pia katika maana za kibotania na kizuolojia na falsafa. Michakato mingine ya uungu ilihusisha maarifa tata ya hisabati ambayo yameanza tu kutambuliwa na mitalaa ya kisasa.[11]

Kutokana na dharau waliyokuwa nayo wale waliosoma katika elimu ya magharibi kwa mifumo ya elimu ya wenyeji, kuenea kwa elimu ya magharibi kumechangia kidogo sana katika maarifa ya kilimo, sanyansi ya afya, sanaa na utengenezaji wa vifaa wa jadi ambao unaendelea kuendeleza maisha vijijini. Watu wengi, hata vijijini, wamekataa kushikilia dini za jadi ambazo ndizo zilizosukuma mifumo ya elimu ya jadi, na wamejitambulisha na Uislamu au Ukristo; lakini maadili ya kijadi hayakukoma kuwa muhimu au kuwafaa. Maono kuhusu ulimwengu, thamani za kijamii na maelezo kuhusiana na ubaya na uzuri, ugonjwa na afya, bado viliendelea kuangaliwa kutokana na utamaduni wa jadi. Jinsi aina za Ukristo wa Kiafrika zilivyoenea vijijini, maadili mengi yanayojumuisha jamii ya utamaduni huu wa jadi, hasa kuhusu asili ya magojwa na utunzaji wa afya, yaliingizwa. Kutokana na kuongezeka kwa ufahamu kuhusu kuendelea kufaa kwa kilimo na sayansi za afya za jadi, kumekuwepo na ufufuaji wa dini za jadi, na ongezeko la kuthamini mafanikio na kuendelea kwa umuhimu wa mifumo ya elimu ya wenyeji.

## Upanuzi na urekebishaji

Viongozi wa Kiafrika walitambua wakati wa uhuru haja ya kupanua na kurekebisha mfumo wa elimu ya kikoloni. Kwa maneno ya Sékou Touré wa Guinea; "Ni lazima tuifanye elimu yetu kuwa ya kiafrika na kuondokana na mambo mabaya na welewa potovu uliorithiwa kutoka kwenye mfumo wa elimu uliolenga mahitaji ya wakoloni."[12] Wote walikubaliana katika haja ya upanuzi. Isipokuwa kwa wachache, kama rais wa Malawi ambaye alitaka shule za umma za Kiingereza zifuatwe bila mabadiliko na kuwa ubora wa elimu unatokana na kujifunza Kilatini na Kigiriki, viongozi wengi wa Kiafrika walikubaliana juu ya haja ya kuifanya elimu kuwa ya

[11] J.F.A. Ajayi, 1987

[12] Katika A. Sékou Touré 1963 kama ilivyonukuliwa katika L.G. Cowan na *wenzake* 1965 uk129

Kiafrika na misingi yake kutokana na utamaduni wa Kiafrika. Labda hakuna kiongozi mwingine aliyejaribu kuunda na kutekeleza falsafa ya elimu ya Kiafrika kwa uwazi kama Julius Nyerere wa Tanzania, yeye mwenyewe akiwa mwalimu hapo awali na kwa kawaida akiitwa *Mwalimu.* Katika kitabu chake cha *Elimu ya Kujitegemea*[13] ambamo alisisitiza juu ya dhima ya elimu katika kufikia lengo lake la Ujamaa kama linavyoelezwa katika Azimio la Arusha, anashauri juu ya marekebisho manne makuu:

(1) kuiingiza elimu ya magharibi katika maisha ya familia na jumuiya;

(2) kukomesha usomi uliokuwepo katika elimu ya kikoloni kwa kuwa na mpango wa elimu ya msingi kwa wote ambayo itaingiza mifumo ya elimu ya magharibi na ya jadi.

(3) kuziba pengo baina ya wasomi na umma kwa wasomi kuthamini zaidi maarifa na busara zilizopo katika jamii za jadi; na

(4) kujenga moyo wa kazi na huduma kwa jumuiya katika utoaji wa elimu.

Ingawa upanuzi na urekebishaji wa elimu vilikwenda sambamba, msisitizo wa awali ulikuwa katika upanuzi. Katika Mkutano wa Addis Ababa wa Mei 1961, uliotayarishwa na UNESCO, wawakilishi wa takriban nchi 35 huru na zilizokaribia kuwa huru walikutana kuangalia upya mifumo yao ya elimu na kupanga kwa ajili ya maendeleo ya muda mfupi na mrefu.[14] Matokeo yake ambayo ni Mpango wa Addis Ababa wa Elimu ya Kiafrika uliweka malengo maalumu ya kuongeza uandikishaji wa wanafunzi na msaada wa fedha unaohitajika. Kutokana na kutokuwepo au udhaifu wa mipango ya maendeleo ya uehumi, uchunguzi kuhusu wafanyakazi, takwimu sahihi na kamili, na kutokana na ukadiriaji wa chini sana wa ongezeko la watu, malengo ya Addis Ababa yanaweza kusemwa, kwa kuangalia nyuma, kuwa yaliakisi zaidi matumaini na matarajio ya washiriki wake kuliko hali halisi ya uchumi wa Afrika. Hata hivyo, mkutano huo uliweka msingi wa majadiliano zaidi na ubainishaji wa dhima na kasi ya maendeleo ya elimu kuhusisana na raslimali zilizopo na mahitaji ya sekta nyingine katika maisha ya taifa.

Mpango wa Addis Ababa ulitambua matumizi madogo sana yaliyofanywa wakati ule kuhusiana na maendeleo ya watu katika ubora na wingi wao. Ulitambua kwamba ni asilimia 40 tu ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule ya msingi

[13] J. Nyerere, 1967c, kur. 10-15.
[14] UNESCO, 1961a, kur. 1 -127; na UNESCO, 1961b.

waliandikishwa kwenye aina yoyote ile ya shule na kwamba asilimia ndogo zaidi ya watoto wenye umri mkubwa waliokwenda shule. Kwa umuhimu uleule, mpango ulitambua ubora usioridhisha wa elimu iliyotolewa. Washiriki wa Mkutano walisisitiza kuwa, kutoka na hali ya Afrika ya wakati ule:


> Yafundishwayo kwenye elimu .... Hayaendani na hali ilivyo Afrika, dhana ya uhuru wa kisiasa, mambo yanayotawala katika enzi ambayo hasa ni ya kiteknolojia, au mahitaji ya maendeleo yaliyo sawa ya kiuchumi ambayo yanahusu ukuaji wa haraka wa kitasnia. Yanatokana na hali isiyo ya Kiafrika, yasiyoruhusu matumizi ya akili ya mtoto wa Kiafrika, uwezo wake wa kuchunguza mambo na ubunifu kukubua kwa uhuru na kumsaidia kupata dira yake ulimwenguni. Mamlaka za elimu za Afrika hazina budi kuangalia upya na kurekebisha yaliyomo katika elimu kwenye maeneo ya mihtasari, vitabu vya kiada, na njia za ufundishaji, ili kutilia maanani mazingira ya kiafrika, makuzi ya mtoto, urithi wa kiutamaduni, na mahitaji ya maendeleo ya kiteknolojia na kiuchumi, hasa ukuaji wa viwanda...[15]

Kulingana na malengo ya idadi, mpango wa mkutano ulitaka uandikishwaji uongezwe kutoka uwiano wa 1960 wa 40:3:05 (yaani asilimia 40 katika ngazi ya msingi, asilimia 3 sekondari na nusu asilimia katika kiwango cha juu) na kuwa 100:30:20 ifikapo 1980. Lengo lilikuwa kufanya elimu ya msingi kuwa ya wote, ya lazima na ya bure. Kati ya wale wanaomaliza shule ya msingi, asilimia 30 iweze kuendelea na hatua ya sekondari, na asilimia 20 ya wale wanaomaliza hatua ya sekondari waendelee na hatua ya juu, hasa katika asasi zilizoko Afrika. Upotevu usiozidi asilimia 20, na wastani wa idadi ya wanafunzi kwa kila mwalimu ungekuwa 35. Walimu zaidi wa kiafrika wangeajiriwa na kufunzwa. Zaidi ya hayo, elimu ya watu wazima ingetolewa katika mashule, mahali pa kazi, na mahali pa ibada. Ili kufikia malengo hayo, serikali za kitaifa zilitakiwa kuongeza misaada ya kifedha kutoka asilimia 3-4 ya Zao la Taifa iliyokuwa ikitumiwa hadi asilimia 4-6 kati ya 1970 na 1980. Serikali za Kiafrika zilishawishiwa pia kuomba msaada wa jumuiya za kimataifa katika juhudi zao hizo za elimu.


[15] UNESCO, 1961a, uk. 23; taz. Pia UNESCO, 1961b.

Tangu 1961, kumekuwa na mikutano ya mawaziri wa elimu katika vipindi mbalimbali kuzungumzia masuala ya elimu katika Afrika. Nairobi 1968, Lagos 1976 na Harare 1982, zaidi ya mkutano wa Tananarive wa 1962 uliohusu hasa elimu ya juu. Kila mkutano ulitokana na maarifa yaliyotokana na mikutano iliyotangulia – ukirekebisha, kuboresha zaidi, kupata maarifa na mazingatio, kupanua mawazo na matarajio ya Waafrika na serikali zao, na kuyaweka katika mfumo wa maendeleo ya elimu ulioratibiwa na kupangwa vyema zaidi. Hivi sasa inawezekana kutathimini maendeleo ya elimu ya Afrika kuhusiana na mipango hiyo na kuona jinsi ilivyosaidia na kufaa katika mahitaji ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ya jumuiya pamoja na hatua iliyopigwa katika kuwa na elimu ya msingi kwa wote na elimu ya watu wazima.

Kwa idadi, kiwango cha ongezeko la uandikishaji kinatia moyo. Bara limefanikiwa kuongeza kiwango kwa hali ya juu ukilinganisha na eneo lolote jingine duniani, pamoja na ongezeko la haraka katika kujua kusoma na kuandika. Katika sehemu kadhaa mipango ya elimu ya msingi kwa wote ilianzishwa, na kwingineko





*Mchoro 22.1 uandikwishaji wa shule katika Afrika, 1960-80; uwiano wa uandikishwaji ghafi uliorekebishwa kwa ngazi (marejeo kutokana na data za UNESCO za 1982)*




Mchoro 22.2 *Uandikishwaji wa shule katika Afrika, 1960-80; Uwiano wa uandikishwaji ghafi uliorekebishwa kwa ngazi na jinsia (marejeo kutokana na data za UNESCO za 1982)*

Elimu ya bure hata kwa kiwango cha sekondari na elimu ya juu. Viongozi wachache walisimamia na kushikilia utoaji wa elimu kwa wote na bure kama Kwame Nkurumah wa Ghana na Obafemi Awolowo wa Nigeria. Hata hivyo, hata Ghana na Nigeria, misukumo mikali ya kiuchumi na ya ongezeko la idadi ya watu ilisababisha kujitoa katika juhudi za kufanya elimu ya msingi iwe kwa wote. Upinzani wa athari za kijamii za elimu ya magharibi – kama vile kuwafanya wasichana wasiolewe mapema na uhamiaji wa mijini kutoka vijijini – umeendelea, hasa kwenye maeneo ya Waislamu. Hivyo licha ya upanuzi mkubwa, malengo ya 1961 ya uandikwishaji katika shule za msingi hayakufikiwa, na hivi karibuni kiwango hicho kimepungua.[16]

[16] Taz. Nyaraka zilizotolewa kwenye mkutano wa Harare na UNECA, OAU na UNESCO, hasa 1982, Nyaraka ED/82/MINEDAF/4 na ED/82/MINEDAF/2 na Benki ya Dunia, 1988.




*Mchoro 22.3 Mielekeo ya uandikishwaji wa shule za msingi katika Afrika, 1960 – 80, ikionyesha idadi ya wanafunzi na waliondikishwa kwa mamilioni, pamoja na uwiano ghafi uliorekebishwa wa uandikishwaji wa shule za msingi (kwa asilimia) (Marejeo: kutokana na data za UNESCO za 1982).*

Kuanzia 1961 hadi 1980, uandikishaji katika ngazi ya msingi uliongezeka kwa asilimia 6.2 kwa mwaka, ukipita asilimia 5.6 zilizoonyeshwa katika Mpango wa Addis Ababa. Hata hivyo, kutokana hasa na data zilizotumiwa kuweka mipango 1961 kutokuwa kamili, elimu ya msingi kwa wote haikuweza kufikiwa na nchi nyingi za Afrika. Kiasi cha nchi 13 tu kati ya 53 ndizo zilizofikia karibu na uandikishaji wa wote. Kwa eneo lote kwa jumla, asilimia 62 ya watoto wenye umri wa kujiunga na shule za msingi walikuwa wameandikishwa mnamo 1980. Kulikuwa na tofauti kubwa ya mafanikio kulingana na nchi na misingi iliyosaidia uandikishaji huo. Mnamo 1960, baadhi ya nchi zilikuwa na uandikishaji wa chini hadi asilimia 3-4 ya watoto wa umri wa miaka 6-11, ambapo nyingine zilikuwa na uwiano wa juu hadi kufikia asilimia 75. Mnamo 1980, uandikishaji wa kiwango cha chini kabisa ulikuwa asilimia 13 iwapo nchi 15 zilikuwa zimefikia zaidi ya asilimia 75. Ili kufikia hatua hiyo ya mafanikio, nchi za kiafrika zilianzisha programu kamambe za ujenzi na mafunzo ya walimu wa shule za msingi, aghalabu kwa kushirikisha jumuiya. Juhudi hizo, hata hivyo, hazikuweza kuboresha hali ya ukosefu mkubwa wa walimu wenye sifa zinazostahili.[17]

Kiwango cha ongezeko katika ngazi ya sekondari kilitia moyo zaidi ingawa hakikuwa sawa kote. Uwiano wa jumla wa uandikishaji uliofikiwa katika ngazi ya sekondari mnamo mwaka 1980 ulikuwa asilimia 20 ya marika husika kukiwa na tofauti baina ya nehi kutoka asilimia 2.1 hadi asilimia 82.3. Katika miaka saba ya nyuma baadhi ya nchi zilizopata uhuru karibuni ziliongeza uandikishaji katika ngazi ya sekondari kwa mara tano. Uandikishaji wa wanawake ulibakia nyuma ya ule wa wanaume katika ngazi zote.

Kipimo kingine cha dhamira ya Afrika kujiletea maendeleo kupitia elimu kilikuwa katika ruwaza za mgawanyo wa raslimali katika eneo hili. Kwa miaka ya 1970 na 1978, matumizi ya serikali kwa ajili ya elimu Afrika yalikuwa dola za kimarekani 2377 na 11,144 bilioni. Ikilinganishwa na mataifa yenye viwanda na maeneo mengine ya nchi zinazoendelea, uwekezaji wa Afrika katika elimu ulikuwa ni wa chini sana. Hata hivyo, kulingana na matumizi kama asilimia ya Zao Ghafi la Taifa, Afrika ilikuwa inashindana na maeneo hayo mengine. Mathalani, Afrika iliwekeza asilimia 3.8 na 4.8 ya Zao Ghafi la Taifa katika elimu mnamo miaka ya 1970 na 1980,

[17] Taz. UNESCO, UNFCA na OAU, 1982, Waraka ED/82/MINEDAF/2.

asilimia kubwa zaidi kuliko nchi zinazoendelea za dunia zikiwekwa zote pamoja, ambapo asilimia 3.3 ilirekodiwa 1970 na asilimia 4.1 kwa 1980. Kwa nchi zenye viwanda ilikuwa asilimia 5.7 na 5.9 kwa miaka hiyo.

Ilipofikia 1980, elimu ilitumia asilimia 25-35 ya matumizi ya kawaida ya serikali katika Afrika. Gharama za kila mwanafunzi kwa mwaka zilifikia dola za Kimarekani 22 kwa shule za msingi, dola 133 shule za sekondari na dola 986 kwa elimu ya juu, ilipofikia mwishoni mwa miaka ya 1970. Hii inawakilisha dhamira ambayo ni ya hali ya juu zaidi kuliko maeneo mengine ya nchi zilizoendelea au zinazoendelea duniani.[18]

Katika nchi nyingi za Afrika, elimu bado inatumia rasilimali zaidi kuliko shughuli nyingine yoyote ya serikali isipokuwa utawala wa kawaida. Swali ni kama, kutokana na raslimali finyu za kifedha za nchi nyingi za eneo hili, viwango vya sasa vya uwekezaji katika elimu vitaweza kuwa endelevu. Jibu hasa linaweza kuwa hapana, na hivyo mataifa mengi yanabidi yajiingize katika njia mpya na zisizo za kawaida za kupata fedha kama vile kucheza na miundo ya motisha na mishahara, kuanzisha masomo ya shifti, kutumia nafasi na wafanyakazi mwaka mzima (pamoja na usiku), na kuongeza matumizi ya elimu huria na kwa kutumia njia za elektroni.

Shinikizo la kujaribu kufikia malengo ya upanuzi ndilo labda lilikuwa sababu muhimu zaidi ya kupingana na mfumo ulioriithiwa wa elimu ya kikoloni. Hakukuwa na muda wa kusimama, kufanya mabadiliko ya msingi, kuwashikilia wafanyakazi na kuunda mielekeo mipya. Aghalabu, maneno ya kusisitiza haja ya kuwa na marekebisho ya kielimu yalileta mabadiliko ya juujuu ambapo mfumo uliokuwapo uliendelezwa kulingana na ongezeko la mahitaji na ongezeko la mgawanyo wa raslimali. Na bado juhudi kubwa zilifanywa katika mikutano iliyofululiza ya mawaziri wa elimu wa Afrika yote na hata katika nchi binafsi[19] kuunda sera za kitaifa za elimu ambazo zingetekeleza kwa kiasi fulani marekebisho yaliyoelezwa na Rais Nyerere ya kuunganisha miundo ya elimu ya jadi na elimu ya magharibi katika mfumo mpya wa elimu; kutumia elimu kukuza maadili, itikadi na falsafa ya kitaifa na kanuni za msingi za jamii mpya inayoshikamana na yenye usawa ambayo inajali dhana ya haki ya jamii; kuifanya elimu isiwe ya kisomi sana, inayoelekeza zaidi manufaa ya jumuiya kuliko ya binafsi kati ya waliosoma; kuwa na mfumo wa

[18] T.G. Wagaw, kinachotarajiwa, sura 10; pia UNESCO, UNECA na OAU, 1982, Warak ED/82/MINEDAF/REF.5.

[19] Taz., kwa mfano, U.Bude, 1980; Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria, Wizara ya Shirikisho ya Elimu, 1981; na K. King, 1976.

elimu inayofaa zaidi katika mahitaji ya jamii ya kiutendaji na yaliyopo kwa kusisitiza utamaduni pamoja na sayansi na mafunzo ya ufundi kwa nia ya kuwa na wahitimu ambao wanaajirika kiurahisi na hivyo kupunguza ukosefu au upungufu wa ajira, na kadhalika.

Marekebisho ya elimu ni zoezi refu, tata na lisilokoma, na enzi ya baada tu ya uhuru ilikuza wepesi wa kufikia marekebisho ya msingi. Hii haina maana kuwa hakuna mafanikio muhimu yaliyofikiwa. Utawala wa Wamisionari wa Kikristo kutoka Ulaya na Marekani katika elimu ya magharibi ulipungua na kupitwa na serikali ambayo ndiyo iliyoshika usukani, licha ya kuwa si pote. Elimu imekuwa ndio njia muhimu ya kuleta mabadiliko ya kijamii na mahali pengi upatikanaji wake umepanuliwa kama sio kuwa wa kidemokrasia kabisa, ingawa kuna makundi mbalimbali ya wasomi na wataalamu ambayo yameweza kuanzisha au kuendeleza manufaa hayo kwa ajili ya watoto wao, kwa kuwa na elimu ya awali ya chekechea na ufahamu mzuri zaidi wa lugha rasmi za Kizungu. Kuendelea kutawala kwa lugha za Kizungu ndio nguzo ya msingi inayozuia marekebisho ya msingi ya mifumo ya elimu ya kikoloni. Lugha za Kiafrika zilizoweza kuleta muungano wa kijamii katika ngazi ya wenyeji na msingi wa marekebisho kamili ya kielimu zimekuwa zikitumiwa kwa kiwango cha chini tu ambapo lugha za Kizungu zimeendelea kukuzwa kuwa zinakubalika zaidi kisiasa kama lugha za kiungo. Hakuna pengine ambapo kipengele hiki cha upanuzi wa nyenzo na upunguzaji wa marekebisho unaonekana vyema zaidi kama katika uwanja wa elimu ya juu.

## Elimu ya juu

Asasi za elimu ya juu ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya kisasa Afrika. Zinawakilisha pia kielelezo cha hali ya juu cha jamii kutafuta kujirudia, kujitaalamisha, kukua na kujikamilisha. Zaidi ya mambo mengine, asasi za elimu ya juu hufunza, hutoa vyeti na ama huwapatia nyenzo wenye akili kali kuwa viongozi wa serikali, biashara na katika utaalamu. Idadi ya watu waliopata nyenzo hizo kwa hiyo ni wachache sana lakini nguvu zao za kuathiri jamii ni kubwa kupita kiasi. Haishangazi kwa hiyo kuona kwamba vituo hivi vya elimu ya juu vinaangaliwa kwa matumaini, mshangao, heshima, hofu au wasiwasi na vijana na wazee, na hasa wanasiasa.


Elimu ya juu si jambo jipya katika bara la Afrika. Chuo Kikuu cha Sankore cha Timbuktu kilishamiri mnamo karne ya kumi na sita kama kituo cha uanazuoni na mafunzo ya sheria, falsafa na theolojia. Asasi nyingine iliyokuwa na umuhimu

kama huo ni Chuo Kikuu cha Azhar cha Kairo, ambacho kimedumu kwa miaka zaidi ya elfu moja. Asasi hii ilijulikana zaidi kwa mafunzo ya dini na sheria ya Kiislamu na bado kinaendelea kufanya kazi hiyo hata kinavyozidi kupanua na kusasisha mawanda yake kwa kuingiza njanja nyingine za mafunzo. Huko Ethiopia, kama tulivyoona uwanazuoni ulikua na kusaidiwa. Kulikuwa na vituo vya masomo ya juu vilivyoenea kwenye nyanda zote za juu ambako wataalamu wa sheria za kawaida pamoja na watendaji wa ngazi za juu walifunzwa. Huko Sierra Leone, Kanisa la Chama cha Wamisheni wa London kilianzisha Chuo cha Ghuba ya Fourah mnamo 1927 kama kituo cha mafunzo ya dini. Baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, asasi hiyo ilikuwa ndio msingi wa chuo kikuu kipya cha serikali.

Kulikuwa na vituo vingine vya masomo ya juu katika maeneo mengine ya bara hili, ikiwa pamoja na vile vilivyoanzishwa na tawala za kikoloni, ambako mafunzo ya sheria, sayansi za jamii pamoja na mafunzo ya ufundi yalitolewa. Kwa kiasi kikubwa, hata hivyo, vyuo thamanini au zaidi kidogo na vyuo vikuu vilivyoko Afrika viliundwa baada ya uhuru wa kisiasa kupatikana, kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1950. Zaidi ya vyuo vikuu, kuna shule mbalimbali za utaalamu, vyuo vya juu vya ualimu, vyuo vya ufundi anuwai na teknolojia.

Mwaka mmoja baada ya mkutano wa Addis Ababa wa 1961, mkutano wa pili ulifanyika Tananarive, Madagaska, kushughulikia hasa maendeleo ya elimu ya juu Afrika kwa miaka inayofuata.[20] Licha ya kuwa hakukuwa na hata data za msingi za ongezeko la watu, mkutano ulijaribu kuamua asasi ngapi za elimu ya juu zinahitajika na zitakuwa na wajibu gani katika maendeleo ya eneo hili. Mwanzoni, mkutano ulijaribu kufafanua malengo na dhamira za elimu ya juu. Kulingana na washiriki wa mkutano huo, lengo kuu la elimu ya juu lilikuwa ni kueleza na kuhakikisha matakwa na matarajio ya jamii husika. Wakati zikidumisha viwango vya kimataifa vya ubora wa kitaaluma, elimu ya juu ya Kiafrika haina budi kuwapatia Waafrika mahali pao wanapostahiki ulimwenguni na kuimarisha umoja wao daima. Kwa upande huo asasi za elimu ya juu zinalazimika kujiona kuwa ni vituo vya utamaduni vya jumuiya zao na walinzi na wasimamizi wa urithi wao wa kisanii, kifasihi na muziki. Zinabidi zifanye utafiti wa urithi huo na kusambaza matokeo ya utafiti kwa kuwa na tamasha, majumba ya maonyesho, makumbusho, maktaba na hifadhi za nyaraka. Vyuo vikuu vya Afrika, kama vyuo vingine vyote, vilitarajiwa

[20] UNESCO, 1963






*PICHA 22. JUU: Maabara ya biolojia ya Chuo cha Elimu, Chuo kikuu cha Lagos, Nigeria, 1968: chini: Asasi ya Ufundi Anuwai na Ufundi ya Kenya, 1968.*

kuendeleza mawanda ya maarifa kwa kufundisha na kufanya utafiti pamoja na ushauri na huduma kwa jumuiya pana.

Vyuo vikuu vilianzishwa kutokana na mifano ya Ulaya ya Magharibi au Amerika ya Kaskazini. Hata hivyo, vimepata msukumo wao kutokana na changamoto za Afrika yenyewe. Mara nyingi, viongozi wa kisiasa wa nchi husika walijishughulisha na uendclezaji wa elimu ya juu. Aghalabu wakuu wa nchi au serikali walikuwa ndio wakuu wa asasi hizo. Rais Julius Nyerere wa Tanzania alivisihi vyuo vikuu vya Afrika kuwa mstari wa mbele "katika mapinduzi ya jamii tunayoyaanzisha" bila wakati huohuo kuwa kitovu cha upinzani wa serikali iliyoundwa kihalali. Juu ya yote, chuo kikuu ni lazima kidumishe "ukweli; ni lazima kisipendelee na kiwe cha kisayansi iwezekanavyo, na hakina budi kupambana na ubaguzi wa aina zote, wakati wote, na mahali pote. Chuo kikuu ni lazima kitusukume kufikiria ubinadamu na sio manufaa ya kikundi chochote".[21] Viongozi wa Ghana, Nigeria, Ethiopia, Ivory Coast na Guinea, kati yao, walieleza matumaini ya namna hiyohiyo kuwa asasi hizo zingesimama kidete kutafuta ukweli, kutopendelea, ubinadamu na kutaalamisha hata kama zimeahidi kutimiza wajibu wao kwa nia ya kuwa watiifu kwa jamii inayowazunguka.

Miongo miwili baada ya mkutano wa Tananavive, uchanganuzi unaonyesha kwamba maendeleo ya elimu ya juu katika Afrika hayakuwa ya usawa. Uandikishaji wa jumla uliongezeka kutoka 140,000 mnamo 1960 hadi 1,169,000 mnamo 1980, ongezeko la zaidi ya mara nne. Mnamo 1980, asilimia 3 ya watu wenye umri wa kuingia chuo waliandikishwa katika vyuo vikuu, ikiwa zaidi ya asilimia 2 iliyodhamiriwa. Ni kweli kwamba uandikishaji katika elimu ya juu unaongezeka kwa haraka zaidi ya uandikishaji katika ngazi nyingine yoyote ya elimu licha ya serikali kujaribu kupunguza kasi ya uandikishwaji kutokana na gharama kubwa. Hali hiyo inaonyesha ukweli wa kisiasa kuhusiana na elimu.

Asasi za elimu ya juu za Afrika ni ghali sana. Gharama ya mwanafunzi mmoja wa chuo inakadiriwa kuwa $ 927-1045 kwa mwaka. Kwa kiasi kikubwa, gharama hizo hulipwa na hazina za taifa. Wanafunzi huchangia kidogo sana, kama wanachangia, katika elimu ya juu. Walimu wa vyuo vikuu ni kati ya wanajumuiya walipwao vizuri. Wataalamu kutoka nje, ambao ni wa kawaida katika asasi hizo, ni

[21] Imenukuliwa katika L. G. Cowan na wenzake, 1965, uk, 309 – 13; taz. Pia kur. 317 – 21 kwa ajili ya madondoo yanayotoka kwenye hotuba za kwame Nkrumah wa Ghana.

ghali zaidi katika malipo ya mishahara yao, usafiri na marupurupu mbalimbali. Huo huwa ni mzigo mkubwa kwa rasilimali chache za taifa katika nchi zinazohusika.

Hata hivyo, kwa kuwa elimu ya juu inachukuliwa kuwa ni njia ya kupata maisha mazuri – madaraka, pesa, hadhi na mvuto – vijana na wazazi wao wanaendelea kudai nafasi za kutosha katika vyuo vikuu. Hata kama hawapendi kiasi gani, wanasiasa inabidi waliangalie suala hilo. Matokeo yake, uandikishwaji katika elimu ya juu unaendelea kuongezeka – mara nyingine kwa kusabilia elimu ya ngazi za chini.

Matatizo kadhaa ya ziada yanabaki bila utatuzi katika ngazi ya elimu ya juu. Ilikuwa ni matarajio ya waunda sera wa Afrika kwamba wanafunzi wengi wa vyuo vikuu wangejiandikisha katika nyanja za sayansi na teknolojia kuliko sayansi za jamii. Kutokana na sababu tata za kijamii na utamaduni, pamoja na ukosefu wa nyenzo za kutosha na walimu wenye sifa zinazotakiwa katika ngazi za chini za mfumo wa elimu, hali hiyo haitimiliki. Matokeo yake ni mkengeuko. Inaacha mahitaji ya watu wenye stadi maalumu za ufundi kutofikiwa, wakati kumekuwepo na ziada ya wafanyakazi waliohitimu katika nyanja nyingine. Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa kupunguza mkengeuko huo ni pamoja na knimarisha mafunzo katika madarasa ya chini, kutoa motisha itakayowatia moyo watu kuchukua mafunzo ya kazi katika sayansi na teknolojia, na kutoa uongozi kuhusu vipaumbele vya taifa katika ngazi zote.[22]

Tatizo jingine ni uchache wa wanafunzi wa kike katika asasi za masomo ya juu. Licha ya matamko yanayopingana na hali hiyo, wanawake wachache wanahudhuria kwenye asasi kama hizo, wengi wao wakiacha masomo kabla ya kuyamaliza, na wale wanaohitimu huwa wengi katika masomo kama vile ya sayansi za jamii ambayo hayako katika vipambele vya taifa.

Kuhusiana na ubora kwa jumla, asasi za elimu ya juu zimetoa watu wenye stadi kwa ajili ya utumishi wa serikali, majeshi na biashara na hivyo kupunguza kutegemea wataalamu kutoka nje. Hata hivyo, wataalamu kutoka nje bado wanaongoza mashirika makubwa ya kibiashara na viwanda katika nchi nyingi za Afrika.

Elimu ya juu ya Afrika imekuwa inapewa changamoto mara kwa mara ya kuwa inayohusu na kufaa mahitaji lukuki ya jamii zinazoendelea. Sehemu kubwa

[22] Taz. T.G. Wagaw, kitakachotoka karibuni; pia A. Habte, 1969; T.M. Yesafu, 1973; na J.F.A. Ajayi, 1987.

ya Afrika ni ya vijijini. Stadi zinazohitajika katika usimamizi wa mashamba, uhandisi kilimo, uchumi wa kujikimu, utengenezaji na utunzaji wa vifaa vya kilimo, ufugaji, afya ya umma na elimu ya ugani hazitoshi. Wengi wanaamini kwamba vyuo vikuu na vyuo vi lazima, zaidi ya mambo mengine yote, vitoe idadi ya kutosha ya watu waliohitimu wenye uwezo wa kukabiliana na kutosheleza mahitaji hayo kufanya utafiti, kuendeleza teknolojia inayofaa, na kusaidia matumizi yake kwa ajili ya kutatua matatizo ya maendeleo ni kazi muhimu ya ziada inayotakiwa kufanywa na asasi za elimu ya juu. Ugunduzi, ukuzaji na upanuzi wa urithi wa kisanii, kifasihi na kihistoria wa Afrika ni wajibu unaopewa asasi hizo.

Masuala ya lugha bado yapo kwenye ajenda. Waafrika walio wengi wanatumia lugha zao mbalimbali katika mahusiano ya kibiashara na kijamii. Lakini bado, katika jamii nyingi, lugha za kiserikali, kibiashara na elimu zimebakia kuwa za kimataifa -- Kifaransa, Kiingereza au Kireno. Lugha hizi ni za kigeni kwani hazina mizizi Afrika na haziendelezi uhai unaotokana na misingi ya kiutamaduni na ya kiyakinifu ya Waafrika. Kama vyombo vya thamani, kujitambua na majivuno, lugha za wenyeji si za kutafitiwa, kuwekewa kanuni na kufunzwa tu, bali pia ni za kutumiwa kufundishia katika ngazi zote na kuwa ni funguo za maarifa na busara zilizokusanywa na jamii za Waafrika kwa karne nyingi. Zaidi ya ilivyokuwa mwanzoni, vyuo vikuu vinatarajiwa na viongozi kutimiza mahitaji hayo muhimu.

Upanuzi na uhuishaji wa mfumo mzima wa elimu ni changamoto iliyopo wakati wote. Asasi za elimu ya juu zinahitajiwa ziongoze juhudi za kutambua na kueleza kwa ufasaha malengo ya elimu, mwelekeo wa mihtasari, uboreshaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, mafunzo ya walimu na mtalaa wa ujifunzaji na maendeleo ya binadamu. Kwa jinsi zanavyokubali kwa makusudi na kwa roho safi wajibu wake kamili wa kielimu, ndivyo zinavyoweza kustahili kutambuliwa na kusaidiwa kwa hali na mali na jamii yake ambayo inafahamu vyema asasi hizo. Kama hazifanyi hivyo vya kutosha, zinastahili kudharauliwa.

Maendeleo muhimu ya elimu ya juu yenye uzito sawa ni kuelezwa upya kwa dhana ya elimu. Maelezo haya mapya yamefuatiwa na marekebisho ya falsafa na sera za elimu. Hata kama kuna tofauti kiasi gani kuhusu madhumuni na makusudi ya elimu baina ya nchi, nyingi zao zimeelekea kuchukua mawazo na sera zifuatazo.

Ya kwanza ni uletaji wa demokrasia na manufaa ya elimu. Elimu inaangaliwa zaidi kuhusiana na aina ya mtu inayotaraji kumkuza. Mtu huyu mpya anaonekana kuwa amejikita katika mazingira ya kiafrika bila kuwa amejitenga na utamaduni

vya makuzi ya mtu: kimwili, kiakili, kimichezo, kijamii, kimaadili na kiroho. Pia, elimu inachukuliwa sasa kuwa ndio njia nzuri zaidi ya kugundua upya, kupanua na kukuza utamaduni na maendeleo ya wenyeji.[23]

Baadhi ya waunda sera na waelimishaji wana hofu kuwa sasa hivi mkazo mkubwa sana unawekwa katika maendeleo ya mtu binafsi bila kutilia maanani asasi za kijamii kama vile familia na asasi za dini na siasa. Wengine wanafikiri kwamba, mawazo hayo yanaweza kuwa na msingi, kwa wakati huu mfumo wa elimu umepangwa vyema zaidi kutoa mazingira thabiti yanayofaa kuwapata watu walioelimika vyema ili kuchapusha maendeleo ya jamii. Kwa upande huu, wanatoa hoja kuwa, elimu, kama inavyochukuliwa kwa mapana yake, haina budi ipatiwe msaada wote unaohitajika.

Jinsi ambavyo asasi hizo zinavyoelekea kuongeza kufaa kwake na kujishughulisha na mahitaji ya jamii, wafanyakazi na wanafunzi wanaweza wakawa na mgongano wa moja kwa moja na mamlaka za kisiasa zilizopo. Wanafunzi na viongozi wao, maprofesa, wanaweza wakagundua na kuchambua ukosefu katika utawala, kutojimudu, ukosefu wa haki au uvunjaji wa haki za msingi za binadamu, na uroho katika vyombo vya kisiasa. Jinsi ambavyo wasomi watarajiwa, wanafunzi na wanataaluma wanavyoeleza mara nyingi au hata kujishughulisha na masuala kama hayo, na aghalabu viongozi wa kisiasa hujibu kwa mabavu, na kama wakifanikiwa basi hutishia maendeleo ya asasi hizo. Aina hiyo ya mahusiano mabaya baina ya vyuo na vyuo vikuu kwa upande mmoja na uongozi wa kisiasa kwa upande mwingine, unaleta hatari kubwa inayotishia kuendelea kwa uhai wa asasi za elimu ya juu. Busara, ustahamilivu na hamu ya kuelewa na kuingia katika majadiliano yenye welewa yanaweza kusaidia kutatua tatizo hili na hivyo kuziachia asasi hizo kutimiza majukumu muhimu kwa Afrika na ubinadamu kwa jumla.

## Hitimisho

Jamii za kiafrika kama ilivyo kwa wengi wengine zilikuwa na mifumo yao ya kienyeji ya elimu kwa ajili ya kurithisha maadili, stadi na mielekeo kwa kizazi kinachofuatia. Baada ya muda, mifumo hiyo ya kienyeji iliunganishwa na ile ya kiislamu na kikristo. Aina iliyo mpya ni ile ya mtindo wa kizungu, ya kidini na ya kidunia. Kutawala kwa mfumo huo ambako kulianza enzi ya ukoloni kuliendelea hata baada ya kuondoka kwa wazungu. Kwa miongo mitatu iliyopita nchi za Afrika

[23] Kwa uchanganuzi zaidi wa sera na madhumuni ya elimu taz. UNESCO, UNECA na OAU, 1982, Waraka ED/82/MINEDAF/3. kur.9-11; na Waraka ED/82/MINEDAF/1, kur. 3-20.

huru zimefanya juhudi kubwa ya kueneza elimu hiyo kwa idadi kubwa ya watu kama inavyoruhusiwa na rasilimali walizonazo lakini hawajafaulu kurekebisha tabia yake ya kigeni.

Ingawa maendeleo yamefanywa katika kuelimisha idadi kubwa ya watu, si kutokana na uamuzi wa kisiasa na kijamii tu, bali kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa asasi za kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kitasnia, hata hivyo juhudi hazijafikia malengo yanayotakiwa yanayohusiana na ubora na idadi ya wahitimu. Hivyo, elimu ya Kiafrika bado ina safari ndefu. Mamihoni ya vijana na watu wazima hawakupata elimu (Jedwali 22.1). Uwezekano wa kupata elimu hauko sawa kwa makundi yote ya watu. Wanawake hawashiriki kwa usawa katika ngazi zote. Vijijini kuna hali mbaya zaidi kuliko mijini. Kwa sababu mbalimbali, baadhi ya makabila hayahudumiwi vya kutosha. Aghalabu mihtasari na njia za kufundishia hubakia kuwa za kitabuni na hazina uhusiano na hali halisi na matatizo yanayoikabili Afrika. Walimu wenye ujuzi ni wachache. Majengo ya shule yenye samani za kutosha, maktaba na vifaa ama havipo au havitoshi. Orodha ya matatizo ni ndefu na tata kutokana na ukweli kwamba vifaa na wafanyakazi hawatoshi na matumizi yake yanakuwa makubwa mno katika mataifa mengi ya Kiafrika.

Mahitaji ya haraka ya nchi za Kiafrika ni pamoja na kuimarisha uhuru wao, kupanua uchumi wao, na kuhuisha na kukuza utamaduni wao wa kweli. Kama kichocheo cha maendeleo na mabadiliko ya kijamii, mifumo ya elimu ya Afrika inatakiwa iwe na kazi zaidi ya kupasha maadili na maarifa kwa vizazi vya watoto. Haina budi kubadili mawazo na mitazamo ya watu binafsi na vikundi kwa njia ambayo itawezesha uundaji wa raia wenye ufahamu, wafanyakazi wazalishaji na wachacharikaji. Na kuzielezea jamii za Kiafrika katika kufikia malengo ya kusonga mbele, haki na uhuru.[24] Kutokana na ufinyu wa bajeti ulioelezwa hapo awali, ubunifu katika matumizi ya rasilimali chache unahitajika katika ngazi zote za elimu.

Elimu halisi ya kisasa inabidi iundwe na kutekelezwa katika mazingira ya elimu ya kudumu na ya maisha yote, itakayowafikia wote na yenye nia ya kuendeleza mielekeo na tabia za watu binafsi ili kuwawezesha kuyaelekeza maisha yao ya baadaye na wachangiaji wa mageuzi ya kijamii.

Kukubaliwa kwa elimu hii iliyoelekea katika uhalisi, usasa na maendeleo kunahitaji kuunda upya kikamilifu mihtasari, njia za ufundishaji, na utayarishaji wa waalimu. Kunahitaji kuendeleza mihtasari ambayo mielekeo yake ya kisayansi na kiufundi itadhihirishwa na uhusiano wa kiubunifu wa elimu kulingana na mazingira

[24] Taz. UNESCO, 1976, kur. 49-50

yake halisi na ya kijamii.

Kama sehemu ya uundaji upya huo, elimu ya juu haina budi kuelezwa upya na kuwa na dhima mpya. Utafiti na mafunzo katika ngazi zote tatu za elimu hayana budi yalingane na hali halisi ya kiuchumi na kijamii kwa njia ambayo elimu itakuwa jibu la mahitaji ya maendeleo. Uigaji wa kanuni na vifani kutoka nje haufai. Uundaji mitazamo mipya na urekebishaji wa ile ya zamani na kuiingiza kwa kufanya ifanye kazi kwa ajili ya Afrika ni mambo muhimu katika shughuli hii. Ukuzaji huu wa elimu asilia ya wenyeji hauna budi ushirikishe na kuchukua majaribio ya kigeni yaliyofanikiwa, na wakati huohuo uyachambue kiuhakiki matokeo ya marekebisho yaliyofanywa au yaliyokopwa na kuyalinganisha na hali halisi ya mambo yaliyoko Afrika.[25] Majaribio ya kuvutia yanafanyika hivi sasa kwa upande huo. Yaliyo ya msingi zaidi yaliyoangaliwa ni: kipindi cha mpito baina ya elimu ya kisomi kuwa elimu ya umma; na uhusianaji wa shule na maisha na usisitizaji wa umoja wa kiutamaduni na wa kitaifa. Mitazamo kama hiyo, pamoja na majaribio na utafiti unaoendelea hivi sasa, inatarajiwa kuwa na mafanikio kufikia malengo yanayotafutwa.

JEDWALI 22.1 Kutokujua kusoma katika Afrika: makadirio na matarajio ya kutojua kusoma kulingana na nchi, watu wenye umri zaidi ya miaka 15. (M = wanaume, K = wanawake).

Jedwali lifuatalo lililotayarishwa na UNESCO linawakilisha, kwa nchi zile ambazo zina takwimu muhimu, makadirio na matarajio ya baadaye ya viwango vya kutojua kusoma kwa kila nchi mnamo 1985, 1990 na 2000; Msomaji inabidi afikirie hali zitakazoweza kuathiri matarajio hayo. Kwa nchi zinazotoa taarifa zinazohitajika, kiwango cha jumla cha kutojua kusoma kimetokana na uchanganuzi wa viwango vya ongezeko la kila kizazi. Kufuatana na kiwango cha watu walioanza kuchunguzwa kutoka kwenye sensa moja hadi nyingine na kutoa mchoro thabiti: urekebishaji wa mchoro huo wa kitakwimu huruhusu ukadiriaji na uwekaji wa matarajio ya viwango vya kutojua kusoma kwa njia inayoridhisha.

Kwa baadhi ya nchi ambazo hazina taarifa za kutosha za kitakwimu, ukadiriaji wa jumla jumla wa kiwango cha kutojua kusoma (miaka 15 na zaidi) ulifanywa, bila kutilia maanani viwango vya kila kizazi. Kwa njia hiyo, kwa kutumia data zote zilizoweza kupatikana kwa nchi zote, uchanganuzi wa awali ulifanywa ili kuamua

[25] Kama ilivyonukuliwa kabla, kur. 22 - 47

| Nchi | Watu wasiojua kusoma (kwa maelfu) 1985 1990 2000 | Viwango vya kutojua kusoma (kwa asilimia) Jumla M K |
|---|---|---|
| Cameroon = | Kameruni | |
| Central Africa = Republic | Jamhuri ya Afrika ya Kati | |
| Equatorial = Guinea = | Guinca ya Ikweta | |
| Libyan Arab = Jamahariya | Jamhuri ya Kiarabu ya Libya | |
| Mozambique = | Msumbiji | |

*Nchi zilizo katika kundi la nchi zisizoendelea zaidi duniani.

Chanzo:UNESCO (1990) Mkusanyiko wa Takwimu kuhusu kutojua kusoma, Na. 31, Idara ya Takwimu za Elimu, Ofisi ya Takwimu (Paris: UNESCO).

uhusiano muhimu uliopo baina ya kutojua kusoma na vipengele vingine vya uchumijamii na elimu. Mrudio mmoja ulioamuliwa mwishowe ulikuwa na vipengele vilivyoeleza: vifo vya watoto, kiwango cha uzazi na uwiano wa uandikishaji katika elimu ya msingi. Kufuatana na njia hii viwango kadha vilikadiriwa, lakini kutokana na ukosefu wa uhakika wa baadhi yao, si vyote vimeingizwa katika jedwali hili. Upunguaji mkubwa wa viwango vya kutojua kusoma unatarajiwa si kwa nchi zile ambazo kampeni kamambe za kisomo zimetekelezwa au zinaendelea hivi sasa. Kampeni hizi zinaweza kubadili kabisa viwango vya kutojua kusoma vya makundi ya watu, lakini kutokana na kutokuwepo na taarifa za kutosha, matokeo ya kampeni hizo za hivi karibuni hazikudhihirishwa kwenye matarajio haya. Vivyohivyo, imeonekana ni vyema kutotoa makadirio kwa nchi kama Ethiopia na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zimekuwa na kampeni muhimu za kisomo hivi karibuni.

Picha:

# 23

# Afrika na Diaspora

Katika karne ya ishirini na hasa baada ya Vita Vikuu vya I vya Dunia, ilikuwa ni Mnegro Mmarekani ambaye alizungumza kwa nguvu sana kuhusu haki za Mnegro Mwafrika wakati wa kutayarisha mkataba wa Versailles na uundaji wa Shirikisho la Mataifa, wakati sisi hatukuwa na nafasi ya kuweza kuzungumza kwa niaba yetu wenyewe[1]. (A. Diop, 1958).

Hatuna budi kukumbuka kwamba wao (watu weusi waliotawanyika) ni sehemu yetu. Hawa vijana wa kiume na mabinti wa Afrika walichukuliwa kutoka pwani zetu, na ... bado hawajasahau viungo vyao na wahenga wao ... Siku nyingi hata kabla wengi wetu hatujatambua kudhalilishwa kwetu, watu hawa walipigania usawa wa taifa na jamia ya Afrika ... Sasa kwa vile sisi tulio ndani ya Afrika tunaelekea kwenye ukombozi ... kamilifu wa bara hili, uhuru wetu utatoa mchango mkubwa kwenye jitihada zao za kupata haki kamili za kibinadamu na heshima kama raia wa nchi yao[2]. (K. Nkrumah, 1958).

Manukuu yaliyo hapo juu yanaonyesha kwamba uhusiano mkubwa wa kihistoria kati ya bara la Afrika na Watu Weusi waliotawanyika uliendelea hata baada ya 1935. Uhusiano huo ulidumu na ulihimiliwa na uzoefu wa kisaikolojia na wa kijamii ambao ulisababisha upinzani, maasi na kuanzishwa kwa jitihada za kimataifa ili kuhakikisha kwamba kunapatikana uhuru na usawa kwa Waafrika na madhuria wao waliokuwa ng'ambo, katika nchi za nje. Uzoefu ambao Waafrika katika bara la Afrika waliupata chini ya ukoloni ulichangia kujenga maoni yao kuhusu Waafrika waliokuwa ng'ambo.

Lakini wazo la "wokozi" wa Afrila la kuwapatia watu weusi uhuru na kuonyesha uwezo wao wa kutawala na kuchangia kwenye ustaarabu wa ulimwengu lilijitokeza

[1] A. Diop. 1958
[2] K. Nkrumah, 1958a

kama nguvu kubwa kwenye Diaspora ya Waafrika, na lilisababisha kuanzishwa kwa vikundi kadhaa vya kimataifa vya watu weusi vya kudai uhuru. Kilele cha mfumko huo wa jitihada za Waafrika na wale wa Diaspora kilijidhihirisha katika vuguvugu la upanafrika (umoja wa Afrika yote) kati ya 1900 na 1935, huku shughuli nyingi zaidi zikiwa kwenye miaka ya 1920, kutokana na jitihada za Marcus Garvey, W.E.B. DuBois na wengine waliokuwa huko Ulaya na Marekani, na wanafunzi wa Kiafrika, hasa huko Ufaransa na Uingereza. Sasa ni kitu gani kilichotokea kwenye uwanja wa Diaspora kuanzia 1935 na kuendelea?

Bila shaka sababu ya msingi ya Diaspora katika karne zote ilikuwa ni biashara ya watumwa iliyovuka Bahari ya Mediterania, Bahari ya Hindi na zaidi Bahari ya Atlantiki. Kuanzia mwanzoni mwa karne hii - hasa kuanzia 1935 hadi kwenye miaka ya 1960, mfumo wa kikoloni ndio uliosababisha msukumo mkubwa zaidi. Idadi kubwa zaidi ya Waafrika waliokuwa wakitafuta uhuru wa kiuchumi na wa kisiasa walikimbilia uhamishoni kwenye miji mikuu ya Ulaya. Hii ilikuwa kweli kwa Afrika ya Kaskazini iliyotawaliwa na Wafaransa na makoloni ya Wabelgiji, na hasa kwa Algeria, ambamo maelfu ya watu walihamia Ufaransa katika kipindi hiki kinachojadiliwa. Wakati wa Vita vya uhuru huko Algeria, walikuwepo kiasi cha Waalgeria 45,000 huko Ufaransa na wachache sana kati yao walirejea nyumbani[3]. Msukumo mwingine mkubwa ulikuwa ni shauku ya elimu ya juu. Kwa hali hiyo idadi ya wanafunzi wa Kiafrika waliokuwa wakienda Ulaya na Marekani iliongezeka sana kati ya 1935 na 1960 na wengi miongoni mwao hawakurudi kabisa nyumbani. Katika kipindi hiki uhamiaji wa Waafrika huko Amerika ya Kusini, Visiwa vya Karibiani na huko India ulikoma kabisa. Idadi yao kubwa ikawa inaelekea huko Ulaya na Marekani. Idadi ya Waafrika waliohusika katika uhamaji huu ilikuwa ndogo, kwani waliohusika zaidi walikuwa ni wanafunzi.

Kuanzia miaka ya 1960 na kuendelea, Diaspora iliendelea ijapokuwa kwa mara nyingine tena hulka na msukumo wake ulibadilika. Wahamiaji wa kipindi hiki zaidi hawakuwa wanafunzi bali mafundi na wataalamu waliobobea kama vile madaktari, wahandisi, wafanyabiashara, wanamuziki, wasanii na wahadhiri wa Vyuo Vikuu. Pia katika kipindi hiki, mwelekeo wa wahamaji hao ulirudia hali iliyokuwepo hapo awali ya kabla ya karne ya ishirini, ambapo watu walihamia pote duniani, kwani Waafrika hawakwenda Ulaya na Marekani tu, bali pia walikwenda Mashariki ya Kati, kwenye nchi za Kijam[illegible], [illegible]da, Australia na nchi za Pasifiki ya Kusini.

[3] Kwa maelezo mazuri zaidi kuhusu uhamiaji wa Waljeria kwenda ulaya, tazama C.R. Ageron, 1979.

Wapo wahadhiri na maprofesa wa Kiafrika wanaofundisha katika Chuo Kikuu cha Papua New Guinea! Hii ni hali ambayo imekuja kujulikana kama "uhamaji wa wataalamu," na kwa kweli hali hii ilitisha sana kwenye miaka ya 1960 na 1970, na kwa bahati sasa inaonekana kupoa moto. Katika kipindi hiki waganga, waganga wa meno, wanasayansi, wahandisi na walimu wa Kiafrika walikuwa ni watu wa kawaida kuwaona huko ng'ambo. Wakati ambapo Afrika ilihitaji sana utaalamu wao, wao walikuwa ni ushahidi chanya kwamba Afrika ilikuwa "imewasili" kiakili, kiutamaduni na kisiasa.

Sura nyingine ya Diaspora ya hivi karibuni inahusu uhamaji wa kijinsia ambao unawahusu wanawake wanaohamia Ulaya, hasa huko Ufaransa, Ujerumani, Uingereza na Marekani, wakitafuta kazi na kujaribisha bahati zao. Kisha kuna sura ya tatu ya Diaspora ya kisasa, yenye kushakini ile ya wanawake, kwa upande wa wanaume wenye elimu kiasi, wasio na ujuzi na wasio na mafunzo yoyote ya kitaalamu, wakitafuta bahati yao kwa njia yoyote ile halali au isiyo halali.

Kategoria mpya na ya mwisho ya Diaspora ya kisasa inawajumuisha wale wanaoziacha nchi zao na kuhamia ng'ambo ama kwa kudumu au kwa muda kwa sababu za kisiasa. Wengine kati yao ni waathiriwa wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, wengine ni waathiriwa wa migogoro ya mipakani, wengine ni wale wanaoshindwa katika mbinu zao za kupindua serikali za nchi zao, na mwisho ni wale wanaofukuzwa nchini kwa sababu moja au nyingine, kama vile kufanya ujasusi kwa ajili ya nchi nyingine.

Sababu kuu za kuendelea kuwepo kwa mabadiliko ya sura ya Diaspora ni kuongezeka kwa uduni wa hali ya uchumi-jamii na wa kisiasa, na haja ya kuwa na ajira ya kuridhisha.

## Waafrika kwenye Diaspora tangu 1935

Je, Waafrika hawa wa Diaspora wamekuwa wakifanya nini kwenye makazi yao mapya katika uwanja wa Upanafrika kuanzia miaka ya 1930? Matukio mawili ya miaka ya mwishoni mwa 1930 — yaani uchokozi wa Italia kwa Ethiopia (1935-41) na kuzuka kwa ufashisti huko Ulaya — yalichochea kwa kiasi kikubwa dhana ya upanafrika na shughuli za Afrika Yote, hasa huko Ulaya na Marekani.

Huko Uingereza, Chama cha Kimataifa cha Marafiki Waafrika wa Ethiopia (IAFÉ) kilianzishwa mnamo 1936. Ofisi ya Kimataifa ya Huduma kwa Mwafrika (IASB) ilianzishwa mnamo 1937 na ilikuwa na ufanisi mkubwa zaidi katika

kushawishi mawazo ya Waingereza juu ya mgogoro wa Ethiopia. IASB ilikuwa imeundwa kwa madhumuni ya kuwahudumia watu weusi nchini Uingereza katika nyanja za elimu, uchumi na siasa.

Mguyana Makonnen, kwa msaada wa wenzake Dkt. Peter Milliard, Jomo Kenyatta wa Kenya, na George Padmore, alianzisha Kampuni ya Uchapishaji ya Panafrika ambayo ilichapisha jarida la kila mwezi la Panafrika. Alikuwa na duka la vitabu lililoitwa "Mchumi" pamoja na msururu wa mikahawa na vilabu. Mtandao huu wa biashara ulitoa mwanya kuwezesha kufanyika kwa mkutano uliofanikiwa zaidi wa watu weusi kabla ya kipindi cha uhuru. Viongozi wakuu walikuwa ni Peter Abrahams wa Afrika Kusini, Wallace-Johnson wa Sierra Leone na baadaye Kwame Nkrumah. Hawa, mnamo 1944, walianzisha Shirikisho la Panafrika, ambalo lilitayarisha Mkutano wa Tano wa Panafrika uliofanyika huko Manchester mwaka 1945.

Huko Marekani, chini ya uongozi wa William Leo Hansberry, watu weusi kutoka Afrika na wale wa Diaspora mwaka 1934 walianzisha Baraza la Utafiti la Ethiopia (ERC) ili kueneza habari kuhusu Ethiopia na kusaidia kuanzisha mtandao wa Kimataifa wa watu weusi ili kufanya kazi kwa niaba ya Ethiopia. Waratibu walitambua kwamba Ethiopia ilikuwa na mvuto mkubwa miongoni mwa watu wa Afrika na kwamba kihistoria utambuzi wa urithi wa Ethiopia uhitia msukumo kwenye itikadi ya ukombozi ambayo iliendelea kujitokeza mara kwa mara kama msukumo wa utambulisho na mshikamano katika Afrika na katika Diaspora. ERC ilianzisha mahusiano ya kiutendaji na watu binafsi katika miji kadhaa ya Marekani, Ethiopia, Uingereza, Ufaransa, Italia na katika Visiwa vya Karibiani.

Wakati Italia ilipoivamia Ethiopia Waafrika wengi walionyesha shauku yao ya kujiunga na jeshi la Ethiopia, lakini Amerika ilitangaza kutojihusisha na upande wowote na hivyo kuwazuia Waafrika kushiriki katika vita hivyo. Pamoja na hali rasmi iliyokuwepo, marubani wawili Maafro-Amerika, Hubert Julian na John Robinson, wakiwa wametiwa moyo na ERC, walikwenda Ethiopia kupigana. Robinson alikuwa rubani binafsi wa mfalme na mshauri wake wa mambo ya usafiri wa anga. Akijulikana kama Brown Condor, Robinson aliruka safari kadhaa za kwenda Ethiopia.

Cha muhimu zaidi katika kushiriki kwao ni michango ya Diaspora ya hali na mali. Walipanga maandamano ya wananchi na kuandika tahariri na makala zilizounga mkono jitihada za Ethiopia. Marafiki wa Ethiopia (FAO) wakiongozwa na Willis Huggins, mwalimu Mwafro-Amerika, kwa kipindi cha mwaka mmoja

tayari walishahamasisha kuanzishwa kwa matawi katika miji 106 na mayambo 19. Mipango ya kuchangisha fedha ilifanywa kwa ushirikiano na Chama cha Kimataifa cha Marafiki wa Ethiopia huko London[4].

Mfano mwingine wa kusifika wa kuunga mkono Ethiopia ulitoka kwenye Kamati ya Afya kwa ajili ya Ulinzi wa Ethiopia, kikundi cha madaktari weusi kutoka Visiwa vya Karibiani na Amerika waliokuwa wakifanya kazi huko New York. Walituma angalau shehena moja au mbili za madawa kwa Waethiopia waliokuwa vitani. Hisia zilizounga mkono Ethiopia zilisikika sana miongoni mwa Marastafaria ambao hapo awali walikuwa wamemtukuza Mfalme Haile Selassie na kujiita cheo chake cha awali cha Ras Tafari[5].

Toleo rasmi la *Sauti ya Ethiopia* lilikuwa ni gazeti la Jumuiya ya watu weusi na Marafiki wa Ethiopia kila mahali. Lilikuwa na dhima kubwa sana katika kuainisha upya watu wa Afrika. Lilipinga matumizi ya istilahi "Mnegro" kama "zana ya matusi" ya kuwagawa watu weusi. Istilahi "weusi" lilipendwa na wengi.

Gazeti la *Sauti* lilichapisha makala za George Padmore, Mnamdi Azikiwe, W.E.B. DuBois, J.A. Rogers na wengine. Maswali ya chemsha bongo kuhusu historia ya watu weusi yalitokea mara kwa mara na taarifa za watu weusi kama vile Toussaint Louverture wa Haiti, Mfalme Menelik wa Ethiopia, James Aggrey wa Gold Coast, Richard Wright wa Amerika na wengine wengi. Matawi ya EWF yalianzishwa kote Marekani na Karibiani; jambo hili linatoa mwanga kuhusu ukubwa wa athari yenyewe.

Wakati Haile Selasie alipoutwaa tena ufalme wake mnamo 1941 aliunga mkono kuanzishwa kwa shule ya mseto ya kwanza ya Ethiopia. Waafro-Amerika kadhaa kutoka Barbados, Guyana, Puerto-Riko na Marekani walikwenda Ethiopia ambapo walifanya kazi kama marubani na mafundi makenika.

Pia uvamizi wa Ethiopia wa mwaka 1937 uliofanywa na Italia ulichochea chama cha Kamati ya Kimataifa ya Afrika ambayo mwaka 1941 ilikuja kuwa Baraza la Mambo ya Afrika[7] na ilianzishwa na Max Yergan. Yeye pamoja na marafiki zake waliamini katika fikra za Umarx na walikuwa na mawasiliano mazuri na Chama cha Kikomunisti cha Marekani, ijapokuwa hawaonekani kama walikuwa wanachama wakati huo huo. Wakati huo, msimamo wa kawaida wa siasa ulikuwa

[4] W.N. Huggins na J.G. Jackson, 1937, uk.90-1, na 1935

[5] Nyaraka za Marekani, 884, 142/19, Picha/Makala, Viambatisho; tazama pia L. Barrett, 1977.

[7] H. Lynch, 1978.



PICHA 23.1: *Watu mashuhuri katika Diaspora ya Waafrika, mashuhuri kwa kupigania haki za watu weusi: juu kushoto, George Padmore; juu kulia, Paul Robeson na W.E.B. DuBois; chini kushoto, Markus Garvey; chini kulia, Max Yergan.*

"kuungana dhidi ya ufashisti" ambao ulijumuisha kushirikiana na wakomunisti. Wanazuoni wengi, wanachama wa vyama vya wafanyakazi na wengine walishirikiana na wakomunisti ili kufikia malengo yao, na watu weusi hawakuwa tofauti na hao.

Malengo ya Baraza hili yalikuwa ni kuhimiza ukombozi wa kisiasa wa Waafrika na kuendeleza hali zao za kijamii, na za kiuchumi, kwa kusambaza taarifa zao muhimu za wakati huo, kusaidia kuwapatia mafunzo Waafrika huko Ulaya na Marekani, na kupanga ziara za kutembeleana na kushirikiana miongoni mwa watu wa Afrika.

Baada ya 1941 Baraza lilijitosa zaidi katika utetezi wa Afrika na upinzani wa ukoloni kwa jumla. Matawi yalianzishwa katika miji mikuu kadhaa ya Marekani na kuwajumuisha kuwa wajumbe watu kama Roseberry T. Bokwe, daktari wa afya kutoka Afrika Kusini ambaye pia alikuwa mwanachama wa African National Congress (ANC). Barua pamoja na malalamiko yalitumwa kwa serikali za Marekani na za Ulaya pamoja na kwenye mashirika ya kimataifa, na vikundi vya Kiafrika vya wafanyakazi na vya kitaifa vilihimizwa. Matokeo ya athari za Baraza hilo yanajidhihirisha pale chapisho lake la *Afrika Mpya* lilipopigwa marufuku huko Kenya, Afrika Kusini na Kongo ya Wabelgiji.

Katika mwaka 1944 kama watangulizi wa kikundi cha ushawishi kuhusu Afrika huko Marekani, wajumbe kadhaa wa Baraza hilo walikutana na maofisa wa Kitengo cha Afrika kilichoundwa wakati huo huo kwenye Serikali ya Marekani na kupendekeza sera ya kuunga mkono Afrika. Matokeo yake yalikuwa ni kuanza kuwatumia wataalamu wachache weusi wa masuala ya Afrika. Katika Mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliofanyika huko San Fransisko mwaka 1945, Yergan na Eslanda Robeson walitoa mwito wa kuendeleza uchumi, siasa na ustawi wa jamii ya Waafrika. Baraza lilihimiza mahsusi kwamba nchi zote zilizokuwa chini ya udhamini na nchi zote za Kiafrika zilizokuwa chini ya Hispania, Ureno na Italia, isipokuwa Eritrea, zote ziwekwe chini ya uamana wa Umoja wa Mataifa, na kwamba Afrika ya Kusini isiwe mjumbe wa baraza hilo la uamana.

Baada ya Vita Vikuu vya Pili ya Dunia, Baraza hilo lilizidisha kuwa mpinzani wa Marekani kwa kauli zake. Hali hii kwa upande mmoja ilitokana na Vita Baridi vilivyokuwa vikizipambanisha Mashariki na Magharibi, lakini pia kutokana na ongezeko la vuguvugu la kudai uhuru katika Afrika na kwenye Diaspora. Baraza lilionyesha wasiwasi maalumu kuhusu Afrika Kusini, sio tu kutokana na uzoefu wa Yergan nchini humo, lakini pia kutokana na vitendo vya kuwadhalilisha watu weusi, hasa kuanzia miaka ya mwisho ya 1940. Njaa iliyotokea Afrika Kusini ilizidisha hali hiyo. Hata hivyo Baraza lilianzisha Kamati ya Msaada dhidi ya Njaa kwa Afrika Kusini ambayo ilituma pesa na chakula ili kupunguza tatizo lililokuwepo.

Kujumuishwa kwa Afrika ya Kusini-Magharibi katika Afrika Kusini kulizuia malalamiko makali.

Mwaka 1949 bodi ya Baraza ilikuwa ya watu weusi tu. Paul Robenson alichaguliwa kuwa mwenyekiti, W.E.B. DuBois makamu mwenyekiti, na Hunton alichaguliwa kuwa katibu mtendaji. Kuongezeka kwa siasa kali kwenye Baraza hilo kulijidhihirisha, na hali hiyo iliwaletea usumbufu mwingi kutoka kwa Serikali ya Marekani; lakini Baraza liliendelea kupigania haki na mambo ya Waafrika hadi lilipofutika mwaka 1955. Kwa hali hiyo lilifungua njia ya ushawishi mpana na wa kufaa zaidi wa Mwafrika-Mmarekani kwa ajili ya Afrika na mambo ya baadaye yaliyohusu dunia ya watu weusi.

## Mkutano wa Tano wa Panafrika

Vyama kadhaa na mikutano iliyoendeshwa huko Ulaya, Afrika na Marekani kwa kuratibu hatua za vitendo kwa niaba ya Waafrika na madhuria wao huko ng'ambo ilisababisha kuitishwa kwa Mkutano wa Tano wa Panafrika (Afrika Yote) uliofanyika huko Manchester, Uingereza mwaka 1945. Mkutano huu chini ya uenyekiti wa DuBois, kusema kweli ndio uhoanzisha dhana ya upanafrika kama vuguvugu la ukombozi wa Afrika, zaidi kuliko huko Ulaya na Marekani. Mkutano huo uliunganisha usomi wa DuBois na utendeti wa Garvey, na kutoa ishara kwa ulimwengu mzima kwamba mapambano halisi ya ukombozi yamehamishiwa Afrika pamoja na kwa viongozi wake. Zaidi ya hayo, pamoja na kwamba watu Weusi wa Marekani na wale wa maeneo yaliyozungumza Kiingereza katika Karibiani ndio waliojulikana zaidi na waliokuwa mashuhuri zaidi kwenye Upanafrika hadi mwaka 1945, katika miaka ya 1950 madai ya usawa katika Marekani yalichukua aula katika shughuli yote.

Hata hivyo, ushirikiano na Afrika bado uliendelea kuwepo. Huko nyuma katika mwaka 1947 Alioune Diop, Msenegali aliyekuwa huko Paris, alianzisha *Présence africaine*, jarida lililojitoa kwa ajili ya utamaduni wa Kiafrika na kusomwa sehemu nyingi. Mwaka 1957 Diop aliitisha mkutano mkuu wa waandishi wote Weusi duniani. Kutokana na mkutano huo kulianzishwa *Société africaine de culture* (SAC) (Chama cha Kitamaduni cha Afrika) ambacho kilileteleza kuanzishwa kwa tawi lake huko Marekani lililoitwa *America Society of African Culture* (AMSAC)

lililoongozwa na John A. Davis. AMSAC ilichapisha jarida lililojulikana kama *African Forum*. SAC na AMSAC vilishirikiana katika mikutano kadhaa, maonyesho na machapisho, na hivyo kuimarisha mahusiano ya Kipanafrika.

Ilipofikia miaka ya katikati ya 1960, Malcolm X, Kiongozi wa Taifa la Waislamu ("Waislamu Weusi") alikuwa tayari ameshajitokeza kama mtu mashuhuri miongoni mwa Waafrika-Wamarekani kwa ujumla, lakini hasa kati ya vijana. Alihimiza mafunzo kuhusu asili ya Uafrika na Kujitawala miongoni mwa Weusi. Mwaka 1964 alianzisha Chama cha Umoja wa Waafrika-Wamarekani ambacho alitarajia kuwa kingewaunganisha Waafrika—Wamarekani wote katika mapambano yao ya kitaifa na kushirikiana na Umoja wa Nchi Huru za Afrika pia. Kuuawa kwake Februari 1965 kulisitisha jitihada zake hizo. Lakini tawasifu yake iliyoandikwa na Alex Haley na kitabu cha *Waliolaaniwa (Wretched of the Earth)* kilichoandikwa na Franz Fanon kutoka Martiniki, vilikuwa ndio vitabu vya kiada kwa viongozi vijana waliokuwa wanazuka kwenye vuguvugu la *Black Power*, (Nguvu ya Weusi) lililojumuisha watu kama Stokely Carmichael, Walter Rodney na wengineo.

Ilipofikia miaka ya mwisho ya 1960, vijana Waafrika—Wamarekani huko Marekani ndio waliokuwa vikosi vya mbele vya mwamko wa Kiafrika wa kimataifa uliokuwa unazuka kwa nguvu. Sio tu kwamba walionyesha fahari katika mitindo yao ya maisha iliyotoka Afrika, bali pia walidai mafunzo ya taaluma ya watu Weusi (taaluma kuhusu Afrika na Diaspora) katika shule na vyuo vyao. Hivyo machapisho mengi yalitokea kasi ili kusaidia juhudi za uanzishaji na upanuzi wa taaluma ya Watu Weusi, taaluma ya Waafrika—Wamarekani, taaluma ya Panafrika, Taaluma ya Uafrika na kadhalika katika vyuo na vyuo vikuu vingi vya Weusi na Weupe. Waafrika kutoka barani na wale wa Diaspora waliongoza na kufundisha programu hizi.

Vuguvugu la Taaluma ya Weusi limepata ushindi mkubwa kutokana na kujitenga kwa idadi kadhaa ya wasomi wa Kiafrika na wale wa Diaspora kwenye mkutano wa Chama cha Taaluma ya Weusi katika Marekani uliofanyika huko Kanada mwaka 1969[8]. Kikundi hiki kilichojitenga, kilichojiita Chama cha Taaluma ya Urithi wa Kiafrika (AHSA), kilianza kuwa na mikutano yake chenyewe, kufadhili machapisho na kuhimiza tafsiri mpya ya historia ya watu weusi kwa mtazamo wa mtu mweusi. Kilihimiza vifaa kuhusu urithi wa Mwafrika visambazwe katika shule zote, na kuhimiza ushirikiano wa kimataifa miongoni mwa wasomi weusi. Kilele

[8] I.S. Reid, 1976.

cha AHSA kilitokea katika mkutano wake wa 1970 ambapo zaidi ya wajumbe 2000 kutoka Afrika na Diaspora walikutana kwenye Chuo Kikuu cha Howard.



PICHA 23. 2 *Malcolm X, mpiganiaji wa dhati wa haki za weusi.*

Pia huko Marekani kulikuwa na kumakinika rasmi kwa viongozi weusi kwenye mambo ya Afrika na ya Diaspora. Kuanzia 1969 wabunge weusi wa Bunge la Marekani walianza mikutano isiyo rasmi chini ya uenyekiti wa Charles Diggs. Kundi hili lilijiunga rasmi mwaka 1971 kama Mkutano wa Siri wa Wabunge Weusi. Pamoja na kusimamia na kupendekeza sera zinazowahusu Waafrika-Wamarekani, Mkutano huo ulifanya vivyo hivyo kwa mambo ya Afrika na ya huko Karibiani. Wajumbe kadhaa wa Mkutano huu walisafiri sana kote Afrika na Karibiani; walilaumu sera za Marekani huko na kuanzisha sheria za kusaidia maeneo hayo. Mara kadhaa kikundi hiki cha Wabunge Weusi kilifanikiwa kuungwa mkono ndani na nje ya bunge lenyewe la Marekani na kwa hali hiyo kuwa msukumo wenye athari kubwa kwa ajili ya uhuru na usawa katika Marekani na huko ng'ambo.

Kuanzia 1969 Weusi huko Marekani wameanzisha vyama vingi vya kiutamaduni, kisiasa na kimaendeleo vikijishughulisha na Waafrika na kuwa na uhusiano na Diaspora, mathalani; Baraza la Wasomi la Waafrika — Wamarekani, Mkutano Mkuu wa Uongozi wa Wanegro wa Marekani kuhusu Afrika, Kamati ya Kuratibu siku ya Uhuru wa Afrika, *Africare* (kujali Afrika), Mkutano wa Watu wa Afrika na vinginevyo. Vyama hivyo — pamoja na maendeleo ya aina hiyo hiyo huko Afrika — vilisaidia kujenga mawasiliano miongoni mwa watu wa Afrika, na kuleteleza kuitishwa kwa Mkutano wa Sita wa Panafrika uliofanyika Dar es Salaam mwaka 1974.

Vuguvugu la Taaluma ya Weusi limepata ushindi mkubwa kutokana na kujitenga kwa idadi kadhaa ya wasomi wa Kiafrika na wale wa Diaspora kwenye mkutano wa Chama cha Taaluma ya Weusi katika Marekani uliofanyika huko Kanada mwaka 1969[8]. Kikundi hiki kilichojitenga, kilichojiita Chama cha Taaluma ya Urithi wa Kiafrika (AHSA), kilianza kuwa na mikutano yake chenyewe, kufadhili machapisho na kuhimiza tafsiri mpya ya historia ya watu weusi kwa mtazamo wa mtu mweusi. Kilihimiza vifaa kuhusu urithi wa Mwafrika visambazwe katika shule zote, na kuhimiza ushirikiano wa kimataifa miongoni mwa wasomi weusi. Kilele cha AHSA kilitokea katika mkutano wake wa 1970 ambapo zaidi ya wajumbe 2000 kutoka Afrika na Diaspora walikutana kwenye Chuo Kikuu cha Howard.

Pia huko Marekani kulikuwa na kumakinika rasmi kwa viongozi weusi kwenye mambo ya Afrika na ya Diaspora. Kuanzia 1969 wabunge weusi wa Bunge la Marekani walianza mikutano isiyo rasmi chini ya uenyekiti wa Charles Diggs. Kundi hili lilijiunga rasmi mwaka 1971 kama Mkutano wa Siri wa Wabunge Weusi. Pamoja na kusimamia na kupendekeza sera zinazowahusu Waafrika-Wamarekani, Mkutano huo ulifanya vivyo hivyo kwa mambo ya Afrika na ya huko Karibiani. Wajumbe kadhaa wa Mkutano huu walisafiri sana kote Afrika na Karibiani; walilaumu sera za Marekani huko na kuanzisha sheria za kusaidia maeneo hayo. Mara kadhaa kikundi hiki cha Wabunge Weusi kilifanikiwa kuungwa mkono ndani na nje ya bunge lenyewe la Marekani na kwa hali hiyo kuwa msukumo wenye athari kubwa kwa ajili ya uhuru na usawa katika Marekani na huko ng'ambo.

Kuanzia 1969 Weusi huko Marekani wameanzisha vyama vingi vya kiutamaduni, kisiasa na kimaendeleo vikijishughulisha na Waafrika na kuwa na uhusiano na

[8] I.S. Reid, 1976.

Diaspora, mathalani; Baraza la Wasomi la Waafrika — Wamarekani, Mkutano Mkuu wa Uongozi wa Wanegro wa Marekani kuhusu Afrika, Kamati ya Kuratibu siku ya Uhuru wa Afrika, *Africare* (kujali Afrika), Mkutano wa Watu wa Afrika na vinginevyo. Vyama hivyo — pamoja na maendeleo ya aina hiyo hiyo huko Afrika — vilisaidia kujenga mawasiliano miongoni mwa watu wa Afrika, na kuleteleza kuitishwa kwa Mkutano wa Sita wa Panafrika uliofanyika Dar es Salaam mwaka 1974.

Mpanafrika Profesa St Clair Drake alibashiri kuwa Sherehe za kwanza za Sanaa ya Mtu Mweusi huko Dakar, Senegal, mwaka 1966, ziliashiria kwamba Upanafrika wa kiutamaduni ungeweka msingi mpana zaidi wa utambulisho na ushirikiano miongoni mwa watu wa Afrika kuliko unaoweza kuletwa na Upanafrika wa kisiasa. Kwa wachunguzi wengine wasiokuwa na ubashiri kama wa Drake, Mkutano Mkuu wa Sita wa Upanafrika mwaka 1974 kwa hakika ulidhihirisha athari ndogo ya kisiasa ya Weusi wa Diaspora katika vikao vya bara zima.

Wawakilishi wa Diaspora kwenye Mkutano huo Mkuu walishuhudia udhalilishaji wa jamia kwa pendekezo lililokosoa "siasa za rangi ya ngozi." Wamarekani-Waafrika walikosolewa pia kwa kutokushirikiana na wafanyakazi weupe[9].

Kwa mara nyingine Drake anasaidia kuchanganua tatizo hilo. Ametofautisha kati ya dhana ya Upanafrika iliyotawaliwa na hisia za rangi ambayo ilishikiliwa na Wapanafrika wa mwanzo na Upanafrika wa kontinenti unaowavutia wale wanaotaka umoja wa bara zima. Dhana hii ya pili haijumuishi tu Afrika Kaskazini, bali pia inawahimiza watu wasiokuwa weusi kutoka Brazil na Kuba hasa idadi kubwa ya jumuiya zilizokuwa na wahenga wa Kiafrika kuwawakilisha na kuwasemea watu weusi ambao mara nyingi walinyimwa haki ya kujiwakilisha, kwa sababu ya kukosa usawa katika siasa, uchumi na elimu.

Wapanafrika wenye kujikita kwenye rangi ya ngozi wanapinga katakata hali hii.

Kwa kweli sasa dhana ya Upanafrika ipo kwenye hatua ya mpito. Waafrika kutoka barani wanajihusisha zaidi na mambo yanayohusu umoja na maendeleo ya kitaifa; matatizo ambayo ni ya kawaida kwa bara zima na ambayo kwa hali hiyo yanahimiza aula ya kujenga umoja wa bara zima. Aina ya rasilimali zinazotakiwa na nchi za Kiafrika kwa ajili ya maendeleo, ukubwa wa mahitaji hayo na miundo

[9] St.C. Drake na R.B. Laporte, 1982.

iliyopo ya kuwezesha upatikanaji wa rasilimali zinazotakiwa, vyote hivi vina upendeleo mkubwa wa uhusiano baina ya nchi na nchi na kugharamiwa na mashirika ya kimataifa na mataifa makubwa. Nchi zinazoongozwa na Waafrika nje ya Afrika nazo zina aula zao za kikanda zenye kuhitaji fedha nyingi. Na Weusi wa Diaspora wasiokuwa na mamlaka juu ya serikali zao wana fursa ndogo sana kutoa msaada unaotakiwa huko Afrika au popote pale penye dunia ya watu weusi, bila kuanzisha miundo imara isiyokuwa ya kiserikali, yenye uhusiano na nchi za ng'ambo.

Marekani ndiyo nchi pekee iliyokuwa na uwezo wa kutoa msaada mkubwa na ambayo ina idadi kubwa ya watu wenye asili ya kiafrika wanaojali masuala ya kiafrika. Lakini watu hao ni wachache wasiokuwa na nafasi ya kutengeneza wala ya kutekeleza sera ya nje. Na hata hivyo, wao na Waafrika wengine wa Diaspora, mara nyingi hukubali utambulisho wa taifa lao. Wazo la awali la upanafrika la kuwarudisha watu wengi Afrika kwa pamoja haliwavutii wengi miongoni mwao, wala miongoni mwa Waafrika, ambao tayari watu wao hawana ajira na hupata huduma chache sana za kijamii. Hivyo, fikra za jinsi ambavyo Waafrika wa Diaspora wangeweza kutia shinikizo kwenye serikali zao na kutoa msaada wa kiuchumi na kisiasa kwa Afrika ndizo zinazotawala kwenye majadiliano ya watu weusi wakati huu.

Kwa kuangalia mgongano wa dhana za umoja wa bara na ule wa rangi katika Afrika, tofauti za itikadi na ukweli wa uraia huko Afrika na katika Diaspora, tunaweza kujiuliza: je, ni nini mustakbali wa uhusiano wa Afrika na Diaspora hapo baadaye? Wote wawili wana utambulisho imara wa kisaikolojia na wa kijamii ambao unaimarisha mtandao wa kimataifa na ambao unaweza kutoa shinikizo kwenye serikali za kitaifa ili kuunga mkono sera na programu zenye manufaa kwa watu wa Afrika. Hii ndiyo falsafa inayohimili Chama cha *TransAfrica* (Uvukaji wa Afrika), ushawishi wa chombo cha Waafrika-Wamarekani kwa ajili ya Afrika na Karibiani. Ni matunda ya ushawishi wa awali wa Waafrika-Wamarekani na sasa wanao utaalamu, jamii ya weusi yenye kuwaunga mkono na msaada kwa juhudi zao.

Mifano ya juhudi za *Trans Afrika* inaweza kuonekana katika mikutano ifuatayo: Tamasha la Utamaduni na Sanaa ya Dunia ya Weusi na Afrika (FESTAC-77) huko Lagos, Nigeria, ambalo lilileteleza kuanzishwa kwa mawasiliano katika Afrika na katika Diaspora kupitia mikutano ya kimataifa, maonyesho na machapisho; Mkutano Mkuu wa Utamaduni wa Mtu Mweusi katika Amerika ambao ulifanyika

huko Kolombia (1977), Panama (1980), Brazil (1982), na kutoa machapisho kadhaa; Tamasha la Diaspora ya Afrika huko Brazil (1979), Haiti (1980), Surinam (1982), Senegal (1983), na Barbados (1985); Mikutano ya Wataalamu wa Diaspora wa UNESCO huko Haiti (1978), Barbados (1980), Benin (1983), Brazil (1985), ambayo imetoa machapisho kadhaa; Taasisi ya Kwanza na ya Pili ya Taaluma ya Diaspora kwenye Chuo Kikuu cha Howard (1979), na Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya (1981), ambapo matokeo yake ni kitabu na kijarida cha Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispania; Mkutano Mkuu wa Dunia juu ya Mapokeo na Utamaduni wa Orisha kwenye Chuo Kikuu cha Ife, Nigeria, (1981). na Bahia, Brazil, (1983); Uhusiano wa Afrika/Afro-Amerika; Kutoka Utegemezi kwenda kwenye Kujitegemea huko Monrovia, Liberia, (1983), mkutano ambao ulitoa "Tamko la Liberia" lililotaka ushirikiano miongoni mwa watu wa Afrika na muunganisho wa rasilimali zao[10]. Mikutano mingine yenye malengo na makusudio na matokeo kama hayo pia imefanyika.

Kuenea kwa vyama na mikutano ya Diaspora tayari kumeimarisha sana njia za mawasiliano miongoni mwa watu wa Afrika, kumeinua viwango vyao vya vitendo na vya kuonea fahari, kumehamasisha miradi ya utafiti na machapisho na kwa hali hiyo kupanua dimbwi la utaalamu na elimu ya watu wa Afrika. Hata hivyo, vikundi kadhaa vya madhuria wa Kiafrika vimebakia bila kujulikana sana kutokana na kiwango kidogo cha utafiti na machapisho kilichopo.

## Upeo wa dunia nzima wa mwamko wa Kiafrika

Ni muhimu kujua kwamba suala la Diaspora ya Afrika ni la dunia nzima na kwamba jumuiya kadhaa za madhuria wa Kiafrika zisizojulikana zinathibitisha kwa nguvu kabisa kwamba wana utambulisho wa Afrika. Huko Amerika ya Kusini, kwa kawaida mkondo rasmi ni kwamba madhuria wa Kiafrika wamekuwa ama bado wanaendelea kusimilishwa kwenye tamaduni za wale wanaozungumza Kireno au Kihispania, utambulisho wa rangi ya ngozi katika ripoti nyingi za sensa za watu ulikoma katika miongo kadha iliyopita, na ni vigumu kubainisha mambo ya kijamia. Hata hivyo Wafrika wa Amerika ya Kusini sio tu kwamba wanaakisi Uafrika wao

[10] Kijarida cha Taaluma za Diaspora ya Kiafrika, juzuu 1, Na.1, lilichapishwa mwaka 1948 kwa Kiingereza, Kifaransa, Kispanishi, na Kireno; Tazama pia *Carib*, 1981.

katika fasihi na nyimbo bali pia wameandaa mipango ya kupinga ubaguzi wa rangi na kuratibu programu za kujisaidia, na za elimu na utamaduni[11].

Ijapokuwa kuwapo kwa Waafrika huko Argentina, Bolivia, Paraguay kumegubikwa kabisa, idadi ndogo ya Waafrika huko Peru ina kikundi cha tamthilia, *Expresion Negra Peruna*, na taasisi ya Utafiti wa Waafro-Peru (*Instituto de Investigaciones Afro-Peruana*.) Huko Equador ambapo kadirio la watu weusi lilikuwa kati ya asilimia 10 na 15, kukiwa na wilaya chache zenye watu weusi zaidi ya asilimia 50 ya wakazi, *Centro de Estudios Afro-Equatorianos* (Kituo cha Taaluma ya Waafro-Equador) ina matawi hadi kwenye miji na vijiji kadhaa. Mwaka 1983 *Centro* iliitisha Mkutano Mkuu wa Panamerika kuhusu Wanawake Weusi. Huko Venezuela kwenye idadi ya Watu Weusi iliyokisiwa kuwa takribani asilimia 30, kwenye *Instituto Autonomo Biblioteca Nacional* ipo Sehemu ya Afrika na Afro-Amerika. Idadi ya Weusi huko Kolombia inakisiwa kuwa kati ya asilimia 30 na 40, na kuifanya kuwa jumuiya kubwa kuliko zote za Kiafrika-Kihispania yenye asili ya Kiafrika. Vyama vikubwa vya Waafrika wa Kolombia ni: Shirika la Utafiti wa Sanaa-jadiya ya Kolombia, Kituo cha Utafiti wa Utamaduni Mweusi na vuguvugu la Utamaduni wa Mweusi. Asasi ya kwanza mnamo 1983 iliandaa kongamano la kitaifa kuhusu bibliografia ya Waafrika wa Kolombia; asasi ya pili ilichapisha jarida la *Presentia Negra* kila mwezi[12].

Kwa upande wa Brazil ambayo ina utamaduni wa kihistoria wa kuendeleza sera ya usimilishaji, ipo idadi kubwa ya kutosha ya Waafrika wa Brazil ambayo itafanya Waafrika wa Brazil kuwa jumuiya ya Diaspora kubwa zaidi kuliko zote, na imekuwa na athari kubwa kwenye utamaduni wa wale wasiokuwa na asili ya Kiafrika. Isipokuwa kwa maelfu ya wahamaji wa hiari Waafrika-Wabrazil waliohamia Gold Coast, Togo, Dahomey na Nigeria katika karne ya kumi na tisa, bado Wabrazil Weusi wanaonekana kutokuwa na mafanikio makubwa sana katika kuanzisha na kuhimili uhusiano na bara la Afrika au hata na Diaspora hadi siku za hivi karibuni.

[11] L. hout, 1976, ni kitabu kizuri sana kwa suala hili; vyanzo muhimu kwa sasa ni pamoja na Palenque, chapisho rasmi la Kituo cha utamaduni cha Waafro-Ekwado [centro cultural Afro-Ecutoriano]; Jarida la Maarifa [Boletin Infomativo], chapisho la mara kwa mara la Taasisi ya Uchunguzi wa Afro-Peruana [the Institutode Investigaeiones Afro Peruana,] Lema, Peni; na J.M.R. Guedez, 1985.

[12] Presentia Negra ni chapisho rasmi la Kituo cha utafiti wa utamaduni wa Kinegro, Bogota, na Kolumbia. [the centro para la Investigacion de la cultura negra, Bogota, Columbia].

Gazeti linaloitwa *Afro-Brazil* linachapishwa huko Salvadore, Bahia, eneo ambalo idadi kubwa ya Waafrika wa Brazil wanaishi. Pia huko Salvadore ipo taasisi ya *Centro de Estudos Afro-Orientais* ambamo kunapatikana *Museo Afro-Brasileiro* (Makumbusho ya Waafrika-Brazil) Kwenye makao makuu, *Brasilia*, kikundi cha watafiti *kwenye Pro Memoria* hushughulikia urithi wa Waafrika wa Brazil.

Kituo cha *Centro de Estudos Afro-Asiaticos* cha Chuo Kikuu cha Candido Mendes huko Rio de Jeneiro kinafadhili mihadhara na machapisho kwa masomo yanayohusu Waafrika wa Brazil. Pia huko Rio kuna taasisi inayoitwa *Instituto de Pesquisas e Estudos Afro-Brasileiros* (IPEAFRO) iliyoongozwa na Abdias Nascimento, na ambayo inachapisha jarida linalojulikana kama *Afrodiaspora*[13].

Chama kinachojulikana kama *Movimento Negro Unificado Contra a Discriminacao Racial* kila mwaka tarehe 20 Novemba kinatoa ufadhili wa kusherekea Siku ya Taifa ya Mwamko wa Mtu Mweusi, siku ambayo Zumbi wa Palmares, Mwafrika mwanzilishi wa Palmares Quilombo, aliuawa na Wareno mwaka 1695. Mnara wa kumbukumbu ya heshima ya Zumbi umekubaliwa kujengwa na serikali ya Brazil. Matawi ya *Movimento Negro* yanapatikana huko Marekani na kwingineko[14].

Nchi za Amerika ya Kati zinashiriki kwenye utamaduni wa Hispania. Baadhi ya nchi hizo zina aina mbili za madhuria wa Kiafrika, wenyeji na wahamiaji. Hao wenyeji ni raia wa kuzaliwa, wahamiaji ni madhuria wa wafanyakazi waliohamia kutoka nchi jirani zilizokuwa zikizungumza lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo mgogoro mkubwa ulizuka kutokana na sera za serikali za "Kuhispanisha." Jambo hili linajionyesha dhahiri huko Kosta Rika ambako maaskari mamuluki wa karne ya kumi na tisa na wafanyakazi wa baadaye wa ujenzi wa reli na wafanyakazi kwenye mashamba ya migomba waliwasili kutoka Jamaika, Trinidad na Visiwa vingine vya Karibiani[15].

[13] *Afrodiaspora*: Revisto Quadrimental Do Mundo Negro (Rio de Janeiro), Limehaririwa na A.D. Nasci-mento; na Estudos Afro-Asiaticos, limechapishwa na Centro de Estudos Afro-Asiaticos [Kituo cha Taaluma za Kiafrika-Kiasia] Rio de Janeiro, yote ni majarida ya kila mara.

[14] Zumbi, Chama cha Utamaduni wa Kiafrika-Kibrazili. New York; Tawi la New York huchapisha, Kijarida kuhusu historia na utamaduni wa Waafrika-Wabrazili.

[15] St. C. Drake na R.B. Laporte, 1982; C. Melendez na Q. Dunean, 1981

Panama ina tatizo linalofanana na hilo, lakini tofauti na Kosta Rika ina idadi kubwa zaidi ya umma wa watu weusi wa makundi ya wenyeji na wahamiaji kuliko maeneo mengine. Kundi la wahamiaji walitokea zaidi huko Barbados, Jamaika, Trinidad na Marekani, na walitumiwa na Marekani kujenga na kuimarisha Mfereji wa Panama. Umoja wa Kampuni ya Matunda pia uliingiza watu weusi kufanya kazi kwenye mashamba yao makubwa. Hawa waajiri wa Kimarekani waliendeleza desturi zao za ubaguzi ambazo zilizidisha mahusiano mabaya. Hata hivyo, vipo vikundi vya mwamko wa Weusi kwenye jumuiya zote mbili za watu weusi.

Idadi ya Watu Weusi huko Meksiko ni ndogo sana na labda haizidi asilimia moja. Kituo kipya cha Taaluma ya Waafrika kinahamasisha shauku ya utamaduni wa Kiafrika pamoja na dhana ya Upanafrika. Huko Kuba, ambako idadi ya watu Weusi inakadiriwa kuwa kati ya asilimia 30 na 40, tofauti na maeneo mengine ya Watu Weusi wanaozungumza Kihispania, Waafrika wa Kuba wamekuwa ni washiriki wenye sauti katika siasa za Kuba kwa karibu karne hii yote. Hata hivyo pamoja na kwamba Nicholas Guillen alianzisha tapo la ushairi wa Kuba lenye dhana ya unegro ambalo lilichota uasili wake kutoka Afrika, serikali ilitilia mkazo kwenye wazo la utaifa badala ya tamaduni hizi tofauti zilizokuwepo. Lakini athari za Kiafrika zimebakia zenye nguvu katika muziki, fasihi, dini na mitindo ya maisha, vyote hivyo labda vikiwa vimeimarishwa na kurishiki kwa Waafrika wa Kuba katika jeshi na mambo yote yaliyohusiana na jeshi huko Ethiopia na Angola[16].

Ijapokuwa kihistoria Asia ilipokea watumwa wengi sana, idadi ndogo ya wafanyabishara huru na wengine kutoka Afrika, hakuna kabisa utafiti unaohusiana na maendeleo ya athari zao kwa wakati huu. Bado utafiti unatakiwa uendeshwe kwa kuzingatia eneo zima la ulimwengu lililofikiwa na Waafrika kuanzia Uturuki hadi Mashariki ya Kati, Asia ya Kusini na ya Mashariki, pamoja na visiwa vya Bahari ya Hindi na ile ya Pasifiki.

Madhuria kadhaa wa Kiafrika huko India wanaendelea kufanya sherehe zao za asili, kuimba na kucheza kwa kufuata muziki wa Kiafrika na wengine kati yao bado wanaweza kuzungumza kwa Kiswahili. Mambo haya ni ushahidi kamili kuwa, Wasiddi au Wahabeshi bado wana utambuzi wa wahenga wao wa Kiafrika. Kwa hakika mwaka 1973 ujumbe wa Waafrika hawa wa Kihindi ulitembelea Uganda, Kenya na Tanzania ili kupata ufahamu zaidi kuhusu mambo ya bara hili na kuangalia


[16] R.F. Thompson, 1983 ni utafiti mzuri sana wa taathira za Kiafrika katika sanaa na filosofia katika Kuba, Haiti na sehemu nyingine za Amerika, ikiwa ni pamoja na Marekani.

maeneo ambayo wanaweza kushirikiana nao. Mbali na athari yoyote iliyoletwa na ujumbe huo, la muhimu ni kwamba ilisaidia kuwajulisha Waafrika wa bara hili kuhusu Waafrika-Wahindi.

Idadi ya Waafrika wa Diaspora huko Ulaya pia imeongezeka sana. Mwaka 1983 kulikuwepo takriban Waafrika 1,572,164 kutoka Afrika Kaskazini huko Ufaransa (866,595 Waalgeria, 492,669 Wamoroko, na 212,909 Watunisia).,Idadi hii inaendelea kusababisha mgogoro sio tu huko Ufaransa bali kati ya nchi hiyo na nchi za Afrika Kaskazini. Idadi kubwa ya Waafrika hao kutoka Afrika ya Kaskazini wanazidi kupatiwa uraia wa kuandikishwa, licha ya vipingamizi kutoka nchi za Afrika Kaskazini, ambazo zinavutiwa zaidi na kuwarejesha watu hao nyumbani. Jinsi hatua hizo za kuwaandikisha uraia zinavyozidi kuendelea uhusiano kati ya Ufaransa na majirani zake wa kusini huko Afrika bila shaka utaendelea kuwa wa wasiwasi, lakini huenda baada ya muda mrefu madhuria hawa watakuwa daraja la kuleta uhusiano mwema[17]. Muhimu pia ilikuwa ni ongezeko la weusi huko Uingereza — hasa kutoka West Indies, Amerika na Afrika — na mwingiliano kati yao na watu wa Uingereza. Leo hii, tamasha la kila mwaka la jumuiya za West Indies huko London limekuwa tukio la utamaduni la kudumu, aidha, muziki wa Watu Weusi, dansi, vyakula na sanaa vimekuwa na athari kubwa kwenye utamaduni wa Waingereza.

Ijapokuwa kuna nyufa za kutisha za elimu yetu kuhusu Waafrika wa Diaspora, ni wazi kwamba wao wamekuwa na historia muhimu ambayo imekuwa na athari kubwa kwenye sehemu nyingine ulimwenguni. Wametoa mchango mkubwa usiopimika kwenye nguvukazi katika kilimo, viwanda na kwenye maendeleo ya kiteknolojia duniani. Dini zao kadhaa hasa huko Brazil na Kuba zimebakiza nduni za Kiafrika na pia zinawafuasi na ishara zisizokuwa za Kiafrika. Lugha zao zimeathiri sana lugha zenye asili ya Kirumi na lugha nyinginezo na zinaendelea kusikika, kwa mfano huko Ulaya, Amerika na India. Sanaa yao iliwaathiri watu kama vile Picasso na wengineo wakati muziki na dansi zao zinaendelea kugeuza midundo ya umma wa ulimwengu.

[17] Kuhusu suala hili, *Tazama La Nouvelle generation de L'immigration maghrebine, essai d'analyse sociologique*, 1982; Esprit, 1985; na *Les Temps Modernes*, 1985.



PICHA 23.3 *Kanivali ya Notting Hill tamasha la mitaani la kila mwaka la jamuiya za West Indies, mjini London*

Wanasayansi wa Diaspora - George Washington Carver katika kilimo, Charles Drew katika plazma ya damu, na Hidrus Poindexter katika madawa ya tropiki, na wengine wengi, wametumia vipaji vyao kuendeleza ustawi wa binadamu. Wanasosiolojia na wanaathropolojia kutoka Diaspora hii wametoa mwanga kuhusiana na utata wa mipangilio ya kijamii. Na jadi yao ya kupambana na ukandamizwaji wa Waafrika na wanadiaspora iliyodumu kwa karne nyingi imewafanya wajitokeze mstari wa mbele katika utetezi wa haki za binadamu kama ilivyodhihirishwa na washindi wa Nishani za Nobel kina Ralph Bunche, Albert Luthuli, Martin Luther King Jr. na Askofu Mkuu Desmond Tutu.

## Changamoto

Waafrika wengi kutoka bara la Afrika, wakijumuisha wakuu wa nchi, watumishi wa serikali na wa kigeni, wanataaluma na wafanyabiashara, wanadumisha uhusiano wa karibu na Waafrika-Wamarekani. Kwa bahati mbaya, uhusiano huo hauna muundo utakaowezesha au kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano huo kwa mtindo wa kudumu. Mbali kabisa na uhusiano wa kibinafsi uliopo, tofauti za kiitikadi, umbali na matatizo ya mawasiliano, matatizo muhimu ya kitaifa na matatizo ya ukosefu wa fedha — vyote hivi vimechangia dhidi ya uanzishwaji wa miundo ya ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya watu weusi.

Zaidi ya hayo viongozi wa serikali na nchi za Kiafrika wanalazimika kuchunguza vipingamizi au matatizo ambayo yanaweza kuletwa na mataifa makubwa na kuathiri mambo yao ya kidiplomasia na ya kiuchumi kutokana na kushiriki kwao kwenye mtandao wa Watu Weusi. Sio viongozi wote wana msimamo wa Upanafrika wa Kwame Nkrumah, na sio wengi walio jasiri kama Julius Nyerere ambaye, akiwa raisi wa Tanzania mwaka 1977, alisisitiza juu ya kutoa mhadhara wake mkuu huko Marekani kwenye Chuo Kikuu cha Howard ambapo watu wengi Weusi waliweza kumfikia. Na ni serikali chache mno za bara zinazoweza kuchukua hadharani msimamo kama wa Nigeria wa kujiona kuwa msemaji wa Watu wa Afrika duniani kote. Na ijapokuwa OAU ilitoa pongezi zake kwa Marekani kwa mafanikio yake ya angani mnamo mwaka 1962 na kukemea ubaguzi wa rangi dhidi ya Waafrika-Wamarekani, na imemkaribisha Mkurugenzi wa *TransAfrica* Randal Robinson kwenye vikao vyake vingi vya siri, hata hivyo kwa kawaida chombo hicho kimekuwa kimya kwenye mambo ya kuendeleza mitandao ya kimataifa ya Waafrika.

Hata hivyo nchi nyingi za Kiafrika zina umri wa kizazi kimoja na zimekumbana na matatizo ya aina nyingi katika kipindi ambacho uamuzi wa tofauti ya sekunde unaweza kumaanisha maisha au kifo, kufaulu ama kushindwa. Na wengi kati ya viongozi hao walikuwa wasomi katika mazingira ya kikoloni na walipokea hatamu za uongozi wa serikali kutoka kwa walezi wa kikoloni waliopenda wahakikishiwe kwamba hawatawahi hata siku moja kurejelea katika walau kudokeza tu mwamko wa rangi au kufanya malipizi kwa unyonyaji wa nyuma wa watu wa Afrika. Lakini kukiwa na viongozi wa kizazi kipya huko Afrika na kwenye Diaspora, na wakithamini zaidi urithi na hali ya kijamii ya kihistoria wanayoishiriki kwa pamoja, upo uwezekano

mkubwa kwamba jitihada mpya zitafanywa ili kujenga upya muundo wa kudumu wa ushirikiano kati ya Afrika na Diaspora yake.

Sio tu kwamba karne ya ishirini na moja itashuhudia makutano ya siasa — uchumi imara ya Kiafrika yenye uwezo wa kufikia bwawa la elimu na ustadi wa Diaspora, bali pia huenda itashuhudia ujumuishaji wa jumuiya zilizosambaa kote zenye asili ya Uafrika kwenye mzingo wenye maana wa Umoja wa Afrika Yote.

24

# Dhana ya Upanafrika na muungano wa Kikanda

Dhamira ya sura hii ni dhana ya Upanafrika (Afrika Yote) kama nguvu ya kuunganisha yenye lengo la kutaka kupata umoja wa kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi au ushirikiano katika Afrika. Historia ya dhana ya Upanafrika inaangukia kwenye awamu tatu zinazojidhihirisha waziwazi: awamu ya ukoloni 1935 hadi 1957, awamu ya uhuru 1957 hadi mwishoni mwa miaka ya 1960, ambayo imeelezewa kama kipindi cha ustawi wa Upanafrika kama vuguvugu la Ukombozi; na awamu ya tatu kuanzia miaka ya 1970. Katika awamu hii ya mwisho, dhana ya Upanafrika kama nguvu ya kuunganisha imepokea msukumo mkubwa kutokana na mabadiliko ya kushangaza yaliyokuwa yanatokea katika uchumi wa ulimwengu pamoja na athari za kutisha zilizoletwa na mabadiliko haya kwenye chumi za Afrika.

Ijapokuwa dhana ya Upanafrika kama vuguvugu la kuunganisha ilizingatiwa sana katika miaka ya 1920, ilipoteza mvuto wake kwenye miaka ya 1930 na 1940, miaka ya neema kwa ukoloni wa Afrika. Dhana hii ilihuishwa kwa kiasi fulani katika miaka ya 1940 kutokana na juhudi za Nkrumah na Padmore huko Uingereza pamoja na juhudi za Msenegali Alioune Diop. Mapema kiasi cha 1942 Nkrumah alisisitiza kwamba makoloni yote ya Afrika ya Magharibi "kwanza yalitakiwa yaungane na kufanya taifa moja, na huru lililozingirwa tena na utawala wa kigeni, kabla ya kuweza kijihusisha na kiwango kikubwa cha ushirikiano wa kimataifa." Pia katika mwaka 1947 kulizaliwa *Présence africaine*, vuguvugu la kiutamaduni ambalo lilichukua mawazo makuu ya wafuasi wa dhana ya Upanafrika pamoja na Mkutano Mkuu wa kwanza wa Upanafrika. Wanazuoni kadhaa wa Kizungu na wa Kiafrika waliungana na Diop, na walihusika katika uchapishaji wa vitabu vya msingi kama vile *Nations négre et culture*, kilichoandikwa na Sheikh Anta Diop. Fikra za jumla za wapigania haki wa *Présence africaine* zilielekea kuashiria

kwamba isingewezekana kwa ua la utamaduni wa Kiafrika kuchanua kwenye hali ya utegemezi wa kisiasa, na kwamba watu weusi walitakiwa kuungana kwa mshikamano katika mapambano haya. Kwa hiyo walitakiwa kujinasua kutoka mikononi mwa wakoloni hao na kudai utu wao.

## Dhana ya Upanafrika na muungano wa Kontinenti zima

Licha ya jitihada za kuungana za miaka ya 1930 na 1940, hakuna jambo kubwa lililokuwa limefanikiwa ilipofikia mwaka 1957. Ilikuwa ni kuanzia tarehe hizo, hasa baada ya Ghana kupata uhuru wake chini ya uongozi wa Kwame Nkrumah, ambapo dhana ya Upanafrika kama vuguvugu kuunganisha kilipojaribiwa tena kwa nguvu zaidi na kwa kuzingatia lengo halisi. Katika kipindi hiki lengo halikuwa tu kufikia muungano wa kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi, bali kufanya hivyo kwa viwango vya kikanda, Kikontinenti na hata kuvuka kanda (yaani kiwango cha Afrika na Jumuiya ya Uchumi wa Ulaya).

Mwongozaji wa mwendo katika kipindi hiki alikuwa Kwame Nkrumah. Hatua yake ya kwanza kwenye mwelekeo huo ilikuwa ni kuunda Umoja wa Ghana-Guinea mnamo 1958 na kisha Umoja wa Ghana-Guinea-Mali kama hatua ya kwanza kuelekea "Umoja wa Nchi za Kiafrika." Hatua ya pili ilikuwa ni Mkutano wa Nchi Huru za Kiafrika, ulioandaliwa huko Akkra Aprili 1958, mwaka mmoja tu baada ya uhuru wa Ghana. Mkutano huu ulihudhuriwa na nchi zote za Afrika zilizokuwa tayari zimepata uhuru, yaani Misri, Ethiopia, Ghana, Libya, Morokko, Sudan na Tunisia. Huu ulifuatiwa na Mkutano wa kihistoria wa Watu wote wa Afrika uliofanyika 1958, kwa mara nyingine tena huko Akkra; Mkutano wa Sanniquelli wa Ghana na Liberia Julai 1959; Mkutano wa Pili wa Nchi Huru za Afrika huko Monrovia, Agosti 1959; na wa Tatu huko Addis Ababa mwaka 1960. Mikutano yote hii mitatu ilitetea, miongoni mwa mambo mengine, uanzishaji wa soko pana la pamoja katika bara hili. Kwa mfano mkutano wa kwanza wa 1958, ulipendekeza kuondolewa kwa ushuru na vikwazo vinginevyo vya kibiashara miongoni mwa nchi za Kiafrika na kufikia hitimisho la makubaliano ya pamoja ya namna ya kulipana kwa lengo la kuimarisha mabadilishano ya kiuchumi na mwishowe kuanzishwa kwa soko la pamoja. Ili kuleta msukumo kwenye jambo hili la kiuchumi, mwaka 1958 kulianzishwa Tume ya Uchumi ya Afrika, ambayo shughuli zake zimejadiliwa kwa kirefu katika sura ya 14.

Mikutano yote hii ilitetea kwa raghba muungano wa kisiasa au umoja wa kisiasa wa Afrika. Kwa Nkrumah, mambo yote mawili yalikuwa ni hali mbili muhimu za

awali kwa ajili ya kupata maendeleo kamili na ya haraka sio tu kwa bara zima bali pia kwa nchi zote huru zikiwa zimeunganishwa kwenye umoja. Alitahadharisha dhidi ya shirikisho za kikanda, ili kuepusha uaminifu wa kikanda usije ukausaidia ubeberu na ukoloni mamboleo kuvua kwenye maji yenye migogoro.

Kiungo hiki cha vuguvugu la umoja wa kisiasa na lile la soko la pamoja la bara kiliwafanya wale viongozi wa Kiafrika waliokuwa wakipinga umoja wa kisiasa kulipa uzito mdogo sana suala la soko la pamoja. Tishio la ukoloni mamboleo kwao halikuonekana kama sababu ya kutosha kwa hatua za haraka zilizotakiwa kuchukuliwa ambazo zingewanyang'anya madaraka ya kitaifa na kuweka nchi zao chini ya utawala mmoja wa kisiasa. Mkutano wa Addis Ababa wa 1960 ulikuwa na maana kubwa sana kwa vile pale ndipo ambapo mgawanyiko miongoni mwa nchi za Kiafrika kuhusu jinsi ya kufikia umoja wa Afrika ulipojitokeza wazi.

Kupatikana kwa uhuru kwa nchi nyingi za Kiafrika kati ya 1960 na 1964 kulitatiza sana katika upatikanaji kwa dhana ya muungano ya Upanafrika. Viongozi wapya wa Kiafrika waligawanyika kwa mlalo kati ya kundi la mrengo wa mashariki na kundi la mrengo wa magharibi, na wima kati ya wanamapinduzi, wapenda maendeleo, wapinga maendeleo, mabepari, wajamaa, wanamapokeo na wale waliokuwa katikati ya njia. Zaidi ya hayo lengo kuu la dhana ya Upanafrika katika miaka ya 1960 lilikuwa ni kuimarisha mapambano ya kisiasa kwa ajili ya uhuru wa nchi ambazo zilikuwa bado chini ya utawala wa kikoloni. Matokeo yake ni kwamba maendeleo ya kiuchumi hayakuwa sehemu kuu ya madhumuni ya sera hiyo. Pia nchi mpya zilizopatiwa uhuru wake zilikuwa zikishughulikia zaidi matatizo ya nchi zao ya wakati ule ya kuunganisha vikundi vya kikabila na vile vya kimkoa, kuimarisha vyama vyao na mamlaka yao juu ya raia wao na dhidi ya viongozi wapinzani, vita dhidi ya umaskini, magonjwa na ujinga, pamoja na usalama wa mataifa yao dhidi ya Vita Baridi na mapinduzi ya serikali ya ndani ya nchi.

Viongozi wa Kiafrika walianza kujigawa kwenye makambi yanayolingana, hasa juu ya hatima ya dhana ya muungano ya Upanafrika. Mnamo 1961, Ghana, Guinea, Misri, Mali, Moroko, Libya na serikali ya Algeria iliyokuwa uhamishoni ziliunda kundi la Kasablanka, wakati nchi nyingine zilizobakia na ambazo hapo awali zilikuwa chini ya ukoloni wa Kifaransa pamoja na Nigeria, Ethiopia, Liberia na Sierra Leone ziliunda kundi la Monrovia. Kwa jumla kundi la Kasablanka lilipendelea umoja thabiti wa kisiasa kulingana na mawazo ya Nkrumah ya kuhusu Umoja wa Madola ya Afrika. Kundi hili lilijumuisha wanamapambano wa Upanafrika, wajamaa, na wakuu wa nchi za Afrika zisizofungamana na upande




PLATE 24.1 *President G. 'Abd al-Nasser of Egypt with President M. Kadhaffi of Libya and General M. Fawsi, the Egyptian war minister, on a military inspection in the United Arab Republic, 24 June 1970*

wowote, ambao waliamini katika ugatishaji wa mipango ya kiuchumi na maendeleo kwa bara zima, ulinzi na mfumo wa usalama wa bara zima, na urejeshaji wa utamaduni wake.

Kundi la Monrovia lilipendelea shirikisho huria la nchi huru za Kiafrika ambalo lingeendeleza ushiriki wa hiari na ushirikiano katika kubadilishana mambo ya kiutamaduni na maingiliano ya kiuchumi. Kundi hili lilishupalia sana haja ya kuheshimu mipaka na utaifa wa kila nchi. Kundi hili lilitilia shaka juu ya tamaa binafsi za viongozi kadhaa katika kundi la Kasablanka, na kuingiliwa kati katika mambo ya ndani ya nchi zao.


Hata hivyo, makundi yote mawili yalishikilia ahadi ya ukombozi kamili wa makoloni yaliyokuwa yamebakia, na sera ya kutofungamana na upande wowote. Kutokana na jitihada zisizokoma za kundi la Kasablanka, Seku Ture na Modibo Keita, na hasa Nkrumah, kuungwa mkono na Mfalme Haile Selassie wa Ethiopia, Mkutano Mkuu wa Nchi za Kiafrika ulifanyika huko Addis Ababa mwaka 1963, ili kusuluhisha mgogoro uliokuwepo, kuunganisha viongozi na kuunda muundo wa pamoja wa Afrika Yote. Viongozi 30 wa ncbi na serikali huru za Afrika walitia sahihi Mkataba wa Umoja wa Afrika ambao uliunda Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU kwa Kiingereza) tarehe 25 Mei, 1963.

Kama malengo, muundo na shughuli za OAU tangu kuanzishwa kwake zinaonyesha nusu mafanikio katika dhana ya muungano ya Upanafrika, basi mafanikio yake ni madogo zaidi kuzingatia matarajio ya Wapanafrika wa zamani na wenye siasa kali walioongozwa na Nkrumah. Kwenye kila Mkutano wa OAU hadi alipopinduliwa mwaka 1966, Nkrumah alifanya kampeni kwa ajili ya kugeuza OAU na kuifanya serikali ya muungano au kuifanya moja kwa moja kuwa Muungano wa Madola ya Afrika.

Kipengee cha muungano cha Upanafrika kilipoteza kasi yake katika nusu ya pili ya miaka ya 1960 kutokana na mambo kadhaa, kama vile kuundwa kwa OAU na kujishughulisha kwake na suala la ukombozi la Upanafrika kama itakavyojadiliwa hapa chini; nchi huru nyingi kumakinikia maendeleo ya ndani ya nchi zao na uimarishaji wa uhusiano na watawala wao wa zamani wa kikoloni; na zaidi ya yote kupinduliwa kwa Nkrumah. Nafasi ya Upanafrika ilitwaliwa na vuguvugu la kuunda vikundi vya Kikanda au mataifa. Ilipofikia mwaka 1977 kulikuwa na zaidi ya vikundi 20 vya mahusiano baina ya serikali, mahusiano ya serikali nyingi, na uhusiano wa kiuchumi katika Afrika kwa lengo la kukuza na kuendeleza ushirikiano wa kiufundi na kiuchumi. Vingi kati ya vyama hivi vilianzishwa katika miaka ya 1960, siku za neema za muungano wa Afrika. Lakini muongo huo ulijulikana pia kwa kufifia kwa vikundi kadhaa vya kikanda. Ilipofikia miaka ya 1970 lau kama si mapema zaidi, ilikuwa dhahiri kwamba jitihada za muungano wa Afrika zilikuwa kwenye matatizo makubwa.

Kwa mfano kulikuwepo na jitihada mbili miongoni mwa nchi za Afrika ya Magharibi zilizozungumza Kifaransa, ambazo zililetelеza kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Afrika ya Magharibi (*UDAO - Union douanière de l'Afrique de l'Ouest*) mnamo Juni 1959 na Chama cha Forodha cha Nchi za Afrika ya Magharibi (UDEAO - *Union douanière et èconomique de l'Afrique de l'Ouest*) mnamo Juni

1966: vyombo vyote viwili vilikufa. Jumuiya ya Uchumi ya Afrika ya Magharibi (CEAO - *Communauté économique de l'Afrique de l'Ouest*) iliyoundwa mwaka 1973, ndiyo jaribio la hivi karibuni katika muungano wa kikanda kwa nchi nyingi zilizokuwa kwenye shirikisho la awali la Afrika Magharibi iliyokuwa chini ya Wafaransa. Chama cha Forodha na Uchumi cha Afrika ya Kati (UDEAC - *Union douanière et èconomique de l'Afrique Centrale*) kilichoanzishwa Januari 1966 nacho hakikufanya vizuri sana; vikwazo kwenye ufunguzi wa masoko na kutokubaliana na sheria zake kulinyonya nguvu zake zote za kuwa mfumo wa kuunganisha nchi. Vivyo hivyo Baraza la Nchi Zinazosikilizana (*Conceil de l'Entente*) lililoanzishwa mwaka 1959 kwa jitihada za Rais Houphouët-Boigny wa Côte d'Ivoire linaonekana kufifia nguvu na umuhimu wake, kutokana na kuelekeza nguvu nyingi mno kwenye mkusanyiko mkubwa zaidi wa CEAO.



PICHA 24.2: *Kuanzia kushoto kwenda kulia: Rais H. Maga wa Dahomey; Rais Houphouet-Boigny wa Cote d'Ivoire; Rais H, Diori wa Niger; Rais M. Yameogo wa Upper Volta: Wakuu wanne wa nchi katika Conseil de l'Entente, baada ya mkutanokatika kasri ya Elysée, Paris April 1961.*


Oganizesheni ya Nchi za Mto Senegal (OERS - *Organisation des états riverains du Sénégal*) ambayo haikuishi kwa siku nyingi, ilirithiwa katika mwaka 1972, na Oganizesheni ya kuendeleza Mto Senegal (OMVS - *Organisation pour la mise en valeur du fleuve Sénénegal*), ambayo hadi leo haijafanikiwa kuanzisha mfumo wa ushirikiano utakaofanya kazi barabara. Pia makubaliano ya ushirikiano kwa wanachama tisa wa Kamati ya Kudumu ya Ushauri wa Maghreb, iliyoundwa Novemba 1965, bado haijaridhiwa.

Katika Nchi za Kiafrika zinazozungumza Kiingereza, hata hivyo (isipokuwa kwa Afrika ya Mashariki ambayo ilipata uhuru wake ikiwa jumuiya ya kiuchumi) hakuna jumuiya za kiuchumi za kikanda zilizoanzishwa katika miaka ya mwanzo ya uhuru. Wakati ambapo Afrika Magharibi iliyozungumza Kifaransa iliendelea kujaribu kudumisha asasi zilizokuwepo kabla ya uhuru pamoja na kuanzisha asasi mpya, wenzao wa nchi zinazozungumza Kiingereza, hasa kwa kushinikizwa na Ghana, walifutilia mbali asasi chache zilizokuwa zimeanzishwa na Waingereza, yaani Bodi ya Fedha ya Afrika Magharibi ya Waingereza, Mahakama ya Rufaa ya Afrika Magharibi, Taasisi ya Utafiti wa Kakao ya Afrika ya Magharibi na Shirika la Ndege la Afrika Magharibi, na hivyo kuendeleza mgawanyiko katika eneo hilo la Afrika.

Jumuiya ya Afrika Mashariki, inayoweza kudaiwa kuwa moja ya mpango wa ushirikiano wa kikanda uliokuwa bora kuliko yote katika Dunia ya Tatu katika kipindi hicho, ilishuhudia mvutano wa hali ya juu katika miaka ya 1960 kiasi kwamba ilipofikia mwishoni mwa muongo huo kiwango cha ushirikiano wa kiuchumi kilikuwa kimeshuka sana. Umuhimu wa muungano huo wa Afrika Mashariki unaweza kueleweka kwa kukumbuka kwamba wakati wa uhuru biashara ya nje, sera za fedha na sarafu, miundo-mbinu ya usafiri na mawasiliano na elimu ya chuo kikuu vyote viliendeshwa kikanda badala ya kitaifa. Hatima yake, yote haya yalivunjiliwa mbali na matumaini makubwa ambayo Kenya, Tanzania na Uganda wangekuwa nayo ya kuanzisha shirikisho kamili chini ya serikali moja yaliyeyuka. Ilipofikia Juni 1977 muundo mzima wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao hapo awali ulionekana kama kielelezo cha ushirikiano wa Afrika kikanda, uliporomoka.

Matatizo na vikwazo vya ushirikiano wa Afrika kikanda katika miaka ya mwanzo ya uhuru vilikuwa ni vingi na labda visivyozuilika. Vilitokana na mambo ya ndani na vilevile kutokana na mambo ya nje na ya kihistoria. Moja ya mambo hayo ni ukuaji wa mwamko wa kitaifa. Ukoloni uliacha nyuma viraka vya nchi

nyingi huru ambazo zilikuwa vitengo vya bandia. Kwa vyovyote vile hazikuwa mataifa, ila ziliwakilisha magamba ya nchi huru ambamo viini vya mwamko wa kitaifa vilikuwa vimepandikizwa na vyama vilivyopigania uhuru. Kwa shauku la kupata muungano wa kitaifa, viongozi wapya walilazimika kuangalia ndani na kuorodhesha aula zao za awali ambazo zilikuwa ni maendeleo ya nchi zao wenyewe ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Wajibu wao mkubwa kwa hali hiyo ulikuwa ni kujenga taifa linalokubalika kwenye msingi wa mila na desturi zao. Kwa vile



PICHA 24.3 *Kutoka kushoto: J. Nyerere wa Tanzania, Rais, 'A.M. Obote wa Uganda na Rais J. Kenyatta wa Kenya, wakitia sahihi mkataba wa ushirikiano mjini Kampala Juni, 1967.*

ushirikiano wa kweli ulimaanisha kujitoa kwa muda mrefu, ni wazi kwamba nchi hizo zilisita kuchukua hatua za haraka ambazo zingeongeza matatizo kwenye uhuru wa nchi zao kwenye maeneo kadhaa miongoni mwao yakiwa uundaji wa mipango ya maendeleo. Ingawa jambo hili halikuondolea mbali uwezekano wa kuunda jitihada za muungano wa pamoja wa kikanda, lakini lilidokeza ni kwa kiasi gani nchi za Kiafrika hazingekubali kuachia au kuunganisha mamlaka yao ya kitaifa.

Katika Afrika yote, nchi za Kiafrika hazikuonyesha nia ya kuyatoa muhanga maslahi yao ya kitaifa kwenye madhabahu ya kikanda. Nchi hizi ziliingia kwenye

makubaliano ya kuhurisha biashara au kupanga viwanda kwa msingi wa kanda pale ambapo madhumuni haya ya kuungana hayakuwa yanapingana na mambo ya kitaifa yanayohusu usalama, hadhi, au manufaa ya kiuchumi. Mwelekeo huu ulikuzwa na tofauti za uhusiano kati ya vikundi mbalimbali vya kiuchumi vya Afrika kabla ya kuanza kwa mikataba ya Lome. Nchi 18 zilizozungumza Kifaransa zilishirikiana na Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC) chini ya mfumo wa Yaoundé; wasiokuwa washiriki wa Jumuiya ya Madola na washiriki wa Jumuiya ya Madola kama vile Nigeria walikuwa na makubaliano maalumu ya biashara na EEC yaliyotiwa sahihi Januari 1966 (na ambayo hayakutekelezwa kamwe); na nchi tatu za Afrika ya Mashariki yaani Kenya, Tanzania na Uganda ziliungana chini ya Makubaliano ya Arusha Septemba 1969.

Mambo mbalimbali yanaweza kusemwa kuwa yalitatiza utendaji kazi wa mifumo iliyowekwa kwa ajili ya ushirikiano wa kiuchumi. Moja ya mambo hayo ni tofauti za kiuchumi na kisiasa za bara la Afrika. Nchi ambazo zilifuata njia tofauti kabisa katika maendeleo yao zisingeweza kuwa wabia wazuri katika mifumo ya ushirikiano wa kiuchumi. Ni kweli kwamba mifarakano ya kisiasa na ya kiitikadi ilitishia hata ile mipango ya ushirikiano iliyokuwa inafanya kazi vizuri kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki. Juu ya haya matatizo tunaweza kuongezea kile Timothy Shaw alichokiita "matatizo ya kuzigeuza oganizesheni kuwa za kisiasa".

Kutokana na matatizo hayo, mara nyingi uanzishaji wa vikundi vya ushirikiano katika Afrika kwenye muongo wa kwanza wa uhuru haukuwa lolote zaidi ya kutamka nia na kuashiria mafungamano ya mataifa katika kontinenti. Kejeli ni kwamba, licha ya rekodi hii mbaya ya kukatisha tamaa, msisimko wenye kupendekeza muungano kama jibu la matatizo ya Afrika umeongezekea sana siku za karibuni. Hii imetokana na zahama ya maendeleo katika Afrika, na hasa kushadidi kwa hali ya kutisha ya Afrika kulikozidishwa na utegemezi kwenye uchumi wa kimataifa uliotawaliwa na Magharibi. Muhtasari mfupi wa kile sasa kinachoitwa "zahama ya bara la Afrika" utasaidia katika kuelewa kiwango cha shauku ya sasa iliyohuishwa ya dhana ya Upanafrika kama msako wa muungano.

## Upanafrika, ushirikiano wa kikanda na maendeleo ya uchumi

Kuanzia miaka ya 1970 kumekuwepo na shauku ya kuhuisha dhana ya Upanafrika kama nguvu ya kulete muungano kwenye kiwango cha kanda. Je, ni nini hulka ya mvuto huu mpya na unaweza kuelezwaje? Sababu kubwa imetokana na kukwama kwa utendaji wa uchumi wa Afrika katika miaka 25 iliyopita. Kwani licha ya

jitihada za kuchochea ukuaji wa viwanda, kuendeleza uzalishaji katika kilimo na kuanzisha programu nyinginezo za kimaendeleo, mageuzi ya bara la Afrika ambayo yalitarajiwa kufuatia kwa karibu kwenye nyayo za uhuru wa kisiasa bado yanaendelea kubaki kama matumaini tu. Hakuna uboreshaji wowote unaoonekana katika chumi nyingi za Afrika tangu 1960.

Mwanzoni mwa miaka ya 1960, viongozi wa Afrika walitarajia kwamba kuchanganya biashara na misaada kutoka kwa mataifa yenye viwanda kungewapatia rasilimali muhimu za kutosheleza matarajio yao ya kitaifa yakawa na maendeleo huru, yenye kujihimili, lakini jambo hili halikutokea. Kwa hiyo rekodi ya miaka ya 1960 ilikuwa ni ya kusikitisha. Si sera ya misada wala ya biashara iliyoendelezwa na mataifa ya viwanda iliyoonekana kuwa na uwezo wa kuchapusha upanuzi wa uchumi. Kwa hali hiyo Afrika ilijitokeza kwenye Muongo wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (1960-1970) kama ukanda ulioorodheshwa ukiwa na kiwango cha chini zaidi cha ukuaji miongoni mwa nchi zilizokuwa zinaendelea - asilimia 2 dhidi ya asilimia 4.1 ya Asia ya Kusini, asilimia 5.6 ya Asia ya Mashariki, asilimia 4.5 ya Amerika ya Latino, asilimia 7.2 ya Mashariki ya Kati. Ishara za awali kutokana na Muongo wa Pili wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (1970-1980) ni kwamba kumetokea mabadiliko kidogo, kama yalikuwepo. Kwa hivyo, pamoja na rasilmali zake nyingi, Afrika inashindwa kuonyesha kiwango cha ukuaji au kielelezo cha kutosha cha ustawi kwa miaka 25 iliyopita.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba kati ya 1970 na 1979 madeni ya nje ya Afrika Kusini mwa Sahara yalipanda kutoka dola bilioni 6 na kufikia dola bilioni 32 na gharama za kuhudumia deni (kwa nchi zilizokuwa zikiagiza mafuta) ziliongezeka kutoka asilimia 6 hadi kufikia asilimia 12 ya mapato ya mahuruji. Kama urithi wa Afrika kutoka kwa wakoloni katika miaka ya 1960 ulikuwa wenye "nuksi", tukikopa maelezo ya Shaw, basi 1980 imeonyesha matumaini kidogo zaidi.

Nchi nyingi za Afrika zimekuwa tegemezi zaidi kwenye riba, uwekezaji, teknolojia na utaalamu wa nje, na kwenye nadharia zao za maendeleo na ukuaji wa uchumi, na zaidi ya yote kwenye uuzaji nje wa mali ghafi na bidhaa za msingi za kilimo kwa nchi tajiri na za viwanda za Magharibi.

Hali hii ya kusikitisha imezidishwa na taathira za hali ya migogoro ya ulimwengu ambayo imejitokeza kwa kuvunjika kwa Makubaliano ya Breton Woods, dharuba zinazohusiana na mafuta zilizosababishwa na Oganizesheni ya Nchi zinazouza Nje Mafuta ya Petroli (OPEC), upungufu wa nishati, na kudumaa kwa maendeleo kuanzia katikati ya 1970 na kuendelea. Ili kukabiliana na ukweli huu usiosuluhika,

viongozi wa Afrika wamelazimika kutathmini upya kwa utulivu chaguzi ambazo wangeweza kuzifuata: je, ni ipi njia sahihi ya kuelekea kwenye maendeleo ya uchumi?

Kutokana na kukaribia kwa maangamizi, na mporomoko, majibu ya kibunifu yanahitajika. Kwani kama kuporomoka kwa utendaji wa kiuchumi kunapaswa kusitishwe na kufanyiwa mageuzi, basi mikondo mipya ya kisera inahitajika. Kwa hali hiyo, matumaini ya Afrika kimsingi, yapo kwenye uelekezaji mpya wa mikakati yake ya maendeleo ya kikanda na kitaifa. Mafanikio ya OPEC yamedhihirisha na kuimarisha dhana ya nguvu ya umoja na mshikamano. Hatua ya aina hiyo inaonekana kuwa ni muhimu kuchukuliwa na Afrika ili kuondoa matatizo ya uchumi wa Afrika. Nchi za Kiafrika zinahisi kwa dhati kabisa kwamba zinatakiwa kulea ushirikiano wa pamoja ili kuzipa nguvu juhudi zao za kitaifa za kuimarisha uhuru wao.

Ni katika kujibu changamoto hii muhimu kwa utendaji wa kukatisha tamaa wa chumi nyingi za Afrika, ukijumuishwa na kushindwa kwa mifululizo ya Majadiliano ya Kaskazini-Kusini katika kufikia malengo ya utaratibu mpya wa uchumi wa kimataifa (NIEO), ndipo Mpango wa Utendaji wa Lagos (LPA) uliamuliwa na kuanzishwa. Mkakati uliyoainishwa kwenye hati hiyo umejikita kwenye dhana ya maendeleo na ukuaji uchumi ya kujitegemea na kujidumisha. Dhamira yake kuu katika Afrika ni kupunguza utegemezi kweye mikakati inayotoka nje.

Kama mbinu-kinzani kwenye hali hii ya utegemezi uliokithiri, nchi za Kiafrika ziliamua kukubali mwelekeo mpana wa kikanda uliojengwa kwenye msingi wa kujitegemea kwa pamoja. Ushirikiano wa kikanda umejadiliwa karibu kwenye kila sura ya Mpango wa Lagos, na ndiyo sharti muhimu la utekelezaji. Bila mjumuiko wa kikanda, LPA ikiwa kama dhana na mkakati, itaanguka.

Ni katika usuli huu ambapo dhana ya Upanafrika kama njia ya kuungana sasa inaonekana kuwa jambo muhimu katika kupunguza utegemezi na kusaidia kuboresha nafasi ya nchi za Afrika katika kujadili masharti na nchi tajiri, na hivyo kuimarisha uwezo wao wa kuendelea kupitia mkakati mpana zaidi wa kukuza NIEO. Zaidi ya manufaa halisi yaliyoahidiwa na vikundi vya kikanda katika umbo la biashara na uwekezaji uliopanuliwa, muungano wa kiuchumi unatetewa kwa nguvu kama kwa njia ya kupunguza uwezekano wa kudhuriwa kutoka nje. Jambo hili linatakiwa kushughulikiwa haraka zaidi kwa vile uhusiano huu wa utegemezi hauonyeshi dalili za kupungua; hasa ikizingatiwa kwamba deni kubwa la nje kwa nchi nyingi za Kiafrika linazidi kuongezeka. Jambo la msingi linaloonekana hapa

ni nia ya viongozi wa Afrika kuukilia kwa kiasi kinachowezekana sera zao wenyewe za uchumi zikihimiliwa kwenye matarajio yao ya kitaifa, rasilimali zao asilja na itikadi za kisiasa, nje ya athari za nchi zilizoendelea.

## Taratibu mpya za kikanda na suala la utegemezi

Miaka michache iliyopia imeshuhudia kufumka upya kwa taratibu za haraka za kikanda za kutaka kushirikiana katika Afrika kama changamoto dhahiri dhidi ya bara hili kutawaliwa kutoka nje kulikorithiwa kutoka kipindi cha ukoloni. Miongoni mwa miundo hiyo yenye kuonyesha ari na nguvu kubwa ni Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Magharibi (ECOWAS) ambayo inajumuisha pamoja nchi zilizoenea kwenye ukanda wa kilomita za mraba milioni 6 kuanzia Mauritania kaskazini-magharibi hadi Nigeria huko kusini-mashariki, ukiwa na idadi ya watu wasiopungua milioni 150. Ikiwa imeanzishwa huko Nigeria, Mei 1975, ECOWAS ni jitihada ya kwanza ya dhati ya kutaka kupata ushirikiano wa kiuchumi na muungano katika ukanda mdogo wa Afrika ya Magharibi, ikiwa imevuka mipaka ya lugha, historia na ushirikiano uliokuwepo pamoja na asasi zake. Kati ya nchi wanachama, tano zinatoka kwenye nchi zinazozungumza Kiingereza kama lugha rasmi, nane kwenye nchi zinazozungumza Kifaransa, mbili zinazozungumza Kireno na moja inayozungumza Kiarabu.

Zaidi ya ECOWAS, jitihada nyingine mbili zimejitokeza huko Afrika ya Kusini. Ya kwanza ni Mkutano wa Kuratibu Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCC sasa SADC), ambayo ilizinduliwa rasmi Aprili 1980 kwa kutiwa sahihi na Nchi Zilizokuwa Mstari wa Mbele (FLS) - Angola, Msumbiji, Tanzania na Zambia — Tamko la Lusaka juu ya Ukombozi wa Kiuchumi; na baadaye kuungwa mkono na Lesotho, Malawi, Swaziland na Zimbabwe. SADCC ilipobuniwa hapo awali ilikuwa kama mwenzi wa FLS katika masuala ya kiuchumi, ambayo kuanzia 1974, imekuwa ikijihusisha kwa karibu sana katika kusaidia na kuongoza kwa kiasi fulani mambo ya kijeshi, kisiasa na kidiplomasia katika mapambano ya ukombozi huko Rhodesia, Namibia, na Afrika Kusini. Hizo nchi tisa za SADCC zimeenea kwenye ardhi ya ukubwa wa kilomita za mraba milioni 5 na zina idadi ya watu wasiopungua milioni 60. Jitihada ya pili ni Eneo la Upendeleo wa Biashara kwa nchi za Afrika ya Mashariki na Kusini (PTA), ambayo mkataba wake ulipitishwa huko Lusaka Desemba 1981 na nchi nane miongoni mwa nchi 18 zenye uwezo wa kuwa wanachama. Mwishowe PTA ilizinduliwa rasmi huko Harare Julai 1984.

Licha ya jina lake, PTA haikuishia kwenye mambo ya biashara peke yake. Inajihusisha karibu kwenye sekta zote zinazohusu uendelezaji wa mahusiano ya kiuchumi katika ukanda huu. Kama ilivyo kwa ECOWAS, PTA ni mtoto wa akili ya Adebayo Adedeji, katibu mtendaji wa ECA. Lakini wakati PTA ilikuwa ni mfano wa maendeleo ya jitihada kutoka chini, SADCC kama ilivyokuwa ECOWAS, zaidi ilikuwa ni hatua iliyonuiwa ya kisiasa, ikiwa imebeba mamlaka binafsi ya maraisi na mawaziri wakuu wa nchi husika. Kama ambavyo wajumbe sita wa CEAO wanaozungumza Kifaransa wamesaini mkataba wa ECOWAS, vivyo hivyo nchi zote wajumbe wa SADCC ni wajumbe wa kutarajiwa kwenye PTA. Na kama ilivyo kwa ECOWAS na CEAO, ijapokuwa madhumuni ya programu za SADCC na PTA kwa kiasi fulani yanafanana na yanazidi kukutana, zipo tofauti zinazoonekana kwenye asili ya mashirika haya mawili, miundo yao ya kiasasi, wafadhili wao wa kifedha, itikadi na mikakati yao.

Dalili nyingine za kujihusisha kwa wakati huu katika ushirikiano wa kikanda katika Afrika ni kuundwa kwa Shirikisho la Senegambia Desemba 1981, ambalo linaunganisha Gambia na Senegal kwenye umoja wa kiuchumi na wa kifedha. Hili ni hitimisho la juhudi za miaka mingi za kuunda ushirikiano wa karibu wa kiuchumi baina ya nchi hizi. Jitihada ya hivi karibuni ni mkataba uliotiwa sahihi huko Libreville, Gabon, Oktoba 1983, wa kuanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS), ikijumuisha wanachama wa sasa wa UDEAC na wale wa Jumuiya ya Uchumi ya Maziwa Makubwa. ECCAS ilitarajiwa kuwa jumuiya ya Afrika ya Kati kinachoweza kulinganishwa na ECOWAS.

Lengo la msingi wa utaratibu huu mpya wa ushirikiano wa kikanda linafanana kote — kupunguza utegemezi wa wanachama wao dhidi ya nguvu kutoka nje ambazo zinaathiri sera na mielekeo ya kiuchumi ya nchi za Afrika; na kuratibu programu za maendeleo katika sekta kubwa na sekta ndogo mbalimbali kama njia ya kuchapusha kiwango cha ukuaji wa uchumi na maendeleo. Kwa mfano, madhumuni ya msingi ya ECOWAS ni kukuza ushirikiano na maendeleo katika nyanja zote za shughuli za kiuchumi kwa lengo la kupunguza polepole hali ya utegemezi wa kiuchumi wa Jumuiya kwa dunia ya nje. Vivyo hivyo SADDC iliundwa kama matokeo ya matamanio ya pamoja ya wajumbe wake tisa ya kupunguza na hatimaye kukomesha kabisa utegemezi wa kiuchumi kwa Afrika Kusini. Kwa upande mwingine, PTA ikiwa na wanachama wengi zaidi haifanyi jitihada zozote za moja kwa moja za kukabiliana na suala la kupunguza utegemezi kwa Afrika Kusini. Badala yake inatetea mwelekeo chanya kwa tatizo hilo, kwa

kudai kwamba kwa kiasi ambacho PTA itafaulu kukuza biashara na maendeleo ya kikanda, basi tatizo la hatari lililopo la utegemezi litapungua. Hali hii ikitazamwa katika muktadha wa NIEO, jitihada zote hizi mpya za kikanda zinatakakiwa zichukuliwe pia kama sehemu ya mjumuiko wa matamanio mapana zaidi ya nchi maskini za Kiafrika ya kuondosha au hata kupunguza ukosefu wa usawa uliopo sasa kwenye mfumo wa uchumi wa kimataifa.

Ni kwa kiasi gani taratibu hizi za kikanda zinaweza kuweka hali ambazo zitaleteleza maendeleo huru na ya kujihimili? Katika mazingira ya Afrika, maendeleo ya aina hiyo yanaweza kupatikana tu kwa kubadilisha miundo ya uzalishaji. Ni lazima isisitizwe kwamba muungano wa kikanda hauwezi kufanikiwa wakati wabia wa kanda hizo wanaendelea kushirikishwa kwenye mifumo ya kimataifa. Kwa maneno mengine kujitegemea kikanda hakupatani kabisa na muungano wa kiulimwengu na wa kuvuka mataifa.

Wananadharia wengi wa maendeleo sasa wanakiri kwamba hatua za mabadiliko ya kikanda sio huru na wala hazitokei zenyewe, bali kutokana na muktadha na kutegemeana na kuingiliana kiulimwengu.

Kwa usuli huu, ni rahisi kuona aina ya matatizo yanayoweza kukabili taratibu mpya za kikanda za kuungana kuhusiana na upenyezi wa nje. Kwa mfano kuna tatizo la kuzinasua nchi wanachama wa ECOWAS, SADCC, na PTA au CEEAC kutoka kwenye mahusiano tegemezi na nchi za nje zenye nguvu kwa kutumia asasi za kitaifa au za kikanda ili kuleta udhibiti mkubwa zaidi juu ya rasilimali zake. Kwa kuona utata wa tatizo hili swali linalojitokeza ni: je, masharti yanayotolewa kwenye mikataba hii mipya ya jitihada za kikanda yanatosheleza katika kukabiliana na suala hili?

Ushahidi unaelekea kuonyesha kwamba hakuna utaratibu wa kikanda hata mmoja ambao una masharti ya kupambana na mambo yote yanayohusiana na upunguzaji wa utegemezi. Kwa mfano, ingawa protokali ya ECOWAS juu ya kanuni zinazohusu asili ilitarajia matatizo yaliyosababishwa na uhusiano wa nje, bado haionyeshi waziwazi jinsi ya kupambana na umiliki wa nje na ushiriki. Kwa muda mrefu ujao, shughuli nyingi za viwanda za Afrika Magharibi zitaendelea kuwa na umiliki wa asilimia kubwa zaidi ya wageni. jambo muhimu hapa ni kwamba ijapokuwa ibara 32 ya mkataba wa ECOWAS inataka kwa nia kabisa Bazara la Mawaziri la ECOWAS kuchukua hatua madhubuti kuelekea kwenye upunguzaji wa utegemezi, hakuna asasi wala chombo chochote cha ECOWAS ambacho kimekabidhiwa jukumu la kuingia kwenye mapatano na watendaji wa nje kwa

niaba ya Jumuiya hiyo. Wala mkataba wa ECOWAS hauna masharti yoyote ya kuwa na utaratibu wa pamoja kuhusu uwekezaji wa nje au uondoaji wa uwekezaji, na wala hakuna asasi yoyote iliyoanzishwa ya kudhibiti uingizaji wa teknolojia kama ilivyo kwa Soko la Pamoja la Andean huko Amerika ya Latino. Kwa hali hiyo uainishaji upya wa mahusiano ya kiuchumi ya ECOWAS na dunia ya nje, jambo ambalo ni la umuhimu mkubwa ikiwa lengo lao ni kupunguza utegemezi, haujashughulikiwa kabisa katika mkataba wa ECOWAS.

Ijapokuwa nchi za SADDC zimebainisha usafiri na mawasiliano kama aula ya kwanza katika upunguzaji wa utegemezi kwa Afrika Kusini na hivyo kuanzisha Tume ya Afrika ya Kusini ya Usafiri na Mawasiliano (SATCC) kwa madhumuni hayo, katika utekelezaji wa utaratibu huu, fumbo kubwa zaidi ni kwamba utaratibu huo bado unategemea upatikanaji wa vyanzo vya nje vya misada na uwekezaji. Matokeo yake ni kwamba SADCC katika siku za nyuma ilianzisha miradi iliyowavutia zaidi wafadhili wa nje badala ya ile miradi iliyofikiriwa kuwa ya manufaa makubwa kwa ukanda huo. Kwa hali hiyo, pamoja na shauku kubwa ya wajumbe wa SADCC kuepuka kikaango cha Afrika Kusini, wanaonekana kutumbukia kwenye moto wa wafadhili wa Magharibi, jambo ambalo linaunda utegemezi wa aina nyingine. Aidha, uamuzi wa SADCC wa kumakinikia suala la ukarabati wa mifumo ya usafiri iliyorithiwa kutoka ukolomi kunaweza kudumisha ruwaza ya biashara na uzalishaji wa "ukoloni mamboleo" na hivyo kuzuia biashara miongoni mwa Wana-SADCC.

## Dhana ya kanda dhidi ya Upanafrika wa kuvuka kanda

Matatizo changamani ya utegemezi yanayozikabili jitihada mpya za kikanda yamezidishiwa uchachu huo kutokana na kuzuka kwa aina mpya ya Upanafrika kwenye kiwango kinachovuka kanda au bara lote, katika umbo la Mkataba wa Lomé kati ya Jumuiya ya Uchumi wa Ulaya (EEC) na Afrika. Kwani ukitazamwa hasa kwa mkabala wa mabadiliko ya muundo, "mfumo" mpya wa Lomé haukuwa na bado si mabadiliko makubwa kwa Ulaya wala kwa Afrika. Mkataba huu ni aina nyingine ya ukoloni mamboleo wa EEC wa kuimarisha na kudumisha hali iliyokuwepo katika utaratibu wa zamani. Wakati ambapo Mkutano Mkuu wa Berlin ulianzisha mageuzi ya kikoloni yasiyo na mpinzani katika Afrika, Mkataba wa Roma, ambao ulileteleza kuzaliwa kwa EEC uliashiria ujio wa ukoloni mamboleo na utegemezi katika Afrika. Kwa hiyo, mkereketwa Kwame Nkrumah alikuwa mwepesi kuikana EEC kama mfumo mpya wa "ukoloni wa pamoja ambao

ungekuwa na nguvu zaidi na wa hatari zaidi kuliko maovu ya zamani tunayojaribu kuyafutilia mbali." Kwani Makubaliano ya Lomé sio hati ya maendeleo iliyoelekezwa kwenye ushirikiano wa kutegemeana wenye uwiano na wa manufaa kati ya Ulaya na Afrika, ila ni ubadilishaji wa hali ya ubeberu. Hivyo, pamoja na misaada mingi ya EEC kupitia Lomé I na Lomé II, haiwezi kupingwa kwamba uhusiano mpya baina ya Ulaya na Afrika umeimarisha sana utegemezi wa pamoja wa Afrika kwa Ulaya kupitia mahusiano ya biashara, ushirikiano katika viwanda, maendeleo ya kiuchumi kupitia msaada wa fedha za EEC na mashauriano kupitia mlolongo wa asasi mbalimbali.

Kwa hivyo, kwa hali nyingi dhana hii mpya ya Upanafrika kwenye kiwango cha kuvuka ukanda inayowakilishwa na Mkataba wa Lomé, sio tu kwamba haitangamani na malengo ya msingi ya *Mpango wa Lagos,* ila kwa uhakika pia iko nje ya matarajio, mbinu za maendeleo pamoja na madhumuni ya msingi ya dhana ya Upanafrika kwenye kiwango cha ukanda (bara zima). Kama ilivyogusiwa hapo juu, vikundi vipya vya kikanda vya Afrika, hasa ECOWAS, SADCC na PTA vimechukua msimamo wa maendeleo ya kujitegemea yaliyolengwa kwenye upunguzaji wa utegemezi kwenye nguvu za wakoloni wa awali na mfumo wa uchumi wa kimataifa (na kwa SADCC na PTA, Afrika Kusini pia). Kwa upande mwingine Lomé inawakilisha mwelekeo wima wa Ulaya-Afrika, wakati taratibu mpya za kikanda zikiakisi shauku ya kuwa na uhusiano wa mlalo wa Kusini-Kusini. Kimuundo kiwango hiki kipya cha dhana ya Upanafrika hakielekezi njia mpya kwa Afrika, na wala hakitoi mtazamo mpya. Badala yake kinapokea na kukubali mwelekeo uliopo katika maendeleo ya Afrika na kinaelekeza zaidi kwenye upenyezaji wa ubepari katika chumi za Afrika. Kwa kifupi, ijapokuwa ni muhimu kujitegemea zaidi kiuchumi ili kuweza kuwa na taratibu za muungano wa kiuchumi katika Afrika, kwa kujitegemea kunawaepusha au angalao kupunguza utegemezi kwa nchi za viwanda na hivyo kuwezesha kupata maendeleo yao, haielekei kama utekelezaji wa mbinu hizi utaweza kufaulu chini ya mfumo wa Lomé.

## Dhana ya Upanafrika na ushirikiano wa kikanda: mapitio na hitimisho

Kwa mema au mabaya Afrika inakomaa. Kipindi cha ustawi wa Upanafrika kama vuguvugu la kufuta ukoloni kimepita. Badala yake kumezuka kipindi kipya cha dhana ya Upanafrika kama chombo cha kuunganisha kanda na kufuta ukoloni wa

kiuchumi. Aina za vyombo vya kikanda vilivyozuka kuanzia miaka ya katikati ya 1970 na kuendelea zote zinahusiana na suala pana la kujitegemea kwa pamoja na tukio la kihistoria la kushirikishwa kwa Afrika kwenye mfumo wa ulimwengu. Leo hii, ushirikiano mwingi katika masuala ya uchumi sio kwa faida ya Afrika bali ni kwa faida ya mawakala wa misaada ya kigeni, washauri na mashirika ya kimataifa. Kwa hali hiyo kuna tatizo kubwa katika Afrika kwa sababu ushirikiano wa kiuchumi, ambao ndio uti wa mgongo wa kujitegemea kwa pamoja, hauwezi kutekelezwa kikamilifu kama chombo cha maendeleo ya kikanda wakati nchi zinazoshiriki hazina udhibiti thabiti juu ya rasilimali zinazoingizwa ndani ya miradi ya pamoja, au hata mamlaka kwenye sekta muhimu za uchumi wao.

Aidha, kutokana na kujiimarisha kwa ukoloni mamboleo katika Afrika, na kiwango cha uanuawi katika masoko na vyanzo vya uwekezaji na teknolojia miongoni mwa watawala tofauti wa kikoloni wa awali, kujinasua ghafla kutoka kwenye uhusiano huu wa karibu na nchi za viwanda huenda kungeleta machungu mengi kwa chumi za Afrika zinazolegalega. Kwa hali hiyo, nchi za Kiafrika zinaweza kuamua kuwa sehemu ya mfumo huo na wakati huo huo zikitafuta njia ambazo zingeziwezesha kupata udhibiti zaidi juu ya dunia yenye viwanda. Hivyo ingelazimu taratibu za muungano wa kikanda katika Afrika kuchukua mwelekeo tendeti na mnyumbufu kwenye suala la utegemezi na mtego wa ukoloni mamboleo.

Katika hali hii, vikundi vya kikanda vya Afrika huenda vikahitajika kusambaza mahusiano yao ya nje ya kiuchumi, wabia wa biashara, na vyanzo vyao vya teknolojia na mtaji. Njia hii ina uwezo wa kuimarisha nafasi za serikali za nchi za Afrika za kushiriki katika majadiliano ya bei na hivyo kuziruhusu kuchezesha nchi zilizoendelea moja dhidi ya nyingine. Umuhimu wa kusambaza mahusiano ya biashara za nje hauwezi kusisitizwa zaidi.

Uchaguzi mwingine uliopo kwa vikundi vya kikanda vya Afrika wa kuvuka mipaka ya utegemezi ni kuanzisha uhusiano wa kiuchumi wa upendeleo na miundo ya muungano wa kikanda za huko Asia na Amerika ya Latino. Kwa maneno madhubuti zaidi, aina hii ya "muungano mlalo" inamaanisha ukuzaji wa ushirikiano wa kiuchumi na nchi zinazoendelea, ambalo ni sharti jipya la maendeleo la miaka ya 1980. Hatua ya pamoja ya aina hiyo inaweza kuwa ya maana sana katika kuziwezesha nchi zinazoendelea kutetea bei za mahuruji ya mali ghafi na kuimarisha utawala wao kwenye rasilimali zao asilia. Hali hii pia inaweza kukuza uwezo wa wazawa katika sayansi na teknolojia, kupata masoko ya bidhaa zao, kusaidia kuongeza uwezo wa viwanda vyao, na zaidi ya yote kuimarisha nguvu zao za kufanya maamuzi kwenye asasi zinazomilikiwa na mataifa mengi.

Kisha, nchi za Kiafrika na viongozi wake zinatakiwa kukubali kuanzisha mabadiliko ya msingi ya kisera na kiasasi. Jambo hili linahitaji uainishaji upya wa malengo ya maendeleo kwenye viwango vya kitaifa na kikanda ili kutambua wazi muungano wa kikanda kama njia ya ufanisi katika kukabili masuala ya utegemezi na maendeleo. Lakini mkakati wa maendeleo ya kikanda hauwezi kupatikana kikamilifu kama nchi zinazohusika hazipo tayari kutayarisha sera ya pamoja ya kukabili tatizo la uwekezaji wa kigeni na utegemezi wa teknolojia kupitia taratibu na mipango ya kikanda. Hili linapaswa liungwe mkono na maelekezo muhimu ya kisera yenye lengo la kuanzisha taasisi ya pamoja ya utafiti na maendeleo ya viwanda, ambapo pia itaainisha teknolojia ya kigeni inayofaa, ununuzi wake, upatikanaji au urekebishaji wake kwa ajili ya matumizi kwenye miradi ya pamoja ya maendeleo.

Mwisho, katika mkakati wowote utakaotumika kuvunja mipaka ya utegemezi, mabadiliko ya sera ya ndani ni lazima yapatiwe aula. Hili linahitaji nidhamu binafsi na kujitoa sadaka. Sisi huku Afrika ni lazima tukubali kupokea nidhamu, kujihini na kujinyima. Mambo yanatakiwa katika kuanzisha kile kinachoitwa utaratibu mpya wa ndani, iwapo tunatarajia kubadilisha mahusiano yetu na nchi za viwanda kutoka hali ya utegemezi wa kudumu na kuingia kwenye hali ya kutegemeana kwa faida ya wote, hali ambayo inaweza kutoa msukumo unaotakiwa, ndani ya jamii ya Kiafrika, wa ukuaji endelevu wa uchumi. Kama ambavyo mwanahistoria maarufu, Ade Ajayi, alitamka hivi karibuni, "matumaini yenye tahadhari":

Mtazamo wa jamii mpya katika Afrika unatakiwa ujengwe *ndani* ya Afrika, uzaliwe kutokana na uzoefu wa kihistoria wa Afrika na hisia ya kuendelea kwa historia ya Afrika. Mwafrika bado hajawa bwana wa majaliwa yake mwenyewe, na wala si mtumwa wa majaliwa moja kwa moja.

# 25 Upanafrika na ukombozi

Ikiwa Upanafrika kama vuguvugu la uunganishi, ilishuhudia kiwango fulani cha kufanikiwa mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960, na baadaye, kuanzia kati ya miaka ya 1970, kupata msukumo mkubwa, dhana hii, kama vuguvugu la ukombozi, ilifika kilele cha mafanikio katika miaka kumi ya mwanzo ya uhuru wa Afrika. Kufuatia uhuru, ile ari iliyouumanisha Upanafrika, yaani mapigano dhidi ya madola ya kikoloni, haikuwa tena na nguvu katika baadhi ya nchi huru za Afrika, licha ya kuendelea kwa mgogoro wa muda mrefu wa Afrika Kusini ambao uliifanya shughuli ya Afrika huru iwe bado haikumalizika.

Ingawa falsafa ya Upanafrika ilianzia huko Marekani katika karne ya kumi na nane na karne ya kumi na tisa ikiwa ni sehemu muhimu ya vita vya watu weusi dhidi ya utawala na unyonyaji wa weupe, kama kitendo cha ukombozi ndani ya Afrika yenyewe, falsafa hii, kama ilivyoelezewa katika sura ya 23, imeanza wakati wa uvamizi uliyofanywa na Mafashisti wa Kitaliano katika Uhabeshi mwaka 1935, na zaidi katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Uafrika uliofanyika huko Manchester mwaka 1945. Wajumbe wa Kiafrika ndio waliokuwa wengi katika mkutano huu na kiini cha mjadala kilihusu ukombozi wa sehemu ya Afrika iliyokuwa chini ya ukoloni. Mkutano huo ulitayarishwa na kamati maalum ya uendeshaji (sekretarieti) ndani yake wakiwemo Peter Milliard wa British Guyana, R.T. Makonnen wa West Indies, Kwame Nkrumah wa Ghana, George Padmore wa Trinidad, Peter Abraham wa Afrika Kusini na Jomo Kenyatta wa Kenya. Kulikuwa washiriki waliozidi 200. Mpanafrika mkongwe, Dubois, alikuwa ndiye mwenyekiti wa kudumu wa vikao vyote. Mijadala iliyofanyika na maazimio yaliyopitishwa yalikuwa ya aina ya mapambano zaidi kuliko ile ya mikutano mikuu iliyopita. Miongoni mwa madai yaliyokuwemo katika Azimio kwa Madola ya Kikoloni ni:-

(1) uhuru kamili kwa Waafrika na makabila mengine yaliyotawaliwa kutokana na utawala wa madola ya Ulaya
(2) kufutwa mara moja kwa sheria zote za kijamia na za ubaguzi
(2) uhuru wa kusema, wa magazeti, wa kuunda vyama na wa kufanya mikutano
(3) haki ya kila mwanamume na mwanamke aliyezidi umri wa miaka 21 kupiga kura na kuweza kuchaguliwa; na
(4) huduma za matibabu, ustawi wa jamii na elimu zitolewe kwa wananchi wote.




Picha 25.1 *Mkutano wa Panafrika huko Manchester, Uingereza, Novemba 1945. Kutoka kushoto, kwenda kulia mwa jukwa: Peter Milliard, Bibi Amy Facques Garvey, Meya wa Manchester na I.T.A. Wallace Johnson.*

Pia, kwa mara ya mwanzo, Waafrika walionya kwa uwazi kwamba ikiwa Wazungu bado walikusudia kuendelea kuitawala Afrika kwa kutumia nguvu, basi Waafrika nao watatumia nguvu kujipatia uhuru.

Wajumbe walipitisha azimio jingine kwa Waafrika wote, ambalo lilisisitiza kwamba mapambano ya kuwania uhuru wa siasa ni hatua ya mwanzo tu. Waliutaka umma ulio mjini na mashambani na pamoja na wasomi na wataalamu wa fani mbalimbali walio Afrika waungane, wajiandae na wawe wastahimilivu ili waweze kujipatia uhuru kamili.

Falsafa ya Upanafrika ilikuwa imekua kutoka kuwa itikadi ya mageuzi na ya utetezi ya watu wenye asili ya Kiafrika walioko katika Dunia mpya na kuwa itikadi ya utaifa kwa ajili ya kulikomboa bara zima la Afrika. Falsafa ya Dubois ya Upanafrika wa dunia nzima, falsafa ya kimapambano ya Garvey ya uhuru wa kujiamulia na kujitegemea, na falsafa ya Césaire ya kuhuisha upya utamaduni wa Kiafrika, haya yote kwa sasa yakawa sehemu muhimu za utaifa wa Kiafrika.

## Upanafrika na Ukombozi wa Afrika, 1945-60

Katika historia ya Upanafrika kama vuguvugu la ukombozi, kipindi kinachoanzia 1950 mpaka 1965 kinaweza kuitwa kipindi cha Kwame Nkrumah ambaye alikusanya viongozi wa Kiafrika waliokuwa katika pilikapilika za ukombozi na wale walioongeza nchi huru kwa ajili ya kuwania Upanafrika. Nkrumah alitayarisha Mkutano Mkuu wa mwanzo wa Nchi Huru za Afrika, uliofanyika katika mji mkuu wa nchi huru mpya ya Ghana na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka Misri, Uhabeshi, Ghana, Liberia, Libya, Moroko, Sudan, Tunisia pamoja na wengi miongoni mwa waliokuwa wajumbe wa Mkutano wa Tano wa Upanafrika. Mkutano huu uliainisha dhamira kuu za Upanafrika baada ya kupatikana uhuru, nazo ni: uhuru wa kisiasa kama lengo kuu; msaada kwa ajili ya harakati za ukombozi, msimamo mmoja katika Umoja wa Mataifa na pia kutofungamana na upande wowote.

Mkutano Mkuu wa Pili wa Nchi Huru za Afrika ulifanyika Monrovia mwaka 1959. Mkutano huu ulipitisha maazimio manne: azimio la kwanza lilishutumu Ufaransa kwa majaribio yake ya bomu la nuklia huko Sahara, azimio la pili lilihimiza kuweko kwa amani ya kisiasa huko Kameruni, la tatu liliwania kupatikana kwa amani Algeria kwa njia ya mapatano, na azimio la nne lilitangaza haki ya nchi zilizokuwa chini ya ukoloni kujiamulia wenyewe mustakbali wao. Mkutano Mkuu wa Tatu ulifanyika Addis Ababa mwaka 1960.

Katika kipindi hiki, Nkrumah na Wapanafrika wenzake wakifanya mikutano ya viongozi wa nchi huru na viongozi wa vyama vya ukombozi kwa ajili ya kubadilishana mawazo na mikakati kuhusu kupigania uhuru. Mkutano wa Kwanza

wa Waafrika wote ulifanyika Akkra mwezi wa Desemba, 1958. Ajenda ya mkutano ilikuwa na vipengele kuhusu kupinga ukoloni, kupinga ubeberu, kupinga ubaguzi wa rangi, umoja wa Afrika na kutotengamana na upande wowote. Mkutano wa Pili wa Waafrika Wote ulifanyika Tunis mwaka 1960. Mkutano huu ulihudhuriwa na wawakilishi wa nchi 73 ambao walipasisha maazimio kadha mengi yakihusika na kuuondoa ukoloni. Mkutano wa Tatu ulifanyika Kairo mwaka 1961. Kulikuwa na jumuiya mbili za Kipanafrika za kikanda zilizoanzishwa hapa kwa ajili ya kuendeleza mapambano yaliyoratibiwa ya ukombozi. Harakati za kupigania uhuru za Upanafrika kwa ajili ya Afrika Mashariki, ya Kati na ya Kusini zilijumuisha nchi za Uhabeshi, Kenya, Somalia, Tanganyika, Uganda, Zanzibar na vyama vya kizalendo vya Afrika ya Kati na Kusini PAFMECSA. Jumuiya ya pili ilikuwa *Ressemblement Democratique Africain* (RDA), umoja wa maenco mbalimbali ulioundwa na viongozi wazalendo katika makoloni ya zamani ya Ufaransa



PICHA 25.2 *Mkutano wa Waafrika wote huko Akkra, Ghana, Desemba 1958: hotuba ya kufungua*

ambao ulikataa utaratibu wa kuwa na serikali za ndani zisizo na mamlaka kamili uliofikiriwa kuanzishwa chini ya Sheria ya Muhtasari (Loicadre) ya mwaka 1946. Kwa kupitia RDA Waafrika walipata jukwaa la kuuzungumzia mpango huo. Lakini

katika kura ya maoni ya de Gaulle ya mwaka 1958, Sekou Toure wa Guinea peke yake ndiye aliyepiga kura dhidi ya Jumuiya ya Kifaransa na kuchagua kuwa na uhuru kamili na kumuunga mkono Kwame Nkrumah katika Muungano wa Nchi Huru za Afrika.

## Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) na Ukombozi

Ikiwa kuzaliwa kwa nchi nyingi huru Afrika kati ya mwaka 1960 na 1964 kulileta utatanishi katika Upanafrika kama vuguvugu la uunganishi, kuzaliwa huko kuliusaidia na kuupa kazi umoja huo kama chombo cha ukombozi. Viongozi wapya wa Kiafrika takribani walikubaliana juu ya umuhimu wa kuuangamiza ukoloni kabisa katika bara la Afrika, na vikundi vya Kasablanka na Monrovia vililetwa pamoja ili kuunda Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), katika mkutano wa kihistoria uliofanyika Addis Ababa mwezi wa Mei, 1963. Je, ni vipi umoja huu wa OAU ulianzishwa na kuundwa? Na umoja huu ulichangiaje katika kupigania Upanafrika? Kama ilivyoelezwa katika sura iliyotangulia, kutokana, kwa kiwango kikubwa, na juhudi za Kwame Nkrumah, Sekou Toure na Modibo Keita kwa upande mmoja, na kwa upande mwengine kutokana na Algeria kujipatia uhuru wake mwaka 1962 mambo ambayo dhahiri yalipunguza mvutano uliokuwepo kati ya kikundi cha Kasablanka na kikundi cha Monrovia, makubaliano ya kuunda kikundi kimoja yaliweza kufikiwa. Tarehe 23 Mei, 1963 Mkutano wa Viongozi wa Nchi Huru na Serikali ulifunguliwa. Nchi huru 30 ziliwakilishwa: Algeria, Bukini, Burundi, Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Kongo Brazaville, Dahomey, Uhabeshi, Gabon, Ghana, Guinea, Cote d'Ivoire, Liberia. Libya, Madagascar, Mali, Mauritania, Niger, Nigeria, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tanganyika, Tunisia, Uganda, Umoja wa Jamhuri ya Kiarabu na Upper Volta. Tarehe 24 Mei, wakuu wa dola na serikali walitia sahihi Mkataba wa Umoja wa Afrika.

Bamba 25.3 Juu kushoto: Dulcie September, mwakilishi wa ANC (African National Congress), Ufaransa, aliuawa Paris mwezi wa Machi, 1988. Juu kulia: Steve Biko wa Afrika Kusini, kiongozi wa Black Consciousness Movement (Chama cha Mwamko wa Weusi), aliuliwa Septemba, 1977; Chini kushoto, Nelson Mandela wa Afrika Kusini, kiongozi wa ANC kabla ya kuhukumiwa kifungo cha maisha (picha iliyopigwa mapema miaka ya 1960). Chini kulia: Chief Albert Lithuli wa Afrika Kusini, rais wa kwanza wa ANC 1952 - 60.

Ibara mbalimbali za Mkataba zilifafanua malengo ya OAU, pamoja na kuelezea misingi yake na kuzitaja asasi zake. Itikeli ya kisiasa iliyofafanuliwa na Mkataba huu ilisimama juu ya misingi ifuatayo:

(1) usawa kati ya nchi zote wanachama
(2) usuluhishi wa mizozo kwa amani kwa njia ya majadiliano, upatanishi, usuluhishi na maamuzi ya mapatano
(3) kushutumu moja kwa moja mauaji ya kisiasa na vitendo vya uchokozi
(4) kujitolea moja kwa moja kwa ajili ya ukombozi kamili wa nchi za Afrika
(5) kuthibitisha sera ya kutofungamana na upande wowote.

Upanafrika uliwapa wanachama misingi yenye lengo la kuimarisha dhamira zao za kufikilia umoja na mshikamano wa nchi za Afrika. Kwa hivyo Upanafrika ulifanikiwa kukusanya matakwa ya mataifa ya Afrika na kuyaingiza ndani ya Mkataba wa Umoja wa Afrika.

Mwaka 1979, Mkutano wa Viongozi wa Nchi na Serikali waliunda kamati ili kuupitia tena Mkataba kutokana na mabadiliko yaliyotokea Afrika ili Mkataba huo uweze kuonesha vizuri zaidi aula iliyotakiwa kupewa shughuli za maendeleo. Mbali ya hayo, Mkataba ulifanyiwa mabadiliko madogo tu ya kimuundo.

Makao Makuu ya Ofisi ya Katibu Mkuu yapo Addis Ababa, Uhabeshi. Mwaka 1963, Katibu Mkuu wa kwanza, Tesfaye Gebre Egzy, aliteuliwa kwa muda. Mwaka 1964, Mkutano Mkuu wa Viongozi wa Nchi na Serikali ulimchaguwa Diallo Telli kutoka Guinea kuwa Katibu Mkuu. Mwaka 1968 alichaguliwa tena. Alifuatiwa na Mkameruni Nzo Ekangaki mwaka 1972 na huyu alifuatiwa na Mkameruni mwenzake William Eteki Mbumua mwaka 1974. Eden Kodjo kutoka Togo alichaguliwa mwaka 1978, Peter Onu kutoka Nigeria mwaka 1983, Ide Umaru kutoka Niger mwaka 1985, Salim Ahmed Salim kutoka Tanzania mwaka 1989. Katibu Mkuu anasaidiwa na makatibu wakuu wasaidizi watano ambao ndio wanaounda "Baraza la Siasa." Kazi ya Katibu Mkuu imefahamika kwa namna mbalimbali. Kwa baadhi ya watu, yeye ni karani tu aliyevishwa kilemba; wengine akiwemo Rais Omar Bongo wangelipenda kumkabidhi shughuli za kisiasa na za uratibu.

Mamlaka ya juu kabisa ya OAU ni Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali. Hukutana mwaka mara moja kwenye kikao cha kawaida na kwenye kila kikao Mkutano unachagua kamati ya uendeshaji ikiongozwa na mwenyekiti. Kwa

miaka mingi sasa, mwenyekiti huyu amekuwa kiutendaji ndiye mwenyekiti halisi wa OAU.

Taasisi ya pili ya OAU ni Baraza la Mawaziri. Baraza hili hufanya vikao viwili vya kawaida kwa mwaka. Baraza hili hutayarisha mikutano ya wakuu wa nchi na hufuatilia utekelezaji wa maamuzi wanayofikia.

## Umoja wa Nchi Huru za Afrika juu ya suala la uondoaji ukoloni na ukombozi

Moja katika shughuli za Kipanafrika za kudumu na zinazoleta ufanisi wa hali ya juu za OAU ni ule msaada wa shirika ambao umoja huu ulitoa kwa vyama vya ukombozi vya kitaifa. Katika mkutano wa kilele uliofanyika Addis Ababa mwezi wa Mei, 1963, nchi huru zilipitisha azimio la kukubali kwa umoja wao "jukumu la kuwaunga mkono wananchi wa nchi za Afrika zinazotawaliwa katika harakati zao za kujipatia uhuru na kujitawala."

Baada ya kuwasikiliza wawakilishi wa vyama vya kitaifa vya ukombozi kutoka Afrika Mashariki, ya Kati na Kusini, wakuu wa nchi hizi walipitisha maazimio kwamba:

(1) kuendelea kwa utawala wa kikoloni ni ukiukaji dhahiri wa haki zisizoondoleka za wakazi halali wa nchi zilizohusika na pia ni tishio kwa usalama wa bara zima;

(2) kwamba Uingereza iheshimu masharti ya Azimio Namba 1515 la Umoja wa Mataifa kuhusu uhuru na isitoe uhuru kwa Wazungu wachache wa Rhodesia Kusini (Zimbabwe);

(3) kwamba Namibia ilikuwa nchi ya Kiafrika chini ya mamlaka ya Umoja wa Mataifa ambayo wananchi wake walikuwa na haki ya kujiamulia wenyewe mustakbali na uhuru wao na kwamba kuwepo kwa Afrika Kusini kulikuwa ni kitendo cha uchokozi.

Walipeleka ujumbe wa Kiafrika kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambalo lilikuwa likizingatia ripoti ya Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Watu ishirini na wanne kuhusu mauaji ya halaiki katika makoloni ya Kireno. Walikubaliana kukata mahusiano ya kibalozi na kugoma kufanya biashara na serikali za Ureno na Afrika Kusini.

Muhimu zaidi, walianzisha kamati ya ukombozi wa Afrika ambayo wanachama wake walikuwa Algeria, Nigeria, Senegal, Misri, Tanzania, Uganda na Zaire, na ilikuwa iwe na makao makuu yake Dar es Salaam, na iwe na dhamana ya kuratibu misaada kutoka nchi huru za Afrika na kudhibiti Mfuko Maalum ulioanzishwa. Mfuko huu ulikuwa utunishwe na michango ya hiari ya kila mwaka kutoka kwa wanachama wa OAU ili kutoa msaada wa fedha kwa vyama mbalimbali vya ukombozi.

Nchi wanachama vilevile zilikubali kupokea na kuwafadhili wazalendo kutoka vyama vya ukombozi kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi, ya taaluma na ya amali. Pia walitangaza tarehe 25 Mei, kama ndiyo siku ya ukombozi wa Afrika.

Katika mkutano huo huo wa kilele, wanachama walipasisha azimio maalum kuhusu mfumo wa ubaguzi wa rangi (*apartheid*) na ubaguzi wenyewe Afrika Kusini. Pia walishutumu ubaguzi wa rangi katika sura zake zote katika Afrika na duniani kote. Kwa kupitia Kamati ya Ukombozi wa Afrika, OAU ilifaulu sana katika kuondoa ukoloni. Nyingi sana kati ya nchi huru ziliendeleza vikwazo vya kidiplomasia na kibiashara dhidi ya Ureno na Afrika Kusini.

Kimataifa, OAU iliweza kufanya ukoloni na mfumo wa ubaguzi wa rangi ushutumiwe ulimwenguni na kuvipatia vyama vya ukombozi misaada ya hali na mali. Waliufanya Umoja wa Mataifa utambue uhalali wa juhudi za ukombozi. Kutokana kwa kiasi fulani, na shinikizo la OAU, Umoja wa Mataifa haukuutambua utangazaji wa upande mmoja wa uhuru, huko Rhodesia ya Kusini, wala serikali yenyewe ya weupe wachache, na ilianzisha Tume ya Namibia kuchukua nafasi ya utawala haramu wa Afrika Kusini.

Mwaka 1970, OAU ilijizatiti kulenga diplomasia yake upande wa nchi za NATO, nchi za Skandinavia, Switzerland na Japan kwa madhumuni ya kuwafanya wasiendelee kuziunga mkono na kuzipatia silaha serikali za kikoloni. Ukaidi wa serikali ya Pretoria, kuendelea kwake kutumia nguvu na ukandamizaji na kuikalia kwake Namibia kiharamu kuliufanya Umoja wa Mataifa, ukishirikiana na OAU kufanya mkutano wa kimataifa kuhusu vikwazo dhidi ya Afrika Kusini huko Paris kuanzia tarehe 20 mpaka 27 Mei, 1981. Mkutano ulitaka ufanyike mkutano wa Baraza la Usalama. Vikwazo vilikataliwa baadaye na Baraza la Usalama, lakini OAU ilitumia fursa ya Mkutano Mkuu wa Paris kuthibitisha mbele ya jumuiya ya kimataifa msimamo wake juu ya Namibia.

Baada ya muda OAU iliweza kuviathiri vibaya vyama vya ukombozi. Kwa OAU kukitambua rasmi chama chochote cha ukombozi na uongozi wake kulikuwa

mara nyingi jambo muhimu katika duru za kimataifa. Kutambuliwa huku kulivipa uhalali na kufanya vikubalike vyama vya FRELIMO, huko Msumbiji, MPLA huko Angola, PATRIOTIC FRONT ya Zimbabwe na ANC ya Afrika Kusini. Kukataa kwa OAU kuzitambua kidiplomasia kulisababisha kugomewa kimataifa kwa "bantustani" za Afrika Kusini, kwa serikali ya Smith na Muzorewa huko Zimbabwe, na kwa Muungano wa Turnhalle, Namibia. Viongozi kama Moise Tshombe wa Zaire, Jonas Savimbi wa Angola ambao walishutumiwa na OAU kwa ajili ya msimamo wao dhidi ya Upanafrika, na kwa upendeleo wao wa upande wa Magharibi, walisusiwa katika ulimwengu wa watu weusi.

Kuundwa kwa OAU na, hasa, kwa Kamati ya Ukombozi wa Afrika, kulisaidia katika kimyanyua imani na kuhamasisha moyo wa kujitolea katika mapambano ya ukombozi. Ile miaka kuanzia 1963 mpaka 1973 ilitumika kwa jumla katika uundaji wa Kamati ya Ukombozi wa Afrika na vyombo vya ukombozi vya kizalendo, utayarishaji wa matamshi mbalimbali na ilani, na uendelezaji wa mafunzo ya kijeshi. Ndani ya kipindi cha miaka kumi iliyofuatia, yaani kutoka 1973 mpaka 1980, kulipatikana matunda zaidi kwa upande wa makoloni ya Kireno ya Guinea Bissau, Angola, Msumbiji, Sao Tome na Prinsipe na pia visiwa vya Ngazija na Ushelisheli na huko Zimbabwe. Baada ya nchi tatu za mwisho kupata uhuru mwaka 1980, bakaa za ukoloni wa Kizungu zilikuwa ule ukoloni wa walowezi wa Afrika Kusini na Namibia, lakini kupatikana kwa ushindi kulikuwa suala la wakati tu.

Nje ya Afrika, OAU ilishughulikia hali ya Mashariki ya Kati na Palestina. Hivyo ilionyesha mshikamano wake na Misri pamoja na zile nchi za Kiarabu ambazo ardhi yake imekaliwa tangu mwezi wa Juni, 1967, kwa kuzitaka nchi wanachama kutumia vishawishi vyao vyote kuifanya Israeli itekeleze Azimio Namba 242 la Baraza la Usalama, na kwa kuwapa majukumu viongozi maalumu wa nchi kushughulikia baadhi ya masuala haya.

Shughuli nyingine ya OAU imekuwa kusawazisha migogoro kati ya nchi wanachama kwa mujibu wa Ibara XIX ya Mkataba Wake. Migogoro mingi ilitokana na matatizo ya mipaka iliyorithiwa kutoka zama za ukoloni. Katika mwaka 1962 Algeria na Moroko walipambana na katika miaka iliyofuatia zilipambana Uganda na Tanzania, Gabon na Equatorial Guinea, Kamerun na Nigeria, Zaire na Angola, Dahomey (Benin hivi sasa) na Niger, Chad na Sudan, Guinea na Cote d'Ivoire. Mgogoro baina ya Uhabeshi na Sudan umekuwa unaendelea kwa muda, kama ule kati ya Chad na Libya na kati ya Kenya na Somalia.

Mwaka 1979, vikundi vidogo vidogo mbalimbali vya kisiasa na vya kijeshi vilivyokuwa vikipambana huko Chad viliamua, baada ya kushikiliwa na majirani zao, kulipeleka suala lao huko kwenye Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika OAU ililipeleka suala hili kwenye Kamati ya Wakuu wa Nchi ambayo iliweza kuvilazimisha vikundi 11 vya Chad kuungana na kufanya serikali ya umoja wa kitaifa ya mpito (GUNT) chini ya uongozi wa Goukouni Oueddei. Umoja huu uliendelea kwa muda mfupi tu na kwa vile ulikabiliwa na kuzuka tena kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe, OAU ilipeleka katika eneo hilo kikosi cha kulinda amani cha nchi za Afrika mwaka 1981. Hatua hii iliangaliwa kwa mitazamo mbalimbali. Ilikuwa hatua ya mwanzo ya aina yake, na pamoja na kasoro zake, iliweza kunusuru maisha mengi ya binadamu.

OAU pia ilijishughulisha na suala la haki za binadamu na haki za watu kujiamulia wenyewe mustakbali wao. Kwa hivyo Upanafrika ulilenga kuondolea mbali athari za baadaye za utumwa ambazo Waafrika wa diaspora bado walikuwa nazo na vitendo viovu vya ukoloni katika Afrika. Mkutano Mkuu wa Afrika juu ya Utawala wa Sheria uliofanyika Lagos mwaka 1961 ulifikia uamuzi kwamba sheria ilihitaji kutumika kuhifadhi haki za kisiasa za watu binafsi.

Pia inafaa kuzingatia kwamba Dr. Nnandi Azikiwe wa Nigeria mnamo mwaka 1961 alisisitiza katika kitabu chake, *The Future of Pan Africanism* (Mustakabali wa Upanafrika) haja iliyoko ya kutayarisha waraka wa Mapatano Kuhusu Haki za Binadamu yatayoweza kutumika katika mazingira ya umoja wa Uafrika Yote. Haya hayakupatikana mpaka miaka 16 baada ya kuanzishwa kwa OAU pale, kutokana na pendekezo la Rais Sedar Senghor, Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali ulipofanyika huko Monrovia, Liberia mwezi Julai, 1979. Mkutano Mkuu wa Monrovia ulithibitisha haja ya kuheshimu haki za msingi za binadamu na haki nyingine za wananchi, hasa haki za kujipatia maendeleo. Mkutano huu pia ulimtaka Katibu Mkuu wa OAU kutayarisha katika mji mkuu wowote Afrika, mkutano wa mabingwa wa hali ya juu peke yao kwa ajili ya kutayarisha muswada wa Mkataba wa Afrika Juu ya Haki za Binadamu na za Jamii za Watu.

Kuanzia tarehe 18 Novemba mpaka tarehe 8 Desemba, 1979 mabingwa wa sheria wa Kiafrika walikutana Dakar kutayarisha muswada wa awali wa mkataba huu, Mkutano wa Mawaziri wa Sheria ulikutana Bangui, Gambia kupitia rasimu ya awali. Rasimu hiyo ilikubaliwa mwezi Julai, 1981 katika mkutano wa kilele wa viongozi wa nchi huko Nairobi.

Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanadamu na Jamii za Watu, baada ya utangulizi mrefu, una ibara 67 zilizogawika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu haki na dhamana za jamii za watu, sehemu ya pili inahusu hatua za kinga na ya tatu inahusu na mambo mchanganyiko. Nchi huru za Kiafrika siyo tu zilitaka kutoa mchango wao katika kuleta maendeleo na katika kutekeleza "wajibu wa kuwa huru" katika Afrika, bali pia walitaka kuwa na silaha ya ziada ya kuweza kupinga maafa ya ukoloni na siasa ya ubaguzi wa rangi.

*Kazi za maendeleo ya kijamii na kitamaduni*

Katika harakati za kizalendo za ukombozi Afrika, kutetea utambulisho wa kitamaduni wa kulikuwa jambo muhimu. Utamaduni ni chombo cha kuleta ukombozi na cha kutoa mwega kwa juhudi za watu waliotawaliwa; kwa hivyo OAU haiwezi kuupuuza utamaduni katika shughuli zake.

Katika mwaka 1965 OAU ilianzisha Idara ya Shughuli za Kisayansi na za Utamaduni katika ofisi ya Katibu Mkuu. Kwa kushirikiana na UNESCO ilifanya huko Akkra Mkutano Mkuu wa Serikali mbalimbali kuzingatia sera za utamaduni katika Afrika. Mwezi Julai, 1976, Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi Huru na Serikali uliidhinisha Mkataba wa Utamaduni wa Afrika ambao ulikuwa kama kikamilishi cha Mkataba wa Siasa wa mwaka 1963.

Mwamko mpya wa utamaduni wa Afrika ulijitokeza pale lilipofanyika Tamasha la Kwanza la Afrika Nzima huko Algeria mwaka 1969 ambalo lilizaa shughuli kubwa za kisanaa. Tamasha la pili lilifanyika Lagos na Kaduna, Nigeria, mwaka 1977. Mikutano iliyofanywa kwa msaada wa OAU ilifafanua kwa uwazi zaidi shughuli za kitamaduni na pahala pake katika maendeleo. Kongamano mbili za mwanzo zilifanyika katika matamasha ya Afrika Yote na la tatu lilifanyika mwaka 1981 huko Libreville, Gabon.

Vyombo mbalimbali vya mashirikiano ya kiutamaduni vilitokea miaka ilivyoendelea. Kwa mfano vituo vya taaluma ya isimu na historia kwa njia ya fasihi simulizi, na mwaka 1980 Mfuko wa Utamaduni kwa nchi mbalimbali za Afrika ulianzishwa. Mahusiano yaliyoanzishwa kati ya OAU na UNESCO na ALESCO yalizipa shughuli za umoja huo sura ya kimataifa. Kwa kushirikiana na UNESCO, OAU ilifanya Mkutano Mkuu wa Mawaziri wa Elimu mwaka 1964 na mwaka 1982. Mwaka 1982 huko Addis Ababa, OAU ilifanya mkutano wa mwanzo wa wakuu wa vyuo vikuu vya Afrika juu ya Mpango wa Utendaji wa Lagos kwa

kushirikiana na ECA, UNDP, UNESCO na Jumuiya ya Vyuo Vikuu vya Afrika. Kadhalika OAU ilichukua hatua mbili katika uwanja wa sayansi. Ilianzisha "Tunzo ya Kiafrika ya Kuzindua Sayansi" na iliitisha Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wanasayansi wa Afrika katika uwanja wa mambo ya kijamii, imefanywa mikutano mingi juu ya hali ya vijana, wanawake na walemavu. Pia tangu mwaka 1967 Ofisi ya Katibu Mkuu wa OAU imekuwa inaushughulikia Mkutano Mkuu wa Mawaziri wa Kazi wa Afrika, ambao ni chombo cha kudumu chenye dhamana ya kuendeleza sera ya pamoja ya kazi na kurahisisha ushirikiano kati ya nchi wanachama. Hatua zilizochukuliwa na OAU zilipelekea kuanzishwa katika mwaka 1972 kwa Umoja wa Jumuiya za Wafanyakazi za Afrika Nzima zenye makao makuu yake Akkra.

## Upanafrika na Upanarabu

Mwanzoni umoja wa Uafrika na umoja wa Uarabu zilikuwa harakati mbili tofauti. Umoja wa Uarabu (Upanarabu) uliangalia upande wa mashariki na lile eneo lenye rutuba la Mashariki ya Kati. Umoja wa Uafrika (Upanafrika) wa kusini mwa Sahara uliangalia upande wa magharibi kuelekea upande wa watu weusi wa Amerika. Upanarabu uliingiza ndani yake mshikamano wa kitamaduni ambao, kwa kiwango fulani, ulitokana na kutafahari na dini (huu ulikuwa urithi wa Uislamu). Upanafrika uliingiza ndani yake mshikamano wa kitamaduni ambao, kwa kiwango fulani, ulitokana na kutafahari na jamia (huu ulikuwa urithi wa watu weusi).

Upanarabu ulipiga jicho nyuma na kuona tawala zake za kale za Waumamaya na Waabbasi. Upanafrika ulipiga jicho nyuma na kuona tawala za kale za Mali, Songhay na Ghana. Kumbukumbu za Waarabu kuhusu utukufu wa kale wa Uislamu uliwapa kariha washairi na waandishi wa tamthiliya iliyoleta mwamko mpya wa fasihi. Kumbukumbu za Waafrika kuhusu busara za wazee wa kale ziliamsha harakati za kifasihi kama vile *negritude*.

Kwa kiasi kikubwa ilikuwa baada ya Vita vya Pili vya Dunia ndipo Upanafrika na Upanarabu ulipoanza kuungana. Sudan (Khartoum) ilikuwa ndiyo ya mwanzo kuunganisha (dhana hizi). Hisia kinzani za kikale ziliwaathiri Wasudan wengi. Jee, wao walikuwa Waarabu au Waafrika?

Muungano usiokamilika kati ya Upanafrika na Upanarabu uliingia katika awamu mpya yalipotokea mapinduzi ya Misri ya 1952. Gamal Abd al Nasser aliiona Misri kama mfano wa kitovu cha maduara matatu, yaani, ulimwengu wa Waarabu, ulimwengu wa Kiislamu na Afrika. Aliwakumbusha wananchi wenzake

kwamba hawawezi kupuuza mapambano ya umwagaji damu yaliyokuwa yakiendelea kusini mwa Sahara dhidi ya ubeberu na ubaguzi. Licha ya kuutilia chumvi umuhimu wa Misri katika majaaliwa ya Afrika, kijitabu cha al-Nasser kiitwacho "*Falsafa ya Mapinduzi*" kilikuwa ni hatua muhimu ya kuleta kiungo kati ya Upanafrika na Upanarabu

Mshikamano ulikuwa ukiendelea kati ya harakati za uzalendo za Afrika na zile za ulimwengu wa Kiarabu. Wapinga ukoloni na wahamasishaji kutoka Afrika nzima na Mashariki ya Kati walikutana Cairo, wakapanga mikakati ya kuleta mabadiliko na kuandaa njama za mapinduzi. Jamhuri ya Muungano wa Kiarabu chini ya al-Nasser iligharimia sehemu kubwa ya shughuli zao.

Radio Kairo ilikuwa ndiyo sauti ya mwanzo ya mapinduzi kutangaza katika bara la Afrika. Ilitoa matangazo siyo tu kwa lugha ya Kiingereza, Kiarabu na Kifaransa bali pia kwa Kiswahili. Lugha nyingine ziliongezwa baadaye. Misri pia ilitoa msaada wa masomo kwa Waafrika na Waarabu kusoma katika asasi za Misri. Serikali za Kikoloni zilishangazwa na mchango wa Muungano wa Jamhuri ya Kiarabu wa al-Nasser katika kuhamasisha siasa kali katika Afrika ya Kusini mwa Sahara.

Msimamo mkali wa al-Nasser uliimarishwa na mgogoro wa Suez wa mwaka 1956 na kufaulu kwake kuutaifisha mfereji wa Suez. Hujuma dhidi ya Misri iliyofanywa na Uingereza, Ufaransa na Israel ilimnyanyua al-Nasser na kumweka katika hadhi ya shahidi pale aliposhindwa, ikifuatiwa na hadhi ya shujaa pale wagomvi wake walipolazimika kurudi nyuma kufuatia shinikizo la kimataifa.

Hatua ya pili katika kuumana kwa kiasi fulani kati ya Upanafrika na Upanarabu ilifikiwa katika hatua za baadaye za vita vya Algeria vya kupigania uhuru. Vita vilianza mwaka 1954. Kwa kipindi fulani, vita vya Algeria viliigawa badala ya kuiunganisha Afrika. Hii ilikuwa kwa sababu nchi nyingi zilizokuwa zikizungumza Kifaransa zilitatizika baina ya kupinga kwao kwa ukoloni na urafiki wao na Ufaransa. Kwa muda mrefu Paris ilidai kwamba Algeria ni sehemu ya Ufaransa na kwa muda fulani maoni ya wapinzani wa mabadiliko yalionyesha kumpa Mfaransa faida ya shaka. Hii iliigawa Afrika katika ya kundi la Kasablanka (lililopendelea serikali ya uhamishoni ya Algeria) na kundi la Monrovia (lililopendelea kutowepo mabadiliko) Jambo muhimu katika mgawanyiko huu lilikuwa ni kwamba haukuwa mgawanyiko wa moja kwa moja kati ya Waarabu waliopendelea Algeria na watu weusi waliopendelea Wafaransa. Katika kikundi cha Kasablanka

ambacho kilipendelea Algeria alikuwemo mshabiki mkubwa kabisa wa Umoja wa Uafrika, Kwame Nkrumah wa Ghana. Miongoni mwa wasiokuwa Waarabu waliokuwemo katika umoja wa Kasablanka ni Guinea na Mali mbali ya Ghana.

Mgawanyiko katika Upanafrika ulipungua kasi siyo tu baada ya Algeria kujipatia uhuru mwaka 1962, bali pale pia Umoja wa Nchi Huru za Afrika ulipoundwa mwaka 1963. Uwanachama wa OAU ulikuwa wa mchanganyiko wa Waafrika na Waarabu uliohamasishwa na wazo la kuwepo kwa bara lenye jangwa la Sahara ambalo lilionekana kama ni daraja ya kuunganisha, na siyo kizingiti cha kuleta mgawanyiko. Kuundwa kwa OAU kulikuwa hatua nyingine katika mshikamano kati ya Upanafrika na Upanarabu.

Baada ya hapo vilikuja vita vya mwezi wa Juni, 1967 kati ya Waarabu na Israeli. Uvamizi wa Israeli wa Sinai ulionekana kama kitendo cha uchokozi dhidi ya mwanachama wa OAU. Kwa hivyo mshikamano wa Upanafrika na Upanarabu ulizidi kuumana. Mashirikiano ya Israeli na utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini ulijenga msingi zaidi wa mshikamano. Wakati wa vita vya Waarabu na Waisraeli vya Oktoba, 1973 kulikuwa na mshikamano wa kutosha kuwezesha nchi za Afrika karibu zote kwa umoja wao kuvunja uhusiano wa kibalozi na Israeli. Siasa za Mashariki ya Kati sasa zilikuwa kweli zimeshonana na siasa za Afrika.

Jee kuchomoza kwa Umoja wa Nchi Zinazosafirisha Mafuta (OPEC) kulikuwa miongoni mwa misingi ya mshikamano wa Waafrika na Waarabu? Hili ni suala la uchambuzi lenye utatanishi. Ni kweli kutokeza kwa OPEC kuliifanya Nigeria iwe nchi muhimu katika mahusiano kati ya Waarabu na Waafrika weusi. Kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia katikati ya miaka ya 1970 hadi kati ya miaka ya 1980 Nigeria ilikuwa ndiyo kiungo katika mkufu uliouumanisha Upanarabu na Upanafrika. Kwa upande mwingine Umoja wa Kiislam (OIC) wenye nchi wanachama karibu 50 unatoa nafasi kwa muungano kati ya vyombo hivi viwili. Karibu ya nusu ya wanachama wa OIC pia ni wanachama wa OAU. Idadi ya wanachama kutoka Afrika ni kubwa kuliko idadi ya Waafrika katika OPEC. Lakini dini na bei ya mafuta huweza wakati mwingine kuwa ndiyo sababu ya mgawanyiko.

## Ushirikiano kati ya Waafrika na Waarabu

Kushiriki kwa Waafrika na Waarabu katika Kikundi cha 77 na katika majadiliano kati ya kaskazini na kusini kumeleta mashirikiano makubwa zaidi na sehemu zilizobaki za Ulimwengu wa Tatu. Hisia za kuwepo kwa Ulimwengu wa Tatu

ulioshikamana zilizaliwa Bandung mwaka 1955 na zikawa na nguvu zaidi katika mkutano wa kilele wa nchi zisizofungamana na upande wowote uliofanyika Algiers mwaka 1973. Kushabihiana kati ya ubaguzi wa rangi huko Afrika Kusini na Uzayuni wa Palestina na katika eneo lililokaliwa na Waisraeli kulizidi kuwaleta pamoja Waarabu na Waafrika.

Matatizo ya kiuchumi na athari zake katika maendeleo ya Ulimwengu wa Tatu yalizifanya serikali zao kuchukua msimamo mmoja katika kupinga sera za nchi zilizoendelea. Kuongezeka kwa bei ya mafuta kulizifanya nchi za Kiarabu zinazosafirisha mafuta ziwe na nguvu kubwa katika masoko ya fedha ya kimataifa. Jambo hili liliupa madhumuni mapya ushirikiano kati ya Waarabu na Waafrika. Uhusiano kati ya Afrika na ulimwengu wa Waarabu uliendelea kama ifuatavyo:

1. Kikao kisichokuwa cha kawaida cha Baraza la Mawaziri la OAU cha tarehe 21Novemba, 1973 kilianzisha kamati ya kufanya mawasiliano na nchi za Umoja wa Waarabu (Arab League) na kutayarisha sera ya ushirikiano kati ya nchi huru za Kiafrika na ulimwengu wa Waarabu.
2. Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Kiarabu uliofanyika Algiers tarehe 26 mpaka 28 Novemba, 1973 ulifikia uamuzi wa kuanzisha Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA).
3. Katika mkutano wa huko Kairo tarehe 23 Januari, 1974, mawaziri wa mafuta wa Kiarabu walifikia uamuzi wa kuanzisha Mfuko Maalum kwa Msaada kwa Afrika (SFAA). Mtaji wake wa awali ulikuwa $ 200 milioni.
4. Lilipokutana mwezi wa Machi, 1974, huko Tunis, Baraza la Umoja wa Waarabu liliidhinisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Kiarabu wa Msaada wa Kifundi kwa ajili ya Afrika, na tarehe 10 Julai huko Kairo, kamati ya mawaziri wa Kiafrika na Kiarabu iliidhinisha muswada wa azimio na ratiba ya utendaji kuhusu mashirikiano ya Waafrika na Waarabu.
5. Mkutano wa kilele uliofanyika mwezi Machi, 1977, ulihudhuriwa na nchi 60 wanachama kutoka Umoja wa Waarabu na OAU. Walifikia uamuzi wa kuukubali mpango wa muda mrefu wa mashirikiano ya kiuchumi, kifundi na kifedha katika kila moja kati ya nyanja maalum zilizoainishwa.

Kama tutaifanyia tathmini miaka michache ya awali ya ushirikiano kati ya Waafrika na Waarabu, tutaona kwamba hakika kulikuwa na nia ya kisiasa ya kutenda na pia uwezo mkubwa. Lakini mapema sana, utendaji wa asasi hizi ulivizwa

na migogoro ya kisiasa katika ulimwengu wa Kiarabu na pande zote mbili zilikereka na ucheleweshaji wa kiutawala uliojitokeza.

Hawilisho za mitaji kutoka nchi za Kiarabu kwenda nchi za Kiafrika ziliongezeka sana kuanzia mwaka 1973 mpaka 1980. Hivyo kwa mwaka 1974 msaada rasmi kwa ajili ya maendeleo kutoka nchi za OPEC kwenda nchi za Ulimwengu wa Tatu ulikuwa sawa na $ 2.5 bilioni au asilimia 1.74 ya Jumla ya Pato la Taifa. Jumla ya hawala kutoka nchi za OPEC kwenda Ulimwengu wa Tatu zilikuwa $ 5 bilioni mwaka 1974 na 9 bilioni mwaka 1975, yaani ongezeko la asilimia 66. Lakini hiyo bado haikutosha. Halafu zahama iliyotokana na kuteremka kwa bei ya mafuta katika mwaka 1980 (kuzidi kwa mafuta) ilipelekea kupunguka kwa msaada kutoka kwa Waarabu kwenda Ulimwengu wa Tatu.

Lakini kwa mujibu wa mawazo ya wale wanaopendelea kuwepo kwa ushirikiano, ushirikiano wa Waarabu na Waafrika siyo tu suala la kuendeleza hawala za kifedha au vitega uchumi vya kibinafsi. Ushirikiano huo lazima utekeleze kwa vitendo matakwa ya pamoja na mafahamiano yaliyokuwepo kati yao. Ndiyo maana pakawa na umuhimu wa kuoanisha Mpango wa Utendaji wa Lagos uliokubaliwa na OAU na Mkakati wa Amman ulioungwa mkono na Umoja wa Waarabu; jambo hili litafungua njia ya kupatikana mipango ya maendeleo ya pamoja. Ule mpango wa OAU. na Umoja wa Waarabu wa kuanzisha Mfuko wa Utamaduni wa Kiarabu na Kiafrika na Taasisi ya Utamaduni ya Kiafrika na Kiarabu ulionyesha ishara ya kuzipa msukumo shughuli za kubadilishana utamaduni na za kuleta maendeleo ya utamaduni.

## Hitimisho

Inaweza kuonekana kutokana na mjadala huu kuwa dhamira mojawapo ya Upanafrika ni ukombozi wa watu weusi kwa jumla, na hasa Waafrika. Licha ya kuwepo kwa tofauti ya maoni kati ya maslahi ya kiuchumi ya kitaifa na udhaifu ulioko miongoni mwa baadhi ya nchi huru na misaada mikubwa ya kiuchumi, ya kijeshi na ya kidiplomasia iliyotolewa kwa serikali za kikoloni na madola ya Magharibi, OAU na vyama vya ukombozi viliweza kuendeleza mapambano ya pamoja ya Upanafrika na kujipatia ushindi dhidi ya ukoloni na ubeberu wa Kiulaya. Upingaji wa ukoloni, ubaguzi na uendelezaji wa siasa isiyofungamana na upande wowote vilikuwa ndivyo viungo madhubuti kabisa katika muungano wa Upanafrika miongoni mwa nchi huru na vyama vya ukombozi. Itikadi ya Upanafrika iliwaingia

wananchi kwa kiasi cha kuwafanya wawe tayari kubeba gharama na kutoa mihanga iliyohitajika kwa ajili ya kuwakomboa Waafrika wenzao.

Lakini kutokana na hali ya uchumi iliyobadilika sana na hasa kuteremka kwa hali ya uchumi katika Afrika, mipaka ya Upanafrika sasa imepanuliwa na kuweza kuingiza Mashariki ya Kati na Ulimwengu wa Tatu kwa jumla. Siku za usoni bila ya shaka zitaleta uhuru halisi wa kiuchumi na kitamaduni kwa Afrika, na hivyo kufanikiwa kwa ile ndoto ya muda mrefu lakini isiyotimilika ya Wapanafrika wenye siasa kali ya kuwa na serikali moja kwa bara zima la Afrika.

## SEHEMU YA VII

## *AFRIKA KATIKA MAMBO YA ULIMWENGU*

# 26 Afrika na nchi za kibepari

Maovu matatu katika historia ya sasa yameathiri mahusiano ya Afrika na Ulimwengu wa kibepari: biashara ya utumwa, ubeberu na ukabila. Je, yale mahusiano kati ya ubepari na maovu matatu haya ni kitu kisichokwepeka? Au inawezekana ubepari kutenganishwa na mambo haya maovu?

Katika kipindi cha nyuma cha mahusiano ya Afrika na ulimwengu wa kibepari, ilionekana kwamba ubepari uliyopea unaweza kuwepo hata baada ya kukomeshwa kwa biashara ya utumwa. Kwa kweli dola ya kibepari iliyokuwa ikiongoza katika ubepari karne ya kumi na tisa, Uingereza, pia ilikuwa ndiyo dola iliyoongoza katika kukomesha biashara ya utumwa. Jee, kama vile biashara ya utumwa mwishowe ilionesha haihitajiki tena katika ubepari wa kimataifa, ubeberu na ukabila pia nao mwishowe hautohitajika?

Kilichodhihirika katika miaka kuanzia 1945 mpaka 1980 ni kukataa kwa ulimwengu wa kibepari kukubali uhuru wa kisiasa wa Afrika. Miaka ya 1990 inaweza kuonesha utayari wa ulimwengu wa kibepari kukubali kumalizika kwa siasa ya ubaguzi wa rangi na ukabila iliyokwisha tia mizizi kutokana na shinikizo la wapigania ukombozi wa Afrika.

Uondoaji wa ukoloni wa kisiasa na kupata uhuru wa kisheria katika Afrika haukumaanisha kumalizika kwa ubeberu. Matokeo haya yalimaanisha kuwepo mabadiliko tu katika sura ya ubeberu. Sura hii inahusika na baadhi ya sura mpya za ubepari katika Afrika. Ulipopatikana uhuru mambo manne yaliyohusiana yaliamua mabadiliko gani nchi huru mpya za Afrika ziliyataka katika uhusiano wake na ulimwengu wa ubepari. Wakuu wa nchi hizo walitaka kuzifanya jamii zao ziwe jamii za kisasa, walitaka zoezi la kumaliza ukoloni wa kisiasa Afrika likamilike, walitaka kukomesha udhalilishaji unaotokana na ukabila, walitaka kuzifanya nchi

zao ziwe na nguvu, ziwe tajiri na ziwe wanachama wanaoheshimika katika ulimwengu ulioendelea kwa upande wa viwanda, haya yote yakipatikana kutokana na maendeleo ya kiuchumi; mwishowe walitaka kuondoa ukoloni wa kiuchumi ili waweze kuepukana na udhibiti wa nchi za Magharibi wa uchumi wao.

Kuleta mambo ya kisasa kulielewcka, miongoni mwa Waafrika na nchi za Magharibi, kuwa ni mipango itakayogeuza jamii za Kiafrika na kuzifanya ziwe kama mfano wa jamii za karne ya ishirini. Kwa hivyo ushirikiano mkubwa uliingizwa kati ya Afrika na nchi za Magharibi katika juhudi za kuanzisha demkrasia ya kimagharibi katika shughuli za dola; katika kuanzisha shule na vyuo vikuu vya aina ya kimagharibi; katika kueneza itikadi ya kibepari miongoni mwa Waafrika; na katika kuanzisha shughuli za kiuchumi za kimagharibi humo Afrika.

Kwa upande wa Magharibi, vile vile miongoni mwa Waafrika, madhumuni ya haya yote yalikuwa kuwafanya Waafrika wayafikilie kwa haraka maisha ya kimagharibi. Lakini wakati Waafrika walitaka kuanzisha viwanda vyao wenyewe vitakavyoweza kuzalisha vifaa walivyovihitaji, nchi za Magharibi ziliona bora kwamba Waafrika waendelee kutegemea nchi za Magharibi katika kujipatia vifaa hivi. Mawazo ya nchi za Magharibi kuhusu maendeleo ya uchumi ya Afrika yaliishia katika kuleta mageuzi katika uwezo wa Afrika wa kuwa ndiyo mtoaji madhubuti wa mali ghafi na kuamsha hamu za Waafrika za kutaka vifaa vya nehi za Magharibi ili Afrika iwe ndiyo soko lenye faida la vifaa hivyo.

Katika suala la kuondoa ukoloni wa uchumi, nchi huru za Afrika na nchi za Magharibi zilikuwa katika mgongano mkali. Nchi za Afrika zilitaka kunyakua udhibiti wa kiuchumi kutoka nchi za Magharibi ambazo zilivinjari kutaka kuung'ang'ania.

Kwa upande wa kuondoa ukoloni wa siasa, ikiwa mgongano haukuwa mkali kama ule upande wa uchumi, ilikuwa tu kwa sababu mamlaka ya kiuchumi ya nchi za Magharibi juu ya Afrika yalikubaliana na mipango kadha ya kisiasa, mfano ukiwa utawala wa watu weupe wachaehe kama vile katika Jamhuri ya Afrika Kusini na katika kule kulikokuwa Rhodesia, ukoloni halisi katika makoloni ya Ureno yaliyokuwa bado kukombolewa, au ukoloni mambo leo kama katika nchi za Afrika zilizopata uhuru karibuni. Katika kujibu matakwa ya Waafrika ya kuuangamiza ukabila na kuumaliza utawala wa kisiasa wa kigeni katika kila inchi ya bara la Afrika, madola ya Magharibi yalikubali hadharani kwamba kuondoa ukoloni wa kisiasa Afrika na kukomesha siasa ya ubaguzi ni jambo zuri, lakini yaliwekea pingamizi matakwa haya kwa kutumia mbinu za ucheleweshaji pamoja na maneno na matendo ya utatanishi ambayo Waafrika waliyaona ya kuudhi mno.

Hali iliyotokana na migogoro hii na kusadifia kuwepo hisia za aina moja kulisababishwa, kwa kiwango kisichokuwa kidogo, na ule mfumo wa taasisi zilizohusisha nchi nyingi ambazo nchi za Magharibi zilianzisha kutokana na maafa ya Vita vya Dunia vya Pili. Umoja wa Mataifa (na hasa vyombo vyake kama UNCTAD, EEC, Benki ya Dunia na shirika la I.M.F.) vilikuwa ndiyo wahusika wakuu katika tokeo lililofuatia.

## Ushirikiano wa pamoja na Mkataba wa Atlantiki

Katika awamu za mwanzo mwanzo za Vita vya Pili vya Dunia, viongozi wa Umoja uliyokuwa dhidi wa Mafeshisti waliona kwamba ushindani mkubwa wa uchumi uliyokuwepo kati ya madola ya kibepari lazima uvizwe ikiwa pasisababishwe vita vingine vya ulimwengu. Kwa hivyo walijizatiti kutayarisha mipango itakayowawezesha kudhibiti amani baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Mkataba wa Atlantiki ulitangazwa mwaka 1941 na Rais wa Marekani Franklin Roosevelt na Waziri Mkuu wa Uingereza, Winston Churchile ulikuwa ndiyo kihamasisho na kariba yao. Msingi wa Mkataba wa Atlantiki ulikuwa na ile falsafa ya ushirikiano wa pamoja ambayo ilikuwa ndiyo msingi katika uundaji wa taasisi muhimu za kisiasa, kiuchumi na kiulinzi katika ulimwengu wa kibepari wa baada ya vita.

Makubaliano ya Bretton Woods ya mwaka 1945 yalianzisha Shirika la Kimataifa la Kifedha (IMF), Benki ya Dunia na Makubaliano ya Jumla ya Kodi ya Forodha na Biashara (GATT). IMF ilipewa kazi ya kuondoa matatizo yaliyosababishwa na kuwepo kwa ziada au upungufu katika biashara ya kimataifa. Benki ya Dunia ilipewa jukumu la kushajiisha uwekaji wa vitega uchumi vya rasilimali kwa ajili ya ujenzi mpya wa maendeleo ya nchi wanachama. Kwa GATT ilikabidhiwa dhamana ya kuendeleza biashara ya ushirikiano wa pamoja kwa kupunguza pingamizi za kibiashara, ushuru wa forodha, kiwango cha uagiziaji bidhaa na kwa kuvunja kasi mtindo wa kufanya makubaliano ya biashara ya upendeleo.


Upande wa kisiasa na kijeshi, Mkataba wa Atlantiki ulihamasisha kuanzishwa kwa vyombo viwili. Cha kwanza ni Umoja wa Mataifa ambao ulianzishwa mwaka 1945. Umoja huu ulikuwa ndiyo jukwaa la kisiasa la kujadili matokeo duniani. Mwaka 1948, Umoja wa Mkataba wa Atlantiki (NATO) ulibeba dhamana ya ulinzi wa pamoja wa madola ya Ulaya na Marekani Kaskazini ya ulimwengu wa ubepari.

Baadaye viliundwa vyombo viwili vya ushirikiano wa pamoja vya uchumi ambavyo vilileta matokeo yaliyoathiri Afrika huru. Umoja wa Uchumi wa Ulaya ulianzishwa kutokana na Mkataba wa Roma mwaka 1957. Mkataba huo ulikusudiwa kuendeleza sera za pamoja za mambo ya nje miongoni mwa wanachama katika nyanja za biashara, kilimo na usafiri. Katika mwaka 1961 klabu ya madola makubwa ya kibepari, yaani, Umoja kwa Ajili ya Mashirikiano na Maendeleo ya Kiuchumi (OECD) ulizaliwa, ili miongoni mwa mambo mengine, kupanua biashara ya ushirikiano duniani.

Bila ya kuulizwa chochote, nchi huru za Kiafrika zilishirikishwa katika taasisi hizi. Zilishawishiwa kujiunga na Umoja wa Mataifa na vyombo vyake, pia IMF, Benki a Dunia na GATT, na zilikuwa ziendeleze mahusiano ya kiwango cha chini na vyombo vya EEC, NATO na OECD. Pia nchi huru za Afrika zilishawishiwa kujiunga na vyombo kama Jumuiya ya Madola ya Kiingereza na Jumuiya ya Kifaransa, ambavyo watawala wao wa zamani waliviunda kama ni vyombo vya kuendeleza mamlaka yao ya kisiasa. Nchi nyingi huru za Kiafrika pia zilitia sahihi ya makubaliano ya ulinzi na mabwana wao wa zamani, mpango ambao uliruhusu watawala wa zamani (hasa Wafaransa) kuweka majeshi katika nchi za Afrika. Kwa hivyo nchi za Kiafrika siyo tu zilijiweka chini ya utiifu wa vyombo vya juu kabisa, bali pia zilijizonga zonga kwa nyaya elfu kwenye taratibu za ndani za mfumo wa kibepari wa ulimwengu.

Na kwa kweli, baada ya kujipatia uhuru, Afrika ya wenyewe kwa wenyewe katika nchi zilizokuwa zamani zimetawaliwa (kama katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Nigeria na Chad) nchi za NATO kawaida huchukua hatua walizoshauriwa kuzichukuwa na watawala wa zamani wa nchi hizo. Lakini kama ilionekana kwamba nchi ambayo zamani ilikuwa chini ya ukoloni imekabili tishio la uchochezi wa zamani ilikuwa chini ya ukoloni imekabili tishio la uchochezi wa kikoministi (kama ilivyokuwa Congo wakati wa Lumumba) basi Marekani, kama kiongozi wa NATO, huingilia moja kwa moja. Uondoaji ukoloni wa kisiasa na mchuano wa Mashariki na Magharibi (1960-1984).

Kampeni za kuondoa kabisa ukoloni wa kisiasa katika Afrika mwishowe zilidhoofisha ulinzi wa NATO na kuugeuza uwe mamlaka ya OECD. Haya yalitokea kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, pale nchi huru za Kiafrika zilipopanua mahusiano yake ya kiuchumi na sehemu nyengine ulimwenguni basi miongoni mwa nchi za kibepari zilizokuwa na mahusiano makubwa ya kiuchumi na Afrika mlikuwa nchi




*PICHA: Mkutano Mkuu wa Wafaransa-Waafrika huko La Baule, Ufaransa, Juni 1990*

za OECD zisizokuwa wanachama wa NATO kama vile Switzerland, Ireland, Sweden na Japan. La pili ni kwamba, kwa kutoa misaada ya kimali kwa harakati za kuondoa ukoloni Afrika, kikundi cha Kisovieti kiliweza kuingilia katika mambo Afrika moja kwa moja na hivyo kuudhoofisha ulinzi wa NATO. Ilipofikia kati ya miaka ya 1970 kikundi cha Kisovieti kilikwisha tia mizizi huko Uhabeshi, Angola na Msumbiji, nchi ambazo zilijitangaza kuwa zinafuata ujamaa wa Kisovieti au siasa ya Kimaksisti.

Zikijaa wasiwasi, dola za Magharibi zilijaribu kuvizuwia vishawishi vya kikundi cha Kisovieti kuingia Afrika. Wazalendo wa Kiafrika hawakuchukizwa hata kidogo na kule kuweza kujipatia msaada wa kikundi cha Kisovieti katika kampeni zao za kumaliza ukoloni wa walowezi wa Kirhodesia huko Zimbabwe, ukoloni wa Kireno Angola, Guinea Biassau na Msumbiji, utawala wa Afrika Kusini, huko Namibia na siasa ya ubaguzi wa rangi na utawala wa walowezi weupe huko Afrika Kusini.

Katika nchi huru za Afrika himaya ya NATO ilihifadhiwa kwa njia kadhaa: kama vile kwa njia ya kampeni za kupendelea nchi za Magharibi dhidi ya Sovieti, kulindwa kisiasa na balozi za Magharibi kwa serikali za Kiafrika, kuingilia kisiasa kichinichini na pale yote mengine yanaposhindwa kufanya uvamizi bayana wa

kijeshi wenye lengo la kutoa mwega kwa serikali zilizoelemea upande wa Magharibi zilizokuwa zikiyumbayumba au kuzipindua serikali zilizoelemea upande wa Kisovieti kwenye zile nchi ambazo serikali ya aina hiyo imeweza kuchomoza. Mara kadha uingiliaji wa kijeshi dhidi ya ukoministi katika Afrika uliongozwa na majeshi ya Magharibi au yale yaliyogharimiwa na Magharibi. Katika uingiliaji wa aina hii, zilikuwemo shughuli za kijeshi za Umoja wa Mataifa huko Kongo (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) kuanzia mwaka 1960 mpaka 1964 za kumuondosha Patrice Lumumba, kuingilia kati kwa Muingereza huko Kenya na Tanganyika mwaka 1964, mapinduzi dhidi ya Nkrumah huko Ghana mwaka 1966, na harakati za Shaba mwaka 1977 na katika mwaka 1978-79 harakati za kumlinda Mobutu kutoka maadui zake wa Kizaire. Pia kulikuwa vikosi kadha vya mamluki vya kupindua serikali za Kiafrika zilizoelemea mrengo wa kushoto kama huko Guinea mwaka 1970 na Ushelisheli mwaka 1979 na mwaka 1982. Njia hizi kwa jumla zilifaulu kuiweka hali ya kupendelea nchi za Magharibi isalie katika nchi zilizohusika.



*Picha 26.2 Ufungaji wa kiwanda cha kupiga chapa CICIBA, Libreville, Gabon na mafundi kutoka kwenye Shirika la Mitsubishi, Japan.*

Nchi za Magharibi kabisa hazikuweza kufaulu sana katika kuzuwia serikali zilizomiliki upande wa Sovieti zisichomoze katika nchi zilizokuwa zimetawaliwa hapo zamani. Juu ya kwamba nchi za Magharibi zilikua na maslahi yake yenyewe zilipoondoa ukoloni wa kisiasa katika makoloni, hofu ya Waafrika waliomiliki upande wa Sovieti kuingia madarakani baada ya kuondoka Wazungu ilizifanya nchi za Magharibi ziunge mkono ukoloni uliosalia wa Ureno, Rhodesia na Afrika Kusini. Kwa hivyo mapambano ya silaha ya muda mrefu yalibidi kuendelezwa dhidi ya ukoloni wa Kireno na wa Kirhodesia. Msaada mkubwa wa kijeshi na wa kidiplomasia kutoka kikundi cha Kisovieti au hata upande wa Kimaksisti.

Huko Uhabeshi tawi la Kimaksisti la mapinduzi ya kijeshi lililokuwa dhidi ya ufalme wa kimwinyi lilishinda katika mchuano wa madaraka uliofuatia kupinduliwa kwa Mfalme Haille Selassie licha ya juhudi kubwa za Magharibi kutaka kuwatawalisha rafiki zao.

Kutokana kufaulu kwa wazalendo wa kimaksisti wa Kiafrika, ulinzi wa NATO katika Afrika ulidhoofika sana. Jambo hili liliamsha tena hofu za nchi za magharibi na nchi hizo ziliona hakuna sababu kubwa ya kusaidia kupatikana kwa utawala wa watu weusi walio wengi huko Afrika Kusini. Kutokana na haya, kampeni ya Wafrika ya kuondoa ukoloni wa kisiasa ilikuwa bado kumalizika ilipofika kati ya miaka ya 1980. Namibia ilikuwa bado ikipigania uhuru wake na licha ya kuwepo kwa shinikizo la kimataifa, mwisho wa siasa ya ubaguzi na utawala wa watu weupe huko Afrika Kusini ulikuwa bado kudhihiri. Mwishoni mwa mwaka 1984, inaweza kutamkwa kwamba wakati NATO ilipoteza himaya yake juu ya yale makoloni ambayo bado himaya hiyo ilikuwepo, katika mwaka 1970, ilifaulu kutetea himaya yake juu ya makoloni mambo leo ambayo iliwapa uhuru wa kisiasa. Haya yote yalithibitisha mkakati wa jumla wa Kimagharibi baada ya vita wa kutoa uhuru wa kisiasa kwa makoloni ili iwezekane kuyadhibiti ndani ya duru la kiuchumi la nchi za Magharibi.

## Maendeleo ya kiuchumi na uondoaji wa ukoloni 1960-73

Kwa vile zilihazimia kuiweka Afrika kama mahamia ya kiuchumi, nchi za Magharibi zilikuwa tayari kwa kiwango fulani kunyanyua uchumi wa Kiafrika na kugharimia maendeleo ya kiwango fulani ambayo dola za kikoloni zilianzisha baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Lakini matakwa ya wazalendo wa Kiafrika yalipindukia kiwango ambacho nchi za Magharibi zingelikidhinisha. Kwa hivyo robo karne ya mwanzo

ya uhuru wa kisiasa wa Afrika ilishuhudia kuongezeka moja kwa moja kwa shinikizo la Waafrika la kutaka maendeleo na kuondolewa kwa ukoloni na juhudi za nchi za Magharibi za kuyawekea vizingiti yote hayo.

Kwa mujibu wa taratibu za kuleta maendeleo zilizokubalika, mifuko ya vitega uchumi na ruzuku za misaada, bidhaa za mzalishaji na ubingwa wa ufundi, vyote hivi vitaingizwa kutoka nchi za nje pamoja na akiba zilizokusanywa ndani ya nchi vitumike kuanzisha viwanda nchini vitakavyochukua nafasi ya uagiziaji bidhaa na pia viwanda vyakutayarisha mali ghafi. Miundo msingi ya kiuchumi itajengwa ili kutekeleza matakwa ya viwanda na kusambaza bidhaa zao. Miundo msingi ya ustawi wa jamii itanyanyua uwezo wa wafanyakazi kutoka nchini ili waweze kuajiriwa. Kilimo na uchimbaji migodi vitazaa bidhaa za kusafirisha ambazo zitasaidia kulipia gharama za bidhaa za matumizi na pia kutoa sehemu ya fedha kwa ajili ya kuendeleza viwanda. Mkakati huu ulitarajiwa kuzalisha kiwango cha ukuwaji wa Jumla ya Pato la Taifa kikubwa cha kutosha ili kuweza kuziba pengo kati ya viwango vya maisha vya nchi za Magharibi na za Afrika.

Kulikuwa na tofauti ya mawazo kati ya wale wanaofuata siasa ya ujamaa na wale wanaofuata siasa ya ubepari katika Afrika kuhusu mipango ya kijamii ya ndani ambayo itumike katika utekelezaji wa mkakati huu wa maendeleo. Kwa wale walioiamini njia ya ujamaa ya kufikilia maendeleo, utekelezaji ulikuwa kwa kupitia umilikaji wa njia kuu za uzalishaji. Kwa upande wa utekelezaji umilikaji wa pamoja maana yake ni umilikaji wa dola. Kwa wale walioamini njia ya ubepari ya kufikilia maendeleo, mkakati huu utatekelezwa kwa mujibu wa misingi ya kibepari ya umilikaji wa njia kuu za uzalishaji na wote wawili kati ya dola na watu binafsi. Kwa hiyo walipendelea uchumi wa mchanganyiko utaojumuisha miradi ya dola na ile ya watu binafsi kwa viwango mbalimbali.

Lakini hata kabla ya miaka ya 1960 kumalizika, ilikuwa wazi kwamba kuna kitu kilichokwenda sivyo kabisa katika zile taratibu za msingi za kuleta maendeleo. Mapema katika mwaka 1970 hapakuwa na dalili ya nchi yoyote ya Kiafrika, na iwe ya kibepari, ya kijamaa au ya kimaksisti iliyoweza kufikia viwango kama vya nchi za Magharibi. Madola tajiri yalizidi kuwa tajiri, wakati nchi maskini, zikiwemo za Kiafrika, zilikuwa zikizidi kuwa maskini. Kabla ya kupanda kwa bei ya mafuta, Waafrika wachache tu ndiyo walionasibisha maendeleo ya uchumi na kuondoa ukoloni katika mahusiano yao ya kiuchumi na nchi za nje. Kuondosha ukoloni, kwa jumla, kulionekana kama sawa na kuleta Uafrika kwa maana ya kuweka Waafrika walio wengi zaidi kwenye vyombo vya kiuchumi vilivyorithiwa kutoka enzi za ukoloni. Kwa upande wake, nchi za Magharibi zilipinga utaifishaji na hata uchukuaji wa sehemu tu ya mali na walipinga mabadiliko katika mahusiano ya kiuchumi kati ya Afrika na nchi za Magharibi.

Ufaransa chini ya Charles de Gaulle ulionyesha mapema sana kwamba majaribio ya Afrika ya kujikwamua na nchi za Magharibi yatatiwa adabu kali kwa kukatwa mahusiano yote kwa mfano huko Guinea yaliyotokea mwaka 1958. Kulingana na taratibu za NATO nchi nyingine za kibepari pia ziliisusia Guinea. Kutengwa kwa Guinea kwa lazima na nchi za kibepari kuliendelea hadi mwaka 1963, na kuliilazimisha Guinea itegemee sana upande wa kikundi cha Kisovieti. Tanzania mwaka 1967 na Angola mwaka 1975 walijichagulia maendeleo ya kijamaa lakini waliendelea kwa busara kuwa na mahusiano na nchi za Magharibi ya kiwango walichokiona kinahitajika.

Kulikuwa na kutofautiana pia miongoni mwa nchi za kibepari. Baadhi yao (kama Cote d'Ivoire, Malawi, Kenya na Zaire) walilindwa sana na nchi za Magharibi katika shughuli zao za kiuchumi. Nyingine kama Nigeria zilihiari kufuata njia ya ubepari chini ya uangalizi na udhibiti mdogo tu. Ghana ilikuwa na hali ya aina yake pekee. Wakati Nkrumah aliunga mkono kwa dhati njia ya ujamaa, hakujafanywa lolote kubwa wakati wake la kukata mahusiano na nchi za kikoloni au kuibadilisha misingi ya kibepari ya jamii na uchumi huko Ghana. Baada ya kupinduliwa kwa Nkrumah mwaka 1966 lugha ya ufasaha ya kiujamaa iliachwa na Ghana kusalia kwenye njia ya ubepari ya maendeleo.

Nchi za ujamaa zilikuwa na hima zaidi katika kutaifisha mali za kigeni kuliko zilivyokuwa nchi za kibepari. Nchi hizi za kibepari zilihiari aghalabu 'kuenyejisha', yaani kutumia taratibu zilizoruhusu dola na Waafrika binafsi kuwa na hisa katika kampuni za kigeni na Waafrika waliingizwa katika ngazi mbalimbali za uongozi.

Uchukuaji mali, ikiwa kwa njia ya kutaifisha au kwa kuwakabidhi wenyeji hakukufanyika bila ya kuleta matokeo fulani kutoka nchi za Magharibi. Serikali za Magharibi katika miaka ya 1960 zilitishia kulipa visasi kwa wale waliotaifisha mali yao. Ufaransa walikuwa hasa wakali kwa makoloni yao ya zamani. Pale ambapo tishio kama hizo hazikuzuia utaifishaji, Wafaransa walidai fidia nzito. Hatua ya muda mrefu wa Wafaransa kwa kuchukuliwa mali yao ilikuwa kutoka kwenye taratibu za kushiriki kwenye hisa kwenda kwenye utumizi mkubwa zaidi wa mikopo na madeni kutoka kwa wauzaji bidhaa. Madola mengine ya Kimagharibi nayo yaliiga. Vile vile kulikuwa mabadiliko kutoka udhibiti wa moja kwa moja wa kampuni tanzu na kampuni mama kwenda kwenye utuaji wa msaada wa kifundi, kwenye kushiriki katika uendeshaji na kwenye kutayarisha mipango ya mafunzo. Wawekezaji vitega uchumi wa Kizungu walianza kutegemea mipango ya bima

iliyotayarishwa na serikali zao ili kujinusuru na hatari zisizokuwa za kibiashara kwa mfano vita, mapinduzi au kupokonywa mali.

Nchi za Kiafrika zilizokuwa na hamu ya kujipatia vitega uchumi vya kigeni zilijikuta zinaingia katika Makubaliano ya Kuhifadhi vitega Uchumi, IPA, na nchi za Magharibi. Mapema tangu mwaka 1960 Ufaransa uliingia katika makubaliano kama haya na Senegal, Madagascar, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kongo Brazaville, Chad na Gabon. Italiana, Uswisi, Ujerumani, Uholanzi, Ubeligiji, Denmark na Ufaransa walianzisha makubaliano kati ya nchi mbili mbili ya aina ya IPA na pia makubaliano yenye masharti yanayohifadhi vitega uchumi kati ya nchi hizi na kiasi nchi 20 za Kiafrika ilipofika mwaka 1981.

Kwa kutumia mbinu kama hizi, nchi za Magharibi ziliweza kuvunja kasi upokonyaji wa mali zao na kuzifanya kampuni za magharibi ziweze kuweka vitega uchumi kwa salama. Katika nchi za Kiafrika ambamo upokonyaji ulitokea, zile kampuni ambazo zilimilikiwa na Waafrika kwa ukamilifu au kwa kiwango fulani mara waligundua kwamba kuna mipaka katika uhuru wao wa kutenda. Haikuwezekana kwao kuongeza bei waliyoweza kupata kwa bidhaa zao za kusafirisha au malipo yao kwa bidhaa walizoagiza kwa vile kampuni chache za Kimagharibi ziliitawala biashara ya dunia ya kila bidhaa. Ilipofikia mapema katika miaka ya 1960, Nkrumah ambaye nchi yake tayari ilikwishapata uhuru wake mwaka 1957, alikuwa akishutumu madaraka yaliyojificha ya vikundi vya wachache vya nchi za Magharibi na kudai kwamba walikuwa pingamizi kwa maendeleo ya uchumi. Lakini alipoleta masuala haya viongozi wa Kiafrika wengi sana waliyapuuza. Lakini ilipofika kati ya miaka ya 1970, mabepari na wajamaa walikuwa wameshaanza kukubaliana na umaizi wake. Walivyotambua umuhimu wa kuondoa ukoloni katika mahusiano ya kiuchumi na nchi za Magharibi, viongozi wa Kiafrika walipata sababu ya kutosha ya kujiunga na harakati za Ulimwengu wa Tatu zilizolenga kubadilisha taratibu za kiuchumi za kimataifa. Msukumo uliowafanya waendeleze kampeni ya kuleta Mpango Mpya wa Uchumi wa Kimataifa ni kule kupandishwa kwa bei ya mafuta na OPEC.

## OPEC kuwa njia panda

Kufaulu kwa nchi za OPEC katika uamuzi wao wa peke yao wa kuongeza bei ya mafuta kwa mara nne kati ya mwaka 1973 na 1974 kulibadilisha hisia kuhusu jambo gani linawezekana kuhusu uchumi wa kimataifa. Hii ilikuwa sawa na kufikia njia panda: kuanzia hapa shughuli za maendeleo na uondoaji wa ukoloni yatafanyika

kwa moyo mwingine. Kitendo cha OPEC kilisababisha mgogoro adhimu katika mizani ya malipo kwa nchi zisizotoa mafuta, mgogoro ulioubadilisha uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na kuzifanya ziwe mfano wa jinamizi. Lakini wakati huo huo haya yalinyanyua matumaini kwamba mwishowe mgogoro utatatuliwa kwa njia ya maongezeko makubwa ya kipato kutoka usafirishaji wa bidhaa ikiwa haya yanaweza kutendeka pia kwa bidhaa nyingine.

Kitendo cha OPEC pia kilionyesha kwamba uwekaji bei na vikwazo vingine vinaweza kukiukwa kwa kuwepo muungano wa wakiritimba pamoja na hujuma za ujima za kisiasa dhidi ya taratibu za mahusiano ya kiuchumi na nchi za nje. Kufuzu kwa OPEC kuligeuza mjadala wa kitaalamu kuhusu mkakati wa maendeleo na kuufanya uwe mjadala wa hadhara, na pia kugeuza matakwa pekee kuhusu uondoaji wa ukoloni katika mahusiano ya kiuchumi ya kimataifa yawe kama kiitikio cha dunia nzima. Ile ndoto ya kubadili muundo wa mahusiano kwa maslahi ya nchi za Ulimwengu wa Tatu ilihamasishwa na kampeni ya kuleta Mpango Mpya wa Kimataifa wa Kiuchumi (NIEO). Kwa Waafrika mfano wa OPEC uliipa nguvu ile nia ya kujipatia masharti bora katika mapatano yaliyokuwa yakiendelea kuhusu mipango ya kiuchumi kati ya nchi za ACP na EEC. Na pale nchi za Kiafrika zilipotumbukia katika hali ya kukwama kwenda katika hali ya kuanguka na baadaye kukabiliwa na mgogoro, haya kwa kiasi fulani yakitokana na kupanda sana kwa bei ya mafuta, nchi hizo ziliendelea kutafuta mikakati madhubuti ya maendeleo na njia za kubadilisha mahusiano na nchi za nje kuhusu uchumi. Ile kampeni ya kuondoa ukoloni katika mahusiano ya kiuchumi kati ya Afrika na nchi za nje ilifuatana na majadiliano ya kikweli kuhusu maendeleo na mtindo wa kutegemea wengine.

## Kampeni ya kuondoa ukoloni, 1974-84

Nchi za Kiafrika ziliendeleza uondoaji wa ukoloni wa kiuchumi kwa kupitia njia mbili kuu: kampeni ya pamoja ya Ulimwengu wa Tatu kwa ajili ya Mpango Mpya wa Uchumi wa Kimataifa, na mapatano kwa ajili ya Makubaliano ya Lome kati ya nchi za Afrika - Karibiani na Pasifiki (ACP) na Umoja wa Kiuchumi wa Nchi za Ulaya (EEC). Kitovu cha juhudi hizi kilikuwa mahusiano ya kiuchumi na nchi za nje; juhudi hizi hazikuzingatia mahusiano yoyote ya kijamii yaliyokuwa ndani ya nchi za Kiafrika ambayo huenda yakachangia katika kukosekana kwa maendeleo.

Kuanzia kati ya 1960, kampeni ya kugeuza miundo ya mahusiano ya kiuchumi ya ulimwengu ilianzishwa na kikundi cha 77 kwa kariha iliyotokana na wataalamu

wa mambo ya uchumi wa huko Marekani ya Kilatini. Katika mwaka 1974 huko Umoja wa Mataifa, kikundi hiki kilipitisha Azimio la Uanzishaji wa Mpango Mpya wa Kiuchumi wa Kimataifa pamoja na Taratibu zake za Utendaji. Pia walipitisha Mkataba wa Haki za Kiuchumi na Dhamana za Dola. Mkataba huu ulieleza kwamba madola yana mamlaka juu ya mali asili zao na juu ya mali za kigeni na za mashirika ya kimataifa yaliyomo nchini mwao, na walikuwa na haki ya kutaifisha na kudhibiti fidia kwa mali ya wageni. Pili ililazimisha nchi zinazoendelea kusawazisha ile hali ya kutowepo usawa katika muundo wa kiuchumi wa kimataifa kwa kuviunda upya vyombo vinavyohusika na kufanya uamuzi katika I.M.F., Benki ya Dunia na jumuiya nyingine za kifedha za kimataifa.

Washington, Paris na London waliisikia mbiu ya mgambo hii kwa taharuki. Masuala ambayo kampeni za NIEO yaliyashughulikia ni kupanda na kushuka kukubwa kuliokuwepo kwa bei za mali ghafi, zikilinganishwa na bei ya bidhaa zilizokwisha kutengenezwa, Ulimwengu wa Tatu kutoweza kujipatia teknolojia ya kuendeleza viwanda, mtiririko usiotosha wa rasilimali kutoka biashara na nchi za nje, misaada ya kigeni na vitega uchumi vya kigeni kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya Ulimwengu wa Tatu. Kusawazisha hali hii, walipendekeza mageuzi katika mfumo wa kifedha, katika kuhawilisha teknolojia katika taratibu za uendelezaji viwanda na katika biashara za kitaifa.

Ili fedha za kusaidia maendeleo ziweze kupatikana kwa wingi kwa nchi za Ulimwengu wa Tatu, walitaka kuwe mabadiliko katika taratibu za uchaguzi katika IMF ili zizipe upendeleo nchi zinazoendelea, kuwa na ongezeko kubwa katika mtaji wa Benki ya Dunia ili iweze kuongeza mikopo kwa nchi maskini sana, kuyagharimia upya na kuyapangia upya malipo ya madeni ya baadhi ya nchi za Ulimwengu wa Tatu na kulengwa kwa msaada kutoka kwa wafadhili yenye kiwango kisichopungua asilimia 0.7 ya Jumla ya Pato la Taifa itakapofikia mwaka 1980.

Kuhusu teknolojia na uendelezaji viwanda, mpango ulikuwa kufanya iwe rahisi kwa nchi za Ulimwengu wa Tatu kujipatia teknolojia ya Kimagharibi kwa kupunguza gharama ya kujipatia ruhusa rasmi ya kuhifadhi kutoka kuigwa kitu kilichovumbuliwa, gharama ya leseni na gharama ya kujipatia alama ya biashara na ya kujipatia mabingwa wa ufundi ili kuzisaidia ziweze kufikilia asilimia 25 ya mazao ya viwanda ifikapo mwaka 2000. Walipendekeza kwamba bidhaa zao zipate upendeleo katika kufikia masoko ya nchi za Magharibi.

Upande wa biashara za kimataifa, Ulimwengu wa Tatu uliona kwamba shida zao zinatokana na muundo wa soko la dunia. Waligundua kwamba udhibiti wa mazao na madini yao ulikuwa mikononi mwa jumuiya za biashara za Magharibi. Ubadilishanaji wa bidhaa mbalimbali ulikuwa mikononi mwa kampuni kubwa chaehe. Kwa mfano kampuni tatu za kimataifa zilidhibiti soko la ndizi la dunia; karibu asilimia 90 ya biashara ya kusafirisha tumbaku ilidhibitiwa na mashirika sita na kampuni nne zilidhibiti soko la aluminium.

Serikali za Ulimwengu wa Tatu zilitafuta njia ya kupunguza udhibiti wa nchi za Magharibi kwa kutumia Makubaliano ya Bidhaa za Kimataifa (ICA) ambayo yalikuwa na taratibu za kuweza kutuliza na kupanua kidogo kidogo kiwango cha mapato ya nchi za Ulimwengu wa Tatu yanayotokana na usafirishaji wa bidhaa. Ili kuhifadhi uwezo wa kununua/kutokana na bidhaa zao za kusafirisha, nchi hizi zilipendekeza kuoanishwa kwa bei ya bidhaa zao za awali na zile za viwandani. Fikra hizi ziliibuka kutoka UNCTAD IV huko Nairobi mwaka 1976, kama pendekezo la kuwepo kwa Mpango wa pamoja wa Bidhaa (IPC).

Madola ya Magharibi hayakupendelea mageuzi yatakayodhoofisha udhibiti wao wa uchumi wa dunia. Lakini hawakutaka kuzagaa kwa muungano wa wakiritimba wa aina ya OPEC kwa ajili ya bidhaa nyingine au kuwepo kwa mazingira ya michuano ya kiuchumi. Kwa hivyo waliingia katika mapatano ili kuvunja kasi shinikizo la nchi za Ulimwengu wa Tatu na kuleta mipango yoyote ambayo nchi za Magharibi zitayakubali yawe chini ya udhibiti wa IMF, Benki ya Dunia na taasisi nyingine zilizotawaliwa na nchi za Magharibi. Kama itavyotarajiwa, mapatano hayo hayakuleta tija kubwa. Mwaka 1980, chapisho la Umoja wa Mataifa liitwalo Development Forum lilikubali kwamba hapajakuwa na mabadiliko makubwa kwenye sheria na miundo iliyotawala viwanda na uhawilishaji wa teknolojia. Ilipofika mwaka 1984, ICA zilikuwepo kwa ajili ya bidhaa tano tu za kusafirishwa: yaani sukari, kakao, kahawa, bati na mpira wa kimaumbile. Na moja tu kati ya hizi zote ndiyo iliyowekewa makubaliano, yaani International Rubber Agreement, badda ya UNCTAD IV.

Vilevile ule Mpango wa Fedha za Fidia yaani, 'Compensatory Finance Facility' ulishindikana kuanzishwa. Ilipofika mwaka 1983 pendekezo la awali la UNCTAD la $44 bilioni lilipunguzwa mpaka kufikia kwenye pendekezo la mfuko wa $ I bilioni tu.

Lile wazo la kuoanisha bei za bidhaa za awali na zile za viwandani lilikufa. Na tamaa yoyote ya mapendekezo ya IPC ilikufa pale Kamati ya muda iliyojumuisha Serikali mbalimbali ilipofanya mkutano wake wa mwisho mwaka 1980.

Licha ya kutofaulu huku, katika mwaka 1980, kikundi cha 77 kilipigania kuwepo kwa malengo yaliyozingatiwa upya. Walitaka ukuaji wa mwaka wa asilimia 7.5 katika Jumla ya Pato la Taifa la nchi za Ulimwengu wa Tatu katika miaka ya 1980. Walitaka fungu la nchi za Ulimwengu wa Tatu katika bidhaa za viwandani kwenye soko la dunia lifikilie asilimia 22 ifikapo mwaka 1990 na asilimia 30 ifikapo mwaka 2000, na kuhawilisha kwa $300 bilioni kwa uchache kwenda nchi za Ulimwengu wa Tatu katika miaka ya 1980.

Mawazo ya Waafrika yalilenga kwenye juhudi za kuyafanya yatulie katika kiwango fulani mapato yao kutoka usafirishaji wa bidhaa na katika kuoanisha bei za bidhaa za awali na zile za viwandani. Na kwa kweli Ulaya ilibaki kuwa ndiye mshirika mkubwa wa kibiashara wa Waafrika, juhudi za Waafrika zilielemea upande wa kufanya mapatano na EEC, Jumuiya ya Ulaya ya Uchumi.

Wakati EEC ilipoundwa, Ufaransa ulishikilia kwamba Jumuiya hiyo ipewe mahusiano maalum na yale makoloni yake yaliyokuwa karibu kuwa huru. Kwa hivyo taratibu ziliwekwa za kuziwezesha nchi zilizokuwa na mahusiano maalum na nchi wanachama wa EEC kuwa wanachama washiriki. Mikataba ya Yaounde ya mwaka 1963 na mwaka 1969 iliyakuza mahusiano haya maalum na kuyafanya yawe ya ushirika kati ya nchi za EEC na nchi 18 za Kiafrika zilizokuwa makoloni ya zamani ya Ufaransa, Ubeligiji na Italiano.

Mwaka 1975, Mkataba wa Yaounde ulifutwa na badala yake kuanzishwa mkataba wa mwanzo wa Lome kati ya nchi tisa za EEC na 46 za ACP. Ilipofika mwaka 1979, pale Lome ya Pili ilipotiwa sahihi, idadi ya nchi za ACP iliongezeka kuwa 58.

Ilipofika mwaka 1984 wakati Lome ya Tatu ilipokuwa ikizingatiwa, kulikuwa na nchi 10 za EEC na 64 za ACP ambazo kati yake 43 zilikuwa za Kiafrika. Kwa hivyo ule uhusiano wa EEC na ACP ambao ulianza katika kiini chake ikiwa kati ya Ufaransa na Afrika uliendelea na kuwa uhusiano kati ya Ulaya na Afrika.

Mikataba ya Lome ilianzisha taratibu (zikiwemo STABEX na baadaye MINEX) za kutuliza bei za bidhaa fulani na kuzikinga nchi za ACP na upungufu katika mapato yanayotokana na kusafirisha bidhaa hizi. Nchi za EEC, kwa upande wake, zilijaribu kuhakikisha kuwepo kwa mtiririko madhubuti wa bidhaa rahisi za awali

katika viwanda vyao na kwa kuzuia kuwepo kwa ushindani wa kibiashara, waweze kusalia na soko lao la bidhaa za matumizi na za uzalishaji mali. Mkataba wa Lome ulitoa haki za upendeleo kwa mashirika ya kimataifa ya EEC dhidi ya washindani wao wa Kimarekani na wa Kijapani lakini mkataba huo haujakubali matakwa ya ACP kwamba mashirika ya kimataifa yaliyokuwa imara katika nchi zao yadhibitiwe. Nchi za ACP zilikuwa na shaka nyingi kuhusu Mikataba ya Lome. Lakini kuwepo kwao na kuweza kwao walau kufanya kazi kulifanya liwe mbele sana ya zile juhudi zisofanikiwa za kufanya mapatano ya kuanzisha mpango mpya wa kimataifa wa uchumi.

## Ubeberu uliyofaulu

Ili kuweza kuufanyia tathmini uchumi wa ile miaka baina ya 1974 na 1985 ni muhimu kuangalia vipi mahusiano ya kiuchumi yaliyokuwa katika utendaji. Je, ile juhudi ya kuondoa ukoloni wa kiuchumi hazikufaulu, na ziliuwacha bila ya kuathirika ule mpango ulioanzishwa na Mkataba wa Atlantiki. Kampeni ya NIED na Mkataba wa Lome havikuwa na athari kubwa juu ya hali ya utegemezi uliotengamana na juhudi za Afrika za kujiingiza katika mfumo wa kibepari duniani. Hapakuwa na mageuzi ya mifumo ya kifedha na ya kibiashara yaliyokuwa na upendeleo kwa Ulimwengu wa Tatu. Licha ya nchi za Afrika kuishutumu IMF, bado zililazimika kufanya biashara nao kwa mujibu wa masharti ya Shirika hilo. Vile vile vikundi vidogo vya nchi za Magharibi viliendelea kudhibiti shughuli za kutafutia soko bidhaa za Afrika za kusafirisha.

Hapakuwa na mabadiliko muhimu kwenye mfumo wa biashara ya nchi za nje wa Afrika hata kama iliongezeka kutoka $ 4.9 bilioni mwaka 1960 na kufikilia $ 89.6 bilioni mwaka 1980. Ulaya Magharibi iliendelea kuwa ndiyo mshirika mkuu wa Afrika katika biashara. Takwimu za mwaka 1981 zinatoa kielelezo kizuri. Kati ya biashara ya jumla iliyofanywa kati ya Afrika na sehemu nyingine za dunia yenye thamani ya $ 106 bilioni, $ 71 bilioni zilitokana na biashara iliyofanywa na nchi za OECD. Biashara kati ya Afrika na nchi zilizoendelea zisizokuwa za Kiafrika ilifikilia $ 16 bilioni, na kati yake na kikundi cha Sovieti, biashara ilifikilia $ 1.3 bilioni tu; vifungu vingine vya biashara visivyoainishwa vilifikilia $ 18 bilioni. Biashara miongoni mwa nchi za Afrika wenyewe kwa wenyewe zilileta $ 6.7 bilioni za ziada iliyo ndogo kabisa.

Ndani ya Afrika uchumi ulibaki na sura ileile iliyokuwa nao wakati wa ukoloni. Muelekeo wake kuhusu soko la dunia uliendelea kuathiri vitega uchumi katika kilimo na katika uchimbaji madini. Hapajakuwa hasa na maendeleo yoyote yenye msingi wa kuwepo kwa orodha kamili wa nyenzo na wa kusarifiwa soko la nyumbani ili liweze kuendeleza uwiano wa sekta mbalimbali za ndani.

Huku zikilindwa na IPA mbalimbali, kampuni za kimataifa ziliendelea kuhodhi shughuli za uzalishaji na usambazaji ndani ya Afrika. Kwa mfano, ile kampuni ya kimataifa ya EEC ya awali kabisa iliyofanya biashara Afrika, Lonhro ya Uingereza, ilikuwa katika mwaka 1982 bado ikijipatia sehemu kubwa kabisa ya faida yake kutokana na shughuli zake kadha ndani ya Afrika. Nyingi miongoni mwa kampuni zake tanzu 800 zilikuwa zimo Afrika; Hako Malawi, Zimbabwe, Kenya, Zambia, Nigeria, Ghana, Mauritius, Uganda, Swaziland na Afrika Kusini. Kwa kweli Lonhro ilikuwa ndiyo mzalishaji chakula mmoja mkubwa kabisa katika Afrika ikilima na kufuga eneo lililozidi ekari 1.5 bilioni. Lonhro pia iliunda na kuuza vifaa, ilichimbua madini na kuendeleza shughuli za ujenzi.

Na kinyume na propaganda za serikali za Kiafrika dhidi ya kampuni za kimataifa zitavyompelekea mtu kutaraji, kampuni za kimataifa zilikuwa zikianiwa na kukaribishwa. Kwa mfano Lonhro ilikaribishwa tena rasmi huko Tanzania mwaka 1983, miaka mitano baada ya kufukuzwa kwa kuingilia katika vita vya uhuru wa Zimbabwe. Ililipwa fidia ya mali ya kampuni zake tanzu 18 zilizotaifishwa na kuombwa kuzitumia fedha hizo katika kufufua shughuli za uchumi zilizodhoofika pale zilipotaifishwa.

Ilipofika miaka ya mwanzo ya 1980, hata zile nchi za Kiafrika za Kimaksisti zilielemea upande wa uchumi wa mchanganyiko na kutafuta mahusiano ya karibu ya kiuchumi na nchi za Magharibi. Guinea na Congo Brazaville zilikuwa zinatafuta suluhu na nchi za Magharibi pamoja na kutafuta misaada na uwekaji vitega uchumi kutoka ulimwengu wa kibepari. Na ndani ya kipindi cha miaka kumi tangu kujitangaza kama ni dola ya Kimaksisti, Uhabeshi, Angola na Msumbiji walikuwa wanaupa mgongo mfumo wa Kisovieti wa maendeleo na kujiunga tena na nchi za Magharibi.

Kwa hivyo badala ya kuachana na nchi za Magharibi, Afrika ilisalia imefungika na mfumo wa kibepari wa dunia kutokana na vyombo vilevile ilivyojaribu kuvikwepa.



PICHA 26.3. *Njaa huko Ethiopia: Wakimbizi wapya katika Kambi ya Korem, 1985.*

Kuendelea kwa hali ya utegemezi katika Afrika na kukosekana kwa maendeleo ya kutosha. Licha ya kufaulu katika kuondoa moja kwa moja ukoloni wa kisiasa Afrika ilishindwa kujipatia maendeleo ya kiuchumi na kuondoa ukoloni wa kiuchumi. Hali ya kisasa iliyoweza kupatikana haikuwa ya kuridhisha na ilikuwa katika sakara; bandari na viwanja vya ndege vichache, miji duni yenye rashio rashio ya vistawishi vya kisasa, viwanda vichache, vijinjia vya kisasa na kadhalika, hivi ndivyo vilivyokuwepo, lakini kiini hasa cha hali ya kisasa hakikuwepo, kwa vile Jumla ya Pato la Taifa iliyozalisha vishawishi hivi haikuwa na vyombo vya kuidumisha katika Afrika. Siyo tu Afrika ilishindwa kuleta hali imara ya kisasa, imepoteza hata uwezo wake wa kijadi wa kujilisha yenyewe. Ilipofika mwaka 1984, lilikuwa ndiyo bara pekee lililoshindwa kujilisha. Njaa ama ilizagaa au kutishia kutokea katika maeneo makubwa ya Afrika. Sura iliyotawala ni ya bara ambalo maisha hayakuwa na ufanisi, hali hii ikiashiriwa na ile hali ya mkimbizi aliyedhofu na kibakuli cha ombaomba mkononi.

Katika kipindi hiki kinachozingatiwa, ilikuwa ni mtindo wa Waafika kuzilaumu nchi za Magharibi kwa shida zao zote, hasa kule kukataa kwa nchi za Magharibi kubadilisha ile hali ya kutowepo usawa katika mahusiano iliyoanzishwa chini ya ukoloni. Lakini mtizamo huu ulikuwa ni dhihirisho kubwa kabisa la dhamana ya Waafrika. Kwa kweli huo uhusiano unaozungumzwa na hali ya Afrika kukosa maendeleo si mambo ambayo hayawezi kubadilika. Maendeleo yaliweza kupatikana bila ya kujipapatua na au kubadilisha ile miundo ya msingi iliyoufanya ubepari wa Magharibi utawale (kama inavyoonekana Singapore, Taiwan, Hong Kong, Korea ya Kusini na nchi mpya za Ulimwengu wa Tatu zenye Viwanda, NIC) na pia maendeleo yaliwezekana hata kwa kukata mahusiano na mfumo wa kibepari (kama ilivyo Uchina baada ya mwaka 1949). Kwa hivyo kwa nini Afrika ilishindwa? Kwa nini hata nchi moja ya Kiafrika haikuweza kuwa NIC?

Baadhi ya nchi hizi za Kiafrika zilipenda kudai kwamba ukosefu wa rasilimali ya fedha ulikuwa ndiyo kikwazo; wengine walidai kwamba hawakuwa na nyenzo au kwamba hawana idadi ya watu wa kutosha kuwezesha soko kubwa la ndani kuendeleza maendeleo. Na iwe kweli kwamba madai haya yanakubalika kwa nchi maskini kabisa miongoni mwa madola madogo mno ya Afrika, lakini kulikuwa na nchi nyingine ambazo, kwa nchi hizo, sababu kama hizi hazina msingi. Bila shaka kwa mabilioni yake kutoka kwenye mafuta, idadi ya watu wake milioni 100 wakiwemo wale wenye ujuzi wa kiufundi, maeneo yake makubwa na uwezekano

wake kwa upande wa madini na kilimo, Nigeria ilikuwa na zana za kuipatia maendeleo mnamo robo karne ya kwanza ya uhuru wake. Sababu ya kutofaulu Nigeria zinaweza kutoa mwanga kuonesha kwa nini Afrika haikuweza kufanikiwa.

Kushindwa kwa Nigeria kukusanya na kuwekea vitega uchumi pato lake kubwa kutokana na mafuta kwa kiwango kikubwa kunatokana na asili, itikadi na matakwa ya tabaka lake tawala. Sehemu kubwa ya wakuu wao ilikuwa ni ya warasimu waandamizi waliotokana na wale ambao hawakuwa wazalishaji miongoni mwa wanatabaka la kati wa zama za ukoloni. Walikuwa hawana uzoefu wa shughuli za uzalishaji na pia walizichukia tume na hatari za shughuli hizi. Kwa upande mwingine walikuwa na uchu mkubwa wa matumizi ya anasa na walielekeza pato lote lililokuwepo katika matumizi hayo badala ya kuyategea uchumi kwenye shughuli za uzalishaji.

Tamko walilokuwa wakilitumia ni 'kujipatia kipande cha keki ya taifa'. Kama keki ikiongezeka, kama ilivyokuwa ikiongezeka, kutokana na kukusanya kodi ambayo ilipatikana pasi na wao kukukuruka, ilikuwa vyema zaidi. Na kama kiwango cha kodi kilishuka, basi nguvu zote zilitumika katika kukiwania vikali hicho kilichobaki. Juhudi za shingo upande za baadhi ya wakuu wa Kinigeria zilishindwa kuzuia mtiririko huu. Udhibiti wa fedha za kigeni, uongezaji wa thamani ya serufi, kuwepo kwa kodi za uagiziaji na ushuru wa forodha wenye mazonge, haya yote, badala ya kuzuwia mtiririko wa fedha iliongeza rushwa tu. Uendelezaji wa viwanda kwa njia ya kuanzisha karakana za kufidia uagiziaji na utengenezaji wa mazao hakukuwezesha kupatikana kwa akiba ya fedha za kigeni kama ilivyotarajiwa, kwa vile hizo karakana zenyewe ilibidi kuagizwa kutoka nchi za nje na kutunzwa kwa kutumia vipuri na wataalamu kutoka nje. Kutokana na msamaha wa ushuru, kusafirisha kwa mgao wa faida, uagiziaji mkubwa wa bidhaa za matumizi na ulaji wa rushwa wa warasimu waliokuwa wakihifadhi fedha zao kwenye mabenki ya ng'ambo, kutokana na haya yote mtiririko wa fedha za rasilimali ulikuwa kutoka Nigeria kwenda nchi za Magharibi. Sababu muhimu ya Nigeria kukosa ufanisi ilitokana na ile nadharia kwamba, kimsingi, maendeleo ni maendeleo kwenye matumizi. Hili lilikuwa jambo la kukubalika kwa nchi za Magharibi, lakini Wanigeria walilikumbatia kwa hiari yao na kulifanya ndiyo maisha yao. Kule kukataa kwa makusudi kwa watukufu wa Kiafrika kushughulikia maendeleo kwa njia ya uzalishaji kulishawishiwa na dhana za kiustawi wa jamii kutoka vyama vya kidemokrasia ya ujamaa kama Chama cha Wafanyakazi, yaani Labour Party, cha Uingereza

ambavyo vilishughulika zaidi na usambazaji, huku wakipuuza moja kwa moja shughuli za uzalishaji. Hali kama hii inaeleweka katika jamii zilizokwishatatua tatizo la uzalishaji. Lakini ustawi wa jamii wa kiusambazaji ulikuwa haufai kwa uchumi wa Afrika ambao tayari ulikuwa na uchache wa uzalishaji. Juu ya hivi, utaratibu huu ulikumbatiwa na viongozi waanzilishi wa Kiafrika ambao walikulia katika mazingira ya kidemokrasia ya kiujamaa ya vyuo vikuu vya Kimagharibi.

Suala moja bado linangoja kushughulikiwa. Ikiwa ustawi wa jamii wa kiusambazaji haukuleta ustawi wa jamii bali umeleta badala yake ustawi wa ufukara, kwa nini uongozi wa Afrika haukutupia mbali mpango huo na badala yake kuchukua jukumu la msingi la kushughulikia uzalishaji? Kwa nini haukutaka kuzipa shughuli za uzalishaji kipaumbele katika kulikabili kwao suala la maendeleo? Kasoro hii, lazima ikumbukwe, ilikuwa ndiyo alama iliyojitokeza katika misimamo yote, ikiwa ya kibepari, ya ujamaa ya Kiafrika au ya Kimaksisti.

Miongoni mwa wakuu wa Kiafrika, kabisa hapakuwa na raghba ya kuendeleza shughuli za uzalishaji. Chambilecho wafanyabiashara wengi wa Kinigeria: 'kwa nini uviunde mwenyewe ikiwa unaweza kuvinunua?' Na wale Waafrika waliokuwa hawana kodi kutokana na madini ya kuwawezesha kununua bidhaa na ambao hubweka kutaka misaada wao wangeliweza kusema: 'kwa nini tuunde ikiwa tunaweza kuomba au kukopa?' Kwa hivyo ilijengeka tabia ya utegemezi iliyowafanya Waafrika washindwe kujipatia yale maendeleo waliodai wanayatafuta.

Lakini kwa nini hii tabia ya utegemezi liendelea kubaki licha ya kuwa ni pingamizi katika kulifikia lengo lililotangazwa? Katika kipindi hiki chote kinachozingatiwa hapakuwa na ukosefu wa kodi na misaada minono kutoka mfumo wa ubepari wa dunia hata kuwafanya wakuu wa Kiafrika walazimike kuzalisha badala ya kununua, kukopa au kuomba. Na madam mipango iliyopo ilikidhi matarajio ya wananchi kwa kulipia kwa kiasi fulani bidhaa za kisasa na kuendelea kutoa tamaa kwamba vinono zaidi karibu lvitapatikana wanakufu hawakuhisi msukumo wa kuwafanya wabadilishe mwendo wao na kujitumbukiza kwenye pirika za kukusanya rasilmali na kuweka vitega uchumi katika nyanja za uzalishaji zinazowezesha kupatikana maendeleo yasiyokuwa ya utegemezi.

Kwa vile walikwisha lemazwa na hali ya utegemezi uliyowanusuru na shida kubwa, hawakuwa na hamu ya kuzitumia fursa zao za kujipatia maendeleo ndani ya mfumo wa kibepari wa dunia (kama nchi za Ulimwengu wa Tatu za NIC zilivyokuwa zikifanya); na pia hawakuwa katika shida ya kubwa kuwafanya wajinasue kutoka

kwenye mfumo huo na kusimama kwa miguu yao wenyewe (kama alivyofanya Mchina); na vile vile hawakuwa na motisha ya kisiasa ya kutaka kujinusuru na kuvamiwa na nchi ya kigeni ambayo ingaliwahamasisha kuendeleza shughuli za uzalishaji viwandani (kama ilivyotokea Japani na katika Muungano wa Kisovieti) inaweza kusemwa kwamba ikiwa kushindwa kwa Afrika kujiondolea ukoloni wa kiuchumi au kujipatia maendeleo kulitokana na mahusiano ya utegemezi waliyoyarithi, yaani kushindwa kwa Waafrika kuyapanga na kuyabadilisha mahusiano yao kwa kuzipa umuhimu nyenzo zao wenyewe za uzalishaji mwishowe kulitokana na ile tabia ya utegemezi ambayo ilitia fora katika uongozi wa Kiafrika.

## Kuelekea kwenye ubepari uliovuliwa ukabila

Ule uwiano kati ya ukabila wa aina ya kizamani na ubepari huko Afrika Kusini huenda ukawa ukingoni mwa kuvunjika. Lakini ingawa kuvunjika kwa uwiano huenda ukaumiza na mpaka kuiua siasa ya ubaguzi, ubepari huko Afrika Kusini huenda ukaendelea bila ya kuathirika baada ya kumalizika kwa mapambano.

Ikiwa kwa mfano mtu ataambiwa achague tukio la kuvutia kabisa Afrika katika kipindi cha kati cha miaka ya 1980, mtu huyo atashawishiwa kuchagua ile hasira ya vijana wa Afrika Kusini wakiandamana kupinga siasa ya ubaguzi. Je yale yalikuwa mapinduzi katika hali ya uchanga? Wale wanaotazama upande mwema wameona mshabaha kati ya tukio hili na ama mapinduzi ya Uhabeshi ya mwaka 1974 au yale ya Iran ya mwaka 1974 kwa vile matukio yote haya mawili yalianza kwa maandamano ya mabarabarani. Kila mojawapo kati ya Iran na Uhabeshi kabla ya mapinduzi ilikuwa ni muungano kati ya umwinyi wa ndani ya nchi na ubepari wa kimataifa. Serikali mbili hizi, yaani za Uhabeshi na Iran, zilidumu kwa maelfu ya miaka na juu ya hivyo ziliweza kupinduliwa baada ya miezi michache tu ya maandamano. Na siasa ya ubaguzi ingeweza kuanguka tu kutokana na mapambano yaliyoandaliwa ndani ya nchi.

Kwa upande wa vikwazo vya uchumi vya nchi za Magharibi, lazima tutafautishe kati ya vikwazo vya kielelezo na vikwazo kama kifaa. Kususia kwa njia ya kielelezo ni kama kupitisha hukumu ya kimaadili, lakini kususia kwa kutumia vikwazo kama ni kifaa ni kutumia zana za kisiasa. Vikwazo vya Kimagharibi vinaweza kusaidia serikali ikiwa na upana wa mawazo lakini vikwazo hivi havitoweza kuleta hali ya 'kila mtu kuwa na haki ya kupiga kura moja'. Mapambano ya silaha ya ndani ya nchi lazima yawe ndiyo kiini cha mapinduzi. Lakini kuna jambo gani linalotokea

katika ule uwiano kati ya ubepari na siasa ya ubaguzi? Kwa nini uwiano huu sasa umo katika mvutano? Kuna sababu kadha. Kwanza uwezo wa watu weusi wa kununua bidhaa sasa uko tayari kuongezeka ikiwa mfumo huu utakuwa wa haki zaidi kwa upande wa kiuchumi. Pili, ujuzi wa watu weusi umefikilia viwango vipya na unaweza kuufanya uzalishaji uwe na ufanisi zaidi. Ubepari wa nchi za Magharibi utakuwa tayari kutumia ujuzi wa watu weusi. Tatu, mfumo bora wa elimu na wa mafunzo unaweza kuigeuza Afrika Kusini mara moja na kuifanya iwe kama ndiyo Australia ya watu weusi, tajiri na yenye maendeleo makubwa upande wa viwanda. Ubepari wa nchi za Magharibi unaweza kuhifadhi maslaha yao. Upinzani dhidi ya siasa ya ubaguzi unaweza kuleta machafuko ambayo yataathiri ubepari. Ukandamizi unaendelea kushamiri huko Afrika Kusini na kutenganisha vikundi vingi vyenye maoni muhimu katika ulimwengu wa Magharibi ambavyo vinaanza kuwekea shinikizo makampuni ya biashara na maduka ya msururu. Taasisi nyingi za Kimagharibi zimehama Afrika Kusini, miongoni mwao ikiwemo Benki ya Barclays, IBM na Coca-Cola ni miongoni mwa taasisi za kibepari zilizoondoka. Ama sasa hivi au baadaye ubepari utabidi kufunga virago na kuvunja mahusiano na siasa ya ubaguzi.

Lakini nini mustakabali wa ubepari Afrika Kusini pale siasa ya ubaguzi wa rangi itavyokuwa imeshindwa? Ushindi dhidi ya siasa ya ubaguzi wa rangi si lazima kumaanisha ushindi dhidi ya ubepari. Kwanza lazima tukumbuke kwamba kuna kiwango cha maendeleo ya ubepari ambacho, kikishafikiwa, kinaufanya ubepari karibu kutoweza kurejea nyuma. Karl Marx alidhania kwamba maendeleo ya kibepari yakifikia kileleni, basi matokeo ni mapinduzi ya kijamaa. Wafuasi wa Marx wa baadaye waliifanyia mabadiliko nadharia hii ieleze kwamba mnyororo wa ubepari unakatika kwenye kile kiungo chake kilicho dhaifu kabisa. Lakini jee vipi kuhusu vile viungo vilivyo imara? Lini vitakatika? Lini kutakuwa na mapinduzi ya kikomunisti Marekani? Kama inavyonekana kuwa jambo hili haliwezekani kwanza ni kwa sababu ongezeko la tabaka la wafanyakazi halikutokezea, kama ilivyotabiriwa na Marx. Lililotokezea ni ongezeko linaloendelea kuzidi la tabaka la kibepari. La pili kule kutabiri kwa Marx kuhusu kuongezeka kwa shida hakujatokezea, isipokuwa miongoni mwa vikundi vya wachache vya kikabila. Wafanyakazi weupe hawakuzidi umaskini bali walizidi kutajirika. Wanamiliki magari na TV. Kwa hivyo kwa nini mfumo wa kibepari upinduliwe? Pia tusisahau kwamba katika nchi za Magharibi hisia za kitabaka hazikuweza kuzishinda hisia za kizalendo.

Kinyume na hayo, hisia dhidi ya ukoministi zinanasibishwa na uzalendo huko Marekani miongoni mwa wafanyakazi. Marx aliudharau uwezo wa ubepari wa kushirikisha, kugeuza na kupotosha wengi iii waunge mkono ubepari. Ubepari unaweza kujipatia marafiki wenye nguvu miongoni mwa haohao walio chini. Lakini je, Afrika Kusini imefikia kiwango cha ubepari usioweza kurejea nyuma, kiwango ambacho nchi nyingi za Magharibi zimefikia. Kwa hali ilivyo, ni bado. Na kwa hivyo chini ya utawala wa watu weusi, Afrika Kusini ina uwezo wa kati na kati, yaani hamsini kwa hamsini, ama kuendelea katika mfumo wa kibepari (lakini bila ya ukabila) au, bora zaidi, kufuata njia ya kujipatia maendeleo kwa kupitia kwenye ujamaa.

## Hitimisho

Tumeona kwamba uondoaji wa ukoloni wa kisiasa katika Afrika haukuweza kuziua nguvu za ubepari wa nchi za Magharibi kwa vile haukuandamana na uondoaji wa ukoloni wa kiuchumi.

Kwa mtazamo wa Kiafrika, ubepari wa kimataifa daima umekuwa na vituo viwili. Katika kipindi cha ukoloni, vituo pacha vilikuwa hasa London na Paris. Lakini katika kipindi kilichofuatia kumalizika kwa ukoloni, ambacho ndicho kilichozungumziwa katika juzuu hii, hadhi ya London ilipungua na ile ya Washington kuongezeka na Paris kuendelea na uongozi wake kwa sura mpya. Kituo pacha cha mahusiano kati ya Afrika na ubepari wa nchi za Magharibi kilihamia Washington na Paris. Lakini kuna dalili kwamba Jumuiya ya Ulaya kwa jumla ndiyo itayorithi joho la Ufaransa katika Afrika. Ikiwa mtindo huu utaendelea, basi, baada ya muda, kituo pacha cha uhusiano wa Afrika na ubepari wa Magharibi kitakuwa Washington na Brussels. Mapambano ya Afrika dhidi ya kukaliwa ardhi yake yanafaulu, mapambano ya bara hili dhidi ya kunyonywa kiuchumi hata bado kuanza. Ama kwa upande wa vita vya Afrika dhidi ya siasa ya ubaguzi na ukabila uliyotia mizizi michuano mikubwa ya mwisho yanaendelea Afrika Kusini, kuna ishara kwamba baada ya muda ubepari wa Kimagharibi utajirekebisha na kumalizika kwa siasa za ubaguzi pamoja na ukabila unaoendeshwa kwa bayana huko Afrika Kusini. Kwa kweli, siasa ya ubaguzi (kama utumwa katika karne ya kumi na tisa) huenda ikawa tayari inaathiri umadhubuti wa ubepari unaoendelezwa kwa mfumo maalum. Ubepari wa Magharibi utaendelea hata baada ya mshituko kutokana na

kumalizika kwa siasa ya ubaguzi wa rangi, kwani sifa kubwa ya ubepari kwa upande mmoja imo katika ule uwezo wake wa kuvumbua njia mpya za udhibiti. Pale Afrika itaposherehekea kumalizika kwa siasa ya ubaguzi kama ilivyosherehekea hapo kale kumalizika kwa biashara ya utumwa iliyopitia Atlantiki au hata kumalizika kwa ukoloni, itafanya vyema kuweka tahadhari dhidi ya sura mpya ya ubepari katika enzi itayofuatia kumalizika kwa siasa ya ubaguzi.

# 27

# Afrika na Nchi za Kisoshalisti

Uhusiano wa Afrika na nchi za kishoshalisti unarudi nyuma hadi kipindi ambapo, mara baada ya mapinduzi ya Bolsheviki ya 1917, Lenin alipoahidi msaada wa dola jipya la Sovieti kwa watu wote waliokuwa chini ya ukoloni. Tangu hapo nchi zote za Kisoshalisti - Umoja wa Urusi na rafiki zake pamoja na Jamhuri Watu wa China – wametoa misaada ya aina mbalimbali kwa nchi za Afrika, kabla na baada ya uhuru wao. Sera za mambo ya nje za nchi za Kisoshalisti, kama ilivyo kwa madola mengine yenye nguvu, zinaongozwa na misingi miwili ambayo inatangamana: wa kiitikadi, ambapo jumuiya ya Kisovieti na Jamhuri ya Watu wa China wana wajibu wa kusaidia nchi zinazoelekea kufuata itikadi ya Marx-Lenin; na wa kimkakati, ambapo hulinda manufaa yao ya kitaifa. Inawabidi Wakomunisti kuunga mkono mapambano ya uhuru ili kuharakisha mapinduzi dhidi ya ukoloni, ambayo ni sehemu ya mapinduzi ya ulimwengu.

Kuongezeka kwa umuhimu wa Afrika katika mambo ya dunia kulizifanya nchi za kisoshalisti kukuza uhusiano wao na nchi za bara hilo. Uhusiano huo umeathiri matukio katika nchi za Afrika kwa njia mbalimbali.

Kwa jumla, sera za nchi za kisoshalisti kuhusiana na Afrika zinaweza kugawanywa katika vipindi vinne.

(1) tangu 1917 hadi 1945 uhusiano wao haukuwa wa moja kwa moja na ulitegemea vyama vya kikomunisti vya Ulaya na viongozi wanaharakati wa umoja wa Afrika waliokuwa Afrika, Indies ya Magharibi (Karibiani) na Marekani;

(2) tangu 1945 hadi 1960, wakitiwa moyo na kudhoofika kwa nguvu ya ukoloni na kuibuka kwa utaifa baada ya Vita vya Pili vya Dunia, nchi za kisoshalisti

ziliunga mkono wazi au kwa kificho vuguvugu za ukombozi wa kitaifa na nchi za Afrika zilizopata uhuru karibuni;

(3) tangu 1960 hadi 1975 kulikuwa na upungufu wa kujishughulisha moja kwa moja kwa nchi za kisoshalisti, hasa Umoja wa Urusi, badala yake walipendelea kutumia njia za kidiplomasia;

(4) tangu 1975, baada ya kumalizika kwa vita vya Vietnam, nchi za kisoshalisti ziliongeza uhusiano wake, kwa mfano kule Angola na nchi za pembe ya Afrika

## Umoja wa Sovieti na Afrika: Uhusiano baina ya Afrika na nchi za kisoshalisti tangu 1935

Wakiandika wakati ambapo ukoloni haukuwa umeendelea sana na ambapo Afrika haikujulikana sana Ulaya, Karl Mark na Friedrich Engels hawakurejea sana kuhusu Afrika kwenye kazi zao. Lenin, hata hivyo alijadili masuala ya Afrika mara kwa mara katika vitabu vyake juu ya ubeberu na suala la utaifa na ukoloni.[1] Kwa hiyo, kwake, Afrika, kutokana na hali yake mahsusi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, ingeweza kufikia mfumo wa Sovieti, na kuingia kwenye ukomunisti bila kupitia hatua ya ubepari.[2] Vuguvugu za Afrika dhidi ya ukoloni zilitiwa moyo kupambana na wakoloni ili kupanua mapambano dhidi ya ubepari. Kwa hiyo Umoja wa nchi za kisoshalisti (Comitern) zilijitahidi kushirikiana kindugu na vyama vya kitaifa, kama vile Ushirikiano wa Kitaifa wa Afrika ya Magharibi iliyo chini ya Waingereza [*National Congress of British West Africa*] (NCBWA)], Chama cha Wakikuyu wa Kati [*Kikuyu Central Association*] au Ushirikiano wa Kitaifa wa Afrika [*African National Congress]* (ANC), hata kama, kwa mtazamo wao, uongozi wa vuguvugu hizi haukuwa mikononi mwa tabaka la wafanyakazi, ambalo kwa vyovyote lilikuwa na watu wachache Afrika ninamo miaka ya 1930, lakini ulikuwa wa mabwanyenye wa kitaifa waliopenda maendeleo. Baadhi ya vyama vilivyohusiana na Umoja wa nchi za kisoshalisti ulijishughulisha sana. Hivyo ni pamoja na Umoja wa Wafanyakazi wa Kimataifa wa Kikomunisti [*Red International Labour Union*] (RILU), Umoja wa Mstari wa Mbele kutoka Chini [*United*

[1] V.I. Lenin, 1966; 1965, juz. 31, uk. 150; na 1920 (tafsiri iliyochapishwa 1950), kur. 360-2

[2] V.I. Lenin, 1965, kur. 153-4

*Front From Below*] (UFFB) na Kamati ya Umoja wa Kimataifa wa Wafanyakazi wa Kinegro [*Internetional Trade Union Committee of Negro Workers* (ITCUNW)[3] . Kati ya Waafrika wa kwanza kushirikina na baadhi ya vyama hivi ni Jomo Kenyatta, ambaye alizuru Umoja wa Urusi mwaka 1929, 1932 na 1934.[4] Alikuwa akiandikiana na ITUC-NW.

Wanademokrasia wa Afrika na Matapo ya Kikomunisti ya Kimataifa. Umoja wa nchi za kisoshalisti wakati mwingine ulipata tabu ya kuhusiana na wapigania uhuru wa Kiafrika katika miaka ya 1920 na 1930, na hivyo uongozi wa kisovieti (Kremlin) ulitumia Waafrika wa Kimarekani na Wanaumoja wa Afrika walio Karibiani pamoja na vyama vya kikomunisti vya nchi za Ulaya kueneza mawazo yao ya kisoshalisti. Huko, mwananchi wa Karebeani, Sylvester Williams, alimwathiri M. Garvey, ambaye alikuwa na nafasi muhimu kati ya wapigania uhuru wa mwanzo wa Afrika, ambapo Mwafrika wa Kimarekani, W.E.B. DuBois, na mwananchi Karibiani, G. Padmore, waliwaathiri wasoshalisti wengi wa Afrika akiwemo Kwame Nkrumah.[5]

Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa, kutokana na umuhimu wake katika maisha ya kisiasa ya Ufaransa, kilikuwa na umuhimu mkubwa katika madola ya kikoloni ya Ufaransa. Oktoba 1921, Kamati ya Utendaji ya Mkutano wa Tatu wa Kimataifa iliutaka Uongozi wa Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa kuunda kwa haraka Baraza la Kikoloni la Kikomunisti kutia moyo shughuli za kupinga ukoloni Afrika na kwingineko.

Mkakati wa Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa ulikuwa ni kuanzisha propaganda ya kiharakati na himilivu dhidi ya vita iliyoelekezwa kwa askari wa zamani na majeruhi wa vita na kwenye mikusanyiko ya majeshi ya kikoloni. Kulikuwa pia na miongozo mahsusi ya shughuli za kuendelezwa Kameruni, Togo, Afrika ya Kifaransa ya Ikweta, Madagaska na Afrika Magharibi ya Kifaransa. Hicho ndicho kilichokuwa chanzo cha kuwa na uchunguzi wa hali ya kijiografia, demografia, kimbari, kiuchumi, kisiasa na kijamii katika makoloni yote. Madhumuni ya uchunguzi huu yalikuwa ni kuwawezesha viongozi wa Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa "kuunda mpango wa kimkakati wa utekelezaji na kuangalia shughuli za kiutendaji

[3] Taarifa ya Joe, 100,20,1930, SLUT, MOMU, sand. Faili 373, faili dogo 51:3, iliyonukuliwa kwenye T. Wilson 1974; F. Meli, n.d

[4] J.M. Brown, 1972, uk. 268

[5] I.Geiss; na A. Langley, 1973

ambazo uongozi huo itabidi uzifanye kushawishi umma wa wenyeji kuunga mkono jitihada za Wakomunisti na wakati huohuo kupambana na ubepari na ubeberu."[6]

Novemba 1922, makala yenye kichwa, "Mbari inayoamka," ya Izvestia ilieleza kwamba "wajumbe weusi walishiriki kwenye Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Kikomunisti". Gazeti liliongeza kuwa "ukweli huu unaoonekana kuwa si wa maana kwetu ni mwanzo wa mwelekeo muhimu wa kihistoria, na ambao unaelekea kuwa na wajibu mkubwa katika mapambano mazima dhidi ya ubeberu ulimwenguni."[7]

Ushiriki wa Waafrika katika shughuli za kikomunisti za kimataifa uliongezeka haraka. Vikundi vilivyopinga ukoloni viliundwa, kama vile Shirikisho dhidi ya Ubeberu na kwa ajili ya Uhuru wa Kitaifa, ambalo lilifadhiliwa na Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa na ambalo wanachama wake walikuwa ni pamoja na Waafrika kama Chadli Ben Mustapha (Tunisia), Gumede (Afrika Kusini), Tiemoko Garang Kouyate na Lamine Senghor (Afrika Magharibi).

Hivyo miaka miwili kabla ya msukosuko mkuu wa kiuchumi wa 1929, misingi ya kiitikadi na kimkakati ya shughuli za kupambana na ukoloni ilikwishawekwa. Umoja wa Kisovieti na vyama marafiki vilikuwa mstari wa mbele katika mafunzo ya kisiasa na kiitikadi ya kada wa shughuli za ukombozi. Shule ya Stalin ilianzishwa Mosko kuwafunza makada wa KiMarx. Athari za msukosuko wa kiuchumi zilizoitingisha dunia zilifanya shughuli za kupambana na ukoloni ziwe rahisi zaidi. Hata hivyo, kuibuka kwa ufashisti huko Ulaya kulisababisha suala la ukoloni kuwa na umuhimu mdogo kwa muda kwa Vyama vya Kikomunisti, hali ambayo iliwakatisha tamaa baadhi ya Wanaumoja wa Afrika kama G. Padmore ambaye aliona mabadiliko hayo kuwa na madhara kwa shughuli za Waafrika.[8]

Baada ya vita, vyama vya kikomunisti vya Ulaya viliendelea kuwa na nafasi muhimu katika Afrika inayozungumza Kifaransa, lakini vikiwa na umuhimu mdogo kwa Afrika inayozungumza Kiingereza ambako Chama cha Kikomunisti cha Uingereza, tofauti na kile cha Ufaransa, hakikuunda ushirikiano wenye nguvu. Chama cha Uingereza kilikuwa kidogo hata hivyo.

Wanaharakati wachache wa Kiafrika waliokuwa wakisoma Uingereza walihusiana na viongozi wa vyama vya kikomunisti ambao waliathiri mawazo yao ya kisiasa. Waafrika hao ni K. Nkrumah wa Ghana, F. Macauly wa Nigeria,

[6] Nayarka za Jamhuri ya Senegali, 1923
[7] Nyaraka za Jamhuri ya Senegali, 1922
[8] G.Padmore, 1935, uk. 320

pamoja na Jomo Kenyatta wa Kenya, F.F. Small wa Gambia na I.K. Musazi wa Uganda. Baadhi yao, kama S. Mulumba wa Chama cha Bataka cha Uganda, alitafuta msaada wa Umoja wa Sovieti, kupitia kwa Chama cha Kikomunisti cha Uingereza, ili kupata uhuru wa kisiasa wa Afrika Mashariki.[9]

Fikra za Marx zilikuwa na nguvu na kupata mashiko katika sehemu nyingine za Afrika. Umoja wa Wanafunzi wa Kiafrika waliokuwa Ufaransa [*Fédération des étudiants d'Afrique noire en France*] (FEANF) ulikuwa nao miongoni mwake, na hasa kati ya makada wake, wengi wao walifuata fikra za Marx, kama Osende Afana wa Kameruni, mwandishi wa kitabu muhimu juu ya uchumi wa Afrika Magharibi. Kupitia kwenye vikundi vya majadiliano vya kikomunisti, vilivyoanzishwa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia au mara baada, na Ushirika Mkuu wa Wafanyakazi, makada wengi wa vyama vya wafanyakazi walizipokea fikra za Marx na mbinu za kuhamasisha umma. Katika nchi za Afrika zinazozungumza Kireno, wasomi wa fikra za Marx waliojifunza Ureno kupitia ushirikiano wao na Chama cha Kikomunisti, kama Agostino Neto na Amilcar Cabral, walianzisha MPLA huko Angola na PAIGC huko Guinea na Ras ya Verde.

Hata hivyo, katika upeo wa vuguvugu la uhuru, mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960, nafasi ya ukomunisti haikuwa wazi. Kwa upande mmoja, kulikuwa na vyama vichache sana vilivyoeleza waziwazi kushikamana kwao na fikra za Marx: na pale vilipokuwapo, hasa Afrika Kusini, Algeria, Misri, Senegali na Sudani, athari yao ilikwamishwa na sababu nyingi, kama vile udhaifu wa tabaka la wafanyakazi, vikwazo vinavyotokana na itikadi za jadi na upinzani wa kidini. Lakini kwa upande mwingine, nchi za kisoshalisti, na hasa Umoja wa Urusi, zilipata heshima kubwa.

## Umoja wa Sovieti, Ulaya Mashariki na Uondoaji wa Ukoloni Afrika

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, ambapo mamlaka ya kikoloni yaliibuka yakiwa yamedhoofika, ndipo wasoshalisti walianza kuwa na raghba na Afrika. Kipindi kati ya 1945 na 1960 kilikuwa ni cha upinzani mkubwa dhidi ya ukoloni. Wasoshalisti walikuwa tayari kutoa msaada kwa shughuli za kuupinga ukoloni ili kumdhoofisha adui yao wa pamoja: ubeberu wa kimataita.[10]

[9] J. Mulira, 1974, uk. 44

[10] Byakov na wenzake, 1981, uk. 143

Hata hivyo Afrika ya kikoloni iliendelea kuwa ni tatizo la kinadharia kwa wanazuoni wa kisoshalisti. Nani angechukuliwa kuwa ataongoza mapinduzi Afrika, na nguvu za kuuondoa ubeberu? Mwaka 1947, mwanataaluma E.M. Zhukov alilaumu wajibu waliojichukulia mabwanyenye wa Afrika katika mapambano ya uhuru.[11] Lakini Profesa mwingine wa Kisovieti; mtaalamu wa masuala ya Afrika I.I. Potekhin, alisema mnamo 1950 kwamba katika nchi nyingi za Afrika ya tropiki na ya kusini wajibu wa kuongoza katika mapambano ya uhuru wa kitaifa umo mikononi mwa mabwanyenye na wasomi wa kitaifa,[12] hivyo kukiri kutokuwapo kwa chama cha kikomunisti chenye umuhimu wowote na udhaifu wa tabaka la wafanyakazi katika makoloni ya Kiafrika.

Kwa kweli, tangu 1950 hadi nchi za Afrika zilipopata uhuru, sera za nchi za kisoshalisti na China zilielekea kuzingatia zaidi mawazo ya udhaifu wa tabaka la wafanyakazi kuliko lile la awali. Hapana shaka wasoshalisti walijitoa kwa dhati kuusaidia umoja wa vyama vya wafanyakazi, lakini wasoshalisti walitafuta kujenga uhusiano na vyama vilivyopinga ukoloni kupitia vyama vilivyokuwa chini yao, kama vile Chama cha Amani Duniani, Umoja wa Urafiki wa Watu wa Afrika na Asia na Umoja wa Kimataifa wa Wanafunzi, kutaja vichache. Walitegemea pia vyama vya kikomunisti vya wenyeji pale vilipokuwapo.

Baada ya kutambua njia ambazo, kama tulivyoona, zingetumika katika shughuli za kupingana na ukoloni, nchi za kisoshalisti zilianza programu ya kuunga mkono kwa dhati shughuli za kuondosha ukoloni kwa kudumu kwa msaada wa vifaa na kidiplomasia. Msaada huo ulitolewa kwa misingi ya fikra za Marx na Lenin kwamba wasoshalisti wana wajibu wa kuwasaidia wale wanaotaka kuondokana na ukoloni. Chama cha CPP cha Ghana kilikuwa kati ya vyama vya kwanza kunufaika na msaada wa USSR, kikifuatiwa na Mau Mau, Jomo Kenyatta na chama chake (KANU), Baraza la Kitaifa la Nigeria na Kameruni [*National Council of Nigeria and the Cameroons*] (NCNC). Chama cha Kongresi cha Uganda [*Uganda National Congress*], PAI na UPC vya Kameruni, Chama cha Kongresi cha Madagaska [*Independence Congress Party*], FLN cha Algeria na Vyama vya aina hiyo vya uhuru, kama vile FRELIMO cha Msumbiji, MPLA cha Angola, na

[11] E.M. Zhukov, 1947

[12] Taz. Soviet Ethnography na. 1, 1950 V.I Popov na wenzake, 1975, kur. 21-4; V.I Lenin, 1965, juz. 28, uk. 125; Pravda, 17 Machi 1957, uk. 1; Tass 1 Februari na 3 Februari 1960; na D. Skvirsky, 1967, kur. 194

ZAPU na ZANU vya Zimbabwe. Hivi karibuni chama cha ANC cha Afrika Kusini na SWAPO cha Namibia vimepata msaada kama huo.

Mswada wa azimio uliowasilishwa na Umoja wa Kisovieti kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika Mkutano wake wa Kumi na Tano mwaka 1960, ambalo liliwataka wakoloni wote kutoa uhuru wa makoloni yao, na azimio lake hililokubaliwa mwaka 1961 juu ya utekelezaji wa mchakato wa kuufuta ukoloni, yalikuwa ni msingi wa sera zilizofuatia za kundi la Kisovieti kuhusiana na ushiriki wake katika kufuta ukoloni Afrika.[13] Ukiwa umekubaliwa na Mkutano wa Ishirini na Moja wa CPSU, ambao ulithibitisha kwa dhati msaada wake kwa shughuli za kupigania uhuru,[14] na kuthibitishwa na Mikutano ya Ishirini na tatu hadi Ishirini na saba, msimamo huo uliupatia Umoja wa Sovicti urafiki wa Waafrika na kuwa ushindi mkubwa wa kidipomasia dhidi ya nchi za ukoloni za Magharibi. Tangu hapo Wasoshalisti wametoa msaada kwa wapigania uhuru wa Afrika kwa moyo mmoja, na wamejiona hivi sasa kama walinzi wa uhuru wa Afrika, mtazamo ambao wengi wao wanakubaliana nao. Oginga Odinga, mwanasiasa wa Kenya, aliwahi kusema, "USSR inatumia hadhi yake kuyasaidia mataifa yanayokandamizwa ambayo yanataka kujikomboa kutokana na aina zote za ukoloni... na iko nasi wakati wote wa mapambano.Hatutasahau hilo kamwe."[15]

Katika awamu hii ya mapambano ya kupigania uhuru msaada huo ulipokewa na vyama vya kupigania uhuru vya nchi mbalimbali kama vile Algeria, Misri, Ghana, Guinea, Mali, Sudani, tunisia, Kenya, Uganda, Tanganyika na Somali. Kusini mwa Afrika, ambako mapambano dhidi ya ukoloni yaliendelea kwa muda urefu zaidi, msaada wa USSR na Ulaya ya Mashariki ulikuwa muhimu zaidi kwa shughuli za chama cha ZAPU cha Zimbabwe, FRELIMO cha Msumbiji na MPLA cha Angola. Katika mapambano yake dhidi ya utawala wa ubaguzi wa rangi, chama cha ANC cha Afrika Kusini na SWAPO cha Namibia vimepata msaada wa kisiasa, kidiplomasia, kifedha na kivita kutoka kwa madola ya kisoshalisti ya Ulaya.[16]

Mara zilipopata uhuru, nchi kadha zilitafuta ushirikiano na USSR na nchi za demokrasia ya watu za Ulaya, ama kwa nia ya kundokana na ukoloni mambolco, ambao mwanzilishi wa ukombozi wa Ghana, Kwame Nkrumah, aliubeza kuwa "ni

[13] D. Skvirsky, 1967, kur 196.215
[14] *Carrent Societ Policies III*, 1960, uk. 20
[15] Radio Moscow, 16 Oktoba 1960; Prauda , 16 Oktoba 1960, uk. 3
[16] H. Donalson na L. Nogee, 1981

hatua ya mwisho ya ubeberu,"[17] au kupingana na athari za kipekee za madola ya kibepari. Tangu 1957, tarehe ya uhuru wa Ghana, hadi 1985, USSR ilitia saini makubaliano na kiasi cha nchi 37 za Afrika. Kipengele cha kuvutia cha ushirikiano huu kinahusu elimu na utafiti, kwa njia ya kuwafunza makada wa Kiafrika huko USSR na Afrika kwenyewe, kupelekwa kwa walimu na watafiti wa Kisovieti katika vyuo vikuu na vituo vya utafiti vya Afrika na kuanzishwa kwa uhusiano wa kisanyansi baina ya asasi za Sovieti na za Afrika: takribani Waafrika 30,000 walipata elimu ya juu na ya kitaaluma huko USSR[18]. Ushirikiano na madola mengine yaliyo wanachama wa ACMS, yaliyojumuisha nyanja pana, ulijengwa katika misingi hiyohiyo.[19]

## Jamhuri ya Watu wa China na Ukombozi dhidi ya Ukoloni Afrika

Kwa sababu za kiitikadi na kitaifa, nchi za Dunia ya Tatu zinajivunia malengo ya sera za nchi za nje ya Beijing na hakuna kinachodhihirisha hali hiyo kama Uhusiano wa China na Afrika, ambao umuhimu wake kwa Beijing umckitwa katika mawazo ya aina tatu.

Kwanza, juhudi za Afrika za kujikomboa zinawakilisha hatua muhimu katika mapambano ya kimapinduzi duniani dhidi ya ubepari: China ya Kisoshalisti ilikuwa na wajibu, kwa hiyo, wa kusaidia juhudi hizo; pili, manufaa ya China yalihitajia kuwapo Afrika ambako hadi karibuni maadui zake wawili, Marekani na USSR, walikuwa tayari wakishindana, na ambako ingeweza kuungwa mkono, angalau kwa kiwango cha kidiplomasia, ambako kungesaidia kufikia malengo ya sera yake ya nchi za nje; mwishowe, China inaamini kwamba imepitia hali ya nusu ukoloni ambayo inafanana na ile ya Afrika na hivyo ina nafasi nzuri ya kuelewa matatizo ya ukoloni na kulisaidia bara hili kupita mchakato wake wa kujikomboa kutokana na ukoloni huo.[20]

[17] K. Nkurumah, 1966

[18] Mawsiliano kutoka A. Letnev, Taafisi ya Afrika, Moskow, 9 Septemba, 1987. Ling. A.A Gronyko, 1984.

[19] Nchi za ACMS ba Afrika: Biashara na Ushirikiano 1980; V. Lopatov, 1987.

[20] G.T.YU, 1975, uk. 67 taz – pia hotuba ya Waziri Mkuu Zhou En Lai katika Kanzalu aliyoitoa kwa Rais Nkurmal, kama awli uk. 89

Ukweli wa aina nyingi unadhihirisha umuhimu uliowekwa na China juu ya Afrika: dhamiri iliyowekwa kwenye Mkutano wa Kibiashara wa Kimataifa uliofanywa Beijing katikati ya miaka ya 1950, kusaidia nchi za Afrika zinazopigania uhuru;[21] msaada uliotolewa kwa Mau Mau ambao Wachina waliuchukulia kama nguvu dhidi ya ubeberu;[22] ziara ya Afrika ya Waziri Mkuu Zhou En Lai mwishoni mwa 1963 na mwanzoni mwa 1964, ambapo alisisitiza kuwa, "Afrika iko tayari kwa mapinduzi;" kulaani "kujitangazia uhuru" kulikofanywa na Wazungu Rhodesia (11 Novemba 1965); msaada uliotolewa kwa wapigania uhuru kwenye makoloni ya Wareno, Zimbabwe, Afrika Kusini na Afrika Kusini Magharibi; na kulaani kuendelea kwa utawala wa ubaguzi wa rangi na utoaji wa msaada kwa wapinzani wa mfumo huo, hasa kwa Pan-African Congress (PAC).

Mchango mkubwa wa kwanza wa China katika ukombozi dhidi ya ukoloni Afrika ulikuwa ni reli ya gharama kubwa ya Tanzania-Zambia, TAZARA, China ilikubali kuijenga baada ya nchi zote tajiri na zilizoendelea kitekuolojia kukataa. Madhumuni ya China ya kuchukua mradi huo wa dola milioni 450 yalikuwa, kulingana na taarifa za ndani ya China, ".... kuzisadia Zambia na Tanzania katika mapambano yao dhidi ya ukoloni na uvamizi kutoka dola za kibaguzi za Rhodesia ya Kusini, Afrika Kusini na Ureno."[23]

TAZARA ilikuwa mradi muhimu kwa Zambia ambayo haina bandari na ambayo mawasiliano yake na nchi za nje yalikuwa yamekatwa na utawala wa kibaguzi wa Rhodesia kwa sababu Rais Kaunda aliendelea kuushutumu na kwa sababu aliwasaidia wapiganaji wa ZANU na ZAPU. Umuhimu wa mradi huu kwa mapambano dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi ulionyeshwa pia na hofu iliyojitokeza kwa utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini, ambao uliuunga mkono utawala wa wachache wa Rhodesia ya Kusini. Waziri Mkuu wa Afrika Kusini alieleza kwa wasiwasi: "Wachina wamejenga daraja Tanzania na uwezekano kwa kupitia ujenzi wa reli ya TAZARA wa kuingia ndani zaidi katikati ya Afrika na kujijenga kwa kudumu ndani ya Tanzania na Zambia".[24]

[21] *Shirika la Habari la China Mpya [New China News Agency]* No. 447, ilivyonukuliwa na B. Larkin, 1971

[22] Peking Review 15 Agosti 1960. Uk 16

[23] *Peking Review*, 17 Julai 1970, uk. 16

[24] Star (Afrika Kusini) 15 Mei 1971; *Africa Research Bulletin*, Mei 1971 uk. 2098C



PCHA 27.1 *Mwenyekiti Mao Zedong wa China akikutana na Rais K.D. Kaunda wa Zambia huko Beijing, Februari 1974*

China aghalabu ilitoa msaada wa kijeshi kwa vikundi kadha vya wapiganaji vilivyokuwa marafiki wa China huko Afrika Kusini kama vile kwa Pan-African Congress ya Afrika Kusini.[25] na hasa wapiganaji wa ZANU, waliopata mafunzo na vifaa kutoka kwa wataalamu wa Kichina kwenye kambi mbalimbali zilizokuwa Tanzania na Msumbiji[26] na ambao, kwa msaada mkubwa wa China waliiongoza Zimbabwe kupata uhuru wa kisiasa. China, inauelezea ushindi huo kama mfano wa mafanikio yake katika mapambano ya ukombozi wa Afrika;[27] kauli hiyo imerudiwa na waziri mkuu wa Zimbabwe ambaye, katika kushukuru nafasi iliyochukuliwa na China katika kuikomboa nchi yake, alisema, "China imekuwa ni matumaini ya kiitikadi na kijeshi kwa shughuli za kitaifa za Zimbabwe."[28]

[25] *African Communist* robo pili 1967, uk. 17

[26] D. Martin na P. Johnson, 1981, kur. 11-12, *Tanzania Standard* (Dar es Salaam) 10 Desemba, 1977; Africa Research Bulletin, Desemba 1977

[27] New China Agency, 30 Juni 1980; Africa Research Bulletin, Julai 1980, uk. 5730

[28] Africa Research Bulletin, Mei 1981, uk. 6059

Viongozi kadhaa wa Afrika, ikiwa ni pamoja na Nyerere, Gowon na Kaunda, wameelezea mawazo kama hayo na wameishukuru dhima iliyochukuliwa na China katika mchakato mzima wa ukombozi dhidi ya ukoloni Afrika.[29] Hadi sasa, shughuli za kupingana na ukoloni na ubaguzi wa rangi bado zinaweza kuendelea kutegemea msaada wa China, kama ilivyosisitizwa na Waziri wao Mkuu wakati alipozuru Afrika mwaka 1980.[30]

## Athari ya Vita vya Vietnam kwa Afrika

Vita vya Vietnam vimekuwa na athari za kisiasa, kisikolojia, kiuchumi na kijeshi kwa Afrika.

Vita hivyo kama ilivyokuwa kwa vita vya ukombozi vya Afrika ilikuwa ni matokeo ya ubeberu na ukoloni, pamoja na uhasama wa nchi zenye nguvu kugombea nchi ya Ulimwengu wa Tatu. Vietnam ya Kaskazini, ikiungwa mkono na Wakomunisti, ilikuwa kwenye vita vya msituni huko kusini (wakiungwa mkono na Marekani) kwa nia ya kuunganisha nchi yao. Marekani ilipeleka huko kusini maelfu ya askari waliokuwa na vifaa vya kutosha dhidi ya Wavietnam wa Kaskazini wenye silaha duni, waliokuwa wakiungwa mkono na nchi za Sovieti na China. Waafrika waliehukulia kupelekwa huko kwa askari wa Kiamerika kupigana na Vietnam Kaskazini kuwa ni kitendo cha uvamizi wa ukoloni mamboleo dhidi ya nchi ndugu na waliamini kuwa hali kama hiyo ingeweza kuitokea nchi yoyote ya Dunia ya Tatu inayopingana na manufaa ya nchi zenye nguvu.[31]

Kutokana na nchi zenye nguvu za Magharibi kushirikiana na utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika kusini, Waafrika wengi waliona kuwa Wavietnam walikuwa wanapigana na adui yuleyule. Udugu wao ulitokana na msingi kuwa nchi za Afrika na Vietnam zote zilikuwa wanachama wa Nchi zisizofungamana na Upande Wowote ambazo usalama na umoja wao ulitishiwa na uvamizi uliofanyiwa Vietnam. Mwishowe, kwa kupata msaada wa China na USSR (marafiki wakuu wawili wa Vietnam) katika juhudi za kuondoa kabisa ukoloni katika makoloni ya Ureno na Kusini mwa Afrika, viongozi wengi wa Afrika waliona hawana budi kuiunga mkono Vietnam

[29] Taz. Kwa mfano, *Times of Zambia*, 22 Februari 1974; New Nirerian, 18 Septemba 1974; Africa Research Bulletin, Machi 1974 uk. 3185

[30] New China News Agency, 30 Juni 1980.

[31] A.A. Mazrui, 1972, uk. 124

Ushindi wa Vietnam Kaskazini dhidi ya Marekani ulikuwa na athari kubwa kwa Afrika. Kwa wapiganaji wengi wa Kiafrika, ulikuwa ni ushindi wa Daudi dhidi ya Goliati. Ulivunja pia imani ya kwamba nguvu za kijeshi ndiyo sababu pekee ya ushindi na kudhihirisha kuwa uamuzi, kujinyima na azma ya watu wanaopigania haki yao ni muhimu zaidi. Ushindi huo uliwatia nguvu watu wa Zimbabwe, Namibia, Angola na Msumbiji, kuwaongezea imani kwamba, kwa dhamira yao, wangezishinda nguvu za kijeshi za ubeberu, ukoloni na tawala za ubaguzi wa rangi. Tangu mwisho wa vita hivyo, wapiganaji wa Afrika walijulishwa na China na Vietnam kuhusu mbinu za Vietnam za vita vya msituni, ambazo zimezisaidia sana baadhi ya nchi, kama Zimbabwe, kupata uhuru.

Matokeo mengine ya vita vya Vietnam yalikuwa ni kushindwa kwa China na USSR kutoa msaada kamili kwa nchi za Kiafrika kujikomboa na ukoloni kutokana na kushikwa mno na mapambano hayo. Marekani nayo ilikuwa imeshikwa mno na mapambano hayo kuweza kujihusisha na matukio ya Afrika. Hata hivyo mara vita vilipoisha, wakati Marekani ikiwa mwangalifu kutokana na matokeo ya vita vya Vietnam, USSR na China ziliongeza kani katika kuathiri na kujidhihirisha katika bara hili, hasa katika makoloni ya awali ya Ureno, Zimbabwe, Zambia, Tanzania na Pembe ya Afrika.

Mwishowe, baada ya kumalizika kwa Vita vya Vietnam, nchi mbili zenye nguvu zaidi duniani zilielekeza nguvu zao barani Afrika ambako nchi za Magharibi na Sovieti zilishindana, kwa mfano Angola na Pembe ya Afrika. Kwa kuhitimisha ushindi wa Vietnam Kaskazini ulielekea kuzipa hadhi nchi za kisoshalisti, hasa USSR na China, kuwa walinzi wa manufaa ya nchi ndogo za Dunia ya Tatu dhidi ya wenye nguvu wa Magharibi.

## Uhusiano wa Afrika na nchi za Kisoshalishi

Ingawa ni kweli kwamba mifumo ya sasa ya kiuchumi na kisiasa ya Afrika inatokana na mifumo yake ya kienyeji, inaweza ikachanganuliwa tu katika muktadha wa maendeleo ya muda mrefu, yaliyowaingiza polepole katika kujihusisha na mabadilishano na ulimwengu mzima na baadaye, takribani katikati ya karne ya kumi na tisa, kushirikishwa kwake moja kwa moja kwenye mfumo huu, na mwishowe, mwanzoni mwa karne ya ishirini, ikawa chini ya mahitaji na malengo ya kiuchumi na kisiasa ya nchi kuu zenye nguvu za Magharibi.[32]

[32] P.C.W. Guthind na I Walleistein, 1976, Juz. 1, uk. 7 Taz pia I Walkerstein, 1976a.

Matukio yaliyoendelea Afrika yaliwadhihirishia wananadharia wa Kisovieti imani yao kwamba shughuli za ukombozi wa kitaifa zilikuwa zinaendana na mapambano dhidi ya ubeberu. Mkutano wa Bandung ulishuhudia kuibuka kwa nguvu ya aina ya tatu kati ya mifumo ya ubepari na usoshalisti na ambayo ilibidi itambuliwe. Huko Misri, jaribio la nchi za Magharibi kuiyumbisha, na hasa misafara ya Ufaransa na Uingereza huko Suezi mnamo 1956, lilisababisha al-Nasser akubali silaha kutoka Moscow. USSR na marafiki zake walichukulia uhuru wa Moroko, Tunisia, Sudani, Ghana na Guinea, na mapambano ya FLN ya Algeria, kuwa ni pigo kubwa dhidi ya ukoloni na ubeberu lililosababishwa na wasio wakomunisti na, kwa macho ya Mosko, uwezekano upo wa kuelekea katika ujenzi wa wanaharakati zaidi. Hivyo, vyombo vya habari vya Sovieti vilieleza kuwa, kama ilivyokuwa kwa Fidel Castro wa Kuba, Waafrika kama Sékou Touré, Kwame Nkrumah na hata Modibo Keita wangeweza kuvuka manufaa ya tabaka lao, ubwanyenye uchwara wa kitaifa, na kuingia katika "njia ya maendeleo isiyo ya kibepari", inayoweza kuendea katika usoshalisti.

Wananadharia wa Kisovieti walielezea njia ya maendeleo isiyo ya kibepari kwa nchi za Kiafrika ambayo ilikuwa na uwezo mkubwa wa kuwa ya kimapinduzi. Njia hii ni ile inayochukuliwa na "demokrasia za kitaifa". Nchi ambayo ni "yenye uhuru wa kweli, inayopinga ubeberu, ukoloni, udikteta, na iliyo ya kidemokrasia na inayoleta maendeleo katika sera zake za ndani na za jamii ndiyo inayoitwa ya kidemokrasia"[33] Kwa ufupi, wananadharia wa Kisovieti walichukulia kwamba kulikuwa na kufanana kwa raghba baina ya dunia ya kisoshalisti, vuguvugu la ukombozi la Afrika na shughuli za wafanyakazi wa kimataifa za mapambano dhidi ya ubeberu.

Hivyo katika miaka ya 1960 nchi za Kiafrika zilizoelekea kwenye njia ya kisoshalisti zilipata msaada kutoka usoshalisti wa Kimataifa kwa kuanzia na Misri, Ghana, Guinea na Mali.

Lakini ukweli ni kwamba nchi nyingi huru za Afrika zilibakia na asasi za kikoloni na kuunda katiba zao kwa mfano wa zile za watawala wao wa awali. Pia, angalau kwa miaka michache ya mwanzo, walibakisha wafanyakazi wengi kutoka nje, aghalabu kutoka kwa watawala wao wa kikoloni, kwenye sekta muhimu kama

[33] Kulingana na maelezo yaliyotolewa na mwananadharia wa Kisovieti B. Ponomarev mnamo 1960 na dhana hiyo ilichambuliwa kwa makini na mwanahistoria wa Kifaransa J. Chesneaux, 1964, kur. 3-19.

vile utumishi wa umma, polisi na jeshini. Hata kwenye nchi kama Ghana chini ya Nkrumah, ambayo ilipenda usoshalisti, kulikuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi kutoka Magharibi ambao walibaki kwenye vyeo vyao hadi 1961. Walikaa kwa muda mrefu zaidi kwenye makoloni mengine ya zamani kama vile Kenya, Nigeria, Senegali na Côte d' Ivoire. Wafanyakazi hao kutoka nje, ambao walikuwa na vyeo muhimu katika vyombo vya serikali, kwa vyovyote vile waliathiri sera za kisiasa na kiuchumi za nchi huru za Afrika na mara nyingi kwa manufaa ya makoloni hayo ya zamani ya Kimagharibi.

Kwa upande wa uchumi makoloni hayo ya zamani yameshindwa kujinasua na minyororo ya kiuchumi na biashara ya watawala wao wa zamani wa kikoloni ambao, pamoja na nchi nyingine zenye nguvu za Magharibi, wanadhibiti vyombo vyote vikuu vya fedha ulimwenguni pamoja na Benki ya Dunia, pesa zinazotumiwa katika nchi za Kiafrika, bei za malighafi na kikomo cha mazao makuu ambayo nchi za Kiafrika zinaweza kasafirisha nje.

Kwa upande wa utamaduni, lugha ya taifa ya nchi nyingi zilizokuwa chini ya ukoloni ilibakia kuwa ile ya wakoloni ambao mifumo yao ya elimu walimakili, na wakati huohuo wakibakisha maadili karibu yote ya utamaduni wa Magharibi, katika mavazi na ulaji, kwa mfano.[34] Urithi huu wa kudumu unatokana na ukweli kwamba makoloni yalikuwa chini ya utawala wa kiutamaduni wa wakoloni kwa muda mrefu na kuwa nchi za Magharibi zimekuwa zikieneza propaganda kwa ufanisi kwa ajili hiyo kwenye makoloni yake ya awali.

Katika mazingira hayo, nchi za kisoshalisti zimepata ugumu wa kufuta au hata kupunguza utegemezi wa nchi za Kiafrika kwa ubepari wa Kimagharibi, na sababu hii, ikiongezwa na ukandamizwaji wa wanaharakati wa kikomunisti na serikali zilizokuwa madarakani, inaelezea kwa nini imekuwa vigumu kwa vyama vya kikomunisti kuundwa katika bara hili. Na imewakatisha tamaa zaidi wasoshalisti kutokana na ukweli kwamba hata nchi zile na viongozi ambao mwanzoni walionyesha kupendelea usoshalisti wamerudi nyuma kwa njia moja au nyingine kutegemea mabepari. Misri, kwa mfano, al-Nasser alifuata sera ya kukikandamiza Chama cha Kikomunisti cha Misri na chini ya al-Sadat, uhusiano wa Misri na Sovieti ukawa mbaya kuliko wakati mwingine wowote. Kwingineko katika Afrika ya Weusi, wasoshalisti walipata pigo jingine. Huko Guinea uhusiano ulioanzishwa 1959 ulizorota. Balozi Daniel Solod alifukuzwa kutoka Conakry mwaka 1961 na,

[34] A. Okolo, 1983, kur. 252-4

licha ya ziara ya Anastase Mikoyan ya mji mkuu wa Guinea Januari 1962, mazungumzo baina ya Muungano wa Sovieti na Guinea haukuweza kuleta utangamano kama ilivyokuwa mwanzo. Guinea polepole ikarudi chini ya matao ya Magharibi.

Huko Ghana wasoshalisti walitumaini kwamba Nkrumah, mwananadharia wa usoshalisti wa Kiafrika, angechukua mawazo ya usoshalisti wa kisayansi na kuboresha uhusiano wa Ghana na dunia ya kisoshalisti. Lakini licha ya msaada walioupokea kutoka jumuiya ya kisoshalisti, utawala wa Akkra ilibidi usubiri kwa muda kabla ya kuitambua Ujerumani Mashariki kwa kuchelea kuiudhi Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani ambayo ilikuwa ikiwapa msaada mkubwa wa kiuchumi.[35] Na mwishowe mapinduzi yaliyomtoa Nkrumah madarakani 24 Februari 1966 na kuunda utawala unaopendelea Magharibi yalikomesha mara moja urafiki na jumuiya ya Sovieti. Tawala zilizofuatia huko Akkra hazijarudisha tena uhusiano mzuri uliokuwapo kati ya dunia ya kisoshalisti na Ghana chini ya Nkrumah. Huko Mali urafiki wa dunia ya kisoshalisti haujaweza kurudi tangu Modibo Keita atoweke kutoka kwenye siasa baada ya kupinduliwa serikali yake 18 Novemba 1968.

Katika Nigeria inayopendelea Magharibi, urafiki na jumuiya ya Sovieti ulijionyesha tu wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Nchi za Mashariki wakati huo zilitoa msaada wa kijeshi kwa nchi hiyo. Baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, hata hivyo, Nigeria ikawa tegemezi tena kwa jumuiya ya Magharibi licha ya kuwa ilikataliwa nayo msaada wa kijeshi. USSR ililalamika mwanzoni mwa vita hivyo kwamba iliukataa msaada wake.[36]

Jambo kama hilo lilitokea pia Afrika Mashariki na ya Kati kama ilivyokuwa kwa Afrika Magharibi na Kaskazini. Kenya, ambayo wakati wa uhuru ilikuwa na uhusiano mzuri na dunia ya kisoshalisti,[37] ikawa katika nusu ya pili ya miaka ya 1960 mojawapo ya nchi zilizopendelea Magharibi katika Afrika. Kipindi hicho kilikuwa cha kichaa cha kupinga ukomunisti katika nchi hiyo, kikiishia kwa kuwafukuza KANU, wale waliotuhumiwa kuwa wakomunisti.[38] Athari za kiuchumi na kisiasa za Magharibi, ambayo ilikuwepo tangu wakati wa ukoloni, imeendelea

[35] W.S. Thompson, 1969, imenukuliwa na R. Legoold, 1970, uk. 25

[36] International Affairs, 1963, uk. 79; na African Communist, 1965, na 2, uk. 41.

[37] O. Odinga, 1969

[38] "Kenya haitakuwa ya kikomunisti." Amesema Waziri Mkuu wa Kenya, *East African Standards* (Nairobi), 1 Machi, 1965, uk. 5.

kuonekana kwa kuwa na uwekezaji mkubwa kutoka Magharibi, na Wakenya waliokuwa na mawazo ya Kiharakati wameonekana kuwa ni wakomunisti na hivyo kuwa ni hatari kwa amani ya raia na maendeleo ya taifa.

Uganda, Zambia na Zimbabwe pia zinategemea Magharibi, ingawa kwa kiwango kidogo zaidi. Jaribio la Obote la kuanzisha programu ya kisoshalisti mwishoni mwa miaka ya 1960 lilikigawa chama chake na kusababisha mgawanyiko nchini humo kati ya "wakomunisti" na wanademokrasia. Rais Julius Nyerere pia alijaribu, mwaka 1967, kupeleka Tanzania kwenye njia ya maendeleo ya kujitegemea kwa kufuata usoshalisti ili kupunguza kutegemea mataifa makubwa ya nje. Licha ya juhudi hizo za dhati, Tanzania bado inategemea nchi za Magharibi, kama Nyerere mwenyewe alivyokiri: "Nchi yetu bado inategemea kiuchumi maamuzi ya kiuchumi na kisiasa yanayofanywa na watu wengine bila sisi kushiriki au kutoa ridhaa yetu."[39] Ni dhahiri, misaada ya China kwa Tanzania imeongezeka katika miaka ya karibuni, lakini hiyo haijaathiri utegemezi wa nchi hiyo kwa mataifa makubwa ya Magharibi. Hata Somalia ya kisoshalisti, Jamhuri ya Demokrasia ya Somalia ya kabla ya 1977 na Ethiopia ya kisoshalisti ya baada ya mapinduzi ziliendelea kutegemea hasa nchi za kibepari na Magharibi kiuchumi na kiutamaduni, licha ya kijeshi, ambapo nchi za kisoshalisti zimechukua nafasi ya nchi za Magharibi, hasa Ethiopia, tangu 1978. Kwa kuhitimisha, athari za kisiasa, kiuchumi na kijamii za mataifa makubwa ya Magharibi kwenye makoloni yake ya zamani zimeingia mno na zimeundwa kwa jinsi ambayo imekuwa vigumu kwa nchi nyingi za Afrika zilizopata uhuru hivi karibuni kujitoa bila kushikishwa adabu na mfumo wa ubepari wa kimataifa. Zaidi ya hapo, nchi za kisoshalisti hazina uhusiano wa kihistoria wa karibu kama huo na wa muda mrefu na nchi hizo za Afrika, na mfumo wa kiuchumi wa nchi za kisoshalisti haujatengemaa vyema duniani kote wala haukuundwa kwa ustadi kama mfumo wa ubepari wa Magharibi.

Eneo moja ambalo dunia ya kisoshalisti imekuwa na athari ya kubwa ni katika itikadi. Itikadi ya kisoshalisti na uwezo wake wa kuhamasisha na kuunganisha watu ilitumiwa na viongozi kadhaa wa Kiafrika, waliopenda maendeleo na wapinga maendeleo pia, kuziweka sawa jamii ambazo kwa jadi ziligongana kimbari na kidini. Wazalendo wa Kiafrika wametumia itikadi hiyo pia kuubeza ukoloni wa Magharibi na kuyaeleza mataifa ya Magharibi juu ya mahitaji ya Afrika.[40]

[39] Hotuba ya J. Nyerere, iliyoripotiwa katika *Daily News* (Tanzania), 25 Machi, 1977; *Africa Diary*, 11-17 Juni 1977, uk. 8525

[40] A.A. Mazrui, 1980b, kur. 44-6

Ushoshalisti ulichukuliwa pia na viongozi kadhaa wa Kiafrika kwa sababu, kama mmoja wao, J. Nyerere, alivyosema, unaendana vyema na maisha ya Kiafrika. Waafrika hawahitaji kufunzwa usoshalisti kwani tayari uko katika jamii zao za jadi.[41] Kiongozi huyo wa Tanzania alieleza kwamba hajaingizwa kwenye usoshalisti kwa kusoma maandiko ya Marx, lakini sababu kubwa iliyomvuta ilikuwa ni athari ya wazazi wake na maisha yake ya ukulima.[42] Viongozi kadhaa wa Kiafrika wanaelekea kuukubali usoshalisti kwa sababu za manufaa ya kiuchumi na kisiasa. Inaelekea kwamba Nkrumah alifuata usoshalisti kwa kiasi fulani ili kupata msaada wa kisiasa na vifaa kutoka jumuiya ya kisoshalisti ambao jumuiya ya Magharibi, kutokana na uadui na kutokubali kushindwa katika msimamo wao, haikuwa tayari kumpatia. Inabidi kuzingatia, hata hivyo, kwamba Nkrumah alibadili msimamo wake kuwa uchaguzi wa kinadharia na kimkakati kuanzia 1968.[43] Inaweza kuonekana kuwa Siad Barre alifanya uchaguzi wake kwa sababu zinazofanana na hizo na kutokana na kwamba ulimsaidia katika sera zake za kutaka uhusiano wa karibu na majirani zake, Kenya na Ethiopia. Msaada huo wa kisoshalisti ulipokoma, alionyesha usoshalisti wake kutokuwa wa msingi kama ifuatavyo: "Mimi ni mzalendo kwanza, pili Mwislamu na tatu Msoshalisti".[44] Sékou Touré ilibidi afuate usoshalisti kwani nchi yake isingeweza kujihimili kwa vyovyote vile baada ya kuondolewa msaada wa Magharibi. Kanali Mengitsu inaelekea ilimbidi kufuata usoshalisti kama jinsi ya kujiletea maendeleo kwa upande mmoja na kama njia ya kuiunganisha Ethiopia baada ya kumwangusha Mfalme aliyependelea Magharibi. Dunia ya kisoshalisti ilitoa msaada bila kusita kwa utawala wake Derg ilikuwa tayari wakati wote kusaidia tawala za Afrika zilizoelekea kupendelea usoshalisti.[45]

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1960 mazungumzo yenye mafanikio yalianza kati ya wawakilishi wa usoshalisi wa kisayansi na usoshalisti wa Kiafrika ambayo yalitoa mchango mkubwa kuleta maelewano ya kimawazo baina yao. Licha ya uhakiki kutoka pande zote mbili na licha ya tofauti za mawazo zilizotambulika, washiriki wa mazungumzo hayo[46] walikuwa na mawazo ya msingi yanayofanana, yaani kupambana na ubeberu na ubaguzi wa rangi, matarajio ya maendeleo ya

[41] kama awali; taz. Pia Africa Report (New York), 1962

[42] P. Enahoro, 1983, kur. 98-122

[43] Taz. S. Ikoku, 1971

[44] D. Lamb, bila tarehe

[45] Pravda, 14 Septemba 1974.

[46] Kwa ufafanuzi, taz. I.I. Potekhin, 1963, kur. 71-5; *Colloque Sovieto-Congolais,* 1988.

jamii na kukubali kujenga uhusiano wa kirafiki baina ya majeshi ya ukombozi wa kitaifa na dunia ya kisoshalisti. Baada ya kuchanganua sababu za msingi, za ndani na za nje, za tawala zinazoelekea kwenye usoshalisti katika kujenga jamii mpya, watafiti wa kisovieti walichukua msimamo uliowezekana kuwepo zaidi. Bila kudharau uwezekano wa kimapinduzi wa watu waliopata uhuru, walianza kushughulikia zaidi kuangalia matatizo makubwa yaliyowakabili wale walioamua kukabiliana na karne nyingi za kutoendelea na kuwepo kwa ukoloni mamboleo ambao hauondoki kiurahisi.

## Afrika na Dunia ya Kisoshalisti katika Uhusiano wa Kiuchumi

> Sema unachohitaji na tutasaidia .......kwa njia ya mikopo, msaada wa kiufundi....hatujaribu kufaidika.....hatuhitaji faida......hatuwaombi mshiriki katika jumuiya yetu....tuko tayari kuwasaidia kama ndugu anavyomsaidia nduguye.[47]

Maelezo haya yanaakisi nadharia ya sera ya uchumi ya jumuiya ya Kisovieti kuhusiana na Afrika.

Nchi za kisoshalisti na Afrika zimekuwa na uhusiano mkubwa wa kiuchumi, kiufundi na kibiashara tangu 1960. Viongozi wa kisoshalisti wamekuwa, tangu wakati wa Lenin, wakichukulia kwamba ni wajibu wao kama wanamataifa kutoa msaada wa kiuchumi na kiufundi kwa nchi za Kiafrika zinazotawaliwa na zilizo huru ili kuziwezesha kujitegemea, wakitoa hoja zaidi kuwa msaada wa kisoshalisti, tofauti na ule wa wafadhili wa kibepari, ni wa kujitolea na hauna masharti.[48]

Iwapo lengo mojawapo la nchi za Magharibi ni kutawala kiuchumi, ili kupata mali ghafi na masoko kwa ajili ya bidhaa zao za viwandani, lengo kuu la Sera ya Afrika ya jumuiya ya Kisovieti lilikuwa si kuzifunga nchi hizo katika eneo lao la mamlaka ya kiuchumi ambalo wao ndio kitovu. Ukweli ni kwamba hifadhi ya madini inayojulikana ya USSR inatosha kwa mahitaji yake, angalau kwa kipindi cha kati, na viwanda vya jumuiya ya kisoshalisti havielekei kuhitaji sehemu za mauzo nje ya soko lake la ndani, ambalo bado halijatoshelezwa kabisa. Lakini jumuiya ya Kisovieti iliona ni muhimu kuzisaidia nchi za Afrika ziweze kutawala

[47] Maelezo ya A.A. Arzumanyan, kiongozi wa msafara wa Kisovieti kwenye Mkutano wa Urafiki wa Watu wa Afrika na Asia uliofanyika Cairo: A.A. Arzumanyan, 1958, kur. 185-6.
[48] V. Rymalov, 1959b.

mali ghafi zao ili kuzizuia zisitawaliwe na Ulaya na Marekani. Nchi za kisoshalisti hata hivyo ziliitegemea Afrika kwa ajili ya baadhi ya bidhaa kama vile samaki na baadhi ya madini adimu.[49] Wakati wa maridhiano, msaada wa jumuiya ya kisovieti ulionyeshwa kama ni njia ya amani ya kushindana na nchi za kibepari: "Mataifa ya kisoshalisti yanashindana na mataifa makubwa ya Magharibi si katika ushindi wa silaha lakini katika kuongeza misaada kwa nchi zilizo nyuma kimaendeleo"[50] Kwa hivyo, fasili ifuatayo ya Bwawa la Aswan ilitolewa: "Bwawa la Aswan ni eneo ambalo usoshalisti na ubepari hushindana, na matokeo ya mashindano haya ni manufaa yasiyo na mashaka kwa usoshalisti."[51] Tangu miaka ya 1960, hata hivyo, wachumi na viongozi wa nchi za kisoshalisti wameelekea zaidi kaika kusisitiza manufaa ya pamoja ya uhusiano wa kiuchumi baina ya Afrika na nchi za kisoshalisti.[52]

Zifuatazo ni baadhi ya sifa za misaada ya nchi za kisoshalisti kwa Afrika: riba ya kiwango cha chini kuliko inayotolewa na wafadhili wengi wa Magharibi, kuanzia kiasi cha asilimia 2.5 hadi 3 kwa mwaka, kukiwa aghalabu na kipindi cha msamaha cha mwaka mmoja na wastani wa kipindi cha malipo cha miaka 12, na msaada kutolewa kama mkopo. Miradi inayogharimiwa kwa njia hii, inapokamilika, huwa ni mali ya anayepokea msaada. Madhumuni, kulingana na Ivan Chernyshev, ofisa anayehusika na uhusiano wa kiuchumi wa Shirikisho la Urusi na nchi za kigeni wa miaka ya mwisho ya 1970, yalikuwa kutoa masharti nafuu kwa Afrika.[53]

Ushirikiano wa kiuchumi wa nchi za Kisovieti na Afrika ulikua sana katika miaka ya 1960 na 1970 kutokana na kuongezeka kwa umuhimu wa bara hilo katika madhumuni ya kiulimwengu ya nchi za kisoshalisti. Kwa mfano, biashara kati ya Shirikisho la Urusi na Afrika iliongezeka mara tano baina ya 1960 na 1975 na idadi ya nchi za Afrika zilizofanya biashara na shirikisho hilo pekee yake ziliongezeka kutoka sita hadi 36 kati ya 1960 na 1976.[54]

Uchaguzi wa mpokeaji na kiasi cha msaada hutawaliwa na sababu zifuatazo: umuhimu wa kimkakati wa nchi pokezi, uwezekano, hadi karibuni, wa kupunguza athari za Marekani na China, kuunga kwake mkono itikadi ya Marx na Lenin; na

[49] Taz, P. Biarnes, 1980 na P. Decraene, 1982.
[50] V. Rymalov, 1959a.
[51] I. Belyana V. 1962; E.M.' Bokolo, 1980
[52] A.A Gromyko, 1967
[53] *Ethiopian Herald* (Addis Ababa), Aprili 1977
[54] Novosti, April 1977; Africa Research Bulletin, 15 April 14 Mei 1977; uk. 4281



PICHA27.2 *A. Mikoyan, waziri wa mambo ya nje wa Urusi, akiwa amewasili Ghana alipokuwa amealikwa na Rais K. Nkrumah, Januari 1962.*

umuhimu wake katika kutoa mali ghafi na usambazaji wa kibiashara.[55] Hayo yamethibitishwa na watoa maelezo wa Kisovieti kwa njia ifuatayo:

> Utoaji wa mikopo wa nchi yetu hautokani na hali yoyote ya kisiasa, kijeshi au kiuchumi isiyokubalika na nchi zinazoendelea. Hata hivyo, *haitakuwa haki kufikia hitimisho kuwa shirikisho la Kisovieti halijali linatoa mikopo kwa nani na kwa masharti gani. Hiyo ingedharau mahitajio ya ukweli.* [56]

Kwa sababu hiyo, Misri ilipata misaada mikubwa hadi 1975 na Ghana chini ya Nkrumah ilikuwa ya pili kwa kupata msaada katika Afrika ya weusi kutoka Shirikisho la Urusi, licha ya udogo wa idadi ya watu na eneo ikilinganishwa na Nigeria ambayo ni kubwa na ilipendelea zaidi Magharibi. Chini ya mpango wa misaada wa nchi za Kisovieti miradi kadha ilianzishwa Ghana, hasa katika sekta za uchimbaji madini na kilimo. Waghana kadha pia walipata mafunzo chini ya

[55] PD Dean na J.A. Vasquez, 1976, kur 7 - 28

[56] V. Romanova na I Tsriklis, 1978. Hati mlalo zimewekwa kwa ajili ya msisitizo.

mpango huo. Katika biashara, Ghana ilipeleka kakao katika nchi za kisoshalisti na kubadilishana na bidhaa za viwandani.

Nchi za kishoshalisti zilipata ugumu wa kuanzisha uchumi na biashara na Nigeria iliyopendelea Magharibi mpaka baada ya vita vya ndani ambapo uhusiano wao ulikuwa mzuri zaidi, lakini Nigeria ilibakia kuwa nchi iliyopata msaada kidogo sana kutoka shirikisho la Kisovieti. Msaada wa kiufundi wa nchi za kisoshalisti kwa Nigeria, hasa katika maeneo muhimu kama ya tasnia za mafuta na chuma cha pua, uliongezeka baada ya 1970, na ulikua na kuchukua nafasi kubwa katika kuwawezesha maelfu ya Wanigeria kupata stadi zinazohitajika kwenye maendeleo ya nchi hiyo.[57] Kuhusiana na biashara, Nigeria ilipeleka nchi za kisoshalisti bidhaa kama vile kokwa za kakao, na kupata badala yake sementi, dawa na mashine.[58] Katika uwanja wa kijeshi, nchi za shirikisho la Sovieti zilichukua nafasi kubwa nchini Nigeria, hasa wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, ambapo serikali ya jumuiya ilipata misaada ya kutosha ya kijeshi kutoka Sovieti ambayo ilisaidia katika ushidi wa utawala wa Lagos, kama ilivyothibitishwa na Jenerali Gowon.[59] Nigeria iliendelea kupokea msaada mwingi wa kijeshi kutoka shirikisho la Urusi, kwa njia ya vifaa na mafunzo. Inakadiriwa kwamba tangu 1974 hadi 1978 Nigeria ilinunua silaha zenye thamani ya dola 80 milioni, zaidi ya nchi nyingine yoyote, na hiyo iliwakilisha asilimia 40 ya silaha ilizoziingiza wakati ule. Nchi nyingine kadha za Afrika Magharibi zilipata msaada kama huo wa kiuchumi kutoka nchi za kisoshalisti na kwa kiasi kidogo, msaada wa kijeshi.

Kati ya nchi za Afrika Mashariki na Kati zilizowahi kutawaliwa na Waingereza, Kenya ilipata msaada mwingi zaidi wa kichumi kutoka Shirikisho la Sovieti, licha ya msimamo wake wa kupendelea Magharibi. Dola 48 milioni ilizozipokea zilikuwa labda na madhumuni ya kukomesha chuki dhidi ya ukomunisti iliyokuwapo huko mnamo miaka ya 1960. Kutokana na hisia hizi za kupinga ukomunisti, sehemu kubwa ya msaada uliotolewa Kenya ulibakia bila kutumiwa,[60] na baadhi ya miradi iliyoitolea fedha, kama vile Taasisi ya Lumumba, ilikatizwa, ambapo msaada wa kijeshi wa Sovieti ulikataliwa.[61] Baadhi ya misaada hiyo iliendelea, ikiwa ni pamoja

[57] *Africa Diary*, 28 Mei – Juni 1973, uk. 6487; na Africa Diary, 6–12 Novemba 1982, kur. 1198-9

[58] *West African Pilot*, 1971

[59] *Daily Times* (Lagos), Jani 1974; na Radio Moskow, 28 Mei, 1974

[60] C Stevens, 1976, uk. 2, akimnukuu T. Mboya, Waziri wa Zamani wa Kenya wa Mipangano ya Uchumi

.[61] Daily Nation (Nairobi), 30 Aprili 1965, uk. 1 ; Kenya, Majadiliano ya Bunge, 3 Machi 1967, safu 741-2

na hospitali ya vitanda 500 ya Kisumu, iliyopatiwa vifaa na kuendeshwa kwa kiasi fulani na madaktari wa Sovieti.[62]

Mnamo miaka ya 1960 Uganda ilipata mkopo wa dola 16 milioni kutoka Sovieti, uliotolewa kwa utawala wa usoshaliti wa Kiafrika wa Milton Obote, kugharimia miradi mikubwa ya ujenzi wa kiwanda cha kusokota nyuzi, cha kwanza cha aina yake katika Afrika Mashariki, na Chuo cha kwanza cha kilimo cha kutumia mashine Afrika Mashariki ambacho bado kipo na kinaendeshwa kwa sehemu fulani na walimu wa Sovieti.[63]

Kuhusu biashara, Uganda imepeleka kahawa, pamba na shaba kwenye nchi za Sovieti ili kubadilishana na mashine na dawa. Katika uwanja wa kijeshi, nchi za Sovieti, hasa Shirikisho la Urusi, ziliipa msaada mkubwa. Inakadiriwa kuwa mnamo 1978 Urusi ilitoa asilimia 92 ya mahitaji ya silaha.

Tanzania, ambayo inaongoza katika mapambano dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi Afrika Kusini, imepata msaada wa kiuchumi kutoka nchi za kisoshalisti. Ilipofikia 1976 ilikuwa imepata dola 40 milioni kutoka Shirikisho la Sovieti, ikiongezwa na dola 13 milioni kutoka nchi za Ulaya Mashariki. Biashara kati ya Tanzania na dunia ya kisoshalisti imekuwa ya wastani. Tanzania imepeleka hasa tumbaku na pamba kwenye nchi za Sovieti, kubadilishana na hasa zana na magari.[64] Kutokana na msimamo wa Tanzania wa kuupinga ukoloni, nchi za kisoshalisti zimeipa msaada mkubwa wa kijeshi kuisaidia kujilinda dhidi ya utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini.

Kwa upande wa Zambia, msaada wa nchi za Sovieti ulikuwa mdogo hadi 1976. Baada ya hayo hata hivyo, Shirikisho la Urusi liliipatia nchi hiyo msaada wa kijeshi wa thamani ya dola 100 milioni ili kuisaidia ijilinde dhidi ya Afrika Kusini. Rais Kaunda alishukuru sana kwa msaada huo, na shukrani hizo alizitoa kwa maneno yafuatayo: "Shirikisho la Urusi limekuwa rafiki wa Zambia daima."[65]

Huko Afrika Kusini na Kati, kama ilivyokwishaelezwa awali, nchi za kisoshalisti zilitoa msaada wa kiuchumi na kijeshi kwa vyama vya ukombozi vya Msumbiji, Angola na Zimbabwe, hivyo kuviwezesha kupata uhuru. Dola 2 bilioni zilizotolewa

[62] C. Stevens 1976, uk. 259
[63] J. Mulirai, 1983, uk. 51
[64] Daily News (Tanzania), Machi 25, 1977; News Agency, Machi 27, 1977
[65] Times of Zambia, 1977

kwa Angola na Shirikisho la Urusi chini ya makubaliano ya Ushirikiano kati ya Sovieti na Angola ya 1982 zilikuwa ndio mkopo mkubwa uliowahi kutolewa kwa nchi ya Afrika. Ulikuwa na madhumuni ya kugharimia mipango mbalimbali ya maendeleo.[66] Viongozi wa vyama vya mapambano ya msituni vya ANC na SWAPO wametoa shukrani zao kwa msaada wa kiuchumi na kijeshi walioupata kutoka nchi za Sovieti.[67]

Kutokana na umuhimu wake wa kimkakati na kiitikadi, Ethopia pia ilipata msaada mkubwa wa kiuchumi, kiasi cha dola 100 milioni mnamo 1974. Msaada huu uliiwezesha kugharimia mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusafishia mafuta.[68] Baada ya mapinduzi, ushirikiano baina ya Ethiopia ya Kisoshalisti na nchi za kisoshalisti ulikua sana 1979, kwa mfano, nchi hizo zilipokea wanafunzi wa Kiethiopia zaidi ya 3,500, idadi kubwa zaidi ya nchi nyingine yoyote ya Afrika.[69] 1978 biashara iliongozeka mara 15. Katika uwanja wa kijeshi, Shirikisho la Sovieti lilitenga kwa ajili ya Ethiopia wakati wa vita vya Ogaden silaha za thamani ya dola 1 bilioni, zaidi ya washauri 1500 wa kijeshi wa Sovieti waliokuwa Ethiopia wakati huo na takribani askari wa Kuba 20,000. Mwaka 1981 msaada wa Sovieti kwa ajili ya Addis Ababa ulikuwa kiasi cha dola 1.5 bilioni.[70] Ethiopia kwa hivyo ikawa bila kupingwa nchi inayoongoza katika kupokea msaada wa kijeshi kutoka Sovieti katika bara hili, isipokuwa kwa misaada ya Misri ya mwanzoni mwa miaka ya 1970. Hali hii iliiwezesha Ethiopia kujenga uwezo usio na kifani wa kujilinda dhidi ya maadui zake, Somalia, na katika migogoro yake ya ndani dhidi ya makundi yaliyotaka kujitenga pamoja na maadui zake wa ndani.

Sera ya misaada ya kiuchumi ya China kwa nchi zinazoendelea ni tofauti kidogo kwa upande mwingine ikilinganishwa na nchi nyingine za kisoshalisti, na, kulingana na maofisa wa Kichina, inatokana na kanuni zifuatazo: msaada unaotolewa uwe na manufaa kwa pande zote mbili, mtoaji na mpokeaji, ambaye uhuru wake ni lazima uheshimiwe, unatolewa bure kwa nia ya kuhakikisha kuwa mpokeaji anajitegemea baada ya hapo; inawekezwa katika miradi ambayo inalipa; ubora wa bidhaa zinazotolewa unazingatiwa; mafundi wenyeji ni lazima wafunzwe kuendesha miradi inayotekelezwa kwa msaada wa wataalamu wa Kichina na

[66] Radio Lisbon, katika African Research Bulletin, Januari 14 – Februari 14, 1982, uk, 6324
[68] *New Chine News agency*, Julai 5, 1981; *Afircan researcha Bulletin*, Julai 1-31 1979, uk.6122
[69] *African Research Bulletin*, Julai 1-31 1979, uk 5355
[70] *African Research Bulletin*, Machi 1-31 1981, kur. 6002-3; *Tass*, Mei 8-10 1977

wataalamu wa China ni lazima wapate marupurupu yaleyale kama wataalamu wenyeji. China hushikilia kwa makini kanuni hizi za ushirikiano wa kiuchumi na Afrika.

Kwa jumla, China imekuwa tayari zaidi kutoa msaada wake kwa nchi zenye mwelekeo wa kisoshalisti zinazofuata sera ya kujitegemea, kama vile Tanzania. Lakini kwa sababu za kiufanisi zimetoa misaada kwa nchi zenye mwelekeo wa Kimagharibi zinazopingana na Umoja wa Sovieti kama[71] Zaire na Ethiopia ya kabla ya 1974. Madhumuni ya msaada wa China kwa Afrika yanaelekea kuwa ni kufuta au angalau kupunguza athari ya Marekani na Sovieti katika bara hili, au kuungwa mkono katika mikusanyiko ya kimataifa kama Umoja wa mataifa, Umoja wa Nchi zisizofungamana, na Umoja wa Urafiki wa watu wa Afrika na Asia, na mwishowe kuisaidia Afrika kukomesha ubeberu na kufanikiwa kujitegemea kiuchumi. Kwa upande mwingine, Beijing imejitahidi kuungwa mkono na bara la Afrika katika mapambano yanayoendelea kuelekea katika mapinduzi ya kimataifa. China, kama inavyodai katika kuongoza nchi za Dunia ya Tatu, ina wajibu wa kuwa na ukarimu katika kuwasaidia wenzake walio wanyonge zaidi, na hasa nchi za Afrika.

Ukarimu dhahiri wa China unaweza kuonyeshwa kutokana na ukweli kwamba tangu 1956 hadi 1977 ilitoa kwa bara hili msaada wa dola 1.4 bilioni ambazo ni asilimia 50 ya jumla ya msaada wa China kwa nchi zote zisizo za kisoshalisti.

Wapokeaji wakubwa wa msaada wa China kwa Afrika Magharibi walikuwa Ghana, Sierra Leone, Gambia na Nigeria na, katika Pembe ya Afrika, Somalia na Ethiopia. Katika kundi la kwanza la nchi, msaada huo ulitumiwa kwa ajili ya miradi ya kilimo na kujenga madaraja na, katika kundi la pili, kwa ajili ya ujenzi wa barabara huko Somalia na viwanda vya nguo huko Ethiopia.[72]

Uganda ilipata msaada wa fedha na kiufundi kutoka China uliotumika kwa ajili ya mradi uliofanikiwa una upandaji mpunga.[73] Kenya ilipata mkopo wa dola 16.8 milioni na ruzuku ya dola 3.1 milioni. Ilipatiwa pia dola 40 milioni kujenga uwanja wa kisasa wa michezo.[74] Mradi mmojawapo ulioendeshwa Kenya kwa msaada

[71] Taz. W. Partke, 1975, kur. 9-12; na A, Lawrence, 1965, kur, 173-4

[72] Taz. *New China Agency*, Februari 13 1973; *West Afrika* (London), Februari 20 1978; *New China News Agency*, Februari 15 1978; na W. Partke, 1975, uk. 113.

[73] *Radio Kampala*, Mei 1 1965; na *New China News Agency*, na. 22, 1973.

[74] *Standard of Kenya*, Septemba 17 1980.

wa China ulihusu tasnia ya mianzi. Zimbabwe, ambayo Waziri wake mkuu aliungwa mkono kwa dhati na China wakati wa vita vya msituni, ilikuwa mojawapo ya wapokeaji wakubwa wa msaada wa China kwa Afrika, ikipata jumla ya dola 82 milioni kwa ajili ya miradi mikubwa mbalimbali ya maendeleo.[75]

Hata hivyo, mpokeaji mkubwa kabisa wa msaada wa China kwa Afrika ni Tanzania, ambayo ina sifa maalumu ambazo zinaipendeza China. Sifa hizo ni pamoja na mapambano ya bila kuchoka ya chama tawala dhidi ya ubaguzi wa rangi. Vilevile, ni pamoja na msimamo wa TANU na hapa baadaye CCM (Chama cha Mapinduzi) wa kupinga ukoloni na kuunga kwake mkono vyama vya ukombozi, sifa hiyo iongezwe katika wasifu wa Tanzania katika uwanja wa kimataifa (kwa mfano kuilazimisha Marekani kufunga kituo chake cha utafutaji wa satelaiti kisiwani Unguja); na sera yake ya ujamaa na kujitegemea, ambayo ina msingi sawa na falsafa inayofuatwa na China.[76] Kwa ufupi, Tanzania inaonekana kwa China kuwa "mshika bendera adhimu dhidi ya ubeberu mkongwe na wa mamboleo".[77] Na Tanzania imeikaribisha China kwa mikono miwili, kwani imeiangalia kama mlinzi wa watu waliotawaliwa na wakoloni na waliokandamizwa.[78] Msimamo huu wa kutangamana baina yao ulizifanya nchi hizi mbili ziwe marafiki asilia.

Ilipofika 1977 China ilikuwa imetenga dola 362 milioni za msaada kwa Tanzania kutokana na jumla ya dola 2.5 bilioni zilizotolewa kwa bara zima la Afrika. Hii iliifanya Tanzania iwe nchi inayoongoza katika kupokea msaada wa China kwa Afrika. Ilipofikia 1971 China ilikuwa ikiongoza katika nchi wahisani, na msaada uliopokelewa na Tanzania ulizidi misaada yake ilizopokewa kutoka kwa wahisani wengine, ikiwa ni pamoja na mchango wa nchi tajiri. Sehemu kubwa ya msaada huo ilitumiwa kugharimia mradi wa TAZARA ambao uligharimu Tanzania na Zambia jumla ya dola 456.3 milioni, zilizogawiwa sawasawa baina ya nchi hizo mbili. Sehemu nyingine ilitumika kwa ajili ya miradi mikubwa mbalimbali hasa ya kilimo, mawasiliano, huduma za afya na elimu.[79]

Msingi mkuu wa Sera ya biashara ya China ni kugharimia msaada kwa biashara kwa mfano, asilimia 60 ya mkopo uliotolewa kwa ajili ya TAZARA ulikuwa ni wa


[75] *New China News Agency*, Septemba 18 1981; na *Africa Research Bulletin*, Desemba 15 1982 Januari 14 1983.

[76] *Xinhua News Bulletin*, 1968, kur. 5-6 na 15

[77] *New China News Agency*, Jui 5 1965.

[78] J.K. Nyerere, 1967d; taz. Pia G.T.Yu, 1975, uk. 7

[79] G.T. Yu, 1975, uk. 80



PICHA 27.3 *Reli ya Uhuru iliyojengwa na Wachina: Tanzania-Zambia; wakitandaza reli katika mpaka wa Tanzania na Zambia; Novemba 1973 mbele ya maofisa wa Kichina na Rais Nyerere wa Tanzania na K. Kaunda wa Zambia.*

muundo wa bidhaa zilizoletwa kuuzwa Tanzania na Zambia.[80] Tanzania ilipeleka tumbaku, mbata na mkonge, ili kubadilishana na bidhaa za viwandani na dawa. Licha ya uhusiano huu mzuri kati ya nchi hizi mbili, nchi za Magharibi zilibakia kuwa mshirika mkubwa wa biashara wa Tanzania; tangu 1970 hadi 1977, asilimia 63 ya bidhaa zake zilizopelekwa nje zilikwenda nchi za Magharibi na asilimia 49 ya bidhaa zake zilizoingizwa.[81]

Uamuzi wa kujenga reli inayounganisha Tanzania na Zambia ulichukuliwa kama ilivyoelezwa, baada ya tawala za wachache za Rhodesia na Afrika Kusini kutishia kukata mawasiliano yote na Zambia isiyokuwa na njia ya kutokea nje. Umuhimu

[80] *Tanzania Standard* (Dar es Salaam), 26, 1976.
[81] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, uk. 40.

wa TAZARA kwa nchi hiyo na vuguvugu zote zinazopinga ukoloni na ubaguzi wa rangi ni wa wazi. Ulielezwa na Waziri Mkuu wa Tanzania kama ifuatavyo:

TAZARA ni mradi wenye hadhi ya pekee Afrika na duniani ni mfano wa msaada unaotolewa kwa mwingine kwa nia ya wema na manufaa ya wote. Hadhi ya TAZARA ni ushindi wa ushirikiano baina ya nchi za Dunia ya Tatu.[82]

Reli hii ya urefu wa maili 1278 ilijengwa na Wachina 15,000 na wafanyakazi wa Kiafrika 30,000, waliomaliza kuijenga 1975, kabla ya wakati uliopangwa. Mkopo ulianza kurudishwa mwaka 1983 kwa kutumia fedha zinazobadilishika kwa urahisi au kwa njia ya bidhaa zibazokubalika China.[83] Mkopo wote ulitarajiwa kurejeshwa katika kipindi cha miaka 30. Haya yalikwa ni masharti mazuri ambayo mpokeaji wa mkopo angeweza kutarajia kupewa na mhisani wa nje. Hata wakati ambapo uendeshaji wa reli ulionyesha hasara ya dola 100 milioni mwaka 1983, kutokana na uwezo mdogo wa uchukuaji mizigo, China ilikubali kutoa msaada wa ziada wa kununulia vichwa vipya kutoka Ujerumani Magharibi na iliweka ratiba mpya ya ulipaji, matokeo yake ni kwamba reli hiyo ilipata faida kwa mara ya kwanza Novemba 1983.[84]

Katika uwanja wa jeshi, Tanzania, kutokana na uhusiano wake maalumu na China, ilipata katika kipindi cha 1967-76 msaada unaokisiwa kuwa dola 75 milioni, ukiwa ni mkubwa zaidi (asilimia 51) katika misaada ya China kwa Afrika. China ilitoa msaada wa kijeshi kwa nchi nyingine za Afrika, hasa Msumbiji, Kameruni na Zambia.

Kwa ufupi, dunia yote ya kisoshalisti, nchi za Kisovieti na pia China, zimetoa msaada wa kiuchumi, kiufundi na kijeshi kwa njia mbalimbali kwa nchi nyingi za Afrika, na msaada huu, uliowawezesha kuwa na njia tofauti na uhisani wa nchi za Magharibi, ulipunguza kutegemea kwao wakoloni wao wa awali na umeiwezesha Afrika kufanya miradi kadha mikubwa ya maendeleo (elimu, viwanda na kilimo) na kwa ajili ya ulinzi.

Uadui wa Kimataifa katika Uhusiano wa Afrika na Nchi za Kisoshalisti

Uhusiano wa kisiasa, kiuchumi na kijeshi baina ya Afrika na nchi za kisoshalisti ulisaidia sana kuongeza uhasama mkali uliokuwapo baina ya madola makuu mawili na Jamhuri ya Watu wa China. Katika matukio mengi Afrika imeleta uhasama

[82] *Peking Review*, na.38, Septemba 22 1978.
[83] G.T. Yu, 1975, uk. 127.
[84] *Africa Now*, 1983; *Africa*, 1984, kur. 18-19.

ama kwa kudhamiria au kwa bahati mbaya. Kwa mfano, migongano inayoendelea ya kimbari au kimkoa katika nchi nyingi za Afrika, ambayo imesababisha kutokuwapo kwa utengamano, imetumiwa na mataifa yenye nguvu yanayopingana. Mgogoro wa Angola, vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Nigeria na mgongano wa Ogaden ni mifano dhahiri. Raslimali ya madini ya Afrika – boksiti, almasi, mafuta na kadhalika – masoko yake yenye utajiri na nafasi ya kimbinu ya bandari na viwanja vyake vya ndege imeifanya iwe mojawapo ya maeneo muhimu ya ulimwengu yanayotamaniwa sana na wenye nguvu duniani. Kisiasa, nchi za Kiafrika zilizoamua kufuata njia ya maendeleo isiyo ya kibepari zimeshutumiwa na nchi zenye nguvu za kibepari za Magharibi, ambazo zimeweka tawala zinazowapendelea wao. Serikali inayopendelea zaidi Magharibi ya Kenya, kwa mfano, imepata msaada mkubwa kutoka Magharibi dhidi ya vyama vinavyoonekana kuwa vya kisoshalisti kama *Kenya People's Union*. [Chama cha Watu wa Kenya]. Ghana ya utawala wa Nkrumah ilinyimwa msaada wa nchi nyingi za Magharibi kwa sababu ya msimamo wake mkali wa kupendelea usoshalisti; katika Pembe ya Afrika, tawala zilizosaidiwa na Wasoshalisti zilipingwa na tawala zilizopendelea Magharibi na kinyume chake pia. Nchi za Kisoshalisti kwa upande wake zilijaribu kuzisaidia na kuziunga mkono tawala zilizopendelea usoshalisti, kama vile Guinea, Mali, Angola na Ethiopia. Mataifa yenye nguvu duniani yanauangalia ukomunisti na uingiaji wa nchi za Magharibi Afrika kwa jicho la kiulimwengu, uadui wa kiulimwengu wa Mashariki na Magharibi na hawafichi ukweli kwamba hiyo huwatia hofu. Kama Ali Mazrui anavyoona:

> itikadi ya kimapinduzi – uMarx – yenye wakili mwenye nguvu – USSR – ikawa ni kitu ambacho mataifa makubwa ya Magharibi wanazidi kukiogopa...ushindani wa kiitikadi na kisiasa baina ya USSR na mataifa ya Magharibi uliongezeka...[85]

Katika juhudi zake za kuathiri bara hili kisiasa, China imegongana na mataifa makubwa ya Magharibi kama ilivyokuwa kwa USSR, zote zikishindana kwa nia ileile. Kutokana na tofauti za kiitikadi dhidi ya USSR, China, licha kuwa nayo ni nchi ya kisoshalisti vilevile, ilivikosoa baadhi ya vipengele vya Sera ya Sovieti kuhusiana na Afrika na iliichukulia USSR kama tu mojawapo ya mataifa yenye nguvu ya Ulaya yanayolikandamiza bara la Afrika.[86] Na USSR kwa upande

[85] A.A. Mazrui, 1977, kur. 179-80

[86] *New China News Agency*, Desemba 27 1967 na Julai 3 1977.

wake iliishutumu China kwa kuanzisha malumbano ya ubaguzi wa rangi katika kukosoa sera yake kuhusiana na Afrika.[87]

Maeneo mengi ya Afrika yametaabishwa na uadui wa kimataifa, lakini hali hiyo imeonekana zaidi Angola na Pembe ya Afrika. Msumbiji imepata taabu sana kutokana na chama cha Upinzani kinachoungwa mkono na Afrika Kusini - *Mozambique National Resistance* (RENAMO) – lakini hakujawa na majeshi ya Kuba ya kuitetea FRELIMO.

Kipengele muhimu cha kukumbuka ni sera iliyofuatwa na Angola ya kuwa vyama vya kitaifa vya huko vimekuwa vikiungwa mkono tangu mwanzo na mataifa makubwa na kwamba hali hiyo iliendelea hata baada ya kupata uhuru. Nchi za Kisovieti, ikiwa ni pamoja na Kuba, siku zote ziliunga mkono MPLA, ambapo nchi za Magharibi, hasa Marekani, zimekuwa zikiunga mkono FNLA na UNITA. Ushindani kati ya pande hizo mbili huko Angola ulikuwa dhahiri kuwa ulitokana na raghba za kiitikadi na kimkakati.

[87] G.V. Astafyev na A.M. Dubinsky, 1974, kur. 112-14

Katibu wa Nchi wa zamani wa Marekani, Henry Kissinger, alichukulia uingiliaji kati wa nchi za Sovieti Angola katika maudhui ya uadui wa kiulimwengu baina ya Marekani na USSR na aliilaumu Kremlin kwa kuanzisha na kushadidia mgogoro huo.[88] Alitetea uingiliaji kati wa Marekani kuwa madhumuni yake yalikuwa ni kuisawazisha hali. Mataifa makubwa ya Magharibi kwa hiyo yalijitolea kuwapatia wapiganaji wa msituni wa FNLA na UNITA msaada unaolingana na walioupata MPLA kutoka USSR. Wasovieti na Wakuba kwa upande wao walitetea kuiunga kwao mkono Angola na kuwepo kwao nchini hapo kwa msingi kwamba watu wa Angola waliomba ulinzi wao dhidi ya mashambulizi ya mabeberu.[89] Tangu wakati huo nchi nyingine zimejiruhusu fulani, na Afrika Kusini, ambayo imeingilia kati moja kwa moja vita vya ndani upande wa UNITA kwa kisingizio kwamba wanailinda Namibia dhidi ya wapiganaji wa msituni wa SWAPO walioshambulia kutoka Angola na kuzuia uMarx usiingie katika eneo hili.

MPLA, ambayo inafuata itikadi ya Marx, ilikubali kwa urahisi msaada kutoka nchi za kisoshalisti, ambapo UNITA, kikundi cha wapiganaji wa msituni kinachopendelea Magharibi, kilipata msaada kutoka Magharibi na Afrika Kusini kupinga madaraka ya MPLA. Lakini zaidi ya sababu hizi za kiitikadi, kuwepo kwa madini ya urani na mafuta huko Angola kunahusishwa na kujishughulisha kwa mataifa makubwa ya nje na nchi hiyo. Marekani, ambayo ilijishughulisha kiuchumi Zaire, Namibia na Afrika Kusini, iliona hatari itakayotokea katika eneo hili kwa USSR kujishughulisha na uchumi wa Angola. Mwishowe, katika kiwango cha kimkakati, Angola iko mahali pazuri kwa sababu mbalimbali. Pwani na bandari zake zilizoko kwenye Bahari ya Atlantiki ni muhimu kwa mataifa yenye majeshi ya wanamaji katika nchi za NATO na kundi la makubaliano la Warsaw.[90]

Matokeo ya kimkakati ndiyo yaliyoshughulisha sana mataifa makubwa hadi karibuni kutokana na kuongezeka kwa mashindano ya silaha, yaliyohitaji suhula mpya za anga na bandari kwa ajili ya majeshi yao ya majini na ya anga. Pembe ya Afrika inatoa mfano mzuri katika bara hili kuhusu kushamiri kwa uadui wa kimataifa katika mahitaji ya kimkakati. Ukweli ni kwamba ina umuhimu wa kimkakati kwa nchi za kisoshalisti kama ilivyo kwa nchi za kibepari kwa sababu ya nafasi yake kama kiungo cha Asia na Afrika, suhula zake nzuri mno za bandari katika Ghuba

[88] R. Lemarchand, 1981, uk. 83.
[89] New Times, Februari 1 1976, uk. 1
[90] B. Hanler, 1970

ya Aden na Bahari ya Hindi na, zaidi ya yote, ukaribu wake wa njia muhimu za baharini zinazounganisha nchi zinazozalisha mafuta na Amerika na Ulaya, ambazo hupitisha asilimia 70 ya mafuta na mali ghafi nyingine zipelekwazo Ulaya Magharibi.[91]

Kuwepo kwa majeshi makubwa ya majini ya Marekani ambayo yangeweza kutumiwa kuishambulia USSR iliifanya Kremlin kutafuta suhula za bahari na viwanja vya ndege katika Pembe ya Afrika kwa ajili ya jeshi lake la majini lililoongezeka katika Bahari ya Hindi. Zaidi ya asilimia 60 ya meli zake zilizozuru eneo hili zilisemekana kuwa zilikuwa zikitia nanga kwenye bandari za Pembe ya Afrika na Ghuba ya Aden.[92] Kutokana na kustushwa na kuwepo kwa suhula za mawasiliano na ulinzi za Kimarekani huko Kagnew, Ethiopia, USSR iliongeza msaada wake wa kiuchumi na kijeshi kwa Somalia na kubadilishana na madaraka ya kutumia bandari muhimu ya Berbera, karibu na mlango muhimu kimkakati wa Bab el-Mandeb ambako meli zote hupitia kutoka Bahari ya Shamu. Taifa kubwa linalodhibiti sehemu hiyo ya Bahari ya Shamu lingekuwa na uwezo wa kuamuru mabadiliko na kuwa na athari juu ya Pembe ya Afrika na Mashariki ya Kati. Hivyo Marekani na marafiki zake waliingiwa na wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa kuwapo kwa USSR katika Bahari ya Hindi na bandari zake.[93]

Uadui wa mataifa makubwa ambayo yalitaka kuathiri Pembe za Afrika ili kuidhibiti ilikuwa ni mojawapo ya sababu ya kuanza kwa Vita vya Ogaden 1977. Ukweli ni kwamba msaada mkubwa wa kijeshi uliotolewa kwa Ethiopia na Somalia na nchi za Mkataba wa Warsaw na NATO ulizihamasisha nchi hizo mbili jirani kusuluhisha migongano yao kwenye uwanja wa vita. USSR na marafiki zake waliishutumu Marekani kwa kuunga mkono matamanio ya Somalia ya kuunganisha mbari dhidi ya Ethiopia kwa kubadilishana na vituo walivyopewa Berbera na Mombasa kwa ajili ya Majeshi ya Dharura, yaliyoanzishwa muda mfupi kabla kutia hofu uhusiano uliokuwa ukijengeka baina ya USRR na Afrika.[94] Kwa upande mwingine Marekani iliushutumu Umoja wa Sovieti na Kuba kwa kuhusika na migogoro kwenye ukanda huo, ikiitahadharisha USSR kuwa kama hali hiyo ikiendelea uhusiano baina ya USSR na Marekani utaathirika, hasa Mazungumzo ya kupunguza silaha za kimkakati (SALT).[95]

[93] S. Turner, 1977, uk.346

[91] Christian Science Monitor, Machi 23 1978.

[94] Radio Moscow, Desemba 17 1982, kwenye Africa Research Bulletin, 1 - 31 Desemba 1982, uk.6688

[95] Africa Research Bulletin, Desemba 1 - 31 1978, uk.4775.

Viongozi mbalimbali wa Afrika kwenye mkutano wa wakuu wa nchi uliofanyika Khartoum 1978, hasa Obasanjo wa Nigeria, walisikitishwa na uadui wa kimataifa uliokuwapo kwenye bara hili, na maoni hayo yalirudiwa pia na Sékou Touré na Nyerere.[96]

Uadui wa mara kwa mara baina ya mataifa makubwa huwa ni wa madhara tu kwa maendeleo ya Afrika.

## Afrika Isiyofungamana na Upande Wowote na Ulaya Mashariki: Nchi za Kisoshalisti na Tapo la Kutofungamana na Upande Wowote

Aghalabu huchukuliwa kuwa nchi za kisoshalisti ni sehemu ya kile kinachoitwa "Jumuiya ya Mashariki" tu. Si hivyo mara zote. Nchi za Kisoshalisti zimekuwa pia sehemu ya Tapo la Nchi Zisizofungamana, na walioanzisha tapo hilo ni pamoja na Yugoslavia iliyokuwa chini ya Marshal Tito. Tito, Nehru, al-Nasser na Nkrumah wakawa ndio wasanifu na watangulizi wa mkakati unaoitwa mara nyingine "kutoelemea kokote kuliko chanya," na ambako ndiko kulikokuwa msingi wa sera ya mambo ya nje ya kila nchi ya Afrika iliyokombolewa.

Kwa kweli, Yugoslavia ilikuwa ni nchi ya kwanza iliyofanya tapo la kutofungamana na upande wowote kuwa tapo la kiulimwengu badala ya kuwa jina jingine tu la urafiki wa Afrika na Asia. Mkutano wa Bandung wa 1955 ulikuwa ni hatua muhimu katika kuunda urafiki baina ya nchi za Asia na Afrika, ingawa ulifanyika miaka miwili kabla ya uhuru wa Ghana. Kama Tapo la Kutofungamana na Upande Wowote lingeanzishwa na Nehru (India), al-Nasser (Misri) na Nkrumah (Ghana), lingeonekana kuwa ni tapo la mataifa yasiyo ya kizungu ya Afrika na Asia. Alikuwa mzungu, Tito, aliyetayarisha njia kwa wanachama wasio wa rangi kama Kupros na baadhi ya nchi za Amerika Kusini. Mpaka ilipofikia Mkutano wa Havana wa 1979, tapo la nchi zisizofungamana lilikuwa na wanachama 95 waliotoka kwenye mabara manne ya dunia.

1986, Mkutano wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote ulifanyika Harare - mahali pa kwanza kusini mwa Sahara. Robert Mugabe, mwenyewe akiwa msoshalisti na ambaye chama chake cha ukombozi ZANU kilipata ushindi wa kijeshi dhidi ya Ian Smith kwa msaada wa nchi za kisoshalisti, akawa mwenyekiti

[96] African Currents (London), Mpukutiko majani 1978/Kipupwe 1979, kur.8-23

wa nguvu ya kimataifa ambayo hapo awali iliongozwa na Tito, Nehru, Nkrumah na al-Nasser.

Kulikuwa na wakati ambapo msimamo wa kutofungamana na upande wowote ulikuwa hauwezekani baina ya Ujerumani Magharibi na Mashariki. Itikadi ya Hallstein ya Jamhuri ya Shirikisho ya Ujerumani ililazimisha nchi za Afrika kuchagua kati ya Ujerumani hizo mbili. Wakati Zanzibar (iliyotambua Ujerumani Mashariki), ilipoungana na Tanganyika (iliyotambua Ujerumani Magharibi), tatizo la kweli la kidiplomasia liliibuka. Julius Nyerere akiwa rais wa Jamhuri mpya ya Muungano wa Tanzania alijaribu kulitatua kwa kuiacha Ujerumani Mashariki iwe na ubalozi mdogo Zanzibar huku Ujerumani Magharibi ikiwa na ubalozi Dar es Salaam. Jamhuri ya Shirikisho ya Ujerumani ilipopinga hata mwafaka huo, vitendo vya Nyerere vilichangia katika kuangalia upya Itikadi ya Hallstein, angalau kama inavyotumika katika Dunia ya Tatu. (Itikadi hiyo ilikuwa imeundwa kuzilazimishwa nchi zote za Dunia ya Tatu zaidi ya USSR kuchagua baina ya Ujerumani mbili katika kuwa na uhusiano wa kibalozi.) Baada ya muda, Jamhuri ya Shirikisho ilibadilisha msimamo wake, kuanzia na Sera za kuafikiana za Willie Brandt kuhusiana na urafiki na Mashariki kwa jumla. Afrika ikaondolewa adha ya kuchagua baina ya Jerumani mbili - ingawa tatizo la kuchagua kati ya Jamhuri ya Watu wa China na Taiwan liliendelea kuwa tata kuliko kupungua miaka ilivyozidi.

Nchi ndogo za Ulaya Mashariki ziliisaidia Afrika katika kutofungamana na upande wowote kwa njia tofauti. Baadhi ya nchi za Afrika zilitaka kuleta urari katika uhusiano wao wa kiutamaduni kati ya Mashariki na Magharibi. Poland ikawa ni mahali pazuri pa kupata wafanyakazi kwa ajili ya vyuo na vyuo vikuu vya Afrika. Idara nyingi katika asasi za elimu ya juu za Afrika zilikuwa na maprofesa na watafiti wageni kutoka Poland. Czechoslovakia na Hungary pia zilikuwa muhimu katika elimu ya juu ya Afrika, hasa katika udhamini wa wanafunzi wa Kiafrika waliosoma katika nchi hizo. Hata hivyo, nchi za Ulaya ya Mashariki hazikuweza kuzipita nchi za Ulaya Magharibi katika kuiathiri Afrika. Ingawaje maendeleo ya urari wa kiutamaduni ulisaidiwa na uhusiano wa kisayansi, kitaaluma na kiutamaduni kati ya Afrika na upande wa ki-Marx wa urithi wa Ulaya.

Kulikuwa na kutofungamana na upande wowote hata katika uchaguzi wa suhula za tiba wakati Waafrika walipopata maradhi yasiyotibika. Watu watatu muhimu katika historia ya Afrika walikwenda upande tofauti wa Vita vya Baridi kwa ajili ya tiba ya maradhi yao yasiyotibika. Kwame Nkrumah alikwenda Romania katika mapambano yake ya mwisho na kansa ya ngozi - na alifia huko 1972. Franz Fanon

alikwenda Marekani katika vita vyake vya mwisho dhidi ya lukemia na alifia huko. Rafiki mkubwa wa zamani wa Kwame Nkrumah, Sékou Touré - alikwenda Marekani kifo kilipomkabili. Alifia Cleveland, Ohio. Maradhi na kifo haviheshimu mipaka ya kiitikadi - na sayansi, katika ulimwengu wake, ndio muundo mzuri kabisa wa kutofungamana na upande wowote.



Picha 27 4 Majeshi ya Kuba huko Angola

## Hitimisho

Kama miaka ya 1960 ilikuwa ni muongo wa mabadiliko makubwa Afrika, miaka ya 1980 ilikuwa ni muongo wa mabadiliko makubwa ya dunia ya kisoshalisti. Badiliko la msingi la Afrika katika miaka ya 1960 lilikuwa kujikomboa dhidi ya ukoloni - kwani zaidi ya nusu ya bara hili lilipata madaraka ya kujitawala katika muongo huo. Badiliko kubwa kabisa la dunia ya kisoshalisti katika miaka ya 1980 lilikuwa uchumi huria - ukiwa na majina ya *glasnost* na *perestroika* katika Shirikisho la Sovieti, lakini likiwa na majina mengine kote tangu Beijing hadi Budapest.

Hakuna shaka kwamba kujikomboa na ukoloni kwa Afrika katika miaka ya 1960 kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na uhusiano wa Afrika na dunia ya kisoshalisti. Kwa vile, uhuru rasmi wa Afrika uliiwezesha nchi moja baada ya nyingine ya Afrika kuanzisha uhusiano wa kibalozi na nchi za kisoshalisti. Lakini kama ukombozi wa Afrika dhidi ya ukoloni katika miaka ya 1960 ulibadili uhusiano na dunia ya ki-Marx, je uchumi huria wa dunia ya ki-Marx wa miaka ya 1980 ulibadili uhusiano wake na Afrika?

Kwa upande wa USSR, uchumi huria chini ya Mikhail Gorbachev mwishoni mwa miaka ya 1980 uliathiri sera ya mambo ya nje pamoja na siasa za ndani. Msimamo mpya wa Sovieti ulijaribu kuepuka migongano na Magharibi, kupunguza nguvu za kivita, kupunguza udhibiti wa mamlaka ya Ulaya Mashariki na kutuliza migongano ya ukanda huo. Hakuna shaka kwamba Shirikisho la Sovieti lilikuwa na athari kwa Kuba na Angola katika kukubali kuhusishwa kwa kuondolewa kwa majeshi ya Kuba huko Angola na Uhuru wa Namibia. Makubaliano ya 1988 kati ya Angola, Kuba na Jamhuri ya Afrika Kusini hayakuwa matokeo ya juhudi za katibu mkuu msaidizi wa nchi wa Marekani, Chester Crocker, pekee. Makubaliano ya Afrika ya Kusini yalikuwa pia matokeo ya athari ya *perestroika* juu ya sera ya mambo ya nje ya Sovieti. Kwa upande wa Namibia, makubaliano hayo yalikuwa mafanikio kwa Umoja wa Mataifa [UN) baada ya miaka mingi ya shinikizo la UN na jumuiya ya kimataifa kwa Afrika Kusini kwa niaba ya watu wa Namibia.

*Maelewano* mpya kati ya jumuiya ya Sovieti na washirika wa Magharibi katika miaka ya 1980 ulikuwa na madhara na faida vilevile. Baadhi ya misaada iliyotolewa na nchi za nje ambayo ilitoka kote kuwili kwenda Afrika ilitokana na msukumo wa kiitikadi na kimkakati wa uadui baina ya pande hizo mbili. Kama uadui kati yao ungepungua, je kungekuwa na msukumo mdogo zaidi wa kutoa kiwango kilekile cha msaada? Ni kweli, amani kati ya mataifa makubwa hayo mawili ilikuwa ni

habari njema kwa kila mtu lakini je, kungekuwa na ukarimu mdogo zaidi kwa nchi za Dunia ya Tatu kwa sababu hiyo?

Madhara mengine yanayotokana na *maelewano mapya* kati ya Magharibi na dunia ya ki-Marx yalihusu msaada wa baadaye wa Sovieti kwa mapambano ya ukombozi ya Jamhuri ya Afrika Kusini yenyewe. Kama msimamo mpya wa kimataifa wa Sovieti utaifanya itake zaidi kutuliza migongano ya kanda, je marafiki wa Sovieti watapunguza kuunga mkono mapambano ya kijeshi ya Dunia ya Tatu kwa jumla? Kama Sovieti iliishinikiza Vietnam kuikubalia Kambodia na *Palestine Liberation Organisation* [Chama cha Ukombozi wa Palestina] (PLO) kuwa na mwafaka na Israeli, na kama shinikizo linaloumiza moyo limewekwa kwa Shirikisho la Sovieti lenyewe kuondoka Afghanistan, je kungekuwa na shinikizo zaidi kutoka kwa wasoshalisti kwa *African National Congress* (ANC) kutoa ridhaa zaidi kwa utawala wa *kibaguzi* wa Pretoria? Je hali hii mpya ya *uhusiano* katika dunia ya ki-Marx inaongezea ugumu ANC na PAC kufuata njia ya mapambano ya kijeshi kwa ajili ya ukombozi wa Afrika Kusini?

Ni kweli, Mei 1989, Rais Gorbachev alifanya ziara rasmi Jamhuri ya Watu wa China kiongozi wa kwanza wa Sovieti kufanya hivyo katika miaka 30. Kupungua kwa mgongano wa kikanda baina ya China na Sovieti kungekuwa pia na athari kwa Afrika na si nzuri mara zote. Uadui kati ya wakomunisti hao wakubwa wawili hapo awali uliathiri sera zao za kijeshi na kiuchumi kuhusiana na misaada kwa Afrika. Msaada wa China kwa ajili ya nchi na vyama fulani vya Afrika aghalabu umetokana na ushindani wake na Shirikisho la Sovieti ni pamoja na msaada wa China kwa ajili ya Robert Mugabe na ZANU wakati wa mapambano dhidi ya ukoloni. (Shirikisho la Sovieti lilimsaidia Joshua Nkomo na ZAPU). Sasa kwa kuwa uadui kati ya USSR na Jamhuri ya Watu wa China umepungua baada ya ziara ya Gorbachev ya 1989, je aula za vya Beijing kwa Dunia ya Tatu zitapangwa upya? Je raslimali chache za Beijing zitatumiwa zaidi kwa ajili ya majirani zake wa Asia pekee? Je Afrika itapungua umuhimu wake katika sera za mambo ya nje za China?

Wakati muongo wa miaka ya 1980 ulikuwa ukifikia mwisho, haya ni baadhi ya maswali yaliyokuwa yakiulizwa na wanahistoria. Majibu ya maswali hayo hayakuwa dhahiri bado. Miaka ya 1960 ilitoa mikondo mipya katika diplomasia ya baada ya ukoloni na kubadilisha uhusiano wa Afrika na dunia ya kisoshalisti. Je nguvu zinazosukuma uchumi huria katika dunia ya kisoshalisti katika miaka ya 1980 na 1990 zitaleta awamu ya pili ya mageuzi? Kama ambavyo Karl Marx angesema,

historia ni nini kama sio ukinzani mkubwa unaojidhihirisha katika hatua yakinifu? Kama dhana ilikuwa mapambano ya kijeshi huko Kusini, dhana kinyume sasa ni *urafiki* huko Kaskazini, na dhana sanisi (unganifu) imefichwa katika tumbo la historia ya baadaye.

# 28

# Afrika na Kanda zinazoendelea

Kati ya mambo muhimu zaidi yaliyotokea baina ya katikati na mwishoni mwa karne ya ishirini ni kuzuka kwa dhana ya mataifa yanayoendelea ambayo pia huitwa "Dunia ya Tatu" au "Mataifa ya Kusini". Ingawa majina haya yote hufikiriwa kuwa yanafaa, lakini katika sura hii Dunia ya Tatu litapendelewa zaidi kwa kuwa linamaanisha sifa ambayo wanaohusika hujitambulisha nayo zaidi na pia limebakia kuwa jina ambalo mataifa na watu wa Afrika, Asia, Amerika ya Kusini na visiwa vya Karibiani hujitambulisha nalo zaidi.

Tukio hili la kukua kwa utambulishi wa Dunia ya Tatu linakuwa na uhalali zaidi tunapofikiria kuwa katika muongo wa 1940 dhana ya Dunia ya Tatu ilikuwa haijulikani; kuwa katika muongo wa 1950 hakukuwa na ama Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote au kikundi cha 77 na, pia, kuwa katika muongo wa 1960 dhana ya kipekee ya Mfumo Mpya wa Kiuchumi Duniani haikuwapo. Katika bara la Afrika, kabla ya muongo wa 1960, uhusiano na mataifa ya Asia, Amerika ya Kusini na Karibiani, kwa jumla, ulisimamiwa au kutekelezwa na tawala husika za kikoloni kutoka Magharibi.

Kwa hiyo ni muhimu kukumbuka kuwa "haiwezekani mtu kuuelewa uhalisi wa dhana ya Dunia ya Tatu ikiwa uchambuzi utajikita katika data ya kisasa tu" kwani dhana ya Dunia ya Tatu ni tukio la kihistoria ambalo ni sehemu ya utaratibu uliouzusha mfumo wa sasa wa ulimwengu ambao chimbuko lake linarudi nyuma kwa "angalao karne mbili zilizopita." Hata hivyo, Vita Vikuu vya Dunia vya Pili vilitokea kuwa mojawapo ya vipindi muhimu zaidi katika historia ya Dunia.

Lengo la sura hii ni kuchunguza, kwa kuzingatia mtazamo wa Afrika, jinsi na kwa kiasi fulani kwa nini changamoto hii ya kutoka Dunia ya Tatu ilizuka na kuimarika katika kipindi cha baada ya Vita Vikuu vya Pili na hasa kuanzia katika muongo wa 1950 na kuendelea hadi kufikia mwaka wa 1980. Sura hii inajaribu kutambua mielekeo ya jumla na taratibu kwa mtazamo wa kimabadiliko, ambazo

zinatuwezesha kuelewa upanukaji na uzidishwaji wa mawasliano kati ya Afrika na sehemu nyingine za Dunia ya Tatu na, pia, mielekeo na taratibu ambazo zinasisitiza mchango wa Afrika na athari zake katika kuanzisha na kupanua michakato ya ushirikiano kati ya nchi za Dunia ya Tatu.

## Hali na umuhimu wa Afrika katika Ulimwengu wa Tatu

Katika hatua hii, kuelezea baadhi ya sifa za hali ya Afrika za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni za wakati uliopita na za kisasa, kutasaidia katika kuonyesha vizuri zaidi umuhimu wa Afrika, kihali na kitabia, katika kundi la Dunia ya Tatu. Umuhimu huu hutokana na hali ya Afrika kama mwakilishi wa Wastani wa dhiki za kiwewe cha Dunia ya Tatu, mara nyingi katika hali iliyotiwa chumvi, na pia kutokana na uwezo wa Afrika wa kuihamasisha Dunia ya Tatu dhidi ya mfumo wa sasa wa kimataifa.

Fikra mbili muhimu za kisiasa hujitokeza. Ya kwanza ni kuwa kasi ya kuondoa ukoloni katika Afrika ilizidi baada ya Ghana kujipatia uhuru wake mnamo mwaka 1957, na ilitokea wakati mmoja na kwa kuzinduwa vuguvugu la Dunia ya Tatu kupitia misingi iliyokuwa imewekwa katika mkutano wa Asia na Afrika ulilofanywa mjini Bandung, Indonesia, Aprili 1955 (baada ya hapa tutauita Mkutano wa Bandung). Fikra ya pili ni kuongezeka kwa haraka kwa mataifa husika ya Afrika kutokana na kujipatia uhuru ambapo kuwepo kwa idadi kubwa ya mataifa huru ya Afrika katika mashirika ya Dunia ya Tatu na ya kimataifa kulisaidia kuyaweka mbele masuala ya Afrika.

Uwakilishi wa Afrika katika Mkutano wa Kwanza wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote katika mwaka wa 1961 ulikuwa tayari umefikia wanachama 11 (au asilimia 44) kati ya wanachama washiriki 25. Kufikia Mkutano wa Sita wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote katika mwaka wa 1979 wawakilishi 50 wa Afrika walikuwa ni kiwango cha asilimia 54 ya wanachama washiriki 92 waliohudhuria Mkutano huo. Uwakilishi wa Afrika katika kundi la 77 umebakia sawa sawa katika kiwango cha asili mia 41 kuanzia na wanachama 32 kati ya wanaehama waanzilishi 77 katika mwaka 1964 na kupanda hadi wanachama 50 kati ya wanachama washiriki 122 katika mwaka wa 1980.

Hata hivyo, zaidi ya Afrika kuwa na uwakilishi mkubwa na wenye uwezo katika Dunia ya Tatu, zipo sifa za kijinsi zinazoambatana na hali ya Afrika. Pahali pa kuanzia uchambuzi wa hali hii, ya Afrika, ni katika medani ya kimataifa ya kiuchumi ambapo ndipo masuala ya Dunia ya Tatu yalilengwa zaidi. Pia ni katika

*JEDWALI 28.1 Mpangilio wa Kijimbo wa Umoja wa Mataifa, 1945-80*

| Mwaka | Afrika | Asia | Karibiani | Amerika ya Kusini | Amerika ya Kaskazini | Ulaya | Bahari | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1945 | 4 | 9 | 3 | 17 | 2 | 14 | 2 | 51 |
| 1950 | 4 | 16 | 3 | 17 | 2 | 16 | 2 | 60 |
| 1955 | 5 | 21 | 3 | 17 | 2 | 26 | 2 | 76 |
| 1959 | 10 | 23 | 3 | 17 | 2 | 26 | 2 | 82 |
| 1965 | 37 | 28 | 5 | 17 | 2 | 27 | 2 | 118 |
| 1970 | 42 | 30 | 7 | 17 | 2 | 27 | 2 | 127 |
| 1975 | 47 | 37 | 10 | 17 | 2 | 29 | 2 | 144 |
| 1980 | 51 | 40 | 13 | 17 | 2 | 29 | 2 | 154 |

medani ya kiuchumi ya kimataifa ambapo Afrika ya baada ya ukoloni hudhihirisha kwa uwazi zaidi viwewe, mitanziko, na mashaka ya Dunia ya Tatu.

Inaonekana kwa urahisi kuwa idadi kubwa zaidi ya mataifa yenye maendeleo madogo zaidi ulimwenguni yamo katika bara la Afrika. Hii ina maana kuwa katika bara la Afrika ndipo "athari ya kutofaulu kwa ahadi za mikakati ya maendeleo ulimwenguni kunaonekana vizuri zaidi kuliko sehemu nyingine popote duniani." Hiyo ndiyo iliyokuwa lugha ya aya ya kwanza katika Dibaji ya azimio, ambako sasa linakuwa ya kihistoria, la *Mpango wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika, 1980 – 2000 wa Lagos* lililopitishwa na OAU mnamo mwaka wa 1980. OAU iliwasilisha wazo kuwa kutoendelea kwa Afrika sio jambo

ambalo haliepukiki na pia kuwa hali ya Afrika ni kweli – kinzani hasa inapolinganishwa na utajiri wake mkubwa wa mali za asili na wa kibinadamu. OAU iliendelea mbele na kusema kuwa sababu za kutoendelea kwa Afrika, kwa jumla, ni muundo wa unyonyaji wa kimataifa.

Uchambuzi huu wa hali mbaya ya kiuchumi ya Afrika umeshikamanishwa na fedheha fulani za kisiasa, kijamia, na kiutamaduni ambazo Afrika ilizipata katika wakati wa ukoloni na ambazo hadi sasa zingali na masalia.

Katika hotuba yake ya kufunga Kongamano la Bandung waziri mkuu wa India, Jawaharlal Nehru, aliona ni busara kusisitiza juu ya uzito wa mzigo, wa kisiasa na kijamia, ambao Afrika ilikuwa nao na kuwashauri Waasia wenzake kuutilia maanani mzigo huo. Ushauri huu hauwezi kufikiriwa kuwa jambo lisilo na maana.

Kuendelea kwa ufidhuli wa utawala wa kibaguzi katika Afrika Kusini kulilitambulisha suala hili la kijamia, kama jambo lenye aula la kundi la Dunia ya Tatu. Kutokana na chagizo za kidiplomasia, za Afrika, jambo hili liliwekwa katika sehemu ya mbele kabisa ya masuala ya kundi la Dunia ya Tatu.

Ingawa Mkutano wa Bandung wa 1955 ndiyo tarehe inayofaa zaidi ya kuanzia kwa uchambuzi wa uhusiano wa Afrika na sehemu zinazoendelea hali na shurutisho fulani za kabla ya mkutano huo ambazo zilisababisha kuzuka kwa kundi la Dunia ya Tatu na ambazo zahitaji kutambuliwa kwa sababu zina umuhimu mwingi katika hali na jukumu la Afrika katika utaratibu wa kimataifa wa walau karne iliyopita.

Jambo linaloelezea zaidi juu ya fikra za Kipanafrika kuhusu mshikamano mpana zaidi wa Dunia ya Tatu ni azimio la Mkutano Mkuu wa Weusi (Pan-African Congress) la 1945 ambalo lilizungumziwa kwa kifupi na Goerge Padmore, aliyekuwa mmoja wa makatibu wa kisiasa wa Mkutano huo. Azimio lenyewe lilielezwa kwa lugha ambayo ilitokea kuwa ya kawaida katika miaka ya mwanzoni ya Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote zaidi ya miaka kumi baadaye:

Mkutano ulitamka tumaini lake kuwa katika muda usio mrefu watu wa Asia na Afrika watakuwa wameivunja minyororo ya ukoloni wa karne nyingi. Baada ya kuwa huru, wangeungana pamoja ili kulinda haki na uhuru wao dhidi ya kurejeshwa kwa ubeberu wa Magharibi na hatari za Ukomunisti.

Kuzuka kwa kundi la Afrika katika Umoja wa Mataifa katika mwisho wa muongo wa 1950 na kuanzishwa kwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mnamo mwaka wa 1963 yalikuwa ni ishara na, pia, nyenzo za Afrika katika utafutaji wa misimamo ya pamoja juu ya mambo yaliyohusu Afrika nzima. Na kama inavyothibitishwa na mifarakano na migawanyiko mingi iliyotokea katika OAU, na ambayo nyakati nyingine ilihatarisha sana kudumu kwake, jambo hili halikuenda kwa utaratibu wa kunyooka.

Hata hivyo mifarakano isiyo mikubwa sana kati ya nchi za Kiafrika imejitokeza juu ya masuala yanayohusiana na Dunia ya Tatu ambayo yalihusiana na maslahi ya Afrika kama sehemu mojawapo ya nchi za Dunia ya Tatu.
Baadhi ya mambo halisi ya hali ya Afrika, ya wakati uliopita na wakati uliopo, yana kina kikubwa zaidi na upana ambao huyaungamisha na masuala ya Dunia ya Tatu kwa namna ambayo yanapaswa kuchambuliwa kwa kuzingatia mtazamo mmoja. Hapa pia ndipo pahali panapofaa pa hatua nyingine ya kuainisha hisia-nafsi na matumaini ya Waafrika yaliyozushwa na wa hali hiyo halisi, na kuzihamasisha nehi za Kiafrika kutafuta upanuaji wa ushirikiano wao na sehemu nyingine za Dunia ya Tatu, na pia kuchukua jukumu katika kuandaa mapambano ya Dunia ya Tatu dhidi ya utaratibu wa kimataifa uliopo sasa.

## Uhusiano kati ya Afrika na sehemu nyingine za Dunia ya Tatu

Uhusiano kati ya Afrika na Asia (Uafro-Asia) ndio mahali panapofaa kuanzia uchambuzi wa ushirikiano kati ya Afrika na sehemu nyingine za Dunia ya Tatu. Katika uhusiano huu, wa Afrika na Asia, lipo wazo la uhusiano kati ya Afrika na mataifa ya Kiarabu ambao unastahili kupewa nafasi maalum katika uchambuzi huu. Mwisho (uchambuzi huu ni muhimu kuangalia) muktadha na maudhui ya upanuzi wa uhusiano kati ya Afrika na Amerika ya Kusini na eneo la Karibiani yamedhihirisha kuimarika kwa hisia za utambulishi wa Dunia ya Tatu wenye kuvuka misingi iliyoanzishwa chini ya ushirikiano kati ya Afrika na Asia.

### Uafro-Asia kama msingi wa Dunia ya Tatu: kutoka uasisi wa Bandung hadi mshikamano wa Dunia ya Tatu.

Kama ilivyoandikwa na David Kimche, kukua kwa maslahi ya pamoja kati ya waliokandamizwa na wakoloni katika mabara ya Afrika na Asia kulikuwa kumejidhihirisha katika miaka ya baina ya Vita Vikuu vya dunia lakini kukaimarika zaidi baada ya Vita Vikuu vya Pili. Hatimaye, ukuaji ulivuka mipaka ya tajiriba za kikoloni na kuwa msingi wa kundi la Dunia ya Tatu la baada ya uhuru. Athari za utaratibu wa kujikomboa kwa nchi za Afrika na Asia juu ya uzukaji wa maslahi ya pamoja kati ya sehemu hizi mbili zaweza kutazamwa katika viwango vitano.

Kwanza, kukaribiana kiwakati wa mapambano dhidi ya ukoloni, na kuwepo kwa wakoloni wakuu walewale (Waingereza na Wafaransa) sehemu zote mbili, kuliwapa Waafrika na Waasia kutokana na usawa wa tajiriba za kikoloni zenye kufananafanana.

*Jedwali 28.2 Zilipo nchi ambazo hazijaendelea, 1981*

| | Afrika | Asia | Karibiani | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Benin | Guinea | Afghanistani | Haiti | |
| Botswana | Guinea-Bissau | Bangaladesh | | |
| Burundi | Lesotho | Blutan | | |
| Cape | Malawi | Laos | | |
| Verde | Mali | Meldiva | | |
| Afrika ya | Niger | Nepali | | |
| kati | Rwanda | Samoa | | |
| Chad | Somali | Yemen[1] | | |
| Komoro | Sudan | Yemen [2] | | |
| Ethiopia | Uganda | | | |
| Gambia | Volta ya Juu | | | |
| | Tanzania | | | |
| Jumla | 21 | 9 | 1 | 31 |

Jambo la pili ambalo lilichangia katika utambuzi wa muunganiko kati ya Waafrika na Waasia waliokandamizwa na ukoloni lilikuwa ni kuwapo kwa idadi kubwa ya wenyeji wa asili ya Kiasia katika baadhi ya sehemu za Mashariki na Kusini mwa Afrika, na pia visiwa vya Bahari ya Hindi ambao walitawaliwa, pamoja na Waafrika, na wakoloni wa Kizungu. Hali hii inadhihirika vizuri zaidi kutokana na tajiriba ya ubaguzi wa kijamia wa kihistoria uliodumu nchini Afrika Kusini. Kwa miaka mingi ubaguzi huu ulizusha upinzani, wa Waasia na Waafrika, ambao ulitokea ama sambamba au kwa pamoja ndani na nje ya Afrika.

Kwa mfano, ni katika Afrika Kusini ambamo, baina ya miaka ya 1893 na 1914, Mahatma Ghandhi alianzisha na kuendeleza mtindo wake wa kisiasa wa uasi wa kijamii (*Satyagraha*). Aliutumia na kuuimarisha mtindo huu katika kipindi chote cha upinzani wa Wahindi wa Afrika Kusini dhidi ya ubaguzi ambao ulidumu miaka saba (1906 hadi 1913) kabla ya Gandhi kuupeleka mtindo huu hadi India na baadaye kuutumia katika kupinga utawala wa kikoloni.

Suala hili lilidhihiririka katika Mkutano Mkuu wa Tano wa Watu Weusi mnamo mwaka wa 1945, ambao ulipitisha azimio la kuunga mkono malalamishi yaliyotarajiwa kutoka kwa serikali ya India dhidi ya serikali ya Afrika Kusini, yakitaka kuwepo kwa haki na usawa kwa jamii ya Kihindi ya Afrika Kusini iliyokuwa ikibaguliwa kama Waafrika. Baada ya muongo mmoja washiriki wa Mkutano wa Bandung walikuwa na hamasa sawa na ile (ya Mkutano Mkuu wa 1945) katika uungaji mkono wao wa ujasiri uliokuwa umeonyeshwa na jamii mbalimbali za Afrika ya Kusini ambazo zilikuwa zikikandamizwa na ubaguzi, hasa zile za asili ya Kiafrika, Kihindi na Kipakistani.

Jambo la Tatu lilikuwa kwamba uhamasisho na mafanikio ya awali ya Waasia katika upinzani wao dhidi ya ukoloni yalitokea kuwa na athari kubwa barani Afrika kwa kuimarisha utetezi wa kitaifa wa Waafrika.

Jambo la nne lilikuwa kwamba ama katika hali ya mapambano dhidi ya ukoloni au kutokana na mapambano haya kulikuwepo na nyakati ambapo mahusiano ya kiuendeshaji yaliundwa kati ya maadui hawa wa himaya. Mfano wa awali wa uunganisho huu ni Mkutano wa Brussels wa 1927 ambao uliitishwa na Shirikisho Dhidi ya Ubeberu na Ukoloni ambapo wazalendo wengi kutoka Asia na Afrika (wakiwemo Jawaharlal Nehrn, kutoka India; Ho Chi Minh, kutoka Vietnama; na Lamine Senghor, kutoka Senegal) washiriki.

Jambo la tano ni kuwa hisia za Waafrika na Waasia juu ya ukandamizaji wa ukoloni hazikumalizika na kupatikana kwa uhuru wa kisiasa. Mataifa huru mapya yalishirikiana sio tu katika kuyamaliza masalia ya ukoloni katika kanda zao, bali pia yalijiandaa ili kulinda, kudhihirisha, na kuimarisha uhuru wao mpya.

Kuanzishwa kwa kundi la Asia na Afrika (*Asian-African* ambalo baadaye liliitwa *Afro-Asian*) chini ya Umoja wa Mataifa mnamo mwaka wa 1950; Mkutano wa Bandung wa mwaka wa 1955; na kuanzishwa kwa Shirika la Mshikamano wa Waasia na Waafrika (Afro-Asian People's Solidarity Organization) mnamo mwaka wa 1957 — yote yalikuwa ni utangulizi na misingi ya vuguvugu pana zaidi la Dunia ya Tatu katika miaka ya mwanzoni ya muongo wa 1960.

Mkutano wa Asia na Afrika uliitishwa mjini Bandung nchini Indonesia, katika mwezi wa Aprili mwaka wa 1955, chini ya ufadhili wa serikali tano za Kiasia (Burma- ambayo sasa yaitwa Myanmar, Ceylon – ambayo sasa yaitwa Sri-Lanka, India, Indonesia na Pakistani) na ulikuwa na nchi shiriki 29 ambapo Afrika iliwakilishwa na nchi 6 na Asia nchi 23. Malengo ya Mkutano, kama yalivyotangazwa na serikali fadhili katika mwezi wa Desemba 1954, yalikuwa haya yafuatayo:

- kuendeleza urafiki na ushirikiano kati ya mataifa ya Asia na Afrika, kuchunguza na kuimarisha maslahi ya pamoja na kusitawisha na kuzidisha urafiki na ujirani mwema;
- kuzingatia matatizo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na pia uhusiano kati ya nchi zinazoshiriki;
- kuzingatia matatizo maalum kwa watu wa Asia na Afrika, kwa mfano matatizo yenye athari juu utaifa na yenye kuhusika na ubaguzi na ukoloni, na
- kuangalia hadhi ya mabara ya Asia na Afrika pamoja na watu wao katika dunia ya sasa na pia mchango wanaoweza kutoa katika kuimarisha amani na ushirikiano duniani.

Bila shaka uwakilishi wa Asia katika Bandung ulikuwa ndio mkubwa. Uwakilishi wa kiwango cha chini wa bara la Afrika ulitokana na ukweli kwamba katika wakati huo ni idadi ndogo tu ya nchi za Afrika ilikuwa huru kisiasa.

Uwakilishi na taathira ya Afrika katika Mkutano wa Bandung ulikuwa muhimu kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni mchango mkubwa wa Rais Gamal Abd al-Nasser wa Misri katika kamati ya uandishi wa maazimio. Zaidi ya hayo, tajiriba na utendaji wa al-Nasser katika Bandung ulimsaidia kuibuka na kuwa mmojawapo wa waasisi na kiongozi muhimu wa kundi la Dunia ya Tatu.

Sababu ya pili ni kwamba taathira ya Afrika katika Mkutano wa Bandung ilidhihirika katika umuhimu uliopewa haki za kibinadamu na pia masuala ya haki ya kujitawala barani Afrika, hasa kwa kuwa mambo haya yalihusishwa na ubaguzi wa kiasasi.

Zaidi ya maazimio juu ya ushirikiano wa kitamaduni, haki za binadamu, haki za kujitawala na matatizo ya watu waliotawaliwa, taarifa ya mwisho ya Mkutano wa Bandung ilionyesha dhahiri kuwa Mkutano huo ulikuwa ishara ya lengo ambalo lilizingatia kanuni mbili zilizodumu kama msingi wa ushikamano wa Dunia ya Tatu, yaani, kuondolewa kwa ukoloni na maendeleo ya kiuchumi.

Kwa kuwa Mkutano wa Bandung ulikuwa sauti muhimu sana ya mabara ya Asia na Afrika iliyokuwa imeratibiwa, msisimko uliotokana na mkutano huo punde

baadaye uliwezesha kuundwa kwa vyombo vingine vya ushirikiano, kama vile Kikundi cha mataifa ya Asia na Afrika *(Afro-Asian caucus)* katika Umoja wa Mataifa, na kuanzishwa kwa vikundi vingine kama vile Shirika la Muungano wa Watu wa Afrika na Asia *(Afro-Asian People's Solidarity Organization)*. Baada ya mwaka wa 1960 kulikuwepo na mabadiliko katika utaratibu wa majina kutoka kundi la Asia na Afrika (Kikundi cha Asia na Afrika) na kuwa Afrika na Asia (*Afro-Asian*), jambo ambalo lilidhihirisha kuongezeka kwa ushawishi wa Afrika katika kundi hilo.

Kuongezeka kwa ushawishi wa Afrika katika Umoja wa Mataifa kulijihidhirisha zaidi mnamo mwaka wa 1959 ambapo upanuaji wa uwakilishi ulitokea baada ya wanachama 16 wa mataifa huru mapya kujiunga na Umoja huo.

Jambo la muhimu zaidi kwa azma yetu ni athari za kundi hili katika miongo yake miwili ya kwanza ambapo lilizusha, katika Umoja wa Mataifa, fikra, ushawishi, na shinikizo juu ya mambo mawili yenye umuhimu mwingi kwa nchi za Afrika. Haya yalikuwa ni suala la kuondolewa kwa ukoloni kwa jumla, na matatizo maalum ya ubaguzi wa rangi na ukoloni Kusini mwa Afrika.

Kupitishwa kwa "Azimio la Kihistoria la Kutolewa Uhuru kwa Watu na Nchi zilizotawaliwa" na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa mnamo Desemba 1960, ambalo lilidhaminiwa na nchi 43 za Kiafrika, kulikuwa ni ishara yenye kuvutia ya kuwasili, katika utaratibu wa Umoja wa Mataifa, kwa kundi la Afrika na Asia lililokuwa limeundwa upya na kupanuliwa. Kwa kutangaza haja ya kuondolea mbali aina zote za ukoloni, kwa haraka na bila masharti, Azimio hilo liliulaani ukoloni kama unyimwaji wa haki za msingi za kibinadamu na pia, kuwa kipingamizi katika kuimarisha amani na ushirikiano duniani. Pia azimio lilisisitiza umuhimu wa kuchukuliwa kwa hatua za haraka kuwakabidhi mamlaka watu walioishi chini ya ukoloni.

Azimio la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa lililofuatia mwaka mmoja baadaye liliunda kamati maalum ya kusimamia utekelezaji wa Azimio la mwaka wa 1960. Azimio hili la pili lilikuwa ni matokeo ya azima ya kundi la Afrika na Asia ya kuiongoza itikadi na kurasimisha mwelekeo wa upinzani wa Umoja wa Mataifa na vitendo vyake vya baadaye dhidi ya ukoloni.

Kadhalika matatizo yaliyotokana na ubaguzi wa kijamii na ukoloni nchini Afrika Kusini yalipewa uzito zaidi katika Umoja wa Mataifa, kutokana na shinikizo za kundi la Afrika na Asia.

Mfano mmoja ulikuwa ni vikwazo vya hiari juu ya uuzaji wa silaha kwa serikali ya Afrika Kusini vilivyowekwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mnamo

Desemba mwaka 1963. Baadaye (mnamo 1977) vikwazo hivyo vilifanywa kuwa vya lazima. Pia, kuna mfano wa vikwazo teule vya lazima vilivyowekwa na baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (mnamo 1966), dhidi ya serikali ya wachache ya kibaguzi ya Rhodesia ambayo katika mwaka wa 1965 ilijitangazia uhuru haramu kutoka utawala wa Uingereza na hivyo kuzusha mapambano ya miaka 15 ambayo yalimalizika kwa kupatikana kwa uhuru wa Zimbabwe katika mwaka wa 1980. Baadaye (mwakani wa 1968) vikwazo hivyo vilipanuliwa na kuhusisha bidhaa zote.

Mfano wa tatu wa taathira ya kundi la Afrika na Asia ulikuwa ni Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, katika mwaka wa 1966, ili kukatiza Udhamini wa Shirikisho la Mataifa juu ya nchi ya Kusini Magharibi mwa Afrika kutokana na historia ndefu ya usaliti wa wajibu na Afrika Kusini. Baadaye, mnamo mwaka wa 1968 Umoja wa Mataifa uliipa nchi hiyo jina la Namibia, tendo ambalo lilitangulia Azimio la Baraza la Usalama la mwaka wa 1970 na pia la mwaka wa 1971 kuwa usimamizi wa Afrika Kusini juu ya Namibia ulikuwa haramu na ulifaa kukatizwa. Mwisho, kulikuwa na Kamati Maalum ya Kupambana na Ubaguzi iliyoanzishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika mwaka wa 1962 kwa madhumuni ya kuzichunguza mara kwa mara sera za kibaguzi za Afrika Kusini.

Sura nyingine ya kiasasi ya kundi la Afrika na Asia kama kichocheo kilichotokana na Mkutano wa Bandung ilikuwa ni kuanzishwa kwa Shirika la Mshikamano wa Waasia na Wafrika *(Afro-Asia People's Solidarity Organization)* mjini Kairo mwaka 1957. Huku ukiungwa mkono kwa dhati na nchi za Muungano wa Kisovieti (Urusi) na Jamhuri ya Watu wa China, Umoja huu uliundwa na makundi yenye maslahi yenye kuwiana, hasa pale mwanzoni, ambayo yalitoka Afrika, Asia, na katika nchi zenye mfumo wa kijamaa.

Siasa kali za utaifa wa Afrika na Asia zilichukua nafasi ya juu zaidi kuliko ujamaa wa kimataifa kutokana na ukweli kuwa Nasser aliweka usimamizi wa Muungano huo chini ya Wamisri. Isitoshe, kama inavyodhihirika kutokana na nchi zilizochaguliwa kuandaa Mikutano Mikuu ya Umoja huo (km Misri mwaka 1957, Guinea mwaka 1960, Tanzania mwaka 1963 na Ghana mwaka 1965), mataifa yenye siasa kali yaliuunga mkono Umoja zaidi ya wengine.

Baina ya miaka ya 1956 na 1965 Mikutano mingi ilipangwa na Muungano ambayo ilihusisha wataalamu wa sekta nyingi kama vile tiba, sheria, uandishi wa habari, uandishi wa kisanaa, uchumi, huduma za kijamii, maendeleo ya sehemu za mashambani, akina mama na vijana.

Kutokana, kwa kiasi fulani, na athari za ugomvi kati ya Usovieti (USSR) na Uchina, Muungano ulianza kufifia katikati ya muongo wa 1960 na kufikia miaka

JEDWALI LA 29.3 Nchi zilizoshiriki kwenye Mkutano wa Asia-Afrika, Bandung, Indonesia, 18–24 April 1955

, In-

| Nchi za Asia (23)[a] | | | Nchi za Afrika (6)[b] |
|---|---|---|---|
| Afghanistan | Iraq | Syria | Egypt |
| Burma* | Japan | Thailand | Ethiopia |
| Cambodia | Jordan | Turkey | Gold Coast |
| Ceylon* | Laos | Vietnam (Kaskazi) | Liberia |
| Jamhuri ya Watu wa China | Lebanon | Vietnam (Kusini) | Libya |
| | Nepal | Yemen | Sudan |
| Indonesia* | Pakistan* | | |
| Iran | Philippines | | |
| | Saudi Arabia | | |

ya 1970 ukawa hauna nguvu tena. Lakini, kabla ya kufikia hali hiyo Muungano ulishuhudia kuundwa kwa shirika sambamba la Umoja wa Waafrika, Waasia na Waamerika wa Kilatino ambao uliundiwa Havana, nchini Kuba mnamo mwaka wa 1966, na ulijulikana zaidi kama Umoja wa Mshikamano wa Mabara matatu (*Tri-Continental Solidarity Organisation*).

Mahatma Gandhi, ambaye alifuatiwa na Jawaharlal Nehru, alitokea kuwa na athari kubwa zaidi katika ukuzaji wa maslahi ya pamoja na uhusiano katika kipindi cha baada ya uhuru. Kwa kiasi fulani hii ilitokana na hisia zake za kibinafsi za mzigo mkubwa wa kisiasa na kijamia "msiba wa Afrika usio na mwisho" kama alivyotamka mwenyewe, kwenye Mkutano wa Bandung.

Katika kiwango cha utendaji Nehru alitimiza jukumu kubwa zaidi katika uundaji wa asasi za kuimarisha na kusukuma mbele maslahi ya pamoja ya India na Afrika.

Alifanya hivi ama katika Muungano wa Waafrika na Waasia wa miaka ya muongo wa 1950 ambao aliuongoza, au katika kundi la Dunia ya Tatu la miaka ya muongo wa 1960 alilolisaidia kwa kuligeuza kuwa Jumuiya mpya ya mataifa mengi.

Kuwepo kwa jamii zenye watu wengi wa asili ya Kihindi katika baadhi ya sehemu za Afrika kumesaidia kuendeleza hisia hii ya uhusiano maalum. Tayari tumedhihirisha jinsi uhusiano huu ulivyosaidia kuimarisha ushirikiano kati ya India na Afrika katika juhudi zao za pamoja za kupambana na mfumo wa kibaguzi wa Afrika Kusini. Kuhusiana na jambo hili, ni muhimu kukumbuka kuwa katika miaka ya mwanzo ya muongo wa 1950 India ndiyo iliyokuwa nchi ya kwanza kuvunja uhusiano wa kibalozi na kiuchumi na Afrika Kusini.

Ikiwa umuhimu wa uhusiano huu maalum ulififia, kwa kiasi, katika miaka ya muongo wa 1960, ilikuwa ni kwa sababu ya mageuzi mapana katika mfumo wa kimataifa wala sio kwa sababu ya matatizo ya ndani. Sababu mojawapo ilikuwa ni kushuka kwa hadhi ya India katika Dunia ya Tatu, hasa baada ya kifo cha Nehru, mwaka 1964.

Kushindwa kwa jitihada za mwaka 1965 za kupanga Mkutano wa pili wa nchi za Afrika na Asia, kwa kuzingatia mtindo wa Mkutano wa Bandung, hutajwa kuwa chanzo na tokeo la kufifia au kuporomoka kwa Muungano huo. Sababu nyingine iliyochangia zaidi kufifia kwa Muungano huo, kama tulivyosema hapo awali, ilikuwa ni kupunguka kwa ushawishi wa Umoja huo katika miaka ya mwisho ya muongo wa 1960. Zaidi ya hayo, katika muongo wa 1970 shughuli za kundi la nchi za Afrika na Asia katika Umoja wa Mataifa zilikoma.

Sababu moja iliyosababisha kutofanyika kwa Mkutano wa Pili la Bandung ilikuwa ukweli kwamba umuhimu wake ulikuwa umeshushwa na Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote ambao ulifanya mikutano yake miwili ya kilele kwenye miaka ya 1961 na 1964.

Kuanzishwa kwa Umoja wa Mshikamano wa Mabara Matatu mjini Havana mwaka 1960, chini ya udhamini wa AAPSO, kulikuwa ni tukio moja zaidi la Muungano wa Afrika na Asia katika juhudi zake za kuenea nje ya mipaka yake ya kijiografia na kuunda hisia za kujitambua kati ya Mataifa ya Dunia ya Tatu. Pia, kwa kuzingatia hamasa na shinikizo za kundi la nchi 77 na lile la Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote la kusaka mfumo mpya wa kiuchumi duaniani, si ajabu kuwa manufaa ya Kikundi cha Afrika na Asia hayakuwepo tena.

Kwa hiyo kushindwa kudumu kwa Muungano wa Afrika na Asia kulitokana na kufaulu kwake kama kichochezi muhimu na pia msingi wa Muungano mpana

zaidi wa Dunia ya Tatu. Jambo hili limekubaliwa na wachambuzi ambao wamechunguza kufifia kwa Muungano huo. Kwa hiyo ni sahihi zaidi kuzungumza juu ya mabadiliko ya Muungano wa Afrika na Asia kuliko kuanguka kwake.

## Afrika na Dunia ya Waarabu; Kontua za uhusiano maalum

Baina ya tarehe 7 na 9 za mwezi wa Machi mwaka 1977, viongozi wa nchi na serikali wa mataifa 59 ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) na Umoja wa Waarabu (Arab League) walikutana mjini Kairo ambamo, kutokana na maelezo rasmi ya Mkutano, lengo lao lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kati ya Waafrika wa Waarabu. Kuna sababu tatu za kuchambua kile ambacho, kirasmi, huitwa mkutano wa Waarabu na Waafrika. Sababu ya kwanza ni kwamba ukiwa mkutano wa kwanza wa wahusika ulikuwa ni ishara ya ushirikiano mpya na wenye kina zaidi wa kisiasa na kiuchumi kati ya Waafrika na Waarabu. Ya pili ni kuwa maendeleo haya yalizidisha hisia za mshikamano kati ya nchi za Dunia ya Tatu, jambo ambalo lilikuwa mojawapo ya sifa za muongo wa 1970.

Sababu ya tatu inahusiana na ufafanuzi wa istilahi ambazo zafaa zifasiliwe mwanzoni. Kwa kuwa baadhi ya nchi zimo katika kundi la nchi za Kiafrika na pia kundi la nchi za Kiarabu, jambo hili limezusha hali ya mwingiliano na kuchangamana, badala ya upishano wa kikanda, kati ya makundi haya mawili. Hali hii ndiyo hasa kiini cha uhusiano maalum uliopo kati ya dunia ya Waafrika na ile ya Waarabu. Kwa hiyo fasili ya tofauti kati ya istilahi zinazotumiwa ni lazima ieleweke kwa kuzingatia matukio haya.

Mabadiliko yaliyotokea katika hali za kitaifa, kikanda, na kimataifa, kuanzia miaka ya muongo wa 1950 yalisaidia zaidi katika uimarishaji wa uhusiano mzuri zaidi na maendeleo, kisiasa, kiuchumi, na kijamii kuliko hapo kabla. Pia, kuweko kwa hali yenye kusaidia ujirani wa kijiografia, uhusiano wa kihistoria wa zaidi ya karne kumi na mbili, na uhusiano uliosambaa sana wa watu na wa kiutamaduni ulileta hisià za udharura katika uhusiano huu.

Kwa mfano idadi isiyopungua asili mia 60 (kuna wengine wanaoiweka idadi hii kuwa asilimia 80) ya Waarabu wote duniani huishi barani Afrika. Inakadiriwa kuwa theluthi moja ya Waafrika ni Waislamu ambao wengi wao huishi katika Afrika.

Kaskazini, na pia katika nchi tisa za Afrika iliyoko Kusini mwa jangwa la Sahara. Pia, kuna Waislamu wasiopungua asilimia 25 katika nchi nyingine saba za Afrika. Zaidi ya hayo maingiliano ya kiutamaduni yanaonekana katika nyanja ya lugha kwa sababu lugha za Kiarabu, Kiswahili, na Kihausa, ambazo ndizo lugha muhimu zaidi zisizo za Kizungu, zimeathiriwa sana na dini ya Kiislamu.



PICHA 28.1 *Mkutano wa Umoja wa Waarabu na Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Kairo 1977.*

Uhusiano huu wa kidemografia na kiutamaduni umekuwa na umuhimu katika miundo ya mashirika fulani ya kimataifa. Ushirikiano wa Nchi za Kiarabu, ambao mara nyingi huitwa Ushirikiano wa Waarabu ulikuwa na nchi moja tu ya Kiafrika (Misri) kati ya waanzilishi wake wanane katika mwaka wa 1945. Kufikia mwaka wa 1980 tisa kati ya nchi wanachama 22 zilikuwa za Kiafrika, zikiwemo nchi tatu zisizo za Waarabu lakini zenye idadi kubwa ya Waislamu (nazo zilikuwa ni Jibuti,

Mauritania na Somalia). Kwa upande mwingine tisa kati ya nchi wanachama va OAU zilikuwa ni Wanachama wa Ushirikiano wa Waarabu. Katika Shirika la Umoja wa Mashauriano wa Kiislamu (OIC) ambao ulikuwa ndio Muungano wa juu zaidi wa serikali za Kiislamu, ulioanzishwa mwaka wa 1971, kufikia mwaka wa 1980 nusu ya nchi wanachama wake (42) zilikuwa nchi za Kiafrika. Kuongezeka kwa harakati dhidi ya ukoloni katika Afrika Kaskazini kwenye miaka ya mwanzo ya baada ya Vita Vikuu vya Pili na ambazo, kwa jumla, zilitangulia zile za nchi za Kusini mwa Sahara, kulikuwa na umuhimu mkubwa katika ukuaji wa ushirikiano huo.

Kuanzishwa kwa taifa la Israeli, ambako kulifanikiwa kwa kuwahamisha Wapalestina kulizifanya hisia za kutofungamana na upande wowote kuwa za kuvutia zaidi kwa Dunia ya Waarabu ambao walihisi kuwa maslahi yao yalikuwa yanakandamizwa kwa manufaa ya siasa za mataifa makubwa. Hata nchi za Mashariki ya Kati ambazo hazikupendelea mabadiliko, pamoja na zile ambazo zilipendelea mfumo wa serikali wa Magharibi, mantiki ya uhusiano wa kimataifa iliyojitokeza katika sehemu hiyo ilizilazimisha kuchukua msimamo wa kiitikadi uliokuwa haukaribiani sana na ama ule wa Magharibi au wa Mashariki. Kwa kuzingatia maslahi ya muda mrefu, urazini wa kuwa na siasa za kutofungamana na upande wowote ulijitokeza kuwa msingi wa uimarishaji wa maslahi ya pamoja kati ya Dunia ya Waarabu na ile ya Waafrika ambao wote waliona utaifa ukitishiwa na mataifa ya nje.

Katika ukuaji huu wa uhusiano jukumu la Misri, ambayo baina ya 1958 na 1970 ilipewa jina jipya la Jamhuri ya Muungano wa Waarabu, lilikuwa na umuhimu maalum. Chini ya uongozi wa al-Nasser kulikuwa na mabadiliko na ongezeko la kasi ya uhamasishaji katika harakati za Wamisri. Harakati hizo zilijumuisha mambo matatu, yaani maslahi ya Waarabu, ya Waafrika na Udugu wa Kiislamu, ambayo kitabu cha al-Nasser cha mwaka wa 1954 cha Falsafa ya Mapinduzi kiliyatambua kuwa kiini cha ujitambulishaji wa Misri. Kuongezeka kwa taathira ya al-Nasser katika siasa za Upanafrika na ukombozi wa Waarabu wote katika miaka ya mwishoni ya muongo wa 1950 kulimtayarisha kujitokeza kuwa muasisi mwenye umuhimu maalum wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote, ambao ndio msingi wa kisiasa wa Dunia ya Tatu.

Kuanzia na kujipatia uhuru kwa taifa la Ghana, katika mwaka wa 1957, kupunguka kwa ukoloni katika Afrika iliyoko Kusini mwa Sahara kuliandaa njia ya ushirikiano zaidi baina ya nchi za Afrika na kujenga mshikamano wenye maana baina ya mataifa ya Kaskazini na yale ya Kusini mwa Sahara.

Kuanzishwa kwa OAU mnamo mwaka wa 1963 kulizalisha shirika la bara la Afrika ambalo lilikuwa sambamba na Umoja wa Waarabu na pia, kwa njia

nyingi kuchangia jukumu lake. Zaidi ya kuchangia baadhi ya wanachama, mashirika haya mawili yaliunganishwa pamoja na sifa ya kuwa mashirika ya kwanza kuanzishwa na mataifa masikini kwa manufaa ya nchi masikini duniani.

Hata hivyo suala sugu zaidi la siasa za Umoja wa Waarabu, ambalo ni kuwepo kwa taifa la Israeli, lilitenganishwa na siasa za OAU za miaka ya awali, japo wanachama wa Umoja wa Waarabu katika OAU walitarajia kuwa mashirika haya mawili yangekuwa na msimamo mmoja juu ya suala hili. Sababu kubwa ya hali hii ilikuwa kwamba mengi kati ya mataifa huru mapya ya Afrika yalikuwa na uhusiano wa kiuchumi na mara nyingine, wa kijeshi wa karibu sana na Israeli. Pia wanachama wengi walihisi kuwa tatizo la Mashariki ya Kati lilikuwa sio la Afrika na kwa hivyo lilipaswa kuwekwa nje ya shughuli za OAU.

Hata hivyo, baada ya Vita vya Siku Sita vya mwaka wa 1967 kulianza kuonekana mabadiliko katika msimamo wa OAU baada ya Israeli kunyakua baadhi ya ardhi ya Waarabu, ikiwemo sehemu ya Sinai ya taifa la Misri. Katika kikao chake cha nane mwaka 1971, OAU, kwa mara ya kwanza, iliamua kuwa kuendelea kukaliwa kwa ardhi ya Waarabu na Israeli kulikuwa ni tisho la amani ya eneo la Afrika. Wakati huo huo OAU iliunda kamati ya kusuluhisha mzozo huo (kati ya Misri na Israeli) ambapo kushindwa kwa kamati hiyo kuleta suluhisho kulisababisha kuungwa mkono zaidi kwa Waarabu na OAU. Matokeo ya hali hii yalikuwa kwamba kufikia mwisho wa mwaka wa 1973 ni nchi wanachama wa OAU nne tu, yaani Malawi, Lesotho, Swaziland na Mauritius, ambazo zilikuwa na uhusiano wa kibalozi na Israeli.

Umuhimu wa matukio haya, ya mwishoni mwa mwaka wa 1973, unaweza kutathiminiwa kwa kukumbuka kuwa katika mwaka wa 1967 wanachama wote wa OAU, isipokuwa wale waliokuwa pia ni wanachama wa Umoja wa Waarabu, walikuwa na uhusiano wa kibalozi na Israeli. Na pia, ni muhimu ikumbukwe kuwa punde tu baada ya Vita vya Siku Sita ni nchi moja tu ya Afrika (Guinea) iliyovunja uhusiano wa kibalozi na Israeli, na kuwa hali ilibaki hivyo hivyo kwa karibu miaka mitano iliyofuata, mpaka kukatokea mabadiliko halisi katika hisia za nchi za Kiafrika.

Matukio matatu muhimu ya mwaka wa 1973 yalisababisha mabadiliko ya kidiplomasia ya mwezi wa Oktoba mwaka huo. Mawili kati ya haya yalihusiana na uchipukaji, katika mazingira ya mshikamano kati ya Waafrika, Waarabu, na Dunia ya Tatu. Mambo hayo ni kufanyika kwa sherehe za miaka kumi ya OAU mjini Addis Ababa mwezi Mei, na pia Mkutano wa nne wa Kilele wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote mjini Algiers uliofanyika mwezi Septemba. Vikao hivyo vilikuwa muhimu katika kupatanisha, kimikakati udiplomasia wa Waarabu, Waafrika na Dunia ya Tatu.

Jambo la tatu ambalo lilisababisha mafarakano ya kidiplomasia ya mwezi wa Oktoba mwaka 1973 lilikuwa ni vita vya Oktoba mwaka wa 1973 (Yom Kippur, Oktoba 6 hadi 24) kati ya Misri na Syria kwa upande mmoja na Israeli kwa upande mwingine. Mambo yalifikia kikomo wakati Waisraeli walipowasukuma nyuma zaidi Wamisri na, kwa mara ya kwanza, (Waisraeli) wakakalia ardhi ya Misri iliyoko Magharibi mwa Mfereji wa Suez amabayo bila ubishi ni sehemu ya bara la Afrika.

Baadhi ya wachambuzi hushikilia kuwa Waafrika walisalimu amri kutokana na matumizi ya mafuta kama silaha ya Waarabu. Sababu halisi zilikuwa ni kukuza kwa hisia za mshikamano wa maslahi ya pamoja kati ya Waafrika na Waarabu.

Badiliko kubwa lenye mshindo lilikuwa ni uamuzi wa Umoja wa Waarabu wa Novemba mwaka 1973, uliopitishwa mjini Algiers wa kuziwekea vikwazo vya mafuta serikali za kikoloni za Ureno, Rhodesia, na serikali ya kibaguzi ya Afrika Kusini. Na wakati huo huo ilipitishwa kuwa asasi tatu kubwa zifuatazo zianzishwe ili kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi. Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika; Mfuko Maalum wa Kiarabu kwa Afrika ambao uliundwa ili kutoa misaada ya dharura ya kifedha kwa mataifa yasiyo ya Kiarabu ya Afrika ili kugharamia uagizaji wa mafuta kutoka nje na maendeleo ya raslimali ya mafuta, na pia Mfuko wa Waarabu na Waafrika wa Misaada ya Kiufundi, uliolenga katika kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi kati ya mataifa ya Kiarabu na Kiafrika. Kuongezeka kwa umuhimu wa masuala ya kiuchumi katika ushirikiano uliokuwa unapanuka kati ya Waarabu na Waafrika kulidhihirika zaidi katika ukuaji wa hisia juu ya jukumu ambalo OPEC ilihitajika kuchukua katika kuimarisha maendeleo ya Dunia ya Tatu, kwa jumla, na hasa ya Afrika.

Dalili hizi za mshikamano kati ya Waarabu na Waafrika hazimaanishi kuondolewa kwa tofauti fulani muhimu katika mitazamo ya kisiasa na aula. Kwa mfano mara nyingi Umoja wa Waarabu haukufanikiwa kuungwa mkono na OAU katika juhudi zake za kuifukuza Israeli kutoka Umoja wa Mataifa. Baada ya kutiliana saini mkataba wa amani na Israeli, uanachama wa Misri katika Umoja wa Waarabu na OIC ulisimamishwa na wakati huo huo makao makuu ya Umoja huo kuhamishwa kutoka Kairo hadi Tunis. Hata ingawa OAU ilishinikizwa, ilikataa kuchukua hatua kama hiyo na kwa hiyo kuendelea kuialika Misri kushiriki vikao vyake. Pia katika Mkutano wa Sita wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote, mnamo mwaka wa 1979, nchi za Kusini mwa Sahara zilisaidia katika kuunda azimio, lililokubaliwa na wote, ambalo lilizuia kufukuzwa kwa Misri kama mataifa ya Kiarabu yalivyotaka.

Katika mwisho wa muongo wa 1980 suala lenye changamoto zaidi lilikuwa ni kama ahadi na matarajio ya ushirikiano na mshikamano yangeweza kustahimili

upandaji wa bei ya mafuta na upanukaji wa ruwaya za mdororo wa kiuchumi wa kimataifa. Kuzungumziwa kwa masuala kama hayo kulikuwa ni ishara kuwa ushirikiano baina ya Waafrika na Waarabu ulikuwa umeimarika sana tangu miaka ya muongo wa 1950. Kufikia muongo wa miaka ya 1970 ushirikiano huu ulifikia kiwango ambacho hapo awali kilikuwa hakijafikiwa. Na katika mwenendo huu ushirikiano huu uliathiri sana mwelekeo wa changamano kutoka Dunia ya Tatu.

Uhusiano na Amerika ya Kilatino na Karibiani: uimarikaji wa hisia za utambulisho na Dunia ya Tatu

Kuweko kwa Waafrika kijamia na kiutamaduni katika Amerika ya Kilatino na Karibiani ni ukumbusho wa milele wa mawasliano ya kina kirefu ya kihistoria baina ya bara la Afrika na Diaspora ya Kiafrika. Hali hii ni ya ukweli zaidi katika sehemu za Karibiani ambamo wingi wa watu na utamaduni wa Kiafrika umerudikana na kuonekana zaidi kuliko sehemu nyingine yo yote ya Amerika Kilatino.

Katika sehemu za Karibiani, ambazo hapa zinaelezewa kuwa visiwa vya eneo hilo pamoja na Belize na maeneo ya Guyana (Guyana, Surinam, na Kayenne), kuna mataifa mengi yenye idadi kubwa zaidi ya watu weusi na mengine yenye idadi muhimu za watu weusi. Rekodi za kihistoria zimejaa mifano mingi ya mipango ya ushirikiano kati ya bara la Afrika na Karibiani katika kuendeleza itikeli ya Upanafrika unaovuka bara la Afrika. Kwa mfano, katika miaka ya mapema ya karne ya ishirini, hasa kuanzia mwaka wa 1900, kulianzishwa mifululizo ya Mikutano Mikuu ya Kipanafrika ambayo iliwahusisha weusi kutoka bara la Afrika na waliotawanyika kwingineko. Pia kulizuka itikadi ya Garvey ambayo ilivuka mipaka ya asili yake katika Karibiani na kuwa kichocheo kikubwa cha utaifa wa weusi kama ilivyodhihirishwa na watu kama Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta na wengineo. Kulianzishwa pia falsafa ya Unegro katika muongo wa 1930 ambayo alianzishwa kwa pamoja na Leopold Senghor wa Senegal na Aimé Césaire wa Martinique. Halikadhalika kulikuwa na Mkutano wa Tano wa Kipanafrika mwaka 1945 uliyotayarishwa pamoja na Nkrumah na George Padmore wa Trinidad.

Kwa jumla maingiliano hayo yalitokea kabla ya Afrika na nchi za Karibiani kuwa huru, na kwa hiyo yalitawaliwa na maslahi yasio ya kiserikali. Kinyume na hayo, kipindi cha miongo ya 1960 na 1970 kilitoa fursa mpya zilizopanua ushirikiano wa weusi ukiwa pia unahusisha serikali.

Tamasha la Kwanza la Sanaa ya Weusi Duniani lililofanyika nchini Senegal mwaka 1966, Mkutano Mkuu wa sita wa Kipanafrika uliotayarishwa na Tanzania katika mwaka wa 1974, na Tamasha la Pili la Sanaa na Utamaduni wa Weusi na

Waafrika Duniani liliyofanyiwa Nigeria katika mwaka wa 1977, yalikuwa ni mifano ya shughuli ambamo uhusiano kati ya Afrika na Karibiani uliendelezwa katika muktadha wa Upanafrika kati ya mabara husika.

Mwaka 1974 Mwalimu Julius Nyerere alikuwa na wasiwasi kuwa Upanafrika ungeyaathiri vibaya mapambano ya ukombozi wa binadamu kama ungezitenganisha sehemu za Afrika na za Karibiani kutokana na sehemu nyinginezo za Dunia ya Tatu. Kwa kweli uhusiano kati ya Afrika na Karibiani hauwezi kujikita katika mambo ya kijamia pekee. Jambo jingine ambalo lilisaidia kuimarisha uhusiano huu lilikuwa kwamba hadi hivi majuzi nchi nyingi za Afrika na Karibiani zilikuwa makoloni na kwa hiyo uzoefu huo uliamsha hisia zao za pamoja juu ya umuhimu wa kuendeleza ujitambulishaji wao wa kisiasa, kitaifa, na kimataifa katika Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote na katika Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa. Uzoefu huu ulisaidia kuimarisha fursa zao za ushirikiano wa kiasasi.

Masuala ya eneo la Kusini mwa Afrika na uonevu wa mfumo wa kiuchumi wa kimataifa yalitokea kuwa mambo mawili muhimu katika shughuli za pamoja. Umuhimu wa uhusiano wa kiuchumi wa kimataifa ulisababisha kuanzishwa kwa kundi la nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (ACP); mnamo mwaka wa 1975, ambalo liliundwa ili kulinda na kuendeleza misimamo ya pamoja katika mazungumzo na Umoja wa Nchi za Ulaya (EC).

Maslahi ya pamoja ya kiuchumi yalitokea kuwa na umuhimu zaidi yakilinganishwa na yale ya kijamii, kiutamaduni, na kisiasa, katika uhusiano baina ya Afrika na eneo pana zaidi nje ya Karibiani la Amerika ya Kilatini.

Licha ya tofauti katika viwango vya maendeleo ya kiuchumi kati ya mabara haya mawili, katika mijadala ya Umoja wa Mataifa juu ya masuala ya kijamii na kiuchumi, Waafrika wameunda ushirikiano wenye nguvu kati yao na Waamerika wa Kilatino. Katika mambo ya kiuchumi na kijamii Waamerika wa Kusini wameulegeza mshikamano wao wa kibara na Marekani, na kuzingatia kanuni ya ushikamano wa mataifa masikini.

Mfano mwingine ni jukumu muhimu liliotekelezwa na nchi za Amerika ya Kusini katika kuanzishwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD), mnamo mwaka wa 1964, na pia katika kuhamasisha kundi la 77. Umuhimu wa mchango wao ulisababisha uteuzi wa katibu mkuu wa kwanza wa UNCTAD, Raul Prebisch, kutoka bara hilo. Prebisch alikuwa mwanauchumi kutoka Argentina na ambaye husifiwa kuwa mwanzilishi wa nadharia za utegemezi, na uendelezaji wa mbinu za majadiliano juu ya uhusiano mpya wa kiuchumi wa



PICHA 28.2 *Fidel Kastro wa Kuba na Kundi la Mataifa 77 mjini Havana, Kuba, 21 Aprili,1987.*

kimataifa (*New International Economic Order- NIEO*) unaodaiwa na kundi la Dunia ya Tatu na ambao ulipendekezwa kwa mara ya kwanza na Rais Luis Eehevevria wa Meksiko.

Uhusiano baina ya jamii za Amerika ya Kilatino na mataifa ya Afrika ni jambo lenye hisia kinzani kimsingi. Mfano mmoja ulikuwa ni tabia ya kusitasita kwa mataifa ya Amerika ya Kusini kujiunga kikamilifu na Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote katika miongo ya 1960 na 1970.

Zipo sababu zisizopungua nne ambazo zaweza kuelezea tabia hii. Ya kwanza ni ukweli kuwa kinyume na ilivyokuwa katika sehemu ya Karibiani, mataifa yote ya Amerika ya Kilatino yalijipatia uhuru wa kisiasa katika karne ya kumi na tisa, na mengi yao kabla ya mwaka wa 1820. Jambo hili lilizitenganisha kiasi nchi hizi na harakati za baada ya Vita Vikuu vya Dunia vya Waafrika na Waasia, ambazo

zilikuwa nd'zo msingi wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote. Sababu ya pili, na inayohusiana na ile ya kwanza, ilikuwa kwamba Hispania ilikuwa haina umuhimu kama mtawala wa kikoloni katika mabara ya Afrika na Asia, jambo ambalo lilififisha uwezekano wa siasa na utamaduni wa Kihispania, ambao ndio wenye umuhimu zaidi katika ujitambulishaji wa Amerika ya Kilatino, kutumiwa katika kuziunganisha nchi hizo na mabara ya Afrika na Asia.

Sababu ya tatu ilikuwa kwamba kusitasita kwa nchi za Amerika ya Kilatino kujiunga na Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote katika miaka ya mwanzoni ambapo ajenda yake haikuzingatia masuala ya kiuchumi kama ilivyotokea baadaye, ilikuwa ni kwamba tayari mataifa hayo yalikuwa sehemu ya mfumo wa kiusalama wa bara la Amerika, Umoja wa Nchi za Amerika, (OAS) ulioanzishwa mwaka 1948. Kuanzishwa kwa Umoja huu kulitokea miaka 13 kabla ya kuanzishwa kwa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote.

Sababu ya nne ilikuwa kwamba kinyume na hali ilivyokuwa katika sehemu ya Karibiani, katika mataifa ya Amerika ya Kilatino, ikiwa ni pamoja na yale yenye idadi inayotambulika ya watu na utamaduni wa asili ya Kiafrika na Kiasia, jamii za asili ya Kiafrika na Kiasia hazijakuwa na athari muhimu ya moja kwa moja juu ya maamuzi ya masuala ama ya ndani au hata ya nje.

Taifa la Brazil limeonyesha tofauti kadha kutokana na hali hii ya jumla, japo tofauti hizo hazikutosha kuifanya ijiunge na Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote ambamo ilichagua kuwa na hadhi ya Mtazamaji tangu mwaka wa 1961. Hata hivyo, tangu miaka ya katikati ya muongo wa 1950 kumekuweko na upanukaji wa shauku juu ya Afrika na Asia katika sera ya kigeni ya Brazil, nchi pekee ya Dunia kutokana na hali ya kipekee ya Brazil kuwa Mpya yenye kuzungumza Kireno, na hivyo kutaka kukuza hisia za ujitambulishaji wa pamoja na mataifa ya Kiafrika yaliyozungumza Kireno.

Kwa sababu ya sera yake ya kikoloni ambayo ilikataa maafikiano na pia, licha ya kuongezeka kwa harakati za Waafrika dhidi ya ukoloni, baina ya muongo wa 1960 na katikati ya muongo wa 1970, Ureno ilipoteza uungwaji mkono, kidiplomasia, ulimwenguni. Sifa hii ya ukinzano juu ya suala la uhuru ilijitokeza katika kipindi cha miaka ya 1973-4, mwaka mmoja au miwili kabla ya Ureno kushurutishwa kujiondoa kutoka Afrika. Brazil ilikuwa nchi pekee ya Amerika ya Kilatino kuiunga mkono Ureno katika Umoja wa Mataifa japo mara nyingi ilijizuia kupiga kura juu ya Afrika ya Kusini na iliungana na mataifa ya Afrika dhidi ya Rhodesia na Namibia.

Baada ya kujiondoa kwa Ureno, ilikuwa rahisi kwa Brazil hasa baada ya miaka ya katikati ya muongo wa 1970, kufuata kwa dhati sera iliyokuwa tayari imeelezwa, ya kuyapanua maslahi yake ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kuvuka maeneo ya nchi za Afrika zilizozungumza Kireno. Uhusiano uliokuwa unaimarika uliundwa kati ya Nigeria na Brazil — nchi mbili zilizokuwa zinapata nguvu katika sehemu zao, na ambazo kwa upande wa idadi ya watu zilikuwa ndizo nchi kubwa zaidi katika mabara yao.

Kwa upande wake, serikali ya kimapinduzi ya Kuba haikuonyesha ukinzani wowote kuhusu umuhimu wa masuala ya Afrika na yaliyohusiana na Dunia ya Tatu. Ikilinganishwa na mataifa mengine ama ya Amerika ya Kusini na Karibiani au nchi yo yote ya Asia na Mashariki ya Kati, uhusiano baina ya Kuba na Afrika, tangu mapinduzi ya 1959, ulikuwa hauna kifani kwa upande ama wa upana au uthabiti wa msimamo.

Matumizi makubwa ya majeshi ya Kuba nchini Angola na katika Pembe ya Afrika, hata ingawa yalikuwa na wapinzani wake barani Afrika, mwishoni yalionekana kutokuwa na utatanishi mkubwa kwa sababu OAU iliiona Somalia kama mchokozi wa eneo la Pembe. Na pia, kwa kuwa malengo ya serikali ya kibaguzi ya Afrika Kusini yalikuwa yamezuiliwa. Ingawa hivyo, matukio haya yalielekea kuzihinikiza sura nyingine za uhusiano kati ya Kuba na Afrika ambao ulikuwa unazidi kuimarika.

Kufikia mwaka wa 1980 kati ya washauri 8500 na 12,200 kutoka Kuba walikuwa wakitoa huduma katika nchi 12 za Afrika, asilimia 70 kati yao walikuwa nchini Angola. Hawa walitoa huduma za kiufundi katika sekta za tiba, kilimo, elimu na uhandisi. Kufikia mwaka wa 1977 Kuba ilikuwa na uhusiano wa kibalozi na nchi 25 za Kiafrika na nchi 12 zilikuwa na mabalozi mjini Havana.

Uthabiti wa msimamo wa Kuba katika kujitambulisha na Dunia ya Tatu ulitoa motisha muhimu kwa uhusiano wake na Afrika. Kuba ilikuwa sio tu (katika mwaka wa 1961) mwanachama pekee mwanzilishi wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote kutoka Amerika ya Kusini na Karibiani, bali pia ilibakia kuwa mwanachama kamili pekee kutoka eneo hilo hadi mataifa huru mapya yaliyozungumza Kiingereza yalipojiunga na Muungano huo katika miaka ya mwishoni mwa muongo wa 1960. Jukumu lake katika uanzishwaji wa shirika la Mshikamano wa Mabara Matatu katika mwaka wa 1966 lilikuwa shughuli nyingine muhimu iliyolenga Dunia ya Tatu. Pia kuchaguliwa kwa Kuba kuwa mwenyekiti wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote baina ya miaka ya 1979 na 1982 kulikuwa ni ushahidi wa sifa zake za kisiasa kati ya maslahi ya Afrika na Asia yaliyoutawala Muungano huu wa Dunia ya Tatu.

Mataifa ya Afrika kila wakati yalijaribu kuyahamasisha mataifa ya Amerika ya Kusini na Karibiani kuziunga mkono harakati zao za kudai uhuru wa Afrika. Jambo hili linaelezea umuhimu wa wasi wasi ulioanza kujitokeza katika miaka ya mwishoni mwa muongo wa 1970 wakati serikali ya kibaguzi ya Afrika Kusini iliyotaka kujipanuwa, ilipoanza kutafuta washirika kwa dhati, na kwa hiyo ikaanza kujenga uhusiano wa kimikakati na kiuchumi na nchi za Amerika ya Kilatino. Hata hivyo mwanzo wa ujenzi wa uhusiano wa kisiasa ulitokea katika muongo wa 1970 shughuli za Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote zilipoingia kwa mara ya kwanza katika eneo la Amerika ya Kilatino na Karibiani hasa katika Kongamano la Tatu la Mawaziri wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote mjini Georgetown nchini Guyana, na katika Mkutano wa Sita wa Kilele mjini Havana mwaka wa 1979. Shughuli hizo ziliongozwa na wahusika kutoka Karibiani pamoja na idadi iliyokuwa inaongezeka polepole ya uwakilishi wa Amerika ya Kilatino. Shughuli hizo zilielekea kuonyesha uwezekano wa kupata uhusiano wenye nguvu zaidi wa kisiasa kati ya Afrika na Amerika ya Kusini.

## Afrika katika Muungano wa Ulimwengu wa Tatu

Upanukaji wa uhusiano wa kisiasa, kiuchumi, na kitamaduni, kati ya Afrika huru, na maeneo mengine ya Dunia ya Tatu, ambao ulikuwa na viwango na vina tofauti, ulisaidia katika kuunda mwelekeo wa Dunia ya Tatu katika kuupinga uhusiano wa kisasa wa kiuchumi ulimwenguni, kwa nia ya kuzibadili desturi na miundo ya kimataifa ambayo, kutokana na historia, ilikuwa inaidunisha Dunia ya Tatu.
Ili kulielewa jukumu la Afrika katika uhusiano huu mpana, itasaidia tukijikita kwanza katika Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote, ambao ndio shirika la Dunia ya Tatu lililojitokeza kuwa lenye nguvu zaidi za kuelezea msimamo wa kisiasa. Pili yafaa tutazame pia (madai ya) mfumo mpya wa kiuchumi ulimwenguni, ambao katika muongo wa 1970 ndio uliojitokeza kama changamoto ya kiuchumi ya Dunia ya Tatu.

## Afrika na Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote

Ingawa falsafa yake ilianzia katika Mkutano wa Bandung wa mwaka 1955, mkutano wa kwanza wa kilele cha Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote ulifanyika mwaka 1961 mjini Belgrade na kuhudhuriwa na mataifa kadhaa ya Afrika na Asia, pamoja na Kuba na Yugoslavia. Kwa kudai kuwa na mtazamo wa kujitegemea kutokana na washirika wa Vita Baridi na uanachama wa mikataba ya kijeshi ya Mashariki na Magharibi, Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana

na Upande Wo Wote uliipita mipaka yake ya kwanza ambayo ilijikita katika masuala ya kimkakati ya kimataifa yaliyotokana na muktadha wa ugomvi kati ya Mashariki na Magharibi na kuwa sauti ya Dunia ya Tatu juu ya ukombozi wa kisiasa, kijamia na kiuchumi.

Baada ya uamuzi wa OAU kuhusu sera ya kutofungamana na upande wowote kulikuweko na mfululizo wa uanachama wa mataifa ya Afrika katika Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote. Kwa upande mmoja mfululizo huu wa uanachama uliifanya itikadi ya Umoja huo kukosa mshikamano thabiti kama ilivyokuwa hapo awali, na kwa upande mwingine ikawa na athari za kuuimarisha Umoja kwa njia nyingi. Kwanza, kutokana na upanukaji wa muundo wake, uhalali wake kama sauti kubwa ya kisiasa ya Dunia ya Tatu ulitekelezwa. Pili, upanukaji wa sifa za itikadi yake ulisaidia kupunguza ugomvi juu ya uanachama, jambo ambalo lilikuwa limeathiri kikao chake cha kwanza ambacho kilijadili sifa za kiitikadi ambazo nchi zinazoomba uanachama zinapaswa kuwa nazo. Tatu, mfululizo wa wanachama kutoka Afrika ulihakikisha kuwa baada ya hapo Muungano ungeshughulika zaidi na masuala mengi yaliyohusiana na mawasiliano kati ya Kaskazini na Kusini kutokana na hisia kali za Waafrika juu ya masuala yaliyohusiana na ukombozi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika bara ambalo lilikuwa katika uchungu wa ukombozi na utaifa mchanga.

Licha ya kuimarisha msingi wa uanachama wa Muungamo wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote Afrika ilichangia katika kutoa baadhi ya viongozi stadi zaidi wa Muungano. Wa kwanza kati ya viongozi hao alikuwa Gamal Abd-al Nasser wa Misri, ambaye pamoja na Rais Tito wa Yugoslavia na Waziri Mkuu wa India J. Nehru, walikuwa nguzo za siasa za kutofungamana na upande wowote. Raisi Kwame Nkrumah wa Ghana, ambaye alikuwa mmojawapo wa waanzilishi wa Muungano huu, ulipoanzishwa rasmi, katika mwaka wa 1961, alitimiza jukumu muhimu sana katika kuendeleza msimamo wa Waafrika wenye kuunga mkono siasa za kutofungamana.

Kuanzia miaka ya mwisho ya muongo wa 1960 hadi muongo wa 1970 viongozi wengine wa Afrika walitoa mchango muhimu katika kupanua na kuyabadili maono ya siasa za kutofungamana. Kwa mfano Rais Kenneth Kaunda wa Zambia, akiwa mwenyeji wa Kikao cha Tatu cha mwaka wa 1970, alisaidia kuuendeleza msimamo mkali na usio badilika wa Muungano kuhusu mahitaji ya ukombozi wa sehemu ya Kusini ya Afrika na pia kuwa mwenyekiti wa Muungano katika kipindi cha mabadiliko, kiprogramu, kuelekea malengo ya ukombozi wa kiuchumi. Na wakati huo huo Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania alijitokeza kuwa mmojawapo wa



PICHA 28.3 *Kutoka kushoto kuelekea kulia: J.B. Tito wa Yugoslavia, A. BenBella wa Algeria, A. M. Obote wa Uganda na H. Bourguiba wa Tunisia kwenye Mkutano wa Pili wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote huko Kairo, 5 - 10 Oktoba, 1964.*




**PICHA 28.4** *Mkutano wa Nne wa Kilele wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote, Algiers, September, 1973.*

vichocheo muhimu sana vya itikadi katika ubadilishaji wa mwelekeo wa Muungano. Alipourithi uwenyekiti kutoka kwa Kaunda, Rais Huari Bumedienne wa Algeria alitokea kuwa hodari sana katika kuuhamasisha Muungano kuzingatia lengo lake jipya la kutafuta mfumo mpya wa kiuchumi ulimwenguni.

Katika miongo miwili ya kwanza ya maisha ya Muungano, maendeleo na masuala ya Afrika yalikuwa na umuhimu mkubwa katika azima na mwelekeo wake. Haya yalikuwa dhahiri tangu mwanzo kwa sababu jambo moja lililoyaleta pamoja Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote lilikuwa umuhimu uliopewa masuala ya Afrika katika mwaka wa 1961. Masuala hayo yalikuwa ni kama vile ukatili uliyooneshwa na serikali ya kibaguzi ya Afrika Kusini katika mauaji ya Sharpeville, katika mwezi wa Machi mwaka huo, kuzidishwa kwa ukatili katika vita vya uhuru nchini Algeria, na kuvurugika kwa amani katika koloni la zamani la Wabelgiji la Kongo.

Kwa hiyo kuweko kwa mwelekeo mkali zaidi katika Muungano dhidi ya ubeberu, ambao ulidhihirika katika muongo wa 1970, pamoja na mabadiliko ya programu ili kulipa aula suala la Mfumo Mpya wa Kiuchumi Ulimwenguni yalikuwa, kwa jumla, ni matokeo ya hali halisi ya kisiasa na kiuchumi ya Afrika katika mfumo wa kimataifa na, pia, majibu ya Waafrika dhidi ya hali hiyo.

## Katika kusaka mfumo mpya wa kiuchumi Ulimwenguni

Tamko la "Mfumo Mpya wa Kiuchumi Ulimwenguni" lilionekana rasmi kwa mara ya kwanza katika Azimio la Kiuchumi la Mkutano wa Nne wa Kilele wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote wa mwezi wa Septemba mwaka wa 1973 mjini Algiers. Punde baadaye azimio hilo lilitumiwa kama msingi wa mazungumzo rasmi ya mwezi wa Aprili mwaka wa 1974 juu ya mali ghafi na maendeleo, ambayo yalikuwa sababu ya kuitishwa kwa mkutano maalum wa Sita wa Kikao Maalumu cha Umoja wa Mataifa ambamo Azimio na Mpango wa Utekelezaji juu ya Kuanzishwa kwa Mfumo Mpya wa Kiuchumi wa Kimataifa lilipitishwa. Mfumo huu mpya ulirasimishwa mwezi wa Desemba mwaka 1974, ambapo Kikao cha Umoja wa Mataifa kilipitisha Mkataba wa Haki za Kiuchumi na Wajibu wa Mataifa.

Kikao Maalum cha Saba cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kilichoitishwa mwezi Septemba mwaka 1975 kujadili maendeleo na ushirikiano kiliupeleka mjadala wa mfumo mpya mbele zaidi. Pia, kuanzishwa kwa mjadala kati ya Kaskazini na Kusini chini ya Umoja wa Mashauriano juu ya Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kimataifa (ambao ulikuja kujulikana kama Mashauriano ya

Jedwali 28.5 Composition of the Group of 77* 1964-80

Kaskazini na Kusini) kati ya mataifa 8 yaliyoendelea na 19 yanayoendelea, na hali uliodumu baina ya 1975 na 1977. Kufikia miaka ya mwisho ya muongo wa 1970, matumaini na mikwamo katika utekelezaji wa ajenda ya Mfumo Mpya wa Kiuchumi Ulimwenguni yalizusha utambuzi, miongoni mwa nchi ya Dunia ya Tatu, wa haja ya kurasimisha zaidi uhusiano wa kiuchumi kati ya Kaskazini na Kusini

Kiini cha Mfumo Mpya wa Kiuchumi kilikuwa ni utafutaji wa Dunia ya Tatu wa mabadiliko makubwa katika uchumi wa ulimwengu hasa katika sekta za biashara ya kimataifa, misaada ya kiuchumi, uwekezaji wa vitega uchumi vya kigeni, uhamishaji wa teknolojia na mabadiliko katika mfumo wa kifedha wa kimataifa. Mambo haya yaliwakilisha msingi na upatanisho wa madai anuwai ya Dunia ya Tatu kuhusu mabadiliko ya uchumi ya kimataifa yaliyofanywa katika miongo miwili iliyopita.

Hatua moja muhimu katika kukua kwa changamoto ya Dunia ya Tatu dhidi ya mfumo wa jadi wa uchumi wa kimataifa ilikuwa ni kuanzishwa kwa chombo cha Mashauriano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo UNCTAD mwaka 1964 kama Chombo cha Kudumu cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa. UNCTAD liliundwa kutokana na kutoridhika kwa Dunia ya Tatu na mfumo wa kibiashara wa kimataifa uliokuwa umewekwa chini ya Mkataba wa Jumla wa Forodha na Biashara (GATT) ambao ulikuwa umeanzishwa na nchi za Magharibi. Mikutano ya UNCTAD ambayo hufanyika kila miaka mitatu au minne ilitoa nafasi

kwa Dunia ya Tatu kuyaeleza na kuyapatanisha maslahi yao ya pamoja kuanzia UNCTAD ya kwanza mnamo mwaka wa 1964 hadi UNCTAD ya tano ya mwaka wa 1979.

Urithi mmoja muhimu kutokana na UNCTAD ulikuwa ni kuweka mazingira ya kuundwa kwa Kundi la 77, ambalo lilitokea kuwa shirika muhimu zaidi katika kuhamasisha Dunia ya Tatu juu ya maslahi ya kiuchumi, na pia kitengo cha kujadilia maslahi hayo. Kufikia mwaka wa 1980 Kundi la 77 lilikuwa limepanuka na kuyashirikisha mataifa yote 122 ya Dunia ya Tatu. Kati ya michango ya kundi la 77 ilikuwa ni pamoja na uundaji wa "Mkataba wa Algiers" mnamo mwaka wa 1967, uliandaliwa katika Mkutano wake wa kwanza wa mawaziri kama mkakati wa majadiliano katika kikao cha pili cha UNCTAD. Mkataba wa Algiers ulitokea kutambuliwa kama msimamo wa kwanza mpana zaidi wa Dunia ya Tatu juu ya maendeleo.

Sembamba na shughuli za kundi la 77 ni mabadiliko dhahiri ya msimamo wa Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana Upande Wo Wote ambao kufikia miaka ya mwisho ya muongo wa 1960 ulikumbatia masuala ya uchumi wa kimataifa kama mambo yenye umuhimu wa kwanza. Katika Mkutano wa Algiers wa mwaka wa 1973 Mfumo Mpya wa Kiuchumi wa Kimataifa ulizungumziwa kwa njia hiyo kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote ulijitokeza kuwa na jukumu muhimu, la kuanzisha uundwaji wa mfumo mpya wa kiuchumi ulimwenguni.

Katika muktadha huu wa maendeleo, hatua zenye ukakamavu zilizochukuliwa na wanachama wa OPEC, mnamo mwaka wa 1973, za kuongezea mapato yao ya mafuta na, pia, za kutaka kusimamia rasilimali hiyo zafaa kuonekana kama mkakati sambamba na Dunia ya Tatu katika majaribio yao ya kutaka kurekebisha ukosefu wa usawa wa uchumi wa kimataifa. Mtindo wa OPEC ulionekana kufaa kama njia iliyoonyesha kuwa uundwaji wa mashirika ya wazalishaji yangewawezesha kuendeleza mamlaka yao ya kiuchumi.

Kwa hiyo Mfumo Mpya wa Uchumi wa Kimataifa uliwakilisha kukutana kwa juhudi za kiasasi za awali za pande zote za Dunia ya Tatu. Kama Waamerika wa Amerika ya Kilatino walikuwa na umuhimu zaidi katika uanzilishwaji wa UNCTAD, Waafrika walikuwa ndio wenye jukumu kubwa zaidi katika kuhamasisha na kuubadili Muungano wa Mataifa Yasiyofungamana na Upande Wo Wote ili uzingatie mwelekeo huo huo. Nao Ulimwengu wa Waarabu na Waislamu ulitoa hamasa ya kuundwa kwa mashirika ya wazalishaji katika harakati za Dunia ya Tatu dhidi ya uchumi wa kimataifa.

Jukumu muhimu lililotimizwa na Waafrika katika uundaji wa Kundi la Afrika, Karibiani na Pasifiki (ACP) kama kundi la kudumu la kujadiliana na Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya mnamo mwaka wa 1975 lilikuwa ukumbusho mwingine wa athari za bara hili katika harakati za kubadilisha uchumi wa kimataifa. Vile vile majukumu yasio ya kawaida yaliyotekelezwa na Misri, katika mwisho wa muongo wa 1950 na miaka ya awali ya muongo wa 1960, na hata zaidi na Algeria, miaka kumi baadaye, katika kuhamasisha changamoto ya kiuchumi ya Dunia ya Tatu. Na kufikia miaka ya mwisho ya muongo wa 1970 Mwalimu Julius Nyerere alijitokeza kuwa kiongozi mmojawapo wa dhamiri ya Dunia ya Tatu, akiwa mtumainifu katika imani yake juu ya haja na uwezekano wa Dunia ya Tatu kujitegemea ndani ya mfumo wa kiasasi wa ushirikiano wa nchi za kusini.

## Afrika na Changamoto Inayoendelea ya Dunia ya Tatu

Wakati wa kuingia muongo wa 1980, ulimwengu ulishuhudia kufifia kwa wingi wa furaha ambayo iliandamana na uongezekaji wa changamoto ya Dunia ya Tatu katika muongo wa 1970. Kuongezeka kwa unyonge wa kiuchumi barani Afrika ambao ulizidishwa hasa na maeneo yaliyokumbwa na ukame na njaa kulikuwa mara nyingi kunatajwa kama unyonge wa Dunia ya Tatu kwa jumla. Mataifa ya Dunia ya Tatu, ambayo yalikuwa yanalemewa na mdororo wa uchumi usio na kikomo na kuongezeka kwa madeni yalikuwa yanazidi kudhoofika. Na majadiliano kati ya Kaskazini na Kusini yalikuwa yanaelekea kukwama.

Katika hali kama hizo ilikuwa ni rahisi kwa waliowaunga mkono watu wa Dunia ya Tatu, hasa Waafrika, kuchukua msimamo wa kukata tamaa. Hapa ndipo ambapo mtazamo wa kihistoria ungefaa kutumiwa, lakini sio kwa kumziba macho mtazamaji ili asione matatizo yanayokuja, bali katika kukumbusha juu ya vikwazo vya hapo awali ambavyo vilivukwa au kukabiliwa.

Kwa kuwa sura hii inakamilika katika miaka ya muongo wa 1980, yafaa kumalizia na kumbukumbu mbili za kihistoria ambazo pia zaturudisha nyuma mpaka mwanzo wa maandishi haya. Mwaka wa 1985 ulikuwa ndio ukumbusho wa kutimiza miaka mia moja tangu Mkutano wa Berlin ambapo mgawanyo wa Afrika uliafikiwa Pia mwaka wa 1985 ulikuwa ndio ukumbusho wa miaka thelathini tangu Mkutano wa Bandung ambao ulikuwa ndio hatua kubwa ya kwanza iliyoratibiwa ya Waafrika na Waasia dhidi ya mfumo uliowakilishwa na Mkutano wa Berlin. Kwa kuzingatia mitazamo hii miwili uhusiano wa Afrika na sehemu nyingine zinazoendelea na jukumu la Afrika katika harakati za Dunia ya Tatu ni mambo yaliyopiga hatua zinazoonekana.

# 29 Afrika na Umoja wa Mataifa tangu 1945

Umoja wa Mataifa (UN) kama tunavyoijua leo ni mtoto wa nguvu mbili kuu za kihistoria za karne ya ishirini. Vita vya Pili vya Dunia na mchakato wa ukombozi dhidi ya ukoloni wa baada ya vita hivyo.[1] Vita vya Pili vya Dunia viliongeza umuhimu wa kuanzisha asasi ya ulimwengu ambayo ingejishughulisha na kuendeleza amani. Ukombozi dhidi ya ukoloni ulibadili uanachama wa chombo hicho cha kiulimwengu na kugeuza urari wa mawazo katika asasi zake za kiuwakilishi.

Migongano iliyotokea duniani na harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni vilikuwa vimeungana, na Afrika ikawa dhahiri sehemu muhimu ya matokeo hayo mawili ya kiulimwengu. Ukatili na uharibifu uliotokea kwenye Vita vya Pili vya Dunia uliyatayarisha mawazo ya kimataifa kwa ajili ya jaribio jingine la kuleta amani ulimwenguni – chombo cha uwakilishi zaidi kuliko Shirikisho la Mataifa, na labda chombo chenye ufanisi zaidi. Ukatili wa mapigano na uhalifu wa kivita, unyama wa mauaji angamizi dhidi ya Wayahudi na wengine, ukubwa tu wa uharibifu wa maisha na mali – sababu hizi zote ziliifanya jumuiya ya kimataifa iwe tayari kwa jaribio jingine la kiulimwengu.

Lakini si vita pekee vilivyokiongoza chombo hiki kipya cha dunia. Kama tutakavyoona, ilikuwa pia enzi ya ukombozi dhidi ya ukoloni. Nchi nyingi zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni zilipata uhuru katika kipindi cha miaka 25 ya mwanzo ya kuwapo kwa Umoja wa Mataifa hivyo idadi ya wanachama wa Umoja huo iliongezeka kutoka 51 hadi 157 mwaka 1980. Kwa hiyo mabadiliko

[1] « Ukombozi dhidi ya ukoloni" unaelezwa hapa kama kumaliza utawala wa kikoloni, kubomoa asasi za kikoloni na kukomesha mitindo na athari za kikoloni. Wakati ambapo uanzishwaji wa ukoloni hufanywa na mamlaka za kifalme, uanzishwaji wa ukombozi dhidi ya ukoloni aghalabu huja kutokana na waliotawaliwa na mapambano yao kwa ajili ya ukombozi.

yaliyotokea Afrika ndiyo yaliyokuwa makubwa. Hivyo Afrika iliibuka tafatibu kutoka kuwa dola la utumwa na ukandamizwaji, na hasa tangu 1960, kwa hakika ilianza kupata hadhi kama bara lenye mataifa yanayojitawala na kuleta urari katika uhusiano wake na sehemu nyingine za dunia. Afrika pia haikuwa na uwakilishi wa kutosha katika Umoja wa Mataifa mnamo 1945, mtu anaweza kusema kuwa iliwakilishwa kwa kuashiriwa na mataifa manne yaliyokuwa huru kinadharia lakini yaliyokuwa tegemezi kiutekelezaji. Mataifa hayo yalikuwa Ethiopia, Liberia, Misri na Afrika Kusini. Wala Afrika haikuwakilishwa kabisa katika viti visivyo vya kudumu ninavyogawanywa sawa kijiografia kwenye Bara la Usalama kama inavyoelezwa katika Kifungu 23, aya 1 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa. Makubaliano yaliyokuwa yakitekelezwa katika chombo hicho tangu 1946 na kuendelea, yalivigawa viti visivyo vya kudumu kati ya maeneo mbalimbali ya dunia kama ifuatavyo: viwili kwa ajili ya Amerika Kusini, kimoja cha Ulaya Magharibi, kimoja cha Ulaya Mashariki, kimoja cha Mashariki ya Kati na kimoja kwa ajili ya Jumuiya ya Madola. Afrika iliachwa, na ilkuwa hadi hapo baadaye, Desemba 17 1963, kwa Azimio la 1991 (XVIII) la Baraza Kuu ndipo ilipofanywa haki kwa kuipatia viti vitano kati ya kumi visivyo vya kudumu vya Baraza la Afrika wa Asia.

Mradi Afrika ilibakia kuwa tegemezi (kama ilivyokuwa tangu 1945 hadi 1960), Umoja wa Mataifa ulichukulia kuwa ulikuwa na wajibu wa kuikomboa. Tangu wakati huo uhusiano wa UN na Afrika ulikuwa wa upande mmoja na hata mara nyingine kuwa wa kiutawala, ili mradi kuwa vitendo vilivyopangwa vilitokana na kuamuliwa na miongozo ya kigeni, kwa hakika ikiwa na nia ya kukanganya matakwa ya Afrika na ile ya jumuiya ya kimataifa au hata matakwa yao wenyewe.

Lakini kwa kuangalia nyuma tunaweza sasa kutambua kwa uwazi zaidi ruwaza pana za uhusiano. Tangu kuundwa kwake huko San Fransisco mwaka 1945 Umoja wa Mataifa umekuwa na majukumu makuu matatu (baadhi yao yakiwa yanagongana) kuhusiana na Afrika: UN kama chombo cha mamlaka ya pamoja ya utawala kilichorithiwa kutoka kwenye Shirikisho la Mataifa; pili, kama rafiki wa ukombozi; na tatu, kama mshirika wa maendeleo. Ni majukumu haya ndiyo yatakayoangaliwa kwenye sura hii, na mbinu yetu hapa itakuwa, kila inapowezekana, ya kuangalia mifano ya majukumu hayo matatu ya Umoja wa Mataifa.

Kwa kuwa jukumu la utawala la chombo hiki cha dunia (kabaila asiyekuwapo) lilikuwa ni la kiusaidizi, haliwezi kutenganishwa kiurahisi na jukumu la chombo hiki la kusaidia ukombozi. Tofauti na tawala nyingine za kigeni, Umoja wa Mataifa

ulikuwa na ari ya kuongeza kasi ya ukombozi dhidi ya ukoloni. UN kwa hiyo mara nyingi iligongana na mamlaka ya kikoloni ambayo yalikuwa yakitawala kwa niaba yao. Haikuwa rahisi kutambua pale ambapo jukumu lake la utawala wa kigeni wa pamoja lilipokwisha na jukumu lake kama msaidizi wa ukombozi lilipoanza. Mifano maalumu ya Namibia na watu wa Ewe ilidhihirisha baadhi ya utata huo. Hebu tuangalie mifano wa tukio hilo la Ewe kwa kirefu.

## UN kama Beberu Mkarimu

Aprili 10 1947, wakati Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa lilipofanya mkutano wake wa kwanza, mwenyekiti wake alipokea simu ya maandishi kutoka Accra (Gold Coast, sasa Ghana) ambayo ilisema ifuatavyo :


> Mkutano wa Waewe wote uliokuwa na Waewe wa Togo ya Wafaransa, Togo ya Waingereza, na Gold Coast, unawasalimu. Tunalaani na kupinga ugawanyaji wa nchi ya Waewe. Tunaomba kuunganishwa kwa nchi ya Waewe chini ya utawala mmoja utakaochaguliwa na watu wenyewe kwa kura ya maoni.

Suala la Waewe lilikuwa limeanza. Tangu mkutano wake huu wa kwanza wa 1947 hadi uhuru wa Togo ya Wafaransa mnamo 1960 Baraza la Udhamini halikuwa na mkutano hata mmoja ambao haukushughulikia swali hili moja kwa moja au kwa njia fulani.

Kwa Baraza la Udhamini hii ilikuwa mada kuu ambayo iliongoza itikadi yao na sehemu ya njia yao ya utekelezaji. Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa akawa mahali ambapo serikali nyingi zilianza kulishughulikia tatizo la siasa za ukoloni na kisha kujiingiza katika kampeni za ukombozi dhidi ya ukoloni.

Makazi ya Waewe yameenea kusini kote kwa Togo ya hivi sasa na kusini mashariki ya Ghana ya hivi sasa, na kidogokidogo kusini mwa Jamhuri ya Watu wa Benin na Nigeria.

Wakati wa mgawanyo wa Afrika baada ya Mkutano wa Berlin wa 1884-5 Waewe wengi walikuwa katika Togo ya Wajerumani, wakiwapo waehache waliozagaa Gold Coast na Nigeria. Togo ya Wajerumani ilipogawanywa katika eneo la Waingereza na eneo la Wafaransa hapo Oktoba 1 1920 (Mchoro 29.1) Waewe walitenganishwa zaidi ; lakini hakukuwa na msukumo mkubwa wa kuungana kwao tena hadi wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. 1943 kampeni ya




*Mchoro 29.1 Togo ya 1919 – Azimio la Wafaransa na Waingereza, London, Julai 10 1919 (kulingana na E.K. Koussi)*

magazetini ilianza huko Gold Coast (Ghana) kutaka Togo ya Wafaransa ichukuliwe ; na 1944 tapo la Waewe wote, " Mkutano wa Waewe Wote" lilianzishwa kwa upande wa Togo ya Wafaransa, *Comité de l' unité togolaise* (CUT) [Kamati ya Umoja wa Togo], hadi wakati huo ukiwa umoja wa utamaduni, lilijigeuza ili kuendesha propaganda kama hiyo, na lilimteua katibu wake mkuu Bw. Sylvanus Olympio, ambaye wakati huo alikuwa ofisa wa Kampuni ya United Afrika (tawi la kundi la Unilever), ambaye baadaye alikuwa rais wa kwanza wa Togo. Hivi ndivyo vilivyokuwa vyombo vilivyoukabili Umoja wa Mataifa mnamo 1947.

Suala la Waewe liliwasilishwa tena mbele ya Baraza la Udhamini katika mkutano wake Novemba 1947. Bw. Sylvanus Olympio aliwasilisha maoni ya Waewe kwenye Baraza hilo, na aliikosoa taarifa ya Wafaransa na Waingereza ambayo aliona kuwa masuluhisho yake yalikuwa hayatoshelezi.

Wakati wa majadiliano ya mwanzo inafaa kukumbukwa kwamba Baraza liliwazingatia sana walalamikaji, ambao waliruhusiwa kutoa maoni yao kwa maneno. Iwapo kwenye Kamati ya Udhamini ya Shirikisho la Mataifa, hililotawaliwa na tawala za kikoloni, wakoloni waliaminiwa kabisa, katika Baraza la Udhamini, ambako walikuwa wachache, hali ilikuwa kidogo ya kupinga ukoloni. Kama wapiga kura hawakuwakosoa Waingereza na Wafaransa ilikuwa kwa upande mmoja inatokana na mshikamano kati ya London na Paris ambao ulilivutia Baraza.

Mwishoni mwa Desemba 1949 – mwanzoni mwa Januari 1950, ziara ya ujumbe wa UN ulikwenda kwenye eneo na kuhakiki vipengele vikuu vya tatizo la Waewe. Ilihitimisha kuwa tatizo lilikuwa la kiuchumi tu :

> Watogo wengi wa pande zote mbili za mpaka wanafuata msimamo mkali wa siasa, na wanaeleza matatizo ya mpaka kama hoja mojawapo tu kati ya hoja nyingine ; *wanaeleza, kuwa muungano ni hatua muhimu katika kufikia serikali ya, madaraka na uhuru.*

Kwa maneno mengine walichukulia kwamba serikali ya madaraka au uhuru, ambao kulingana na Mkataba ni madhumuni ya misingi ya mfumo wa udhamini, hauna budi kupatikana kwa misingi ya dola la Togo lenye mipaka inayofanana na ile ya Togo ya Wajerumani ya zamani na kuwa kudumisha tawala mbili kulikuwa hakukubaliani na kufikiwa kwa matarajio yao.

Mwaka 1950 mamlaka ya utawala yalipendekeza kuongezwa kwa ukubwa wa Kamati ya Ushauri kuwashirikisha wanachama waliochaguliwa, sio walioteuliwa, katika kuwasilisha maoni. Ilikuwa dhahiri kuwa kwa upande uliokuwa chini ya

Waingereza, watu wa kaskazini walitaka wawe sehemu ya Gold Coast, ambapo kwa upande uliokuwa chini ya Wafaransa walitaka hali iendelee kama ilivyo. Katika hali hii, tatizo lilikuwa kwa Waewe pekee, ilionekana kuwa isingewezekana kuunda upya Togo ya Wajerumani ya zamani.

Uchaguzi kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa Kamati ya Ushauri ulifanywa wakati wa majira ya mpukutiko wa majani ya 1950. Haukuwa wa matatizo yoyote maalumu katika Togo ya Waingereza. Katika Togo ya Wafaransa kwa upande mwingine, CUT, ikitambua kuwa wangekosa ushindi kwa sababu ya mfumo wa uchaguzi uliochukuliwa, waliwatoa wagombea wake wote siku nne kabla ya uchaguzi. Viti vilivyotengwa kwa ajili yake vilitolewa kwa wapinzani wao. Parti togolais du progrés (PTP) [Chama cha Maendeleo cha Togo]. Kati ya wanachama 47 waliochaguliwa, wanane (Togo ya Waingereza) walitaka wawe sehemu ya Gold Coast, 15 walitaka muungano wa Waewe, na 24 walitaka hali iendelee kama ilivyo. Kamati ilikutana Novemba, lakini wajumbe sita wa Togo ya Waingereza walisusia kikao na wawakilishi wa CUT wakichukuliwa nafasi zao na PTP, hivyo upande wa mamlaka tawala ikipata ushindi kwa vyovyote vile. Hivyo wengi walipinga muungano wa Waewe.

Kamati ya Nne ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, ambayo wakati huo ilikuwa ikianza mkutano wake, ilipokea malalamiko ya kuilaumu serikali ya Ufaransa kwa jinsi ambavyo iliendesha uchaguzi na kwa kukamatwa ovyo kwa watu. Wajumbe kadha waliukosoa mwelekeo wa Serikali ya Ufaransa, ambayo ilitakiwa iunde tume ya uchunguzi wa utaratibu wa upigaji kura. Kwa mara ya kwanza katika Umoja wa Mataifa, nchi tawala ilishutumiwa vikali na wajumbe wasiotoka jumuiya ya Kikomunisti. Kwenye mkutano wa nane wa Baraza la Udhamini (Februari-Machi 1951) Waingereza na Wafaransa walijikuta kwenye utetezi, ingawa walijitayarisha kwa makini huko Washington na New York. Mawazo yaliyotawala ni kwamba mamlaka tawala zilikuwa zikitumia mbinu ya ucheleweshaji, na kwamba hatua thabiti ni lazima ichukuliwe kuzikomesha: Wamarekani na Wairaqi walipendekeza kuwapo kwa uchaguzi mpya, kwa vyovyote vile huko kusini. Mwishowe Baraza liliwataka watawala watafute suluhisho la tatizo kupitia kwenye Kamati kubwa zaidi.

Katika mkutano wa tisa wa Baraza la Udhamini wa Mei 1951, Uingereza na Ufaransa zilionekana kukosa ubunifu wa kuwasilisha mpango wa kuridhisha kwa Baraza. Waingereza walijali zaidi matokeo ya serikali ya madaraka ya Gold Coast, ambapo Wafaransa walikuwa wakipanga mabadiliko makubwa Afrika ya Magharibi: kwa hiyo pande zote mbili ziliona ni afadhali zisibadili hali ya Togo

zote mbili. Mradi mabadiliko hayo hayakuwa suluhisho la tatizo la Waewe lakini ni njia tu ya kuboresha maisha yao; walikosolewa na wawakilishi wa vyombo mbalimbali vya siasa vilivyotoa ushahidi mbele ya Baraza, na pia Wadachi, Wadominika na Waargentina, ambao waliona kuwa mpango hautoshelezi.

Waingereza na Wafaransa walipendekeza kuundwa kwa "Baraza jipya la Pamoja la Masuala ya Togo", ambalo madhumuni yake yangekuwa "kuwapatia mahali pa kukutania wawakilishi wa watu wa Togo zote mbili ambapo wangeweza kubadilishana mawazo juu ya maendeleo ya nchi hizo mbili, na hatua zinazochukuliwa ziratibiwe na kufuatiliwa ili kuhakikisha maendeleo katika nyanja zote." Novemba suala hilo liliwasilishwa kwenye mkutano wa saba wa Baraza Kuu. Wazo hilo lilitolewa tena, na lilikosolewa na "wazalendo wa Ewe".

Kamati ya Nne ilipendekeza kwamba watawala washauriane na vyama na makundi kabla ya kuunda Baraza la Pamoja, na pia kupanua mawanda ili kuweza kushughulikia matatizo yote ya Waewe na muungano. Ililiomba pia Baraza la Udhamini kutayarisha ziara ya kutathmini kwa kina tatizo na kutoa mapendekezo. Hivyo mamlaka ya juu zaidi (Kamati ya Nne ya Baraza Kuu) yalionyesha kuwa wakali dhidi ya tawala kuliko mamlaka ya chini yake (Baraza la Udhamini). Wakati huu suala la Waewe likaacha kuwa suala pekee na kuwa sehemu tu ya matatizo matatu ya pamoja, mengine mawili yakiwa: muungano wa Togo ya Waingereza na Gold Coast na serikali ya madaraka ya Gold Coast; na muungano wa karibu kati ya Togo ya Wafaransa na Umoja wa makoloni ya wafaransa, na wakati huohuo mwanzo wa serikali ya madaraka. Jambo ambalo lilianza kama tatizo la kimbari na kiutamaduni likawa sasa la nchi na siasa.

Tume maalumu ya Baraza la Udhamini ilikaa katika eneo hilo kati ya Agosti na Septemba 1951, ilitembelea nchi zote kwa majuma matano, na kupokea malalamiko 2,896. Taarifa yake ilitoa muhtasari wa hali ilivyokuwa. Watu wengi walitaka uhuru, lakini kwa masharti kwamba Watogo waliokuwa chini ya Uingereza, kuwa Waghana; na kwa wale waliokuwa chini ya Ufaransa, kujiunga na Umoja wa makoloni ya Ufaransa, masharti ambayo yaliongezeka juu ya madai ya muungano.

Kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Ziara, Baraza la Udhamini la Novemba 1955 lilikubali utaratibu wa kura ya maoni kuthibitisha matakwa ya watu. Katika Togo ya Waingereza kura ya maoni ilionyesha kuwa kuna 93,000 zilitaka wawe sehemu ya Gold Coast na 67,000 zilipinga ; lakini kusini-yaani kwenye maeneo ya Waewe hasa – wengi walipinga kuwekwa chini ya Gold Coast. Baraza la Udhamini likaamua Togo ya Waingereza iwe sehemu ya Gold Coast na kufuta makubaliano ya udhamini siku ya uhuru. Ghana, ambayo ilikuwa ni matokeo ya Gold Coast ya

zamani na kusini mwa Togo ya Waingereza, ikiwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa mnamo 1957.

Kwa upande wa Togo ya Wafaransa, uhuru wa Gold coast ulileta serikali ya madaraka kwa Togo. Mwaka 1956 Jamhuri ya Togo inayojitawala ilitangazwa, na kura ya maoni ilipigwa Oktoba. Kura 331,000 zilitaka mfumo mpya na 22,000 zilitaka mfumo wa udhamini uendelee.


Ikiwa, kwa maneno ya Mkataba, imefikia "uwezo wake wa kujitawala," Togo ingeweza kujitoa kwenye makubaliano ya udhamini. Lakini Baraza la Udhamini lilikataa kutangua makubaliano yake, lilitaka baraza la sheria la Togo kuchaguliwa upya kwa kura za wananchi wote na kuwa uchaguzi huo usimamiwe na tume ya

Hivyo suala la Waewe lilifikia kikomo, miaka 13 tangu lianze: Ghana ilikuwa huru; Togo ilikuwa huru; na Waewe walikuwa bado wamegawanyika. Umoja wa Mataifa ulikuwa umemaliza jukumu lake moja la mamlaka ya ubeberu wa pamoja.

## Kongo: mpito wa ubeberu wa pamoja

Kama kuna nchi ambayo historia yake ya ukombozi dhidi ya ukoloni inahusiana kwa karibu na kazi ya Umoja wa Mataifa, basi kwa hakika ni koloni la zamani la Ubelgiji la Kongo, sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Mchoro 29.2).

Masharti ya mwanzo ya maendeleo ya Afrika ni: kwanza umoja wa kitaifa, na pili, utangamano wa kimsingi wa kisiasa. Bila mambo hayo mawili, maendeleo endelevu huwa ni hadithi isiyotimilika. Mipaka ya jumuiya ya kisiasa ni lazima iwe salama (umoja wa kitaifa) na misingi ya mamlaka yake ya kisiasa ni lazima iwe ya kudumu vya kutosha (utangamano wa kimsingi wa kisiasa). Changamoto kubwa iliyoukabili Umoja wa Mataifa kama mshirika wa maendeleo ya Afrika ilitokea hasa wakati wa uhuru wa Kongo ya Ubelgiji – sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Umoja wa kitaifa (mipaka) pamoja na utangamano wa kisiasa (mamlaka) wa dola huru jipya vilikuwa vya mashaka: na Umoja wa Mataifa uliwekwa kati. Lakini swali bado linabakia je Tume ya Kongo ya UN ilikuwa aina mpya ya ubeberu wa pamoja wa Shirika la dunia? Au ulikuwa mfano wa UN kama mshirika halisi wa Afrika? Mwanzoni Marekani ilikuwa ikiunga mkono zaidi umoja wa taifa la Kongo (ilizuia mgawanyiko wa Kongo) kuliko utangamano wa kimsingi wa kisiasa (kuunga mkono serikali iliyochaguliwa kihalali ya Patrice Lumumba kama Waziri mkuu). Kuyumba kwa Katibu Mkuu wa UN na Marekani




29.2 *The Congo-Léopoldville*

mwishowe kulisababisha kuuawa kwa Patrice Lumumba. Utangamano ulilipiwa kwa gharama ya uhalali wa kisiasa. Na chanzo cha mgogoro huu kilirudi nyuma hadi karibu na siku ya Uhuru katika Leopoldville ya wakati ule, mji mkuu wa Kongo ya Ubelgiji "iliyokombolewa" karibuni. Ni mgogoro huu ndio tutakaouangalia kama mfano maalumu wa Umoja wa Mataifa kama mshirika wa maendeleo ya Afrika, msaidizi wa ukombozi wa Afrika na, kinyume chake, kama mamlaka ya ubeberu wa pamoja wakati huohuo.

Watekelezaji wakuu wawili wa tukio la 1960-1 la Kongo walipoteza maisha yao wakati wa mapigano hayo yasiyoeleweka: Lumumba aliuawa na Hammarskjöld alikufa kwenye ajali ya ndege ambayo bado haijaweza kuelezwa.[2]

Tangu Julai 15 1960, wakati wanajeshi wa kwanza wa UN walipofika kwenye mji mkuu wa Kongo Leopoldville, hadi Januari 14 1963, wakati serikali ya Katanga hatimaye ilikubali kumaliza mapigano, hakuna mabadiliko ya historia ya Kongo yanayoweza kuchanganuliwa bila kurejea kwenye mwelekeo wa UN. UN ilibidi iitikie wito wa serikali kuu ya kwanza ya Kongo. Mgogoro ulihusu pamoja na mambo yafuatayo:

(1) Hali ya kutokuwa tayari kwa Kongo kwa ajili ya uhuru uliotolewa rasmi na Ubelgiji;
(2) Kutokuwepo kwa wafanyakazi wenye ujuzi katika ufundi, siasa na jeshi; na
(3) Majivuno ya wawakilishi wa watawala wa kikoloni wa zamani.

Katika amri ya kila siku ya Julai 5 1960, Jenerali wa Kibelgiji Jansens, kamanda wa Jeshi la Kongo, aliwaambia watu wake wazi: "Uhuru ni sawa kwa raia. Kwa askari kuna nidhamu tu. Kabla ya Juni 30 mlikuwa na maofisa Wazungu... Hakuna kilichobadilika."

Kwa askari wa Kikongo waliokuwapo kwenye sherehe za uhuru na kuisikia hotuba ya Lumumba aliyoitoa mbele ya Mfalme wa Wabelgiji, huo ulikuwa uchokozi dhahiri kwa historia ya Afrika: kwao wao kipo kilichobadilika. Maasi yalianza kwenye kambi za "Leopold II" kando ya mji mkuu; na Thysville, kilometa

[2] C. Roire, 1967

200 kutoka hapo, majeshi yalitaka Afrikanaizesheni ya vyeo vya juu jeshini. Uasi huu, uliosababishwa na msimamo wa maofisa wa Kibelgiji, ulikuwa ndio mwanzo wa mgogoro mzima. Usiku wa Julai 5 Lumumba alijaribu kurudisha utulivu kwenye makambi yaliyoasi; Julai 6 Lumumba alimfukuza kazi Jansens na kumteua mjomba wake Lundula na katibu wake wa zamani Mobutu kuwa makamanda wa jeshi. Aliwapandisha vyeo maofisa wote wa Kikongo wa vyeo vya chini. Lakini vurugu za jeshi zilizidi.

Baadhi ya Wazungu waliteswa, wengine walitishwa, na uasi huu wa watumishi wao wa zamani. Suala hili la jeshi liliwapa sababu Wabelgiji ya kuimarisha majeshi yao yaliyobakia nchini. Vikosi kadha vya askari wa miavuli vilipelekwa Léopoldville, Luluabourg na Elisabethville kuwalinda wananchi wa Ubelgiji. Katika mji mkuu wa jimbo la Katanga haikuwa tu haja ya kurudisha udhibiti wa jeshi bali kufanikisha umalizaji wa vurugu. Siku tatu baada ya kuwasili askari wapya wa Kibelgiji – yaani, Julai 11 – Tshombe alitokea na kutangaza "uhuru" wa jimbo hilo.

Katika kujibu mapigo, serikali kuu ilimwomba Bw. Timberlake, balozi wa Marekani, askari 3000 wa Kimarekani wapelekwe Kongo, na Lumumba na Kasavubu walimpelekea simu Katibu Mkuu wa UN, wakati huo huko Geneva, kuomba msaada wa kijeshi wa UN. Serikali ya Leopoldville ilitaka Umoja wa Mataifa uingilie kati kumaliza uingiliaji kati wa Ubelgiji na katika suala hilo waliungwa mkono na Asia na nchi za kisoshalisti pamoja na nchi zenye msimamo mkali za Afrika ambazo baadaye ziliunda kundi la Kasablanka. Wajumbe wengi wa Baraza la Usalama lililokutana Julai 13, na Katibu Mkuu, kutokana na pendekezo la mmojawapo wa watu muhimu katika kipindi hicho chote, Mtunisia Mongi Slim, waliamua kupeleka jeshi la Umoja wa Mataifa huko Kongo ili kurudisha utulivu.

Hivyo dadu ilitupwa siku hiyo, Julai 14 1960: azimio la Mongi Slim (liliungwa mkono na Marekani, ambapo Waingereza na Wafaransa walibaki kuwa waaminifu kabisa kwa Brussels na kutotaka kulifanya jambo hilo kuwa la kimataifa) lilitaka tu "Serikali ya Ubelgiji iondoe majeshi yake," na kutoa msaada wa kijeshi wa UN kwa serikali ya Kongo hadi "Majeshi ya Usalama ya Kitaifa" yatakapokuwa "na uwezo, kwa mawazo ya serikali, kutimiza wajibu wake." Hii ilikuwa tofauti kabisa na ombi la Lumumba na Kasavubu. Kwenye simu yao ya pili kwa Hammarskjöld, walisema : "msaada unaotafutwa si wa kurudisha hali ya ndani ya Kongo bali ni kuwalinda wananchi dhidi ya mashambulizi ya majeshi ya nchi mama ya Ubelgiji."

Jioni ya Julai 15 majeshi ya kwanza ya UN, Watunisia 300 na Waghana 800, walifika Léopoldville chini ya kamanda wa Kiswidi Jenerali Van Horn. Jeshi la UN lilianza kazi siku chache baadaye ; na wakati Lumumba alipokwenda Marekani mwishoni mwa Julai jeshi la usalama lilikuwa na askari 11,155. Jeshi kubwa zaidi, ambalo lingekuwa na athari kubwa katika siasa kwa majuma machache baadaye, yalikuwa yale ya Moroko (askari 2465), Ghana (askari 2,412) na Tunisia (askari 2,151). Lakini kwa jicho la serikali ya Kongo, kuwepo kwa majeshi ya UN hakukuleta suluhisho la matatizo yao kuweza kuhalalisha kuwepo na kufanya kazi nchini hapo : kujitenga kwa Katanga kulikuwa kunaimarika na majeshi ya Wabelgiji bado yalikuwapo.

Mkutano mwingine wa Baraza la Usalama ulifanyika Julai 21 na 22, na kutoa azimio jingine. Baraza la Usalama liliamua kushikilia tafsiri yake ya mwanzo ya jukumu la majeshi ya UN : kuhakikisha utulivu. Kusita kwa Hammarskjöld katika kipindi hiki, kulihalalishwa na kutokea kwa mfarakano katika serikali ya Kongo. Iwapo Lumumba, na mawazo yake ya umoja na serikali kuu, alitaka kujitenga kwa Katanga kukomeshwa, kwa kutumia nguvu ikiwa lazima, Rais Kasavubu aliendelea kupendelea suluhisho la Shirikisho ; mwanzoni mwa Agosti alituma simu kwa Baraza la Usalama kuelezea hoja hiyo. Uchaguzi huu wa Shirikisho ulikuwa na maana kwamba bado kulikuwa na uwezekano wa kushauriana na Tshombe.

Utata na mkanganyiko ukaongezeka. Hivyo Baraza la Usalama lilipokutana kwa mara ya tatu Agosti 8 na 9, 1960, lilikuwa ni kwa ajili ya kumsikiliza katibu mkuu akiulizia mipaka ya mamlaka yake. Alitaka kujua kama majeshi ya UN yaende kuingia jimbo la Katanga kwa namna yoyote ile. Swali hili la wazi lilipata tena jibu lisilo dhahiri kutoka kwa Baraza la usalama : azimio la tatu la Mongi Slim lilitambua wazi kuwa ilikuwa "lazima kabisa" kwa majeshi ya UN kuingia Katanga, lakini lilisema vilevile katika aya iliyofuatia kwamba jeshi la UN "halitashiriki katika mgogoro wowote wa ndani, halitaingilia kati kwa njia yoyote ile mgogoro wa namna hiyo, na halitatumikiwa kuathiri matokeo yake. "

Katika hali hiyo, Hammaskjöld ilimbidi atoe maamuzi muhimu peke yake. Agosti 10, wakati ambapo hakuna mtu, hata Ubelgiji, aliyetambua uhuru wa Katanga, Hammarskjöld alituma simu kwa Tshombe kutaka UN "mabadilishano ya mawazo ya ukweli" juu ya " mipango ya majeshi ya Umoja wa Mataifa kufanya kazi Katanga. " Agosti 12 alitua Elisabethville na Jenerali Kettani wa Moroko ya Wafaransa na wanajeshi 300 wa Kiswidi : na baada ya siku mbili za mazungumzo Tshombe alimfanya akabaliane na masharti manane kati ya kumi aliyoyaweka

kuhusiana na kuingia kwa majeshi ya UN Katanga. Kati yao ni kuwa UN wataingilia kati mambo ya ndani au ya utawala wa Katanga ; kutoruhusu njia yoyote ya usafiri, ndege au nyingineyo, kuwaruhusu watu watakaotumwa na Léopoldville au marafiki zao kuingia Katanga, mpaka katiba ya Kongo itakapotungwa na kuthibitishwa na Katanga : hali iliyopo itaendelea kwa kutumia katiba ya Katanga. Kwa kukubaliana na masharti hayo, katibu mkuu alikuwa amekubali kanuni ya kuwepo kwa pamoja jeshi la UN na Katanga, na kumaanisha kutoisaidia Serikali kuu ya Kongo kuweza kulidhibiti tena jimbo hilo lililojitenga. Kwa kumwamini Tshombe, na kupitia kwake Wabelgiji, katibu mkuu alikuwa amefanya kosa kubwa. Hakuwa tu ameridhia [illegible]

kibeberu.

Agosti 14 1960, Lumumba aliyapinga makubaliano ya Hummarskjöld, na aliwasilisha Umoja wa Mataifa matakwa matano ya wazi ambayo yalikuwa yakipingana kabisa na mwafaka wa Elisabethville. Waziri Mkuu wa Kongo alitaka chombo hicho cha kimataifa.

(1) kiipe askari na polisi wa Kongo kazi ya kulinda viwanja vya ndege vya Kongo;

(2) kupeleka mara moja majeshi ya Waafrika Katanga;

(3) kuipatia serikali kuu ya Kongo ndege ya kusafirishia majeshi yake popote nchini;

(4) kwenda mara moja kukamata silaha zote zilizogawanywa na Wabelgiji Katanga na kuziwasilisha silaha hizo serikali kuu; na

(5) kuondoa mara moja majeshi yasiyo ya Waafrika Katanga.

Mgogoro uliongezeka na mielekeo ya ubeberu mamboleo kwa upande wa maofisa na majeshi ya Umoja wa Mataifa ikawa dhahiri wakati hapo Septemba 5, baada ya mkutano na wajumbe wawili wa Ubelgiji, Mabwana Denis na Van Bilsen, Rais Kasavubu aliamua kumfukuza kazi Lumumba ambapo alitangaza redioni saa 2.15 usiku. Mgongano baina ya watu hao wawili ulifukuta tangu wakati wa mapambano ya uhuru. Kasavubu aliamua kuuibua wakati ambapo Lumumba alionekana kupoteza nguvu zake za kimataifa: ni nchi za kikomunisti, pamoja na Jamhuri ya Muungano ya Uarabu na Indonesia, walimuunga mkono kikamilifu katika

kutokubaliana kwake na Hammaskjöld. Kwa hakika waziri mkuu alijaribu kujibu kabla ya saa moja kufika tangu tangazo la adui yake, alikwenda kwenye stesheni ya redio na kutoa hotuba ambapo alisema kuwa "hakuna tena mkuu wa nchi".

## Juu ya Ushahidi na Mageuzi

Hapa tunakuja kwenye tukio moja linalosumbua zaidi katika shughuli za wawakilishi wa UN. Adhuhuri ya Septemba 6, Andrew Cordier, rafiki wa karibu wa Dag Hammarskjöld aliamuru kikosi cha Waghana chini ya amri ya Kanali Ankrah kulinda jengo la stesheni ya redio, na alimpelekea kijibarua cha kumkataza asiongee tena na wananchi wake hapo mbele. Wakati huohuo kikosi cha Moroko cha jeshi la UN kilichokuwa chini ya Kettani kiliizingira nyumba ya Waziri Mkuu. Ubeberu wa pamoja ulikuwa ukiwatumia askari wa Kiafrika kumzuia Lumumba kuendeleza uhuru wa kimagharibi na umoja wa nchi ya Kongo.

Wakati Lumumba aliomba bila mafanikio kupatiwa kiti kwenye ndege iliyokuwa ikienda New York, ambako alitaka kwenda akatoe maelezo yeye mwenyewe juu ya msimamo wa serikali yake UN, Kasavubu, ambaye UN wakati huo ikimchukulia kuwa ndio mamlaka pekee halali yasiyokuwa na mgogoro, alikwenda Manhattan bila tatizo lolote. Katika kuhitimisha majadiliano, kwenye chumba cha mkutano wa kwenye shoroba, mkutano ambao ulidumu tangu Novemba 7 hadi 22, Kasavubu alitambuliwa kuwa ndiye Mkongo pekee anayestahili kuteua ujumbe wa kuiwakilisha nchi yake.

Kasavumbu aliporudi Leopaldulle kwa ushindi mkubwa jioni ya Novemba 27, Lumumba alikuwa ameshindwa hatimaye. Mkuu pekee wa serilai kuu ya Kongo aliyetawazwa kihalali na bunge alikuwa ametupwa nje. Tegemeo lake pakee wakati huo lilikuwa Antoine Gizenga, ambaye Novemba 13 alichukua nafasi ya Finant kama mkuu wa serikali ya jimbo la Stanleyville. Katika kujaribu kutoroka kutoka L'iopoldville Desemba 1960 kwenda jimbo la Mashariki, alikamatwa na majeshi ya Mobutu na baadaye kupalekwa Katanga ambako alipigwa risasi mbele ya Tshombe na mawaziri wake Januari 17 1961. Ulikuwa ni msimamo huu wa kumpinga Lumumba kwa upande wa Umoja wa Mataifa, hadi kutangazwa rasmi kwa kifo cha Lumumba na Muuongo Februari 13 kulikoudhi duniani wakati huo.

Lumumba hakufa bure, nchi za Asia na Afrika, ambazo ziliyumba kati ya pande hizo mbili lakini sasa walikuwa thabiti kikweli, ziliweza kutoa azimio, ambalo lilizipa nguvu mpya shughuli UN. Waraka wa Februari 21, uliokubaliwa wakati habari zilipopokelewa, tena kupitia kwa Dayal, juu ya mauaji ya viongozi sita wa



*PICHA 29.1 Juu kushoto: Dag Hammarskjöld (kushoto), katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa na Joseph Kasavubu (aliyekaa kulia, mbele), rais wa Kongo, walipokutana Leopoldville Julai 29 1960; juu kulia: Tshombe, Waziri Mkuu wa jimbo lililojitenga la Katanga (sasa Shaba), Elisabethville (sasa Lubumbashi), Agosti 1960; chini kushoto; P. Lumumba, waziri mkuu wa Jamhuri ya Kongo; chini kulia: Kanali J.D. Mobutu, mnadhimu mkuu wa Jeshi la Kongo, Septemba 1960.*

tapo la Lumumba yaliyofanywa na Kalondji huko Kasai, ulitoa amri kwa majeshi ya UN kuepuka hatari ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kutumia nguvu iwapo ni lazima kama njia ya mwisho" katika kurudisha amani. Azimio, ambalo pia lilitoa wito wa kuchukuliwa hatua za kuondoa askari wa kulipwa na "wanajeshi na wasaidizi wa jeshi wote wa Kibelgiji na washauri wa kisiasa", waliorejea wazi umoja na ukamilifu wa nchi ya Kongo. Hammarskjöld hivyo angeweza, kama angependa, kukomesha kujitenga kwa Katanga na kuingilia kati kwa Wabelgiji

kwa kutumia nguvu. Hata hivyo, Kasuvubu ambaye mamlaka yake yalitambuliwa na Umoja wa Mataifa, aliukatalia Umoja wa Mataifa haki ya kuingilia kati. Lakini Aprili 17 Kasuvabu alikubaliana na hoja za wajumbe wawili wapya wa Katibu mkuu, Gardiner kutoka Ghana na Nwokedi kutoka Niger: alikubali kushirikiana na Umoja wa Mataifa kwa yeye kukubaliwa ahadi mbili (ambazo zilitimizwa) – kurudishwa kwa Mhindi Dayal na msaada wa fedha kwa ajili ya utawala wa Léopoldville.

Matokeo ya makubaliano haya ni Mkutano wa Coquilhatville wa majimbo yote yaliyokuwa yakimpinga Lumumba. Kasavubu alisema kuwa anatambua maazimio yote ya UN na alitaka kuitisha bunge la Kongo. Wakati Tshombe alipoonyesha kutokubaliana kwake majeshi yaliyomtii Kasavubu yalimkamata kiongozi huyo wa Katanga, alibakia chini ya kifungo cha nje huko Leopdville hadi alipokubaliana na pendekezo la mkutano wa bunge. Kwa muda mfupi ilionekana kama suluhisho la matatizo ya Kongo lilikuwa linakaribia. Lakini matarajio hayo yalikufa pale Tshombe alipogeuka kabisa baada ya kurudi Elisabethville. Bunge la Kongo lilikutana Julai 27; na kukiwa na wingi dhahiri wa tapo la Lumumba, waliichagua serikali ya umoja wa kitaifa iliyoongozwa na Adoula. Lakini tatizo lilibaki palepale: jeshi la Kongo lilifuata sera yake tofauti, na juu ya yote Tshombe na walinzi wake waliimarisha kujitenga kwao. Jumla ya mamluki na "washauri" waliokuwa Katanga wakati huo wanakadiriwa kuwa 1500. Bado, hadi mwisho, maofisa wa UN huko Kongo walidhani kwamba wangeweza kutimiza kazi yao bila kutumia nguvu.

Kwa amri iliyotiwa saini na Kasavubu, majeshi ya India na Sweden yalijaribu kuwakamata na kuwaondoa mamluki kuanzia Agosti 28 1961. Majeshi ya UN yalishika kiwanja cha ndege na sehemu nyingine muhimu za Elisathethville bila kupiga risasi hata moja, na yaliwachukua wafungwa 273 "wasio Waafrika" ikiwa pamoja na Wabelgiji 237. Hadi Septemba 13 kila kitu kilikwenda vizuri. Lakini majeshi ya UN ya askari wa Kihindi, kwa makubaliano na mwakilishi wa UN na eneo hilo, O'Brien, walipojaribu kulishughulikia suala hilo kwa dhati – kuwanyang'anya silaha mamluki wa Falgues na Lasimone – kukawa na mpigano makali, Kila mahali, huko Katima na Jodotville, majeshi ya UN yalitengwa na kuzingirwa.

Mapigano hayo ya Septemba 13, yaliyanza vibaya bila matayarisho, na bila ruhusa dhahiri ya maofisa waandamizi wa Umoja wa Mataifa, yalikuwa ni ushindi kwa Hammaiskjöld. Kwa upatanishi wa Waingereza, ambao walijishughulisha sana wakati huo, Bw. Hammarskjöld alitafuta na kupata ahadi ya Tshombe ya kukomesha mapigano na kujadiliana. Lakini hilo halikutokea. Septemba 17 mara

baada ya saa sita usiku, ndege iliyokuwa ikimsafirisha Hammarskjöld kwenda Ndola, Rhodesia kasikazini (sasa Zambia) iligeuka kwa haraka kiwanjani na kuanguka kilometa 12 kutoka hapo. Kifo cha Hammarskjöld, kama cha Lumumba, hakikuwa cha bure, kwani kilisababisha uamuzi thabiti wa kukomesha kujitenga kwa Katanga kwa njia yoyote ile, kama ilivyodhihirishwa kwenye azimio la Novemba 21 1961 lililodhaminiwa na UThant, katibu mkuu mpya. Azimio hili lilieleza wazi matumizi ya nguvu ya vikosi vya UN vilivyokuwa Kongo kama ni lazima ili kuwakomesha mamluki na kumaliza kujitenga kwa Katanga. Jeshi la UN sasa lilipewa zana ambazo huwakuwa nazo; hasa Waamerika ambao walitoa ndege za jet. Madhumuni ya mapigano yaliyoanzishwa na majeshi ya UN Desemba 18 yalikuwa ya kisiasa; kumfanya Tshombe ajadiliane. Hivyo, mji wa Elisabethville ulipokamatwa, wale waliounga mkono amri mpya ya UN, yaani Wamerikani, nao walijitolea kumaliza hali hiyo kwa kuungana. Tshombe akakubali kujadiliana na L'eopoldville. Majadiliano hayo yalipoharibiwa na kuyumbayumba na ukwepaji wa Tshombe, UN ikiungwa mkono kikamilifu na Wamarekani walianzisha mapigano ya kumalizia. Mapigano hayo yaliyofanywa kwa makini siku ya mwanzo za January 1963, yalimalizwa kwa tangazo la kusalimu amri la mawaziri wa Katanga. Wakati ngome yake ya mwisho ya Kolwezi iliposalimu amri Januari 21, Tshombe alikuwa tayari amekwishashindwa: juma moja kabla, umoja wa wachimba madini ulikuwa tayari umekwishatangaza kuwa kuanzia wakati huo wako tayari kulipa mrabaha wa uchimbaji kwa serikali kuu. Mamluki kwa upande wao waliamua kukimbilia Angola kwa muda. Tshombe, baada ya kujaribu kubakia kwenye siasa kwa miezi michache zaidi, alikwenda Ulaya Juni 15 1963.

Hakurudi tena Kongo hadi mwaka mmoja baadaye, Juni 26 1964, siku nne kabla majeshi ya UN hayajaondoka, ambayo licha ya kuyumba kwa wakubwa wao waliweza mwishowe kukomesha kujitenga kwa Katanga. Je UN ilikuwa imemaliza kazi ya kijeshi kweli? Kama madhumuni yake yalikuwa kurudisha amani Kongo, basi majeshi ya UN yangebidi yabaki huko kwa muda mrefu zaidi: 1964 ulikuwa, kusema kweli mwaka wa vita vibaya zaidi, nchini humo vilivyowahi kutokea tangu uhuru. "Maasi" yalizagaa, lakini Umoja wa Mataifa haikuingilia kati.

Katika miezi ya mwisho ya kukaa kwao, askari 5350 wa UN waliobaki hawakufanya chochote zaidi ya kuwa amana ya uhalali wa serikali kuu ya Adoula. Hakuna aliyependekeza kuendelea kuwapo kwa majeshi ya UN Kongo alfajiri ya Juni 30 1964.

Je UN ilitimiza wajibu wake Kongo? Je Kongo ingeondokana na vurugu

mapema kama shirika hilo la kimataifa lingechukua hatua haraka na kwa uthabiti dhidi ya kijitenga kwa Katanga na wasaidizi wake wa nchi za Ulaya? Je Umoja wa Mataifa ulihakikisha mafanikio kwa niaba ya raghba ya jumuiya yote kimataifa, au ya upande mmoja tu? Maswali haya, ambayo historia pekee ndiyo labda inaweza kuyajibu, hayawezi kubadili ukweli: kuingilia kati kwa Umoja wa Mataifa, ambako kuliombwa na Patrice Lumumba, kulikuwa muhimu; "vita baridi" havikuingizwa Kongo na shirika hilo la kimataifa, vilimgia huko kwa sababu Afrika (kwa sababu ya madini yake) na pia mojawapo ya nchi zilizokuwa rahisi zaidi kudhuiriwa (kwa sababu ukoloni wa ubelgiji haukujali). Je kungetokea nini Kongo bila Umoja wa Mataifa? Kwa kuwapo UN angalau iliweza kuendelea kuwapo.

UN ilikuwa imetimiza majukumu yake matatu huko Kongo yanayohusiana na Afrika. Wakati mwingine UN ilikuwa mamlaka ya ubeberu wa pamoja na dhambi zake za dharura na utendaji zimelipwa na maisha ya Patrice Lumumba. UN ilikuwa pia mshirika wa maendeleo ya Afrika huko Kongo - ikijaribu kulinda sharti kuu la umoja wa kitaifa na utangemano wa kisiasa kwa ajili ya Kongo iliyokuwa rahisi kuvunjika. Lakini UN ilikuwa pia msaidizi wa ukombozi wa Afrika kwani ilijaribu kuzuia aina mpya ya kurudi tena kwa ukoloni wa Wabelgiji na wengine huko Kongo.

Katika jukumu lake hili la kuwa msaidizi wa ukombozi wa wa Afrika UN ilikuwa ikiendeleza desturi yake mpya ya kusaidia kukomesha ukoloni – desturi ambayo ilipata jaribio kubwa katika suala la madai ya Ufaransa juu ya Algeria. Hebu sasa tuangalie ukombozi dhidi ya ukoloni huko Algeria na kwingineko.

## UN Kama msaidizi wa ukombozi

Kwa UN kuwa rafiki wa kuondoa ukoloni na ukombozi wa Afrika, tatizo la Algeria lilikuwa ndilo gumu zaidi katika miaka ya 1950. Mamlaka chache ya kibeberu yamepinga kupoteza makoloni yake kama ilivyokuwa kwa Ufaransa katika kuipoteza Algeria. Na bado Ufaransa ilikuwa mjumbe wa kudumu wa Baraza la Usalama (mwenye kura ya turufu) na rafiki wa Marekani katika North Atlantic Treaty Oranisation (NATO) [Shirika la Kujihami la Atlantiki Kaskazini] tangu 1948 na kuendelea. Kwa hali hiyo, chombo hiki cha dunia kilikuwa na nafasi gani ya kuunga mkono vuguvugu la ukombozi wa Algeria? Hebu tuangalie maendeleo ya suala la hili la Algeria kwa kina zaidi.

Ni jambo linalojulikana dhahiri kwamba UN ilijishughulisha na kuzisaidia nchi za Afrika zilizopata uhuru wake karibuni kuharakisha mchakato wa kuondolewa kwa ukoloni. Hii ni kweli kwa Afrika ya Kaskazini na Afrika ya watu weusi.

Oktoba 16 1952 Baraza Kuu liliamua kuingiza kwenye ajenda yake tatizo

lililojitokeza kutokana na majukumu ya Ufaransa huko Tunisia na Moroko. Ufaransa ilitoa hoja bila mafanikio kwamba Umoja wa Mataifa hauna mamlaka, wakitumia kifungu maarufu cha 2, aya 7, cha Mkataba ambacho kinaizuia UN kuingilia kati mambo ya ndani ya nchi wanachama. Bw. Robert Schumaun hakuweza kuliridhisha Baraza kuwa mambo ya nchi hifadhi hizo yanaihusu Ufaransa pake yake, na azimio la kwanza kuzihusu lilipitishwa Desemba 1952.

Baraza liliweza kutoa shinikizo kubwa na kuwa makini katika maendeleo ya mgogoro wa Algeria, ambao ulikua hadi kuwa vita dhahiri baada ya 1954. Serikali ya Ufaransa ilidhani ilikuwa imara zaidi kisheria juu kutoingiliwa kati katika suala la Algeria. Lakini (na tunanukuu hotuba ya Ben Bella aliyoitoa kwenye Baraza Kuu Oktoba 9 1962, baada ya kura ya kauli moja iliyoingiza nchi yake Umoja wa Mataifa).

Kwa miaka saba suala la Algeria limekuwa likiletwa mara kwa mara katika kila mkutano wa Baraza. Malumbano yalivyojitokeza yamegeuza mwelekeo wa mgogoro, na wajumbe walikuwa na nafasi ya kuelewa mawanda ya mgogoro huu na kufahamu mazingira yake.

Kesi ya Algeria (mchoro 29.3) inaonyesha hasa jukumu lililochukuliwa na Umoja wa Mataifa katika kuondoa ukoloni. Mambo yote yaliyofanywa na Serikali ya Ufaransa kwao kuhusiana na suala la Algeria yalionekana kwenda sambamba na jinsi ambavyo Baraza Kuu lilichukua suala hilo. Kwa mfano, malumbano ya bunge la Ufaransa ya 1957 na kupitishwa kwa sheria huria zaidi kuhusu Algeria yalikuwa na nia ya kutoa urari kwa athari za mawazo ya kimataifa juu ya Ufaransa kuimarisha vita vyake huko.


Septemba 1955 katika Baraza Kuu la Kumi, nchi za Asia na Afrika zilijaribu kwa mara ya kwanza kuufanywa Umoja wa Mataifa kuliangalia tatizo la Algeria kama jambo linaloweza kutishia amani duniani. A. Pinay, Waziri wa mambo ya nje wa Ufaransa, alirudia hoja kufuatana na msingi wa Kifungu 2 aya 7: Algeria imekuwa kwa miaka 125 sehemu halali ya Ufaransa, kwa hivyo hapo kifungu hicho cha Mkataba kitumiwe. Lakini licha ya mbinu za kushawishi zilizofanywa ilikuwa Septemba 30 1955, kura 28 zilipotoka suala hilo liwe kipengee cha ajenda, 27 zilipinga na 5 zilijitoa. Ni wakati huo Ufaransa "ilifunga mlango", kwa muda ilichukua msimamo wa kuwa nje na kufanya ieleweke kuwa ilikuwa tayari hata kutoka kwenye Umoja. Hivyo Baraza lilibidi liangalie upya uamuzi wake: Novemba 25 1955, tatizo la Algeria liloondolewa kwenye agenda, na Ufaransa ilianza tena kuhudhuria vikao. Suala lilokuwa limeahirishwa tu: Mwakilishi wa Front de liberation

nationale (FLN) [Chama cha Ukombozi wa taifa], pamoja na kundi la Afrika na Asia, punde waliunda kamati ndogo ya kulishughulikia suala hilo (ilikuwa chini ya uenyekiti wa U Thant, wakati huo akiwa mjumbe wa Burma).

Juni 1956 Baraza la Usalama lilipokea ombi la kulitaka likutane baada ya kukabiliwa na nchi za Kiarabu kulingana na vifungu 34 na 35 vya Mkataba (ambapo nchi mwanachama yoyote inaweza kulitakabalisha Baraza la Usalama juu ya "ugomvi au haki yoyote... inayoweza kuhatarisha kuwapo kwa amani na usalama wa kimataifa"). Hivyo pia ilishindwa. Kundi la Afrika na Asia, wakitoa hoja kwamba Ufaransa (ambayo ilishutumiwa kupigana vita vya maangamizi) ilivunja Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu, kwa hiyo walikuwa wakitoa ombi upya la kuliingiza suala hilo katika ajenda ya Baraza kuu la Novemba 1956, na walipata bila malumbano. Azimio la kimwafaka la Amerika ya Kusini lilipitishwa Februari 1957, baada ya mswada wa kundi la Afrika na Asia kukataliwa na Kamati ya siasa. Azimio jipya – lililoundwa kwa nia ya kutowaudhi Wafaransa sana – wala halikutaja haki ya watu wa Algeria kujiamulia mambo yao wenyewe lakini lilitamka tu matarajio kwamba "katika hali ya ushirikiano, suluhisho la demokrasia, amani na haki litapatikana kutumia njia mwafaka, kulingana na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa."

Hata hivyo, kura hii ilikuwa ni mafanikio kwa FLN kwa kuwa ilithibitihsa kwa namna fulani mamlaka ya Umoja wa Mataifa. Mfuatano wa matukio katika mkutano wa Septemba 1957 yalikuwa hivyohivyo: kuingizwa kwenye ajenda bila mdahalo na bila kupingwa na Ufaransa, ambayo (japo bado ilikuwa ikiendelea na hoja yake ya kisheria ya mamlaka ya ndani) ilitegemea kuchukua fursa ya majadiliano hayo "kujibu shutuma na kashfa" zilizoelekezwa kwao na kutoruhusu wapinzani wao kutawala jukwaa.

Suala la Algeria lilikuwa ishara ya hali mpya ya kuupinga ukoloni iliyokuwa kwenye chombo hiki cha dunia. 1958 kikundi cha Afrika kiliundwa kilichopinga kwa dhati ubeberu. Ghana (ambako viongozi wa *Union des populations du Camoroun* (UPC) [Umoja wa Watu wa Kameruni], walikuwa wakiishi) na Guinea waliunga mkono mswada wa azimio lililotaka kuondolewa kwa kupigwa marufuku UPC na kufanya upya uchaguzi wa Kameruni chini ya udhibti wa Umoja wa Mataifa. India na nchi nyingi za Asia ziliunga mkono pendekezo la Ufaransa lililolenga katika kuipatia uhuru Kameruni bila kuwepo uchaguzi mpya. Azimio hilo lilipita. Shinikizo liliwekwa pia na nchi za Kiafrika kuunga mkono FLN ya Algeria, na hii ilileta uhasama kwa Ufaransa katika kila kikao. Zaidi ya hapo kampeni za




*MCHORO 29.3 Algeria (Kulingana na E.K. Kouassi)*

kupinga ubaguzi wa rangi zilikuwa zikiendeshwa na kikundi kidogo cha Áfrika katika mwaka 1958.9 zilisababisha Marekani ipige kura kuunga mkono maazimio yaliyoilaani Afrika Kusini badala ya kujitoa.

1960 ulikuwa mwaka wa Afrika. Ulikuwa mwaka huo pia Ukatibu wa Umoja wa Mataifa ulitambua majukumu yake ya jumla kwa bara hilo. Hivyo Januari 1960 Dag Hammarskjöld, katibu mkuu, alikwenda kwenye ziara kubwa ya wiki sita Afrika, ambako alikutana na viongozi wengi wa baadaye wa nchi za Afrika. Hammarskjöld alitambua tangu hapo kazi kubwa iliyobidi itimizwe; na "hali" ilifuatiwa katika mwaka huo, 1960, na kampeni kubwa ya kijitangaza katika vyombo vya habari.

Tukio kubwa lisilokuwa la kawaida pia lilitokea 1960. Hili lilikuwa mauaji ya Shapeville ya Afrika Kusini, ambayo Maelni 25 yalisababishwa kuitishwa kikao cha Baraza la Usalama na kupitishwa kwa Azimio maarufu la Aprili 1 lililoitaka Afrika Kusini kuachana na ubaguzi wa rangi. Huu ulichukuliwa kuwa ni ushindi na kundi la Afrika na kwa hakika haukuhusiana na uamuzi wa Pretoria wa kuruhusu ziara ya katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa ya Julai. Mwishoni mwa 1960 wajumbe wa Afrika kwenye Baraza Kuu walipata mafanikio mengine makubwa kwa kupitishwa, baada ya kukataliwa kwa pendekezo la Sovieti, azimio dhidi ya ukoloni Afrika kwa kura 90 kwa bila, na tisa kujitoa. UN ikawa rafiki kamili zaidi wa mapambano ya ukombozi wa Afrika.

Licha ya migogoro yao ya ndani, nchi za Kiafrika zichukua nafasi muhimu katika kasri ya vioo ya Manhattan.

Hata hivyo 1961 ulikuwa mwaka mbaya katika Umoja wa Mataifa. Kama ilivyoelezwa kwenye sera zilizotangulia, wajumbe wa Afrika waligawanyika kati ya kundi la Kasablanka (Ghana, Guinea, Mali Moroko, Jamhuri ya Muungano wa Uarabuni na serikali ya muda ya Jamhuri ya Algeria) na kundi la Brazaville, lililokuwa na karibu nchi zote za kilichokuwa Afrika ya Wafaransa.

1961 ilianza na suala la Angola (maasi ya Luanda na Februari, na upinzani wa Machi), ambalo lilipelekwa UN mara tatu Machi na Aprili na kuishia kwenye kupigiwa kura kwenye Baraza la Usalama (kura tisa ziliunga mkono, na kujitoa kwa wawili) kuwataka Wareno waache vitendo vyao vya ukandamizaji. Mwaka uliendelea na mgogoro wa Ufaransa na Tunisia wa Bizerta, ambao ulimalizwa katika kikao maalumu cha Agosti kwa azimio lililoitaka Ufaransa kuondoa majeshi yake kutoka nchi nzima ya Tunisia . Azimio hili, lililopitishwa kwa kura 66, kukiwa na 30 waliojitoa, lilipata kura 8 kutoka kwenye kundi la Brzaville.

Juu ya tatizo la kukomesha ukoloni mwisho wa mwaka 1961 kulikuwa na

mapendekezo kadha kwa ajili ya kuweka muda wa mwisho wa kutoa uhuru wa makoloni ya Afrika 1962, iliyopendekezwa na Sovieti, ilikataliwa kuwa ni karibu mno; ambapo 1970, iliyopendekezwa na Nigeria na Liberia ilionekana mbali mno na wajumbe wengi. Mwishowe iliamuliwa usiweke muda wa mwisho lakini azimio lilipitishwa la kuunda kamati Maalumu ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya nchi ambazo bado ziko chini ya ukoloni. Kamati hii, iliyokuwa na wawakilishi wa nchi za Asia na Afrika, watawala wa kikoloni, Marekani na Shirikisho la Sovieti, na kujulikana kama Kamati ya Wajumbe Kumi na Saba, iliundwa Januari 1962.
Tangu 1963 na kuendelea hali ilikuwa nzuri kwa kiasi kikubwa, shukrani hasa ziende kwa kumalizwa kwa vita vya Algeria na kipindi cha vurugu cha Kongo. Kama tulivyokwishaona, Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) uliundwa ukiashiria enzi mpya na tofauti katika maendeleo ya uhusiano kati ya Afrika na Umoja wa Mataifa. Kwa kuanzishwa kwa OAU Mei 1963, Afrika iliweza kuangalia kwenye Umoja huo kwa ajili ya usikivu, majadiliano na ushauri na sehemu nyingine za dunia.

Kutokana na maendeleo hayo uhusiano wa UN na Afrika ulikuwa na mabadiliko makubwa ya ukubwa na ubora pia. Kwa upande mmoja ujumbe wa bara hili uliongozeka kutoka kumi ya moja mwaka 1945 hadi karibu theluthi moja 1963 (uwiano huu ulibakia hivyo hadi 1980). Kwa upande mwingine, nchi za Afrika zilikuja kutambua kuwa urari wa nguvu ulikuwa umegeuka na kuwapendelea na kuwa baadhi ya matakwa yao yalikuwa maalumu. Walitoa madai maalumu, na madhumuni yao ya kimsingi yalikuwa kuwa na athari ya kidiplomasia, na hasa kisiasa inayowiana na wingi wao.

Muungano wa falsafa ya msingi ya Umoja wa Mataifa, ambao ulijengwa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia na washindi, na madai ya nchi za Afrika ambayo kwa sababu mbalimbali yalikuwa tofautitofauti ulisababisha kuwepo kwa uhusiano na Afrika ulio tata, usoeleweka kiurahisi na mara nyingine mgumu.
Kama ilivyokuja kutokea, urafiki katika ukombozi baina ya UN na Afrika ulikuwa rahisi zaidi kuliko ushirika katika maendeleo. Baadhi ya migongano migumu kabisa katika mtazamo kuhusu maendeleo ilikuwa kati ya vyombo vya UN na mwelekeo wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Sasa inatubidi tuangalie tofauti hizo.

## UN kama mshirika wa maendeleo

Uhusiano wa Afrika na Umoja wa Mataifa katika uwanja wa kiuchumi unafanywa kwa kiasi fulani kupitia Umoja wa Nchi Huru za Afrika na United Nations Economic

Commission for Africa (ECA) [Tume ya uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika]; uundwaji wa shughuli zake zimeelezwa katika sura za awali. Hapa, tutaeleza tu juu ya uhusiano baina ya mashirika hayo mawili katika hali ya kawaida. Aprili 1958 Umoja wa Matifa uliunda Tume ya uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika (ECA), kazi yake ikiwa kuharakisha maendeleo ya uchumi na kijamii ya bara la Afrika, kufanya utafiti, na kulipa taarifa Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa, ambalo ndilo lililoanzisha na linaisimamia, juu ya hali ya eneo hilo.

Lakini OAU, ilipoundwa 1963, tangu mwanzo ilithibitisha uwezo wake wa kuratibu, kuimarisha na kulinganisha ushirikiano baina ya watu wa afrika katika nyanja zote, ikiwa pamoja na zile za ECA. Hivyo, kifungu XX cha Mkataba wa Addis Ababa kililipa mamlaka Baraza la Wakuu wa Nchi kuunda tume tano maalumu, ikiwemo Tume ya Uchumi na Jamii ambayo kazi yake ilikuwa kukuza ushirikiano wa kiuchumi Afrika.

Katika kikao chake cha kwanza kilichofanyika Niamey Desemba 1964, Tume hii ya Uchumi na Jamii, ambayo iliundwa na Baraza la Wakuu wa nchi na Serikali Julai 1964, ilitoa kanuni zitakazoendesha uhusiano wa OAU na ECA. Ikiwa umejieleza wenyewe kama chombo cha juu kabisa cha mipango na utekelezaji ulilifinya jukumu la ECA katika masuala ya kiufundi na ushauri: kwa maneno mengine ECA ilikuwa ifanye utafiti na ukaguzi utakaotumiwa kuongoza maamuzi ya OAU.

Jaribio hilo la kuweka chombo cha UN chini ya OAU lilitamkwa wazi na katibu mkuu wa kwanza wa OAU 1966, alipowaambia wawakilishi wa nchi wanachama kanuni zinazotawala uhusiano kati ya OAU na ECA zilitumiwa pia katika uhusiano wa OAU na mashirika mengine maalumu ya Umoja wa Mataifa.[3] Kinyume na azma ya OAU ya kudhibiti shughuli za ECA, Katibu mtendaji wa ECA alinukuu sheria za shirika lake: Ziliezea kuwa chombo cha Idara ya Masuala ya Uchumi na Jamii ya Umoja wa Mataifa, ambacho kilisimamiwa na Baraza la Uchumi na Jamii la Umoja wa Mataifa na ambacho sera zake zinaelezwa na kugharamiwa na Umoja wa Mataifa, hakiwezi kukubali kuwa chini ya masharti yanayotolewa na nchi za Afrika kupitia OAU. OAU inaweza tu kusaidiana na ECA na kuwa tayari kuunga mkono shughuli zake katika uwanja wa uchumi na jamii, mapendekezo

[3] Taz. Nyaraka za OAU CM/101/Rev. 1, uk. 8

yake, ingawa yanakaibishwa na Baraza la Uchumi na Jamii, hayawezi kulazimishwa kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Mgongano kati ya vyombo hivi viwili tofauti, sembuse kuwa vinapingana, vilileta mawazo yanayopigana kati ya nchi wanachama wa OAU kuhusiana na ECA, ikiunganishwa na matatizo ya fedha yaliyokuwapo, ilisababisha shughuli za OAU za uchumi na jamii zisimamishwe.

Ilikuwa katika hali hii makubaliano kati ya Umoja wa mataifa na OAU juu ya ushirikiano wa OAU na ECA yalitiwa saini Novemba 15 1965. Lakini makubaliano haya, ambayo yanaweza kufupishwa kama azimio la dhamiri kwa pande zote mbili kushirikana",[4] yalizidi kutafuta mwafaka baina ya mawazo mawili tofauti ya ECA na OAU lakini hayakutatua tatizo halisi la mgawanyo wa kazi kati yao. Yaliwezesha tu kuwepo kwa utaratibu wa kushauriana juu ya maswali madogomadogo ya utekelezaji na utawala. Hivyo James Magee aliyetezea makubaliano hayo kuwa yaliyoruhsu mashirika hayo mawili kutambua mipango ya kazi ya kila mmoja.[5]

Kwa vile kila upande hukubadili msimamo wake, matatizo yaliendelea kuwapo katika mabadiliko ya uhusiano kati ya OAU na ECA. 1968, kwenye maadhimisho ya miaka kuni ya ECA, Katibu Mkuu wa Umoja wa Matifa, U Thant, alielezea upya mawazo ya shirika hilo la dunia kama ifuatavyo: ECA, alisema, ni "dirisha la Afrika linaloruhusu Umoja wa Mataifa kuona matatizo ya uchumi na jamii ya bara hili kwa mtazamo wa Kiafrika, kayaona katika muktadha wa muundo mzima wa uchumi wa kimataifa".[6]

Katika tukio hilo Katibu mkuu wa OAU alizungumzia haja ya ushirikiano kati ya EAC na OAU, ambazo shughuli zake inabidi zikamilishane "ili kuweza kutumia vyema uwezo wa kiufundi na teknolojia wa ECA na pia maamuzi ya kisiasa na kiutawala ya vyombo vya juu vya OAU". Ukuu wa OAU ulisisizwa tena katika maazimio ya Septemba 1967 na Februari 1969.[7] Ushirikiano kati ya OAU na ECA umeshindikana hadi sasa.

Kulikuwa na sababu kuu mbili za kushindwa huko, kulikuzwa na uadui binafsi: kwanza mtazamo finyu wa OAU wa Afrika na, pili dhana tofauti za mashirika hayo juu ya matatizo ya Afrika. OAU ikiwa imeundwa na serikali za Afrika ambazo zinatarajiwa kuidhibiti, heshima na uhalali wake ulikuwa unatambuliwa na

[4] A. Mamador, 1971

[5] J. Magee, 1970

[6] Waraka wa UN E/4651 E/CN 14/453, Juz. 1 uk, 297

[7] Ushirikiano kati ya OAU na ECA umeshindikana hadi sasa.

kuthibitishwa ikilinganishwa na ECA, ambayo ilichukuliwa kuwa ni chombo kinachojali mambo ya nje na hakitoshelezi kuwa cha Kiafrika kuhusiana na uajiri wa wafanyakazi na uundaji wa sera.

Lalamiko kubwa lililojitokeza dhidi ya ECA ni kwamba vyeo vya upangaji mipango na utekelezaji vilishikwa na watu wasio Waafrika, ambayo ilimaanisha kwa kiasi fulani kuwa sera za uchumi za ECA kuhusiana na Afrika zilipokelewa kutoka New York na hazikuwa zikiamuliwa Addis Ababa. ECA ilichukulia matatizo ya Afrika kwa kigezo cha uchumi pekee: maendeleo ya Afrika yatakuja tu iwapo kutakuwa na muungano wa kiuchumi wa bara hili na kuundwa kwa Soko la Pamoja la Afrika, kwani kuwepo kwa vikwazo vya ushuru ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo yake.

OAU, kwa upande mwingine, ilibakia kujali zadi watu katika maendeleo, isingeweza kutotilia maanani vikwazo vya lugha, dini, utamaduni na itikadi ambavyo vingeweza kutokea kama muungano utakuwa wa haraka mno. Mwelekeo wa hatua – yaani, kwanza kuwepo na eneo la biashara huru kuliko kuwa na jumuiya ya muungano wa kiuchumi – ulionekana kuwa njia ya busara.

Mtazamo huu wa aina mbili kuhusiana na ukweli wa uchumi wa Afrika ambao haukuruhusu ushirikiano unaotangamana aghalabu ulitatanishwa.

Na tabia na malengo yaliyopingana ya maofisa wa OAU na ECA. Kuyumba kwa uhusiano kati ya Mghana Robert Gardiner aliyekuwa mkuu wa ECA na Mguinea Diallo Telli wa OAU kuliakisiwa katika mivutano na matatizo ya kuendelea kwa uhusiano kati ya Mnigeria Adedeji Adebayo wa ECA na Mtogo Edem Kodjo wa OAU.[8]

Hivyo licha ya kukatana kwa katibu zote mbili na mikutano ya pamoja, uhusiano kati ya mashirika hayo mawili ulikuwa ukijidhihirisha kwa uadui katika uwanja wa uchumi na jamii.

Haikuwa hadi 1980 ambapo mashirika yote mawili yalikubaliana juu ya mkakati mpya wa maendeleo uliokuwa kwenye *Mpango wa Utekelezaji wa Lagos* uliopitishwa April 1980. Nchi za Kiafrika ziliikataa kimsingi miongozo ya kiuchumi iliyopendekezwa na "Taarifa ya Berg" juu ya *Maendeleo ya Haraka ya Afrika Kusini mwa Sahara; Ajenda ya Utekelezaji* iliyochapishwa na Benki ya Dunia mwaka 1981. Wakati ambapo *Mpango wa Utekelezaji wa Lagos* ulikuwa na

[8] Taz. S. Gharbi, 1981.

madhumuni ya kuwa na maendeleo yanayoilenga Afrika yenyewe kwa msingi wa kupunguza utegemezi wa nchi za nje na kujitosheleza kwa chakula katika kiwango cha taifa na bara zima, taarifa ya Benki ya Dunia ilishawishi uchumi wa Afrika unaozingatia nchi za nje na kuweka msisitizo katika kuongeza upelekaji nje mazao ya fedha kutoka Afrika.[9]

## Kuelekea kwenye Mpango wa Uchumi wa Kimataifa'

Kama ilivyoonyeshwa dhahiri kwenye Sura 25, ilikuwa ni Afrika iliyoanzisha majadiliano juu ya dhana ya Mpango Mpya wa Uchumi wa Kimataifa (NIEO) mwaka 1979. Kusema kweli fasiri ya kwanza ya NIEO kama inavyoonekana kwenye maazimio ya Mei 1974 ni fasiri iliyopangwa upya tu ya madai yaliyofanya nchi za Dunia ya Tatu tangu UNCTAD (Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Maendeleo) ilipoanzishwa. Kutokana na ukweli huo, kazi na jukumu la kamati ya pamoja ya ECA - OAU juu ya Biashara na Maendeleo ya kutayarisha msimamo wa pamoja wa Afrika lilijidhihirisha.

Kamati hiyo ya pamoja ilikuwa na wajibu wa aina mbili: kwanza, kuangalia matatizo yote ya muda mfupi katika uwanja wa biashara na maendeleo, na pia jinsi ya kuyagharimia; na, pili, kuona jinsi gani matatizo hayo yanaweza kuzingatiwa kwa ufanisi na kuwasilishwa kwenye mikutano ya Baraza la Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Maendeleo. Kamati hii ya Pamoja ya ECA-OAU kwa hiyo ina tatizo la kukagua uchumi la kulisuluhisha kwa kiwango cha bara zima na mkakati wenye mwelekeo wa kisiasa wa kuchukua kuhusiana na makubaliano makubwa ya kimataifa katika uwanja wa biashara, fedha na ushuru. Kwa hivyo basi, mikutano ya pamoja ya ECA na OAU "imelenga katika kuhakikisha ushirikiano kamili kati ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika na Tume ya Uchumi kwa ajili ya Afrika katika juhudi zao za kuhakikisha nafasi ya nchi za Afrika kwenye mashauriano na makubaliano yanayoendelea katika UNCTAD, kufuatia Azimio 135 (VIII) la ECA na Azimio 158 (IX) la OAU."[10]

Ili kutimiza wajibu wake Kamati kwa kawaida hufanya vikao viwili kwa mwaka, kimoja mwanzoni mwa Januari au Machi na kingine, kilicho muhimu zaidi na kinachofanyika kwa kawaida zaidi, cha Agosti cha kutayarisha kwa ajili ya mkutano

[9] A. d'Almeida, 1983; E.K. Apkevon, 1983; E.K. Kouassi, 1983; UNESCO, 1983; Umoja wa Nchi Huru za Afrika, 1981.

[10] Taz. Waraka wa UN, ECA E/CN/14/449, E/CN/14/WP 1/15; OAU/TRANS/14 wa Januari 1969.

wa mwaka wa Baraza la Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Maendeleo.

Ukawaida na kudumu kwa Kamati hii kunaweza kuanuliwa na kuwepo kwa umakini kunakoendelea ambapo, tangu kikao cha tatu, mapendekezo ya mikutano yote ya awali ya kamati huzingatiwa na tarehe na mahali pa mkutano unaofuatia huwekwa mapema.[11] Kamati hii ya pamoja huonekana kuwa inafanya kazi kwa kiasi cha kuridhisha mashirika yote mawili; na ni kutokana na kazi yake hasa, pamoja na juhudi za kundi la Afrika la UNCTAD, msimamo wa pamoja wa Afrika juu ya matatizo ya uchumi ya bara hili ulipitishwa na kuwasilishwa kwenye mikutano ya pili na tatu ya UNCTAD.

Msaada wa kiufundi wa UN unapitia Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), ambao uliundwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1965. Mashirika kumi na tano ya mfumo wa UN (ILO, FAO, UNESCO, WHO, IBRD, UNCTAD, na kadhalika) hushiriki katika utekelezaji wa miradi ya UNDP.

Hadi 1971 maombi ya kugharimia miradi yaliwasilishwa na serikali kulingana na miradi. Tangu wakati huo, kila nchi iliyofaidika imeorodhesha maombi yake kulingana na vipaumbele vyake vinavyohitaji msaada wa UNDP kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano. Katika kila mradi nchi inayoendelea inagharimia asilimia 50 ya mradi unaofanywa kwa msaada wa UNDP. Hivyo wakuu wengi wa Afrika wanalalamika juu ya gharama kubwa za msaada unaotolewa na UNDP. Huko Liberia mwaka 1966, kwa mfano, msaada wa kiufundi uliotolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya mpango wa ujenzi wa barabara ulimaanisha kuwa serikali ya Liberia ilipie mishahara ya makontrakta wanaotoa huduma za kiufundi, bila kutaja riba ya mikopo ya muda mrefu inayodaiwa na Benki.

Sasa utaratibu unaoendesha utoaji na ugawanyaji wa msaada wa UNDP haitoi fursa kwa OAU kufanya chochote katika hatua yoyote ile ya utekelezaji wa programu za UN. Hivyo msaada wa kiufundi unaofanywa kwa makubaliano ya nchi nyingi kwa ajili ya Afrika ni eneo linaloongozwa na Umoja wa Mataifa pekee.

Zaidi ya hayo, rasilimali za UNDP kutoka hasa kwenye nchi za magharibi, ambazo si lazima zizitendee nchi zote za Afrika sawa: hivyo kulingana na OAU

[11] Ling: mapendekezo ya Kamati kwenye kikao chake cha 3 katika: E/CW/14/449, E/CN/WP 1/15, OAU/TRANS/14 wa Januari 1969, uk.9; mapendekezo ya kikao cha 4 katika: E/CN/ 14/459, E/CN/14/WP 1/14 Res. 3, OAU/TRANS/23/Res.3 ya Agosti 1969, Kiamb. 1, uk.5; mapendekezo ya kikao cha 5 katika: E/CN/14/490, E/CN/14/WP 1/31, OAU/TRANS/30 ya Agosti 24 1970, uk. 16.

msaada hugawanywa bila haki, aghalabu kulingana na matakwa yanayofuata mielekeo ya kisiasa na itikadi.

Kwa hiyo OAU ingependa kuona Shirika la Afrika Nzima likiwa njia ya kawaida ya kuratibu na kugawanya msaada na msaada unaotolewa kwa makubaliano ya nchi nyingi.

Mashirika ya UN kwa upande wao yanaonekana kuogopa kuwa OAU, ambayo si chombo cha wanachama wanaofanana kwa kila hali, haiwezi kuchukua jukumu hilo la kuwa mshika dau na kutopendelea katika kuratibu na kugawa msaada wa kimataifa. Pia hawapendi kugharimia shughuli za OAU zinazohusiana na vuguvugu la ukombozi wa kitaifa Afrika.

Kwa hiyo kuna kutoaminiana kwa pande zote mbili kati ya OAU na mashirika ya mfumo wa UN katika uwanja wa misaada ya mikataba ya nchi nyingi kwa Afrika.

Uhusiano kati ya OAU na Umoja wa Mataifa juu ya matatizo ya ushirikiano wa kiuchumi unadhihirishwa kwa vipengee viwili uhusiano wa usio wa kirafiki katika bara hili, na "uhifadhi wa Sekta" wa UN. Lakini katika mielekeo yao kuhusiana na uhusiano wa Kaskazini na Kusini, kunakuwa na utangamano zaidi. Afrika, Umoja wa Mataifa na mashirika yake maalumu yanakubaliana zaidi katika kiwango cha ulimwengu kuliko wanavyokubaliana wanapoilenga Afrika yenyewe. Ushirikiano wa Kimataifa juu ya Wafanyakazi inabidi tutofautishe kati ya ushirikiano wa kile kinachoonekana kuwa masuala ya kiufundi "yasiyo na madhara" na ushirikiano wa kisiasa, ambao unaweza kukasirisha utawala wa dola. Ushirikiano wa kiufundi unafanyika hasa kati ya Afrika na mashirika maalumu ya Umoja wa Mataifa kuendeleza maisha mazuri ya watu wa Afrika. Hebu tuiangalie Afrika na Shirika la Kazi Duniani (ILO), kwa mfano. Hadi mwanzoni mwa miaka ya 1960, Afrika na ILO hawakuwa na uhusiano mkubwa wa moja kwa moja, kwani uhusiano huo ulikuwa na utawala wa kikoloni. Wanachama waanzilishi 29 wa 1919 walikuwa pamoja na Liberia, ikifuatiwa na Ethiopia (1922), Misri na Muungano wa Afrika Kusini (1939), Libya (1952) na Ghana (1957). Hata hivyo Shirika la Kazi Duniani liliweza kuunda kamati maalumu katika kipindi cha ukoloni, Kamati ya Wataalamu wa Nguvukazi, kushauri njia bora zaidi ya kuwalinda wafanyakazi katika nchi zilizo chini ya ukoloni; ilitambulika kutokana na mapambano yake dhidi ya kazi za kulazimishwa Afrika.

Nchi nyingi za Afrika zilijiunga na ILO kati ya 1960 na 1964, na wakati huohuo zikijenga uhusiano na waajiri wa Kiafrika na vyama vya wafanyakazi. Madhumuni makubwa ya Afrika yalikuwa kuweka masharti na asasi zinazohitajika

kufasiri maadili ya uchumi na jamii yaliyoelezwa na nchi changa na kukubaliwa yaweze kutimizwa.

Ni katika muktadha wa matatizo haya ndipo mkutano wa kwanza wa eneo la Afrika uliofanyika Lagos, Nigeria, mwaka 1960 uliitanabahisha ILO katika haja ya msaada wa mafunzo ya kiufundi, kibiashara na kilimo, na pia juu ya mafunzo ya wasimamizi. Umuhimu mkubwa uliowekwa katika uajiri na mafunzo ulithibitishwa 1964, wakati kamati maalumu juu ya kazi za wanawake ilisisitiza haja ya kutatua matatizo yafuatayo:

(1) ajira na hali ya wanawake katika Afrika inayobadilika kwa haraka;
(2) haja ya kutumia wafanyakazi wanawake; na
(3) haja ya kuwapatia wanawake na wasichana njia bora zaidi za mafunzo ya kiutaalamu.

Kwa kutambua matatizo haya, ILO iliongeza shughuli zake Afrika kwa kuwa na Ofisi ya Kanda Addis-Ababa na kufanya mabadiliko thabiti kwenye mpango wake. Hivyo ongezeko la ghafla la msaada wa kiufundi lilitokana kwa kiasi na haja ya kutimiza maombi yaliyotoka kwenye nchi za Kiafrika zenyewe. Afrika polepole ilianza kupata sehemu kubwa zaidi ya raslimali za ushirikiano wa kiufundi zilizokuwapo ILO kutoka kwenye bajeti yake ya kawaida, Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) na vyanzo vingi vya makubaliano ya nchi na nchi na nchi nyingi kwa pamoja.

Kwa sababu ya uzito wa matatizo pacha ya ukosefu wa ajira na upungufu mkubwa wa wafanyakazi stadi, ILO ilichukulia kuwa kazi yake ya msingi ni kuisaidia Afrika kuwaendeleza wafanyakazi wake. Ikiwa na madhumuni hayo, mwaka 1963 ilianzisha Kituo chake cha Kimataifa cha Mafunzo ya Kitaalamu na Kiufundi Turin, Italia, kwa nia ya kutoa mafunzo kwa wale ambao baadaye nao wangefunza wengine. Tangu kituo hicho kilipoanzishwa, Waafrika wengi wamekwenda huko kwa udhamini wa masomo, kwa hivyo kuhakikisha kuendelea kwa "kitalu" cha Wataalamu wa Kiafrika. Kwa ajili ya kusisitiza umuhimu wa Utafiti ILO ilianzisha mwaka 1961 Taasisi ya Kimataifa ya Mitalaa ya Kazi, ambayo kazi yake kubwa ilikuwa kuchunguza matatizo ya kijamii ya maendeleo ya uchumi. Kwa muda mrefu iliongozwa na Mwafrika, Profesa Albert Tevoedjre.

Zaidi ya hapo, kwa kupitia Mkutano wa Mawaziri wa Kazi wa Afrika OAU hushughulikia masuala yanayoihusu ILO ambayo yanajadiliwa katika kikao kinachoufuatia kwenye mkutano wa kimataifa. ILO imebidi ibadili mipango na

muundo wake kupitia maanani kuibuka kwa nchi mpya katika sura ya kimataifa, na kujizatiti kwenye masuala kama vile ya maendeleo ya wafanyakazi; mafunzo ya kitaalamu na kiufundi; kugawanya madaraka ya ILO na kuwaingiza maofisa wa Kiafrika; uchaguzi wa rais wa mkutano wa kimataifa, na masharti ya utekelezaji; uendelezaji wa ofisi ndogo za kanda na washirika wa Afrika. Mkutano wa ILO uliangalia pia uteuzi wa wagombea wa Kiafrika katika utawala na Kamati ya Ushauri ya Afrika; mchango wa nchi za Kiafrika katika mfuko wa wakfu wa Taasisi ya Kimataifa ya Mitalaa ya Kazi; na tatizo la kuunganisha vyama vya wafanyakazi Afrika. Tatizo hili la mwisho, likiwa limeunganishwa na wajibu wa vyama vya wafanyakazi katika maendeleo ya nchi za Kiafrika, bado linachunguzwa na OAU. Shughuli za namna hiyohiyo zinaangaliwa kuhusiana na uhusiano kati ya OAU na UNESCO.



*PICHA 29.2 Amadou- Mahtar M'BOW wa Senegali, mkurugenzi mkuu wa UNESCO, 1974-87*

Kuhusiana na ushirikiano kati ya Afrika na UNESCO, ilikuwa Novemba 1960, katika kikao chake cha kumi na sita, ndipo Mkutano Mkuu wa UNESCO uliingiza idadi kubwa ya nchi za Kiafrika kama wanachama. Mkutano huo ulipitisha azimio ambapo waliamua kuitisha mkutano wa nchi za Kiafrika mwaka 1961 kwa nia ya "kuorodhesha mahitaji ya elimu na mpango wa kuyatimiza katika miaka inayofuata." Ulitoa waraka wenye kichwa *Outline plan for African educational development.* [Muhtasari wa mpango wa maendeleo ya elimu ya Afrika] ambao ulipitishwa na Halmashauri ya Utendaji ya UNESCO katika kikao chake cha hamsini na mbili. Iliamuliwa kuunda kundi kuu la mipango kuhusu ujenzi wa shule huko Khartoum na kituo cha uchapishaji wa vitabu vya kiada huko. Yaoundé, na mwishowe kuweka walimu 50 tayari kwa baadhi ya nchi za Kiafrika.

Kwa kutiwa moyo huko, nchi za Afrika ziliifanya UNESCO kufanya mkutano mwingine huko Antananarivo tangu Septemba 3 hadi 12 1962 uliohusu elimu ya juu Afrika, ikiwa pamoja na mada kama vile uchaguzi wa mihtasari ya masomo, marekebisho ya elimu hiyo kulingana na hali halisi na mahitaji ya Afrika, mafunzo ya wafanyakazi wenye utaalamu wa utawala wa umma na mbinu za maendeleo, na kadhalika. Kutokana na msukumo huo mawaziri wa elimu wa Afrika waliamua kuanzisha Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Nchi za Afrika kufuatilia utekelezaji wa mipango inayowekwa na UNESCO.

Wakati OAU ilipoanzishwa mwaka 1963 ilihitajika kudhihirisha uhusiano wake na vyombo vya UN: na hii ililetwa mbele ya Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika katika kikao chake cha kwanza cha Machi 17 - 24 1964 huko Abdijan. OAU iliunda Kamati ya Elimu na Utamaduni kukamilisha juhudi za UNESCO. Mipango ya ushirikiano wa kanda na kimataifa ilikuwa ni kipengee cha makubaliano yaliyotiwa saini Julai 10, 1968 kati ya OAU na UNESCO. Kuanzia hapo ushirikiano wa nguvu uliendelezwa kati ya mashirika hayo mawili. Ushirikiano huo ulidhihirika katika Tamasha la Afrika la Utamaduni, katika uandaaji wa Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika, kwenye Mkutano wa Matumizi ya Sayansi na Teknolojia Afrika uliofanyika Dakar kuanzia Januari 22 hadi 31 1974, katika kutatua matatizo ya tatizo la wakimbizi wa Afrika, na kadhalika. Mkurugenzi Mkuu wa nne wa UNESCO alikuwa Mwafrika, Bw. Amadou Mahtar M'Bow, ambaye alimaliza mihula miwili ya kazi akiwa mkuu wa shirika hilo.

Katika nyanja hizi zote kazi ya OAU na UNESCO zilioanishwa.

OAU inashirikiana pia na mashirika mengine ya UN. Hii hutokea chini ya usuli mpana wa kiasasi unaoelezwa katika uhusiano wa pande hizo mbili. Uwanja unaopendwa zaidi ni ule wa maendeleo ya vijijini na kilimo Afrika. Kamati ya

Kanda inayounganisha Mashirika yote inaleta pamoja shughuli za OAU na mashirika makuu ya UN na inaratibu kazi ya ECA na mashirika mengine ya kujitolea katika utekelezaji wa mpango wao wa maendeleo changamani ya vijiji vya Afrika. Kwa upande huo jukumu la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) ni la umuhimu wa juu: unagharimia miradi, na kugawa mbegu, mbolea, dawa za kuua wadudu waharibifu na dawa za kuua vimelea.

Kwa muktadha wa ushirikiano huu, mashirika yanayohusika yamepanga mipango kwa ajili ya shirika la kanda la ukulima wa mpunga la Afrika Magharibi, mradi ambao kuanzishwa kwake kulisimamiwa na OAU.

Uhusiano wa namna hiyo upo kuhusiana na tatizo la vijana, ajira, mafunzo ya kiufundi na kisomo.

Aina nyingine za uhusiano pia zinaendelea kwa kuwa na kamati za pamoja kati ya OAU, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusiana na chakula na lishe Afrika, kampeni dhidi ya sotoka, malale, na uanzishaji wa vituo vya afya za mimea, na kadhalika.

Kuna ushirikiano wenye manufaa pia kati ya mashirika ya kiserikali kwa ajili ya kuwapatia makazi mapya na elimu ya wakimbizi (UNO, UNDP, UNHCR, ECA, UNESCO, OAU) ambayo yanashiriki kwenye kundi la utekelezaji wa Ofisi ya Wakimbizi wa Afrika ya OAU. Ushirikiano hapa ni muhimu sana kwa sababu ya umuhimu wa suala lenyewe. Kati ya mabara yote, Afrika ina idadi kubwa zaidi ya wakimbizi, ambao ni jumla ya 3.5 milioni ilipofika 1979. Hivi sasa, nusu ya wakimbizi 10 milioni walioko duniani nusu wanaishi Afrika, jambo ambalo linahalalisha ukubwa wa ushirikiano na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) kuweza kushughulikia matatizo makubwa yanayosababishwa na kuwapo kwao.

Hivyo mwaka 1967 OAU, UNHCR na ECA walichukua jukumu la kuandaa mkutano Addis Ababa kuchanganua na kutathmini hali ya Wakimbizi Afrika, kudurusu sera za sasa na mikakati, na inapokuwa lazima kuunda mpya kulingana na matatizo yanayozidi kuongezeka. Baada ya mkutano huu Wakuu wa Nchi na Serikali wa OAU mwaka 1969 walipitisha *Makubaliano yanayotawala vipengele maalumu vya matatizo ya Wakimbizi wa Afrika* ambayo yalianza kutumiwa 1974.

Mkutano wa pili wa Afrika nzima juu ya hali na haki za Wakimbizi wa Afrika uliandaliwa na OAU, UNHCR na ECA tangu Mei 7 hadi 17 1979 Arusha, Tanzania. Mkutano huu ulikuwa na malengo matatu:

(1) kuvifanya vyombo vyote vinavyohusika (Serikali, mashirika ya kiserikali,

mashirika ya kujitolea na mashirika ya msaada kwa wakimbizi) viwe na taarifa ya kutosha juu ya hali inayozidi kuwa mbaya ya matatizo ya wakimbizi wa Afrika na uwezekano wa utatuzi;

(2) kuchunguza na kutathmini hali ya sasa na matatizo ya Wakimbizi wa Afrika; na

(3) kuchunguza na kutathmini sheria za kitaifa zinazohusu wakimbizi na kupendekeza jinsi ya kuziboresha.

Tangu hapo UNHCR imeendelea kutoa umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa mapendekezo ya mkutano huu. Shughuli zilizofanywa 1983 ni pamoja na mradi wa utafiti uliofanywa na wataalamu watatu katika nchi 21 za Afrika juu ya athari za udhamini wa masomo Afrika, na semina juu ya hali ya wakimbizi wa Afrika Magharibi.

Tokeo mojawapo la mkutano huu lilikuwa ni kufanyika huko Geneva Aprili 1981 kwa Mkutano wa Kwanza wa Kimataifa kwa ajili ya Msaada wa Wakimbizi wa Afrika (ICARA I). Ulitimiza madhumuni yake, yaani kutanabahisha juu ya wakimbizi wa Afrika na kukusanya kwa niaba yao.

Desemba 18 1982 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, likiwa limepata ujuzi kutokana na jaribio hili, walipitisha Azimio 37/197, ambalo aya ya 5 inamtaka katibu mkuu, kwa kushirikiana kwa karibu na Umoja wa Nchi Huru za Afrika na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa, kuandaa Mkutano wa pili wa Kimataifa kwa ajili ya kuwasaidia Wakimbizi wa Afrika (ICARA II). Wakati wa matayarisho ya ICARA II umuhimu wa kupata utatuzi wa kudumu wa matatizo ya wakimbizi wa Afrika ulisisitizwa.

Mojawapo ya malengo ya Azimio 37/197 ni kusaidia kazi ya UNHCR kwa kuwasilisha kwenye ICARA II mipango ya utoaji misaada inayohusu zaidi maendeleo na kuzingatia athari za kuwapo wakimbizi katika uchumi wa kitaifa. Mfuko wa Udhamini wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika Kusini ulitoa dola 300,000 kwa UNHCR kwa ajili ya kuwasaidia wakimbizi wa Afrika Kusini katika kipindi cha Julai 1 1982 – Juni 30, 1983; iwapo mwaka 1982 UNHCR ilitenga dola 134.7 milioni kwa ajili ya kugharimia shughuli za utoaji misaada Afrika.[12]

Katika uwanja mwingine, ule wa hifadhi ya makazi na mazingira, Baraza Kuu

[12] *Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa, 1982.3.*

la 1974 liliunda Mfuko wa Nyumba na Makazi ya Binadamu wa Umoja wa Mataifa, kwa sababu ya umuhimu wa matatizo ya nyumba na matatizo mengine yanayohusika na makazi ya binadamu. 1978 Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makazi ya Binadamu (Habitat) kilianzishwa katika mfumo wa UN kuwa kiungo cha shughuli zinazohusika na makazi ya binadamu; kiko Nairobi (Kenya), kama ulivyo Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), ulioanzishwa na Baraza Kuu kufuatia mapendekezo ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira ya Binadamu uliofanyika Stockholm Juni 1972.

Mei 1982 Halmashauri ya Utendaji ya UNEP ilifanya mkutano maalumu Nairobi wa kuadhimisha miaka kumi ya mkutano wa Stockholm. Azimio la Nairobi, lililopitishwa kwa kauli moja, linaeleza mahsusi kwamba:

> Mazingira ya binadamu yatanufaika sana kutokana na hali ya amani na usalama wa kimataifa, bila vitisho vya vita vyovyote, hasa vita vya nyuklia, na kupotea kwa raslimali za kitaaluma na asili kutokana na silaha, pamoja na ubaguzi wa rangi utengano wa mataifa na aina zote za ubaguzi, ukoloni na aina nyingine za ukandamizaji na utawala wa kigeni.

Hiyo ndiyo picha ya ushirikiano ambayo imekuwa ikijengwa kati ya Afrika na vyombo vya mfumo wa UN katika nyanja za kiufundi na kijamii. Ushirika uliojengwa kati ya Afrika na chombo hicho cha dunia unaendelea kuwa mchakato wenye sura nyingi.

Jukumu la chombo hiki cha dunia la kuwa rafiki wa ukombozi lilikuwa zaidi ya kuharakisha uhuru wa dhamana zake. Hasa baada ya India kupata uhuru mwaka 1947, na kuingia kwa nchi hiyo kwenye UN, sauti dhidi ya ubeberu na ukoloni katika vyumba vya Shirika hilo la dunia ziliongezeka nguvu. 1960 zaidi ya nchi 15 za Afrika zilijiunga na UN katika mwaka mmoja. Kabla ya muda mrefu kupita, maazimio yalikuwa yakipitishwa kwenye Baraza Kuu kulaani ubeberu, ukoloni, ubaguzi wa rangi na mwishowe uzayuni kama makosa ya kimaadili dhidi ya kanuni mpya za haki ya mataifa.

Jukumu la UN kama mshirika wa maendeleo ya Afrika – ingawa ni ndogo kulingana na mahitaji ya Afrika – hata hivyo limekuwa muhimu. Iliokoa Kongo ya Ubelgiji ya zamani kutoka kwenye kumeguka kinchi ambako kulikuwa muhimu si kwa hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo lakini pia kwa nchi zote zilizokosa utengamano Afrika. Kama kujitenga kwa Katanga kungefanikiwa mapema baada ya uhuru wa Afrika, athari ambayo ingeonyeshwa kwa vikundi vingine vinavyotaka

kujitenga katika sehemu nyingine za Afrika zingekuwa na madhara makubwa kwa kanuni muhimu ya umoja wa taifa Afrika nzima.

Lakini ushirika wa maendeleo ya Afrika umechukua miundo mbalimbali jinsi miaka ilivyopita. Licha ya misukosuko na mivutano katika uhusiano na Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Afrika imefanya kazi kubwa kwenye masuala ambayo yanaanzia tangu kwenye majukumu ya Benki ya Maendeleo ya Afrika hadi uundaji na uendelezaji wa *Mpango wa Utekelezaji wa Lagos.*

Ushirika katika maendeleo ya Afrika umehusisha pia michango ya Shirika la Chakula na Kilimo, UNESCO, Shirika la Afya Duniani, Shirika la Kazi Duniani na mashirika mengine maalumu mbalimbali ya familia ya UN.

Swali la hali ya baadaye ni kama nchi za Afrika zinaweza kuwa na muungano wa kutosha kulipia madeni mawili ya msingi ambayo zinadaiwa na chombo hiki cha dunia. Kama ambavyo Umoja wa Mataifa hapo mwanzo ulikuwa rafiki wa ukombozi wa Afrika, je Afrika inaweza sasa kuhesabiwa kuwa rafiki wa ukombozi wa UN? Kama ambavyo shirika hilo la dunia na mashirika yake yameendelea kwa washirika wa maendeleo ya Afrika, je nchi za Afrika nazo zitakuwa washirika wenye ufanisi katika maendeleo ya shirika hilo la dunia? Kwa namna fulani Umoja wa Mataifa hauna uthabiti kama nchi za Kiafrika ambazo umezisaidia. Chombo hiki cha dunia nacho kinahitaji maendeleo na kukua. Kinahitaji utengamano na umoja. Kinahitaji kupanua "mapato yake ya kila kichwa" na kuwa na "marekebisho yake ya miundo." Lakini, kama Afrika, kinahitaji kutimiza hayo yote bila kuingia kwenye machungu ya "kurudi tena chini ya ukoloni".

Fursa ya uhusiano zaidi kati ya Afrika na UN ilipotea kwa huzuni wakati Marekani "ilipopiga kura ya turufu" katika uchaguzi wa mwananchi wa Tanzania, Salim Ahmed Salim, wa cheo cha katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa. Utawala wa Reagan ulimwona Salim Ahmed Salim kuwa ni mtu "hatari mwenye msimamo mkali." Washington kwa hiyo ilifunga mlango wake wa dhati dhidi ya uwezekano wa katibu mkuu wa UN wa kwanza Mwafrika.

Lakini maisha ya mbele huwa na maajabu yake.* Bado yanaweza kuonyesha kuwa ushirika wa kihistoria kati ya chombo hicho cha dunia na baadhi ya wanachama wake maskini na dhaifu kabisa bado unaweza kufikia maajabu ya ukombozi wa pamoja katika masuala ya dunia katika miaka ya mbele.

* Bw. Boutros Boutros-Ghali (Misri) alichaguliwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Desemba 1991.

## Hitimisho


Tumeangalia uhusiano wa Afrika na Umoja wa Mataifa kwenye Sura hii kwa kuyatazama maeneo matatu yanayohusiana.

Katika jukumu lake la kuwa kabaila wa kibeberu asiyekuwapo, shirika hilo la dunia lilitumiwa kama chombo cha usimamizi wa utawala wa makoloni ya zamani ya Wajerumani ya Tanganyika, Ruanda-Urundi, Togo, Kameruni, Afrika Kusini Magharibi (dhamana za zamani za Shirikisho la Mataifa). Kwa kweli Jamhuri ya Afrika Kusini – ambayo ndiyo iliyokuwa na mamlaka ya kuitawala Afrika Kusini



*PICHA 29.3 S. Nujoma, rais wa kwanza wa Namibia na J. Perez de Cuellar, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kwenye maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Namibia, Machi 21 1990*

Magharibi chini ya Shirikisho hilo – haikuutambua Umoja wa Mataifa kama mrithi wa Shirikisho hilo na hivyo kukataa kuwajibika kwa UN juu ya "nchi hiyo tegemezi." Kama tulivyoonyesha, ilikuwa ni baada ya mapambano kadha ndani ya




*MCHORO 29.4 Mfumo wa Umoja wa Mataifa (Chanzo: Umoja wa Mataifa)*

Umoja wa Mataifa na katika Mahakama ya Kimataifa ya Hague ndipo mamlaka ya UN juu ya Afrika Kusini Magharibi (baadaye iliitwa Namibia na Wapigania Uhuru) yaliweza kuthibitishwa kikamilifu, bila kujali kuendelea kutowafiki kwa Afrika Kusini.

Tukiwa kwenye mizani, msisitizo wa UN wa kutaka kuendelea kuwa na mamlaka Namibia ulitokana na haja ya kuiondoa nchi hiyo kwenye udhibiti wa Afrika Kusini. Ilikuwa ni mfano wa UN kusisitiza kuwa mamlaka ya ubeberu wa pamoja Namiba kwa nia ya kuwa msaidizi wa ukombozi wa nchi hiyo matakwa ya UN ya "kuikamata" upya Namibia ili kuiachia huru.

Zaidi ya Namibia, jukumu la UN kama mamlaka ya ubeberu wa pamoja lilikwisha hasa na uhuru wa tunu ya dhamana ya Tanganyika mwaka 1961. Dhamana nyingine zilikuwa zimekwishapata uhuru mapema zaidi.

# 30 Kuelekea mwaka 2000

Juzuu hili limejaribu kusawiri sifa maalumu za awamu ya historia ya Afrika tangu 1935, kipindi kwa kipindi. Miaka kuanzia 1935 hadi 1945 inajitokeza kama mwongo wa mgogoro wa kiulimwengu – kuanzia uvamizi wa Italia kwa Ethiopia mnamo mwezi Oktoba 1935 na kufikia kujisalimisha kwa Japani mnamo mwezi Agosti 1945. Miaka 15 kuanzia 1945 hadi 1960 ilishuhudia, kama tulivyokwishaonyesha, kuongezeka kwa mapambano dhidi ya ukoloni ambayo hatimaye matokeo yake yalikuwa ni nchi 16 za Kiafrika kupata uhuru katika mwaka wa 1960 peke yake. Ama kuhusu kipindi baada ya uhuru, kimeshuhudia majaribio ya kuimarisha uhuru, ujenzi wa mataifa, urasimishaji wa taratibu na mapambano kwa ajili ya maendeleo. Hebu tuchukue kila moja ya dhamira hizi za juzuu hili kwa zamu.

## Dunia iliyoshika moto

Iwapo mwaka 1935 Italia ilikuwa mrithi wa moja ya himaya za kale kabisa ya Ulaya (Roma ya kale), Ethiopia ilikuwa mwendelezo wa moja ya staarabu za kale kabisa Afrika. Mgogoro kati ya Italia na Ethiopia mnamo miaka ya 1930, ulielekea kuashiria mgongano wa mambo ya kale baina ya Ulaya na Afrika – mgongano wa magari mawili ya utamaduni wa kale.

Lakini ni wazi kulikuwa na upande wa kutisha wa uvamizi wa Italia kwa Ethiopia pia. Uvamizi huu ulikuwa ni tukio la ubeberu wa kisasa wa Ulaya kuvurumisha kwa mara ya mwisho Afrika ya wakati huo. Ethiopia – ambayo kwa muda mrefu sana ilikuwa oasisi ya mamlaka ya Kiafrika katika upekee bora ndani ya bara lililotamalakiwa na wakoloni – hatimaye ilitekwa kwa uroho wa Ulaya wa kushika nchi.

Juzuu hili limejadili athari ya muda mrefu ya Vita vya Pili vya Dunia barani Afrika – kutoka kuwezesha mapambano ya ukombozi hadi ujumuishaji wa Afrika kwa uthabiti zaidi katika mzingo wa ubepari wa Magharibi[1]. Miezi miwili baada ya kutangaza vita dhidi ya Ujerumani, serikali ya Uingereza ilitangaza kuwa iko tayari kununua kakao yote ya Afrika Magharibi. Unyonyaji wa uchumi wa Afrika kukidhi ruwaza za matumizi za Ulaya uliingia katika awamu mpya chini ya uchochezi wa vita.

Lakini Vita Vikuu vya Pili ya Dunia haikubadilisha tu hatima ya Afrika; bali pia iligeuza kimsingi hali ya siku za baadaye ya Ulaya yenyewe. Kutokana na mgogoro wa kiulimwengu kulitokea mgawanyo mpya wa Ulaya katika makambi ya ukomunisti na ubepari. Kwa mpopotoo wa ajabu wa majaliwa, mgawanyo wa kibara wa Ulaya uliashiriwa na mgawanyo wa *Berlin* - jiji ambamo mgawanyo wa Afrika ulifanyika miongo sita nyuma. Kudra ya Kiafrika ililipiza kisasi cha mwisho. Jiji lilolotamka laana ya kinyang'anyiro cha Afrika mnamo 1885 lilikuwa pia jiji lililopatwa na laana ya mgawanyo wa Ulaya toka 1945 na kuendelea. Kama mgawanyiko wa Afrika ulivyoonekana kuwa hauwezi kugeuzika katika kipindi cha karibuni ambacho matokeo yake yanatabirika, ndivyo mgawanyo wa Ulaya ulivyokuwa kufuatia Vita vya Pili vya Dunia; pamoja na maono ya Mikhail Gorbachev ya miaka ya 1980. Mara tu wahenga wa Afrika walipofaulu kulipiza kisasi chao cha dhati – lakini wakiacha mabara haya mawili yenye majonzi yakipata uchungu wa kugawanywa.

Jambo ambalo halipaswi kusahauliwa ni kuhusika kwa Afrika katika mgogoro wa dunia ambao uliyatangulia yale matukio na kubadilisha sura za Ulaya baada ya vita na Afrika baada ya vita. Kwa mfano, Waganda elfu hamsini na tano walishiriki katika kikosi cha Waafrika cha jeshi la mfalme wa Uingereza. Baadhi ya Watanganyika 87,000 waliotoa huduma vitani walishiriki katika uvamizi wa Madagascar wa mwaka 1942 dhidi ya Vichy na kwa ajili ya de Gaulle. Askari wengi wa Kiafrika walihusika katika vita dhidi ya Japan huko Burma. Tangu mwaka 1939 Kikosi cha Kinigeria kilikuwa kimeunda bataliani 15. Na maelfu ya askari wa Afrika Kaskazini walitoa maisha yao kwa miaka kadhaa katika bahati zilizokuwa zikibadilikabadilika kati ya Rommel, Montgomery, Eisenhower na wapiganaji wengine maarufu kaskazini mwa Sahara.

Lakini hatimaye awamu yenye kutia uchungu kabisa ya vita kwa Afrika ilitokea mapema sana katika mgogoro wa kiulimwengu. Italia, iliyojifanya kuchukua upya

[1] Kwa tafiti nyingine, tazama pia R. Oliver na M. Crowder, 1981. P. Duignwan na L.H. Gann 1973 na 1975 na G.S.P. Freeman – Grevlle 1973.

urithi wa Roma ya kale, ilikuwa miongoni mwa nchi za kwanza kushindwa. Upinzani ndani ya Ethiopia ulishindikana kuzimwa. Makombora yalitupwa kwa Kaimu Mfalme aliyeteuliwa na Italia huko Addis Ababa; Abuna Abraham alipofushwa na gesi ya sumu Waitalia walipojaribu kumfanya kuwa kiongozi wa Kanisa la Ethiopia.

Upinzani wa Ethiopia uliziteka bataliani 56 za Waitalia. Mnamo tarehe 20 Januari 1941 Mfalme Haile Selassie alivuka kutoka Sudan na kuingia Ethiopia kwa miguu. Mnamo tarehe 7 Machi 1941, askari wa Kiingereza na wa kifalme walijipenyeza kwa wingi nchini kwa ruhusa ya mfalme wa Ethiopia. Waingereza, na askari wa Kiafrika waliiteka Addis Ababa mnamo Aprili 1941. Mfalme alichukua tena uongozi mwishoni mwa Januari 1942.

Na hivyo vita vya watu maarufu baina ya mrithi wa Kaisari na mrithi wa Malkia wa Sheba vilikwisha kwa fedheha ya ndoto za Kaisari. Dunia hii ilikuwa imekuwa na utata mkubwa. Ushindani wa kibeberu baina ya mataifa makubwa ya Ulaya yenye kukinzana ulisaidia bahati za mnasaba wa Sheba aliyekuwa amezingirwa: Mrithi wa Kaisari alitengwa na baadhi ya mikoa yake ya siku za nyuma. Mnamo tarehe 18 Aprili 1945, Benito Mussolini alinyongwa na Wazungu wenzake. "Hivi ndivyo wanavyoanguka wenye majivuno".

## Mapambano dhidi ya ukoloni

Kipindi kidogo cha pili cha juzuu hili kinahusu miaka ya 1945 hadi 1960 - iliyokuwa na ongezeko la mapambano ya kitaifa dhidi ya ukoloni. Kulikuwa na sehemu tatu za msingi za mapambano haya. Sehemu moja ilikuwa ya ndani kwa kila koloni - jaribio la kuhamasisha umma uliokuwa ukinyanyaswa dhidi ya ubaguzi wa rangi na utawala wa kigeni ndani ya jamii fulani maalumu. Sehemu ya pili ilikuwa ndani ya utawala wa kibeberu - jaribio la kuorodhesha wanaharakati wa kimaendeleo ndani ya mamlaka ya dola. Kwa namna fulani huu ulikuwa mkakati wa kumgawanya adui - kuanzisha vurugu ndani ya nchi zenyewe za kibeberu.

Sehemu ya tatu ilikuwa dunia yenyewe - jumuiya ya kimataifa kwa jumla. Je itakuwaje maoni ya dunia yaelekezwe upande wa waliotaka kuondolewa kwa wakoloni?

Kuhamasisha umma katika makoloni yenyewe kulikuwa ni mkakati muhimu kuliko yote. Lakini hata kabla ya kuanza kwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, wanaharakati wa Afrika Kaskazini kama vile Bourguiba walikuwa wamekwishaanza uhamasishaji wa maeneo yao. Chama cha *Parti populaire algerien* (PPA) kiliundwa na Messali Hadj mwaka 1936. Na katika Morocco

iliyotawaliwa na Wahispania, 'Abd al-Khalik Tares alianzisha Chama cha Islah mwaka huo huo. Vilevile mwaka 1936 uzalendo wa Kimisri hatimaye ulifanikiwa kuwalazimisha Waingereza kuacha kuikalia Misri kijeshi isipokuwa katika Ukanda wa Mfereji wa Suez. Lakini mapambano ya Misri dhidi ya kuwepo kwa Waingereza kijeshi katika Ukanda wa Mfereji wa Suez yaliendelea hata baada ya kukamilika kwa Mkataba wa Uingereza na Misri wa mwaka 1936. Mnamo Januari 1944, uhuru wa Morocco ulidaiwa na Chama cha Kizalendo. Ahmed Balafredj alitiwa nguvuni na ghasia zilizuka huko Rabat na Fez mnamo mwezi Machi. Huko Algeria pia mnamo 1944 Ferhat 'Abbas alianzisha chama cha AML(*Amis da manifeste et de la liberte)*. Chama hiki kwa haraka kilipata wanachama nusu milioni.

Kwingineko barani Afrika kuvuvumka kwa uzalendo na uhamasishaji wa ndani kulikuwa wazi kukichukua sura tofauti. Kuanzia 1933 hadi 1946, Ufaransa ililazimishwa kumpeleka uhamishoni Leon Mba kutoka Cameroon kwa "uchochezi'. Mnamo 1940, chama cha Tonsi kilianza huko Angola kama "kundi la Tawa", katika uasi wa kiutamaduni dhidi ya amali za kigeni. Mnamo Septemba 1946, Jomo Kenyatta alirejea Kenya baada ya kuwa ng'ambo kwa miaka 15. Alijiwekea ajenda ya kufanya uhamasishaji wa kisiasa nyumbani.

Haikuchukua muda mrefu kabla ya vyama kuanza kuchipuka kote barani Afrika - kutoka chama cha *Union des population du Cameroun* (UPC) hadi chama cha Convention Peoples Party (CPP) huko Ghana, kutoka chama cha *Rassemblement democratique africain* (RDA) katika himaya ya Ufaransa hadi chama cha Tanganyika African National Union (TANU). Upinzani dhidi ya ukoloni ulikuwa ukisimikwa na kuongozwa vizuri. Uhamasishaji wa kisiasa nyumbani ulikuwa umeanza kwa dhati.

Lakini ingawa sehemu ya nyumbani ilikuwa ya msingi pia ilikuwa muhimu kuwatafuta washirika kutoka katika nchi za wakoloni wenyewe. Japo kwa kiasi kidogo kabisa, hii ingeweza kuwa namna ya "kumgawanya adui' - kumgonganisha Mfaransa na Mfaransa., Mwingereza na Mwingereza. Ikiwa ukoloni uliendeshwa kwa msingi wa "gawa na shinda', mapambano dhidi ya ukoloni yangeweza kutumia mkakati kinyume cha huo wa "gawa na ukomboe'. Mahusiano ya asili ya chama cha RDA na Chama cha Kikomunisti cha Ufaransa yangeweza kuhalalishwa kwa msingi kama huo kama hakuna mingine.

Sera ya kikoloni ya Wafaransa ya jumuiya na muungano wa kisiasa ilifaa sana kwa harakati dhidi ya ukoloni huko Ufaransa kwenyewe. Kwa vyovyote vile, makoloni ya Ufaransa Afrika yaliwakilishwa moja kwa moja katika asasi za kisheria na kikoloni huko Paris kwenyewe-namna ya uwakilishi wa kikoloni ambayo

haikufanana na mtindo wa Waingereza wa kuendesha makoloni. Ilikuwa mnamo Novemba 1945, Leopold Sengho na Lamine Gueye (wa Senegal), Felix Houphouet - Boigny (Cote d' Ivoire), Apilth Sourou Migan (Dahomey), Fily Dabo Cissoko (Sudan iliyotawaliwa na Ufaransa) na Yacene Diallo (Guinea) walichaguliwa kuwakilisha nchi za Afrika Magharibi zilizokuwa chini ya Ufaransa katika Bunge la Ufaransa. Wiki chache kabla Mwana wa mfalme Alexandre Douala - Manga Bell na Dkt L. P. Anjoulet walichaguliwa kama manaibu wa kwanza wa Cameroon. Isingeweza kueleweka kwa Jomo Kenyatta, Obafemi Awolowo au Nnamdi Azikiwe kuchaguliwa kuingia kwenye Bunge la Uingereza huko London. Badala ya kuwakilishwa moja kwa moja katika asasi za makao makuu, wazalendo wa Kiafrika katika makoloni ya Waingereza walijaribu kushawishi maoni ya Waingereza kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja kwa kuwatumia Waingereza wa msimamo huria au wa mrengo wa kushoto. Wabunge wa bunge la Uingereza kama vile Fenner Brockway na Barbara Castle walitumiwa na wazalendo wa Kiafrika kupitisha madai yao kwenda bungeni. Na magazeti ya Kiingereza kama vile *Daily Worker*, *New Statesman* na *Manchester Guardian* yalisaidia katika mapambano dhidi ya ukoloni ndani ya nchi yenyewe iliyomiliki makoloni.

Waalgeria kwa upande mwingine, walikuwa wakiingia Ufaransa kwenyewe kwa kiwango kilichokuwa kimeruhusiwa kwa makoloni mengine ya Kifaransa. Katika siku ya mwisho wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, sheria ya Kifaransa iliwapa Waislamu wa Algeria wawakilishi 15 katika Bunge la Taifa na Maseneta saba katika Baraza la Jamhuri. Ridhaa hii ilitolewa mnamo mwezi Machi 1944 kwa matarajio ya ukombozi wa Ufaransa. Kufikia Agosti 1946 iliwezekana kwa Ferhat "Abbas, kiongozi wa chama *cha Union democratique du manifeste algerien* kuwasilisha mbele ya Bunge la Taifa huko Paris, rasimu ya sheria ya Jamhuri ya Algeria iliyoshirikishwa na Ufaransa. Na bado miaka kumi baadaye Ferhat "Abbas alikuwa kiongozi wa kisiasa wa serikali ya Algeria uhamishoni katika uasi dhidi ya utawala wa Kifaransa huko Algeria.

Wajibu huu wa baadaye wa Ferhat "Abbas unaturudisha katika sehemu ya tatu ya mapambano dhidi ya ukoloni - sehemu ya jumuiya ya kimataifa kwa jumla. "Abbas alikuwa msemaji mkuu wa kimataifa wa chama cha *Front de liberation nationale* - FLN (Chama cha Ukombozi wa Taifa) cha Algeria. "Abbas alisafiri toka mji mkuu wa nchi moja hadi mwingine kutetea haki ya Algeria na kutafuta kuungwa mkono.

Umoja wa Mataifa nao ulikuwa mshirika muhimu na medani nzuri kwa ajili ya wazalendo wa Kiafrika. Lakini sehemu za msingi kabisa za jumuiya ya kimataifa

ilibidi ziwe ni majirani wa Algeria. Kwa Algeria, hii ilikuwa na maana ya nchi nyenzake za Kiafrika, hasa Maghreb yote na Misri kwanza. Lakini Aligeria pia ilijaribu kuzishawishi nchi nyingine za Kiafrika zilizobaki. Mojawapo ya juhudi hizi za dhati ilifanyika katika Mkutano Waafrika Wote huko Accra mnamo 1958.

Lakini bara la Afrika halikuwa tu mpokeaji wa athari za nje. Lilikuwa pia linasaidia kubadilisha ajenda ya marekebisho duniani. Utaifishaji wa Gamal "Abd al-Nasser wa Mfereji wa Suez mwaka 1956 ulikuwa moja ya juhudi muhimu za Kiafrika za karne ya ishirini. Miaka mitano tu kabla (1951) Iran chini ya Muhammad Mosadeq ilitaifisha rasilimali yake ya mafuta. Shirika la Ujasusi la Marekani lilimwondoa madarakani Mosadeq na kumweka mtu wa ukoo wa Pahlavi wa ukoo wa Shah ambao ulikuwa ukiunga mkono upande wa nchi za Magharibi zaidi. Hii mwanzoni ilielekea kufunga jaala ya nchi yoyote ya Dunia ya Tatu inayotaka kutaifisha na kudhibiti rasilimali yake.

Milango ya juhudi za Dunia ya Tatu katika kudhibiti rasilimali zao ilifunguliwa tena na Gamal "Abd al-Nasser mnamo Julai 1956. Rasilimali wakati huu haikuwa mafuta - kama katika Iran ya Mosadeq - bali mfereji wa Misri uliojengwa kwa nguvukazi ya Wamisri kwa gharama kubwa kwa binadamu. Maelfu mengi ya maisha ya Wamisri yalipotea katika ujenzi wake karibu miaka mia moja kabla ya al-Nasser hatimaye mfereji ulitaifishwa. Tofauti na Mosadeq, al- Nasser alifaulu katika jaribio lake hili la kijasiri. Baada ya mfereji wa Suez, utaifishaji na ujamiishaji wa rasilimali za Kiafrika ulizidi kuwa hatua salama za kisiasa kwa serikali za Kiafrika kuzitafakari.

Mfereji wa Suez na matokeo yake ya baadaye ulikuwa msingi wa tofauti kubwa baina ya Urusi kama tishio la Ubeberu kwa Afrika na Urusi kama mshirika katika mapambano ya kuleta uhuru. Urusi ilipatia Misri mabaharia kwa ajili ya Mfereji wa Suez pale mabaharia wa nchi za Magharibi walipoondolewa katika mgogoro uliokuwa ukiongezeka baada ya utaifishaji uliofanywa na Al - Nasser. Urusi ilichukua hata jukumu kubwa la kuisaidia Misri kujenga Bwawa la Aswan ambalo Uingereza, Marekani na Benki ya Dunia zilivunja ahadi yao ya kusaidia. Tokea wakati huo, Urusi inaelekea iliondoa hamu yote ya kutwaa nchi za Afrika, na kumbukumbu zinaonyesha kuwa kwake tayari kuunga mkono mapambano ya uhuru Afrika. Mfereji wa Suez ulikuwa muhimu. Hatua kubwa za Al-Nasser zilikuwa za Afrika kujenga urafiki na jumuiya za kimataifa - walau hadi awamu ya karibuni zaidi ya mapambano ya dunia dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Kwa hiyo, hizi zilikuwa awamu za mapambano dhidi ya ukoloni - kwanza, uhamasishaji wa watu ndani ya nchi, pili, upenyaji wa duru za wakoloni katika jaribio la "gawa na komboa', na tatu, kutafuta urafiki na kuongoa jumuiya ya

kimataifa, kwa kuanza na kuwapanga majirani wao. Katika sura iliyotangulia tulirejea sharti la Kwame Nkrumah. *"Tafuteni kwanza ufalme wa kisiasa na mengine yote mtaongezewa'*. Baada ya kupata ufalme wa kisiasa inabidi tuirejea dhamira hii kwa mara nyingine.

Sura za awali zimeshughulikia kwa uangalifu mkubwa mpito kutoka mapambano ya Kiafrika kwa ajili ya uhuru hadi kuendelea kujaribu kujenga taifa. Sura nyingine zilijadili juhudi ya kuupatia *Utaifa* wa Kiafrika mfungamano zaidi wa kiutamaduni wa kutoa uhalali na mamlaka makubwa zaidi kwa *dola* ya Kiafrika. Mapambano haya yamezidi kuimarisha uhuru, kuhakikisha umoja wa nchi na kuwezesha usitawi na maendeleo.

Lakini tunaelekea wapi kutokea hapa? Mapinduzi mawili muhimu kabisa yanayoisubiri Afrika ni, kwanza, M*apinduzi ya kijinsia katika wajibu* na pili, *Mapinduzi ya kisayansi katika stadi.* Mapinduzi haya mawili katika *jinsia* na katika *sayansi* yanafungana kwa karibu. Hebu tuutazame kwa karibu upembuzi huu maalumu.

Mabadiliko ya msingi katika mahusiano baina ya jinsia, kwa hakika, yalikuwa yakitokea kwa sehemu fulani kwa sababu ya kuingiliana kwa Afrika na tamaduni nyingine katika kipindi hiki. Uislamu na ukoloni wa Magharibi vilikuja na vielelezo vibadala vya uhusiano baina ya watu wa jinsia tofauti. Familia na jamii ya Kiafrika kwa jumla vimenaswa katika mivutano hii ya mabadiliko ya kiutamaduni. Ni suala hili la jinsia katika jamii ya Kiafrika tangu mwaka 1935 ambalo tutalishughulikia sasa.

## Dhima ya jinsia katika Mpito

Afrika tangu 1935 imeshuhudia mabadiliko muhimu katika dhima na kazi za wanaume na wanawake barani Afrika. Katika tamaduni nyingi za kimapokeo tumekuwa na imani kwamba Mungu alimfanya mwanamke mwangalizi wa *moto*, *maji* na *ardhi.* Mungu mwenyewe alishikilia kipengele cha nne cha ulimwengu - *hewa* iliyopo wakati wote.

Kusimamia moto kulikuwa na maana ya jukumu la kufanya nishati ipatikane. Na chanzo kikuu kabisa cha nishati katika Afrika ya vijijini ni kuni. Mwanamke wa Kiafrika alikuwa na wajibu usiolingana wa kutafuta na kubeba mzigo mkubwa wa kuni, ingawaje mara nyingi wanaume ndio waliokata miti mikubwa mwanzoni.

Kusimamia maji kulihusisha kioevu ambacho kilikuwa alama ya kuendelea kuwepo na usafi. Mwanamke wa Kiafrika alipata wajibu wa kuhakikisha kwamba dutu hii muhimu ilikuwa inapatikana kwa ajili ya familia. Ametembea umbali mkubwa

kutafuta maji. Lakini pale kisima kilipohitaji kuchimbwa mara nyingi ni wanaume ndio walifanya kazi ya kuchimba.

Kusimamia ardhi kumekuwa sehemu ya imani ya *rutuba mara mbili* . Mwanamke anahakikisha kuendelea kuwepo kwa kizazi hiki kwa kuendelea kuwa na wajibu mkuu katika kilimo - na kuhifadhi rutuba ya udongo. Mwanamke anahakikisha kuwasili kwa kizazi kinachofuata kwa wajibu wake kama mama - rutuba ya maji na mimba. Rutuba mara mbili, huwa hali ya dhima tatu ya usimamizi wa kuwa mwanamke wa Kiafrika, ingawaje wakati wote kwa ushirikiano na mwanaume wa Kiafrika.[2]

Je ni nini kimetokea kwa imani hii ya usimamizi wa aina tatu katika kipindi tangu 1935? Vipengele tofuati vya tajriba ya kikoloni viliathiri dhima za wanaume na wanawake barani Afrika kwa njia tofauti.

Miongoni mwa vipengele vilivyoongeza dhima ya mwanamke kwenye ardhi ni kibarua kwa ajili ya wanaume. Kwa mujibu wa Margaret Jean Hay, kibarua kwa wanaume kilichukua muda kabla ya kuanza kuathiri wajibu wa wanawake kwenye ardhi. Kazi yake Hay ilifanyika miongoni mwa wanawake wa Kiluo nchini Kenya.

Kufikia mwaka 1930 idadi kubwa ya wanaume walikuwa wameondoka Kowe walau mara moja kwenda kutafuta ajira njè... Zaidi ya nusu ya kundi hili ilikaa huko kwa vipindi vya miaka kumi na mitano au zaidi... Huku kusafirisha nje nguvukazi kunakoongezeka kutoka majimboni kunaweza kufikiriwa kuwa kumeongeza mzigo wa kazi za kilimo kwa wanawake... Tangu 1920, waendeshaji walilalamikia ukweli kwamba Nyanza ilikuwa inakuwa kisima cha nguvu kazi kwa koloni zima... Hata hivyo, wahamaji wa muda mfupi wa miaka ya 1920 kwa kawaida walikuwa vijana ambao hawajaoa, ambao walikuwa na wajibu mdogo katika uchumi wa mahali hapo zaidi ya kuchunga na kuteka ng'ombe wakati wa vita. Zaidi ya hayo, vibarua wahamaji wa muda mfupi wangeweza na mara nyingi walipanga kuwa mbali wakati wa upungufu wa kazi nyakati za kilimo... Hivyo uhamaji wa nguvukazi katika kipindi kabla ya 1930, uliondoa nguvukazi kidogo, kutoka kwenye uchumi wa mahali hapo na haukubadilisha sana mgawanyo wa kazi kijinsia.[3]

Nimemshukuru marehemu Okot P' Bitek, mwanaanthropolojia wa Kiganda na mshairi wa msisimko na taarifa kuhusu visasili vya wanawake kaskazini mwa Uganda. Mimi na Okot pia tulijadili mifanano na Tofauti kati ya dhana za Kiafrika za maji na mwazo ya Empedocles, mwanafalsafa wa Kiyunani wa karne ya tano kabla ya enzi za Ukristo. Chunguza pia O. p' biteka, 1971

M.J. Hay, 1976, kur. 98-99. Kwa mtazamo wa kike tazama pia M.R. Cutrufelli, 1983

Lakini Margaret Hay anaendelea kuonyesha jinsi kudorora kwa uchumi Duniani na Vita vya Pili vya Dunia vilivyobadilisha hali ya vibarua wahamaji na kuandikisha wanaume jeshini kulivyochukua idadi kubwa ya wanaume kutoka katika shughuli za ardhi. Hii ilichanganyika na kukua kwa viwanda vya uchimbaji madini kama vile machimbo ya dhahabu huko Kowe kuanzia 1934 na kuendelea.

> Huku kutokuwepo kwa wanaume kwa muda mrefu kulikuwa na athari katika mgawanyo wa kazi kijinsia, kwa wanawake na watoto kuchukua kazi zaidi za kilimo kuliko ilivyokuwa hapo awali... Miaka ya 1930 inawakilisha mpito kuhusiana na mgawanyo wa kazi kijinsia; na ilikuwa wazi wanawake walibeba mzigo wa mpito katika maeneo ya vijijini.[4]

Wanawake katika kipindi hiki, kutoka miaka ya 1930 na kuendelea, walijihusisha zaidi kama wasimamizi wa ardhi. Huko Kusini mwa Afrika uhamaji wa wanaume kwenda migodini ulizidi kutia shauku. Kufikia miaka ya 1950 mgawanyiko wa ajabu ulikuwa ukifanyika katika jamii fulani za Kusini - mgawanyo baina ya wafanyakazi waume tabaka la wafanyakazi wa viwanda na wakulima wa kike. Sheria za Afrika Kusini dhidi ya familia kujiunga na waume katika migodi ulizidisha uwekezaji kwenye ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa watu wa jinsia tofauti. Wanawake wengi katika nchi za mstari wa mbele ilibidi watimize wajibu wao wa usimamizi wa aina tatu wa moto, maji na ardhi katika utengano mkubwa mno.

Vita vya ukombozi huko Kusini mwa Afrika kutoka miaka ya 1960 viliathiri utengamano wa familia na mgawanyo wa kazi kijinsia wa kimapokeo. Baadhi ya wapiganaji hawakuwa na wake zao. Kwa hakika, majeshi ya ukombozi kama vile ZANLA na ZIPRA huko Zimbabwe na FRELIMO huko Msumbiji yalijumuisha wapiganaji wachache wa kike. Lakini kwa jumla athari za vita ilivuruga maisha ya familia na mgawanyo wa kazi kijinsia wa kimapokeo.

Baada ya uhuru kulikuwa na vita vya kupinga mapinduzi miongoni mwa nchi za mstari wa mbele. Moja ya vita vya baada ya uhuru vilivyoundwa na binadamu ni vile vya Msumbiji vilivyoanzishwa na chama cha upinzani wa Kitaifa cha Msumbiji (MNR au RENAMO).

Vilevile, kumekuwa na taathira kwa mahusiano baina ya jinsia. Zaidi ya matokeo ya kawaida yanayovuruga ya vita kwa familia, kufikia miaka ya 1960, chama cha RENAMO kilikuwa kimetia hasara ya kutosha kwenye miundombinu huko Msumbiji kiasi kwamba wafanyakazi wahamiaji wengi walishindwa kufika nyumbani kwenye familia zao katikati ya mikataba yao na migodi ya Afrika Kusini.

Si wazi kabisa jinsi hali hii ilivyoathiri imani ya 'rutuba mara mbili' kuhusiana na dhima ya mwanamke wa Kiafrika. Uwezekano mmoja ni ule wa kutokuwepo kwa waume kwa muda mrefu sana kupunguza viwango vya rutuba katika baadhi ya jumuiya huko Msumbiji. Uwezekano mwingine ni kwamba ruwaza ya wafanyakazi wahamaji huko Kusini mwa Afrika kwa jumla imechochea mwelekeo katika mfumo usiopingika wa mke kuwa na waume wengi. Mwanamke anayeachwa nyumbani hupata, kwa muda mume wa ziada.[5]

Ikiwa ruwaza iliyoenea zaidi ni ile ya kupungua kwa rutuba ya uzazi kama matokeo ya kutokuwepo kwa waume kwa muda mrefu, kanuni ya rutuba mara mbili imepunguza shughuli za kijamii za rutuba ya mji wa mimba na kuzidisha kuhusika mwanamke katika mambo yanayohusu rutuba kwa ardhi.

Kwa upande mwingine, ikiwa mwelekeo muhimu zaidi katika jamii zinazojihusihsa na uchimbaji madini huko Kusini mwa Afrika zinalenga kwenye mfumo wa mke kuwa na waume wengi, kiungo kipya kizima cha mahusiano ya kijamii kinaweza kuwa kinaanza kuundwa huko Kusini mwa Afrika.[6]

Mabadiliko mengine barani Afrika wakati wa kipindi hiki ambayo yaliathiri mahusiano baina ya wanaume na wanawake yalikuwa ni pamoja na teknolojia mpya kuhusu dhima za kijinsia. Kilimo cha jembe bado kilimwacha mwanamke wa Kiafrika akihusika kikamilifu katika kilimo lakini matumizi ya mashine katika kilimo barani Afrika yameelekea kuwaweka pembezoni wanawake. Dhima yao kama 'wasimamizi wa ardhi' unatishiwa na haki za kiume katika teknolojia mpya na za hali ya juu zaidi.

Tishio jingine kwa dhima kuu ya mwanamke wa Kiafrika katika uchumi katika kipindi hiki limetokana na hali ya elimu ya Magharibi. Ni kweli kwamba mwanamke wa Kiafrika aliyeathiriwa na mambo ya magharibi kwa kawaida ana uhuru mkubwa wa kwenda sehemu mbalimbali na mwenye uhuru zaidi kwa ajili ya maslahi yake kuliko mwenzake wa kijadi. Lakini tafsiri kutoka msimamizi wa moto, maji na ardhi kwenda kwenye mtunza tapureta kwa hakika ni namna ya kuwekwa pembezoni kwa mwanamke wa Kiafrika. Kupiga taipu kuna umuhimu mdogo kwa maisha kuliko kilimo. Mwanamke wa Kiafrika aliyeathiriwa na mambo ya Magharibi katika nusu ya pili ya karne ya ishirini ameelekea kuwa huru lakini mwenye umuhimu mdogo kwa chumi za Kiafrika kuliko mwanamke wa jadi katika maeneo ya vijijini.

[5] Hapana shaka kuwa mipangilio kama hii iko huko Msumbiji. Jambo lisilokuwa wazi ni jinsi mfumo wa mke wa waume wengi ulivyoenea huko Kusini mwa Afrika

[6] Ninamshukuru kwa utafiti wa uwandani na mahojiano huko Kusini mwa Afrika yaliyoandamana na mradi wa television wa BBC/WETA, tazama A Mazrui, 1986.

Tishio la tatu kwa dhima ya mwanamke wa Kiafrika katika kipindi hiki lilitokana na uchumi wa Kiafrika kufanywa wa kimataifa. Shughuli za uchumi za Kiafrika zilipokuwa za mahali hapohapo, wanawake walikuwa na wajibu wa kuweza kutoa uamuzi katika masoko na kama wafanyabiashara. Lakini mielekeo ya kikoloni na ya kipindi baada ya ukoloni ya kupanua kiwango cha uchumi imezidi kumsukuma pembeni mwanamke katika ufanyaji maamuzi ya kimataifa. Ni kweli kwamba wanawake wa Nigeria hasa wamekataa kuwekwa pembezoni kabisa, hata katika biashara ya kimataifa. Lakini kwa jumla, Waafrika wanaojishughulisha na soko la Kimataifa na wanaokaa katika bodi za mashirika ya kimataifa kwa kiasi kikubwa ni wanaume. Katika mikutano ya Shirika la Nchi Zinazouza Mafuta Nje - walipo Waislamu wengi - kuna vizuizi vya ziada kuhusu hata Nigeria kuwakilishwa na mjumbe wa kike.

Lakini ni ipi njia ya siku za baadaye inayoweza kubadilisha uwiano baina ya wanaume na wanawake katika maisha ya hadharani barani Afrika? Sababu ambazo zinawaweka wanawake chini kisiasa haziko katika tofauti za kiuchumi. Wanawake barani Afrika wanajishughulisha sana kiuchumi; wanawake huko Saudi Arabia wamekwamishwa kiuchumi. Na bado katika aina hizi mbili za jamii wanawake wako chini kisiasa. Na hivyo tofauti za kiuchumi siyo sababu kamili ya kutawaliwa kwa wanawake kisiasa.

Kitu ambacho ni cha jumla kwa hakika si dhima ya kiuchumi ya wanawake bali dhima yao ya kijeshi. Kote barani Afrika (na kwa hakika kote duniani) wanawake wamewekwa pembezoni kijeshi. Kitu ambacho siku moja kitabadilisha uwiano wa kisiasa baina ya wanaume na wanawake ni pale jeshi litakapokuwa la jinsia zote mbili. Jeshi la Somalia limeanza kuwaandikisha wanawake. Jeshi la anga la Algeria limeanza kuwaajiri marubani wanawake. Jamii mbili hizi za Kiislamu barani Afrika zimeanza kuwapatia wanawake dhima ya kijeshi. Lakini hali ya siku za baadaye inahitaji hatua za dhati zaidi za wajibu wa kijinsia. Katika bara hili lenye mapinduzi ya kijeshi tunaweza kulazimika kusubiri siku ambapo tangazo la mapinduzi ya kijeshi huko Afrika Magharibi litataja yafuatayo : Brigedia Jenerali Janet Adebiyi ameshika madaraka katika mapinduzi ya kijeshi mjini Lagos?[7]

## Upanafrika: Shirikisho la jinsia

Upanafrika umekuwa ukitazamwa kama mahusiano baina ya Waafrika yanayovuka mipaka ya nchi. Lakini umajumui huu unapaswa kufafanuliwa upya kujumuisha

[7] Suala hili linajadiliwa kwa misingi hiyohiyo katika A. A. Mazrui, 1990

mahusiano ya Waafrika wote kuvuka mgawanyo wa kijinsia. Haitoshi tu kuvuka migawanyo ya utaifa na urithi wa nchi vilivyopatikana kutokana na kinyang'anyiro cha Afrika. Kuna haja ya kuvuka hata mgawanyo mkongwe wa kisiasa baina ya Waafrika pengo la kisiasa baina ya wanaume na wanawake katika eneo la mambo ya umma.

Kwa maelezo ya Nkrumah, upanafrika ulifafanuliwa kama kuwa tayari kugawana madaraka katika shirikisho la nchi. Lakini kuna ulazima mkubwa zaidi wa kugawana madaraka katika ushirikiano wa jinsia.

Afrika ya jadi kabla ya ukoloni wa Wazungu ilijua matukio makubwa ya kugawana madaraka baina ya jinsia. Enzi za Hatshepsut wa Misri (karne ya kumi na tano kabla ya enzi ya Ukristo), Nzinga wa Angola yapata 1581-1663), Yaa Asantewa wa Ashanti (yapata 1830-1921) na Nehanda wa Zimbabwe (yapata 1863-98) ni miongoni mwa mifano dhahiri ya upanafrika katika fahiwa hii maalumu ya kugawana madaraka baina ya jinsia. Baadhi ya enzi hizi tayari zimekwishashughulikiwa katika mfululizo huu wa majuzuu ya awali ya UNESCO.

Je, athari ya kikoloni imesaidia au imedhuru mgawano wa madaraka baina ya jinsia barani Afrika? Tumedokeza kwamba kumbukumbu katika mahusiano ya kijinsia zimechanganyika. Utawala wa kikoloni na athari za nchi za Magharibi kiuchumi zimewaweka pembezoni wanawake katika baadhi ya dhima zao – wakati zikiwainua katika sehemu nyingine. Upanafrika kama suala la mahusiano ya jinsia umeathirika na vilevile kunufaika kutokana na athari za Magharibi kwa Afrika.

Kwa sababu kipindi tangu 1935 kimeshuhudia kujumuishwa kikamilifu kwa Afrika katika mfumo wa dunia, dunia ya nje, kwa ufafanuzi, imejihusisha zaidi katika maisha ya kawaida ya wanaume na wanawake wa Afrika kuliko ilivyokuwa hapo awali. Migongano kadhaa ya kijamii imetokea. Kuhusiana na dhima ya wanawake, kujumuishwa kwa Afrika katika mambo ya kimataifa kumewadidimiza kiuchumi na kuanza kuwainua katika diplomasia.

Tumeonyesha kwamba katika kipindi hiki tangu 1935, uchumi wa ndani ya Afrika umetoa majukumu makubwa kwa wanawake kuliko uchumi uliokuwa wa kimataifa. Tumetaja kwamba kihistoria wanawake wa Kiafrika mara nyingi walikuwa na uwezo wa kuuza ziada ya mazao ya kilimo na vilevile kuwa washiriki halisi katika taratibu za uzalishaji vijijini. Pale uzalishaji na uuzaji ulipoongezeka kuwa wa kimataifa katika Afrika ya wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni, sehemu ya wanawake katika kudhibiti taratibu za kiuchumi ilianza kupungua kama tulivyoona. Kama tulivyoonyesha, Waafrika waliokaa katika bodi za wakurugenzi za mashirika ya kimataifa wengi wao walikuwa wanaume. Hapana shaka kuwa

uchumi kufanywa wa kimataifa wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni, hadi sasa, kumekuwa kukiwaweka pembezoni wanawake. Upanafrika kiuchumi kwa jinsia zote umeathirika katika kipindi hiki.

Kwa upande mwingine, diplomasia kama kazi baada ya uhuru iliongeza fursa ya upanafrika mpya kwa wanawake wa Kiafrika walioelimika sana enzi ya baada ya ukoloni. Mnamo Septemba 1969, Anjie E. Brooks wa Liberia (kama ilivyoonyeshwa katika sura ya 1) aliteuliwa kuwa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa - mwanamke wa pili kushika wadhifa huo. (Wa kwanza alikuwa Mama Pandit wa India, mwanafamilia wa familia ya Nehru). Jijini New York Angie Brooks alikuwa mwanadiplomasia mwandamizi wa Kiafrika. Upanafrika katika jinsia zote ulinufaika.[8]





*PICHA 30.1 kushoto; Angie Brooks wa Liberia, ambaye alikuwa rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo 1969-70; kulia: Binti mfalme Elizabeth Bagaya wa Uganda, Waziri wa mambo ya nchi za nje, akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Septemba 1974*

Balozi Brooks alikwishaonyesha njia nyingine za kidiplomasia mapema - ikiwa ni pamoja na huduma zake kama mwanamke wa kwanza na Mwafrika wa kwanza kuongoza Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa. Aliposhika nafasi ya urais wa Baraza Kuu mwaka 1969, Bi Brooks alithibitisha: "Ninajivunia bara langu,

8 Kwa msisimko kwenye dhamira hii, ninashukuru kwa majadiliano na Delores Mortimer mtaalamu mwandamizi anayeongoza mipango ya Kimataifa ya kubadilishana Elimu katika Shirika la Habari la Marekani (USIA) huko Washington D.C kwa sasa yuko likizoni huko Chuo Kikuu cha Michigan

nchi yangu na jinsia yangu". Sauti ya mamlaka makubwa kabisa katika Baraza Kuu kwa muda ilikuwa sauti ya mwanamke wa Kiafrika.

Elizabeth Bagaya wa Uganda (ambaye hapo awali alikuwa Binti wa Mfalme wa Toro) alikuwa balozi anayezunguka wa Idi Amini na baadaye waziri wa mambo ya nchi za nje katika miaka ya 1970. Lakini Binti wa Mfalme Elizabeth alikuwa huru mno kiasi cha kutoweza kuendelea katika nafasi kama hiyo chini ya serikali kama hiyo ya kijeshi inayobadilikabadilika. Kwa hakika, alikuwa huru mno kiasi cha kutoweza kuendelea kama balozi wa Uganda huko Marekani mwishoni mwishoni mwa miaka ya 1980 chini ya Rais Yoweri Museveni. Alikataa 'kuharakishwa' kuhamia Paris - na badala yake akaamua kujiuzulu. Hata hivyo, Elizabeth Bagaya Nyabongo, kwa muda, alikuwa moja ya sauti halisi za umajumui upanafrika kinchi na kijinsia.

Uganda imekuwa na wanawake wengine katika kazi mashuhuri za kidiplomasia kutoka Bonn (Balozi Bernadette Olowo) hadi Ottawa (Balozi Anna Amailuk). Mwishoni mwa miaka ya 1980 hawa walikuwa ni pamoja na Freda Blick kama Balozi Ufaransa. Pia huko Ufaransa, kama balozi wa Ghana, alikuwa Theresa Strictner - Scott. Kuiwakilisha Afrika ng'ambo kukuwa mfano wa upanafrika uliohamishiwa nje katika fahiwa hii ya kidiplomasia. Baadhi ya hawa wanawake mabalozi pia waliwakilisha nchi moja ya Kiafrika katika nchi nyingine ya Kiafrika. Kwa mfano, balozi Amailuk wakati fulani aliwakilisha Uganda huko Ghana.

Dhima ndogo za kidiplomasia zilizohusisha shughuli za kimaaifa usiokuwa rasmi pia ulianza kujitokeza kwa wanawake. Angie Brooks alikuwa rais wa Shirikisho la Kimataifa la Wanawake Wanasheria na alitunukiwa na serikali kadhaa za kigeni ikiwa ni pamoja na Brazili, Ujerumani, Yugoslavia, Cameroon na jamhuri ya Watu wa China.

Wanawake wa Kenya ambao wamewahi kufanya kazi za kidiplomasia kwa miaka ni pamoja na Margaret Kenyatta, Grace Ogot na wengine. Huduma za nchi za nje za Kenya zimewajumuisha pia maafisa na mabalozi wanawake wa ngazi za juu - mara nyingi wakiwa wanafanya kazi barani Afrika na nchini mwao.

Wakati wa uhuru wa Zambia mnamo 1964, mwanamke wa nchi hiyo aliyepata umaarufu mkubwa hakuwa balozi: alikuwa Alice Lenshina, nabii wa kike aliyeongoza Kanisa la Lumpa (tazama sura ya 17 ya juzuu hili). Alice kutoijali serikali ya Zambia na chama tawala kulizusha mgogoro mkubwa. Lakini upande wowote ule atakaopendelea mtu kuuchukua katika makabiliano baina ya Alice Lenshina na serikali mpya ya Zambia chini ya Kenneth Kaunda, tukio hili la Alice lilikuwa kiashirio kimojawapo kwamba Afrika ingeweza kuwatoa viongozi thabiti wa kike,

wenye uwezo wa kuwazindua wafuasi wao kufanya matendo makuu ya ujasiri na kujitolea.

Wanawake wengine nchini Zambia tangu wakati huo wamekuwa na majukumu madogo ya kidiplomasia muda hadi muda - ikiwa ni pamoja na Dkt. Mutumba Bull kama mwanasiasa na kama mwanazuoni. Wanawake kama hao wamefanya kazi nchini kwao na barani.

Wake wa viongozi fulani wa Afrika katika kipindi hiki walijitokeza sana kidiplomasia na kisiasa wenyewe. Katika miaka ya 1980, Sally Mugabe alijishughulisha katika masuala kadhaa ya kibinadamu na kimataifa, hasa suala maalumu la ustawi wa watoto wa Afrika kwa jumla. Bibi Mugabe aliingia katika ushirikiano wa kidiplomasia na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) - na akawa mwenyeji wa mikutano ya upanafrika huko Harare ya



*PICHA 30.2 Kushoto: Jehan al-Sadat wa Misri, mtetezi wa uendelezaji wa haki za wanawake; kulia: Winnie Mandela wa Afrika Kusini, kiongozi katika mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi, Johannesburg, Oktoba 1985*

kukuza mambo ya watoto wa Afrika. (Mfano wa karibu kabisa wa Marekani kwa Bibi Mugabe ni Bibi Eleanor Roosevelt katika kazi yake ya kidiplomasia na kibinadamu, kabla na baada ya kifo cha mumewe).

Mke mwingine wa rais ambaye alijishughulisha kidiplomasia kwa muda alikuwa Bibi Jehan Anwar al-Sadat wa Misri. Miongoni mwa wanaume wa Kiislam wasiotaka mabadiliko wa Mashariki ya Kati, msimamo na kujitokeza kwa Bibi al-Sadat mara nyingi kilikuwa hasara badala ya faida. Lakini kwa wanawake huko

Uarabuni, Bibi al-Sadat, kwa muda alikuwa mfano wa dhima. Alilazimishwa kuingia katika hali ya kusahaulika baada ya kuuawa kwa mumewe mnamo 1981.

Huko Kusini mwa Afrika kwa jumla katika kipindi hiki, upanafrika wa Waafrika umekuwa katika machafuko makubwa kabisa kisiasa na kimahusiano ya jinsia. Katika Jamhuri ya Afrika Kusini mwanamke maarufu wa taifa lolote katika miaka ya 1980 alikuwa Winnie Mandela. Ingawa hakuwa na wajibu wa moja kwa moja wa kidiplomasia wala ofisi rasmi ya kisiasa katika mapambano dhidi ya Ubaguzi, Winnie Mandela alikuwa mwanamke wa Kiafrika maarufu kabisa katika miaka ya 1980. Alijikuta katikati ya taratibu mbalimbali za kihistoria na za upanafrika katika sehemu yake ya bara. Haikuwa siasa ya utaifa pekee iliyomuathiri. Aliathiriwa pia siasa za jinsia na makundi ya rika.

Huko Kusini mwa Afrika kwa jumla, madaraja yalihitaji kujengwa si ya rangi tu bali pia baina ya jinsia na baina ya vizazi. Mahusiano baina ya wanaume na wanawake yalikuwa yamevurugwa na ukandamizaji, na vita vya ukombozi na uhamaji wa nguvukazi. Na mahusiano baina ya vijana wa Kiafrika na vizazi vikongwe yaliendelea kubinywa na hasira na fikra kali zilizochochewa na ubaguzi.

Katikati ya hizi seti tatu za mahusiano ya upanafrika jinsia, utaifa na kizazi - ulikuja mzozo wa Winnie Mandela mnamo mwishoni mwa miaka ya 1980. Kama mwanamke ambaye mume wake (Nelson Mandela) alikuwa amefungwa kwa zaidi ya robo ya karne, Winnie Mandela alikuwa ishara ya maumivu ya mapambano ya kisiasa juu ya mahusiano ya kijinsia. Kama mwanamke aliyejaribu kuwazatiti wanaharakati vijana kwa wajibu wa kijamii Winnie alikuwa mmoja wa wajenzi wa daraja la kuunganisha vizazi.

Lakini mnamo 1988 na 1989, mambo yalimharibikia vibaya Bibi Winnie Mandela - kiasi fulani kwa sababu ya shughuli za vijana hao wadogo aliojaribu kuwaongoza. Mwanamke aliyekuwa shahidi kwa ubaguzi tangu mumewe alipohukumiwa kifungo cha maisha mwaka 1964, mwanamke ambaye mwenyewe aliathirika na kupigwa marufuku na kuzuiwa kupita katika mtaa wa watu weusi maskini kwa muda mrefu, sasa alikuwa mtu wa kushutumiwa na kukejeliwa katika duru fulani ambazo zilimchukulia kama 'mama wa taifa.

Lakini hadhi yake hiyohiyo ilikuwa sehemu ya hadithi pana kuhusu mahusiano ya kijinsia Kusini mwa Afrika. Ukandamizaji na vita mara nyingi vimeacha 'wajane wa mapinduzi' - wajane wa mashahidi wa mapambano ya kuleta uhuru. Kumekuwepo pia 'wajane wa kizimba' - wake wa waume waliotupwa kizuizini maisha. Winnie Mandela alikuwa amekuwa mfano mkubwa kabisa kimataifa wa 'wajane wa kizimba'.

Nyuma ya yote haya kulikuwa na mielekeo muhimu ya kisosiolojia. Kwa vijana weusi wa Kusini mwa Afrika, ziliibuka aina mpya za kuwafunda watu kuwa mashujaa. Vijana wengi walikuwa wameingizwa katika majeshi ya ukombozi. Na huko mijini hali hii mpya ya upiganaji wakati mwingine ulichukua sura ya mkabiliano na vyombo vya usalama katika mitaa ya Soweto. Majaribio ya Winnie Mandela ya timu ya mpira ya vijana yenye majukumu ya ziada ya kumlinda yangeweza kuwa kifani kinachostahili kuigwa. Lakini likawa jaribio lililoshindwa. Timu yake ya mpira iligeuka kuwa genge linalopigana na vijana wengine. Vita vya magenge ya vijana vilipatana na ndoto za Winnie Mandela.

Afrika Kusini pia iliunda aina maalumu ya utofauti baina ya jinsia na tabaka. Katika jamii za wachimba madini wa Afrika Kusini wanaume hawakuruhusiwa kuishi na wake zao. Tulivyoonyesha ubaguzi wa jinsia uliongezwa kwenye ubaguzi wa rangi. Tumedokeza kwamba wanawake mara nyingi walibaki mashambani kama wakulima wadogo wadogo - wakati waume zao waliposafiri maili nyingi kutafuta vibarua. Matokeo yake kama tulivyoonyesha, yalikuwa ni kuunda mfanyakazi wa kiume mhamaji na mkulima wa kike mkazi. Kama mke aliyelengwa na mume wake na mfumo usiokuwa na haki, Winnie Mandela pia alikuwa mfano wa dhima kwa wanawake wakulima wa vijijini.

Katika mapambano ya kujenga madaraja kuvuka rangi, Afrika Kusini, kipindi hiki kiliwatoa washindi wa tuzo ya amani ya Nobel - Albert Luthuli na Desmond Tutu. Lakini hapakuwa na TUZO za Nobel katika mapambano ya kujenga madaraja baina ya jinsia au madaraja ya kuviunganisha vizazi. "Amani" kwa msingi wa Tuzo ya Nobel ilikuwa haijafafanuliwa kwa kipimo cha ama kuupiga vita ujinsi au kusuluhisha mgogoro baina ya vizazi. Winnie Mandela alikuwa mtu wa ubishani mkubwa mnamo miaka ya 1980 kuweza kuwa na nafasi ya kuwa mwanamke mweusi wa kwanza kushinda Tuzo ya Nobel hata kama juhudi zake za kuunganisha jinsia na vilevile vizazi zingefaulu. Hata hivyo, kwa kuwa kazi ya kisiasa ya Bibi Mandela ilikuwa bado sana kufikia mwisho wake, makisio ya mwisho ya mchango wake katika umajumui wa Waafrika ungeweza tu kukokotolewa na historia yenyewe muda ukamilikapo.

Vilevile muda utafichua mambo yote iwapo Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika mwanamke atapatikana **kabla** au **baada** ya rais kwa kwanza mwanamke wa nchi ya Kiafrika.[9]

[9] Tazama A.A. Mazrui, 1990

## Elimu ya Kikoloni: inakomboa lakini si ya maendeleo.

Jambo litakalolikumba Afrika mapema katika mapinduzi ya jinsia ni zamu ya pili kuu ambayo tumeirejea - marekebisho ya jumla zaidi ya kiwango cha Afrika cha utaalamu. Ingawa bara hili inawezekana linasubiri mapinduzi ya jinsia na ya kisayansi, matarajio kuhusu haya ya baadaye yanaweza yakawa ya karibu zaidi kuliko ya kwanza.

Jambo kuu la kutilia maanani ni kwamba stadi zilizokuja Afrika wakati wa utawala wa kikoloni zilitokea kuwa na utata mmoja mkubwa wa kihistoria. Stadi hizi zilitokea kuwa za manufaa kwa ukombozi lakini zisizofaa kabisa kwa maendeleo. Stadi zilizoingizwa na wakoloni zilikuwa zaidi zile za mawasiliano - na utaalamu katika aina hizi mpya za mawasiliano ya maandishi na ya mdomo zilisaidia harakati za kuuondoa ukoloni. Kitu ambacho ukoloni ulishindwa kukihamisha kwa dhati ni stadi za uzalishaji. Ni katika fahiwa hii ndio urithi wa kikoloni wa elimu na mafunzo ulishindwa kukuza maendeleo halisi katika 'nchi' za Afrika, kama tulivyoonyesha katika sura husika.

Athari ya Kudorora kwa Uchumi wa Dunia na Vita vikuu vya Pili vya Dunia kwa Ulaya ilisaidia kama tulivyokwishaonyesha, kufanya ubepari kuwajibika zaidi na kisha kufanya ubeberu nao kuwajibika. Ilikuwa hasa baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia ndipo mataifa makubwa yalipoanza kutilia maanani elimu na mafunzo ya kikoloni barani Afrika. Stadi mpya za mawasiliano zilikuwa zinaundwa. Ilikuwa mnamo 1948 ndipo Chuo Kikuu Kishiriki cha Gold Coast kilipoanzishwa - na Ibadan ilifungua milango yake kwa wanafunzi wake kikiwa Chuo Kikuu Kishiriki. Mnamo mwezi Februari mwaka uliofuata (1949), Chuo Kikuu cha Lovanium kilianzishwa kwa amri huko Kongo ya Wabelgiji, ingawaje ilikuwa hadi 1954 ndipo Waafrika 30 wa kwanza walipoingizwa katika kozi za matayarisho ya kujiunga na Chuo Kikuu, ambao miongoni mwao ni 10 tu ndio waliotangazwa kuwa wamefaulu.

Huko Uganda, Makerere ilifanywa Chuo Kikuu Kishiriki- mwishoni mwa 1949. Ama kuhusu asasi za utafiti zilizokuwa zinaibuka, hizi zilikuwa ni pamoja na Taasisi ya Taaluma ya Magonjwa ya Macho ya Tropiki iliyojengwa huko Bamako, Sudani ya Wafaransa mnamo 1953 na Taasisi ya ORANO (*Organisation pour la recherche sur l'alimentation et la nutrition en Afrique*), ilianzishwa huko Dakar. Mashirika ya utafiti ya aina hii yalikuwa na taathira za kimaendeleo na hayakuwa yamekitwa tu kwenye stadi za mawasiliano tu. Lakini mafunzo ya lishe na magonjwa ya macho si sawa na mafunzo ya mbinu za uzalishaji. Kwa vyovyote vile, asasi hizi za utafiti zilikuwa sehemu ndogo tu ya msukumo wa elimu ya kikoloni. Msukumo mkuu ulikuwa bado umeelekezwa kwenye stadi za kuandika na kusema.


Baadhi ya hizo mbinu za mawasiliano zilitumiwa na wazalendo wa Kiafrika katika makao makuu ya utawala, na hata kuwasiliana na jumuiya ya kimataifa kwa jumla. Kama ilivyoonyeshwa katika sura zilizopita, dhana ya Unegro ilizaliwa miongoni mwa wazalendo weusi huko Ufaransa - hasa Aime Cesaire na Leopold Senghor. Harakati za unegro zilianza mwanzoni mwa kipindi kilichojadiliwa na juzuu hili. Harakati za karibu kabisa na unegro katika nchi zilizotawaliwa na Waingereza kama uthibitisho wa utamaduni katika kipindi hiki cha mapema, zilikuwa, kama ilivyoonyeshwa awali, kitabu cha Jomo Kenyatta cha *Facing Mount Kenya* (Kuelekea Mlima Kenya), ambacho pia kilikuwa tangazo la uthibitisho wa utamaduni, na kilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1938. Unegro na kuuelekea Mlima Kenya vilikuwa vipengele muhimu vya stadi mpya za mawasiliano za Afrika - zikiwa zimelengwa kwa wakoloni na kwa dunia kwa jumla. Katika hali kama hii, stadi hizi zilikuwa zikitumiwa kama sehemu ya harakati za ukombozi. Mnamo 1947, Aliuone Diop alianzisha *Presence africaine* huko Paris - silaha nyingine ya mawasiliano katika mapambano ya uthibitisho wa Afrika.

Baada ya kufikiria yote, hizi stadi zilizotolewa na wakoloni za maandishi na kuzungumza kwa lugha ya Ulaya, kwa hakika, zilisaidia vizuri mikakati ya ukombozi. Haikuwa bahati mbaya kuwa harakati dhidi ya ukoloni ziliongozwa kwa namna isiyolingana na wazalendo wa Kiafrika walioathiriwa kikamilifu au kwa kiasi fulani na mambo ya nchi za magharibi. Waasisi wa mataifa mapya ya Kiafrika; kwa kiasi kikubwa, walikuwa matokeo ama ya shule za misionari Afrika au vyuo vya nchi za magharibi huko ng'ambo - au; mara nyingi vyote kwa pamoja. Hawa walikuwa ni pamoja na marais waasisi wa Ghana (Nkrumah), Senegal (Senghor), Tanzania (Nyerere), Malawi (Banda), Kenya (Kenyatta) na wengine wengi. Ushahidi ni mwingi mno kwamba ingawa wazalendo wa Kiafrika waliothiriwa na nchi za Magharibi walikuwa ni wachache tu katika jumla ya watu wote wa bara, walikuwa viongozi wa mapambano ya uhuru wa kisiasa. Kama tulivyoonyesha katika sura za siasa za juzuu hili, hawa Waafrika waliopata elimu katika nchi za Magharibi baadaye waliwapiku watawala wa jadi - na kurithi mamlaka kutoka kwa wakoloni waliokuwa wakiondoka. Ni katika fahiwa hii ndipo stadi za mawasiliano zilizohamishiwa Afrika katika kipindi cha ukoloni ziliposaidia harakati za uhuru wa kisiasa Afrika.

Vitu ambavyo wakoloni hawakuvihamisha vilikuwa stadi halisi za uzalishaji. Kwa kiwango hicho elimu ya kikoloni - ingawa ni ya thamani kubwa katika awamu ya ukombozi wa Afrika - haijalingana katika kazi ya kuendeleza Afrika. Mbinu za kilimo katika Afrika zinaendelea kuwa za hali ya chini kwa kiasi kikubwa, viwanda

inabidi viagize karibu kila kitu, mabwawa mara nyingi hayawezi kutengenezeka, vifaa vinafikia hatua ya kutofanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa vipuri. Uwezo wa viwanda vya Afrika kutumia madini yake ni ya kusikitisha. Hata uwezo wetu wa kuchimba madini haya bila vyombo, utaalamu na mipangilio ya kigeni, ni mdogo sana. Bara bado linazalisha kutoka katika migodi yake, vile ambavyo haliwezi kutumia na kuagiza kwa ajili ya matumizi vitu ambavyo haliwezi kuzalisha.

Hitimisho ni lazima lifikiwe. Wakati utawala wa kikoloni uliwaandaa wachimba kaburi wake kwa kuelimisha tabaka la juu la kisiasa, ukoloni haukuweza kuwaandaa



PICHA 30.3 Mtambo wa nyuklia wa Triga, Zaire 1965.

viongozi wa kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya Afrika. Wito wa kujikomboa kwa Afrika ulisaidiwa sana na elimu ya kikoloni; lakini wito wa maendeleo ya Afrika hauwezi kutimizwa kwa njia ya urithi wa kikoloni peke yake. Stadi za mawasiliano lazima sasa ziunganishwe na stadi za uzalishaji na maendeleo.

## Kuhusu Utawala na Maendeleo

Afrika iliingia katika enzi mpya ya uhuru ikiwa na pengo kubwa la stadi kuliko pengo la uzalishaji, tofauti kubwa kati ya asasi zake mpya za baada ya ukoloni na uwezo wa kuzidhibiti kwa uthabiti.

Kwanza kulikuwa na ubepari wenye upogo ambao nchi nyingi za Kiafrika ziliurithi kutoka enzi za ukoloni. Bara lilipokea ruwaza ya matumizi ya nchi za Magharibi bila mbinu za Magharibi za Uzalishaji, vionjo vya Magharibi bila utendaji wa Magharibi, ujenzi wa miji bila ujenzi wa viwanda, uroho wa kibepari bila nidhamu ya kibepari. Tukimkariri mshairi wa Magharibi (Alexander Pape):

> Ubepari mdogo ni kitu cha hatari;
>
> Kunywa sana, au usionje chemchemi ya Magharibi.

Afrika haikunywa kutoka katika chemchemi ya ubepari kwa wingi jinsi zilivyofanya nchi za Asia Kusini-Mashariki, wala Afrika haikuruhusiwa kuonja ladha ya ubepari kabisa. Matokeo katika Afrika yakawa msiba wa uroho bila upatanisho wa ufanisi.

Kisha kulikuwa na asasi za kisiasa ambazo Afrika baada ya ukoloni ilizirithi. Miundo ya asili ya utawala ya Afrika ama ilipigwa marufuku au kudhoofishwa na watawala wa kikoloni. Na wazo la jeshi la Kiafrika lilizinduliwa kwa silaha zilizotengenezwa, kwa teknolojia iliyoendelea kuliko kiwango kilichokwishafikiwa mahali penyewe. Afrika iliibuka katika uhuru ikiwa na stadi za uharibifu zilizo kubwa kuliko stadi zake za uzalishaji. Hata hivyo, seti hizi zote za stadi bado zilikuwa zikitegemea sana mifano ya nje na wasambazaji kutoka nchi za nje. Hii ilivuruga mahusiano ya raia na majeshi katika Afrika, na urithi mzima wa mapinduzi na upinga mapinduzi. Kwa sababu ya pengo la stadi, uundaji wa majeshi barani Afrika haujasaidia kujengwa kwa viwanda uraiani. Hakujawa na uhusiano wa kutegemeana baina ya ulinzi na maendeleo. Ukiacha kando Misri na Jamhuri ya Afrika Kusini, hakuna kabisa nchi nyingine ya Kiafrika yenye «kiwanda cha vifaa vya kijeshi». Majeshi mengi ya Kiafrika hayaagizi kila kifaru na kila roketi tu; bali pia yanaagiza kila bunduki, kila risasi; wakati mwingine hata sare za majeshi ya Afrika zinaagizwa kutoka nje.

Uundaji wa majeshi bila ujenzi wa viwanda umeyumbisha mifumo ya kisiasa na kiuchumi. Ndoa kati ya siasa na majeshi imekuwa tatizo moja; talaka baina ya ulinzi na maendeleo imekuwa tatizo jingine. Kuna pengo linaloharibu stadi katika maeneo yote haya - siasa, uchumi na kutoendelea kiteknolojia.

Miongoni mwa majeruhi ya hali hii ni haki za binadamu katika Afrika. Kushindwa kwa asasi huria za nchi za Magharibi katika sehemu kubwa ya Afrika sio kumetokana na ugeni wake tu, bali pia na uwezo hafifu wa Afrika kuongoza ama vyama vya kisiasa vyenye nidhamu au mamlaka ya pamoja yenye ufanisi au vyama thabiti vya wafanyakazi. Hata hivyo, demokrasia ya nchi za Magharibi ililazimishwa huko Ujapani na vilevile huko Afrika. Wamarekani waliilazimisha Japan kwa kipindi

kisichozidi mwongo mmoja; Afrika ilikuwa na muda mrefu wa kulelewa na Ukoloni. Na bado asasi za Kimagharibi zilishamiri katika ardhi ngeni ya Japan, lakini zimedumu kwa tabu katika ardhi ngeni ya Afrika. Pengo la stadi katika usimamizi linaweza likawa sehemu ya maelezo, na vilevile, msingi wa ubepari hafifu barani Afrika ikilinganishwa na sababu zifuatazo zinazohusiana:

(1) Serikali ina ukubwa gani

(2) Kiasi kinachofanywa na serikali (DHIMA)
(3) Ni kwa kiasi gani serikali inafanya vizuri (UTHABITI)
(4) Uwakilishi na mgawano sawa wa serikali (UHALALI)

Suala la kwanza la "ukubwa" limejumuisha wingi sio tu wa watumishi wa serikali bali pia wa mashirika ya serikali. Suala la pili la dhima limehusu dhima ya dola katika uchumi na hali ya kazi za serikali. Suala la tatu limehusu umilisi, uthabiti na kiwango cha uzalendo katika tabia ya serikali. Kipengele cha nne kinahusu demokrasia na uwakilishaji au kutokuwepo kwa mambo haya mawili.

Ni muhimu kukumbuka kwamba, barani Afrika, uwakilishi katika enzi baada ya ukoloni mara nyingi unapimwa kikabila badala ya kiuchaguzi. Hesabu za kikabila mara nyingi zinasaidia kuyahakikishia makundi tofauti kuwa ni sehemu ya chombo kweli au la na ni miongoni mwa wanufaikaji au la. Serikali inachukuliwa kuwa na uwakilishi mzuri au usioridhisha kwa kiasi ambacho kinaonyesha ujumuisho wa makabila katika jamii pana. Huko Nigeria kanuni hii ya uwakilishi kwa kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe mara nyingi vinarejewa kama "sifa za shirikisho" la taifa.

Nguvu ya uwakilishi na kikabila imekuwa na uwezo wa kupanua asasi za kiserikali na za kirasimu. Watumishi wa Serikali na Mashirika ya Umma mara nyingi "yamefirishwa, kama hatua ya kuleta uwiano katika hesabu za ukabila.

Kwa upande mwingine, kushindwa kuhisi haja ya kuwa na uwiano wa kikabila katika Afrika baada ya ukoloni wakati mwingine kunaweza kuleta mvurugano. Kutokuwepo kwa uwakilishi wa kikabila katika nchi kama Nigeria au Uganda mara nyingi kumekuwa jambo la hatari kubwa kisiasa kuliko kukosa uwakilishi wa kiuchaguzi katika sanduku la kura. Hesabu ya ukabila mara nyingi imekuwa kitu cha lazima kuliko kura katika fahiwa ya uhuria.

Ama kuhusu kigezo cha utendaji wa serikali, mtanziko mmoja mkuu katika Afrika baada ya ukoloni unahusu uhusiano baina ya ulegezaji masharti ya kiuchumi na ulegezaji masharti ya kisiasa. Kuna nchi fulani barani Afrika ambako uwingi wa kisiasa umekuwa na mwelekeo wa kuleta mvurugano kiuchumi. Nigeria chini

ya Shehu Shagari (1979-83) ilikuwa wazi na ya ushindani kisiasa, lakini kiuchumi, nchi ilikuwa vurugu tupu. Ghana chini ya Limann na Sudan chini ya Sadiq al-Mahdi pia zilikuwa wazi kisiasa lakini jamii ziliteketea kiuchumi. (Kusini mwa Sudani haikuwa huru kisiasa wala kuwa na ulinzi kiuchumi. Ilikuwa imeteketea kisiasa na kiuchumi).

Katika nchi kama hizi za Afrika kumekuwa na mtanziko halisi na wa uadili. Uwingi wa kisiasa umekuwa katika hatari kubwa ya kuwa uozo wa kiuchumi. Hatimaye, mara nyingine imekuwa chaguo gumu sana baina ya ama uhuru wa kisiasa au maendeleo ya kiuchumi - lakini si yote pamoja. Katika hali kama hiyo ni nini jukumu la wahisani na asasi za kimataifa? Je kumekuwa na hatari kwamba asasi kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa zingependelea serikali za kijeshi kama zile za Ibrahim Babangida na Jerry Rawlings badala ya zile zilizochaguliwa kwa kura kama vile serikali za Shaghari, Limann na al-Mahdi?

Je kuna hatari katika miaka ya 1990 kwamba vyombo vya nje vinaweza kuhimiza ulegezaji wa masharti ya kiuchumi wakati wakipinga ulegezaji wa masharti ya kisiasa? Je hii ya nyuma ungehimiza kuibuka kwa serikali za kijeshi wakati mwingine hata bila kukusudia?

Ama kuhusu dhima ya ubadhirifu katika utawala baada ya uhuru, hii mara nyingine imechukua sura ya kubinafsishwa kwa dola. Ubinafsishaji wa ukabila umekwishatokea wakati uwakilishi wa kikabila ulipoachwa - na mojawapo ya makabila kuhodhi au kudhibiti dola. Wanubi katika Uganda ya Idi Amin walikuwa mfano wa kinachoelezwa hapa.

Ubinafsishaji wa Kinasaba ulitokea wakati rasilimali na alama za dola ziliposhikiliwa na mtu mmoja na wanafamilia wa karibu zaidi. Bokassa katika Himaya ya Afrika ya Kati alijaribu kwa dhati kuunda nasaba ya kifalme.

Ubinafsishaji wa vurugu umetokea wakati mali na mamlaka ya dola yanatapanywa katika kinyang'anyiro huria kwa wote kwa ajili ya faida. Nigeria chini ya Shehu Shagari ilikuwa mfano wa ubinafsishaji wa vurugu hasa kutoka 1981 na kuendelea.

Katika uwanja wa siasa, maovu makubwa kabisa ya Afrika tangu uhuru ni hatari ya udhalimu kwa upande mmoja na hatari ya vurugu upande mwingine. Udhalimu ni serikali kujitanua kupita kiasi, vurugu ni serikali kuwa na nguvu kidogo. Mielekeo ya udhalimu mara nyingi ni kung'angania ama jefule. Mwelekeo wa vurugu kimsingi ni kugawanya jefule - mara nyingi jirani dhidi ya jirani.

Katika uwanja wa uchumi, maovu makubwa ya Afrika ni hatari ya kuwa na utegemezi wa kiuchumi kwa upande mmoja na hatari ya kuanguka kwa uchumi

kwa upande mwingine. Utegemezi ni ufupisho wa uwezo wa kujitegemea. Uozo ni ufupisho wa uwezo wa maendeleo.


Mgogoro wa utawala katika Afrika unahusu uhusiano kati ya maovu ya kisiasa ya udhalimu na vurugu kwa upande mmoja na maovu ya kiuchumi ya utegemezi na uozo kwa upande mwingine. Je, dawa kwa yote haya ni nini? Miongoni mwa stadi muhimu kabisa ambazo zinahitaji kuendelezwa kutoka miaka ya 1990 na kuendelea ni zile ambazo zitaushughulikia vizuri zaidi mgogoro mkuu wa utawala.

Waafrika si lazima waige asasi huria za nchi za Magharibi ili kuleta utulivu na usawa. Lakini watu wa bara hili wanahitaji kuendeleza stadi za kutosha na kujizatiti kupigania na kutetea haki zao hata dhidi ya serikali zao. Watawala kila mahali wana mwelekeo wa kuwa vigeugeu isipokuwa kunapokuwa vyombo vya kudhibiti matendo yao mabaya. Pengo la stadi katika Afrika ni sehemu kamili ya ukiukwaji uliokithiri wa haki za binadamu barani. Jeshi la Yoweri Museveni huko Uganda katika miaka ya 1980 lilikuwa jaribio la kwanza la serikali ya Kiafrika ambayo haikuwa ya kidemokrasia. Lakini matatizo yalibakia makubwa. Utulivu na usawa bado viko mashakani.

## Kuhusu idadi ya watu na mazingira.

Matatizo ya Afrika katika miongo ijayo yataenea kuvuka haja ya utulivu wa kisiasa na chumi zinazojitosheleza. *Ikolojia* yenyewe ya Afrika iko hatarini; ukataji wa misitu na kuongezeka kwa jangwa vinaacha sehemu nyingi za Afrika katika ukiwa. Sehemu ya tatizo ni uwezo duni wa upangaji mipango katika bara zima kwa jumla. Ingawa serikali nyingi za Afrika zinapendelea mipango ya maendeleo ya kitaifa, idadi kubwa ya mipango hiyo inaheshimiwa zaidi kwa kuvurugwa kuliko kwa kungatiwa. Misitu inamalizwa bila kuwapo juhudi za kutosha za kupanda miti. Misitu ya kitropiki ya Cote d'Ivoire imeharibiwa kabisa na makampuni ya Kifaransa na Kilebanoni yakishirikiana na utawala wa nchi. Kumefanyika juhudi ndogo sana kuhusu uharibifu wa mazingira au haja ya upandaji miti kufidia uharibifu. Senegal - baada ya uharibifu mkubwa wa mazingira - imeanzisha jaribio la kupanda miti mipya. Stadi za upangaji mipango bado ziko nyuma ya ulinzi wa ikolojia.

Pengo la stadi linahusu pia matumizi ya kuni kama aina ya nishati iliyoenea sana katika maeneo ya vijijini Afrika. Kuni pia ni aina ya kale kabisa ya nishati ya nyumbani. Lakini vijiji barani Afrika lazima vijifunze jinsi ya kutumia nishati hii kiuchumi. Mabadiliko madogo katika mbinu za kupika na katika uthabiti wa kutumia moto yanaweza kupunguza sana matumizi ya kuni. Na hii kwa upande wake



PICHA 30.4 Kuenea kwa jangwa katika Sahel



PICHA 30.5 Uharibifu wa misitu Afrika

ingeweza kupunguza au hata kukomesha kasi ya ukataji misitu na ueneaji wa jangwa katika sehemu za bara.

Kisha kuna tatizo la kuhusisha mifugo na maeneo ya kuchungia yaliyopo katika jamii ambamo ng'ombe, mbuzi au ngamia ni amali kubwa za kiutamaduni. Serikali zimepata tabu kuwashawishi wafugaji kwamba idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi au ngamia ina athari kubwa ya kuharibu ikolojia na kuathiri upatikanaji wa nyasi katika siku *zijazo. Ng'ombe wa ziada na nakisi ya stadi* mara nyingi ni muunganiko wa hatari.

Je vipi ile dhana ya uadilifu wa wasiwasi kuhusu "ziada ya *watu*" katika bara lenye nakisi ya stadi? Uwezo mdogo wa upangaji mipango pia umeathiri suala la kuongezeka idadi ya watu katika bara hili. Je Afrika inazalisha watu wengi zaidi ya uwezo wake wa kuwalisha? Ingawa miaka ya 1980 ilitoa ishara tofauti kuhusu uhusiano baina uzalishaji wa chakula na uongezekaji wa idadi ya watu barani Afrika, hatari ya uzalishaji wa chakula kidogo kwa kila kichwa ilikuwepo bado. Suluhisho kwanza lilikuwa kuboresha kiwango cha uzalishaji wa chakula; jingine lilikuwa, kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Masahihisho yoete mawili yalihitaji stadi.

Kuhusu uzalishaji wa chakula, sura zinazohusika katika kitabu hiki zimeshughulikia suala hilo. Je, vipi kuhusu ukuaji wa idadi ya watu?

Kufikia miaka ya 1980 kulikuwa na watoto wachanga wengi waliozaliwa Afrika kuliko kwingine kote duniani. Kasi ya ongezeko la idadi ya watu katika Afrika ya weusi ilikuwa ya juu kabisa katika historia ya binadamu - na bado ilikuwa ikipamba

moto (Jedwali 30.1). Kasi ya ukuaji ilikuwa asilimia 2.5 kwa mwaka mnamo 1960 - 70, asilimia 2.7 mnamo 1970 - 80, asilimia 3.1 mnamo 1980 - 86, na kufikia 1989 ilikadiriwa kuwa asilimia 3.2. Nchi kama Kenya ilivuka kiwango cha ukuaji cha asilimia 4 kwa mwaka.

Upendo wa Afrika kwa watoto ulikuwa utukufu wake na vilevile tanzia yake. Katika miaka ya 1980, utafiti ulionyesha kwamba familia za Kiafrika zilitamani kuwa kubwa zaidi ya jinsi zilivyokuwa. Kwa wastani mwanamke wa Kiafrika alitaka watoto sita au zaidi. Mnamo 1988, mwanamke wa Kenya aliwania kuwa mama wa watoto wanane. Ukubwa uliopendelewa wa familia katika Afrika kwa jumla ulikuwa wa watoto watano huko Ghana na tisa huko Mauritania.
Sababu moja kubwa ya kuwapenda watoto ilikuwa ni dhana ya Afrika ya *kutokufa*. Kutokufa Afrika hakukuwa tu suala la kwenda mbinguni. Kulikuwa pia ni kuacha damu inayoendelea kutitirika kwenye mishipa ya walio hai. Kwa misingi ya kisasa, hakuna aliyechukuliwa kuwa amekufa wakati jeni zake zilikuwa bado ni sehemu ya walio hai. William Wordsworth[10] alikuwa akiisogelea falsafa ya Afrika aliposema:

Oh Shangwe! Kuwa katika majivu yetu
Kuna kitu kinachoishi;
Ambacho Ulimwengu bado hukikumbuka
Kilichokuwa kikipita.

Kwa sababu ya kiwango kikubwa cha vifo vya watoto, wazazi wa Kiafrika katika miaka ya 1980 walikuwa na watoto sita ili kuwa na hakika kuwa walau watabaki na wanne. Kuweka nafasi kwa ajili ya vifo vya watoto kwenyewe kulikuwa aina ya mpango wa uzazi. Katika vijiji vingi vya Afrika kifo kilikuwa mgeni maarufu kuliko daktari.

Kwa hiyo, Afrika ilichohitaji zaidi haikuwa kuzuia uzazi, bali *kuzuia vifo* - si jinsi ya kuwa na watoto wachache, bali jinsi ya kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya watoto wanaishi. Kwa kawaida, kuzuia vifo; mara ya kwanza kunaongeza ukuaji wa idadi ya watu. Lakini baada ya muda kunapaswa kuwapa wazazi hakika ya kutosha kuwafanya wajaribu kuwa na watoto wachache. Hata hivyo, hadi kufikia miaka ya 1980, mpito huu wa idadi ya watu ulikuwa haujatokea Afrika.

Watoto barani Afrika wameathriwa na migogoro ya aina tatu. Kwanza kulikuwa na mgogoro baina ya watu (hasa mikabiliano ya rangi na kikabila). Pili, kulikuwa na mgogoro baina ya ukuaji wa idadi ya watu na mazingira (aina ya vita vya kiikolojia). Na, tatu kulikuwa na mapambano dhidi ya umaskini na ujinga (kampeni

[10] W. Wordsworth Ode on Intimations of immortality

kwa ajili ya kuwainua watu kijamii na kwa ajili ya walau kutosheleza mahitaji ya msingi ya binadamu).

Mikabiliano ya rangi na kikabila katika vita vya wenyewe kwa wenyewe na vita vya ukombozi inazaa *watoto wa vita* - mara nyingi hawana mmoja wa wazazi, mara nyingi hawaishi vijijini kwao. Watoto katika makambi ya wakimbizi ni mfano thabiti wa ukiwa huu.

Mapambano dhidi ya ukuaji wa idadi ya watoto na vipengele vya asili yalikuwa ni miadi ya mwanzo zaidi. Wakati mwingine nguvu za asili ziliiandama Afrika kwa ukatili - ukame mwaka huu, mafuriko mwaka unaofuata, vyote vikileta uharibifu mkubwa. Wazazi na watoto walikumbwa katika misukosuko hiyo ya mazingira.

Mapambano ya tatu ya watoto wa Afrika yalikuwa dhidi ya umaskini na ujinga. Wakati mwingine mchanganyiko wa kawaida wa kuwaongezea maji watoto, au kurejesha chumvi mwilini, unaweza kuokoa maisha ya mamilioni ya watu Afrika. Kampeni za chanjo zile zinazofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika miaka ya 1980 zilizuia vifo katika baadhi ya vijiji. Mafunzo kuhusu lishe pia yaliokoa maisha.

Aina hizi tatu za migogoro mara nyingi zilifungamana. Kupiga vita ujinga kuhusu mmomonyoko wa ardhi, kimsingi, ilikuwa ni mapambano kuhifadhi ardhi na kulinda mazingira. Migongano ya rangi na kikabila ilikuwa na athari kwa umaskini kwa upande mmoja, na ikolojia, kwa upande mwingine.

Je, ni nini ilikuwa dhima ya Waafrika wenye stadi katika mapambano haya yote? Je, ni nini ilikuwa dhima ya wasanii, waelimishaji, na wasomi? Dhima yao ilikuwa kuelimisha na vilevile kuhamasisha. Walikuwa na wajibu wa kuelimisha umma na wafanya maamuzi. Walikuwa pia na dhima ya kuchochea ufungano na hamu ya sera ambazo zingewalinda watoto katika aina zote za hali ya dhiki na migogoro.

Lakini mhamasishaji alihitaji kuhamasishwa kwanza - mwelimishaji alihitaji kuelimishwa kwanza. Wasanii, walimu na wasomi walihitaji kuonyeshwa matatizo ya watoto wa vita, matatizo ya maangamizi ya mazingira na ya kupokwa kijamii, kuliko ilivyowahi kuwa kawaida yao.

Kutoka miaka ya katikati ya 1980, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) lilianza kuwajumuisha wasanii, wasomi na Waafrika wengine wenye stadi katika harakati za kuokoa watoto wa Afrika.

Lakini je, Afrika ilikuwa inawezaje kuhakikisha kushuka kwa idadi ya vifo vya watoto? Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNCEF) lilionyesha kwamba baadhi ya mbinu zilihitaji stadi za kawaida sana. Hata hivyo, stadi hizo za

kawaida zilikuwa hazijatumiwa. Mamilioni ya watoto wachanga katika Afrika ya wakati na baada ya ukoloni walikufa kwa ugonjwa wa kuhara. Mbinu rahisi za kurudisha maji mwilini na kuongeza chumvi zingeweza kuokoa wengi wa watoto hao. Watu wa nje wenye ujuzi wameanza kuwapa pakiti ndogondogo za "chumvi-na-maji" akina mama katika vijiji barani Afrika. Maji mazuri ya kunywa ni sharti jingine muhimu kuhusiana na hili, na serikali za Kiafrika na mashirika ya kimataifa yafikirie kushughulikia suala hili.

Zaidi ya hayo, chanjo dhidi ya magonjwa mengine yanayowaua watoto barani Afrika ingeweza kuleta tofauti kubwa kwa maisha. Magonjwa ya hatari kwa watoto kama dondakoo, kifaduro, surua na kuharisha damu yangeweza kuzuiwa kwa haraka kwa kutoa chanjo kwa watoto wengi. Nchi kama Burkina Faso imeanzisha mipango kama hiyo.

Lakini katika kipindi kilichoshughulikiwa na juzuu hili kulikuwa na ugonjwa mmoja ambao pengo la stadi liliathiri nchi za Magharibi na Afrika kwa namna moja. Ugonjwa ambao watu wa Magharibi waliuita UKIMWI pengine ulikuwa ugonjwa mkubwa kushambulia binadamu katika kipindi hiki cha historia ya ulimwengu.

Ugonjwa huu unaoshinda mengine yote umejitokeza katika robo ya mwisho ya karne ya ishirini, hasa kutoka miaka ya 1980 na kuendelea. Kwanza ulishinda kanuni zote za mapambano ya kitabaka na ya mgawano wa mali ya kimataifa. Wengi wa waliokumbwa na ugonjwa huu mwanzo walikuwa ama Wamarekani katika miji maarufu kama New York na San Francisco au Waafrika katika baadhi sekta maskini kabisa za bara. Pengo la ujuzi lilikuwepo huko Magharibi na Afrika.

Kwa mara mara moja katika kipindi hiki cha kihistoria Magharibi ilikosa kujua tiba kama Afrika. Matajiri na maskini waliteseka kwa namna sawa. Watu wa nchi za Magharibi na Waafrika wote walipigwa bumbuazi kitabibu.

Lakini hebu tusiruhusu muda huu mfupi wa wote kukosa ujuzi kuficha umbali baina ya wale walio juu na wale wa chini kabisa. Suala la stadi ni la msingi si tu kwa ufanyaji maamuzi ndani ya kila nchi ya Kiafrika. Kama ilivyoonyeshwa mapema, ni jambo la msingi kwa watu wa Kaskazini na Kusini, kwa mgawanyo wa dunia katika nchi zilizoendelea na zile zisizoendelea. Hatimaye huu ni mzigo wa kipindi hiki cha historia ya binadamu.

## Hitimisho

Miaka iliyojadiliwa katika juzuu hili (1935 hadi leo) ni ya kipindi kikuu kinachounganisha enzi za ukoloni na enzi mpya ya uhuru. Tumegawanya muda

huu mfupi wa historia ya Afrika katika, kwanza, mwongo wa mgogoro wa dunia (1935 - 1945); pili, mwongo na nusu wa mapambano dhidi ya ukoloni (1945 - 60) na, tatu, mawio ya uhuru yanayong'ara lakini ya mashaka na hamu yake ya maendeleo, hasa kuanzia 1960 na kuendelea. Matatizo yameongezeka.

Lakini wanahistoria wanakabili changamoto yao kuu pale wanapotafiti si vipindi vilivyopita tu bali pia matumizi ya maarifa yao kujaribu na kuelewa wakati wa sasa na kubainisha mielekeo inayowezekana kwa siku zijazo. Kipindi kilichoshughulikiwa katika juzuu hili kinatokea pamoja na mapinduzi makubwa kabisa ya kiteknolojia katika historia ya binadamu - kutoka ugunduzi wa anga hadi athari ya kompyuta kwa dunia. Wakati Afrika imekuwa ikielekea kwenye uhuru, wengine wametembea mwezini.

Tumeeleza katika juzuu hili (na katika yale yaliyotangulia) ushiriki wa Afrika katika historia ya sayansi. Lakini ukoloni ulivuruga badala ya kuwezesha, mapinduzi ya kiteknolojia ya Afrika. Kama Walter Rodney anavyoiweka, Ulaya *iliididimiza Afrika*[11]. Stadi ambazo Ulaya ilizihamishia Afrika za maandishi na mazungumzo ni stadi za mawasiliano zaidi badala ya zile za uzalishaji na maendeleo.

Lakini Afrika iliweza kuzitumia vizuri stadi chache. Tumeonyesha jinsi tabaka la waliosomeshwa Magharibi lilivyotumia mbinu mpya kuhamasisha umma nchini mwao na kugawa maoni katika nchi iliyokuwa ikitawala, na kuvuta jumuia pana ya kimataifa upande wa Afrika. Mapambano yanaendelea kuboresha utawala, kulinda mazingira, kufanikisha maendeleo na kuwalinda watoto wa Afrika. Lakini matatizo mengi yameendelea kuwepo.

Mabadiliko mawili hasa yanahitajika ikiwa hali ngumu ya Afrika itabidi kubadilishwa kimsingi-mabadiliko ya kijamii katika mahusiano baina ya wanaume na wanawake na mabadiliko ya kimuundo ya mahusiano baina ya watu na mazingira. Mahusiano ya kijinsia ni misingi mikongwe ya jadi. Sayansi ndio msingi mpya kabisa wa usasa.

Afrika inabidi ipate makutano baina ya mambo mawili - baina ya mapinduzi katika mahusiano ya binadamu (wanaume na wanawake) na mapinduzi katika utendaji wa mwanadamu (stadi na thamani). Kipindi hiki hasa cha historia ya Afrika tangu 1935 kinaweza kikawa cha maandalizi kwa ajili ya mabadiliko haya mawili ya Afrika.

[11] W. Rodney

JEDWALI 30.1 Afrika: jumla ya idadi ya watu na kiwango cha ongezeko kwa mwaka 1950 - 2025 utofautiano wa kati

| Idadi ya watu maelfu | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1985 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | |
| AFRIKA | 221984 | 247954 | 279316 | 317056 | 361768 | 413298 | 477232 | 552884 |
| MASHARIKI MWA AFRIKA | 64984 | 72774 | 82326 | 94165 | 108228 | 123675 | 144172 | 16785 |
| Nchi za Uingereza za Bahari ya | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| Hindi | 2456 | 2691 | 2948 | 3224 | 3522 | 3680 | 4132 | 4731 |
| Burundi | 173 | 194 | 215 | 240 | 274 | 320 | 392 | 463 |
| Komoro | 60 | 69 | 80 | 114 | 168 | 243 | 304 | 354 |
| Djibouti | 19573 | 21680 | 24191 | 27150 | 30623 | 34309 | 38750 | 43083 |
| Ethiopia | 6265 | 7189 | 8332 | 9749 | 11498 | 13741 | 16632 | 220096 |
| Kenya | 4230 | 4718 | 5309 | 6016 | 6742 | 7595 | 8785 | 10237 |
| Madagascar | 2881 | 3169 | 3529 | 3975 | 4518 | 5244 | 6183 | 7340 |
| Malawi | 493 | 571 | 660 | 753 | 826 | 892 | 966 | 1020 |
| Mauritius[a] | 6198 | 6744 | 7461 | 8338 | 9395 | 10498 | 12095 | 13711 |
| Msumbiji | 257 | 293 | 339 | 393 | 441 | 484 | 508 | 547 |
| Réunion | 2120 | 2391 | 2742 | 3183 | 3728 | 4384 | 5163 | 6102 |
| Rwanda | 34 | 38 | 42 | 47 | 53 | 59 | 63 | 65 |
| Seychelles | 2423 | 2657 | 2935 | 3267 | 3668 | 4156 | 5345 | 6370 |
| Somalia | 4762 | 5556 | 6562 | 8047 | 9806 | 11183 | 13120 | 15647 |
| Uganda | 7886 | 8803 | 10029 | 11586 | 13513 | 15900 | 18867 | 22748 |
| Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 2440 | 2753 | 3141 | 3614 | 4189 | 4841 | 5738 | 7006 |
| Zambia | 2730 | 3257 | 3812 | 4466 | 5260 | 6143 | 7126 | 8292 |
| Zimbabwe | 26316 | 28792 | 31811 | 35343 | 39599 | 45243 | 52183 | 60209 |
| AFRIKA YA KATI | 4136 | 4437 | 4816 | 5180 | 5588 | 6520 | 7723 | 8754 |
| Àngola | 4467 | 4843 | 5297 | 5874 | 6610 | 7520 | 8653 | 10051 |
| Cameroon | 1314 | 1414 | 1534 | 1677 | 1849 | 2057 | 2320 | 2646 |
| Jamhuri ya Afrika ya Kati | 2658 | 2838 | 3064 | 3334 | 3652 | 4030 | 4477 | 5018 |
| Chad | 808 | 889 | 988 | 1111 | 1263 | 1447 | 1669 | 1939 |
| Congo | 226 | 238 | 252 | 270 | 291 | 225 | 217 | 312 |
| Guinea ya Ikweta | 469 | 477 | 486 | 495 | 504 | 637 | 806 | 985 |
| Gabon | 60 | 62 | 64 | 68 | 73 | 81 | 94 | 107 |
| Sao Tome and Principe | 12184 | 13595 | 15310 | 17335 | 19769 | 22726 | 262251 | 30398 |
| Zaire | 51798 | 57994 | 65115 | 73297 | 83158 | 93799 | 07240 | 123348 |
| MAGHARIBI MWA AFRIKA | 8753 | 9715 | 10800 | 11923 | 13746 | 16018 | 18740 | 21788 |
| Algeria | 20330 | 22990 | 25922 | 29389 | 33053 | 36289 | 40875 | 46511 |
| Misri | 1029 | 1126 | 1349 | 1623 | 1986 | 2446 | 3043 | 3786 |
| Libyan Arab Jamahiriya | | | | | | | | |

[a] Ikiwa ni pamoja na Agalesa, Rodrigues na St. Brandon.

JEDWALI 30.1 (cont.)

| | (Idadi ya watu maelfu) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *1990* | *1995* | *2000* | *2005* | *2010* | *2015* | *2020* | *2025* |
| AFRIKA | 642 111 | 746 819 | 866 585 | 1 001 349 | 1 148 474 | 1 301 371 | 1 452 067 | 1 596 855 |
| MASHARIKI MWA AFRIKA | 196 873 | 232 243 | 273 594 | 321 148 | 374 399 | 431 034 | 487 868 | 542 536 |
| Nchi za Uingereza za Bahari ya Hindi | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| Burundi | 5 472 | 6 362 | 7 358 | 8 469 | 9 657 | 10 841 | 11 950 | 12 976 |
| Komoro | 550 | 658 | 789 | 945 | 1 123 | 1 315 | 1 510 | 1 697 |
| Djibouti | 409 | 474 | 552 | 644 | 748 | 862 | 979 | 1 094 |
| Ethiopia | 49 240 | 57 140 | 66 364 | 76 961 | 88 889 | 101 753 | 114 313 | 126 618 |
| Kenya | 24 031 | 28 978 | 35 060 | 42 389 | 50 905 | 60 071 | 69 799 | 79 113 |
| Madagascar | 12 004 | 14 113 | 16 627 | 19 529 | 22 827 | 26 476 | 30 272 | 34 014 |
| Malawi | 8 754 | 10 494 | 12 458 | 14 654 | 17 104 | 19 701 | 22 278 | 24 730 |
| Mauritius* | 1 082 | 1 142 | 1 201 | 1 258 | 1 309 | 1 354 | 1 391 | 1 419 |
| Mozambique | 15 656 | 17 922 | 20 493 | 23 365 | 26 456 | 29 592 | 32 593 | 35 416 |
| Réunion | 598 | 647 | 692 | 735 | 777 | 817 | 855 | 889 |
| Rwanda | 7 237 | 8 602 | 10 200 | 11 973 | 13 791 | 15 511 | 17 196 | 18 847 |
| Seychelles | 69 | 72 | 75 | 78 | 80 | 82 | 83 | 84 |
| Somalia | 7 497 | 8 441 | 9 736 | 11 312 | 13 114 | 15 035 | 16 905 | 18 701 |
| Uganda | 18 794 | 22 666 | 26 958 | 31 730 | 36 982 | 42 561 | 48 101 | 53 144 |
| Jamhuri ya Muungano Tanzania | 27 318 | 32 971 | 39 639 | 47 460 | 56 333 | 65 845 | 75 485 | 84 917 |
| Zambia | 8 452 | 10 222 | 12 267 | 14 632 | 17 328 | 20 264 | 23 286 | 26 260 |
| Zimbabwe | 9 709 | 11 340 | 13 123 | 15 012 | 16 974 | 18 951 | 20 870 | 22 616 |
| AFRIKA YA KATI | 70 054 | 81 933 | 95 981 | 112 344 | 130 958 | 151 395 | 172 266 | 192 342 |
| Angola | 10 020 | 11 531 | 13 295 | 15 317 | 17 561 | 20 004 | 22 438 | 24 731 |
| Cameroon | 11 833 | 14 037 | 16 701 | 19 897 | 23 665 | 27 893 | 32 264 | 36 547 |
| Jamhuri ya ican Afrika ya Kati | 3 039 | 3 511 | 4 074 | 4 740 | 5 497 | 6 325 | 7 154 | 7 947 |
| Chad | 5 678 | 6 447 | 7 337 | 8 352 | 9 491 | 10 728 | 12 013 | 13 245 |
| Congo | 2 271 | 2 678 | 3 167 | 3 746 | 4 406 | 5 130 | 5 860 | 6 568 |
| Guinea ya Ikweta | 352 | 400 | 455 | 519 | 592 | 671 | 752 | 828 |
| Gabon | 1 172 | 1 382 | 1 612 | 1 827 | 2 052 | 2 309 | 2 594 | 2 875 |
| Sao Tome and Principe | 121 | 135 | 151 | 167 | 184 | 201 | 219 | 235 |
| Zaire | 35 568 | 41 813 | 49 190 | 57 780 | 67 509 | 78 135 | 88 972 | 99 366 |
| MAGHARIBI MWA AFRIKA | 140 553 | 159 245 | 178 949 | 199 330 | 219 580 | 238 925 | 256 728 | 274 390 |
| Algeria | 24 960 | 28 704 | 32 904 | 37 286 | 41 510 | 45 279 | 48 484 | 51 950 |
| Misri | 52 426 | 58 388 | 64 210 | 70 099 | 75 746 | 81 050 | 85 768 | 90 355 |
| Libyan Arab Jamahiriya | 4 545 | 5 446 | 6 500 | 7 695 | 8 976 | 10 276 | 11 567 | 12 841 |

JEDWALI 30.1 (inaendelea)

| | (Idadi ya watu (maelfu) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *1950* | *1955* | *1960* | *1965* | *1970* | *1975* | *1980* | *1985* |
| KASKAZINI MWA AFRIKA 'AFRICA (cont.) | | | | | | | | |
| Moroko | 8 953 | 10 132 | 11 626 | 13 323 | 15 310 | 17 305 | 19 382 | 22 025 |
| Sudan | 9 190 | 10 150 | 11 165 | 12 359 | 13 859 | 16 012 | 18 681 | 21 822 |
| Tunisia | 3 530 | 3 860 | 4 221 | 4 630 | 5 127 | 5 611 | 6 384 | 7 261 |
| Magharibi mwa Sahara | 14 | 21 | 32 | 50 | 76 | 117 | 135 | 155 |
| KUSINI MWA AFRIKA | 15 736 | 17 639 | 19 892 | 22 623 | 25 581 | 28 866 | 32 379 | 36 372 |
| Botswana | 389 | 433 | 481 | 549 | 623 | 755 | 902 | 1 083 |
| Lesotho | 734 | 794 | 870 | 963 | 1 064 | 1 187 | 1 339 | 1 538 |
| Namibia | 666 | 736 | 817 | 910 | 1 016 | 1 141 | 1 306 | 1 518 |
| Afrika Kusini | 13 683 | 15 385 | 17 396 | 19 832 | 22 458 | 25 301 | 28 270 | 31 569 |
| Swaziland | 264 | 291 | 326 | 370 | 419 | 482 | 563 | 664 |
| MAGHARIBI MWA AFRIKA | 63 150 | 70 754 | 80 173 | 91 628 | 105 202 | 121 715 | 141 258 | 165 141 |
| Benin | 2 046 | 2 111 | 2 237 | 2 430 | 2 693 | 3 033 | 3 459 | 3 985 |
| Burkina Faso | 3 654 | 4 012 | 4 452 | 4 961 | 5 550 | 6 202 | 6 957 | 7 877 |
| Cape Verde | 146 | 169 | 196 | 229 | 267 | 278 | 289 | 324 |
| Côte d'Ivoire | 2 775 | 3 221 | 3 799 | 4 527 | 5 515 | 6 755 | 8 194 | 9 933 |
| Gambia | 294 | 313 | 352 | 404 | 464 | 548 | 641 | 745 |
| Ghana | 4 900 | 5 759 | 6 774 | 7 828 | 8 612 | 9 831 | 10 736 | 12 839 |
| Guinea | 2 550 | 2 826 | 3 136 | 3 488 | 3 900 | 4 149 | 4 461 | 4 987 |
| Guinea-Bissau | 505 | 522 | 542 | 524 | 525 | 627 | 795 | 873 |
| Liberia | 824 | 914 | 1 039 | 1 195 | 1 385 | 1 609 | 1 876 | 2 199 |
| Mali | 3 520 | 3 911 | 4 375 | 4 922 | 5 484 | 6 169 | 6 863 | 7 915 |
| Mauritania | 825 | 901 | 991 | 1 096 | 1 221 | 1 371 | 1 551 | 1 766 |
| Niger | 2 400 | 2 689 | 3 028 | 3 660 | 4 165 | 4 771 | 5 586 | 6 608 |
| Nigeria | 32 935 | 37 094 | 42 305 | 48 676 | 56 581 | 66 346 | 78 430 | 92 016 |
| St Helena[b] | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 | 6 |
| Senegal | 2 500 | 2 811 | 3 187 | 3 626 | 4 158 | 4 806 | 5 538 | 6 375 |
| Sierra Leone | 1 944 | 2 081 | 2 241 | 2 429 | 2 656 | 2 931 | 3 263 | 3 665 |
| Togo | 1 329 | 1 414 | 1 514 | 1 627 | 2 020 | 2 285 | 2 615 | 3 028 |

[b] Including Ascensión and Tristan de Cunha

*Source:* United Nations (1990) *World Population Prospects*, ST/ESA/SER. A/120.

JEDWALI 30.1 (inaendelea)

| | *Idadi ya watu (maelfu)* | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *1990* | *1995* | *2000* | *2005* | *2010* | *2015* | *2020* | *2025* |
| KASKAZINI MWA AFRIKA | | | | | | | | |
| Moroko | 25 061 | 28 301 | 31 559 | 34 648 | 37 586 | 40 408 | 43 022 | 45 647 |
| Sudan | 25 203 | 29 128 | 33 625 | 38 647 | 44 017 | 49 416 | 54 627 | 59 605 |
| Tunisia | 8 180 | 9 076 | 9 924 | 10 702 | 11 464 | 12 188 | 12 925 | 13 630 |
| Magharibi mwa Sahara | 178 | 202 | 228 | 254 | 280 | 308 | 335 | 362 |
| KUSINI MWA AFRIKA | 40 928 | 45 972 | 51 416 | 57 168 | 63 108 | 69 074 | 74 821 | 80 133 |
| Botswana | 1 304 | 1 549 | 1 822 | 2 124 | 2 451 | 2 779 | 3 095 | 3 397 |
| Lesotho | 1 774 | 2 053 | 2 370 | 2 731 | 3 138 | 3 579 | 4 013 | 4 427 |
| Namibia | 1 781 | 2 079 | 2 437 | 2 847 | 3 303 | 3 776 | 4 245 | 4 698 |
| Afrika Kusini | 35 282 | 39 348 | 43 666 | 48 139 | 52 662 | 57 150 | 61 446 | 65 363 |
| Swaziland | 788 | 943 | 1 121 | 1 326 | 1 554 | 1 790 | 2 023 | 2 249 |
| MAGHARIBI MWA AFRIKA | 193 702 | 227 426 | 266 645 | 311 360 | 360 430 | 410 942 | 460 383 | 507 455 |
| Benin | 4 630 | 5 421 | 6 369 | 7 486 | 8 745 | 10 065 | 11 369 | 12 587 |
| Burkina Faso | 8 996 | 10 396 | 12 092 | 14 080 | 16 349 | 18 822 | 21 327 | 23 710 |
| Cape Verde | 370 | 438 | 515 | 595 | 676 | 757 | 841 | 922 |
| Côte d'Ivoire | 11 997 | 14 535 | 17 600 | 21 218 | 25 503 | 30 069 | 34 776 | 39 334 |
| Gambia | 861 | 984 | 1 119 | 1 271 | 1 434 | 1 593 | 1 736 | 1 864 |
| Ghana | 15 028 | 17 608 | 20 564 | 23 845 | 26 931 | 29 884 | 32 708 | 35 442 |
| Guinea | 5 755 | 6 700 | 7 830 | 9 162 | 10 667 | 12 252 | 13 820 | 15 273 |
| Guinea-Bissau | 964 | 1 073 | 1 197 | 1 338 | 1 491 | 1 649 | 1 791 | 1 918 |
| Liberia | 2 575 | 3 032 | 3 575 | 4 207 | 4 921 | 5 689 | 6 477 | 7 245 |
| Mali | 9 214 | 10 799 | 12 685 | 14 885 | 17 350 | 19 918 | 22 439 | 24 774 |
| Mauritania | 2 024 | 2 335 | 2 702 | 3 129 | 3 612 | 4 129 | 4 642 | 5 119 |
| Niger | 7 731 | 9 104 | 10 752 | 12 694 | 14 884 | 17 167 | 19 406 | 21 482 |
| Nigeria | 108 542 | 127 694 | 149 621 | 174 307 | 201 266 | 228 753 | 255 393 | 280 890 |
| St Helena[b] | 7 | 8 | 10 | 11 | 13 | 15 | 17 | 19 |
| Senegal | 7 327 | 8 423 | 9 716 | 11 172 | 12 730 | 14 269 | 15 685 | 16 988 |
| Sierra Leone | 4 151 | 4 740 | 5 437 | 6 250 | 7 172 | 8 161 | 9 139 | 10 045 |
| Togo | 3 531 | 4 138 | 4 861 | 5 711 | 6 687 | 7 750 | 8 821 | 9 842 |

# Maelezo ya mwisho na Kronolojia ya Mambo ya Sasa ya Afrika katika miaka ya 1990[1]

Mwanzoni mwa miaka ya 1990 ulikuwa na mabadiliko ya kisiasa yakiwa ni pamoja na matukio ya kushtua kama kuanguka kwa Ukuta wa Berlin na serikali za kikomunisti za Ulaya Mashariki, na Vita vya Ghuba. Kuporomoka kwa ukomunisti kumeuacha ubepari bila mshindani na kumeacha wazi njia kwa demokrasia huria na uchumi unaotegemea masoko, ambavyo kwa leo hii ndivyo vinavyofafanua jinsi jamii zinavyopaswa kubadilika. Toka sasa na kuendelea hii inakuja ndani ya mawanda ya mfumo wa mahusiano ya dunia nzima ambavyo yamewezeshwa na mapindizi ya kiteknolojia na kimawasiliano: huku kufanya kuwa ya kimataifa mabadilishano baina ya watu sasa hivi yanajumuisha mataifa yote na tamaduni zote bila kubagua.

Kama sehemu kamili ya mfumo huu wa dunia, Afrika haijakwepa mabadiliko haya. Afrika katika miaka ya 1990 inaweza ikafafanuliwa kwa misingi ya mgogoro wa kiuchumi na kisiasa, mvutano na vita, kuukosea rajua Uafrika, lakini pia ujenzi

[1] Tunamshukuru Bi J.M. Kambo (Mwanahistoria, PhD) na Bi. S. Serbin (mwana historia na mwanahabari) kwa kazi na michango yao. Maelezo haya ya mwisho yanayotazama mambo ya nyuma na Kronolojia ya mambo ya sasa ya Kiafrika katika miaka ya 1990 (tazama uk. 940) vimeandikwa mno kwa kutumia mambo na data iliyotolewa na majarida yauatayo: *Afrigul contemporaire* na *Monde arabe, Maghreb Machrek;* machapisho ya robo mwaka yanayotolewa na Hifadhi ya Hati ya Ufaransa ya huko Paris. Jarida Politique Afrieaine, matoleo ya Karthala huko Paris. Matoleo yote ya kipindi cha 1989-97 yamechunguzwa. Tumetazama pia matole ya 1994 –97 ya Marches tropicaux et mediterranien the African and Indian Ocean kila wik, CIRAD –CA' Montpeller.

wa demokrasia na haki za binadamu. Bila kugaagaa katika kisasili cha Afrika iliyolaaniwa, ilipoanza kuoza kwa sababu ya maradhi ya ajabu, iliyoangamizwa na watawala dhalimu wabadhirifu na vita vya kikabila, inafaa kukiri kwamba Afrika si mshindi. Kwa kutafakari changanuzi katika juzuu hili, swali linalobakia kuulizwa ni zitakazokuwa aula mpya za bara hili, kwa jinsi inavyokabiliwa na mizozo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika miaka ya 1990. Tutagusia suala hili kwa kifupi, na kuachia kronolojia ya matukio makuu kumulika njia ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii barani Afrika, bara ambalo kinyume na kupooza kabisa kwa maradhi, linaficha matarajio makubwa ya uvumbuzi.

Utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia mnamo 1989 unaonyesha kwamba kwa miaka thelathini, umaskini umeendelea kuwepo katika nchi za Afrika, ambazo zilikuwa na matumaini makubwa ya kuboreka kwa hali ya watu wake baada ya uhuru. Katika miaka ya 1970, kupanda kwa bei ya malighafi na kumwagwa kwa fedha zilizotokana na uuzaji wa mafuta viliwawezesha viongozi wa nchi zinazoendelea na hususani viongozi wa Kiafrika, kugharimia miradi ya maendeleo iliyokuwa na athari ndogo katika kiwango cha hali ya maisha ya watu. Lakini baada ya migogoro miwili ya mafuta ya 1973 na 1979, iliyotikisa uchumi wa dunia, kushuka kwa uzalishaji viwandani ulisababisha kupungua kwa matumizi ya malighafi. Hivyo, miaka ya 1980 ikawa ya kushuka kwa jumla, hususani barani Afrika kutokana udhaifu uliokuwepo wa muundo wa uchumi wake isipokuwa Afrika Kusini.

Katika miaka ya 1990, utendaji wa kiuchumi barani Afrika ulizidi tena kuwa wa kukatisha tamaa. Jumla ya Pato la Ndani lilibakia chini ya kiwango cha mwaka 1980. Umaskini uliokithiri kwa kiasi unahusishwa na ongezeko la idadi ya watu, linalokisiwa kuwa asilimia 2.8 mnamo 1996, kiwango ambacho ni cha juu kuliko kile cha ongezeko katika uzalishaji wa chakula (wa asilimia 2.2 kwa mwaka). Barani Afrika, asilimia 60 ya watu ni mafukara wa kutupwa na katika nchi 48 zilizoainishwa kama nchi zenye mandeleo duni kabisa duniani, 33 ni za Kiafrika. Afrika inapata tu asilimia 5 ya jumla ya vitegauchumi vya kigeni vya moja kwa moja, yaani dola za Kimarekani bilioni 110 mnamo mwaka 1996, ambavyo humo barani, kiasi kikubwa huingia Afrika Kusini, Misri, Morocco na Nigeria, na kupungua kwa msaada kwa jumuiya kwa ajili ya maendeleo kunatisha.

Nchi za kaskazini zinajizatiti upya na kuhamasisha mtaji wao ili kuimarisha Ulaya. Mtaji huu sasa hivi unaelekezwa katika nchi zilizokuwa za kikomunisti za Ulaya ya Kati na Mashariki, Amerika Kusini ambayo ina matokeo mazuri zaidi ya kiuchumi na nchi za Asia ambazo masoko yake yanaelekea kuwa na uwezo zaidi wa kifedha. Mgao wa Afrika katika mabadilishano duniani umeshuka hadi asilimia

1 tofauti na asilimia 3 ya miaka ya 1960. Hili ndilo bara lenye deni kubwa mno kwa kila mkazi; deni la Afrika katika miaka ya 1990, inalingana na asilimia 265 ya mapato kutokana na mauzo nje. Ulipaji wa madeni kwa nchi nyingi umebakia karibu na asilimia 20 na kwa baadhi ya nchi huzidi asilimia 30 ya mapato kutokana na mauzo nje.

Tangu mwisho wa ukomunisti na kupokelewa kwa uhuria duniani kote, Afrika imeacha kuwa eneo la maslahi kimkakati. Kwa hiyo tunashuhudia hasa kuanguka kwa hadhi ya bara la Afrika katika miaka ya 1990. Tajriba za maendeleo kutoka nje katika bara hili zimekwama vibaya. Baada ya kushindwa kujibadilisha kama mwanachama thabiti wa mfumo wa uchumi wa dunia, Afrika imejikuta ikizidi kubwagwa, na inadhoofishwa na migogoro yake ya kisiasa na udhaifu katika matokeo yake ya kiuchumi. Hali hii inaandamana na mkondo mpya katika fikra: kuukosea rajua Uafrika.

Matatizo yanayohusishwa na ulipaji wa madeni ya ndani na ya nje, na vilevile kushuka kwa mapato ya umma, vimesababisha viongozi wa Kiafrika kutafuta msaada wa Asasi za Bretton Woods, Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia ambavyo vimechukua nafasi ya wawekezaji wa nje na vinajaribu kuingiza tena nishati katika uchumi mahututi wa Afrika kwa kutumia Mipango ya Kufufua Uchumi. Mipango hii ya Kufufua Uchumi ina taratibu za kufufua uchumi kwa kurejesha uwiano katika uchumi mpana wa ndani na nje na utekelezaji wa mipango ya kurekebisha miundo. Shirika la Fedha la Kimataifa linatetea ulegezaji masharti ya uchumi wa Afrika na linanuia kuondoa serikali katika usimamizi wa uchumi; na kuuachia sekta ya watu binafsi. Kitendo chake hiki kinachukua sura ya hatua nyingi zikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi ya huduma kwa umma, ambako kunaathiri huduma za jamii, kuanzishwa kwa sera zilizokitwa katika sekta zinazopendelea shughuli za watu binafsi, kupunguzwa kwa wafanyakazi katika utumishi wa taifa, wanaochukuliwa kuwa wengi kupita kiasi, na kusimamisha ajira zote n.k. Ili iweze kupewa mtaji, nchi zinazohusika zinatakiwa kujadili mikataba yenye masharti na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Katika miaka ya 1990, karibu nchi zote za Kiafrika ziliingia katika utaratibu huu wa kujibana na kujiimarisha. Kupunguzwa kwa thamani ya faranga (CFA), kulikolazimishwa katika nchi zinazozungumza Kifaransa mnamo Januari 12, 1994, ni moja ya mafanikio makubwa kabisa ya Asasi za Bretton Woods. Asasi hizi zilikuwa zikilalamikia thamani kubwa ya sarafu hii tangu miaka ya 1970. Muundo usio linganifu wa uchumi huo wa Afrika katika ukanda huo unaotumia faranga, ulidhurika kutokana na maendeleo duni na mzigo ulioendelea kuongezeka wa msaada ambao ilibidi Ufaransa iutoe ili kusaidia uchumi wa nchi hizi ulisababisha serikali ya Ufaransa kuhusisha misaada

yake na utiaji saini wa mipango ya kurekebisha uchumi na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kuunga mkono kanuni ya kupunguza thamani ya fedha.

Katika nchi hizi ambazo tayari zilikuwa maskini, mipango hii mikali ilisababisha kubomoka kwa miundo ya kiuchumi na kijamii, kuongezeka kwa ukosefu wa ajira na kuzidi kuzorota kwa hali ya maisha ya watu. Walioathirika zaidi ni wale wanaoishi mijini ambamo mbinu za kuondolewa na kutengwa kijamii zinajitokeza zaidi. Uanzishaji wa miji katika dunia ya tatu ni moja ya mambo makubwa kwa mwisho wa karne hii. Viwango vya uanzishwaji wa miji vya nchi za Kiafrika vinafikia asilimia 40 na idadi ya wakazi wa mijini inaongezeka kila mwaka kwa asilimia 5.5. Mbali na mapigo haya ya uanzishwaji wa miji, idadi ya watu vijijini barani Afrika bado inaongezeka kwa kiwango cha jumla cha ukuaji cha asilimia 3.1.

Kuchukuliwa kwa hatua za mipango ya kurekebisha uchumi kumezusha tabu nyingi, malalamiko, migomo ya wafanyakazi na wanafunzi; migomo ya siku mojamoja ya wenye maduka imetokea mara kwa mara katika miji ya Afrika katika miaka ya 1990 (kwa mfano, huko Cameroon, Kenya, Togo na Zaire). Ikiwa madhara ya mipango ya kurekebisha uchumi yana peo nyingi tofauti, ni vizuri kutaja yale ya kutia shauku zaidi miongoni mwake, ambayo yana athari kwa afya, chakula na elimu. Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF) limeona kwamba kati ya nchi kumi ambazo ziliingia katika mpango wa kurekebisha uchumi, sita zimeonyesha kupungua kwa kiwango cha lishe na kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza, na tano zimeshuhudia kuzorota kwa elimu. Pia ni muhimu kutaja tukio la ugonjwa wa UKIMWI ambao umewakumba zaidi Waafrika kutokana na hali zao za maisha. Pamoja na tofauti kubwa toka nchi hadi nchi, UKIMWI katika muda wa chini ya mwongo, umekuwa chanzo cha kwanza cha vifo miongoni mwa Waafrika.

Madhara ya migogoro yamewatweza vijana wa Afrika, hususani wale wa umri wa kwenda shule, na wanafunzi wa vyuo vikuu, ambao kwao miaka ya 1990 ilikuwa kipindi cha mashaka. Sera za kurekebisha uchumi hubana ajira ya watumishi wa serikali na hivyo walimu katika bara lenye mlipuko wa idadi ya watoto wa shule kutokana kwa kiasi fulani na ongezeko la idadi ya watu. Kila mahali familia zinaishi kwa ujanja wake na shule huwekwa kando pale swali muhimu linapokuwa ni kujaribu kuishi. Katika Afrika Kusini mwa Sahara, ambako chini ya asilimia 2 ya vijana wana uwezo wa kupata elimu ya juu, mazingira ya kusomea wanafunzi ni ya kusikitisha. Mambo haya mara zote yalisababisha migomo ya wanafunzi ambayo inavuruga masomo vyuoni ama ilisababisha vyuo kufungwa au miaka mitupu ambapo mitihani haifanyiki kama ilivyowahi kutokea Ivory Coast, Kenya, Senegal, Niger Gabon na hivi karibuni Burkina Fano. Barani Afrika, vyuo vikuu ni

alama ya maarifa, maslahi ya yeyote aliye madarakani ambamo migongano yote ya jamii wakati wa mgogoro inaunganika. Kwa hiyo vinaweza kujumuisha mkwamo ambamo Afrika imo, ikiwa imezidiwa pia na mzigo wa madeni, bara ambamo kushindwa kwa mifumo ya elimu kuna maana kwamba upatikanaji wa elimu ni kwa watu waliobahatika, na hivyo kuzidi kuongeza hali ya kutokuwa sawa kijamii.

Wanawake pia ni waathirika katika utekelezaji wa mipango ya kurekebisha uchumi. Wenyewe ndio wengi kwa idadi na ni miongoni mwa sehemu ya jamii zenye uwezekano mkubwa wa kuathirika. Kukiwa na mgogoro wa kiuchumi, ambao pia ni mgogoro wa jamii, wanawake wako mstari wa mbele pale kunapotokea haja ya kusuluhisha matatizo ya maisha ya kila siku ya familia, mara nyingi kwa kupitia sekta isiyo rasmi ambayo wanaimudu vizuri. Katika soko la ajira lililodorota kutokana na migogoro, ambamo jumla ya kiwango cha wasiokuwa na ajira ni karibu asilimia 18 tofauti na asilimia 10 mnamo 1970, mikakati ya watu ya kuishi haiwezi kufika mbali na hii huibua kuongezeka kwa uhalifu na umalaya.

Dunia ya kisiasa kwa kiasi kikubwa bado inashikiliwa na wanaume: kama nyongeza kwa vipingamizi vya kimuundo vya kiutamaduni, kijamii, kihistoria na amri za kisheria, vizuizi kutokana na hali za sasa hukwamisha lushiriki kwa wanawake katika siasa. Hawawakilishwi kwa kiasi kinachozidi asilimia 8 katika mamlaka ya juu ya dola yanayofanya maamuzi.

Hata hivyo, hatua kwa hatua wanawake wameanza kuachana na wajibu wao kama mwenzi wa mwanaume na pamoja na vijana wanaunda uongozi wa umma kwa kutoa changamoto kwa mamlaka ya kisiasa wa aina moja. Matendo yao thabiti katika taratibu za mpito wa Kidemokrasia yamejitokeza katika siasa barani Afrika katika miaka ya 1990, kama ilivyoonyeshwa Mali, Togo na Algeria.

Tangu uhuru, historia imeonyesha mwelekeo wa kusahau uwezo wa jamii za Kiafrika katika kuachana na taratibu zilizopo. Katika miji ya Afrika mnamo miaka ya 1990, migomo shuleni na katika vyuo vikuu, migomo ya vyama huru vya wafanyakazi, uhamasishaji wa wanawake, vyote vimekuwa na dhima ile ile. Waafrika wengi, wakiwa hawajiwezi wanapokabiliwa na athari za marekebisho, wanajaribu kufanya maisha yawe na maana kwa kujiunga na madhehebu na vyama vya kidini au makanisa mapya. Wengi wengine wanaanza mapambano ya kisiasa kudai kuongezwa kwa demokrasia na kuheshimiwa zaidi kwa haki za binadamu. Utafutaji huu wa mabadiliko unatokana na muktadha wa Kiafrika na athari za nje.

Jambo hili kwa hakika haliwezi kutengwa na mabadiliko yanayoathiri jamii za Kiafrika tangu mwisho wa mwongo wa kwanza wa uhuru. Katikati ya haya yote, ni lazima kutaja dhima ya vijana waliozaliwa baada ya uhuru, hususani upinzani

wao wa mamlaka yaliyoanzishwa katika jamii za Kiafrika ambapo mshikamano uliokuwepo awali sasa hivi unavurugwa na uanzishwaji wa maji na kuzorota kwa uchumi. Kwa miaka thelathini viongozi wa Afrika wametawala kwa mabavu kwa kutumia mfumo wa chama kimoja na kuhalalishwa na nia ya kumalizia ujenzi wa nchi na muungano wa taifa. Mamlaka haya yameshikiliwa kadri hali ya uchumi ilivyotoa nafasi kwa ajili ya maendeleo. Leo hii, vijana hawakubali tena kutia hatarini maisha yao ya baadaye kwa mbinu hizo za utawala na uongozi. Hii imesababisha kuenea kwa upinzani. Miji ndiyo mandhari ya mabadiliko katika miundo ya kijamii ya kijadi na pia shule ya demokrasia. Vijana wamepata uwezo maalumu wa kuanzisha hali ya kutoridhika. Katika kuingiliana huku kwa vipengele vya ndani, makanisa ya Kikristo yasisahauliwe, kwa kuwa yamechukua msimamo wa kupendelea ujenzi wa demokrasia na haki za binadamu na hivyo kuharakisha mabadiliko ya mifumo ya kisiasa katika nchi nyingi kama vile Afrika Kusini, Benin, Congo, Sudan, Togo na Zaire.

Hamu hizi za kufanya mambo zimeathiriwa pia na mabadiliko ya kisiasa ambayo yametokea Ulaya Mashariki ambako kukataliwa kwa ukomunisti kumeporomosha utaratibu wa dunia uliolazimishwa na mikataba ya Yalta. Washirika wa Magharibi hawahoji tena nchi za Kiafrika kuingizwa katika ukomunisti. Wahisani ambao hapo awali walikuwa mbele katika kuziunga mkono serikali za kiimla, sasa hivi wanawasihi Waafrika kuikubali mifumo ya kidemokrasia. Kwa kutilia maanani milipuko ya kijamii iliyotokea katika sehemu kadhaa za bara, Ufaransa, katika mkutano wa wakuu wa nchi (mnamo Juni 19-21,1990) iliweka wazi kwa washirika wake wa Kiafrika kwamba msaada wake toka wakati huo na kuendelea, utaenda kwa nchi zinazofuata njia ya demokrasia. Hivyo demokrasia inakuwa sharti kwa ajili ya maendeleo na msaada wa nchi za Magharibi ? ni kusaidia ujenzi wa demokrasia, na wa utawala wa kisiasa. Nchi za Kiafrika, zikiongozwa na Benin, zilijibu maombi haya kwa kuandaa mikutano ya taifa iliyolenga kueleza katiba mpya na sheria za msingi zinazoleta uwingi katika siasa.

Uhuru wa kusema uliopatikana punde tu umekuwa na matokeo ya kuongezeka kwa vyama vya siasa, vikitofautiana idadi kutoka vinne huko Sao Tome na Principe hadi zaidi ya mia moja huko Nigeria na Zaire. Uchaguzi wa ushindani umefanyika katika karibu kila nchi ya Afrika.

Dalili dhahiri ya kwanza ya uhuru huu mpya imekuwa ni kujitokeza tena au kuanzishwa kwa magazeti mengi na vituo binafsi vya radio. Pamoja na mazingira yasiyokuwa mazuri, mashirika mengi yasiyokuwa ya kiserikali yamejitahidi kudai kuheshimiwa kwa haki za binadamu barani. Tangu 1992 shirika la kutetea haki za binadamu barani Afrika la *Union Interafricaine des droits de l'homme* (UIDH)

ambalo lina makao yake makuu nchini Burkina Faso lina malengo ya kutekeleza sera ya hakika ya kuhami, kuendeleza na kulinda haki za binadamu katika nchi tofauti za Afrika. Robo tatu ya nchi zote za Kiafrika zimekwishakujiunga, na shirika linaajiri idadi kubwa ya wanasheria. Sehemu za kitaifa huwa vipingamizi halisi ikiwa serikali itajaribu kuwa katika mwelekeo wa kukiuka haki za binadamu.

Lakini neno la kutia hamasa katika siasa katika Afrika ya miaka ya 1990 linabakia kuwa demokrasia na "utawala bora' ambalo lilichangia sana ukombozi wa Nelson Mandela, hasa ukipima athari maelezo ya vyombo vya habari yaliyokuwa nayo juu ya vyama duniani kote na hususani barani Afrika. Hata hivyo, utaratibu wa mpito kuelekea katika demokrasia haujakosa kukabiliwa na matatizo, mikwaruzo na fadhaa ambavyo wakati mwingine vilisababisha kupooza katika siasa, na mapinduzi ya kijeshi. Huko Ghana, Mali na Chad, utaratibu wa kidemokrasia umeanzishwa na majeshi, wakati kwingineko majeshi bado yamenyakua madaraka kwa lengo la kutaka kukomesha migogoro kama huko Nigeria mnamo 1993, huko Niger na Visiwa vya Comoro mnamo 1995, huko Burundi mnamo 1996, huko Sierra Leone mnamo 1997, jambo ambalo limeibua hofu kubwa ya mapinduzi ya kijeshi kama ilivyokwisha jitokeza katika siasa za Afrika katika miongo miwili iliyotangulia. Migororo mingine inayohusishwa na matatizo ya kutekeleza demokrasia na "utawala bora', imekuwa changamani zaidi, huko Kongo na huko Afrika ya Kati matatizo kadhaa ya kisiasa na kikabila yamefanya makundi yapigane na kuuana mijini.

Ikiwa mwanzo wa miaka ya 1990 ulishuhudia mwisho wa vita vya ukombozi na uhuru ukitolewa kwa Eretrea, Namibia, weusi walio wengi kushika madaraka huko Afrika Kusini, kukomesha mfumo dhalimu wa ubaguzi wa rangi, vita vilivyoendelea katika baadhi ya nchi za Afrika katika mwongo vilikuwa vya aina tofauti. Vita vya wenyewe kwa wenyewe vimeibuka kutokana na matatizo ya kiuchumi na kisiasa ambayo huchukua sera ya migororo ya kikabila, kiutamaduni na kidini. Mauaji ya halaiki yaliendelea huko Burundi na Rwanda, mauaji ya kikatili huko Aligeria, mapigano ya kikatili huko Liberia na Sierra Leone vinaendelea kujitokeza katika magazeti na vyombo vya habari kwa jumla. Baadhi ya harakati za kujitenga huko Casamance, Visiwa vya Comoro, Sudan, madai ya kutambuliwa (tatizo la Watouareg huko Mali na Niger), migororo ya mipaka (Cameroon/Nigeria) vinakamilisha picha ya migogoro ya Afrika.

Lakini kutwaliwa kwa madaraka na chama Laurent-Desire Kabila cha *Allied Democratic Forces for the Libertion of Congo* (AFDL) katika iliyokuwa Zaire, ambayo kwa miaka saba iliyopita ilikwama katika utaratibu wa mpito wa

Lakini kutwaliwa kwa madaraka na chama Laurent-Desire Kabila cha *Allied Democratic Forces for the Libertion of Congo* (AFDL) katika iliyokuwa Zaire, ambayo kwa miaka saba iliyopita ilikwama katika utaratibu wa mpito wa kidemokrasia, kwaonekana kuwa tukio kubwa la kisiasa la 1997. Hapana shaka kwa sababu kwa mara ya kwanza tangu mwisho wa Vita Baridi mgogoro muhimu wa Kiafrika ulimalizwa kikamilifu na Waafrika wenyewe hususani migogoro katika Afrika Mashariki, Kusini na Kati. Itakuwa jambo lenye mantiki kuuliza ikiwa mgogoro huu hautabiri marekebisho katika muundo wa kijiografia na kisiasa barani, kwa msingi wa mamlaka baina ya nchi zinazozungumza Kifaransa na zinazozungumza Kiingereza kwa upande mmoja na nchi zenye madini na mafuta kwa upande mwingine. Hivyo, swali linalohitaji jibu ni je Afrika hatimaye itaonekanaje mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja?

Matumaini yaliyoelezwa na viongozi wa serikali katika mkutano wa Umoja wa nchi za Afrika mnamo Juni 1977, wakizungumzia "mvuvumko', hutuondoa katika Afrika ya Magharibi ya kuukosea Rajua uafrika. Afrika ya Kati, Mashariki na Kusini vimejaliwa maliasili nyingi na rasilimali kubwa ya watu, na zinafikiria kuunda "Soko la Pamoja la Afrika'. Muungano katika kanda, kwa hakika, ni moja ya suluhisho kwa mgogoro uliopendekezwa na Waafrika kushuhudia uundaji wa mashirika mengi ya uhusiano baina ya serikali na serikali ya aina na uwezo unaotofautiana uthabiti, lakini ambayo huweka nchi pamoja katika makundi kulingana na sehemu zilipo kijiografia. Kwa mfano: *Union du Maghreb Arabe* (UMA), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) *Communaute economi aue et monetaire des Etats de l'Afrigue centrale (CEMAC), Communaute economique des Etats de l'Afrugues Ouest (EDEAO), Union economigue et monetaire quest africaine (UEMOA)* ambayo yananuia kuunganisha maeneo ya kiuchumi ya kitaifa kwa kuondosha vizuizi dhidi ya mizunguko huru ya bidhaa na watu, asasi ya ushuru unaopendelewa kwa ajili ya biashara ya kikanda na utekelezaji wa sera za pamoja zilizokitwa katika sekta kwa mfano, sekta za kilimo, viwanda na nishati. Kutangazwa kwa sheria za biashara pia kunafikiriwa. Ili kukamilisha mipango ya muungano wa kiuchumi na kisiasa

| | AFRIKA KASKAZINI NA KASKAZNI MASHARIKI | AFRIKA MAGHARIBI |
|---|---|---|
| 1990 | **Algeria:** Matatizo kuhusiana na vitendo vya Waislamu wanaotaka kufungwa kwa mabaa na madanguro (Januari 10-25)<br>**Misri**. Vifo vya watoto vimeshuka kutoka 84 hadi 4 kwa kila watoto elfu moja kutokana na chanjo kwa asilimia 90 ya watoto wachanga waliozaliwa. Jumla ya idadi ya watu milioni 56 (Julai 26)<br>**Libya:** Kuendelezwa na Marekani kwa vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na Umoja wa Mataifa mnamo 1986 (Januari 5), kutia saini mkataba wa kuungana na Sudan (Juni 10), kutia saini mkataba na Chad kuhusu usalama na mjongeo wa watu (Septemba 5)<br>**Moroko:** Mahusiano ya kidiplomasia yaanzishwa na **Namibia** (Machi 26)<br>**Somalia**: Kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi (Oktoba 6)<br>**Sudan**: Mahusiano ya kidiplomasia na Jamhuri ya Afrika ya kati yarejeshwa (Februari 12), kupunguzwa kwa asilimia 10 ya wafanyakazi waendeshaji na watumishi wa umma kama sharti la Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) | **Benin:** Mkutano wa Kitaifa wa kisiasa kuchunguza kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi na demokrasia (Februari 19-28) kupitishwa kwa katiba mpya (Desemba 2)<br>**Cote dIvoire**: Maandamano ya wanafunzi yenye ghasia, migomo shuleni kutaka mabadiliko ya kimuundo (Februari 19-20) kuchaguliwa tena kwa Rais Houphouet – Boigny kama Rais wa Jamhuri (Oktoba 28)<br>**Gninea Bissau:** Mkutano wa taifa kuhusu mpito kuelekea kwenye vyama vingi (Oktoba 8-12)<br>**Liberia:** Serikali ya muda ya Amos Sawyer inaanzishwa Monrovia (Novemba 22)<br>**Mali:** Idadi ya watu inakisiwa kuifikia 7696,000<br>**Niger:** Kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi Novemba 15)<br>**Senegal:** Mapigano baina ya majeshi ya Senegal na yale ya Guinea Bussau kwenye mpaka wa nchi hizo Mei (19 – 23) matukio huko Casamance yalifikia kuwa na kundi linalotaka kujitenga la Casamance (Mei-Juni)<br>Sahara Magharibi: kutambuliwa kwa Jamhuri ya kidemokrasia ya Waarabu wa Sarhoki na Namibia (Aprili 30) |

| AFRIKA YA KATI | AFRIKA MASHARIKI NA KUSINI | AFRIKA NA DUNIA |
|---|---|---|
| **Cameruni:** Sheria kuhusu mfumo wa vyama vingi (Desemba 6)<br>**Chad**: Majeshi ya Idris Derby yanaingia Ndjamena (Desemba 2). Idris Derby anateuliwa kuongoza nchi (Desemba 4)<br>**Kongo:** Maandamo mitaani yaliyochochewa kisiasa na kijamii na migomo inaimarika nchini (oktoba-Novemba) mfumo wa vyama vingi unaingizwa katika katiba (Desemba 6)<br>**Rwanda:** Mfumo wa vyama vingi unaanzishwa (Novemba 13), askari wa chama cha **National Patriotic Front** waliokimbilia Uganda wanajaribu kuvamia nchi (Oktoba 1-3)<br>**Zaire:** Rais Mobutu Seseseko atangaza kuanzishwa kwa vyama visivyozidi vitatu (Aprili 24), vyama vya upinzani vinadai kwamba mkutano wa vyama vingi uitishwe kupanga uchaguzi huru, migomo na maandamano vinazidi kuwa vya mara kwa mara (Mei 1-25). | **Visiwa vya Komoro:** Bw. Ahmed Abdallah achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 14)<br>**Lesotho:** Mwana wa Mfalme Mohato Seeisa atangazwa kuwa mfalme badala ya baba yake ambaye amelazimishwa kwenda uhamishoni na jeshi (Novemba 11).<br>**Malawi:** Inajiunga na mkataba wa Haki za Binadamu wa Umoja wa nchi Huru za Afrika (Februari 23)<br>**Msumbiji:** Adhabu ya kifo inafutwa (Oktoba 22)<br>**Namibia:** Bunge linapitisha katiba. Bw. Sam Nujoma achaguliwa Rais wa Namibia pale itakapokuwa huru. Na Namibia yawa huru (Machi 21); Namibia inakuwa rasmi mwanachama wa 18 wa Umoja wa Mataifa (Aprili 23); Namibia inajiunga na Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia (Septemba 25) na Kundi la Lome lV (Desemba 19)<br>**Jamhuri ya Afrika Kusini:** Kuhalalishwa kisheria kwa vyama vya ANC, PAC na Chama cha Kikomunisti cha Afrika Kusini (Februari 2); Nelson Mandela naachwa huru baada ya kukaa jela kwa miaka 27 (Februari 11)<br>**Tanzania:** Rais Ali Hassan Mwinyi achaguliwa tena kuwa Ras wa Jamhuri (Oktoba 28)<br>**Zambia:** Kuhalalishwa kisheria kwa mfumo wa vyama vingi (Desemba 7)<br>**Zimbabwe:** Bw. Robert Mugabe achaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri (Aprili 1) | **Ufaransa na Afrika:** Mkutano wa 16 wa viongozi huko La Baile. Rais wa Ufaransa Francois Mitterand anatangaza katika hotuba yake kwamba ili kufaidi msaada kutoka Ufaransa, nchi za Afrika ni lazima zifanye juhudi za kujenga demokrasia (Juni 19-21)<br>**Tunisia:** Kuundwa kwa kituo cha mafunzo cha Kiafrika kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu (Mei 19)<br>**Vatican:** Papa Johana Paulo wa II anafanya ziara ya sita Afrika Visiwa vya Cape Verde, Barkina Faso, Guinea Bissau, Mali, Jamhuri ya Afrika Kusini, Chad (Januari 21 – Februari 1) |

| | | |
|---|---|---|
| 1991 | **Algeria:** Mfumo wa elimu ya juu kuendeshwa kwa lugha ya Kiarabu tu (Julai 22); bei yapanda kwa asilimia 35 kwa bidhaa muhimu kulingana na masharti ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) (Agosti 17)<br>**Ethiopia:** Mengistu Haile Mariam anajiuzulu wadhifa wake kama kiongozi wa nchi (Mei 28) Bandari ya Asmarra yachukuliwa na wapiganaji wa EPLF (Juni 10)<br>**Libya:** Kuondolewa kwa vituo vya ushuru na sheria za mpakani na Misri (Agosti 7); kuzinduliwa kwa sehemu ya kwanza ya kazi kuhusu 'Mto Mkuu' , mfereji wa umwagiliaji wa kilomita 630 unaoleta maji ya chini ya ardhi hadi Benghazi.<br>**Somalia:** Jenerali Aideed ashika madaraka (Novemba 18)<br>**Sudani:** Amri ya kubadilisha Sudani kuwa shirikisho (Februari 5) maandamano ya wanafunzi kuhusu suala la nyumba. | **Benin:** Bw. Nicephore Soglo achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 25)<br>**Burkina Faso:**<br>Kapteni Blaise Compaore achaguliwa kuwa Rais wa BurkinaFaso (Desemba 8)<br>**Cape Verde:** Bw. Mascarenhas Monteiro achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Februari 17).<br>**Coted'Ivoire:** Matokeo ya karibuni kabisa ya sensa: Wakazi 10,815,694 (Novemba 19)<br>**Liberia:** Mwongozo wa mkutano wa taifa (Machi 16).<br>**Mali:** Mkataba wa kusitisha mapigano (Januari 6) maandamano ya maelfu ya watu wanaodai mfumo wa vyama vingi (Machi 3-4) ghasia mjini Bambako na miji mingine mikubwa nchini, ukandamizaji wa polisi unasababisha Vifo vya watu 148. Rais Moussa Traore akamatwa. Luteni Kanali Amodou Toumani Toure aongoza Baraza la upatanishi (Machi 17-27).<br>**Niger:** Mkutano wa taifa kuhusu mpito kuelekea katika demokrasia utafanyika (Septemba 19 – Novemba 3)<br>**Togo:** Maandamano mengi mitaani ya kudai mkutano wa taifa kuchunguza mpito kuelekea katika demokrasia (Machi hadi Juni) |

| | | |
|---|---|---|
| **Angola:** Sheria inayoanzisha mfumo wa vyama vingi (Machi 25)<br>**Burundi:** Matokeo ya sensa yanaonyesha kuwa mnamo Januari 16,1990 idadi ya watu ilikuwa 5,356, 266 yaani msongamano wa wakazi 207 kwa kilomita mraba, ambao ni wa juu kabisa Afrika. Rais Pierrre Buyoya athibitisha kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini (Mei 1)<br>**Cameroon:**Kifungu cha mahusiano ya kibalozi na Japan (Januari 28)<br>**Congo:** Mkutano wa taifa watafanywa kuanzisha **asasi** kidemokrasia (Februari 25)<br>**Equatoria Guninea:** Katiba mpya inayoanzisha mfumo wa vyama vingi yapitishwa (Novemba 22)<br>**Jamhuri ya Afrika ya Kati:** Kiongozi wa nchi atangaza kupitishwa kwa mfumo wa vyama vingi (Aprili 22)<br>**Zaire:** Ghasia na wizi wa ngawira vinaendelea Kinshasa. Utaratibu wa kidemokrasia unazuiwa (Septemba – Oktoba) | **Kenya:** Maaskofu wa Kiangalikana na Kikatoliki wanaanzisha wito wa kupendelea mfumo wa vyama vingi na kuheshimu haki za hinadamu (Aprili).<br>**Jamhuri ya Afrika Kusini** Serikali yatangaza Juni 30 kama siku ya kumalizika kwa ubaguzi wa rangi (Mei 28) inatangazwa kwamba Afrika Kusini itashiriki katika michezo ya ya Olimpiki ya'22 huko Barcelona (Novemba 6)<br>**Zambia:** Bw. Frebrick Chiluba anachaguliwa Rais wa Jamhuri (Novemba 2) kuanzisha asasi za kidemokrasia (Februari 25) | **Afrika:** Shirika la Umoja wa Mataifa la Sanyansi na Utamaduni (UNESCO) linatoa nishani ya Houphonet Boigry ya kutafuta amani kwa Nelson Mandela na Frederick de Klerk kwa pamoja (Januni 27)<br>Nchi zinazozungumza kifaransa: Mkutano wa 4 wa viongozi wa nchi zinazozungumza Kifaransa huko Paris. nchi za Kiafrika zahimizwa kuendelea na ujenzi wa demokrasia (Novemba 19-21).<br>**Maziwa Makuu:** Mkutano wa Maaskofu wa Kikatoliki wa Burundi, Rwanda Uganda, Tanzania na Zaire kujadili matatizo ya kijamii na kisiasa katika eneo la Maziwa Makuu(Oktoba 1)<br>**Umoja wa Nchi Huru za Afrika:** Kufunguliwa huko Bamako kwa mkutano wa mawaziri wa Umoja wa nchi Huru za Afrika kubusu mazingira hususani kutupwa kwa madawa ya sumu barani Afrika na nchi zenye viwanda (Januari 28) |

| | | |
|---|---|---|
| 1992 | **Algeria:** Maandamano makubwa dhidi ya Waislamu baada ya chama cha Kiislamu kushinda uchaguzi (Januari 2), kufutwa kwa Bunge kwa amri ya Rais (Januari 4). Kujiuzulu kwa Rais Chadli kwa kushinikizwa na jeshi (Januari 11) Kuundwa kwa kamati Kuu ya Taifa chini ya Uenyekiti wa Bw. Mohamed Boudiaf (Januari 14) ghasia kubwa katika vyuo vikuu, vyuo vikuu nchini vyafungwa (Februari 5 – Machi 4); hali ya hatari inatangazwa kwa miezi 12; FIS (Chama cha Ukombozi cha Kiislamu) kinavunjwa (Aprili 29); sheria mpya inaruhusu vitegauchumi vya kigeni hadi asilimia 49 katika migodi na mafuta (Novemba 16).<br>**Djibouti:** katiba mpya ya kuanzisha mfumo wa vyama vingi inapigiwa kura (Septemba 4)<br>**Misri:** Mashambuzlizi dhidi ya watalii yaliyofikiriwa kufanywa na kundi la Kiislamu (oKtoba – Desemba)<br>**Libya:** Baraza la Usalama la Umoja wa Matifa linapitisha Azimio la 738 la kuiwekea Libya vikwazo vya anga na kijeshi (Machi 31)<br>**Morocco:** Mikataba ya Ushirikiano na Brazili (Agosti 19)<br>**Somalia:** Umoja wa mataifa unaanzisha (ONUSOM)Jeshi kwa ajili ya kusimamia usalama na mahitaji ya chakula kwa ajili ya Somalia (Juni, Julai, Agosti). Azimio la 794 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linaunga mkono operesheni 'Rejesha Matumaini' likiwaandaa askari 40,000 kutoka nchi 20, wakiwemo Wamarekani 30,000 ili kuokoa wenye njaa (Desemba 3).<br>**Sudani:** Bei yapanda kwa asilimia 50 kwa bidhaa muhimu na kulegezwa kabisa kwa masharti kuhusu viwango vya kubadilisha fedha kama sharti la Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) (Februari 10); polisi waongezwa ili kutumiwa kwa sheria za Kiislamu. | **Gambia:** Sir Dawda Jawara achaguliwa Rais wa Jamhuri (Aprili 29).<br>**Mali** Alpha Oumar Konare achaguliwa Rais wa Jamhuri (Aprili 28); kutiwa saini mkataba wa kurekebisha uchumi na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)na Benki ya Dunia (Agosti 19).<br>**Mauritania:** Kanali Maosiya Ould Taya achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Januari 29)<br>**Niger** : Matokeo ya sensa: wakazi 7,200, 000<br>**Nigeria:** Matokeo ya sensa ya Novemba 1991: wakazi 88,5000,000 (Machi 19)<br>**Senegal:** Mashambulizi mapya ya Wacasamance wanaodai uhuru yasababisha vifo vya karibu watu 40 (Oktoba – Novemba)<br>**Sierra Leone:** Akiongoza jeshi, Kapteni Valentine Strasser, achukua Madaraka Freetown (Aprili 29)<br>**Togo:** Kuidhinishwa kwa katiba mpya inayoanzisha mfumo wa vyama vingi (Septemba 28); maandamano ya wanawake mjini Lome dhidi ya kukosekana kwa usalama na kutaka demokrasia (Januari 25) |

| | | |
|---|---|---|
| **Angola:** Ugeni wa Papa (Juni 1 – 8); Jamhuri ya watu wa Angola inakuwa Jamhuri ya Anmmmgola kutokana na uamuzi wa Bunge.<br>**Buruudi:** Baada ya uchaguzi, •katiba iliyopendekezwa inayoanzisha vyama vingi inapitishwa (Machi 10)<br>**Kameruni:** Bw. Paul Biya achaguliwa tena kuwa rais wa Jamhuri (Oktoba 23)<br>**Kongo:** Katiba mpya inapitishwa inayoanzisha uwingi wa kisiasa (Machi 15); Bw. Pascal Lissouba achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Agosti 16); mgogoro mkubwa wa kiserikali unasababisha vifo vingi (Novemba 19-Desemba 6) | **Madagascar:** Uidhinisho kwa njia ya kura ya maoni kwa katiba inayoanzisha vyama vingi (Agosti 19)<br>**Malawi:** Fujo na vurugu za kijamii kutaka serikali iwe ya kidemokrasia (Aprili 29 – Mei 24)<br>**Mauritius:** Nchi hii yawa Jamhuri (Machi 12).<br>**Namibia:** Namibia inakuwa mwanachama wa 105 wa GATT (Septemba 15) (kwa sasa Shirika la Biashara Duniani).<br>**Jamhuri ya Afrika Kusini** Uidbinisho kwa kura ya maoni kusitisha ubaguzi wa rangi (Machi 18)<br>**Tanzania:** Kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi (Februari 19); mji mkuu wa nchi unahamishwa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambayo iko katikati ya nchi (Septemba 10) | **Afrika:** Nelson Mandela na Frederik de Klerk wapokea kwa taadhima tuzo ya Felix Houphouet-Boigny kwa ajili ya kutafuta amani iliyotolewa katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (UNESCO) (Februari 3)<br>**Umoja wa Mataifa:** Uchaguzi wa naibu Waziri Mkuu wa Misri B. Boutros Ghali kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (Novemba 21) na Baraza Kuu (Desemba 3). Ni mara ya kwanza kwa nafasi hii kushikwa na Mwafrika.<br>**Ufaransa-Afrika:** Mkutano wa 17 wa viongozi wa nchi za Afrika zinazoongea Kifaransa unafanyika Libreville. Ufaransa inatangaza kuundwa kwa mfuko kwa ajili nchi zinazoendelea zenye pato la kati (Oktoba 5); Mkutano wa viongozi wa Ufaransa na nchi za Afrika huko Paris, Rais Francois Mitterand anazihimiza nchi za Kiafrika kufanya serikali zao kuwa za kidemokrasia na anaomba nchi tajiri kupunguza mzigo wa madeni kwa nchi maskini (Novemba 19-21)<br>**Shirika la Kiislamu Duniani ICO:** Mkutano wa Shirika la Kiislamu Duniani huko Dakar wakati ambapo Saudi Arabia ilifuta madeni ya nchi maskini (Desemba 9-12).<br>**Namibia:** Nchi kumi za Ukanda zinatia saini mkataba wa kuanzisha COMESA, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Agosti 17)<br>**Senegal:** Jiwe la kwanza la kumbukumbu ya Gore-Alma-dies linawekwa kwa kumbukumbu ya biashara ya watumwa na Bw. Abdou Diouf rais na Jamhuri ya Senegal mbele ya viongozi wa nchi na serikali walioshiriki katika mkutano wa 28 wa viongozi wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika. Bw. B. Boutros-Ghali, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Federiko Mayor, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la (UNESCO) Umoja wa Mataifa la Science na Utamaduni, mhubiri wa Kimarekani Jesse Jackson na Amadou Moktar Mbow, Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa UNESCO na Rais wa Kamati ya Taifa ya Makumbusho. |

| | | |
|---|---|---|
| 1993 | **Tunisia:** Mikataba miwili ya kiuchumi na mmoja kuhusu ushirikiano katika viwanda inatiwa Saini na Brazil (Januari 30); hatua za kupendelea wanawake kwenye sheria za kuvunjika ndoa (Agosti 13)<br>**Algeria:** Algeria yatambua uhuru wa Eritrea (Mei 4); kuongezeka kwa ghasia za kigaidi na mashambulizi dhidi ya raia kwa mwaka mzima vilivyofanywa na vikundi vya Kiislamu.<br>**Djibouti:** Bw. Hassan Gouled achaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri (Mei 7).<br>**Misri:** Kuchaguliwa tena kwa Rais Moubarak (Oktoba 4 - 5)<br>**Eritrea:** Kutangazwa kwa uhuru wa nchi (Mei 24); mnamo Mei 28, ikawa mwanachama wa Umoja wa Mataifa; na Juni 5, ikawa mwanachama wa 52 wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU)<br>**Ethiopia:** Kura ya maoni kuhusu uhuru wa Eritrea (Mei 22-23)); Ethiopia yaitambua rasmi Eritrea mnamo Mei 3 **Libya**: Libya yaambua rasmi uhuru wa Eritrea (April 29; Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linapiga kura kwa ajili ya vikwazo vipya dhidi ya Libya, kuzuiliwa kwa fedha za Libya zilizo nje ya nchi, vikwazo dhidi ya vifaa vya kuchimba mafuta (Oktoba 11); mikataba ya ushirikiano inatiwa saini na Ethiopia na Niger (Desemba 23)<br>**Sudani:** Mkutano wa Tume ya pamoja ya Sudani na Jamhuri ya Afrika ya Kati kuhusu usalama mipakani na mapambano dhidi ya magendo (Januari 27); Papa atembelea Khartoum; kubarikiwa kwa mtumwa wa Kisudani, Mama Bakhita (Februari 10); matokeo ya sensa ya Aprili 1993; wakazi 24,940,000 (Agosti 21).<br>**Tunisia:** Tunisia yaondoa kikwazo dhidi ya Benki za Afrika Kusini (Oktoba 19) | **Cote d'Ivorre:** Kifo cha Rais Houpheout Boigny (Desemba 7). Bw. Henri Konan Bedie, rais wa Bunge, anatangazwa kuwa Rais wa Jamhuri wa muda kabla ya uchaguzi kufanyika.<br>**Gambia:** Sheria inayopiga marufuku adhabu ya kifo inapitishwa (Aprili 7).<br>**GuineaConakry:** Jenerali Lansana Conte achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Desemba 23).<br>**Niger:** Mahamane Ousmane achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 27).<br>**Nigeria:** Katika uchaguzi wa Rais, Bw. M.K.O. Abiola ashinda katika majimbo 11 na katika mji mkuu. Matokeo haya yanafutwa Juni 23 kutokana na uchochezi wa wanaounga mkono serikali ya kijeshi. |

| | | |
|---|---|---|
| **Burundi:** Bw. Melchior Ndandaye achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Juni 3). Anaangushwa kwa mapinduzi ya kijeshi Oktoba 21 na kifo chake kinatangazwa siku mbili baadaye.<br>**Kongo:** Makabiliano ya ghasia baina ya jeshi na vikundi vya upinzani yenye silaha (Oktoba 15-Desemba 14);<br>**Gabon:** Matokeo ya Sensa; Wakazi 1,011,710 (Oktoba 17); Rais Omar Bongo achaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri (Desemba 5);<br>**Jamhuri ya Afrika ya Kati:** Bw. Ange Felix Patasse achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Septemba 1). | **Malawi:** Wanaounga mkono mfumo wa vyama vingi washinda katika kura ya maoni (Juni 14-16). | **Algeria na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni** (UNESCO): Hatua kuhusiana na mauaji: Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO atoa mwito wa kuundwa kwa kituo cha uchunguzi wa ghasia (Desemba 13).<br>**CEDEAO** (Jumuiya ya Uchumi na Forodha ya nchi za Afrika Magharibi): Kutiwa sahihi mkataba mpya unaotoa haki kwa jumuiya hii kuingilia migogoro ya kisiasa katika eneo hili (Julai 24).<br>**Jamhuri ya Afrika Kusini:** Tuzo ya Amani la Nobel ilitolewa kwa Frederik de Klerk na Nelson Mandela (Oktoba 15); katiba ya kwanza ya baada ya ubaguzi Afrika Kusini inapigiwa kura Bungeni (Desemba 22) |

| | | |
|---|---|---|
| 1994 | **Algeria:** Wágeni wengi wauawa kiasi kwamba Balozi zinawashauri raia wao kuondoka nchini humo (Machi); thamani ya dinari, yapunguzwa kwa asilimia 40.17 (Aprili 9).<br>**Eritrea:** Nchi hii inajiunga na Shirika la Fedha la Kimataifa (Julai 6).<br>**Libya:** Kalenda inayofuata kuonekana kwa mwezi inapitishwa (Januari 4); Mkutano Mkuu wa Watu unaamua kutumia **Sharia,** au Sheria ya Kiislamu (Januari); Mahakama ya Dunia inatambua ukanda wa Aouzou kama mali ya Chad; mkataba wa ushirikiano na Zimbabwe unatiwa sahihi (Julai 17). Tuzo ya Haki za Binadamu ya Kadhafi ya Dola za Kimarekani 250,000 inatolewa kwa Umoja wa Haki za Binadamu barani Afrika (IUDH) (Agosti 21).<br>**Moroko:** Uhusiano wa kibalozi na Madagascar unaanzishwa na (Aprili 15); Mkutano wa kwanza kuhusu haki za watoto (Mei 25-27); uhusiano wa kibalozi na Eritrea unaanzishwa (Mei 30); Kiberiberi kinafundishwa shuleni (Agosti 20).<br>**Somalia:** Operesheni 'Rejesha Matumaini' inasitishwa Mei 3,<br>na nafasi yake kuchukuliwa na ONUSOM II; Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linatangaza tarehe ya<br>mwisho ya ONUSON kuwa Novemba 4.<br>**Sudan**: Gaidi 'Carlos' arejeshwa Ufaransa (Agosti 15); Matokeo ya sensa: wakazi<br>milioni 25.<br>**Tunisia:**Kutiwa sahihi mpango wa ushirikiano na<br>Indonesia kuhusu kukuzwa kwa dhima ya wanawake (Januari 28); wanawake, wasomi na viongozi wa Tunisia (walaani kuvurugwa kwa uhuru (Mei 4) | **Gambia:** Rais Dawda Jawara anapinduliwa na jeshi likiongozwa na Luteni Yaya Jammeh (Julai 26).<br>**Guinnea-Bissau:** Bw. Joao Bernardo Vieira achaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri (Agosti 20).<br>**Guinea-Conakry**: Guinea yawa mwanachama wa 125 wa Shirika la Biashara Duniani.<br>**Liberia**: Mkutano wa taifa unawasilisha mpango wa kurejesha amani na kuvinyang'anya silaha vikundi vinavyopigana (Oktoba 9).<br>**Nigeria**: Mkutano wa Taifa wa Katiba unapiga kura kukubali mfumo wa vyama vingi na kwa nafasi ya Rais kubadilishana kati ya Kaskazini na Kusini (Oktoba 7).<br>**Togo**: Vyama vya upinzani vinashinda uchaguzi wa Bunge (Machi 14); Rais Gnassingbe Eyadema achaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri (Septemba 9). |

| | | |
|---|---|---|
| **Burundi:** Sylvestre Ntibatunganya anachaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Septemba 30). **Cameroon/Nigeria:** Nchi mbili hizi zinaingia katika mgogoro wa mpaka kuhusu ghuba ya Bakassi (Machi 31). **Chad:** Libya inarejesha ukanda wa Aouzou kwa Chad baada ya kuikalia kwa miaka 25 (Mei 30). **Rwanda:** Ofisi ya Msaada wa Umoja wa Mataifa kwa Rwanda yazinduliwa rasmi (Novemba 1); Maraisi - wa Burundi na Rwanda wauawa kwenye ajali ya ndege (Aprili 6); mapigano baina ya majeshi ya serikali na ya wapigaji wa RPF. Mauaji ya halaiki yanaenea nchini kote na kufikia karibu watu milioni (Aprili 12 - Juni 14). Wapiganaji wa RPF wanateka Kigali (Julai 6), mchungaji Bizimungu anateuliwa kuwa Raisi wa Jamhuri (Julai 19). | **Kenya**: Matokeo ya karibuni kabisa ya sensa: wakazi milioni 25 (Machi 12). **Malawi**: Bw. Bakili Muluzi anachaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Mei 22) **Namibia:** Afrika Kusini inatambua mamlaka ya Namibia juu ya Walvis Bay, iliyotawaliwa kwa miaka 84 na Pretoria (Februari 28). **Jamhuri ya Afrika Kusini**: Uchaguzi wa kwanza usiokuwa wa kibaguzi. Chama cha ANC kinashinda, mnamo Mei 9, Nelson Mandela atangazwa kuwa Raisi wa Jamhuri. Mnamo Mei 23, Jamhuri ya Afrika Kusini inakubaliwa kuwa mwanachama wa 53 wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Pretoria inarejeshewa kiti chake katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. (Juni 16) | **CEAO** (Jumuiya ya Kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi): Jumuiya inavunjwa (Machi 13) kufuatia kuundwa kwa UEMOA (Umoja wa Kiuchumi na Kifedha wa nchi za Afrika Magharibi mnamo Januari **Eneo la Faranga**: kupunguzwa thamani kwa faranga ya CFA kwa asilimia 50 na kupunguzwa kwa thamani ya faranga ya Komoro kwa asilimia 33 (Januari 12). **Umoja wa Nchi Huru za Afrika:** Utafiti wa umoja huu unaonyesha kwamba bara hili lina wakimbizi milioni 7 na watu walioondolewa katika makazi yao milioni 15 (Februari 17). **Kusini mwa Afrika:** Soko la Pamoja Kusini Mashariki mwa Afrika (COMESA) lazinduliwa rasmi, likijumuisha nchi 22 (Desemba 8). **UDEAC** (Umoja wa Kiuchumi na Forodha wa nchi za Afrika ya Kati): Viongozi wa nchi wanatia sahihi huko Njamena mkataba wa kuanzisha jumuiya ya kiuchumi na kifedha Afrika ya Kati (Machi 16). **UNESCO:** Tuzo ya Houphouet-Boigny kwa juhudi za kutafuta amani mwaka 1993 inatolewa kwa Kiongozi wa Palestina Yasser Arafat, Bw. Y. Rabin Waziri Mkuu wa Israel na Bw. S. Peres Waziri wa mambo ya nje wa Israeli na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO mbele ya Abdou Diouf, Rais wa Senegal na Henri Konan Bedie; Rais wa Cote d'Ivoire (Julai 5). |

| | | |
|---|---|---|
| 1995 | **Algeria**: Mkutano wa vyama vya upinzani vya Algeria huko Roma kujadili suluhisho la vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea nchini (Januari 8); kifo cha mwandishi Rachid Mimouni (Februari 13); shambulio la treni ya chini ya ardhi huko Paris lililofikiriwa kufanywa na vikundi vya Kiislamu vyenye silaha, watu 7 walifariki na zaidi ya 80 kujeruhiwa (Julai 25); kuidhinishwa kwa Mkataba wa kupiga marufuku silaha za sumu (Agosti 16); uchaguzi wa Liamine Zeroual kama Rais wa Jamhuri (Novemba 29).<br>**Misri:** Balozi wa kwanza wa Afrika Kusini ateuliwa Cairo (Machi 7); kutengenezwa kwa Nile Sat, setlaiti ya kwanza ya Misri (Mei 29).<br>**Libya:** Kufukuzwa kwa raia 1, 117,000 kutoka nchi 11 za Afrika kwa sababu ya mgogoro wa kiuchumi (Oktoba 4 – Novemba 24).<br>**Morocco:** Sensa: milioni 26, kiwango cha ongezeko cha asilimia 2.6, wakazi wa mjini asilimia 51.4 (Januari 8); Hassan wa II azindua Chuo Kikuu kinachotumia Kiingereza huko al-Akhawayne d'Ifrante (Januari 16); Balozi wa kwanza ma Morocco Afrika Kusini ateuliwa (Februari 4)<br>**Sudan:** Kuanza tena kwa ushirikiano wa kijeshi baina ya Kartoum na Moscow, uliokuwa umeachwa tangu 1971 (April 6)<br>**Tunisia**: Pretoria na Tunis zatia sahihi mikataba miwili ya ushirikiano (Aprili 4-7); wanawake wadai elimu kama masharti ya uhuru wa jinsia zote (Novemba 20) | **Benin:** Upinzani dhidi ya serikali ya Nicephore Soglo unashinda uchaguzi wa wabunge (Aprili 3)<br>**Burkina Faso:** Kuzinduliwa huko Ouagadougou kwa maktaba ya kwanza wa filamu Afrika kusini mwa Sahara (Machi 1)<br>**Cote d'Ivoire:** Bw. Konan Bedie achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Oktoba 23)<br>**Mauritania :** Wanawake waandamana huko Nouakchott kupinga kuongezeka kwa bei ya mkate na kudai kuachiwa huru kwa viongozi wa upinzani (Januari 24).<br>**Niger :** Vyama vya upinzani vyashinda uchaguzi wa Bunge (Januari 15) |

| | | |
|---|---|---|
| **Burundi:** Umoja wa Mataifa waanzisha tume ya kimataifa ya uchunguzi kuhusu mauaji ya halaiki yaliyofanyika mnamo 1993 huko Burundi (Agosti 29)<br>**Kameruni:** Katiba mpya inaanzisha serikali ya rais asiye na mamlaka yote na mabunge mawili (Desemba 21)<br>**Sao Tome na Principe:** Kisiwa cha Principe chapata serikali yake (Aprili 29); wanajeshi waasi wapanga mapinduzi na kumtia mbaroni Rais Miguel Trovoada lakini wanarejesha mamlaka mara jumuiya ya kimataifa ilipotishia kusitisha misaada yote (Agosti 15-22) | **Visiwa vya Komoro:** Majaribio ya mapinduzi yakiongozwa na mamluki wa Kifaransa Bob Denard. Ufaransa inaingilia kati kuyazima (Septemba 28 Oktoba 4)<br>**Lesotho:** Baada ya kuondolewa kwa miaka 5, Mfalme Moshoeshoe anarejeshwa madarakani na jeshi (Januari 25)<br>**Tanzania** Bw. Benjamini Wiliam Mkapa anachaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Novemba 21) | **Jumuiya ya Madola:** Mnamo Novemba 12, Msumbiji ilijiunga na Jumuiya ya Madola wakati wa mkutano wa viongozi huko Aukland. Mkutano huo wa viongozi pia ulishuhudia kuingizwa kwa Cameroon na kurejea kwa Afrika Kusini.<br>**Misri :** Mkutano huko Cairo wa wataalamu wa Afrika na wa nchi za Magharibi kuchunguza uundaji wa jeshi la kutunza amani katika Afrika (Januari 9).<br>**Jumuiya ya Ulaya/ ACP:** Kupitiwa kwa mkataba wa Lome IV. Mkataba unatoa msaada kuanzia sasa kwa sharti kwamba taratibu za kidemokrasia zinaheshimiwa (Novemba 4).<br>**Ukanda wa sarafu ya Faranga :** Nchi kumi na moja katika ukanda wa sarafu ya Faranga zapitisha huko Bangui, sheria inayosanifisha sheria za biashara (Februari 10).<br>**Umoja wa Nchi Huru za (OAU) Afrika :** Mkutano huko Tunis wa Chombo Kikuu cha kuzuia, kusimamia na kusuluhisha migogoro kujadili migogoro inayoendelea huko Augola, Burundi, Liberia, Rwanda, Sierra Lone na Somalia (Juni 19 – 21).<br>**Afirka Kusini :** Ziara ya 1l ya Papa barani Afrika huko Afrika Kusini (Septemba 14)<br>**Umoja wa Mataifa :** Mkutano huko Cairo kuhusu mauaji ya kupangwa, ubadhirifu na biashara ya binadamu (Aprili 29) |

| | | |
|---|---|---|
| 1996 | **Algeria** : Katiba mpya inapiga marufuku kuunda vyama vya siasa vyenye misingi ya kidini (Oktoba 22-Novemba 28) ; sheria inapitishwa inayofanya lugha ya Kiarabu kutumika kila mahali (Desemba 17) ; kutekwa na kuuawa kwa Watawa saba wa Trrap huko Tiberine (Machi 27-Mei 30).<br>**Misri** : Mikataba ya ushirikiano wa kisayansi, kiteknolojia na kiutamaduni na Afrika Kusini (Aprili 10-11) ; Shirika la Umoja wa Mataifa wa Mipango ya Maendeleo (UNDP) linaona kwamba ukuaji unazorota kutokana sera za marekebisho za Shirika la Fedha la Kimataifa (Aprili 23) ; kituo cha mafunzo kwa wanaoweza kushiriki katika jeshi la kulinda amani kinafunguliwa (Juni 3) ; ukeketaji unapigwa marufuku hospitalini (Julai 18) ; kesi za kundi la Kiislamu tangu 1982, 83 wahukumiwa kifo na miongoni mwao 54 wamekwishanyongwa (Oktoba 1).<br>**Morocco** : Kuidhinishwa kwa mkataba unaopiga marufuku silaha za kemikali (Januari 4) ; kuundwa huko Rabat kwa mahakama ya Kiarabu ya jefule dhidi ya wanawake (Desemba 2).<br>**Somalia** : Huko Nairobi mkataba wa amani unatiwa sahihi na makundi matatu katika vita vya wenyewe kwa wenyewe (Oktoba 15)<br>**Sudan** : Jenerali El-Bechir achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 22).<br>**Tunisia** : Kuidhinishwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za mtoto (Januari 11) ; Papa azuru Tunis (April 14). | **Benin** : Jenerali Mathew Kerekou anachaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Aprili 24).<br>**Cape Verde** : Antonio Mascarenhas Monteiro anachanguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Februari 19).<br>**Cote d'Ivorie** : Mnamo 1995, Taasisi ya Taifa ya Takwimu inatathmini idadi ya watu nchini kufikia wakazi 14,208,000 (Januari 11).<br>**Gambia** : Kanali Yaya Jammeh ashida uchaguzi wa Rais (Mei 27).<br>**Ghana** : Kapteni Jerry Rawlings anashinda uchaguzi wa Rais kwa mara ya pili (Desemba 10).<br>**Guinea-Bissau** : Guinea Bissau yakubaliwa kujiunga na ukanda wa sarafu ya faranga kuanzia Mei 2.<br>**Liberia** : Mkataba wa kuacha mapigano kati ya viongozi wa makundi (Julai 31) ;<br>Ruth Sando Perry ateuliwa Rais wa Baraza la taifa mamlaka ya muda ya kuongoza nchi (Agosti 17).<br>**Niger** : Mnadhimu Mkuu wa Majeshi, Kanal Barre Mainassara atangaza kuondolewa kwa Rais wa Jamhuri na serikali (Januari 27) ; Jenerali Mainassara ashinda uchanguzi wa rais (Julai 7).<br>**Sierra Leone** : Kapteni Strasser anapinduliwa na majeshi yakiongozwa na Jenerali Maada Bio (Januari 17) ; serikali ya kijeshi inakutana na wapiganaji wa chinichini kwa lengo la kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu kwa miaka mitano (Januari 26)<br>Mnamo Machi 17, Bw. Ahmad Tejan Kabbah achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri. Mnamo Aprili 23, mktaba wa kuacha mapigano na waasi; mnamo Novemba 30 huko Abidjan Rais Kabbah atia sahihi mkataba wa amani na Koplo Foday Sanko, na hivyo kumaliza vita vya zaidi ya miaka mitano. |

| | | |
|---|---|---|
| **Burundi:** Mapinduzi ya kijeshi. Aliyekuwa rais zamani Buyoya achukua nafasi ya Sylvestre Ntibatunganya (Julai 25).<br>**Chad**: Rais Idris Derby ashinda uchaguzi wa rais (Julai 11).<br>**Jamhuri ya Afrika ya Kati:** Uasi wa Kijeshi wasababisha makabiliano ya jeshi na serikali Aprili 10-Juni 6).<br>**Sao Tome na Pincipe:**<br>Rais Miguel Trovaoda anachaguliwa tena (Septemba 3).<br>**Uganda**: Yoweri Museveni achaguliwa Rais wa Jamhuri miaka kumi baada ya kuchukua mamlaka kwa nguvu (Mei 11).<br>**Zaire**: Vita katika jimbo la Kivu waasi walipojiunga kuunda AFDL au majeshi ya kidemokrasia ya kuikomboa Congo yakiongozwa na Laurent Desire Kabila na kudai kujiuzulu kwa Rais Mobutu (Septemba 21-Desemba) | **Visiwa vya Comoro**:<br>Bw. Mohammed Taki Abdoulkarim achanguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 16).<br>**Lesotho**: Mwana wa Mfalme David Mohato Beeng Seeiso achukua kiti cha enzi kufuatia kifo cha baba yake katika ajali (Januari 18).<br>**Madagascar**: Albert Zafy, Rais wa Jamhuri ananyang'anywa mamlaka na mahakama kuu ya Katiba ambayo inathibitisha kuondolewa kwake kwa kura na Bunge mnamo Julai.<br>**Jamhuri ya Afrika Kusini**: Katiba mpya inapitishwa na kusitisha sheria zilizorithiwa kutoka katika mfumo wa ubaguzi (Mei 8).<br>**Zimbabwe**: Bw. Robert Mugabe achaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri (Machi 19). | **Afrika**: Nchi 53 za Afrika zinatia sahihi huko Cairo, mkataba wa kuunda ukanda usiokuwa na silaha za nyuklia (Aprili 11).<br>**Ufaransa-Afrika**: Mkutano wa 19 wa viongozi wa Ufaransa na Afrika unafunguliwa Ouagadougou. Rais wa Ufaransa Jacques Chirac aeleza dhana yake ya 'utawala bora' (Novemba 5).<br>**Umoja wa Mataifa**:<br>Baraza Kuu la moja wa Mataifa lamteua Mghana Kofi Annan kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (Desemba 17)<br>**Umoja wa Nchi Huru za Afrika:** Mkutano wa 32 wa viongozi wa Umoja unafanyika kujadili migogoro iliyoikumba Afrika (Julai 6).<br>**Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**: Jumuiya hii inaiunda huko Gaberone kamati ya usalama kwa ajili ya kulinda amani katika kanda **UEMOA**: Ushuru na Forodha unapitishwa (Januari 15); nchi saba wanachama zina kiwango cha ukuaji cha asilimia 5.8 cha Pato lao la Ndani. |

| | | |
|---|---|---|
| 1997 | **Algeria**: Kuongezeka kwa ghasia wakati wa Ramadhani, mamia ya wanavijiji wanauawa na wanaofikiriwa kuhusika ni vikundi vya Kiislamu (Januari-Machi).<br>**Morocco**: Kuchukua lugha mbili ni lazima katika kiwango cha Chuo Kikuu (Machi 6). | **Liberia**: Kiongozi wa vita Charles Taylor ashinda uchaguzi wa rais (Agosti 2) baada ya miaka minane ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoua zaidi ya watu 200,000 na kusababisha watu zaidi ya milioni kuwa wakimbizi au walioondolewa makwao.<br>**Nigeria**: Ikiwa imezungukwa na nchi zinazozungumza Kifaransa, Nigeria inajiandaa kuanza kutumia Kifaransa kama lugha rasmi ya pili. (Januari 1); kifo cha mwanamuziki Fela Anikulapo Kuti, aliyebuni mtindo wa Afro-beat inayojumuisha mitindo ya high life, jazz, funk na blues (Agosti 2)<br>**Sierra Leone**: Mapinduzi ya kijeshi yakiongozwa na J.P. Koroma anayemwondoa Rais Tejan Ahmad Kabbah (Mei 25) |

| | | |
|---|---|---|
| **Angola**: Serikali inadhibiti mikoa ile iliyokuwa ikitawaliwa na waasi wa UNITA (Februri 19). **Jamhuri ya Afrika ya Kati**: Mkataba wa Bangui wa kuingilia kati na kusimamia, mpango (MISAB), mapigano baina ya waasi na jeshi la serikali (Januari-Februari). **Zaire**: Waasi wanatuibia shaba (Februari 4); mji wa Kisangani unatekwa na waasi wa AFDL (Machi 15), askari wa AFDL wanaingia Kinshasa (Mei 16); siku inayofuata Laurent Desire Kabila atangazwa raisi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, jina jipya la Zaire. | **Madagascar**: mkuu wa jeshi la wanamaji Didier Ratsiraka anashinda uchaguzi wa rais (Januari 4). | Mkutano wa Kimataifa kuhusu demokrasia katika kanda ya maziwa makuu huko Montreal (Januari 20). |

barani, mkataba wa Abuja wa Juni 3, 1991 uliunda Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika (AEC) ambayo ilibuni wazo kuu: Bunge la Afrika yote.

Nguvu ya asasi hizi zimo, kwa upande mmoja, katika kujalizana kwa rasilimali na mabadilishano baina ya nchi ambayo huweza kuzalishwa na asasi hizi, na kwa upande mwingine, ni moyo wa washirika wa kiuchumi kutegemea uwezo wa ndani wa nchi za Afrika. Pamoja na udhaifu wa kimuundo katika uchumi wa Afrika, lakini kwa kuzingatia juhudi katika usimamizi ulioanzishwa na asasi za fedha za kimataifa na mipango mipya kuhusu bei ya malighafi, mnamo 1995 kukua kwa uzalishaji wa jumla kulifikia kiwango chake cha juu kabisa katika miaka sita. Ili kufanya ukuaji huu udumu Afrika haijapungukiwa kwani ina utajiri wa kilimo, hifadhi ya migodi, rasilimali ya watu na kuongezcka kwa idadi ya watu. Lakini maendeleo hayawezi kupatikana bila amani. Hivyo, Waafrika wanajaribu kuwavutia wawekezaji kwa kuweka miundo ya kinga na kudhibiti migogoro kwa namna itakayokomesha vita na jamii za nchi za Kiafrika kufaidi utulivu. Huko Afrika magharibi kuna Jeshi la Afrika la kulinda amani (ECOMOG) lililoundwa kutokana na nchi za CEDEAO. Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) nao unafikiria namna ya kuunda shirika la kulinda, kusimamia na kusuluhisha migogoro.

Pamoja na maovu yaliyoikumba Afrika (kutoendelea, vita vya wenyewe kwa wenyewe, migogoro mikubwa ya kijamii), miali ya matumaini imeanza kuonekana tangu 1994: kukua kwa uchumi kunaonekana katika nchi kadhaa, taratibu za kidemokrasia zimeanzishwa kote barani na wazo la kuunda makundi ya nchi zinazoshirikiana vinaipatia Afrika imani ya kutegemea rasalimali zake. Ni jambo muhimu kwamba kuteuliwa kwa Waafrika wawili katika nafasi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kunatokea wakati mmoja na juhudi hizi mpya ambazo ziko katika ajenda kila mahali. Nafasi ya Boutros Boutros Ghali wa Misri ilichukuliwa na Kofi Annan kutoka Ghana, nchi ambayo iliongoza moyo wa umajumui wa Afrika, kuimarika kwa uchumi na uwazi wa kidemokrasia. Hapana shaka uteuzi wake unaibua matumaini haya mapya kwamba Afrika itashika nafasi yake miongoni mwa mataifa na watu. •

# *Wanakamati wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

*Tarehe zilizotajwa zinawakilisha tarehe za wanachama.*

Profesa J.F.Ade Ajayi
(Nigeria), tangu 1971
Mhariri Juzuu VI

Prof. F.A. Albuquerque Mourão
(Brazil), tangu 1975

Profesa D. Birmingham
(Uingereza), tangu 1985

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971-8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dakta (Bibi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Hayati Profesa D. Chanaiwa
(Zimbabwe), tangu 1975;
alifariki 1993

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

Hayati H.E.M. El Fasi
(Morocco), tangu 1971; alifariki 1991
Mhariri Juzuu III

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971- 81 (alijiuzulu)

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa Dakta V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Hayati Profesa E. Haberland
(Ujerumani Magharibi), tangu 1971; alifariki 1992

Dakta Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

Hayati H.E.A. Hampâté Bâ
(Mali), 1971 - 8; (alijiuzulu); alifariki 1991

Dakta I.S. El-Hareir
(Libya), tangu 1978

Profesa M. Difuila
(Angola), tangu 1978

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal),1971- 86; alifariki 1986

Hayati AbbéAlexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I na IV

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dakta A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dakta G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975

Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa Bethwell A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Ravoajanahary
(Madagascar), tangu 1971

Hayati Dakta I. Hrbek
(Czechoslovakia), tangu 1971; alifariki 1993
Mhariri Msaidizi Juzuu III

Dakta (Bibi) A. Jones

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dakta E. Williams
(Trinidad na Tobago), 1976-8;
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo Mwanakamati

Profesa C. Wondji (Côte d'Ivoire)
Mhariri Msaidizi Juzuu VIII
Siyo Mwanakamati

*Ukatibu wa Kamati ya*
*Kimataifa ya Kisayansi*
A. Gatera
Kitengo cha Taaluma za Utamaduni na Sera
1, rue Miollis
75015 Paris

# Wasifu wa Waandishi

| | |
|---|---|
| SURA YA 1 | Ali A. Mazrui (Kenya); Mtaalamu wa sayansi ya siasa na taaluma za kimataifa; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu historia ya sasa ya Afrika; Mkurugenzi, Taasisi ya Taaluma ya Utamaduni wa Kimataifa, Chuo Kikuu cha Taifa cha New York, Binghaton; Profesa wa Albert Schweitzer, Chuo Kikuu cha New York; Profesa wa Albert Luthuli, Chuo Kikuu cha Jos, Nigeria, Profesa wa Andrew D. White, Chuo Kikuu cha Ithaca, New York. |
| SURA YA 2 | T. Chenntouf (Algeria); Mtaalamu wa historia ya Algeria na Magharibi; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu somo hili, Mkurugenzi wa Sehemu ya Utafiti wa Historia kuhusu Algeria, Afrika Magharibi na Mediterani, Chuo Kikuu cha Oran. |
| SURA YA 3 | M. Diop (Senegal); Mtaalamu wa historia ya Afrika Maghreb; Mchunguzi, Taasisi ya Sayansi ya Jamii, Bamako, Mali, Mwanakemia, kiongozi wa sasa. |
| | D. Birmingham (Uingereza); Mtaalamu wa historia ya nchi zinazozungumza Kireno Afrika na Afrika ya Kati, alikuwa Mkuu wa Taaluma za Afrika, Chuo Kikuu cha London, Profesa na Historia ya Sasa, Chuo Kikuu cha Canterbury. |
| | I. Hrbek (Chekoslovakia), Mtaalamu wa Historia ya Kiarabu, Kiafrika na Kiislamu. Mchunguzi kwenye taasisi ya Taaluma ya Kiarabu, Prague; Mshauri wa kisayansi kwenye Akademia ya sayansi ya Chekoslovakia. |
| | A. Margarido (Ureno); Mtaalamu wa historia ya nchi zinazozungumza Kireno Afrika.<br>D.T. Niane (Senegal); Mtaalamu wa Mande; alikuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya L.S. Senghor. |
| SURA YA 4 | M. Crowder (Uingereza); Mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi Amefariki. |
| SURA YA 5 | Ali A. Mazrui (Kenya) |
| SURA YA 6 | I.Herbek (Chekoslovakia) |
| SURA YA 7 | J. Suver –Canale (Ufaransa), Mtaalamu wa historia kabla na wakati wa ukoloni Afrika Magharibi; hususan Guinea |
| | A.Adu Boahen (Ghana); Mtaalamu wa historia ya ukoloni ya Afrika Magharibi. Alikuwa Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Ghana. Amestaafu. |
| SURA YA 8 | E.M'Bokolo (Jamhuri ya Watu wa Kongo)., Mtaalamu wa historia ya Afrika. |
| SURA YA 9 | M. Twaddle (Uingereza), Mtalaamu wa historia ya Afrika ya Mashariki<br>L. Rabearimanana (Madagaska), Mtaalamu wa historia ya Madagaska karne ya kumi na tisa na ya ishirini. |
| | I.Kimambo (Tanzania); Mtaalamu wa historia ya Tanzania, Profesa wa Historia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. |

| | |
|---|---|
| SURA YA 10 | D. Chaiwa (Zimbabwe), Mtaalamu wa historia ya Kusini mwa Afrika |
| SURA YA 11 | C. Coquery-Vidrovitch (Ufaransa), Mtaalamu wa historia ya Afrika. |
| SURA YA 12 | M. Owusu (Ghana), Mtaalamu wa mabadiliko ya Afrika kijamii, kisiasa na kiuchumi. |
| SURA YA 13 | P. Kipre (Côte d'Ivoire). Mtaalamu wa historia ya Afrika Magharibi |
| SURA YA 14 | A. Adedeji (Nigeria) mchumi, alikuwa Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Katibu Mtendaji waTume ya Uchumi ya Afrika, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Afrika cha Taaluma za Maendeleo na Mikakati, Ijebu-Ode, Niger. |
| SURA YA 15 | J.I. Elaigwu (Nigeria), Mtaalamu wa maendeleo ya kisiasa Afrika.<br>Ali A. Mazrui (Kenya) |
| SURA YA 16 | J. Ki-Zerbo (Burkina Faso) mtaalamu wa historia ya Afrika, Profesa, Chuo Kikuu cha Dakar<br><br>Ali A. Mazrui (Kenya)<br>A. Wondji (Cotede 'Ivoire),Mtaalamu wa historia<br>A. Adu Boahen (Ghana) |
| SURA YA 17 | T. Tshibangu (Kongo), kasisi, mtaalamu wa utamaduni<br>J.F. Ade Ajayi (Nigeria)<br>L. Sanneh (Gambia) |
| SURA YA 18 | A.I. Sow (Ufaransa), Mwanaisimu<br>M.H. Abdulaziz (Kenya), Mwanaisimu |
| SURA YA 19 | Ali Mazrui (Kenya)<br><br>M.de Andrade (Angola), Mwanaelimu-jamii, mshairi, mwanasiasa, mwandishi. Amefariki<br><br>M. Alaoui Abdalaoui (Moroko), mwanafasihi<br>D.P. Kunene (Afrika ya Kusini); mwanafasihi<br>J. Vansina (Ubelgiji), mtaalamu wa historia |
| SURA YA 20 | J. Vansina (Ubelgiji) |
| SURA YA 21 | Ali A. Mazrui (Kenya)<br>J.F. Ade Ajayi (Nigeria)<br>A. Adu Boahen (Ghana)<br>T. Tshibangu (Zaire) |
| SURA YA 22 | Aklilu Habte (Ethiopia) mtaalamu wa elimu<br>Teshome Wagaw (Marekani), mtaalamu wa elimu |
| SURA YA 23 | J.E. Harris (Marekani) Mtaalamu wa historia<br>S. Zeghidour (Algeria) mwandishi na mtafiti |

| | |
|---|---|
| SURA YA 24 | S.K.B. Asante (Ghana)<br>D.Chanaiwa (Zimbabwe) |
| SURA YA 25 | D. Chanaiwa (Zimbabwe)<br>E. Kodjo (Togo) mtaalamu wa uchumi |
| SURA YA 26 | Chinweizu (Nigeria) mwandishi, mshairi, mwana historia |
| SURA YA 27 | Iba Der Thiam (Senegal)<br>J. Mulira (Uganda)<br>C.Wondji (Cote d' Ívoire) |
| SURA YA 28 | L. Edmodson (Jamaica) |
| SURA YA 29 | E.K. Kouassi (Togo) |
| SURA YA 30 | Ali K. Mazrui |

# BIBLIOGRAFIA

**Abalogu, U.N., Asiwaju, G.** na **Amadi-Tshiwala, R.** (wah.) (1981) *Oral Poetry in Nigeria* (Lagos: Nigeria Magazine).

**Abba, I. A.** (1985) 'Changing patterns of local authority and the evolution of the District Head system in Gombe Emirate, 1830-1960' (Tasnifu ya Ph.D), Bayero University, Kano).

**'Abbas, F.** (1962) *La nuit Coloniale* (Paris: René Julliard).

**'Abd al-Rahman, M.** (1969) *Imperialism and Nationalism in the Sudan: A Study in Constitutional and Political Development, 1899-1956* (Oxford: Clarendon Press).

**Abdel-Malek, A.** (1962) *Egypte, sociéte militaire* (Paris: Editions du Seuil).

**Abdel-Malek, A.** (1966) 'Problematique du socialisme dans le monde arabe', *L'homme et la sociéte*, kur. 125-48. .

**Abdel-Malek, A.** (1969) *Idéologic et renaissance nationale: L'Egypte moderne* (Paris: Editions du Seuil).

**Abdel-Malek, A.** (mh.) (1980) La pensée politique arabe contemporaine (toleo la 3, toleo la 1 1970; Paris: toleo la Seuil).

**Akin, E.** (1965) 'Preface to a study of Nigerian music', Ibadan Journal, 21, kur.53-62.

**Akin, E.**(1970) 'Traditional elements as the basis of new African art music', *African Urban Notes*, 5,4, kur. 52-6.

**Alarinjo, M. A.** (1981) 'The travelling Yoruba heatre', katika Y. Ogubiyi (mh.) Drama and Theatre katika Nigeria: A Critical Source Book (London).

**Alexandre, P.** (1967) *Langues et langage en Afrique noire* (Paris: Payot; toleo la Kiingereza 1972).

**al-Fasi, A.** (1954) *The Independence Movement in Arab North Africa* (Washington: American Council of Learned Societies)

**Ali, T.** na **O'Brien, J.** (1984) 'Labour, community and protest in Sudanese agriculture', katika J. Barker ( mh.) kur. 205-38.

**Allan, W.** 91965) *The African Husbandsman* (Edinburgh; Oliver na Boyd).

**Almond,G** na **Powell, B.** (1966) *Comparative Politics: A Developmental Approach* (Boston: Little, Brown).

**Aluko, S. A.** (1975) 'Rural economic development', katika M. Owusu (mh.) *Colonialism and Change* (The Hague: Mouton), kur. 231-54.

**Amiji, H. M.** (1984) 'Religion in Afro-Arab relations', katika *Historical and Socio-cultural Relations between Black Africa and the Arab World from 1935 to the Present,* General History of Afriea, Studies and Documents, Na.7) (Paris: UNESCO), kur. 101-29.

**Amin, S.** (1965) *Léconomie du Maghreb* (Paris: Toleo la Minuit).

**Amini, S.** (1970a) *Le Maghreb moderne* (Paris: Toleo la Minuit).

**Amini, S.** (1970b) *The Maghreb in the Modern World* (Hardmondsworth: Penguin Books).

**Amini, S.** (1974a) *Accumulation on a World Scale; A Critique of the Theory of Underdevelopment,* Juzuu 1 na 2; imefasiriwa na B. Pearce (New York na London: Monthly Review Press).

**Amin, S.** (1974b) *Neo-Colonialism in West Africa* (New York: Monthly Review Press).

**Amini, S.** (91976) *Unequal Development,* imefasiriwa na B. Pearce (New York na London: Monthly Review Press).

**Amini, S.** (1977) *Imperialism and Unequal Development* (New York: Monthly Review Press).

**Amini, S.** (1982) *Dynamics of Global Crisis* (New York: *Monthly Review Press).*

**Amoda M.** *(1978) Reflections on the FESTAC Colloquium* (Lagos: Nigeria Magazine).

**Amselle, E. M.** (1985) *La découvrte.*

**Anderson, D.** na **Throup, D.** (1985) 'Africans and agricultural production in colonial Kenya: the myth of the war as a watershed', *JAH,* 26, 4, kur. 327-45.

**Anderson, M.** (1981) *Music in the Mix: The Story of South African Popular Music* (Johannesburg).

**Aning, B. A.** (1967) *An Annotated Bibliography of Music and Dance in English-speaking Africa (Legon).*

**Ansprenge, F.** (1961) *Politiki im Schwartzen Afrika* (Köln na Opladen: Westdeutscher Verlag).

**Anstey, R.** (1977) *King Leopold's Legacy* (London: OUP).

**Anthonio, Q.B.O** (1973) 'Problems of marketing agricultural produce with special reference to foodstuffs in Nigeria', katika I. M. Ofori (mh.), kur 251-62.

**Anya, A. O.** (1986) *Scientific Research and Public Policy* (Lagos: Nigerian Institute of International Affairs, Muendelczo wa Mhadhara Na. 38).

**Anya, A.O.** (1987) 'Traditions, the pursuit of the intellectual life and Nigeria's future', Nsukka Journal of the Humanities, 1, Juni, kur.141-69.

**Apkevon, K.** (1983) *L'Afrique face au Plan d'action de Lagos et au rapport de la Banque mondiale* (Lome: ESACJ-UB).

**Appadorai, A.** (1956) *The Bandung Conference* (New Delhi: Indian Council of World Affairs).

**Applebaum, R.** (1970) *Theories of Social Change* (Chicago: Markham Publishing Co.).

**Arar, A.** (1980) 'The role of rainfed agriculture in the Near East region: summary of present situation, potential and constraints', katika *Rainfed Agriculture in the Near East and North Africa* (FAO: Rome).

**Archer, R.** 'The revolt of 1947-8 in Madagascar' tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha London).

**Armstrong, R. G.** (1964) *The Study of West African Languages* (Ibadan: IUP).

**Arnold, G.** (1979) *Aid in Africa* (London: Kegan Paul).

**Arrighi, G.** (1970) 'The political economy of Rhodesia', katika I. L. Markovitz (mh.), kur. 393-426.

**Arrighi, G.** na **Saul, J. S.** (1973) Essays on the Political Economy of Africa (New York and London: Monthly Review Press)

**Arzumanyan, A. A.** (1958) 'Statement: Report on promotion of economic cooperation', katika Afro-Asian Peoples' Solidarity Conference, Kairo, 26 Desemba 1957-1 Januari 1958 (Moscow: Moscow Foreign Language Publishing House).

**Asane, S. K. B.** (1977) *Pan-African Protest and the Italo-Ethiopian Crisis 1934-194*1 (London: Longman).

**Asante, S. K. B.** (1984) 'ECOWAS, the EEC and the Lome Convention', katika D. Mazzeo (mh.), *African Regional Organizations* (Cambridge: CUP), kur. 171-95.

**Asante, S. K. B.** (1986) *Pan-African Protest: West Africa and the Italo-Ehiopian Crisis* 1934-1941 (Harlow: Longman).

**Ashby, Sir, E** na **Anderson, M.** (1966) *Universities; British, Indian, African - A Study in the Ecology of Higher Education* (Cambridge, M.A: HUP).

**Ashford, D. E.** (1961) *Political Change in Morocco* (Princeton: PUP).

**Astafyev, G.V.** na **Dubinsky, A.M.** (wah.) (1974) *From Anti-Imperialism to Anti-Socialism:* The Evolution of Peking's Foreign Policy (Moscow: Progress Publisher).

**Astrow, A.** (1983) Zimbabwe: *A Revolution that Lost Its Way?* (London: Zed Press).

**Aujoulat, P.** (1958) *Aujourd'hui l'Afrique* (Paris and Tournai: Cantermain).

**Austin, D.** (1964) *Politics in Ghana 1946-1960* (Oxford: OUP).

**Austin, D.** (1980) 'The transfer of power: how and why', katika W.H.M. Jones na G. Fischer (wah.) *Decolonization and After; the British and French Experience* (London: Frank Cass), kur. 3-35.

**Awolowo, O.** (1960) *Awo: The Autobiography of Chief Obafemi Awolowo* (Cambridge; CUP).

**Ayache, A.** (1956) *Le Maroc: bilan d'une colonisation* (Paris: Editions sociales).

**Ayari, C.** (1983) 'African economies; what strategy for Africa's development', *Africa Report*, 28, 3 (Septemba - Oktoba). kur.8-11.

**Ayres, R. L.** (1983) *The World Bank and World Poverty: Banking on the Poor* (Cambridge: MIT Press).

**Azikiwe, N.** (1961) *Ziki: A Selection from the Speeches of Nnamdi Azikiwe* (Cambridge: CUP).

**Azonga, T. M.** (1986) 'TV steals the show', *West Africa*, 11 Agosti, kur. 1674-5.

**Bachy, V.** (1983) 'Panoramiaque sur les cinemas sud-sahariens', katika J. Binet, F. Boughedir na V. Bachy (wah.), Cinémas noirs d'Afrique (Paris), kur.23-43.

**Baeta, C. G.** (1962) *Prophetism in Ghana* (London; SCM Press).

**Bairoch, P.** (1977) *The Economic Development of the Third World Since 1900* (Berkely na Los Angels: UCP).

**Bakhtri, N.** (1980) 'Introduction of medic/wheat rotation in the North African and Near East countries', katika *Rainfed Agriculture in the Near East and North Africa* (FAO: Rome).

**Balandier, G.** (1973) *Sociologie actuelle de l'Afrique noire: Dynamique Sociale en Afrique centrale* ( toleo la 2, Paris: PUF).

**Balans, J. L, Coulon, C.** na **Ricard, A.** (wah.) (1972) *Problemés et perspectives de l'éducation dans un Eta du Tiers-Monde: le cas du Sénegal* (Institut d'études politiques de Bordeaux).

**Bamgbose, A.** (1976) *Mother Tongue Education: The African Experience* (London: Hodder na Stoughton; Paris: UNESCO press).

**Baran, P. A.** (1968) *The Political Economy of Growth* (New York: Modern Reader Paperbacks).

**Barker, J.** (mh.) (1984) *The Politics of Agriculture in Tropical Africa* (Beverly Hills na London: Sage).

**Barneet, D.** na **Harvey, R.** (1972) *The Revolution in Angola: MPLA, Life, Histories and Documents* (New York: Bobbs-Merrill).

**Barnes, J.A** (1952) 'History in a changing society', kwenye Human *Problems in British Central Africa, Juz. 11* (London: OUP), kur. 1-9.

**Barongo, Y. R.** (mh.) (1983) *Political Science in Africa* (London: Zed Press).

**Barrett, D. B.** (1982) *World Christian Encyclopedia* (London: OUP).

**Barrett, L.** (1977) *The Rastafarians* (London: Heinemann).

**Barron, S.** 91983) *German Expressionist Sculpture* (Los Angels).

**Bates, R. H.** (1981) *Markets and States in Tropical Africa: The Political Basis of Agricultural Policies* (Berkely, Los Angeles na London: UCP).

**Bates, R. S.** na **Lofchie, M. F.** (wah.) (1980) *Agriculture Development in Africa: Issues of Public Policy* (New York: Praeger).

**Bauer, P. T.** (1981) *Equality, the Third World and Economic Delusion* (Cambridge, MA. HUP).

**Bayart, J. F.** (1979) *L'Etat au Cameroun* (Paris; Presses de la Fondation nationale de sciences politiques).

**Bayen, M:** (1939) 'The march of blackmen' (New York).

**Beckford, G. L.** (1972) *Persistent Poverty: Under-Development in Plantation Economies of theThird World* (New York: OUP.

**Beier, U.** (1960) *Art in Nigeria* (Cambridge: CUP).

**Beier, U.** (1968) *Contemporary Art in Africa* (London: Pall Mall Press).

**Beier, U.** 'Yoruba opera: The magic spell of Duro Lapido', *Gangan*, 3, kur. 14-23.

**Beier, U.** 'Signwriters art in Nigeria', *African Arts*, 4, 3, kur. 22-7.

**Beinart, J.** (1968) 'Wall painting: popular art in two African Communities,' *African arts*, 2,3, kur. 26-9.

**Belal, A.** (1972) *Renaissance de monde arabe* (Paris: Doclot).

**Belaouane Gherari, R.** (1984) 'L'Afriquc dans les relations Sud/Sud', *Le mos en Afrique* (Paris), 225-226 (Oktoba-Novemba), kur. 104-19.

**Bellonce, G.** (1978) 'A la recherche de nouvelles formules éducatives pour le Tiers-Monde: l'éducateur dc base au Mali, 44, kur. 77-96.

**Bemba, S.** (1984) 'Cinquante ans de musique du Congo-Zaire 1920-1970: de Paul Kamba é Tabu-Ley', *Présence Africaine* (Paris).

**Benachenou, A.** (1978) *Formation du sous-developpement en Algérie: Essai sur les limites du developpement du capitaqlisme en Algérie*, 1830-1962 (Algiers).

**Ben Bella, A.** (1965) Contribution to *Le Monde*, 23 Januari.

**Bender, G. J.** (1978) *Angola under the Portuguese: The Myth and the Reality* (London: Heinemann).

**Bennett, G.** na **Rosberg, C.** (1961) *The Kenyatta Election 1960-1961* (Oxford: OUP).

**Benomar, J.** (1988) 'The monarchy, the Islamist Movement and religious discourse in Morocco', *Third World Quarterly, 10, 2* (Aprili).

**Benot, Y.** (1969) *Idéologies des Indépendances Africaines* (Paris: Maspero).

**Ben Salah, A.** (1980) Contributions to A. Abdel-Malek (mh.)

**Benson, P.** (1986) *Black Orpheus: Transition and Modern Cultural Awakening in Africa* (Berkeley and Los Angeles: UCP).

**Berg, E.** (1980) *Non-alignement et Nouvel Ordre Mondial* (Paris: PUF).

**Berger, R.** (1967) 'African and European dance', *Nigerian Magazine*, 92, kur. 87-92.

**Berman, E.** (1983) *Art and Artists of South Africa* (Cape Town: Balkema; toleo la 1 1974).

**Bernal, M.** (1987) *Black Athena: The Afro-Asiatic Roots of Classical Civilization, Vol. 1* (New Brunswick, NJ: Rutgers University Press)

**Bernard-Duquenet, N.** (1976a) 'Le Front populaire au Sénégal' (tasnifu ya Ph.D, University of Paris VII, Paris).

**Bernstein, S.** (1978) 'Problems of African agriculture: food and export crop production in the seventies', katika R. Synge (mh.) *Africa Guide* (Chicago: Rand McNally and Co.), kur. 57-63.

**Berstein, S.** (1981) 'Concepts for the analysis of contemporary peasantries', katika R. E. Galli (mh.).

**Berque, J.** (1960) *Les Arabes d'hier a demain* (Paris: Seuil).

**Berque, J.** (1964) *The Arabs: Their History and Future* (London: Faber and Faber).

**Beshir, M. O.** (1968) *The Southern Sudan; Background to Conflict* (London: Hurst).

**Bettelheim, J.** (1985) 'The Lantern Festival in Senegambia', *African Arts*, 18, 2, kur. 50-3.

**Biame, K. N.** (1968) 'Comic play in Ghana', *African Arts*, 1, 4, kur. 30-4.

**Biarnes, P.** (1980) *L'Afrique aux Africains* (Paris: A. Colin).

**Biaya, T. K.** (1984) 'De l'aube des temps jusqu'alors: l'histoire contemporaine des Luluwa par Nynnyi wa Luimba', katika B. Jewsiewicki (mh.), kur. 23-34.

**Bienen, H.** (1974) *Kenya: The Politics of Participation and Cont*rol (Princenton, NJ: PUP).

**Biko, B. S.** (mh.) (1972) *Black Viewpoint* (Durban: Black Community Programmes).

**Binet, J., Boughedir, F.** na **Bachy, V.** (wah.) (1983) *Cinémas noirs d'Afrique*, Cinema Action 26 (Paris).

**Bloch-Lainé, F.** na **Bouvier, J.** (1986) *La France restaurée, 1944-1954* (Paris: Fayard).

**Blundell, Sir, M.** (1964) *So Rough a Wind* (London; Weidenfeld and Nicolson).

**Boahen, A. A.** (mh.) (1985) *Africa under Colonial Domination*, 1880-1935, UNESCO General History of Africa, Ju. VII (Paris: UNESCO; London: Heinemann; Berkeley: UCP).

**Boahen, A. A.** (1986) *Topics in West African History* ( toleo la 2, Harlow: Longman).

**Bochkargov, Y.** (1966) 'The outlook in Africa', *New Times* (Moscow), 22 Januari.

**Boctor, G.** (1969) 'La peinture en Egypte moderne', *African Arts*, 3,. 28-33 na 86-7.

**Boeke, J. H.** (1953) *Economics and Economic Policy as Exemplified by Indonesia* (New York: Institute of Pacific Relations).

**Boganda, B.** *Erits ed discours* ( Juz. 3, Bangui: J. D. Penel).

**Bogatyrev, P.** (1971) *The Functions of Fold Costume in Moravian Slovakia* (The Hague; original: Matica Slovenska, 1937).

**Bohanna, P.** na **Dalton, G.** (1965) *Markets in Africa: Eight Subsistence Economies in Transition* (Garden City: Doubleday na Co, Inc.)

**Bomole, N.** (1970) 'Le Congo et l'Enseignement Programmé', *Cahiers Congolais*, 2, Juni-Julai, kur. 72-88.

**Bonneau, R.** (mh.) (1972) 'Les prétendants rivaux', *Afrique Littéraire et Artistique*, 26, kur. 83-8.

**Bonner, P. L.** (mh.) (1974) *Working Papers in Southern African Studies* (London: Frank Cass).

**Boserup, E.** (1985) 'Economic and development interrelationships in sub-Saharan Africa', *Population and Development Review*, 11, 3 (Septemba, kur. 383-99.

**Boubou Hama** (1981) 'The living tradition', katika J. Ki-Zirbo (mh.) kur. 62-72.

**Boulby, M.** (1988) 'The islamic challenge: Tunisia since independence', *Third World Quarterly*, 10, 2 (Aprili), kur. 590-614.

**Boutros-Ghali, B.** (1969) 'LOUA et la coopération économique'. *Revue egyptienne de droit international*, 25, Aprili, kur.171-85.

**Boutros-Ghali, B.** (1975) 'The League of Arab States and the Organizaiton of African Unity', katika Y. El-Ayouty (mh.) kur. 47-61.

**Bowman, L.** (1973) *Politics in Rhodesia* (Cambridge, MA: HUP).

**Bown, L.** na **Crowder, M.** 91964) *The Proceedings of the First International Congress of Africanists* (London: Longmans, Greens na International Cogress of Africanists).

**Bozzoli, B.** (mh.) (1979) *Labour, Townships and protest* (Johannesburg: Raven Press).

**Brandt, H.** (1956) *Namades du soleil* (Lausanne: La guilde du livre).

**Bray, M., Clarke, P. B** na **Stephens, O.** (1986) *Education and Society in Africa* (London: Edward Arnold).

**Breidenbach, P. S.** na **Ross, D. H.** (1978) 'The Holy Placc: Twelve Apostles Healing Gardens', *African Arts*, 11,4, kur. 28-35, 95.

**Brenner, L.** (1984) *West African Sufi* (London: Hurst).

**Brett, E. A.** (1973) *Colonialism and Underdevelopment in East Africa: The Politics of Economic Change 1919-1939* (New York: Nok Publishers, Ltd).

**Brett, E. A.** na **Belshaw, D. G., R.** (wah.) (1973) *Politics and Agriculture* (London: Frank Cașs).

**Brevie, J.** (1930) *Discours d'ouverture au Conseil de Gouvernement de l'AOF.*

**Brokensha, D.** (1966) *Social Change in Lartech* (London: OUP).

**Brokes, D** na **Hodge, P.** (1969) *Community Development: An Interpretation* (San Francisco: Chandler Publishing Co.)

**Brown, A. C.** (1988) *A History of Scientific Endeavour in South Africa: A Collection of Essays Published on the Occasion of the Centenary of the Royal Society of South Africa* (Capetown; RSSA).

**Brown, B.** (1983) 'The impact of male labour migration on women in Botswana', *African Affairs*, 82-328 (Julai), kur. 367-88.

**Brown, B. G. N.** na **Hiskett, G.** (1975) *Conflict and Harmony in Education in Tropical Africa* (London: George Allen na Unwin Ltd).

**Brown, J. M.** (1972) *Kenyatta* (London: George Allen na Unwin Ltd).

**Brown, P.** (1970) 'Patterns of authority in West Africa', katika I. L. Markovitz (mh.).

**Brutents, K.** (1967) 'Africa's revolution, gains and problems', *International Affairs* (Moscow), Januari.

**Bude, U.** (mh.) (1980) *Education for Kogisano in Botswana* (Bonn: DAAD).

**Buijtenhuijs, R.** (1982) *Contribution to Mau Mau Historiography* (Leiden: African Studies Centre).

**Buraimoh, J.** (1971) 'Painting with beads', *African Arts*, 5, 1, kur. 16-19.

**Burt, E. C.** (1984) 'Mural painting in western Kenya', *African Arts*, 16, 3, kur. 60-3 na 80.

**Busia, K. A.** (1969) 'Social attitudes to agriculture', katika C. Legum na J. Drysdale (wah.), *Africa Contemporary Record: Annual Survey and Documents 1968-1969* (London: Africa Research Limited).

**Bustin, E.** (1975) *Lunda under Colonial Rule: The Politics of Ethnicity* (Cambridge, MA: HUP).

**Byakov et al.** (wah.) (1981) *The Prioriities of Soviet Foreign Policy Today* (Moscow: Progress Publishers).

**Cabral, A.** (1975) *Unité et lutte: oeuvres d'Amilcar Cabral* (Paris: F. Maspero)

**Cadoux, C.** (1969) *La République malgache* (Paris: Berger-Levrault).

**Caetano, M.** (1954) *Os nativos na economia africana* (Coimbra).

**Callaway, H.** (1975) 'Indigenous education in Yoruba society', katika G. N. Brown na G. Hiskett (wah.) kur. 26-39,

**Camara, C.** (1973) Une ville précoloniale au Nigeria:Ondo', CEA, 13, 51.

**Cameroun, D.** (1934) *The Principles of Native Administration and their Application* (Lagos: Government Printer).

**Campion-Vincent, V.** (1970) 'Systéme d'enseignement et mobilité sociale au Sénégal', *Revue Française de Sociologie*, 11, Aprili-Juni.

**Capet, M.** (1958) *Traite d'économic tropicale* (Paris: Pichon and Durand-Auzias).

**Cardoseo, P. M.** (1984) *Folclore caboverdeano* (toleo la 2, Lisbon: Porto).

**Carnoy, M.** (1974) *Education as Cultural Imperialism* (New York: McKay).

**Carsow, M.** (1935) *Queques aspects du commerce impérial de la France* (Paris: Geuthner).

**Carter, G.** (1959) *The Politics of Inequality* (New York: Praeger).

(mh.) (1966) *National Unity and Regionalism in Eight African States* (Ithaca: Cornell University Press).

**Cary, J.** (1944) *The Case for African Freedom* (London: Secker na Warburg).

**Castagno, A. A** (1966) 'Somali Republie', katika J. Coleman na C. G. Rosberg (wah.) kur. 512-60.

**Centro Cultural Afro-Ecuatoriano,** Palenque (Quito, Ecuador).

**Cervenka, Z.** ('1977) *The Unfinished Quest for Unity: Africa and the OAU* (New York: African publishing Co.).

**Césaire, A.** (1969) *Return to My Native Land,* imefasiriwa na J. Berger na A. Bostock (London: Penguin).

**Chagnoux, H.** na **Haribu, A.** (1980) *Les Comores* (Paris: PUF).

**Cham, M. B.** (1984) 'Art and ideology in the work of Sembene Ousmane and Haile Gerima', *Présence africaine,* 129, 1, kur. 79-91.

**Cham, M. B.** (1982) Film production in West Africa, 1979-1981)', *Présence afracaine*, 124, 4, kur. 168-89.

**Chambers, R.** (1969) *Settlement Schemes in Tropical Africa* (London: Routledge and Kegan Paul).

**Chanaiwa, D.** (1976) *Profiles of Self-Determination: African Responses to European Colonialism in Southern Africa, 1952-Present* (Northridge, CA: California State University Foundation).

**Chanaiwa, D.** (1980) 'African humanism in Southern Africa: the utopian, traditionalist, and colonialist worlds of mission-educated élites', katika A. G. Mugomba na M. Nyaggah (wah), kur. 9-40.

**Chandos, Lord** (1964) *The Memoirs of Lord Chandos* (London: Bodley Head).

**Cheeks, J.** (1936) 'Wings over Ethiopia', *New Masses*, 7 Julai.

**Chenntouf, T.** (1969) L'Assembleé algérienne 1947-1956 (Paris: Faculté des lettres et des sciences humaines de Paris).

**Chesneaux, J.** (1964) 'Qu'est-ce que la démocratie nationale?', La Pensée, 118 (Desemba), kur. 3-19.

**Chibwe, E. C.** (1976) *Arab Dollars for Africa* (London: Croom Helm).

**Chibwe, E. C.** (1977) *Afro-Arab Relations in the New World Order* (London: Julian Friedmann).

**Chikwendu, E.** (1983) The African peasantry: neglected by African political science', katika Y. R. Barongo (mh.), kur. 37-48.

**Chinweizu** (1975) *The West and the Rest of Us* (New York: Vintage Books).

**Chinyee,O.** (1980) 'Parallelism versus influence in African literature: the case of Efua Sutherland's Edufa', *Kiabara,* 3, 1 (Rains), kur. 113-31.

**Chrétien, J. P.** (1972) 'L'enseignement au Burundi', *Revue francaise d'etudes politiques africaines,* 76, Aprili, kur. 61-80.

**Clark, E.** na **Ogunde, H.** (1979) *The Making of Nigerian Theatre* (Oxford: OUP),

**Clayton, A.** (1976) *Counter-insurgency in Kenya, 1952-1960* (Nairobi: Trans-Africa Publishers).

**Clayton, E. S.** (1981) *The Zanzibar Revolution and its Aftermath* (London: C. Hurst).

**Clayton, E. S.** (1964) *Agrarian Development in Peasant Economies: Some Lesson from Kenya* (Oxford: Pergamon).

**Cliffe, L.** (1976) 'Rural political economy of Africa', katika P.C.W. Gutkind na I. Wallerstein (wah.), kur. 112-31.

**Cliffe, L.** na **Cunningham, G.** (1973) 'Ideology, organization and settlement experience in Tanzania', katika E. A. Brett na D. G. R. Belshaw (wah.)

**Clute, R. E.** (1982) 'The role of agriculture in African development', African Studies Review, 25, 4 (Desemba), kur. 1-21.

**Cohen, R.** (1979) 'Albert Nzula', katika B. Bozzoli (mh.), kur. 325-40.

**Cole, H.** (1975) 'Art festival in Ghana,' *African Arts*, 8, 3, (toleo maalum), kur. 12-24.

**Coleman, J. S.** na **Rosberg, C. G.** (1970) *Political Parties and National Integration in Tropical Africa* (Berkeley: UCP).

**Constantine, S.** (1984) *The Making of British Colonial Development Policy 1914-1940* (London: Frank Cass).

**Constantine, S.** (1985) 'The making of an imperial slum: Nyasaland and its railways, 1895-1935', *JAH,* 16.

**Cook, D.** (mh.) (1965) *Origin East Africa: A Makerere Anthology* (London na Ibadan: Heinemann).

**Cooper, P.** na **Doornbos, M.** (1982) "Rwenzururu protest songs', Africa, 52, 1, kur. 50-1.

**Cooper, F.** (1980) *From Slaves to Squa tters* (New Haven: YUP).

**Cooper, F.** (1981) 'Africa and the world economy', *African Studies, 17, 2/3 (Juni/Septemba), kur. 1-86.*

**Coser,L.** (1956) The Functions of Social Conflict (New York: The Free Press).

**Cosgrove-Twitchett, C.** (1978) *Europe and Africa: from Association to Partnership* (Farnborough: Saxon House)

**Coulet-Western, D.** (1975) *A Bibliography of the Arts of Africa* (Waltham, MA).

**Courriére, Y.** (1968-72) La Guerre d'Algérie (Paris: Fayard).

**Court, F.** na **M'Wangi, M.** (1976) 'Maridadi fabrics', *African Arts,* 10, 1, kur.38-41 na 99.

**Cowan, L. G., O'Gonnell, J** na **Scanlon, D.** (wah.) (1965) *Education and Nation Building* (New York: Frederick Praeger).

**Cowen, M.** (1981) 'Commodity production in Kenya's Central Province', katika J. Heyer na wengine (wah.), kur. 121-43.

**Craveirinha, J.** (1964) *Chifugo* (Lisbon: Casa dos Estdantes do Imperio).

**Crocker, C.** (1976) 'The African dimension of the Indian Ocean policy', Orbis, 20, 3 (Kuanguka), kur. 637-69.

**Crowder, M.** (1970) 'The white chiefs of tropical Africa', katika L.H. Gann na P. Duignan (wah.) *Colonialism in Africa, II: The History and Politics of Colonialism 1914-1960* (Cambridge: CUP), kur. 320-50.

**Cworoder, M.** (1978) 'The contemporary Nigerian artist: his patrons, his audience, his critics', *Présence africaine,* 105/106, 1/2, kur. 130-45.

**Crowder, M.** (1980) *West Africa under Colonial Rule* (London: Hutchinson; toleo la 1, 1968).

**Crowder, M.** (mh.) (1984) *The Cambridge History of Africa, Juz. 8: kutoka 1940 mpaka* 1975 (Cambridge: CUP)

**Crowder, M.** (1995) 'World War II and Africa', *FAII, 26, 4, KUR. 287-9.*

**Crowder, M.** na **Osuntokun, J.** (1986) 'The First World War and West Africa', katika J. F. A. Ajayi na M. Crowder (wah.) *History of West Africa, Juz. II* (Harlow: Longman), kur. 546-78.

**Cunha da Silva, J. M.** (1955) *O trabaiho indigena* (Lisbon: Agencia Geral do Ultramar, Divisão de Publicaçaoes e Biblioteca).

**Cuper, K.** (1958) 'Kwela: how it all began', *Melody Maker,* 33, 7 Juni, uk. 1283.

**Curtin, P., Feirman, S., Thompson, L.** na **Vansina, J.** (wah.) (1978) *African History* (Boston: Little and Brown; London: Longman).

**Curtrufelli, M. R.** (1983) *Women of Africa: Roots of Oppression* (London: Zed Press).

**Cutter, C. H.** (1968) 'The politics of music in Mali', *African Arts,* 1, 3, kur. 38-9 na 74-7.

**Dakin, J., Tiffen, B** na **Widdowson, H. G.** (1968) *Language in Education* (London: OUP)

**Dalby, D.** (1970) *Language and History in Africa* (London: Frank Cass and Co. Ltd).

**Dauber, R.** na **Cain, M. L.** (wah.) (1980) *Women and Technological Change in Developing Countries: AAAS Selected Symposium 53* (Boulder, Co: Westview Press).

**Davidson, B.** (1969) *The Africans: An Entry to Cultural History* (London and Harlow: Longman).

**Davidson B.** (1972) *L'Angola au coeur des tempetes* (Paris: Maspero).

**Davidson, B.** (1978) *Africa in Modern History* (Guildford: Allen Lane).

**Davidson, B.** (1980) 'The movement of national liberation', *Tarikh,* 6, 4.

**Davidson, B. Slovo, J** na **Wilkinson, A. R.** (1976) *Southern Africa: The New Politics of Revolution* (Harmondsworth: Pelican).

**de Almeida, P. R.** (1979) *Historia de colonialismo portugués em Africa: cronoligia* (Lisbon: Editorial estampa).

**de Andrade, M.** na **Ollivier, M.** (1971) La guerre en Angola: étude socio-économique (Paris: Maspero).

**de Benoist, J.** (1980) *La Balkanisation de l'Afrique Occidentale française* (Dakar: NEA).

**De Castro, A.** (1978) *O sistema colonial portuges em Africa* (Lisbon: Editorial Caminho).

**De Gaulle, C.** (1968) katika *Africa Research Bulletin* (London), 9, 5, uk. 1186.

**De Gennaro, B. M.** (1981) 'Ujamaa: the aggrandizement of the state', katika R. E. Galli (mh.), ukr. 111-55.

**De Haes. R.** (1982) Les Sectes: une interpellation (Kinshasa).

**De Jager, E. J.** (1973) Contemporary African Art in South Africa (Cape Town: C.Struik)

**De St Jorre, J.** (1972) *The Nigerian Civil War* (London: Hodder and Stoughton).

**De Wilde, J. C.** (1967) *Experience with Agricultural Development in Tropical Africa* (Majuzuu 2; Baltimore: The Johns Hopkins Press).

**Decraene, P.** (1982) *Vieille Afrique, jeunes nations* (Paris: PUF).

**DeGraft-Johnson, J.C.** (1958) *African Experiment; Cooperative Agriculture and Banking in British West Africa* (London: Watts).

**Derman, W.** (1984) 'USAID in Sahel: development and poverty', katika J. Barker (mh.), kur. 77-99.

**Dia, M.** (1975) *Islam, sociétés africaines et culture industrielle* (Dakar: NEA).

**Diawara, M.** (1986) 'Who is in control?', *West Africa*, 17 Februari, kur. 348-9

**Diawara, M.** (1987) 'Images of children', *West Africa*, 23 Machi, kur. 558-9

**Dickens, C.** (1975) *Great Expectations* (London; OUP).

**Diop, A.** (1958) 'Our Amsac brothers', katika *Africa seen by American Negro Scholars* (Dijon: Présence africaine, New York, 1963).

**Diop, C. A.** (1974) *The African Origin of Civilization: Myth and Reality*, mh. na mfasiri M. Cook (Chicago: Lawrence Hill Books).

**Dodge, B.** (1965) 'The significance of religion in Arab nationalism', katika J. H. Proctor (mh.) kur. 94-120.

**Donalson, H.** na **Nogee, L.** (1981) *Soviet Foreign Policy since World War II* (New York: Pergamon).

**Doresse, J.** (1970) *Histoire de l'Ethiopie* (Paris: PUF).

**Dornowitz, S** na **Mandirola, R.** (1984) 'Grave monuments in the Ivory Coast', *African Arts*, 17, 4, kur. 46-52.

**Dorward, D.** (1986) 'British West Africa and Liberia', katika *The Cambridge History of Africa, Juz. III* (Cambridge: CUP).

**Drachler, J.** (mh.) (1969) *African Heritage: An Anthology of Black African Personality and Culture* (London: Collier-Macmillan Ltd).

**Drake, St. C.** (1982, 'Diaspora studies and pan-Africanism', katika J. E. Harris (mh.) uk. 341-402.

**Droogers, A.** (1980) *The Dangerous Journey: Symbolic Aspects of Boys' Initiation among the Wagenia of Kisangani, Zaire* (The Hague: Mouton).

**Drysdale, J.** (1964) *The Somali Dispute* (New York: Praeger).

**Dubresson, A.** (1979) *L'espace Dakar- Rufisque* (Paris: ORSTOM).

**Dzidzienyo, A** na **Turner, J. M.** (1981) 'African-Brazilian relations: a rcconsideration', katika W. A. Selcher (mh.), kur. 201-18.

**Dzobo, N.K.** (1975) 'Values in indigenous edueation', katika G. N. Brown na M. Hiskett (wah. Kur. 76-91.

**Echenber, M.** (1978) 'Tragedy at Thiaroye: the Senegalese soldiers' uprising of 1944', katika *African Labour History* (Beverly Hills: Sage), kur. 109-28.

**Einstein, C.** (1915) *Negeplastik* (Munich; kurt Wolff Verlag).

**Eisenstadt, S. N.** na Rokkan, S. (wah.) (1973) *Building States and Nations* (majuzuu 2; Beverly Hills; Sage).

**El-Ayouty, Y.** (1971) *The United Nations and Decolonization: The Role of Afro-Asia* (The Hague: Martinus Nijhoff).

**El-Ayouty, Y.** (1975) 'The OAU and the Arab-Israeli conflict: a case of mediation that failed', katika Y. El-Ayouty (mh.), kur. 189-212.

**El Fasi, M.** (1967) Chants anciens des femmes de Fés (Paris: Editions Seghers).

**El-Hareir, I. S.** (1985) *'North Africa and the Second World War'*, katika UNESCO (1985), kur. 27-36.

**Elkan, W.** (1958) 'The East African trade in woodcarving', *Africa,* 28, 4, kur. 314-23.

**El-Khawas, M.** (1971) 'The Third World stance on apartheid: the UN record', *Journal of Modern African Studies*, 9, 3, (Oktoba, kur. 443-52.

**El Mansury, S.** (1984) Modern trends in Egyptian arts', *Prism*, 6, kur. 83-7.

**Elnaccash, A.** (1968) 'Egyptian cinema: a historical outline', *African Arts,* 2, 1, kur. 52-5 na 70-1.

**Elungu, E. P.** (1984) *Eveil philosophique africain* (Paris: L'Harmattan).

**Emerson, R.** (1962) *From Empire to Nation: The Rise to Self-Assertion of Asian and African Peoples* (Cambridge, MA: HUP).

**Evans-Pritchard, E.E.** (1949) *The Sanusi of Cyrenaica* (Oxford: Clarendon Press).

**Ewens, G.** (1987) 'The Zaiko cult', *West Africa,* 3621, 2 Februari, kur. 202-4.

**Eybers, G. W.** (1918) *Select Constitutional Documents Illustrating South African History, 1795-1910* (London: Routledge)

**Eyongetah, T.** na **Brain, R.** (1974) *A History of the Cameroon* (London; Longman).

**Fabian, J.** (1978) 'Popular culture in Africa: findings and conjectures', *Africa,* 48, 4, kur. 315-34.

**Fabubmi, L. A.** (1960) *The Sudan in the Anglo-Egyptian Relations* (London: Longmans).

**Fanon, F.** (1967a) *Toward the African Revolution: Political Essays,* imefasiriwa na H. Chevalier (New York: Mnthly Review Press).

**Fanon, F.** (1967b) *Black Skin; White Masks,* imefasiriwa na C. L. Markmann (New York: Grove Press Inc.; toleo la 1970, London: Paladin)

**Fanon, F.** (1968) *Sociology of Revolution* (Paris: Maspero).

**Feit, E.** (1967) *African Opposition in South Africa: The Failure of Passive Resistance* (Stanford, CA: Hoover Institution Press).

**Ferrnandez, J.** (1982) *Bwiti: An Ethnography of the Religious Imagination in Africa* (Princeton: PUP).

**Fernea, R. A.** (mh.) (1973) *Nubians in Egypt: A Peaceful People* (Austin: University of Texas Press).

**Ferreora. E. S.** (1974) *Portuguese Colonialism in Africa: The End of an Era* (Paris).

**Ferreira, M.** (1986) 'Portuguese Afriea: the new militancy', katika A. Gérard (mh.) Juz. 1.

**Fetter, B.** (1976) *The Creation of Elisaberthville 1910-1940* (Standord: Hoover Colonial Studies).

**Fieldhouse, D. K.** (1996) *Black Africa 1945-1980: Economic Decolonization and Arrested Development* (London na Boston: Allen na Unrich).

**Fig, D.** (1984) 'South African interests in Latin America', katika South African Research Scrvice (mh.) *South African Review II* (Johannesburg: Raven Press), kur. 239-55.

**Fortes, M.** na **Evans-Pritchard, E. E.** (wah.) 91940) *African Political Systems* (London: OUP).

**Foster, M.** (1961) *Masters of Political Thought, Juz. I* (London: George G. Harrap).

**Foster, P.** (1965) *Education and Social Change in Ghana* (London: Routledge and Kegan Paul).

**Fosu, K.** (1986) *Twentieth-Century Art of Africa* (Zaria).

**Fox, L. K.** (mh.) (1967) *East African Childhood* (London: OUP)

**Fraginals, M. M.** (1984) *Africa En America Latina*, imefasiriwa na L. Blum (Paris: UNESCO).

**Frank, A. G.** (1980) *Crisis in the World Economy* (New York and London: Holmes and Meier Publisher)

**Frankel, S. H.** (1938) *Capital Investment in Africa: Its Causes and Effects* (London: OUP)

**Federick, A. Duke of Mecklenburg** (1910) *In the Heart of Africa* (London).

**Freeman, L.** (1984), 'CIDA and agriculture in East and Central Africa', J. Barker (mh.).

**Freeman-Grenville, G.S.P** (1973) *Chronology of African History* (London: OUP)

**Freund, B.** (1981) *Capital and Labour in the Nigerian Tin Mines* (Harlow: Longman).

**Furedi, F.** (1974) 'The social composition of the Mau-Mau movement in the White Highlands', *Journal of Peasant Studies*, 1, 4, kur. 486-505.

**Furley, O. W.** na **Watson, T.** (1978) A history of Edueation in East Africa (New York: NOK Publisher).

**Fyle, C. M.** (1981) *The History of Sierra Leone* (London: Evans Brothes).

**Galbraith, J. K.** (1979) *Nature of Mass Poverty* (Cambridge, MA: HUP)

**Galli, R. E.** (1981) *The Political Economy of Rural Development: Peasants, International Capital and the State* (Albany: State University of New York Press).

**Galtung, J.** (1976) 'The Lome Convention and neo-capitalism', *The African Review*, 6,1, kur. 33-43.

**Gann, L. H.** (1968) *Burden of Empire: An Appraisal of Western Colonialism in Africa South of the Sa*hara (London: Pall Mall Press).

**Garrett, R. M.** (1984) *Education and Development* (New York: St Martin's Press).

**Gaskin, L. J. P.** (1965a) *A Bibliography of African Art* (London: IAI).

**Gaskin, L. J. P.** (1965b) *A Select Bibliography of Music in Africa* (London).

**Greertz, C.** (1963) *Old Societies and New States* (Glencoe: The Free Press).

**Geiss, I.** (1974) *The Pan-African Movement* (London; Methuen).

**Gellar, S.** (1972) *State-Building and Nation-Building in West Africa* (Bloomington: International Development Centre, Indiana University).

**Gerard, A. S.** (mh.) (1986) *European Language-Writing in Sub-Saharan Africa*, Juzuu 1 na 2 (Budapest: Akademia Kiadó).

**Gerhart, G. M.** (1979) *Black Power in South Africa: The Evolution of an Ideology* (Los Angeles: UCP).

**Gertzel, C.** (1976) 'Kingdom, districts and the unitary state: Uganda 1945-1962', katika D. A. Low na A. Smith (wah._ kur. 65-106.

**Gertzel, C. Goldschmidt, M.** na **Rothechild, D.** (wah.) (1972) *Government and Politics in Kenya* (Nairobi: EAPH).

**Gibson, R.** (1972) *African Liberation Movements: Contemporary Struggles Against White Minority Rule* (London: OUP).

**Gifford, P.** na **Louis, W. R.** (wah.) (1982) *The Transfer of Power in Africa: Decolonization 1940-1960* (New Haven: YUP).

**Gifford, P.** na **Louis, W. R.** (wah.) (1988) *The Transfer of Power in Africa, 1956-1980* (New Haven: YUP).

**Gilkes, P.** (1975) *The Dying Lion: Feudalism and Modernization in Ethiopia* (London: Julian Friedman).

**Gillon, W.** (1984) *A Short History of African Art* (Harmondsworth: Viking).

**Goldworth, D.** (1971) *Colonial Issues in British Politics, 1945-1961* (Oxford: Clarendon Press).

**Gordon, G. C.** (1966) *The Passing of French Algeria* (Oxford: OUP).

**Gorer, G.** (1945) *Africa Dances* (toleo la 2, London: Lehmann).

**Green, R. H.** (1977) *Toward Socialism and Self-Reliance: Tanzania Striving for Sustained Transition Projected* (Uppsala: Scandinavian Institute of African Studies).

**Green, R. J** na **Seidman, A.** (1968) *Unity or Poverty: The Economics of Pan-Africanism* (Baltimore: Penguin Books).

**Grillo, Y. A.** na **Highet, J.** (1968) 'Appreciations of Idubor', *African Arts*, 2, 1, kur. 33-5.

**Gromyko, A. A.** (1967) 'Soviet foreign policy in Africa', *International Affairs*, Septemba.

**Gromyko, A. A.** (mh. (1984) *The October Revolution and Africa* (Moscow: Progress Publishers).

**Grove, A. T.** (1974) 'Desertification in the African environment', *African Affairs*, 73, 291 (Aprili, kur. 137-52).

**Gugler, J.** na **Flanagan, W. G.** (1978) *Urbanization and Social Change in West Africa* (London: CUP).

**Guralniki, D. B.** (mh.) (1970) *Websters New World Dictionary, Vol. II* (New York: The World Publishing Company).

**Guthrie, M.** (1948) *The Classification of Bantu languages* (London: OUP.
**Gwanga, J.** na **Miller, E. J.** (1971) *The World of African Song: Miriam Makeba* (Chicago).

**Habte, A.** (1969) *A Look Forward: A Special Report from the President* (Addis Ababa: Haile Selassie I University Press).
**Haim, S. G.** (1962) *Arab Nationalism; An Anthology* (Berkely na Los Angeles: UCP).
**Halfani, M. S.** na **Barker, J.** (1984) 'Agribusiness and agrarian change', katika J. Barker (mh.) uk. 35-65.
**Hamilton, V.** (1988) *In the Beginning* (New York and London: Harcourt Brace Jovanovich)
**Harris, J. E.** (1971) *The African Pesence in Asia: Consequences of the East African Slave Trade* (Evanston, Ill: Northwestern Illinois University Press).
**Harris, J. E.** (1974) *Pillars in Ethiopian History: William Leo Hansberry African History Note-Book* (Washington: Howrd University Press).
**Harris, J. E.** (mh.) (1982b) *Global Dimensions of the African Diaspora* (Washington, D. C.: Howard University Press).
**Harrison-Church, R. S. Clarke, J. I. Clarke, P. J. H.** na **Henderson, H. J. R.** (1971) *Africa and its Islands* (toleo la 3; London: Longman).
**Hartland Rowe, M.** (1985) 'The textile prints of the Phutadikobo Museum', *African Arts,* 18, 3, kur. 84-6.
**Hasting, A.** (1979) *A History of African Christianity* (Cambridge: CUP).
**Heseltine, N.** (1971) *Madagascar* (London: Pall MallPress).
**Heyer, J., Maitha, J. K.** na **Senga, W. M.** (wah.) (1981) *Rural Development in Tropical Africa* (New York: St. Martin's Press and London: Macmillan).
**Hill, P.** (1970) *Studies in Rural Capitalism in West Africa* (Cambridge: CUP).
**Hiskett, M.** (1974) 'Traditional Islamic and modern Western education in tropical Africa: the problems of integration', *World Development, 2*, kur. 41-3.
**Holt, P. M.** (1961) *A Modern History of the Sudan* London: Weidenfeld na Nicolson; toleo la 2 1967).
**Hopkins, A. G.** (1973) *An Economic History of West Africa* (London: Longman).
**Hopkins, N. S.** (1971) 'Persuasion and satire in the Malian theatre', *Africa*, 42, 3, kur. 217-28.
**Huggins, W. N.** na **Jackson, J. G.** *The Friends of Ethiopia* (pamphlet; New York).
**Huggins, W.N.** na **Jackson, J. G.** (1935) *The Afro-American* (Baltimore), 27 Julai,
**Huggins, W. N.** na **Jackson, J. G.** (1973) *An Introduction to African Civilization* (NewYork: Negro Universities Press).
**Hunter, G.** (1964) *The new Societies of Tropical Africa: A Selective Study* (New York: Praeger).
**Huntington, S.** (1968) *Political Order in Changing Societies* (New Haven: YUP)
**Hyden, G.** (1983) *No Short Cuts to Progress* (Berkely: UCP).

**Ikime, O.** (1980) *Groundwork of Nigerian History* (Ibadan: Heinemann).
**Iliffe, J.** (1979) *A Modern History of Tanganyika* (Cambridge: CUP).

**Ismael, T. Y.** (1971) *The U.A.R. in Africa: Egypt's Policy under Nasser* (Evanston, III: Northwestern University Press).

**Issawi, C.** (1963) *Egypt in Revolution: An Economic Analysis* (London and New York: OUP)

**Issawi, C.** (1982) *An Economic History of the Middle East and North Africa* (London: CUP)

**Italiaander, R.** (1937) *Neue kunst in Afrika* (Mannheim: Bibliographisches Institut AG).

**Jabavu, D. D. T.** (1920) *The Black Problem: Papers and Addresses on Various Native Problems* (Lovedale, South Africa: Lovedale Press).

**Jackson, J. G.** (1970) *Introduction to African Civilizations* (Secaucus, NY: The Citadel Press).

**Jaipal, R.** (1983) *Non-Alignment: Origins, Growth and Potential for World Peace* (New Delhi: Allied Publishers).

**Jans, P.** (1960) 'Godsdienstige muziek voor inlandes in the apostolisch Vicariaat ban Coquilhatstad', *Band*, 19, 2-3, kur. 66-82.

**Jansen, G. H.** (1966) *Non-Alignment and the Afro-Asian States* (NewYork: Praeger)

**Japhet, K.** na **Japhet, S.** (1967) *The Meru Land Case* (Nairobi: EAPH).

**Jaritz, H.** (1973) 'Notes on Nubian architecture and architectural drawings', katika R. A. Fernea (mh.), kur. 49-60

**Jawiewicki, B.** (1977) 'Unequal development: capitalism and the Katanga economy, 1914-40', katika R. Palmer na N. Parsons (wah.), kur. 317-45.

**Jewsiewicki, B.** (1986) 'Collective memory and the stakes of power; A reading of popular Zairian historical discourses', *History in Africa*, 13, kur. 195-223.

**Johnson, W. R.** (1983) 'The role of thetArab Bank for Economic Development in Africa', *Journal of Modern African Studies*, 21, 4, (Desemba, kur. 625-44.

**Jorgensen, J. J.** (1981) *Uganda: A Modern History* (London: Croom Helm).

*Journal of African History* (1985) 'World War II and Africa', 26, 4.

**Jules-Rosette, B.** (1984) *The Messages of Tourist Arts: An African Semiotic System in Comparative Perspective* (New York and London: Plenum Press).

**Kaba, L.** (1974) *The Wahabiyya: Islamic Reform and Politics in French West Africa* (Evanston, III: Northwestern University Press).

**Kadalie, C.** (1971) *My Life and the ICU* (London: Frank Cass).

**Karabel, J.** na **Halsey, A.H.** (1972) *Power and Ideology in Education* (New York: OUP).

**Kariara, J.** (1965) 'The Dream of Africa', katika D. Cook (mh.).

**Kay, D.** (1970) *The New Nations in the United Nations, 1960-1967* (New York: Columbia University Press).

**Kay, S.** (1978) 'Peter Nzuki: calabash carver of Kenya', *African Arts*, 12, 1, kur. 40-1 na 108.

**Kazadi, F. S. B.** (1978) 'Mobutu, MPR and the politics of survival', *Africa Report*, 23, 1 (Januari, kur. 11-16.

**Keatley, P.** (1963) *The Politics of Partnership* (London: Penguin Books).

**Khadduri, M.** (1970) *Political Trends in the Arab World: The Role of Ideas and Ideals in Politics* (Baltimore:Johns Hopkins University Press).

**Khalidi, I. R.** (1956) *Constitutional Development in Libya* (Beirut: Khayat).

**Kiggundu, I.** (1984) *A Planned Approach to a Common Market in Developing Countries* (Nairobi: Coign Publications).

**Kilby, P.** (1969) *Industrialization in an Open Economy: Nigeria 1945-1966* (Cambridge: CUP).

**Kimche, D.** (1973) *The Afro-Asian Movement: Ideology and Foreign Policy in the Third World* (Jerusalem: Israel University Press).

**King, K.** (mh.) (1971) *Pan-Africanism and Education* (London: OUP).

**King, K.** (mh.) (1976) *Education and the Community in Africa* (Edinburgh: University of Edinburgh, Centre for African Studies).

**Kinney, E. S.** (1970) 'Urban West African music and dance', *African Urban Notes*, 5, 4, kur. 3-10.

**Kinyongo, J.** (1974) 'Philosophie en Afrique: une existence', *African Philosophical Journal*, 3-4, kur. 205-11.

**Ki-Zerbo, J.** (1972) *Histoire de l'Afrique noire* (Paris: Hatier).

**Ki-Zerbo, J.** (mh.) (1981) *Methodology and African Prehistory*, UNESCO Historia Kuu ya Afrika Juz.1 (Paris: UNESCO; London: Heinemann, Berkeley, CA: University of California Press)

**Kleiu, M.** (1968) *Islam and Imperialism in Senegal* (Stanford na Edinburgh).

**Klein, M.** (1980) *Peasants in Africa: Historical and Contemporary Perspectives* (Beverly Hills na London: Sage).

**Kubiki, G.** (1981) 'Neo-traditonal popular music in East Africa since 1945', katika I. R. Middleton na D. Horn (wah.) Juz. 1.

**Kuper, H.** (1978) *Sobhuza II, Ngwenyama and King of Swaziland* (London: Duckworth).

**Kuper, L.** na **Smith, M. G.** (wah.) (1971) *Pluralism in Africa* (Los Angeles: UCP).

**Kwaabena Nketia, J. H.** (1957) 'Modern trends in Ghana music', *African Music*, 1, 4, kur. 13-17.

**Kwabena Nketia, J. H.** (1965) *Ghana: Music, Dance and Drama* (Accra).

**Kwabena Nketia, J.H.** (1967) 'The language problem and the African personality', *Présence africaine*, 67-2, kur. 157-72.

**Kwabena Nketia, J. H.** (1975) *The Music of Africa* (London: Gollancz).

**Kwabena Nketia, J. H.** (1978) 'Tradition and innovation in African music', *Jamaica Journal*, 11, 3 kur. 3-9.

**Lamb, D.** (n.d) 'Russia in Somalia: they helped to develop', *Los Angeles Times*

**Langdon, S.** 91986) 'Industrial dependence and export manufacturing in Kenya', katika J. Ravenhill (mh.), kur. 181-213.

**Langley, A.** (1973) *Pan-Africanism and Nationalism in West Africa 1900-1945* (Oxford: Clarendon Press).

**Langley, J. A.** (1975) *Pan-Africanism and Nationalism in West Africa 1900-1945; A Study in Ideology and Social Classes* (London: OUP).

**Larkin, B.** (1971) *China and Africa, 1949-1970* (Berkeley; UCP)

**Laroui, A.** (1967) *L'idéologie arabe contemporaine* (Paris: Maspero).

**Laya, D.** (mh.) (1972) *La tradition orale: methodologie et sources de l'histoire africaine* (Niamcy: CRDTO).

**Legvold, R.** (1970) *Soviet Policy Towards West Africa* (Harvard, MA: HUP).
**Leiris, M.** na **Delange, J.** (1967) *Afrique noire: la creation plastique* (Paris: Gallimard).
**Lelong, M. H.** (1946) *Mes freres au Congo* (Algiers).
**Lemarchand, R.** (1970) Rwanda and Burundi (London: Pall Mall Press).
**Lemarchand, R.** (mh.) (1981) *American Policy in Southern Africa* (Washington, DC: University of America Press).
**Leslau, C.** na **Leslau, W.** (wah.) (1962) *African Proverbs* (New York: Peter Pauper Press).
**Levine, B.** (mh.) (1983) The New Cuban Presence in the Caribbean (Boulder, CO: Westview Press).
**Le Vine, V.** ((1975) *Polical Corruption: The Ghana Case* (Stanford: Hoover Institution Press).
**Le Vine, V. T.** na **Luke, T. W.** (1979) *The Arab-African Connection: Political and Economic Realities* (Boulder, CO: Westview Press).
**Lewis, A.** (1953) *Industrialization in the Gold Coast* (Accra: Mchapaji wa Serikali.
**Lewis, W. A.** (1969) *Some Aspects of Economic Development: The Aggrey-Fraser-Guggisberg Memorial Lectures 1968* (Accra-Tema: The Ghana Publishing Corporation).
**Leys, C.** (1975) *Underdevelopment in Kenya: The Political Economy of Neo-Colonialism 1964-1971* (Berkely na Los Angeles: UCP).
**Liebenow, . G.** (1969) *Liberia; the Evolution of Privelege* (Ithaca and London: Corenell University Press)
**Lijembe, J. A.** (1967) 'The valley between', katika L.K. Fox (mh.) *East African Childhood* (London: OUP), ukr. 1-45.
**Lindfors, B.** (1980) 'Nigerian high school plays: 1950-1972', *Kiabéra,* 3,1 (Rains), kur. 47-88.
**Ling, D. L.** (1967) *Tunisia: From Protectorate to Republic* (Bloomington: Indiana University Press).
**Liniger-Goumaz, M.** (1979a) *Historical Dictionary of Equatorial Guinea* (Methuen, NJ na London).
**Littlefield Kasfir, S.** (1980) 'Patronage and Makonde carvers', *African Arts,* 13, 3, kur. 67-90 na 91-2.
**Lloyd, P. C.** (1967) *Africa in Social Change: Changing Traditional Societies in the Modern World* (Harmondsworth: Penguin Books).
**Lloyd, P. C.** (1971) *Classes, Crises and Coups: Themes in the Sociology of Developing Countries* (London; Paladin).
**Lloyd, P. C.**(1974) *Power and Independence: Urban Africans' Perception of Social Inequality* (London: Routledge and Kegan Paul).
**Lofchie, M. F.** (1965) *Zanzibar: Background to Revolution* (Princeton: PUP).
**London, J. B.** (mh.) (1976) *Social Anthropology and Medicine* (London and New York: Academic Press).
**Lonoh, M.** (n.d) *Essai de commentaire de la musique congolaise moderne* (Boulogne)
**Lopatov, V.** (1987) *The Soviet Union and Africa* (Moscow: Progress Pulishers).
**Lopes, H.** na **Tri, H.C.** (1981) 'The poverty trap: the plight of the least developed countries', *UNESCO, Courier* (Paris), 34, 9 0ktoba, kur. 5-9.

Love, K. (1969) *Suez: The Twice-fought War; A History* (toleo la 1, New York; McGraw-Hill).
Low, D. A. (1971) *Buganda in Modern History* (London: Weidenfeld and Nicolson).
Low, D. A. (1982) *'The Asian mirror to tropical Africa's independence'*, katika P. Gifford na W. R. Lous (wah.), kur. 1'-29.
Low, D. na Smith, A (wah.) (1976) *History of East Africa, Juz. 3* (Oxford; Clarendon Press).
Loxley, J. (1984) 'The World Bank and the model of accumulation', katika J. Barker (mh.), kur. 65-76.
Lugard, Lord (1922) *The Dual Mandate in Tropical Africa* (London: Blackwood and Sons).
Ly, Abdoulaye (1957) *Mercenaires noirs* (Paris: Présence africaine).

Macmillan, W. M. (1938) *Africa Emergent* (London: Faberand Faber).
Macmillan, W. M. (1941) *Democratise the Empire* (London: Kegan Paul and Co.)
Macmillan, W. M. (1963) *Bantu, Boer, and Briton: The Making of the South African Native Problem* (Oxford: Clarendon Press).
Macmillan, W. M. (1970) *The African Voice in Southern Rhodesia 1898-1930* (London: Heinemann).
Mamdani, M. (1976) *Politics and Class Formation in Uganda* (Nairobi: Heinemann).
Mandela, N. (1965) *No Easy Walk to Freedom: Articles, Speeches and Trial Addresses of Nelson Mandela* (London: Heinemann).
Manghezi, A. (1976) *Class, Elite and Community in African Development* (Uppsala: Taasisi ya Skandinavia ya Taaluma za Kiafrika).
Marcus, H. G. (1972) *The Modern History of Ethiopia* (Stanford: University Press).
Markovitz, I.L. (mh.) (1970) *African Politics and Society* (New York: The Free Press).
Markovitz, I.L.(1977) *Power and Class in Africa* (Englewood Cliff, NJ: Pentice Hall).
Marlowe, J. (1954) *Anglo-Egyptian relations,* 1800-1953 (London: Cresset Press).
Martin, D. na Johnson, P (waht.) (1981) *The Struggle for Zimbabwe* (London and Boston: Faber and Faber).
Martin, S. H. (1982) 'Music in urban East Africa: five genres in Dar es Salaam', *Journal of African Studies*, 9, 3, kur. 155-63.
Mazrui, A. A (1967) *Towards a Pax Africana* (Chicago; Chicago University Press, London: Weidenfeld na Nicolsn).
Mazrui, A. A. (1969a) *'Violent contiguity and the politics of retribalization in Africa', International Affairs*, 23, 1.
Mazrui, A. A. (1969b) Violenee and Thought: Essays on Social Tensions in Afriea (London and Harlow: Longman).
Mazrui, A. A. (1970) 'The robes of rebellion', *Encounter*, 34, 2, kur. 19-30.
Mazrui, A. A. (1972) *Africa's International Relations* (London: Heinemann).
Mazrui, A. A. (1975a) *The Political Sociology of the English Language* (The Hague: Mouton).
Mazrui, A. A. (1975b) 'The resurrection of the warrior tradition in African political culture', *Journal of Modern African Studies*, 13, 3, kur. 67-84.
Mazrui, A. A. (1975c) 'Black Africa and the Arabs', *Foreign Affairs*, 53, 4 (Julai, kur. 725-42.

**Mazrui, A. A.** (1975d) 'The African university as a multinational corporation: problems of penetration and dependency', *Harvard Education Review*, 45, 2, kur. 191-210.
**Mazrui, A. A.** (1977) *Africa's International Relations: The Diplomacy of Dependency and Change* (Boulder, Co: Westview Press).
**Mazrui, A. A.** (1978) *Political Values and the Educated Class in Africa* (Berkeley;UCP).
**Mazrui, A. A.** (1980) *The African Condition: The Reith Lectures* (London: Heinemann).
**Mazrui, A. A.** (1986) *The Africans: A Triple Heritage* ((New York: Little Brown; London: BBC Publications).
**Mazrui, A.A.** (1990) *Culture Forces in World Politics* (London: James Currey Publishers).
**Mazrui, A. A.** na **Bakari,M** (1986) "The triple heritage in East African literature', katika A. S. Gerard (mh.), Juz.2, kur. 1045-60.
**Mazrui, A. A.** na **Tidy, M.** (1984) *Nationalism and New States in Africa* (London: Heinemann).
**Mbiti, J.** (1969) *Africa Religions and Philosophy* (London and Nairobi: Heinemann).
**Mboya, T.** (1963a) A letter of reply (African Socialism), *Transition*, 2, 11, uk.6.
**Mboya, T.** (1963b) *Freedom and After* (London: André Deutsch).
**Mbughuni. L. A.** (1976) 'Old and new drama from East Africa', *African Literature Today*, 8 kur. 85-98.
**McCarthy, J.** (1977) *Guinea-Bissau and Cape Verde Islands: A Comprehensive Bibliography* (New York and London Gerland Publishing).
**McEwen, F.** (1972) 'Shona art today', *African Arts*, 5, 4, kur. 8-11.
**Messenger, J. C.** (1962) 'Anang art, drama and social control', *African Studies Bulletin*, 5,2, kur. 29-35.
**Messenger, J. C.** (1971) 'Ibibio drama', *Africa*, 41, 3, kur. 208-22.
**Mestri, E.** (1980) *Les Cubains et l'Afrique* (Paris: Karthala).
**Mhina, G. A.** (1971) 'The place of Kiswahili in the field of translation', Présence africaine, 78, robo ya pili, kur. 200-12.
**Micaud, E.** (1968) 'Three decades of Tunisan art', *African Arts*, 1, 3, kur.46-55 na 78-84.
**Mitchell, Sir P.** (1939) *Native Administration* (Entebbe: Government Printer).
**Mitchell, R. P.** (1969) *The Society of Muslim Brothers* (London: OUP).
**Mlambo, E.** (1972) *Rhodesia: The Struggle for a Birthright* (London: C. Hurst and Co.)
**Monroe, E.** (1963) *Britain's Moment in the Middle East, 1914-1956* (Baltimore: Johns Hopkins Press).
**Montagu, A.** (1974) *Culture and Human Development* (Englewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall Inc.).
**Moore, C.** (1982) *Fela: This Bitch of a Life* (London: Allison and Busby).
**Moore, C. H.** (1965) *Tunisia since Independence* (Berkeley: UCP).
**Morgan, D. J.** (1980) *The Official History of Colonial Development* (1924-1970) ( majuzuu 4, London: Macmillan).
**Morgenthau, H. J.** (1973) *Politics Among Nations: The Struggle for Power and Peace* (toleo la 5, New York: A.A. Knopf)
**Morris M.** (1976) 'The development of capitalism in South African agriculture', *Economy and Society*, 5, 3, kur. 292-344.

**Morris Jones, W. H.** na **Fischer, G.**. (wah.) (1980) *Decolonization and After: The British and French Experience* (London: Frank Cass).

**Morrison, D. G. Mitchell, R. C.** na **Paden, J. N.** (1989) *Understanding Black Africa: Data Analysis of Social Change and Nation Building* (New York: Paragon House Irvington Publishers)

**Mortimer, R. A.** (1980) *The Third World Coalition in International Politics* (New York: Praeger).

**Mosley, L.** (1964) *Haile Selassie: The Conquering Lion* (London: Weidenfeld and Nicolson).

**Moumouni, A.** (1964) *Lèducation en Afrique* (Paris: Maspero).

**Mount, M. W.** (1973) *African Art: The Years since* 1920 (Bloomington, IN)

**Mshengu-Kavanagh, R.** (1979) 'After Soweto: people's theatre and the political struggle in South Africa', *Theatre Quarterly*, 9, 33, kur. 31-9.

**Mshengu-Kavangh, R.** (1981) *South African People's Plays* (London: Heinemann).

**Mutiso, G. C.** na **Rohio, S. W.** (wah.) (1975) *Readings in African Political Thought* (London: Heinemann).

**Nabudere, D. W.** (1977) Imperialism and Revolution in Uganda (Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

**Naguibu, M.** (1955) *Egypt's Destiny: An autobiographical Account of the Egyptian Revolution* (London: Gollancz).

**Nduka, O.**(1964) *Western Education and the Nigerian Cultural Background* (Ibadan: OUP)

**Nisbet, R. A.** (1969) *Social Change and History: Aspects of the Western Theory of Development* (New York: OUP)

**Niven, D.** (1985) 'Africa and the arts', *African Affairs*, 84, 335, kur. 183-93.

**Nkashama, N.** (1979) 'Ivresse et vertige: les nouvelles danses des jeunes au Zaïre', *Afrique littéraire et artistique* 51, kur.94-103.

**Nkrumah, K.** (1958a) 'All African Peoples Congress' (Accra).

**Nkrumah, K.** (1958b) 'African prospects', *Foreign Affairs*, 37, 1 (Oktoba), kur. 45-53.

**Nkrumah, K.** (1961) *I Speak of Freedom: A Statement of African Ideology* (London: Heinemann; New York: Frederick A. Praeger).

**Nkrumah, K.** (1962) *Towards Colonial Freedom* (London: Heinemann; toleo la 1 1945).

**Nkrumah, K.** (1963) *Africa Must Unite* (New York: Praeger; London: Heinemann).

**Nkrumah, K.** (1964) *Consciencism* (London: Heinemann).

**Nkrumah, K.** (1969) 'African socialism revisited', katika Y. Benot (mh.)

**Nkrumah, K.** (1970) *Class Struggle in Africa* (New York: International Publisher).

**Nkurumah, K.** (1966) *Neo-Colonialism: The Last Stage of Imperialism* (London).

**Norman, J.** (1963a) *Labour and Politics in Libya and Arab Africa* (New York: Bookman).

**Ntiro, S. J.** (1982) *Modern Creative Makonde Sculpture* (Dar es Salaam) (Mimeograph).

**Nuseibeh, H. Z.** (1956) *The Ideas of Arab Nationalism* (Ithaca: Cornell University Press).

**Nutting, A.** (1967) *No end to a Lesson: The Story of Suez* (London: Gollancz).

**Nye, J. S., Jr.** (1966) *Pan-Africanism and East African Integration* (Cambridge, MA:HUP).

**Nyerere, J. K.** (1960) 'Africa's place in the world', katika *Symposium on Africa* (Wallesley College, MA).

**Nyerere, J. K.** (1962) *'Democracy and the Party System* (Dar es Salaam: Tanganyika Standard).

**Nyerere, J. K.** (1963a) *Julius Caisar* (Nairobi and London: OUP).

**Nyerere, J. K.** (1963b) 'Les foundements du scialisme africain', *Présence africaine*, 47, 19, kur. 8-19.

**Nyerere, J. K.** (1967a) *Uhuru na Umoja (London*: OUP).

**Nyerere, J. K.** (1967b) *Socialism and Rural Development* (Dar es Salaam: Government Printer).

**Nyerere, J. K.** (1967c) *Education for Self-reliance* (Dar es Salaam: Ministry of Information and Tourism).

**Nyerere, J. K.** (1968a) *Essays on Socialism* (Dar es Salaam:OUP)

**Nyerere, J. K.** (1968b) *Ujamaa: Essays on Socialism* (London: OUP).

**Nyerere, J. K.** (1968c) *Freedom and Socialism (London: OUP)*

**Nyerere, J. K.** (1969) *Mabepari wa Vanisi* (Dar esSalaam: OUP)

**Nyerere, J. K.** (1970a) *Socialisme, democratie et unité africaine* (Paris: Présenee Africaine).

**Nyerere, J. K.** (1970b) *Non-alignment in the 1970s* (Dar es Salaam: Government Printer).

**Nyerere, J. K.** (1970c) 'Developing tasks of non-alignment', katika J. K. Nyerere, *Freedom and Development: A Selection from Writings and Speeches, 1968-1973* (London: OUP), kur. 159-71.

**Nyerere, J. K.** (1972) *Decentralization* (Dar es Salaam: Government Printer).

**Nyerere, J. K.** (1977) 'The Arusha Declaration, ten years,' *Daily News* (Tanzania); *International Herald, African Diary,* 11-17 Juni, uk. 852.

**Nyerere, J. K.** (1979a) *'South-South dialogue: a brief report', Third World Quarterly, 1,2,* (Aprili, kur. 117-22.

**Nzewunwa,N.** (1982) *The Masquerade in Nigerian History and Culture* (Port Harcourt: University of Poret Harcout Press).

**O'Brien, D. C.** (1971) *The Mourides of Senegal* (Oxford: Clarendon Press).

**O'Brien, J.** (1981) 'Sudan: an Arab breadbasket?', *Merip Report*, 99, Septemba.

**Oduho, J.** na **Deng,W.** (1963) *The Problem of the Southern Sudan* (London: OUP)

**Ogot, B.** (1977) 'Politics, culture and musie in colonial Kenya: a study of Mau-Mau hymns 1951-1956'. *Kenya Hisitorical Review*, 5, 2, kur. 275-86.

**Ogunba, O.** (!977) 'Le theatre au Nigeria'. *Présence africaine*, 58, 2, kur. 67-90.

**Ogunbiyi, Y.** (1981) *Drama and Theatre in Nigeria: A Critical Source Book* (Lagos: Nigeria Mazine).

**Ogunwale, T.** (1971) 'Lamidi Fakeye: Nigerian traditional sculptor', *African Arts*, 4, 3, kur.66-7.

**Okello, J.** (1967) *Revolution in Zanzibar* (Nairobi: EAPH)

**Okolo, A.** (1983), 'Dependency in Africa: stages of African political economy'. *Alternatives: Journal of World Policy* 9, 2, (Juni), kur. 252-4.

**Okonjo, C.** (1971) 'Africa: a decade of independence (an economic assessment)', katika *Présence Africaine,* Namba maalum, kur. 119-36.

**Okore, O.** (1984) 'The film world of Ousmane Sembene', (tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Columbia)..

**Okumu, T. M.** (1962) *Angola in Ferment: The Background and Prospects of Angolan Nationalism* (Boston: Beaco Press).

**Olatunbosum, D.** (1967) *Nigerian Farm Settlements and School Leavers' Farms* (East Lansing and Ibadan: CSNRD, Na. 9)

**Oliver, R.** na **Crowder, M.** (wah.) (1981) *The Cambridge Encyclopaedia of Africa* (Cambridge and New York: CUP).

**Olusola, S.** (1979) *Some Notes on 20 Years of Television in Nigeria* (Yuba: Ariya Productions).

**O'Meara, D.** (1974) 'The 1946 African mineworkers' strike in the political economy of South Africa', katika P.I. Bonner (mh.) kur. 179-235.

**Omo-Fadaka, J.** (19780 'Drought and famine', katika R. Synge (mh.)

**Onoh, J. K.** (1982) *Money and Banking in Africa* (London: Longman).

**Opubor, A.** na **Nwuneli, O.** (1979) *The Development and Growth of the Film Industry in Nigeria* (Lagos).

**Osia, K.** (1983) *Israel, South Africa and Black Africa: A Study of the Primacy of Politics of Expediency* (New York: University Press of America).

**Owusu, M.** (1972) 'The search for solvency: background to the fall of Ghana's Second Republic, 1969-1972', *Africa Today*, 19, 1, kur. 52-61.

**Owusu, M.** (1975) 'Economic nationalism, pan-Africanism and the military: the National Redemption Council of Ghana', *Africa Today*, 22, 1 (Januari-Machi), kur. 31-53.

**Oyugi, W. O.** na **Gilongo, A.** (wah.) (1987) *Democratic Theory and Practice in Africa* (London: Heinemann).

**Padmore, G.** (1956) *Pan-Africanism or Communism? The Coming Struggle for Africa* (London: Dennis Dobson).

**Palmer, R.** (1977) *Land and Racial Discrimination in Rhodesia* (London: Heinemann).

**Palmer, R.** (1986) 'Working conditions and workers responses on Nyasaland tea estates, 1930-1935', *JAH*, 25, 1, kur. 105-26

**Palmer, R.** na **Parsons, N.** (wah.) (1977) *The Roots of Rural Poverty in Central and Southern Africa* (London: Heinemann).

**Pankhurst, L. E. S.** na **Pankhurst, R. K.** (1953) *Ethiopia and Eritrea: the Last Phase of the Reunion Struggle* (Woodword: Green).

**Pankkhurst, R. K.** (1955) *Ethiopia: A Cultural History* (London).

**Park, R. L.** (1965). 'Indian-African relations', *Asian Survey* (Berkeley, CA), 5, 7 (Julai), kur. 350-8.

**Partke, W.** (1975) *Chinese Economic Aid* (London: C. Hurst and Co.).

**P'Bitek, O.** (1971) *African Religions in Western Scholarship* (Nairobi: EALB)

**Pearce, R. D.** (1982) *The Runing Point in Africa: British Colonial Policy 1938-48* (London: Frank Cass).

**Pearce, R. D.** (1984) 'The Colonial Office and planned decolonization in Afriea', *African Affairs*, 83, 330, kur. 77-93.

**Peel, J. D. Y.** (1983) *Ijeshas and Nigerians: the Incorporation of a Yoruba Kingdom, 1890s-1970s* (Cambridge: CUP).

**Peil, M.** (1977) *Consensus and Conflict in African Societies* (London: Longman).

**Peil, M.** na **Sada, P.O** *African Urban Society* (Chichester: John Wiley and Sons).

**Pfaff, F.** (1984) *The Cinema of Ousmane Sembene: A Pioneer of African Film* (Westport: Greenwood Press).

**Peifer, K.** (1981) 'Algeria's agrarian transformation', *Merip Reports, 99* (Septemba), kur. 7-14.

**Pheto, M.** (1981) 'Black film makers', *Index on Censorship*, 10, 4.

**Ponsionene, J. A.** (1971) *Education and Political Values* (Nairobi: EAPH).

**Popov, V. I.** (1975) *Studies of Soviet Foreign Policy* (Moscow: ProgressPublishers).

**Portmer, R. A.** (1972) 'Ousmane Sembene and the cinema of decoloniztion', *African Arts*, 5, 3, kur. 26-31 na 62.

**Post, K.** (1964) *The New States of West Africa* (Harmondsworth: Penguin).

**Potekhin, I. V.** (1963) 'Reply to my opponents on African Socialism', *International Affairs* (Moscow), Januari, kur. 71-5.

**Pratt, R. C.** (1976) *The Critical Phase in Tanganyika 1945-1968: Nyerere and the emergance of a Socialist Strategy* (Cambridge: CUP.

**Présence Africaine** (1961) *Colloque sur les religions, Abidjan, April* 5 - 12 (Paris: Présence africaine).

**Présence Africaine** (1972) *African Religions as a Source of Civilization Values, Cotonou Symposium, 16-22 Agosti, 1970* (Paris: Présenee Afreaine).

**Priebatsch, S.** na **Knight, N.** (1979) 'Ndebele figurative art', *African Arts*, 12, 2, uk. 32.

**Pritchertt, O.** (1979) 'Nigerian truck art', *African Arts*, 12, 2, kur. 27-31.

**Proctor, J. H.** (mh.) (1965) *Islam and International Relations* (New York: Praeger).

**Proshin, N. J.** (1975) *Istoriya Livii* [History of Libya] (Moscow; Nauka).

**Pye, L.** (1962) *Aspects of Political Development* (Boston: Little, Brown).

**Queuille, P.** (1965) *Histoire de l'Afro-Asiatisme jusqu'a Bandoung* (Paris: Payot).

**Quimby,I. M. G.** na **Swank, S. T.** (1980) *Perspective on American Folk Art* (new York Norton).

**Rabearimanana, L** (1980a) *La presse do'opinion é Madagascar de 1947 é 1956* (Antananarivo: Librairie Mixte).

**Rabemananjara, R. W.** (1952) *Histoire de la nation malgache* (Paris: Lachaud).

**Ramchandani, R. R.** (mh.( 1980) *India and Africa* (New Delhi: Radiant Publishers).

**Ranger, T. O.** (1975) *Dance and Society in Eastern Africa* (London: Heinemann).

**Ranger, T. O.** (1983) *Peasant Consciousness and Guerrila War in Zimbabwe* (London: James Currey).

**Ranger, T. O.** (1968a) *Emerging Themes of African History* (Nairobi: EAPH).

**Ranger, T. O.** na **Weller, J.** (wah.) 1975) *Themes in the Christian History of Central Africa* (Berkeley: UCP)

**Rauning, W.** (1985) *Catalogue of Exhibition on Ethiopian Art* (Munich: Munich Museum).

**Ravenhill, J.** (1985) *Collective Clientelism: The Lome Conventions and North-South Relations* (New York: Columbia University Press).

**Revenhil, J.** (mh.) (1986) *Africa in Economic Crisis* (Basingstoke: Macmillan; New York: Columbia University Press).

**Raymond, A.** (1955) *La Tunisie* (Paris: (PUF)

**Read, M.** (1936) 'Tradition and prestige among the Ngoni', *Africa,* 9, 4, kur. 453-84.

**Read, M.** (1955) *Education and Social Change in Tropical Areas* (London: Thomas Nelson and Sons Ltd).

**Richards, A.** (1982) *Egypt's Agricultural Development 1800-1980: Technical and Social Change* (Boulder, CO: Westview Press).

**Richards, P.** (1983) 'Ecological change and the politics of African land use', *African Studies Review,* 26, 2 (Juni), kur. 1-72.

**Robert, M.** (1976) *La Réunion: Combats pour l'autonomie* (Paris: L'Harmattan).

**Roberts, R.** (1974) *French Development Assistance: A Study in Policy and Administration* (London: Sage).

**Robson, P.** (1983) *Integration, Development and Equity: Economic Integration in West Africa* (London: George Allen and Unwin).

**Rood, L. L.** (1976) 'Nationalization and indigenization of Africa', *Journal of Modern African Studies,* 14, 3, kur. 427-47.

**Rosberg, C. G.** na **Nottingham, J.** (1966) *The Myth of 'Mau Mau', Nationalism in Kenya* (Nairobi: EAPH).

**Roseyear, D. R.** (1984) 'Cross River tombstones', *African Arts,* 18, 1 kur. 44-7 na 94.

**Ross, A.** (1977) 'the Capricorn Africa Society and European reactions to African nationalism in Tanganyika, 1949-60', *African Affairs,* 76, kur. 519-35.

**Rout, L.** (1976) *The African Experience in Spanish America* (Cambridge: CUP)

**Rubin, L.** na **Weinstein, B.** *(1974) Introduction to African Politics: A Continental Approach (New York:* Preaeger).

**Rweyemamu, J. F.** (1973) *Underdevelopment and Industralization in Tanzania* (Nairobi: OUP)

**Rweyemamu, J. F.** (1978) 'African and the New International Economic Order', katika R. Synge (mh.), kur. 36-43.

**Rycroft, D.** (1959) 'African music in Johannesburg: African and non-African features', *International Folk Music Council,* 11, kur. 25-30.

**Sadat, A.** 11- (1957) *Revolt on the Nile* (London: Wingrate).

**Sadie, J.** (1960) 'The social anthropology of economic underdevelopment', *Economic Journal,* 70, 278, kur. 294-303.

**Sauvant, K. P.** (1981) *The Goup of 77: Evolution, Structure, Organiztion* (New York: Oceana Publications).

**Sawant, A. B.** (1981) *Egypt's Africa Policy* (New Delhi: National Publishing House).

**Sayegh, F. A.** (mh) (1964) *The Dynamics of neutralism in the Arab World: A Symposium* (San Francisco: Chandler).

**Scanlon, D. G.** (1964) *Traditions of African Education* (New York: Columbia University Teachers College Press)

**Schipper, M.** (1982) *Theatre and Society in Africa* (Johannesburg: Raven Press).

**Schneider, B.** (1972) 'Malangatana of Mozambique', *African Arts*, 5, 2, kur. 40-5

**Schneider, E. A.** (1985) 'Ndebele mural art', *African Arts*, 18, 3, kur. 60-7.

**Schoepf, B. G.** (1984) 'Man and biosphere in Zaire', katika J. Barker (mh.), kur. 269-91.

**Schram, R.** (1981) 'Traditional medicine and modern medicine', katika R. Oliver na M. Crowder (wah.) kur. 391-2 na 293-6.

**Segal, A.** (1983b) 'Cuba and Africa: militiary and technical assistance', katika B. Levine (mh.) kur. 123-47.

**Seidman, A.** (1972) *An Economics Textbook for Africa* (London: Methuen).

**Sèkoe Toure, A.** (1963) *Guinean Revolution and Social Progress.*

**Sèkoe Toure, A** (1977) *'L'Afrique et la revolution, Vol XIII'*, katika L. Sylla (mh.)

**Selcher, W. A.** (mh.) (1981) *Brazil in the International System: The Rise of a Middle Power* (Boulder, CO: Westview Press).

**Serfontein, J. H. P.** (1979) *Brotherhood of Power: An Expose of the Secret Afrikaner Broederbond* (London: Rex Collings).

**Scrumaga, R.** na **Johnson, J.** (1970) 'Uganda's experimental theatre', *African Arts*, 3, 3, kur. 52-5.

**Shaath, N. A.** (1975) 'Africa manpower needs and the role of technical assistance', katika A. M. Rweyemanu na G. Hyden (wah.) kur. 97-109.

**Shamrai, I. V.** (1968) 'The problems of realizing economic co-operation between socialist and developing countries', *Narodvi Azii I Afriki*, 4, kur. 3-15.

**Shamuyarira, N. M.** (1965) *Crisis in Rhodesia* (London: Deutsch).

**Shariff, I. N.** (1988) *Tungo Zetu* (Renton, NJ: The Red Sea Press).

**Sharma, D. N.** (1969) *Afro-Asian Group in the United Nations* (Allahabad: Chaitanya Publishing House).

**Shenton, R.** (1986) *The Devlopment of Capitalism in Northern Nigeria* (London: James Currey).

**Sheriff, A** na **Ferguson, E.** (wah.) (1991) *Zanzibar under Colonial Rule* (London: James Currey).

**Shirazi, M** (1987) 'Film festival host', *West Africa*, 3628, 23 Machi, kur. 558-9.

**Shivji, I. G.** (1976) *Class Struggles in Tanzania* (New York and London: Monthly Review Press).

**Singer, C.** (1959) *A Short History of Scientific Ideas* (Oxford: Clarendon Press).

**Sithole, N.** (1959) *African Nationalism* (London: OUP)

**Skvirsky, D.** (1967) *Milestones of Soviet Foreign Policy 1917-1967*) (Moscow: Progress Publishers).

**Smelser, N.J.** (1968) *Essays in Sociological Explanation* (Englewood Cliffs, NJ: Prentice Hall).

**Smith, A.** (1976) 'The end of the Arab Sultanate: Zanzibar 1945-1964', katika D. A. Low na A. Smith (wah.).

**Smith, E. W.** (1962) 'Polular music in West Africa', *African Music*, 3, 1 kur. 11-17.

**Smith, F.** na **Eicher, J.** (wah.) (1982) *African Arts*, 15, 3.

**Smith, M. G.** (1971) 'Institutional and political conditions of pluralism', katika L. Kuper na M. G.

Smith (wah), kur. 27-67.

**Soyinka, W.** (1963)*The Lion and the Jewel* (London: OUP).

**Soyinka, W.** (1985) 'The arts in Africa during the period of colonial rule'., katika A. A. Boahen (mh. 581-609.

**Spencer, J.** (1985) *The Kenya African Union* (London: KPI)

**Stamp, D. L.** *(1960) Our Developing World* (London: Faber na Faber).

**Stavenhagen, R.** (1975) *Social Classes in Agrarian Societies* (Garden City: Anchor Press; Doubleday).

**Stevens, C.** (1976) *The Soviet Union and Black Africa* (London: Macmillan).

**Stevens, R. P.** (1976) *Lesotho, Botswana and Swaziland: The Former High Commission Territories in Southern Africa* (London: Pall Mall Press).

**Sticter, S.** (1982) *Migrant Labour in Kenya: Capitalism and African Response 1895-1975* (Harlow: Longman).

**Stil, M. H. Lelong** (1946) *Mes fréres du Congo* (Algiers: Editions Bacconier).

**Stout, A. J.** (1966) *Modern Makonde Sculpture* (Nairobi: Kibo Art Gallery Publications).

**Streeten, P.** (1972) *Aid to Africa: A Policy Outline for the 70s* (New York:Praeger).

**Sundkler, B.** (1961) *Bantu Prophets in South Africa* (London: OUP).

**Szombati-Fabian, I.** na **Fabian, J.** (1976) 'Art, history and society', *Studies in the Antropology of Visual Communication*, 3, 1, kur. 1-21.

**Teisen, M.** (1968) *Tingatinga* (Copenhagen).

**Tempels, R. P.** (1949) La philosophie bantoue (*Paris: Presence africaine*).

**Tessler, M. A., O'Barr, W. M.** na **Spain, D. H.** (1973) *Tradition and Identity in Changing Africa* (New York: Harper na Row).

**Thiel, J. E.** na **Helf, H.** (1984) *Christliche Kunst in Africa* (Berlin: D. Riemer).

**Thompson, V. M** na **Adloff, R.** (1965) *The Malagasy Republic* (Stanford: Stanford University Press).

**Thompson, R. F.** (1983) *Flash of the Spirit* (New York).

**Thompson, V. M.** na **Adloff, R.** (1968) *Djbouti and the Horn of Africa* (Stanford: Stanford University Press)

**Thompson, V. V. P.** (1969)*Africa and Unity: The Evolution of Pan-Africanism* (London: Longman)

**Thompson, W. S.** (1969) *Ghana's Foreign Policy, 1957-1966: Diplomacy, Ideology and the New State* (Princeton: PUP).

**Throup, D.** (1985) 'The origins of Mau Mau', *African Affairs*, 84, 336, kur. 399-435.

**Throup, D.** (1987) *Economic and Social Origins of Mau Mau* (London: James Currey).

**Touval, S.** (1963) *Somali Nationalism* (Cambridge, MA: HUP).

**Tracey, H.** (1952) *African Dance of the Witwatersrand* (Johannesburg: Gold Mines).

**Trimingham, S. J.** (1952) *Islam in Ethiopia* (London: OUP).

**Trincaz, P. X.** (1984) *Colonisation et régionalisme; Ziguinchor en Casamance* (Paris: ORSTOM).

**Twitchett, C. C.** (1979) *Europe and Africa: From Association to Partnership* (Farnborough: Saxon

House).

**Uchendu, V. C.** (1967) 'Some principles of haggling in peasant markets', *Economic Development and Cultural Change,* 16, 1 (Oktoba) kur. 37-51.

**Uchendu, V. C.** na **Anthony, K. R. M.** (1975) *Agricultural Change in Teso District, Uganda* (Nairobi, Kampla, Dar es Salaam).

**Vacono, S.** (1974) *Les étapes de la décolonisation française* (Paris: PUF)

**Vail, L.** (1975) 'The making of an imperial slum: Nyasaland and its railways, 1895-1935', *JAH,* 16, 1, KUR. 89-112.

**Vail, L.** (1977) 'Railway development and colonial underdevelopment: The Nyasaland case', katika R. Palmer na N. Parswons (wah.) kur. 365-95.

**Van den Bossche, J.** (1955) *Madya, graveur de calebasses* (Brussels: ARSOM).

**Van Donge, J. K.** (1985) 'An episode from the independence struggle in Zambia: a case-study from Mwase Lundazi', *African Affairs,* 84, 335, kur. 265-78.

**Van Sertima, I.** (1977) *They Came Before Columbus: The African Presence in Ancient America* (NewYork: Random House).

**Van Sertima, I.** (1984) 'Nile valley presence in Ameriea B.C.', katika I. Van Sertima (mh.)

**Van Sertima, I** (mh.) (1985) *Nile Valley Civilizations* (Atlanta, GA: Journal of African Civilizations).

**Van Sertima, I.** (mh.) (1986) *Blacks in Science: Ancient and Modern* (New Brunswick and London: Transaction Books).

**Van Sertima, I.** (1989) *Great African Thinkers, Vol. 1: Cheikh Anta Diop* (New Brunswick. Transaction Books).

**Vansina, J.** (1961) *The Oral Tradition; A Study in Historical Methodology* (Chicago; Aldine Publishing Co.)

**Vatikiotis, P.J.** (1961) *The Egyptian Army in Politics* (Bloomington: Indiana University Press).

**Vatikiotis, PJ** . (1969) *The Modern History of Egypt* (London: Weidenfeld and Nicolson).

**Vatikiotis, P. J.** (1980) *Egypt from Muhammad Ali to Sadat* (Baltimore).

**Waiguru, J.** (1965) 'The round mud hut', katika D. Cook (mh.), kur. 4-10.

**Wallerstein, I.** (1976a) 'The three stages of African involvement in the world economy', katika P. C. W. Gutkind na I. Wallerstein (wah.) kur. 35-64.

**Wallerstein, I.** (1976b) *The Modern World System* (New York; Modern Reader).

**Wallerstein, I.** (1983) *Historical Capitalism* (London: Verso).

**Walls, A. F.** (19780 'Religion and the press in the enclave in the Nigeria Civil War', katika G. R. Fashole-Luke (wah.) kur. 207-15.

**Walshe, P.** (1971) *The Rise of African Nationalism in South Africa: The African National Congress,* 1912-1952 (Los Angeles: UCP)

**Walters, R. W.** (1987) *South Africa and the Bomb: Responsibility and Deterrence* (Lexington, MA: D. C. Heath Lexington Books).

**Wandira, A.** (1977) *The African University in Development* (Johannesburg: Zenitt Printers).

**Wangwe, S. M.** na **Skarstein, R.** (1986) *Industrial Development in Tazania: Some Critical Issues*

(Uppsala na Dar es Salaam: Taasisi ya Scandinavia ya Taaluma za Kiafrika na Tanzania Publishing House).

**Wanyande, P.** (1987) 'Democracy and the one-party state: The African experience', katika W. Oyugi na A. Gilonga (wah.)

**Wanyoike, F. N.** (1974) *An African Pastor: The Life and Works of the Rev. Wanyoike Kamawe, 1888-1970* (Nairobi: EAPH).

**Wass, B.** (1979) 'The Kabah sloth', *African Arts*, 12, 3, kur. 62-5 na 96.

**Waterbury, J.** (1970) *The Commander of the Faithful: The Moroccan Political Elite* (new York: Columbia University Press).

**Watt, I.** (1969) *The Rise of the Novel* (Harmondsworth: Penguin Books).

**Watts, M.** na **Shenton R.** (1984) 'State and agrarian transformation in Nigeria', katika Barker (mh.) kur. 173-205.

**Wauthier, C.** (1966) *The Literature and Thought of Modern Africa: A Survey* (London: Pall Mall Press).

**Weber, M.** (1949) *The Theory of Social and Economic Organization* (New York: Grove Press).

**Webster, J. B** na **Boahe, A. A.** (1980) *The Revolutionary Years: West Africa since 1800* (toleo jipya; London; Longman).

**Weinstein, B.** (1966) *Gabon: national building on the Ogooue* (Cambridge, MA: MIT Press).

**Weinstein, B.** (1983) *The Civic Tongue: Political Consequences of Language Choices* (New York na London Longman).

**Welch, C. E. Jr na Smith, A. K.** (1974) *Military Role and Rule* (Massachusetts: Duxbury Press).

**Weman, H.** (1960) *African Music and the Church in Africa* (Uppsala: Svenska Institutet for Missionforskning).

**Wemba-Rashid, J. A. R.** (1972) 'Tingatinga of Tanzania', *African Arts*, 5, 4, kur. 20-1.

**Wenzel, M.** (1972) *House Decoration in Africa* (London; Duckworth).

**Whiteley, W.** (1974) *Swahili: The Rise of a National Language* (London: Methuen).

**Wilcocks, C.** (1962) *Aspects of Medical Investigation in Africa* (London na New York: OUP).

**Willet, F.** (1971) *African Art* (London; Thames and Hudson).

**Willetts, P.** (1978) *The Non-Aligued Movement: The Origins of a Third-World Alliance* (London: Frances Pinter Ltd).

**Williams, G.** (1981) *Third World Political Organizations* (London: Macmillan).

**Wilson, M.** na **Thompson, L.** (wah.) (1985) *The Oxford History of South Africa, Juz. 1* (London: OUP); Juz. II, 1971 (Oxford; Clarendon Press).

**Wilson, T.** (1974) *Russia and Black Africa before World War II* (Holmes na Meir).

**Yesufu, T. M.** (1973) *Creating the African University* (Ibadan: OUP).

**Yu, G. T.** (1975) *China's African Policy: A Study of Tanzania* (New York: Praeger).

**Zartman, W.** (1976) 'Europe and Africa: decolonization or dependency?' *Foreign Affairs*, 54, 1, kur. 325-44..

**Zimmer, W.** (1985) *Réprertoire du théâtre camerounais* (Paris: L'Harmattan).

**Zins, M. J.** (1983) 'L'Inde et l'Afrique: le Non-alignement au service des intérêts nationaux', *Politique Africaine* (Paris), 10, 10 Juni, kur. 39-54.

**Zoctizoum, Y.** (1983) *Histoire de la Centrafrique*; Tome I: 1879-1959 (Paris: L'Harmattan).

**Zulu, J. B.** na **Nsouli, S. M.** (1984) 'Adjustment programs in Africa', *Finance and Development*, 1 (Machi), kur. 5-10.

# FAHARASA


## A

A. Awolowo –95
A. Langley – 634
A. Letnev - 639
A.A. Mazrui – 642
A.M. Obote -579
ABAKO – 121,463
Abbe Fulbert Youlou – 110
Abd al- Nasser –83
Abd al-'Aziz Ta 'albi – 24
Abd al-Kadir aal-Jazairi – 63
Abd al-Khalik Tares – 743
Abd al-Nasser - 514 521,-575,693
Abdallah Hassan – 63
Abdias Nascimento - 566
Abdul Rahman Muhammad Babu – 147
Abeid Karume – 148 122,179
Abena Busia - 438
Abercrombie –214
Abidjani - 387,387
Abram Fischer –186
Abubakari II - 508
Abuna Abraham – 742
Academie francaise - 431
ACCT - 407
ACMS – 639
ACP – 270,618 621,.687,698
Adam na Eva – 509,- 497, 531, 592,- 595
Addo –228
Ade Ajayi - 589
Adebayo Adedeji - 505, 438, - 584
Adedeji – 303,305, 313, 726
Adelino Gwambe –175
adhabu –78
Adloff – 130
Adotevi - 515
Adoula – 716
Afewerk Tekle- 456, 460
Afika ya Kusini – 344
Africa Research Bulletin – 642, 640, 641
*African Communist* – 641
*African Dances* – 469
African Jazz – 468
African National Congress - 594 - 557
Africare - 561
Afrika – 568, 390, 390,347 557, 1, 105 366,- 558, 35

**Afrique-sur-Seine** – 478
Afro-Brazil - 566
Afrodiaspora - 566
Afro—Kubano – 468
Agano la Kale - 395
*Agbaya* – 466
Agostinho Neto – 430,– 344,– 636
Ahadi la Monrovia 496
Ahmadiyya - 390
Ahmadu Ahijo – 123
Ahmed Balafredj - 743
Ahmed Sekou Toure – 377
Aida ya Verdi – 465
Aimé Césaire - 515 - 758,- 428,-686
Akhir al-Saman - 508
Akkra – 405, - 573, - 593
*Al-Ahram* - 439
*al-Ashikka* - 31
Al-Azharya - 528
Albert Eistein, , 92,167, – 490, 569, 756 151,730
ALESCO - 600
Alex Haley - 559
Alexander Pape – 760
Alexandre Dauala – Manga Bell 744
*Al-Fikr* (Fikra) - 436
Ali A. Mazrui – 438 – 296, - 505,- 659
Alice Lenshina – 753
Aline Sitoè – 40
Alioune Diop - 387 - 558,- 572, 758
*Al-Islah* - 391
Al-Latif – 24
almasi - 499
ALN –77,–78
Al-Naser – 252 187, 251, 466 472, 64, 644 645, 663, 664,207,683,84, 370
*Alpenrosen* – 464
Alphonse Laverane - 493
Al-Sadat – 645,–188 – 755, 500,620
Amadou Hampate Ba – 392, 400, 1
*American Society of African Culture* - 558
Amharic –347
Amikar Kabral - 430 512, 513, 106, 370, 372
Amikulapo Kuti Fela, - 468
Amin –231,216
*Amnesty International* – 361
Amodou Mahtar M'Bow – 732
Amy Facques Garvey - 591

Anastase Mikoyan – 646
ANC -- 12,- 167, 168, 170, 594 598, 633, 638 654, 667, 170 173, 179, 184
Andre Matsoua – 111
André Resamp – 130
Andrew Cohen – 145, 714
Andrianamanjato – 130
Angie Brooks 752, 752, 753
*Anglo-American* - 500
Angola - 567
Ankrah - 714
Anna amailuk - 753
Anon, - 450
Anthonio –221
Anthony - 515
Antoine Gizenga – 130, 714
ANU-PF –180
Anwar al-Sadat –187
Apilth Sourou Migan – 744
Apkevon – 726
Appiah - 515
APROSOMA – 119
Archipenko – 480
Argentina - 565
Aristide Pereira –106
*Aroti* - 394
Arrighi –171, –232
Arthur Lewis - 520
Arzumanyan – 649
Asantewa –751
Woods –581
ASP – 147, – 148
Assemien Dèbylè, - 473
Astafyev – 660
Atieno Odhiambo - 438
Aton Muziwakhe Lembede –168
Aujoulat – 116
Awolowo – 432,525
Ayi Kwei Armah - 435
Azikiwe -92, – 744

# B

Ba Ndiaye – 456
Badawi – 465
Bagtes –221
bahari – 8
Bahia – 564,- 566
Bakari II - 508
Balewa –349
*Ballets africains*, - 469
Bamba – 42
Banda – 345,– 758
Vatican la 1964 – 465
Baraza la Udhamini 62, 703, 705 706,- 707,- 597 711, 712, 718, 720, 722,82, 596
Baraza la Utafiti la Ethiopia - 554
Baraza la utawala– 37
baraza la utendaji – 85
Baraza la Wasomi la Waafrika - 561
baraza la wawakilishi – 100, 107,
Barbados – 564, 567, 555
Barbara Castle – 744
Barker – 230, –231
Barmeet –174
Barnett – 142
Barthelemy Boganda – 118
Baraza la Uchumi bei-57
Belyana – 650
Ben Bella – –694, - 719
Ben Enwonwu – 456
Bender – 113
Benin - 564
Benito Mussolini – 742
Bennett – 143
Bernadette Olowo – 753
Bernard – 249
Bernard B. Dadie –104
Bernstein –231
Bey Munsif – 30
*Black Orpheus* - 428
Black Power - 559
Blair –235,237
Blaise Diagne – 43
Blum – 24
*bobongo*, - 469
Boda –102
Bonde la al-Midakk - 436
Bonde la Nili – 506,- 508
Bopp Centre - 393
Botswana –340
Boumedienne – 254, 255
Bourguiba – 742, 370, 74, 75
Bownam –171
Bretton Woods –610
British Guyana - 590
Buganda –344
Buijtenhuijs – 140, 142
Bundo - 529
Bunge -, 18, 23, 24, 31, 34, 43, 86, 101
Bunge la Marekani - 560
bunge la Misri –82
Bunge la Shirikisho – 45
bunge la Sudani -85
bunge la taifa –99
Bunuel – 478
bustani ya Eden - 509
Bwana Pléven - 44
Bwawa la Aswan – 650
*Bwiti* - 395
Byakov – 636

# C

CAF – 144, 145
Cain –234
Camara Laye - 433

Camp David –188
Canaan Banana –180, 181
Carter –166
*Casa dos Estudantes do Imperio* - 430
Casgrove-Twitchett –200
*Centro de Estudos Africanos* - 430
Centro de Estudos Afro-Asiaticos - 566
Centro de Estudos Afro-Orientais -566
Césaire – 428,- 431 - 592
Chadli Ben Mustapha – 635
Chagnous – 150, 138
Clayton – 148
Cliffe –217
Cohen –192,-190
Columbus - 508
Cooper – 147
Copernicus - 490
Coquery –Vidrovitch – 190, –200
Crahay - 515
Craveirinha – 430, - 431
Crazada Nacional de Liberacion – 119
Credo Mutwa – 475
CRUA –77
CUF –105
Cunningham –217
CUT - 705,– 706
Cutrufelli – 747

**D**

D. Lamb – 648
D. Martin – 641
D. Niven – 483
D'Almeida – 726
Dag Hammarskjöld – 714
Dalton –221
Dan Nabudere - 438
Daniel Solod – 645
Daoud –235
Dauber –234
Daudi – 643,673
Davidson Abdioseh Nicol - 445
Dayal – 714
de Bemis – 255
de Gaulle – 118, 26, 131, 149, 741, 109, 185,-594, 78, 79, 88
*DeBeers* - 500
Decraene – 650
*Deima* - 395
Delores Mortimer 752,375
Denis – 713
Dennis Brutus - 440
*Derg* – 648
Desmond Tutu –756,– 65, -569
*Destur* – 24
Destur-Mamboleo -73,– 74
*Destur-Mamboleo* -75
Devlin – 145
Dharm –230
Diallo Telli - 595
Dickens, - 436
Dien Bien –102, – 123
Diop - 551
Dirk Mudge – 182
Peter Milliard - 554
Donatus Nogwa, - 429
Dubinsky – 660
Dubois – 592,-558 -590
Duffy – 165
Duggan –166
Duignwan – 741
Dulcie September - 594
Duro Lapido, - 474

**E**

E.M. Zhukov – 637
E.T. Sutherland – 474
E.W. Blyden –369
EAC – 725
ECA – 270,– 307
ECA – 325, 496,- 505, 584, 601, 724, 724, 725, 726, 727 733 , 324
ECCAS –
Echemberg –195
ECOWAS – 270, 308, 584, 587
Edem Kodjo – 726
Eden Kodjo - 595
Edmund Burke -429
Eduardo Chivanbo Mandlane – 175,165,514,176
Edward Blyden - 513
Edward Mutesa -339
Edward Twining – 137
EEC – 270, 610 618,618, -621,623 611
*Egyptology* - 506
Eindstrand –216
Eisenhower – 741
Eleanor Roosevelt – 754
*Elisabethville* - 395
Eliud Mathu – 138, 140
Elizabeth Bagaya – 752, 753,753
El-Khawas –174
Emir Idris –80
Enwonwu – 456,460
Ephraim Amu, - 465
Equador - 565
Eritrea - 557
Ernest Ouandie – 122
Eslanda Robeson - 557
F. Houphouet Boigny – 45

**F**

F. Macauly – 635
F. Meli – 634

F.F. Small – 636
F.K. Fiawoo – 474
Fanon – 515, 521
Farouk – 252,85
Favoureu – 150
*FEFATUSA* – 170
Felix – 122
Fèlix Eboué – 40
Felix Houphouet – Boigny – 744
Felix Houphouet-Boigny –100,494,102
*fellaghas* –74
Feni Osofisan, - 474
Fenner Brockway – 744
Ferdinanda Oyono –104
Ferhat Abbas – 744, 743,31,494,78
Fidel Castro – 644, 688
FIDES – 112, 113, 249
Fily Dabo Cissoko – 744
Finant – 714
FLCS –88
FLN – 13,644, 720, 78,78,124 124
Flobert – 150
FNLA – 11,660 661,344
Fodeba –104, 469, 470,473
Foland Moumie – 122
Fourah Bay - 492
Franco – 35
Franklin D. Roosevelt – 62, 610
Franz Fanon - 435, 512, 513,664,367, 559
Freda Blick – 753
Freeman - Grevlle – 741
Freeman –231,598 637, 638, 660, 748,175,176 178,79
Frente Nacional de Libertacao de Angola –344
Friedrich Engels – 633
Fulbe –340
Fumban – 450

## G

G. Gorer – 469
G. Padmore – 635
G.E. Moore -92
Gabriel d' Arboussier – 104
Gaffar Nimeiri - 519
Galal –226
Galandou Diouf - 43
Galileo - 490
Gamal 'Abd al-Nasser – 11,, 83, 64, 68, 512,693 601, 6,63, ,675, 676 745
Gardiner – 716
Garvey – 558,592 686
Gaston Deferre –102
Gatsha Buthelezi – 169
GATT –244 245, 611
Boisson – 40
Gavana-54
GECS –100
*General Graduates Congress* – 25
George Awoonor –104
George Padmore – 590,369,555, 686, 556 , 569
Gerard Sekoto – 456
Germaine Dieterlen - 488
Gertzed – 132
Gibson Kente – 475, 144
Gifford – 145
GNP –202
Goliati – 643
Gorbachev – 667
Goukouni Oueddei - 599
Gowon – 642,652
GPRA –78
Grace Ogot – 753
Graft-Johnson-104
Green – 291
Greenberg - 506
Grigg –228
Gromyko – 650, 639
Guerin du Marteray – 128
Gumede – 635
GUNT - 599
Guthind – 643

## H

H. Bourguiba – 24
H. Diori - 577
H. Kokole –245
H. Maga -577
H. Ogunde – 474
H.Donalson – 638
H.W. Turner - 394
Habib Bourguiba – 61,73,514
*Haddarat* – 465
Haile Selasie - 27, 31, 555, 742,379
Menelik - 555
Hallstein – 664
Hammarskjold – 710, 711,712,713 714,716,717
Hanler – 661
Harold G. Lawrence - 508
Harold Macmillan – 145
*Harrism* - 394
Harrison –Charch –229
Harry Nkumbula –171
Harvey –174
Hassan al-Banna –88, 89
Hastings Banda – 65, 145,95,344
Hatshepsut - 751
Hawa - 444
Hay – 747

Hegel - 444
Hegemonia-52
Helleiner – 286
Henri Nicolle - 493
Henry Kissinger – 661,187
Herbert Chitepo - 174
Heyer –221,230
Hidrus Poindexter - 569
hija, - 393
Hill –232
himaya – 11, 21,23, 25,35,40, 43, 45, 46, 47, 62, 81, 68 379,55,56,58
Hirsch –197
Hiseltine – 127
Hispania – 566,557
Historia – 5, 6,7, 8, 9 11,12,13, 36, 47, ,58,
Hitler – 9,62,192, 163
Ho Chi Minh –675
homa – 21, 507
Hong Kong --625
hospitali na zahanati - 386
Houari Boumedienne – 256
Houbert – 149,150
Houphouet-Boigny – 577,101,376
Huari Bumedienne –695
Hubert Julian - 554
huduma – 38,50, 54,68, 81,103,438,
Hugh Trevor-Roper - 444
Hunton - 558
Huntonji - 515
huru -- 34,40,73,86, 594

# I

I.Geiss – 634
I.I. Potekhin – 637
I.K. Musazi – 636
Ian Douglas Smith –173
Ian Macleod – 143, 146
Ian Smith – 663
ibada za kienyeji –105
Ibadan - 492,433, 388
IBM -629
Ibrahim Babagida –213
Ibrayima Njoga – 455
IBRD – 728
ICA -620
ICARA – 734
IDA –245
idadi ya watu – 15,21 22,22
Ide Umaru - 595
Idi Amin – 11,360 753
IFAN - 493
IFC –245
*Ikati elimnyama* – 478
Iliffe – 135
'ilm - 528
ILO – 728,729, 730 731
imani – 397,47,48,62 62,89,63
IMF – 505,245,611 619, 620,622
India – 477,552
*indigenat* – 38,100
Injili ya Kikristo - 388
insha - 426
*Institut African d'éndes Prospectus* INADEP – 497, - 493, 493,565,566
International Rubber Agreement -620
ionosifia - 492
IPA –617,617,623
IPC -620
IRASAC - 493
Ireland –612
Isaac Newton - 501
Israel – 603,598
Issa Shivji – 438, 90
istilahi - 402
Italia – 553,554,557
Italiana –617
Italiano -621
itikadi – 65,89, 90, 91,511,363,364 370, 664, 609,104,
itikeli –376
Ivan Chernyshev – 650, 405,507
Izvestia – 635

# J

J. Kenyatta - 579
J. Nehru –693
J. Nyerere -579
J.A. Rogers - 555
J.K. Nyerere – 291
J.M. Brown – 634
J.Mulira – 636
J.P. Clark – 474
J.R. Leferink, - 396
jadi – 49,62, 62, 63, 63, 62, 62,51
jalaba-462
Jamaica –369,567, 566
Jamal al Din al Afghani - 514
James Aggrey – 555, 174,725,151
Jamhuri – 65,100, 103,85,83,76,88,80 602
jamia – 501,562,601 38, 531
jando – 433,529,47
Jane Goodall - 507
Janet Adebiyi – 750
jangwa la Sahara - 603
Jan-Paul Sartre - 517
Jansens – 710,711
Japan – 597,612,628
Jarida la Maarifa - 565
Jawaharlal Nehrn – 675,672,679
jazi – 480
*Jehan al-Sadat* – 754
Jehan Anwar al-Sadat – 754

Jenerali – 35,103,108
99,43,442,85,27
jenetiki - 492
jeshi – 23, 27,28
30,38, 43, 64,46,73
74,82,82,92, 25,85
73, 29, 40,92, 40
Jihadi – 68
jimbo – 48,102
jiolojia – 497
Joe – 634
John A. Davis - 559
519,147, 554
Jomo Kenyata
*Kukabiliana na Mlima Kenya* - 506
139,140,143, 554, 61,
634,636, 637
743,744, 758,369
590,686,95,
Jonas Savimbi – 598,
344,433
Joseph – 113,115
123, 121,122,715
715, 129
Joshua Nkomo – 171
667
*juju* – 468
*Julius K. Nyerere* –
136,65,364, 10,137,
371,519, 531,542, 570,
647, 664, 343, 687,
693,698
juma la vizuizi –79
Jumba jipya la Opera la
583,580, 601,46,56


# K


Kairo – 465
Jumiya ya Kidemokrasia
–86
Jumla ya Pato la Taifa –
615
Jumuiya -103, 531,
578,580, 594, –611
580,190,611,646,646
573, 586, 577,584
K. Nkrumah – 635,
639
Ka'ba – 455
*Kabaka* – 134, 145, 348,
344,340,134, 343,344
Kabral – 513, 521
Kabylie – 63
Kadhaffi - 393
KADU – 143
Kaduna - 600
Kaetano –179
kahawa – 20,620
*Kairo* – 387,439,
472,593
Kaisari – 742,169
kakao -620
Kalek – 118
Kaligrafia-460
*Kalondji* –715
kamanda wa jeshi – 36,
37
Kamarck –238
Kamati ya Afya kwa ajili ya Ulinzi wa Ethiopia-555, 578, 561, 705, 43,11,597,634 ,706,-248
*Kambi ya Korem* - 624
Kambo –
kamili –82
kamishina wa makoloni –
44,99
kampeni – 103,43,61
66,100,87,91,95,96
66
kampuni – 38,49
50,41, 567,19,53
58
Kamuzu Banda – 494
Kanada - 552
kanisa – 65,86,39
105,387, 65, 394,527
kanival – 471
Kanivali ya notting Hill -
569
Kanogo – 140
KANU – 143,368, 482
Kaprikon – 8
Kapteni Muammar
Kdhaffi –82
Kar Marx – 667
*Karaguz*, - 472
Karakana ya Massengo –
451
karanga – 41,42,52
Karibiani – 407,428
558, 560,563,566
Karl Mark – 633,513
70,629
karne – 22,62,94
karne ya ishirini – 20
22,8,51,42
Karungire – 135
Kasablanka – 10,594
Kasavubu – 711,712
713, 714
kasida - 430
kasisi - 530
kaskazini mwa Ikweta – 5
Kasuvubu – 716
katiba – 34,100,100
101,103, 80,86,86
96,725
katuni za watoto – 480
*KAU* – 139,140,143
Kauavubu – 716
kauli mbiu za kitaifa –376
Kaunda – 653,640
642, 669,370,669
695
Kazadi wa Mukuna – 466
kazi ya kulazimisha –
102,37, 70,591
106, 38
kibwanyeye – 61
Keita –104
kemia - 492
Kenekou –376
Kenneth Kaunda –
145,148,66,753,171
693
Kenyataa – 758

Kettani – 712,714
Khartoum – 459
Kiafrikaani - 403
Kiakan - 403
Kiama - 508
Kiamerika –369
kiangazi – 27
Kiarabu – 10,443
347
Kiasia –78
Kibamana – 478
Kibambara - 402
kibeberu – 35,47
62,62,95,70
kibinadamu -89
Kichewa - 505
Kidemografia – 21,4
13,15,31,34,627
kidini – 36,86,89
90
kidiplomasia – 10,27
84
Kiduala - 403
kienyeji – 63,101
Kiewe – 474,403
kifalme – 39,474
Kifaransa – 403,347
kifashisti – 22,35,36
45 45,104
kifo - 509
kigaidi –89
Kiganda – 475
Ki-Gandhi – 66
Kigiriki - 530
Kihausa – 402, 403
Kiigbo - 403
Kiingereza – 400,402
Kiislamu – 64,89,91
kijadi – 36,39
kijahidina –89
Kijamaa –78
kijeshi – 26
kijimbo -97
*Kijiometri* – 481
kikabaila –377,46
Kikamba – 453
kikatiba –98
Kikatoliki – 39
Kikikuyu – 475
kikoloni – 29,35
36,38,39,42,46,46
47,60,61,101,106
76,81
kikomi – 39
Kikomonisti – 29,
100,101
Kikorombezo - 485
Kikrio - 402
Kikristo –104,86
Kikronolojia – 63
Kikundi cha 77 - 603
618,621,669,594,612
594
Kilatini – 443, 530
kilimo – 17,18,19
20,29, 38,39,40
4949, 530,76,81,81
487,52,106, 4, 53, 55
Kilingala - 402
kiloni – 22
kilowezi – 46
Kilulua – 464
Kiluo – 475
Kimamluk – 450
Kimande – 473
Kimarx –103,95
Kimasai – 450
kimataifa – 23,65
68,73,78,– 45
kimbari –86,97
Kimberley - 501
Kimble –232
Kimeksika – 459
kimila – 49
Kindebele - 505
King Kong – 475
Kinomadi –81
Kinshasa – 459,446
Kintu - 509
kinyang'anyiro cha
Afrika – 741
kiongozi – 40,63
102,72,77,97,594
Kipato cha mwaka –76
Kipijini, - 402, 521,
503,65
Kipolisi-56
Kireno – 402,403
Kirhodesia –614
kisayansi – 8
kisiasa – 22, 23, 24, 25,
29,34,39,42, 43,
43,47,50,69,
105,106,72,76, 78,
85,88,89,90,92,98 99
Kisiwa cha Fernando
Poo, - 35
Kisoshalisti –100 101,102
Kiswahili – 402,403
475,344
kitaalamu – 8,81
kitabaka – 6
kitaifa – 24,70,73
76,87,95,97,98
kitamaduni – 36,85,
104,90
Kitchener – 20
Kitching –223,234
Kiteknolojia - 484
kitheolojia, - 42
Kitigre - 443
Kitigrinya - 443
Kituo cha Dini za
Kiafrika cha 495,
474, 497,565
565
kiuchumi – 20,22,26
29,32,36,41,43,4770,7
2,82,91
kiukoo – 61
kiutamaduni – 63
kivita – 26
kiwango cha maendeleo –
70,21
Kiwolof, - 443
Kixhosa - 505
Kiyoruba - 403
505
Kiyunani – 473
kizalendo – 24,72
87,94

Koba - 562
kobalti – 520,499
kodi – 20,38,50,106
54, 50,52,53,58
Kofi Antubam – 456,
460
Kolombia – 564,565
koloni – 19,22,35,37
38,39, 40,46,47,48,
49,65,103,82,94,9697
kompyuta - 424
kondi ya kichwa – 37
Kongamano la Bandung –
672, 496
Kongo – 394,- 557
493
Koran –369,509
Korea ya Kusini --625
Kosomali - 443
Kosta Rika – 566, 567
Kotonu - 387
*Kouassi* – 721,726
704
Kremlin – 634
*Kristo Maskini wa Bomba*
- 433
kromu - 499
kuanguka kwa
ukomunisti –374
Kuba – 380,39,567
kuchagua –99
*Kuelekea Amani ya Afrika Nzima* - 505
kuheshimu – 24
kuhiji - 389
Kuingiliana kwa
utamaduni –360
Kujali Afrika - 561
kujitawala –78, 44
kujitegemea –102,81
86,72
kujiuzulu – 5
Kulima-52
Kundi la 77 –697, 574,
575, 602,661, 575,
602,574,680
kupambana – 60
kupanda kwa bei-57
kupiga kura - 591
kupinga mapinduzi –
68,94
kura – 12,24,31,100
102,103,99,103,79
88,84
Kurani – 430,443, 528
kusawazisha migogoro -
598
kushikilia dini za jadi -
530
Kusini mwa sahara-52,
587
kusoma na kuandika -
524
kustaafu – 5
kutafsiri Biblia - 386
kutofungamana na
upande wowote –
592,373
Kutokujua kusoma -
Kuwaiti - 393
kuzuizini – 64
kuzuru kaburi – 42
Kwabena Nketia – 465
Kwame Anthony Appiah
–10 , 60, 65,66, 69,71
95, 97,521, 254,502
505, 512, 542,554
586,590, 592, 594,634
638,644, 746,369
570,686,693,405, 534
Kyle – 147

# L

L.P. Anjoulet – 744
L.S. Senghor –104
*L'Exil d'Albouri* – 473
*La Noire de...* - 478
La-Anyame –218, 230
La-anyane –211
A. Labaki – 455
Labour Party -626
Lacroix – 113,114
259
Lagos - 600,533,446
563
Lalibela - 490
Lamine Guaye –
100,43,744,99
Lamine Senghor –
635,675
Lamu - 528
Larkin – 640
Lawrence – 655
Le Corbusier – 482
*Le mandat* – 482
*Le regard du roi* - 433
Leakey - 506
Legoold – 646
Legos - 492
*Leila* na *Zainab* – 476
Lemarchand – 117,
119,661
Lenin – 11,430,632
633,650,178
Lenini –186
Léon M'Ba – 112, 743
Leopold – .758
250,65,371,428,
444,744,12,291
517,686
Lesieur – 41
Leslie - 438
Leslie L. Rood – 304
Lewis – 294
Leys –231
Libreville – 497
584,600
Ligi ya Tanganyika – 62
liginati – 28
*likembe* – 468
Ling. A.A - 639
Lithuli - 520
liturgia - 388
Lodi – 20
Lofchie – 147
Lon sadale – 131
London –619,630
Lonhro -623
Lonsdale – 142
Louvre, - 482

Lovanium - 492
Low – 131
Loxley –231
LPAI –88
Luambo (Franco) – 468
Luanda – 446
Lubumbashi – 395, 455,459
Lugha – 400,45,505 404, 85, 524, 85,386,405, 424, 539,524, 539 , 400
Luis Echevevria –688
Lumumba – 1,3, 44,61, 652 711, 712, 714, 715,716,717, ,713,
Luteni gavana – 37
Luthuli – 167
Lyolo-460

## M

MLSTP – 119
MNC – 121
MNR – 748
*Mobil* - 500
Mobogunje –232
Mobutu - 198, 613, 711, 714, 715
Modibo Keita - 576 594, 644, 646
Mohamed Diawara – 257
Mohamed V.- 450
Mohammad Idris –80
Mohammad V 1956-61, 366
Moise Tshombe –344, 598
*Molara ogundipe-Leslie* - 437
Monckton – 146
Mondlane – 178
Mongi Slim – 711, 712
Mongo Bet - 104, 433
Monja Jona – 131
Monnet – 197
Monrovia – 10, 496
564, 592, 573 594,
Montgomery – 741
Moore, - 480
Morard – 249
Morgan – 193
Moroko –339, 366
Morris –231, 232
Mosadeq – 745
MPLA – 11, 124, 178, 179, 186, 598, 660, 636, 637, 638, 661,
MTDL –77
MTLD –76
mto Nili – 20, 25, 383
Mtukufu Agha Khan III - 391
Muammar Kadhaffi – 11, 514
Mugabe – 180
Muhamad Hassan Abdulaziz - 506
Muhammad Abduh –369
Muhammad Ali – 251
Muhammad Mosadeq – 745
Muhammad Sid-Ahmed - 439
Muhausa –341
Muigbo – 341
Mukikuyo –341
Mulirai – 653
MULPOC – 307
Mungu –91
Mungu wa Afrika - 395
Museo Afro-Brasileiro – 566
Mussolini – 1, 19, 163, 192
Mutesa 11 - 134
Mutisya Munge – 452
Mutumba Bull – 754
Turnhalle, -598
Muzorewa –180, 598
Mwami Kigerri – 120

## N

Nabii Muhammad - 391
Nabudere – 133
NAC – 145
Nagib Mahfuz 83, 436
Nahhas Pasha – 23
Naipaul – 283
Nasser –678
*Nations négre et culture* - 572
NATO – 124, 611, 614, 661, 662, 718
NCBWA – 633
NCNC – 637
Ndabaningi Sithole – 171
NDP – 173
Nebab Bet - 527
negritude – 8, 104, 601
Nehanda – 751
Nehru – 207, 663, 664, 679, 680, 752
Nelson Mandela – 170, 186, 594, 755
*Neo-Destur* – 24,31,
Neto - 431
*New China Agency* – 641
New China News – 642
New York - 555
Nguema –360
NIC - 625
Nicholas Guillen - 567
Nicolas – 111
NIEO – 324, 325, 585, 619, 622
Nietzche –428
Nigeria Magazine – 471
Nixon –204
Nkrumah – 10, 11, 98, 108, 223, 234, 255, 348, 370, 384, 517, 521, 551, 572, 576, 613, 616, 645, 646, 648, 651, 663, 664, 669, 751, 758,
Nkiri Nzugwu - 521
Nkomo – 180

Nnandi Azikiwe – 555, 599
Nogee – 638
Nottingham – 138
Nu'man Ashur – 472
*Nuba* – 465
*Nujoma* – 737
Nukrashi Pasha – 32
Nuruddin Farah - 442
Nwokedi – 716
*Nyamaton* – 477, 478
Nyerere - 10, 138, 217, 148, 347, 368, 370, 376, 518, 642, 648, 656, 663, 669, 758
Nzinga – 751
Nzo Ekangaki - 595

## O

O'Brien – 716
OAS –79
Oasisi – 22
OAU – 10, 11, 12, 119, 124, 152, 270, 307, 324, 497, 570, 576
Oginga Odinga – 638, 646
Ogotommeli - 513
OIC –683
Okeke – 259, 267
Okello – 148
Okot p' Bitek - 434, 438, 747
Oku Ampofo – 456
Okuma –174
Olatunbosun –217
Oliver – 741
Olympio – 705
Onabolu – 455
opali - 499
OPEC – 196, 324, 325, 499, 603, 617, 618,620, 685, 697,
opera – 475
Osende Afana – 636
Oshogbo, - 459
*Ossi Zadkine*, - 481
OUA –671
Ousmane Sembene –104
Owusu –221
ozoni – 510

## P

P. Biarnes – 650
P. Enahoro – 648
P. Johnson – 641
P.J. Hontonji - 513
PAC – 667, 170, 179, 184,
PADESM – 128, 129
Padmore -572
Padre Tempel - 519
PAFMECSA - 593
Pahlavi - 745
PAI – 637
PAIGC - 106, 349, 636
Palengue -565
Palestina – 598, 604
Palmares Quilombo - 566
*Pan Africanism* – 10
Panama – 564, 567
Pandit – 752
*Papa Shenouda* - 387
paredi.za *asafo* – 471
PARMEHUTU – 119
Partke – 655
Pathé Diagne – 506, 508
Patice Lumumba – 121, 122, 613, 708, 710, 718
PATRIOTIC FRONT - 598
Paul Chauvet – 118
Paul Robenson – 558, 556
Pbohannam –221
PDCI –102, 349
*Perez de Cuellar* – 737
Petain – 31
*Peter* - 591
Peter Abraham - 590
Peter Milliard - 590
Peter Onu - 595
Philbert Tsiranana – 130, 131
Philip Mitchell-54
Picasso - 568
Pinay – 719
PLO – 667
Ponomarev – 644
*Popular Front* – 23, 24, 37, 41
Poro - 529
Potekhin – 648
Potopoto – 459
Pravda – 637, 638, 648
Présence Africaine – 387, 428, 558, 572,
Presentia Negra - 565
PSD – 130
PTA – 584, 587,
PTP -706
Puerto-Riko – 555

## Q

*Quedasse Bet* – 527

## R

R. De Haes, - 396
Rabearimana – 125, 129
Radwan – 230, 259, 262
Ralph Bunche -569
Randal Robinson - 570
Ras Tafari - 555
*Rashidiyya,* - 465
Raul Prebisch –687
RDA – 101, 102, 104, 111, 118, 743
Reberto Holden -344
reli – 20, 22, 41, 43, 48, 54, 88
RENAMO – 660, 748
Rene – 152
Rene Pleven –369
Rhodesia – 493, 614
Richard Wright - 555
Richards –227, 230, 233

RILU – 633
Robert – 149
Robert Buijenhuijs – 143
Robert Gardiner – 726
Robert Mangaliso Sobukwe –170
Robert Mugabe – 65, 663, 667, 171, 180, 181
Robert Schumauh – 719
Robert Sobukwe – 169
Robinson – 133
Robinson Kruso - 435
Rogin – 135
Romanova – 651
Rommel – 741
Rood – 304
Rosberg – 138, 143, 148
Roseberry T. Bokwe - 557
Rothchild – 135
Rousseau - 518
RPI –88
Rubeari – 125
Ruth Wiliams –177
Rwenzururu – 464
Rymalov – 650

## S

S. Ikoku – 648
S. Mulumba – 636
SADCC - 584, 587
SADR – 12
Sahara – 10, 35, 79, 592
SAID –234
Salah bin Yusuf –73, 74
Salazar – 35, 430
Saliha, - 465
Salim Ahmed Salim – 595, 736
Sally Magabe – 754, 181
Salvadore - 566
Samir Amin - 505
Samoff – 290
Samory – 478, 480
Samora Machel –178
*Satyagraha* – 66
Saul –232
Saussure - 406
Savimbi –182
Sayed Muhammad – 63
Sayed Muhammad Abdalla Hassan -442
Sayuni - 396
Sayyed Darwish – 465
SDP – 151, 152
Sekou Toure –102 104, 530, 594, 594 644, 648, 663, 665, 108, 364, 370, 371, 576
Sembene, - 435
Seneta Victor Biaka –102
Senghor – 292, 331, 370, , 439, 518, 521, 758
Seretse Khama –176
Setif – 63
Sevens – 653
Shaath – 303
Shah – 745
Shakespeare – 430, 442
Sharif –73
Shaw - 581
Shaykh Ahmadu Bamba - 389
Shehu Shagari - 503
Sheikh Ahmadu – 42
*Sheikh Amadu Bamba* - 390
*Sheikh Anta Diop* - 484, 485, 4, 93, 516, 522, 572,
Sheikh Hamallah - 42
Sheikh-Umar Sissoko, - 477
Shekh al-Islam Moulay al-Arbi Alawi - 514
*Shell* - 500
Siad Barre – 442, 648
Sidi –Bekkai –73
Simon Kimbangu – 65, 111, 394, 395
Simon Muzenda –181
Sinai -603
Singapore -625
Sir Arthur Lewis - 504
Sissoko, - 478
Sithole –180
Skvirsky – 637, 638
Smith – 148, 174, 180, 598
Société Africaine de culture – 405, 558
Songhay - 601
Soweto – 446, 475
Soyinka – 475, 520
Spence – 164, 165
Spenser – 138
Spinola –179
SPUP – 151, 152
Sputniki - 501
St Clair Drake - 562
STABEX –245, 621
Stalin – 635
Stavenhagen –232
Steve Biko – 170, 184, 594
Stevens – 164, 652
Stokely Carmichael, - 559
Strictener –Scott – 753
*Subbanu al-Muslim* - 391
Suleimani Cissè – 478
Sultani Mohamed bin Yusufu –72
Sultani Mohamed V – 24
sultani Sidi Mohammed Ben Yusef – 32
Sultani wa Zanzibar - 391
Sundkler –166
Suret-Canale – 272
Surinam - 564
Surrealism II - 428
Suru-Migan Apithy -100
SWAPO – 638, 654, 661, 179, 182
Sykes –174
Sylavanus Olympio – 10

Sylvanus – 705
Sylvester Williams – 634

# T

T. Wilson – 634
T.M. Azonga – 479
TAA – 136
TAA – 137
*Taa ya Umm Hashim* - 437
Tangri – 144
tantali - 499
TANU – 136, 137, 138, 349, 656, 743
*Tanzania Standard* – 641
Tawfik al-Hakim – 437, 472
TAZARA – 640, 656, 658
*Texaco* - 500
TFAL –88
Theodore W. Shiltz - 504
Theresa – 753
Thomas Jefferson -444
Thompson – 130, 646
Throp – 138, 140
Tiecouta Diop - 42
Tiemoko – 635
Timberlake- 711
Timbuktu - 539
Timothy Shaw - 580
Tinduf – 41
Tito – 207, 664, 693, 694
Tom Mboya – 65, 364
Toussaint Louverture - 555
Tronchon – 126, 127, 128
Tshombe – 711, 712, 713, 714, 715, 716, 717
Tsriklis – 651
Tubman –107
Tubman –108
TUC –96, 103
Tutu - 520
Twaddle – 125, 135,

# U

U Thant – 720, 725
UANC – 6, 8, 36, 45, 61, 63, 64, 65, 83, 84, 89, 180, 368, 574, 608, 622
Ubeligiji –617, 621
UDAO - 576
UDEAC – 270
UDEAO - 576
UDENAMO –175
UDI –173
UDMA –76
UFFB – 634
Uganda Peoples Congress UPC- 344
UGTAN –104
Uislamu – 1, 36, 39 41, 63, 65, 68, 78, 82, 83, 85, 89, 105, 370, 379, 382, 383, 384, 389, 393, 402, 443, 464, 508, 530
Ujamaa –69, 70, 89, 91, 291, 292 364, 369, 375, 432, 503, 519, 531, 615, 630
Ujerumani - 553, 617
ukombozi – 4, 11 12, 30, 38, 40, 45, 66, 68, 69, 80,91, 594
Ukomunisti –105
Ukristo – 36, 41, 65, 383, 384, 389, 482, 386, 509, 530
Ulaya - 4, 390, 552, 553, 557, 610
Um Nyobe – 123
Umagharibi -433
Umar Sissoko – 478
Umarx - 555
Umarx-Lenin - 518
Umm Khulthum, - 466, 467
Umma Party – 147
Umoja – 33
Umoja wa Mataifa – 8, 23, 32, 34, 62, 73, 78, 80, 82, 84, 87, 88, 119, 182, 185, 188, 207, 291, 304, 557, 592, 611, 619, 675, 677, 678, 685, 687, 701, 702, 706, 708, 710, 711, 713, 714, 715, 716, 717, 719, 720, 722, 723, 724, 725, 727, 728, 729, 735, 737, 738, 739, 744, 752,
*Umukonto we Sizwe* – 170
*Umunsif* – 31
Umuridi – 42
UN – 701, 702 703, 705, 708 710, 711, 712 713, 715, 716, 717, 718, 719, 722, 728, 732, 733, 735, 736, 737, 739
UNA – 124
UNC – 133, 134
UNCTAD – 245, 610, 687, 696, 697, 727, 728
UNCTAD IV -620 207
UNDATS – 307
UNDP - 601 728, 730, 733
Unegro – 387, 428, 460
UNEP – 16, 205, 405, 406, 496, 497, 502, 531, 600, 601, 728, 731, 732, 735, 736, 751
UNFAO –234
UNHCR – 733, 734
UNI –88
UNITA -344
UNICEF – 754, 767

*Union Minière* - 500
*Union Culturelle Musulmane* - 391
UNIP – 11, 124, 145, 146
UNITA – 11, 124, 660, 661, 178, 182, 660, 661
178,182,186
*United Gold Coast Convention* –366
*United Native African Church of Nigeria* - 394
Upanafrika - 64, 552, 553, 558, 567, 570, 572, 576, 580, 601, 606
Upanarabu - 601
UPC – 111
122, 123, 135
637, 720, 743
UPRONA –120
Usmani Sembene – 478
Uswisi –617
utaifa – 34, 60
63, 64, 89, 90, 91, 95, 350, 364, 369,
UTP – 137
Uzalendo – 25, 31, 36, 45, 77

## V

V. Lopatov – 639
V. Rymalov – 649
V. Turner – 471
Van Bilsen – 121
Van Bilsen – 713
Van Donge – 144
Van Horn - 712
vanadiamu - 500.
Vasquez – 651
Verwoerd – 168
Vichy – 31, 63, 149, 126, 185, 192, 194, 741
Vita – 19, 20, 23, 25, 27, 29, 30, 35, 38
40, 41, 43, 45, 47, 50, 55, 56, 57, 58, 61, 62, 68, 73, 76, 78, 81, 84, 89, 93, 94, 96, 99, 102, 104
Viteix – 456, 458
Viwanda – 15, 18, 19, 20, 27, 28, 29, 29, 38, 41,52, 55, 70, 71, 81, 78, 103

## W

W. Soyinka – 474
W.E. DuBois – 61, 369, 552, 555, 556, 558, 634
556
Waabbasi - 601
Waamhara, - 6
Waarabu – 6, 390
Waasia - 501
Wabarabeg - 517
Wabeba – 6
Wabelgiji – 492, 552
Waberberi - 73, 487, 512
Wadesturi – 24
Wad-Halula (Mahdist) – 24
Wadogon - 488
Wafd – 23, 30, 83
Wafulbe - 488
Wagadugu – 497
Wagenya – 450
Wahabeshi - 567
Wahausa –340, 487
wahenga – 380, 385
Wahhabi - 391
Wahhabiyya - 391
wahujaji – 42
Waigbo – 340, 377, 487
Waingereza – 22
23, 366, 338, 492
Waishe – 167
Waislamu – 6, 24, 29, 61, 63, 76, 77, 85, 98, 385, 534
Waitaliano – 6
Wajapani – 1
Wajerumani – 1, 368
wajumbe –43, 100, 101
Wakamba – 452
Wakarimajong - 517
wakatoliki-58
Wakikuyu –6, 377
Wakomunisti – 24, 556
Wakristo - 65, 86, 98, 385
*Wallace Johnson* - 591
Wallacel-Johnson - 554
Walleistein – 643
walowezi – 18, 24
39, 42, 48, 51, 53, 74, 76, 78, 99, 401
Walter Rodney – 559, 769
Walter Sisulu – 170
walumbi - 426
Waluo –374, 461
Wamakonde – 452
Wamangbetu – 450, 464
Wamarekani - 561
Wamasai - 488
wamisionari – 41, 384, 386, 389, 403, 539
Wamisri – 6
Wa-Muride – 389, 390
Wamuridi – 42
Wandebele – 454
Wandembu, - 471
wapagani – 49
wapiga ramli – 494
Wapiganaji – 63
Waprotestanti –434
warabiti - 339
Wareno - 492
Warumi - 444
Washia - 393
Washona –368
Wasiddi - 567
wasifu - 426

Wasomali –368
*watoto wa vita* – 767
Watsogho – 471
Watswana – 340
Waumaya - 601
Wavell – 26
Wawakilishi – 24, 73, 99, 100, 101,
wawakilishi wa Kiafrika –101
Wayoruba - 6, 340, 459, 489, 512
Wayunani - 434
Wazanaki – 343
Wazaramo – 452
wazawa – 65
Wazulu – 6, 512
Wazungu – 6, 8, 22
West Indies - 568
weusi – 15
Weusi wa Diaspora – 563
WHO – 728
733, 767, 205
Wicker –193
Willett, - 449
William Eteki Mbumbua - 595
William Leo Hansberry - 554
William Tubman – 252
Willie Brandt – 664
Willis Huggins - 554
Wilson – 30
Windstrand –231
*Winnie Mandela* - 754, 755, 756
Winston Churchill – 62
Winston Field –173
Wole Soyinka - 435 436, 441

## Y

Yaaa – 751
Yahya Hakki -437
Yamusukro – 496
Yasini Diallo –100
*Yeli* -427
Yergan - 557
Yoweri Museven –339, 753
Yu – 656, 658
Yusuf Ben Khedda –78
Yusuf Idris – 472
*Yusuf na Kaka Zake* - 442

## Z

ZANLA – 748
ZANU – 173, 174, 638, 640, 663, 667, 179, 180
ZAPU – 638, 640 667, 173, 174, 179, 180
Zhou En Lai – 639, 640
ZIPRA – 748
ZNP – 147
ZPPP – 147
Zumbi wa Palmares - 566

## Historia Kuu ya Afrika

*Historia* hii inatoa mwanga juu ya umoja wa kihistoria wa Afrika pamoja na uhusiano wake na mabara mengine, hasa Amerika na Karibian. Kwa muda mrefu aina zote za taarifa za kubuni na hisia pendelevu zimeficha historia ya kweli ya Afrika kwa ulimwengu kwa jumla.

Kwa kujumuisha maarifa yetu juu ya Afrika, tukiweka bayana maoni mbalimbali kuhusu tamaduni za Afrika na kwa kupitia upya historia, *Historia* hii ina manufaa ya kutoa mwanga na uvulivuli na kueleza bayana tofauti za mawazo ambazo zinaweza kuwepo baina ya wasomi.

## Mapitio ya Majuzuu yote

"Mazao ya mwanzo ya UNESCO ni lazima yasifiwe kuwa ni mchango mkubwa wa kitaaluma."
**Roland Oliver**, *Times Literary Supplement*

"Ni mojawapo wa miradi mikubwa ya kitaaluma iliofanyika katika karne hii."
*West Africa*

"Majuzuu haya yametolewa kwa unadhifu mkubwa lakini yana bei nafuu sana ... Yanawakilisha matumizi mazuri kabisa ya pesa ambayo mnunuzi yeyote wa vitabu anaweza kuyapata ..."
**Basil Davidson**, *Third World Quarterly*

# Afrika Kuanzia 1935

Sura ya baadaye na wendo wa matukio ya Afrika wakati huu wa miaka ya 1990 ni vitu vilivyoongezwa kwenye toleo la kwanza la kitabu cha jalada jepesi la *Historia Kuu ya Afrika* UNESCO. Jinsi ambavyo ukombozi dhidi ya utawala wa kikoloni unavyoendelea, ndivyo ambavyo mawanda ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni barani yanavyochambuliwa.

Kwa Afrika, mwaka 1935 ulidhihirisha mwanzo wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, kwa Mussolini kuivamia Uhabeshi. Migongano ya kimataifa inatawala sehemu ya kwanza ya juzuu hili, ambayo inaelezea migogoro kwenye Pembe ya Afrika na Afrika ya Kaskazini, pamoja na maeneo mengine chini ya utawala wa Wazungu.

Sehemu tatu zinazofuatia zinashughulikia mapambano ya Afrika nzima kwa ajili ya mamlaka ya kisiasa kuanzia 1945 hadi wakati wa uhuru, maendeleo duni na kupigania uhuru wa kiuchumi, na mabadiliko ya kijamii na kisiasa kuanzia wakati wa uhuru, zikiangalia ujenzi wa taifa na miundo na maadili ya kisiasa yanayobadilika. Sehemu ya tano inahusika na mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni kuanzia 1935, kuanzia kwenye dini hadi fasihi, lugha hadi falsafa, sayansi na elimu.

Sehemu mbili za mwisho zinazungumzia maendeleo ya Afrika nzima na dhima ya Afrika huru kwenye mambo ya dunia. Kwa kukiri kichekesho cha awali kuwa ilikuwa ni ulazimishaji wa ubeberu wa Wazungu ambao uliziamsha hisia za Waafrika, juzuu hili linaelezea mwingiliano wa uhusiano ambao ni muhimu na unaokua baina ya Afrika na sehemu zingine za dunia.

**TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO**

**S.L.P 35110, Dar es Salaam**

**ISBN 9976 911 42 4**